

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Kwanza

Al-Fatihah mpaka Al-Baqrah

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.


Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Kwa Jina la Allah Mwingi Rehema Mwenye Kurehemu

Utangulizi wa Tarjama ya Kiswahili Tafsiri ya Ibn Kathir

Tarehe 30 Juni 2001 mpaka 1 Julai 2001 katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kiislam ya wavulana ya Ununio, jijini Dar es salaam, Tanzania, palifanyika warsha ya kuzungumzia vitabu kama njia muhimu ya utawanyaji wa elimu ya Kiislam kwa umma. Warsha hii ilihudhuriwa na baadhi ya Masheikh maarufu nchini (bara na visiwani) na kiongozi wa semina hiyo alikuwa *Al Marhum* Sheikh Abubakar Juma Mwilima.

Warsha ilitambua kuwa kuna mkuza mkubwa baina ya Waislam na Uislam kwa sababu ya upungufu wa Elimu sahihi ya Uislam. Na mkuza huu kwa njia moja umesababishwa na kukosekana vitabu vya elimu ya Dini katika lugha inayofahamika na wakazi wa sehemu zetu hizi ambayo ni Kiswahili. Ndipo ilipoazimiwa kuwa pawepo na juhudi za makusudi za kutarjumi vitabu vya Dini kutoka kwenye lugha nyingine, hasa lugha ya Kiarabu na Kiingereza, kuja kwenye Kiswahili. Pakaundwa kamati ya kushughulikia maeneo mbalimbali ya tarjama. Maeneo hayo yalikuwa ni: Tafsiri ya Qur'an, Vitabu vya Hadithi za Mtume (saw) na vitabu vingine mbalimbali na utafiti.

Kutokana na sababu kadhaa, utekelezaji wa maazimio hayo kwa muda mrefu ukawa ni wa kudorora. Ndipo Ibn Hazm Media Center, kwa kushirikiana na masheikh na wasomi wengine wa Kiislam wakaamua kulifufua suala hili. Matokeo yake yakawa kushughulikiwa kwa tarjama ya vitabu muhimu vifuatavyo: *Minhajil Muslim, Raheeq al Makhtum, Lu'ulu Walmarjan, Tafsir Ibn Kathir, Sahihil Bukhari, Sahihi Muslim, Tarbiyatul Awlad fy islam, Ulumul al-Qur'an, Ahkamil Janaiz, al-Kabair, Fiqhi Awlawiyaat, Shaksiyyat al Muslim, Shakhsiyyat al Muslimah* n.k.

Tarjama hii ya Kiswahili ya kitabu "*Tafsir Ibn Kathir*" ambayo ni Tafsiri ya Qur'an iliyoandikwa kwa Kiarabu na kutarjumiwa katika lugha ya Kiingereza na zingine ni katika mlolongo wa shughuli hii.

Tafsiri hii ya Qur'an Takatifu ambayo ni maarufu kwa jina la Tafsiri ya *Ibn Kathir* iliandikwa na Al-Hafidh Abu Al-Fida 'Imad Ad-Din Ismail bin Umar bin Kathir Al-Quraishi Al-Busrawi (Aliyekufa Mwaka 744 H) ni tafsiri maarufu sana kati ya Tafsiri za Qur'an katika lugha ya Kiarabu, na Waislam wengi wanaiona kuwa ni yenye marejeo mazuri kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Kazi hii ya Kiarabu ina kurasa elfu tatu na mia mbili katika juzuu nne.

Ili kupitia marejeo yote, Ibn Kathir amekusanya baadhi ya Hadithi dhaifu na visa vya Kiisraeli (*Israiliyyaat*). *Darussalam* ya Saudi Arabia walichagua jopo la Wanazuoni wa Kiislam kuandika muhtasari wa *Tafsiri Ibn Kathir* katika lugha ya asili ya Kiarabu. Sheikh Abu Al-Ashbal Ahmad Shaqif wa Rabitah Al-Alam Al-Islami, Makka, na Sheikh Safiur-Rahman Al-Mubarakpuri, Mkuu wa kamati ya Utafiti ya *Darussalam* walifanya kazi na kikundi cha wanazuoni kwa takriban miaka minne kufanikisha azma hiyo. Na *Darussalam* wakaja na toleo lililofupishwa katika lugha ya Kiarabu, kwa jina la *Al-Misbah Al-Munir Fi-Tahdhib Tafsir Ibn Kathir*. Tafsiri hii ya Kiswahili ni ya Kitabu hiki cha Kiarabu *Al-Misbah Al-Munir Fi-Tahdhib Tafsir Ibn Kathir*.

Katika kufanikisha zoezi la kupata mbinu bora ya kuisimamia Tarjama ya *Tafsiri* hii muhimu iliandaliwa semina maalum. Mnamo Oktoba 2005 katika Hoteli ya Njuweni Kibaha, ambayo lengo lake kuu lilikuwa ni kujadili Rasimu ya Juzuu ya kwanza na kuweka misingi muhimu ya kufuatwa katika kutarjumi Juzuu 9 zinazofuatia. Semina hii ilihudhuriwa na baadhi ya Masheikh maarufu nchini na wataalamu wengine wa fani mbalimbali katika Tarjama.

Hatuna maneno fasaha ya kuelezea "*Tafsir Ibn Kathir*" kama itavyojieleza yenyewe kwa msomaji. Hii ni tafsiri *Bil Ma'thur au kwa jina lingine Tafsir bil Rriwaya* ambayo imejengwa katika msingi wa aya kutafsiriwa na aya zingine, na aya kutafsiriwa na maneno ya Mtume na maelezo ya masahaba kuhusu ufahamu wao kama walivyofundishwa na Mtume Muelekeo wake mkubwa ni kumuelekeza Muislam kwenye kuyajua na kuyafanyia kazi maneno ya Mwenyezi Mungu katika uhalisia wa maneno hayo kama yalivyokusudiwa na Muumba Mwenyewe. Tumeamua kutarjumi tafsiri hii ya Qur'an kwa sababu ni Tafsiri inayokubalika na Waislamu wengi bila ya mijadala.

Kutarjumi kitabu kutoka lugha moja kwenda nyingine ni kazi inayohitaji umahiri wa hali ya juu, na inapokuwa ni Tafsiri ya Qur'an au Hadithi linakuwa ni jukumu kubwa zaidi, ambalo linahitaji umahiri wa lugha zote husika na maarifa ya Dini na *istilahiza* Dini. Hivyo basi katika kuuendea mradi huu, msaada, ushauri, mwongozo na ushirikiano mwingi ulitolewa na watu wengi katika hatua mbalimbali za mradi.

Tarjama hii ni juhudi kubwa iliyoshirikisha Masheikh na wataalamu wetu wa fani mbalimbali za Dini ya Kiislamu na lugha zote husika. Katika kipindi cha miaka 17, Mradi huu wa Tarjama hii imepitia awamu mbalimbali, tutajitahidi kuzielezea hapa zile awamu muhimu tu na pia tutajitahidi kuwataja wale wote

walioshiriki katika juhudi hii kwa njia moja au nyingine, na ikitokea tumewasahau, tunasema Mkamilifu ni Mwenyezi Mungu, na aliyetusahaulisha sisi si mwingine ni Shetani.

Walioshiriki moja kwa moja katika mradi huu katika rasimu ya awali ni, *Al Marhum* Maalim Hassan 'Uthman Mnjeja kwa kutarjumi Ibn Kathir ya Kiingereza kwa asilimia 70; Ustadh Muhammad Abdallah Swaleh El-Maawy, kwa kutarjumi Suratul Israi na Suratul Kahf, na Ustadh Abu Ja'far Chifu Sasya kwa kutarjumi baadhi ya Sura zilizokamilisha Tafsiri hii.

Kwa lengo la kuhakikisha ubora wa Tarjama, Rasimu hii ya awali, ikapitia awamu mbalimbali za uboreshaji. Katika awamu hizo, awamu kuu ni kama ifuatavyo:

1. Tarjama hii ya Kiswahili imehaririwa kwa kupitiwa mara tano na Ustadh Yassir Salim Awadh Masoud, Msimamizi Mkuu wa Mradi huu.
2. Tarjama hii ya Kiswahili kwa kulinganisha na Kiarabu imepitiwa mara moja kwa ukamilifu na mara ya pili kwa kupitia maeneo mengi kwa lengo la kuiboresha na kuifanyia uhakiki na Sheikh Seif Abubakar Ruga.
3. Pia Tarjama hii ya Kiswahili kwa kuilinganisha na ya Tarjama ya Kiingereza imepitiwa mara moja na Ustadh Abdulsamad Salim Awadh.
4. Tarjama hii pia imepitiwa mara moja, Mijalada mitano, na Dada Arafa Sharif, bingwa wa lugha ya Kiswahili, kwa lengo la kuboresha lugha ya Kiswahili iliyotumika ndani yake na kuboresha muundo na mtiririko wa Mada. Alhamdulillah, juhudi zake na ushauri wake umesaidia sana katika kuboresha Tarjama hii na kuonekana katika muundo mzuri huu tuliokuwa nao.
5. Katika kuipitia rasimu ya pili iliyohakikiwa, kwa lengo la kuiboresha na kuihakiki zaidi, ilibidi tuwashirikishe Wataalamu wetu wengine zaidi wa Dini ya Kiislamu. Kwa sababu tafsiri ina kurasa zaidi ya elfu saba (7000), si rahisi kazi hii ikafanywa na mtu mmoja wa enzi hizi, hivyo basi tukazigawanya sura na juzuu kwa kuwapa Masheikh kuzipitia na kuzihakiki kwa kulinganisha na Tarjama asili ya Kiarabu. Hivyo basi, baadhi ya Sura na juzuu zilipitiwa na Masheikh wafuatao, Al Marhum Sheikh Suleyman Amran Kilemile, Sheikh Muharram Juma Doga, Sheikh Seif Abubakar Ruga, Sheikh Khatib Mussa Giragiza, Sheikh Mohamed Ali Kibabu, Sheikh Ali Asaa, Sheikh Khamisi Liyenike, na Sheikh Said Bawazir.

6. Walioshiriki katika uhariri wa lugha ya Kiswahili na maeneo mengine muhimu ya muundo wa lugha ya Kiswahili ni Masheikh wafuatao: Muhandisi Ally Shaaban Kilima, Sheikh Shaaban bin Musa, Ustadh Jumbe Ali, Ustadh Said Salim Bawazir, Ustadh Khalfan Njama, Yusuf Rajab Kanyama, Ismail Mereng, na Suleyman Dadi.

7. Walioshiriki katika kuhakikisha tunapata Tarjama nzuri zaidi ya baadhi ya aya na hadithi zinazohusiana na Itikadi na zisizohusiana na Itikadi ni Masheikh wafuatao Sheikh Seif Abubakar Ruga na Sheikh Shaaban Musa.

8. Tarjama imepigwa chapa na Mzee Athumani Mangube, Saada Tewe na Abdul Khamisi Sharifu.

9. Tarjama imesanifiwa na kutiwa katika programu ya Kompyuta na kupangwa katika njia zote nzuri kwa ajili ya hatua za uchapishaji na Ustadh Ali Said Abdallah.

Hadithi nyingi za Mtume zimewasilishwa kwa lugha ya Kiarabu. Vichwa vya habari vimeongezwa katika Tarjama hii kuwasaidia wasomaji wawe na uelewa mzuri juu ya majadiliano ya Aya za Qur'an. Lugha na mtindo uliotumika katika kutarjumi ni wenye kueleweka na mwepesi.

Lazima tukubali, kuwa katika Tarjama hii kuna kupishana kidogo katika uandishi, kiherufi na utamkaji wa majina ya Mitume, Masahaba, Tabi'i, Maulamaa na miji n.k katika baadhi ya kurasa. Kwa kuwa tarjama ina kurasa karibu elfu nane na imehusisha wataalamu wengi, upishano huo ni wa kibinaadamu. Tunawaomba wasomaji wa tarjama hii pale panapotajwa Jina la Mwenyezi Mungu wafuatishie na neno **تعالى**, anapotajwa Mtume wafuatishie na neno **ﷺ**, anapotajwa Sahaba wafuatishie meneno 'Allah Awawie Radhi', wanapotajwa waja wema wafuatishie **رحمته الله تعالى** kwa maana Allah Awerehemu, n.k. Hizi ni katika adabu za Kiislamu, hapana budi tuzifuate na tuziheshimu.

Tungependa wasomaji wetu wafahamu kuwa tafsiri ya Qur'an ya Kiswahili tuliyoitumia kwa kiasi kikubwa ni ile ya *Al-Muntakhab* iliyofasiriwa na Al-Marhum Sheikh Ali Muhsin Al Baruani kwa lugha ya Kiswahili, na ile iliyotafsiriwa na Marhum Sheikh Abdallah Saleh Al-Farsi, na pia tumetumia nyenzo zingine nyingi.

Pia, Tunapenda wasomaji wetu wafahamu Tarjama zote za Kiswahili tulizozitumia, Masheikh wetu wamezipitia na kurekebisha maeneo yote muhimu

ambayo wameona hayajatarjumiwa vizuri. Katika hili, aya zote zinazohusiana na *Aqidah* zimetarjumiwa inavyotakiwa kama zilivyotafsiriwa na waja wema waliotangulia.

Tunawashukuru Masheikh wote, wasaidizi na washauri ambao walishirikiana nasi katika ukamilishaji wa mradi huu.

Wana tarjama wote waliohusika na kazi hii, wanafhamu fika, na wanawaomba wasomaji pia wafhamu vivyo, kuwa tarjama yoyote (ikiwemo kazi hii) si tafsiri iliyokusanya maana kamilifu ya Qur'an kama maneno ya Allah, ila ni katika jitihada na ufhamu wa kibinadamu wa kuchambua maneno ya Qur'an ili kujulisha makusudio ya Allah katika Kitabu Chake. Kunaweza kukawepo kuswibu na pia kuna uwezekano wa kuwepo upungufu. Ninawashukuru Masheikh wote, wafanyakazi wote, wasaidizi na washauri ambao walishirikiana nasi katika ukamilishaji wa mradi huu.

Natoa shukurani mahsusi kwa Ally Said Abdallah, Sheikh Seif Abubakar Ruga, Muhandisi Ally Shaaban Kilima, Sheikh Said Bawazir, Abdulsamad Salim Awadh, Arafa Issa Sharif, Abdul Khamisi Sharifu na Abdulkarim Ebrahim (Mkurugenzi Mtendaji wa Ibn Hazm) kwa juhudi zao kubwa kabisa katika kufanikisha kukamilika kwa Tarjama hii.

Tumejitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kazi hii isiwe na makosa, lakini udhaifu wa kibinadamu utafanya yawepo makosa. Tunawaomba wasomaji wetu watusamehe kwa makosa watakayoyaona na watuarifu tuyasahihishe katika matoleo yajayo, In Shaa Allah. Katika mradi huu, makosa yanatokana nasi na Shetani, ambapo mazuri yanatokana na Rehema za Allah. Endapo watu watafaidika na Tarjama tafsiri hii katika kuielewa Qur'an, tunahesabu kuwa ni baraka kubwa na tunamuomba Allah Atulipe thawabu siku ya Hesabu.

Allah Ndiye Mjuzi wa kila jambo.

Yassir Salim Awadh Masoud
Msimamizi Mkuu wa Mradi Huu
Mkurugenzi
Ibn Hazm Media Center
Dar es Salaam 2021

Yaliyomo:

Tafsiri ya Suratu Al-Fatihah.....	1
Maana ya <i>Suratul Fatihah</i> na Majina Yake Mengine.....	1
Idadi ya Aya zake.....	2
Idadi ya Maneno na Herufi katika <i>Suratul Al-Fatiha</i>	2
Kwa nini Imeitwa <i>Umm Al-Kitab</i>	2
Fadhila za <i>Al-Fatihah</i>	3
Kusoma <i>Al-Fatihah</i> katika Swala.....	7
Kusoma <i>Al-Fatihah</i> ni lazima kwa Kila Rakaa.....	9
Tafsiri ya <i>Isti'adhah</i> (Kujikinga) na Hukumu Zake.....	10
Kujikinga kabla ya Kusoma Qur'an.....	13
Kujikinga kwa Allah تعالى Mtu Anapokasirika.....	14
<i>Istia'dhah</i> ni Wajibu au Sunna?.....	15
Ubora wa <i>Istia'dhah</i>	16
Nini Maana ya <i>Istia'dhah</i> ?.....	16
Sababu ya Kuitwa Shaytan.....	18
Maana ya <i>Ar-Rajim</i>	19
<i>Bismillahi</i> ni Aya ya Mwanzo ya <i>Al-Fatihah</i>	20
Kusoma <i>Bismillahi</i> kwa Sauti na kwa Siri katika Swala.....	21
Utukufu wa <i>Al-Fatihah</i>	23
Imependekezwa Kusoma <i>Bismillah</i> kabla ya Kufanya Kila Jambo.....	24
Maana ya <i>Lafdhal - Jalaal "Allah"</i>	25
Maana ya <i>Ar-Rahman Ar-Rahim</i>	26
Maana ya <i>Al-Hamd</i>	30
Tofauti Iliyopo Baina ya <i>Al-Hamdu</i> na <i>Ash-shukru</i>	31
Kauli ya Wanazuoni (Salaf) kuhusu <i>Al-Hamd</i>	32
Fadhila za <i>Al-Hamd</i>	32
Maana ya ' <i>Al'</i> Kabla ya Neno <i>Hamd</i>	33
Maana ya <i>A-Rabb</i> , Bwana.....	34
Maana ya <i>Al-'Alamin</i> (viumbe vyote).....	34
Kwa nini Uumbaji Unaitwa ' <i>A'lam</i> ?.....	35
Maana ya Allah تعالى Kuuhusisha Utawala wake na Siku ya Malipo.....	36
Maana ya <i>Yawm Ad-Diin</i>	37
Allah ni Malik (Mfalme Mwenye Mamlaka Makuu au Mmiliki).....	37
Maana ya <i>Ad-Din</i> (siku ya malipo).....	38
Maana ya Neno "Ibada" Kilugha na Kidini.....	39
Faida ya Kutanguliza Kumtaja Mtendwa Kabla ya Kitendo.....	39
<i>Al-Fatihah</i> Inaonesha Umuhimu wa Kumsifu Allah تعالى	41
Tawhid <i>Al-Uluhiyyah</i>	42
Tawhid <i>Ar-Rububiyyah</i>	43

Allah تعالى Kumuita Mtume Wake عبد 'Abd (Mja).....	43
Mwongozo wa Kufanya Ibada Wakati wa Msongo wa Mawazo.....	44
Siri ya Kuanza Kumsifu Allah تعالى kabla ya Maombi.....	45
Maana ya Mwongozo Uliotajwa katika Surah.....	46
Maana ya <i>As-Sirat Al-Mustaqim</i> , Njia Iliyonyooka.....	47
Watiifu Huwa Wanaomba Uongofu.....	48
Kuna Hadithi za Mtume na Kauli Mbalimbali za <i>Salaf</i>	51
Muhtasari wa <i>Al-Fatihah</i>	52
Uneemeshaji Unatokana na Allah تعالى	53
Kuitikia Amin baada ya Kusoma <i>Surat Al-Fatihah</i>	54
Tafsiri ya Surat Al-Baqarah	57
Fadhila ya <i>Surat Al-Baqarah</i>	57
Fadhila za <i>Surat Al-Baqarah</i> na <i>Surat Al-Imran</i>	60
<i>Surat Al-Baqarah</i> imeteremshwa Madina	62
Herufi <i>Muqata'at</i> (Herufi Moja Moja).....	64
Herufi za Mwanzoni mwa Surah.....	64
Herufi Hizi Zinathibitisha Muujiza wa Qur'an.....	65
Hamna Shaka Ndani ya Qur'an.....	67
Muongozo ni kwa wale wenye <i>Taqwa</i>	68
Maana ya <i>Al-Muttaqin</i>	69
Kuna aina mbili za <i>Hidayah</i>	70
Maana ya <i>Taqwa</i>	71
Maana ya <i>Iman</i>	71
Maana ya <i>Al-Ghaib</i>	73
Maana ya <i>Iqamat As-Salah</i>	75
Maana ya "Kutoa".....	76
Maana ya <i>Salah</i>	77
Sifa za Waumini.....	78
Jazaa ya Waumini ni Uongofu wa Kufuzu	81
Maana ya <i>Khatama</i>	84
Maana ya neno " <i>Ghishawah</i> " na Ubainifu wake	86
Wanafiki.....	86
Maana ya <i>Nifaq</i>	87
Mwanzo wa Unafiki.....	87
Maana ya "Maradhi" katika Ayah	92
Maana ya Uharibifu.....	95
Aina za Uharibifu Zinazofanywa na Wanafiki.....	96
Hila na Ulaghai wa Wanafiki.....	99
Mashetani ya Kijini na ya Kibinadamu.....	99
Maana ya Kucheza Shere.....	100
Hila za Wanafiki na kuadhibiwa kwao.....	101

Maana ya “Kuwaacha katika Upotovu Wao Wakitangatanga Ovyo”.....	102
Mfano wa Wanafiki.....	106
Mfano Mwingine wa Wanafiki.....	108
Aina za Waislamu na Aina za Makafiri na Wanafiki.....	113
Aina za Nyoyo.....	115
Tawhid <i>Al-Uluhiyyah</i>	118
Dalili za Kuwepo Allah <i>تعالى</i>	123
Kuthibitisha Ujumbe wa Mtume ﷺ ni wa Kweli.....	124
Changamoto na Kutoigika kwa Qur’an	125
Mifano ya Miujiza ya Qur’an	128
Qur’an ni Muujiza Mkuu Kabisa Aliopewa Mtume ﷺ.....	131
Maana ya “Mawe” katika Aya	131
Hivi Sasa Jahannam Ipo?.....	133
Malipo ya Waumini Wema.....	136
Kufanana kwa Matunda ya Peponi.....	137
Wake wa Watu wa Peponi Wametoharishwa.....	138
Mifano Kuhusu Maisha ya Dunia	140
Maana ya Khasara.....	146
Ubainifu wa Dalili ya Uweza wa Allah <i>تعالى</i>	149
Mwanzo wa Uumbaji.....	150
Ardhi Iliumbwa kabla ya Mbingu.....	151
Ardhi Ilitandazwa Baada ya Kuumbwa Mbingu.....	152
Khalifa Adam <i>عليه السلام</i> na Wanawe Duniani.....	153
Ulazima wa Kumteua Khalifa	157
Utukufu wa Adam <i>عليه السلام</i> Juu ya Malaika.....	159
Udhahirisho wa Utukufu wa Adam <i>عليه السلام</i>	164
Kutukuzwa Adam <i>عليه السلام</i> kwa Kusujudiwa na Malaika.....	166
Iblis Kuingia Miongoni mwa Walioamriwa Wamsujudie Adam <i>عليه السلام</i>	166
Malaika Kumsujudia Adam <i>عليه السلام</i> ni Kutii Amri ya Allah <i>تعالى</i>	167
Kiburi cha Iblisi.....	168
Kutukuzwa kwa Adam <i>عليه السلام</i> Mara Nyingine.....	169
Bi. Hawa Aliumbwa kabla ya Adam <i>عليه السلام</i> Kuingia Peponi.....	170
Allah <i>تعالى</i> Anampa Mtihani Adam <i>عليه السلام</i> na Mti wa Matunda.....	171
Wasifu wa Adam <i>تعالى</i>	172
Adam <i>عليه السلام</i> Alikaa Peponi kwa Muda Kisha Akateremka Ardhini.....	172
Utata na Jawabu Lake.....	173
Toba ya Adam <i>عليه السلام</i> na Maombi Yake kwa Allah <i>تعالى</i>	174
Wana wa Israel Wanahimizwa Kuupokea Uislam.....	178
Israel ni lakabu - Jina la Kupanga jina halisi ni Yaqubu <i>عليه السلام</i>	179
Neema za Allah <i>تعالى</i> kwa Wana wa Israel.....	179
Wana wa Israeli Wanakumbushwa Ahadi Waliyopewa na Allah <i>تعالى</i>	180

Kukatazwa Kuuficha Ukweli na Kuupotosha.....	184
Kulaumu Kitendo cha Kuamrisha Wengine Kutenda Mema.....	187
Kuomba Msaada kwa Subira na Swala.....	190
Kuwakumbusha Wana wa Israel Kufadhilishwa Kwao.....	194
Ummah wa Muhammad ﷺ ni Bora kuliko Wana wa Israel.....	195
Maombezi, Fidia au Msaada Hautakubaliwa kwa Makafiri.....	197
Wana wa Israel kuokolewa kutoka kwa Firauni na kuzamishwa.....	200
Funga ya Ashura.....	203
Wana wa Israel Waliabudu Ndama.....	204
Toba ya Wana wa Israel Ilikuwa Kuuana Wao kwa Wao.....	205
Wakuu wa Wana wa Israel Walitaka Kumuona Allah تعالی.....	207
Kuwafunika Kiwingu Wana wa Israel.....	209
Utukufu wa Masahaba wa Muhammad ﷺ.....	212
Mayahudi badala ya Kumshukuru Allah تعالی kwa kupata Nusura.....	214
Kuzibuka kwa Chemchemi Kumi na Mbili.....	219
Kutaka Kwao Vyakula Duni Badala ya <i>Manna</i> na <i>Salwa</i>	220
Mayahudi Walipigwa Unyonge na Umasikini.....	223
Maana ya Kiburi.....	224
Imani na Kufanya Amali Njema ni Msingi wa Kuokoka.....	226
Maana ya Muumini.....	227
Kwa nini Mayahudi Wanaitwa " <i>Yahuud</i> ".....	227
Kwa nini Wakristo Waliitwa " <i>Nasara</i> ".....	228
Waumini.....	228
<i>Sabiin - Saibuun</i>	229
Kuchukua Ahadi Kutoka kwa Mayahudi, Kuinuliwa Mlima Turi.....	230
Mayahudi Walivunja Ibada ya Mapumziko (Sabato).....	232
Nyani na Nguruwe Waliopo Hawatokani na Vizazi vya Wale.....	233
Kisa cha Myahudi Aliyeuawa, na Kisa cha Ng'ombe.....	235
Ukorofi wa Mayahudi kuhusu Wasifu wa Ng'ombe.....	238
Kuhuishwa Aliyeuliwa, na Kubainika kwa Muuaji.....	241
Ugumu kwa Nyoyo za Mayahudi.....	243
Kuwepo kwa nguvu ya utambuzi katika Vitu Yabisi.....	245
Kukatia Tamaa Imani ya Mayahudi zama za Mtume ﷺ.....	250
Mayahudi Walijua Ukweli wa Utume wa Muhammad ﷺ.....	251
Maana ya " <i>Ummi</i> ".....	254
Maelezo kuhusu Neno <i>Amaaniyya</i>	255
Ole wao Mayahudi hawa wanaobadili maneno ya Allah تعالی.....	255
Mayahudi Wanatumaini kwamba Watakaa Motoni kwa Siku Chache.....	257
Mkusanyiko wa Madhambi Madogo Husababisha Maangamivu.....	260
Ahadi Aliyochukua Allah تعالی kutoka kwa Wana wa Israel.....	261
Masharti ya Ahadi na Kuivunja Kwake.....	266

Kiburi cha Mayahudi Kupinga kwao Mitume na Kuwaua.....	270
Jibril ni <i>Ruh Al-Qudus</i> Roho Mtakatifu.....	272
Mayahudi walijaribu kumuua Mtume ﷺ.....	273
Mayahudi Walikuwa Wakisubiri Ujio wa Mtume ﷺ.....	276
Mayahudi kudai kwao kuamini huku wakikanusha Haki.....	281
Mayahudi Waliasi baada ya Kuchukua Ahadi Yao.....	284
Kuwaita Mayahudi Katika Kuapizana.....	287
Makafiri Wanatamani Kama Wangeishi Muda Mrefu.....	290
Uadui wa Mayahudi Kwa Jibril عليه السلام.....	291
Kutofautisha Baina ya Malaika , ni sawa na Kutofautisha Baina ya Mitume.....	293
Dalili za Utume wa Muhammad ﷺ.....	298
Mayahudi walitupa kitabu cha Allah تعالى.....	299
Uchawi ulikuwepo kabla ya Suleiman عليه السلام.....	301
Kisa cha Harut na Marut na ufafanuzi ya kuwa Wao ni Malaika.....	302
Kujifunza Uchawi ni Kufuru.....	305
Kusababisha Kuvunjika kwa Ndoa ni Moja ya Madhara ya Uchawi.....	306
Hukumu ya Allah تعالى Iko Juu ya Kila Kitu.....	307
Adabu katika Kuchagua Maneno.....	310
Ukubwa wa Uadui wa Makafiri.....	312
Maana ya <i>Naskh</i> na Maelezo Yake.....	313
Ubainifu wa Kusihi kwa <i>Naskh</i> na Majibu kwa Mayahudi.....	316
Katazo la Kukithirisha Maswali.....	319
Kukatazwa Kufuata Njia za Watu wa Kitabu.....	322
Kutiwa Moyo Kufanya Amali Njema.....	325
Matarajio ya Watu wa Kitabu.....	328
Mayahudi na Wakristo Wanakanushana Wenyewe kwa Wenyewe.....	332
Madhalimu wakubwa ni Wale wanaowazuia Watu katika Misikiti.....	335
Habari Njema kwa Ushindi wa Uislamu.....	337
Kuelekea Qiblah Wakati wa Swala.....	339
Qibla kwa Watu wa Madinah ni Baina ya Mashariki na Magharibi.....	341
Kuwajibu wanaosema kuwa Allah تعالى Ana Mwana.....	342
Kila Kitu Kinamnyenyekea Allah تعالى na Kumtii.....	344
Maana ya Muumbaji " <i>Badii</i> "......	346
Mtume ﷺ alivyoelezewa ndani ya Tawrati.....	351
Maana ya Kusoma Kitabu Ipasanyo.....	354
Ibrahim Al-Khalil عليه السلام Kipenzi cha Allah تعالى.....	358
Ibrahim عليه السلام Alijaribiwa kwa Maneno Yapi?.....	361
Madhalimu Hawatapata Ahadi ya Allah تعالى.....	363
Utakatifu wa Nyumba ya Allah تعالى.....	365
<i>Maqam</i> Ibrahim عليه السلام.....	366
Amri ya Kusafisha Al-Ka'abah Nyumba ya Allah تعالى.....	370

Makkah ni Mahali Patakatifu.....	372
Ibrahim عليه السلام Anamuomba Allah تعالى Aifanye Makkah Eneo Salama.....	374
Ujenzi wa Al-Ka'abah na Kumuomba Allah تعالى Aridhie Amali hiyo.....	379
Utajo wa Makureishi Kujenga Upya Al-Kaabah.....	384
Mvutano Katika Kuweka Jiwe Jeusi Mahali Pake.....	386
Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما, Ajenga Al-Ka'bah Kama Alivyotaka Mtume ﷺ.....	387
Mhabeshi Ataivunja <i>Al-Ka'bah</i> kabla ya Kiyama.....	390
Dua ya <i>Al-Khalil</i>	391
Maana ya <i>Manasik</i> (Ibada).....	393
Ibrahim عليه السلام Anamuomba Allah تعالى Amlete Mtume.....	394
Maana ya <i>Al-Kitab Wal – Hikmah</i>	396
Haachi Mila ya Ibrahim عليه السلام Isipokuwa Mpumbavu.....	397
Kudumu na Tawhid (Kumpwekesha Allah تعالى) Mpaka Kufa.....	401
Usia wa Yaaqub عليه السلام kwa Watoto Wake Alipofikwa na Kifo.....	402
Muislam Anaamini Yote Yaliyoteremshwa na Allah تعالى.....	406
Kubadilishiwa Qiblah:.....	415
Ubora wa Umma wa Muhammad ﷺ.....	419
Hikima ya Kubadilishwa Qiblah.....	422
Hukumu ya Kwanza Kufutwa katika Qur'an ni Mabadiliko ya Qiblah.....	426
Hivi Qiblah ni Ka'aba yenyewe au Mwelekeo wa Mahali Ilipo?.....	427
Hukumu ya Kubadilishwa Qiblah Mayahudi walikuwa wanaifahamu.....	427
Ukorofi na Ukafiri wa Mayahudi.....	428
Mayahudi Waliujua Ukweli wa Mtume ﷺ Lakini Waliuficha.....	430
Kila Umma Una Qiblah.....	432
Kwa Nini <i>Naskh</i> Mabadiliko ya Qiblah Yamekaririwa Mara tatu?.....	433
Hekima ya Kubadilishwa (<i>Naskh</i>) Qiblah.....	434
Utume wa Muhammad ﷺ ni Neema Kubwa ya Kumkumbuka.....	436
Ubora wa Subira na Sala.....	440
Uhai wa Waliokufa Wakiwa Mashahidi.....	441
Subira ya Muumini Kutokana na Mateso Humfanya Alipwe Thawabu.....	443
Ubora wa Kurejea kwa Allah تعالى Wakati wa Msiba (<i>Istirjaa</i>).....	445
Sababu ya Allah تعالى kusema Si kosa Kufanya Saayi.....	447
Hukumu ya <i>Sa'i</i> (Kuenda matiti) baina ya <i>As-Safa</i> na <i>Al-Marwa</i>	449
Laana ya Milele kwa Wanaoficha Sheria za Dini.....	452
Ruhusa ya Kuwalaani Makafiri.....	454
Uthibitisho wa <i>Tawhid</i>	457
Hali za Washirikina Duniani na Akhera.....	460
Amri ya Kula Vllivyohalalishwa.....	465
Tabia ya Washirikina inatokana na Kuiga.....	468
Kafiri ni kama Hayawani.....	469
Amri ya Kula Vyakula vya Halali.....	470

Vilivyoharamishwa vinaruhusiwa kwa wenye Dharura.....	473
Shutuma kwa Mayahudi kwa kuficha yaliyoteremshwa na Allah <small>تعالى</small>	476
Mjumuiiko wa Wema.....	481
Sharia ya Kisasi na Ubainifu wa Maslahi Yaliyomo ndani yake.....	487
Ndugu wa Aliyeuliwa wana Hiari ya Mambo Matatu.....	489
Faida ya Sheria ya Usawa na Hekima yake.....	491
Amri ya Kutoa Wasia kwa Wazazi Wawili na Jamaa.....	493
Wasia ni kwa Jamaa wasio na Haki ya Kurithi.....	494
Wasia lazima uzingatie haki.....	495
Ubora wa kufanya uadilifu katika wasia.....	496
Amri ya Kufunga.....	497
Hatua mbalimbali za Funga.....	499
Fidiya ya kutofunga kwa wazee na wagonjwa.....	500
Utukufu wa Ramadhani na Kuteremshwa kwa Qur'an.....	502
Utukufu wa Qur'an.....	502
Kufaradhiwa kwa Funga ya Ramadhani.....	503
Hukumu kadhaa kuhusu Funga ya Safari.....	504
Ni wepesi wala hakuna mazito.....	505
Kumdhukuru Allah <small>تعالى</small> wakati inapotimia Ibada.....	506
Allah <small>تعالى</small> Anasikia dua za Waja wake.....	508
Dua hupokelewa na h akuna inayopotea	509
Dua za watu wa aina tatu hazikataliwi	510
Kula, kunywa na kujamiiana vinaruhusiwa usiku wa Ramadhani.....	512
Mwisho wa wakati wa Kula Daku.....	514
Sunnah ya kula Daku na wakati wake.....	516
Hapana Ubaya kwa Mwenye Janaba Kufunga.....	518
Funga huisha pale jua linapozama.....	519
Kuharamishwa kwa funga ya mfululizo (<i>Wisal</i>).....	520
Hukumu za Itikafu.....	521
Rushwa imekatazwa na ni Haramu	525
Hukumu ya Kadhi (Hakimu, Jaji n.k) Haihalalishi cha Haramu.....	525
Suala la miezi Miandamo.....	526
Kipimo cha Wema Kizingatiwe kwa Kumchamungu.....	527
Amri ya kupigana na wale wanaowapiga.....	530
Makatazo ya Kuvuka Mipaka katika Ulipizaji Kisasi.....	531
Ushirikina ni mbaya kuliko kuua.....	532
Uharamu wa vita katika maeneo matakatifu.....	532
Amri ya kupigana ili pasiwe na fitnah.....	535
Imeharamishwa kupigana katika miezi mitukufu.....	538
Amri ya Kutoa kwa Ajili ya Allah <small>تعالى</small>	540
Amri ya kutimiza Hajj na Umrah.....	543

Endapo Mtu Atazuiwa Akiwa Njiani, Atachinja Hapohapo.....	545
Yeyote atakayenyoa kichwa chake akiwa Katika Nia ya Hijja.....	549
Ubainifu wa <i>Hijja</i> ya <i>Tamattui</i>	550
Yeyote Anayefanya <i>Tamattui</i> Lazima Afunge Siku Kumi Ikiwa Hana.....	551
Wakazi wa Makka hawaruhusiwi kufanya <i>Tamattui</i>	554
Wakati wa kuhirimia Hija.....	555
Miezi ya Hajj.....	557
Kuharamishwa kwa tendo la ndoa kwa aliyehirimia Hajj.....	558
Kuharamishwa kwa Ufuska wakati wa Hajj.....	559
Uharamu wa kubishana wakati wa Hajj.....	561
Kushajiisha katika Kutenda kheri na Kuandaa Zawadi ya <i>Hija</i>	561
Zawadi ya Safari ya Kwenda Nayo Akhera.....	562
Kufanya biashara wakati wa Hija:.....	563
Kusimama Arafat	564
Muda wa kuondoka Arafat na Muzdalifah.....	566
<i>Al-Masha'r Al- Haram</i> (Maeneo Matukufu).....	567
Amri ya kusimama na kuondoka Arafat.....	568
Amri ya kuomba maghufira (Msamaha) na dua zake.....	569
Amri ya kumdhukuru Allah تعالى na kuomba maisha mema.....	571
Kumdhukuru Allah تعالى katika siku za Tashriq	575
Maelezo ya siku zinazohisabiwa.....	577
Tabia na hali za Wanafiki.....	579
Miongoni mwa sifa za Mnafiki ni kukataa kupokea Nasaha.....	583
Miongoni mwa sifa za Muumini mtiifu ni kutafuta radhi za Allah تعالى	584
Imefaradhihwa kuingia katika Uislam kwa ukamilifu wake.....	586
Msisitizo wa kutokuchelewa kusilimu (kutamka Shahada).....	588
Adhabu kwa kubadilisha neema za Allah تعالى na kuwakejeli waumini.....	592
Kubishana baada ya kuona ishara zilizo wazi ni alama ya ujeuri.....	595
Ushindi na kuingia peponi havipatikani isipokuwa baada ya kufaulu.....	598
Kina nani wanastahiki Nafaka	602
Kuwajibishwa kwa Jihadi.....	603
Kikosi cha <i>Nakhlah</i> na Sheria ya Kupigana	605
Kuharamishwa pombe ' <i>Khamr</i> ', hatua kwa hatua.....	612
Amri ya Kutoa Sadaka kwa Kilichozi Katika Mali.....	614
Kutunza mali za mayatima.....	616
Kuharamishwa Ndoa na Washirikina Wanaume na Wanawake.....	618
Makatazo ya kumwingilia mwanamke mwenye Hedhi.....	622
Uharamu wa Kulawiti	625
Sababu Iliyofanya Kushuka Kauli ya Allah تعالى	625
Makatazo ya kuapa kuacha kufanya amali njema.....	631
Viapo vya <i>Laghw</i> (Upuuzi).....	633

Kiapo cha <i>Iy'laa</i> na Hukumu zake.....	636
Ubainifu wa Eda ya mwanamke aliyeachwa.....	638
Maana ya <i>Al-Qur'uu</i>	638
Kauli ya mwanamke kuwa yupo hedhini au katika tohara	639
Katika kipindi cha <i>idda</i> , mume ndie mwenye haki	640
Haki za mume na mke.....	640
Daraja ya wanaume juu ya wanawake.....	641
Kwa nini talaka ni tatu tu na talaka rejea ni ipi? na <i>Bain</i> ni ipi?.....	643
Makatazo juu ya kuomba kurejeshewa mahari.....	644
Ruhusa ya Kujivua Mwanamke katika Ndoa (<i>khulu'u</i>) na Kurejesha Mahari.....	645
<i>Iddah</i> ya <i>Khulu'u</i> - Eda ya Mke Aliyekomboa kwa Mumewe.....	647
Kuchupa Mipaka ya Allah تعالى ni Dhulma.....	647
Kutoa Talaka Tatu kwa Pamoja ni Haramu.....	647
Hakuna rejea baada ya Talaka ya Tatu.....	648
Wamelaaniwa wahalalishaji na wahalalishiwa.....	649
Ni wakati gani Mke Aliyeachwa Talaka Tatu anahalalika	650
Amri ya kumfanyia wema Mke aliyeachwa.....	653
Makatazo kwa Walii wa Mwanamke Aliyeachwa	655
Ndoa Haisihi Bila Kuwepo Walii (Msimamizi) wa Mwanamke.....	655
Madhumuni ya Kuteremshwa Ayah (2:232).....	656
Muda wa kunyonyesha usizidi miaka miwili.....	668
Kunyonyesha baada ya miaka miwili.....	660
Kunyonyesha kwa malipo ya fidia	660
Hapana <i>Dharar</i> (madhara) au <i>Dhirar</i> (Kulipiza Kisasi).....	661
Mtoto kuachishwa ziwa kufanyike kwa maridhiano.....	662
Eda ya Mjane.....	664
Hekima ya kufaradhiwa Kukaa Eda ya kufiwa.....	666
Eda ya mjakazi aliyefiwa na bwana wake.....	666
Uwajibu wa Msiba wakati wa Eda ya kufiwa.....	667
Kuruhusiwa posa kwa ishara wakati wa Eda, na kukatazwa ndoa.....	669
Talaka kabla ya kufanyika tendo la ndoa.....	673
<i>Mut'ah</i> (zawadi) ya Talaka.....	673
Mke hupewa nusu ya mahari iwapo atachwa kabla ya kuingiliwa.....	674
Sala ya katikati.....	678
Ushahidi kuwa Sala ya Alasiri ni Sala ya katikati.....	678
Imekatazwa Kuzungumza Wakati wa Sala.....	681
Sala ya Khofu.....	682
Amri ya kutimiza Sala wakati wa amani.....	683
Kufutwa kwa Aya hii 2:240.....	685
Uwajibu wa <i>Mut'ah</i> (Zawadi) wakati wa kutaliki.....	689
Kisa cha watu hawa waliokufa.....	691

Kukwepa Jihadi Hakubadilishi Hatima ya Mtu.....	693
Karadha Njema na Malipo Yake.....	694
Kisa cha Mayahudi Ambao Walitaka Wateuliwe Mfalme.....	697
Allah تعالی Amewatukuza Baadhi ya Mitume Juu ya Wenzao.....	709
Ubora wa <i>Ayatul-Kursiyyu</i>	712
Jina Kuu la Allah تعالی limo katika <i>Ayat Al-Kursi</i>	715
Hapana kulazimisha katika Dini.....	721
Tawhid ni kishikio madhubuti.....	722
Mjadala Kati ya Nabii Ibrahim <i>Khalilul-Llah</i> عليه السلام na Numrud.....	727
Kisa cha Uzayr.....	730
Ibrahim عليه السلام Alimuomba Allah تعالی Amuoneshe	733
Majibu kwa Maombi ya Ibrahim <i>Al-Khalil</i> عليه السلام	734
Malipo ya kutoa kwa Ajili ya Allah تعالی.....	737
Makatazo ya Kutoa Sadaka kwa Masimango na Masimbulizi.....	739
Mfano wa Amali Mbaya Zinavyoharibu Amali Njema.....	745
Kuhimizwa Kutoa Mali Halali kwa Ajili ya Allah تعالی.....	748
Sheitani Huwatia Shaka Wasiwasi na Khofu.....	750
Maana ya <i>Al-Hikmah</i>	752
Fadhila za Kudhirisha Au Kuficha Sadaka.....	755
Kuwapa Sadaka Washirikina.....	757
Wanaostahiki Zaidi Kupatiwa Sadaka.....	759
Kuwasifu Wenye kutoa Sadaka.....	762
Ubaya wa Kula Riba.....	765
Allah تعالی Haibariki Riba.....	771
Allah تعالی Huzilea (Huziongeza) Sadaka.....	772
Allah تعالی Hawapendi Makafiri Wafanyao Dhambi.....	773
Kuwasifu Wanaomshukuru Allah تعالی.....	773
Amri ya Kuwa Wachamungu (<i>Taqwa</i>) na Kuiepuka Riba.....	774
Riba ni Kutangaza Vita Dhidi ya Allah تعالی na Mjumbe Wake ۞.....	775
Kuwahurumia Wadaiwa Wenye Matatizo ya Kifedha.....	776
Umuhimu wa Kuandikiana Miamala Yenye Kuwekewa Muda.....	781
Mashahidi Lazima Wahudhurie Imla ya Mikataba.....	785
Ubainifu wa Rehani.....	791
Je, Waja Wataulizwa kwa Yale Waliyoyaficha Katika Nyoyo Zao?.....	794
Hadithi juu ya Utukufu wa Ayah Mbili Hizi.....	799
Tafsiri ya Aya Mbili za Mwisho za Surat <i>Al-Baqarah</i>	801

Mwongozo Muhimu Kuhusu Usahihi wa Mapokezi na Nukuu katika Tafsiri ya Ibn Kathir.

Mapokezi yanayohusishwa na Masahaba wa Mtume ﷺ

Mapokezi yanayohusishwa na Masahaba wa Mjumbe wa Allah kwa kawaida yanatumika kama maelezo ya ziada ya maana ya Qur'an. Ama kwa nukuu ambazo Ibn Kathir amezitaja, kwa kupitia nukuu hizi zinaweza au kutoweza kuhusishwa na Masahaba. Popote patapotajwa kuwa mmoja wao alisema jambo, na kauli hiyo ikakhitalafiana na nyingine iliyo halisi, basi kauli ya aina hiyo haiwezi kuchukuliwa kuwa ni ushahidi badala ya ile inayojulikana kuwa ni kauli sahihi. Taarifa ya ziada kuhusu suaia hili inapatikana katika Utangulizi wa Ibn Kathir رحمه الله تعالى.

Isnadi ya Upokezi Isiyo Kamili

Ifuatayo ni orodha ya kawaida ya silsila za usimulizi isiyokamilika ambayo mara nyingi Al-Hafidh Ibn Kathir رحمه الله تعالى ameinukuu.

-Ali bin Ali Talhah (Al-Walibi) aliripoti kuwa Ibn Abbas alisema.....

-(Atiyah) Al-Awfi aliripoti kuwa Ibn Abbas alisema

-Adh-Dhahhak kutoka kwa Ibn Abbas.

-As-Suddi aliripoti kutoka kwa Abu Malik na Abu Salih kutoka kwa Ibn Abbas, Ibn Masud na (au) baadhi ya watu miongoni mwa Masahaba.

-Al-Hasan Al-Basri akiripoti kutoka au kuhusu Mtume ﷺ

-Qatadah akiripoti kutoka au kuhusu Mtume ﷺ

Masimulizi yote yanayokuja kutokana na silsila hizi siyo halisi kwa mujibu wa *Ulumul Hadith*. Maana zake, hata hivyo, zinaweza kuwa sahihi kama zilivyofahamika katika maandishi halisi, na kwa sababu hii ndiyo maana hurejewa. Mapokezi kutoka kwa Wafuasi wa Maswahaba na Wale Wanaowafuata.

Ifuatayo ni orodha ya watu ambao hawakumwona Mtume ﷺ, lakini wanaripoti kutoka kwa Masahaba wa Mtume ﷺ. wakati kila mara wananukuliwa katika *Tafsiri*. Ripoti zinazotokana nao zinatumiwa na Ibn Kathir رحمه الله تعالى kama ziada

ya kuunga mkono ili baadhi ya mambo yaeleweke. Nukuu hizo zinaweza kuwa au kutokuwa zimehusiana nao kwa usahihi. Popote itakapotajwa kuwa mmoja wao alisema jambo, na kauli hiyo ikakhitilafiana na kauli nyingine sahihi, hivyo kauli za aina hiyo haziwezi kuchukuliwa kuwa ushahidi halisi. Orodha yenyewe ni hii ifuatayo:-

Abu Al-Aliyah, Said bin Jubayr, Said bin Al-Musayyib, 'Ata (bin Abu Rabah), 'Ata Al-Khurasani, Muqatil bin Hayyaan, Ar-Rabi bin Anas, Ash-Sha'bi, Qatadah, Mujahid, Ikrimah, Ad-Dhahhak, Abdur Rahman bin Zayd bin Aslam (Ibn Zayd), Ibn Jurayj.

Wanazuoni Wengine Baada ya Masahaba,

Wafuatao ni baadhi ya wanazuoni ambao Ibn Kathir رحمه الله تعالى anawanukuu kila mara. Kwa kuwa wanazuoni hao hawafahamiki kwa wasomaji wa Kiingereza wa kawaida, unatakiwa kuchukua hadhari kuwa kauli zao peke yao kuhusu Mtume ﷺ, Masahaba zake, au mazingira yanayohusu kushushwa kwa Qur' an, hayawezi kuwa na uzito sawa na masimulizi halisi. Waqii, Sufyan Ath-Thawri, Muhammad bin Is-haaq, Ibn Atiyah, Ibn Abu Hatim, Ibn Jarir (At-Tabari).

Wasifu wa Ibn Kathir رحمه الله تعالى

Umeandikwa na Mheshimiwa Shaykh Abdul- Qadir Al-Arna'ut, Allah Ampe Ulinzi.

Yeye ni Imamu anayeheshimika, Abu Al-Fida, Imad Ad-Din Ismail bin Umar bin Kathir Al-Quraishi Al-Busrawi - asili yake Busra; alipata elimu yake na makazi yake huko Damascus.

Ibn Kathir alizaliwa katika jiji la Busra mwaka 701 Hijriya, 1302 Miyadiya. Baba yake alikuwa khatibu wa Ijuma, Kijiji cha Mijdal, lakini alifariki dunia Ibn Kathir alipokuwa na umri wa miaka minne. Kaka yake Ibn Kathir, Shaykh Abdul - Wahhab, alimlea na kumfundisha mpaka alipohamia Damascus mwaka 706 H, alipokuwa na umri wa miaka mitano.

Walimu wa Ibn Kathir رحمه الله تعالى:

Ibn Kathir رحمه الله تعالى alisoma *Fiqh* kwa Burhan Ad-Din, Ibrahim bin Abdur Rahman Al-Fizari رحمه الله تعالى aliyejulikana kama Ibn Al-Firkah (aliyefariki 729H).

Ibn Kathir رحمه الله تعالى alisikiliza Hadith kutoka kwa Isa bin Al-Mutim, Ahmad bin Abu Talib, (Ibn Ash- Shahnah) (aliyefariki 730 H), Ibn Al-Hajjar رحمه الله تعالى (aliyefariki 730 H), na Msimulizi wa Hadith wa Ash-Sham (leo Syria na maeneo yanayozunguka); Baha Ad-Din Al-Qasim bin Muzaffar bin Asakir رحمه الله تعالى (aliyefariki 723 H) na Ibn Ash- shirazi رحمه الله تعالى, Is-haaq bin Yahya Al-Ammuddi رحمه الله تعالى pia alijulikana kama Afif Ad-Din, Shaykh wa Zahiriyyah aliyefariki 725 H, na Muhammad bin Zarrad رحمه الله تعالى. Aliendelea na Jamal Ad-Din رحمه الله تعالى, Yusuf bin Az-Zaki Al-Mizzi رحمه الله تعالى aliyefariki 742H, alifaidika na elimu yake na pia alimuoa binti yake. Aidha alisoma na Shaykh *Ai-Islam*, Taqi Ad-Dill Ahmad bin Abdul Halim bin Abdus-Salam bin Taymiyyah aliyefariki 728 H. Aidha alisoma na Imam Hafidh na mwana historia Shams Ad- Din, Muhammad bin Ahmad bin Uthman bin Qayrnaz Adh-Dhahabi رحمه الله تعالى, aliyefariki 748 H. Pia Abu Musa Al-Qarafai, Abu Al-Fath Ad-Dabbusi رحمه الله تعالى na Ali bin Umar As-Suwani رحمه الله تعالى na wengine waliompa ruhusa kuifundisha elimu aliyojifunza Misri.

Katika kitabu chake, *Al-Mujam-Mukhtas*. Al-Hafidh Adh-Dhahabi رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Kathir رحمه الله تعالى alikuwa, "Imamu, mwanachuoni wa *Fiqh*, bingwa wa Hadith, *Faqlh* mashuhuri na mwanachuoni wa *Taftir* ambaye aliandika vitabu vingi vyenye manufaa."

Zaidi ya hayo, katika kitabu, *Ad-Durar Al-Kaminah*. Al-Hafidh Ibn Hajar Al-Asqalani رحمه الله تعالى alisema, 'Ibn Kathir رحمه الله تعالى alishughulikia somo la Hadith katika maeneo ya maandiko na silsila ya Wasimulizi. Alikuwa na kumbukumbu nzuri, vitabu vyake vilikuwa maarufu wakati wa uhai wake, na watu walifaidika navyo baada ya kufariki dunia."

Aidha, mwana historia maarufu, Abu Mahasin, Jamal Ad-Din Yusuf bin Sayf Ad-Din (Ibn Taghri Bardi رحمه الله تعالى), aliserna katika kitabu chake, *Al- Manhal As-Swafi' wal Mustwawf*, "Yeye ni Shaykh, Imam, mwanachuoni mkubwa Imad Ad-Din Abu Al-Fida. Alisoma nyanja nyingi na alikuwa hodari kujifunza na kuandika. Alijifunza elimu mbalirnbali, aliandika vitabu, alifundisha, alisimulia Hadithi na kuziandika. Alikuwa na elimu ya kutosha katika nyanja za Hadithi, *Tafsir*, *Fiqh* na lugha ya Kiarabu na kadhalika. Alikuwa akitoa fatwa na alikuwa akifundisha mpaka alipofariki, Allah Amuwie Radhi. Alifahamika kwa umakini, wake na uandishi, na bingwa wa Historia, Hadith na *Tafsir*.

Wanafunzi wa Ibn Kathir رحمته الله تعالى:

Wanafunzi wa Ibn Kathir ni wengi akiwemo Ibn Hajji, na alimuelezea Ibn Kathir رحمته الله تعالى kuwa, "Alikuwa na kumbukumbu nzuri ya maandiko ya Hadith. Alikuwa pia na elimu kuhusu wasimulizi na uhalisi wao, watu wa rika lake na walimu wake wanakiri kuwa alikuwa na sifa hizo. Kila wakati nilipomtembelea nilijifunza kitu kipya." Aidha, Ibn Al-Imad Al-Hanbali alisema katika kitabu chake, *Shadharat Adh-Dhahab fy Akhbari man Dhahaba*, "Ni mtu maarufu, Hafidh Imam Ad-Din, ambaye kumbukumbu yake ilikuwa nzuri sana, hakuwa msahaulifu alikuwa na ufahamu mzuri na mcheshi na alikuwa na maarifa mazuri katika lugha ya Kiarabu na alikuwa akishiriki katika midahalo ya lugha ya Kiarabu." Pia Ibn Habib alimuelezea Ibn Kathir رحمته الله تعالى. "Aliisikiliza elimu na akaikusanya na akaandika vitabu mbalimbali. Aliyafariji masikio kwa fatwa zake na alisimulia Hadithi na akawanufaisha wengine. Nyaraka zenye Fatwa zake zilipelekwa kwenye majimbo mbalimbali yaliyokuwa yakiongozwa na *Shariah* za Kiislam. Zaidi ya hivyo alikuwa mtu makini na mwandishi.

Vitabu vya Ibn Kathir رحمته الله تعالى:

1. Moja kati ya vitabu vyake vikubwa ambavyo Ibn Kathir رحمته الله تعالى aliandika ilikuwa *Tafsir* yake ya Qur'an Takatifu, ambayo ni moja kati ya *Tafsir* zilizotegemea masimulizi (ya Hadith, *Tafsir* ya Masahaba n.k). *Tafsir* ya Ibn Kathir ilichapishwa mara nyingi na wanazuoni kadha wameandika muhtasari wake.
2. Mkusanyiko wa Historia unaoitwa *Al-Bidayah*, ambayo ilichapishwa katika Juzuu 14 kwa jina la *Al-Bidayah Wan-Nihayah*, na ina Hadithi kuhusu Mitume na mataifa yaliyopita, *Sirah* ya Mtume na Historia ya Uislamu mpaka zama hizi. Aliongeza kitabu kingine *Al-Fitan*, juu ya Alama za Kiyama na mambo ya Akhera.
3. *At-Takmil fi Ma'rifat Ath- Thiqai wa Adh-Dhuafa wal Majahil* ambacho Ibn Kathir رحمته الله تعالى alikusanya kutoka vitabu vya Mashaykh wake wawili, Al- Mizzi رحمته الله تعالى na Adh-Dhahabi; *Al-Kamal na Mizan Al-I'tidal*. Aliongeza faida nyingi kuhusu somo la *Al-Jarh na At-T'adil*.
4. *Al-Hadi was-Sunan fi Ahadith Al-Masanid was-Sunan*, ambayo pia inajulikana kwa, *Jami Al-Masanid*. Katika kitabu hiki Ibn Kathir رحمته الله تعالى alikusanya masimulizi ya Imam Ahmad bin Hanbal, Al-Bazzar, Abu Ya'la Al-Mawsili, Ibn

Abi Shaybah na kutoka makusanyo sita ya Hadithi: Sahih mbili (*Al-Bukhari na Muslim*) na *Sunan Nne* (*Abu Dawud, At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah*). Ibn Kathir رحمه الله تعالى alikigawanya kitabu kwa mujibu wa maeneo ya *Fiqh*.

5. *Tabaqaat Ash-Shafiyah*, kitabu cha wastani ambacho pia kinaeleza wasifu mzuri wa Imam Ash-Shafi.

6. Ibn Kathir رحمه الله تعالى aliandika marejeo ya Hadith za *Adillat At-Tanbih* kwa madhehebu ya Shafi katika *Fiqhi*.

7. Ibn Kathir رحمه الله تعالى alianza kuandika maelezo juu ya *Sahih Al-Bukhari* lakini hakumaliza.

8. Alianza kuandika juzuu kubwa juu ya *Ahkam* (Sharia), lakini alimaliza mpaka ibada za Hajj.

9. Aliandika Muhtasari wa *Al-Bayhaqi - Al-Madkhal*. Katika Vitabu hivi vingi havikuchapishwa.

10. Aliandika Muhtasari wa *Um Al-Hadith* cha Abu Amr bin As-Salah na akakiita *Mukhtasar Ulum Al-Hadith*, Shaykh Ahmad Muhammad Shakir, *Multaddith* wa Kimisri, alikichapisha kitabu hiki pamoja na maelezo na akakiita, *Al-Ba'ithu Al-Hathith fi Sharh Mukhtasar Ulum Al-Hadith*.

11. *As-Sirah Al-Nabawiyyat*, ambayo imo ndani ya kitabu chake - *Al-Bidayah*, na vyote vimechapishwa.

12. Aliandika utafiti juu ya Jihadi katika kitabu kilichoitwa *Al-Ijtihad fi Talabi Al-Jihad*, ambacho kilichapishwa mara kadha.

Kifo cha Ibn Kathir رحمه الله تعالى:

Al-Hafidh Ibn Hajar Al-Asqalani رحمه الله تعالى alisema, "Ibn Kathir رحمه الله تعالى alipofuka macho kabla ya kufariki. Alikufa mwaka 774/Hijriya/1373 Miyladiya, jijini Damascus, katika kijiji cha Al-Mahrusa." Allah Amrehemu Ibn Kathir رحمه الله تعالى na Amfanye mmoja wa wakazi wa Peponi. *Amin*.

Utangulizi

Utangulizi wa Ibn Kathir

Shukurani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, ambaye ameanza Kitabu Chake kwa Kujifakharisha kwa Kusema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾ مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٣﴾

“Shukurani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mala wa Walimwengu wote, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu, Mwenye Kumiliki siku ya malipo.” (1:2-4)

1. Ambaye Alianza Kuumba kwake kwa *Hamd* (kwa Kujisifu) kwa Kusema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ۚ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ
يَعْدِلُونَ ﴿١﴾

“Sifa zote njema zinamthubutikia Mwenyezi Mungu Aliyeumba mbingu na ardhi na Akafanya giza na nuru. Na juu ya haya wale waliokufuru wanamfanya Mola wao sawa (na vijiungu vya uongo).” (6:1)

2. Na Alimalizia kwa Kujisifu baada ya Kutaja hatma ya watu wa Peponi na watu wa Motoni,

وَتَرَى الْمَلَائِكَةَ حَافِينَ مِنْ حَوْلِ الْعَرْشِ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ ۖ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ
وَقِيلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٥﴾

“Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa Arshi (Kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu), wakimtukuza na kumsifu Mola wao. Na pakahukumiwa baina yao kwa haki na pakasemwa: “Sifa zote Njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.” (39:75)

Na kwa ajili hiyo Allah تعالی Akasema,

وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُولَى وَالْآخِرَةِ ۗ وَلَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٧٠﴾

“Naye Ndiye Mwenyezi Mungu hakuna aabudiwaye kwa Haki ila Yeye Sifa zote Njema mwanzoni na mwishoni, duniani na Akhera ni Zake Yeye tu. Na Hukumu pia ni Yake, nanyi mtarudishwa Kwake (kadhalika).” (28:70)

Basi, Shukurani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu duniani na akhera (mwanzoni na mwishoni) kwa Alivyoviumba na Atakavyoviumba. Mwenyezi Mungu Ndiye Anayestahiki kushukuriwa kwa yote hayo, kama mtu anayesali Anavyosema, *“Ewe Mala wetu, Sifa Njema zote ni zako zijae ujazo wa mbingu na ardhi na ujazo wa kila kitu kingine unachokitaka baada ya hizo.”*

Shukurani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye Aliwatuma wajumbe Wake ambao Amewaeleza kama ni:

مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَعَلَّ يُكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ

“Wenye kutoa habari nzuri (kwa watu wema) na wanaowaonya (wabaya), ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya (kuletwa hawa) Mitume.” (4:165)

Na Alimalizia kwa Kumtuma Mtume *Ummu* (asiyejua kusoma wala kuandika) Mwarabu wa Makka, ambaye anaongoza kwenye njia safi ya njia zote. Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ kwa viumbe vyake wote, Majini na binadamu, tokea utume wake ulipoanzia mpaka kitaposimama kiyama. Kama Alivyosema Allah تعالى,

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ ۗ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ

وَكَلِمَاتِهِ ۗ وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿٢١٣﴾

“Sema (ewe Nabii Muhammad): “Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote; (Mungu) Ambaye Allah Ufalme wa mbingu na Ardhi ni Wake, hakuna aabudiwae (kwa haki) ila Yeye; Yeye Ndiye Ahuishaye na Ndiye

Afishaye. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, aliye Nabii Ummy, (asiyejua kusoma wala kuandika) ambaye humuamini Mwenyezi Mungu na Maneno Yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.” (7:158)

Na Allah تعالى Amesema,

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“(Imefunuliwa kwangu) ili kwa hiyo nikuonyeni nyinyi na kila imfikiaye.” (6:19)

Basi atakayefikiwa na Qur’an hii awe ni Mwarabu au asiye mwarabu, mweusi au mwekundu, binaadamu au Jini, Qur’ an hii ni onyo kwake. Ndiyo sababu Allah تعالى Akaserna,

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالِنَارُ مَوْعِدُهُ

“Na watakoikataa katika makundi (ya maadui), basi moto ndio mahali pa miadi yao.” (11:17)

Kwa hiyo yeyote atakayeikanusha Qur’ an miongoni mwa hao tuliowataja, hivyo basi, kwa mujibu wa Allah تعالى, makazi ya watu hao yatakuwa Motoni. Allah تعالى Amesema,

فَذَرْنِي وَمَنْ يُكذِّبْ هَذَا الْحَدِيثِ سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾

“Niache na wanaokadhibisha Hadithi hii; (Qur’an). Tutawavuta kidogo kidogo katika adhabu yetu kwa mahali wasipopajua.” (68:44)

Aidha Mtume ﷺ amesema,

«بُعِثْتُ إِلَى الْأَحْمَرِ وَالْأَسْوَدِ»

“Nimetumwa kwa wekundu na weusi”¹

Mujahid alifafanua kwa kuserna, “Maana yake ni binadamu na majini.” Ahmad (5:145) Hivyo, Muhammad ﷺ ni mjumbe kwa wanadamu na majini, akiwasilisha

¹Muslim: 1/343

wahyi alioupokea kutoka kwa Allah تعالى, uliyomo ndani ya Kitabu Chake Kitakatifu, Kitabu ambacho:

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤١﴾

“Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye Hekima, Ahimidiwaye.” (41:42)

Amri ya kufahamu qur’an

Hakika Mtume ﷺ aliwajulisha wao kuwa Qur’an inatoka kwa Allah تعالى, Yeye ndiye aliyewataka wao waifahamu Qur’an. Allah تعالى amesema:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ﴿٤٢﴾

“Hebu hawaizingatii hii Qur’ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.” (4:82)

Kadhalika Allah تعالى amesema:

كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبْرَكٌ لِّيَدَّبَّرُوا آيَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٣٨﴾

Na hiki Kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili. (38:29)

Kadhalika Allah تعالى amesema:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٤٧﴾

“Je! Hawaizingatii hii Qur’ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?” (47:24)

(Lilo wajibu) kwa wanazuoni kufafanua maana ya maneno ya Allah تعالى na kuifasiri na kutafuta maana hayo katika vyanzo vyake, wanazuoni wanatakiwa kujifunza maana hayo na kuwafundisha wengine. Kama Allah تعالى Anavyosema:

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَاءَ

ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَوْا بِهِ مِمَّا قَلِيلًا فَبُئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿٤٧﴾

“Na (wakumbushe) Mwenyezi Mungu: Alivyofunga ahadi na wale waliopewa kitabu (Akawaambia), Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtaficha. Lakini walikitupa nyuma ya migongo yao na walikhitari mali chache (ya kidunia kuliko walivyoamrisha kuyafuata katika kitabu hicho). Basi ubaya ulioje kwa kuhitari kwao huko.” (3:187)

Na Allah تعالى Amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَٰئِكَ لَا خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨٧﴾

“Hakika wale wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa ajili ya thamani ndogo ya kilimwengu hao ndio hawatakuwa na sehemu ya kheri katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu Hatasema nao (maneno mazuri) wala Hatawatazama (Jicho la rehma) siku hiyo ya kiyama, wala Hatawatakasaa (madhambi yao), nao watapata adhabu iumizayo.” (3:77)

Allah تعالى Aliwakosoa watu waliopewa Kitabu (Mayahudi na Wakristo) ambao walikuwapo kabla yetu kwa kukataa kitabu cha Allah تعالى kilichofunuliwa kwao, na wakaendekeza mambo ya kidunia na wakaachana na kushikamana na waliyoamrisha katika Kitabu cha Allah تعالى, Sisi Waislamu kwa hiyo tunatakiwa kujuzuia kufanya yale Allah تعالى Aliyowakosoa kwayo Watu wa Kitabu na kutekeleza Yale Aliyotuamrisha; pia tunatakiwa kujifunza na kukufundisha Kitabu cha Allah تعالى kilichoteremshwa kwetu, kukifahamu na kuwafahamisha watu wengine.

Allah تعالى Amesema:

﴿١٨٨﴾ أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿١٨٩﴾ أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَمِيُّ الْأَرْضِ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٩٠﴾

“Je Wakati haujafika tu kwa wale walioamini kwamba nyoyo zao zinyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kwa mambo ya haki yaliyoteremka? Wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu zamani; (Mayahudi na Manasara), na muda wao (wa kuondokewa na Mitume) ukawa mrefu; kwa hivi nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa waasi. Jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu Huihuisha ardhi baada ya mauti yake. Bila shaka Tumekubainishieni alama (za Uweza Wetu wa Kuweza Kufufua) ili mpate kufahamu,” (57:16-17)

Hivyo Allah تعالى Anapoitaja Aya hii (57:17) baada ya Aya iliyotangulia Anatumzindua katika ukweli kuwa, kama Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa. Pia Anailainisha mioyo yetu kwa imani, na Kutupa mwongozo baada ya mioyo hiyo kuwa migumu kwa sababu ya kufanya madhambi. Tunamuomba Allah تعالى atupe mwisho mwema. Yeye Ndiye Mwenye Huruma na Mkarimu.

Kanuni za Tafsiri

Endapo mtu atauliza juu ya njia nzuri ya *Tafsiri*, tutamjibu kwamba njia sahihi zaidi ni kutafsiri Qur'an kwa Qur'an yenyewe. Kinachotajwa kwa ujumla (kwa kufupishwa) katika sehemu moja ya Qur'an, kwa kawaida hufafanuliwa na sehemu nyingine. Iwapo mtu atakosa tafsiri ya Quran kutoka katika Qur'an basi aangalie kwenye Sunna (Hadithi) kwa sababu Sunna huibainisha Qur'an na kufafanua maana yake. Allah تعالى Amesema,

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ بِمَا أَرْنَاكَ اللَّهُ وَلَا تَكُنَ لِلْخَائِبِينَ

حَصِيمًا ﴿١٠٥﴾

“Hakika Tumekuteremshia Kitabu (hiki) hali ya kuwa kimeshikamana na haki ili upate kuhukumu baina ya watu kama Alivyokufahamisha Mwenyezi Mungu; wala usiwe mwenye kuwatetea wale wafanyao khiyana.” (4:105)

Na Amesema:

وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ إِلَّا لِتُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي اخْتَلَفُوا فِيهِ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ

يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٦﴾

“Na hatukukuteremshia Kitabu: (hiki) isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitilafiana kwayo na (pia kiwe) uongofu na rehema kwa watu wanaoamini.” (16:64)

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٦٤﴾

“ Na Tumekuteremshia mawaidha (Qur’an) ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, na ili wapate kufikiri.” (16:44)

Kwa sababu hii Mtume ﷺ alisema,

«أَلَا إِنِّي أُوتِيتُ الْقُرْآنَ وَمِثْلَهُ مَعَهُ»

“Eleweni Mimi nimepewa Qur’an na mfano wake pamoja nayo,”

Akimaanisha Sunnah. Sunnah vilevile ni ufunuo kutoka kwa Allah تعالى kama ilivyokuwa Qur’an, japokuwa haisomwi (kwa kupewa thawabu) kama Qur’an inavyosomwa. Hivyo Qur’an inafasiriwa na Qur’an yenyewe au na Sunnah. Iwapo haitawezekana kupata Tafsiri ndani ya Qur’an au Sunnah itabidi twende kwenye kauli za Masahaba ambao walikuwa na elimu kubwa ya Tafsiri, kwani wao walizishuhudia hali na matukio yaliyohusiana na Aya za Qur’an. Aidha walikuwa na uwezo mkubwa wa kufahamu, elimu sahihi na uadilifu wa hali ya juu. Hususan wanazuoni na viongozi miongoni mwao, kama vile Makhalfi wanne waongofu na Maimamu waadilifu, na Abdullah bin Masud Imam Abu Ja’far bin Jarir At-Tabari alisimulia kwamba, Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Naapa ya kuwa hapana Mola isipokuwa Allah تعالى! Hapana Ayah iliyoteremshwa kwenye Kitabu cha Allah تعالى isipokuwa najua iliteremshwa wapi na kwa ajili gani. Kwa hakika, Lau ninamjua mtu yeyote anayekijua zaidi Kitabu cha Allah تعالى kuliko mimi, ambaye Kipando kinamfikia, ninge-mwendea.”¹

Aidha miongoni mwa wanazuoni katika Masahaba ni mwanachuoni, bahari ya elimu, Abdullah bin Abbas رضي الله عنهما binamu wa Mtume na mfasiri wa Qur’an, na hayo ni matokeo ya baraka na Dua za Mtume ﷺ, Mtume ﷺ alimwomba Ibn Abbas رضي الله عنهما kwa Mwenyezi Mungu,

¹ Ahmad 4/131)

«اللَّهُمَّ فَفِّهْ فِي الدِّينِ وَعَلِّمَهُ التَّأْوِيلَ»

“Ewe Mwenyezi Mungu mfundishe elimu ya Dini na Tafsiri ya ndani.”¹

Aidha, Ibn Jarir At Tabari رحمه الله تعالى alitoa taarifa kuwa Abdullah bin Masud رضي الله عنه alisema, “Mfasiri bora wa Qur’an ni Ibn Abbas.”² Hadithi hii ina isnadi sahihi ya wapokezi.’ Ibn Mas’ud رضي الله عنه alifariki mwaka wa thelathini na mbili wa Hijrah na Abdullah bin Abbas رضي الله عنه aliishi miaka thelathini na sita baada ya hapo. Unafikiriaje kuhusu elimu ya Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyopata kutoka kwa ibn Mas’ud? Al-A’mash alisema kutoka kwa Abu Wail: Ali alimteua Abdullah bin Abbas رضي الله عنهما kuongoza msimu wa Hijja, Ibn Abbas رضي الله عنهما alihotubu na katika hotuba hiyo alisoma na akatoa maelezo ya *Sural Al-Baqarah* (kwa mujibu wa mapokezi mengine, *Sural An-Nur*) kwa namna ambayo kama Warumi, Waturuki na Daylami wangemsikia basi wote wangesilimu.”³

Hii ndiyo sababu ya kuwa Elimu nyingi aliyokuwa nayo Abdul Rahman As-Suddi Al-Kabir kuhusu *Tafsiri* aliipata kutoka kwa watu hawa wawili; Ibn Masud na Ibn Abbas رضي الله عنهما. Hata hivyo wakati mwingine hutaja yale waliyo-yasimulia kutoka kwa watu waliopewa Kitabu (Waisrail) ambayo Mtume ﷺ aliyaruhusu pale aliposema;

«بَلِّغُوا عَنِّي وَلَوْ آيَةً وَحَدِّثُوا عَنِ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَا حَرَجَ، وَمَنْ كَذَبَ عَلَيَّ مُتَعَمِّدًا فَلْيَتَّبِعْ مَقْعَدَهُ مِنَ النَّارِ»

“Nifikishieni japo kuwa Ayah moja, na simulieni kutoka kwa wana wa Israel, kwani si vibaya kufanya hivyo. Na anayenizuilia uongo kwa makusudi, ajichagulie makazi Motoni.”

Hadithi hii kutoka kwa Abdullah bin Amr رضي الله عنهما ilikusanywa na Bukhari (*Fat’h Al- Bari* 6:572). Abdullah Bin Amr alipata mifuko miwili ya vitabu vya

¹At-Tabari) 1/80.

²Fat’hu Al’Bari 1/205.

³At-Tabar 1/90.

⁴At-Tabar 1/81.

Watu wa Kitabu siku ya Vita vya Yarmuk na akawa akisimulia, kwa mujibu wa ruhusa aliyoifahamu kupitia Hadithi hii.

Hukumu Kuhusu Simulizi za Hadithi za *Israiliyat*.

Simulizi na Hadithi za *Israiliyat* zinatakiwa zitumike kama nyongeza ya ushahidi na siyo kutilia nguvu ushahidi wenyewe. Riwaya za *Israiliyat* zinagawanyika katika mafungu matatu; moja ya mafungu hayo ni lile ambalo tuna uhakika na usahihi wake kwa sababu tuna maandiko yanayohititisha ukweli wake. Fungu la pili, ni kile tunachojua kuwa si sahihi kwa ushahidi wa maandiko yetu. Fungu la tatu ni yale yaliyonyamaziwa, hayapo katika fungu la kwanza wala la pili. Hivyo hatuyaamini wala kuyakanusha, aina hii tunaruhusiwa kuisimulia kwa mujibu wa *Hadithi* tuliyoitaja. Simulizi nyingi za *Israiliyat* hazina faida katika Dini. Mathalan, simulizi ya wana wa Israil zinataja majina na idadi ya watu wa Pangoni (*Al-Kahf*) na rangi ya mbwa wao. Pia huzungumzia mti uliotengenezwa fimbo ya Mtume Mussa عليه السلام, majina ya ndege waliohuishwa na Mtume Ibrahim عليه السلام kwa uweza wa Allah تعالى, sehemu ya ng'ombe iliyotumika kumpigia Myahudi ili afufuke, na aina ya mti ambao Allah تعالى Alizungumza na Mussa عليه السلام kupitia mti huo na vinginevyo ambavyo Allah تعالى Hakuvitolea maelezo ndani ya Qur' an havina umuhimu wowote katika maisha ya kila siku wala ya kidini kwa watu wazima wenye majukumu katika jamii.

Nafasi ya Tafsiri ya *Tabiin*

Unaposhindwa kupata Tafsiri ndani ya Qur'an, Sunnah au kutoka kwa Masahaba, wanazuoni wengi waliangalia Tafsiri ya *Tabiin* (kizazi cha pili cha Uislam) kama Mujahid bin Jabri ambaye alikuwa bingwa katika kutafsiri. Muhammad bin Is-haaq alisimulia kwamba Abban bin Salih alisema kuwa Mujahid alisema, "Niliupitia Msahafu kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما mara tatu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho huku nikimuonyesha na kuuliza maana yake kila Ayah.¹ Aidha, Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abii Mulaykah alisema; "Nilimuona Mujahid akimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu Tafsiri ya Qur' an huku akiwa ameshika mbao zake, na Ibn Abbas رضي الله عنهما akimuambia, "Andika" hadi Mujahid alimuuliza Tafsiri yote.² Ndiyo sababu

¹At-Tabar 1/90.

²(At-Tabari 1/91)

Sufyan Ath-Thawri akisema, “Endapo utapokea Tafsiri kutoka kwa Mujahid basi inakutosha kabisa.”¹

Wanazuoni wa *Tafsiri* wanawajumuisha Said bin Jubayr, Ikrimah mtumwa aliyeachwa huru na Ibn’ Abbas, Ata Bin Abu Rabah, Al-Hassan Al-Basri, Masruq bin Al-Ajda, Said bin Al-Mussayib, Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas, Qatadah, Ad-Dhahhak bin Muzahim na wengine miongoni mwa *Tabiin* na vizazi vilivyofuatia. Kauli za Maimamu hao zinatajwa katika kutafsiri. Hutokea kupishana katika matamko yao, asiyefahamu anadhanika kuwa wame-tofautiana, kwa hiyo anaeleza kuwa ni kauli mbalimbali, na haikuwa hivyo bali baadhi ya wanazuoni wanakielezea kitu kwa kile kinachotokana na tamko, na wengine kwa kisawe chake, na mwengine anataja dhati ya kitu chenyewe, na yote hayo katika sehemu nyingi yana maana moja. Mwenye akili aelewe hilo. Allah تعالى Ndiye Aongozaye na Aelekezaye kwenye ufanisi.

Tafsiri kwa Maoni.

Ama *Tafsir* kwa maoni matupu ni haramu kwa alichopokea Muhammad bin Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَالَ فِي الْقُرْآنِ بِرَأْيِهِ أَوْ بِمَا لَا يَعْلَمُ فَلْيَتَّبِعْهُ مِنْ النَّارِ»

“Yeyote anayeielezea Qur’an kwa maoni yake au kwa kutokuwa na elimu nayo, basi achukue nafasi yake Motoni”.²

Imepokelewa na At-Tirmidhi, An-Nasai na Abu Daud. Kwa mujibu wa ‘At-Tirmidhi Hadithi hii ni *Hasan* (Njema).

Kuinyamazia Tafsiri Isiyofahamika.

Ahly-Salaf walikuwa wakijizuia kuelezea jambo ambalo hawakuwa na elimu nalo, Mathalan, ibn Jarir (At-Tabari) رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Abu Ma’mar alisema: Abubakar As-Sidiq رضي الله عنه alisema, “Ardhi gani itanichukua na mbingu gani itakayonifunika (kivuli) iwapo nitaserna jambo kuhusiana na

¹ At-Tabari 1/91.

² At-Tabari 1/77, Tuhfatul Ahwadhi 8/277. An-Nisai katika Fadhila za Qur’an (uk. 114), Abu Daudi katika mlango wa elimu kutoka katika riwaya ya Abu Hasan Ibin Id. Haya ameyasema, Al-Miz katika kitabu cha Al-Atraf 4/423.,

Kitabu cha Allah تعالى Ambalo sina elimu nalo?"¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kutoa kwa Anas رضي الله عنه kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisoma Aya ifuatayo,

﴿وَفَكَهَةً وَأَبًّا﴾

"Na matunda na Abba (malisho ya wanyama)." (80:31)

Alipokuwa amesimama juu ya mimbari. Kisha akasema, "Matunda tunayajua, lakini Abba ni nini?" Kisha akasema. "Ewe 'Umar! Huku ni kukuza mambo."² Kauli hii ina maana kuwa 'Umar رضي الله عنه ametaka kuelewa undani wa elimu ya Abba, laa si hivyo Abba kuwa ni mmea ulio ardhini liko wazi analijua, kama Allah تعالى Alivyosema,

﴿فَأُنَبِّتْنَا فِيهَا حَبًّا﴾ ﴿وَعِنَبًا وَقَضْبًا﴾

"Kisha Tukaotesha humo (vyakula vilivyo) chembe chembe Na mizabibu na mboga." (80:27-28)

Na amesimulia Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abu Mulaykah alisema kuwa, Ibn Abbas رضي الله عنهما aliulizwa tafsiri ya Ayah, "Endapo mmoja wenu angeulizwa Juu ya Ayah hiyo angetoa Tafsiri yake." Bila kusita Ibn Abbas رضي الله عنهما alikataa kusema lolote kuhusu Ayah hiyo (akiwa na maana kutoa maoni yake). Hadithi hii ina isnadi ya Wapokezi wanaoaminika.³ Aidha amepokea kuwa mtu fulani alimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu;

﴿بِئْسَ يَوْمٌ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ﴾

"Siku moja ambayo kipimo chake ni sawa na miaka elfu moja."

Ibn Abbas رضي الله عنهما akamuuliza mtu yule, "Nini maana ya

﴿بِئْسَ يَوْمٌ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ﴾

"Siku moja ambayo kipimo chake ni sawa na miaka elfu Hamsini,?"

Mtu yule akasema, 'Nilikuuliza ili unieleze maana yake.' Ibn Abbas رضي الله عنهما akamuambia, "Hizo ni siku mbili ambazo Allah تعالى Amezitaja ndani ya Kitabu

¹At-Tabari 1/78.

²At-Tabari 1/86.

³At-Tabari 1/86.

Chake na Yeye Ndiye Mwenye Kuzielewa. Hakupenda kutolea maelezo ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambayo hakuwa na elimu nayo.¹

Al-Layth alisimulia kuwa Yahya bin Said alisema kwamba Said bin Al-Mussayyib alikuwa hapendi kuzungumzia katika Qur'an isipokuwa yale aliyoyafahamu (At-Tabari 1:86). Pia Ayyub, Ibn' Awn na Hisham Ad- Dastawai alisimulia kwamba Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى alisema, "Nilimuuliza Ubaydah (akiwa na maana As-Salmani) kuhusu Ayah ya Qur'an na akanijibu, "Wale waliokuwa wanafahamu mazingira yaliyokuwepo wakati wa kushushwa Qur'an wamekwisha kufa. Hivyo mche Allah تعالى na fuata njia iliyo sawa." Ash-Shab alisimulia kuwa Masruq alisema, "mnapofasiri kuweni makini, kwa sababu Allah تعالى."

Kwa hiyo mapokezi haya sahihi na mengineyo yaliyopokelewa kutoka kwa Masahaba na Maimamu wa *Salaf* (*Mababa* Waadilifu) yanathibitisha kusita kwao kujiingiza katika *Tafsiri* ya mambo ambayo hawakuwa na elimu nayo. Ama wale wanaozungumzia mambo ambayo wana elimu nayo kwa muktadha kilugha na kisheria hawana kosa lolote. Hivyo, wanazuoni na Maimamu ikiwa pamoja na wale tuliowataja, walitoa maelezo ya *Tafsiri* na wakazungumza kuhusu mambo waliyoyafahamu, lakini walitahadhari kuzungumzia yale ambayo hawakuwa na elimu nayo. Wajibu wa kujizuia kuzungumzia usilolijua ni la kila mtu, kama ilivyo wajibu kwa kila mmoja wetu anatakiwa kufikisha elimu aliyonayo kama Allah تعالى Alivyoamrisha,

لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ

"Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtakificha." (3:187)

Kadhalika hadithi iliyosimuliwa kupitia isnadi ya wapokezi kadha isemayo,

«مَنْ سئِلَ عَنْ عِلْمٍ فَكْتَمَهُ، أُلْجِمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِلِجَامٍ مِنْ نَارٍ»

*Mwenye kuulizwa juu ya jambo ambalo ana elimu nalo na akalificha, atafungwa mdomo kwa kifungo cha moto siku ya Kiyama.*²

¹At-Tabari 23/602.

²At-Tabari 1:86.

³Ahmad, 2/263, 305 na 495, Tuhfatul Al-Ahwadhi 7/407, Al-Hakim 1/101 At-Tirmidhi na wengineo.

Namna Mbalimbali za *Tafsiri*

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, Muhammad bin Bashir رحمه الله تعالى alituambia, Muammal alituambia, Sufyan alitueleza, 'Kutoka kwa Abu Zinad kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, *Tafsiri ziko* namna nne: (1) namna ya kwanza hufahamiwa na waarabu kwa kuwa ni lugha yao. (2) Nyingine ni *Tafsir* ambayo mtu yeyote hana udhuru wa kutokuijua. (3) *Tafsir* wanayoifahamu watu wenye elimu tu, (4) *Tafsir* ambayo hakuna anayeifahamu, isipokuwa Mwenyezi Mungu tu.

Sura za Makkah na za Madinah

Hammam alisimulia ya kuwa Qatadah alisema sura zilizoteremka Madina katika Qur'an ni: *Al-Baqarah* (2), *Al-Imran* (3), *An-Nisa* (4), *Al-Maidah* (5), *Baraah* (9), *Ar-Rad* (13), *An-Nahl* (16), *Al-Hajj* (22), *An-Nur* (24), *Al-Ahzaab* (33), *Muhammad* (47), *Al-Fat-h* (48), *Al-Hujurat* (49), *Ar-Rahman* (55), *Al-Hadid* (57), *Al-Mujadalah* (58), *Al-Hashr* (59), *Al-Mumtahanah* (60) *As-Saff* (61), *Al-Jumuah*: (62) *Al-Munafiqun* (63), *At-Taghlabun'* (64) na *At-Talaq*(65), na

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ

"Ewe Mtume Mbona (kwa nini) unaharamisha." (66:1)

Mpaka aya ya kumi, na pia na

إِذَا زُلْزِلَتْ

"Itakapotetemeshwa." (99:1) na

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ

"Itakapofika Nusura ya Mwenyezi Mungu" (110:1)

Hizi ndizo Sura zilizoteremka Madina na Sura zilizosalia ziliteremka Makkah.¹

¹ Taz: Al-Itqaan 1/28.

Idadi ya Aya za Qur'an Tukufu

Idadi ya Aya za Qur'an Tukufu walizoafikiana wanazuoni ni aya elfu sita. Na wametofautiana wanazuoni kuhusu ziada ya idadi hiyo. Na tofauti hii ni ya kimuundo, Qur'an Tukufu haizidishwi kitu wala haipunguzwi, hakika si vingine tofauti hiyo ya wanazuoni imejikita katika uinishaji wa mwisho wa aya, na ujumuishaji wa "Bismillah" zilizopo. Mwanzoni mwa kila sura isipokuwa Sura ya tisa (ya At-Tawba) miongoni mwa mifano ya kutofautiana wanazuoni katika idadi ya Aya za Qur'an, Sura ya Ikhlas, sura ya (112) ina aya nne, kwa wanazuoni wanaozingatia kauli yake Allah تعالی:

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

"Hakuzaa wala hakuzaliwa." (112:3)

Ni ya moja. Na kuna baadhi waliozingatia sura hiyo ina aya tano, kauli yake Allah تعالی

لَمْ يَلِدْ

"Hakuzaa." (112:3) wamesoma ni aya na kauli yake Allah تعالی:

وَلَمْ يُولَدْ

"Wala hakuzaliwa." (112:3) ni aya nyingine.

Idadi ya Maneno na Herufi za Qur'an

Al-Fadhli bin Shadhan alisema kuwa Ataa bin Yasar alisema kuwa idadi ya maneno ya Qur'an Takatifu ni, "Maneno Eflu sabini na saba mia nne thalathini na tisa."

Kuhusu idadi ya herufi za Qur'an, Abdullah bin Kathir alisema kuwa Mujahid alisema, "Hesabu yetu ya herufi za Qur'an ni: Mia tatu ishirini na moja elfu, mia moja na themanini." Zaidi ya hayo, Al-Fadhil alisema kuwa Ata bin Yasar alisema, "Qur'an ina herufi mia tatu ishirini na tatu elfu na kumi na tano." Kwa nyongeza, Salam Abu Muhammad Al-Hamani alisema, "Al-Hajjaj aliwakusanya wasomaji (wa Qur'an) wale waliohifadhi na waandishi, kisha akawauliza, 'Nielezeni Qur'an nzima ina herufi ngapi?'" Wakajibu, "Tulihesabu na kupata herufi mia tatu arobaini elfu mia saba na arobaini."

Na sababu ya tofauti ya Idadi ya herufi za Qur'an ni tofauti iliyopo ya wanazuoni kuhusu (Bismillah), Je ni aya mwanzoni mwa kila sura au sio aya? Kadhalika tofauti ya herufi ya mada (uvutaji wa herufi) je ni herufi za Qur'an au la? na sababu nyinginezo.

Migawanyo Mingine ya Qur'an

Al-Hajjaj akawauliza tena, "Niambieni ni wapi katikati." Walikuta katikati ni katika herufi ya "fa" ya neno 'walyatalat-twaf katika Surat ya (18) ya Al-Kahf, yaani katika maelezo ya Allah تعالیٰ،،

وَلْيَتَأَطَّفْ

"Na afanye mambo haya kwa busara." (18:19)

Theluthi ya kwanza ya Qur' an ipo katika Ayah ya mia katika Surat Baraah (9), na Theluthi ya pili inaishia katika aya ya mia au mia na moja ya Surah Ash-Shu' araa (26) na theluthi ya mwisho inaishia mwisho wa Qur' an. Moja ya saba ipo katika herufi Daal iliyo katika maneno ya Allah تعالیٰ yasemayo,

فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ بِهِ وَمِنْهُمْ مَّنْ صَدَّ

"Basi kuna miongoni mwao waliyoyaamini hayo, na wako miongoni mwao waliojipusha nayo." (4:55)

Sehemu ya pili ya moja ya saba inaishia katika herufi Ta iliyo katika Kauli iliyopo ndani ya Surat Aaraf,

حَبِطَتْ

"Zimeharibika" (7:147) Sehemu ya tatu ya moja ya saba inaishia katika herufi Alif ya pili katika Kauli ya Allah تعالیٰ katika Surat Ar-Ra'd,

أَكْهَأَ

"Matunda yake" (13:35) Sehemu ya nne ya moja ya saba inaishia katika herufi Alif katika Kauli Yake iliyopo katika Surat Al-Hajj,

جَعَلْنَا مَنَسْكَ

"Tumewafanyia mahali" (22:34) Sehemu ya tano ya moja ya saba inaishia herufi haa iliyo katika kauli ya Allah تعالیٰ katika Surai Al-Ahzaab"

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ

“Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini.” (33:36)

Sehemu ya sita ya moja ya saba inaishia kwenye herufi *Waw* iliyo katika Kauli ya Allah تعالى katika *Sural Al-Fath*.

الظَّالِمِينَ بِاللَّهِ ظَرْبِ السَّوْءِ

“Wanaomdhanja Mwenyezi Mungu dhana mbaya” (48:6)

Sehemu ya saba ya mwisho inaishia mwisho wa Qur’an.

Kisha Salam bin Muhammad alisema “Tulijifunza ukweli huu kwa miezi minne.” Baadhi ya watu walisema kuwa Al-Hajjaj alikuwa akisoma robo ya Qur’ an kwa usiku mmoja, Robo ya kwanza inaishia mwisho wa *Sural Al-An’am* (6) ya pili.

وَلْيَتَلَطَّفْ

“Na afanye mambo haya kwa busara” (18:19)

Ya tatu mwisho wa Az- Zumar (39) na sehemu ya nne, mwisho wa Qur’an. Sheikh Abu Amri Ad-Dani alisema katika kitabu chake, *Al-Bayan*, kuwa kuna maoni tofauti kuhusu maelezo hayo. Allah تعالى ni Mjuzi wa yote.

Kuigawa katika Hizbu na Juzuu

Kuna Juzuu thelathini ambazo ni maarufu katika taasisi za elimu na sehemu nyingine na tumetaja Hadithi ambayo inaelezea kuwa Maswahaba walikuwa wakigawanya Qur’ an katika hizbu. Hadith hii iko katika Musnad ya Imam Ahmad, Sunan Abu Dawud na Ibn Majah na wengine.

Kutoka kwa Aws bin Hudhayfah alisema kuwa aliwauliza Masahaba wa Mtume ﷺ katika uhai wake Mtume walikuwa wakiigawa vipi Qur’ an? Walijibu, “Theluthi, khumsi, moja ya saba, moja ya tisa, moja ya kumi na moja, moja ya kumi na tatu na hizbu ya *Mufassal* (sura ndogo ndogo) mpaka mwisho.” (Ahmad, Abu Dawud, na Ibn Majah)

Maana ya *Surah* na Mnyambuliko Wake

Kuna rai tofauti kuhusu maana ya neno ‘*Sura!*’ na chimbuko lake linasemekana kuwa *Surah* maana yake mwinuko na kufafanua.

An-Nabighah - mshairi maarufu wakati wa enzi za Jahiliyah alisema (alipokuwa akimsifu Mfalme).” Unatambua kuwa Allah Amekupa *Sura* kila mfalme awe chini kabisa?” Zaidi ya hayo, *Surah* ina maana ya kuwa msomaji anahama kutoka hatua moja kwenda nyingine. Aidha *Suran* ina maana ya urefu, kama kuta zinazouzunguka mji. Inaelezwa ya kuwa iliitwa *Surah* kwa sababu ni sehemu ya Qur’an. Aidha imeelezwa kuwa *Surah* iliitwa kwa jina hilo kwa sababu ni kamilifu, kama Waarabu walivyokuwa wakimuita ngamia mkamilifu - *Surah*. Mimi nasema neno *Surah*. maana yake kukusanya na kuziunguka Aya katika munasaba huu, kama ukuta unavyouzunguka mji na unazunguka majumba. Wingi wa neno *Surah* ni *Suwar*, *Suwarat* na *Surat*.

Maana ya Ayah

Ayah ni alama ambayo inatenganisha maneno ya kabla na ya baada yake. Ina maana Ayah inatenganisha sentensi iliyotangulia na inayofuata, Allah تعالى Amesema;

إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِ

“*Hakika Alama ya Ufalme Wake*” (2:248)

Pia imeelezwa kuwa iliitwa ‘Ayah’ ikiwa na maana ya ‘maajabu’ kwa sababu binadamu hawezi kuunda maneno kama hayo. Wingi wa Ayah ni Aay, Ayaat na Ayay.

Maana ya Kalimah

Neno *Kalimah* lina maana “tamko moja”, ambalo linaweza kuwa na herufi mbili kama *Ma* na *La*. Aidha *Kalimah* moja inaweza kuwa na herufi zaidi hadi kufikia kumi kama vile,

لَيْسَتْ حَلْفَنَّهُمْ

“*Layastakhlifanannahum*” (24:55)

أَنْزَلْنَا مُكْمُوها

“*Anulzimukumuha*” (11:28) na

فَأَسْقَيْنَكُمُوهُ

“Fa-Asqaynakumuh” (15:22)

Pia Kalimah inaweza kuwa Ayah nzima, kama,

وَالْفَجْرِ

“Wal-Fajr” (89:1)

وَالضُّحَىٰ

Waddhuha” (93:1) na,

وَالْعَصْرِ

“Wal-Asr” (103:1)

Zaidi ya hayo wanazuoni wa Kufah walisema kuwa kila, *Alif Lam Mim, Ta Ha, Yasin, Ha Mim* ni Kalimah. Kwa wao, ‘*Ha Mim, ‘Ain Syn Qaf* (Ash-Shuraa: 1-2) ni maneno mawili. Wengine wanasema kwamba hivyo ni vyanzo vya *Surah*, Kwa nyongeza, Abu’ Amr Ad-Dani alisema, “siielewi kalima moja tu yenye aya kamili isipokuwa Kauli ya Allah تعالى,

مُدَّهَامَّتَانِ

“Mud-hammatan,” katika *Surat Ar-Rahman* (55:64)


Je, Qur’an Ina Maneno Yasiyo ya Kiarabu?

Al-Qurtubi amesema, “Kuna makubaliano kuwa Qur’an haina muundo usiokuwa wa kiarabu katika maneno yake; Wanazuoni wanakubaliana pia kuna majina yasiyokuwa ya kiarabu, kama vile, Ibrahim, Nuh na Lut. Hawakubaliani kuwa hakuna ambacho sio Kiarabu. Jee kuna kingine zaidi ya hayo si ya kiarabu, Al-Baqillani na At-Tabari wamekataa na wamesema, “Kilicho ndani ya Qur’an na kinachoafikiana na lugha: isiyokuwaya kiarabu basi hicho kiko katika mlango wa yalioafikiwa katika lugha.”

Tafsiri ya Suratul Fatihah

Sura ya 1

Iliteremshwa Makkah



Maana ya *Suratul Fatihah* na Majina Yake Mengine

Surah hii inaitwa *Al-Fatihah*, Maana: Mwanzo wa Kitabu kwa maandishi. Surah hii husomwa katika Sala zote. Pia inaitwa *Ummul Kitaab* (Mama wa Kitabu), haya ni kwa mujibu wa wanazuoni wengi.

Na Imethibiti katika Hadithi Sahihi iliyonukuliwa na At-

Tirmidhiy ambaye aliipa Daraja la Sahih kuwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alisema,

«الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ أُمَّ الْقُرْآنِ وَأُمَّ الْكِتَابِ وَالسَّبْحُ الْمُنَافِي وَالْقُرْآنُ الْعَظِيمُ»

“*Al-Hamdu lillahi-Rabbil – ‘alamin ni Ummul Qur’an (Mama wa Qur’an), Ummul Kitaab (Mama wa Kitabu) na Aya saba zinazosomwa mara kwa mara (katika Sala) na ni Qur’an Tukufu*”.

Pia inaitwa *Al-Hamd* na *As-Swalah*, kwa kauli yake Mtume ﷺ kutoka kwa Mola Wake Mlezi,

«قَسَمْتُ الصَّلَاةَ بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي نَضْمَيْنِ، فَإِذَا قَالَ الْعَبْدُ: الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، قَالَ اللَّهُ: حَمِيدِي عَبْدِي»

“*Nimeigawa Sala (yaani Al-Fatihah) baina Yangu na Mja Wangu, nusu mbili. Mja Wangu anaposema, Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote, Allah Husema, “Mja Wangu amenishukuru”*”.¹

¹ At-Tirmidhiy, *Tuh’fatul Al-Ahwadhiy* 8:283.

Al - Fatiha inaitwa *As-Salah* kwa sababu ni nguzo katika kusihi kwa Sala. *Al - Fatiha* pia inaitwa *Ash-shifa* (Ponyo). Pia inaitwa *Ar-Ruqyah* (Zinguo). Katika *sahih* kuna masimulizi ya Abu Said akielezea Hadithi ya Masahaba wa Mtume ambao waliitumia *Al - Fatiha* kama dawa ya kumtibu kiongozi wa kabila fulani aliyegongwa na n'ge. Baadaye Mtume ﷺ alimuambia Sahaba:

«وَمَا يُدْرِيكَ أَنَّهَا رُقْيَةٌ»

“Ulijuaje kuwa ni *Ruqyah* (Zinguo)?”¹

Al-Fatihah iliteremshwa Makkah kama Ibn Abbaas, Qatadah na Abul-'Aliyah رضي الله عنهم walivyoeleza. Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِي

“*Na Tumekupa (hizi Aya) saba (tukufu za Al-Fatihah – za Al-Hamdu) zisomwazo mara kwa mara...*” (15:87)² Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi Zaidi.

Idadi ya Aya Zake

Hakuna mabishano ya kuwa *Al-Fatihah* ina Ayah saba. Wasomaji wengi wa Qur'ani wa Al-Kufah, na kundi la Masahaba, *Tabiin* na Wanazuoni wa vizazi vinavyofuata wamesema *Bismillah* ni Aya inayojitegemea peke yake mwanzoni. Mada hii tutajadili tena Allah تعالى Akipenda na sisi ni waaminifu Kwake.³

Idadi ya Maneno na Herufi Katika Suratul *Al-Fatihah*

Wanazuoni wanasema *Al-Fatihah* ina maneno ishirini na tano na ina herufi mia moja na kumi na tatu.

Kwa nini Iliitwa *Umm Al-Kitab*

Mwanzoni mwa Kitabu cha Tafsir (katika Sahih Yake), Bukhari anasema; “Imeitwa *Umm Al-Kitab*, kwa sababu Qur'an inaanza na Sura hiyo na kila Sala inaanza kwa Kusomwa kwayo.” Aidha imeelezwa kuwa Imeitwa *Umm Al-Kitab* kwa sababu imebeba maana ya Qur'an nzima. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema,

¹ *Fat'hul Al-Baari* 4:529.

² Maana, kwa sababu Aya hii, ambayo inaifanua *Al-Fatihah*, hiyo yenyewe nayo iliteremshwa.

³ *Fat'hul Al-Baari* 8:6.

“Waarabu huita jambo *Umm* ambalo limekamilika kwa kukusanya vipengele mbalimbali mahsusi. Mathalan, ngozi inayozunguka ubongo inaitwa *Umm Ar-Ra’s*. Pia bendera inayowakusanya askari wenye vyeo inaitwa *Umm*. Pia aliongezea kusema kuwa Makka iliitwa *Umm Al-Qura* (Mama wa Miji) kwani ni mkubwa kuliko Miji mingine iliyoizunguka. Inasemekana kuwa dunia ilianza kuumbwa kuanzia Makka.¹ Zaidi ya hayo, Imam Ahmad alinukuu kwamba Abu Hurayrah رضى الله عنه alisimulia kuhusu *Umm Al-Qur’an*, kwamba Mtume ﷺ alisema,

«هِيَ أُمُّ الْقُرْآنِ وَهِيَ السَّبْعُ الْمَثَانِي وَهِيَ الْقُرْآنُ الْعَظِيمُ»

“Hiyo ni *Umm Al-Qur’an* (Mama wa *Qur’an*), Aya Saba zenye kurudiwa rudiwa, nayo ni katika *Qur’an* Tukufu.”²

Aidha Abu Ja’far, Muhammad bin Jariri At-Tabari رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Hurayrah رضى الله عنه akisema ya kuwa Mtume ﷺ alizungumzia kuhusu *Al-Fatihah*,

«هِيَ أُمُّ الْقُرْآنِ وَهِيَ فَاتِحَةُ الْكِتَابِ وَهِيَ السَّبْعُ الْمَثَانِي»

“Hiyo ni *Umm Al-Qur’an*, nayo ni ufunguzi wa *Qur’an* na Aya Saba zinazosomwa mara kwa mara.”³

Fadhila za *Al-Fatihah*

Imam Ahmad bin Hanbal amenukuu katika Musnad kuwa Abu Said bin Al-Mu’alla رضى الله عنه alisema, “Nilipokuwa nasali Mtume aliniita lakini sikumuitikia mpaka nilipomaliza kusali. Kisha nikamuitikia na akaniambia, “Kitu gani kilichokuzuia kuja?” Nikamjibu: “Ewe Mjumbe wa Allah! Nilikuwa nasali. Akaniambia: “Je, Allah تعالى Hakusema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

“**Enyi mliaoamini! Muitikeni Allah (kwa kuitikia Amri Zake) na Mjumbe Wake Atakapokuiteni kwa lile linalokupeni uhai?...” (8:24)**

Kisha akasema,

«لَأَعْلَمَنَّكَ أَعْظَمَ سُورَةٍ فِي الْقُرْآنِ قَبْلَ أَنْ تَخْرُجَ مِنَ الْمَسْجِدِ»

“Nitakufundisha Surah kuu katika *Qur’ani* kabla haujatoka Msikitini.”

¹ At-Tabari 1:107.

² Ahmad 2:448.

³ At-Tabari 1:107.

Amesema, 'Alinishika mkono na alipokuwa anatoka Msikitini, nilimuambia: "Ewe Mjumbe wa Allah! Ulisema; Nitakufundisha Surah kuu katika Qur'an." Akajibu: "Ndiyo". Akasema,

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

"Al-Hamdu Lillahi Rabbil – Alamin."

«نَعْمَ هِيَ السَّنْعُ الْمَنَائِي وَالْقُرْآنُ الْعَظِيمُ الَّذِي أُوتِيَتْهُ»

*"Naam ni Ayah saba zinazosomwa mara kwa mara na Qur'an Takatifu niliyopewa."*¹

Na hivi hivi ameipokea Bukhari², Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah.³

Imam Ahmad pia alirekodi kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alitoka nje wakati Ubbay bin Ka'b رضى الله عنه alikuwa anasali. Akamuita, "Ewe Ubbay". Ubbay رضى الله عنه alisali haraka kisha akaenda kwa Mtume ﷺ akisema, "Amani iwe kwako, Ewe Mjumbe wa Allah!" Mtume ﷺ akajibu, "Amani iwe kwako, Ewe Ubbay kitu gani kilichokuzuia usiniitokie nilipokuita?" Akajibu: "Ewe Mjumbe wa Allah! Nilikuwa nasali." Akamuambia, "Husomi miongoni mwa yale aliyoniteremshia Allah?"

أَسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا تَحْيِيكُمْ

"Muitikieni Allah (Mtii) na Mjumbe Wake anapokuiteni kwa ajili ya yale yanayokupeni uhai". (8:24)

Akasema, "Ndiyo Ewe Mjumbe wa Allah! Sitofanya tena." Mtume ﷺ akamuambia,

«أَتُحِبُّ أَنْ أَعْلَمَكَ سُورَةَ لَمْ تَنْزِلْ لَا فِي التَّوْرَةِ وَلَا فِي الْإِنْجِيلِ وَلَا فِي الزَّبُورِ وَلَا فِي الْفُرْقَانِ مِثْلَهَا؟»

"Je, utapenda nikufundishe Surah ambayo hakuna mfano wake ndani ya Tawrat, Injili, Zaburi au Furqan (Qur'an)?"

¹ Ahmad 4:211.

² Fat'hul Al-Baari 8:6,716.

³ Abu Dawud 2:150, An-Nasai 2: 139 na Ibn Majah 2:1244.

Akamjibu, "Ndiyo ewe Mjumbe wa Allah." Akamuambia, "Nataraji sitovuka kizingiti cha mlango huu mpaka umejifunza Surah hiyo." Ka'ab رضي الله عنه akasema, "Mtume ﷺ alinishika mkono wakati akinisemesha. Wakati huo nikawa naenda taratibu nikichelea asije akafika mlangoni kabla ya kumaliza mazungumzo. Alipofika mlangoni nilimuambia: "Ewe Mjumbe wa Allah! Je, ni Surah ipi uliyoahidi kunifundisha?" Akajibu: "Unasoma nini katika Sala?" "Hivyo nikamsomea *Umm Al-Qur'an*". Naye akaniambia,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِي التَّوْرَةِ وَلَا فِي الْإِنْجِيلِ وَلَا فِي الزَّبُورِ وَلَا فِي
الْفُرْقَانِ مِثْلَهَا إِنَّهَا السَّبْعُ الْمَنَابِي»

"Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Allah Hajawahi Kuteremsha ndani ya Tawrat, Injili, Zaburi au Furqan Surah mfano wake, kama hii. Hakika hiyo ni Surah yenye ayah saba zinazosomwa mara kwa mara."

Pia At-Tirmidhiy amerekodi Hadithi hii na katika simulizi yake, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّهَا مِنْ السَّبْعِ الْمَنَابِي وَالْقُرْآنِ الْعَظِيمِ الَّذِي أُعْطِيَتْهُ»

"Hakika ni ayah saba zinazosomwa mara kwa mara, na Qur'ani Takatifu ambayo nilipewa." At-Tirmidhi amesema kwamba hii ni Hadith Hasan Sahihi.¹

Kuna Hadith sawa na hii kuhusu mada hii iliyosimuliwa na Anas bin Malik رضي الله عنه.² Zaidi ya hayo, Abdullah, mtoto wa Imam Ahmad aliirekodi Hadith hii kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه ambaye ametaja kwa urefu lakini yenye maneno sawa na hayo tuliyoyataja hapo juu.³ Kwa nyongeza, At-Tirmidhi na An-Nasai wameirekodi Hadith hii kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه ambaye ameelezea kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِي التَّوْرَةِ وَلَا فِي الْإِنْجِيلِ مِثْلَ أَمِّ الْقُرْآنِ وَهِيَ السَّبْعُ الْمَنَابِي وَهِيَ
مُتْسَوْمَةٌ بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي رَضْفَيْنِ»

¹ Ahmad 2:412, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:283.

² Al-Hakim 1:560.

³ Ahmad 2:357 na 5:114.

“Allah Hajawahi Kuteremsha ndani ya Tawrat wala ndani ya Injili, Surah kama mfano wa hii. Surah yenye aya saba zinazosomwa kila mara na zimegawanywa nusu mbili kati ya Allah na Watumwa wake”.

Haya ni maneno yaliyoripotiwa na An-Nasai: At-Tirmidhi alisema Hadithi hii ni *Hasan Gharib*.¹

Aidha Imam Ahmad alirekodi kuwa Ibn Jabir رضي الله عنه alisema, *“Nilikwenda kwa Mjumbe wa Allah baada ya kuwa alijimiminia maji (kwa ajili ya udhu) na nikatamka, “Amani iwe kwako, Ewe Mjumbe wa Allah! - Hakuniitikia.” Hivyo nikasema tena, “Amani iwe kwako, Ewe Mjumbe wa Allah! - Hakunijibu.” Hivyo nikasema tena, “Amani iwe kwako, Ewe Mjumbe wa Allah!” Bado Hakunijibu, Nilimfuata nyuma Mjumbe wa Allah mpaka alipowasili nyumbani kwake. Nilikwenda Masjid nikakaa sina raha na nimevunjika moyo. Baada ya kumaliza kutawadha, Mjumbe wa Allah alitoka nje na kusema, “Amani na Huruma za Allah Ziwe kwenu, Amani na Huruma za Allah Ziwe kwenu, Amani na Huruma za Allah Ziwe kwenu.” Kisha akasema, “Ewe Abdullah bin Jabir! Nikueleze Surah bora ndani ya Qur’an?” Nikamjibu: “Ndiyo Ewe Mjumbe wa Allah!” Akaniamrisha, “Soma, “Shukrani zote Anastahiki Allah, Mola wa Walimwengu wote.” mpaka umalize”.*²

Hadithi hii ina silsila nzuri ya wasimulizi. Baadhi ya wanazuoni waliitegemea Hadithi hii kama ushahidi kuwa baadhi ya Ayah na Surah zina ubora (Utakatifu) kuliko nyengine. Hadithi nyingine kuhusu fadhila za Qur’an, Bukhari amerekodi kuwa Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه alisema, “Siku moja tulipokuwa safarini, mtumishi wa kike alitukabili na kutueleza, “Kiongozi wa kitongoji hiki amegongwa na ng’e na hapana watu wa kumtibu, Je kuna mganga kati yenu?” Alisimama mtu ambaye hatukujua ujuzi wake katika tiba, alimsomea *Ruqyah* yule kiongozi akapona. Na akaamuru msomaji apewe Kondoo thelathini na maziwa ikiwa ni zawadi yake. Tulimuuliza, “Unajua *Ruqyah* au uliwahi kufanya kabla ya leo?” Akawajibu: “Hapana, Sikupata kufanya isipokuwa nimetumia *Umm Al-Kitab* kuwa *Ruqyah*”. Tukamuambia, “Tusifanye jambo lingine lolote mpaka tukamuulize Mtume ﷺ.” Tuliporejea Madina tulimsimulia Mtume ﷺ. Naye akasema:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhiy 8:553 na An-Nasai katika Al-Kubra 1:318.

² Ahmad 4:177 na Al-Muwatta 1:84.

«وَمَا كَانَ يُدْرِيهِ أَتَتْهَا رُحِيَّةٌ أَمْ قِسْمَةٌ آتَتْهُمُ لِأَيِّ شَيْءٍ فَعَرَضُوا كَأَنَّهُمْ مُّشْرِكُونَ»

“Ni nini kilichomfahamisha kuwa hiyo (Surat Al-Fatiha) ni Ruqyah? (Yaani hiyo ndio Ruqya yenyewe) Gawaneni hao kondoo nami mnipatie fungu langu.”¹

Imamu Muslim aliandika katika Sahih yake, An-Nasai katika Sunan yake kuwa Abbas رضي الله عنهما alisema: *“Jibril alipokuwa na Mtume alisikia sauti kutoka juu. Jibril aliangalia juu na akasema, “Huo ni mlango wa peponi unafunguliwa na haujawahi kufunguliwa kabla ya leo. Malaika alishuka kupitia katika mlango na akafika kwa Mtume na akamuambia, “Pokea habari za kufurahisha kuhusu nuru mbili ulizopewa ambazo hapana Mtume mwingine kabla yako aliyepewa; Mwanzo wa Kitabu na Ayat tatu za mwisho za Surat Al-Baqarah. Hutasoma herufi zake bali utapata manufaa yake.” Hayo ni maneno yaliyokusanywa na An-Nasai² na Muslim alirekodi maneno sawa na hayo (1:554).*

Kusoma Al-Fatihah Katika Sala

Imamu Muslim alipokea kwamba Abu Hurayrah رضي الله عنه alielezea kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ صَلَّى صَلَاةً لَمْ يَتْرَأَ فِيهَا أُمَّ الْقُرْآنِ فَبِي خِدَاجٍ ثَلَاثًا غَيْرُ تَمَامٍ»

“Atakayesali Sala yoyote bila kusoma Umm Al-Quran, basi Sala yake hiyo haikukamilika.” Alirejea maneno haya mara tatu.

Abu Hurayrah رضي الله عنه aliulizwa, “Hali inakuwaje tunaposimama nyuma ya Imam?” Akawajibu; “Soma mwenyewe kwani nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

« قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: قَسَمْتُ الصَّلَاةَ بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي نَضْفَيْنِ وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ فَإِذَا قَالَ: الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، قَالَ اللَّهُ: حَمِدَنِي عَبْدِي وَإِذَا قَالَ: الرَّحْمَنُ الرَّحِيمِ، قَالَ اللَّهُ: أَشْنَى عَلَيَّ عَبْدِي، فَإِذَا قَالَ: مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ، قَالَ اللَّهُ: مَجَدَّنِي عَبْدِي وَقَالَ مَرَّةً: فَوَضَّ إِلَيَّ عَبْدِي فَإِذَا قَالَ: إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ، قَالَ: هَذَا بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ، فَإِذَا قَالَ: اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ۝ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ، قَالَ اللَّهُ: هَذَا لِعَبْدِي وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ»

¹ Fat'hul-Bari 4:671.

² Muslim 1:554, An-Nasai katika Al-Kubra 5:12.

“Allah Aliyetukuka Alisema: “Nimeigawanya Sala (Al-Fatihah) katika nusu mbili kati Yangu na Mja Wangu, na Mja Wangu Nitampa atakachokiomba”.

Kama atasema,

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

“Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote”. (1:2)

Allah تعالى Anasema, “Mja Wangu amenishukuru.” Mja anaposema,

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾

“Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.” (1:3)

Allah تعالى Anasema, “Mja Wangu amenitukuza.” Anaposema,

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٣﴾

“Mwenye kumiliki siku ya malipo”. (1:4)

Allah تعالى Anasema, ***“Mja Wangu ameninyenyekea.”*** au ***“Mja Wangu ameyategemezea mambo yake yote Kwangu.”*** Anaposema,

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٤﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunayekuomba msaada.”(1:5)

Allah تعالى Anasema, ***“Hii ni kati Yangu na Mja Wangu na Mja Wangu Nitampa alichokiomba.”*** Anaposema,

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٥﴾ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا

الضَّالِّينَ ﴿٦﴾

“Tuongoze njia iiyonyooka. Njia ya wale uliowaneemesha, sio (ya wale) waliokasirikiwa, wala (ya) wale waliopotea.” (1:6-7)

Allah تعالى Anasema, ***“Hili ni la Mja Wangu na Mja Wangu Nitampa alichokiomba.”***

Haya ni maneno ya An-Nasai na Muslim. Na An-Nasai kwa pamoja wanaelezea Hadithi kwa maneno yafuatayo, “Nusu yake ni Yangu na nusu ni ya Mja Wangu,

na Mja Wangu atapata alichokiomba.”¹

Ufafanuzi wa Hadithi Hiyo.

Hadithi ya mwisho imetumia neno “Salah” ikikusudiwa kusoma Qur’an, (Al-Fatihah katika munasaba huu) kama ambavyo Allah تعالى Alivyosema katika Ayah nyengine.

وَلَا تَجْهَرُ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافُتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١١٠﴾

“Unaposali usitoe sauti ya juu au sauti ya chini bali iwe kati na kati.” (17:110)

Ikiwa na maana unaposoma Qur’ani kama ilivyo katika Sahih iliyopokelewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.² Aidha katika Hadithi ya mwisho Allah تعالى Amesema, “Nimeigawa Sala (Al-Fatihah) katika nusu mbili kati Yangu na Mja Wangu, na Mja Wangu Nitampa atakachokiomba.” Baada ya hapo Allah تعالى Akaelezea mgawanyo unaohusu kusoma Al-Fatihah, Akionesha umuhimu wa kusoma Qur’ani ndani ya Sala, ambayo ni moja ya nguzo kuu za Sala. Kwa hivyo neno “Sala” halikutumika kikamilifu kwani hapa linamaanisha kusoma Qur’ani. Vivyo hivyo neno “kusoma” lilitumika likiwa na maana ya “Sala” Kama ilivyojidhihirisha kwenye Kauli ya Allah تعالى:

وَقُرْآنَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿٧٨﴾

“Soma Qur’an Alfajiri. Kwa hakika usomaji wa Qur’ani Alfajiri unashuhudiwa.” (17:78)

Na madhumuni ni Sala ya Alfajiri. Sahihi mbili zimerekodi kuwa malaika wa usiku na mchana wanahudhuria Sala hii.³

Kusoma Al-Fatihah ni lazima kwa Kila Rakaa Awe Imamu, Maamuma au Anayesali Peke

Ukweli tulioeleza ni ushahidi tosha kuwa kusoma Qur’ani (Al-Fatihah) ndani ya Sala ni lazima, na kuna makubaliano ya wanazuoni kuhusu hukumu hii.

¹ Muslim 1:296, na An-Nasa’i katika al-Kubra 5:11, 12.

² Fat’hul al-Bari 8:257.

³ Fat’hul Al-Bari 8:251. Na Muslim 1:439

Aidha Hadithi tuliyoitaja inathibitisha ukweli huo. Kuhusiana na hili Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ صَلَّى صَلَاةً لَمْ يَتْرَأْ فِيهَا بِأَمِّ الْقُرْآنِ فَهِيَ خِدَاجٌ»

“Yeyote atakayesali na asisome Umm Al-Quran, basi Sala yake haijatimia.”¹

Pia Sahihi mbili zilirekodi kwamba Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema kwamba Mtume ﷺ alisema,

«لَا صَلَاةَ لِمَنْ لَمْ يَتْرَأْ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ»

“Hana Sala yeyote ambaye hakusoma Fa-tihatul-Kitab (Mwanzo wa Kitabu).”²

Aidha, Sahih za Ibn Khuzaima na Ibn Hibban zilirekodi kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema ya kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تُجْزَى صَلَاةٌ لَا يُتْرَأُ فِيهَا بِأَمِّ الْقُرْآنِ»

“Haisihi Sala ambayo haikusomwa Umm Al-Quran.”³

Kuna Hadithi nyingine nyingi kuhusiana na mada hii.

Tafsir ya *Isti'adhah* (Kujikinga) na Hukumu Zake

Allah تعالى Amesema,

حُذِّ الْعَفْوَ وَأُمِّرَ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿٢٠٠﴾ وَإِنَّمَا يَنْزَعُكَ مِنَ الشَّيْطَانِ
نَزْعٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٠١﴾

“Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuze masafihi. Na kama wasiwasi wa Shetani ukikusumbua (kuona kwa nini nisiwajibu masafihi hawa) basi (sema Audhu Billahi) jikinge kwa Mwenyezi Mungu (na kuchezeza na Shetani; ukaacha wasia wake Mwenyezi Mungu); Bila shaka Yeye Ndiye Asikiaye na Ajuaye.” (7:199-200).

¹ Ahmad 2:250.

² Fat'hul al-Bari 2:276 na Muslim 1:295.

³ Ibn Khuzaymah 1:248 na Ibn Hibban 3:139.

Na Allah تعالى Akasema;

أَدْفَعْ بِأَلْتِي هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةِ ۖ خُنْ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٢٣﴾ وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ
هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٢٤﴾ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ تَحْضُرُونِ ﴿٢٥﴾

“Ondosha mabaya (unayofanyiwa) kwa (kulipa) mema; Sisi Tunajua wanayoyasema. Na sema: “Mola Wangu! Najikinga Kwako (Uniepushe) na wasiwasi wa shetani. Na najikinga Kwako, Mola Wangu, ili wasinihudhurie”. (23:96-98) na,

أَدْفَعْ بِأَلْتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٢٦﴾ وَمَا
يُلْقِيهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٢٧﴾ وَإِنَّمَا يَنزَعَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ
نَزْعٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٢٨﴾

“Ondosha baya unalofanyiwa kwa wema; tahamaki yule ambaye baina yako na yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia chungu. Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Mwenyezi Mungu). Na kama shetani akikushawishi kwa tashwishi (zake ili ugombane na hao wanaokufanyia ubaya), wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu (kwa kusema): “Audhu Billahi Mina Shaytaani Rajym.” Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua”. (41:34-36)

Hizi ndizo Aya tatu pekee zinazobeba maana hii. Allah تعالى Ametuasa tuwatendee utu na wema maadui zetu, kwani anaweza kubadilika kuwa rafiki na mwenzu. Pia Anatuasa tujikinge na adui shetani kwani shetani hamhurumii adui yake hata kama tutamtendea mema na kumhurumia. Shetani alikula kiapo kumuangamiza Mtoto wa Adam kutokana na uadui aliokuwa nao siku zote na baba wa binadamu, Adam عليه السلام. Allah تعالى Amesema,

يٰٓبَنِي ٓءَادَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ الشَّيْطٰنُ كَمَا ٓاَخْرَجَ ٓاَبُوۡيَكُم مِّنَ الْجَنَّةِ

“Enyi wanadamu! Shetani (iblisi) asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo.” (7:27) Na Allah تعالى Akasema;

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦﴾

“Kwa yakini Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui (yenu; kwa Hivyo msimtii) kwani analiita, kundi lake liwe katika watu wa Motoni.” (35:6)

Na, Amesema;

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

“Je! Mnamfanya yeye na kizazi chake kuwa marafiki (zenu) badala Yangu, hali wao ni maadui zenu? Ni mbaya kabisa kwa madhalimu badala (hii).” (18:50)

Shetani alimhakikishia Adam عليه السلام kuwa alitaka kumshauri, lakini alikuwa anasema uongo. Hivyo ni vipi atatutendea wema baada ya kuvunja kiapo. Na hakika amesema;

فِعِزَّتِكَ لَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٢﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٨٣﴾

“Naapa kwa haki ya Utukufu Wako, bila shaka nitawapoteza wote (hao watoto wa huyu adui yangu – Adamu. Isipokuwa wale waja Wako miongoni mwao waliosafishwa (Uliowasafisha).” (38:82-83)

Pia, Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿٦١﴾ إِنَّهُ لَيْسَ لَهُ سُلْطَانٌ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٦٢﴾ إِنَّمَا سُلْطَانُهُ عَلَى الَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُ وَالَّذِينَ هُمْ بِهِ مُشْرِكُونَ ﴿٦٣﴾

“Na ukitaka kusoma Qur’an piga Audhu (kwanza jikinge) kwa Mwenyezi Mungu (Akulinde) na Shetani aliyefukuzwa (Katika Rehema Yake Mwenyezi Mungu. Anza kwa kusoma Audhu). Hakika yeye (Shetani) hana nguvu juu ya wale walioamini na wanaomtegemea Mola wao. Nguvu zake ni juu ya wale wanaomshirikisha (Mwenyezi Mungu) naye”. (16:98-100)

Kujikinga Kabla ya Kusoma Qur'an

Allah تعالى Amesema,

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿١٠٠﴾

“Utakaposoma Qur'an, jikinge kwa Allah dhidi ya Shetani, aliyelaaniwa.” (16:98)

Ikiwa na maana, Jikinge kabla hujasoma Qur'an. Allah تعالى pia Anasema,

إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ

“Mnaposimama kwa ajili ya kusali, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu.”

(5:6) Ina maana kabla hujasimama kusali kama ilivyotolewa ushahidi na Hadithi za Mtume ﷺ kuhusu jambo hilo. Imam Ahmad bin Hanbal aliripoti kuwa Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ aliposimama kwa ajili ya Sala za usiku, alianza Sala kwa *Taqbir* (*Allahu Akbar* - Allah ni Mkubwa), kisha huomba Dua:

«سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، وَتَبَارَكَ اسْمُكَ، وَتَعَالَى جَدُّكَ، وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ»

“Kutakasika ni Kwako Wewe, Ewe Mola Wetu, Unayestahiki Shukrani, Limetukuka Jina Lako, Uko Juu Utukufu Wako, (Ufalme Wako) na hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe.”

Kisha Mtume ﷺ akasema maneno yafuatayo mara tatu;

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ»

“Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah”. Kisha Mtume ﷺ husema,

«أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ هَمَزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ»

“Najikinga kwa Allah, Msikivu, Mjuzi kutokana na Shetani aliyelaaniwa, kutokana na nguvu zake na ufedhuli wake; ushawishi wake na ushairi wake.”

Wakusanyaji wanne wa Sunan waliirekodi Hadithi hii ambayo Tirmidh anaichukulia kuwa ni maarufu katika mada hii.¹ Abu Dawud na Ibn Majah walirekodi kuwa Jubayr bin Mutim alisema ya kuwa baba yake aliwaeleza, “Mtume ﷺ alipoanza Sala, alisoma:

¹ Ahmad 3:69, Abu Dawud 1:490, Tuhfat al-Ahwadhi 2:47, an-Nasa'i 2:132 na Ibn Majah 1:264.

«اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا - ثَلَاثًا - الْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا - ثَلَاثًا - سُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا -
ثَلَاثًا - اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ هَمَزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ»

"Allah ni Mkubwa mno, (Mkubwa wa kweli) (mara tatu), Shukrani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu (mara tatu) na Sifa zote Anastahiki Allah, usiku na mchana (mara tatu). Ewe Allah! Najikinga Kwako kutokana na Shetani aliyelaaniwa kutokana na (Hamz) zake, (Nafkh) zake na (Nafth) zake."

Amr alisema: "Hamz - maana yake kunyima pumzi; na Nafkh - maana yake Usafihi, na Nafth - maana yake ni Ushairi."¹ Ibn Majah pia alirekodi kuwa Ali bin Al-Mundhir alisema kuwa Ibn Fudhayl alisimulia kuwa Ata bin As-Saib alisema kuwa Abu Abdur – Rahmaan As-Sulami alisema kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ وَهَمَزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ»

"Ewe Allah! Najikinga Kwako na shetani aliyelaaniwa, kutokana na kuangamiza (Hamz) kwake, kiburi (Nafkh) chake na Ushairi (Nafth) wake."

Alisema: "Hamz maana yake ni Kifo, Nafkh maana yake ni Kibri na Nafth maana yake ni "ushairi."²

Kujikinga kwa Allah تعالی Mtu Anapokasirika

Katika Musnad wake Al-Hafidh Abu Ya'la Ahmad bin Ali bin Al-Muthanna Al-Mawsili aliripoti kuwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه alisema, "Watu wawili waligombana na Mtume ﷺ akiwepo. Pua ya mmoja wao ilivimba kutokana na hasira iliyovuka mpaka. Mtume ﷺ alisema:

«إِنِّي لِأَعْلَمُ شَيْئًا لَوْ قَالَ لَذَهَبَ عَنْهُ مَا يَجِدُ: أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ»

*"Nayajua maneno ambayo akiyatamka, zitapotea hisia alizonazo,
"Najikinga kwa Allah kutokana na shetani aliyelaaniwa."*

An-Nasai pia alirekodi Hadithi hii ndani ya kitabu chake, *Al-Yawm wal-Laylah*.³

¹ Abu Dawud 1:486 na Ibn Majah 1:265.

² Ibn Majah 1:266.

³ An-Nasa'i katika Al-Kubra, Na. 10233.

Bukhari alirekodi kuwa Sulayman bin Surad رضى الله عنه alisema, "Watu wawili waligombana na Mtume ﷺ alikuwepo pamoja nasi. Mmoja wao alikuwa akitukana wenzake na uso wake ukawa mwekundu kwa hasira.' Mtume ﷺ akasema,

«إِنِّي لِأَعْلَمُ كَلِمَةً لَوْ قَالَهَا لَذَمَبَ عَنْهُ مَا يَجِدُ، لَوْ قَالَ: أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ»

"Nayajua maneno ambayo akiyatamka, zitapotea hisia alizonazo, nayo ni, "Najikinga kwa Allah kutokana na shetani aliyelaaniwa."

Wakamuambia mtu yule, "Je, Hukumsikia Mtume alivyosema?" Akajibu, "Mimi si mwenda wazimu." Pia Muslim, Abu Dawud na An-Nasai katika *Al-Kubra* wameirekodi Hadithi hii.¹ Kuna Hadithi nyingi nyingine kuhusu kujikinga kwa Allah تعالى. Mada hii unaweza kuipata katika vitabu vya Dhikri na Fadhila za Matendo Mema. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Istia'dhah ni Wajibu au Sunna?

Wanazuoni wengi wanaeleza kuwa kusoma *Istia'dhah*, kwa maana, "*Audhu billah Mina Sshaitwan Rajiim.*" (katika Sala au wakati wa kusoma Qur'an) ni Sunna na sio lazima. Hivyo kutoisoma hakumpatishi mtu dhambi. Hata Hivyo Ar-Razi رحمه الله تعالى amerikodi kuwa Ata bin Abi Rabah alisema kuwa *Istia'dhah* ni wajibu kwenye Sala na nje ya Sala na mtu anaposoma Qur'an. Ar-Razi رحمه الله تعالى aliunga mkono kauli ya Ata kwa kutegemea maana ya Aya,

فَاسْتَعِذْ

"...Jikinge..." (16:98)

Alisema kuwa Aya hii ina amri ambayo inahitaji kutekelezwa. Aidha Mtume ﷺ alikuwa akisoma *Istia'dhah* kila wakati. *Istia'dhah* pia huondoa uovu wa shetani na kufanya hivyo ni lazima. Kanuni za Kifikhi zinasema kuwa, **njia inayohitajika kutekeleza ulazima wa kidini, basi njia hiyo nayo inakuwa lazima.** Mmoja wenu anaposema, "*Audhu billah Mina Sshaitwan Rajiim*" "Najikinga kwa Allah تعالى kutokana na shetani aliyelaaniwa". Hivyo hii itakuwa imetosheleza.

¹ *Fat'hul Al-Bari* 6:388 Muslim 4:2015, Abu Dawud 5:140 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 7:104.

Ubora wa *Istia'dhah*

Istia'dhah, kwa maana ya kujikinga na shetani, husafisha kinywa kutokana na maneno machafu aliyoyatamka mtu. Pia inakisafisha kinywa na kukiandaa kusoma maneno ya Allah تعالى. Zaidi ya hayo ni kutafuta Msaada wa Allah تعالى na kutambua Uwezo Wake wa Kufanya kila kitu. *Istia'dhah* inathibitisha unyenyekevu wa mja, udhaifu na kushindwa kwake kumkabili adui na mwovu wa ndani bila msaada wa Allah تعالى, Ambaye Alimuumba huyu adui, na Ndiye Mwenye Uwezo wa Kumfukuza na Kumshinda. Adui huyu hakubali kuhurumiwa kinyume cha adui wa kibinadamu. Kuna Ayah tatu katika Qur'an zinazothibitisha ukweli huu. Pia Allah تعالى Amesema,

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٦٥﴾

“Hakika waja Wangu huna mamlaka juu yao. Na Mola Wako Anatosha kuwa Mlinzi (wao)”. (17:65)

Inafaa tueleze hapa kuwa Waumini wanaouliwa na maadui wa kibinadamu hufa shahidi, lakini wale waathirika wa adui - Shetani - huwa maharamia. Zaidi ya hayo Waumini wanaoshindwa na adui (Wasioamini) wanapata thawabu, wakati wale wanaoshindwa na adui wa ndani (shetani) wanapata dhambi na wanakuwa wapotofu. Kwa kuwa Shetani humuona binadamu ambapo binadamu hawezi kumuona Shetani. Hivyo inastahili Waumini wajikinge kutokana na Shetani ambaye hawamuoni. *Istia'dhah ni njia ya kujikurubisha kwa Allah na kujikinga Kwake kutokana na ufisadi wa kila kiumbe muovu.*

Nini Maana ya *Istia'dhah*?

Istia'dhah “*Audhu billah Mina Sshaitwan Rajiim.*” Maana yake, “Najikinga kwa Allah تعالى kutokana na Shetani aliyelaaniwa, ili azuiwe kuathiri mambo yangu ya kidini na kidunia, au kutokana na kunizuia kutekeleza yale niliyoamrishwa kutekeleza au kunishawishi kutenda yaliyoharamishwa.” Hakuna anayeweza kuzuia vitimbi vya shetani dhidi ya mwana wa Adam isipokuwa Allah تعالى Pekee. Hii ndiyo sababu ya Allah تعالى kuturuhusu kuwa laini, na wapole kwa mafisadi wa kibinadamu kwani kwa kufanya hivyo kunaweza kuwafanya waache maovu na kuwa watu wema. Hata Hivyo Allah تعالى Alitutaka tuombe hifadhi Kwake kutokana na ufisadi wa shetani, kwa sababu yeye ni muovu asiyebadilika. Hivyo, mwenye uwezo wa kuzuia uovu wa shetani ni Yule Aliyemuumba. Maelezo haya yanafafanuliwa katika Ayah tatu za Qur'an. Allah تعالى Anasema katika *Surat Al-A'raf*.

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿١١١﴾

“Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze masafihi.” (7:199). Muongozo huu, unahusu Miamala pamoja na Maadui wa Kibinadamu. Kisha Allah تعالى Akasema;

وَأِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٠٠﴾

“Na kama wasiwasi wa Shetani ukikusumbua (kuona kwa nini nisiwajibu masafihi hawa) basi (sema Audhu Billahi) jikinge kwa Mwenyezi Mungu (na kuchezewa na Shetani, ukaacha wasia Wake Mwenyezi Mungu) Bila shaka Yeye Ndiye Asikiaye na Ajuaye.” (7:200)

Pia Allah تعالى Anasema katika Surat Al-Muuminun,

أَدْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةِ ۗ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٩٦﴾ وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٩٧﴾ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ يَحْضُرُونِ ﴿٩٨﴾

“Ondosha mabaya (unayofanyiwa) kwa (kulipa) mema; Sisi Tunajua wanayoyasema. Na sema: “Mola Wangu! Najikinga Kwako (Uniepushe) na wasiwasi wa shetani. Na najikinga Kwako, Mola Wangu, ili wasinihadhurie.” (23:96-98)

Zaidi ya hayo Allah تعالى Anasema katika Surat As-sajdah,

وَلَا تَسْتَوِ الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ۗ أَدْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿١٠١﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿١٠٢﴾
وَأِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ ۗ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٠٣﴾

“Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa) kwa wema; tahamaki yule ambaye baina yako na yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia chungu. Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Mwenyezi Mungu). Na kama shetani akikushawishi kwa tashwishi (zake ili ugombane na hao wanaokufanyia ubaya), wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu (kwa kusema): (“Audhu Billahi Mina Shaytaani Rajym.”) Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua”. (41:34-36)

Sababu ya Kuitwa *Shaytan*.

Katika lugha ya kiarabu, neno "*Shaytan*" ni nomino na linatokana na kitenzi *Shatana*, chenye maana ya kitu kilicho mbali. Hivyo *Shaytan* ana maumbile tofauti na binadamu, na njia zake za uovu ni mbali kabisa na aina za mambo mema. Aidha imeelezwa kuwa neno "*Shaytan*" linatokana na *Shata* (kwa maneno halisi "kuchomwa"), kwa sababu aliumbwa kwa moto. Baadhi ya wanazuoni wanasema maana zote ni sahihi, japo wanasema maana ya mwanzo ni sahihi zaidi. Siybawayhi (mwana Isimu wa Lugha ya Kiarabu) alisema, "Waarabu wanasema, "Fulani na fulani 'ana *Tashaytan*', anapofanya mambo ya kishetani. Iwapo neno *Shaytan* linatokana na *Shata* wangelisema, *Tashayyata* badala ya "*Tashaytan*." Hivyo, *Shaytan* inatokana na neno lenye maana, "mbali sana", kwa sababu hii wale wanaoasi miongoni mwa majini na binadamu wanaitwa '*Shaytan*'. Allah تعالى Amesema,

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرَفَ
الْقَوْلِ غُرُورًا

"Na namna hii Tumemfanyia kila Nabii maadui; (Nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupamba ili kuwadanganya". (6:112)

Kwa nyongeza, katika Musnad wa Imam Ahmad amepokea kwamba Abu Dharr رضي الله عنه alisema ya kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يَا أَبَا ذَرٍّ تَعَوَّذْ بِاللَّهِ مِنْ شَيْطَانِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ»

"Ewe Abu Dharr! Jikinga kwa Allah kutokana na mashetani wa kibinadamu na kijini."

Abu Dharr رضي الله عنه akasema, "Nikamuuliza Mtume ﷺ, Je, kuna mashetani ya kibanaadamu?" Akajibu, "Ndiyo".¹ Pamoja na hayo imerekodiwa katika Sahih Muslim kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kwamba Mtume ﷺ alisema;

«يَقْطَعُ الصَّلَاةَ الْمَرْأَةُ وَالْجِمَارُ وَالْكَلْبُ الْأَسْوَدُ»

"Mwanamke, Punda na Mbwa mweusi wanakatisha Sala (endapo watapita mbele ya wanaosali kama mbele yao hapatakuwa na kinga.)"

¹ Ahmad 5:178.

Abu Dharr رضي الله عنه akasema, “Niliuliza, kuna tofauti gani kati ya mbwa mweusi, mwekundu au wa rangi ya njano?” Akanijibu,

«الْكَلْبُ الْأَسْوَدُ شَيْطَانٌ»

“Mbwa mweusi ni Shetani.”¹

Aidha Ibn Jarir At-Tabari رحمه الله تعالى alirekodi kwamba Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه Siku moja alimpanda *Berthawn* (ngamia mkubwa) ambaye alianza kupiga shoti kwa kiburi. Umar رضي الله عنه akaendelea kumpiga yule Ngamia lakini akaendelea kwenda kwa jeuri. Umar رضي الله عنه akashuka juu ya yule mnyama na kusema, “Naapa kwa Allah تعالى, *nimempanda Shaytan*. *Sikushuka kutoka kwa mnyama mpaka nilipohisi kitu moyoni mwangu.*” Hadithi hii ina silsila ya wapokezi thabiti.²

Maana ya *Ar-Rajim*

Ar-Rajim maana yake kufukuzwa kutoka aina zote za kheri. Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيَاطِينِ

“Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na Tumeifanya ili kuwapigia mashetani...” (67:5)

Allah تعالى pia Amesema;

إِنَّا زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِرِيْنَةِ الْكَوَاكِبِ ۖ وَحِفْظًا مِّنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَّارِدٍ ۖ لَا يَسْمَعُونَ إِلَى الْمَلَأِ الْأَعْلَىٰ وَيُقَذَّفُونَ مِّنْ كُلِّ جَانِبٍ ۖ دُخُورًا ۖ وَهُمْ عَذَابٌ وَأَصِْبٌ ۖ إِلَّا مَنِ خَطِيفَ الْخَطِيفَةِ فَاتَّبَعَهُ شَهَابٌ ثَاقِبٌ ۖ

“Bila shaka Sisi Tumeipamba mbingu ya karibu (hii) kwa pambo la nyota. Na Tumezilinda na kila shetani asi: Wasiweze kusikiliza (yanayosemwa na hao) viumbe watukufu (Malaika): na wana fukuzwa huko kila upande. Kwa hizaya; na wanayo adhabu

¹ Muslim 1:365.

² At-Tabari 1:111.

(inayowazuia kufika huko) inayodumu kwao. Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo hivi (katika maneno yanayosemwa huko); mara kikamfuata kimondo (kijinga cha moto) king'aracho (kitamuangamizilia mbali)". (37:6-10)

Allah تعالیٰ Pia Amesema;

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَزَيَّنَّاهَا لِلنَّاظِرِينَ ﴿٦﴾ وَحَفِظْنَاهَا مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿٧﴾ إِلَّا مَنْ أَسْرَقَ أَلْسَمَعْنَا فَاتَّبَعُهُ شِهَابٌ مُبِينٌ ﴿٨﴾

“Na hakika Tumeweka katika mbingu, vituo (vya nyota) na Tumezipamba (hizo mbingu) kwa ajili ya wale wanaotizama. Na Tumezilinda na kila shetani ambaye hufukuzwa (kila anapotaka kuja kusikiliza yanayopita huko mbinguni). Lakini asikilizaye kwa wizi, basi mara humfuata kijinga kilicho dhahiri.” (15:16-18)

Kuna ayah nyingi mfano wa Aya hii. Imeelezwa kuwa *Rajim* ina maana ya mtu anayeshambulia kwa maneno. Kwa kuwa shetani hujenga fikra na wasi wasi katika mioyo ya watu. Maana ya kwanza: Ni maarufu na sahihi zaidi.

Bismillahi ni Aya ya Mwanzo ya Al-Fatihah

Masahaba walikuwa wakianza kusoma kitabu cha Allah تعالیٰ kwa *Bismillah*:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu”

Wanazuoni pia wanakubaliana kuwa *Bismillah* ni sehemu ya Ayah katika *Suratu An-Naml*.¹ Wanatofautiana kuwa je ni Aya inayojitegemea kivyake mwanzo wa kila Surah, au ni sehemu ya Aya pale ambapo *Bismillah* ipo mwanzo mwa Surah. Ad-Daraqutni pia amerikodi Hadithi kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ ambayo inaunga mkono Hadithi ya Ibn Khuzaimah. Kauli za aina hiyo zimenasibishwa na Ali, Ibn Abbas na wengineo رضي الله عنهم.²

¹ Surah ya 27.

² Ad-Daraqutni 1:303 na 306.

Rai ya kuwa *Bismillah* ni Ayah ya kila Surah ukiacha *al-Baraah* (Surah ya 9) ilinasibishwa na (Masahaba) Ibn Abbas, Ibn Umar, Ibn Zubayr, Abu Hurayrah na Ali رضي الله عنهم. Rai hii pia ilihusishwa na *Tabiin*: 'Ata', Tawus, Sa'id bin Jubayr, Makhul na Az-Zuhri. Haya pia ni maoni ya 'Abdullah bin Al-Mubarak, Ash-Shafi'i, Ahmad bin Hanbal, Ishaq bin Rahwayh na Abu 'Ubayd, Al-Qasim bin Salam. Kwa upande mwingine, Malik, Abu Hanifa na wafuasi wao walisema kuwa *Bismillah* sio Ayah katika *Al-Fatihah* au Surah yoyote nyingine. Dawud alisema kuwa ni Ayah tofauti mwanzoni mwa kila Surah na sio sehemu ya Surah yenyewe, na rai hii pia ilinasibishwa na Ahmad bin Hanbal.

Kusoma *Bismillahi* kwa Sauti na kwa Siri katika Sala za Kudhihirisha Sauti.

Kusoma *Bismillahi* kimya kunakubalika na wale wanaosema kuwa *Bismillah* sio sehemu ya *Al-Fatihah*. Wanazuoni wanaosema *Bismillahi* ni sehemu ya kila Surah (isipokuwa Surah ya 9) walikuwa na maoni tofauti, baadhi yao, kama Ash-Shafii alisema kuwa *Bismillahi* pamoja na *Al-Fatihah* zisomwe kwa sauti. Haya pia ni maoni ya Masahaba wengi, *Tabiin* na Maimamu wa Waislamu kuanzia *Salaf* na kisha vizazi vilivyofuatia. Mathalan, hii ni rai ya Abu Hurayrah, Ibn 'Umar, Ibn 'Abbas, Muawiyah, 'Umar na Ali رضي الله عنهم – maelezo ni kwa mujibu wa Ibn Abdul Barr na Al-Bayhaqi. Aidha Makhalfu wanne kama alivyori pota al-Khatib walikuwa na rai hii japokuwa ripoti hiyo ina utata. Wanazuoni - *Tabiin* waliotoa *Tafsir* hii ni pamoja na Sa'id bin Jubayr, Ikrimah, Abu Qilabah, Az-Zuhri, Ali bin Al-Hasan, mwanawe Muhammad Said bin Al-Musayyab, Ataa, Tawus, Mujahid, Salim, Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi, Abubakar bin Muhammad bin 'Amr bin Hazam, Abu Wail, Ibn Sirin, Muhammad bin Al-Munkadir, 'Ali bin Abdullah bin 'Abbas, mwanawe Muhammad, Nafi mtumwa aliyeachwa huru na Ibn Umar, Zaydi bin Aslam, 'Umar bin 'Abdul-Aziz, Al-Azraq bin Qays, Habib bin Abi Thabit, Abu Ash-Sha'tha, Mak'hul na 'Abdullah bin Ma'qil bin Muqarrin. Al-Bayhaqi aliwaongeza kwenye orodha 'Abdullah bin Safwan na Muhammad bin Al-Hanafiyyah. Kwa nyongeza Ibn 'Abdul-Barr alimuongeza 'Amr bin Dinar.

Ushahidi walioutegemea wanazuoni hao ni kuwa *Bismillahi* ni sehemu ya *Al-Fatihah*. Hivyo, husomwa kwa sauti kama Aya zingine katika sura hiyo. Aidha an-Nasa'i 2:134 amerekodi katika Sunan yake, Ibn Hibban 3:143 na Ibn Khuzaymah 1:251 katika Sahihi zao na Al-Hakim 1:232 katika Mustadrak, kuwa

siku moja Abu Hurayrah رضى الله عنه alisali na alisoma *Bismillahi* kwa sauti. Alipomaliza kusali alisema, “Nimesali takriban kama alivyokuwa akisali Mtume ﷺ.” (Hadithi hii ni Sahih kwa mujibu wa Ad-Daraqutni 1:307, Al-Khatib na Al-Bayhaqi 2:46). Zaidi ya hayo, katika Sahih Bukhari imerekodiwa kuwa Anas bin Malik رضى الله عنه aliulizwa kuhusu usomaji wa Qur’ani wa Mtume akajibu: “Usomaji wake ulikuwa wa taratibu.” Kisha alionesha mfano kwa kusoma *Bismillahi Ar-Rahman Ar-Rahiim* kwa kuvuta.¹ Pia katika Musnad ya Imam Ahmad, na Sunan ya Abu Dawud, Sahihi ya Ibn Habban na Mustadrak wa Al-Hakim. Imerekodiwa kuwa Umm Salamah رضى الله عنها alisema Mtume ﷺ alikuwa akitenganisha Aya wakati wa kusoma,

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣﴾
مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Shukrani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Mwenye kumiliki siku ya malipo.” (1:1-4).

Ad-Daraqutni ameipa daraja ya Sahih silsila ya upokezi wa hadithi hii². Zaidi ya hayo, Imam Abu Abdullah As-Shafii na Al-Hakim katika Mustadrak, alirekodi kuwa Muawiyah alikuwa Imam, Madina na hakusoma *Bismillah* kwa sauti. Muhajirini waliokuwepo walimkosa kwa hilo. Muawiyah aliposalisha Sala iliyofuatia alisoma *Bismillahi* kwa sauti.³ Hadithi zilizotajwa hapo juu zinatupa ushahidi wa kutosha kuhusiana na rai ya kuisoma *Bismillahi* kwa sauti. Ama kuhusu ushahidi ulio dhidi ya huo ni mchanganuo unaoonesha udhaifu wa usimulizi wa riwaya hizo. Hapa si mahala pa kujadili hilo. Wanazuoni wengine wana msimamo wa kuwa *Bismillahi* haitakiwi kusomwa kwa sauti katika Sala na kuwa hili si jambo lililodumishwa na Makhalifa wanne, pia huo ni msimamo wa ‘Abdullah bin Mughaffal na wanazuoni chungu nzima miongoni mwa *Tabiin* na vizazi vilivyofuatia. Pia ni msimamo wa Madhhabu ya Abu Hanifa, Ath-Thawri na Ahmad bin Hanbal. Imam Malik alisema kwamba *Bismillah* haisomwi kwa sauti wala kimya. Kundi hili limeegemeza hoja yao kutokana na yale aliyoyarekodi Imam Muslim katika sahihi yake kutoka kwa mama Aishah

¹ Fat’hul al-Bari 8:709.

² Ahmad 6:302, Abu Dawud 4:294, Ibn Khuzaymah 1:248, Al-Hakim 2:231, Ad-Daraqutni 1:233.

³ Musnad al-Imam Ash-shafi’i 1:80, Al-Hakim 1:233

ambaye alisema Mtume ﷺ alikuwa akianza Sala kwa kusoma *Takbir* (*Allahu Akbar – Mwenyezi Mungu ni Mkubwa*) na kisha husoma,

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١﴾

“Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote.”

Aidha Sahihi mbili zilirekodi kuwa Anas bin Malik عنه رضي الله alisema, “Nilisali nyuma ya Mtume ﷺ, Abubakar, ‘Umar na ‘Uthman رضي الله عنهم na walikuwa wakianza Sala na,

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٢﴾

“Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote”.

Muslim aliongeza, “Na hawakusoma,

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴿٣﴾

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.”¹

Mwanzo au mwisho wa kisomo.² Hadithi sawa na hii imerekodiwa katika Vitabu vya Sunan kutoka kwa ‘Abdullah bin Mughafal.³

Haya ni maoni ya Maimamu wanaoheshimika na kauli zao zinafanana kwani wanakubaliana kuwa Sala za wanaosoma *Al-Fatihah* kwa sauti au kwa siri zote ni sahihi. Fadhila zote zinatoka kwa Allah تعالى .

Utukufu wa *Al-Fatihah*

Imam Ahmad (5:59) amerikodi ndani ya Musnad wake kuwa mtu alikuwa amempanda mnyama, nyuma ya Mtume ﷺ, akasema, “Mnyama wa Mtume alijikwaa.’ Hivyo nikasema, “Amelaaniwa shetani.” Mtume ﷺ akasema,

«لَا تَقُلْ: تَعَسَّ الشَّيْطَانُ، فَإِنَّكَ إِذَا قُلْتَ: تَعَسَّ الشَّيْطَانُ، تَعَاظَمَ وَقَالَ: بِقُوَّتِي صَرَغَتْهُ، وَإِذَا قُلْتَ: بِاسْمِ اللّٰهِ تَصَاغَرَ حَتَّى يَصِيرَ مِثْلَ الذُّبَابِ»

¹ Ibn Abii Hatim 1:12.

² *Fat’hul Al-Bari* 2:265 na Muslim 1:299.

³ At-Tirmidhi Na. 244.

*“Usiseme, “Amelaaniwa shetani, kwani ukisema maneno haya, Shetani hujigamba na kusema, “Kwa nguvu zangu nimemfanya aanguke.”
“Unaposema “Bismillah, “Shetani atakuwa mdogo kama nzi”.*

Zaidi ya hivyo, An-Nasai aliandika kwenye kitabu chake, *Al-Yawm wal-Laylah*, na pia Ibn Marduwyah katika *Tafsir* ambayo ‘Usamah bin ‘Umar رضي الله عنه alisema, “Nilipanda mnyama nyuma ya Mtume ﷺ...” Na akataja sehemu iliyobaki ya Hadithi ya hapo juu. Mtume ﷺ alisema katika masimulizi yake,

«لَا تَقُلْ هَكَذَا فَإِنَّهُ يَتَعَاظَمُ حَتَّى يَكُونَ كَالنَّبِيِّ، وَلَكِنْ قُلْ: بِسْمِ اللَّهِ، فَإِنَّهُ يَضَعُرُ حَتَّى يَكُونَ كَالذُّبَابَةِ».

“Usiseme maneno haya kwani Shetani atakuwa mkubwa kama nyumba. Bali sema, “Bismillah” kwa sababu Shetani anakuwa mdogo kama nzi.”¹

Hizi ni Fadhila za kusoma *Bismillah*.

Imependekezwa Kusoma *Bismillah* Kabla ya Kufanya kila Jambo.

Imependekezwa kusoma *Bismillah* kabla ya kuanza jambo au kufanya kitendo. Matalani, *Bismillah* inapendekezwa kusomwa kabla ya Khutba. *Bismillah* pia inapendekezwa kusomwa kabla mtu hajaingia mahali pa kujisaidia, kuna hadithi inayoelezea suala hili.² Zaidi ya hivyo *Bismillah* inapendekezwa kusomwa wakati wa kuanza kutawadha. Inaelezwa kuwa Imam Malik na wakusanyaji wa Sunan walirekodi kutoka kwa Abu Hurayrah, Sa'id bin Zayd na Abu Sa'id رضي الله عنهم walipokea kutoka kwa Mtume ﷺ,

«لَا وَضُوءَ لِمَنْ لَمْ يَذْكُرِ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ»

“Hakuna Udhu kwa ambaye hakutaja Jina la Mwenyezi Mungu juu yake.”³

Hadithi hii ni Hasan (nzuri). Aidha *Bismillah* imependekezwa kabla ya kuanza kula kwani Muslim alirekodi katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alimuambia, ‘Umar bin Abi Salamah رضي الله عنه alipokuwa mtoto chini ya ulezi wake,

¹ An-Nasa'i katika Al-Kubra 6:142.

² 'Awn Al-Ma'bud 1:6.

³ Ahmad 3:41, Abu Dawud 1:75, Tuhfat Al-Ahwadhi 1:115, an-Nasa'i 1:61 na Ibn Majah 1:140.

«قُلْ بِسْمِ اللَّهِ وَكُلُّ بِيَمِينِكَ وَكُلُّ مِمَّا يَلِيكَ»

“Sema Bismillahi, kula kwa mkono wako wa kulia na ule kilicho mbele yako.”¹

Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa *Bismillah* kabla ya kula ni wajibu. *Bismillah* kabla ya jimai imekokotezwa. Sahih mbili zimerikodi kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ إِذَا أَرَادَ أَنْ يَأْتِيَ أَهْلَهُ قَالَ: بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُمَّ جَنَّبْنَا الشَّيْطَانَ وَجَنَّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا، فَإِنَّهُ إِنْ يَقْدَرُ بَيْنَهُمَا وَلَدٌ لَمْ يَضُرَّهُ الشَّيْطَانُ أَبَدًا»

“Mmoja wenu kabla hajajamiiana na mkewe aseme, “Bismillah, Ewe Allah tukinge na shetani na tuhifadhie utakachoturuzuku (yaani watoto) kutokana na shetani, na endapo wameandikiwa kuwa na mtoto, abadani shetani hatoweza kumdhuru mtoto huyo.”²

Maana ya *Lafdhul - Jalaalah “Allah”*

Allah تعالى ni Jina la Bwana, Aliyetukuka. Inasemwa kuwa Allah تعالى ni Jina Kubwa kuliko mengine ya Allah تعالى kwani linatumika wakati wa kumuelezea Allah تعالى kwa Sifa Zake mbalimbali. Matalani, Allah تعالى Amesema,

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلِيمٌ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿١٧﴾ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٨﴾ هُوَ اللَّهُ الْخَلِيقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٩﴾

“Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Ambaye Hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu. Anayeyajua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri. Mwenye Kuneemesha Neema kubwa kubwa na Mwenye Kuneemesha Neema ndogo ndogo. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu, Mfalme,

¹ Muslim 3:1600.

² Fat’hul Al-Bari 9:136, Muslim 2:1058.

Mtakatifu, Mwenye Salama, Mtoaji wa Amani, Mwenye Kuyaendesha Mwenyewe mambo Yake, Mwenye Shani, Anayefanya Analotaka, Mkubwa, Mwenyezi Mungu Yu mbali na hao wanaomshirikisha Naye. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mfanyaji wa sura (za namna za viumbe); Mwenye Majina (Sifa) Mazuri. Kinamtukuza kila kilichomo mbinguni na ardhini. Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hekima.” (59:22-24).

Hivyo Allah تعالی Ametaja Majina Yake mengi kama Sifa za Neno Lake Allah تعالی. Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا^ط

“Na Mwenyezi Mungu Ana Majina Mazuri Mazuri basi muombeni kwayo....” (7:180) na, Allah تعالی Amesema;

قُلْ ادْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ^ط

“Sema, “Muombeni (Mwenyezi Mungu) kwa (Jina la) Allah au Muombe (kwa Jina la) Rahman; kwa Jina lolote mnalomuita (katika haya itafaa); kwani Ana Majina Mazuri Mazuri.” (17:110)

Aidha, Sahih zimerikodi kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِلَّهِ تِسْعَةَ وَتِسْعِينَ اسْمًا، مِائَةٌ إِلَّا وَاحِدًا، مَنْ أَحْصَاهَا دَخَلَ الْجَنَّةَ»

“Hakika Allah Ana Majina tisini na tisa, mia moja kasoro moja, yeyote atakayeyahifadhi, ataingia Peponi.”¹

Majina haya yalitajwa ndani ya Hadithi iliyorekodiwa na At-Tirmidhi na Ibn Majah na kuna tofauti nyingi kati ya Masimulizi (Mapokezi) hayo mawili.

Maana ya Ar-Rahman Ar-Rahim – Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

Ar-Rahman Ar-Rahim ni majina mawili yaliyotokana na *Ar-Rahmah* (Huruma), lakini *Rahman* ina maana zaidi inayohusika na huruma kuliko *Ar-Rahim*. Kuna kauli ya Ibn Jarir رحمه الله تعالی ambayo inaonesha kuna makubaliano katika maana tuliyoieleza. Kwa ziada Al-Qurtubi رحمه الله تعالی alisema; “Ushahidi kuwa maneno

¹ Fat'h Al-Bari 11:218, Muslim 4:2062.

haya yanatokana na 'Ar-Rahmah' ni kama alivyorikodi At-Tirmidhi na kupewa daraja la Sahih kutoka kwa 'Abdur-Rahman bin 'Awf, kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«قَالَ اللهُ تَعَالَى: أَنَا الرَّحْمَنُ خَلَقْتُ الرَّجِمَ وَشَقَقْتُ لَهَا اسْمًا مِنْ اسْمِي، فَمَنْ
وَصَلَّيَهَا وَصَلَّتْهُ رَمَنْ قَطَعَهَا قَطَعْتَهُ»

"Allah Aliyetukuka Amesema, Mimi ni Ar-Rahman. Niliumba Rahim. (fuko la uzazi) na Nikatoa (Nikalipa Rahima) jina kutokana na Jina Langu. Hivyo atakayeunga na kuenzi udugu nalo, Nitaunga mahusiano naye, na yeyote atakayeukata udugu, Nitamkata mahusiano naye."

Kisha akasema, "Haya ni maandiko yanayoonesha chimbuko la neno." Kisha akasema, "Waarabu walikanusha neno Ar-Rahman kwa sababu ya ujinga wao kuhusu Allah na Sifa Zake."

Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema, "Ilisemwa kuwa maneno yote mawili, Ar-Rahman na Ar-Rahiim yana maana sawa, kama ilivyo kwa maneno Nadman na Nadiim, kama Abu Ubayd alivyofahamisha. Abu Ali Al-Farisi alisema, "Ar-Rahman"¹ ambalo ni mahsusi kwa Allah تعالى, ni Jina ambalo linajumuisha aina zote za huruma Alizonazo Allah تعالى. Ar-Rahiim ni huruma inayowahusu Waumini tu. Kwa hivyo Allah تعالى Amesema,

وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴿٣٣﴾

***"Naye ni Mwenye Kuwarehemu sana Waislamu."* (33:43)**

Aidha Ibn Abbas عنهما رضي الله عنهما alizungumzia juu ya Ar-Rahman na Ar-Rahiim, "Ni maneno yenye huruma, moja linaonesha huruma zaidi kuliko jengine."² Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema; as-Sarri bin Yahya at-Tamimi kutoka kwa Uthman bin Zufar alielezea kuwa Al-Azrami alizungumzia kuhusu Ar-Rahman na Ar-Rahiim, "Yeye ni Ar-Rahman kwa viumbe wote na Ar-Rahiim kwa Waumini tu."³ Hivyo Kauli ya Allah تعالى Inaelezea,

ثُمَّ أَسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ عَلَى الرَّحْمَنِ

"Kisha Akakaa juu ya Arshi (Yake), (na hali ya kuwa ni) Mungu Mwenye Huruma..." (25:59) na Amesema,

¹ Tuh'fatu Al-Ahwadhi 6:33.

² Tafsir Al-Qurtubi 1:105.

³ At-Tabari 1:127.

الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿٢٠﴾

“Ndiye Mungu Mwenye Rehema Aliyekaa juu ya Kiti (Chake) cha Enzi.” (20:5).

Allah تعالى Ametaja Istawa – Aliyekaa juu ya Kiti cha Enzi pamoja na Jina Lake, Ar-Rahman, kuonesha kuwa Huruma inawaenea viumbe Wake wote. Allah تعالى pia Amesema,

وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴿٤٣﴾

“Na daima Anawarehemu Waumini.” (33:43)

Hivyo kuwajumuisha Waumini na Jina Lake Ar-Rahiim. Wamesema, “Hii inathibitisha ukweli kwamba Ar-Rahman inachukua maana pana zaidi inayofungamana na Huruma ya Allah تعالى kwa viumbe Vyake duniani na Akhera. Hata hivyo Ar-Rahiim ni mahsusi kwa Waumini tu.” Ijapo imekuja katika dua neno “Rahiim” kwa matumizi yote ya Duniani na Akhera,

«رَحْمَنَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَرَحِيمَهُمَا»

“Arrahman’ - Mwingi wa Rehema wa dunia hii na Akhera na Ndiye “Rahiim” - Mwenye Kuwaonea huruma viumbe Vyake vyote.”

Jina la Ar-Rahman ni maalumu Kwake Allah تعالى. Mathalani, Allah تعالى Anasema,

قُلْ أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيُّمَا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ﴿١١٠﴾

“Sema (Ewe Muhammad), “Muombeni (Mwenyezi Mungu) kwa (Jina la) Allah au Muombeni (kwa Jina la) Rahman; kwa Jina lolote mnalomuita (katika haya Inafaa); kwani Ana Majina Mazuri Mazuri.” (17:110). Na Allah تعالى Amesema,

وَسَأَلَ مَنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾

“Na kawaulize Mitume Wetu Tuliowaleta kabla yako; “Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Mwingi wa Rehema.” (43:45).

Zaidi ya hayo, wakati Musaylamah mrongo alipojiita Rahman wa Yamamah, Allah تعالى Alimfanya atambulike kwa jina la Mrongo wa Al-Yamama na kumfedhehesha. Hivyo kila Musaylama alipotajwa, alielezwa kama “Mrongo”. Alipigiwa mfano wa mtu muongo katika wakazi wa mji, vijiji na mabedui - wakazi wa Jangwani.

Kwa hiyo kwanza, Allah تعالى Alitaja Jina Lake – Allah تعالى – ambalo ni mahsusi Kwake na Akalielezea Jina hili kwa *Ar-Rahman* ambalo hakuna yeyote mwingine anayeruhusiwa kulitumia. Kama Allah تعالى Alivyosema,

قُلْ أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيُّمَا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

“Sema (Ewe Muhammad), “Muombeni (Mwenyezi Mungu) kwa (Jina la) Allah au Muombeni (kwa Jina la) Rahman; kwa Jina lolote mnalomuita (katika haya inafaa); kwani Ana Majina Mazuri Mazuri.” (17:110).

Musaylamah ndiye aliyejipachika jina la *Ar-Rahmani*. Na wafuasi wake wapotofu nao walimuita kwa jina hilo.

Ama kuhusu Jina la Allah تعالى, *Ar-Rahim*, Allah تعالى Amewaelezea wengine kwa jina hilo. Kwa mfano Allah تعالى Alisema,

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ

بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٩٨﴾

“Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.” (9:128).

Allah تعالى Ameelezea baadhi ya Viumbe Vyake Akitumia Majina Yake mengine. Mathalani, Allah تعالى Amesema,

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢٠٠﴾

“Kwa hakika Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika; (ya mwanaume na mwanamke) ili Tumfanyie mtihani (kwa Amri Zetu na Makatazo Yetu); kwa hivyo Tukamfanya ni mwenye kusikia (na) mwenye kuona.” (76:2).

Kwa kuhitimisha, kuna Majina Mengi ya Allah تعالى yanayotumika kwa viumbe. Na kuna mengine hayafai kutumika kwa viumbe. Baadhi ya Majina ya Allah تعالى ni mahsusi kwa Allah تعالى Peke Yake, kwa mfano, Allah تعالى, *Ar-Rahman*, *Al-Khaliq* (Muumba), *Ar-Razaq* (Mliahaji) na kadhalika.

Hivyo, na kwa kuzingatia hilo, ameanza kwa jina la “Allah تعالیٰ” na Akaelezea kwa wasifu wa “Ar-Rahman”. Kwa maana, Mwingi wa Rehema limeonesha huruma zaidi ya Ar-Rahim na linawahusu wengi. Majina yenye heshima zaidi yametajwa mwanzo kama Alivyofanya Allah تعالیٰ hapa.

Katika Hadithi iliyosimuliwa na Umm Salamah رضي الله عنها ameeleza kuwa usomaji wa Qur'an wa Mtume ﷺ ulikuwa taratibu na wa wazi, herufi kwa herufi,

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣﴾
مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾

“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Shukrani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Mwenye Kumiliki siku ya malipo.” (1:1-4).¹

Na hivi ndivyo baadhi ya wanazuoni walivyoisoma. Wengine waliunganisha usomaji wa Bismillah na Al-Hamdu.

﴿١﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾

“Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu wote”.

Maana ya Al-Hamd

Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى amesema, “Maana ya,

الْحَمْدُ لِلَّهِ

“Al-Hamdu Lillah.” Ni ‘Shukrani zote Anastahiki Mwenyezi Mungu.’ Shukrani zote Anastahiki Mola Pekee na sio vitu vinavyoabudiwa badala ya Allah تعالیٰ au viumbe Vyake. Shukrani hizi ni stahiki ya Ukarimu na Fadhila za Allah تعالیٰ zisizo na kifani, bali Yeye Pekee Ndiye Anayefahamu. Ukarimu wa Allah تعالیٰ ni pamoja na Kuumba chombo ambacho kinasaidia viumbe kumuabudu Yeye, mwili ambao wanaoutumia kutekeleza Maamrisha Yake, na uhimili Anaowapatia katika maisha, na maisha ya raha Aliyowapatia waja Wake bila ya kutaraji malipo au kulazimishwa kufanya hivyo. Allah تعالیٰ pia Aliwaonya

¹ Musnad Ahmad (26042) lakini kwa tamko la Aya kwa Aya.

viumbe Wake na Akawataka wawe makini kufuata njia ambazo zitawafikisha katika makazi ya kudumu ya nyumba yenye furaha ya milele. Shukrani zote zinamstahikia Allah تعالى kwa Ukarimu Wake kuanzia mwanzo mpaka mwisho.”¹

Ibn Jariri رحمته الله تعالى pia ameitolea maelezo yafuatayo Ayah hii,

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ

“**Al-Hamdu Lillah**” Ina Maana: “Sifa Alizojisifu Allah تعالى ikiwa ni ishara kwa waja Wake kuwa nao wamsifu pia.” Katika Ayah hii kana kwamba Allah تعالى Anasema, “Sema; Shukrani na Sifa zote Anastahiki Allah تعالى.” Pia ilisemwa kuwa kauli hii,

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ

“**Shukran na Sifa zote Anastahiki Allah.**” Inahitaji kumshukuru Allah تعالى kwa kuyataja Majina Yake Mazuri na Sifa Zake Adhimu. Mtu anaponadi, “Shukrani zote Anastahiki Allah تعالى (As-Shukru Lillah), atakuwa anamshukuru kwa Ukarimu na Fadhila Zake.”²

Tofauti Iliyopo Baina ya **Al-hamdu** na **Ash-shukru** (Kusifu na Kushukuru)

Uhakiki wa kina umefanywa kubainisha tofauti baina ya maneno mawili haya, kwa mujibu wa sarufi ya lugha ya kiarabu. Maneno haya hutumika kwa maana pana zaidi, vilevile yana maana mahususi, kulingana na matumizi ya maneno hayo.

Neno “**Hamdu**,” Maana yake ni: Kusifu, lina matumizi mapana zaidi kuliko neno “**shukru**,” Lenye maana ya: Shukrani kulingana na mahali lilipo. Kwa sababu neno “**Hamdu**” hutumika katika sifa zinazolazimiana na muhusika tu, na wala hazipenduki kwa mwengine. Mfano, “Nimempa **Hamdu** kutokana na uhodari wake wa kwenda mbio na farasi.” Vilevile neno “**Hamdu**” hutumika kwa sifa zinazopenduka kwa mtu mwengine. Mfano, “Nimemsifia kwa sababu ya ukarimu wake juu yangu.” Kwa upande mwengine neno “**Hamdu**” linakuwa na maana mahususi. Kwa sababu halitumiwi isipokuwa kwa njia ya kauli tu.

Na neno “**Shukru**” Kwa maana: Shukrani, lina matumizi mapana zaidi kulingana na mahali lilipo. Kwa sababu hutumika kwa njia ya kauli, kitendo na dhamira.

¹ At-Tabari 1:135.

² At-Tabari 1:137.

Na kwa upande mwingine neno “*Shukru*” linakuwa mahususi matumizi yake, kwa mtu mwingine. Mfano, “Nimemshukuru kwa ukarimu wake juu yangu na wema alionitendea.” Na huwezi kutumia kwa kusema, “Nimemshukuru kwa kwenda kwake mbio na Farasi.” Allah تعالى Ndio Mjuzi.

Kauli ya Wanazuoni (*Salaḥ*) kuhusu *Al-Hamd*

Hafsa رضي الله عنها ametaja kuwa ‘Umar رضي الله عنه alimuuliza Ali رضي الله عنه, “Tunajua La ilaha illallah, Subhana Llahna Allahu Akbar. Vipi kuhusu *Al-Hamdu Lillah*?” Ali رضي الله عنه akajibu, “Ni kauli ambayo Allah تعالى Aliipenda kwa ajili Yake na Alipendezwa nayo. Alipenda isemwe.”¹ Pia Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema,² “*Al-Hamdu Lillah* ni tamko la Shukrani.” Mja anaposema: “*Al-Hamdu Lillah*, Allah Husema, “Mja Wangu amenishukuru.” Hadithi hii imenukuliwa na Ibn Hatim رحمه الله تعالى.³

Fadhila za *Al-Hamd*

Imam Ahmad bin Hanbal aliandika kuwa Al-Aswad bin Sari رضي الله عنه alisema, “Nilisema, Ewe Mtume! nikusomee maneno ya kumsifu Bwana Wangu, Mwenye Cheo, ambayo nimeyakusanya?” Akasema,

«أَمَّا إِنَّ رَبَّكَ يُحِبُّ الْحَمْدَ»

“Kwa hakika Mola Wako Anapenda *Al-Hamd*.”

An-Nasa’i pia ameandika Hadithi hii.⁴ Zaidi ya hivyo Abu Isa at-Tirmidhi, An-Nasa’i na Ibn Majah wameandika kuwa Musa bin Ibrahim bin Kathir walisimulia kuwa Talha bin Khirash alisema kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَفْضَلُ الذِّكْرِ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَفْضَلُ الدُّعَاءِ الْحَمْدُ لِلَّهِ»

“*Dhikr (Kumkumbuka Allah) bora ni La ilaaha illallah, na dua bora ni Alhamdulillah.*”

At-Tirmidhi amesema Hadithi hii ni Hasan *Gharib*.⁴ Ibn Majah pia, amesimulia kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:15.

² Hii haikuthibiti kutoka kwa Ibn Abbas, katika isnadi kuna Ali bin Zayd ambaye ni dhaifu

³ Ibn Abi Hatim 1:13.

⁴ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:324, An-Nasa’i katika Al Kubra 6:208, Ibn Majah 2:1249.

«مَا أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيَّ عَبْدِي نِعْمَةً فَقَالَ: الْحَمْدُ لِلَّهِ، إِلَّا كَانَ الَّذِي أُغْطِيَ أَفْضَلَ مِنِّي
أَخَذَهُ»

“Hakika Allah Hajamneemesha mja yoyote neema na akasema, “Al-Hamdu Lillah” ila kinakuwa kile alichopewa ni bora kuliko alichochukua.”¹

Aidha, katika Sunan yake, Ibn Majah (2:1249) ameandika kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ عَبْدًا مِنْ عِبَادِ اللَّهِ قَالَ: يَا رَبِّ لَكَ الْحَمْدُ كَمَا يَنْبَغِي لِجَلَالِ وَجْهِكَ وَعَظِيمِ سُلْطَانِكَ. فَعَصَلْتُ بِالْمَلَائِكِينَ فَلَمْ يَذَرِيَا كَيْفَ يَكْتُبَانِيهَا فَصَعِدَا إِلَى اللَّهِ فَقَالَا: يَا رَبَّنَا إِنَّ عَبْدًا قَدْ قَالَ مَقَالَةً لَا نَدْرِي كَيْفَ نَكْتُبُهَا، قَالَ اللَّهُ، وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا قَالَ عَبْدُهُ: مَاذَا قَالَ عَبْدِي؟ قَالَا: يَا رَبِّ إِنَّهُ قَالَ: لَكَ الْحَمْدُ يَا رَبِّ كَمَا يَنْبَغِي لِجَلَالِ وَجْهِكَ وَعَظِيمِ سُلْطَانِكَ. فَقَالَ اللَّهُ لَهُمَا: اكْتُبَاهَا كَمَا قَالَ عَبْدِي، حَتَّى يَلْقَانِي فَأَجْزِيَهُ بِهَا.»

“Mmoja miongoni mwa waja wa Allah alisema, Ewe Allah! (Himd) Shukrani zote ni Zako kadiri Unavyostahiki kwa Utukufu wa Dhati Yako na Ukubwa wa Mamlaka Yako.” Malaika wawili wakatatizika namna ya kuyaandika. Wakapanda kwa Allah na kusema, “Kwa hakika. Mja Wako ametamka maneno ambayo hatujui namna ya kuyaandika.” Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi wa alichokisema Mja Wake. Akasema, “Mja Wangu ametamka nini?” Wakasema, “Ewe Mola Wetu! Amesema, “Shukrani zote ni Zako kadiri Unavyostahiki Utukufu wa Dhati Yako na Ukubwa wa Mamlaka Yako.” Mwenyezi Mungu Akawaambia, “Yaandikeni kama alivyoyasema mja Wangu, hadi atakapokutana na Mimi, Nitamlipa.”²

Maana ya ‘Al’ Kabla ya Neno *Hamd*

Al kabla ya *Hamd* inajumuisha aina zote za Shukrani kwa Allah تعالى. Herufi *Alif* na *Lam* kabla ya neno *Hamd* zinajumuisha aina zote za Shukrani kwa Allah تعالى. Hadithi inaeleza,

¹ Ibn Majah 2:1250.

² Ibn Majah 2:1249.

«اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ كُلُّهُ، وَلَكَ الْمُلْكُ كُلُّهُ، وَبِيَدِكَ الْخَيْرُ كُلُّهُ، وَإِلَيْكَ يُرْجَعُ الْأَمْرُ كُلُّهُ»

“Ewe Mola! Shukrani zote ni Zako, Miliki yote ni Yako, kila lililo la kheri limo Mkononi Mwako, na mambo yote hurejea Kwako.”¹

Maana ya *Ar-Rabb*, Bwana.

Ar-Rabb ni Mmiliki ambaye ana madaraka yote juu ya mali yake. *Ar-Rabb* kilugha ya kiarabu ina maana ya Bwana au yule mwenye mamlaka ya kuongoza. Maana zote hizi ni sahihi kwa Allah تعالى. Neno *Rabb* linatumika kwa Allah تعالى Peke Yake. Matumizi ya *Rabb* kwa viumbe wengine inaweza kutumika kwa kuongeza neno lingine, kwa mfano, *Rabb Ad-Dar*, yaani Mmiliki wa nyumba. Aidha imeelezwa kuwa *Ar-Rabb* ni jina kubwa kuliko yote ya Allah تعالى na linatumika Kwake Yeye tu.

Maana ya *Al-'Alamin* (viumbe wote)

Al-'Alamini ni wingi wa “*Alam*” ambayo inajumuisha kila kitu kinachoishi isipokuwa Allah تعالى. Neno ‘*Alam* pia ni wingi na hapana umoja wake. ‘*Awalim* ni aina tofauti ya viumbe vinavyoishi mbinguni na ardhini, juu ya ardhi na baharini. Kila kizazi cha uumbwaji kinaitwa *Alam*. Al-Farra na Abu Ubayd wamesema, “*Alam* ni pamoja na vyote vyenye akili, Majini, Binadamu, Malaika na Mashetani lakini sio Wanyama...” Pia Zayd bin Aslam na Abu Muhaysin wamesema, “*Alam*” inahusisha vyote vyenye roho vilivyoyumbwa na Allah تعالى.” Zaidi ya hayo Qatadah amesema kuhusu,

رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١١﴾

“Bwana wa *Alamin*”. “Kila aina ya uumbaji ni ‘*Alam*.” Az-Zajjaj pia amesema, “‘*Alam* inajumuisha kila kilichoumbwa na Allah تعالى, katika maisha ya dunia na akhera.” Al-Qurtubi رحمه الله تعالى amethibitisha kuwa, “Maana hii ni sahihi, yaani ‘*Alam* inahusisha kila kitu Alichokiumba Allah تعالى katika dunia zote (Mbingu na Ardhi).” Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

قَالَ فِرْعَوْنُ وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿١١﴾ قَالَ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ إِنَّ

كُنتُمْ مُوقِنِينَ ﴿١٢﴾

¹ At-Tarhib wa Tarhib 2:253.

“Firauni akasema: Na nani huyo Mola wa Walimwengu? (Musa) Akasema: “Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, ikiwa nyinyi ni wenye yakini (ya jambo, bora yakinisheni hili).” (26:23-24)

Kwa nini Uumbaji Unaitwa ‘Alam?

‘Alam inatokana na ‘Alamah kwa sababu ni alama inayothibitisha kuwepo kwa Muumbaji Wake na Tawhidi Yake.¹

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١٥﴾

“Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.” Ar-Rahman (Mwingi wa Rehema), Ar-Rahim (Mwenye Kurehemu). Tumeyaeleza Majina haya katika Bismillah. Al-Qurtubi رحمه الله تعالى amesema, “Allah تعالى Amejielezea Mwenyewe kuwa ni Ar-Rahman, Ar-Rahim baada ya kusema, “Bwana wa Alamin.” Hivyo Kauli Yake hapa inahusu onyo na kisha kushajiisha.” Aidha Allah تعالى Anasema:

* نَبِيَّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٥﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿١٦﴾

“Waambieni waja Wangu ya kwamba Mimi ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu. Na hakika Adhabu Yangu ni Adhabu inayoumiza kweli kweli.” (15:49-50)² Allah تعالى Amesema,

إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٦﴾

“Hakika Mola Wako ni Mwepesi wa Kuadhibu, na hakika ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu kwa wale wanaorejea Kwake.” (6:165)

Hivyo Rabb inamaanisha onyo, wakati Ar-Rahman Ar-Rahim, Ina maana kutia moyo. Zaidi ya hayo, Muslim ameandika katika Sahihi yake kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَوْ يَعْلَمُ الْمُؤْمِنُ مَا عِنْدَ اللَّهِ مِنَ الْعُقُوبَةِ مَا طَمَعَ فِي جَنَّتِهِ أَحَدٌ، وَلَوْ يَعْلَمُ الْكَافِرُ مَا عِنْدَ اللَّهِ مِنَ الرَّحْمَةِ مَا قَنَطَ مِنْ رَحْمَتِهِ أَحَدٌ»

“Lau Waumini wangejua Adhabu zilizoandaliwa na Allah, hapana ambaye atakayetaraji kuipata Pepo, na makafiri wangejua Huruma ya Allah, hapana Kafiri ambaye angeikatia tamaa kuipata Huruma Yake.”²

¹ Al-Qurtubi 1:139.

² Al-Qurtubi 1:139.

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿١٧﴾

“Mwenye Kumiliki Siku ya malipo.”

Maana ya Allah تعالی Kuuhusisha Utawala Wake na Siku ya Malipo.

Allah تعالی Ametaja Utawala Wake Siku ya Malipo, lakini hii haitengui Utawala kwa vitu vingine. Kwani Allah تعالی Ametaja kuwa Yeye ni Bwana wa Maisha ikiwa ni pamoja na Maisha ya Dunia na Akhera. Allah تعالی Ametaja Siku ya Malipo hapa kwa sababu siku hiyo, hakuna mwingine isipokuwa Yeye tu Ndiye Atadai umiliki wa vitu vyote. Siku hiyo hakuna atakayeruhusiwa kusema chochote bila ruhusa Yake. Aidha Allah تعالی Amesema,

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلٰئِكَةُ صَفًّا لَا يَتَكَلَّمُونَ اِلَّا مَنْ اٰذِنَ لَهُ الرَّحْمٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿١٧﴾

“Siku ambayo zitasimama Roho (za viumbe wote) na Malaika safu safu, hatasema siku hiyo ila yule ambaye (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema Amempa idhini (ya kusema) na atasema yaliyo sawa.” (78:38). Na Allah تعالی Amesema,

وَحَشَعَتِ الْاَصْوَاتُ لِلرَّحْمٰنِ فَلَا تَسْمَعُ اِلَّا هَمْسًا ﴿١٨﴾

“Na sauti zote zitamnyenyekea Ar-Rahman Mwingi wa Rehema. Basi husikii ila mchakato na mnong’ono.” (20:108)

يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلَّمُ نَفْسٌ اِلَّا بِاِذْنِهِ ؕ فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ ﴿١٩﴾

“Wakati itakapokuja (siku hiyo) kiumbe chochote hakitasema ila kwa ruhusa Yake (Mwenyezi Mungu); basi baadhi yao watakuwa wenye hali mbaya (Nao ni wale waasi) na (wengine) wenye hali nzuri (Nao ni wale wema).” (11:105)

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿١٧﴾

“Mwenye Kumiliki siku ya Malipo.”

“Allah تعالی Amesema, “Siku hiyo hapana mtu atakayemiliki chochote katika vile alivyokuwa akimiliki duniani.”

Maana ya *Yawm Ad-Diin* (Siku ya Malipo)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Yawm Ad-Diin* ni Siku ya Fidia kwa viumbe, ikiwa na maana ya Siku ya Hukumu. Siku hiyo Allah تعالى Atawalipa viumbe kwa matendo yao, uovu kwa uovu, mema kwa mema, isipokuwa wale Atakaowasamehe.”¹ Kadhalika wamesema kama hivyo, Masahaba wengine, *Tabiin* na Wanazuoni wa *Salaf* walisema kama hivyo, kwani maana hii ni dhahiri na wazi kutoka katika Aya.

Allah تعالى ni *Malik* (Mfalme Mwenye Mamlaka Makuu au Mmiliki)

Allah تعالى Ndiye Mmiliki wa Kweli (*Malik*) wa kila kitu na kila mmoja. Allah تعالى Amesema,

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ

“Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu; Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Salama...”
(59:23)

Aidha Sahihi mbili zimeandika, Abu Hurayra رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَخْبَعُ اسْمَ عِنْدَ اللَّهِ رَجُلٌ تَسْمَى بِمَلِكِ الْأَمْلاكِ وَلَا مَالِكَ إِلَّا اللَّهُ»

“Jina dhalili mno kwa Allah ni mtu anayejiita Mfalme wa wafalme, wakati hakuna mmiliki wa vyote isipokuwa Allah.”²

Pia Sahihi mbili zimeandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُقْبِضُ اللَّهُ الْأَرْضَ وَيَطْوِي السَّمَاءَ بِيَمِينِهِ ثُمَّ يَقُولُ: أَنَا الْمَلِكُ، أَيْنَ مُلُوكِ الْأَرْضِ؟ أَيْنَ الْجَبَّارُونَ؟ أَيْنَ الْمُتَكَبِّرُونَ؟»

“(Siku ya Hukumu) Allah Ataishika Dunia na Atazikunja mbingu kwa Mkono Wake wa Kulia na Atatangaza, “Mimi Ndiye Mfalme! Wako wapi wafalme wa duniani? Wako wapi madikteta? Wako wapi mafidhuli?”³

Aidha ndani ya Qur’an tunasoma:

¹ Ibn Abi Hatim 1:19.

² Fat’hul 1:604 na Muslim 3:1688.

³ Fat’hul Al-Bari 13:404 na Muslim 4:2148.

لَمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ ۖ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٦﴾

“...Leo Ufalme ni wa nani? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye Nguvu (za Kufanya Atakalo).” (40:16)

Kuhusu kumuita mtu Mfalme zaidi ya Allah تعالى katika maisha ya duniani imefanyika kama tamathali ya usemi. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا

“Mwenyezi Mungu Amekuchagulieni Taluti kuwa Mfalme”. (2:247)

وَكَانَ وَرَاءَهُمْ مَلِكٌ

“Kwani mbele yao kulikuwa na Mfalme.” (18:79)

جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُلُوكًا

“Alipowafanya Manabii kwenu (wenyewe) na Akakufanyeni watawala.” (5:20) Maana: Wafalme.

Pia Sahihi mbili zimeandika,

«مِثْلُ الْمُلُوكِ عَلَى الْأَسِيرَةِ»

“Mfano wa wafalme waliotandawaa katika viti vyao vya enzi.”¹

Maana ya Ad-Din (Malipo)

Ad-Din maana yake ni kuhesabiwa, malipo au adhabu. Vivyo hivyo Allah تعالى Anasema,

يَوْمَئِذٍ يُؤْقِرُ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ

“Siku hiyo Mwenyezi Mungu Atawapa sawasawa malipo yao ya haki.” (24:25) Na Allah تعالى Amesema;

أَنَا لَمَدِينُونَ ﴿٥٣﴾

“... (Tutafufuliwa) tulipwe (kwa tuliyoyafanya).” (37:53)

Maana: Tatalipwa na kuhesabiwa. Na imekuja katika Hadithi ya Mtume ﷺ;

¹ Fat’hul Al-Bari 6:89 and Muslim 3:1518.

«الْكَيْسُ مَنْ دَانَ نَفْسَهُ وَعَمِلَ لِمَا بَعْدَ الْمَوْتِ»

“Mtu mwerevu ni yule anayejihesabu Mwenyewe na anafanya amali njema kwa ajili ya maisha yajayo baada ya mauti.”¹

Maana yake: Mtu mwenye kuwajibika anaihesabu nafsi yake. Pia, Umar رضي الله عنه alisema, “Jiwajibishe Mwenyewe kabla hujawajibishwa, jipime kabla hujapimwa, na jiandae na mkusanyiko mkubwa mbele ya Yule Ambaye Elimu Yake imefunika matendo yenu.”

يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَىٰ مِنكُمْ حَافِيَةٌ ﴿١٨﴾

“Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yenu yeyote.” (69:18)

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba Msaada.” (1:5)

Maana ya Neno “Ibadah” Kilugha na Kidini

Kilugha ‘*ibadah*’ ina maana ya udhalili (utii). Kwa mfano, barabara inaelezwa kama *Mu’abbadah*, au ngamia *Mu’abbad* ikiwa na maana kwamba amefanywa dhalili (ametiishwa). Katika maana ya kidini, *Ibadah* maana yake ni ibara inayojumuisha ukamilifu katika upendo, unyenyekevu na woga.

Faida ya Kutanguliza Kutaja Mtendwa Kabla ya Kitendo na Kugeuka

Allah تعالى Amemtanguliza mtendewa, kwa kusema: “Wewe...” Maana yake tunakuabudu Wewe Peke Yako na hapana mwingine, na tunakutegemea Wewe Pekee na hapana mwingine. Huu ndio utiifu uliokamilika na Dini yote imejengwa katika misingi ya maana mbili za maneno haya. Na kwa kuzingatia hilo, baadhi ya *Salaf* wamesema, *Al-Fatihah* ni siri ya Qur’an wakati maneno haya mawili ni siri ya *Al-Fatihah*.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba Msaada.” (1:5)

¹ Ibn Majah 2:1423.

Sehemu ya kwanza ni tangazo la kutojihusisha na ushirikina, wakati sehemu ya pili inakanusha kuwa na nguvu au uwezo wowote, na inaonesha kutambua kuwa mambo yote yanaongozwa na Allah تعالیٰ Pekee. Maana hii inatajwa katika sehemu tofauti ndani ya Qur'an.

Kwa mfano, Allah تعالیٰ Anasema,

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ۗ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٢٣﴾

“Basi muabudu Yeye, umtegemee Yeye. Na Mola Wako Mlezi Haghafiliki na yale mnayoyatenda...” (11:123)

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ أَمَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا ۗ

“Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na Yeye tu tunamtegemea”. (67:29)

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٧٣﴾

“(Yeye Ndiye) Mola wa Mashariki na Magharibi – hakuna muabudiwa ila Yeye, basi mfanye kuwa Mlinzi (wako).” (73:9) na

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba Msaada.” (1:5)

Katika aya hii, aina ya kauli imebadilika kutoka nafsi ya tatu kuwa kauli halisi kwa kutumika Kaf katika neno Iyyaka (Wewe).

Hii ni kwa sababu baada ya mja kumtukuzi na kumshukuru Allah تعالیٰ, anasimama mbele Yake na kumuambia Yeye moja kwa moja: Na kwa kuzingatia hilo, ndio Allah تعالیٰ Amesema;

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba Msaada”. (1:5)

***Al-Fatihah* Inaonesha Umuhimu wa Kumsifu Allah تعالى. Ni Lazima Isomwe Katika Kila Sala**

Mwanzo wa *Surat Al-Fatihah* inaonesha Allah تعالى Anavyojisifu kwa Sifa Zake nzuri na Anaonesha kwa waja Wake, nao pia wanamsifu kwa utaratibu huo. Hivyo Sala haikamiliki mpaka mmoja wetu asome *Al-Fatihah* kama anaweza. Sahihi mbili zimeandika kuwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا صَلَاةَ لِمَنْ لَمْ يَقْرَأْ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ»

“Hapana Sala kwa yule ambaye hatasoma Fatihatul-Kitab.”¹

Aidha imerikodiwa katika Sahih Muslim kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى : قَسَمْتُ الصَّلَاةَ بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي نَضْفَيْنِ، فَنَضْفُهَا لِي وَنَضْفُهَا لِعَبْدِي وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ، إِذَا قَالَ الْعَبْدُ: الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، قَالَ اللَّهُ: حَمِدَنِي عَبْدِي، وَإِذَا قَالَ: الرَّحْمَنُ الرَّحِيمِ، قَالَ اللَّهُ: أَثْنَى عَلَيَّ عَبْدِي فَإِذَا قَالَ سَلَامٌ يَوْمَ الدِّينِ، قَالَ اللَّهُ: مَجَّدَنِي عَبْدِي، وَإِذَا قَالَ: إِنَّا نَعْبُدُكَ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ، قَالَ: هَذَا بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي، وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ، فَإِذَا قَالَ: أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ، قَالَ: هَذَا لِعَبْدِي، وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ»

“Allah Amesema: “Nimeigawa Sala (A-Fatiha) katika nusu mbili kati Yangu na Mja Wangu, nusu ni Yangu na nusu ni ya Mja Wangu. Mja Wangu atapata alichoomba. Akisema,

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾

“Shukran zote Anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.”

Allah تعالى Anasema: “Mja Wangu Amenishukuru Mimi.” Mja anaposema:

¹ Fat’hul Al-Bari 2:276 na Muslim 1:295.

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

“Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu”.

Allah تعالى Anasema; “Mja Wangu Amenienzi.” Mja anaposema:

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٢﴾

“Mwenye kumiliki siku ya malipo”.

Allah تعالى Anasema; “Mja Wangu amenisifu.” Mja anaposema:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٣﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba msaada.”

Allah تعالى Anasema, “Hii ni kati Yangu na Mja Wangu na Mja Wangu atapata anachoomba.” Mja anaposema:

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٤﴾ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا

الضَّالِّينَ ﴿٥﴾

“Tuongoze njia iliyonyooka. Njia ya wale uliowaneemesha, sio (ya wale) waliokasirikiwa, wala (ya) wale waliopotea.”

Allah تعالى Atasema, “Hii ni ya Mja Wangu na Mja Wangu atapata alichoomba.”

Tawhid Uluhiyyah

Adh-Dhahhak alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

إِيَّاكَ نَعْبُدُ

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu”,

Ina maana: “Ni Wewe tu tunaye kupwekesha, tunayekuogopa na kukutegemea Wewe Pekee, Bwana wetu na hapana mwingine.”

Tawhid Ar-Rububiyah

وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuomba msaada.”

Kukutii katika kila jambo.¹ Zaidi ya hivyo, Qatadah alisema kuwa Aya:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu, na Wewe tu Ndiye tunaye kuomba msaada.” (1:5)

“Allah تعالى Anatuamrisha tumuabudu kwa uaminifu, na tumuombe Msaada kuhusiana na mambo yote.”² Allah تعالى Ametaja,

إِيَّاكَ نَعْبُدُ

“Wewe tu Ndiye tunayekuabudu.”

Kabla hajasema,

وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu Ndiye tunayekuomba msaada.”

Kwa sababu lengo hapa ni kuabudu, wakati Msaada wa Allah تعالى ni zana ya kutekeleza lengo hilo.

Kwa hakika mtu huzingatia kwanza lililo muhimu zaidi na kisha lenye umuhimu kidogo. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Allah تعالى Kumuita Mtume Wake ﷺ ‘Abd (Mja) Katika Minasaba Mitukufu

Allah تعالى Alimuita Mjumbe Wake *Abd (Mja)* Alipoelezea kumpelekea Kitabu Chake, na Mtume ﷺ kumshukuru, na wakati alipotaja *Isra* (Safari ya usiku mmoja kutoka Makkah kwenda *Baitul Muqaddas* na kisha mbinguni), na hii ni minasaba mitukufu sana kwa Mtume ﷺ. Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:19.

² Ibn Abi Hatim 1:19.

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيَّ عَبْدِهِ الْكِتَابَ

“Sifa Njema Zinamstahiki Mwenyezi Mungu Ambaye Amemteremshia Mja Wake (Nabii Muhammad) Kitabu (Kitukufu)...” (18:1)
na,

وَأَنْتَ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ

“...Na hakika mja wa Mwenyezi Mungu (Nabii Muhammad) aliposimama kumuomba (Mola Wake Mmoja tu)...” (72:19)

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا

“Utukufu ni Wake Yeye tu Ambaye Amempeleka Mja Wake (Muhammad) usiku (mmoja tu).” (17:1)

Basi Amemuita *Abd* (mtumwa, mja) wakati wa kumteremshia Kitabu, wakati wa kusimama kwa ajili ya kuhubiri wito Wake na katika safari yake ya *Israa*.

Mwongozo wa Kufanya Ibada Wakati wa Msongo wa Mawazo.

Allah تعالى pia Alimfundisha Mtume Wake ﷺ afanye ibada anapohisi dhiki na msongo wa mawazo kwa sababu ya kupingwa na washirikina walio muasi na kumkataa.

Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أُنُوكَ يَضِيقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ ﴿٧٧﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِنَ

السَّاجِدِينَ ﴿٧٨﴾ وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿٧٩﴾

“Na kwa yakini Sisi Tunajua ya kwamba kifua chako kinadhikika kwa yale wasemayo (na wafanyayo katika kuipinga Dini ya Uislamu). (Lakini stahmili) umtukuze Mola Wako pamoja na Kumsifu (kwa Sifa Zake njema), na uwe miongoni mwa (hao wanaosifiwa kuwa) wanamsujudia (Mwenyezi Mungu). Na umuabudu Mola Wako mpaka ikufikie hiyo yakini (Nayo ni mauti).” (15:97-99)

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١﴾

“Tuongoze njia iliyonyooka” (1:6)

Siri ya Kuanza Kumsifu Allah تعالی Kabla ya Maombi.

Kwa kuwa Sifa kwa Allah تعالی, Ambaye Huombwa Msaada zilitangulia kutajwa kwanza, hivyo basi ni sahihi kwa Sifa hizo zikafuatiwa na maombi. Kama Mwenyewe Alivyosema katika Hadithi Qudsi,

«فَنَضْفُهَا لِي وَنَضْفُهَا لِعَبْدِي، وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ»

“Nusu kwa ajili Yangu na nusu ni kwa ajili ya Mja Wangu na mja Wangu atapata alichokiomba.”

Hii ndiyo njia nzuri kabisa ya kuomba msaada, kwa kuanza kumsifu Yule anayeombwa msaada na kisha kuomba shida yake na shida za nduguze Waislam kwa kusema,

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١﴾

“Tuongoze njia iliyonyooka.”

Njia hii ni mwafaka zaidi na inafanya kazi kwa ufanisi kwa kutoa majibu chanya kwa maombi, na ndiyo sababu Allah تعالی Alifundisha njia hii nzuri na timilifu.

Kuomba Msaada inaweza ikachukua Surah inayoonesha hali ya mtu anayeomba Msaada. Kwa mfano, Mtume Musa عليه السلام alisema,

رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ﴿٢٨﴾

“...Mola Wangu! Bila shaka mimi ni mhitaji wa kheri Utakayo niteremshia.” (28:24)

Aidha unaweza ukataja sifa za huyo anayeombwa, kama alivyosema Dhun-Nun عليه السلام,

لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾

“Hakuna aabudiwaye isipokuwa Wewe, Mtakatifu, hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (Nafsi zao).” (21:87)

Zaidi ya hayo, Mtu anaweza kumsifu anayemuomba bila hata ya kumtaja shida yake. Kama mshairi mmoja asemavyo:-

Je nianze kutaja shida yangu au ukarimu wako

Unatosha kutatua shida yangu.

Hakika tabia yako yote ni ukarimu

Mtu atakapokusifu wewe siku moja tu.

Shida yake inatatuliwa kwa kutaja sifa Zako.

Maana ya Mwongozo Uliotajwa Katika Surah

Mwongozo uliotajwa katika Surah unaonesha kuelekezwa kwenye mafanikio, Allah تعالى Amesema,

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١﴾

“Tuongoze njia iliyonyooka.”

Ikiwa na maana tuongoze, tuelekeze na tupe mwongozo sahihi. Pia,

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾

“Na Tukambainishia njia zote mbili – (iliyo njema na iliyo mbaya).”
(90:10)

Ina maana: ‘Tulimuelezea njia nzuri na njia mbaya.’ Aidha Allah تعالى Amesema,

أَجْتَبَيْنَاهُ وَهَدَيْنَاهُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾

“Akamchagua na Kumuongoza katika njia iliyonyooka.” (16:121)

na,

فَأَهْدُوهُمْ إِلَى صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٣﴾

“Waongozeni njia ya Jahannamu.” (37:23)

Kwa maana: Ya Muongozo na ufahamisho.

Vile vile Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٢﴾

“Na kwa yakini wewe (Ewe Muhammad) unaongoza katika njia iliyonyooka.” (42:52)

Na kauli ya watu wa Peponi,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا

“Sifa zote Njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Ametuongoza katika (neema) hizi.” (7:43)

Ikiwa ina maana ya kutuongoza na kutuelekeza ili mwisho wetu uwe Peponi.

Maana ya *As-Sirat Al-Mustaqim*, Njia Iliyonyooka

Akielezea maana ya *As-Sirat Al-Mustaqim*, Imam Abu Jaafar At-Tabari رحمه الله تعالى alisema, “Ummah ulikubaliana kuwa *As-Sirat Al-Mustaqim* ni njia iliyo wazi isiyokwenda upogo (upande) kwa mujibu wa lugha ya Waarabu.

Kwa mfano, Jarir bin Atiyah Al-Khalafi alisema katika shairi lake, “Kiongozi wa waumini yuko juu ya njia ambayo itabaki imenyooka, japo njia nyingine zitaenda upogo.”¹

At-Tabari رحمه الله تعالى aliendelea kusema, “Waarabu wanatumia neno *Sirat* kuelezea matendo na kauli zote, ikiwa ni njema au mbaya kwa njia ya sitiari.

Hivyo Waarabu watamuelezea mtu muaminifu kama aliyenyooka na mtu muovu kama aliyepinda.

Njia iliyonyooka iliyotajwa ndani ya Qur’an ina maana ya Uislam:

Imam Ahmad ameandika katika *Musnad* wake kuwa An-Nawwas bin Sam’an رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 1:170.

«ضَرَبَ اللهُ مَثَلًا صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا، وَعَلَىٰ جَنَّتَيْهِ الصِّرَاطِ سُرْرَانِ فِيهِمَا أَبْوَابٌ مُّفْتَحَةٌ، وَعَلَىٰ الْأَبْوَابِ سُورٌ مُّرْخَاةٌ، وَعَلَىٰ بَابِ الصِّرَاطِ دَاعٍ يَقُولُ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ ادْخُلُوا الصِّرَاطَ جَمِيعًا وَلَا تَغْوُجُوا، وَدَاعٍ يَدْعُو مِنْ فَوْقِ الصِّرَاطِ، فَإِذَا أَرَادَ الْإِنْسَانُ أَنْ يَفْتَحَ شَيْئًا مِنْ تِلْكَ الْأَبْوَابِ قَالَ: وَيْحَكَ لَا تَفْتَحْهُ فَإِنَّكَ إِنْ فَتَحْتَهُ تَلَجُّهُ فَالصِّرَاطُ: الْإِسْلَامُ وَالسُّورَانِ: حُدُودُ اللهِ وَالْأَبْوَابُ الْمُفْتَحَةُ مَحَارِمُ اللهِ وَذَلِكَ الدَّاعِي عَلَىٰ رَأْسِ الصِّرَاطِ كِتَابُ اللهِ، وَالدَّاعِي مِنْ فَوْقِ الصِّرَاطِ وَاعِظُ اللهُ فِي قَلْبِ كُلِّ مُسْلِمٍ»

“Allah Amepiga mfano: Sirat (njia iliyonyooka) imezungukwa pande zote na kuta mbili, na kila ukuta una milango, iliyo wazi, iliyofunikwa na mapazia. Kuna mlinganiaji katika lango la Sirat akipiga mbiu, “Enyi watu kaeni kwenye njia na msipite pembeni; wakati huo huo mlinganiaji juu ya njia anamuonya mtu yeyote anayetaka kufungua hiyo milango, ‘Masikitiko kwenu! Msifungue kwani mkifungua mtapita ndani yake!’ Njia iliyonyooka ni Uislam, kuta mbili ni mipaka Aliyoiweka Allah, na milango inafanana na yale Aliyoyaharamisha Allah. Mlinganiaji katika lango la Sirat ni Kitabu cha Allah, ambapo mlinganiaji juu ya Sirat ni maonyo ya Allah yaliyo ndani ya kila nafsi ya Muislamu.”¹

Watiifu Huwa Wanaomba Uongofu na Wanashikamana na Mwongozo

Endapo mtu atauliza, “Kwa nini Muumini anamuomba Allah تعالی Amuongoze kila anaposali na nyakati nyingine, wakati ameshaongozwa? Je, bado hajapata mwongozo?”

Majibu ya maswali haya ni kuwa kama sio ukweli kwamba Muumini anatakiwa kuomba kuongozwa mchana na usiku, Allah تعالی Asingemuelekeza Amuombe Yeye ili apate mwongozo. Mja ni mwenye kumuhitaji Allah تعالی kila saa ya maisha yake ili Amsaidie kubaki kwenye njia ya mwongozo na kumfanya madhubuti na kudumu katika njia hiyo. Mja hana uwezo wa kujinufaisha au kujidhuru isipokuwa kwa idhini ya Allah تعالی. Kwa hiyo Allah تعالی Amemuelekeza mja kumuomba Yeye wakati wote, ili Ampe Msaada Wake na uimara na ufanisi.

¹ Ahmad 4:182.

Hali hii hutokea hasa pale mtu anapohitaji Msaada wa haraka kutoka kwa Allah تعالى, mchana au usiku. Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ءَالِكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَى رَسُولِهِ ءَالِكِتَابِ
الَّذِي نَزَّلَ مِن قَبْلُ

“Enyi mlioamini! Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Alichokiteremsha juu ya Mtume Wake, na Vitabu Alivyo-viteremsha zamani.” (4:136)

Hivyo, katika Aya hii Allah تعالى Amewaamrisha Waumini wawe na imani, wala si kwa ajili ya kupata imani nyingine, kwani kinachotakiwa hapa ni uimara na kuendelea kufanya matendo yatakayomsaidia kubaki katika njia iliyo sahihi.

Pia Allah تعالى Amewaamrisha waja Wake wanaoamini kuomba,

رَبَّنَا لَا تُرِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٨﴾

“(Hao wenye akili husema), “Mola wetu! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kutuongoza, na Utupe Rehema itokayo Kwako, hakika Wewe Ndiwe Mpaji Mkuu.” (3:8).

Hivyo basi maana ya Kauli Yake Allah تعالى,

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٨﴾

“Tuongoze njia iliyonyooka.” Maana yake: Tuthibitisha tuendeleo katika njia ya mwongozo na usituruhusu tupotee.

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٧﴾

“Njia ya wale uliowaneemesha, siyo (ya wale) waliokasirikiwa, wala (ya) wale waliopotea.” (1:7)

Tulitaja Hadithi ambayo kwayo mja akisema,

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٨﴾

“Niongoze njia iliyonyooka.” Na Allah تعالى husema, “Hii ni kwa ajili ya mja Wangu, na mja Wangu atapata atakachokiomba.” Kauli ya Allah تعالى,

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ

“Njia ya wale Uliowaneemesha.” Inabainisha Njia. Wale Aliowaneemesha ni waliotajwa katika Surat An-Nisa (Surah ya 4) Allah تعالى Aliposema,

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ
وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٦﴾ ذَلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللَّهِ وَكَفَى

بِاللَّهِ عَلِيمًا ﴿٦٧﴾

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu katika Manabii, wafuasi wa mwanzo kabisa wa mtume, na waliokufa Mashahidi na watu wema. Na uzuri ukoje (kwa mtu) watu hao kuwa rafiki (zake). Hiyo ni Fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa Kutosha, (hapana Asilolijua).” (4:69-70) Kauli ya Allah تعالى,

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٧٧﴾

“Siyo (ya wale) waliokasirikiwa, wala (ya) wale waliopotea.”

Ina maana tuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale Uliowaongoza, yaani watu wenye mwongozo, uaminifu na utiifu kwa Allah تعالى na Wajumbe Wake. Hawa ndio watu wanaoshikamana na Maamrisha ya Allah تعالى na wanajiepusha kutenda Aliyoyakataza. Lakini tusaidie ili tuepukane na njia ya wale waliokasirikiwa na Allah تعالى, ambao wana dhamira mbaya, ambao wanaujua ukweli lakini wanaukupuka. Aidha tusaidie tuepukane na njia ya wale waliopotezwa, waliopoteza maarifa ya kweli na kwa sababu hiyo, wana hangaika katika upotevu, wakishindwa kufuata njia sahihi. Allah تعالى Anatilia mkazo kuwa hizo njia mbili mbaya Alizozielezea hapa zinapotosha. Njia mbili hizo ni za Wakristo na Wayahudi, ukweli ni kwamba Waumini lazima wawe macho ili kuepukana nazo. Njia ya Waumini imefungamana na elimu ya kweli na kushikamana nayo. Tunapowalinganisha, ni kuwa Wayahudi waliitelekeza dini yao wakati Wakristo walipoteza elimu ya kweli. Hii ndio sababu hasira iliwashukia Mayahudi, upotofu uliwapata Wakristo. Wale wanaojua, lakini wakaacha kufuata ukweli, wanastahiki kukasirikiwa, tofauti na wale wasiojua. Wakristo wanataka kutafuta elimu ya kweli lakini hawaitafuti kwa njia sahihi,

hii ndiyo sababu iliyowafanya wapotee. Inafaa pia tutaje kuwa wote Wayahudi na Wakristo wamekasirikiwa na kupotea lakini hasira ni moja ya sifa mahsusi kwa Mayahudi. Allah تعالی Anatueleza kuhusu Mayahudi,

مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ وَعَضِبَ عَلَيْهِ

“Ni ambao Mwenyezi Mungu Amewalaani na Kuwakasirikia.” (5:60)

Sifa wanazostahili Wakristo ni ile ya upotofu, kama Allah تعالی Alivyoelezea,

قَدْ ضَلُّوا مِنْ قَبْلُ وَأَضَلُّوا كَثِيرًا وَضَلُّوا عَنْ سَوَاءِ السَّبِيلِ ﴿٦٧﴾

“Walikwishapotea toka zamani na wakawapoteza wengi, na (sasa) wanapotea njia iliyo sawa (hawataki kumfuata Nabii Muhammad).” (5:77)

Kuna Hadithi za Mtume na Kauli za Salaf Kuhusu Somo Hili.

Imam Ahmad ameandika kuwa ‘Adiy bin Hatim alisema, “Wapanda farasi wa Mtume ﷺ walimkamata shangazi yangu pamoja na watu wengine. Walipowa-fikisha kwa Mtume ﷺ walitakiwa kusimama msitarini mbele yake. Shangazi yangu akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Anayeniunga mkono mimi, yuko mbali. Watoto hawazaliwi, nami ni ajuza, siwezi kutoa huduma yoyote naomba unihurumie, na Allah تعالی Akuhurumie!” Akamuuliza, “Nani mtetezi wako?” Akajibu, “Adiy bin Hatim.” Akasema, “Yule aliyemkimbia Allah تعالی na Mjumbe Wake?” Akasema, “Hivyo Mtume ﷺ akaniachia huru.” Mtume ﷺ aliporejea, alikuwepo mtu pembezoni mwake, nadhani alikuwa Ali, ambaye alimuambia yule Mwanamke, “Muombe usafiri.” Alimuomba Mtume ﷺ, na akaamrisha apewe mnyama.” Kisha Adiy akasimulia, “Baadaye yule mwanamke alimuendea na kusema, “Yeye (Muhammad ﷺ) amenifanyia hisani ambayo baba yako (aliyekuwa mtu mkarimu) asingeweza kufanya. Mtu fulani alikuja na akamfanyia hisani, akaja mwingine naye akamfanyia hisani. “Nilienda kwa Mtume ﷺ ambapo nilikuta mwanamke na watoto wamejikusanya karibu sana naye, hivyo hakuwa Mtume ﷺ kama Kisra (Mfalme wa Persia) au Kaizari. Mtume ﷺ akasema, “Ewe Adiy! Kitu gani kilichokukimbiza, kalima *Lailaha illallah* isitangazwe? Je kuna ambaye anastahiki kuabudiwa isipokuwa Allah? Kitu gani kilichokufanya ukimbie, *Allahu Akbar* (Allah Mkubwa) isitangazwe?”

Hivi kuna mkubwa zaidi ya Allah?" Nikasilimu na nikauona uso wake unameremeta kwa furaha na akasema,

«إِنَّ الْمَغْضُوبَ عَلَيْهِمُ الْيَهُودَ وَإِنَّ الضَّالِّينَ النَّصَارَى»

*"Hakika waliokasirikiwa ni Mayahudi na waliopotea ni Wakristo."*¹

Hadithi hii ilikusanywa pia na at-Tirmidhi ambayo iko katika daraja la *"Hassan Gharib"*. Aidha Zayd bin Amr bin Nufayl na baadhi ya rafiki zake – kabla ya Uislamu – walikwenda As-Sham kutafuta dini ya kweli, Mayahudi walimuambia, "Hutaweza kuwa miongoni mwa Mayahudi mpaka utakapokuwa na hisa ya hasira za Allah تعالی ambazo tumezipata." Akasema, "Mimi natafuta kuepuka hasira za Allah تعالی." Aidha Wakristo wakamuambia, "Hutaweza kuwa miongoni mwetu mpaka uwe na hisa ya kukasirikiwa na Allah تعالی." Akasema, "Siwezi kubeba mzigo huo." Hivyo akabaki katika hali yake safi akijiepusha kuabudu masanamu na kujiepusha na kutenda mambo ya kikafiri. Hakuwa Yahudi wala Mkristo. Ama marafiki zake walikuwa Wakristo kwani waliuona ni sahihi zaidi ya Uyahudi. Waraqah bin Nawfal alikuwa miongoni mwa watu hao mpaka alipoongozwa na Allah تعالی kupitia kwa Mtume Wake ﷺ, pindi Alipompa Utume, na Waraqah aliamini Wahyi alioteremshiwa Mtume ﷺ.

Muhtasari wa Al-Fatihah

Surah tukufu ya *Al-Fatihah* ina Ayah saba ikiwa ni pamoja na Shukrani na Sifa kwa Allah تعالی, Kumtukuzwa Yeye na Kumshukuru Yeye kwa kuyataja Majina Yake Mazuri na Sifa Zake. Pia inataja Akhera, ambayo ni Siku ya kufufuliwa, na inawaelekeza waja wa Allah تعالی kumuomba Yeye na kunadi Nguvu zote na Uweza wote unatoka Kwake. Pia inawataka wamuabudu Allah تعالی Pekee kwa unyenyekevu, Uungu Wake ni wa Pekee na Ukamilifu Wake, Asiyehitajia mshirika, hana wapinzani au wanaolingana Naye. *Al-Fatihah* inawaelekeza Waumini kumuomba Allah تعالی Awaongoze njia iliyonyooka, ambayo ni Dini ya kweli, na Awasaidie wabaki katika njia hiyo na wapite juu ya *Sirat* (daraja lililo juu ya moto wa Jahannam ambapo kila mtu atapita) katika siku ya *Hukumu*. Siku hiyo, Waumini watapita katika njia hiyo kuelekea kwenye bustani zenye raha, wakiwa jirani pamoja na Mitume, Wasemao kweli, Mashahidi na Wachamungu. *Al-Fatihah* pia inashajiisha watu kutenda mema, ili wapate

¹ Ahmad 4:378 na Tuhfatu Al-Ahwadhi 8:289.

kuingia peponi – siku ya kiama. Surah hii pia inaonya dhidi ya kufuata njia zilizopotoka, ili hatima yake isiwe kukusanywa pamoja na waliozama katika dhambi, katika siku ya kufufuliwa, nao ni wale waliokasirikiwa na waliopotea (Mayahudi na Wakristo).

Uneemeshaji Unatokana na Allah تعالى na Upotofu ni Matokeo ya Mtendaji.

Allah تعالى Alipotaja suala la Kuneemeshaji Aliliegemeza Kwake Yeye. Katika Kauli Yake;

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ

“Njia ya wale Uliowaneemeshaji.” Alipotaja Fadhila Zake. Alipotaja Hasira Zake, Allah تعالى Amesema,

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ

“Siyo ya wale walioghadhikiwa.” Hapa hakujitaja, japokuwa kiuhakika Yeye Ndiye Aliyewakasirikia. Ni kama Allah تعالى Alivyotaja katika Ayah nyingine,

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ تَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“Huwaoni wale waliofanya urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu Amewakasirikia?” (58:14)

Aidha Allah تعالى Anawazungumzia wale waliojiingiza kwenye upotevu, japokuwa walipotoshwa kwa mujibu wa Kadari na Utashi wa Allah تعالى kama Allah تعالى Anavyosema;

﴿ مَنِ يَهْدِ اللَّهُ فَبُهِتَ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۗ وَمَنْ يُضِلِلْ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرْشِدًا ۗ

“Ambaye Mwenyezi Mungu Anamuongoza basi yeye ndiye aliyeongoka; na Anayemuachia kupotea, basi Hatampatia Mlinzi mwongozi.” (18:17) Na Amesema tena;

﴿ مَنْ يُضِلِلْ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ ۗ وَيَذُرُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ۗ

“Ambao Mwenyezi Mungu Anawaachia kupotea (kwa kuwa hawatatusikiliza), basi hawana mwongozi. Na (Mwenyezi Mungu) Anawaacha katika upotofu (upotovu) wao wakitangatanga ovyo.” (7:186)

Aya hizi na nyingine zinashuhudia ukweli kwamba Allah تعالى Peke Yake Ndiye

Aongozaye na Apotoshaye, kinyume na imani ya madhehebu ya *Qadiriyyah*, ambao wanadai kuwa mja ndiye anayechagua na kuamua mwisho wake. Wanategemea Aya ambazo zina utata katika kuzifahamu, na wanaziacha ambazo maelezo yake yapo wazi kabisa. Na ambazo ni dhidi ya utashi wao. Njia yao ni ile ya watu wanaofuata uovu na upotofu. Imenukuliwa katika Hadithi Sahihi,

«إِذَا رَأَيْتُمُ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ سَمَى اللَّهُ فَاخَذُوا مِنْهُمْ»

“Ukiwaona watu wanafuata mambo ambayo siyo wazi (Qur’an) hao watakuwa ni wale waliotajwa na Allah (Katika 3:7). Hivyo waepuke.”¹

Mtume ﷺ alikuwa anarejea Kauli ya Allah تعالى،

فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ^٢

“Wale ambao nyoyoni mwao mna upotofu wanafuata zile zinazobabaisha kwa kutaka kuwaharibu watu na kutaka kujua hakika yake vipi.” (3:7)

Kwa hakika hakuna mzushi katika Dini atakayetegemea ushahidi wa kweli ndani ya Qur’an unaothibitisha bidaa zao. Qur’an imekuja kubainisha ukweli na uongo, na mwongozo na upotofu. Qur’an haina tofauti wala Aya zake hazikinzi, kwa sababu ni Wahyi kutoka kwa Mwenye Hekima Anayestahiki Shukrani zote.

Kuitikia Amin Baada ya Kusoma Surat Al-Fatihah

Imehimizwa kusemwa Amin baada ya kumaliza kusoma *Al-Fatihah*. Amin maana yake, “Ewe Allah تعالى yakubali maombi yetu”. Ushahidi kuwa *Amin* imehimizwa upo katika Hadithi zilizoandikwa na Maimamu; Ahmad, Abu Dawud na At-Tirmidhi kuwa Wail bin Hujr رضي الله عنه alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisoma,

غَيْرَ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٢٠﴾

“Sio wale Uliowaghadhabikia wala Uliowapoteza”, na akasema “Amin” akituta sauti yake.²

¹ Fat’hul Al-Bari 8:57.

² Ahmad 4:315, Abu Dawud 1:574, *Tuh’fatul Al-Ahwadhi* 2:65.

Masimulizi ya Abu Dawud yaliongeza, "Alikuwa akipandisha sauti wakati wa kusema *Amin*." At-Tirmidhi alielezea Hadithi hii kuwa ni Hasan na pia ilisimuliwa na Ali na Ibn Masu'd رضي الله عنهما¹. Aidha Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa kila Mtume ﷺ aliposoma,

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٧﴾

"Sio wale waliokasirikiwa wala waliopotea", alisema "Amin" mpaka alisikika na wale waliokuwa safu ya kwanza.²

Abu Dawud na Ibn Majah waliandika Hadithi hii na nyongeza, "Kisha Msikiti ulitikisika kwa *Amin*³ ya maamuma na ya Mtume ﷺ." Pia Ad-Daraqutn aliandika Hadithi hii na kuipa daraja la Hasan. Zaidi ya hayo Bilal رضي الله عنه alisimulia kuwa alimuambia, "Ewe Mtume ﷺ usimalize kusema "*Amin*" kabla sijaunga nawe.⁴ Imependekezwa kwa wale watakaokuwa nje ya Sala (wakati wanasoma *Al-Fatihah*) na imehimizwa kwa wale wanaosali mmoja mmoja au jamaa. Sahihi mbili zimeandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا أَمَّنَ الْإِمَامُ فَأَمَّنُوا، فَإِنَّهُ مَنْ وَاَفَّقَ تَأْمِينُهُ تَأْمِينَ الْمَلَائِكَةِ غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

*"Imam atakaposema Amin, na nyie semeni Amin, kwa sababu yeyote anayesema Amin na ikaafikiana na ile ya Malaika, atasamehewa madhambi yake yaliyopita."*⁵

Muslim aliandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا قَالَ أَحَدُكُمْ فِي الصَّلَاةِ: آمِينَ، وَالْمَلَائِكَةُ فِي السَّمَاءِ: آمِينَ، فَوَاقَقَتْ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

*"Mmoja wenu anaposema katika Sala, "Amin", na Malaika mbinguni nao wakasema "Amin", mojawapo ikawafikiana na nyingine. Basi atasamehewa madhambi yake yaliyopita."*⁶

¹ Tuhfat ul Al-Ahwadh 2:67.

² Abu Dawud 1:575.

³ Abu Dawud 1:575 na Ibn Majah 1:279.

⁴ Ad-Daraqutn 1:335.

⁵ Fat'hul Al-Bari 11:203 na Muslim 1:307.

⁶ Muslim 1:307.

Hadithi inazungumzia wote Malaika na Waislam kusema *Amin* kwa pamoja. Aidha Hadithi inahusu "*Amin*" inaposemwa na Malaika na Waislam kwa unyenyekevu (hivyo kuleta msamaha). Aidha imeandikwa katika Sahihi Muslim kuwa Abu Musa رضي الله عنه alipokea kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema,

«إِذَا قَالَ - يَعْنِي الْإِمَامَ - : وَلَا الضَّالِّينَ، فَقُولُوا: آمِينَ، يُجِيبُكُمْ اللَّهُ»

*"Imam anaposema, "Waladh-dhwaal-liin", semeni "Amin" na Allah Atakupendeni."*¹

Zaidi ya hivyo, At-Tirmidhi alisema kuwa, "*Amin*" Maana yake, "Usituvunje moyo." Japo wanazuoni wengi wamesema kuwa ina maana ya, "Tukubalie maombi yetu." Aidha katika *Musnad*, Imam Ahmad ameandika kuwa Aisha رضي الله عنها alisema kuwa wakati Mayahudi walipotajwa kwake, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّهُمْ لَنْ يَخْسُدُونَا عَلَى شَيْءٍ كَمَا يَخْسُدُونَا عَلَى الْجُمُعَةِ الَّتِي هَدَانَا اللَّهُ لَهَا وَضَلُّوا عَنْهَا، وَعَلَى الْقِبْلَةِ الَّتِي هَدَانَا اللَّهُ لَهَا وَضَلُّوا عَنْهَا وَعَلَى قَوْلِنَا خَلْفَ الْإِمَامِ: آمِينَ»

*"Hawatatuonea husda kwa kitu zaidi ya wanavyotuhusudu kwa kupewa Ijuma ambayo tumeongozwa nayo, (wakati wao walipotea) na wakapotea kutokana nayo. Na kwa Qibla tulichoongozwa nacho, na walipotoshwa kutokana nacho na kwa ajili ya kusema "Amin" nyuma ya Imam."*²

Aidha Ibn Majah aliandika Hadithi hii kwa maneno yafuatayo,

«مَا حَدَّثْتُكُمْ الْيَهُودُ عَلَى شَيْءٍ مَا حَدَّثْتُكُمْ عَلَى السَّلَامِ وَالْتَأَمِينَ»

*"Mayahudi hawajakuoneeni husda zaidi ya salamu (maamkizi ya Kiislam) na kusema "Amin."*³

* * *

¹ Muslim 1:303.

² Ahmad 6:134.

³ Ibn Majah 2:278.

Tafsiri ya Surat Al-Baqarah

Sura ya 2

Iliteremshwa Madinah

سُورَةُ الْبَقَرَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْم ﴿١﴾ ذَلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ

﴿٢﴾ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا

رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣﴾ وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا

أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُولَئِكَ عَلَى

هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾

Fadhila za Surat Al-Baqarah.

Katika Musnad wa Imamu Ahmad, Sahih Muslim, Tirmidhi, na An-Nasa'i, imeandikwa kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قُبُورًا فَإِنَّ الْبَيْتَ الَّذِي تَقْرَأُ فِيهِ سُورَةَ الْبَقَرَةِ لَا يَدْخُلُهُ الشَّيْطَانُ»

“Msigeuze nyumba zenu

makaburi. Kwani shetani haingii nyumba ambamo Surat Al-Baqara inasomwa.” At-Tirmidhi amesema Hadithi hii ni “*Hasan Sahih*.”¹

Aidha Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema, “Shetani hukimbia kutoka katika nyumba inayosikika Surat Al-Baqarah.” Hadithi hii ilikusanywa na An-Nasa'i katika *Al-Yawm Wal-Laylah*,² na Al-Hakim ameandika katika *Mustadrak*, na kisha akasema *Silsila* yake ya upokezi ni sahihi japokuwa Sahihi mbili hazikuikusanya.³ Katika Musnad yake, Ad-Darimi aliandika kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Shetani anaihama nyumba ambamo inasomwa Surat Al-Baqarah, na anapondoka hujamba.” Ad-Darimi pia aliandika kuwa Ash-Shabi alisema kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Yeyote atakayesoma Aya kumi katika Surat Al-Baqarah usiku, shetani hataingia nyumbani kwake

¹ Ahmad 2:284, Muslim 1:539, *Tuhfatul Al-Ahwadhi* 8:180, An-Nasai (*Al-Kubra* 5:13).

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:240.

³ Al-Hakim 2:260.

usiku huo. (Aya hizo kumi), nne za mwanzo, Aya Al-Kursi (255), na Aya mbili baada yake (256 – 257) na Ayat tatu za mwisho.” Katika masimulizi mengine, Ibn Mas’ud رضى الله عنه amesema, “Shetani hatomkaribia yeye na familia yake, wala hatoguswa na kitu chochote asichokipenda.” Pia Aya hizi akisomewa mwendawazimu, atazinduka.”¹

Zaidi ya hivyo, Sahli bin Sa’d رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِكُلِّ شَيْءٍ سَنَامًا، وَإِنَّ سَنَامَ الْقُرْآنِ الْبَقْرَةُ، وَإِنَّ مَنْ قَرَأَهَا فِي بَيْتِهِ لَبَلَّةٌ لَمْ يَدْخُلْهُ الشَّيْطَانُ ثَلَاثَ لَيَالٍ، وَمَنْ قَرَأَهَا فِي بَيْتِهِ نَهَارًا لَمْ يَدْخُلْهُ الشَّيْطَانُ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ»

“Kila kitu kina nundu (au sehemu iliyoinuka juu inayomuezesha mtu kuangalia vilivyoko chini, yaani kilingo) na Al-Baqarah ndio nundu ya Qur’an. Yeyote anayesoma Al-Baqara usiku nyumbani kwake, Shetani hatoingia ndani ya nyumba hiyo, kwa siku tatu. Yeyote atakayesoma mchana ndani ya nyumba yake, shetani hatoingia ndani ya nyumba hiyo kwa siku tatu.”

Hadithi hii ilikusanywa na Abu Al-Qasim At-Tabarani, Abu Hatim ibn Hibban katika Sahih yake na Ibn Marduwyah.²

At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah wameandika kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema, Mtume ﷺ alipeleka kikosi chenye watu wengi, na alimuuliza kila mmoja kiasi cha Qur’ani alichohifadhi. Mtume ﷺ alimfikia kijana mdogo kuliko wote na akamuuliza, “Umehifadhi kiasi gani cha Qur’an, ewe fulani?” Akajibu, “Nimehifadhi Surah kadha na kadha na pia Al-Baqarah.” Mtume ﷺ akamuuliza, “Umehifadhi Surat Al-Baqarah?” Akajibu, “Ndiyo.” Mtume ﷺ akasema, “Basi wewe ndio kamanda wao.” Mmoja wa watu maarufu (au chifu) alisema, “Wallahi! Sikujifunza Surat Al-Baqarah kwa kuchelea kutotekeleza mafundisho yake.” Mtume ﷺ akasema,

«تَعَلَّمُوا الْقُرْآنَ وَاقْرَءُوهُ، فَإِنَّ مَثَلَ الْقُرْآنِ لِمَنْ تَعَلَّمَهُ فَقَرَأَ وَقَامَ بِهِ كَمَثَلِ جِرَابٍ مَحْسُورٍ مَسْكًا يَفُوحٌ رِيحُهُ فِي كُلِّ مَكَانٍ، وَمَثَلُ مَنْ تَعَلَّمَهُ فَيَرْتَدُّ وَهُوَ فِي جَوْفِهِ كَمَثَلِ جِرَابٍ أَوْكِيٍّ عَلَى مِسْكِ»

¹ Ad-Darimi 2:322.

² At-Tabarani 6:163 na Ibn Hibban 2:78.

“Jifunzeni Al-Qur’an na muisome, kwani mfano wa Mtu ajifunzaye Qur’an, akaisoma na akaitekeleza, ni mfano wa chupa iliyojaa miski na harufu yake imeenea kila mahali. Mfano wa mtu anayejifunza Qur’an na akawa mvivu kuisoma wakati Qur’an imo katika kifua chake, ni mfano wa chupa yenye miski lakini imezibwa.”

Haya ni maneno yaliyokusanywa na At-Tirmidhi, ambaye amesema Hadith hii ni *Hasan*. Katika usimulizi mwengine, At-Tirmidhiy ameandika Hadith hii ipo katika daraja la *Mursal*. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.¹

Aidha Bukhari ameandika kuwa Usayd bin Hudhayr رضي الله عنه alisema kuwa kuna wakati fulani usiku alipokuwa anasoma *Surat Al-Baqarah* na farasi wake alikuwa amefungwa pembezoni mwake. Farasi alianza kutapatapa. Usayd رضي الله عنه aliposita kusoma Qur’an, naye Farasi akatulia. Aliporudia kusoma, Farasi alianza kutapatapa. Alipoacha kusoma, Farasi akatulia na aliporejea kusoma, Farasi alianza kuzungukazunguka tena. Wakati huo mwanae, Yahya alikuwa karibu na Farasi, na akaogopa huenda Farasi angemkanyaga. Alipomrudisha mtoto wake nyuma, aliangalia mbinguni na akaona mawingu yanatoa mwanga mithili ya taa. Kulipopambazuka alikwenda kwa Mtume na akamueleza yaliyojiri. Mtume ﷺ akasema: “Sema ewe Ibn Hudhair!” Akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Mwanangu Yahya alikuwa karibu na Farasi na nilichelea angeweza kumkanyaga. Nilipokuwa namhudumia niliangalia mbinguni, niliona wingu lina mwanga mithili ya taa. Hivyo nikaenda lakini sikuona kitu.” Mtume ﷺ akamuuliza, “Unajua kilikuwa kitu gani?” Akajibu, “Hapana”. Mtume ﷺ akamuambia,

«تِلْكَ الْمَلَائِكَةُ ذَنَّتْ لِعَصْوَتِكَ وَلَوْ قَرَأْتَ لِأَضْبَحْتَ يَنْظُرُ النَّاسُ إِلَيْهَا، لَا تَتَوَارَى مِنْهُمْ»

“Hao walikuwa Malaika, walikuja karibu kusikiliza sauti yako (ukisoma Surat Al-Baqarah), na kama ungeendelea kusoma mpaka asubuhi, watu wangewaona Malaika na kusingalikuwa na kizuizi cha kuwaonea.”²

Haya ni masimulizi yaliyoandikwa na Imam Abu Ubayd Al-Qasim bin Salam katika kitabu chake *Fadha’il Al-Qur’an*.

¹ *Tuhfatul Al-Ahwadhi* 8:186, An-Nasai katika *Al-Kubra* 5:227 na Ibn Majah 1:78.

² *Fat’hul Al-Bari* 8:680.

Fadhila za Surat Al-Baqarah na Surat Al-Imran

Imam Ahmad alisema kuwa Abu Nu'aym aliwasimulia kuwa, Bishri bin Al-Muhajir alisema kuwa 'Abdullah bin Buraydah alimsimulia aliyoyasikia kwa baba yake, "Nilikuwa nimekaa na Mtume ﷺ na nilimsikia akisema,

«تَعَلَّمُوا سُورَةَ الْبَقَرَةِ فَإِنْ أَخَذَهَا بَرَكَتُهُ، وَتَرَكَهَا حَسْرَةً، وَلَا تَسْتَطِيعُهَا الْبَطَلَةُ»

"Jifunzeni Surat Al-Baqarah kwa sababu ukiisoma utapata Baraka na ukiiipuuza utapata hasara, na ni kinga dhidi ya uchawi na wachawi."

Mtume ﷺ alinyamaza kidogo kisha akasema,

«تَعَلَّمُوا سُورَةَ الْبَقَرَةِ وَآلَ عِمْرَانَ فَإِنَّهُمَا الزَّهْرَاوَانِ، يُظَلَّلَانِ صَاحِبَهُمَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَأَنَّهُمَا غَمَامَتَانِ أَوْ غَيَابَتَانِ أَوْ فِرْقَانِ مِنْ طَيْرٍ صَوَافٍ، وَإِنَّ الْقُرْآنَ يَلْقَى صَاحِبَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حِينَ يَنْشَقُّ عَنْهُ قَبْرُهُ كَالرَّجُلِ الشَّاجِبِ فَيَقُولُ لَهُ: هَلْ تَعْرِفُنِي؟ فَيَقُولُ: مَا أَعْرِفُكَ. فَيَقُولُ: أَنَا صَاحِبُكَ الْقُرْآنَ الَّذِي أَظْمَأْتِكَ فِي الْهَوَاجِرِ وَأَسْهَرْتَ لَيْلَكَ وَإِنَّ كُلَّ نَاجِرٍ مِنْ وَرَاءِ بِنَارَتِهِ، وَإِنَّكَ الْيَوْمَ مِنْ وَرَاءِ كُلِّ بِنَارَةٍ فَيُعْطَى الْمَلِكُ يَمِينَهُ وَالْخُلْدَ بِشِمَالِهِ وَيُوضَعُ عَلَى رَأْسِهِ تَاجُ الْوَقَارِ، وَيُكْسَى وَالِدَاهُ حُلَّتَانِ لَا يَتَّوَمُّ لَهُمَا أَهْلُ الدُّنْيَا، فَيَقُولَانِ: بِمَا كُسِينَا هَذَا؟ فَيَقَالُ: بِأَخْذِ وَلَدِكُمَا الْقُرْآنَ ثُمَّ يُقَالُ: اقْرَأْ وَاصْعَدْ فِي دَرَجِ الْجَنَّةِ وَعُرِّبْهَا، فَهُوَ فِي ضَعُودٍ مَا دَامَ يَقْرَأُ هَذَا كَانَ أَوْ تَرْتِيلًا»

"Jifunzeni Surat Al-Baqara na Al-Imran kwa sababu hizo ni taa mbili na zitawapa watu kivuli siku ya Kiama, kama mawingu mawili, anga mbili za kivuli au safu za makundi mawili ya ndege wanaoruka. Qur'an itakutana na sahiba yake akiwa kama vile mtu aliyekwajuka siku ya kufufuliwa, kaburi lake litakapofunuliwa Qur'an itamuuliza, "Je, unanijua?" Binadamu atajibu, "Sikufahamu." Qur'an itasema, "Mimi ni sahiba yako, Qur'an, iliyokusababishia kiu wakati wa joto na iliyokufanya ukeshe. Kila mfanya biashara ana aina ya bidhaa anazouza. Lakini, siku ya leo biashara yako inatawalia aina zote za biashara!" Atapewa Ufalme katika mkono wake wa kulia, maisha ya milele katika mkono wa kushoto na taji la rehema litawekwa juu ya kichwa chake. Wazazi wake watapewa nguo mbili za mapambo ambazo watu wa hapa duniani hawamudu kuzinunua. Watauliza,

“Kwa nini tumepewa mapambo haya?” Watajibiwa, “Kwa sababu mtoto wenu alikuwa anabeba Qur’an!” Msomaji wa Qur’an ataambiwa, “Soma na panda katika daraja za Pepo!” Atapanda juu kama anavyosoma Qur’an ima kwa haraka ama polepole.”¹

Ibn Majah ameandika sehemu ya Hadithi hii kutoka kwa Bishri bin Al-Muhajir² na *Silsila* ya wasimulizi wake ina daraja la *Hasan*, kwa mujibu wa vigezo vya Imam Muslim. Sehemu ya *Hadith* hii pia inaungwa mkono na *Hadith* nyingine. Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Umamah Al-Bahili رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«افْرَأُوا الْقُرْآنَ فَإِنَّهُ شَافِعٌ لِأَهْلِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ اقْرَأُوا الزَّهْرَاوَيْنِ، الْبَقْرَةَ وَآلَ عِمْرَانَ، فَإِنَّهُمَا يَأْتِيَانِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَأَنْهُمَا عَمَامَتَانِ، أَوْ كَأَنْهُمَا غَيَابَتَانِ أَوْ كَأَنْهُمَا فِرْقَانِ مِنْ طَيْرٍ صَوَافٍ، يُحَاجَّانِ عَنْ أَهْلِهِمَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ».

“Someni Qur’an, kwa sababu itawashufaia watu waisomayo siku ya Kiama, someni taa mbili, Al-Baqarah na Al-Imran, kwa sababu zitakuja katika maumbile ya mawingu mawili au safu za makundi mawili ya ndege siku ya Kiama na zitaomba kwa niaba ya watu wake siku hiyo.”

Mtume ﷺ kisha akasema,

«افْرَأُوا الْبَقْرَةَ فَإِنَّ أَخَذَهَا بَرَكَتٌ وَتَرَكَهَا حَسْرَةٌ وَلَا تَسْتَطِيعُهَا الْبَطَلَةُ»

“Isomeni Al-Baqarah kwa kuwa ukiwa nayo utapata Baraka, na ukiipuuza utapata hasara, na ni kinga dhidi ya uchawi na wachawi.”³

Aidha, Imam Muslim alihadithia *Hadith* hii katika Kitabu cha Sala.⁴ Imam Ahmad amesimulia kuwa An-Nawwas bin Sam’an رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُرْتَى بِالْقُرْآنِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَأَهْلِيهِ الَّذِينَ كَانُوا يَعْمَلُونَ بِهِ تَقْدِمُهُمْ سُورَةُ الْبَقْرَةَ وَآلَ عِمْرَانَ»

“Siku ya Kiama, Qur’an na watu waliokuwa wakitekeleza mafunzo

¹ Ahmad 5:352.

² Ibn Majah 2:1242.

³ Ahmad 5:249.

⁴ Muslim 1:553.

yake, wataletwa mbele, wakitanguliwa na Surat Al-Baqarah na Al-Imran.”

An-Nawaas رضى الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alitoa mifano mitatu kwa Surah mbili hizi na sikusahau mifano hiyo toka wakati huo.” Mtume ﷺ alisema,

«كَأَنَّهُمَا عَمَامَتَانِ، أَوْ ظُلَّتَانِ سَوْدَاوَانِ بَيْنَهُمَا شَرْقٌ، أَوْ كَأَنَّهُمَا فِرْقَانِ مِنْ طَيْرٍ صَوَافٍ، يُحَاجَّانِ عَنِ صَاحِبَيْهِمَا»

“Watakuja kama mawingu mawili, vivuli vyeusi viwili baina yao kuna nuru, au njia mbili za ndege wakiwatetea watu wao.”¹

Pia iliandikwa katika Sahih Muslim² na At-Tirmidhi alisimulia *Hadith* hii, ambayo iko katika daraja la *Hasan Ghaarib*.³

Surat Al-Baqarah iliteremshwa Al-Madina.

Hakuna ubishi juu ya hoja kuwa Surat *Al-Baqarah* iliteremshwa yote Al-Madinah.

Al-Baqarah ilikuwa moja ya Surah za mwanzo kuteremshwa Al-Madina, isipokuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَأَتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ط

“Na iogopeni siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu...”
(2:281)

Ilikuwa Aya ya mwisho ya Qur’an kuteremshwa. Pia Aya zinazohusu riba zilikuwa miongoni mwa *Ayat* za mwisho kushuka. Khalid bin Ma’dan alikuwa anaiita *Al-Baqarah*, “Hema la Qur’an”. Baadhi ya wanazuoni wanasema ina habari za matukio elfu, amri elfu na makatazo elfu. Wale wanaohesabu wanasema *Al-Baqarah* ina Aya mia mbili na themanini na saba, na maneno elfu sita mia mbili na ishirini na moja na herufi zake ni elfu ishirini na tano na mia tano. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Ibn Jurayj amesimulia kutoka wa ‘Ata’ kuwa alisema kuwa Ibn Abbas رضى الله عنهما alisema “Surat *Al-Baqarah* limeremshwa Madina.” Khusaif amesema kuwa Abdullah bin Zubeir رضى الله عنه amesema: ‘Suratul *Al-Baqarah* imeshuka Madina.’ Maimamu kadhaa, wanazuoni na

¹ Ahmad 4:183.

² Muslim 1:554.

³ Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:191.

wafasiri walitoa kauli sawa na hiyo; na hakuna tofauti ya maoni kuhusu suala hili kama tulivyosema mwanzoni.

Sahihi mbili zimeandika kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنهما alisimama Ka'bah ikiwa upande wake wa kushoto na Mina upande wake wa kulia na akatupa vijiwe saba katika Jamrah na akasema, "Yule aliyeteremshiwa Surat *Al-Baqarah*, Mtume ﷺ, alifanya Ramyi (kitendo cha kutupa mawe wakati wa *Hajj*).” Sahihi mbili zimeandika Hadith hii.¹

Zaidi ya hivyo, Ibn Marduwaih aliandika *Hadith* ya Shu'bah kutoka kwa Aqil bin Talhah kutoka kwa Utbah bin Marthad kuwa, "Mtume ﷺ hakuwaona Masahaba wake kuchelewa katika safu za mwanzo na akasema,

«يَا أَصْحَابَ سُورَةِ الْبَقَرَةِ»

"Enyi watu wa Surat *Al-Baqarah*!" Nadhani tukio hili lilijiri wakati wa vita vya Hunayn wakati Masahaba waliporejea nyuma. Kisha Mtume ﷺ alimuamrisha Al-Abbas (Ammi yake) رضي الله عنه awaite. Akawaita:

«يَا أَصْحَابَ الشَّجَرَةِ»

"Enyi watu wa mti!" Ikiwa na maana Masahaba walioshiriki katika *Baiah* ya *Ar-Ridhwan* (chini ya mti). Katika masimulizi mengine, Al-Abbas رضي الله عنه alipiga kelele, "Enyi Watu wa Surat *Al-Baqarah*!" Alikuwa akiwatia ari ili warejee hivyo wakarejea kutoka kila upande. Aidha wakati wa vita vya Al-Yamamah, dhidi ya jeshi la Musaylimah mwongo, kwanza Masahaba walirejea nyuma kwa sababu jeshi la Musaylimah lilikuwa na askari wengi. Muhajirina na Ansar waliitana kwa usemi; "Enyi watu wa Surat *Al-Baqarah*." Allah تعالى Aliwawezesha kulishinda jeshi la adui, Allah تعالى Awawie radhi Masahaba wote na Wajumbe wote wa Allah تعالى.²

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu".

الم

1. Alif Lam Mim.

¹ Ad-Durr Al-Manthur 1:47.

² Al-Majma 6:180.

Herufi *Muqata'at* (Herufi Moja Moja):

Herufi *Muqata'at* katika mwanzo wa Surah ni miongoni mwa mambo ambayo hakuna ajuaye isipokuwa Allah تعالی Mwenyewe. Hili lilielezwa kutoka kwa Abubakar, 'Umar, 'Uthman, 'Ali na Ibn Mas'ud رضي الله عنهم. Imeelezwa kuwa herufi hizi ni majina ya baadhi ya Surah. Pia imelezwa kuwa ni mwanzo ambao Allah تعالی Amekhitari Surah za Qur'an zianze na herufi hizo. Khusait alidhukuru kuwa Mujahid alisema, "Mwanzo wa Surah kama *Qaf, Sad, Ta, Sin, Mim na Alif Lam Ra*, na herufi zingine ni herufi za kutajiisha zilizowekwa (Abjadi)." Baadhi ya wana Isimu ya lugha ya Kiarabu wamesema kuwa hizo ni herufi za Abjadi na kuwa Allah تعالی Alizozitaja mwanzoni zimewakilisha herufi zote ishirini na nane. Mathalan, walisema mtu anaweza akasema, "Mtoto wangu anasoma *Alif, Ba, Ta, Tha...*" Anakusudia Abjadi zote ishirini na nane japo amesita kabla ya kuzitaja zote. Rai hii ilitajwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.¹

Herufi za Mwanzoni Mwa Surah.

Endapo tutaondoa herufi zinazojirudia, hivyo Idadi ya herufi zilizotajwa mwanzoni mwa Sura ni kumi na nne: *Alif, Lam, Mim, Sad, Ra, Kaf, Ha, Ya, Ayn, Ta, Sin, Ha, Qaf, Nun*. Hizi zilizotajwa ni nusu ya herufi zote ishirini na nane. Na zilizotajwa ni bora zaidi kuliko zilizoachwa. Hivyo Utakatifu ni Wake Aliyefanya kila kitu kwa umahiri unaoonesha Hekima Yake. Pamoja na hayo, wanazuoni wamesema, "Hakuna shaka kuwa Allah تعالی Hakudhihirisha herufi hizi kama mchezo au utani. Ikiwa kwa ujinga, mtu atasema kuwa baadhi ya Qur'an haina maana yoyote, (akiwa na maana herufi kama hizi), atakuwa amefanya kosa kubwa sana." Kinyume na hayo, herufi hizi zina maana mahsusi. Zaidi ya hayo, endapo tutapata *Hadith* yenye usimulizi unaotufikisha kwa Mtume ﷺ inayoelezea herufi hizi, tutakubaliana na kauli ya Mtume ﷺ. Vinginevyo tutasimama pale tuliposimamia na kusema,

ءَامَنَّا بِهِ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ رَبِّنَا^١

"Tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu." (3:7). Wanazuoni hawakukubaliana na rai moja au maelezo kuhusiana na mada hii. Kwa hiyo, anayedhani kuwa rai ya mwanazuoni fulani ni sahihi, ana khiari kuifuata, vinginevyo ni bora kujiepusha kutoa hukumu kuhusu suala hili. Allah تعالی Ndiye Mjuzi wa Yote.

¹ At-Tabari 1:208.

Herufi Hizi Zinathibitisha Muujiza wa Qur'an.

Hekima ya kutaja herufi hizi mwanzoni mwa Surah, bila kujali maana halisi ya herufi hizi, ni kuwa zinathibitisha muujiza wa Qur'ani. Hapana shaka waja wameshindwa kutunga kitu kinachofanana na Qur'an, japo imeundwa na herufi zile zile zinazotumika katika mazungumzo. Rai hii ilitajwa na Ar-Razi رحمه الله تعالى katika *Tafsir* yake aliyoihusisha na Al-Mubarrad na wanazuoni wengi wengine. Al-Qurtubi رحمه الله تعالى aliihusisha rai hii na ile ya Al-Farra na Qutrub. Az-Zamakhshari رحمه الله تعالى alikubaliana na rai hii katika tafsiri yake, *Al-Kashshaf*. Kwa nyongeza, Imam na mwanachuoni, Abu Al-Abbas Ibn Tayyiyah رحمه الله تعالى na Sheikh wetu Al-Hafiz Abu Al-Hajjaj Al-Mizzi رحمه الله تعالى wanakubaliana na rai hii. Al-Mizzi رحمه الله تعالى aliniambia kuwa hiyo pia ni rai ya Sheikh Al-Islam Ibn Taymiyyah رحمه الله تعالى. Az-Zamakhshari رحمه الله تعالى alisema kuwa herufi hizi, "Hazikutajwa mara moja, mwanzoni mwa Qur'an. Bali zilirudiwa ili iwe ni changamoto katika kuleta mfano wake, na kuwa Qur'an ni hoja ya nguvu kwamba imetoka kwa Allah تعالى. Vivyo hivyo, visa vingi vimetajwa mara nyingi, na pia changamoto dhahiri zimerejewa sehemu nyingi. Wakati mwingine herufi moja imetajwa peke yake, kama vile; *Sad, Nun na Qaf*. Wakati mwingine herufi mbili zimetajwa, kama vile;

حَم

"Ha Mim." (44:1) Wakati mwingine herufi tatu zimetajwa, kama vile,

الْم

"Alif Lam Mim." (2:1) Na herufi nne, kama vile,

الْمَر

"Alif Lam Mim Ra." (13:1) Na

الْمَص

"Alif Lam Mim Sad." (7:1), Wakati mwingine herufi tano zimetajwa,

كَهَيْعَص

"Kaf Ha Ya Ayn Swad." (19:1) Na

حَمَّ عَسَق

"Ha Mim Ayn Sin Qaf." (42:1-2).

Kwa sababu muundo wa maneno yao upo hivi, yapo maneno yaliyoundwa kwa herufi moja, mbili, tatu, nne na tano si zaidi ya hapo. Nikasema; Na kwa kuzingatia hilo, kila sura iliyoanza kwa herufi, ni lazima itataja ndani yake kuitetea Qur'an na kubainisha Miujiza na Utukufu wake. Na jambo hili linafahamika vema. Na limejiri katika sura ishirini na tisa. Na kwa kuzingatia hilo. Allah تعالى Anasema;

الْم ﴿١﴾ ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ

“Alif Lam Mim. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake...” (2:1-2)

الْم ﴿٢﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٣﴾ نَزَّلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا
لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“Alif Lam Mim. Allah! hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Yeye, Mwenye Uhai wa Milele na Mwendeshaji wa mambo yote. Amekuteremshia (Muhammad) Kitabu (Qur'an) kwa haki kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake.” (3:1-3) na

الْمص ﴿٤﴾ كِتَابٌ أَنْزَلَ إِلَيْكَ فَلَا يَكُنْ فِي صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ

“Alif Lam Mim Sad (Hii Qur'an ni) Kitabu (Kitakatifu) Kilichoteremshwa kwako (Ewe Muhammad). Basi isiwe dhiki kifuni kwako kwa ajili yake...” (7:1-2)

Aidha Allah تعالى Amesema,

الر ﴿٥﴾ كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ

“Alif Lam Ra (hiki ni) Kitabu Tulichokiteremsha kwako (Ewe Muhammad) ili uwatoe watu katika giza uwapeleke katika nuru, kwa Idhini ya Mola wao...” (14:1)

Aidha Allah تعالى Amesema,

الْم ﴿٦﴾ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧﴾

“Alif Lam Mim. Uteremsho wa Kitabu (hii Qur'an) hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Mola wa walimwengu.” (32:1-2)

﴿حَمْرٌ﴾ تَنْزِيلٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

“Ha Mim. Uteremsho (huu) umetoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Kurehemu.” (41:1-2) na

﴿حَمْرٌ﴾ عَسَقٌ ﴿٢﴾ كَذَلِكَ يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ

“Ha Mim Ayn Sin Qaf. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu (na) Mwenye Hekima Anavyokuletea Wahyi (Anavyokufunulia) na wale waliotangulia”. (42:1-3)

Kuna Aya nyingi zinazohitisha yaliyotajwa hapo juu iwapo mtu atazifuatilia kwa umakini. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

ذَلِكَ أَلْكُتُبِ لَا رَبَّ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٣﴾

2. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu!.

Hamna Shaka Ndani ya Qur'an.

Kitabu hapa ni Qur'an, na Rayb maana yake “shaka”. As-Suddi amepokea kutoka kwa Abu Malik, kutoka kwa Abu Salih, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na Murrah Al-Hamadan alipokea kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه na Masahaba wengi wengine wa Mtume ﷺ kuwa,

لَا رَبَّ فِيهِ

“Hakuna Rayb ndani yake.” Ina maana haina wasiwasi ndani yake.¹ Abu Ad-Darda, Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Abu Malik, Nafi, Ata, Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas, Muqatil bin Hayyan, As-Suddi, Qatadah na Ismail bin Khalid walisema vivyo hivyo. Kwa nyongeza, Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alisema, “Sijui kama kuna kutokukubaliana katika maelezo haya.”² Maana yake ni kuwa hiki ni kile Kitabu, Qur'an, kisichokuwa na shaka, kilichoteremshwa kutoka kwa Allah تعالى. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema katika Surat As-Sajdah,

﴿الْم﴾ تَنْزِيلُ أَلْكُتُبِ لَا رَبَّ فِيهِ مِنَ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤﴾

“Alif Lam Mim. Uteremsho wa Kitabu (hii Qur'an) hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Mola wa walimwengu.” (32:1-2)

¹ At-Tabari 1:228.

² Ibn Abi Hatim 1:31.

Baadhi ya wanazuoni wameeleza kuwa Aya (2:2) ni habari, na maana yake ni kukataza, "Msiitilie shaka Qur'an." Zaidi ya hivyo baadhi ya Wasomaji wa Qur'an wanapumzika wanaposoma,

لَا رَيْبَ ۙ

"Hapana shaka..." Kisha huanza kwa Kauli Yake تعالیٰ،

فِيهِ ۙ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

"...Ndani yake kuna muongozo kwa Muttaqin (waja wacha – Mungu)." Hata hivyo inafaa kupumzika wakati wa kusoma. Kauli Yake تعالیٰ،

لَا رَيْبَ فِيهِ ۙ

"...hakuna shaka ndani yake." Kwa sababu katika hali hii,

هُدًى

"Muongozo." Inakuwa sifa (kivumishi) ya Qur'an na inakuwa na maana nzuri zaidi kuliko,

فِيهِ ۙ هُدًى

"Ndani yake kuna muongozo."

Muongozo ni kwa Wale Wenye Taqwa.

Hidayah – Muongozo sahihi – wanapewa wale wenye Taqwa – wanaomcha Allah تعالیٰ. Allah Amesema,

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ

عَلَيْهِمْ عَمًى ۗ ؕ أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٤١﴾

"Sema: Hii (Qur'an) ni uwongofu na pozo kwa wale walioamini; na wale Wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo (Qur'an) ni giza kwao. (Hawasikii kama kwamba) hao wanaitwa, na hali ya kuwa wako mbali kabisa." (41:44) Na,

وَنُنزِّلُ مِنَ الْقُرْءَانِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۗ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٤٧﴾

"Na Tunateremsha katika Qur'an (hayo mafundisho yake) ambayo ni ponyo (pozo la nyoyo) na rehema kwa wanaoamini. Wala

hayawazidishi (mafundisho haya) madhalimu ila khasara tu (kwani hawakubali kuifuata).” (17:82)

Hiki ni kielelezo cha Aya chungu nzima zinazoonesha kuwa Waumini hasa ndio wanaofaidika na Qur’an. Hii ni kwa sababu Qur’an yenyewe ni aina ya mwongozo, lakini muongozo ni kwa wale tu wafanyao mema, kama Allah تعالی Anavyosema,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُمْ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ
لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

“Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu na poza la (dawa ya) yale yaliyomo vifuani, na uwongofu (mkubwa) na rehema kwa wanaoamini: (Nayo ni Qur’an ambayo ikifuatwa vilivyo humtengenezea mtu dunia yake au Akhera yake).” (10:57)

Ibn Abbas na Ibn Mas’ud na Masahaba wengine رضي الله عنهم wa Mtume ﷺ wamesema,

هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾

“Muongozo kwa Muttaqin (wacha – Mungu na watenda mema).” Maana yake ni mwanga kwa wale wenye Taqwa.

Maana ya Al-Muttaqin.

Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia,

هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾

“Muongozo kwa Wamchao Mungu.” Maana: “Hao ni Waumini wanaojiepusha kumshirikisha Allah تعالی na wanaomtii Yeye.” Ibn Abbas رضي الله عنهما pia alisema Al-Muttaqin maana yake, “Wale wanaoogopa adhabu ya Allah تعالی, ambayo wataipata endapo wataacha muongozo ulio sahihi ambao wanautambua na kuujua. Pamoja na hayo wanataraji Huruma za Allah تعالی kwa kuamini yale Aliyoyateremsha kwa njia ya wahyi. Qatadah alisema kuwa,

لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾

“Al-Muttaqin.” Ni wale ambao amewaelezea sifa zao kwa Kauli Yake,

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ

“Ambao huyaamini yasiyoonekana (Maadamu yamesemwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake), na husimamisha Sala.” (2:3)

Na Aya inayofuata. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alieleza kuwa Ayah (2:2) inajumuisha maana zote hizi zilizotajwa na wanazuoni, na haya ndiyo maoni yaliyo sahihi. Aidha, At-Tirmidhi na Ibn Majah walisimulia kuwa Atiyah As-Sadi رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا يَبْلُغُ الْعَبْدُ أَنْ يَكُونَ مِنَ الْمُتَّقِينَ حَتَّى يَدَعَ مَا لَا بَأْسَ بِهِ حَذْرًا مِمَّا بِهِ بَأْسٌ»

“Mja hatofikia daraja la Muttaqin (uchamungu) mpaka atakapoacha ambacho hakina madhara akichelea kufanya kile chenye madhara.”¹ At-Tirmidhi amesema, Hadithi hii ni Hasan Ghaarib.

Kuna Aina Mbili za Hidayah (Mwongozo)

Huda (muongozo) hapa, ina maana ya Imani ambayo mahali pake ni kwenye moyo, na ni Allah تعالى Pekee Awezaye Kuiweka katika moyo wa mja. Allah تعالى Amesema,

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

“Kwa hakika, wewe (Muhammad ﷺ) huwezi kumuongoa umpendaye.” (28:56). Aidha Amesema;

* لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ

“...Si juu yako (Muhammad) kuwaongoa.” (2:272). Aidha Amesema;

مَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ^ع

“Ambao Allah Anawaachia kupotea (kwa kuwa hawataki kusikiliza), basi hawana muongozo.” (7:186) Na Amesema tena;

مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ^ط وَمَنْ يُضِلِلْ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرْشِدًا^و

“Ambaye Allah Anamuongoza basi yeye ndiye aliyeongoka; na Anayemuachia kupotea, basi Hatampatia Mlinzi mwongozi.” (18:17). Na Ayat nyingine zisizokuwa hizo.

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 7:47 na Ibn Majah 2:1409.

Huda (mwongozo) pia ina maana ya ubainifu wa haki, uwazi wake na mwongozo wake. Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٢﴾

“Na kwa yakini wewe unaongoza katika njia iliyonyooka.” (42:52).

Aidha Amesema;

إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ ﴿٧﴾

“Hakika wewe ni Muonyaji, na kila kaumu ina muongozo (wake na namna yake ya kuongoza).” (13:7)

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ

“Na Thamud Tuliwaongoa (kupitia Mjumbe wetu) lakini walipenda upofu kuliko uongofu.” (41:17)

Kuthibitisha maana hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾

“Na Tukambainishia njia zote mbili – (iliyo njema na iliyo mbaya).” (90:10)

Hii ni rai ya wanazuoni ambao walisema kuwa njia mbili ina maana ya njia iliyo njema na iliyo mbaya, ambayo pia ni maelezo sahihi. Allah تعالى ni Mjuzi wa yote.

Maana ya Taqwa

Maana ya asili ya Taqwa (uchamungu) ni kuepuka vile asivyovipenda mtu. Ilikeleza kwamba Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuuliza Ubayy bin Kaab رضي الله عنه kuhusu Taqwa (uchamungu). Ubayy رضي الله عنه alisema, “Je, umewahi kutembea juu ya njia yenye miiba?” Umar رضي الله عنه akajibu, “Ndiyo.” Ubayy رضي الله عنه akasema, “Ulifanya nini?” Akajibu, “Nilijizatiti na nikawa muangalifu.” Ubayy رضي الله عنه akasema, “Hiyo ndiyo Taqwa.”

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ

“Wale wanaoamini ya Ghaib”.

Maana ya Iman

Abu Ja'far Ar-Razi رحمه الله تعالى alisema kutoka kwa Al-'Ala bin Al-Musayyib bin Rafi, kutoka kwa Abu Ishaq, kutoka kwa Abu Al-Ahwas, kutoka kwa Abdullah رضي الله عنه alisema,

*"Iman ni kusadikisha."*¹ Ali bin Abu Talhah na wengineo walisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

يُؤْمِنُونَ

"Wenye Iman." Ina maana wanaosadiki.² Pia Maamar alipokea kutoka kwa Az-Zuhri kuwa alisema, *"Iman ni matendo mema."*³ Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى alisema kuwa Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa, *"Wana Imani,"* maana yake wanamcha (Allah تعالى).⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, "Msimamo wenye nguvu ni ule ambao wanaoelezea kuwa ni wale Wanaoamini visivyoonekana kwa kauli, vitendo na itikadi. Katika muktadha huu, kumhofu Allah تعالى kumeingizwa katika maana ya jumla ya *Iman* ambayo inalazimisha kutekeleza kwa vitendo yanayotamkwa na ulimi. Hivyo *Iman* ni istilahi ambayo inajumuisha kukiri na kumuamini Allah تعالى, Vitabu Vyake, na Mitume Wake na kutambua kukiri huku kwa kutekeleza kwa dhathi yaliyotamkwa na kuthibitishwa na moyo. Nikasema; Ama katika Muktadha wa Kilugha, neno *Iman* haina maana zaidi ya kusadikisha, na wakati mwingine hutumiwa ndani ya Qur'an kwa maana hiyo. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ

***"Anamuamini Allah na anawasadiki wanaoamini."* (9:61)**

Na kama Ndugu wa Yusuf عليه السلام walivyomuambia baba yao,

وَمَا أَنْتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صَادِقِينَ ﴿١٧﴾

***"Lakini (wewe) hutatuamini (kwa haya tunayokuambia) ingawa tunasema kweli."* (12:17)**

Aidha neno *Iman* kuna wakati linatajwa pamoja na vitendo (amali) kama Allah تعالى Anavyosema,

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

***"Ila wale wenye kuamini na kutenda mema..."* (95:6)**

Pamoja na hivyo, neno *Iman* linapotumiwa katika hali hiyo linakusanya itikadi; imani, vitendo na kauli zinazotamkwa kwa ulimi. Tukalazimika kutaja kwamba:

¹ At-Tabari 1:235.

² At-Tabari 1:235.

³ At-Tabari 1:235.

⁴ At-Tabari 1:235.

'Imani huongezeka na kupungua.' Na kuhusiana na Maudhui hii, zimekuja kauli nyingi za Masahaba na Hadithi za Mtume ﷺ, ambazo tumeziwekea mlango wake mahususi mwanzoni mwa ufafanuzi wa sahihil Bukhari. Na ni za Kwake Allah تعالى Sifa Njema na Kusifiwa. Na wapo baadhi ya wanazuoni waliofasiri "Imani" kwa maana ya kumuogopa Allah تعالى. Kama Allah تعالى Alivyosema;

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ

"Hakika wale wanaomuogopa Mola wao, hali ya kuwa hawamuoni." (67:12).

Na Kauli Yake Allah تعالى,

مَنْ حَشِيَ الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ بِقَلْبٍ مُنِيبٍ ﴿٣٣﴾

"Na anayemuogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Kurehemu, na hali ya kuwa hamuoni, na akaja kwa moyo ulioelekea (kwa Mwenyezi Mungu)." (50:33)

Kuogopa ni kiini cha *Iman* na Elimu, kama Allah تعالى Alivyosema,

إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

"Kwa hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanazuoni)..." (35:28)

Maana ya *Al-Ghaib*.

Ama kuhusu maana ya *Ghaib*, *Salaf* wana maelezo yanayotofautiana, yote ni sahihi yenye kuonesha maana ya jumla. Kwa mfano, Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى alimnukuu Ar-Rabi bin Anas, kama alivyopokea kutoka kwa Abu Al-Aliyah kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ

"Wale wanaoamini ya *Ghaib*."

Wanamuamini Allah تعالى, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Yake, siku ya Mwisho, Pepo Yake, Moto na kukutana Naye. Pia wanaoamini maisha baada ya kufa na Ufunuo. Yote haya ni *Ghaib*. Qatadah bin Diamah amesema hivyo.¹

¹ At-Tabari 1:236.

Said bin Mansur alieleza kutokana na alivyosikia kutoka kwa Abdur-Rahman bin Yazid ambaye alisema, "Tulikuwa tumekaa na Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه tulipowataja Masahaba wa Mtume na ubora wa amali zao kuliko zetu. Abdullah رضي الله عنه alisema, "Mambo ya Muhammad ﷺ yalikuwa wazi kwa wale waliomuona. Naapa kwa Jina la Yule ambaye hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye! Hakuna mtu anayeweza kufikia imani zaidi ya kuamini *Al-Ghaib*." Kisha akasoma,

الْم ﴿١﴾ ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ

"Alif Lam Mim. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni muongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasiyoonekana..." (2:1-3) mpaka Kauli Yake Allah تعالى¹

الْمُفْلِحُونَ ﴿٣﴾

"..na hao ndio wenye kuongoka." Kama hivyo wamesimulia Ibn Abu Hatim, Ibn Marduwyah; na Al-Hakim katika *Mustadrak*² aliandika *Hadith* hii. Al-Hakim aliitolea maoni *Hadith* hii kuwa ni sahihi na kuwa *Shaikhain* – Masheikh wawili wa *Hadith* – Al-Bukhari na Muslim – hawakuikusanya japokuwa inakidhi vigezo vyao.

Imamu Ahmad aliandika *Hadith* yenye maana sawa na hiyo kutoka kwa Ibn Muhayriz ambaye alisema, Nilimuambia Abu Jumuah رضي الله عنه, "Tusimulie *Hadith* ambayo uliisikia kutoka kwa Mtume ﷺ." Akasema, "Ndio, nitakusimulia *Hadithi* nzuri. Kuna siku tulikuwa tuna kula chakula cha mchana na Mtume ﷺ. Abu Ubaydah رضي الله عنه, aliyekuwa pamoja nasi alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Kuna watu walio bora zaidi yetu? Tumesilimu mbele yako na tukapigana Jihad pamoja nawe." Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ قَوْمٌ مِنْ بَعْدِكُمْ يُؤْمِنُونَ بِي وَلَمْ يَرَوْنِي»

"Ndio, watu watakaokuja baada yenu, ambao wataniamini japokuwa hawakuniona."³

¹ Said bin Mansur 2:544.

² Ibn Abu Hatim 1:34 na Al-Hakim 2:260.

³ Ahmad 4:106.

Hadithi hii ina njia nyingine ya Mapokezi kutoka kwa Abubakar bin Marduwyah katika Tafsir yake, kutoka kwa Salih bin Jubayr ambaye alisema, Abu Jumuah Al-Ansari رضي الله عنه, Sahaba wa Mtume ﷺ alikuja *Bayt Al-Maqdis* (Jerusalem) kusali. Raja bin Hawyah alikuwa pamoja nasi, hivyo Abu Jumuah رضي الله عنه alipomaliza, tulitoka nje kumsalimu. Alipokaribia kuondoka alisema, “Mna haki na zawadi.” Nitakusimulieni *Hadith* niliyoisikia kutoka kwa Mtume ﷺ.” Tukamuambia, “Fanya hivyo, na Allah تعالى Akurehemu.” Alisema, “Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ, watu kumi pamoja na Muadh bin Jabal رضي الله عنه. Tukasema, “Ewe Mtume! Je, kuna watu watakaolipwa zaidi yetu? Tulimuamini Allah تعالى na tukakufuata wewe.” Mtume ﷺ akasema,

«مَا يَمْتَعُكُمْ مِنْ ذَلِكَ وَرَسُولُ اللَّهِ بَيْنَ أَظْهُرِكُمْ يَأْتِيكُمْ بِالْوَحْيِ مِنَ السَّمَاءِ، بَلْ قَوْمٌ
بَعْدَكُمْ يَأْتِيهِمْ كِتَابٌ مِنْ بَيْنِ لَوْحَيْنِ يُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَعْمَلُونَ بِمَا فِيهِ، أُولَئِكَ أَكْثَرُ
أَجْرًا مَرَّتَيْنِ»

“Kitu gani kinachokuzuieni kufanya hivyo, wakati Mjumbe wa Allah ni miongoni mwenu, akiwaleteeni Wahyi utokao mbinguni? Kuna watu watakuja baada yenu ambao watapewa kitabu chenye majalada mawili (Qur’an) na wataamini yaliyomo na watatekeleza Maamrisha yake. Wana malipo makubwa kuliko nyie, ujira mara mbili.”¹

وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢٠٠﴾

“Wanasimamisha Sala, na wanatoa vile Tulivyowaruzuku.”

Maana ya *Iqamat As-Salah* (Kusimamisha Sala)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ

“Wanasimamisha Sala.” – Maana yake: “Kusali kwa kuzingatia nguzo na sharti zake.” Ad-Dhahhak alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, *Iqamat As-Salah* maana yake ni kukamilisha rukuu, sajdah, kusoma Qur’an, unyenyekevu na kuhudhuria katika Sala.² Qatadah alisema, *“Iqamat As-Salah”* maana yake kuchunga wakati, udhu, rukuu na sijda za Sala.³

¹ Ibn Asakir 6:368.

² At-Tabari 1:241.

³ At-Tabari 1:241.

Muqatil bin Hayyan alisema *Iqamat As-Salah* ina maana ya, “Kuchunga wakati, kujitwahirisha kwa ajili yake, kukamilisha rukuu, sijida na kusoma Qur’an, *Tashahud* na kumuomba rehema Mtume ﷺ. Hii ndiyo *Iqamat As-Salah*.¹

Maana ya “Kutoa” katika Aya hii.

Ali bin Abu Talhah (na wengineo) aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢٠٤﴾

“Na wanatoa katika vile Tulivyowaruzuku”

Ina maana, “Zaka ya mali.”² As-Sudi alisema kutoka kwa Abu Malik, kutoka kwa Abu Salih, kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما, kutoka kwa Murra, kutoka kwa Bin Mas’ud رضي الله عنه na wengi katika Masahaba wa Mtume ﷺ kuwa,

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢٠٤﴾

“Na wanatoa katika vile Tulivyowaruzuku”

Ina maana: “Mtu kutumia kwa ajili ya familia yake. Hii inakuwa kabla ya Aya ya Zakah haijateremshwa.”³ Juwaybir amepokea kutoka kwa Adh-Dhahhak, “Kutoa Sadaka ilikuwa ni njia ya kujikurubisha kwa Allah تعالى, kwa mujibu wa utashi wa Mtu na uwezo wake. Mpaka nguzo ya kutoa ilipotemshwa katika Ayat saba za *Surat Al-Baraah* (Sura ya 9). Hizo zilifuta zilizotangulia.”⁴

Katika sehemu nyingi; Allah تعالى Ametaja Sala na kutoa mali pamoja. Sala ni haki ya Allah تعالى na ni aina ya kumuabudu. Ni pamoja na Kumpwekesha katika Kumnyenyekea, Kumshukuru, Kumtukuza, Kumuomba msaada na Kumtegemea. Kutoa ni sehemu ya kuwahurumia viumbe kwa kuwapa kitakachowasaidia, na watu wanaostahili sadaka hiyo kwanza ni jamaa, mke, watumishi kisha watu wengine. Hivyo kila aina ya kukimu kulikowajibishwa na Zaka iliyofaradhihwa kumejumuishwa katika maneno ya Allah تعالى.

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢٠٤﴾

“Na wanatoa kutokana na vile Tulivyowapa.” Sahihi mbili zimeandika kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Ibn Abu Hatim 1:37.

² Ibn Abu Hatim 1:37.

³ At-Tabari 1:243.

⁴ At-Tabari 1:243.

«بُئِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَنَسٍ: شَهَادَةٌ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَإِقَامُ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ، وَصَوْمِ رَمَضَانَ، وَحَجِّ الْبَيْتِ»

“Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kukiri kwa moyo kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Allah, kusimamisha Sala, kutoa Zaka, kufunga Ramadhan na Kuhiji katika Nyumba ya Allah.”¹

Kuna *Hadith* nyingi zinazohusu somo hili.

Maana ya Sala

Katika lugha ya Kiarabu, maana ya msingi ya neno *Sala* ni dua. Katika istilahi ya Kidini, Sala ina maana ya vitendo vya kuinama na kusujudu, na vitendo vingine vinavyohusiana nayo, vyenye sifa zake maalumu, vinavyofanywa katika muda maalumu, kwa masharti yanayofahamika vema.

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾

4. Na ambao wanaoamini yaliyoteremshwa kwako, na yaliyoteremshwa kabla yako na wanaoamini (kuwa iko) Akhera.

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa:

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ

“Na ambao wanaoamini yaliyoteremshwa kwako, na yaliyoteremshwa kabla yako...”

Ina maana, “Wanaamini yale Allah تعالى Aliyokutuma kuyafikisha, na kwa yale ambayo Mitume waliopita waliteremshiwa, hawayatofautishi katika kuyaamini na wala hawayakanushi waliyokuja nayo kutoka kwa Mola wao.”²

وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٥﴾

“Na wanaoamini (kuwa iko) Akhera.” Maana: Kufufuliwa, (siku ya Kufufuliwa), Pepo, Moto, Kuhesabiwa na Mizani inayopima uzito wa amali (Mizani).² Akhera imetajwa hivyo kwa sababu inakuja baada ya maisha ya duniani.

¹ At-Tabari 1:243.

² Fat’hul Al-Bari 1:64 na Muslim 1:45.

miongoni mwao. Na semeni, "Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja..." (29:46).

Pia Allah تعالى Amesema;

يَتَّيِبُهَا لِّلَّذِينَ ءَاتَوْهَا آلِكِتَابَ ءَامِنُوا بِمَا نَزَّلْنَا مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ

"Enyi mliyopewa Kitabu! Aminini Tuliyoateremsha (kwa Muhammad) yanayosadikisha yale yaliyo nanyi." (4:47).

Na Allah تعالى Amesema;

قُلْ يٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَآبِ لَسْتُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ حَتَّىٰ تُقِيمُوا ٱلتَّوْرَةَ وَٱلْإِنجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ مِّن رَّبِّكُمْ

"Sema (Ewe Muhammad), "Enyi watu wa Kitabu! (Mayahudi na Wakristo) Hamko juu ya chochote (katika Dini yenu) mpaka msimamisha Taurati na Injili na haya yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu (Nayo ni Qur'an)." (5:68).

Allah تعالى Amewaelezea waumini kuwa wote muamini hivyo. Allah تعالى Amesema;

ءَامَنَ ٱلرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ ۖ وَٱلْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَمَلَآئِكَتِهِ ۖ وَكُتُبِهِ ۖ وَرُسُلِهِ

"Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu (pia wameamini hayo); wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Yake ..." (2:285)

وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا بِٱللَّهِ وَرُسُلِهِ ۖ وَلَمْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ

"Na waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Yake wala wasiwafarikisha yeyote katika wao (bali wamewaamini wote)...". (4:152)

Pamoja na Aya zinazoonesha kuwa Waumini wa kweli wote wanamuamini Allah تعالى, Mitume Yake na Vitabu Vyake.

Waumini miongoni mwa Watu waliopewa Kitabu wana umuhimu wa pekee hapa, kwa kuwa wanaamini Vitabu vyao na yote yanayoambatana navyo, hivyo watu kama hao wanaposilimu na wakaamini Dini ya Uislamu kwa ukamilifu wake, watapata malipo ya aina mbili.

Ama wasiokuwa wao, huamini vitabu vilivyotangulia kwa ujumla wake.

Kama ilivyokuja katika Hadithi Sahihi ya Mtume ﷺ kuwa amesema,

«إِذَا حَدَّثَكُمْ أَهْلَ الْكِتَابِ فَلَا تُكذِّبُوهُمْ وَلَا تَصَدَّقُوهُمْ وَلَكِنْ قُولُوا: آمَنَّا بِالَّذِي
أُنزِلَ إِلَيْنَا وَأَنْزَلَ إِلَيْكُمْ»

“Watu waliopewa Kitabu watakapokusimulieni, msiwakanushe wala msiwaamini. Bali semeni, “Tunaamini tuliyoteremshiwa na mliyo teremshiwa.”¹

Hata hivyo, inawezekana Imani waliyonayo Waarabu wengi kuhusumafunzo ya Dini ya Kiislam kama alivyoteremshiwa Muhammad ﷺ imekamilika, inayokusanya na na yenye ithibati kuliko imani ya watu wa Kitabu waliosilimu.

Kwa hiyo, endapo wataamini Uislam miongoni mwa Watu wa Kitabu wanapata malipo mara mbili. Waislam wengine wenye Imani thabiti wanapata malipo sawa ukilinganisha na mbili watakazopata watu wa Kitabu (baada ya kusilimu).

Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa Yote.



¹ Abu Dawud (4:59).

أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾

“Hao wako juu ya uongofu utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu”. (2:5)

Jazaa ya Waumini ni Uongofu na Kufuzu.

Allah تعالیٰ Anasema,

أُولَئِكَ

“Hao”

Inaturejesha kwa wale wanaoamini yasiyoonekana (*ghaib*), wanaosimamisha Sala, wanatoa katika vile walivyo pewa na Allah تعالیٰ, wanaoamini yale aliyo teremshiwa Mtume ﷺ na Mitume walio tangulia, wanaoamini maisha yajayo na wanaandaa mahitajio yao kwa maisha hayo kwa kufanya matendo mema na kuepuka yaliyokatazwa.

Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

عَلَىٰ هُدًى

“Katika uongofu.”

Maana yake, wanafuata nuru, muongozo na wamepata utambuzi kutoka kwa Allah تعالیٰ.

أُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾

“Na hao ndio wenye kufaulu.”

Maana yake, duniani na Akhera. Watapata yale waliyoyatafuta na wataokolewa na maovu waliyokuwa wakijiepusha nayo.

Kwa hiyo watapata malipo ya maisha ya kudumu peponi na kuwa salama na adhabu ambayo Allah تعالیٰ Amewaandalia maadui Zake.

* * *

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ
 ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ
 لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ حَتَّمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ
 وَعَلَى أَبْصَارِهِمْ غِشْوَةً وَلَهُمْ
 عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾ وَمِنَ
 النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ
 وَيَأْتِيهِمُ الْآخِرُ وَمَا هُمْ
 بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا
 يُخَدِّعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا
 يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾ فِي قُلُوبِهِمْ
 مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا
 وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا
 يَكْذِبُونَ ﴿١٠﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ
 لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا
 إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾ أَلَا
 إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن
 لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾ وَإِذَا قِيلَ
 لَهُمْ ءَامِنُوا كَمَا ءَامَنَ
 النَّاسُ قَالُوا أَنُؤْمِنُ كَمَا
 ءَامَنَ السُّفَهَاءُ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ
 السُّفَهَاءُ وَلَكِن لَّا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾
 وَإِذَا لُقُوا بِالَّذِينَ ءَامَنُوا
 قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَى
 شَيْطَانِهِمْ قَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ
 إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِئُونَ ﴿١٤﴾
 اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ
 فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٥﴾
 أُولَئِكَ الَّذِينَ اسْتَرَوْا
 الضَّلَالََةَ بِالْهُدَىٰ فَمَا
 رَاحَتِ يُجُرَّتُهُمْ وَمَا كَانُوا
 مُهْتَدِينَ ﴿١٦﴾

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ
 ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا
 يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾

**6. "Hakika wale waliokufuru
 (kwa ukaidi tu na inadi) ni
 sawa kwao ukiwaonya au
 usiwaonye; hawataamini."
 (2:6)**

Allah تعالى Anasema,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا

"Hakika wale waliokufuru"

Inamaana walioficha ukweli
 kwa kuwa Allah تعالى
 Ameandika kuwa watafanya
 hivyo, si muhimu kama
 (Muhammad ﷺ) atawaonya
 au hatawaonya bado
 wangekanusha yale waliyo-
 teremshiwa. Vivyo hivyo
 Allah تعالى Anasema,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ
 كَلِمَتُ
 رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ
 كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوْا
 الْعَذَابَ
 أَلَا لَيْمٌ ﴿٧﴾

**"Hakika wale ambao neno la Mola wako limekwishathibitika juu yao,
 hawataamini. Ijapokuwa kila ishara itawajia; mpaka iwajie adhabu
 inayoumiza." (10:96-97)**

Kuhusu watu wa Kitabu walioasi, Allah تعالى Amesema,

وَلَيْنَ أَتَيْتَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ بِكُلِّ آيَةٍ مَّا تَبِعُوا قِبْلَتَكَ

“Na hao waliopewa Kitabu, hata ukawaletea hoja za kila namna hawatafuata Kibla chako.” (2:145)

Aya hizi zinadhihirisha kuwa yeyote aliyehandikiwa na Allah تعالى kuharibikiwa, hatompata yeyote wa kumsaidia, na yeyote ambaye Allah تعالى Amempotosha, hatompata wa kumuongoza. Hivyo usiwaonee huruma – Ewe Muhammad ﷺ wafikishie ujumbe. Kwa hakika yeyote miongoni mwao atakayeukubali ujumbe wako atapata malipo bora. Ama wale wanaoupa mgongo ujumbe, usiwa-huzunikie wala usijishughulishie nao.

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٤٠﴾

“...Basi juu yako ni kufikisha tu (uliyoamrishwa kuyafikisha), na juu Yetu ni Kuwahesabu (siku ya Kiama).” (13:40)

إِنَّمَا أَنْتَ نَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٢﴾

“Wewe ni Muonyaji tu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa kila kitu.” (11:12)

Ali bin Abu Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْتَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾

“Hakika wale waliokufuru (kwa ukaidi tu na inadi) ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye; hawataamini.” (2:6)

“Kuwa Mtume ﷺ alikuwa na hamu watu wote waamini na wafuate muongozo aliowaletea. Allah تعالى Akamfahamisha kuwa hakuna atakayemuamini isipokuwa wale Aliowakadiria wema toka awali, na hakuna atakayekwenda kombo isipokuwa wale Allah تعالى Aliowaandikia uovu tokea awali.”¹

¹ At-Tabari 1:252.

خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَعَلَى سَمْعِهِمْ وَعَلَى أَبْصَارِهِمْ غِشْوَةً وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾

7. (Kama kwamba) Mwenyezi Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana kifuniko; basi watakuwa na adhabu kubwa.

Maana ya *Khatama* (Amepiga Muhuri)

As-Sudi amesema,

خَتَمَ اللَّهُ

“Khatama Allah...”

Maana yake: “Allah تعالى Amepiga muhuri.”¹ Qatadah alisema kuwa Aya hii ina maana, “Shetani aliwadhibiti walipomtii.” Hivyo, Allah تعالى Alifunga mioyo yao, usikivu wao na uoni wao, na hawawezi kuona uongofu wala kusikia au kufahamu.”² Ibn Jurayj alisema kutoka kwa Mujahid,

خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ

“Allah Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao.”

“Upigaji Muhuri hutokea wakati dhambi inapokaa kwenye moyo na kuuzingira kutoka pande zote, na huku kuzama moyo kwenye madhambi kuna kuwa na muhuri, ikiwa na maana ya lakiri.”³

Ibn Jurayj pia alisema kuwa muhuri unapigwa kwenye moyo na usikivu.⁴ Kwa nyongeza, Ibn Jurayj alisema kuwa Abdullah bin Kathir alisimulia kuwa Mujahid alisema, “Doa si baya kama muhuri, na muhuri si mbaya kama kufuli ambayo ni aina mbaya zaidi.”⁵

¹ Ibn Abu Hatim 1:44.

² Ibn Abu Hatim 1:44.

³ Ibn Abu Hatim 1:44.

⁴ At-Tabari 1:259.

⁵ At-Tabari 1:259.

Al-A'mash alisema kuwa, Mujahid aliashiria kwa mkono wake huku akisema, "Walikuwa wakisema kuwa moyo uko kama hivi – yaani kitanga cha mkono. Mja anapotenda dhambi, sehemu ya moyo itajikunja, akaviringisha kidole cha shahada, kama hivi. Mja anapofanya dhambi nyingine, sehemu ya moyo itajiviringisha, akaviringisha kidole kingine mpaka akaviviringisha vidole vyote. Kisha akasema, "Halafu moyo utapigwa muhuri." Mujahid pia alisema kuwa waliona kwamba maelezo yalibusu *Ran* (kutu) (rejea 83:14).¹

Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema, "Ummah unakubaliana kuwa Allah تعالى Amejieleza Mwenyewe katika Kupiga muhuri na Kuifunga mioyo ya makafiri kama adhabu kwa kukanusha kwao." Aidha Allah تعالى Amesema,

بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ

"Bali Mwenyezi Mungu Amezipiga muhuri kwa kufuru zao..."
(4:155)

Kisha Ametaja *Hadith* kuhusu kubadilika mioyo (ambayo Mtume ﷺ aliomba dua),

«يَا مُقَلَّبَ الْقُلُوبِ ثَبِّتْ قُلُوبَنَا عَلَى دِينِكَ»

"Ewe Unayebadilisha nyoyo, zithibitisha nyoyo zetu katika Dini Yako."

Pia alitaja *Hadith* kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه iliyoandikwa katika Sahih, ambapo Mtume ﷺ alisema,

«تُعْرَضُ الْفِتْنَةُ عَلَى الْقُلُوبِ كَالْخَصِيرِ عُوْدًا عُوْدًا، فَأَيُّ قَلْبٍ أَشْرَبَهَا نُكِبَتْ فِيهِ نُكْتَةٌ سَوْدَاءٌ وَأَيُّ قَلْبٍ أَنْكَرَهَا نُكِبَتْ فِيهِ نُكْتَةٌ بَيْضَاءٌ حَتَّى تَصِيرَ عَلَى قَلْبَيْنِ: عَلَى أَيْضٍ وَيَثَلِ الصَّفَا، فَلَا تَضُرُّهُ فِتْنَةٌ مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَالْأَخْرُ أَسْوَدُ مُرْتَابًا كَالْكُوْزِ مُجَخَّبًا لَا يَتَعْرِفُ مَعْرُوفًا وَلَا يُنْكِرُ مُنْكَرًا»

"Fitna (maonjo na mitihani) hupewa nyoyo, kama vile mabua yanayoshonwa kuwa mkeka uliofumwa, moja baada ya nyingine. Moyo wowote unaokubali fitna, basi doa jeusi litatiwa juu yake. Na

¹ At-Tabari 1:258.

Moyo wowote unaokataa fitina huwekwa alama ya doa jeupe. Nyoyo zitakuwa za aina mbili: Mweupe, kama jabali lisilo na kitu; hakuna Fitna itakayoathiri aina hii madhali mbingu na ardhi bado vipo. Aina nyingine ni nyeusi, kama vile kikombe kilichofunikwa, kwani moyo huu hautambui mema wala kukana uovu.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Ukweli kuhusu somo hili ni kile ambacho *Hadith* sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ kimeeleza, Abu Hurayra رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الْمُؤْمِنَ إِذَا أَذْنَبَ ذَنْبًا كَانَتْ نُكْتَةٌ سَوْدَاءَ فِي قَلْبِهِ، فَإِنْ تَابَ وَتَرَعَّ وَاسْتَعْتَبَ صَقَلَ قَلْبُهُ وَإِنْ زَادَ زَادَتْ حَتَّى تَغْلُوَ قَلْبُهُ، فَذَلِكَ الرَّأْيُ الَّذِي قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: ﴿كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ﴾»

“Muumini anapofanya dhambi, doa jeusi hutiwa moyoni mwake. Atakapotubu, akajizuia na kujutia, moyo wake utapigwa msasa tena. Atakapofanya makosa zaidi, madoa yataongezeka mpaka yaufunike moyo wake.”

Hii ni *Ran* (kutu) ambayo Allah تعالى Ameielezea,

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾

“Sivyo hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (kwa maovu) waliokuwa wakiyachuma.” (83:14)²

At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah waliandika *Hadith* hii na At-Tirmidhi alisema kuwa ni *Hasan Sahihi*.³

¹ Muslim 1:128.

² At-Tabari 1:260.

³ Tuhfatul - Ahwadhi.

Maana ya neno “Ghishawah” na Ubainifu wake.

Jua kuwa hapa pana kanuni ya usomaji Qur’an, kuna kisimamo timilifu katika Kauli Yake Allah تعالى;

حَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَعَلَى سَمْعِهِمْ

“Mwenyezi Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao.” (2:7)

Kisha kuna mapumziko na halafu inaendelea,

وَعَلَى أَبْصَارِهِمْ غِشْوَةٌ

“...na juu ya macho yao pana kifuniko.”Ni sahihi, kwani muhuri unapigwa juu ya moyo na masikio ambapo *Ghishawah*, kifuniko kimewekwa sawa sawa, juu ya macho. Katika *Tafsir* yake, As-Sudi alisema kuwa Ibn Abbas na Ibn Mas’ud walizungumzia Kauli ya Allah تعالى، رضي الله عنهما

حَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَعَلَى سَمْعِهِمْ

“Mwenyezi Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao.”

Anasema, ili wasisikie wala kuelewa. Allah تعالى pia Amesema kuwa Aliweka kifuniko kwenye macho yao na hivyo hawaoni.¹

Wanafiki

Tulitaja mwanzoni mwa *Surat Al-Baqarah* kuwa Aya nne za mwanzo zinawaelezea Waumini. Aya ya 6 na 7 zinawaelezea Makafiri. Baada ya hapo Allah تعالى Anaanza Kuwaelezea Wanafiki ambao wanaonesha kuamini kwao na wanaficha ukafiri wao. Kwa kuwa suala la Wanafiki lina utata, watu wengi hawafahamu ukweli wake, Allah تعالى Ameeleza sifa zao kwa urefu. Kila sifa ambayo Allah تعالى Ameitumia Kuwaelezea ni aina ya unafiki. Allah تعالى Aliteremsha *Surat Tawbah* (Surah ya 9) na *Surat Munafiqun* (Surah ya 63) kuhusu Wanafiki. Pia amewataja Wanafiki katika *Surat An-Nur* (Surah ya 24) na Surah nyingine, ili watu waweze kuelewa vizuri hali zao ili wajiepushe nazo, na wajiepushe na yule mwenye sifa hizo. Allah تعالى Amesema:

¹ At-Tabari 1:266.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَيَأْتِيهِمُ الْآخِرُ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٦﴾ تَخَذِعُونَ لِأَلَّهِ
وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا تَخَذِعُونَ إِلَّا أُنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٧﴾

8. Na katika watu wako (Wanafiki) wasemao: “Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na hali wao si wenye kuamini.

9. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini lakini hawadanganyi ila nafsi zao; na hawatambui!.

Maana ya Nifaq (Unafiki)

Nifaq (unafiki) maana yake ni kuonesha kheri na kuficha uovu. Kuna aina nyingi za *Nifaq*: Kufanya *Nifaq* katika imani kutawafanya watu kuishi motoni milele, na kufanya *Nifaq* katika matendo ambayo ni moja katika madhambi makuu kama tutakavyoeleza karibuni, Allah تعالی Akipenda. Ibn Jurayj ameeleza, Mnafiki, “Vitendo vyake ni tofauti na kile anachokitangaza, anachokificha ni tofauti na anachokitamka, utokaji na uingiaji wake na kuwepo na kutokuwepo kwake.”¹

Mwanzo wa Unafiki

Wahyi kuhusu sifa bainifu za Wanafiki uliteremshwa Madina hii ni kwa sababu katika kipindi cha Makka hawakuwepo Wanafiki. Bali ilikuwa kinyume chake, watu walilazimishwa na hali ya wakati ule kujifanya sio Waumini, na kuficha imani katika mioyo yao. Ilihali ndani ya Mioyo yao ni waumini. Baadaye, Mtume ﷺ alihamia Madina ambapo alikuta wenyeji wa hapo Ansar ni mchanganyiko wa makabila ya Aws na Khazraj. Walikuwa wakiabudia masanamu wakati wa *Jahiliyyah* – kabla ya Uislam, kama walivyokuwa washirikina wa Kiarabu enzi hizo. Kadhalika Makabila matatu ya Kiyahudi yaliishi Madina, Banu Qaynuqa - maswahiba wa Khazraj, Banu An-Nadhir na Banu Quraydha - maswahiba wa Aws. Watu wengi kutoka makabila ya Aws na Khazraj walisilimu. Hata hivyo Mayahudi wachache waliukubali Uislam, kama vile Abdullah bin Salam. Katika siku za mwanzo hawakuwepo Wanafiki Madina kwa sababu Waislamu hawakuwa na nguvu kiasi cha kuogopewa. Kinyume chake, Mtume ﷺ alitiliana mikataba ya amani na Mayahudi na Makabila kadha ya Kiarabu yaliyokuwa pembezoni mwa Madina. Muda si mrefu vita vya Badr vilipiganwa na Allah تعالی Aliwapa Waislam ushindi. Kiongozi wa Madina alikuwa Abdullah bin Ubayy

¹ At-Tabari 1:270.

bin Salul. Alikuwa Mtawala wa Al-Khazraj, na wakati wa kipindi cha *Jahiliyyah* alikuwa bwana wa makabila mawili – Aws na Khazraj. Walikuwa wamekaribia kumteua kuwa Mfalme wao. Wakati ujumbe ulipofika Madina na wengi wakasilimu, wengi wakaacha kujishughulisha naye. Moyo wa Ibn Salul ulijaa chuki dhidi ya Uislam na wafuasi wake. Vita vya Badr vilipotokea alisema, “Dini ya Allah imekuwa dhahiri.” Hivyo alijifanya Muislamu kama walivyokuwa wengine, pia wengi miongoni mwa Watu wa Kitabu. Hapa ndipo unafiki ulipoanza katika Madina na pembezoni walipokuwa wakiishi makabila yanayo hamahama. Ama miongoni mwa *Muhajirin* hapakuwa na Wanafiki, kwa kuwa walihama kwa khiyari yao ili kupata radhi za Allah تعالی. Bali kila Muislamu aliyekaa Makka, alilazimika kuacha mali yake yote, familia yake na ardhi yake, na alifanya hivyo akitarajia malipo kutoka kwa Allah تعالی siku ya Kiyama.

Tafsiri ya Aya (2:8)

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالی alisimulia kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَيَأْتِيهِمُ الْآخِرُ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

“Na katika watu wako (Wanafiki) wasemao: “Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na hali wao si wenye kuamini”

Hii inawakusudia Wanafiki miongoni mwa Aws na Khazraj na waliokuwa na tabia kama hiyo.”¹

Hivi ndivyo Abu-Al’Aliyah, Al-Hasan, Qatadah na As-Sudi walivyoielezea Aya hii. Allah تعالی Aliteremsha sifa bainifu za Wanafiki, ili Waumini wasije wakahadaiwa na umbile lao la nje, na hivyo kusababisha Waumini kukosa kujihadhari kutokana na uovu wao mkubwa. Vinginevyo Waumini wangeweza kudhani kuwa Wanafiki ni Waumini wakati ukweli ni kuwa wao hawakuamini. Kuwachukulia watenda dhambi kama wacha-Mungu ni jambo la khatari sana. Allah تعالی Amesema,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَيَأْتِيهِمُ الْآخِرُ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

“Na katika watu wako (Wanafiki) wasemao: “Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na hali wao si wenye kuamini.”

¹ At-Tabari 1:269.

Maana: Wanatamka kauli batili kwa ndimi zao tu, Kama Allah تعالى Alivyosema,

إِذَا جَاءَكَ الْمُتَنَفِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ

“Wanapokuja Wanafiki husema: “Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini Wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa wewe ni Mtume Wake...” (63:1).

Aya hii ina maana kuwa Wanafiki wanatamka maneno tu wanapokutana nawe sio kwa sababu wanayaamini wasemayo. Wanafiki wanasisitizia imani yao kwa Allah تعالى na Siku ya Mwisho kwa maneno tu, wakati huo sio uhakika wa mambo, kwa hiyo Allah تعالى Amewaelezea Wanafiki kuwa ni waongo wanapotamka Imani, Aliposema:

وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُتَنَفِقِينَ لَكَذِبُونَ ﴿٦٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia ya kuwa hakika Wanafiki ni waongo, (wanasema wasiyoyasadiki)...” (63:1) na

وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٦٤﴾

“...na hali ya kuwa sio wenye kuamini.”

Allah تعالى Amesema,

مُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا

“Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale Walioamini”.

Wanafiki wanadhihirisha kuamini lakini wanaficha kutoamini kwao wanadhani kwa kufanya hivyo watampotosha Allah تعالى; au kauli wanazotoa zitawasaidia mbele ya Allah تعالى, na huu ndio ushahidi kuwa wamezama katika lindi la ujinga. Wanadhani kwa tabia yao hiyo watamhadaa Allah تعالى, kama wanavyowadanganya baadhi ya Waumini. Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكَرَّ وَخَسَّبُونَ عَنْهُمْ عَلَى شَيْءٍ آلَا إِنَّهُمْ

هُمُ الْكَذِبُونَ ﴿٥٨﴾

“(Wakumbushe) siku Atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuapie (Mwenyezi Mungu kwa uongo) kama wanavyoapa kwenu, na watadhani ya kwamba wamepata kitu kwa kusema uongo huo! Kwa hakika hao ndio waongo hasa.” (58:18)

Hivyo Allah تعالى Amekanusha njia yao kwa kusema,

وَمَا تَخْتَدِعُونَ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٦﴾

“Lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui!”

Allah تعالى Amesema kuwa Wanafiki wanajidanganya wenyewe kwa tabia hii, japo wenyewe hawajui ukweli huu. Allah تعالى pia Amesema,

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ

“Wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu. Naye Atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko)...” (4:142)

Aidha Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Jurayj alitoa maelezo kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ

“Wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu. Naye Atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko)...” (4:142)

Wanafiki wanatangaza, “Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى”, wakitaka uhakika wa kutakaswa damu yao na mali yao, wakati huo huo wakificha kukanusha imani.”¹ Said amesema kuwa Qatadah alisema,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٦﴾ تَخَدِعُونَ اللَّهَ
وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا تَخَدِعُونَ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٦﴾

“Na katika watu wako (Wanafiki) wasemao: ‘Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na hali wao si wenye kuamini. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini lakini hawadanganyi ila nafsi zao; na hawatambui!”

Hizi ndizo sifa za Mnafiki. Kigeugeu, anasema ukweli kwa ulimi wake na anakanusha kwa moyo na vitendo vyake. Anaamka na hali tofauti na ile aliyokwenda nayo wakati wa kulala. Na anakwenda kulala katika hali tofauti na ile aliyooamka nayo. Hubadili fikra zake kama vile meli inavyopelekwa na upepo uvumao.²

¹ Ibn Abu Hatim 1:46.

² Ibn Abu Hatim 1:47.

فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿١٠﴾

10. "Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu Amewazidishia maradhi. Basi watakuwa na adhabu iumizayo kwa sababu ya kusema kwao uongo."

Maana ya "Maradhi" Katika Ayah hii.

As-Suddi alipokea kutoka kwa Abu Malik, naye kutoka kwa Abu Salih, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, naye kutoka kwa Murrah Al-Hamdani kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه na Masahaba wengine kuhusu aya hii,

فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ

"Nyoyoni mwao mna maradhi." Ina maana ya "wasiwasi"¹. Mujahid, Ikrimah, Al-Hasan Al-Basri, Abu Al-A'liyah, Ar-Rabi bin Anas na Qatadah pia walisema vivyo hivyo.² Abdrur-Rahman bin Zayd bin Aslam alitoa maoni juu ya,

فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ

"Nyoyoni mwao mna maradhi." Maradhi katika Dini, sio maradhi ya mwili. Wao ni Wanafiki na maradhi ni shaka walioleta katika Uislamu.

فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا ۗ

"Na Mwenyezi Mungu Amewazidishia maradhi." Ikiwa na maana Kuwazidishia tabia ya uovu.³ Aidha Alisoma,

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٢٤﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ

مَّرَضٌ فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ

"Ama wale walioamini inawazidishia imani, nao wanafurahi. Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao..." (9:124-125)

Na akasema yafuatayo, "Uovu kwa uovu na mkengeuko kwa mkengeuko wao."

¹ At-Tabari 1:280.

² Ibn Abu Hatim 1:48.

³ At-Tabari 1:280.

Kauli hii ya Abdur-Rahman ni sahihi, na ina adhabu ambayo inalingana na dhambi, kama walivyodhukuru wanazuoni wa mwanzo. Vivyo hivyo Allah تعالى Anasema,

وَالَّذِينَ آهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَءَاتَيْنَهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾

“Na wale wanaokubali kuongoka Anawazidishia uongofu na Anawapa (jaza) ya uchaMungu wao.” (47:17)

Allah تعالى Amesema baada ya hapo,

بِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿١٨﴾

“Kwa sababu ya kule kusema kwao uongo.” Wanafiki wana sifa bainifu, wanasema uongo na wanakanusha yasiyoonekana (*Ghaib*).

Wanazuoni waliosema ya kuwa Mtume ﷺ aliwajua Wanafiki wa nyakati zake wanategemea Hadithi moja tu ya Hudhayfah bin Al-Yaman رضي الله عنه kama ushahidi. Katika Hadithi hiyo Mtume ﷺ alitaja majina ya Wanafiki kumi na wane wakati wa vita vya Tabuk. Hawa Wanafiki walikula njama za kumuua Mtume usiku, juu ya kilima kilichokuwepo katika eneo lile. Walipanga kumchokoza ngamia wa Mtume ﷺ, ili wamtie taharuki amuangushe Mtume ﷺ na aporomoke chini ya kilima. Allah تعالى Alimfahamisha Mtume ﷺ kuhusu njama hizo, na Mtume ﷺ alimueleza Hudhayfah رضي الله عنه majina ya wanafiki hao. Ama kuhusu Wanafiki wasiokuwa hawa, Allah تعالى Alieleza khabari zao,

وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ مُنْفِقُونَ ۗ وَمِنْ أَهْلِ الْمَدِينَةِ مَرَدُوا عَلَىٰ النِّفَاقِ لَا تَعْلَمُهُمْ ۗ نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ ۗ

“Na katika Mabedui wanaokaa pembezoni mwenu katika vitongoji vya karibu yenu hapo (Madinah) kuna Wanafiki. Na katika wenyeji wa Madina (pia kuna wengine Wanafiki) wamebobeza katika unafiki; (hata) huwajui (Ewe Muhammad) (kuwa ni Wanafiki) sisi Tunawajua.” (9:101)

* لِّئِن لَّمْ يَنْتَهِ الْمُنْفِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْمُرْجِفُونَ فِي الْمَدِينَةِ لَنُغْرِبَنَّكَ بِهِمْ ثُمَّ لَا يُجَاوِزُونَكَ فِيهَا إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٠١﴾ مَلْعُونِينَ ۗ أَيُّهَا تُقِفُوا أُخِذُوا

وَقَاتِلُوا تَقَاتِلُوا ﴿١٠٢﴾

“Kama Wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao na waenezao fitna katika Madina hawatoacha, basi kwa yakini Tutakusalitisha juu yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda mchache tu, (kisha litawafika la kuwafika). Wamelaanika! Popote watakapoonekana wakamatwe na wauliwe kabisa.” (33:60-61).

Aya hizi zinathibitisha kuwa Mtume hakufahamishwa kuhusu kila Mnafiki wa zama zake. Bali, Mtume ﷺ alielezwa juu ya sifa bainifu, na akadhania kuwa baadhi ya watu walikuwa na sifa hizo. Aidha Allah تعالى Amesema,

وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ فَلاَعْرِفْتَهُمْ بِسِيمَاهُمْ^ع وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ^ع

“Na kama Tungelipenda Tungelikuonesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao; lakini bila ya shaka utawajua kwa namna na msemu wao.” (47:30)

Mnafiki mwenye sifa mbaya kabisa katika zama zile alikuwa Abdullah bin Ubayy bin Salul. Zayd bin Arqan رضي الله عنه – Sahaba wa Mtume - alitoa ushahidi unaoaminika kuhusu suala hili. Zaidi ya hayo, kuna wakati Umar bin al-Khattab رضي الله عنه alizungumzia suala la Ibn Salul kwa Mtume ﷺ, naye alisema,

«إِنِّي أَكْرَهُ أَنْ تَتَحَدَّثَ الْعَرَبُ أَنَّ مُحَمَّدًا يَقْتُلُ أَصْحَابَهُ»

“Sitopenda Waarabu kuambizana kuwa Muhammad anawaua Masahaba wake.”¹

Hata hivyo, Ibn Salul alipokufa, Mtume ﷺ alimsalia na akahudhuria mazishi yake kama alivyokuwa akifanya kwa Waislamu wengine. Iliandikwa katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنِّي خَيْرْتُ فَاخْتَرْتُ»

“Nimepewa hiyari ya kumsalia, basi nikachagua.” Na katika masimulizi mengine,

«لَوْ أَعْلَمْتُ أَنِّي لَوْ زِدْتُ عَلَى السَّبْعِينَ بِغَفْرٍ لَهُ لَزِدْتُ»

“Kama ningelijua kwamba kwa kumuomba (Allah) zaidi ya mara sabini angemsamehe, ningefanya hivyo.”

¹ Bukhari 4905, na Muslim 2584.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ
الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ ﴿١٢﴾

11. Na wanapoambiwa: Msifanye uharibifu ulimwenguni Husema:
“Sisi ni watengenezaji.”

12. Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui. (2:11-12)

Maana ya Uharibifu

Katika Tafsiri yake, As-Suddi alisema kuwa Ibn Abbas, Ibn Mas’ud رضي الله عنهما na Masahaba wa Mtume ﷺ wanazungumzia aya,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١﴾

“Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu ulimwenguni” Husema:
“Sisi ni watengenezaji”.

Hao ndio Wanafiki. Kwa Mintarafu yao,

لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ

“Msifanye uharibifu ulimwenguni.” Huo ni ukanushaji na kitendo cha kukosa utii.¹ Abu Jafar رحمه الله تعالى alisema kuwa Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa Abu Al-A’liyah alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ

“Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu ulimwenguni.”

Maana yake: “Msifanye vitendo vya kuvunja utiifu ulimwenguni.” Uharibifu wao ni kutomtii Allah تعالى, kwa sababu kutomtii Allah تعالى duniani, au kutotii Maamrisha ya Allah تعالى, ni uharibifu ulimwenguni. Amani ulimwenguni na Mbinguni inapatikana kwa kumtii Allah تعالى.² Ar-Rabi bin Anas na Qatadah walisema kama hivyo.³

¹ Fat’hul Al-Bari 8:184, Muslim 4:2141.

² At-Tabari 1:288.

³ Ibn Abu Hatim 1:50.

Aina za Uharibifu Zinazofanywa na Wanafiki.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Wanafiki wanafanya uharibifu ulimwenguni kwa kumuasi Bwana wao huku wakiendelea kufanya yaliyokatazwa. Aidha huacha yale waliyofaradhishiwa na Allah تعالى, na wanaitilia shaka Dini Yake, japo Yeye hakubali amali ya mtu yeyote isipokuwa mwenye Imani thabiti katika Dini Yake. Aidha Wanafiki wanawadanganya Waumini kwa kuwaeleza kinyume cha shaka na kusita waliyoyaficha katika mioyo yao. Wanapopata fursa wanatoa misaada mingi kwa kadri ya uwezo wao dhidi ya wapenzi wa Allah تعالى, na wanawaunga mkono wale wanaomkanusha Allah تعالى, Vitabu Vyake na Mitume Wake. Hivyo ndivyo Wanafiki wanavyofanya uharibifu ulimwenguni, wakati wakidhani wanafanya kazi njema duniani.¹

Kauli hii ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى ni sahihi, kuwachukulia Wasioamini kuwa marafiki ni moja ya aina ya uharibifu ulimwenguni. Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُن فِتْنَةً فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٣﴾

“Na wale waliokufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipofanya hivi itakuwako chokochoko katika ardhi na maharibiko makubwa.” (8:73)

Kwa njia hii Allah تعالى Alikata mahusiano kati ya Waumini na Makafiri. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكٰفِرِينَ اَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ؕ اٰتُرِيْدُونَ اَنْ يٰجْعَلُوْا لِلّٰهِ عَلَيْكُمْ سُلْطٰنًا مُّبِيْنًا ﴿١٤٤﴾

“Enyi mlioamini! Msiwafanye Makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Mnataka awe nayo (Mtume wa) Mwenyezi Mungu hoja dhahiri juu yenu (ya kuwa nyinyi wabaya)?” (4:144)

اِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ فِي الدَّرَكِ الْاَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ يٰجِدَ لَهُمْ نٰصِرًا ﴿١٤٥﴾

“Bila shaka Wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika Moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yeyote).” (4:145).

¹ Ibn Abu Hatim 1:51.

Kwa kuwa sura ya nje ya Mnafiki inaonesha uaminifu, anawatatiza Waumini wa kweli. Tabia ya udanganyifu waliyo nayo Wanafiki ni kitendo cha uharibifu, kwa sababu wanawadanganya Waumini kwa kudai wasichokiamini, na kwa sababu wanawaunga mkono Makafiri dhidi ya Waislamu.

Iwapo Mnafiki atabaki kuwa Kafiri (badala ya kujifanya Muislamu), madhara yanayotokana naye yatakuwa machache. Na kama akiwa muaminifu kwa Allah تعالى na akatamka yaliyo sawa na vitendo vyake, atapata ufanisi. Na kwa kuzingatia hili Allah تعالى Anasema,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ ﴿١١٠﴾

“Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu ulimwenguni” Husema: “Sisi ni watengenezaji.”

Maana yake: “Tunataka kufanya marekebisho baina ya makundi mawili, Waislamu na Watu wa Kitabu.”¹

Allah تعالى Anasema;

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ ﴿١١١﴾

“Hakika wao ndio waharibuji, lakini hawatambui.”

Aya hii ina maana kuwa tabia ya Wanafiki, na madai yao kuwa wanataka amani, hiyo peke yake ni uharibifu, japokuwa kutokana na ujinga wao hawaoni kuwa huo ni uharibifu.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ءَامِنُوا كَمَا ءَامَنَ النَّاسُ قَالُوا أَنُؤْمِنُ كَمَا ءَامَنَ السُّفَهَاءُ ۗ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ

السُّفَهَاءُ وَلَكِن لَّا يَعْلَمُونَ ﴿١١٢﴾

13. “Na wanapoambiwa: “Amini kama walivyoamini watu.” Husema: “Oh! Tuamini kama walivyoamini wale wapumbavu?” Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui.”

Allah تعالى Amesema kuwa endapo Wanafiki wataambiwa,

¹ At-Tabari 1:289.

ءَامِنُوا كَمَا ءَامَنَ ٱلنَّاسُ

“Aminini kama walivyoamini watu.”

Ikiwa na maana, “Aminini kama Waumini wanavyomuamini Allah تعالى, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Ufufuo baada ya Kufa, Pepo, Jahanam nk. Na mumtii Allah تعالى na Mjumbe Wake kwa kutekeleza Maamrisho na kujiepusha na makatazo.” Pamoja na hivyo Wanafiki walijibu kwa kusema,

قَالُوا أَنُؤْمِنُ كَمَا ءَامَنَ ٱلسُّفَهَاءُ

“Tuamini kama walivyoamini wale wapumbavu?”

Walikuwa wanawakusudia (Allah تعالى Awalaani Wanafiki) Masahaba wa Mtume ﷺ. Tafsir hii ni sawa na ile ya Abu Al-'Aliyah na As-Suddi katika Tafsir yake yenye Isnadi ya upokezi mpaka kwa Ibn Abbas, Ibn Mas'ud na Masahaba wengine رضي الله عنهم. Hii pia ni Tafsir ya Ar-Rabi bin Anas na Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Wanafiki walisema, “Sisi na wao tunakuwa sawa, tunafuata njia moja, ilhali wao ni wapumbavu?” Mpumbavu maana yake ni mtu punguani mwenye maarifa kidogo juu ya maeneo ya hatari na maeneo yenye faida kwake. Kwa mujibu wa wanazuoni wengi hii ndio sababu Allah تعالى Ametumia neno mjinga kwa kuwajumuisha watu wote wa aina hiyo pale Aliposema,

وَلَا تُؤْتُوا ٱلسُّفَهَاءَ ٱمۡوَالِكُمۡ ٱلَّتِي جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُمۡ قِيۡمًا

“Wala msiwape wapumbavu mali zenu (mali zao mlizonazo) ambazo Mwenyezi Mungu Amezijaalia kwa ajili ya maisha yenu (nyote)...”
(4:5)

Allah تعالى Aliwajibu Wanafiki katika matukio haya yote. Mathalan, Allah تعالى Alisema,

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ ٱلسُّفَهَاءُ

“Hakika wao ndio waharibifu.”

Hivyo Allah تعالى Alithibitisha ya kuwa Wanafiki kwa hakika ni waharibifu, bado,

وَلَكِن لَّا يَعْلَمُونَ

“Lakini hawatambui.”

Kwa kuwa ni wajinga mno. Wanafiki hawajui kiwango cha upotofu kwao na ujinga wao, na hali hii ni ya hatari sana kwao, inawatia upofu mkubwa, na kuwatupa mbali kabisa na uongofu.

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ شَيَاطِينِهِمْ قَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ إِنَّمَا نَحْنُ

مُتَّبِعُونَ ﴿١٤﴾ اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٥﴾

14. "Na wanapokutana na walioamini husema: "Tumeamini" na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao husema: "Hakika sisi tu pamoja nanyi, tunawachezea shere tu."

15. "Mwenyezi Mungu Atawalipa shere yao na Kuwaacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo."

Hila na Ulaghai wa Wanafiki

Allah تعالى Amesema Wanafiki wanapokutana na Waumini, wanatangaza imani yao na kujifanya Waumini, Watiifu na marafiki. Wanafanya hayo ili kupotosha na kuwadanganya Waumini. Wanafiki walitaka kuwa na sehemu ya faida na mapato ambayo yamkini Waumini watayapata. Bado,

وَإِذَا خَلَوْا إِلَىٰ شَيَاطِينِهِمْ

"Na wanapokuwa peke yao na mashetani wao."

Maana yake: Wanapokuwa peke yao na mashetani wao, kama vile viongozi wao na mabwana wao miongoni mwa Viongozi wa dini ya Mayahudi, Wanafiki na Washirikina.

Mashetani ya Kijini na ya Kibanadamu.

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, "Mashetani ya kila kizazi ni wale waharibifu miongoni mwao. Kuna mashetani ya kibinadamu na Mashetani ya kijini. Allah تعالى Amesema,

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيَاطِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرَفَ

الْقَوْلِ غُرُورًا ۝

“Na namna hii Tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) Mashetani katika watu na (Mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenzi wao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya...” (6:112)

Maana ya Kucheza Shere.

Allah تعالى Amesema,

قَالُوا إِنَّا مَعَكُمْ

“Wanasema: “Hakika sisi tu pamoja nanyi...”

Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii maana yake, “Tuko pamoja nanyi.”

إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِءُونَ ﴿١١٢﴾

“Kwa hakika, tunawacheza shere tu.”

Maana yake: Kazi yetu kuwacheza shere watu (Waumini) na kuwadanganya.¹ Adh-Dhahhak alisema amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya,

إِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِءُونَ ﴿١١٢﴾

“Kwa hakika, tunawachezea shere tu.”

Maana yake: “Sisi (Maana: Wanafiki) tunawacheza shere Masahaba wa Muhammad.”² Pia, Ar-Rabi bin Anas na Qatadah walisema vivyo hivyo.¹ Kauli ya Allah تعالى,

اللَّهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٣﴾

“Mwenyezi Mungu Atawalipa shere yao na Kuwaacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo.”

Anawajibu Wanafiki na Anawaadhibu kwa mwenendo wao. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alitolea maelezo, “Allah تعالى Alitaja Atakachowafanyia Siku ya Ufufuo, pale Aliposema,

¹ At-Tabari 1:300.

² At-Tabari 1:300.

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُوا انظُرُونَا نَقْتِسِبْ مِنْ نُورِكُمْ قِيلَ
 أَرْجِعُوا وَرَاءَكُمْ فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَهُدٍ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ
 مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٣﴾

“Siku watakaposema Wanafiki wanaume na Wanafiki wanawake kuwaambia walioamini: “Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.” Waambiwe (kwa stizahi), “Rudini nyuma yenu mkaitafute nuru yenu (labda mmeisahau).” Utiwe baina yao ukuta wenye mlango; ndani yake mna rehema na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu.” (57:13)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّمَا نُمَلِّهِمْ خَيْرًا لَّأَنفُسِهِمْ ۚ إِنَّمَا نُمَلِّهِمْ لِيَزِدَادُوا إِثْمًا ۚ

“Wala wasidhani wale waliokufuru kwamba huu muda Tunawapa (wakaishi kwa starehe) ni bora kwao. Hakika Tunawapa muda na (Inatokea ya kuwa) wanazidisha madhambi (katika muda huo)...” (3:178)

Kisha Akasema, “Katika Aya hii na nyingine kama hii Allah تعالى Amewacheza shere Wanafiki na Washirikina.”

Hila za Wanafiki na Kuadhibiwa Kwao

Allah تعالى Amesema ya kuwa Atawaadhibu Wanafiki kwa shere zao, Alitumia maneno yale kuelezea matendo na adhabu, japo yana maana tofauti. Vile vile Allah تعالى Amesema,

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۚ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ

“Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na (ubaya) huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi, ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu...” (42:40) na,

¹ At-Tabari 1:300.

فَمَنْ أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَأَعْتَدُوا عَلَيْهِ

“...na wanaokushambulieni, nanyi pia washambulieni...”(2:194)

Kitendo cha kwanza ni cha dhuluma, wakati cha pili ni cha uadilifu. Hivyo matendo yote yana njia moja, lakini kwa hakika ni tofauti. Hivi ndivyo wanazuoni wanavyoelezea ‘ulaghai’, hila na ‘kucheza shere’ vilipoelezwa na Allah تعالى ndani ya Qur’an. Vitimbi, hadaa na shere vinatazamwa kwamba ni mchezo tu, na havina manufaa yoyote. Lakini suala la kujitetea na kukabaliana na dhulma kwa njia ya haki na kuipata haki hilo halikatazwi.

Maana ya “Kuwaacha Katika Upotovu Wao Wakitangatanga Ovyo”.

Allah تعالى Amesema,

وَيَمُدُّهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٥١﴾

“Mwenyezi Mungu Atawalipa shere yao na Kuwaacha katika upotofu wao wakitangatanga ovyo.”

As-Suddi aliripoti kuwa Ibn Abbas, Ibn Mas’ud na Masahaba kadha رضي الله عنهم wa Mtume ﷺ walisema kuwa,

وَيَمُدُّهُمْ

“Na kuwaacha katika...”

Maana yake: “Anawapa muda.” Pia Mujahid alisema, “Yeye Anawazidishia (upotofu).” Allah تعالى Amesema,

أَتَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَنِينَ ﴿٥١﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا

يَشْعُرُونَ ﴿٥٢﴾

“Je! Wanafikiri ya kuwa yale Tunayowapa – (nayo ni) mali na watoto. Ndio Tunawatangazia katika kheri (zao)? (Wapi hayo!) Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Ibn Jarir رحمه الله تعالى ametoa maelezo, “Maana Sahihi ya Aya hii ni, “Tunawaongezea kwa kuwapa muda zaidi na kuwaacha waendeleo katika

upotofu na uasi." Allah تعالى Amesema,

وَتُقَلَّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَدَّرَهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ

يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

“(Hawataamini) na Tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama wasivyoamini mara ya kwanza; na Tutawaacha katika maasiya yao wakitangatanga ovyo.” (6:110)¹

Neno *Tughyan* kama lilivyotumika katika Aya ina maana ya kuchupa mipaka (kuzidi mno) kama Allah تعالى Alivyosema katika Ayah nyingine,

إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكِ فِي الْجَارِيَةِ ﴿٦٩﴾

“Maji yalipofurika (katika zama za Nuhu), Sisi Tulikupandisheni katika hicho kinachokwenda (Baharini, jahazi).” (69:11)

Aidha, Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa neno “*Amah*” katika Ayah hii lina maana, “Kupotoka”, kama vile kusema, “Fulani kapotoka.” Pia alizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

“Katika maasiya yao wakitangatanga ovyo.”

Wamezingirwa na kupotoka na kutoamini, ambayo inawafanya wachanganyikiwe kiasi cha kutojua njia ya kutokea. Hii ni kwa sababu Allah تعالى Ameipiga mihuri mioyo yao, Akaitia lakiri na Akawatia upofu macho yao dhidi ya uongofu na Kuyawekea kifuniko. Kwa hiyo, hawatambui au kutafuta njia ya kutoka kwenye upotofu.²

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ فَمَا رَبِحَت تَّجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿١١٠﴾

16. “Hao ndio waliohiari upotofu kuliko uongofu; lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.”

Katika Tafsir yake, As-Suddi ameripoti kuwa Ibn Abbas na Ibn Mas’ud رضي الله عنهما na baadhi ya watu wengine katika Masahaba wametoa maelezo kuhusu,

¹ At-Tabari 1:307.

² At-Tabari 1:309.

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ

“Hao ndio waliokhiari upotofu kuliko uongofu.”

Wakisema kuwa ina maana, “Walifuata upotofu na wakaacha uongofu.” Mujahid amesema, “Wameamini Halafu wakakufuru.” Qatadah amesema, “Wamekhitari upotofu badala ya uongofu.” Maelezo ya Qatadah yanafanana na Maneno ya Allah تعالى kuhusu Thamud,

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ

“Na Thamud Tuliwaongoza lakini walipenda upotofu kuliko uongofu.” (41:17)

Kwa Muhtasari, kauli tulizozitaja kutoka kwa wanazuoni wa *Tafsiri* zinaonesha kuwa Wanafiki walipotoka kutoka uongofu wa kweli na wakachagua upotofu, wakibadilisha uovu mahali pa wema. Maana hii inaelezea Kauli ya Allah تعالى,

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ

“Hao ndio waliohiari upotofu kuliko uongofu...”

Maana yake: Walibadilisha uongofu kwa kununua upotofu. Maana hii pia inawahusu wale ambao kwanza waliamini kisha wakakufuru baadaye ambao Allah تعالى Anawaeleza,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ

“Na hayo ni kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo muhuri umepigwa juu ya nyoyo zao...” (63:3)

Aya inawajumuisha wale waliokhitari upotofu badala ya uongofu. Wanafiki wako makundi mbalimbali.

Ndiyo sababu Allah تعالى Akasema,

فَمَا رَیَحَتْ تُجْرَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٦٣﴾

“Lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.”

Maana yake: Biashara yao haikufanikiwa wala hawakuwa na maadili au kuongozwa katika suala hili. Zaidi ya hayo, Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Qatadah alitolea maelezo Aya hii,

﴿فَمَا رِيحَتُ تَجْرَتُهُمْ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ﴾

“Lakini biashara yao haikupata faida wala hawakuwa wenye kuongoka.”

Wallahi! Nimewaona wakiacha uongofu na kufuata upotofu, wakaacha *Jamaah* (Jamii ya Waumini) na kufuata makundi, wakaacha amani na kufuata hofu, na wakaacha *Sunnah* na kufuata *Bid'a*.¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى pia alielezea kauli zinazofanana na hizo.²

* * *

¹ At-Tabari 1:316.

² Ibn Abu Hatim 1:60.

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِينَ اسْتَوْقَدُوا نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُمْ
 ذَهَبَ اللَّهُ بِنُورِهِمْ وَتَرَكَهُمْ فِي ظُلُمَاتٍ لَا يُبْصِرُونَ ﴿١٧﴾
 صُمُّ بَكُمْ عُمَىٰ فَهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٨﴾ أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ
 السَّمَاءِ فِيهِ ظُلُمَاتٌ وَرَعْدٌ وَبَرْقٌ يَجْعَلُونَ أَصْبِعَهُمْ فِي
 آذَانِهِمْ مِنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ الْمَوْتِ ۗ وَاللَّهُ مُحِيطٌ
 بِالْكَافِرِينَ ﴿١٩﴾ يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ كُلَّمَا أَضَاءَ
 لَهُمْ مَشَوْا فِيهِ وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ
 لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ ۗ إِنَّا اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ
 قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾ يَتَأْتِي النَّاسَ آعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ
 وَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢١﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ
 الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً
 فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۗ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أُندَادًا
 وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾ وَإِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا
 عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّن مِّثْلِهِ ۚ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِّن
 دُونِ اللَّهِ ۖ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٣﴾ فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا وَلَن
 تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي أُوتِيهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ
 أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿٢٤﴾

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِينَ اسْتَوْقَدُوا نَارًا
 فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُمْ ذَهَبَ اللَّهُ
 بِنُورِهِمْ وَتَرَكَهُمْ فِي ظُلُمَاتٍ لَا
 يُبْصِرُونَ ﴿١٧﴾ صُمُّ بَكُمْ عُمَىٰ فَهُمْ
 لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٨﴾

17. "Mfano wao (hawa Wanafiki) ni kama mfano wa wale (wasafiri walio kumbwa na kiza) waliokoka moto, (na) ulipowaonesha yaliyo pembezoni mwao, Allah Aliiondoa nuru yao hiyo na kuwawacha katika viza, hawaoni."

18. "Viziwi, mabubu, vipofu kwa hivyo hawatarejea."

Mfano wa Wanafiki.

Allah تعالى Aliwapigia mfano Wanafiki pale walipokhitari upotofu na kuacha uongofu, na kugeuka kwao kuwa vipofu baada ya kuona.

Mfano wao ni kama mtu aliyewasha moto. Moto

ulipowaka, na ukaangaza eneo lililomzunguka, yule mtu alifaidika na akawa salama. Kisha ghafla moto ukazimika. Hivyo kiza totoro kikamzingira, na hakuweza kuona kitu wala njia ya kuondokea pale. Zaidi ya hivyo mtu yule

akawa kiziwi, hakuweza kusikia; bubu, hakuweza kusema na akawa kipofu kiasi ambacho hata kama kungekuwa na mwanga, asingeweza kuona. Hii ndio sababu inayomfanya asiweze kurejea katika hali yake kabla ya tukio hilo. Hii ni sawa na hali ya Wanafiki ambao walichagua upotofu badala ya uongofu. Mfano huu unaonesha kuwa mwanzo Wanafiki waliamini, kisha wakakufuru, kama Allah تعالى Alivyoieleza katika sehemu nyingine za Qur'an.

Kauli ya Allah تعالى،

ذَهَبَ اللَّهُ بِنُورِهِمْ

“Allah Aliiondoa nuru yao...”

Maana yake: Allah تعالى Aliyaondoa yaliyokuwa yanawanufaisha, na huo ndio mwanga na Akawaachia yale yaliyokuwa yanawadhuru, ambayo ni kiza na moshi. Allah تعالى Amesema،

وَتَرَكَّهُمْ فِي ظُلْمَةٍ

“Na kuwaacha katika viza.”

Maana: Wasiwasi wao, kukufuru na unafiki.

لَا يُبْصِرُونَ

“(Hivyo) hawaoni.” Maana yake: Wanashindwa kuona njia iliyo sawa au kufuata mwelekeo. Kwa nyongeza ni،

صَمٌّ

“Viziwi.” Na hivyo hawawezi kusikia kheri wala kujjua.

بُكْمٌ

“Mabubu.” Na hawawezi kutamka maneno ambayo yangewasaidia.

عُمَىٰ

“Na vipofu.” Katika kiza na upotofu. Aidha Allah تعالى Amesema،

فَلَيْسَ لَهَا لَمْ تَعْمَىٰ إِلَّا بَصَرٌ وَلَكِنْ تَعْمَىٰ الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ

“Kwa hakika macho hayapofuki (yakadhuru katika Dini) lakini nyoyo ambazo zimo vifuani ndizo zinazopofuka (zikadhuru katika Dini).” (22:46)

Na hii ndio sababu hawawezi kurejea katika uongofu waliokuwamo kabla kwa kuwa waliuza kwa upotofu.

أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ السَّمَاءِ فِيهِ ظُلُمَاتٌ وَرَعْدٌ وَبَرْقٌ يَجْعَلُونَ أَصْبَعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ مِّنَ الصَّوَاعِقِ
 حَذَرَ الْمَوْتِ ۗ وَاللَّهُ مُحِيطٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿١٧﴾ يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ ۗ كُلَّمَا أَضَاءَ لَهُمْ
 مَشْوَاهُ فِيهِ وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 عَلِيُّ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٨﴾

19. "Au (mfano wao pia) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni; ndani yake mkawa mna viza na radi na umeme; wakawa wakitia vidole vyao masikioni mwao kwa ajili ya miungurumo, kwa kuogopa kufa; (na kufanya hivyo hakuwasaidii kitu). Na Mwenyezi Mungu Anawajua vyema hao makafiri (Wanafiki)."

20. "Unakaribia umeme huo kunyakua macho yao; kila unapowaangazia huenda ndani yake na unapowafanyia giza husimama. Na Mwenyezi Mungu Angependa Angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu."

Mfano Mwingine wa Wanafiki.

Huu ni mfano mwingine ambao Allah تعالیٰ Ameutoa kuhusu Wanafiki ambao baadhi ya wakati wanaujua ukweli na wakati mwingine huutilia shaka. Basi nyoyo zao zipo katika hali ya mashaka, kuchanganyikiwa na kukufuru,

كَصَيْبٍ

"Ni kama mvua sayyib." Maana yake: "Mvua" kama ilivyothibitishwa na Ibn Mas'ud, Ibn Abbas, na Masahaba wengine wengi رضي الله عنهم¹, pia Abu Al-'Aliyah, Mujahid, Said bin Jubayr, Ata, Al-Hasan Al-Basri, Qatadah, Atiyah, Al-Awfi, Ata Al-Khurasani, As-Suddi na Ar-Rabi bin Anas.² Adh-Dhahhak³ alisema, "Ni Mawingu." Hata hivyo, maoni yanayokubalika ni kuwa ina maana ya mvua inayonyesha chini wakati wa viza,

¹ At-Tabari 1:334.

² Ibn Abu Hatim 1:66.

³ Ibn Abu Hatim 1:67.

ظَلَمْتُمْ

“Viza” Maana yake Hapa ni: shaka, kukufuru na unafiki.

وَرَعَدٌ

“Radi” Ni inayotia hofu mioyoni. Wanafiki wakati wote wamejawa na woga na mashaka. Kama Allah تعالى Alivyowaelezea,

يَحْسِبُونَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ

“Wanadhani kila kishindo (kinachozuka) ni juu yao...” (63:4)

Na Allah تعالى Amesema,

وَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ إِيَّاهُمْ لِمَنْكُمُ وَمَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرُقُونَ ﴿٦٣﴾ لَوْ يَخْتَدُونَ مَلَجًا أَوْ مَغْرَبًا أَوْ مُدْخَلًا لَوْلَا إِلَیْهِ وَهُمْ يَجْمَعُونَ ﴿٦٤﴾

“Na wanaapa kwa (Jina) la Mwenyezi Mungu kwamba wao ni pamoja nanyi. Wala wao si pamoja nanyi. Bali wao ni watu wanaogopa (ndio maana wanasema huku kwa Waislamu na huko kwa Makafiri). Kama wangalipata pa kukimbilia au mapango au mahali (pengine) pa kuingia, (bila shaka) wangekimbilia mbio huko, wanakwenda shoti (kama mafarasi waliochafuka).” (9:56-57)

وَبَرْقٌ

“Umeme.”

Ni mwangaza wa imani ambao wakati fulani unahisiwa katika nyoyo za Wanafiki. Na kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema,

يَجْعَلُونَ أَصْبَعَهُمْ فِيْءِآذَانِهِمْ مِنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ الْمَوْتِ وَاللَّهُ مُحِيطٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٦٥﴾

“Wakawa wakitia vidole vyao masikioni mwao kwa ajili ya miungurumo, kwa kuogopa kufa; (na kufanya hivyo hakuwasaidii kitu). Na Mwenyezi Mungu Anawajua vyema hao makafiri (Wanafiki).”

Ina maana kuchukua kwao tahadhari hakuwasaidii kwa sababu wanafungwa na Utashi na Uamuzi wa Allah تعالى. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ ﴿١٧﴾ فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ ﴿١٨﴾ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿١٩﴾
وَاللَّهُ مِنْ وَرَائِهِمْ مُحِيطٌ ﴿٢٠﴾

“Je, zimekuwasilia habari za majeshi ya makafiri. Firauni na Thamud? Lakini waliokufuru wamo katika kukukadhibisha tu. Na Mwenyezi Mungu Amewazunguka kote kote (hawawezi kuikimbia Adhabu Yake).” (85:17-20)

Kisha Allah تعالى Akasema,

يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ^ط

“Unakaribia umeme huo kunyakua macho yao.”

Ina maana kwa sababu umeme wenyewe una nguvu, na kwa sababu uwezo wao wa kufahamu ni dhaifu na hauwawezeshi kuipa nguvu imani. Pia Ali Ibn Abu Talha aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo Aya hii,

يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ أَبْصَارَهُمْ^ط

“Unakaribia umeme huo kunyakua macho yao.”

Qur'an imetaja karibu siri zote za Wanafiki.¹ Ali Ibn Abu Talhah pia amesimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

كُلَّمَا أَصَاءَ لَهُمْ مَشَوْا فِيهِ

“Kila unapowaangazia huenda ndani yake.”

Kila mara Wanafiki wanapopata hisa katika ushindi wa Waislam, hutulia na hisa hiyo. Kila Uislam unapopatwa na maafa, wanakuwa tayari kurejea kwenye ukafiri.² Hali kadhalika Allah تعالى Amesema,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ فَإِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ بِهِ^ط

“Na katika watu wako wanaomuabudu Mwenyezi Mungu ukingoni. Ikiwafikia kheri, hutulia kwayo...” (22:11).

¹ At-Tabari 1:349.

² At-Tabari 1:349.

Pia Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما رحمة الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضى الله عنهما alisema,

كُلَّمَا أَصَاءَ لَهُمْ مَشَوْا فِيهِ وَإِذَا أُظْلِمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا

“Kila unapowaangazia huenda ndani yake na unapowafanyia giza husimama.”

Maana: Wanatambua ukweli na wanauzungumzia mazungumzo yaliyo sahihi, lakini wanaporejea kwenye ukafiri huchanganyikiwa.¹

Haya yalisemwa pia na Abu Al-‘Aliyah, Al-Hasan, Al-Basri, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas na As-Suddi, walipokea kutoka kwa Masahaba kuwa maelezo hayo ni sahihi zaidi, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.²

Hivi ndivyo watakavyokuwa katika Siku ya Hukumu, watu watapewa nuru kwa mujibu wa viwango vya imani zao.

Baadhi yao watapewa nuru itakayoangaza umbali wa maili kadhaa, wengine zaidi na wengine umbali mfupi.

Baadhi ya watu, nuru zao zitakuwa zinaangaza kwa muda na kuzimwa kwa muda. Kwa hiyo watatembea juu ya *Sirat* (daraja lililo juu ya Moto) wakati nuru inapoangaza na kusimama inapozimwa.

Baadhi ya watu hawatakuwa na nuru kabisa, hao ni Wanafiki ambao Allah تعالى Amewaelezea Aliposema,

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُوا انظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِنْ نُورِكُمْ قِيلَ

أَرْجِعُوا وَرَاءَكُمْ فَالْتَمِسُوا نُورًا

“Siku watakaposema Wanafiki wanaume na Wanafiki wanawake kuwaambia walioamini: “Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.” Waambiwe (kwa stihizahi), “Rudini nyuma yenu mkaitafute nuru yenu (labda mmeisahau).” (57:13)

¹ At-Tabari 1:346.

² Ibn Abu Hatim 1:75.

Allah تعالى Aliwaelezea Waumini,

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ بُشْرَانُكُمْ الْيَوْمَ
جَنَّاتٌ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Siku utakapowaona Waislam wanaume na Waislam wanawake, nuru zao zinakwenda mbele yao na kuliani kwao, (Wanaambiwa) “Furaha yenu leo; (mnapewa) bustani zipitazo mito mbele yake.” (57:12)

Na Allah تعالى Akasema,

يَوْمَ لَا تَحْزَى اللَّهُ النَّبِيَّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ نُورُهُمْ يَسْعَى بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ
يَقُولُونَ رَبَّنَا آتِنَا نُورَنَا وَاعْفِرْ لَنَا إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦٦﴾

“Siku ambayo Mwenyezi Mungu Hatamdhalilisha Mtume (Muhammad) wala wale walioamini pamoja naye; Nuru yao itakuwa inakwenda mbele yao na pande zao za kulia (na kushoto); na huku wanasema; “Mola wetu! Tutimize nuru yetu, na Utughufirie, hakika Wewe ni Mwenye Uwezo juu ya kila kitu.” (66:8).

“Hadithi zilizokuja kueleza suala hili.” Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alitolea maelezo Aya hii,

نُورُهُمْ يَسْعَى بَيْنَ أَيْدِيهِمْ

“Nuru zao zinakwenda mbele yao.”

Watapita juu ya *Sirat* kulingana na amali zao. Nuru watakuwa nayo baadhi yao itakuwa kubwa kama mlima, wakati nuru ya wengine itakuwa na ukubwa kama wa mtende. Watu watakaokuwa na nuru kidogo ni wale ambao vidole gumba vyao vitatoa mwangaza na kuzimika wakati mwingine.¹ Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى pia alisema kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kila mtu miongoni mwa watu wa *Tawhid* watapata nuru katika Siku ya Kufufuliwa. Ama

¹ At-Tabari 23:3179.

Mnafiki, nuru yake itazimishwa. Waumini wakishuhudia nuru ya Mnafiki ikizimwa, watakuwa na wasiwasi. Hivyo wataomba dua,

رَبَّنَا أَنْعِمْ لَنَا نُورَنَا

“Mola Wetu! Tutimizie nuru yetu...”¹

Adh-Dhahhak bin Muzahim alisema, “Katika Siku ya Kufufuliwa, kila mmoja aliyepokea imani, atapewa nuru. Watakapowasili katika *Sirat*, nuru ya Wanafiki itazimwa. Waumini watakapoona hivyo, watakuwa na wasiwasi na kuomba dua,

رَبَّنَا أَنْعِمْ لَنَا نُورَنَا

“Mola wetu! Tutimizie nuru yetu...” (66:8)

Aina za Waislamu, Aina za Makafiri na Wanafiki.

Kuna aina tofauti za watu. Kuna Waislamu safi ambao wameelezwa katika Aya nne za mwanzo (2:2-5) za *Surat Al-Baqarah*, kuna Makafiri ambao wameelezwa katika Aya mbili zinazofuatia. Na kuna aina mbili za Wanafiki waliopigiwa mfano wa mto, na wanafiki wenye kusitasita, ambao nuru yao ya imani kuna wakati inawashwa na kuna wakati inazimwa. Mfano wao ni mvua, hali zao sio mbaya kama aina ya kwanza. Kisha kuna mfano uliopigwa kuwaelezea makafiri wafanyao ibada na kudhani kuwa wataambulia kitu kumbe hawana lolote. Hawa wana ujinga uliokithiri. Kama Allah تعالی Alivyosema,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُمْ كَسْرَابٍ بِقَيْعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْثَانُ مَاءً حَتَّى إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ

شَيْئًا

“Wale waliokufuru, vitendo vyao (wanavyoviona vizuri) ni kama mazigazi (mangati-sura ya maji) jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji, akiyaendea haoni chochote (na wao watakapoziendea amali zao siku ya Kiyama. Hawatapata chochote kwani waliupinga Uislamu, na hali ya kuwa wanajua kuwa ndio Dini ya haki).” (24:39)

¹ Al-Hakim 2:495.

Kisha Allah تعالى Akapiga mfano wa Makafiri wajinga, ambao Amewazungumzia kwa Kusema;

أَوْ كَظَلَّمْتِ فِي بَحْرِ لُجِّي يَغْشَاهُ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ سَحَابٌ ظَلَمْتِ
بَعْضُهَا فَوْقَ بَعْضٍ إِذَا أَخْرَجَ يَدَهُ لَمْ يَكِدْ يَرْنَهَا وَمَنْ لَمْ يَجْعَلِ اللَّهُ لَهُ نُورًا فَمَا
لَهُ مِنْ نُورٍ ﴿٤٠﴾

“Au (amali zao zile mbaya) ni kama giza katika bahari kuu, iliyofunikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia asiuone (kwa kiza kilivyoshitadi); na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru.” (24:40)

Kwa hiyo, Allah تعالى Aliigawa kambi ya Makafiri katika makundi mawili, watetezi na wafuasi. Allah تعالى Ameyataja makundi mawili haya; watetezi na wafuasi mwanzoni mwa Surat Al-Hajj.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ ﴿٣﴾

“Na katika watu wako wanaobishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo elimu, na wanamfuata kila shetani asi.” (22:3)

Na Amesema;

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّنبِئٍ ﴿٨﴾

“Na katika watu wako wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila elimu wala muongozo wala Kitabu chenye nuru.” (22:8)

Zaidi ya hivyo, Allah تعالى Ameligawa kundi la Waislamu mwanzoni mwa Surat Al-Waqiah (56) na mwishoni. Halikadhalika Ameyagawa katika Surat Al-Insan (76) katika makundi mawili, Sabiqun (wale waliotangulia), ndio walio karibu (Muqaribun) na As-hab Al-Yamin (masahiba wa ukweli) na ni watenda mema (Abrar). Kwa Muhtasari, Aya hizi zinawagawa Waislam katika makundi mawili, walio karibu na walio na uadilifu. Pia Makafiri wako makundi mawili, watetezi na wafuasi. Kwa nyongeza, Wanafiki wamegawika katika makundi mawili,

Wanafiki halisi na wenye unafiki kiasi. Sahih mbili zimepokea kuwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«ثَلَاثٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ كَانَ مُنَافِقًا خَالِصًا، وَمَنْ كَانَتْ فِيهِ وَاجِدَةٌ مِنْهُنَّ كَانَتْ فِيهِ خُصْلَةً
مِنَ النِّفَاقِ حَتَّى يَدْعَهَا: مَنْ إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اتَّخَذَ خَانَ»

“Matatu yanapokuwa ndani ya mtu, atakuwa mnafiki halisi. Na atakayekuwa na moja katika sifa tatu hizo atakuwa na sehemu ya unafiki mpaka atakapoiacha. Anapozungumza, husema uongo. Anapoweka ahadi, huvunja. Anapoaminiwa, huvunja uaminifu.”¹

Hivyo mtu anaweza kuwa na vyote; sehemu ya imani na sehemu ya unafiki, ima kwa vitendo, kama Hadithi hii inavyoelezea, au unafiki wa kiitikadi kama Aya ya (2:20) Inavyoeleza.

Aina za Nyoyo.

Imam Ahmad amerikodi kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْقُلُوبُ أَرْبَعَةٌ: قَلْبٌ أَجْرَدٌ فِيهِ مِثْلُ السَّرَاجِ يَزْهُرُ وَقَلْبٌ أَغْلَفٌ مَرْبُوطٌ عَلَى غِيَلِهِ
وَقَلْبٌ مَنكُوسٌ وَقَلْبٌ مُضْفَعٌ، فَأَمَّا الْقَلْبُ الْأَجْرَدُ فَقَلْبُ الْمُؤْمِنِ فَيَسْرَاجُهُ فِيهِ نُورُهُ،
وَأَمَّا الْقَلْبُ الْأَغْلَفُ فَقَلْبُ الْكَافِرِ، وَأَمَّا الْقَلْبُ الْمَنكُوسُ فَقَلْبُ الْمُنَافِقِ الْخَالِصِ
عَرَفَ نَمَّ أَنْكَرَ وَأَمَّا الْقَلْبُ الْمُضْفَعُ فَقَلْبٌ فِيهِ إِيْمَانٌ وَنِفَاقٌ وَمِثْلُ الْإِيْمَانِ فِيهِ كَمَثَلِ
الْبُتْلَةِ يَمُدُّهَا الْمَاءُ الطَّيِّبُ وَمِثْلُ النِّفَاقِ فِيهِ كَمَثَلِ الْقُرْحَةِ يَمُدُّهَا النِّعِجُ وَالِدَّمُ فَأَيُّ
الْمَادَّتَيْنِ غَلَبَتْ عَلَى الْأُخْرَى غَلَبَتْ عَلَيْهِ»

“Nyoyo ni aina nne: Moyo uliong’arishwa na kung’aa kama taa yenye mwanga unaonururisha, moyo uliofungwa kwa fundo lililofungwa kuzunguka lakiri, moyo uliogezwa juu – chini na moyo uliozingwa. Ama kuhusu moyo uliong’arishwa, ni moyo wa Muumini na taa yake ni nuru ya imani. Na moyo uliopigwa muhuri ni moyo wa Kafiri. Na moyo uliogezwa juu – chini ni moyo wa Mnafiki halisi, kwa sababu amefahamu lakini akakanusha. Ama moyo uliozingwa, ni moyo

¹ Fat’hul Al-Bari 1:111, Muslim 1:78.

ambao una imani na unafiki. Mfano wa imani katika moyo huu, ni mfano wa mmea ulioendelezwa na maji safi. Mfano wa unafiki ndani yake, ni mfano wa donda linalostawi ndani ya mishipa na damu. Itategemea kitu gani kati ya viwili hivyo 'kitashinda', pia kitatawala katika moyo huo." Hadithi hii ina daraja la Jaiyyid Hasan katika Isnadi ya upokezi.¹

Allah تعالیٰ Amesema,

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ^٤ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu Angependa Angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uwezo juu ya kila kitu.”

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالیٰ aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَذَهَبَ بِسَمْعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ^٤

“Na Mwenyezi Mungu Angependa Angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao.”

Kwa kusema kwa sababu waliitelekeza kweli baada ya kufahamu.

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”

Ibn Is-haq رحمه الله تعالیٰ alisema, “Allah تعالیٰ Ana Uwezo wa Kuadhibu au Kusamehe waja Wake kama Apendavyo.”² Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ alitolea maelezo, “Allah تعالیٰ Amejielezea Mwenyewe kuwa Ana Uwezo wa kufanya jambo lolote kwa sababu Ametahadharisha ubaya wa unafiki na adhabu yake. Pia Amewajulisha Wanafiki kwamba Yeye Anawajua vyema. Tena Amewajulisha kuhusu Uwezo Wake wa Kuwaondolea kusikia na kuona kwao.”³ Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ na wanazuoni kadha wa *Tafsir* wameeleza kuwa mifano hii miwili inahusu aina moja ya Wanafiki. Hivyo neno ‘au’ lililotajwa katika,

¹ Ahmad 3:17.

² Ibn Abu Hatim 1:76.

³ At-Tabari 1:361.

أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ السَّمَاءِ

“Au (mfano wao pia) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni...”

Tamko ‘au’ katika Aya lina maana ya ‘na’ kama ilivyotumika katika Aya nyingine,

وَلَا تُطِيعُ مِنْهُمْ عَائِمًا أَوْ كَفُورًا ﴿٢٤﴾

“Na usimtii mfanya dhambi au kafiri miongoni mwao.” (76:24).

Kwa hiyo ‘au’ kwenye Aya inaonesha hiyari ya kutumia mfano mmoja wapo katika mifano miwili. Pia Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema ‘au’ maana yake, “Kuonesha kuwa mojawapo ni sawa na nyingine, kama mtu akisema, “Kaa na Al-Hasan au Ibn Sirin.” Kwa mujibu wa mtazamo wa Az-Zamakhshari رحمه الله تعالى, ina maana kila mmoja kati ya watu hawa ni sawa na mwingine, hivyo unaweza kukaa na mmoja wao. Kwa hiyo maana ya ‘au’ inakuwa ‘yeyote’. Allah تعالى Alitoa mifano hii miwili ya Wanafiki, kwa sababu yote inawaelezea vizuri. Mimi (Ibn Kathir) nasema, maelezo haya yanahusiana na aina mahsusi ya Mnafiki, kwa sababu kuna tofauti kati yao kama tulivyoeleza. Kwa mfano, Allah تعالى Alizitaja aina hizo katika Surat Tawbah (Surah ya 9) Aliporudia Kauli, **“Na miongoni mwao”** mara tatu, akielezea aina zao, sifa bainifu, kauli na vitendo. Hivyo mifano miwili iliyotajwa hapa inaelezea aina mbili za Wanafiki ambao sifa zao zinafanana, Mathalan, Allah تعالى Alitoa mifano katika Surat An-Nur, moja kwa watetezi wa imani na moja kwa wafuasi wa kufuru. Alisema,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُمْ كَسْرَابٍ بِقَيْعَةٍ

“Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani.”
(24:39). Mpaka,

أَوْ كَطَّلُمْتِ فِي بَحْرٍ لُّجِّيٍّ

“Au (amali zao zile mbaya) ni kama giza katika bahari yenye maji mengi.” (24:40)

Mfano wa kwanza ni wa watetezi wa kufuru ambao wana ujinga wenye mchangamano, ambapo wa pili ni juu ya wafuasi ambao wana ujinga mwepesi. Allah تعالى Anajua zaidi.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَعْبُدُوا رَبَّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢١﴾ الَّذِي
 جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ
 رِزْقًا لَكُمْ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أُندَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

21. "Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Ambaye Amekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu; ili mpate kuokoka."

22. "(Mwenyezi Mungu) Ambaye Amekufanyieni hii ardhi kuwa kama busati (mliotandikiwa mstarehe), na mbingu kuwa kama paa, na Akateremsha maji kutoka mawinguni; na kwa hayo Akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua (kuwa hana mshirika)."

Tawhid Al-Uluhiyyah.

Allah تعالى Ametaja Upweke Wake katika Uungu na Akaeleza kuwa Amewafanyia Fadhila Waja Wake Kuwapa uhai wakati hawakuwepo. Pia Amewazingira kwa Rehema zilizo wazi na zilizo jificha. Na Akaifanya dunia mahali pao pa kupumzika, kama kitanda, na ipo madhubuti na yenye milima imara.

وَالسَّمَاءَ بِنَاءً

"Na mbingu kuwa kama paa."

Maana yake: 'Dari'. Hivyo hivyo, Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَحْفُوظًا وَهُمْ عَنْ آيَاتِهَا مُعْرَضُونَ ﴿٢١﴾

"Na Tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa, lakini wanazikengeuka ishara Zake (Mwenyezi Mungu)." (21:32)

وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ

"Na Akakuteremshieni maji kutoka mawinguni..." (27:60).

Ikiwa na maana kupitia mawingu, wakati wanapotaka mvua. Hivyo Allah تعالى Akasababisha mimea anuwai na matunda kumea kama njia ya kuwafanya

binadamu na mifugo yao ili waweze kuishi. Allah تعالی Amerejea Kuitaja zawadi hii katika sehemu mbalimbali za Qur'an.

Kuna Aya nyingine inayofanana na Aya (2:22), ni kuwa Kauli ya Allah تعالی,

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ
وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٢﴾

“Mwenyezi Mungu ni yule Aliyekufanyieni ardhi kuwa mahali penu pa kukaa, na mbingu kuwa dari (isiyoanguka); na Akakutieni sura na Akazifanya nzuri sura zenu na Akakuruzukuni vitu vizuri. Huyo Ndiye Mungu, Mola wenu. Basi Mwenye Baraka zote hizi ni Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.” (40:64)

Maana yake: Ni kuwa Allah تعالی ni Muumbaji, Mtoaji Riziki, Mmiliki wa Ulimwengu wote na vilivyomo ndani yake. Naye Ndiye Mpaji riziki wao. Hivyo, Yeye Peke Yake Ndiye Anayestahiki Kuabudiwa, hapana yeyote wala chochote kinachofaa kushirikishwa Naye.

Ndio sababu Allah تعالی Alisema,

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أُندَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

“Basi msimfanyie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua (kuwa hana mshirika).” (2:22)

Sahihi mbili zimeandika kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Nilimuuliza Mtume ﷺ, “Ni kitendo gani kiovu kabisa mbele ya Allah تعالی?’ Akasema,

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدًّا وَهُوَ خَلَقَكَ»

“Kumchukulia Allah kwamba Ana mwenza, wakati Yeye Peke Yake Alikuumba.”¹

Aidha, Muadh رضي الله عنه alisimulia kauli ya Mtume ﷺ,

¹ Fat'hul Al-Bari 8:350 na Muslim 1:90.

«أَتَدْرِي مَا حَقُّ اللَّهِ عَلَى عِبَادِهِ؟ أَنْ يَعْبُدُوهُ وَلَا يُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا»

“Unajua haki ya Allah kwa waja Wake? Ni kumuabudu Yeye wala wasimshirikishe na kitu chochote.”¹

Hadithi nyingine inasema,

«لَا يَقُولَنَّ أَحَدُكُمْ مَا شَاءَ اللَّهُ وَشَاءَ فُلَانٌ، وَلَكِنْ لِيَقُلْ: مَا شَاءَ اللَّهُ ثُمَّ شَاءَ فُلَانٌ»

“Asiseme mmoja wenu, “Apendacho Allah na fulani bali aseme, “Apendacho Allah na kisha atakacho fulani.”¹

Hadithi Yenye Maana Sawa.

Imam Ahmad alisimulia kuwa Al-Harith Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ أَمَرَ يَحْيَى بْنَ زَكَرِيَّا عَلَيْهِ السَّلَامُ بِخَمْسِ كَلِمَاتٍ أَنْ يَعْمَلَ بِهِنَّ، وَأَنْ يَأْمُرَ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنْ يَعْمَلُوا بِهِنَّ وَأَنَّهُ كَادَ أَنْ يُنْطَىءَ بِهَا، فَقَالَ لَهُ عِيسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ: إِنَّكَ قَدْ أَمَرْتَ بِخَمْسِ كَلِمَاتٍ أَنْ تَعْمَلَ بِهِنَّ وَتَأْمُرَ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنْ يَعْمَلُوا بِهِنَّ فِيمَا أَنْ تُبَلِّغَهُمْ وَإِنَّمَا أَنْ أُبَلِّغَهُنَّ، فَقَالَ: يَا أَحْسَى إِنِّي أَخَشَى أَنْ سَبَقْتَنِي أَنْ أُعَذِّبَ أَوْ يُخَسَفَ بِي قَالَ: فَجَمَعَ يَحْيَى بْنُ زَكَرِيَّا بَنِي إِسْرَائِيلَ فِي بَيْتِ الْمَقْدِسِ حَتَّى امْتَلَأَ الْمَسْجِدَ، فَقَعَدَ عَلَى الشَّرَفِ فَحَمِدَ اللَّهَ وَأَثْنَى عَلَيْهِ ثُمَّ قَالَ: إِنَّ اللَّهَ أَمَرَنِي بِخَمْسِ كَلِمَاتٍ أَنْ أَعْمَلَ بِهِنَّ وَأَمُرَّكُمْ أَنْ تَعْمَلُوا بِهِنَّ أَوْ لَهُنَّ: أَنْ تَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا، فَإِنَّ مَثَلَ ذَلِكَ كَمَثَلِ رَجُلٍ اشْتَرَى عَبْدًا مِنْ خَالِصِ مَالِهِ بِوَرِيٍّ أَوْ ذَهَبٍ فَجَعَلَ يَعْمَلُ وَيُؤَدِّي غَلَّتُهُ إِلَى غَيْرِ سَيِّدِهِ، فَأَيُّكُمْ بِسُرِّهِ أَنْ يَكُونَ عَبْدُهُ كَذَلِكَ، وَإِنَّ اللَّهَ خَلَقَكُمْ وَرَزَقَكُمْ فَأَعْبُدُوهُ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا. وَأَمُرَّكُمْ بِالصَّلَاةِ فَإِنَّ اللَّهَ يَنْصِبُ وَجْهَهُ لِرُجُوهِ عَبْدِهِ مَا لَمْ يَلْتَفِتْ فَإِذَا صَلَّى لَكُمْ فَلَا تَلْتَفِتُوا. وَأَمُرَّكُمْ بِالصِّيَامِ فَإِنَّ مَثَلَ ذَلِكَ كَمَثَلِ رَجُلٍ مَعَهُ صُرَّةٌ مِنْ مِسْكِ فِي عِصَابَةٍ كُلُّهُمْ يَجِدُ رِيحَ الْمِسْكِ وَإِنْ خَلُوفَ نَمِ الصَّائِمِ أَطْيَبَ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ رِيحِ الْمِسْكِ. وَأَمُرَّكُمْ بِالصَّدَقَةِ

¹ Fat'hul Al-Bari 13:350 na Muslim 1:59

² Ahmad 5:384, 394, 398.

فَإِنَّ مَثَلَ ذَلِكَ كَمَثَلِ رَجُلٍ أَسْرَهُ الْعَدُوُّ فَشَدُّوا يَدَيْهِ إِلَىٰ عُنُقِهِ وَقَدَّمُوهُ لِيَضْرِبُوا عُنُقَهُ فَقَالَ لَهُمْ: هَلْ لَكُمْ أَنْ أَتَيْتَنِي نَفْسِي مِنْكُمْ فَجَعَلْتُ بِتَيْدِي نَفْسَهُ مِنْهُمْ بِالْقَلِيلِ وَالكَثِيرِ حَتَّىٰ فَكَّ نَفْسَهُ. وَأَمْرُكُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ كَثِيرٌ وَإِنَّ مَثَلَ ذَلِكَ كَمَثَلِ رَجُلٍ طَلَبَهُ الْعَدُوُّ سِرَاعًا فِي أَثَرِهِ فَأَتَىٰ حِصْنًا حَصِينًا فَتَحَصَّنَ فِيهِ وَإِنَّ الْعَبْدَ أَحْصَنَ مَا يَكُونُ مِنَ الشَّيْطَانِ إِذَا كَانَ فِي ذِكْرِ اللَّهِ

“Allah Alimuamrisha Yahya bin Zakariya kutekeleza amri tano na kuwaamrisha Wana wa Israel kuzitekeleza, lakini Yahya alikuwa mzito kuzitekeleza amri hizo. Isa akamuambia Yahya, “Uliamrisha kutekeleza amri tano na kuwaamrisha Wana wa Israeli kuzitekeleza. Hivyo ama wafikishie vinginevyo nitawafikishia mimi!” Yahya akasema, “Ndugu yangu! Nachelea kama utafanya kabla yangu, nitaadhibiwa au ardhi itatikisika chini ya nyayo zangu!” Hivyo, Yahya bin Zakariya aliwaita Wana wa Israeli kuja Bayt Al-Maqdis (Jerusalem) mpaka Msikiti ukajaa. Alikaa kwenye kibaraza, alimshukuru Allah na akasema, “Allah Aliniamrisha amri tano nizitekeleze na nikuamrisheni mshikamane nazo. Ya kwanza ni kuwa Mumuabudu Allah Peke Yake na msimshirikishe Yeye na yeyote. Mfano wa amri hii ni mfano wa mtu aliyemnunua mtumwa kwa mali zake, fedha au dhahabu. Mtumwa akaanza kumtumikia bwana mwingine. Nani miongoni mwenu angependa mtumwa wake afanye hivyo? Allah Alikuumbeni nyinyi na Kukulisheni. Hivyo muabuduni Yeye Peke Yake na msimshirikishe Yeye na chochote. Pia nawaamrisha kusali, kwa kuwa Allah Anauelekeza Uso Wake kwa uso wa Mja Wake, pindi mja huyo asipogeza uso wake. Hivyo mnaposali, msigeuze nyuso zenu mbele na nyuma. Pia nakuamrisheni kufunga, mfano wake (mwenye kufunga) ni mfano wa mtu katika kundi la watu na ana miski iliyofungiwa katika kipande cha nguo, na hivyo watu wote wanasikia harufu ya miski hiyo. Kwa hakika harufu itokayo kinywani mwa mfungaji ni bora mbele ya Allah kuliko harufu ya Miski. Pia ninawaamrisha kutoa Zaka, mfano (wa mtoaji Zaka) wa hili ni mfano wa mtu aliyeshikwa na adui wakamfunga mikono yake kwenye shingo yake na wakamleta mbele kumkata shingo yake. Akawaambia, “Je, ninaweza kujilipia fidia?”

Akawa analipa Fidia kidogo na kingi mpaka akajikomboa. Pia ninawaamrisha kumtaja Allah wakati wote; mfano wa amali hii ni mfano wa mtu anayefuatwa na adui wakati wote, anajificha katika ngome imara. Mja anapomkumbuka Allah, atakuwa amechagua mahali pa kujikinga dhidi ya shetani."

Al-Harith رضي الله عنه kisha alisimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«وَأَنَا أَمْرُكُمْ بِحَمْسِ اللَّهِ أَمْرِي بِهِنَّ: الْجَمَاعَةِ وَالسَّنْعِ وَالطَّاعَةِ وَالْهِجْرَةِ وَالْجِهَادِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ. فَإِنَّهُ مَنْ خَرَجَ مِنَ الْجَمَاعَةِ قِيدَ شِبْرٍ فَقَدْ خَلَعَ رَبَّنَةَ الْإِسْلَامِ مِنْ عُنُقِهِ إِلَّا أَنْ يُرَاجِعَ وَمَنْ دَعَا بِدَعْوَى جَاهِلِيَّةٍ فَهُوَ مِنْ جُنَى جَهَنَّمَ» قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ وَإِنْ صَامَ وَصَلَّى؟ فَقَالَ: «وَإِنْ صَلَّى وَصَامَ وَرَزَعَمَ أَنَّهُ مُسْلِمٌ، فَادْعُوا الْمُسْلِمِينَ بِأَسْمَائِهِمْ عَلَى مَا سَمَّاهُمْ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ الْمُسْلِمِينَ الْمُؤْمِنِينَ عِبَادَ اللَّهِ»

"Nami nakuamrisheni amri tano ambazo Allah Kaniamrisha nishikamane nazo, Ameamrisha kushikamana katika jamaah (jamii ya Waumini), usikivu na utiifu (kwa viongozi) na Hijrah (kuhama) na kupigana Jihad kwa ajili ya Allah. Yeyote anayeacha Jamaah, japo umbali wa shubiri moja, atakuwa ameondoa tai ya Uislamu kwenye shingo yake, isipokuwa arejee. Yeyote anayetumia kauli mbiu ya Jahiliyah (kabla ya Uislamu) atakuwa miongoni mwa wale wanaopiga magoti Jahannam." Wakasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Hata kama anasali na kufunga?" Akajibu, "Hata kama anasali na kufunga na kudai kuwa ni Muislamu. Hivyo waite Waislam kwa majina yao aliyowaita Allah: "Waislam, Waumini, Waja wa Allah."¹

Hadithi hii ni *Hasan*, na ina kauli mbiu, "Allah تعالى Amewaumba na Anawalisheni, hivyo muabuduni Yeye na msimshirikishe na chochote katika kumuabudu".

Kauli mbiu hii inapatikana katika Aya (2:21-22) tunayojadili hapa na inakubaliana na Kumpwekesha Allah تعالى katika ibada bila washirika.

¹ Ahmad 4:130.

Dalili za Kuwepo Allah تعالیٰ.

Wanazuoni kadha wa *Tafsir*, kama Ar-Razi رحمه الله تعالیٰ na wengine, walizitumia Aya hizi kama moja ya kuwepo kwa Muumba, na ni njia sahihi kabisa ya hoja. Kwa hakika, mtu anapotafakari juu ya vitu vinavyoishi, viumbe wa juu na chini, sura zao anuai, rangi, tabia, faida na majukumu yao ya kiekolojia, hapo atatambua Uwezo, Hekima, Maarifa, Ukamilifu na Utukufu wa Muumba wao. Siku moja bedui aliulizwa juu ya ushahidi wa kuwepo Allah تعالیٰ, alijibu, “Shukrani zote zinamstahikia Allah تعالیٰ! Kinyesi cha ngamia kinathibitisha kuwepo kwa ngamia na alama za nyayo zinaonesha kuwa anayeenda, na ardhi yenye milima na mabonde na bahari zenye mawimbi, vyote hivi ni uthibitisho wa kuwepo Mwenye Huruma, Mpole na Mjuzi wa kila kitu.”¹

Hivyo, yeyote anayeangalia mbinguni kwa ukubwa wake, kuenea kwake, ataona sayari kubwa na ndogo zilizomo ndani yake, baadhi yake zinaonekana zimetulia angani, yeyote anayeangalia bahari ambazo zimezunguka ardhi kutoka pande zote, na milima iliyowekwa juu ya ardhi kuiimarisha, ili viumbe wanaoishi juu ya ardhi, wakiwa na maumbile na rangi za aina mbalimbali, waweze kuishi na kutononoka, ataona Uwepo wa Allah تعالیٰ. Yeyote anayesoma Kauli ya Allah,

وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌ بَيضٌ وَحُمْرٌ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ ﴿٢٧﴾ وَمِنَ النَّاسِ
وَالدَّوَابِّ وَالْأَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ كَذَلِكَ ۗ إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ۗ

“Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbalimbali, na (mengine) myeusi sana. Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni mbalimbali. Kwa hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanazuoni).” (35:27-28)

Yeyote anayefikiri kuhusu mito inayosafiri kutoka eneo moja kwenda jengine ikileta manufaa, mtu yeyote anayetafakari jinsi Allah تعالیٰ Alivyoviumba juu ya ardhi, wanyama tofauti na mimea yenye ladha tofauti, harufu, maumbile na rangi ambayo ni matokeo ya muungano kati ya ardhi na maji, yeyote

¹ Ar-Razi 2:91.

anayetafakari yote haya, atatanabahi kuwa ukweli huu unathibisha kuwepo kwa Muumba, Uwezo Wake uliotimia, Hekima, Huruma, Upole, Ukaramu na Mwingi wa Kurehemu waja Wake. Hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, wala hapana Bwana asiyekuwa Yeye na Kwake tunakimbilia kutubia. Zipo Aya nyingi za Qur'an kuhusu mada hii.

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِمَّنْ دُونِ اللَّهِ إِنَّ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٣﴾ فَإِنْ لَمْ تَفْعَلُوا وَلَنْ تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿٢٤﴾

23. "Na ikiwa (Mapagani, Mayahudi na Wakristo) mna shaka kwa hayo Tuliyoumteremshia mtumwa Wetu (Muhammad) (kuwa hakuteremshiwa na Mwenyezi Mungu), basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake, na muwaite waungu wenu bighairi ya Mwenyezi Mungu (wakusaidieni); ikiwa mnasema kweli."

24. "Na Msipofanya – na hakika hamtafanya kamwe – basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, umewekewa makafiri."

Kuthibitisha Ujumbe wa Mtume ﷺ ni wa Kweli.

Allah تعالی Anaanza kuthibitisha ukweli wa utume baada ya Kueleza kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye. Allah تعالی Aliwaambia Makafiri,

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا

"Na ikiwa (Mapagani, Mayahudi na Wakristo) mna shaka kwa hayo Tuliyoumteremshia (Qur'an) mtumwa Wetu..."

Ikiwa na maana ya Muhammad ﷺ.

فَأْتُوا بِسُورَةٍ

"Basi leteni sura moja."

Maana yake: Mithili ya aliyowaitea. Hivyo, endapo mnadai kuwa alichoteremshiwa hakikutoka kwa Allah تعالى, basi leteni kitu mfano wa kile alichokuleteeni, kwa kutumia msaada wa yeyote asiyekuwa Allah تعالى. Hamtofanikiwa hilo. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

شُهِدَ آءُكُمْ

“Waungu wenu.”

Ikiwa na maana: “Wasaidizi.”¹ Pia As-Suddi ameripoti kuwa Abu Malik alisema Aya hii, “Washirika wenu...” Maana yake: Watu wengine wa kumsaidia katika hilo. Ina maana kisha waende kutafuta msaada kutoka kwa waungu wao ili wawaunge mkono na kukusaidieni.² Aidha Mujahid alisema kuwa,

وَأَدْعُوا شُهِدَ آءُكُمْ

“...na muwaite waungu wenu.”

Maana yake: “Watu, wenye busara, werevu na wambuji ambao watatoa ushahidi wa hilo.”³

Changamoto na Kutoigika kwa Qur’an

Allah تعالى Anawapa changamoto Makafiri katika sehemu mbalimbali ndani ya Qur’an, kuwa wao hawawezi kuiga Qur’an abadani. Mathalan, Allah تعالى Alisema katika *Surat al-Qasas* (28:49).

قُلْ فَأَتُوا بِكِتَابٍ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَا أَتَّبِعُهُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٩﴾

“Sema (kwao, Ewe Muhammad), “Basi leteni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu ambacho kina uongofu ulio bora kuliko hivi viwili (Taurati ya Nabii Musa na hii Qur’an) ili nikifuate kama nyinyi mnasema kweli.”

Pia Allah تعالى Amesema katika *Surat Al-Isra* (17:88),

¹ At-Tabari 1:376.

² Ibn Abu Hatim 1:84.

³ Ibn Abii Hatim 1:85.

قُلْ لِيْنَ أَجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَيَّ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ
كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيراً ﴿١٧﴾

“Hata wakajikusanya watu (wote) na majini ili kuleta mfano wa hii Qur’an basi hawangaliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao.”

Allah تعالى Amesema katika Surat Hud (11:13),

أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرَنَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِثْلِهِ مُفْتَرِيْنَ وَأَدْعُوا مَنْ أَسْتَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ
اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿١٤﴾

“Ndivyo kweli wanasema kuwa, “Amekitunga mwenyewe (Muhammad kitabu hiki)?” Sema: “Basi leteni sura kumi za uongo zilizotungwa mfano wa hii, na waiteni muwezao (kuwaita) badala ya Mwenyezi Mungu (waje wakusaidieni kutunga hivyo) ikiwa mnasema ukweli.”

Na katika Surat Yunus (10:37-38), Allah تعالى Amesema,

وَمَا كَانَ هَذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَى مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ
وَتَفْصِيْلَ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيْهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ ﴿٣٧﴾ أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرَنَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِسُوْرَةٍ
مِثْلِهِ وَأَدْعُوا مَنْ أَسْتَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿٣٨﴾

“Na haiwezekani kuwa Qur’an hii: imetungwa, haitokani na Mwenyezi Mungu (kama mnavyodai). Bali (imetokana na Mwenyezi Mungu), inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelekezo ya Vitabu (vilivyopita). Haina shaka kuwa imetoka kwa Mola wa walimwengu (wote).” “Je! Ndiyo wanasema: (Muhammad) ameitunga?’ Sema: “Hebu (tungeni na nyie) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje) – isipokuwa Mwenyezi Mungu – (wa kuwasaidieni) kama nyie mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad).”

Aya zote hizi ziliteremshwa Makkah. Allah تعالى pia Aliwapa changamoto Makafiri ya kuiiga Qur'an katika Aya zilizoshuka Madina, katika Aya hii, Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ

“Na ikiwa (Waarabu Mapagani, Mayahudi na Wakristo) mna Rayb.” Maana: Shaka,

مِمَّا تَزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا

“Katika Tuliyomteremshia mtumwa Wetu.” Maana: Muhammad ﷺ.

فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّمَّنْ مِثْلِهِ

“Basi leteni sura moja mfano wake.” Maana: Sawa na Qur'an. Hii ni *Tafsir* ya Mujahid, Qatadah, Ibn Jarir At-Tabari, Az-Zamakhshari na Ar-Razi. Ar-Razi amesema hii ni *Tafsir* ya Umar, Ibn Mas'ud, Ibn Abbas, al-Hasan al-Basri na wanazuoni wengi. Na aliupa kipaumbele mtazamo huu na akataja kuwa Allah Aliwapa changamoto Makafiri mmoja mmoja na kwa kundi, bila kujali kuwa wana elimu au hawana, hivyo kuifanya changamoto kamili. Aina hii ya changamoto ni ya ujasiri mkubwa kuliko kutoa tu changamoto kwa Makafiri mambumbumbu ambao hawana elimu. Ndiyo sababu Akasema,

فَأْتُوا بِعَشْرِ سُورٍ مِثْلِهِ

“Basi leteni sura kumi (za uongo zilizotungwa) mfano wa hii.” (11:13). Na,

لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ

“...hawangaliweza kuleta mfano wake.” (17:88).

Kwa hiyo, hii ni changamoto kwa Makafiri wa Kiarabu, wenye umbuji wa lugha kuliko mataifa yote. Allah تعالى Amewapa changamoto Makafiri wa Kiarabu kote Makkah na Al-Madina mara nyingi, hususan walivyokuwa na chuki kuu na uadui dhidi ya Mtume na Uislamu. Pamoja na hayo walishindwa kukabiliana na changamoto hiyo, na ndio sababu Allah تعالى Akasema,

فَإِنْ لَّمْ تَفْعَلُوا وَلَنْ تَفْعَلُوا

“Na Msipofanya – na hakika hamtafanya kamwe.” Akionesha kuwa hawatoweza kuzijibu changamoto hizo. Huu ni muujiza mwingine katika hilo, Allah تعالى Ameeleza wazi tena kwa uhakika kuwa Qur'an hakuna wa kuiiga na

kuileta mfano wake, tokea zama hizo mpaka dahari. Hii ni kauli sahihi ambayo haijabadilika mpaka zama za leo na haitobadilika abadani. Inawezekanaje mtu akaleta mfano wa Qur'an, wakati Qur'an ni Neno la Allah تعالی Ambaye Ameumba kila kitu? Itawezekanaje maneno ya kiumbe yakawa sawa na Maneno ya Muumbaji?

Mifano ya Miujiza ya Qur'an.

Yeyote anayesoma Qur'an atatambua kuwa ina ubora wa daraja mbalimbali na yenye maana zilizo dhahiri na zilizo jificha inazozitaja. Allah تعالی Amesema,

الرَّكَّبُ أَحْكَمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ ﴿١١﴾

“Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu ambacho aya Zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye Hekima na Mwenye Ujuzi wa kila kitu.” (11:1)

Hivyo upambanuzi katika Qur'an ni kamilifu na maana zake zimeelezwa. Zaidi ya hivyo kila neno na maana yake katika Qur'an yana umbuji na hayawezi kupikwa. Qur'an pia inataja Hadithi za watu waliopita, na matukio ya simulizi hizo yanakuwa vile vile kama Qur'an ilivyotaja. Aidha Qur'an iliamrisha kila jambo la uadilifu na ikakataza kila aina ya upofu, kama Allah تعالی Alivyosema,

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola Wako, kwa ukweli na uadilifu...”. (6:115).

Maana yake: Habari zake na Sharia zake ni za kweli. Qur'an ni ya kweli, ya haki na iliyojaa uongofu. Haina mambo yaliyotiwa chumvi, uongo au upotoshaji, kinyume na washairi wa Kiarabu na wengineo ambao tungo zao hujaa uongo na upotoshaji, kama shairi moja lilivyoeleza, “Hotuba yenye umbuji wa hali ya juu ni ile yenye uongo mwingi.” Wakati mwingine utakuta utenzi mrefu ambao kwa kiasi kikubwa unaelezea wanawake, farasi au pombe, au utenzi utakuwa na wasifu au maelezo kuhusu mtu fulani, farasi, ngamia, vita, tukio, woga, mnyama mkali au vitu vingine. Sifa au maelezo hayo hayaleti faida yoyote, bali yanatoa mwanga juu ya uwezo wa mshairi na umbuji wake katika kuelezea vitu mbalimbali. Pamoja na hayo utakuta ubeti mmoja au miwili katika mashairi marefu yanayofanua kiini cha shairi, wakati shairi lililobaki lina maelezo yasiyo na umuhimu, pia kunakuwa na mambo yanayojirudiarudia.

Ama Qur'an yote ina umbuji katika hali iliyo sahihi, kama wale wenye maarifa juu ya mambo fulani na wanaelewa njia za mazungumzo ya maneno ya lugha ya Kiarabu kuwa vinawiana. Mmoja anaposoma habari fulani ndani ya Qur'an, ataona kuwa zina faida, ama ni ndefu au fupi, zimerudiwa au hazikurudiwa. Jinsi hadithi hizo zinaporudiwa basi faida huongezeka na uzuri wake kuzidi. Qur'an haiwi ya kale mtu anaporudia kuisoma, wala wanazuoni hawajachoshwa nayo. Qur'an inapotaja mada ya kuonya na kutoa ahadi, inawasilisha ukweli ambao utaifanya milima isiyumbe, sasa vipi kuhusu mioyo iliyoelewa na inayozingatia? Qur'an inapoahidi, inafungua mioyo na masikio, inawafanya watu kuwa na ghera ya kupata amani – Pepo na kuwa majirani na Ufalme wa Mwingi wa Kurehemu. Kwa suala la kushajiisha, Qur'an inasema,

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

“Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko peponi): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.” (32:17). Aidha Amesema,

وَفِيهَا مَا تَشْتَهِيهِ الْأَنْفُسُ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ۗ وَأَنْتُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٧١﴾

“...Na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele.” (43:71)

Katika somo la kuonya na kutoa vitisho,

أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ تَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ

“Je, mumejaminisha ya kuwa (Mungu) Hatokudidimizeni upande wowote wa nchi kavu...” (17:68) na,

ءَأَمِنْتُمْ مَّن فِي السَّمَاءِ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ ﴿١٨﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ مَّن فِي

السَّمَاءِ أَنْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ ﴿١٩﴾

“Je, Mnadhani mko salama kwa (Mwenyezi Mungu) Ambaye Yuko Mbinguni (Ufalme Wake Mkubwa) ya kuwa Yeye Hatakididimizeni ardhini, tahamaki hiyo inataharaki (na nyinyi, inakudidimizeni ardhini, kama walivyodidimizwa hao wa zamani)? Au mnadhani

(Ufalme Wake Mkubwa), ya kuwa Yeye Hatakuleteeni kimbunga chenye changarawe (zikauangamizeni changarawe hizo)? Mtajua vipi maonyo Yangu.” (67:16-17)

Kuhusu somo la kuonya, Qur'an imesema,

فَكَلَّا أَخَذْنَا بِذُنُوبِهِمْ

“Basi kila mmoja Tulimtesa kwa sababu ya dhambi zake...” (29:40). Pia juu ya nasaha, Qur'an imesema,

أَفَرَأَيْتَ إِنْ مَتَّعْنَاهُمْ سِنِينَ ﴿٢٦﴾ ثُمَّ جَاءَهُمْ مَا كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٢٧﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ
مَا كَانُوا يُمْتَعُونَ ﴿٢٨﴾

“Unaonaje kama Tukiwastarehesha kwa miaka. Kisha iwafike (adhabu) waliyokuwa wakiahidiwa? Yatawafaa nini yale waliyostareheshewa?” (26:205-207).

Kuna mifano mingine mingi ya umbuji, balagha na manufaa ya Qur'an. Qur'an inapojadili Sharia, Maamrisha na Makatazo, inaanamrisha kila jambo la uadilifu, zuri, linaloridhisha na lenye manufaa. Pia inakataza kila aina ya uovu na baya lenye kuchukiza. Ibn Mas'ud رضي الله عنه na wanazuoni wa *Salaf* walisema, unaposikia Allah تعالى ndani ya Qur'an Anasema,

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Enyi mlioamini...” Basi sikiliza kwa makini, kwani ima itakuwa ni aina ya kheri ambayo Allah تعالى Ameiamrisha au shari ambayo Ameikataza. Kwa mfano Allah تعالى Amesema,

يَأْمُرُهُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثَ
وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ؕ

“...Ambaye Anawaamrisha mema na Anawakataza yaliyo mabaya, na Kuwahalalishia mazuri na Kuwaharamishia vibaya, na Kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani Sharia ngumu za zamani na Mila za Kikafiri).” (7:157)

Na pindi zinapokuja Aya zinazotaja Ufufuo na vitisho vitakavyotokea siku hiyo, na katika kusifia ambayo Allah تعالى Amewaandalia wapenzi Wake na maadui

Zake miongoni mwa Pepo na Moto, raha na adhabu Chungu. Aya hizi zinakuwa na Maamrishi ya mambo mema au maonyo. Kisha Aya zinalingania kufanya amali njema na kuepuka vitendo viovu, na kufanya maisha ya hapa duniani yanafaa kidogo na ya Akhera yanafaa zaidi. Aya pia zinaongoza katika njia sahihi na kuitia ithibati njia ya Allah تعالى iliyo sawa na kanuni za haki, na wakati huo kuondosha katika mioyo uchafu wa shetani aliyewekwa mbali na Rehema za Allah تعالى.

Qur'an ni Muujiza Mkubwa Kabisa Aliopewa Mtume ﷺ.

Sahihi mbili zimeandika Abu Hurayrah عنه رضي الله alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ نَبِيٍّ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ إِلَّا قَدْ أُعْطِيَ مِنَ الْآيَاتِ مَا آمَنَ عَلَىٰ مِثْلِهِ الْبَشَرُ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَحْيًا أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيَّ فَأَزْجُرُ أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*"Hakuna Mtume yoyote, isipokuwa alipewa miujiza, ambayo iliwafanya watu kuamini na kwa hakika nilichopewa mimi ni wahyi ambao Allah Alinishushia. Nataraji nitakuwa na wafuasi wengi siku ya Kiama."*¹

Hivi ndivyo alivyosimulia Muslim. Mtume ﷺ alisema kuwa alipewa Ufunuo, maana yake dhamana mahsus ya Qur'an yenye muujiza ambayo ni changamoto kwa binadamu, walete mfano wake. Ama kuhusu Vitabu vingine vitakatifu vilivyoteremshwa havikuwa na muujiza, haya ni kwa mujibu wa wanazuoni wengi. Allah تعالى Ndiyo Mjuzi zaidi. Mtume ﷺ pia alikuwa na ishara nyingi zinazothibitisha ukweli wa utume wake na kila alichotumwa nacho, shukrani zote zinamstahikia Allah تعالى.

Maana ya Mawe katika Aya hii:

Allah تعالى Amesema,

فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿٢٤﴾

***"Basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, uliowekewa makafiri."* (2:24)**

"Nishati" ni kuni au kitu kinachofanana nazo, kinachotumiwa kuwashia na kuoka moto. Hivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

¹ Fat'hul-Bari 8 / 619, Muslim 1:134.

وَأَمَّا الْقَدَسِيُّونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا ﴿٧٢﴾

“Na wanaokengeuka hao watakuwa kuni za Jahanamu.” (72:15)

Aidha Allah تعالى Amesema;

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرَدُونَ ﴿٧٣﴾ لَوْ
كَانَ هَتُولَاءِ ۖ إِلَهَةً مَا وَرَدُوهَا ۖ وَكُلٌّ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٧٤﴾

“Hakika nyinyi na wale mnaowaabudu, mkamuacha Mwenyezi Mungu, ni kuni za Jahanamu; nanyi mtaifikia (hiyo Jahanamu mkae humo). Lau hawa wanalikuwa miungu wasingefikia (hiyo Jahanamu). Na wote humo watakaa milele.” (21:98-99)

Mawe yaliyotajwa hapa ni mawe ya kibiriti (salfa), makubwa, meusi, magumu, yanukayo na yenye joto kali pindi yanapochomwa. Allah تعالى Atuokoe na mwisho muovu huo. Aidha imeelezwa kuwa mawe yaliyotajwa hapa ni masanamu na washindani ambao walikuwa wakiabudiwa badala ya Allah تعالى, kama Alivyosema Allah تعالى,

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

“Hakika nyinyi na wale mnaowaabudu, mkamuacha Mwenyezi Mungu, ni kuni za Jahanamu.” (21:98)

Na Kauli ya Allah تعالى,

أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿٧٥﴾

“Uliwekewa Makafiri.”

Inaonekana wazi kabisa unakusudiwa Moto ambao kuni zake ni watu na mawe, na pia inaweza kuwa mawe yenyewe. Hakuna mgongano kati ya rai mbili hizi kwani kila moja inajitegemea yenyewe.

أُعِدَّتْ

“Uliwekewa.” Maana yake: Umewekwa na kwa hakika utawapata wale wasiomuamini Allah na Mjumbe Wake. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Muhammad kutoka kwa Ikrimah au Said bin Jubayr alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

أَعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ

“Uliowekewa Makafiri...”

Maana: “Kwa waliokufuru kama nyinyi.”¹

Hivi Sasa Jahannam Ipo.

Maimamu wengi wa Sunnah wameitumia Ayah hii kuthibitisha kuwa Moto upo kwa sasa. Hii ni kwa sababu Allah تعالى Amesema, “Uliowekewa” maana yake, ulioandaliwa na uliowekwa. Kuna Hadithi nyingi juu ya maudhui haya. Kwa mfano, Mtume ﷺ alisema,

«تَحَاجَّتِ الْجَنَّةُ وَالنَّارُ»

“Pepo na Moto vilikuwa vikibishana...”²

Aidha, Mtume ﷺ amesema,

«اسْتَأْذَنَتِ النَّارُ رَبَّهَا فَقَالَتْ: رَبِّ أَكَلْ بَعْضِي بَعْضًا فَأُذِنَ لَهَا بِتَفْسِي: نَفْسٍ فِي الشَّيْءِ وَنَفْسٍ فِي الصَّيْبِ»

“Moto uliomba ruhusa kwa Bwana wake. Ukasema, “Ewe Mola wangu! Baadhi ya sehemu zangu zinakula sehemu zangu nyingine. Hivyo Allah Aliuruhusu kutoa pumzi mbili, pumzi moja wakati wa kusi na pumzi moja wakati wa kaskazi.”³

Aidha, kuna Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه kuwa Masahaba walisikia sauti ya kitu kilichokuwa kikianguka. Walipouliza kuhusu hilo, Mtume ﷺ alisema,

«هَذَا حَجَرٌ أُلْقِيَ بِهِ مِنْ سَفِيرِ جَهَنَّمَ مُنْذُ سَبْعِينَ سَنَةً، الْآنَ وَصَلَ إِلَى قَعْرِهَا»

“Hili ni jiwe lililotupwa juu ya Jahannamu miaka sabini iliyopita, lakini sasa limefika kwenye kina chake.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:87.

² Ibn Abi Hatim 1:88.

³ Ibn Abi Hatim 1:90.

Hadithi hii imo katika Sahih Muslim.¹ Kuna Hadithi nyingi ambazo ni *Mutawatir* (zilizothibiti kwa njia zisizokubali shaka) kuhusu mada hii, kama vile Hadithi za kupatwa Jua na usiku wa Israai nk. Tamko la Allah تعالى;

فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ

“Basi leteni sura moja mfano wake...” (2:23) na

بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ

“Mlete sura moja mfano wake...” (10:38).

Hii ni pamoja na Surah za Qur’an fupi na ndefu. Hivyo, changamoto kwa viumbe ni kuhusu Surah ndefu na fupi, na hakuna tofauti niliyojua mimi kati ya wanazuoni wa zamani na wapya. Kabla ya kusilimu, Amr bin Al-As alikutana na Musaylimah muongo ambaye alimuuliza, “Kitu gani kimeteremshwa kwa jamaa yako hivi karibuni (akimkusudia Muhammad ﷺ akiwa Makka)?”. Amr alisema, “Surah fupi yenye umbuji.” Akauliza, “Ni ipi hiyo?” Akasema,

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٢﴾

“Naapa kwa zama (zako ewe Nabii Muhammad). Kuwa Binadamu yuko katika hasara.. (103:1-2).

Musaylimah alifikiri kwa muda kisha akasema, “Sura sawa na hiyo iliteremshwa Kwangu.” Amr akauliza, “Ni ipi hiyo?” Akajibu, “Ewe Wabr, Ewe Wabr (maana yake, paka shume), wewe si chochote isipokuwa masikio mawili na kifua na vilivyobaki havina thamani na ni vyembamba.” Amr akasema, “Wallahi! Unajua kuwa mimi najua wewe ni muongo.”

* * *

¹ Ibn Abi Hatim 1:90.

وَبَشِّرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَى مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ كُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِنْ
ثَمَرَةٍ رِزْقًا قَالُوا هَذَا الَّذِي رُزِقْنَا
مِنْ قَبْلُ وَأْتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا وَلَهُمْ
فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ وَهُمْ فِيهَا
خَالِدُونَ ﴿٢٥﴾

25. "Na wabashirie walio-
amini na kufanya vitendo
vizuri, kwamba watapata
bustani zipitazo mito mbele
yake; kila mara wataka-
popewa, matunda humo
kuwa ni chakula watasema:
"Haya ndiyo yale tuliyo-
pewa zamani (ulimwe-
nguni)." Kwani wataletewa
(matunda hayo) hali ya
kuwa yamefanana (na yale
waliyokuwa wayajua uli -
mwenguni. Wataletewa

وَبَشِّرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ
تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ كُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِنْ ثَمَرٍ رِزْقًا
قَالُوا هَذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ وَأْتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا
وَلَهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ وَهُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥﴾ *
إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَعِيزُ أَنْ يُضْرَبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةٌ فَمَا فَوْقَهَا
فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ وَأَمَّا
الَّذِينَ كَفَرُوا فَيَقُولُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَذَا مَثَلًا
يُضِلُّ بِهِ كَثِيرًا وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا وَمَا يُضِلُّ بِهِ إِلَّا
الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾ الَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ
مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ
فِي الْأَرْضِ أُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٢٧﴾ كَيْفَ
تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أُمَمًا قَلِيلًا فَآخَيْكُمْ ط ثُمَّ يُمَيِّتْكُمْ
ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٨﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَ
لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ أَسْتَوَى إِلَى السَّمَاءِ
فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٩﴾

kwa sura hiyo; lakini utamu mwingine kabisa); na humo watapata wake
waliotakasika (na kila mabaya na machafu); na watakaa milele humo."

Malipo ya Waumini Wema.

Baada ya kutaja adhabu ambayo Allah تعالی Amewawekea maadui Zake waovu ambao wanamkanusha Yeye na Mitume Wake, Anataja hali ya rafiki Zake waumini wema ambao wanamuamini Yeye na Mitume Wake, wanaamini kwa dhiti na kufanya amali njema. Kwa sababu hii Qur'an Imeitwa *Mathani*, kwa mujibu wa maoni sahihi ya wanazuoni. Mada hii tutaifafanua baadaye. *Mathani*: maana yake ni kutaja kuamini na kisha kutaja kupinga au kinyume chake. Au, Allah تعالی Anataja wema na kisha uovu, au kinyume chake. Ama kutaja vitu vinavyofanana, hiyo inaitwa *Tashaabuhu*, kama tutakavyokuja bainisha hilo Inshaallah. Kwa muktadha huo Allah تعالی Amesema,

وَدَيْتِرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ هُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwamba watapata bustani zipitazo mito mbele yake (Pepo)...”

Hata hivyo, Allah تعالی Ametaja kuwa Pepo ina mito inayopita chini yake, yaani chini ya miti na vyumba. Tunajifunza kutokana na Hadithi kuwa mito ya Peponi haipiti kwenye mabonde, na kuwa kingo za *Al-Kawthar* (Mto wa Mtume uliopo Peponi) umetengenezwa kwa makuba ya lulu yaliyofunuliwa, wala hakuna mgongano wa maelezo ya Qur'an na Hadithi za Mtume ﷺ, udongo wake ni wa kunukia na vijiwe vyake ni lulu na vito vingine. Tunamuomba Allah تعالی Atujaalie Pepo, kwani kwa hakika, Yeye ni Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالی aliripoti kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَنْهَارُ الْجَنَّةِ تَفَجَّرُ تَحْتَ بِلَالٍ أَوْ مِنْ تَحْتِ جِبَالِ الْمِسْكِ»

“Mito ya Peponi inachimbuka kutoka chini ya vilima au milima ya miski.”

Pia alipokea kutoka kwa Masruq kuwa Abdullah alisema, *“Mito ya Peponi inachimbuka kutoka chini ya milima ya Miski.”*¹ Hali kadhalika imenukuliwa kutoka kwa Masruq kuwa Abdullah amesema, *“Mito ya Peponi inachimbuka kutoka chini ya vilima au milima ya miski.”*²

¹ At-Tabari 1:391.

² At-Tabari 1:392.

Kufanana kwa Matunda ya Peponi Baadhi Yake kwa Mengine

Allah تعالی Amesema,

كُلَّمَا زُرِقُوا مِنْهَا مِنْ ثَمَرَةٍ رِزْقًا قَالُوا هَذَا الَّذِي زُرِقْنَا مِنْ قَبْلُ^١

“Kila mara watakapopewa, matunda humo kuwa ni chakula watasema: “Haya ndiyo yale tuliyoopewa zamani (ulimwenguni).”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Yahya Abu Kathir رحمه الله تعالى alisema, “Nyasi za peponi zimetengenezwa kwa Zafarani, na vilima vyake kutokana na miski na ina watumishi mabarobaro wenye ujana wa kudumu watawahudumia Waumini kwa kuwapa matunda ambayo watayala. Kisha wataletewa matunda mengine yanayofanana, watasema, “Haya ni sawa na yale mliyotuletea kabla.” Mabarobaro watawaambia, “Kuleni kwani rangi yake ni sawa, lakini ladha yake ni tofauti.” Hivyo Allah تعالی Amesema,

وَأُتُوا بِمِثْلِهَا^٢

“Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yanafanana.”¹

Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى alisimulia Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa Abu Al-‘Aliyah alisema kuwa,

وَأُتُوا بِمِثْلِهَا^٣

“Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yanafanana.”

Yanafanana kwa maumbo lakini ladha tofauti. Pia Ikrimah amesema kuhusu Aya hii,

وَأُتُوا بِمِثْلِهَا^٣

“Kwani wataletewa (matunda hayo) hali ya kuwa yanafanana.”

Yanafanana na matunda ya duniani, lakini matunda ya Peponi ni matamu zaidi.² Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى aliripoti kutoka kwa al-Amash, kutoka kwa Abu Thubyan, kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Hakuna kitu kilichopo Peponi kinachofanana na maisha ya duniani, ila kwa jina.” Katika masimulizi mengine Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Majina tu ndiyo yanafanana kati ya maisha haya na yaliyopo Peponi.”³

¹ At-Tabari 1:295.

² At-Tabari 1:396.

³ Ibn Abi Hatim 1:91.

Wake wa Watu wa Peponi Wametoharishwa

Allah تعالى Amesema,

وَلَهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ

“Na humo watapata wake waliotakasika (na kila mabaya na machafu).”

Ibn Abu Talhah alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Waliotakaswa na mabaya na uchafu.”¹ Pia, Mujahid alisema. “Kutokana na damu ya mwezi, kwenda haja, kukojoa, kukohoa, kutema mate, kutoa manii na kubeba mimba.”² Aidha Qatadah alisema, “Waliotakasika kutokana na uchafu na madhambi.” Katika masimulizi mengine alisema, “Kutokana na damu ya mwezi na kubeba mimba.”³ Zaidi ya hayo, Ata, al-Hasan, Adh-Dhahhak, Abu Salih, Atiyah na As-Suddi wameripotiwa kuwa walisema vivyo hivyo.⁴ Kauli ya Allah تعالى,

وَهُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥﴾

“Na watakaa milele humo.”

Maana: Hii ndio furaha ya kudumu, Waumini watafurahia maisha ya kudumu, wataepukana na kifo kitakacholingilia furaha yao ya milele, ambayo haina mwisho. Tunamuomba Allah تعالى Atufanye miongoni mwa Waumini hao, kwani Yeye ni Mkarimu sana, Mwema sana na Mwenye Huruma sana.

* إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحْيِي أَنْ يَضْرِبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةٌ فَمَا فَوْقَهَا ۗ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ ۗ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَيَقُولُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَذَا مَثَلًا ۗ يُضِلُّ بِهِ كَثِيرًا وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا ۗ وَمَا يُضِلُّ بِهِ إِلَّا الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾ الَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ أُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٢٦﴾

¹ Ibn Abi Hatim 1:91.

² At-Tabari 1:398.

³ At-Tabari 1:399.

⁴ At-Tabari 1:398.

26. "Hakika Mwenyezi Mungu Haoni haya Kutoa mfano wowote wa mbu na ulio wa zaidi yake. Ama wale wanaoamini, wao hujua ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wao; lakini wale waliokufuru husema: Ni nini Analotaka Mwenyezi Mungu kwa mfano huo?" (Mwenyezi Mungu) Huwaachia wengi kupotea kwa mfano huu na Kuwaongoza wengi kwa mfano huo pia; lakini hamuachii yeyote kupotea kwa mfano huo (na mwingineo) isipokuwa wale wavunjao Amri Zake."

27. "Wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga na kuyakataa aliyoamrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na kufanya ufisadi katika ardhi. Hao ndio wenye hasara."

Katika *Tafsir* yake, As-Suddi aliripoti kuwa Ibn Abbas, Ibn Mas'ud na baadhi ya Masahaba رضي الله عنهم walisema, "Allah تعالى Alipotoa mifano hii miwili ya wanafiki." Kwa Kauli Yake,

مَتْلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا

"Mfano wao (hawa Wanafiki) ni kama mfano wa wale (wasafiri waliokumbwa na kiza) wakakoka moto." (2:17)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ السَّمَاءِ

"Au (mfano wao pia) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni." (2:19).

Hizo ni Aya tatu mfululizo (Aya ya 17, 18 na 19). Wanafiki walisema, "Allah تعالى ni Mwenye Cheo Kikubwa kwa Yeye Kutoa mifano ya aina hiyo." Hivyo Allah تعالى Aliteremsha Aya (2:26-27) hadi Kauli Yake,

هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٢٧﴾

"Hao ndio wenye hasara."¹ Saidi alisema kuwa Qatadah alisema, "Allah تعالى Haoni haya kusema ukweli, wakati anapotaja jambo, bila kujali ukubwa au udogo wa jambo hilo." Allah تعالى Alipotaja nzi na buibui katika Kitabu Chake,

¹ At-Tabari 1:398.

watu waliopotea walisema, “Kwa nini Allah تعالى Alitaja vitu hivi.” “Allah Akateremsha,

﴿ إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحْيِي أَنْ يَضْرِبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةٌ فَمَا فَوْقَهَا ۗ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Haoni haya Kutoa mfano wowote wa mbu na ulio wa zaidi yake.”¹

Mifano Kuhusu Maisha ya Dunia

Abu Ja'far Ar-Razi رحمه الله تعالى alieleza kuwa Ar-Rabi bin Anas aliitolea maelezo Aya hii (2:26), “Huu ni mfano kuwa Allah تعالى Ameupa uhai ulimwengu huu. M-bu anaishi akiwa na njaa, lakini anaponenepa hufa. Huu pia ni mfano wa watu ambao Allah تعالى Amewataja ndani ya Qur'an: Watakapopata maisha ya neema katika dunia hii, kisha Allah Anawaondoa.”

Kisha Akasoma Kauli ya Allah تعالى,

﴿ فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمَ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ ۗ ﴾

“Basi walipopuuzia yale waliyokuwa wakikumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu (walichokuwa wakikitaka)...”. (6:44)²

Katika Aya hii (2:26) Allah تعالى Alisema kwamba Haoni haya au kusita kutoa mifano au hadithi au chochote, ama mfano huo unahusu kitu kidogo au kikubwa. Kauli ya Allah تعالى,

﴿ فَمَا فَوْقَهَا ۗ ﴾

“Au ulio wa zaidi yake.” “Fama fawqaha.” Ina maana: Kitu kikubwa kuliko M-bu ambacho ni kiumbe dhalili na kidogo sana. Muslim amesimulia kuwa Aisha رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

﴿ مَا مِنْ مُسْلِمٍ يُشَاكُ شِرْكَهَ فَمَا فَوْقَهَا إِلَّا كُنَيْتَ لَهُ بِهَا دَرَجَةً، وَمُحِبِّتٌ عَنْهُ بِهَا خَطِيئَةٌ ۗ ﴾

“Hakuna Muislamu atakayedhuriwa na mwiba, “Fama Fawqaha” (au kitu kikubwa), bali ataandikiwa amali njema, na amali mbaya itafutwa kwenye kumbukumbu zake.”³

¹ At-Tabari 1:399.

² At-Tabari 1:398.

³ Muslim 4:1991.

Hivyo Allah تعالى Ametufahamisha kuwa hakuna kitu kidogo kitakachoachwa kutumiwa katika mfano, hata kama kitakuwa kidogo kama M-bu au Buibui. Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ ضَرْبٍ مِّثْلُ مَا سَمِعُوا لَهُ^٤ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ^٥ وَإِنْ يَسْأَلْهُمْ الذُّبَابُ شَيْئًا لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ^٤ ضَعُفَ

الطَّالِبِ وَالْمَطْلُوبِ ﴿٧٧﴾

“Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni; hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawawezi kuumba (hata) nzi, wajapokusanyika kwa jambo hili. Na kama nzi, akiwanyang’anya kitu hawawezi kukipokonya kwake. Amedhoofika kweli kweli huyu mtaka (kupokonya) na mtakiwa (kupokonywa), (atakaye na anayetakiwa).” (22:73)

مِثْلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنْكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا^٥ وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

“Mfano wa wale waliofanya waungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa buibui ajitandiaye nyumba (yake ili imhifadhi, nayo haimhifadhi na lolote); na bila shaka nyumba iliyo dhaifu kuliko zote ni nyumba ya buibui; laiti wangalijua!” (29:41) Na Allah تعالى Amesema;

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ﴿٧٩﴾ تُوْتِي أَكْلَهَا كُلَّ حِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا^٥ وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٨٠﴾ وَمِثْلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ مِنْ فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٨١﴾ يَثْبُتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ^٥ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ^٤ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿٨٢﴾

“Je! Hakuona jinsi Mwenyezi Mungu Alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri (ambao) mizizi yake ni imara na matawi

yake yamenyooka juu. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola Wake; (basi ndivyo neno zuri linavyoleta kheri). Na Mwenyezi Mungu Huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka. Na mfano wa neno baya ni kama mti mbaya ambao umeng'olewa katika ardhi hauna uimara. Mwenyezi Mungu Huwathubutisha wale walioamini kwa kauli thabiti, katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu Huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu (nafsi zao). Na Mwenyezi Mungu Hufanya Apendavyo (kwani kila Alifanyalo ni la kheri tu)." (14:24-27)

Allah تعالیٰ Anasema,

﴿ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا عَبْدًا مَمْلُوكًا لَا يَقْدِرُ عَلَىٰ شَيْءٍ ﴾

"Mwenyezi Mungu Anapigia mfano wa mtumwa anayemilikiwa, asiyeweza chochote." (16:75). Kisha Akasema,

﴿ وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلَيْنِ أَحَدُهُمَا أَبْكَمُ لَا يَقْدِرُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُوَ كَلٌّ عَلَىٰ مَوْلَاهُ أَيْنَمَا يُوَجِّههُ لَا يَأْتِ بِخَيْرٍ ۗ هَلْ يَسْتَوِي هُوَ وَمَنْ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ ﴾

"Na Mwenyezi Mungu Anapigia mfano wa watu wawili (wengine). Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo juu ya bwana wake, Popote amuelekezapo haleti kheri. Je! Huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu..." (16:76). Pia Allah تعالیٰ Amesema,

﴿ ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ هَلْ لَكُمْ مِّنْ مَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَاءَ فِي مَآ رَزَقْنَاكُمْ ﴾

"Amekupigiani mfano kwa hali ya nafsi zenu, je, katika hao iliyowatamalaki mikono yenu ya kuume (kulia) mna washirika katika yale Tuliyokupeni." (30:28)

Mujahid aliyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالیٰ,

﴿ إِنَّ اللَّهَ لَا يَسْتَحْيِي ۗ أَنْ يَضْرِبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةٌ فَمَا فَوْقَهَا ﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Haoni haya Kutoa mfano wowote wa M-bu na ulio wa zaidi yake..." (2:26)

“Waumini wanaamini mifano hii, bila kujali inahusu vitu vikubwa au vidogo kwa sababu wanajua huo ni ukweli kutoka kwa Mola wao, na Allah تعالی Anawaongoza waumini kwa mifano hii.”¹

Katika Tafsiri yake, As-Suddi amesimulia kuwa Ibn Abbas, Ibn Mas’ud na watu wengine miongoni mwa Masahaba رضي الله عنهم walisema,

يُضِلُّ بِهِ كَثِيرًا

“**Huwaachia wengi kupotea kwa mfano huo.**” Maana: Wanafiki. Allah تعالی Anawaongoza Waumini kwa mifano hii. Wale ambao waliokwishapotea Allah تعالی Anazidi Kuwapoteza kwa kuyakanusha kwao yale ambayo walikuwa wakiyafahamu kwa yakini katika mifano waliyokuwa wakipigiwa na Mwenyezi Mungu. Hivi ndivyo Allah تعالی Anavyowapoteza.²

وَيَهْدِي بِهِ كَثِيرًا

“**Na Huwaongoza wengi kwa mfano huo pia.**”

Kutoka watu wanaoamini na kusadikisha. Allah تعالی Anawaongezea uongofu katika uongofu wao, na Imani katika Imani yao. Kwa sababu wanaamini kwa dhati yale wanayoyajua kuwa ni ukweli, yaani, mifano ambayo Allah تعالی Ameidaja. Huu ni uongofu ambao Allah تعالی Amewapatia.

وَمَا يُضِلُّ بِهِ إِلَّا الْفَاسِقِينَ ﴿٢٥﴾

“**Lakini hamuachii yeyote kupotea kwa mfano huo (na mwingineo) isipokuwa wale wavunjao Amri Zake.**”

Ikiwa na maana ya Wanafiki. Na neno “Fasiq” katika muktadha wa lugha ya Kiarabu lina maana ya kutoka nje ya utiifu. Waarabu wanasema, “Fasaqti Arut’bah”, Maana: Tende inapotokeza katika ngozi yake, na wanamuita panya Fuwaysiqah, kwa sababu huwa anatoka shimoni mwake ili afanye uharibifu.

Sahihi mbili zimemrikodi Aisha رضي الله عنها akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«خَمْسٌ فَوَاسِقٌ يُفْتَلَنُ فِي الْجِلِّ وَالْحَرَمِ: الْغُرَابُ وَالْحِدَاةُ وَالْعَفْرَبُ وَالْفَارَةُ
وَالْكَلْبُ الْعَقُورُ»

¹ Ibn Abi Hatim 1:93.

² At-Tabari 1:408.

“Wanyama watano ni waharibifu (Fawasiq), wanauawa wakati wa kawaida au wakati wa Ihram: Kunguru, mwewe, nge, panya na mbwa mwenye kichaa.”¹

Mtu Fasiki ni pamoja na kafiri na Asi. Hata hivyo ufasiki wa kafiri ni mbaya zaidi. Na ufasiki uliomaanishwa katika Aya hii, una maana ya mtu kafiri. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi, kwa sababu Allah تعالى Amewaelezea wao,

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ
وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٢٧﴾

“Wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuifunga na kuyakataa aliyoamrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na kufanya ufisadi katika ardhi. Hao ndio wenye hasara.”

Hizi ndizo sifa bainifu za Makafiri na ni kinyume na sifa za Waumini. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema katika Surat Ar-Radi.

۞ أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ ۚ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ
﴿٢٨﴾ الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ ﴿٢٩﴾ وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ
أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٣٠﴾

“Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako ni haki (akayafuata basi) ni kama aliye kipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia. (Nao ni hawa) ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu wala hawavunji ahadi (za wanadamu wenzao). Na ambao huyaunga Aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe, na humuogopa Mola wao, na huiogopa hesabu mbaya (itakayowapata wabaya huko Akhera, kwa hivyo wakajitahidi kujiepusha na vitendo vyao hao wabaya).” (13:19-21)

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ
وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٣١﴾

¹ Fat’hul Al-Bari 6:408 na Muslim 2:856.

“Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu (na za wanadamu wenzao) baada ya kuzifunga, na wanakata Aliyoamuru Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanafanya uharibifu katika nchi, hao ndio watakaopata laana, na watapata nyumba mbaya.” (13:25)

Ahadi ambayo hawa watu walioasi waliyoivunja ni ahadi ya Allah تعالی na viumbe wake, yaani, kumtii Yeye na kuacha madhambi ambayo Ameyakataza. Ahadi hii imerejewa katika Vitabu vya Allah تعالی na katika maneno ya Mitume Yake. Kuvunjwa kwake ni kule kuiacha bila kuitekeleza.

Ilisemwa kuwa Aya (2:27) ni kuhusu makafiri na wanafiki miongoni mwa watu waliopewa Kitabu. Katika hali hii, ahadi waliyoivunja ni ahadi ya utii Aliyoichukua Allah تعالی kutoka kwao ndani ya Taurati kuwa watamfuata Muhammad ﷺ atakapotumwa kama Mtume, na kumuamini pamoja na alichokuja nacho (Uislamu). Kuvunja ahadi ya Allah تعالی katika hali hii kulitokea pindi watu wa Kitabu walipomkataa Mtume ﷺ baada ya kujua ukweli kuhusu Mtume ﷺ; na wakauficha ukweli huo kuwafikia watu, japokuwa walimuapia Allah تعالی kuwa wangeudhihirisha, si kuuficha.

Allah تعالی Alitufahamisha kuwa walitupa ahadi nyuma ya migongo yao na wakaiuza kwa thamani duni. Na huu ni mtazamo wa bin Jariri رحمه الله تعالی. Na ndio kauli ya Mukatil bin Hayan.

Aidha imepokelewa kuwa Aya (2:27) inawahusu wote Makafiri, Washirikina na Wanafiki. Allah تعالی Alipokea ahadi ya utii ya kumuamini Yeye Peke Yake, huku Akiwaonesha alama zinazothibitisha Uungu Wake. Aidha Alichukua ahadi kutoka kwao ya kutii Amri Zake na kujiepusha na Yale Aliyoyakataza, Akijua kuwa Mitume Yake wataleta ushahidi na miujiza ambayo hapana kiumbe atakayeweza kuleta mfano wake. Miujiza hii inathibitisha ukweli wa Mitume wa Allah تعالی. Ahadi ilivunjika wakati makafiri walipokanusha yaliyothibitishwa kwao kuwa ya kweli na wakawakataa Mitume wa Allah عزوجل na Vitabu japokuwa walijua kuwa ni kweli. *Tafsiri* hii iliripotiwa kutoka kwa Muqatil bin Hayyan, na nzuri mno. Pia, hiyo ni rai ya Az-Zamakshari رحمه الله تعالی.

Kauli ya Allah تعالی inayofuatia,

وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ

“Na kuyakataa Aliyoamrisha Mwenyezi Mungu kuungwa.”

Kilichokusudiwa katika Aya hii ni kufanya mahusiano mazuri na jamaa na kuenzi udugu, kama Qatadah alivyosema kuwa Aya hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى،

فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ ﴿٢٥﴾

“Ndiyo yanayotarajiwa kwenu kufisidi katika ardhi na kuwakata jamaa zenu wakati mkipata ukubwa?” (47:22)¹

Ibn Jarir At-Tabari رحمه الله تعالى alipendelea maoni haya. Hata hivyo, Inasemwa kuwa maana ya Aya (2:27) hapa ni ya ujumla wake. Hivyo, kila kitu ambacho Allah تعالى Aliwaamrisha watu wajifunze na kukifanya lakini wakavunja maagizo hayo na kuyaacha yanaingia katika maana yake.

Maana ya Khasara

Muqatil bin Hayyan alitoa maelezo kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

أُولَئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٢٦﴾

“Hao ndio wenye hasara.”

Huko Akhera.² Aidha Allah تعالى Amesema،

أُولَئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٧﴾

“...Hao ndio watakaopata laana, na watapata nyumba mbaya.” (13:25)

Aidha, Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kila sifa bainifu ambayo Allah تعالى Amewaelezea watu ambao si Waislamu – kama walikula khasara – sifa hiyo inamaanisha ukafiri. Hata hivyo, pindi zinapowahusu Waislamu, basi maneno hayatakuwa na maana ya dhambi.”³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالى،

أُولَئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٢٦﴾

“Hao ndio wenye hasara.” “Wenye hasara”

¹ At-Tabari 416.

² Ibn Abi Hatim 1:101.

³ At-Tabari 1:417.

Ni wingi wa “mwenye hasara”, Neno hili linamhusu yeyote aliyepunguza sehemu yake ya huruma za Allah تعالى kwa kumuasi Yeye. Ni kama mfanyabiashara anavyopata hasara katika biashara zake kwa kuanguka mtaji wake. Hali hii pia ndio aliyonayo Mnafiki na Kafiri ambao hupoteza sehemu yao ya huruma ambayo Allah تعالى Amewawekea Waja Wake siku ya Ufufuo. Na wakati huo Kafiri na Mnafiki wanahitajia sana huruma za Allah تعالى. Husemwa katika lugha ya Kiarabu “Khasira Arrajulu” pindi mtu anapopata hasara. Kwa kuzingatia maana hayo amesema mshairi Jarir bin Attwiya katika kuwasema vibaya ukoo wa Salit, “Hakika ukoo wa Salit umeangukia katika hasara. Hakika hali ilivyo, ni kizazi kilichoumbwa kutumikia utumwa maisha yao yote...”

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَانًا فَأَحْيَيْكُم مَّا تُمَيِّتُكُم مَّا تُمَيِّتُكُم ثُمَّ تُحْيِيكُم ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٥﴾

28. “Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu, na hali mlikuwa wafu, Akakuhi sheni; kisha Atakufisheni; kisha Atakuhi sheni; kisha Kwake mtarejeshwa (Atakufufueni).”

Allah تعالى Anathibitisha ukweli kwamba Yeye Yupo na kuwa Yeye ni Muumba na Mmiliki Ambaye Ana Mamlaka kamili juu ya Waja Wake.

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ

“Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu.”

Vipi mnakanusha kuwepo kwa Allah تعالى, au mnamuabudu pamoja na vitu vingine,

وَكُنْتُمْ أَمْوَانًا فَأَحْيَيْكُم مَّا

“Na hali mlikuwa wafu, Akakuhi sheni.”

Maana: Aliwaleta kwenye uhai kutoka hali ya kutokuwa na uhai. Vile vile Allah تعالى Amesema,

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ ﴿٢٦﴾ أَمْ خَلِقُوا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بَلْ لَا

يُوقِنُونَ ﴿٢٦﴾

“Je wameumbwa pasipo kitu, au wao ndio waliojiumba. Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini (ya jambo lolote).” (52:35-36)

Na Allah تعالى Amesema,

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿٣٥﴾

“Hakika ulimpitia Binadamu wakati mrefu katika dahari, hakuwa kitu kinachotajwa (Binadamu ndiye kiumbe cha mwisho kuletwa ulimwenguni).” (76:1)

Kuna Aya nyingi kuhusu somo hili. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ata kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَكُنْتُمْ أَمْوَانًا فَأَحْيَاكُمْ

“Na hali mlikuwa wafu, Akakuhiisheni.”

Maana yake: Mlikuwa wafu katika migongo ya baba zenu.” Hamkuwepo kabla ya hapo. Hamkuwa chochote mpaka Allah تعالى Alipowaumba. Atakufisheni kifo cha kweli, kisha Atakuhiisheni siku ya Ufufuo”. Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, “Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى;

قَالُوا رَبَّنَا أَمْثَلْنَا أُمَّتَيْنِ وَأَحْيَيْتَنَا أُمَّتَيْنِ

“Watasema: “Mola wetu! Umetufisha mara mbili na Umetuhuisha mara mbili.” (40:11)¹

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ

سَمَوَاتٍ ۚ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣٦﴾

29. “Yeye Ndiye Aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi (kabla hajakuumbeni ili mkute kila kitu tayari) kisha Akanyanyua mbingu; na Akazifanya mbingu saba. Naye Ndiye Ajuaye kila kitu.”

¹ At-Tabari 1:419.

Ubainifu wa Dalili ya Uwezo wa Allah تعالى.

Baada ya Allah تعالى Kutaja ushahidi wa Kuwaumba, na yale yanayoshuhudiliwa na nafsi zao.

Hapa Anataja ushahidi ambao wanaweza kuushuhudia, maana, Uumbaji wa mbingu na ardhi.

Allah تعالى Amesema,

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ ۗ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi (kabla hajakuumbeni ili mkute kila kitu tayari) tena Akakusudia Kuumba mbingu na Akazifanya mbingu saba.”

فَسَوَّاهُنَّ

“Akazifanya mbingu.”

Maana: Alizifanya mbingu saba. Neno “Assamaa” hapa limetajwa kwa umoja, lakini lina maana ya wingi katika sarufi ya kiarabu.

Kwa kuzingatia hilo ndio maana limevumishwa na kivumishi cha neno “Saba” Katika Kauli Yake Allah تعالى,

فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٦﴾

“Na Akazifanya mbingu saba. Naye Ndiye Ajuaye kila kitu.”

Maana yake: Elimu Yake Imevienea viumbe Vyake vyote, kama Alivyosema katika Aya nyingine,

أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ

“Oh! Asijue Aliyeumba!...” (67:14)

Mwanzo wa Uumbaji.

Ayah hii (2:29) imeelezwa kwa urefu katika Surat As-Sajdah:

* قُلْ أُنَبِّئُكُمْ لَتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ وَتَجْعَلُونَ لَهُمْ أَنْدَادًا ۗ ذَٰلِكَ رَبُّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٢٩﴾ وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ مِنْ فَوْقِهَا وَبَدَرَكَ فِيهَا وَقَدَّرَ فِيهَا أَقْوَامًا فِي أَرْبَعَةِ أَيَّامٍ
 سَوَاءً لِّلسَّالِبِينَ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ وَهِيَ دُخَانٌ فَقَالَ لَهَا وَلِلْأَرْضِ ائْتِيَا طَوْعًا
 أَوْ كَرْهًا قَالَتَا أَتَيْنَا طَائِعِينَ ﴿٣١﴾ فَقَضَيْنَهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ فِي يَوْمَيْنِ وَأَوْحَىٰ فِي كُلِّ
 سَمَاءٍ أَمْرَهَا ۗ وَزَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ وَحِفْظًا ۗ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٢﴾

“Sema (Ewe Muhammad): Mnamkanusha yule (Mwenyezi Mungu) Aliyeumba ardhi katika siku mbili (tu), na mmempa washirika? Huyu Ndiye Mola wa walimwengu wote. (Mshirika huyo ametoka wapi).” Na Akaweka humo milima juu yake (ya uso wake), na Akabarikia humo na Akakadiria humo chakula chake (cha kuwatosha watakaokaa humo). (Ameyafanya haya) katika siku nne, (mida minne). Haya ni sawa kabisa kwa hao wanaouliza (mambo wakataka kuyajua). Kisha Akazielekea mbingu na zilikuwa moshi, basi Akaziambia (mbingu) na ardhi: “Njoooni, mkipenda msipende.” Vyote viwili vikasema: “Tumekuja, hali ya kuwa wenye utiifu.” Basi Akazifanya mbingu saba katika siku mbili, na kila uwingu Akaufunulia kazi yake. Na Tumeipamba mbingu ya karibu yenu kwa taa na kulinda. Hiki ndicho kipimo cha Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.” (41:9-12)

Aya hizi zinaonesha kuwa Allah تعالیٰ Alianza Kuumba ardhi, na kisha Akaziumba mbingu saba.

Hivi ndivyo ujenzi unavyoanza, kwa kujenga ghorofa za chini kwanza na kisha ghorofa za juu, kama wanazuoni wa Tafsir walivyorejea, kama tutakavyofahamu, Insha'Allah.

Ama kuhusu Kauli Yake Allah تعالیٰ,

ءَأَنْتُمْ أَشْدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بِنَهَا ﴿٢٧﴾ رَفَعَ سَمَكَهَا فَسَوَّيْنَهَا ﴿٢٨﴾ وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا
 وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿٢٩﴾ وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحْنَهَا ﴿٣٠﴾ أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَهَا ﴿٣١﴾
 وَالْجِبَالَ أَرْسَنَهَا ﴿٣٢﴾ مَتَّعْنَاكُمْ وَأَلْتَمِعْكُمْ ﴿٣٣﴾

“Je, nyinyi ni wagumu zaidi Kuumbwa au mbingu? Yeye Amezijinga. Akainua kimo chake na Akazitengeneza vizuri. Na Akautia giza usiku wake na Akautokezesha mchana wake. Na ardhi baada ya hayo Akaitandaza. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake. Na Milima Akaisimamisha. (Kafanya haya yote) kwa ajili ya Kukustarehesheni nyinyi na Wanyama wenu (Basi aliyefanya yote haya si muweza wa kufufua?)” (79:27-33).

Imesemwa kuwa kuunganisha “Kisha” katika Aya (2:29) kinahusu utaratibu tu wa usomaji wa taarifa ilivyotolewa, lakini haihusu utaratibu wa matukio yalivyotajwa kutokea, hili lilipokelewa kutoka kwa Ibn Abbas na Ali bin Abu Twalhah.¹ Ni kama mshairi alivyosema;

Muambie aliyepata utukufu, kisha akawa Mtukufu baba yake.

Kisha akawa mtukufu kabla ya hapo babu yake.

Ardhi Iliumbwa kabla ya Mbingu.

Mujahid alitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى،

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا

“Yeye Ndiye Aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi.”

Allah تعالى Aliumba ardhi kabla ya mbingu, na Alipoumba Ardhi, moshi ulitoka. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ اسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ وَهِيَ دُخَانٌ

“Kisha Akazielekea mbingu na zilikuwa moshi.” (41:11)

¹ At-Tabari 1:437.

فَسَوَّيْنَهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ^ع

“Na Akazifanya mbingu saba.”

Maana: Moja juu ya nyingine, wakati ardhi saba maana yake, moja chini ya nyingine.¹ Aya hii inathibitisha ukweli kwamba ardhi iliumbwa kabla ya mbingu, kama Allah تعالى Alivyoonesha katika Aya iliyotangulia ya *Surat Sajdah*. Hii nayo inathibitisha hilo.

Ardhi Ilitandazwa Baada ya Kuumbwa Mbingu.

Sahihi Al-Bukhari imeandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alipoulizwa juu ya suala hili, alisema kuwa ardhi iliumbwa kabla ya mbingu, na ardhi ilitandazwa baada ya Kuumbwa mbingu.²

Wanazuoni wengi wa Tafsir wa kale na wa leo wamesema vivyo hivyo, kama tulivyofafanua katika *Tafsir ya Surat An-Naziat* (Surah ya 79). Matokeo ya mjadala huo ni kuwa neno *Daha* (limefasiriwa hapo juu kama “kutandaza”) limetajwa na kuelezwa katika Kauli ya Allah تعالى,

وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحْنَهَا ﴿٣١﴾ أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَهَا ﴿٣٢﴾ وَأَلْجَبَالَ أَرْسَنَهَا ﴿٣٣﴾

“Na ardhi baada ya hayo Akaitandaza. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake. Na milima Akaisimamisha”. (79:30-32)

Kwa hiyo, *Daha* maana yake hazina za dunia zililetwa juu baada ya kumalizika Kuumbwa vyote vitakavyoishi duniani na mbinguni. Wakati ardhi ilipokuwa *Daha*, maji yalichimbuka nje na kila aina ya rangi, maumbo na aina tofauti za mimea ziliota. Nyota zilianza kuzunguka pamoja na sayari ambazo zinazunguka. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

* * *

¹ At-Tabari 1:436.

² Fat’hul al-Bari 8:417.

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰئِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً ۗ قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَآءَ وَيَحْنُ نُسُجُوحًا يَّحْمَدُكَ وَتُقَدِّسُ لَكَ ۗ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾ وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلٰئِكَةِ فَقَالَ أَنْبِئُونِي بِأَسْمَاءِ هٰؤُلَاءِ إِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِينَ ﴿٣١﴾ قَالُوا سُبْحٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَا بِهٰذَا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣٢﴾ قَالَ يَا قَوْمِ أُوذِيَ بِأَسْمَائِهِمْ فَلَمَّا أَنْبَأَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٣﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰئِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ ۖ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكٰفِرِينَ ﴿٣٤﴾ وَقُلْنَا يَا آدَمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هٰذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّٰلِمِينَ ﴿٣٥﴾ فَأَزَلَّهُمَا الشَّيْطٰنُ عَنْهَا فَأَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيهِ ۗ وَقُلْنَا اهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتَاعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٣٦﴾ فَتَلَقَىٰ آدَمُ مِنْ رَبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ ۗ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰئِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً ۗ قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَآءَ وَيَحْنُ نُسُجُوحًا يَّحْمَدُكَ وَتُقَدِّسُ لَكَ ۗ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

30. “(Wakumbushe watu khabari hii;) Wakati Mola Wako Alipowaambia Malaika: “Mimi Nitaleta viumbe vyengine kukaa katika ardhi.” (Nao ndio Wanadamu). Wakasema (Malaika): “Utawaweka humo watakaofanya uhari-bifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutukuza kwa Sifa Zako na kukutaja kwa Utakatifu Wako?” Akasema (Allah): “Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua.”

Khalifa Adam عليه السلام na Wanawe Duniani na Wali-yoyasema Malaika Kuhusu Wao.

Allah تعالی Alirejea Fadhili Zake kwa Wana wa Adam

aliposema kuwa Aliwataja katika upeo wa juu kabla ya Kuwaumba, Allah تعالی Amesema,

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰئِكَةِ

“(Wakumbushe watu khabari hii;) Wakati Mola Wako Alipowaambia Malaika.”

Aya hii ina maana, “Ewe Muhammad! Waambie watu wako yale Allah تعالى Aliyowaambia Malaika.”

إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً

“Mimi Nitaleta viumbe vyengine kukaa katika ardhi.” (Nao ndio Wanadamu).

Maana yake: Watu wanaozaliana, kizazi baada ya kizazi, na karne baada ya karne, kama Allah تعالى Alivyosema,

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خُلَافَةَ الْأَرْضِ

“Na Ndiye Aliyekufanyieni washikaji wa mahali pa hao walio-ondoka katika ardhi.” (6:165)

Na Amesema;

وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ

“Na Kukufanyeni wenye kuendesha dunia (siye bora?).” (27:62)

Na Amesema;

وَلَوْ دَشَاءَ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿٤٣﴾

“Na kama Tungalipenda Tungewafanya Malaika (kuwa wakazi) wa ardhi hii badala yenu.” (43:60) na,

فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ

“Basi wakawaandamia nyuma yao (yaani baada ya wale Mayahudi wazuri, Mitume na wengineo, kikaja) kizazi kibaya...” (7:169).

Na sura ya Mariam Aya ya (59).

Inaonesha kuwa Allah تعالى Hakukusudia Adam عليه السلام hasa ndiye Khalifah, vinginevyo kauli ya Malaika ingekuwa haipendezi,

أَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ

“Utawaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu.”

Malaika walikuwa na maana kuwa aina hii ya viumbe walikuwa wanafanya uharibifu walioutaja. Malaika walijua ukweli huu, kwa mujibu wa uelewa wao wa maumbile ya binadamu, kwani Allah تعالى Alishasema kuwa Atamuumba binadamu kutokana na udongo utokanao na matope meusi yaliyovunda. Au Malaika walijua ukweli kutokana na neno Khalifa, ambalo pia lina maana ya mtu anayehukumu migogoro inayotokea kati ya watu, akiwazuia kudhulumu na kutenda dhambi, kama Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alivyosema. Kauli waliyoitoa malaika si ya kubishana na Allah تعالى, wala sio kwamba waliwaonea wivu Wana wa Adam عليه السلام, kama wadhaniavyo baadhi ya wafasiri. Allah تعالى Amewaelezea Malaika kuwa ni viumbe wasiomtangulia Yeye katika kuzungumza, ina maana kuwa hawamuulizi Allah تعالى chochote bila Idhini Yake. Pale Allah تعالى Alipowaambia kuwa Atawaumba viumbe katika ardhi, na walikuwa wanajua kuwa viumbe hao wataleta uharibifu duniani kama Qatadah alivyotaja, wakasema,

أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ

“Utawaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu.”

Hili ni swali la kujifunza Hekima iliyomo, kama kwamba walisema, “Ewe Bwana! Kuna Hekima gani ya Kuumba viumbe hivyo ambavyo vitafanya uharibifu humo na kumwaga damu?”¹ Kama Hekima ya kitendo hiki ni ili uabudiwe sisi tunakushukuru na kukutukuza Wewe, hatujiingizi katika uharibifu, hivyo kuna haja gani Kuumba viumbe wengine.” Allah تعالى Aliwaambia Malaika katika kujibu maulizo hayo.

إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾

“Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua.”

Maana yake: “Najua manufaa ya Kuwaumba hawa viumbe ambayo yanazidi madhara mliyoyataja, ambayo hamna maarifa nayo. Nitawaumba miongoni mwao Mitume, na nitatuma Wajumbe. Aidha Nitaumba miongoni mwao watu Waaminifu, Mashahidi, Waumini, Waadilifu, Wanaoabudu, Watu wasiojivuna,

¹ At-Tabari 1:464.

Wachamungu, Wanazuoni wanaotumia elimu yao, Watu wapole na ambao wanampenda Allah تعالى na wanawafuata Mitume Yake." Sahihi imeandika kuwa Malaika wanapopanda kwa Allah تعالى na taarifa za amali za waja, Allah تعالى Huwauliza, japo Anajua kila kitu, "Mmewaacha vipi Waja Wangu?" Wanamjibu, "Tuliwakuta wanasali na tumewaacha wakisali."¹ Hii ni kwa sababu Malaika wanafanya kazi kwa zamu wanapokuwa na binadamu, na wanabadilishana zamu wakati wa Sala ya Alfajiri na Alasiri. Malaika walioshuka wanabaki nasi, na wale waliobaki nasi wanapanda na amali zetu. Mtume ﷺ amesema,

«يُرْفَعُ إِلَيْهِ عَمَلُ اللَّيْلِ قَبْلَ النَّهَارِ وَعَمَلُ النَّهَارِ قَبْلَ اللَّيْلِ»

*"Amali za usiku zinanyanyuliwa kwenda kwa Allah kabla ya mawio na amali za mchana kabla ya usiku haujaingia."*²

Hivyo kauli ya Malaika, "Tuliwajia wakiwa wanasali na tunawaacha wakiwa wanasali." Inaelezea Kauli ya Allah تعالى,

إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٠١﴾

"Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua."

Ilisemwa kuwa maana ya Kauli ya Allah تعالى,

إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٠١﴾

"Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua."

Ni, "Nina Hekima mahsusi ya Kuwaumba wao, ambayo hamuijui." Aidha imesemwa ni majibu ya,

وَحَنُّنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ^ط

"Hali sisi tunakutukuza kwa Sifa Zako na kukutaja kwa Utakatifu Wako?"

Baada ya hapo Allah تعالى Akasema,

¹ Fat'hul Al-Bari 13:426.

² Muslim Namba 179 na *Musnad Abi'Awanah* 1:145.

إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

“Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua.”

Maana yake: “Najua kuwa Iblis si kama nyinyi, japokuwa ni miongoni mwenu.”
Wengine walisema inakusudia Neno Lake kwamba,

أَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ ۗ

“Utawaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutukuza kwa Sifa Zako na kukutaja kwa Utakatifu Wako?”

Ni maombi yao kuwa waruhusiwe kuishi duniani badala ya Wana wa Adam.
Hivyo Allah تعالى Akawaambia,

إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣١﴾

“Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua.”

Iwapo kuishi kwenu peponi ni vema au ni vibaya. Ar-Razi رحمه الله تعالى na wengine wameyasema hayo. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Ulazima wa Kumteua Khalifa na Baadhi ya Masuala ya *Khilafah*

Al-Qurtubi رحمه الله تعالى na Wanazuoni wengine, walisema kuwa Aya (2:30) inathibitisha wajibu wa kuteuliwa Khalifa wa kuhukumu migogoro baina ya watu, kuwasaidia wanyonge dhidi ya wakandamizaji, kutekeleza Sharia za Kiislamu na kukanya maovu. Kuna majukumu mengine mengi ambayo yanaweza kutekelezwa tu kwa kumteua kiongozi. Na kanuni ya kisharia inasema kilicho muhimu katika utekelezaji wa wajibu, basi chenyewe ni wajibu. Tunalazimika kutaja hapa kuwa uongozi unapatikana kupitia njia ya maandiko. Kama wasemavyo baadhi ya *Ahlu Sunna* katika tukio la kumteua Abubakar رضي الله عنه au kwa njia ya kuashiria kutaja mrithi, kama kundi la Wanazuoni wengine wa *Ahl As-Sunnah* walivyosema ilitokea kwa Mtume – katika suala la Abubakar رضي الله عنه, au kumpendekeza Khalifa mwengine baada yake kama Khalifa Abubakar رضي الله عنه alivyofanya kwa 'Umar رضي الله عنه. Au Khalifa anaweza kuyaacha mambo Mikononi mwa “*Majlis Shura*” au kikundi cha watu Waadilifu,

kama Umar رضى الله عنه alivyofanya. Au, watu mashuhuri wenye maono na busara wanakusanyika na kumteua mmoja wao, au wanamteua mmoja miongoni mwao kumpendekeza kiongozi. Kwa mujibu wa Wanazuoni wengi akichaguliwa kwa njia hizo ni wajibu kumfuata.

Khalifa lazima awe Muislamu, Mwanaume, Baleghe, Mwenye dhima anayeweza kufanya *Ijtihad* (maamuzi binafsi ya kisheria), siha ya mwili, muadilifu, mwenye maarifa ya mambo ya kivita na siasa. Lazima, atokane na kabila la Quraysh, kwa mujibu wa msimamo sahihi, lakini si lazima atokane na ukoo wa Bani Hashim au awe na kinga ya kufanya makosa (*ma'asum*), kama *Ar-Rawaafidh* (Mashia) wanavyodai. Khalifah anapokuwa na maadili machafu (*fasiq*). Je aondolewe? Kuna kutokubaliana kwa wanazuoni juu ya suala hili, lakini msimamo sahihi ni kuwa hataondolewa, kwa sababu Mtume ﷺ alisema,

«إِلَّا أَنْ تَرَوْا كُفْرًا بَوَاحًا عِنْدَكُمْ مِنَ اللَّهِ فِيهِ بُرْهَانٌ»

*"Mpaka mtakapoona kufuru ya wazi mbele yenu ambayo mna hoja (ushahidi) kutoka kwa Allah."*¹

Je, Khalifa ana haki ya kujiuzulu mwenyewe? Kuna mitazamo tofauti katika suala hili. Ni kweli kuwa Al-Hasan bin Ali رضى الله عنهما alijiondoa mwenyewe kwenye nafasi ya Ukhalifa na akausalimisha kwa Muawiyah. Hata hivyo, hili lilitokea kwa sababu ya ulazima, na Al-Hasan رضى الله عنه alisifiwa kwa kitendo hicho. Hairuhusiwi kuteua Makhaliifa wawili kuwa watawala au zaidi kwa wakati mmoja. Hairuhusiwi kwa sababu Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ جَاءَكُمْ وَأَمْرُكُمْ جَمِيعٌ يُرِيدُ أَنْ يُفَرِّقَ بَيْنَكُمْ فَأَقْتُلُوهُ كَأَنَّا مِنْ كَانٍ»

*"Atakayewajia kujaribu kuwatenganisha ilhali mko pamoja, muueni yoyote awaye."*²

Haya ni maoni ya wanazuoni wengi. Imam Al-Haramayn رحمه الله تعالى alisema kuwa Abu Is-haq رحمه الله تعالى aliruhusu kuteuliwa Makhaliifa wawili au zaidi wakati majimbo yanapokuwa mbalimbali na kutanuka. Hata hivyo, Imam Al-Haramayn رحمه الله تعالى mwenyewe hakuwa muwazi katika rai yake hii.

¹ Al-Bukhari 7056 na At-Tabari 1:477.

² Muslim 3:1470.

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ فَقَالَ أَنْبِئُونِي بِأَسْمَاءِ هَٰؤُلَاءِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٠﴾ قَالُوا سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣١﴾ قَالَ يَتَقَدَّمُ أُنْبِئُهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ فَلَمَّا أَنْبَأَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنْزِي أَعْلَمُ غَيْبِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٢﴾

31. *“Na (Mwenyezi Mungu) Akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote, kisha Akaviweka mbele ya Malaika na Akasema (kuwaambia Malaika), “Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa mnasema kweli (Kuwa nyinyi ndio wajuzi wa mambo).”*

32. *Wakasema (Malaika): “Utakatifu ni Wako! Hatuna elimu isipokuwa ile Uliyotufundisha; bila shaka Wewe Ndiye Mjuzi na Ndiye Mwenye Hekima (Mwenye Kuweka kila kitu mahali pake).”*

33. *Akasema: “(Mwenyezi Mungu) “Ewe Adam! Waambie majina yake. Alipowaambia majina yake Alisema (Mwenyezi Mungu), “Sikukuambieni kwamba Mimi Ninajua siri za mbingu na ardhi, tena Najua mnayoadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha.”*

Utukufu wa Adam عليه السلام Juu ya Malaika.

Allah تعالى Anaelezea Utukufu wa Adam عليه السلام juu ya Malaika, kwa sababu Alimfundisha Adam عليه السلام, badala yao, majina ya kila kitu. Hili lilitokea baada ya kumsujudia. Mjadala huu unathibitisha tukio hilo hapa, ili kuonesha umuhimu wa nafasi yake, na Malaika kutofahamu kuhusu Kuumbwa kwa Adam عليه السلام wakati walipouliza habari zake. Hivyo Allah تعالى Akawafahamisha Malaika kuwa Anajua wasiyoyajua, kisha Akataja haya ili Kuwaonesha ubora wa Adam عليه السلام juu yao katika elimu. Allah تعالى Amesema,

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا

“Na (Mwenyezi Mungu) Akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote.”

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliitolea maelezo Aya hii,

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا

“Na (Mwenyezi Mungu) Akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote.”

Maana yake: Majina yanayotumiwa na watu, kama binadamu, wanyama, mbingu, dunia, ardhi, bahari, farasi, punda nk. Pamoja na majina ya viumbe wengine.¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Asim bin Kulayb alisimulia kutoka kwa Said bin Ma'abad kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliulizwa:

وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا

“Na (Mwenyezi Mungu) Akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote.”

“Je, Allah تعالى Alimfundisha majina ya sahani na chungu?” Akajibu, “Ndiyo, na hata istilahi ya kutokwa na upepo!”²

Na imesemwa majina ya nyota zote. Na imesemwa majina ya kizazi chake chote.

Na rai ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى ni kwamba Allah تعالى Alimfundisha Adam عليه السلام majina ya Malaika na kizazi chake.

Na kauli sahihi ni kwamba, Allah تعالى Alimfundisha Adam عليه السلام maneno ya kila kitu, majina halisi, majina ya sifa bainifu na kazi zao, kama Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alivyosema kuhusu kutoa upepo.

Katika Sahihi yake, Al-Bukhari ameielezea Aya hii katika Kitabu cha Tafsir pamoja na ripoti kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه ambaye alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 1:458.

² At-Tabari 1:485.

“Nendeni kwa Isa, ni mja wa Allah, pia ni Mjumbe Wake na neno Lake.” Watakwenda kwa Issa na atawaambia, “Sitofanya mliyoniomba. Nendeni kwa Muhammad, mja ambaye amesamehewa madhambi yake yaliyotangulia na ya baadaye.” Watakuja kwangu, na nitakwenda kwa Mola Wangu kumuomba ruhusa na Atanipa Ruhusa. Nitakapomuangalia Mola Wangu, Nitasujudu na Allah Ataniruhusu nibaki hivyo kama Apendavyo. Kisha nitaambiwa, “Ewe Muhammad inua kichwa chako; omba, kwani utapewa utakachoomba, na maombezi yako yatakubaliwa.” Nitainua kichwa changu na nitamshukuru na kumsifu Allah kwa sifa Atakazonifundisha. Nitawaombea na Atanikubalia. Idadi maalumu Atawaingiza Peponi. Nitarejea Kwake tena, na nitakapomuona Mola Wangu, Nitawaombea na Atanikubalia idadi maalumu Atawaingiza Peponi. Nitafanya hivyo kwa mara ya tatu, na ya nne. Nitasema, “Hakuna watu waliobaki motoni isipokuwa wale ambao Qur’an imewafunga watabaki motoni milele.”¹ Hadithi hii ilikusanywa na Muslim, An-Nasai na Ibn Majah.²

Sababu ya kuitaja *Hadith* hii hapa ni kauli ya Mtume ﷺ,

«فَيَأْتُونَ آدَمَ فَيَقُولُونَ: أَنْتَ أَبُو النَّاسِ خَلَقَكَ اللَّهُ بِيَدِهِ وَأَسَجَدَ لَكَ مَلَائِكَتُهُ وَعَلَّمَكَ
أَسْمَاءَ كُلِّ شَيْءٍ»

“Watamuendea Adam na kumuambia! Wewe ni baba wa watu wote, Allah Alikuumba kwa Mikono Yake, Akawaamrisha Malaika wakusujudie na Akakufundisha majina ya kila kitu.”³

Sehemu hii ya Hadith inathibitisha kuwa Allah تعالى Alimfundisha Adam عليه السلام majina ya viumbe wote. Ndiyo sababu Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى الْمَلَائِكَةِ

“**Kisha Akaviweka mbele ya Malaika.**” Maana yake: Vitu na viumbe. Abdur-Razzaq alisimulia kuwa Ma’mar alisema kuwa Qatadah alisema, “Allah تعالى

¹ Fat’hul Al-Bari 8:10.

² Muslim 1:181, Nasai katika *Al-Kubra* 6:284.

³ Muslim 1:181, Nasai katika *Al-Kubra* 6:364 na Ibn Majah 2:1442.

Alivisimamisha vitu mbele ya Malaika.

فَقَالَ أَنْبِئُونِي بِأَسْمَاءِ هَؤُلَاءِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٠﴾

“Na Akasema, “Niambieni majina ya vitu hivi ikiwa mnasema kweli.”¹

Kauli ya Allah تعالى ina maana, nitajieni majina ya nilivyovisimamisha mbele yenu, Malaika ambao walisema,

أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ

“Utawaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu.”

Waliuliza, “Je, Unateua Khalifa kutoka kwetu au kutoka Viumbe wengine? Tunakushukuru na kukutukuza.” Kwa hiyo, Allah تعالى Alisema, “Kama mtasema ukweli, kuwa kama Nitamteua Khalifa duniani ambaye si malaika, yeye na kizazi chake waniasi, kufanya uharibifu na kumwaga damu, lakini endapo Nitawawekeni nyie kuwa Makhalifa, mtanitii, mtafuata Amri Zangu na Kuniheshimu na Kunitukuza. Hata hivyo, kwa kuwa hamjui majina ya vitu nilivyovisimamisha mbele yenu, basi hamjui chochote kitakachotokea juu ya dunia ambayo haipo.”

قَالُوا سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣١﴾

“Wakasema (Malaika): “Subhanaka. Wewe Umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa Uliyotufunza Wewe. Hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mwenye Hikima.”

Hapa Malaika wanamshukuru Allah تعالى Aliyetakasika na Kila Aina ya Upungufu, na wanathibitisha ya kuwa hapana kiumbe atakayepata sehemu ya Ujuzi wa Allah تعالى, isipokuwa kwa Utashi Wake, pia hakuna atakayejua chochote isipokuwa kile watakachofundishwa na Allah تعالى. Na kwa kuzingatia hilo walisema;

سُبْحَانَكَ لَا عِلْمَ لَنَا إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٣١﴾

“Subhanaka. Wewe Umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa Uliyo tufunza Wewe - Hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mwenye Hikima.”

¹ 'Abdur-Razzaq 1:42.

Maana yake: Allah تعالى ni Mjuzi wa kila kitu, Mwenye Hekima, kuhusu viumbe Vyake, na Anafanya Maamuzi yenye Hekima, na Anawafundisha na Anawanyima wengine elimu kama Apendavyo. Kwa hakika, Hikima na Uadilifu wa Allah تعالى katika mambo yote ni timilifu.

Udhihirisho wa Utukufu wa Adam kwa Sababu ya Elimu Aliyopewa na Allah.

Allah تعالى Amesema,

قَالَ يَتَقَادِمُ أَنْبِيَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ ۖ فَلَمَّا أَنْبَأَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبَ
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٣﴾

“Ewe Adam! Waambie majina yake. Alipowaambia majina yake Alisema (Mwenyezi Mungu), “Sikukuambieni kwamba Mimi Ninajua siri za mbingu na ardhi, tena Najua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha.” (2:33)

Zaid bin Aslam alisema, “Adam alitaja Wewe ni Jibril, wewe ni Mikail, wewe ni Israfil, mpaka akamtaja Kunguru.”¹ Mujahid alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

قَالَ يَتَقَادِمُ أَنْبِيَهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ

“Ewe Adam! Waambie majina yake.”

Jina la njiwa, kunguru na kila kitu. Kauli² zenye maana sawa na hii zilipokelewa kutoka kwa Said bin Jubayr, Al-Hasan na Qatada.³ Utukufu wa Adam عليه السلام ulipodhihirika, baada ya kutaja majina aliyofundishwa na Allah تعالى, Allah تعالى Aliwaambia malaika,

أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ غَيْبَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٣٣﴾

“Sikukuambieni kwamba Mimi Ninajua siri za mbingu na ardhi, tena Najua mnayoyadhihirisha na mliyokuwa mnayaficha.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:118.

² Ibn Abi Hatim 1:119.

³ Ibn Abi Hatim 1:119.

Ina maana: "Sikuwaambieni Najua yaliyo dhahiri na ya siri?" Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ مَجْهَرٌ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿٧﴾

"Na ukinyanyua sauti kwa kusema...basi hakika Yeye Anajua siri na duni kuliko siri." (20:7)

Aidha, Allah تعالى Alizungumzia Ndege Hudihudi aliyemuambia Sulayman عليه السلام:

أَلَّا يَسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبَاءَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ

﴿٢٥﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٢٦﴾

"Na hawamsujudii Mwenyezi Mungu Ambaye Huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi, na Anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza. Mwenyezi Mungu – hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi tukufu..." (27:25-26)

Walikuwa na maelezo mengine kuliko yale tuliyoyasema kuhusu maana ya Kauli ya Allah تعالى,

وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٢٧﴾

"Na Ninajua mnayo yadhahirisha na mliyokuwa mnayaficha."

Imepokewa kutoka kwa Adh-Dhahhak kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٢٧﴾

"Na Ninajua mnayoyadhahirisha na mliyokuwa mnayaficha."

Ina maana: "Najua siri, kama ninavyojua mambo ya dhahiri, kama vile, aliyoyaficha Iblis ndani ya moyo wake wa ufedhuli na majivuno.¹ Abu Ja'far Ar-Razi رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa,

وَأَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٢٧﴾

"Na Ninajua mnayoyadhahirisha na mliyokuwa mnayaficha."

¹ At-Tabari 1:498.

Maana yake: “Sehemu ya maneno ya dhahiri waliyosema yalikuwa, “Unaumba na kupeleka ambao watafisidi na kumwaga damu?” Maana ya maneno waliyoyaficha yalikuwa, “Tuna elimu na heshima zaidi ya kiumbe chochote atakachokiumba Mola wetu.” Lakini walikuja kujua kuwa Allah تعالی Alimfadhilisha Adam عليه السلام zaidi yao katika elimu na utukufu.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ

الْكٰفِرِيْنَ ﴿٣٤﴾

“Na Tulipowaambia Malaika - Msujudieni Adam, wakamsujudia wote isipokuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika makafiri.” (2:34).

Kutukuzwa Adam عليه السلام kwa Kusujudiwa na Malaika

Aya hii inaeleza heshima kubwa ya Adam عليه السلام aliyopewa na Allah تعالی, na Allah تعالی Akawakumbusha watoto wa Adam عليه السلام juu ya ukweli huo. Allah تعالی Aliwataka Malaika wasujudu mbele ya Adam عليه السلام, kama Aya hii na *Hadith* nyingi zinavyohibitisha, mojawapo ya *Hadith* inayohusu maombezi hayo tumeijadili. Kuna *Hadith* inayohusu maombi ya Musa عليه السلام, “Ewe Bwana Wangu! Nioneshe Adam ambaye alisababisha sisi na yeye kutolewa Peponi.” Musa عليه السلام alipokutana na Adam عليه السلام, alimuambia, “Wewe ndiye Adam ambaye Allah تعالی Alikuumba kwa Mikono Yake, Akakupulizia uhai na Akawaamrisha Malaika wakusujudie?”¹

Iblis Kuingia Miongoni mwa Walioamriwa Kumsujudia Adam عليه السلام, na Hakuwa Malaika.

Allah تعالی Alipowaamrisha Malaika wamsujudie Adam عليه السلام, Iblis alijumuishwa katika amri hii. Japokuwa Iblis hakuwa Malaika ila alishabihiana na wao katika kuiga tabia na vitendo vyao Malaika, na hii ndio sababu ya kuhusishwa katika amri ya Malaika ya kumsujudia Adam عليه السلام. Shetani alikosolewa kwa kutotii amri ile, kama tutakavyoielezea kwa urefu, Allah تعالی Akipenda, tutakapotaja Kauli ya Allah تعالی,

¹ Abu Dawud 5:28.

Desturi ya kusujudu iliruhusiwa na mataifa yaliyopita, lakini sisi tumekatazwa. Mu'adh رضي الله عنه alimuambia Mtume ﷺ, "Nilitembea Ash-Sham na nikakuta wanawasujudia makasisi na wanazuoni wao. Wewe Mtume ﷺ, unastahiki zaidi kusujudiwa." Mtume ﷺ akamuambia,

«لَا لَوْ كُنْتُ أَمِيرًا بَشَرًا أَنْ يَسْجُدَ لِبَشَرٍ لَأَمَرْتُ الْمَرْأَةَ أَنْ تَسْجُدَ لِزَوْجِهَا مِنْ عِظَمِ حَقِّهِ عَلَيْهَا»

*"Hapana, Lau ningetaka kumuamrisha binadamu amsujudie binadamu mwenzake, ningemuamrisha mke amsujudie mume wake kwa sababu ya haki nyingi juu yake."*¹

Ar-Razi رحمه الله تعالى alikubaliana na maoni haya.

Kiburi cha Iblisi.

Qatadah amesema katika kuifafanua Kauli Yake Allah تعالى،

فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَأَسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٥﴾

"Wakamsujudia wote isipokuwa Iblis, alikataa na akajivuna na akawa katika makafiri."

Iblis, adui wa Allah تعالى، alimuonea wivu Adam عليه السلام kwa sababu Allah تعالى Alimtukuza Adam عليه السلام. Alisema, "Nimeumbwa kutokana na moto, na yeye ameumbwa kutokana na udongo!" Kwa hiyo, kosa la kwanza kufanywa lilikuwa ni kiburi, kwani adui wa Allah تعالى alikuwa na kiburi sana kumsujudia Adam عليه السلام.² Mimi (Ibn Kathir) nasema yafuatayo yameandikwa katika Sahih.

«لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ حَبَّةٍ مِنْ خُرْدٍ مِنْ كِبَرٍ»

*"Hataingia Peponi ambaye ndani ya moyo wake ana kiburi uzito wa punje ya hardali."*²

¹ Tirmidhi 1109, *Majma' Az-Zawai'd* 4:310.

² Ibn Abi Hatim 1:123.

³ Muslim 1:93.

Iblis alikuwa kafiri, mwenye kiburi na muasi, yote haya yalimsababishia kufukuzwa kutoka katika Hadhara Tukufu ya Allah تعالى na Huruma Zake.

وَقُلْنَا يَتَقَادُمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ
الْشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٣٥﴾ فَأَزَلَّهُمَا الشَّيْطَانُ عَنْهَا فَأَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيهِ
وَقُلْنَا اهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتْنَعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٣٦﴾

35. *“Na Tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani, na Kuleni humo maridhawa Popote mpendapo lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale waliodhulumu.”*

36. *“Lakini Shetani aliwatelezesha hao wawili na akawatoa katika waliyokuwamo, na Tukasema, Shukeni nanyi ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Katika ardhi yatakuwa makazi yenu na starehe kwa muda.”*

Kutukuzwa kwa Adam عليه السلام Mara Nyingine

Allah تعالى Alimtukuza Adam عليه السلام kwa Kuwaamrisha Malaika wamsujudie, wote walitii isipokuwa Iblis. Kisha Allah تعالى Alimruhusu Adam عليه السلام aishi na kula mahali popote na chochote alichokitaka Peponi. Al-Hafidh Abubakar bin Marduawayh alimnukuu Abu Dharr رضي الله عنه akisema, “Nilimuuliza, Ewe Mjumbe wa Allah! Adam عليه السلام alikuwa Nabii?” Alijibu,

«نَعَمْ نَبِيًّا رَسُولًا كَلَّمَهُ اللَّهُ قُبَلًا»

“Ndiyo, alikuwa Nabii Mtume ambaye Allah Alizungumza naye mubashara.”

Alimuambia,

اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ

“Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani.”¹

¹ Al-Adhamah 5:1553.

Bi. Hawa Aliumbwa Kabla ya Adam عليه السلام Kuingia Peponi.

Aya (2:35) inaashiria kuwa Hawa aliumbwa kabla ya Adam عليه السلام hajaingia Peponi, kama alivyosema Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى. Ibn Ishaq رحمه الله تعالى amesema; "Baada ya Allah تعالى kumkosoa Iblis na baada ya Adam عليه السلام kutaja majina ya kila kitu, Alisema,

يَتَقَادَمُ أَنبِيُّهُمْ بِأَسْمَائِهِمْ^ط

"Ewe Adam! Waambie majina yake."

إِنَّكَ أَنْتَ أَعْلَمُ الْحَكِيمُ ﴿٣٦﴾

"Hakika Wewe Ndiye Mjuzi Mwenye Hikima."

Kisha Adam عليه السلام akatiwa usingizini, kama walivyoeleza Watu wa Kitabu cha Taurati na wanazuoni wengine kama Ibn Abbas رضي الله عنهما, Allah تعالى Alichukua ubavu mmoja wa kushoto wa Adam عليه السلام na Akafanya nyama iote mahali pake, wakati Adam عليه السلام akiwa usingizini na hafahamu chochote. Kisha Allah تعالى Akamuambia Adam عليه السلام mke, Hawa, kutokana na ubavu wake na Akamfanya mwanamke, ili awe liwazo kwake. Adam عليه السلام alipoamka alimuona Hawa pembezoni mwake, ilidaiwa kuwa alisema Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi, "Nyama yangu, damu yangu na mke wangu! Hivyo Adam عليه السلام akaegemeana na Hawa." Allah تعالى Alimuozesha Adam عليه السلام, Hawa, na Akampa utulivu, na kisha Allah تعالى Alimuambia Adam عليه السلام moja kwa moja,

يَتَقَادَمُ أَسْكُنَ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةَ

فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٣٧﴾

"Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani, na Kuleni humo maridhawa popote mpendapo lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale waliodhulumu."¹

¹ At-Tabari 1:514.

Allah تعالی Anampa Mtihani Adam عليه السلام na Mti wa Matunda na Aina Yake

Allah تعالی Alimuambia Adam عليه السلام,

وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةَ

“Lakini msiukaribie mti huu.” Ni mtihani kwa Adam عليه السلام kutoka kwa Allah تعالی. Kuna maoni yanayotofautiana kuhusu aina ya mti uliotajwa hapa. Baadhi walisema ulikuwa ni Mzabibu, Ngano, Mtende, M-tini na kadhalika. Wengine wanasema ulikuwa ni aina fulani ya mti, na yeyote atakayekula matunda yake hatokwenda haja. Pia ilielezwa ulikuwa mti ambao uliliwa na Malaika ili waishi milele. Imam Abu Ja’far bin Jarir رحمه الله تعالی alisema, “Rai iliyo sahihi ni kuwa Allah تعالی Hajataja chochote ndani ya Qur’an au Sunnah kuhusu aina ya mti huu. Ilisemwa ulikuwa Shayiri, Mzabibu au M-tini. Inayumkinika kuwa ulikuwa moja ya miti hiyo. Hata hivyo ni elimu isiyo na manufaa yoyote, kama ilivyo kutojua aina yake hakuleti madhara yoyote. Allah تعالی ni Mjuzi zaidi.”¹ Maoni Haya ni sawa na alivyodhukuru Ar-Razi رحمه الله تعالی katika *Tafsir* yake, na haya ndiyo maoni sahihi. Kauli ya Allah تعالی,

فَأَزَلَّهُمَا الشَّيْطَانُ عَنْهَا

“Lakini Shetani aliwatelezesha hao wawili.”

Hapa unaweza ukatafsiri ya kuwa Shetani aliwatelezesha na Pepo, kama ilivyo rai ya Asim bin Abi An-Naajud kwamba hiyo ilikuwa sababu ya kuondolewa Peponi.² Kadhalika unaweza ukatafsiri ya kuwa Shetani aliwatelezesha na mti huo wa matunda. Kama ilivyo rai ya Qataadah na Hasan³. Ni sawa na Allah تعالی Alivyosema,

يُؤْفِكُ عَنْهُ مَنْ أُفِكَ

“Angegeuzwa na haki kwa kauli hiyo mwenye kugeuzwa”. (51:9)

Ina maana: Mtu aliyeasi anageuzwa kutokana na haki kwa sababu kadha wa kadha. Hii ndio sababu Allah تعالی Alisema,

فَأَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيهِ

“Na Akawatoa katika waliyokuwamo.” Maana yake: Nguo, makazi bora kabisa na starehe inayodumu.

¹ At-Tabari 1:520.

² Ibn Abi Hatim 1:128.

³ Ibn Abi Hatim 1:128-129.

وَقُلْنَا أَهْبِطُوا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ وَلَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَمَتْنَعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٣٧﴾

“Na Tukasema - Shukeni nanyi ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Katika ardhi yatakuwa makazi yenu na starehe kwa muda.”

Maana yake: Kukaa na kupata riziki kwa muda mfupi mpaka itakapofika siku ya Ufufuo.

Wasifu wa Adam عليه السلام.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ubayy bin Ka'b عنه رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ خَلَقَ آدَمَ رَجُلًا طَوَّالًا كَثِيرَ شَعْرِ الرَّأْسِ كَأَنَّهُ نَخْلَةٌ سَحُوقٌ، فَلَمَّا ذَاقَ الشَّجَرَةَ سَقَطَ عَنْهُ لِبَاسُهُ فَأَرُّوْهُ مَا بَدَأَ مِنْهُ عَوْرَتُهُ، فَلَمَّا نَظَرَ إِلَىٰ عَوْرَتِهِ جَعَلَ يَشْتَدُّ فِي الْجَنَّةِ فَأَخَذَتْ شَعْرَهُ شَجَرَةٌ فَتَارَعَهَا، فَتَادَاهُ الرَّحْمَنُ: يَا آدَمُ مِنِّي تَغْرُبُ؟ فَلَمَّا سَمِعَ كَلَامَ الرَّحْمَنِ قَالَ: يَا رَبِّ لَا وَلَكِنِ اسْتَحْيَاءٌ»

“Allah Alimuumba Adam akiwa mrefu na nywele nyingi kichwani, kama mtende uliojaa matawi. Adam alipokula chakula kutoka mti aliokatazwa, nguo zake zilimvuka, na kitu cha mwanzo kuonekana ilikuwa ni sehemu zake za siri. Alipoona sehemu zake za siri alikimbilia peponi na nywele zake zikashikwa kwenye mti. Alijaribu kujinasua na Ar-Rahman Akamuita, “Ewe Adam! Unanikimbia?” Adam aliposikia maneno ya Ar-Rahman (Allah) alisema, “Hapana Mola Wangu! Lakini naona haya.”¹

Adam عليه السلام **Alikaa Peponi kwa Muda Kisha Akateremka Ardhini.**

Al-Hakim aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Adam عليه السلام aliruhusiwa kukaa Peponi katika kipindi baina ya Sala ya Alasiri mpaka machweo ya jua.” Al-Hakim alithibitisha kuwa Hadith hii ni sahihi kwa mujibu wa Shaikhain (Bukhari na Muslim). Lakini hawakuingiza katika makusanyo yao.² Aidha, Ibn Abu Hatim alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالى Alimteremsha Adam عليه السلام duniani katika sehemu inayoitwa, *Dahna*, kati ya Makkah na Taif.”³ Al-Hasan Al-Basri alisema kuwa Adam عليه السلام

¹ Ibn Abi Hatim 1:129.

² Al-Hakim 2:542.

³ Ibn Abi Hatim 1:131.

aliteremshwa India, wakati Hawa aliteremshwa Jeddah. Iblis alipelekwa Dustumaysar, umbali wa maili kadha kutoka Mji wa Basra. Zaidi ya hivyo nyoka alishushwa Asbahan. Haya yalipokewa toka kwa Abu Hatim.¹ Pia Muslim na an-Nasai waliandika kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«خَيْرُ يَوْمٍ طَلَعَتْ فِيهِ الشَّمْسُ يَوْمَ الْجُمُعَةِ فِيهِ خُلِقَ آدَمُ وَفِيهِ أُدْخِلَ الْجَنَّةَ وَفِيهِ أُخْرِجَ مِنْهَا»

“Siku bora iliyochomozewa jua ni Ijumaa. Humo aliumbwa Adam, alilingizwa peponi, na humo alitolewa Peponi (siku hiyo).”²

Utata na Jawabu Lake.

Endapo mmoja atauliza, “Iwapo Pepo aliyofukuzwa Adam عليه السلام iko mbinguni, kama Wanazuoni wengi wanavyosema, hivyo Iblis aliwezaje kuingia Peponi, ilihali alifukuzwa kwa Uamuzi wa Allah تعالى (alipokataa kumsujudia Adam)?”

Kwa msingi, jibu kwa suali hili litakuwa, Pepo aliyokuwemo Adam عليه السلام ilikuwa duniani na wala sio mbinguni, kama tulivyoeleza mwanzoni mwa kitabu chetu, *Al-Bidayah wa-Nnihayah*.

Wanazuoni wana majibu mengi, mojawapo ni kuwa, Shetani toka mwanzo alizuiwa kuingia Peponi, lakini kuna nyakati alipenya ndani kwa siri. Kwa mfano, Taurati inaeleza kuwa Iblis alijificha ndani ya kinywa cha nyoka na akaingia Peponi. Baadhi ya Wanazuoni walisema inawezekana Shetani aliwapoteza Adam عليه السلام na Hawa alipokuwa duniani, wakati wao walikuwa bado mbinguni, kama ilivyoelezwa na Az-Zamakshari رحمه الله تعالى, Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alitaja *Hadith* nyingi zenye faida kubwa kuhusu nyoka na hukumu ya kuwaua.

فَتَلَقَّى آدَمُ مِنْ رَبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

37. “Kisha Adam akapokea maneno kutoka kwa Mola Wake Mlezi, na Mola Wake Mlezi Alimkubalia toba yake; hakika Yeye Ndiye Mwingi wa Kukubali toba na Mwenye Kurehemu.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:132.

² Muslim 2:585 na Nasai 3:90.

Toba ya Adam عليه السلام na Maombi Yake kwa Allah تعالى.

Imepokewa kuwa Aya iliyo juu inatafsiriwa na Kauli ya Allah تعالى,

قَالَ رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾

“Wakasema: Mola Wetu Mlezi Tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutatusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kuhasirika.” (7:23)

Kama walivyosema Mujahid, Said bin Jubayr, Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas, Al-Hasan, Qatadah, Muhammad bin Ka'b Al-Quradhi, Khalid bin Ma'dar, Ata Al-Khurasani na Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam.¹ As-Suddi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo juu ya maneno,

فَتَلَقَىٰ آدَمُ مِن رَّبِّهِ كَلِمَاتٍ

“Kisha Adam akapokea maneno kutoka kwa Mola wake Mlezi.”

Adam عليه السلام akasema, “Ewe Mola! Hukuniumba kwa Mikono Yako Mwenyewe?” Akamjibu, “Ndiyo.” Akasema, “Na Ukanipulizia uhai?” Akasema, “Ndiyo” “Na nilipokwenda chafya, Ulisema, ‘Akurehemu Mwenyezi Mungu.” Na, “Huruma Yako Huzidi Hasira Zako?” Akajibiwa, “Ndiyo” Akasema, “Na Ukaniandikia nifanye hayo?” Akajibu, “Ndiyo.”² Akasema, “Endapo nitatubia, utanirejesha Peponi?” Allah تعالى Akasema, “Ndiyo”. Vile vile imepokewa kutoka kwa Al-Awfi, Said bin Jubayr, Said bin Ma'bad na Ibn Abbas رضي الله عنهم.³ Al-Hakim aliandika *Hadith* hii katika Mustadrak wake⁴ kutoka kwa Ibn Jubayr, ambaye alisimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Al-Hakim alisema, Silsila yake ni *Sahih* na wao (Al-Bukhari na Muslim) hawakuandika. Na Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٢٤﴾

“Yeye Ndiye Mwingi wa Kukubali toba na Mwenye Kurehemu.”

Maana yake: Allah تعالى Humsamehe yeyote anayejutia makosa na anayetubia Kwake. Ni kama Kauli Yake Allah تعالى,

¹ Ibn Abi Hatim 1:136 na At-Tabari 1:543,546.

² At-Tabari 1:543.

³ At-Tabari 1:542.

⁴ At-Tabari 2:545.

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

“Je, hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anapokea toba ya waja Wake...”. (9:104).

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake...” (4:110)

Aidha Kauli Yake،

وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا

“Na anayetubu na akafanya mema...” (25:71).

Aya zilizotajwa hapo juu zinathibitisha ukweli kuwa Allah تعالى Husamehe dhambi za yeyote anayetubia, Akio nesha Wema Wake na Huruma kwa viumbe na waja Wake. Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى، Msamehevu na Mwingi wa Rehema.

* * *

قُلْنَا أَهْبَطُوا مِنْهَا جَمِيعًا ۗ فَلَمَّا يَأْتِينَكُمْ مِّنِي هُدًى فَسَمِعَ تَعِ
 هُدَايَ فَلَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ
 كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
 خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾ يٰٓبَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ
 عَلَيْكُمْ وَأَوْفُوا بِعَهْدِي أُوْفٍ بِعَهْدِكُمْ وَإِنِّي فَارِهُونَ ﴿٤٠﴾
 وَءَامِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ وَلَا تَكُونُوا أَوْلَ
 كَافِرٍ بِهِ ۗ وَلَا تَشْتَرُوا بِآيَاتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَإِنِّي فَاتِقُونَ ﴿٤١﴾
 وَلَا تَلْبَسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْمُونَ ﴿٤٢﴾
 وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَءَاتُوا الزَّكَاةَ وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿٤٣﴾
 * أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ
 تَتْلُونَ الْكِتَابَ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾ وَأَسْمِعِينَا بِالصَّبْرِ
 وَالصَّلَاةِ ۗ وَإِنَّا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿٤٥﴾ الَّذِينَ
 يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقَوْنَ رَبَّهُمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٤٦﴾ يٰٓبَنِي
 إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ
 عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾ وَأَتَّقُوا يَوْمًا لَا تَجْزِي نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ
 شَيْفًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا شَفَعَةٌ وَلَا يُؤْخَذُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا هُمْ
 يُنصَرُونَ ﴿٤٨﴾

قُلْنَا أَهْبَطُوا مِنْهَا جَمِيعًا ۗ فَلَمَّا يَأْتِينَكُمْ
 مِّنِي هُدًى فَسَمِعَ تَعِ هُدَايَ فَلَا
 خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ
 أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

38. "Tukasema: Shukeni nyote; na kama ukufikieni uongofu utokao Kwangu, basi watakoafuata uongofu Wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawata-huzunika."

39. "Na wenye kukufuru na kuzikanusha ishara Zetu, hao ndio watako kuwa watu wa Motoni, humo watadumu".

Allah تعالیٰ Ameeleza Alipowapeleka duniani kutoka Peponi, Adam عليه السلام, Hawa na Shetani, Aliwawonywa kuwa Atateremsha Vitabu na kutuma Mitume na Wajumbe kwao, maana kwa vizazi vyao. Abu 'Aliyah alisema, uongofu "Al-Huda",

inakusudiwa Manabii na Mitume, alama na ishara zilizo wazi na maelezo mepesi.¹

¹ Ibn Abi Hatim 1:139.

فَمَنْ تَبِعَ هُدَايَ

“Basi watakaofuata uongofu.”

Maana yake: Yeyote atakayeyakubali yaliyomo ndani ya Vitabu Vyangu na Nilichowapeleka nacho Wajumbe Wangu.

فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“Haitakuwa khofu juu yao.” Kuhusu Kiyama.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٢٣﴾

“Wala hawatahuzunika.”

Kuhusiana na maisha ya hapa duniani. Vile vile katika *Surat Ta Ha*, Allah تعالى Amesema,

قَالَ أَهْبِطَا مِنْهَا حَمِيمًا ۖ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنِ اتَّبَعَ

هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَى ﴿١٢٤﴾

“Akasema: Ondokeni humu nyote, hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Na ukikufikieni uwongofu kutoka Kwangu basi atakayeufuata uwongofu Wangu, hatapotea wala hatatabika.”
(20:123)

Ibn Abbas رضي الله عنهما ameitolea maelezo, “Hatapotea katika maisha ya hapa duniani au kubabaika siku ya Kiyama.”¹ Aya inayofuatia inasema,

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾

“Na, atakayejipusha na mawaidha Yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya Kiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu.” (20:124)

Kama Allah تعالى Alivyosema Hapa,

¹ At-Tabari 18:389.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٤٠﴾

“Na wenye kukufuru na kuzikanusha ishara Zetu, hao ndio watakao kuwa watu wa Motoni, humo watadumu.”

Ina maana: Watabaki Motoni milele na hawatapata njia ya kutoka.

يَذَرِيْنَ إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَوْفُوا بِعَهْدِي أُوفِ بِعَهْدِكُمْ وَإِيَّايَ فَارْهَبُونِ ﴿٤١﴾ وَءَامِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ وَلَا تَكُونُوا أَوَّلَ كَافِرٍ بِهِ ۗ وَلَا تَشْتَرُوا بِآيَاتِي ثَمَنًا قَلِيلًا وَإِيَّايَ فَاتَّقُونِ ﴿٤٢﴾

40. “Enyi Wana wa Israil! Kumbukeni Neema Zangu, Nilizoku-neemesheni na tekelezeni Ahadi Yangu na Mimi Nitatimiza ahadi yenu, na Niogopeni Mimi tu”.

41. “Na Aminini Niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha mliyo nayo, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiuze Ishara Zangu kwa thamani ndogo. Na Niogopeni Mimi tu.”

Wana wa Israel Wanahimizwa Kuupokea Uislam.

Allah تعالى Aliwaamrisha Wana wa Israel kuupokea Uislam na kumfuata Muhammad ﷺ.

Pia Aliwakumbusha mfano wa baba yao Israel, Mtume wa Allah Ya'qub عليه السلام, kama alikuwa anasema, “Enyi watoto wa mchamungu, mja mwadilifu wa Allah Aliyemtii Allah! Kuweni kama baba yenu katika kufuata ukweli.” Kauli hii ni sawa na ile isemayo, “Ewe mtoto wa yule mtu mkarimu”, au “Ewe mtoto wa mwanazuoni, tafuta elimu”, na kadhalika.

Hivyo, Allah تعالى Amesema,

ذُرِّيَّةَ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿٤٣﴾

“Enyi kizazi Tuliowachukua pamoja na Nuhu! Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.” (17:3)

Israel ni lakabu - Jina la Kupanga, Jina Halisi ni Ya'qubu عليه السلام.

Israel ni Mtume Ya'qubu عليه السلام kwa uthibitisho wa simulizi, Abu Dawud At-Tayalisi alipokea kuwa Abdullah Ibn Abbas عنهما رضي الله alisema, "Kundi la Mayahudi walikuja kwa Mtume ﷺ na aliwaambia,

«مَلَّ تَلْمُؤَنَ أَنَّ إِسْرَائِيلَ يَغْفُوبُ؟»

"Je, mnajua kuwa Israel ni Ya'qub?"

Wakamjibu, "Ndiyo, Wallahi" Mtume ﷺ alisema kuwaambia,

«اللَّهُمَّ اشْهَدْ»

"Ewe Allah, shuhudia."¹

At-Tabari رحمه الله تعالى ameandika kuwa Abdullah ibn Abbas عنهما رضي الله amesema kuwa, "Israel maana yake ni: "Mja wa Allah."²

Neema za Allah تعالى kwa Wana wa Israel.

Allah تعالى Amesema,

أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ

"Kumbukeni Neema Yangu, Nilizokuneemesheni..."

Mujahid alielezea Aya hii, "Neema Alizowapa Allah تعالى Mayahudi ni kuwa Aliyafanya maji kububujika kutoka katika mawe, Aliwateremshia *Manna* na *Salwa*, na Aliwaokoa kufanywa Watumwa na Firauni."³

Abu Al-Aliyah pia alisema, "Neema za Allah تعالى zilizotajwa hapa ni Kupeleka Kwake Mitume na Wajumbe miongoni mwao, na Kuwateremshia Vitabu."⁴

Mimi (Ibn Kathir) nasema kuwa Aya hii ni sawa na vile Musa عليه السلام alivyowaambia Wana wa Israeli,

¹ Musnad At-Tayalisi Na. 356

² At-Tabari 1:553.

³ At-Tabari 1:556.

⁴ At-Tabari 1:556.

يَنْقُورِ أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُلُوكًا وَءَاتَاكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ ﴿٢٠﴾

“Enyi watu wangu! Kumbukeni Neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowateua Manabii kati yenu na Akakufanyeni watawala, na Akakupeni ambayo Hakuwapa wowote katika walimwengu.” (5:20)

Ina maana: Kwa zama zao. Aidha Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, kuhusu Kauli Yake تعالى,

أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ

“Kumbukeni Neema Yangu, Nilizokuneemesheni...”

Maana yake: “Msaada Wangu kwenu na baba zenu.” Hayo ni wakati Alipowaokoa kutoka kwa Firauni na watu wake.

Wana Israeli Wanakumbushwa Ahadi Waliyopewa na Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى,

وَأَوْفُوا بَعْدِي أَوْفٍ بِعَهْدِكُمْ

“Na timizeni Ahadi Yangu na Mimi Nitatimiza ahadi yenu.”

Ina maana: “Ahadi Yangu Niliyokupeni kuhusu Muhammad ﷺ, atakapotumwa kwenu, Nitakupeni Niliyowaahidi endapo mtamuamini na kumfuata.

Kisha nitaondoa minyororo na vikwazo vilivyowekwa shingoni mwenu, kutokana na makosa mliyoyafanya.¹

Pia Al-Hasan Al-Basri² رحمه الله تعالى alisema, “Ahadi” inarejea Kauli ya Allah تعالى,

¹ At-Tabari 1:555 na 557.

² At-Tabari 1:109.

﴿ وَلَقَدْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَوَعَّضْنَا مِنْهُمْ اثْنَيْ عَشَرَ نَفِيسًا ۗ وَقَالَ اللَّهُ إِنِّي مَعَكُمْ ۖ لَئِنْ أَقَمْتُمُ الصَّلَاةَ وَآتَيْتُمُ الزَّكَاةَ وَآمَنْتُمْ بِرُسُلِي وَعَزَّرْتُمْهُمْ وَأَقْرَضْتُمُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا لَأُكَفِّرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَلَأُدْخِلَنَّكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ ﴾

“Na Mwenyezi Mungu Alifanya agano na Wana wa Israeli. Na Tukawateua kutokana nao wakuu kumi wa wawili. Na Mwenyezi Mungu Akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja Nanyi. Mkisali, na mkatoa Zaka na mkawaamini Mitume Wangu, na mkawasaidia, na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, hapana shaka Nitakufutieni maovu yenu na Nitakuingizeni katika bustani zipitazo mito kati yake.” (5:12)

Wanazuoni wengine walisema, “Ahadi Aliyoichukua Allah تعالی katika Taurati, ni kuwa Atampeleka Mtume Mkuu (Maana: Muhammad ﷺ) kutokana na kizazi cha Ismaili عليه السلام, ambaye atasikilizwa na watu wote. Kwa hiyo yeyote atakayemuamini, Allah تعالی Atamsamehe dhambi zake, Atamuingiza Peponi na Atampa zawadi mbili.” Inafaa tutaje hapa kuwa Ar-Razi رحمه الله تعالی alitaja taarifa na Ishara mbalimbali zilizotolewa na Mitume wa mwanzo kuhusu kuja kwa Muhammad ﷺ. Zaidi ya hayo, Abu Al-Aliyah alisema kuwa,

وَأَوْفُوا بِعَهْدِي

“Na timizeni Ahadi Yangu...”

Ina maana: “Ahadi Yake na waja Wake ni kuupokea Uislam na kudumu humo.”¹

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, *“Nititimiza Ahadi Yangu kwenu.”* Maana yake, “Mimi (Allah) Nitawaridhia na Nitakuingizeni Peponi.”²

As-Suddi, Adh-Dhahhak, Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi bin Anas walisema vivyo hivyo. Na Kauli Yake Allah تعالی,

¹ At-Tabari 1:558.

² Ibn Abi Hatim 1:143.

وَأَيُّهَا فَآرْهَبُونَ ﴿٣٨﴾

“Na Niogopeni Mimi tu”.

Maana: Mniogope. Abu Al-Aliyah, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na Qatadah wamesema hivyo.

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى, **“Na Niogopeni Mimi tu.”** Ina maana: “Ogopeni mateso ambayo huenda Nikawapa kama Nilivyowafanyia baba zenu, kama vile mabadiliko, n.k.”¹ Aya hii inashajiisha na ina maonyo. Mwanzo Allah تعالى Aliwaita Wana wa Israel Akitumia maneno ya Kushajiisha, kisha Akawaonya, ili warejee kwenye ukweli na kumfuata Mjumbe na kuwaidhika na mafundisho ya Qur’an, na makatazo Yake, na kufuata Amri Yake, na kusadikisha habari Zake. Kwa hakika, Allah تعالى Huwaongoza Awatakao katika njia iliyonyooka. Kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

وَأَمِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ

“Na aminini Niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha mliyonayo (Taurati na Injili).”

Ina maana: Qur’an ambayo Allah تعالى Alimteremshia Muhammad ﷺ, Mtume Mwarabu asiyejua kusoma na kuandika, kama mletaji habari zinazofurahisha, Mwonyaji na taa yenye nuru. Qur’an ina ukweli kutoka kwa Allah تعالى na inathibitisha yaliyoteremshwa kabla ndani ya Taurati na Injili. Abu – Aliyah alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

وَأَمِنُوا بِمَا أَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ

“Na aminini Niliyoyateremsha ambayo yanasadikisha mliyonayo (Taurati na Injili).”

Ina maana: “Enyi Watu wa Kitabu! Aminini Nilichokuteremshieni kinachokubaliana na mlicho nacho.” Hii ni kwa sababu wanakuta maelezo yanamhusu Muhammad ﷺ yaliyoandikwa ndani ya Taurati na Injili. Kauli za aina hiyo zilinasibishwa na Mujahid, Ar-Rabi bin Anas na Qatadah. Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:144.

وَلَا تَكُونُوا أَوَّلَ كَافِرٍ بِهِ^ط

“Wala msiwe wa kwanza kuyakataa.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Aya hii, Msiwe wa kwanza kukanusha yaliyomo ndani ya Qur’an (Au Muhammad ﷺ), wakati mnafahamu zaidi kuliko watu wengine.¹ Abu Al-Aliyah alitoa *Tafsiri*, “Msiwe wa kwanza kutomuamini Muhammad ﷺ.” Ikiwa na maana kutoka miongoni mwa Watu wa Kitabu, “Baada ya kusikia kuwa alitumwa kama Mtume.² Kauli sawa na hizo zilitolewa na Al-Hasan, As-Suddi na Ar-Rabi bin Anas. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alieleza kuwa Kauli Yake Allah تعالى, **‘kuyakataa’** (2:41) inakusudiwa Qur’an iliyotajwa mapema katika Aya,

بِمَا أَنْزَلْتُ

“Niliyoyateremsha (Qur’an hii)...”

Kauli zote ni sahihi kwa sababu zinahusiana. Kwa kuwa, yeyote asiyeamini Qur’an atakuwa hamuamini Muhammad ﷺ, na yeyote asiyemuamini Muhammad ﷺ atakuwa haiamini Qur’an. Kauli ya Allah تعالى,

أَوَّلَ كَافِرٍ بِهِ^ط

“Wa kwanza kuyakataa.”

Maana yake: Msiwe wa kwanza miongoni mwa Wana wa Israeli kuyakataa, kwani walikuwepo watu kutokana na Maquraysh na Waarabu kwa ujumla waliomkataa Muhammad ﷺ kabla ya kukataliwa na watu wa Kitabu. Lazima tueleze hapa kuwa Aya hii inawahusu wana wa Israeli tu, kwa sababu Mayahudi waliokuwepo Madinah, walikuwa wa kwanza miongoni mwa Wana wa Israeli kufikiwa na Qur’an. Hivyo kukataa kwao Qur’an ina maana walikuwa wa kwanza miongoni mwa Watu wa Kitabu kukataa. Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَشْتَرُوا بِعَآيَتِي ثَمَنًا قَلِيلًا

“Wala msiuze Ishara Zangu kwa thamani ndogo.”

Ina maana, “Msiache kuamini Aya Zangu na kumuamini Mtume Wangu kwa maisha ya dunia na furaha yake ya muda mfupi ambayo haidumu.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:145.

² Ibn Abi Hatim 1:145.

Allah تعالی Amesema,

وَإِنِّي فَاتَّقُونَ ﴿٤١﴾

“Na Niogopeni Mimi tu.”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالی alipokea kutoka kwa Talq bin Habib alisema, “Uchamungu “*Taqwa*” ni kumtii Allah تعالی, kwa kutarajia rehema za Allah, kwa nuru ya Allah, na kutomuasi, kwa kuogopa adhabu ya Allah تعالی.¹ Kauli ya Allah تعالی,

وَإِنِّي فَاتَّقُونَ ﴿٤١﴾

“Na Niogopeni Mimi tu.” Ina maana: Allah تعالی Aliwaonya watu wa Kitabu dhidi ya ufichaji wa ukweli na kueneza upinzani kwa makusudi, vile vile, dhidi ya kumuasi Mjumbe.

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْمُونَ ﴿٤٢﴾ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا
الزَّكَاةَ وَأَرْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿٤٣﴾

42. “Wala msichanganye ukweli na uwongo na mkauficha ukweli nanyi mnaujua.”

43. “Na shikeni Sala, na toeni Zaka; na inameni pamoja na wanaoinama.”

Kukatazwa Kuuficha Ukweli na Kuupotosha.

Allah تعالی Aliwakataza Mayahudi kutochanganya haki na batili na kupotosha ukweli kwa makusudi na kuuficha ukweli na kueneza upotofu,

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْمُونَ ﴿٤٢﴾

“Wala msichanganye ukweli na uwongo na mkanificha ukweli nanyi mnaujua.” (2:42)

Hivyo Allah تعالی Aliwakataza mambo mawili kwa pamoja; Aliwalazimisha kudhihirisha ukweli, na pia kuuelezea. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliitaja Aya,

¹ Ibn Abi Hatim 1:147.

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ

“Wala msichanganye ukweli na uwongo.”

Maana yake: “Msichanganye ukweli na batili na ukweli na uongo.”¹ Qatadah alisema kuwa,

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ

“Wala msichanganye ukweli na uwongo.”

Ina maana: “Msichanganye Uyahudi, Ukristo na Uislam.”

وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

“...nanyi mnaujua.”

Kuwa Dini ya Allah تعالى ni Uislamu na kuwa Uyahudi, Ukristo ni bidaa na uzushi si katika muongozo wa Allah تعالى.² Iliripotiwa kuwa Al-Hasan Al-Basri alisema vivyo hivyo.³ Aidha, Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

“...na mkauficha ukweli nanyi mnaujua.”

Maana yake, “Msifiche kujua kwenu kuwa mnaye Mjumbe Wangu na ujumbe Tuliompa. Wasifu wake ambao mnaujua umeandikwa kwenye Vitabu mlivyonavyo.”⁴

Nikasema mimi bin Kathir, Inawezekana pia ina maana kuwa, “Japokuwa mnajua madhara makubwa ambapo uovu utawasababishia watu kupotoka na kuwafanya waingie Motoni, kwa sababu Walifuata upotofu uliochanganyika na ukweli katika madai yenu.” **“Na mkauficha ukweli nanyi mnaujua..”** Muqatil anasema, “Allah تعالى Aliwaambia Watu wa Kitabu,

¹ Ibn Abi Hatim 1:147.

² At-Tabari 1:569.

³ Ibn Abi Hatim 1:107.

⁴ Ibn Abi Hatim 1:147.

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ

“Na shikeni Sala.”

Anawaamrisha wasali nyuma ya Mtume ﷺ.

وَأَتُوا الزَّكَاةَ

“Na toeni Zaka.”

Anawaamrisha walipe Zaka kwa Mtume ﷺ. Na,

وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿١٤٦﴾

“Na inameni pamoja na wanaoinama.”

Anawaamrisha wainame pamoja na wanaoinama miongoni mwa Ummah wa Muhammad ﷺ.¹ Kwa nyongeza, Allah تعالى Anasema,

وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿١٤٦﴾

“Na inameni pamoja na wanaoinama.”

Maana yake: “Na muwe miongoni mwa waumini wanaotenda amali njema kwa ufanisi, ambayo ya kwanza ni Sala.”

Wanazuoni wengi wanasema Aya (2:43) ni uthibitisho wa ulazima wa kusali kwa jamaa (kwa wanaume tu).

Nitaelezea hukumu hii kwa kirefu katika, kitabu *Al-Ahkam Al-Kabir*, Allah تعالى Akipenda.

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴾

44. “Je, Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu hali mnasoma Kitabu (cha Allah) Basi Je Hamfahamu.”

¹ Al-Kashaf 1:133.

Kulaumu Kitendo cha Kuamrisha Wengine Kutenda Mema na Kuacha Nafsi Yake.

Allah تعالى Amesema, “Inakuwaje, enyi Watu wa Kitabu, mnaamrisha watu kufanya wema *Al-Birr*, ambao unajumuisha kila aina ya uadilifu, kisha mnajisahau, hamuyafuati yale mnayowalingania wengine? Na mnasoma kitabu cha Allah تعالى (Taurati) na mnajua walichoahidiwa wale walioshindwa kutekeleza Maamrishi ya Allah تعالى.”

أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

“...Basi je, hamzingatii.”

Mnayo jifanyia wenyewe, ili muweze kuzindukana kwenye usingizi na mkarejea kwenye mwanga? Abdur-Razaq alisema kuwa Maamar alieleza kuwa Qatadah alitoa maoni juu ya Kauli ya Allah تعالى,

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ ﴾

“Je, Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu...”

Wana wa Israeli walikuwa wakiwaamrisha watu kumtii Allah تعالى, kumuogopa Allah تعالى na kufanya *Al-Birr*. Bado walikwenda kinyume na amri hizi, hivyo Allah تعالى Akawakumbusha ukweli huu.¹ As-Suddi na Ibn Jurayj walisema kuwa Aya,

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ ﴾

“Je, Mnawaamrisha watu kutenda mema...”.

Ni juu ya Watu wa Kitabu na wanafiki. Walikuwa wakiwaamrisha watu kusali na kufunga. Hata hivyo wao hawakutekeleza waliyowaamrisha wengine. Allah تعالى Aliwakumbusha juu ya tabia hii. Hivyo yeyote anayewaamrisha watu kufanya mema, basi naye awe wa kwanza kutekeleza amri hiyo.² Aidha, Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

¹ Abdur-Razaq 1:44.

² At-Tabari 2:8.

وَتَنَسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ

“Na mnajisahau nafsi zenu...”

Ina maana mnasahau wenyewe kutekeleza.

وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٨﴾

“Na hali nyinyi mnasoma Kitabu (Taurati)? Basi je, hamzingatii?”

Mnawakataza watu kukataa Utume na ahadi iliyotajwa ndani ya Taurati, wakati nyie wenyewe mmeshaisahau, maana yake mmeisahau ahadi Niliyofanya nanyi kuwa mtampokea Mjumbe Wangu. Mmevunja Ahadi Yangu na mmekataa mnachokijua kilichomo ndani ya Kitabu Changu.¹ Kwa hiyo Allah تعالى Aliwarudi Mayahudi kwa mwenendo wao na Akawazindua kwa makosa yanayowahusu wao wenyewe, kwa kuamrisha maadili mema, na wala hawayatekelezi. Tunawajibu na kutamka kuwa Allah تعالى Hawakosoi Watu wa Kitabu kwa kuamrisha mema na kuacha kuyatekeleza bali wanalaumiwa kwa kuacha kuyatekeleza hayo mema, kwa sababu kuamrisha mema ni sehemu ya uadilifu na ni jukumu la wanazuoni. Hata hivyo, mwanazuoni mwenyewe anatakiwa kufuata na kushikamana na kile anachokihubiri. Kwa mfano, Mtume Shu'ayb عليه السلام alisema,

وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَا أَنْهَيْتُمْ عَنْهُٓ إِنَّا نُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَمَا

تَوْفِيقِي إِلَّا بِاللَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿٨٨﴾

“...Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyoweza. Na Sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ninategemea, na Kwake Yeye naelekea.” (11:88)

Kwa hiyo kuamrisha mema na kufanya mema, vyote vinahitajika. Hakuna lisilo la muhimu kwa kutenda mojawapo na kuacha jingine, kwa mujibu wa rai sahihi kabisa ya wanazuoni miongoni mwa *Salaf* na *Khalaf*.²

¹ At-Tabari 2:7.

² Hawa ni Wanazuoni waliokuja baada ya kupita kizazi cha tatu.

Imamu Ahmad alipokea kuwa Abu Wa'il alisema, "Nilipopanda mnyama nyuma ya Usamah رضي الله عنه, aliulizwa, "Kwa nini humshauri Uthman رضي الله عنه?" Akamjibu, "Unadhani nitapomshauri nitakupa fursa usikie? Nitamshauri kwa siri na sitoanzisha kitu ambacho nitakuwa wa mwanzo kukianzisha. Sitomuambia mtu; "Wewe ni bora", hata kama angekuwa kiongozi wangu, baada ya kusikia kutoka, kwa Mtume ﷺ akisema. Wakauliza, "Alisema nini?" Akasema, "Nilimsikia akisema,

«بِجَاءِ بِالرَّجُلِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَيُلْقَى فِي النَّارِ فَتَنْدَلِقُ بِهِ أَقْتَابُهُ فَيَدُورُ بِهَا فِي النَّارِ كَمَا يَدُورُ الْحِمَارُ بِرَحَاهُ فَيُطِيفُ بِهِ أَهْلُ النَّارِ فَيَقُولُونَ: يَا فُلَانُ مَا أَصَابَكَ؟ أَلَمْ نَكُنْ نَأْمُرُنَا بِالْمَعْرُوفِ وَنَنْهَانَا عَنِ الْمُنْكَرِ؟ فَيَقُولُ: كُنْتُ أَمْرُكُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَلَا آتِيَهُ وَأَنْهَأَكُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَآتِيَهُ»

"Mtu ataletwa siku ya Kiyama na kutupwa Motoni. Matumbo yatamwagika na ataendelea kuzunguka huku akiburuza matumbo yake, kama ambavyo punda anavyozungusha Jiwe la kusagia. Watu wa Motoni watamuendea na kumuuliza, "Ewe fulani! Umepatwa na nini? Haukuwa ukituamrisha kutenda mema, na kutukanya kufanya maovu?" Atajibu, "Nilikuwa nikiamrisha mema, lakini sikuwa nafanya mambo mema, na nilikuwa nikiwaonya msifanye maovu wakati mimi mwenyewe nikiyafanya."

Hadithi hii iliandikwa pia na Al-Bukhari na Muslim.¹ Pia, Ibrahim An-Nakhai alisema, "Nasita kuwashauri watu kutokana na Aya tatu; Kauli Yake Allah تعالی,

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ

"Mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu."

Na Kauli Yake Allah تعالی,

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦١﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا

لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦٢﴾

"Enyi mlio amini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda? Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyoyatenda." (61:2-3)²

¹ Fat'hul Al-Bari 6:381, Muslim 4:2291 na Ahmad 5:205.

² Al-Qurtubi 1:367.

Na Allah تعالى Alitufahamisha kuwa Mtume Shu'ayb عليه السلام alisema,

وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَا أَنْتَهُكُمْ عَنْهُ ۚ إِنَّ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ مَا اسْتَطَعْتُ ۚ وَمَا تَوْفِيقِي إِلَّا بِاللَّهِ ۗ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿٣٨﴾

“...Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayo kukatazeni sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyo weza. Na sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ninategemea, na Kwake Yeye naelekea.” (11:88)

وَأَسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ ۚ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿٣٩﴾ الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا رَبِّهِمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٤٠﴾

45. “Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.”

46. “Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake.”

Kuomba Msaada kwa Subira na Sala.

Allah تعالى Amewaamrisha waja Wake kusubiri na kusali, ili kupata maisha mazuri ya duniani na kesho Akhera, “Fanya subira na Sali Sala za Faradhi kwa kuitafuta Akhera.” Hii ndio maana ya Aya hii kwa mujibu wa Muqatil bin Hayyan. Na subira hapa imetumika kwa maana ya Saumu.¹ Kuna maandishi yenye maana hiyo yaliyoandikwa na Mujahid. Al-Qurtubi رحمه الله تعالى na wanazuoni wengine wametoa maoni, “Hii ndio sababu Ramadhan imeitwa mwezi wa subira.”² Kama ilivyoelezwa na *Hadith*. Imeelezwa kuwa “subira” katika Aya hii ina maana, kujiepusha na maovu, na hii ndio sababu “Subira” imetajwa pamoja na kufanya vitendo vya ibada, hususan, Sala. Aidha Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Umar bin Al-Khattab عنه رضي الله عنه alisema, “Kuna aina mbili za subira: Subira nzuri wakati yanapotokea maafa, na subira nzuri zaidi wakati wa kuepuka yaliyokatazwa na Allah تعالى.” Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisema kuwa Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى aliripotwa kusema sawa na haya.³ Ama Kauli Yake Allah تعالى,

¹ Ibn Abi Hatim 1:154.

² Al-Qurtubi 1:372.

³ Ibn Abi Hatim 1:155.

وَالصَّلَاةِ

“Na Sala.” Sala ni moja ya njia bora za kupata msaada kwa kushikamana na maamrishi ya Allah تعالى, kama Allah تعالى Alivyosema,

أَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ ۖ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ
وَالْمُنْكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ

“Soma uliyofunuliwa katika Kitabu na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa.” (29:45)

Kiwakilishi nomino cha nafsi ya kwanza katika Aya,

وَأَنَّهَا لَكَبِيرَةٌ

“Na kwa hakika jambo hilo ni gumu.” Kinaashiria Sala, kama Mujahid alivyosema, na pia mtazamo wa Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Kadhalika inayumkinika kuwa kiwakilishi nomino kikawa kinaashiria nasaha katika kusubiri na kusimamisha Sala – kulikotajwa katika Aya hiyo hiyo. Hii ni sawa na Kauli Yake Allah تعالى katika kusimulia kisa cha Qarun,

وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ ثَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ لِّمَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا وَلَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الصَّابِرُونَ ﴿٤١﴾

“Na wakasema wale waliopewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira.” (28:80)

Pia Allah تعالى Alisema,

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ۗ ادْفَعِ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٤٢﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٤٣﴾

“Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa kila jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki na jamaa wa kukuonea chungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanaosubiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.” (41:34-35)

Ina maana, Nasaha hizi hutekelezwa na wale wenye kusubiri na wenye hadhi. Kwa vyovyote vile iwavyo. Kauli ya Allah تعالى, “...**na jambo hili ni gumu...**” lina maana, Sala ni, “nzito na ni mzigo.”

إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿٣٨﴾

“Isipokuwa kwa Al-Khashi’in (wanyenyekevu).”

Ibn Abu Talhah alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maoni juu ya Aya hii, “Wao (Al-Khashi’in) ni wale wanaoamini yale yaliyoteremshwa na Allah تعالى.”¹ Kauli ya Allah تعالى,

الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا رَبِّهِمْ وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٣٩﴾

“Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea Kwake.”

Anaendeleza somo lililoanza katika Aya iliyopita. Kwa hiyo, Sala, au subira ni nzito,

إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿٤٠﴾ الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا رَبِّهِمْ

“Isipokuwa kwa wanyenyekevu. Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi...”

Maana yake: Wanajua kuwa watakusanywa na kukutana na Mola wao siku ya Kiyama.

وَأَنَّهُمْ إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٤١﴾

“Na ya kuwa hakika watarejea Kwake.”

Maana yake, mambo yao yanategemea Utashi Wake, na Huamua kama Apendavyo. Kwa kuwa wana uhakika kuwa atarejeshwa kwa Allah تعالى na kuhesabiwa, ni rahisi kwao kufanya vitendo vya kuonesha utiifu na kuacha yaliyokatazwa. Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameeleza Kauli ya Allah تعالى,

يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا رَبِّهِمْ

“Wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao.”

¹ At-Tabari 2:16.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema; "Waarabu wanaita *"yakini"* na pia *"wasiwasi"*, *"Dhwann"*. Kuna hali nyingine pia katika lugha ya Kiarabu wakati kiima na kinyume chake vinakuwa na maana sawa. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

وَرَاءَ الْمَجْرُمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَاقِعُوهَا

"Na wakhaliifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo..." (18:53)

Neno *"Dhwann"* limetumika kwa maana ya yakini. Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Mujahid amesema; Kila neno *"Dhannu"* katika Qur'an lina maana ya *Yakini* na kujua.

Na kauli hii Sanadi yake ni Sahihi. Mimi bin Kathir ninasema; Imeandikwa ndani ya Sahih kuwa siku ya Kiyama, Allah تعالى Atamuambia mja Wake, "Sikukuruhusu kuoa, nikakupa heshima, nikawafanya farasi na ngamia kukutumikia na nikakufanya mkuu na bwana?" Atasema, "Ndiyo."

Allah تعالى Atamuambia, "Ulifikiria (*Dhann*) kuwa utakutana na Mimi?" Atajibu, "Hapana" Allah تعالى Atamuambia, "Siku hii, Nitakusahau kama ulivyonisahau Mimi."¹

Allah Akipenda, tutalifafanua somo hili wakati tutakapoelezea Kauli ya Allah.

سُئِلَ اللَّهُ فَتَسَبَّهَهُمْ

"...Wamemsahau Mwenyezi Mungu, basi na Yeye pia Amewasahau..." (9:67)

يَنْبِيَّ إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٦٧﴾

47. "Enyi wana wa Israeli! Kumbukeni zile Neema Zangu Nilizo Kuneemesheni, na Nikakutukuzeni kuliko viumbe wote wengineo (wa wakati huo)."

¹ Muslim 4:2279.

Kuwakumbusha Wana wa Israeli Kufadhilishwa Kwao Kuliko Mataifa Mengine.

Allah تعالى Anawakumbusha Wana wa Israeli Fadhila Alizowapa baba na babu zao, Aliwapa kipaumbele Alipowateua Manabii miongoni mwao na Akawateremshia Vitabu, zaidi ya Alivyowafanyia Ummah uliotangulia. Vivyo hivyo, Allah تعالى Anasema,

وَلَقَدْ آخَرْتَنَّهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ عَلَىٰ الْعَالَمِينَ ﴿٤٤﴾

“Na Tukawachagua kwa Ujuzi Wetu kuliko walimwengu wenginewe.” (44:32),

Aidha amesema;

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَنْقُومِ يَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ
مُلُوكًا وَءَاتَاكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ ﴿٥٠﴾

“Na pale Musa alipowaambia watu wake: “Enyi watu wangu! Kumbukeni Neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipo wateua Manabii kati yenu, na Akakufanyeni watawala, na Akakupeni ambayo Hakuwapa wowote katika walimwengu.”(5:20)

Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa Abu Al-Aliyah alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَىٰ الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾

“Na Nikakuteueni kuliko wote wengineo.”

Maana yake: “Ufalme, Unabii na Vitabu ambavyo walipewa badala ya kupewa mataifa mengine ambayo yalikuwepo kabla yao, kwani katika kila zama kuna Taifa.”¹ Pia iliripotiwa kuwa Mujahid, Ar-Rabi bin Anas, Qatadah na Ismail bin Abu Khalid walisema vivyo hivyo.²

¹ At-Tabari 2:24.

² Ibn Abi Hatim 1:158.

Ummah wa Muhammad ﷺ ni Bora kuliko Wana wa Israel.

Hiyo ndiyo njia pekee ya Aya hiyo inavyoweza kufahamika, kwa sababu Ummah huu ni mbora kuliko wao, sawa na Kauli ya Allah تعالى،

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ
بِاللَّهِ وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ^٤

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa watu wa Kitabu nao wangeliamini ingelikuwa bora kwao...” (3:110)

Aidha ndani ya vitabu vya Musnad na Sunan imeandikwa kuwa Mu’awiyah bin Haydah Al-Qushayri عنه رضي الله عنہ alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَنْتُمْ تَوْفُونَ سَبْعِينَ أُمَّةً أَنْتُمْ خَيْرُهَا وَأَكْرَمُهَا عَلَى اللَّهِ»

“Nye (Waislamu) ni Taifa la sabini, lakini nye ni bora kuliko wote na mmetukuzwa na Allah.”¹

Kuna *Hadith* nyingi juu ya somo hili na zitatajwa wakati tunajadili Kauli ifuatayo ya Allah تعالى،

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

“Nye mmekuwa bora ya umma waliotolewa watu.” (3:110)

وَأَتَّقُوا يَوْمًا لَا تَجْزِي نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا شَفَعَةٌ وَلَا يُؤْخَذُ مِنْهَا عَدْلٌ
وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤٨﴾

“Na iogopeni siku ambayo mtu hatomfaa mtu kwa lolote wala hayatakubaliwa kwake maombezi, wala hakitapokelewa kikomboleo kwake; wala hawatanusuriwa.” (2:48)

¹ Ahmad 4:447, 5:3, Tuh'fatul Al-Ahwadhi 8:352 na Ibn Majah 2:1433.

Baada ya Allah تَعَالَى kuwakumbusha kwanza neema Alizowapa Wana wa Israeli, hatimaye, Aliwaonya kuhusu kipindi cha mateso ambacho Atawaadhibu kwa kipindi hicho Siku ya kufufuliwa. Alisema,

وَأَتَّقُوا يَوْمًا

“Na iogopeni siku.”

Maana: Siku ya Kufufuliwa.

لَا تَجْزِي نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ شَيْئًا

“Mtu hatomfaa mtu kwa lolote...”

Ina maana katika siku hiyo, hakuna mtu atakayeweza kumsaidia mwingine. Vivyo hivyo Allah تَعَالَى Amesema,

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَى^ع

“Na mbebaji habebi mzungu wa mwingine.” (35:18).

Pia (17:15) (6:164) Na Kauli Yake,

لِكُلِّ أَمْرٍ مِّمَّنْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿١٧﴾

“Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtoshia.” (80:37).

Na Kauli Yake,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَتَقُوا رَبَّكُمْ وَأَحْشَوْا يَوْمًا لَا تَجْزِي وَالِدٌ عَنْ وَلَدِهِ وَلَا مَوْلُودٌ هُوَ جَارٍ
عَنْ وَالِدِهِ شَيْئًا^ع

“Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi, na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwana, wala mwana hatamfaa mzazi kwa lolote.” (31:33).

Kwa hakika hii inatosha kuwa onyo kubwa kwani baba na mtoto hawatoweza kusaidiana siku hiyo.

Maombezi, Fidia au Msaada Hautakubaliwa kwa Makafiri.

Allah تعالى Amesema,

وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا شَفَعَةٌ

“Wala hayatakubaliwa kwake maombezi.”

Maana: Kutoka kwa makafiri. Vile vile Allah تعالى Amesema,

فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَعَةُ الشَّافِعِينَ ﴿٧٤﴾

“Basi hautawafaa kitu uombezi wa waombezi.” (74:48).

Na Akawaelezea watu wa Motoni Akisema,

فَمَا لَنَا مِنْ شَافِعِينَ ﴿٢٦﴾ وَلَا صَدِيقٍ حَمِيمٍ ﴿١٠١﴾

“Basi hatuna waombezi. Wala rafiki wa dhati.” (26:100-101).

Kauli ya Allah تعالى hapa (2:48),

وَلَا يُؤْخَذُ مِنْهَا عَدْلٌ

“Wala hakitapokelewa kikomboleo kwake.” Maana: Allah تعالى Hatowakubalia Makafiri kujikomboa wenyewe. Vile vile Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ مِلَّةٌ مِنَ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوْ
أَفْتَدَى بِمِئَةِ

“Hakika wale waliokufuru na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangelitoa...” (3:91) Na Allah تعالى Amesema;

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لِيَفْتَدُوا بِهِ مِنْ
عَذَابِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَا تُقْبَلُ مِنْهُمْ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٣﴾

“Hakika waliokufuru lau wangukuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama, yasingelipokewa kwao; na watapata adhabu chungu.” (5:36) Na Allah تعالى Amesema;

وَإِنْ تَعَدِلَ كُلٌّ لَأٍ يُؤْخَذَ مِنْهَا

“Na ingatoa kila fidia haitokubaliwa.” (6:70) Na;

فَأَلْيَوْمَ لَا يُؤْخَذُ مِنْكُمْ فِدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مَأْوَانُكُمُ النَّارُ هِيَ مَوْلَانُكُمْ

“Basi leo haitapokelewa kwenu fidia, wala kwa wale waliokufuru. Makazi Yenu ni Motoni, ndio bora kwenu.” (57:15)

Allah تعالی Ameeleza kuwa wapo watu hawatomuamini Mjumbe Wake na kufuata Alichowateremshia, basi watakapokutana Naye Siku ya Ufufuo, baada ya kuwa katika upotofu, vizazi vyao na lau mabwana wao wakiwaombea haitowasaidia kitu. Haitakubaliwa kwao, hata kama wangelipa fidia ya dhahabu inayojaza dunia. Allah تعالی Amesema,

مِن قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفْعَةٌ

“Kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwepo biashara, wala urafiki, wala uombezi.” (2:254) Aidha Allah تعالی Amesema;

لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خِلَالٌ

“...isiyokuwa na biashara wala urafiki.” (14:31)

Kisha Kauli ya Allah تعالی isemayo,

وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ

“Wala hawatanusuriwa.” Maana yake: “Hapana mtu atakayewaonea huruma au kuwa na hamu na kuwapatia msaada, au kujaribu kuwaokoa kutokana na adhabu ya Allah تعالی.” Kama ilivyoelezwa kabla, siku hiyo si jamaa wala mtu mwenye madaraka atakayewahurumia Makafiri, wala fidia kupokelewa kama ukombozi. Hivyo, hawatasaidiwa na wengine wala kujisaidia wenyewe. Yaani Allah تعالی Hapokei fidia wala uombezi kwa ajili ya Kafiri, wala hapana yeyote atakayewanusuru ili wasiadhawiwe, wala hakuna wa kuwaokoa au kuwaondoshea adhabu.

وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ

“Naye Ndiye Anayelinda, wala hakilindwi chochote kinyume Naye.” (23:88) Na Allah تعالی Amesema;

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ أَحَدًا ۗ وَلَا يُوثِقُ وِثْقَاهُ أَحَدًا ۗ

“Basi siku hiyo hataadhibiwa yeyote namna ya Kuadhibu Kwake. Wala hatafunga, yeyote kama Kufunga Kwake.” (89:25-26) Na Amesema;

مَا لَكُمْ لَا تَنصُرُونَ ۗ بَلْ هُمْ آيَوْمَ مُسْتَسْلِمُونَ ۗ

“...Mna nini? Mbona hamsaidiani? Bali hii leo, watasalimu amri.” (37:25-26) Na Amesema;

فَلَوْلَا نَصْرُهُمُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ قُرْبَانًا ءِلهِطَ بَلْ ضَلُّوا عَنْهُمْ ۗ

“Basi mbona wale miungu waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa ati hao ndio wawakurubishe, hawakuwanusuru? Bali waliwapoteza!” (46:28)

Pia Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

مَا لَكُمْ لَا تَنصُرُونَ ۗ

“Mna nini? Mbona hamsaidiani?” (37:25)

Ina maana: “Mbona leo hamtuzuilii kukuadhibuni? Ah wapi! Leo hamna nafasi hiyo.”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema kuwa Kauli Yake,

وَلَا هُمْ يُنصُرُونَ ۗ

“..Na wala hawatanusuriwa.” Ina maana: “Hapana aina ya msaada au ushirikiano utakaopatikana siku hiyo. Siku hiyo hakuna tena upendo kwa watu, rushwa na utetezi utafutika. Hukumu itakuwa siku hiyo juu ya Mkuu kuliko wote, Muadilifu kuliko wote, ambaye hakuna maombezi au msaidizi anayeweza kutoa msaada dhidi Yake. Atawalipa adhabu waovu na Atawazidishia waliofanya amali njema. Haya ni sawa na Kauli ya Allah تعالى isemayo,

وَقَفَّوهُمْ ۗ إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ ۗ مَا لَكُمْ لَا تَنصُرُونَ ۗ بَلْ هُمْ آيَوْمَ مُسْتَسْلِمُونَ ۗ

“Na wasimamisheni: Hakika hao watasailiwa. Mna nini? Mbona hamsaidiani? Basi leo hii, watasalimu amri.” (37:24-26)²

¹ At-Tabari 2:36.

² At-Tabari 2:35.

وَإِذْ نَجَّيْنَكُمْ مِنَ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُدَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۗ وَفِي ذَلِكُمْ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٤٩﴾ وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمْ الْبَحْرَ فَأَنْجَيْنَكُمْ مِّنْ غَرَقَتَا ۗ آلَ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٠﴾ وَإِذْ وَعَدْنَا مُوسَىٰ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً نَّمُ أَخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِن بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ ظَالِمُونَ ﴿٥١﴾ ثُمَّ عَفَوْنَا عَنْكُمْ مِمَّن بَعْدَ ذَلِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٢﴾ وَإِذْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ وَالْفُرْقَانَ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿٥٣﴾ وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَنْقُورِ إِن كُمْ ظَلَمْتُمْ أَنْفُسَكُمْ بِاتِّخَاذِكُمُ الْعِجْلَ فَتُوبُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ فَاقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ۚ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِندَ بَارِيكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ ۚ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٥٤﴾ وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَىٰ اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٥﴾ ثُمَّ بَعَثْنَاكَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٦﴾ وَظَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّاءَ وَالسَّلْوَىٰ ۗ كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ ۗ وَمَا ظَلَمُونَا وَلَكِن كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٥٧﴾

وَإِذْ نَجَّيْنَكُمْ مِنَ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُدَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۗ وَفِي ذَلِكُمْ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٤٩﴾ وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمْ الْبَحْرَ فَأَنْجَيْنَكُمْ مِّنْ غَرَقَتَا ۗ آلَ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٠﴾

49. "Na vile Tulipokuokoeni kwa watu wa Firauni walio-kupeni adhabu mbaya, wakiwachinja wana wenu wa kiume na wakawaacha hai wanawake; na katika hayo ulikuwa ni mihani mkubwa uliotoka kwa Mola wenu Mlezi."

50. "Na Tulipoipasua bahari kwa ajili yenu na Tuka-kuokoeni, Tukawazamisha watu wa Firauni, na huku mnatazama."

Wana wa Israeli Kuokolewa Kutoka kwa Firauni na Kuzamishwa Watu Wake
Allah تعالیٰ Aliwaambia Wana wa Israeli, "Kumbukeni Fadhila Zangu kwenu,

وَإِذْ نَجَّيْنَكُمْ مِنَ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ

"Na vile Tulipokuokoeni kwa watu wa Firauni waliokupeni adhabu mbaya."

Maana yake: Mimi – Niliwaokoeni kutoka kwao na Nikakutoeni kutoka mikononi mwao mkiwa pamoja na Musa عليه السلام, baada ya kuteswa sana. Fadhila hizi zilikuja baada ya Firauni mlaaniwa kuota na kuona moto ukitokea *Bayt Maqdis* (Jerusalem), na kisha moto uliingia ndani ya nyumba za Makibiti nchini Misri, ukiwaacha Wana wa Israeli. Maana ya ndoto hiyo ilikuwa kwamba Ufalme wake ungeangushwa na mtu miongoni mwa Wana wa Israeli. Walisema kuwa Wana wa Israeli walikuwa wanamtarajia mtu miongoni mwao ambaye atajitokeza na kuunda dola yao. Tutaitaja Hadithi juu ya somo hili tutakapotoa maelezo juu ya *Surat Ta Ha* (20), Allah تعالى Akipenda. Baada ya ndoto, Firauni aliamrisha kuwa kila mtoto wa kiume auawe na wasichana waachwe. Pia alitoa amri Wana wa Israeli wapewe kazi ngumu na wapewe kazi zinazodhalilisha. Katika Aya hii “Adhabu” imetafsiriwa kwa kuwaua watoto wachanga wa kiume, katika *Surat Ibrahim* (14) maana hii imeelezwa kwa uwazi, kama Allah تعالى Alivyosema;

يَسْأَلُونَكَ سَاءَ الْعَذَابِ يُذَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ

“...Walikupeni adhabu mbaya kabisa, wakiwachinja watoto wenu wanaume, na wakiwaacha hai wanawake wenu.” (14:6)

Tutaitolea maelezo Aya hii mwanzoni mwa Surat Al-Qasas (28), Allah تعالى Akipenda, na utegemezi wetu na Imani iko Kwake. Na Maana ya Kauli Yake,

يَسْأَلُونَكَ

“Walikupeni adhabu.” Maana: “Walikudhalilisheni”. Kama Abu Ubaydah alivyosema. Ilisemwa pia kuwa ina maana, “Walikuwa wakizidisha kuwatesa”, kwa mujibu wa Al-Qurtubi رحمه الله تعالى. Na hakika si vingine Allah تعالى katika Aya hapa Amesema;

يُذَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ

“Wakiwachinja watoto wenu wanaume, na wakiwaacha hai wanawake wenu.” Ili iwe ni ufafanuzi wa neema Aliyowapa. Katika Kauli Yake;

يَسْأَلُونَكَ سَاءَ الْعَذَابِ

“Walikupeni adhabu mbaya kabisa”. Kisha hapa inaelezea maana ya neema Alizowapa, kama alivyotaja katika Kauli Yake,

أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ

“...Kumbukeni zile Neema Zangu Nilizokuneemesheni...” (2:40)

Ama katika *Surat Ibrahim*, Aliposema;

وَذَكِّرْهُمْ بِأَيِّمِ اللَّهِ

“..na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu.” (14:5) Maana yake: Neema na Baraka Alizowapa, Hivyo ikanasibia huko Kusema,

يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ وَيُدْحِثُونَ أَيْدِيَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ

“...Walikupeni adhabu mbaya kabisa, wakiwachinja watoto wenu wanaume, na wakiwaacha hai wanawake wenu.” (14:6)

Hivyo Allah تعالى Ameitaja hapa adhabu mbaya hiyo kuwa ni kuwachinja watoto wao ili kuwakumbusha Neema nyingi ambazo Aliwapatia Wana wa Israel.

Inafaa tueleze hapa kuwa Firauni ni cheo alichopewa kila Mfalme Kafiri Aliyetawala Misri, ama alitokana na Amaliq au vinginevyo, kama ilivyo kwa Kaisari ni cheo kwa wafalme makafiri waliotawala Roma na Damascus. Pia Kisra ni cheo cha wafalme Makafiri waliotawala Iran, wakati Tubba ni cheo cha wafalme wa Yemen, na wafalme wa Ethiopia waliitwa An-Najashi. Allah تعالى Amesema,

وَفِي ذَلِكُمْ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ

“Na katika hayo ulikuwa ni mtihani mkubwa uliotoka kwa Mola wenu Mlezi.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alitoa maoni kuwa Aya hii ina maana, “Kitendo Chetu cha Kuwaokoa baba zenu kutokana na mateso waliyoyapata Mikononi mwa Firauni, ni neema kubwa kutoka kwa Mola.”¹ Na wakati mwingine mtihani unakuwa katika kheri na shari, kama Allah تعالى Alivyosema;

وَتَبْلُوكُم بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً

“...na Tunakujaribu kwa mtihani wa shari na kheri.” (21:35) na

وَيَلْوَنُهُمْ بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

“Na Tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea.” (7:168)

Kauli inayofuata ya Allah تعالى,

¹ At-Tabari 2:48.

وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمْ الْبَحْرَ فَأَنْجَيْنَاكُمْ وَأَغْرَقْنَا آلَ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٦﴾

“Na Tulipoipasua bahari kwa ajili yenu na Tukakuokoeni, Tukawazamisha watu wa Firauni, na huku mnatazama.”

Ina maana: “Baada ya Kuwasalimisha kutokana na Firauni na mkaokoka pamoja na Musa; Firauni alitaka kuwafuata na Tukawapasulia bahari.” Kama Allah تعالى Alivyokieleza kisa hicho kwa urefu. Kama ambavyo tutakieleza itakapofika sehemu yake Inshaallah. Na sura iliyoeleza kisa hiki kwa ufupi ni sura ya (26) Ashuaraa,

فَأَنْجَيْنَاكُمْ

“...**na Tukakuokoeni.**” Maana yake: Tuliwaokoa kutokana nao, Tukawazamisha wakati mkitazama, mkipata faraja mioyoni mwenu na faza kwa adui zenu.

Funga ya Ashura.

Imepokelewa kuwa ile siku Wana wa Israeli waliyookolewa kutokana na Firauni iliitwa siku ya “Ashura”. Imam Ahmad aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alifika Madina na akawakuta Mayahudi wakifunga siku ya “Ashura”. Aliwauliza, “Ni siku gani hii mnayofunga?” Wakajibu, “Hii ni siku njema ambayo Allah تعالى Aliwaokoa Wana wa Israeli kutoka kwa adui yao, na Musa عليه السلام alikuwa akifunga siku hii.” Mtume ﷺ akasema,

«أَنَا أَحَقُّ بِمُوسَى مِنْكُمْ»

“Mimi nina haki zaidi kwa Musa kuliko nyinyi.” Mtume ﷺ alifunga siku hiyo na akawaamrisha Waislam kufunga. Hadithi hii imekusanywa na Al-Bukhari, Muslim, An-Nasai na Ibn Majah¹.

وَإِذْ وَعَدْنَا مُوسَىٰ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً ثُمَّ أَخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ ظَالِمُونَ ﴿٥٧﴾ ثُمَّ

عَفَوْنَا عَنْكُمْ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٨﴾ وَإِذْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ وَالْفُرْقَانَ

لَعَلَّكُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٥٩﴾

¹ Ahmad 1:291, Fat'h Al-Bari 4:287, Muslim 2:796, An-Nasai katika Al Kubra 2:157 na Ibn Majah 1:553.

51. *"Na Tulipomuahidi Musa masiku arubaini, kisha mkachukua ndama (mkamuabudu) baada yake, na mkawa wenye kudhulumu."*

52. *"Kisha Tukakusameheni baada ya hayo, ili mpate kushukuru."*

53. *"Na Tulipompa Musa Kitabu (Taurati) na pambanuo baina ya haki na batili ili mpate kuongoka."*

Wana wa Israeli Waliabudu Ndama

Kisha Allah تعالى Akasema, "Kumbukeni Neema Zangu Nilipokusameheni kwa kumuabudu ndama." Hili lilijiri baada ya Musa عليه السلام kwenda kukutana na Mola Wake kwa siku arubaini. Siku hizi arubaini zimetajwa katika Surat Al-A'raf, Allah تعالى Aliposema,

﴿وَوَاعَدْنَا مُوسَىٰ ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتَمَّمْنَاهَا بِعَشْرِ﴾

"Tulipomuahidi Musa masiku thelathini na Tukayatimiza kwa kumi..." (7:142)

Inasemekana kuwa siku hizi zilikuwa katika mwezi wa Dhul-Qa'dah akiongeza siku kumi za Dhul-Hijjah, baada ya wana wa Israeli kuokolewa kutoka kwa Firauni na kuvuka bahari kwa salama. Allah تعالى Anasema,

﴿وَإِذْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ﴾

"Na (Kumbukeni) Tulipo mpa Musa Kitabu." Maana: Taurati.

﴿وَالْفُرْقَانَ﴾

"Na pambanuo." Ambalo linatofautisha kati ya ukweli na batili, uwongozi na upotofu.

﴿لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ﴾

"Ili mpate kuongoka." Baada ya kuvuka bahari, kama Ayah nyingine katika Surat Al-Araf inavyoeleza wazi.

﴿وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَ الْأُولَىٰ بِصَآئِرٍ لِلنَّاسِ وَهَدَىٰ

﴿وَرَحْمَةً لِّعَلَّاهُمْ يَتَذَكَّرُونَ﴾

"Na hakika bila ya shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo, ili kiwafumbue macho watu, na kiwe kiongofu, na rehema, ili wapate kukumbuka." (28:43)

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يُقَوْمِ إِنَّكُمْ ظَلَمْتُمْ أَنفُسَكُمْ بِاتِّخَاذِكُمُ الْعِجَلَ فَوُتُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ فَاقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِنْدَ بَارِيكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ ۗ إِنَّهُ هُوَ التَّوَّابُ

الرَّحِيمُ ﴿٥٤﴾

54. “Na Musa Alipowaambia watu wake, Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmezidhulumu nafsi zenu kwa kuchukua kwenu ndama (kumuabudu). Basi tubuni kwa Muumba wenu. Na ziueni nafsi zenu. Haya ni bora kwenu mbele ya Muumba wenu. Naye Atapokea toba yenu. Hakika Yeye Ndiye Apokeaye toba na Mwenye Kurehemu.”

Toba ya Wana wa Israeli Ilikuwa Kuuana Wao kwa Wao.

Hii ni toba waliotakiwa kufanya Wana wa Israeli kwa kosa la kuabudia ndama. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema katika maelezo ya Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يُقَوْمِ إِنَّكُمْ ظَلَمْتُمْ أَنفُسَكُمْ بِاتِّخَاذِكُمُ الْعِجَلَ

“Na Musa Alipowaambia watu wake, Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmezidhulumu nafsi zenu kwa kuchukua kwenu ndama (kumuabudu).”

Hilo lilitokea katika, “Nyoyo zao zilipofikiria kumuabudu ndama.” Hadi pale Allah تعالى Aliposema,

وَلَا سُقِطَ فِي أَيْدِيهِمْ وَرَأَوْا أَنَّهُمْ قَدْ ضَلُّوا قَالُوا لَئِن لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا

“Na walipojuta na wakaona ya kwamba wamekwishapotea, walisema: Ikiwa Mola wetu Mlezi hakuturehemu na Akatusamehe...” (7:149)

Amesema hapa ndipo Musa عليه السلام aliwaambia,

يُقَوْمِ إِنَّكُمْ ظَلَمْتُمْ أَنفُسَكُمْ بِاتِّخَاذِكُمُ الْعِجَلَ

“Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmezidhulumu nafsi zenu kwa kuchukua kwenu ndama (kumuabudu).”¹

¹ Ibn Abi Hatim 1:167.

Abu Al-Aliyah, Said bin Jubayr na Ar-Rabi bin Anas walitoa maoni kuhusu Ayah hii,

فَتُوبُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ

“Basi tubuni kwa Bari wenu.” Ina maana kwa Muumba wenu¹. Kauli ya Allah تعالیٰ.

إِلَىٰ بَارِيكُمْ

“Kwa Muumba Wenu.” Ina wazindua Wana wa Israeli juu ya ukubwa wa kosa lao na ina maana, “Tubieni kwa Yule Aliyewaumba baada ya kumshirikisha na vitu vingine katika kumuabudu.”

An-Nasai, Ibn Jariri na Ibn Abu Hatim wamepokea Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, “Allah تعالیٰ Aliwaambia Wana wa Israeli kuwa toba yao itakuwa kumkata kichwa kila watakayekutana naye, bila kujali alikuwa baba au mtoto wa kiume au mtu mwingine. Ama wale ambao Musa عليه السلام na Harun عليه السلام hawakujua makosa yao, walikiri makosa, na wakafanya kama walivyoamrisha. Hivyo Allah تعالیٰ Akawasamehe wauaji na waliouawa.”² Haya ni sehemu ya maelezo kuhusu majaribu ambayo tutayataja katika *Surat Ta Ha* (20), Allah تعالیٰ Akipenda. Ibn Jariri رحمه الله تعالیٰ alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Musa عليه السلام aliwaambia watu wake,

فَتُوبُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ فَاقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِنْدَ بَارِيكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ إِنَّهُ هُوَ

التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿٥٧﴾

“Basi tubuni kwa Muumba wenu. Na ziueni nafsi zenu. Haya ni bora kwenu mbele ya Muumba wenu. Naye Atapokea toba yenu. Hakika Yeye Ndiye Apokeaye toba na Mwenye Kurehemu.”

Allah تعالیٰ Alimuamrisha Musa عليه السلام awaamuru watu wake wauane. Aliwaamrisha wale waliomuabudia ndama wakae kitako, na ambao hawakumuabudia ndama wasimame wakiwa na visu mikononi mwao. Walipoanza kuwaua, ghafla kiza totoro kikawafunika. Baada ya kiza kuondoka, walikuwa wameshawaua elfu sabini kati yao. Wale waliouawa walisamehewa na waliobaki walisamehewa pia.³

¹ Ibn Abi Hatim 1:167, 168.

² An-Nasai katika al-Kubra 6:404, At-Tabari 18:306 na Ibn Abi Hatim 1:168.

³ At-Tabari 2:73.

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَىٰ اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ
 ثُمَّ بَعَثْنَاكُم مِّنْ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٥﴾

55. “Na mliposema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumuone Mwenyezi Mungu waziwazi. Ikakunyakueni radi nanyi mnaangalia.”

56. “Kisha Tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.”

Wakuu wa Wana wa Israeli Walitaka Kumuona Allah تعالی Mubasharah, Allah تعالی Akawaua Kisha Akawafufua Tena.

Allah تعالی Alisema, “Kumbukeni Neema Zangu nilipowafufueni baada ya kunyakuliwa na radi mlipodai kuniona moja kwa moja, hilo haliwezekani kwenu au kwa wengine. Haya yalisemwa na Ibn Jurayj. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii,

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَىٰ اللَّهَ جَهْرَةً

“Na mliposema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumuone Mwenyezi Mungu waziwazi.”

Maana yake: “Hadharani.”¹ “Ili Tumuone Allah تعالی.”² Aidha Urwah bin Ruwaym alisema kwa Kauli ya Allah تعالی,

فَأَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ

“Ikakunyakueni radi.” Maana yake: “Walikufa, na Musa عليه السلام Alisimama akilia na kumuomba Allah تعالی, “Ewe Mola! Nitawaambia nini Wana wa Israeli nitakaporejea kwao, baada ya kuwaangamiza viongozi wao,

وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٥٦﴾

“Nanyi mnaangalia.” Maana yake: “Baadhi yao walipigwa na radi wakati wengine wakitazama.”³ Allah تعالی Aliwafufua, na wengine wakapigwa kwa radi. As-Suddi alitolea Aya hii maoni.

¹ At-Tabari 2:81.

² Ibn Abi Hatim 1;170.

³ Ibn Abi Hatim 1:173.

لَوْ شِئْتَ أَهْلَكْتَهُمْ مِّن قَبْلُ وَإِنِّي أَتْلُوكُنَّا بِمَا فَعَلَ السُّفَهَاءُ مِنَّا

“Ungalitaka ungeliwahiliki wao na mimi zamani! Unatuhiliki kwa waliyoyafanya wajinga katika sisi?” (7:155).

Allah تعالی Alimteremshia Musa عليه السلام kuwa hao watu sabini walikuwa miongoni mwa watu walioabudia ndama. Baadaye, Allah تعالی Aliwafufua mmoja baada ya mwingine, wakati waliobaki walikuwa wakiangalia namna Allah تعالی Alivyokuwa Akiwafufua. Ndio sababu Allah تعالی Akasema,

ثُمَّ بَعَثْنَاكَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢٠٠﴾

“Kisha Tukakufuueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.”

Ar-Rabi bin Anas alisema, “Kifo kilikuwa adhabu yao, na walifufuliwa baada ya kufa ili wamalizie maisha yao.” Qatadah alisema hivyo hivyo.² Abdur-Rahman bin Zayd Aslam alielezea Aya hii, “Musa عليه السلام alirejea kutoka kwenye mkutano na Mola Wake akibeba mbao zilizoandikwa Taurati. Alitambua kuwa walikuwa wakiabudia ndama katika kipindi ambacho hakuwepo. Hivyo Musa عليه السلام akawaamuru kuuana wao kwa wao kama Toba juu yao, wakatekeleza amri hiyo, Allah تعالی Akakubali Toba yao. Akasema, “Hakika hiki ni Kitabu cha Allah تعالی kikiwa na yale Aliyokuamrisheni na Aliyokukatazeni.” Wakasema, “Hivi Tuamini maneno haya kwa sababu tu wewe umeyasema? Wallahi! Hatutoamini mpaka tumuone Allah تعالی waziwazi na Atuoneshe Mwenyewe na Aseme, “Hiki ni Kitabu Changu, shikamaneni nacho. Kwa nini Hazungumzi nasi kama Alivyozungumza nawe, ewe Musa?” Kisha Abdur-Rahman bin Zayd alisoma Kalima ya Allah تعالی,

لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّى نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً

“Hatutakuamini mpaka tumuone Mwenyezi Mungu waziwazi.”

Na akasema, “Hivyo adhabu ya Allah تعالی iliwashukia, radi iliwapiga na wote wakafa. Kisha Allah تعالی Akawahuisha baada ya kuwaua.” Kisha Abdur-Rahman alisoma Maneno ya Allah تعالی,

¹ Ibn Abi Hatim 1:173.

² Ibn Abi Hatim 1:173.

ثُمَّ بَعَثْنَاكَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٧﴾

“Kisha Tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.”

Musa عليه السلام Aliwaambia, “Chukueni Kitabu cha Allah تعالى.” Wakasema, “Hapana.” Akasema, “Mna nini nyinyi?” Wakasema, “Tatizo ni kuwa tulikufa na tukafufuka.” Akawaambia, “Chukueni Kitabu cha Allah تعالى.” Wakasema, “Hapana.” Hivyo Allah تعالى Aliwapeleka baadhi ya Malaika ambao waliwaangushia majabali.¹ Hii inaonesha kuwa Wana wa Israeli walitakiwa kutii amri baada ya kufufuliwa. Hata hivyo, Al-Mawardy رحمه الله تعالى alisema kuwa kuna rai mbili juu ya suala hili. Rai ya kwanza ni kuwa baada ya Wana wa Israeli kuushuhudia miujiza, walilazimika kuamini, hivyo hawakutakiwa kutii maamrisha. Rai ya pili inaelezea kuwa, walitakiwa kutii maamrisha, ili isije kudhaniwa kuwa Mtu mzima mwenye akili amesamehewa kubeba majukumu. Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema rai hii ndio sahihi, kwa sababu, japo Wana wa Israeli walishuhudia haya maafa ya kutosha, haikuwa na maana kuwa hawakuwajibika kutii maamrisha tena. Bali, wanawajibika kwa hayo, na hii ndio rai ya wazi. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

وَوَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّانَ وَالسَّلْوَىٰ كُلُّوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَمَا

ظَلَمُونَا وَلٰكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٥٧﴾

57. “Na Tukakutilieni kivuli kwa mawingu na Tukakuteremshieni Manna na Salwa; (Tukakuambieni) Kuleni vitu vizuri hivi Tulivyo kuruzukuni. Nao hawakutudhulumu sisi lakini walikuwa wakijidhulumu nafsi zao.”

Kuwafunika Kiwingu Wana wa Israel (Kivuli), na Kuteremshiwa Manna na Salwa.

Baada ya Allah تعالى Kutaja Alivyowaokoa wana wa Israeli kutokana na maafa, Alizitaja Neema Alizowapa,

وَوَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ

“Na Tukakutilieni kivuli kwa mawingu.”

¹ At-Tabari 2:88.

Aya hii inataja mawingu meupe ambayo yaliwapatia kivuli Wana wa Israeli, yakiwahifadhi na joto na jua katika miaka ya kutangatanga katika Jangwa la Tihi. Katika *Hadithi* inayohusu majaribu, An-Nasai alirekodi Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,¹ "Allah تعالی Aliwafunika Wana wa Israeli kwa mawingu katika miaka ya kutapatapa. "Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالی alisema, "Masimulizi sawa na yale ya Ibn Abbas رضي الله عنهما yaliripotwa kutoka kwa Ibn Umar, Ar-Rabi bin Anas, Abu Mijlaz, Adh-Dhahhak na As-Suddi." Al-Hasan na Qatadah walisema kuwa,

وَوَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ

"Na Tukakutilieni kivuli kwa mawingu."

Hili lilijiri walipokuwa jangwani na mawingu yakawakinga na jua.² Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema kuwa wanazuoni wengi walisema kuwa aina ya mawingu iliyotajwa na Aya, "Yalikuwa baridi na bora kuliko aina tuijuayo."³ Ali Ibn Abu Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maoni Kauli ya Allah تعالی,

وَأَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّاءَ

"Tukakuteremshieni Manna."

Manna ilikuwa ikiwashukia kutoka kwenye miti, nao walikuwa wakila kila wakitakacho kutokana nayo. Aidha Qatadah alisema kuwa *Manna* ambayo ilikuwa nyeupe kuliko maziwa na tamu kuliko asali, ilikuwa ikiwabubujikia Wana wa Israeli kama theluji inavyodondoka huanzia macheo mpaka machweo. Kila mtu akakusanya ya kumtoshia kwa siku ile na wasisaze. Kwani ikisazwa huchacha. Katika siku ya sita ya juma, Ijumaa, kila mmoja alikusanya ya kutosha kwa hiyo siku ya sita na ya saba, ambayo ilikuwa Sabato. Ilikuwa ni Sikukuu, na haikuruhusiwa katika siku hiyo kujitafutia riziki au kufanya jambo jingine lolote. Yote haya yalitokea bila kuwepo utaratibu maalumu (shaghala baghala).⁴ *Manna* (kama tuijuavyo) kilikuwa chakula tosha kuliwa peke yake, kwa sababu kilikuwa na virutubisho na ladha tamu. *Manna* inapochanganywa na maji huwa kinywaji kitamu. Na inapochanganywa huwa aina nyengine ya

¹ Ibn Abi Hatim 1:174.

² Ibn Abi Hatim 1:174.

³ At-Tabari 2:91.

⁴ Ibn Abi Hatim 1:176.

chakula. Hata hivyo hii sio aina pekee. Ushahidi wa ukweli huu ni kama alivyosimulia Al-Bukhari, kuwa Said bin Zayd رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْكَمَاءُ مِنَ الْمَنْ وَمَاؤُهَا شِفَاءٌ لِلْعَيْنِ»

“Kam’ah (Uyoga) ni aina ya manna, na maji yake ni dawa ya macho.”¹

Hadithi hii pia ilikusanywa na Imam Ahmad.² Kundi la wakusanyaji wa Hadith minghairi ya Abu Dawud pia waliikusanya, At-Tirmidhi aliipa daraja la *Hasan Sahih*.³ At-Tirmidhi alipokea kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْعَجْوَةُ مِنَ الْجَنَّةِ وَفِيهَا شِفَاءٌ مِنَ السَّمِّ وَالْكَمَاءُ مِنَ الْمَنْ وَمَاؤُهَا شِفَاءٌ لِلْعَيْنِ»

“Ajwah (tende kavu) ni kutoka peponi na ni tiba ya sumu na Al-Kam’ah (uyoga) ni aina ya manna, na maji yake yanatibu macho.”⁴

At-Tirmidhi ndiye pekee aliyerekodi Hadithi hii.

Ama kuhusu ndege (*Salwa*) aliye tajwa, Ali bin Abu Talha alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, “*Salwa* ni ndege anayefanana na tondoro.”⁵ Rai hii ni sawa na iliyopokewa na Mujahid, Ash-Shabi, Adh-Dhahhak, Al-Hasan, Ikrimah na Ar-Rabi bin Anas, Allah تعالى Awarehemu wote.⁶ Pia Ikrimah alisema kuwa *Salwa* ni ndege wa peponi mwenye umbile sawa na Shorewanda (*Jurawa*).⁷ Qatadah alisema kuwa “*Salwa*” ni ndege sawa na Shorewanda. Wakati huo, Myahudi angewachinja shorewanda wa kumtoshia siku ile, vinginevyo nyama ingalichacha. Siku ya sita, Ijumaa angalikusanya wa kutosha kwa siku ya sita na ya saba, sabato, siku ambayo hawakuruhusiwa kutoka majumbani na kwenda kutafuta chochote.⁸ Allah تعالى Amesema,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:14.

² Ahmad 1:187.

³ Fat’hul al-Bari 8:14, Muslim 3:1619, Tuhfatul Al-Ahwadhi 6:235, An-Nasai katika al-Kubra 4:370 na Ibn Majah 2:1143.

⁴ Tuhfat Al-Ahwadhi 6:233

⁵ Tuhfat Al-Ahwadhi 235.

⁶ At-Tabari 2:96.

⁷ Ibn Abi Hatim 1:178.

⁸ Ibn Abi Hatim 1:179.

كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ^٥

“Kuleni vitu vizuri hivi Tulivyokuruzukuni.” Aina hii ya amri ni amri ya rukhsa inayoelekeza kwenye mema. Allah تعالى Amesema,

وَمَا ظَلَمُونَا وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٥٧﴾

“Nao hawakutdhulumu sisi lakini walikuwa wakijidhulumu nafsi zao.”

Ina maana, “Tuliwaamrisha wale kutokana na Tulivyowaruzuku, na kufanya ibada (lakini waliasi).” Aya hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

كُلُوا مِنْ رِزْقِ رَبِّكُمْ وَأَشْكُرُوا لَهُ^٥

“Kuleni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, na mumshukuru.” (34:15)

Bado Wana wa Israeli waliasi, wakakanusha ujumbe, wakatendean maovu kati yao, japokuwa waliona dalili za wazi, miujiza ya kustaajibisha na matukio yaliyokiuka ada.

Utukufu wa Masahaba wa Muhammad ﷺ juu ya Masahaba wa Mitume Wengine.

Hapa ni muhimu kuelezea utukufu wa Masahaba wa Muhammad ﷺ juu ya Masahaba wa Mitume wengine. Hii ni pamoja na jinsi walivyoshikamana na Dini, subira na kutokuwa na kiburi, Allah تعالى Awawie radhi. Japokuwa Masahaba walifuatana na Mtume ﷺ katika safari zake na vita, kama vile wakati wa vita vya Tabuk, katika joto kali na ugumu, hawakutaka miujiza, japo hili lilikuwa sahihi kwa Mtume ﷺ kwa uwezo wa Allah تعالى. Na Masahaba walipokuwa na njaa, walimuomba Mtume ﷺ kumuomba Allah تعالى ili aongeze chakula. Walikusanya vyakula walivyo kuwa navyo na kuvileta kwa Mtume ﷺ, na alimuomba Allah تعالى kuteremsha mvua, na mawingu ya mvua yalitokea. Walikunywa, waliwanyweshwa ngamia wao na wakajaza viriba vyao. Walipotazama pembezoni waliona kuwa mvua imenyeshwa kwenye hema lao tu. Huu ni mfano bora wa wale waliokuwa tayari kukubali Maamuzi ya Allah تعالى na kumfuata Mtume ﷺ.

وَإِذْ قُلْنَا أَدْخُلُوا هَذِهِ الْقَرْيَةَ فَكُلُوا مِنْهَا حَيْثُ شِئْتُمْ
 رَغَدًا وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُولُوا حِطَّةٌ نَغْفِرْ لَكُمْ
 خَطِيئَتِكُمْ^{٥٨} وَسَنَزِيدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾ فَبَدَّلَ الَّذِينَ
 ظَلَمُوا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِي قِيلَ لَهُمْ فَأَنْزَلْنَا عَلَى الَّذِينَ
 ظَلَمُوا رِجْزًا مِّنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٥٩﴾ * وَإِذْ
 اسْتَسْقَىٰ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ فَقُلْنَا اضْرِبْ بِعَصَاكَ الْحَجَرَ^{٦٠}
 فَانفَجَرَتْ مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا^{٦١} قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ
 مَّشْرِبَهُمْ^{٦٢} كُلُوا وَاشْرَبُوا مِن رِّزْقِ اللَّهِ وَلَا تَعْتُوا فِي
 الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٦٠﴾ وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نَّصْبِرَ عَلَىٰ
 طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ لَنَا مِمَّا تُثَبِتُ الْأَرْضُ
 مِنْ بَقْلِهَا وَقِثَّائِهَا وَفُومِهَا وَعَدَسِيهَا وَبَصِلَهَا^{٦٣} قَالَ
 أَتَسْتَبْدِلُونَ الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ^{٦٤}
 أَهْبِطُوا مِصْرًا فَإِنَّ لَكُمْ مِمَّا سَأَلْتُمْ^{٦٥} وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ
 الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
 كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّنَ بِغَيْرِ
 الْحَقِّ^{٦٦} ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٦٦﴾

وَإِذْ قُلْنَا أَدْخُلُوا هَذِهِ الْقَرْيَةَ
 فَكُلُوا مِنْهَا حَيْثُ شِئْتُمْ رَغَدًا
 وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُولُوا
 حِطَّةٌ نَغْفِرْ لَكُمْ خَطِيئَتِكُمْ^{٥٨}
 وَسَنَزِيدُ
 الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾ فَبَدَّلَ الَّذِينَ
 ظَلَمُوا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِي قِيلَ لَهُمْ
 فَأَنْزَلْنَا عَلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا رِجْزًا مِّنَ
 السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٥٩﴾

58. "Na Tuliposema: Ingieni mji huu, na humo mle mpendavyo maridhawa, na ingieni katika mlango wake kwa unyenyekevu, na semeni: Tusamehe dhambi zetu. Tutakusameheni makosa yenu na Tutawazidishia wema wafanyayo wema."

59. "Lakini waliodhulumu waliibadili kauli isiyokuwa waliyoambiwa. Kwa hiyo Tukaiteremsha juu ya wale

waliodhulumu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya walivyokuwa wamepotoka."

Mayahudi Badala ya Kumshukuru Allah تعالى kwa Kupata Nusura Wanaendeleza Ukaidi

Allah تعالى Aliwaonya Mayahudi kwa kukwepa *Jihad* na kukataa kuingia ardhi Takatifu kama walivyoamrisha kufanya walipokuja wakitoka Misri wakiwa na Musa عليه السلام. Pia waliamrisha kuwapiga Makafiri wa ki-Amaliq (*Cannanites*) waliokuwa wanaishi katika ardhi tukufu zama zile. Lakini hawakutaka kupigana, kwa sababu walikuwa dhaifu na walikuwa wachovu. Allah تعالى Aliwadhibu kwa Kuwafanya wapotee, na waliendelea kuhangaika, kama Allah تعالى Alivyoeleza katika *Surat Al-Maidah* (5).

Maoni sahihi kuhusu ardhi Takatifu iliyotajwa hapa ni *“Bayt Al-Maqdis”* (Jerusalem), kama As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas¹, Qatadah na Abu Muslim Al-Asfahani na wengine walisema hivyo. Musa عليه السلام alisema,

يَقَوْمِ ادْخُلُوا الْأَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوا

“Enyi watu wangu! Ingieni katika nchi Takatifu Mwenyezi Mungu Amekuandikieni. Wala msirudi nyuma...” (5:21)²

Hata hivyo baadhi ya Wanazuoni walisema kuwa Ardhi Takatifu ni Jericho (*Ariha*) na maoni haya yaliyotajwa ni ya Ibn Abbas na Abdur-Rahman bin Zayd.

Baada ya kuisha miaka ya kutangatanga, miaka arubaini baadaye, wakiwa pamoja na Yuwsha (Joshua) bin Nun, Allah تعالى Aliwaruhusu Wana wa Israeli kuiteka Ardhi Takatifu kuamkia Ijumaa. Siku hiyo jua lilizuiwa kidogo kuzama, mpaka ushindi ulipopatikana. Wana wa Israeli walipoiteka Ardhi Takatifu, waliamrisha kuingia lango lake kwa,

سُجَّدًا

“Kunyenyekoa.”

Kwa kumshukuru Allah تعالى kwa Kuwapa ushindi wa mafanikio, Kuwarejesha katika ardhi yao na Kuwaokoa baada ya kupotea na kuhangaika. Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

¹ Ibn Abi Hatim 1:181.

² Ar-Razi 3:82.

وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا

“Na ingieni katika mlango wake kwa kunyenyekoa.”

Maana: Kwa kuinama.¹ Ibn Jarir رضي الله عنهما ابن عباس ame sema kuwa رضي الله عنهما ابن عباس alisema kuwa,

وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا

“Na ingieni katika mlango wake kwa kunyenyekoa.”

Ina maana: “Kupitia mlango mdogo wakati mmeinama.” Al-Hakim alisimulia, na Abu Hatim aliongezea, “Na waliingia kupitia mlango kwa kusota na makalio yao!”

Al-Hasan Al-Basri رضي الله تعالى عنه alisema kuwa waliamrisha kusujudu nyuso zao wakati wa kuingia mjini, lakini Ar-Razi رحمه الله تعالى aliyakataa maelezo haya. Tena imetajwa kuwa neno *Sujud* hapa linamaanisha unyenyekevu kwani isingewezekana kuingia kwa kusujudu.

Khusaif رضي الله تعالى عنه alisema kuwa Ikrimah amesema, Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kwamba mlango ulikuwa umeelekea kibra.

Ibn Abbas, Mujahid, As-Suddi, Qatadah na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم wamesema kuwa huo ni mlango wa *Hittah* huko lilya, *Baytul –Maqdis*. Ar-Razi رحمه الله تعالى amesema kwamba baadhi yao wamesema kwamba ni mlango mmojawapo wa upande wa kibra.

Pia Khusaif رضي الله تعالى عنه alisema kuwa Ikrimah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Wana wa Israel waliingia kupitia mlango kiubavu ubavu. As-Suddi alisema kutoka kwa Abu Said Al-Azdy, kutoka kwa Abu Al-Kanud, kutoka kwa Abdullah bin Masud رضي الله عنه kuwa waliamrisha,

وَأَدْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا

“Ingieni katika mlango wake kwa kunyenyekoa.”

Lakini badala yake waliingia huku wakiinua vichwa vyao kwa kukataa kutii amri.²

¹ At-Tabari 2:113.

² Ibn Abi Hatim 1:183.

Baadaye Allah تعالى Akasema,

وَقُولُوا حِطَّةً

“Na semeni: Tusamehe dhambi zetu.” Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo, “Ombeni msamaha kutoka kwa Allah تعالى.”¹ Al-Hasan na Qatadah walisema hiyo ilikuwa na maana, “Semeni, “Tusamehe madhambi yetu.”²

نَغْفِرْ لَكُمْ خَطَايَكُمْ وَسَيِّرِدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾

“Tutakusameheni makosa yenu na Tutawazidishia wema wafanyao wema.”
Haya ni malipo kwa kutii maamrisha ya Allah تعالى.

Aya hii ina maana, “Endapo mtatekeleza yale Tuliyoukamrisheni, Tutakusameheni dhambi zenu na Tutakuzidishieni thawabu zenu.” Kwa Muhtasari, kwa kupata ushindi Wana wa Israeli waliamrishwa kujisalimisha kwa Allah تعالى kwa kauli na vitendo na kukiri madhambi yao na kuomba msamaha, kumshukuru Allah تعالى kwa neema Alizowapa, kujitahidi kufanya amali Azipendazo Allah تعالى, kama Alivyosema,

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿٥٩﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٦٠﴾

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٦١﴾

“Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi, na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi, zitakase Sifa za Mola wako Mlezi, na umuombe msamaha; hakika Yeye Ndiye Anayepokea toba.” (110:1-3)

Na Kauli Yake,

فَبَدَّلَ الَّذِينَ ظَلَمُوا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِي قِيلَ لَهُمْ

“(Lakini wale) waliodhulumu (nafsi zao) waliibadili kauli isiyokuwa waliyoambiwa.”

Al-Bukhari alimrikodi Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«قِيلَ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُولُوا: حِطَّةً، فَدَخَلُوا يَزْحَفُونَ عَلَى أَشْتَاهِمِمْ فَبَدَّلُوا وَقَالُوا، حَبَّةٌ فِي سَعْرَةٍ»

¹ Ibn Abi Hatim 1:183.

² Ibn Abi Hatim 1:185.

“Wana wa Israeli waliamrisha kuingia kupitia mlangoni huku wamesujudu na waseme “Hittah”. Bado waliingia kwa kusota na makalio yao, walipotisha maneno. Wakasema: Habbat Fiy Sha’rah (mbegu ndani ya nafaka).”¹

An-Nasai alirikodi sehemu hii kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه peke yake, lakini isnadi yake inatoka kwa Mtume ﷺ, akielezea Kauli ya Allah تعالى,

حِطَّةٌ

“Hittah” – (Tusamehe dhambi zetu)” kasema, “Hivyo wakapotoka na wakasema, “Habbah.”² Vivyo hivyo ilipokewa na Abdur-Razzaq na pia ilikusanywa na Al-Bukhari, Muslim na at-Tirmidhi alisimulia sawa na Hadith hii, At-Tirmidhi alisema ni Hasan Sahih.³

Muhtasari wa yale waliyoyasema wanazuoni juu ya somo hili ni kuwa Wana wa Israeli walipotisha maamrisha ya Allah تعالى ambayo yaliwataka wajisalimishe Kwake kwa ulimi na vitendo. Waliamrisha kuingia mjini huku wamesujudu, lakini waliingia huku wakisota kwa makalio yao, huku wameinua vichwa! Waliamrisha waseme “Hittah” maana yake, “Tufutie dhambi zetu.” Hata hivyo waliifanyia istihzai kauli hii na wakasema, “Hintah” (mbegu ya nafaka) ndani ya Shairah (Shayiri). Hii inaonesha aina mbaya kabisa ya uasi na ufedhuli. Hii ndiyo sababu Allah تعالى Aliwakasirikia na Akaweteremshia Adhabu, yote haya kwa sababu ya dhambi zao na kuasi Amri Zake. Allah تعالى Amesema,

فَأَنزَلْنَا عَلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا رِجْزًا مِّنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٥٨﴾

“Kwa hiyo Tukaiteremsha juu ya wale waliodhulumu Adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya kuasi kwao.”

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضى الله عنهما alisema, “Kila neno katika Kitabu cha Allah linalosema Rijz maana yake, “Adhabu”⁴. Mujahid, Abu Malik, As-Suddi, Al-Hasan na Qatadah waliripotiwa kuwa wamesema kuwa Rijz ina maana ya “adhabu.”⁵ Ibn Abi Hatim alisimulia kuwa Sa’d bin Malik, Usamah bin Zayd na Khuzaymah bin Thabit walisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:14.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:286.

³ Tufhat Al-Ahwadhi 8:291.

⁴ At-Tabari 2:118.

⁵ Ibn Abi Hatim 1:187.

«الطَّاعُونَ رَجَزٌ. عَذَابٌ عُذِّبَ بِهِ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ»

"Tauni ni karipio na adhabu ambayo Allah Aliwaadhibu nayo watu waliotangulia."¹

Hivi ndivyo An-Nasai alivyoipokea *Hadithi* hii kwa nyongeza², msingi wa *Hadithi* hii ulikusanywa katika Sahihi mbili,

«إِذَا سَمِعْتُمُ الطَّاعُونَ بِأَرْضٍ فَلَا تَدْخُلُوهَا»

"Pindi msikiapo kuna tauni katika mji, basi msiuingie."³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kuwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ هَذَا الْوَجَعَ وَالسَّمَّ رَجَزٌ عُذِّبَ بِهِ بَعْضُ الْأُمَمِ قَبْلَكُمْ»

"Maafa haya ya ugonjwa (tauni) ni karipio na adhabu ambayo baadhi ya mataifa ya kabla yenu, waliadhibiwa kwayo."⁴

Hivi ndivyo jinsi Nasai alivyoisajili *Hadithi* hii.⁵ Msingi wa *Hadithi* hii ulikusanywa katika Sahihi mbili.⁶

✽ وَإِذْ أَسْتَسْقَىٰ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ فَقُلْنَا اضْرِبْ بِعَصَاكَ الْحَجَرَ ۖ فَانفَجَرَتْ مِنْهُ أُنثَىٰ
عَشْرَةَ عَيْنًا قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ مَّشْرَهُمْ ۖ كُلُوا وَاشْرَبُوا مِن رِّزْقِ اللَّهِ وَلَا تَعْتُوا فِي
الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٦٠﴾

60. "Na Musa alipoomba maji kwa ajili ya watu wake, Tulimuambia: lipige jiwe kwa fimbo yako. Mara zikabubujika chemchemu kumi na mbili; kila kabila ikajua mahali pake pa kunywea. (Tukawaambia) Kuleni na kunyweni riziki ya Mwenyezi Mungu, wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu."

¹ Ibn Abu Hatim 1:186.

² An-Nasai katika Al-Kubra 4:362.

³ Fat'hul Al-Bari 10:189 na Muslim 4:1739.

⁴ At-Tabari 2:116.

⁵ Fat'hul Al-Bari 6:512 na Muslim 4:1737.

⁶ An-nasai katika Al-Kubra 4:11739.

Kuzibuka kwa Chemchemu Kumi na Mbili

Allah تعالى Amesema, “Kumbukeni Fadhila tangu Nilipoijibu dua ya Mtume wenu, Musa عليه السلام akataka Niwapeni maji. Niliwapatieni maji, Nikiyafanya yabubujike kutoka katika mawe. Chemchemu kumi na mbili zilizochimbuka kutoka katika mawe, na kila chemchemu lilipewa kabila moja. Mnakula *manna* na ndege na mnakunywa maji Niliyokupeni bila juhudi zozote au taabu yoyote. Hivyo Muabuduni Mmoja Aliyewadhalilishieni yote hayo.”

وَلَا تَعْتَوُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٥٨﴾

“**Wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu.**” Ina maana, “Msilipe Fadhila kwa kufanya vitendo vya uasi ambavyo vitasababisha Fadhila kutoweka.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Wana wa Israeli, “Walikuwa na jiwe lenye umbo mraba ambalo Musa عليه السلام aliamrisha kulipiga kwa fimbo yake na matokeo yake ni kuchimbuka kwa chemchemu kumi na mbili kutoka katika jiwe hilo, chemchemu tatu kila upande. Kila kabila lilipewa chemchemu moja, na walikuwa wakinywa kutoka katika chemchemu hiyo. Hawakusafiri kutoka maeneo hayo, bali waliyapata maji hapo, na vile vile waliyapata walipokuwa katika eneo la mwanzo.”¹ Masimulizi haya ni sehemu ya *Hadithi* ndefu ambayo An-Nasai, Ibn Jarir na Ibn Hatim waliandika kuhusu mitihani.

Na kisa hiki kinashabihiana na kisa kilichopo katika *Surat – Araf (7)* isipokuwa *Surat* hiyo alishushiwa Makkah. Hivyo Allah تعالى Alitumia “nafsi ya tatu” kwa kuwa Anamueleza Mtume wake ﷺ kuhusu Alichowafanyia wana wa Israel, ndani ya *Surat Al-Araf*.

Ama katika Surah hii, *Al-Baqarah* ambayo ilishushiwa Madina, mazungumzo ni ya moja kwa moja wanaambiwa wahusika. Katika *Surat Al-Araf* Allah تعالى Ameeleza kwa Kusema:

فَأَنْبَجَسْتُمْ مِنْهُ ثَلَاثًا عَشْرَةَ عَيْنًا ۗ

“**Mara zikabubujika humo (jiweni) chemchemu kumi na mbili.**” (7:160)

Inaeleza kilichotokea mwanzo wakati maji yalipoanza kububujika humo. Katika Ayah hii katika *Surat Al-Baqarah*, Allah تعالى Alielezea yaliyojiri baadaye. Maana Yake Maji yalipotoka kwa nguvu. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

¹ At-Tabari 2:120.

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نَصْبِرَ عَلَىٰ طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ لَنَا مِمَّا تُثْبِتُ الْأَرْضُ
 مِنْ بَقْلِهَا وَقِثَّائِهَا وَفُومِهَا وَعَدَسِيهَا وَبَصَلِهَا ۗ قَالَ أَتَسْتَبْدِلُونَ الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ
 بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ ۚ اهْبُطُوا مِصْرًا فَإِنَّ لَكُمْ مَّا سَأَلْتُمْ ۗ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ
 وَالْمَسْكَنَةُ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ
 وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّنَ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٦١﴾

61. "Na mliposema: "Ewe Musa! Hatuwezi kuvumilia chakula cha namna moja tu, basi tuombe kwa Mola Wako Mlezi Atutolee vile vilivyomea katika ardhi, kama mboga zake, na matango yake, na thomu zake, na adesi zake, na vitunguu vyake. Akasema: Mnabadili kilicho duni kwa kilicho bora? Shukeni mjini, huko mtapata mlivyoviomba. Na wakapigwa na unyonge, na umasikini na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa Maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabii pasipo haki. Hayo ni kwa walivyoasi na wakapindukia mipaka."

Kutaka Kwao Vyakula Duni Badala ya Manna na Salwa.

Allah تعالی Alisema, "Na Kumbukeni Fadhila Zangu Nilipokuteremshieni kipatikanacho kwa urahisi. Na kumbukeni ukosefu wenu wa fadhila kwa yale Tuliyo kupatieni. Kumbukeni jinsi mlivyomtaka Musa عليه السلام awabadilishieni chakula hiki kwa chakula cha hali ya chini ambacho ni pamoja na mboga mboga na kadhalika." Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی aliwaelezea Watoto wa Israeli, "Walikuwa wamechoshwa na wakakosa uvumilivu na aina ya chakula walichopewa. Aidha walikumbuka maisha waliyokuwa wanaishi, wakati chakula chao kilikuwa pamoja na vitunguu maji, vitunguu swaumu na viungo." Wakasema,

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نَصْبِرَ عَلَىٰ طَعَامٍ وَاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ لَنَا مِمَّا تُثْبِتُ الْأَرْضُ
 مِنْ بَقْلِهَا وَقِثَّائِهَا وَفُومِهَا وَعَدَسِيهَا وَبَصَلِهَا ۗ

“Ewe Musa! Hatuwezi kuvumilia chakula cha namna moja tu, basi tuombe kwa Mola Wako Mlezi Atutolee vile vilivyomea katika ardhi, kama mboga zake, na matango yake, na thom zake, na adesi zake, na vitunguu vyake.”

Na hakika si vingine wamesema,

عَلَىٰ طَعَامٍ وَاجِدٍ

“Chakula cha namna moja tu.”

Maana yake: *Manna* na Ndege, kwa sababu walikula aina moja ya chakula kila siku. Aya ilitaja matango, vitunguu na ngano, ambavyo ni vyakula vinavyofahamika. Ama kwa *Fum*, Ibn Masud رضي الله عنه alisoma, *Thum* (thomu), kwa *Tha*. Pia, Ibn Hatim alisimulia kuwa Al-Hasan alizungumzia Aya,

وَقَوْمِهَا

“Fum yake.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa *Fum* maana yake ni *Thoum*¹. Aidha alisema kuwa usemi, “*Fumu – la-na*.” Maana yake: “Tuokoe” kwa mujibu wa lugha za kale, Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameitolea maoni, kwa kusema, “Kama haya ni sahihi, hivyo *Fum* ni moja ya maneno ambayo lafudhi yake ilibadilishwa, herufi “fa” ilibadilishwa kuwa herufi “tha” kwa vile yana sauti inayofanana.² Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Wengine walisema kuwa *Fum* ni ngano, aina inayotumika kwa kuoka mikate. Al-Bukhari alisema, “Baadhi yao walisema kuwa *Fum* ni punje au mbegu zote zinazoliwa.”

قَالَ أَتَسْتَبْدِلُونَ الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ

“Akasema: Mnabadili kilicho duni kwa kilicho bora?”

Aliwakosoa Mayahudi kwa kutaka chakula duni, japokuwa walikuwa wakiishi maisha mepesi, wakila chakula chenye ladha, chakula safi na chenye faida. Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ibn Abi Hatim 1:193.

² At-Tabari 2:130.

أَهْبِطُوا مِصْرًا

“Nendeni kwenye mji.”

Ina maana: “Mji wowote.” kama Ibn Abbas رضي الله عنهما alivyosema.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى pia aliripoti kuwa Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi bin Anas walisema kuwa Aya ina maana Misri ya Firauni.² Ukweli ni kuwa Aya ina maana ya mji wowote, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما na wanazuoni wengine walivyoeleza. Hivyo maana ya kauli ya Musa عليه السلام kwa Wana wa Israeli inakuwa, “Mnachokitaka ni chepesi, kwani kinapatikana kwa wingi mji wowote mtakaoingia.”

Kwa kuwa mlichokiomba kinapatikana katika miji yote. Sitomuomba Allah تعالى Atupatie, hasa kwa vile ni chakula dhalili. Hii ndio sababu Musa عليه السلام aliwaambia,

أَسْتَبْدِلُونَ الَّذِي هُوَ أَدْنَىٰ بِالَّذِي هُوَ خَيْرٌ أَهْبِطُوا مِصْرًا فَإِنَّ لَكُمْ مَا سَأَلْتُمْ³

“Mnabadili kilicho duni kwa kilicho bora? Shukeni mjini, huko mtapata mlivyoviomba.”

Kwa maana mlichokidai, kwa kuwa maombi yao yalikuwa kwa njia ya kuchosha na ufedhuli hakukuwa na haja ya kutekelezwa. Maombi yao yalikataliwa, Allah تعالى Anajua zaidi.

وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ⁴ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا

يَكْفُرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّنَ بِغَيْرِ الْحَقِّ⁵ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا

يَعْتَدُونَ ﴿٥٨﴾

“...Na wakapigwa na unyonge, na umasikini na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa Maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabii pasipo haki. Hayo ni kwa walivyoasi na wakapindukia mipaka.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:194.

² At-Tabari 2:134.

Mayahudi Walipigwa Unyonge na Umasikini

Allah تعالى Amesema,

وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ

“Na wakapigwa na unyonge, na umasikini”.

Aya hii inaonesha kuwa Wana wa Israeli walipigwa na unyonge, na hali hii ni endelevu. Wataendelea kuwa wanyonge mbele ya wale watakaoingiliana nao, pamoja na kuhisi fedheha. Al-Hasan alitoa maoni kuwa, “Allah تعالى Aliwadhalilisha na hawatakuwa na mkombozi. Allah تعالى Amewaweka chini ya nyayo za Waislam, ambao walianza kuwepo wakati Majus wakitoza Jizyah (kodi) kutoka kwa Mayahudi.” Aidha¹, Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas na As-Suddi walisema neno, “Umasikini” lina maana ya ‘ufukara uliotopea’². Atiyah Al-Awfi alisema kuwa “Umasikini” lina maana “kulipa kodi”. Kwa nyongeza Adh-Dhahhak ameitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى,

وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ

“Na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.”

Walistahiki Hasira za Allah تعالى.³ Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa,

وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ

“Na wakastahili Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.”

Walistahiki Hasira na Ghadhabu. Kitenzi “Baa” katika Mukdadha wa lugha ya kiarabu, maelezo yake yanaweza yakafuatana na utendaji wa jambo la kheri au shari. Kwa kuzingatia hilo, ndio maana Allah تعالى Akasema katika Sura ya *al-Maida*.

إِنِّي أُرِيدُ أَنْ تَبُوءَ بِإِثْمِي وَإِثْمِكَ

“Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako.” (5:29).

¹ Ibn Abi Hatim 1:195 na 196.

² Ibn Abi Hatim 1:196.

³ At-Tabari 2:138.

Ina maana, “Utaishia kubeba dhambi zangu na zako badala yangu.” Hivyo, maana ya Ayah inakuwa, “Walirejea wakiwa na Ghadhabu ya Allah تعالى. Ghadhabu ya Allah تعالى iliwashukia; walistahili Hasira za Allah تعالى.”¹ Kauli ya Allah تعالى,

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيِّنَ بِغَيْرِ الْحَقِّ

“Na haya ni kwa sababu walikuwa wakiyakataa Maneno ya Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabii pasipo haki.”

Maana yake: “Haya ndio Tuliowapa Wana wa Israeli: unyonge na umasikini. Ghadhabu za Allah تعالى ziliwashukia Wana wa Israeli ilikuwa ni sehemu ya unyonge walioupata, kwa sababu ya Kukengeuka ukweli, kutoamini Aya za Allah تعالى na kuwadharau wachukuzi wa Sheria za Allah تعالى, Mitume na wafuasi wao. Wana wa Israeli waliwakataa Manabii na hata waliwaua. Kwa hakika hapana ukafiri mbaya kama kukanusha Aya za Allah تعالى na kuwaua Mitume wa Allah تعالى.

Maana ya Kiburi.

Hadith zilizoandikwa ndani ya Sahihi mbili zinasema Mtume ﷺ alisema,

«الْكِبْرُ بَطْرُ الْحَقِّ وَرَعْمَطُ النَّاسِ»

“Kibr ni kukanusha ukweli na kuwadhalilisha watu.”²

Imam Ahmad aliandika, Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَشَدُّ النَّاسِ عَذَابًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ رَجُلٌ قَتَلَهُ نَبِيٌّ أَوْ قَتَلَ نَبِيًّا: وَإِمَامٌ صَلَّى وَنَمَلٌ مِنَ الْمُتَمَلِّينَ»

“Mwenye adhabu kali zaidi siku ya kiyama ni mtu aliyeliwa na Mtume au aliyemuua Mtume, kiongozi mpotevu na mtu anayekata viungo vya maiti.”³

¹ Rejea.

² Muslim 1:93.

³ Ahmad 1:407.

Kauli ya Allah تعالى،

ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ

“Hayo ni kwa walivyoasi na wakapindukia mipaka.”

Inataja sababu nyingine iliyowafanya wana wa Israeli waadhibiwe hivyo, kwani walikuwa wakiasi na kupindukia mipaka. Kuasi ni kufanya yaliyokatazwa, wakati kupindukia mipaka ina maana kuruka mipaka ya yale yaliyoruhusiwa na yale yaliyokatazwa. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

* * *

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّٰدِقِينَ
 وَالصَّٰدِقِينَ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ
 صَالِحًا فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا
 هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾ وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ
 الطُّورَ خُذُوا مَا ءَاتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ وَاذْكُرُوا مَا فِيهِ لَعَلَّكُمْ
 تَتَّقُونَ ﴿٦٣﴾ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ مِنْ بَعْدِ ذَٰلِكَ فَلَوْلَا فَضْلُ
 اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَكُنْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٤﴾ وَلَقَدْ
 عَلَّمْنَا الَّذِينَ ءَاعْتَدُوا مِنْكُمْ فِي السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا
 قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿٦٥﴾ فَجَعَلْنَاهَا نَكَالًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا
 خَلْفَهَا وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٦٦﴾ وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ
 إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذْبَحُوا بَقَرَةً قَالُوا أَتَتَّخِذُنَا هُزُوًا
 قَالَ أَعُوذُ بِاللَّهِ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٦٧﴾

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا
 وَالصَّٰدِقِينَ وَالصَّٰدِقِينَ مَنْ ءَامَنَ
 بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِلَ صَالِحًا
 فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ
 عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

62. "Hakika Walioamini, na
 Mayahudi na Wakristo, na
 Wasabai; yeyote atakaye-
 muamini Mwenyezi
 Mungu na Siku ya Mwisho
 na akatenda mema basi
 watapata malipo yao kwa
 Mola wao Mlezi, wala
 haitakuwa khofu juu yao,
 wala hawatahuzunika."

Imani na Kufanya Amali
 Njema ni Msingi wa
 Kuokoka Zama Zote

Baada ya Allah تعالی Kuelezea masharti – na adhabu kwa wote waliovunja Amri Zake, wakaasi Aliyoyakataza na wakapindukia mipaka, Ameerleza kuwa mataifa adilifu na tiifu walipata malipo mazuri kwa amali zao njema. Hali hii itadumu mpaka siku ya Hukumu. Kwa hiyo yeyote atakayemfuata Nabii na Mtume ﷺ asiyejua kusoma na kuandika atapata furaha ya kudumu na hataogopa yatakayotokea siku zijazo au kuwa na huzuni kwa yale yaliyompata siku zilizopita. Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

"Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika." (10:62)

Malaika watawatangazia waumini wanaokufa, kama ilivyotajwa,

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا
وَأُبَشِّرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٥﴾

“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa.” (41:30)

Maana ya Muumini.

Ali Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Abbas رضي الله عنه kuhusu,

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالنَّصَارَى وَالصَّبِيَّانَ مَن ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
“Hakika Walioamini, na Mayahudi na Wakristo, na Wasabai; yeyote atakayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”¹

Kuwa Allah تعالى Aliteremsha Aya ifuatayo baadaye,

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٨٥﴾

“Na anayetaka Dini isiyokuwa ya Uislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa mwenye hasara kubwa.” (3:85)

Kauli hii ya Ibn Abbas رضي الله عنهما inaashiria kuwa Allah تعالى Hakubali kutoka kwa mtu yeyote utaratibu na amali yoyote, mpaka ikubaliane na Sharia ya Muhammad ﷺ ambayo ni, baada ya Allah تعالى Kومتوما Muhammad ﷺ. Kabla ya hapo kila mtu aliyefuata muongozo wa Mtume wake alikuwa katika njia sahihi, akifuata muongozo sahihi.

Kwa nini Mayahudi Wanaitwa “Yahuud”

Mayahudi walikuwa wafuasi wa Mtume Musa عليه السلام ambaye walikuwa wakihukumiana kwa kufuata Taurati katika zama zao. Yahuud ni neno litokanalo na neno Al-hawaadah, nalo ni Al-Mawaddah, au At-Tahawwud lenye maana, “kutubu” kama Musa عليه السلام alivyosema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:198.

إِنَّا هُدْنَا إِلَيْكَ

“Kwa hakika tunatubia (Hudna) kwako.” (7:156)

Maana yake: Tunatubia kwako. Hii inaonesha kuwa mwanzo waliitwa *Yahuud* kwa sababu walitubia na, kupendana wao kwa wao. Pia Inasemekana kwamba waliitwa *Yahuud* wakirejea kwa Yahuda (Yudah) mtoto wa kwanza wa Mtume Yaqub عليه السلام. Abu Amr bin Al-Ala amesema kuwa waliitwa *Yahuud* kwa sababu walikuwa wakiyumba yumba wakati wa kusoma Taurati.

Kwa nini Wakristo Waliitwa “Nasara”

Isa عليه السلام alipopelekwa kwa Wana wa Israeli walitakiwa kumfuata na kumtii. Wafuasi wa Isa عليه السلام na masahaba wake waliitwa *An-Nasara*, kwa sababu walisaidiana na kunusuriana baina yao. Aidha wanaitwa *Ansar* (Wasaidizi) kama Isa عليه السلام alivyosema,

مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ

“Nani Wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu? Wakasema wanafunzi (Al-Hawariyyun): Sisi ni Wasaidizi wako kwa Mwenyezi Mungu!” (61:14).

Inasemwa kuwa walikuwa wanaitwa “*Nasara*” kwa sababu waliishi katika ardhi iliyoitwa *An-Nasirah* (Nazareth) kama Qatadah, Ibn Jurayj na Ibn Abbas walivyoripotiwa.¹ Allah تعالى Ndiye Mjuzi. *Nasara* ni wingi wa *Nasran*.

Waumini.

Allah تعالى Alipomtuma Muhammad ﷺ kama Nabii na Mtume wa mwisho kwa Wana wa Adam wote, binadamu walitakiwa kumuamini, kumtii na kuyaacha yote aliyowakataza, waliotekeleza haya, ndio Waumini wa kweli. Ummah wa Muhammad ﷺ waliitwa “*Mu'min*” (Waumini) kwa sababu ya Imani yao thabiti, na kwa sababu waliwaamini Mitume wote waliopita na waliamini mambo ya ghaibu.

¹ Ar-Razi 3:97.

Sabiin - Saibuun

Kuna maoni tofauti kuhusu nani ni *Sabiin*. Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema kutoka kwa Layth bin Abu Sulaym kutoka kwa Mujahid alisema “*Sabiin*” ni watu kati ya Majusi, Mayahudi na Wakristo. Hawana dini maalumu.¹ Maelezo sawa na hayo yameripotiwa kutoka kwa Ibn Abu Najih.² Kauli sawa na hizo zinanasibishwa na Ata na Said bin Jubayr.³ Wengine wanasema kuwa *Sabiin* ni madhehebu miongoni mwa Watu wa Kitabu ambao walikuwa wakisoma Zabur. Wengine wanasema ni watu waliokuwa wakiabudu malaika na nyota. Na rai iliyo karibu sana na ukweli, Allah تعالى Ndiye Ajuaye zaidi. Ni ya Mujahid na wale wanaokubaliana naye, kama Wahb bin Munabih, kuwa *Sabiin* si Mayahudi au Wakristo au Majusi au Wapagani. Bali hawakuwa na dini maalumu waliyoifuata na kuitia nguvu, kwani waliendelea kuishi kwa mujibu wa *Fitrah*, yaani kama walivyo bila ya kufuata dini yoyote. Hii ndio sababu washirikina wakiwaita wale waliosilimu, “*Sabi*.” Maana yake waliacha dini zote zilizokuwepo duniani, wakati huo. Baadhi ya wanazuoni walieleza kuwa *Sabiin* ni wale wasiopokea ujumbe kutoka kwa Mtume yeyote. Na Allah تعالى ni Mjuzi wa Yote.

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ وَاذْكُرُوا مَا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٦٣﴾ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَكُنْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٤﴾

63. “Na Tulipochukua ahadi yenu, na Tukaunyanyua mlima juu yenu (Tukakuambieni): Shikeni kwa nguvu haya Tuliyokupeni, na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kuwa Wachamungu.”

64. “Kisha mligeuka baada ya haya. Na lau kuwa si Fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na Rehema Zake, mngelikuwa miongoni mwa wenye kuhasirika.”

¹ At-Tabari 2:146.

² Rejea.

³ Ibn Abi Hatim 1:199-200.

Kuchukua Ahadi kutoka kwa Mayahudi, Kuinuliwa Mlima Turi Juu Yao na Kukengeuka Kwao Baadaye.

Allah تعالی Anawakumbusha Wana wa Israeli kuhusu ahadi juu ya utii na agano, Aliyoichukua kutoka kwao, Kumuamini Yeye Pekee, bila mshirika, na kufuata Manabii Wake.

Allah تعالی Aliyasema haya wakati Alipochukua ahadi kutoka kwao, Aliinua mlima juu ya vichwa vyao ili wathibitisha ahadi waliyompa Allah تعالی na kushikamana nayo kwa ukamilifu na uaminifu.

Hivyo Allah تعالی Alisema,

﴿ وَإِذْ نَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَأَنَّهُمْ كَانُوا ظُلَّةً وَظَنُّوا أَنَّهُمْ وَقِيعٌ حَرِيمٌ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ
وَأَذْكُرُوا مَا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴾

“Na pale Tulipounyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilichowafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (Tukawaambia): Kamateni kwa nguvu Tuliyokupeni na yakumbukeni yaliyomo ndani yake ili mpate kumcha Mungu.” (7:171).

Mlima uliotajwa hapa ni *At-Tur*, kama ilivyoielezwa ndani ya *Surat Al-Araf*, kwa mujibu wa *Tafsir* ya Ibn Abbas, Mujahid, Ata, Ikrimah, Al-Hasan, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi bin Anas na wengine رضي الله عنهم.¹

Hii iko wazi. Kuna ripoti nyingine kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, “*Tur* ni aina ya mlima ambapo mimea inaota, na kama hauna mimea, huitwi kwa jina hilo.”²

Na kuhusu hadithi inayozungumzia mitihani, Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Mayahudi walipokataa kumtii Allah تعالی, Allah تعالی Akawanyanyulia mlima juu yao ili wapate kusikia.”³

¹ Ibn Abi Hatim 1:203.

² Ibid. Isnadi yake ni dhaifu.

³ An-Nasai katika Al-Kubraa 6:396.

خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ

“Shikeni kwa nguvu haya Tuli yokupeni.”

Maana yake: Taurati.¹ Mujahid alisema kuwa Ayah iliamrisha, “Shikamaneni nayo kwa dhati.”² Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi walisema kuwa,

وَأَذْكُرُوا مَا فِيهِ

“Na yakumbukeni yaliyomo ndani yake.”

Maana yake, “Isomeni Taurati na mtekeleze mafunzo yake.”³ Na Kauli Yake Allah تعالى,

ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ مِّنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ

“Kisha mligeuka baada ya haya. Na lau kuwa si Fadhila za Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: “Pamoja na ahadi mliyoitoa, bado mlikengeuka na mkavunja miadi.”

فَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ

“Na lau kuwa si Fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na Rehema Zake.”

Maana yake: Kwa Kukusameheni na kwa Kukuleteeni Mitume na Manabii.

لَكُنْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٧﴾

“Mngelikuwa miongoni mwa wenye kuhasirika.”

Ina maana katika maisha ya leo na kesho kiama kutokana na kuvunja kwao ahadi.

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِينَ آَعْتَدُوا مِنكُمْ فِي السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِرِينَ ﴿٦٧﴾ جَعَلْنَاهَا

نَكَالًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٦٧﴾

¹ Ibn Abi Hatim 1:204.

² Ibn Abi Hatim 1:205.

³ Ibn Abi Hatim 1:205.

65. “Na hakika mlikwishayajua yale ya wale miongoni mwenu walioivunja Sabato, (siku ya mapumziko, Jumamosi) na Tukawaambia: Kuweni manyani wadhhalilifu.”

66. “Kwa hiyo Tukayafanya hayo kuwa onyo kwa wale waliokuwa katika zama zao na waliokuja baada yao, na mawaidha kwa Wachamungu.”

Mayahudi Walivunja Ibada ya Mapumziko (Sabato) na Kugeuzwa Manyani na Nguruwe.

Allah تعالی Amesema,

وَلَقَدْ عَلَّمْتُمُ

“Na hakika mlikwisha yajua.”

Aya hii ina maana, “Enyi Mayahudi! Kumbukeni kuwa Adhabu ya Allah تعالی Aliyoituma katika kijiji kilichomuasi Yeye, na kuvunja ahadi ya utii na miadi ya mapumziko ya Sabato. Walianza kutumia njia za udanganyifu ili kukwepa kuitukuza Sabato kwa kuweka nyavu, kamba na madimbwi ya maji ya kutengeneza, kwa lengo la kuvua kabla ya Sabato. Samaki walipokuja kwa wingi kama ilivyo ada siku ya Jumamosi, walishikwa katika kamba na nyavu kwa siku nzima ya Jumamosi, Usiku, Mayahudi walikusanya samaki baada ya kwisha sabato. Walipofanya hayo, Allah تعالی Aliwageuza kutoka binadamu na kuwa nyani, wanyama wanaofanana na binadamu. Hivyo ndio Vitendo vyao viovu na udanganyifu ulioonekana kwa sura ya nje ni jambo jema, lakini kwa uhakika ndani yake ni uhabithi. Haya yameelezwa kwa urefu katika *Surat Al-Araf*, ambayo Allah تعالی Amesema,

وَسَأَلْتَهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ إِذْ يَعْدُونَ فِي السَّبْتِ إِذْ تَأْتِيهِمْ
حِيَتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرْعًا وَيَوْمَ لَا يَسْبِتُونَ لَا تَأْتِيهِمْ كَذَلِكَ نَبْلُوهُمْ بِمَا كَانُوا

يَفْسُقُونَ ﴿١٦٣﴾

“Na waulize habari za mji uliokuwa kando ya bahari, wakiivunja Sabato (Jumamosi ya mapumziko). Samaki walikuwa wakiwajia juu juu siku ya mapumziko yao, na siku zisiokuwa za kupumzika hawakuwa wakiwajia. Kwa namna hiyo Tuliwajaribu kwa sababu walikuwa wakifanya upotovu.” (7:163)

Katika Tafsiri yake, al-Awfi aliripoti kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema,

فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿٦٦﴾

“Tukawaambia: Kuweni manyani wadhalifu.”

Ina maana: “Allah تعالى Alivibadili viwiliwili vyao vikawa vya nyani na nguruwe. Vijana walikuwa nyani na wazee waligeuzwa kuwa Nguruwe.”¹ Shayban An-Nahwi aliripoti kuwa Qatadah aliitolea maelezo Aya hii.

فَقُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿٦٦﴾

“Tukawaambia: Kuweni manyani wadhalifu.”

Hawa watu waligeuzwa manyani wanaolia wenye mikia baada ya kuwa wanaume na wanawake.²

Nyani na Nguruwe Waliopo Hawatokani na Vizazi vya Wale Waliobadilishwa.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Wale waliokiuka Utakatifu wa Sabato waligeuzwa nyani, kisha wakapotea bila kuzaa.”³ Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالى Aliwabadilisha na kuwa nyani kwa sababu ya madhambi yao. Waliishi duniani kwa siku tatu tu, kwani hapana mtu aliyegeuzwa anayeweza kuishi zaidi ya siku tatu. Hawakula, hawakunywa wala hawakuzaa. Allah تعالى Aliwaumba nyani, nguruwe na viumbe wengine ndani ya siku sita ambazo Amezitaja ndani ya Kitabu Chake.”⁴ Hivyo Allah تعالى Aliwageuza watu hawa katika umbile la Nyani. Na Allah تعالى ndio hivyo, Huamua na Kufanya kwa Amtakaye kile Anachotaka. Na Anamgeuza umbile Analotaka. Kauli ya Allah تعالى,

فَجَعَلْنَاهَا نَكَالًا

“Kwa hiyo Tukayafanya hayo kuwa onyo.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:210. Isnadi yake dhaifu.

² Ibn Abi Hatim 1:209.

³ Ibn Abi Hatim 1:209. Isnadi yake ni dhaifu.

⁴ At-Tabari 2:167. Isnadi yake ni dhaifu.

Maana yake Allah تعالى Aliwafanyia hawa watu wa kijiji, ambao walikiuka Utakatifu wa Sabato.

نَكَلًا

“Kuwa onyo.”

Maana: Tuliwapa Adhabu ili yawepo mazingatio. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema kuhusiana na Firauni.

فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٦٥﴾

“Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo.” (79:25)

Kauli ya Allah تعالى,

لَمَّا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا

“Kwa wale walio kuwa katika zama zao na walio kuja baada yao.”

Ina maana kwa vijiji vingine. Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maoni. Maana yake, “Tulikifanya kijiji hiki kuwa mfano kwa vijiji vingine vilivyokuwa pembezoni mwake. Kwa namna Tulivyowaadhibu watu wake.” Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ أَهَلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِّنَ الْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦٧﴾

“Na hakika Tuliangamiza miji iliyo jirani zenu, na Tulitimiza Ishara ili wapate kurejea.” (46:27)

Kwa hiyo Allah تعالى Aliwafanya mfano kwa wale walioishi katika zama zao na wale wa baada ya zama zao, kwa kukihifadhi kisa chao. Hii ndio maana Allah تعالى Akasema,

وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٦٨﴾

“Na mawaidha kwa Wachamungu.” Maana yake: Ukumbusho. Aya hii ina maana, “Mateso na adhabu waliyoyapata wanakijiji hao, ni matokeo ya kujiingiza katika makatazo ya Allah تعالى na udanganyifu wao. Hivyo wale wenye Taqwa lazima wawe makini na kuepuka tabia zao mbaya, ili yaliyokipata kijiji kile yasije kuwapata nao vile vile.” Pia Imam Abu Abdullah bin Battah رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَزْكِبُوا مَا آزَتْكَبْتِ الْيَهُودُ فَتَسْتَجِلُّوا مَحَارِمَ اللَّهِ بِأَذْنَى الْحَيْلِ»

“Msifanye makosa waliyoyafanya Mayahudi, wakakiuka Aliyoyakataza Allah kwa kufanya hila duni.”¹

Hadithi hii ina isnadi ya upokezi ulio mzuri (Jayyid). Allah تعالى ni Mjuzi wa Yote.

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذْخَبُوا بَقْرَةَ ط قَالَوٓا أَنْتَخِذْنَا هٰزُوا ط قَالَ أَعُوذُ

بِاللَّهِ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٦٧﴾

67. “Na Musa alipowaambia watu wake: Hakika Mwenyezi Mungu Anakuamrisheni mchinje ng’ombe. Wakasema, je! Unatufanyia mzaha? Akasema: (Audhubillahi!) Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wajinga.”

Kisa cha Myahudi Aliyeuawa, na Kisa cha Ng’ombe.

Allah تعالى Alisema, “Enyi Wana wa Israeli! Kumbukeni Neema Yangu juu yenu katika muujiza wa ng’ombe ambao ulibainisha na kumtambua muuaji, wakati Allah تعالى Alipomfufua mtu aliyeuliwa, na kisha kumtaja katika wao aliyeua.” Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kutoka kwa Abidah As-Salmani, “Alikuwepo mtu miongoni mwa Wana wa Israeli ambaye alikuwa mgumba. Alikuwa na mali nyingi, na alikuwepo mpwa wake aliyestahiki kumrithi. Hivyo mpwa wake akamuua na akauhamisha mwili wake usiku, na akauweka nje ya mlango wa mtu fulani. Siku ya pili mpwa yule alipiga kelele kuwa angelipiza kisasi na watu wakachukua silaha karibu wapigane. Watu wenye hekima miongoni mwao wakasema, “Kwanini muuwane wakati Nabii wa Allah bado tunaye?” Hivyo wakaenda kwa Musa عليه السلام na wakamuelezea kisa chenyewe, Musa عليه السلام akasema,

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذْخَبُوا بَقْرَةَ ط قَالَوٓا أَنْتَخِذْنَا هٰزُوا ط قَالَ أَعُوذُ بِاللَّهِ أَنْ أَكُونَ مِنَ

الْجَاهِلِينَ ﴿٦٧﴾

¹ Irwah Al-Ghalil 5:375.

“...Hakika Mwenyezi Mungu Anakuamrisheni mchinje ng’ombe. Wakasema, je! Unatufanyia mzaha? Akasema: Audhubillahi! Najikinga kwa Mwenyezi Mungu nisiwe miongoni mwa wajinga”.

Amesema: “Kama wasingedadisi, ingewatosha wao kumchinja ng’ombe yoyote. Hata hivyo walizidi kudadisi, na suala likafanywa gumu kwao, mpaka ikabidi watafute ng’ombe mwenye sifa maalumu waliyeamrishwa kumchinja. Walimkuta ng’ombe mteule kwa mtu pekee aliyemiliki ng’ombe huyo mmoja tu. Alisema, “*Wallahi!* Nitamuuza kwa ujazo wa dhahabu wa ngozi yake. Hivyo walilipa ujazo wa dhahabu kwa ngozi yake, wakamchinja na wakamgusisha maiti sehemu ya nyama. Maiti ilisimama na wakamuuliza, “Nani aliyekuuu?” Akajibu, “Huyu hapa!” Akamuonesha mpwa wake. Akafa tena, na mpwa wake hakuruhusiwa kumrithi.”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliripoti kisa kinachofanana na hicho. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.²



¹ Ibn abu Hatim 1:114.

² At-Tabari 2:183.

قَالُوا أَدْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَنَا مَا هِيَ ۚ
 قَالَ إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَا فَارِضٌ
 وَلَا بَكْرٌ عَوَانُ بَيْنَ ذَلِكَ ۗ فَافْعَلُوا
 مَا تُؤْمَرُونَ ﴿٦٨﴾ قَالُوا أَدْعُ لَنَا
 رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَنَا مَا لَوْثُهَا ۗ قَالَ إِنَّهُ
 يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ صَفْرَاءُ فَاقِعٌ لَوثُهَا
 تَسْرُ الْأَنْظُرِينَ ﴿٦٩﴾ قَالُوا أَدْعُ لَنَا
 رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَنَا مَا هِيَ ۚ إِنَّ الْأَبْقَرَ تَشْبَهُ
 عَلَيْنَا وَإِنَّا إِن شَاءَ اللَّهُ لَمُهْتَدُونَ ﴿٧٠﴾ قَالَ
 إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَا ذَلُولٌ تُثِيرُ الْأَرْضَ وَلَا تَسْقِي
 الْحَرْتَ مُسَلِّمَةٌ لَا شِيَةَ فِيهَا ۗ قَالُوا الْكَيْفَ جِئْتَ بِالْحَقِّ ۗ
 فَذَخَّوْهَا وَمَا كَادُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧١﴾ وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا
 فَآذَرْتُمْ فِيهَا ۗ وَاللَّهُ مُخْرِجُ مَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٧٢﴾ فقلنا
 أَصْرَبُوهُ بِبَعْضِهَا ۗ كَذَلِكَ يُخَيِّئُ اللَّهُ الْأَمْوَثَ وَيُرِيكُمْ
 ءَايَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٧٣﴾ ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُمْ مِنْ بَعْدِ
 ذَلِكَ فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً ۗ وَإِنَّ مِنْ الْحِجَارَةِ
 لَمَا يَتْفَجِرُ مِنْهُ الْأَنْهَارُ ۗ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَشَّقِقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ
 الْمَاءُ ۗ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ
 عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٧٤﴾

68. "Wakasema: Tuombe kwa Mola wako Mlezi Atupambanulie ni ng'ombe gani? Akasema: Hakika

Yeye Anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu wala si kindu, bali ni wa katikati baina ya hao. Basi fanyeni mliyoamrisha."

69. "Wakasema: Tuombe kwa Mola wako Atupambanulie nini rangi yake? Akasema: Yeye Anasema, kuwa ng'ombe huyo ni wa manjano, na rangi yake imekoza, huwapendeza wanaomtizama."

70. “Wakasema: Tuombe kwa Mola wako Mlezi Atupambanulie ni yupi? Hakika tunaona ng’ombe wamefanana. Na kwa yakini, Inshaalah, Mwenyezi Mungu Akipenda, tutaongoka.”

71. “Akasema: Yeye Anasema kuwa huyo ni ng’ombe asiyetiwa kazini kulima ardhi wala kumwagia maji mimea, mzima, hana baka. Wakasema: Sasa umeleta haki. Basi wakamchinja, na walikaribia kuwa wasifanye hayo.”

Ukorofi wa Mayahudi Kuhusu Wasifu wa Ng’ombe; na Allah تعالی Alivyowafanyia Ugumu Juu Yake.

Allah تعالی Alitaja ukorofi wa Wana wa Israeli pamoja na maswali mengi yasiyo na maana waliyoyauliza kwa Manabii wao.

Hii ndio sababu walipofanya ukorofi, Allah تعالی Alifanya maamuzi magumu kwao. Wangemchinja ng’ombe yoyote angekuwa ametosheleza, kama Ibn Abbas na Ubaydah رضي الله عنهما walivyosema. Baada yake walilifanya suala kuwa gumu, na hii ndio sababu iliyomfanya Allah تعالی Kulifanya hilo kuwa gumu kwao. Walisema,

أَدْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَنَا مَا هِيَ

“Tuombe kwa Mola wako Mlezi Atupambanulie.”

Maana yake: “Ni Ng’ombe wa aina gani na ana sifa zipi?” Musa عليه السلام alisema,

إِنَّهُ يَقُولُ إِنَّهَا بَقَرَةٌ لَا فَارِضٌ وَلَا بَكْرٌ

“Akasema: Hakika Yeye Anasema kwamba ng’ombe huyo si mpevu wala si kindi.”

Maana yake: Si mkongwe wala Ndama. Haya ni maoni ya Abu Al-Aliyah, As-Suddi, Mujahid, Ikrimah, Atiyah Al-Awfi, Ata, Al-Khurasani, Wahb bin Munabbih, Adh-Dhahhak, Al-Hasan, Qatadah na Ibn Abbas.¹ Adh-Dhahhak aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

¹ Ibn abi Hatim 1:216.

عَوَانٌ بَيْنَ ذَلِكَ^ط

“Bali ni wa katikati baina ya hao.”

Maana yake: “Si mpevu wala kindu. Bali alikuwa na umri ambao Ng’ombe anakuwa na nguvu na anafaa kuliwa.”¹ Na Mujahid amesema: “Hakika huyo alikuwa ni ng’ombe wa rangi ya njano.”² Mkolezo wake unakurubia katika weupe. Ibn Abuu Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Al-Hasan katika Kauli Yake Allah تعالى:

فَاقِعٌ لَوْنُهَا

“Rangi yake imekoza.”

Amesema: Mwenye weusi uliokoleza mno. Na mtazamo huu si sahihi. Mtazamo ulio sahihi ni wa mwanzo. Na kwa kuzingatia hilo, amesisitiza umanjano wake kuwa ni “Manjano iliyokoza.” As-Suddi alisema,

تَسْرُ النَّظِيرِينَ

“Huwapendeza wanaomtizama.”

Maana yake: “Kuwa anamridhisha anayemtazama.”³ Hii pia ni rai ya Abu Al-Aliyah, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas.⁴ Zaidi ya hayo, Wahb bin Munabbih alisema, “Ukiangalia ngozi ya ng’ombe utadhani miale ya jua inatoa mwanga kupitia ngozi yake.”⁵ Toleo jipya la Taurati linataja kuwa ng’ombe aliyetajwa katika Ayah alikuwa mwekundu, lakini ni kosa. Au, inawezekana kuwa rangi ya ng’ombe huyo ilikuwa njano iliyokoza na kuonekana nyeusi au nyekundu. Allah تعالى ni Mjuzi wa yote.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ الْبَقَرَ تَشَبَهَ عَلَيْنَا

“Hakika tunaona Ng’ombe wamefanana?”

Ina maana: Kuwa Ng’ombe wako wengi basi tueleze sifa za Ng’ombe huyo.

¹ Ibn abi Hatim 1:217.

² Ibn abi Hatim (706) 1:139.

³ Ibn abi Hatim 1:222.

⁴ At-Tabari 2:219.

⁵ At-Tabari 1:202.

وَإِنَّا إِن شَاءَ اللَّهُ

“Na kwa yakini, Inshaalah...” Endapo utatupa maelezo zaidi,

لُمَهْتَدُونَ ﴿٦٧﴾

“Tutaongoka.”

قَالَ إِنَّهُ يُقُولُ إِنَّهَا بَقْرَةٌ لَا ذَلُولٌ تُثِيرُ الْأَرْضَ وَلَا تَسْقِي الْحَرْثَ

“Akasema: Yeye Anasema kuwa huyo ni ng’ombe asiyetiwa kazini kulima ardhi wala kumwagia maji mimea.”

Ina maana: “Hatumiki kulima au kumwagilia maji mashamba. Bali awe amehifadhika na anayependeza.” Abdur-Razaq alisema kutoka kwa Ma’mar kutoka kwa Qatadah alisema kuwa,

مُسَلَّمَةٌ

“Hana baka.” Maana: “Ng’ombe asiye na dosari yeyote.”¹ Hii pia ni rai ya Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi. Mujahid alisema pia kuwa Ayah hii ina maana ya Ng’ombe asiye na kasoro.² Zaidi ya hayo, Ata al-Khurasani alisema kuwa Aya ile ina maana kuwa miguu yake na mwili wake haukuwa na upungufu wowote.³

فَذَنُّوْهَا وَمَا كَادُوا يَفْعَلُونَ ﴿٦٨﴾

“Basi wakamchinja, na walikaribia kuwa wasifanye hayo.”⁴

Addhahak amesimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa maana yake ni: “Hawakutaka kumchinja.” Ina maana: Hata baada ya maswali na majibu yote juu ya sifa za ng’ombe, Mayahudi walikuwa hawajaridhia kumchinja ng’ombe. Sehemu hii ya Qur’an inakosoa tabia ya Mayahudi, kwa sababu shabaha yao ilikuwa kufanya ukorofi, na hii ndio sababu walikuwa karibu wasimchinje ng’ombe. Pia Ubaydah, Mujahid, Wahb bin Munabbih, Abu Al-Aliyah na Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam walisema, “Mayahudi walimnunua ng’ombe kwa fedha nyingi.”⁵ Na ndani yake kuna mitazmo tofauti Kuna rai nyingine kuhusu hili.

¹ At-Tabari 2:214.

² Ibn Abi Hatim 1:225.

³ Ibn Abi Hatim 1:226.

⁴ At-Tabari 2:219.

⁵ At-Tabari 2:221.

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادْرَأْتُمْ فِيهَا ^ط وَاللَّهُ مَخْرُجٌ مَّا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٦٨﴾ فَعَلْنَا آصْرَهُهُ بِبَعْضِهَا
كَذَلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَىٰ وَيُرِيكُمْ ءَايَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦٩﴾

72. "Na mlipomuua Mtu, kisha mkakhitilafiana kwayo, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyatoa hayo mliyo kuwa mnayaficha."

73. "Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (ng'ombe huyo). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu Huwahuisha wafu; na Anakuonesheni Ishara Zake ili mpate kufahamu."

Kuhushwa Aliyeuliwa, na Kubainika kwa Muuaji

Al-Bukhari alisema kuwa,

فَادْرَأْتُمْ فِيهَا ^ط

"Kisha mkakhitilafiana kwayo."

Maana yake: "Walibishana."³ Hii pia ndio Tafsir ya Mujahid. Ata Al-Khurasani na Adh-Dhahhak walisema, "Mlibishana kuhusu suala hili."⁴ Aidha, Ibn Jurayj amesema:

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادْرَأْتُمْ فِيهَا ^ط

"Na mlipomuua tu, kisha mkakhitilafiana kwayo."

Maana yake: Baadhi yao walisema, "Mlimuua" wengine wakasema, "Hapana, nyie ndio mliomuua."⁵ Hii pia ni *Tafsir* ya Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Mujahid alisema kuwa,

وَاللَّهُ مَخْرُجٌ مَّا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٦٨﴾

"Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyatoa hayo mliyokuwa mnayaficha."

Maana yake: "Yale mliyokuwa mkiyaficha."⁴ Allah تعالیٰ Amesema,

¹ Fat'hul Al-Bari 6:506.

² Ibn Abu Hatim 1:229.

³ At-Tabari. 2:225.

⁴ At-Tabari 2:255.

فَقُلْنَا أَضْرِبُوهُ بِبَعْضِهَا

“Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (ng’ombe huyo).”

Maana yake: “Sehemu yoyote ya Ng’ombe itatoa muujiza endapo maiti yule atapigwa nayo.” Hatukuambiwa ni sehemu gani ya ng’ombe iliyotumika, kwa kuwa suala hili halina faida katika maisha au Dini. Vinginevyo Allah تعالى Angetubainishia. Na wala pia hakuna maandiko sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ yaliyobainisha hilo, hivyo nasi tuliache kama lilivyo.

Kauli ya Allah تعالى،

كَذَلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَى

“Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu Huwahuisha wafu.”

Ina maana: “Walimpiga na sehemu ya nyama hiyo, na akafufuka.” Ayah hii inaonesha Uwezo wa Allah تعالى Kuhuisha kilichokufa. Allah تعالى Alifanya tukio hili ili iwe dalili dhidi ya Mayahudi kwa kuwa kufufuliwa kutakuwepo, na lilimaliza ubishi na ukaidi wao kuhusu mtu yule aliyekufa. Allah تعالى Ametaja kufufua waliokufa katika matukio matano ndani ya *Surat Al-Baqarah*. Mwanzo Allah تعالى Alisema،

ثُمَّ بَعَثْنَاكُمْ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكُمْ

“Kisha Tukakufufueni baada ya kufa kwenu.” (2:256)

Kisa hiki cha Ng’ombe. Allah تعالى pia Ametaja kisa cha wale waliosalimika kutokana na kufa katika nchi yao, wakati idadi yao ilikuwa maelfu (Al-Baqara 243). Pia Alieleza kisa cha Mtu aliyepita kwenye kijiji kilichoangamizwa (Al-Baqara 259), kisa cha Ibrahim na ndege wane (Al-Baqara 260). Na ardhi inayohuika baada ya kufa. Matukio na visa vyote vinatuzindua kuwa miili itarudia hali yake ya mwanzo baada ya kuoza.

Pia kufufuliwa kumerejewarejewa katika Kauli ya Allah تعالى،

وَأَيُّهُمْ الْأَرْضُ الْأَمْيَةُ أَحْيَيْنَاهَا وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٢٥٧﴾ وَجَعَلْنَا

فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْنَابٍ وَفَجَّرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٢٥٨﴾ لِيَأْكُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ وَمَا

عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٢٥٩﴾

“Na Ishara hiyo kwao - ardhi iliyokufa, nasi Tukaifufua, na Tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila! Na Tukafanya ndani yake bustani za mitende na mizabibu, na Tukatimbua chemchemi ndani yake. Ili wale matunda yake, na hayo hayakufanywa na mikono yao! Basi je hawashukuru?” (36:33-35)

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُمْ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً وَإِنَّ مِنَ الْحِجَارَةِ لَمَا يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الْأَنْهَارُ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَشَقَّقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْمَاءُ وَإِنَّ مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٧٤﴾

74. “Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi; kwani kuna mawe yanayotimbuka mito, na kuna mengine yanayopasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na mnayo yafanya.”

Ugumu wa Nyoyo za Mayahudi.

Allah تعالی Aliwakosoa Wana wa Israeli kwa sababu walishuhudia miujiza mingi na Aya za Allah تعالی, ikiwa ni pamoja na kuhuishwa kwa maiti, bado,

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُمْ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ

“Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo.” Hivyo mioyo yao ilikuwa kama mawe na haikuwa laini. Hii ndio sababu Allah تعالی Aliwakataza Waumini kuwaiga Mayahudi, aliposema,

• أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ

أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَسِقُونَ ﴿٥٧﴾

“Je! Wakati haujafika bado kwa walioamini zikanyenyekea nafsi zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyoteremka? Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotofu.” (57:16)

Katika Tafsir yake, Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Yule maiti alipopigwa na sehemu ya ng'ombe, alikaa na akawa hai kuliko alivyowahi kuwa." Akaulizwa, "Nani aliyekuua?" Akajibu, "Wapwa wangu ndio walioniua." Kisha akafa tena. wapwa wake wakasema baada ya Allah تعالى Kuchukua uhai wake, "Wallahi! Hatukumuuu". Wakakanusha ukweli japo waliujua. Allah تعالى Amesema,

فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً

"Hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi."¹ Baada ya muda kupita, nyoyo za Wana wa Israeli hazikutaka kuonyeka, hata baada ya kuona miujiza na ishara. Mioyo yao ilikuwa migumu kuliko mawe bila matarajio ya kulainika kamwe. Wakati fulani, chemchemi na mito zilipasuka kutoka kwenye mawe, baadhi ya mawe yalipasuka na yakatoka maji, hata ambapo hazikuwepo chechemi au mito pambezoni mwake. Baadhi ya mawe yalianguka kutoka kileleni mwa milima kwa kumnyenyekea Allah تعالى. Na hilo linafahamika na Allah تعالى Mwenyewe. Kama Allah تعالى Alivyosema:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿١٧﴾

"Zinamtakasa mbingu zote saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghfira." (17:44)

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَإِنْ مِنْ الْحِجَارَةِ لَمَا يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الْأَنْهَارُ وَإِنْ مِنْهَا لَمَا يَشْقُقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْمَاءُ وَإِنْ مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ

"Kwani kuna mawe yanayotimbuka mito, na kuna mengine yanayopasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu."

¹ At-Tabari 2:234.

Maana yake: “Baadhi ya mawe ni laini kuliko mioyo yenu, yanajua ukweli ambao mmelinganiwa.”

وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na mnayoyafanya.”

Kuwepo kwa Nguvu ya Utambuzi katika Vitu Yabisi

Baadhi wanadai kuwa Aya kutaja kuwa baadhi ya mawe ni manyenyekevu ni lugha ya sitiari kama ambavyo ukuta ulipewa sifa ya kuwa na utashi.

Katika Kauli Yake Allah تعالى:

يُرِيدُ أَنْ يَنْقُضَ

“...ukuta unataka kuanguka” (18:77)

Hata hivyo, Ar-Razi رحمه الله تعالى, Al-Qurtubi رحمه الله تعالى na Maimamu wengine walisema hapana haja ya maelezo haya, kwa sababu Allah تعالى Huumba sifa hizi za unyenyekevu kwenye vitu kwa mfano, Allah تعالى Alisema,

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ تَحْمِلَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا

“Kwa hakika Sisi Tuliidhihirisha Amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa.” (33:72)

Aidha Allah تعالى Amesema:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ

“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake.” (17:44)

Na Amesema,

وَالنَّجْمُ وَالشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ﴿٥٥﴾

“Na mimea yenye kutambaa, na miti, inanyenyekea.” (55:6)

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ يَتَفَيَّؤُا ظِلَالُهُ

“Je! Hawavioni vitu Alivyoviumba Mwenyezi Mungu – ambavyo vivuli vyake vinazunguka...” (16:48)

قَالَتَا أَتَيْنَا طَائِعِينَ ﴿١١﴾

“Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni Watiifu.” (41:11)

لَوْ أَنزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَىٰ جَبَلٍ

“Lau kuwa Tumeteremsha hii Qur’an juu ya mlima.” (59:21) Na,

وَقَالُوا لَجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدْتُمْ عَلَيْنَا ط قَالَوَا أَنْطَقْنَا اللَّهُ

“Na wao wataziambia ngozi zao, kwa nini mmetushuhudia? Nazo zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu.” (41:21)

Imepokewa katika sahihi kuwa Mtume ﷺ alisema,

«هَذَا جَبَلٌ يُحِبُّنَا وَنُحِبُّهُ»

“Huu Mlima (Uhud) unatupenda na sisi tunaupenda.”¹

Vivyo hivyo, mapenzi ya kisiki cha mtende kwa Mtume ﷺ kama ilivyothi - bitishwa na masimulizi sahihi. Katika Sahihi Muslim imepokewa kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنِّي لَأَعْرِفُ حَجْرًا بِمَكَّةَ كَانَ يُسَلِّمُ عَلَيَّ قَبْلَ أَنْ أُبْعَثَ إِنِّي لَأَعْرِفُهُ الْآنَ»

“Mimi nalifahamu jiwe moja lililoko Makka ambalo lilikuwa likinitolea salamu kabla sijatumwa. Sasa nalifahamu jiwe hilo.”²

Akizungumzia wasifu wa Jiwe Jeusi kuwa,

«إِنَّهُ يَشْهَدُ لِمَنْ اسْتَلَمَ بِحَقِّ يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Siku ya kufufuliwa litawatolea ushahidi wale waliolibusu.”³

¹ Fat’hul Al-Bari 6:98.

² Muslim 3:1782.

³ Ahmad 1:266.

Kuna maandiko mengine kadhaa yenye maana hii. (Angalizo): Wanazuoni wa sarufi ya lugha ya Kiarabu wametofautiana mitazamo yao juu ya maana ya Kauli ya Allah تعالى،

فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً

“Hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi.”

Baada ya kuwafikiana wote kuwa kiunganishi “au” kilichopo katika Aya hii hakikutumika kwa maana ya shaka. Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa “au” hapa ina maana ya “na”. Hivyo, maana inakuwa, “Inakuwa ngumu kama jiwe, na ngumu zaidi.” Hii inafanana matumizi yake na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَلَا تُطِيعُ مِنْهُمْ ءِثِمًا أَوْ كَفُورًا ﴿٧٦﴾

“Wala usimtii miongoni mwao mwenye dhambi au mwenye kufuru.” (76:24)

عُذْرًا أَوْ نُذْرًا ﴿٧٧﴾

“Kwa udhuru au kuonya.” (77:6)

Wanazuoni wengine walisema kuwa “au” hapa ina maana “bali”. Hivyo maana inakuwa, “Ngumu kama jiwe. Bali, ngumu zaidi.” Hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى،

إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً

“...Mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumuogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi...” (4:77)

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٤٧﴾

“Na Tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi.” (37:147)

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٩﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.” (53:9)

Baadhi ya wanazuoni wengine walisema Ayah hii ina maana, mioyo yao ilikuwa ya aina mbili, migumu kama jiwe au migumu kuliko jiwe. Zaidi ya hivyo, Ibn

Jariri رحمه الله تعالى alitolea maelezo kuwa baadhi ya nyoyo ni ngumu kuliko jiwe. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, alipendelea tafsir ya mwisho japokuwa nyingine zinakubalika. Mimi Ibn Kathir nasema Tafsir ya mwisho ni sawa na Maneno ya Allah تعالى,

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا

“Mfano wao ni kama mfano wa aliyeoka moto.” (2:17),

Kadhalika Kauli Yake,

أَوْ كَصَيْبٍ مِّنَ السَّمَاءِ

“Au ni kama mvua kubwa itokayo mbinguni.” (2:19).

Pia ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ

“Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mangati) katika jangwa...” (24:39),

Pia ni sawa na Kauli Yake,

أَوْ كَظُلُمَاتٍ فِي بَحْرٍ لُّجِّيٍّ

“Au ni kama giza katika bahari kuu.” (24:40),

Ina maana: Baadhi yao ni kama mfano wa mwanzo, na baadhi yao ni kama mfano wa pili. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

* * *

* أَفَتَطْمَعُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا لَكُمْ وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ
يَسْمَعُونَ كَلِمَ اللَّهِ ثُمَّ يُحَرِّفُونَهُ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ
يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾ وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا
خَلَا بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ قَالُوا أَتُحَدِّثُونَهُمْ بِمَا فَتَحَ اللَّهُ
عَلَيْكُمْ لِيُحَاجُّوكُمْ بِهِ عِنْدَ رَبِّكُمْ ؕ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٧٦﴾
أَوَلَا يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٧﴾
وَمِنْهُمْ أُمِّيُونَ لَا يَعْلَمُونَ الْكِتَابَ إِلَّا أَمْثَارًا وَإِنْ هُمْ إِلَّا
يُظُنُّونَ ﴿٧٨﴾ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ يَكْتُمُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ
يَقُولُونَ هَذَا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ لِيُشْرَوْا بِهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ فَوَيْلٌ
لَّهُمْ مِمَّا كَتَبَتْ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَهُمْ مِمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٧٩﴾
وَقَالُوا لَنْ نَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَةً ۗ قُلْ أَتُحَدِّثْتُمْ عِنْدَ
اللَّهِ عَهْدًا فَلَنْ تُخْلَفَ اللَّهُ عَهْدَهُ ۗ أَمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا
لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨٠﴾ بَلَىٰ مَنْ كَسَبَ سَيِّئَةً وَأَحَظَّتْ بِهِ
خَطِيئَتُهُ ۗ فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٨١﴾
وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ
الْجَنَّةِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٨٢﴾ وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي
إِسْرَائِيلَ لَا تَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَذِي
الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا
وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا
مِّنْكُمْ وَأَنْتُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٨٣﴾

* أَفَتَطْمَعُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا لَكُمْ وَقَدْ
كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَسْمَعُونَ كَلِمَ اللَّهِ
ثُمَّ يُحَرِّفُونَهُ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ
يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾ وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ
ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَا بَعْضُهُمْ
إِلَىٰ بَعْضٍ قَالُوا أَتُحَدِّثُونَهُمْ بِمَا فَتَحَ
اللَّهُ عَلَيْكُمْ لِيُحَاجُّوكُمْ بِهِ عِنْدَ
رَبِّكُمْ ؕ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٧٦﴾ أَوَلَا
يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ
وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٧﴾

75. "Mnatumai wataku aminini na hali baadhi yao walikuwa wakisikia Maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha wakayabadili baada ya kuwa wameyafahamu, na hali wanajua."

76. "Na wanapokutana na wale walioamini husema: Tumeamini. Na wanapokuwa peke yao, wao kwa wao, husema: Mnawaambia aliyo-kufunulieni Mwenyezi Mungu ili wapate kukuhojini mbele ya Mola wenu Mlezi? Basi hamna akili?"

77. "Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha na wanayo yatangaza?"

Kukatia Tamaa Imani ya Mayahudi Zama za Mtume 𐤀𐤃𐤁𐤏

Allah تعالی Amesema,

﴿ أَفَتَطْمَعُونَ ﴾

“*Mnatumai*” Enyi waumini.

﴿ أَلَا يُؤْمِنُوا لَكُمْ ﴾

“*Watakuaminini.*” Maana yake: Watu hawa watakutiini? Wao ni sehemu ya Mayahudi ambao baba zao walishuhudia dalili zilizo wazi lakini mioyo yao ikawa migumu baadaye. Kisha Allah تعالی Akasema,

﴿ وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَسْمَعُونَ كَلِمَ اللَّهِ ثُمَّ خَرَّفُونَهُ ﴾

“*Na hali baadhi yao walikuwa wakisikia Maneno ya Mwenyezi Mungu (Taurati) kisha wakayabadili.*”

Maana: Walipotosha maana.

﴿ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ ﴾

“*Baada ya kuwa wameyafahamu.*” Wakafahamu, lakini wakapotosha ukweli.

﴿ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴾

“*Na hali wanajua.*” Wakijua dhahiri upotoshaji katika tafsiri zao na ufiisadi waliokuwa wakiufanya. Kauli hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالی,

﴿ فِيمَا نَقُضُوا مِيثَاقَهُمْ لَعَنَّاهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَنَاسَةً يَكْفُرُونَ أَكَلِمَةٍ عَنِ مَوَاضِعِهِ ۗ ﴾

“*Basi kwa sababu ya kuvunja agano lao Tuliwalaani, na Tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanayabadili Maneno kutoka mahali pake.*” (5:13)

Qatadah anazungumzia Kauli ya Allah تعالی,

﴿ ثُمَّ خَرَّفُونَهُ مِنْ بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴾

“*Kisha wakayabadili baada ya kuwa wameyafahamu, na hali wanajua?*”

Kuwa, hawa ni Mayahudi waliokuwa wakiyasikia Maneno ya Allah تعالی, wakayapotosha baada ya kufahamu na kuzingatia.¹

¹ Ibn Abi Hatim 1:236.

Pia Mujahid alisema, “Wale waliokuwa wakibadili na kuficha ukweli, walikuwa wanazuoni wao.”¹ Pia Ibn Wahb alisema kuwa Ibn Zayd alitoa maoni juu ya Kauli ya Allah تعالى,

يَسْمَعُونَ كَلِمَ اللَّهِ ثُمَّ تَحَرَّفُونَهُ

“Walikuwa wakisikia Maneno ya Mwenyezi Mungu (Taurati) kisha wakayabadili.”

“Walibadilisha Taurati waliyoshushiwa na Allah تعالى na kuifanya ihalalishe waliyoharamishiwa, na yaliyokatazwa kuruhusiwa, na sahihi kuwa kosa na kinyume chake. Hivyo mtu akija kutaka ukweli huku akiwa na rushwa, wanahukumu suala lake kwa Kitabu cha Allah تعالى, lakini awajiapo mtu anayetaka kutenda uovu, naye akiwa na rushwa, hutoa kitabu kingine kilichopotoshwa, ambamo imeelezwa kuwa yuko sahihi. Akija mtu asiyetafuta lililo haki na hatoi rushwa, basi wanamlingania kufanya mambo mema. Ndio sababu Allah تعالى Amewaambia,

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴾

“Je! Mnawaamrisha watu mema na manajisahau nafsi zenu, na hali nyinyi mnasoma Kitabu? Basi je, hamzingatii?” (2:44)²

Mayahudi Walijua Ukweli wa Utume wa Muhammad ﷺ na Wala Hawa-kumuamini

Allah تعالى Alisema,

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامِنَّا وَإِذَا خَلَا بِعَضُوبِهِمْ إِلَى بَعْضٍ

“Na wanapokutana na wale walioamini husema: Tumeamini. Na wanapokuwa peke yao, wao kwa wao...”

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى amepokea maelezo kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامِنَّا

“Na wanapokutana na wale walioamini husema: Tumeamini.” “Wanaamini kuwa Muhammad ﷺ ni Nabii wa Allah تعالى lakini alitumwa kwenu (Waarabu).”³

¹ At-Tabari 2:245.

² At-Tabari 2:246.

³ At-Tabari 2:250.

Hata hivyo wakikutana wao kwa wao husema, “Msiwafikishie Waarabu habari za Mtume huyu, kwa sababu mlikuwa mkimuomba Allah تعالى Akupeni ushindi juu yao. Wakati alipokuja, alipelekwa kwao (na si kwenu).” Kisha Allah تعالى Akateremsha,

وَإِذَا لَقُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَا بِبَعْضِهِمْ إِلَىٰ بَعْضٍ قَالُوا أَتُحَدِّثُونَهُمْ بِمَا فَتَحَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ لِيُحَاجُّوكُم بِهِ عِندَ رَبِّكُمْ

“Na wanapokutana na wale walioamini husema: ‘Tumeamini.’ Na wanapokuwa peke yao, wao kwa wao, husema: ‘Mnawaambia Aliyokufunulieni Mwenyezi Mungu ili wapate kukuhojini mbele ya Mola wenu Mlezi?’”

Ina maana: “Kama mtakiri kwao kuwa huyu ni Mtume, huku mkijua kwamba Allah تعالى Alichukua ahadi kutoka kwenu kuwa mtamfuata, watajua kuwa Muhammad ﷺ ni Mtume tuliyekuwa tukimngojea na kuja kwake kulikwisha tabiriwa ndani ya Kitabu chetu. Kwa hiyo msimuamini na mumkane.” Allah تعالى Amesema,

أُولَٰئِكَ يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

“Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza?” (2:77).

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Mayahudi walipokutana na Waislamu walikuwa wakisema, “Tumeamini.” Wakikutana wao kwa wao, baadhi yao husema, “Msiwaambie wafuasi wa Muhammad ﷺ yale Allah تعالى Aliyoyasema ndani ya Kitabu chenu, ili habari kuwa Muhammad ﷺ ni Mtume wa Mwisho haziwi na ushahidi kwao dhidi yenu mbele ya Allah تعالى, na hivyo, mtashinda ubishani huu.”¹

Zaidi ya hivyo, Abu Al-Aliyah alitolea maoni Kauli hii ya Allah تعالى,

أُولَٰئِكَ يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

“Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza?”

¹ Ibn Abi Hatim 1:239.

Ina maana: Kukanusha kwa siri na kumkataa Muhammad ﷺ, japokuwa kuja kwake kumerekodiwa ndani ya Kitabu chao. Hii pia ni *Tafsir* ya Qatadah. Al-Hasan ametoa maoni juu ya,

أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ

“Kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha.”

“Wanayoyaficha.” Inaashiria wakati wakiwa peke yao mbali na Masahaba wa Muhammad ﷺ.

Kisha wakakatazana kufikisha habari kwa Masahaba za kuwa Allah تعالى Aliwateremshia katika Kitabu chao, wakichelea kuwa Masahaba wangelizitumia habari hizi kuhusu ukweli wa Muhammad ﷺ dhidi yao mbele ya Mola wao.¹

وَمَا يُعْلِنُونَ

“Na wanayoyatangaza?”

Ina maana, waliposema kwa Masahaba wa Muhammad ﷺ.

ءَامِنًا

“Tumeamini.”

Kama Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi na Qatadah walivyoelezea.²

وَمِنْهُمْ أُمِّيُونَ لَا يَعْلَمُونَ الْكِتَابَ إِلَّا أَمَانِي وَإِنَّهُمْ إِلَّا يُظُنُّونَ ﴿٧٥﴾ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ
يَكْتُبُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ هَذَا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ لَيْسَتْ رَأْيَ نَمْنًا قَلِيلًا ﴿٧٦﴾ فَوَيْلٌ
لَهُمْ مِمَّا كَتَبَتْ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَهُمْ مِمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٧٧﴾

78. “Na wako miongoni mwao wasiojua kusoma, hawakijui Kitabu ila kwa matamano ya nafsi zao, nao hawana ila ni kudhanja tu.”

79. “Basi ole wao wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu, ili wachumie kwacho pato dogo. Basi ole wao kwa yale iliyoandika mikono yao, na ole wao kwa yale wanayoyachuma.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:239.

² Ibn Abii Hatim 1:240.

Maana ya "Ummi"

Allah تعالى Amesema,

وَمِنْهُمْ أُمِّيُونَ

"Na wako miongoni mwao wasiojua kusoma." Maana yake: Miongoni mwa Watu wa Kitabu, kama alivyosema Mujahid. *Ummiyyun* ni wingi wa *Ummi*, yaani, mtu asiyejua kusoma wala kuandika. Kama abu Al-Aliyah, Ar-Rabi, Qatadah, Ibrahim An-Nakhai na wengine walivyosema. Maana hii inafafanuliwa na Kauli ya Allah تعالى,

لَا يَعْلَمُونَ الْكِتَابَ

"Hawakijui Kitabu." Maana yake: Hawajui kilichomo ndani yake.¹ *Ummi* ilikuwa moja ya sifa za Mtume ﷺ kwa sababu alikuwa hajui kusoma wala kuandika. Kama Allah تعالى Alivyosema,

وَمَا كُنْتُمْ تَتْلُوا مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُمْ بِيَمِينِكُمْ إِذَا لَأَزْتَابِ الْمُبْطِلُونَ ﴿٤٨﴾

"Na hukuwa mwenye kusoma Kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume (ingekuwa hivyo) wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki)." (29:48)

Aidha Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّا أُمَّةٌ أُمِّيَّةٌ لَا نَكْتُبُ وَلَا نَحْسِبُ، الشَّهْرُ هَكَذَا وَهَكَذَا وَهَكَذَا»

*"Sisi ni ummah ummi, hatuandiki wala kuhesabu. Mwezi mwandamo, ni kama hivi, hivi na hivi (yaani siku thelathini au ishirini na tisa)."*²

Hadith hii ilielezea kuwa Waislam hawahitajii kutegemea vitabu vya mahesabu ili kujua nyakati za vitendo vya ibada. Allah تعالى pia Alisema,

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِنْهُمْ

"Yeye Ndiye Aliyempeleka Mtume kwa watu wasiojua kusoma..." (62:2).

¹ Ibn Abi Hatim 1:241.

² Fat'hul Al-Bari 4:151.

Maelezo Kuhusu Neno *Amaaniyya*

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Allah تعالى Amesema,

إِلَّا أَمَانِيَّ

“Isipokuwa amaaniyya (uongo wanaoutamani).” Ina maana: “Watatoa kauli za uongo kwa ndimi zao.”¹ Ilisemekana kuwa *Amaaniyya* maana yake, “Matakwa na matarajio!” Mujahid alitoa maoni, “Allah تعالى Aliwaelezea *Ummiyyin* ni watu wasioelewa chochote kwenye Kitabu cha Allah تعالى alichoteremshiwa Musa عليه السلام, bado wakazua uongo na upotoshaji.”² Kwa hiyo, neno *Amaaniyya* hapa lina maana kusema uongo na upotoshaji. Mujahid alisema kuwa Allah تعالى Alitoa Kauli,

وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ

“*Nao hawana ila ni kudhanian tu.*” Maana yake, “Wanasema uongo.”³ Qatadah, Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi walisema kuwa ina maana, “Wana fikira potofu kuhusu Allah تعالى.”

Ole Wao Mayahudi Hawa Wanaobadili Maneno ya Allah تعالى.

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ يَكْتُمُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ هَذَا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ لِيَشْتَرُوا بِهِمْ ثُمَّ نَمَّا قَلِيلًا

“Basi ole wao wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu, ili wachumie kwacho pato dogo.”

Hili ni kundi jingine la Mayahudi ambao walikuwa wakilingania upotofu kwa kusema uongo kuhusu Mwenyezi Mungu na kufanikiwa kukusanya mali za watu bila haki. “*Waylun* (ole wao)” ina maana ya kuhiliki na kuangamia, na ni neno linalofahamika sana katika lugha ya Kiarabu. Az-Zuhri رحمه الله تعالى alisema kuwa Ubaydullah bin Abdullah رضي الله عنه alisimulia kuwa Ibn Abbas عنهما رضي الله عنهما alisema, “Enyi Waislamu! Inakuwaje mnawauliza Watu wa Kitabu juu ya jambo lolote, ambapo kitabu cha Allah تعالى Alichomteremshia Mtume wake ﷺ, ndio

¹ At-Tabari 2:261.

² At-Tabari 1:262.

³ Ibn Abi Hatim 1:242.

kitabu cha zama hizi kuhusu sharia za Allah تعالى mnakisoma kikiwa kinyemi. Allah تعالى Amewaambia kwamba watu wa Kitabu walikibadilisha Kitabu cha Allah تعالى, na wakaandika kitabu kingine kwa mikono yao. Kisha wakasema, “Hiki kitabu kinatoka kwa Allah تعالى”, ili wapate kunufaika kidogo. Kwani elimu iliyokujieni haijakukatazeni kuwauliza wao jambo? Na *Wallahi!* Hatujamuona yeyote miongoni mwao akiwauliza kuhusu kilichoteremshwa kwenu.”¹

Hadithi hii ilikusanywa pia na Al-Bukhari.² Al-Hasan bin abu Al-Hasan Al-Basri alisema, “Kiasi kidogo” Hapa, ina maana dunia hii na vyote vilivyomo.³ Kauli ya Allah تعالى,

فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ كَفَرُوا مِمَّا كَتَبَتْ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُمْ مِمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٧٦﴾

“Basi ole wao kwa yale iliyoandika mikono yao, na ole wao kwa yale wanayoyachuma.”

Maana yake: “Ole wao kwa sababu ya yale waliyoyaandika kwa mikono yao, ambayo ni uongo, upotoshaji na ubadilishaji. Ole wao kwa sababu ya kutwaa mali kinyume cha sheria.” Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maoni,

فَوَيْلٌ لَّهُمْ

“**Ole wao**” Maana yake: Wanastahiki adhabu kali kwa sababu waliandika uongo kwa mikono yao. Na,

وَوَيْلٌ لَّهُمْ مِمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٧٦﴾

“**Ole wao kwa yale wanayoyachuma**” Alisema, ni vile wanavyokula wao na watu wa chini yao na wengineo.⁴

وَقَالُوا لَنْ نَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَةً ۚ قُلْ أُنذِرْتُمْ عِنْدَ اللَّهِ عَهْدًا فَلَنْ تُخْلَفَ ۚ اللَّهُ

عَهْدُهُ ۗ أَمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

80. “Na walisema: Hautatugusa Moto ila kwa siku chache tu. Sema: Mmechukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu? Kweli Mwenyezi Mungu Hatokwenda kinyume na Ahadi Yake. Au mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyo yajua?”

¹ Ibn Abi Hatim 1:245.

² Fat’hul Baari 5:244, 13:345 na 555.

³ Ibn Abi Hatim 1:247.

⁴ At-Tabari 2:273.

Mayahudi Wanatumaini Kwamba Watakaa Motoni Kwa Siku Chache.

Allah تعالی Anatoa habari za Mayahudi kuhusu madai yao kwamba Moto utawachoma kwa siku chache tu na kwamba wataokolewa. Allah تعالی Amewakatalia madai hayo na Kusema,

قُلْ أَخَذْتُمْ عِنْدَ اللَّهِ عَهْدًا

“Sema: Je Mmepata Ahadi kwa Mwenyezi Mungu?” Maana: Kuhusu jambo hilo, na kwamba ikiwa Ahadi hiyo ipo, basi Yeye Hatoacha Kuitimiza. Hata hivyo haipo bali mnachokisema juu ya Allah تعالی hamna ujuzi nacho, ni uongo na uzushi tu. Al-Awfi alisema kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما amezungumza haya,

وَقَالُوا لَنْ تَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَةً

“Na walisema: Hautatugusa Moto ila kwa siku chache tu.”

Mayahudi walisema, “Moto utatugusa kwa siku arubaini.”¹ Wengine wameongeza kuwa hiki kilikuwa kipindi ambacho Mayahudi waliabudia ng’ombe. Aidha, Al-Hafidh Abubakar bin Marduwyah رحمه الله تعالی aliripoti kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema,

لَمَّا فُتِحَتْ خَيْبَرُ أُهْدِيَتْ لِرَسُولِ اللَّهِ ﷺ شَاةٌ فِيهَا سَمٌّ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «اجْمَعُوا لِي مَنْ كَانَ مِنَ الْيَهُودِ هَهُنَا». فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «مَنْ أَبُوكُمْ؟» قَالُوا: «فُلَانٌ قَالَ: «كَذَّبْتُمْ بِلِ أَبُوكُمْ فُلَانٌ». فَقَالُوا: صَدَقْتَ وَبَرَزْتَ ثُمَّ قَالَ لَهُمْ: «هَلْ أَنْتُمْ صَادِقِي عَنْ شَيْءٍ إِنْ سَأَلْتِكُمْ عَنْهُ؟» قَالُوا: نَعَمْ يَا أَبَا الْقَاسِمِ وَإِنْ كَذَّبْنَاكَ عَرَفْتَ كَذْبَنَا كَمَا عَرَفْتَهُ فِي آيِنَا فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «مَنْ أَهْلُ النَّارِ؟» فَقَالُوا: نَكُونُ فِيهَا يَسِيرًا ثُمَّ تَخَلَّفُونَا فِيهَا فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «اخْسُوا وَاللَّهِ لَا نَخْلُفُكُمْ فِيهَا أَبَدًا». ثُمَّ قَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «هَلْ أَنْتُمْ صَادِقِي عَنْ شَيْءٍ إِنْ سَأَلْتِكُمْ عَنْهُ؟» قَالُوا: نَعَمْ يَا أَبَا الْقَاسِمِ، قَالَ: «هَلْ جَعَلْتُمْ فِي هَذِهِ الشَّاةِ سُمًّا؟» فَقَالُوا: نَعَمْ قَالَ: «فَمَا حَمَلَكُمْ عَلَى ذَلِكَ؟» فَقَالُوا: أَرَدْنَا إِنْ كُنْتَ كَادِبًا أَنْ نَسْتَرِيحَ مِنْكَ وَإِنْ كُنْتَ نَبِيًّا لَمْ يَضُرَّكَ.

“Khaibar ilipokombolewa, Mtume ﷺ aliletwa zawadi. Nyama ya kondoo yenye sumu ililetwa kwa Mtume kama zawadi na Mayahudi.

¹ At-Tabari 2:276.

Mtume wa Allah aliamrisha, "Waambieni Mayahudi waliopo hapa waje mbele yangu! Mayahudi walikusanyika na Mtume akawaambia, "Nani baba yenu?" Wakajibu, "Fulani" Mtume akasema, "Mmeongopa bali baba yenu ni fulani" Wakasema: umesema kweli. Kisha Mtume akawauliza "Je, sasa mtanieleza ukweli endapo nitawauliza kitu?" Wakajibu, "Ndiyo, Ewe Abul Qasim; endapo tutasema uongo, utajua uongo wetu kama ulivyojua kuhusu baba yetu". Kwa hilo akawauliza, "Ni nani watu wa motoni?" Wakajibu, "Tutabaki motoni kwa kipindi kifupi tu, na baada ya hapo nyie mtachukua nafasi yetu." Mtume akasema, "Mlaaniwe na muangamizwe ndani yake! Wallahi katu hatutachukua nafasi yenu.." Kisha akawauliza, "Je, mtaniambia ukweli nikiwaulizeni swali?" Wakajibu, "Ndiyo, ewe Abul Qasim" Akawauliza, "Je, mmetia sumu, hii nyama ya kondoo?" Wakajibu, "Ndiyo" Akauliza, "Kitu gani kilichowafanya mtende hilo?" Wakajibu, "Tulitaka kujua kama wewe ni muongo, ili tuondokane nawe, na kama wewe ni Mtume basi sumu isingekudhuru."¹ Imam Ahmad, Al-Bukhari na an-Nasai waliandika vivyo hivyo².

بَلَىٰ مَنْ كَسَبَ سَيِّئَةً وَأَحَاطَتْ بِهِ خَطِيئَتُهُ فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا
 خَالِدُونَ ﴿٧٥﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا
 خَالِدُونَ ﴿٧٦﴾

81. "Naam, anayechuma ubaya na makosa yake yakamzunguka hao ndio watu wa Motoni; humo watadumu."

82. "Na wale walioamini na wakatenda wema, hao ndio watu wa Peponi, humo watadumu."

Allah تعالیٰ Anasema, suala lenyewe lilivyo, si kama mlivyotaka na mlivyotarajia liwe. Bali yeyote anayefanya vitendo viovu na kwa makusudi akabobea katika makosa, akaja siku ya Kiyama na amali mbovu peke yake, basi atakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.

¹ Dalaail An-Nubuwwah 4:256.

² Ahmad 2:451, Fat'h Al-Bari 6:314 na An-Nasai katika Al-Kubra 6:413.

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Na wale walioamini na wakatenda wema.”

Maana yake: “Wanamuamini Allah تعالى na Mjumbe Wake na wanaotenda mema kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi.” Allah تعالى Amesema sawa na haya.

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ الْكِتَابِ ۗ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ وَلَا يَجِدْ لَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٢٣﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظَلَّمُونَ فِيهَا ۗ ﴿١٢٤﴾

“Si kwa matamano yenu, wala matamano ya Watu wa Kitabu! Anayefanya ubaya atalipwa kwalo, wala hatajipatia Mlinzi wala wa kumnusuru, isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na Anayefanya mema, akiwa mwanaume au mwanamke, naye ni Muumini basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata kadiri ya tundu ya kokwa ya tende.” (4:123-124)

Aidha, Abu Hurayrah, Abu Wail, Ata na Al-Hasan رضي الله عنهم walisema kuwa,

وَأَحْنَطْتُ بِهِ خَطِيئَتُهُ

“Na makosa yake yakamzunguka.”

Maana yake: “Ushirikina wake” umemzunguka.¹ Pia Al-A'mash alipokea kutoka kwa Abu Razin kuwa Ar-Rabi bin Khuthaym alisema,

وَأَحْنَطْتُ بِهِ خَطِيئَتُهُ

“Na makosa yake yakamzunguka.”

“Yeyote atakaye kufa kabla ya kutubia dhambi zake.”² As-Suddi na Abu Razin walisema vivyo hivyo.³ Abu Al-Aliyah, Mujahid, Al-Hasan, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas walisema kuwa,

¹ Ibn Abi Hatim 1:252.

² Ibn Abi Hatim 1:252.

³ Ibn Abi Hatim 1:253.

وَأَحْطَطَتْ بِهٖ حَاطِيَّتُهُۥ

“Na makosa yake yakamzunguka.”

Inakusudiwa madhambi makubwa.¹ Kauli zote hizi zina maana sawa, na Allah تعالى Anajua zaidi.

Mkusanyiko wa Madhambi Madogo Husababisha Maangamivu.

Hapa Tutataja Hadith iliyoandikwa na Imam Ahmad, ambayo Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِيَّاكُمْ وَمُحْتَرَاتِ الذُّنُوبِ فَإِنَّهِنَّ يَجْتَمِعْنَ عَلَى الرَّجُلِ حَتَّى يُهْلِكَنَّهُ»

“Jihadharini na madhambi madogo, kwa sababu yanajikusanya kwa mtu mpaka yanamuangamiza.”

Kisha akasema kuwa Mtume ﷺ aliwapigia mfano,

«كَمَثَلِ قَوْمٍ نَزَلُوا بِأَرْضِ فَلَاةٍ، فَحَضَرَ صَنِيعُ الْقَوْمِ فَجَعَلَ الرَّجُلُ يَنْطَلِقُ فَيَجِيءُ بِالْعُودِ وَالرَّجُلُ يَجِيءُ بِالْعُودِ، حَتَّى جَمَعُوا سَرَاذِمًا وَأَجْجُوا نَارًا فَأَنْضَجُوا مَا قَدَّفُوا فِيهَا»

“Huu ni mfano wa watu waliopiga kambi katika ardhi tambarare na kisha akaja mtumishi wao. Mmoja wao alikusanya mti mmoja wa kuni na mwingine alikusanya mti mmoja wa kuni mpaka zikawa nyingi za kutosha. Kisha wakaoka moto na wakapika vyakula.”²

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٨٢﴾

“Na wale walioamini na wakatenda wema, hao ndio watu wa Peponi, humo watadumu.” (2:82)

¹ Ibn Abi Hatim 1:253.

² Ahmad 1:402.

“Yeyote anayeamini katika yale mliyoyakanusha enyi Mayahudi na akatekeleza yale mliyojizua kuyatekeleza ya Dini ya Muhammad ﷺ, basi hao watakaa Peponi milele. Allah تعالى Amesema kuwa malipo ya mema na maovu yatabaki na wala hayaachani na wahusika wake milele.”¹

وَأَذِّحْنَا مَيْثَقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ لَا تَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَذِي الْقُرْبَىٰ
وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ
إِلَّا قَلِيلًا مِّنْكُمْ وَأَنْتُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٨٣﴾

83. “Na Tulipochukua ahadi na Wana wa Israeli: Hamtamuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu; na muwafanyie wema Wazazi na jamaa na mayatima na masikini na semeni na watu kwa wema, na shikeni Sala na toeni Zaka. Kisha mkageuka isipokuwa wachache tu katika nyinyi; na nyinyi mnapuuza.”

Ahadi Aliyochukua Allah تعالى Kutoka kwa Wana wa Israeli.

Allah تعالى Aliwakumbusha Wana wa Israeli Amri Alizowapa na ahadi Aliyochukua kutoka kwao kuwa watatekeleza Amri hizo, na jinsi walivyozipa mgongo kwa makusudi na kwa kujua. Allah تعالى Aliwaamrisha wamuabudu Yeye na wasimshirikishe na chochote katika kumuabudu, kama Alivyo-waamrisha viumbe Wake wote, kwani hii ndio sababu ya Allah تعالى Kuwaumba. Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾

“Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana muabudiwa isipokuwa Mimi. Basi Niabuduni Mimi tu.” (21:25) Aidha Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ﴿٣٦﴾

“Na kwa hakika kwa kila Ummah Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani.” (16:36)

¹ Ibn Abi Hatim 1:254.

Hii ni haki ya juu na muhimu, maana, Haki ya Allah تعالى ya Kuabudiwa Yeye Peke Yake bila mshirika.

Baada ya hapo inakuja haki ya viumbe, mwanzo kabisa, haki ya Wazazi. Kwa kawaida Allah تعالى Hutaja haki za Wazazi pamoja na haki Zake. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

﴿أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلَوْلَدَيْكَ إِلَى الْمَصِيرِ﴾

“Tumemuusia: Nishukuru Mimi na Wazazi wako. Ni Kwangu Mimi ndiyo marudio.” (31:14),

Pia Allah تعالى Alisema,

﴿وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola wako Mlezi Ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na Wazazi wawili muwatendee wema.” (17:23) Mpaka

وَأَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ

“Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na maskini na msafiri...” (17:26)

Sahihi mbili zimeandika kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema,

قُلْتُ: «يَا رَسُولَ اللَّهِ أَيُّ الْعَمَلِ أَفْضَلُ؟ قَالَ: «الصَّلَاةُ عَلَىٰ وَتَيْهَا» قُلْتُ: ثُمَّ أَيٌّ؟ قَالَ: «بِرُّ الْوَالِدَيْنِ» قُلْتُ: ثُمَّ أَيٌّ؟ قَالَ: «الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Niliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ni amali gani bora?” Akajibu, “Kusali kwa wakati!” Nikauliza, “Kisha ipi?” Akajibu, “Kuwatendea wema Wazazi wawili.” Nikauliza, “Kisha ipi?” Akajibu, “Jihadi katika njia ya Allah”¹.

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَأَلْيَتَمَىٰ

“Na mayatima.” Maana yake: Watoto wasiokuwa na baba wa kuwakimu.

¹ Fat’h al-Bari 6:5 na Muslim 1:89.

وَالْمَسْكِينِ

“Na masikini”

Wingi wa *Miskin*, mtu ambaye hawezi kupata mahitaji yake na ya familia yake. Tutazijadili aina hizi wakati tunaelezea Ayah katika *Surat An-Nisa* ambayo Allah تعالى Ametuamrisha suala hili kwa uwazi, katika Kauli Yake,

﴿وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۚ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

**“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote.
Na wafanyieni wema Wazazi wawili.” (4:36)**

Kauli ya Allah تعالى،

وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا

“Na semeni na watu kwa wema.”

Maana yake: Sema maneno mazuri na uwahurumie, hii ni pamoja na kuamrisha mema na kukataza maovu. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى aliyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالى.

وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا

“Na semeni na watu kwa wema.”

“Maneno Mazuri” Maana Yake: Kuamrisha mema na kukataza maovu, na kuwa na subira na msamehevu.” Maneno mazuri kwa watu, kama Allah تعالى Alivyoamrisha, pia ni pamoja na kila jema linaloridhiwa na Allah تعالى.¹ Imam Ahmad alisimulia kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَحْفِرَنَّ مِنَ الْمَعْرُوفِ شَيْئًا وَإِنْ لَمْ تَجِدْ فَاتَّقِ أَخَاكَ بِوَجْهِ مَنْطَلِقٍ»

“Msidunishe aina yoyote ya jambo jema, hata kama hukuweza kufanya jambo jema basi mlaki nduguyo kwa uso mkunjufu.”

Hadith hii ilikusanywa pia na Muslim katika sahih yake, na At-Tirmidhi aliipa daraja la Sahihi.²

¹ Ibn Abi Hatim 1:258.

² Ahmad 5:173, Muslim 4:2026 na Tuhfatul Al-Ahwadhi 5:526.

Allah تعالی Anawaamrisha waja kusema na watu kwa wema, baada ya Kuwaamrisha kuwahurumia wao kwa vitendo. Hivyo Akataja aina mbili za tabia; kauli nzuri na matendo mazuri. Kisha Akasisitizia Amri ya kumuabudu Yeye na Amri ya kufanya mema, na Akafaradhisha Sala na Zakah, akasema:

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ

“Na shikeni Sala na toeni Zaka.”

Allah تعالی Ametufahamisha kuwa watu wa Kitabu, ukiacha wachache miongoni mwao, walidharau amri hizi, yaani, kwa kujua na kwa makusudi waliziacha. Allah تعالی Aliuamrisha Ummah vivyo hivyo, katika Surat An-Nisai aliposema,

﴿ وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا
مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴾

“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema Wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wenye kiburi wanaojifakhiri.” (4:36)

Kati ya amri hizi, Ummah umezitekeleza kwa vitendo kuliko mataifa yaliyopita. Na Shukrani zote Anastahiki Allah تعالی.

* * *

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ دِمَاءَكُمْ وَلَا تَحْرِجُونَ
 أَنْفُسَكُمْ مِنْ دِينِكُمْ ثُمَّ أَقْرَضْتُمْ وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٨٤﴾ ثُمَّ
 أَنْتُمْ هُنَّؤَلَاءِ تَقْتُلُونَ أَنْفُسَكُمْ وَتَحْرِجُونَ فَرِيقًا مِنْكُمْ
 مِنْ دِينِهِمْ تَظْهَرُونَ عَلَيْهِمْ بِالْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَإِنْ يَأْتُوكُمْ
 أُسْرَى تُمْسِكُوهُمْ وَهُوَ مُحْرَّمٌ عَلَيْكُمْ إِخْرَاجُهُمْ ۗ
 أَفَتُؤْمِنُونَ بِبَعْضِ الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ ۗ فَمَا جَزَاءُ
 مَنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ
 وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ
 عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا
 بِالْآخِرَةِ ۗ فَلَا تُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٨٦﴾
 وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهِ بِالرُّسُلِ ۗ
 وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ ۗ
 أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنْفُسُكُمْ اسْتَكْبَرْتُمْ
 فَفَرِيقًا كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ ﴿٨٧﴾ وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ
 بَلْ لَعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ
 دِمَاءَكُمْ وَلَا تَحْرِجُونَ أَنْفُسَكُمْ مِنْ
 دِينِكُمْ ثُمَّ أَقْرَضْتُمْ وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ
 ﴿٨٤﴾ ثُمَّ أَنْتُمْ هُنَّؤَلَاءِ تَقْتُلُونَ
 أَنْفُسَكُمْ وَتَحْرِجُونَ فَرِيقًا مِنْكُمْ
 مِنْ دِينِهِمْ تَظْهَرُونَ عَلَيْهِمْ بِالْإِثْمِ
 وَالْعُدْوَانِ وَإِنْ يَأْتُوكُمْ أُسْرَى
 تُمْسِكُوهُمْ وَهُوَ مُحْرَّمٌ عَلَيْكُمْ
 إِخْرَاجُهُمْ ۗ أَفَتُؤْمِنُونَ بِبَعْضِ
 الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ ۗ فَمَا جَزَاءُ
 مَنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يُرَدُّونَ
 إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ
 عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ
 اشْتَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ ۗ فَلَا
 تُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ
 يُنصَرُونَ ﴿٨٦﴾

84. "Na Tulipochukua Ahadi yenu kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu; nanyi mkakubali nanyi mnashuhudia."

85. "Kisha nyinyi mnawaua watu wenu, na mnawatoa baadhi yenu katika nyumba zao; mnasaidiana juu yao (katika kuwadhuru) kwa (njia za kukupatisheni) dhambi na (kuonesha) uadui. Na wakikujieni mateka mnawakomboa, na hali imeharamishwa kwenu kuwatoa. Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na kukataa baadhi (yake)?. Basi hakuna malipo kwa

mwenye kufanya haya katika nyinyi ila fedheha katika maisha ya dunia; na Siku ya Kiama watapelekwa katika adhabu kali. na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.”

86. “Hao ndio walionunua uhai wa dunia kwa (uhai wa) Akhera; kwa hivyo hawatapunguziwa adhabu wala hawatanusuriwa.”

Masharti ya Ahadi na Kuivunja Kwake.

Allah تعالی Aliwakosoa Mayahudi waliokuwa wakiishi Madina wakati wa zama za Mtume ﷺ. Walikuwa wakipata taabu, kwa sababu ya mapigano kati ya makabila ya Madina, Aws na Khazraj, wakiabudu masanamu, na kupigana vita vingi baina yao. Yalikuwepo makabila matatu ya Kiyahudi Madina wakati ule, Banu Qaynuqa na Banu an-Nadhir, marafiki wa Khazraj, na Banu Quraydhah, ambao walikuwa ni marafiki wa Aws. Vilipozuka vita baina ya Aws na Khazraj, marafiki zao wa Kiyahudi waliwasaidia. Yahudi alimuua adui yake wa Kiarabu, na wakati mwingine waliwaua Mayahudi waliokuwa marafiki wa Waarabu wengine, japokuwa Mayahudi walizuiwa kuuana wenyewe kwa wenyewe kwa mujibu wa maandiko yaliyo wazi ya Vitabu vyao. Waliweza kufukuzana katika nyumba na kupora kila kitu ikiwa ni pamoja na samani na fedha. Baada ya vita kumalizika, Mayahudi walioshinda waliwaachia wafungwa wa kundi lililoshindwa, kwa kuzingatia maamrishi ya Taurati. Kwa sababu hiyo Allah تعالی Alisema,

أَفْتَوْمُنُونَ بَعْضِ الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضِ

“Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na mnakataa baadhi yake?”

Allah تعالی Alisema,

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُونَ دِمَاءَكُمْ وَلَا تُخْرِجُونَ أَنْفُسَكُمْ مِنْ دِينِكُمْ

“Na Tulipochukua Ahadi yenu kuwa hamtamwaga damu zenu, wala hamtatoana majumbani mwenu.”

Ina maana: “Msiuane wenyewe kwa wenyewe wala msifukuzane kwenye majumba yenu, wala msipigane wenyewe kwa wenyewe” Kama Alivyosema katika Aya nyingine.

فَتُوبُوا إِلَىٰ بَارِيكُمْ فَاقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِنْدَ بَارِيكُمْ

“Basi tubuni kwa Muumba wenu na ziueni nafsi zenu. Haya ni bora kwenu mbele ya Muumba wenu.” (2:54)

Kwa sababu wafuasi wa dini moja ni kama nafsi moja. Aidha Mtume ﷺ alisema,

«مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادُّهِمْ وَتَرَاحُمِهِمْ وَتَوَاصُلِهِمْ بِمَنْزِلَةِ الْجَسَدِ الْوَاحِدِ إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَىٰ لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالْحَمَىٰ وَالسَّهْرِ»

“Mfano wa Waumini katika kufanyiana wema, kurehemeana na kuhurumiana kwao ni mfano wa mwili mmoja, kiungo kimoja kinapougua, mwili mzima hukisaidia kwa kuugua na kukesha.”¹

Kauli ya Allah تعالى

ثُمَّ أَقْرَبْتُمْ وَأَنْتُمْ تَسْهَدُونَ ﴿٥٥﴾

“Nanyi mkakubali nanyi mnashuhudia.”

Ina maana: “Mlitolea ushahidi kuwa mnaijua Ahadi na kuwa mlikuwa Mashahidi.”

ثُمَّ أَنْتُمْ هَتُّوْلَآءٍ تَقْتُلُوْنَ ۖ أَنْفُسَكُمْ وَأَخْرَجُونَ فَرِيقًا مِّنْكُمْ مِّن دِيَارِهِمْ

“Kisha nyinyi mnawaua watu wenu, na mnawatoa baadhi yenu katika nyumba zao...”

Muhammad bin Ishaq bin Yasar رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Abbas رضي الله عنه kuhusu Aya.

ثُمَّ أَنْتُمْ هَتُّوْلَآءٍ تَقْتُلُوْنَ ۖ أَنْفُسَكُمْ وَأَخْرَجُونَ فَرِيقًا مِّنْكُمْ مِّن دِيَارِهِمْ

“Kisha nyinyi mnawaua watu wenu, na mnawatoa baadhi yenu katika nyumba zao.”²

¹ Muslim 4:1999.

² Ibn Abi Hatim 1:262.

Allah تعالی Alitaja waliyokuwa wakiyafanya, na ndani ya Taurati Aliwakataza kuuana wenyewe kwa wenyewe, na Akawataka wawaache huru mateka wao. Wakati huu walikuwa wameshagawika katika makundi mawili walipokuwa Madina, Banu Qaynuqa, ambao walikuwa marafiki wa Khazraj, na An-Nadhir na Quraidhah, ambao walikuwa marafiki wa Aws. Vita vilipozuka baina ya Aws na Khazraj. Banu Qaynuqa, walipigana upande wa Khazraj wakati Banu Nadhir na Quraidhah walipigana upande wa Aws. Kila kundi la Mayahudi lilipigana dhidi ya Ndugu zao wa upande mwingine. Walimwaga damu japokuwa walikuwa na Khazraj ambao walikuwa makafiri walioabudia masanamu. Hawakujua lolote kuhusiana na Pepo, Moto, Kufufuliwa, Vitabu Vitakatifu, Halali na Haramu. Vita vilipokwisha, Mayahudi walilipa fidia ya kuwakomboa wafungwa wao na kutekeleza mafunzo ya Taurati. Vivyo hivyo, Banu Qaynuqa waliwakomboa mateka wao waliotekwa na Aws, ambapo Banu an-Nadhir na Quraydhah waliwakomboa mateka wao waliotekwa na Khazraj. Pia walidai fidia. Wakati wa vita hivi walimuua yeyote (Myahudi au Mwarabu) kwa ajili ya kuwatetea washirikina. Katika Kuwajulisha hilo Allah تعالی Alisema,

أَفْتُوْمُونَ بَعْضِ الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضِ

“Je! Mnaamini baadhi ya Kitabu na mnakataa baadhi yake?”

Ayah hii ina maana, “Je, mnawalipia fidia kwa mujibu wa hukumu ya Taurati, bado mnawaua wakati Taurati iliwakataza kuwaua na kuwatoa majumbani mwao?” Taurati iliwaamrisha kutowasaidia Makafiri wanaomshirikisha Allah katika ibada dhidi ya Ndugu zenu. Mnafanya yote haya ili mnufaike na maisha ya hapa duniani. Nilielezwa kuwa tabia ya Mayahudi kuingilia ugomvi wa Aws na Khazraji ndio ilikuwa sababu ya kuteremshwa Aya hizi. Aya takatifu ziliwakosoa Mayahudi kwa kufuata mafundisho ya Taurati kwa baadhi ya wakati na kuikanusha kwa wakati mwingine, japokuwa waliamini Taurati na walijua waliyokuwa wakiyafanya sio sahihi. Kwa sababu hii haifai kuaminiwa kuihifadhi au kuifundisha Taurati. kwani usalama wake ni mdogo mno. Zaidi ya hayo, wasiaminiwe wanapoeleza sifa za Mitume wa Allah, kuja kwake na kufukuzwa kutoka ardhi yake na *Hijrah* na taarifa walizopewa na Mitume waliotangulia kuhusu Mtume ambazo walizificha. Mayahudi waangamie kwa laana ya Allah تعالی, walificha ukweli wote huu, na ndio sababu Allah تعالی Akasema,

فَمَا جَزَاءُ مَنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ط

“Basi hana malipo mwenye kutenda hayo miongoni mwenu ila hizaya katika maisha ya duniani.”

Kwa sababu waliasi sheria za Allah تعالى na Maamrisho Yake.

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يُرَدُّونَ إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ ط

“Na siku ya Kiyama watapelekwa kwenye Adhabu kali kabisa.”

Kama adhabu ya kuasi Kitabu cha Allah تعالى walichokuwa nacho.

وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ ط

“Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na yale mnayo yatenda. Hao ndio walionunua uhai wa dunia kwa (uhai wa) Akhera.”

Wanachagua maisha ya dunia kuliko ya Akhera,

فَلَا تَخْضَعُونَ لَهُمْ ط

“Kwa hivyo hawatapunguziwa adhabu.”

Hata kwa saa moja.

وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٨٦﴾

“Wala hawatanusuriwa.”

Na hawatapata msaidizi atakayewaokoa kutokana na adhabu ya milele, wala hawatapata mahali pa kukimbilia.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهِ بِالرُّسُلِ ط وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْكِتَابَ

وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ ط أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنْفُسُكُمْ اسْتَكْبَرْتُمْ فَفَرِّقُوا

كُدِّبْتُمْ وَفَرِّقًا تَقْتُلُونَ ﴿٨٧﴾

87. “Na hakika Tulimpa Musa Kitabu na Tukafuatisha baada yake Mitume wengine. Na Tukampa Isa, mwana wa Mariamu, hoja zilizo wazi wazi na Tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu. Basi kila walipokufikieni Mitume kwa yale ambayo hayapendwi na nafsi zenu, mlijivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawaua.”

Kiburi cha Mayahudi Kupinga Kwao Mitume na Kuwaua

Allah تعالى Alielezea ufasiki wa Wana wa Israeli, kuasi kwao, inadi na ufidhuli kwa Mitume wao, wakifuata hawaa na tamaa zao. Allah تعالى Ametaja kuwa Alimpa Musa عليه السلام Kitabu, Taurati na kwamba Mayahudi waliibadilisha, wakaipotosha, na wakaasi Amri Zake, pia kubadilisha maana zake.

Allah تعالى Alituma Manabii na Mitume baada ya Musa عليه السلام waliohukumu kwa Sharia Zake, kama Allah تعالى Alivyosema,

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ تَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا
وَالرَّهْبَانِيُّونَ وَالْأَحْبَارُ بِمَا اسْتَحْفَظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءً

“Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walionyenyekia Kiislamu, na Wachamungu, na wanazuoni, waliwahukumu Mayahudi, kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Nao wakawa ni Mashahidi juu yake.” (5:44)

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema hapa,

وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهِ بِالرُّسُلِ ط

“Na Tukafuatisha baada yake Mitume.”

As-Suddi alisema kuwa Abu Malik alisema, *Qaffayna* maana yake “Tukafuatisha”, wengine wanasema, “Tukapeleka.”¹ Maana zote zinakubalika, kwani Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn abi Hatim 1:268.

ثُمَّ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا تَتْرًا^ط

“Kisha Tukawatuma Mitume wetu, mmoja baada ya mmoja.” (23:44)

Baadaye, Allah تعالی Alimtuma Mtume wa mwisho miongoni mwa Wana wa Israeli, Isa mwana wa Mariam عليه السلام, ambaye alikuja na sharia ambazo baadhi zilitofautiana na zile za Taurati. Hii ndio sababu Allah تعالی Alipeleka miujiza ili kumsaidia Isa عليه السلام. Hiyo ni pamoja na kuhuisha wafu, kutengeneza umbile la ndege kutokana na udongo na kuwapulizia, baada ya hapo wakawa ndege hai kwa Uweza wa Allah تعالی, kuponya wagonjwa na kubashiri ghaibu, kama ibn Abbas رضي الله عنهما alivyosema.¹ Pia Allah تعالی Alimsaidia kwa *Ruh – Al-Qudus*, yaani Jibril عليه السلام. Alama zote hizo zilithibitisha ukweli wa Isa عليه السلام na ujumbe aliokuja nao. Pamoja na hayo Wana wa Israeli walikuwa masafihii na wakamuonea wivu kutokana na baadhi ya yaliyokuwa ndani ya Taurati. Kama Allah تعالی Alivyotaja kuhusu Isa عليه السلام,

وَلِأَجْلِ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ^ع وَجِئْتُمْ بِقَايَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ

“Na ili Nikuhalalishieni baadhi ya yale mliyoharamishiwa, na nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu.” (3:50)

Hivyo, Wana wa Israeli waliwatendea ubaya Mitume, wakiwakataa baadhi yao na wengine baadhi wakiwaua. Yote haya yalijiri kwa sababu Mitume walikuwa wakiwaamrisha Mayahudi yale yaliyokuwa tofauti na maoni na utashi wao. Pia Mtume ﷺ waliyatetea maamrishi ya Taurati ambayo Mayahudi waliyabadilisha, na hii ndio sababu ilikuwa vigumu kwao kuwaamini Mitume hao. Kwa hiyo, waliwakataa Mitume na waliwaua baadhi yao. Allah تعالی Amesema,

أَفَلَمْ يَأْتِكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُكُمْ أَسْتَكْبِرْتُمْ فَحَرِيقًا كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ ﴿٢٧٠﴾

“Basi kila walipokufikieni Mitume kwa yale ambayo hayependwi na nafsi zenu, mlilivuna; wengine mkawakanusha, na wengine mkawaua.”

¹Ibn abi Hatim 1:268.

Jibril ni *Ruh Al-Qudus* - Roho Mtakatifu

Uthibitisho kwamba Jibril عليه السلام ni *Ruh Al-Qudus* ni kauli ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه alipokuwa anaitolea maelezo Ayah hii.¹ Hii pia ni rai ya Ibn Abbas, Muhammad bin Ka'ab, Ismail bin Khalid, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas, Atiyah al-Awfi na Qatadah رضي الله عنهم.² Nyongeza ya hayo Allah تعالى Amesema,

نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾

“Ameteremsha Roho muaminifu, juu ya moyo wako, ili uwe katika waonyaji.” (26:193-194)

Al-Bukhari aliandika kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alijenga Mimbari ndani ya Masjid ambapo Hasan bin Thabit رضي الله عنه (mshairi maarufu) alikuwa akimtetea Mtume ﷺ (kwa mashairi yake). Mtume ﷺ alisema,

«اللَّهُمَّ أَيِّدْ حَسَانَ بَرُوحِ الْقُدْسِيِّ كَمَا نَافَعَ عَنْ نَبِيِّكَ»

“Ewe Allah! Msaidie Hassan kwa Ruh Al-Qudus kama alivyomlinda Mtume Wako.”³

Abu Dawud aliandika *Hadith* hii katika Sunan yake⁴ kama alivyofanya At-Tirmidhi aliyeipa daraja la Hasan Sahih.⁵ Zaidi ya hayo, Ibn Hibban رضي الله عنه aliandika katika Sahih yake kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ رُوحَ الْقُدْسِيِّ نَفَتْ فِي رُوعِي أَنَّهُ لَنْ تَمُوتَ نَفْسُ حَتَّى تَسْتَكْمَلَ رِزْقَهَا وَأَجَلَهَا، فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَجْمِلُوا فِي الطَّلَبِ»

“Hakika Ruh Al-Qudus alinifahamisha kuwa hakuna roho itakayokufa mpaka imalize riziki yake na muda wake. Kwa hiyo Mcheni Allah na fanyeni vizuri katika kutafuta.”⁶

¹ Ibn Abi Hatim 1:269.

² Ibn Abi Hatim 1:270.

³ Fat'hul al-Bari 10:562.

⁴ Abu Dawud 5:279.

⁵ Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:137.

⁶ Angalia As-Sunnah 14:304.

Mayahudi Walijaribu Kumuuu Mtume ﷺ.

Az-Zamakhshari رحمه الله تعالى aliyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالى،

﴿فَفَرِيقًا كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ﴾

“Wengine mkawakanusha, na wengine mkawaua.”

Allah تعالى Hakusema “mmewaua” kwa wakati uliopita, kwa kuwa Allah تعالى Anataka kubainisha ya kuwa bado Mayahudi tabia hiyo wangalinayo, wangejaribu kumuua Mtume ﷺ siku zijazo, kwa kutumia sumu au uchawi. Wakati akiagua kabla ya kufikwa na kifo, Mtume ﷺ alisema,

«مَا زَالَتْ أَكْلُهُ خَيْرٌ نَعَارِدُنِي، فَهَذَا أَرَأَيْتَ أَنْتِ قَطَاعِ أَبْهَرِي»

“Niliendelea kuhisi madhara ya kile nilichokula (kondoo aliyetiwa sumu) siku ile ya Khaibar, mpaka sasa, wakati ni muda wa kukatwa mkole (maana yake mauti yako karibu).”¹

Mimi bin Kathir nasema: Hadith hii imenukuliwa na Bukhari na wengineo.²

﴿وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۚ بَلْ لَعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ﴾

88. “Na walisema: Nyoyo zetu zimefunikwa. Bali Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru zao: kwa hivyo ni kidogo tu wanayo-yaamini.”

Muhammad ibn Is-Haq رحمه الله تعالى alipokea kuwa Ibn abbas رضي الله عنهما alisema،

﴿وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ﴾

“Na walisema: Nyoyo zetu zimefunikwa”.

Maana: “Nyoyo zetu zimezibwa.”³

Mujahid pia alisema،

¹ Ibn ‘Adi 3:1239.

² Fat’hul Al-Bari 7:737.

³ At-Tabari 2:326.

وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ

“Na walisema: Nyoyo zetu zimefunikwa.”

Maana: “Zimefichwa.”¹ Ikrimah alisema, “Zilipigwa muhuri.”² Abu Al-Aliyah alisema, “Hazizingatii.”³ Mujahid na Qatadah walisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisoma Aya katika njia ambayo ilikuwa ina maana, “Mioyo yetu imejaa kila aina ya elimu na hatuhitaji elimu uliyo nayo (Ewe Muhammad).”⁴ Alisoma, “*Qulubuna ghulufu...*” kwa kuipatia herufi “*Lamu*” irabu ya *dhwammah*. Neno *ghulf* ni wingi wa neno *ghulufu*. Hii ni rai ya Ata na Ibn Abbas رضي الله عنهما.

بَل لَّعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ

“Bali Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru zao”

Ina maana: Allah تعالى Aliwafukuza na Kuwapokonya kila aina ya uadilifu. Qatadah alisema kuwa Aya hii,

فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ

“Kwa hivyo ni kidogo tu wanayoyaamini.”

Maana yake: Wachache tu ndiyo wanaoamini.⁵ Kauli ya Allah تعالى,

وَقَالُوا قُلُوبُنَا غُلْفٌ

“Na walisema: Nyoyo zetu zimefunikwa.”

Ni sawa na Kauli Yake hii,

وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي أَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ

“Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko kwa hayo unayotuitia.” (41:5)

Na hii ni rai iliyopewa uzito na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.

¹ Rejea.

² Ibn Abi Hatim 1:274.

³ Ibn Abi Hatim 1:273.

⁴ Al-Qurtubi.

⁵ Ibn Abi Hatim 1:274.

Hii ndiyo sababu Allah تعالى Alisema hapa,

بَل لَّعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٤﴾

“Bali Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru zao: Kwa hivyo ni kidogo tu wanayoyaamini.”

Maana yake: Si kama wanavyodai. Bali, mioyo yao imelaaniwa na kupigwa mihuri, kama Allah تعالى Alivyosema ndani ya Surat An-Nisai.

وَقَوْلِهِمْ قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۚ بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥٥﴾

“Na kusema kwao: Nyoyo zetu Zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu Amezipiga mihuri kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu.” (4:155)

Kuna rai tofauti kuhusu maana ya Kauli ya Allah تعالى,

فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٤﴾

“Kwa hivyo ni kidogo tu wanayo yaamini.” Na Kauli Yake,

فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥٥﴾

“Basi hawaamini ila kidogo tu.” (4:155)

Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa Aya inaonesha kuwa wachache kati yao wataamini, au imani yao ni ndogo sana, kwa sababu wanaamini Kiyama na Malipo na Adhabu ya Allah تعالى kama walivyowahi kuelezwa na Musa عليه السلام. Pamoja na hayo, imani hii haitowasaidia kwani ilifunikwa na kutoamini aliyokuja nayo Muhammad ﷺ. Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa Mayahudi kwa hakika hawakuamini chochote na kuwa Allah تعالى Amesema,

فَقَلِيلًا مَّا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٤﴾

“Kwa hivyo ni kidogo tu wanayo yaamini.”

Maana yake: Hawaamini. Maana hii ni sawa na msemu wa Kiarabu, “Jambo hili nimeliona kwa nadra.” Maana yake: “Sijaona kabisa jambo kama hili.”

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ وَكَانُوا
 مِن قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا
 عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ ۗ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾
 بِئْسَمَا اشْتَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ أَنْ يَكْفُرُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 بَغْيًا أَنْ يَنْزِلَ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ عَلَى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ
 فَبَاءُوا بِغَضَبٍ عَلَى غَضَبٍ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُّهِينٌ
 ﴿٩٠﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ءَامِنُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا تَوْحِينٌ
 بِمَا عَلَيْنَا وَكَفْرُونَ ۗ بِمَا وَرَّاءَهُ وَهُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا
 لِّمَا مَعَهُمْ ۗ قُلْ فَلِمَ تَقْتُلُونَ أَنْبِيَاءَ اللَّهِ مِنْ قَبْلُ إِنْ كُنْتُمْ
 مُّؤْمِنِينَ ﴿٩١﴾ * وَلَقَدْ جَاءَكُمْ مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ
 اتَّخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ ظَالِمُونَ ﴿٩٢﴾ وَإِذْ
 أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ خُذُوا مَا
 ءَاتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ وَاسْمِعُوا ۗ قَالُوا سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَأَشْرَبْنَا
 فِي قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ ۗ قُلْ بِئْسَمَا يَأْمُرُكُمْ بِهِ
 إِيمَانُكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٩٣﴾

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ
 مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ وَكَانُوا مِن قَبْلُ
 يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا
 فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ ۗ
 فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾

89. "Na kilipowajia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinachothibitisha waliyo nayo na wao wali-kuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri yalipowajia yale waliyokuwa waki-yajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao."

Mayahudi Walikuwa Waki-subiri Ujio wa Mtume ﷺ, Lakini Walimkanusha Ali-potumwa.

Allah تعالى Amesema,

وَلَمَّا جَاءَهُمْ

"Na kilipowajia." Maana yake, 'Mayahudi'.

كِتَابٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ

"Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu."

Maana yake: Qur'an ambayo Allah تعالى Aliishusha kwa Muhammad ﷺ.

مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ

“Kinachothibitisha waliyo nayo.”

Maana yake: Taurati. Zaidi ya hivyo Allah تعالى Amesema,

وَكَاثِرُونَ مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا

“Na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri.”

Ina maana, kabla ya kuja kwao Nabii huyu, walikuwa wakimuomba Allah تعالى Amtume ili awasaidie dhidi ya maadui zao washirikina iwapo watapigana nao katika vita. Walikuwa wakiwaambia washirikina, “Mtume atatumwa kabla ya mwisho wa dunia, na sisi, tukishirikiana naye tutakuangamizeni, kama mataifa ya ‘Ad na Iram walivyoangamizwa.” Pia Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mayahudi walikuwa wakimuomba Allah تعالى (Amlete Muhammad ﷺ) ili awawezeshe kuwashinda Aws na Khazraj, kabla ya kutumwa Mtume. Allah تعالى Alipompeleka kwa Waarabu, walimkataa na wakamkanusha kuwa walikuwa wakimtaka. Hivyo, Muadh bin Jabal na Bishr bin Al-Bara bin Ma’rur رضي الله عنهما ndugu wa kabila la Bani Salamah, waliwaambia, “Enyi Mayahudi, Mcheni Allah تعالى na ingieni kwenye Uislamu. Mlikuwa mkimuomba Allah تعالى Akuleteeni Muhammad ﷺ wakati sisi tukiwa katika ushirikina na mlikuwa mkituambia kuwa atakuja na mkawa mnatuelezea alivyo.” Salam bin Mushkam wa kabila la Bani An-Nadhir alijibu, “Hakuleta chochote tunachokitambua. Huyu siye Mtume tuliyekuelezeni habari zake.” Kisha Allah تعالى Akateremsha Aya hii kujibu kauli yao,

وَلَمَّا جَاءَهُمْ كِتَابٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ

“Na kilipowajia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinachothibitisha waliyonayo.”¹

Abu Al-Aliyah alisema, “Mayahudi walikuwa wakimuomba Allah تعالى Amtume Muhammad ﷺ ili waweze kuwashinda washirikina wa Waarabu. Walikuwa wakisema, “Ewe Allah! Mtume Nabii ambaye tunasoma habari zake ndani ya Taurati – ili tuwapige na tuwaue washirikina tukiwa naye.” Allah تعالى

¹ At-Tabari 2:333.

Alipompeleka Mtume Muhammad ﷺ na wakasema hakuwa miongoni mwao, walimkataa na wakawaonea inda Waarabu, japokuwa walikuwa wakifahamu alikuwa Nabii wa Allah تعالى. Hivyo Allah تعالى Akasema,

﴿ فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِمْ ۗ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴾

“Yalipowajia yale waliyokuwa wakiyajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao.”¹

﴿ يَسْمَا أَشْتَرُوا بِهِمْ أَنْ يَكْفُرُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ بَغْيًا أَنْ يُنَزِّلَ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ عَلَىٰ

مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ فَبَاءُوا بِغَضَبٍ عَلَىٰ غَضَبٍ ۖ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُهِيبٌ ﴾

90. “Kiovu kweli walichojiuzia nafsi zao, nacho ni kule kukataa kwao Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya kuona mapya kwa kuwa Mwenyezi Mungu Humteremshia Fadhila Yake Amtakaye miongoni mwa waja Wake. Basi wamejiletea wenyewe ghadhabu juu ya ghadhabu. Na makafiri watapata mateso ya kudhalilisha.”

Mujahid alisema,

﴿ يَسْمَا أَشْتَرُوا بِهِمْ أَنْفُسَهُمْ ﴾

“Kiovu kweli walichojiuzia nafsi zao.”

Mayahudi waliuza ukweli kwa batili na walificha ukweli juu ya Muhammad ﷺ.² As-Suddi alisema kuwa Aya,

﴿ يَسْمَا أَشْتَرُوا بِهِمْ أَنْفُسَهُمْ ﴾

“Kiovu kweli walicho jiuzia nafsi zao.”

Maana yake: “Mayahudi walijiuzia wenyewe.”³ Maana yake: Ubaya ulioje kwa wao, kujichagulia kwao kukanusha yale Allah تعالى Aliyomteremshia Muhammad ﷺ badala ya kumuamini, kumsaidia na kumuunga mkono. Tabia yao hii ndio matokeo ya dhuluma, inda na chuki.

¹ Ibn Abi Hatim 1:276.

² At-Tabari 2:340.

³ Ibn Abi Hatim 1:277.

أَنْ يُنَزَّلَ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ عَلَيَّ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ^ط

“Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Humteremshia Fadhila Yake Amtakaye miongoni mwa waja Wake.”

Hapana inda mbaya kama hii kwa hiyo,

فَبَاءُوا بِغَضَبٍ عَلَيَّ غَضَبٍ^ع

“Basi wamejiletea wenyewe ghadhabu juu ya ghadhabu.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما aliielezea Aya hii, “Allah تعالى Aliwakasirikia kwa sababu walipuuza baadhi ya mafunzo ya Taurati na walimkana Mtume ambaye Alitumwa kwao.”¹ Mimi (Ibn Kathir) nasema kuwa maana ya,

فَبَاءُوا

“Basi wamejiletea wenyewe.”

Ni kuwa walistahili kupata ghadhabu juu ya ghadhabu. Pia, Abu Al-Aliyah alisema, “Allah تعالى Aliwaghadhabikia, kwa sababu ya kukadhibisha yaliyomo katika Injili na kumkadhibisha Isa عليه السلام na Akawaghadhabikia tena, kwa sababu walimkanusha Muhammad ﷺ na Qur’an.”² Sawa na haya yalisemwa na Ikrimah na Qatadah.³ Allah تعالى Amesema,

وَاللَّكَفِرِينَ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿٦٠﴾

“Na makafiri watapata mateso ya kudhalilisha.”

Kwa kuwa kukufuru kwao kulikuwa ni matokeo ya kuchupa mipaka na inda ambavyo vilisababishwa na usafihi, waliadhibiwa kwa kuteswa na kudhalilishwa duniani na Kiyama. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦١﴾

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhaliike.”(40:60)

¹ Ibn Abi Hatim 1:279.

² Ibn Abi Hatim 1:278.

³ Ibn Abi Hatim 1:279.

Maana yake: "Hali ya kuwa dhalili, duni na wanyonge." Imam Ahmad alisimulia kutoka kwa Amr bin Shua'ybu alisema kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُحَسَّرُ الْمُتَكَبِّرُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَمْثَالَ الذَّرِّ فِي صُورِ النَّاسِ، يَغْلُوهُمْ كُلُّ شَيْءٍ مِنَ الصَّغَارِ حَتَّى يَدْخُلُوا سِجْنًا فِي جَهَنَّمَ يُقَالُ لَهُ. بَوَّاسٌ تَغْلُوهُمْ نَارُ الْأَنْتَارِ يُسْتَوْنَ مِنْ طَيْبَةِ الْخَبَالِ عُصَارَةَ أَهْلِ النَّارِ»

*"Watakusanywa wenye kiburi mafidhuli siku ya Kiyama, wadogo kama sisimizi, lakini katika umbile la binadamu. Kila kitu kitakuwa juu yao, kwa sababu ya kudhalilishwa, mpaka waingizwe ndani ya gereza, Jahannam inayoitwa, "Bawlasu" ambapo watazingirwa na moto kutoka juu. Watakunywa kutokana na usaha wa tupu za watu wa Motoni."*¹

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ءَامِنُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا تَقُولُوا نَحْنُ مُؤْمِنُونَ بِمَا وَرَأَاهُ
 وَهُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِمَا مَعَهُمْ قُلْ فَلِمَ تَقْتُلُونَ أَنْبِيَاءَ اللَّهِ مِنْ قَبْلُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ
 ﴿٢٠٦﴾ * وَلَقَدْ جَاءَكُمْ مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ أَخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَنْتُمْ
 ظَالِمُونَ ﴿٢٠٧﴾

91. "Na wanapoambiwa: Yaaminini Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu. Wao husema: Tunaamini tuliyoteremshiwa sisi. Na huyakataa yasiyokuwa hayo. Na hali ya kuwa hii ndiyo haki inayothibitisha yale waliyonayo wao. Sema: Mbona mliwaua Manabii wa Mwenyezi Mungu hapo zamani ikiwa kweli mlikuwa Waumini."

92. "Na alikufikieni Musa na hoja zilizo waziwazi, kisha mkamchukua ndama (kumuabudu) baada yake, na mkawa wenye kudhulumu."

¹ Ahmad 2:179.

Mayahudi Kudai kwao Kuamini Huku Wakikanusha Haki.

Allah تعالیٰ Amesema,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ

“Na wanapoambiwa.”

Maana yake: “Mayahudi na Watu wa Kitabu”.

ءَامِنُوا بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ

“Yaaminini Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu.”

Kwa Muhammad ﷺ, kuyasadiki na kumfuata.

قَالُوا نُوْمِنُ بِمَا أَنْزَلَ عَلَيْنَا

“Nao husema: Tunaamini tuliyoteremshiwa sisi.”

Maana yake: Inatosha kwetu kuamini yaliyoteremshwa kwetu ndani ya Taurati na Injili, na hii ndio njia tuliyoichagua.

وَيَكْفُرُونَ بِمَا وَرَاءَهُ

“Na huyakataa yasiyokuwa hayo.”

Maana yake: Baada ya Taurati na Injili.

وَهُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَهُمْ

“Na hali ya kuwa hii ndiyo haki inayothibitisha yale waliyonayo wao.”

Maana yake: Wakati wanajua aliyoteremshiwa Muhammad ﷺ.

الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَهُمْ

“Haki inayothibitisha yale waliyonayo wao.”

Ina maana kuwa, kwa vile yale aliyoteremshiwa Muhammad ﷺ yanafanana na yale waliyoteremshiwa Watu wa Kitabu, hivyo Ukweli huu una ushahidi dhidi yao.

Vivyo hivyo Allah تعالیٰ Amesema,

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ آبْنَاءَهُمْ^ط

“Wale Tuliowapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao.” (2:146)

Baada ya hapa Amesema,

فَلِمَ تَقْتُلُونَ أَنْبِيَاءَ اللَّهِ مِنْ قَبْلُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤٦﴾

“Mbona mliwaua Manabii wa Mwenyezi Mungu hapo zamani ikiwa kweli mlikuwa Waumini.”

Ina maana: “Endapo mnadai kuwa mnaamini mliyoteremshiwa ni kweli, basi kwa nini mliwaua Mitume waliokuja wakithibitisha Sharia za Taurati, japokuwa mlijua ni Mitume wa kweli? Mliwaua kwa kuchupa mipaka, ukorofi na dhuluma kwa Manabii wa Allah تعالى; kwa hivyo mnafuata tamaa zenu, maoni na utashi.” Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema,

أَفَكُلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنْفُسُكُمْ أَسْتَكْبِرْتُمْ فَفَرِيقًا كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ ﴿١٤٧﴾

“Basi kila walipokufikieni Mitume kwa yale ambayo hayependwi na nafsi zenu, mlijivuna: Wengine makawakanusha, na wengine mkawaua.”. (2:87)

Aidha, As-Suddi alisema, “Katika Aya hii Allah تعالى Anawaumbua na Kuwafedhehesha Watu wa Kitabu”.

فَلِمَ تَقْتُلُونَ أَنْبِيَاءَ اللَّهِ مِنْ قَبْلُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤٨﴾

“Sema: Mbona mliwaua Manabii wa Mwenyezi Mungu hapo zamani ikiwa kweli mlikuwa Waumini?”¹

* وَلَقَدْ جَاءَكُمْ مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ

“Na alikufikieni Musa na hoja zilizo waziwazi.”

¹ Ibn Abi Hatim 1:281.

Ina maana: Kwa dalili za wazi na ushahidi ulio wazi ya kwamba, alikuwa Nabii wa Allah تعالى na kuwa hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Alama za wazi au miujiza – iliyotajwa hapa ni mafuriko, nzige, chawa, vyura, damu, bakora na mkono. Miongoni mwa miujiza ya Musa عليه السلام ni pamoja na kupasuka kwa bahari, Mayahudi kufunikwa na mawingu, *manna* na *salwa*, jiwe linalobubujika maji n.k.

ثُمَّ آخَذْتُمْ الْعِجْلَ

“Kisha mkamchukua ndama (kumuabudu).”

Maana yake: Kama mola badala ya Allah تعالى, wakati wa Musa عليه السلام. Kauli ya Allah تعالى,

مِنْ بَعْدِهِ

“Baada yake.”

Maana yake: Baada ya Musa عليه السلام kwenda Mlima Tur kuzungumza na Allah تعالى. Vivyo hiyo Allah تعالى Amesema,

وَأَخَذَ قَوْمُ مُوسَىٰ مِنْ بَعْدِهِ مِنْ خُلَيْبِهِمْ عِجْلًا جَسَدًا لَهُ خُورٌ

“Na baada yake (baada ya kuondoka kwake kuenda kupokea Taurati) watu wa Musa walifanya kwa mapambo yao, ndama kiwiliwili tu kilichokuwa na sauti.” (7:148)

وَأَنْتُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٤٨﴾

“Na mkawa wenye kudhulumu.”

Maana yake: Hamkuwa katika haki mlipo muabudia ndama, japokuwa mlijua kuwa hapana mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema,

وَلَكَا سَقِطَ فِي أَيْدِيهِمْ وَرَأَوْا أَنَّهُمْ قَدْ ضَلُّوا قَالُوا لَئِن لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا

لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾

“Na walipojuta na wakaona ya kwamba wamekwishapotea, walisema: “Kama hataturehemu Mola wetu na Kutusamehe, bila shaka tutakuwa miongoni mwa waliopata hasara.” (7:149)

وَإِذْ أَخَذْنَا مِيثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّورَ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ بِقُوَّةٍ وَأَسْمِعُوا^ط قَالُوا
 سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَأَشْرَبُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ^ع قُلْ بِئْسَمَا يَأْمُرُكُم بِهَا
 إِيمَانُكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٩٣﴾

93. “Na Tulipochukua ahadi yenu na Tukauinua mlima juu yenu (Tukakuambieni): Kamateni kwa nguvu haya Tuli yokupeni na sikieni. Wakasema: Tumesikia na tumekataa! Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (imani ya) ndama kwa kufuru yao. Sema: Ni uovu mno iliyokuamrisha imani yenu ikiwa ni wenye kuamini.”

Mayahudi Waliasi Baada ya Allah تعالی Kuchukua Ahadi Yao, na Kuona Kwao Mlima (Tur) Juu ya Vichwa Vyao.

Allah تعالی Aliwakumbusha Mayahudi makosa yao, kuvunja ahadi Yake, kuchupa mipaka na ufedhuli, Alipouinua Mlima Tur juu yao ili wapate kuamini na wakubali masharti ya ahadi. Bali waliivunja muda si mrefu,

قَالُوا سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا

“Wakasema: Tumesikia na tumekataa!”

Tumetaja *Tafsir* ya mada hii hapo kabla. Abdur-Razaq alisema kutoka kwa Ma’amur kutoka kwa Qatadah kuwa,

وَأَشْرَبُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ^ع

“...Na wakanyweshwa nyoyoni mwao (imani ya) ndama kwa kufuru yao.”

Maana yake: Walikunywa mapenzi yake mpaka yakafanya kazi ndani ya mioyo yao.¹

Hii pia ni rai ya Abu Al-aliyah na Ar-Rabi bin Anas.²

¹ Abdur-Razaq 1:52.

² Ibn Abi Hatim 1:283.

Kauli ya Allah تعالى،

قُلْ بِئْسَمَا يَأْمُرُكُمْ بِهِ إِيمَانُكُمْ إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٨٩﴾

“Sema: Ni uovu mno iliyokuamrisha imani yenu ikiwa ni wenye kuamini.”

Ina maana: “Mbaya zaidi ni mwenendo wenu mliouonesha zamani na hata sasa, kukufuru Aya za Allah تعالى na kuwakataa Mitume. Pia mlimkanusha Muhammad ﷺ ambayo ni amali mbovu kabisa na kosa baya kabisa mlilolifanya.”

Mlimkufuru Nabii wa mwisho na Bwana wa Mitume wote, ambaye alitumwa kwa binadamu wote.

Vipi mnaweza kudai kuwa mnaamini, wakati mnafanya dhambi ya kuvunja Ahadi ya Allah تعالى, mnakufuru Aya za Allah تعالى na mnaabudu ndama badala ya Allah?

* * *

قُلْ إِنْ كَانَتْ لَكُمْ أَلْدَارُ الْآخِرَةُ عِنْدَ اللَّهِ خَالِصَةً مِّنْ دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٤﴾
 وَلَنْ يَتَمَنَّوَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ
 ﴿٩٥﴾ وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاتِهِمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا يَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحِّزِهِمْ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يُعَمَّرَ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾
 قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيْلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٩٧﴾ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيْلَ وَمِيكَائِيلَ فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِلْكَافِرِينَ ﴿٩٨﴾

قُلْ إِنْ كَانَتْ لَكُمْ أَلْدَارُ الْآخِرَةُ عِنْدَ اللَّهِ خَالِصَةً مِّنْ دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٤﴾ وَلَنْ يَتَمَنَّوَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٩٥﴾ وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاتِهِمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا يَوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحِّزِهِمْ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يُعَمَّرَ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾

94. "Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama nyinyi mnasema kweli."

95. "Wala hawayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyotangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema wanaodhulumu."

96. "Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi, na kuliko Washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angelipewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondolei adhabu; na Mwenyezi Mungu Anayaona wanayoyatenda."

Kuwaita Mayahudi katika Kuapizana

Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Allah تعالى Alimuambia Mtume Wake ﷺ,

قُلْ إِنْ كَانَتْ لَكُمْ أَلْدَارُ الْأَخِرَةُ عِنْدَ اللَّهِ خَالِصَةً مِّنْ دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِنْ

كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٤﴾

“Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama nyinyi mnasema kweli.”

Maana yake: “Muombe Allah تعالى Awaue wale wanaosema uongo miongoni mwa kambi mbili (Waislamu na Mayahudi).” Mayahudi walikataa ahadi ya Mtume ﷺ.¹

وَلَنْ يَتَمَنَّوْهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٩٥﴾

“Wala hawayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyo tangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema wanaodhulumu.”

Maana yake: “Kwa kuwa wanajua, walikutambua na bado wakakukanusha.” Iwapo wanalikhitari kifo siku ile, hakuna Yahudi angalibaki hai juu ya uso wa dunia. Hata hivyo Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ

“Basi tamanini mauti.”

Maana yake: Muombeni (Allah تعالى) Akuueni.² Pia Abdur-Razzaq amesimulia kuwa Ikrimah alisema kuwa, Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maoni,

فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ

“Basi tamanini mauti.”

¹ Ibn abi Hatim 1:284.

² At-Tabari 2:366.

Lau Mayahudi wanguemomba Allah تعالى Awaue, wangeangamia.¹ Pia, Ibn Abu Hatim alimrekodi Said bin Jubayr akisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kama Mayahudi wangeomba kifo, mmoja wao angesongwa na mate yake mwenyewe.”² Kauli hizi zina *Isnadi* sahihi za wapokezi mpaka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Zaidi ya hayo Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema katika *Tafsir* yake, “Tulielekezwa kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ أَنَّ الْيَهُودَ نَمَتُوا الْمَوْتَ لَمَاتُوا وَلَرَأَوْا مَقَاعِدَهُمْ مِنَ النَّارِ، وَلَوْ خَرَجَ الَّذِينَ
يَبَاهِلُونَ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ لَرَجَعُوا لَا يَجِدُونَ أَهْلًا وَلَا مَالًا»

“Lau Mayahudi wangetamani kufa, wangalikufa na wakapata makazi motoni. Na wale waliyoionba hiyo laana dhidi ya Nabii wa Allah, wasingelizikuta familia zao, au mali baada ya kurudi majumbani mwao.”³

Iliyo sawa na Aya hii ni Kauli ya Allah تعالى katika *Surat Al-Jumu'ah*,

قُلْ يَتَّيِبُهَا الَّذِينَ هَادُوا إِنْ زَعَمْتُمْ أَنَّكُمْ أَوْلِيَاءُ لِلَّهِ مِنْ دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِنْ
كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٦٦﴾ وَلَا يَتَمَنَّوْنَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيَهُمْ ؕ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٦٧﴾
قُلْ إِنَّ الْمَوْتَ الَّذِي تَفِرُّونَ مِنْهُ فَإِنَّهُ مُلْقِيكُمْ ۖ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلْمِ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ فَيُنذِرُكُم بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

“Sema: Enyi Mayahudi! Ikiwa nyinyi mnadai kuwa ni vipenzi vya Mwenyezi Mungu pasipo kuwa watu wengine, basi yatamanini mauti, ikiwa mnasema kweli. Wala hawayatamani kabisa, kwa sababu ya iliyokwisha yatanguliza mikono yao. Na Mwenyezi Mungu Anawajua waliodhulumu. Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye Kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Hapo atakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.” (62:6-8).

¹ Ibn Abi Hatim 1:285.

² Ibn Abi Hatim 1:284.

³ At-Tabari 2:362.

Hivyo walidai kuwa wao ni wana wa Allah تعالى na wanaopendwa na walisema, “Wale tu ambao ni Wakristo au Mayahudi ndio watakaoingia Peponi.” Kwa hiyo, walilinganiwa kumuomba Allah تعالى Aliangamize kundi lililokuwa linasema uongo, iwe ni wao au Waislamu. Mayahudi hawakufanya kwani kila mtu alikuwa anajua makosa yake, kwani wangekuwa na uhakika wa madai yao, basi wangekubali mwito huo. Uongo wao ulifichuliwa baada ya wao kukataa kuomba laana. Vile vile Mtume ﷺ aliutaka ujumbe wa Wakristo wa Najran kujiapiza baada ya mjadala ambapo walionesha ukorofi na Inadi. Allah تعالى Akasema,

فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ آبَاءَنَا وَأَبْنَاكُمْ وَنِسَاءَنَا

وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَلْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾

“Watakaokuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.” (3:61)

Wakristo waliposikia changamoto hii, baadhi yao wakaambizana, “Wallahi! Endapo mtafanya hilo na Mtume huyu, hapana kati yenu jicho lake litapepesa.” Ndipo walipoamua wawe salama na wakalipa Jizyah kwa aibu. Mtume ﷺ aliridhia Jizyah yao na alimpeleka Ubaydah bin Al-Jarah رضي الله عنه pamoja nao kama mdhamini. Mithili ya maana haya au yanayokaribiana nayo ni Amri ya Allah تعالى kwa Mtume ﷺ awatangazie washirikina.

قُلْ مَنْ كَانَ فِي الضَّلَالَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمَنُ مَدًّا

“Sema (Ewe Muhammad) walio katika upotofu basi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema Atawaongezea muda.” (19:75)

Maana yake: “Yeyote miongoni mwenu aliyekengeuka, tunamuomba Allah تعالى Aongeze na Aurefushe upotofu wake.” Tutaizungumzia mada hii baadaye, Allah تعالى Akipenda. Aidha kuna mtazamo wa walioitafsiri Aya hii kwa maana ya kutamani Mauti na wala sio kuapizana. Lakini mtazamo wa kwanza ndio sahihi zaidi. *Mubahalah* (dua ya kumuomba Allah تعالى Awaangamize waongo)

Imeitwa hapa “utashi” kwa sababu kila mtenda haki anataraji Allah تعالی Atamuangamiza mkinzani wake dhalimu ambaye anajadiliana naye, hususan, wakati muadilifu ana ushahidi ulio wazi kuhusu ukweli anaoulingania. Pia, *Mubahalaha* unahusu kumuomba Allah تعالی Awaue madhalimu, kwa sababu kwa makafiri, maisha kwao ni bora sana, hasa wanapojua mwisho wao mbaya baada ya kufa.

Makafiri Wanatamani kama Wangeishi Muda Mrefu.

Hii ndio maana Allah تعالی Akasema,

وَلَنْ يَتَمَنَّوْهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٩٤﴾ وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ
النَّاسِ عَلَىٰ حَيٰوةٍ

“Wala hawayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyotangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema wanaodhulumu. Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi.”

Maana yake: Tamaa ya kuishi muda mrefu, kwa sababu wanajua mwisho wao mbaya, na malipo wayatarajiayo kutoka kwa Allah تعالی yamejaa hasara tupu. Maisha ya dunia ni gereza kwa Waumini na Pepo kwa makafiri. Kwa hiyo, Watu wa Kitabu wanatamani Kiyama kingecheleweshwa sana kufika. Hata hivyo, watakutana na kila wanachojaribu kukiepa, japokuwa wana hamu ya kucheleweshwa Kiyama kuliko hata washirikina ambao hawana kitabu Kitakatifu. Mujahid amesema kuhusu Aya, **“Mmoja wao anatamani lau angelipewa umri wa miaka elfu moja.”** Kwamba mmoja wao anapenda afanye madhambi maisha yote. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالی alisimulia kuwa Ibn abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo Aya hii,

وَمَا هُوَ بِمُزَحَّزَجِهِ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يُعْمَرَ

“Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondolei adhabu.”

Maisha marefu hayatawaokoa kutokana na adhabu. Kwa hakika Makafiri hawaamini kufufuka baada ya kifo, na wangependa waishi maisha marefu. Mayahudi wanajua udhalili watakaoupata siku ya Kiyama kwa kuupuuza ukweli

kwa makusudi.¹ Pia Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema, Mayahudi wanapupia maisha haya. Wanatamani kama wangaliishi miaka elfu. Pamoja na hayo, kuishi miaka elfu hakutawaokoa na adhabu – kama ilivyo kwa Iblis – shetani – maisha marefu hayakumsaidia kwa kuwa ni kafiri.”²

وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anayaona wanayoyatenda.”

Maana yake: “Allah تعالى Anayajua yafanywayo na waja Wake, ima ni mema au mabaya, na Atamlipa kila mmoja kulingana na amali yake.”

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ
وَهُدًى وَمُتْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٩٧﴾ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ
وَمِيكَائِيلَ فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِلْكَافِرِينَ ﴿٩٨﴾

97. “Sema: Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeteremsha Qur’an moyoni mwako kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, inayothibitisha yaliyokuwa kabla yake, na ni uongofu na bishara njema kwa Waumini.”

98. “Aliyekuwa adui wa Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na Mitume Wake na Jibril na Mikail, basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.”

Uadui wa Mayahudi kwa Jibril عليه السلام.

Imamu Abu Ja’far bin Jariri At-Tabari رحمه الله تعالى alisema, “Wanazuoni wa *Tafsir* wanakubaliana kuwa Aya (2:97-98) iliteremshwa ili kuwajibu Mayahudi ambao wanadai kuwa Jibril عليه السلام ni adui wa Mayahudi na kuwa Mikail عليه السلام ni Sahibu yao (At-Tabari 2:377).” Al-Bukhari alisema, Kuhusu Kauli Yake Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:288.

² At-Tabari 2:377.

مَنْ كَانَتْ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ

“Anayemfanyia Jibril uadui.”

Ikrimah alisema, “*Jibr, Mika na Israfil* – yote maana yake, mwenye kuabudu, wakati *il* maana yake Allah تعالى”. Kisha Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Abdullah bin Salam aliposikia kuwasili kwa Mtume ﷺ akamuambia, “Nitakuuliza mambo matatu ambayo kwayo hakuna anayeyafahamu isipokuwa Mtume. Ni ipi itakuwa alama ya kwanza ya Kiyama? Ni aina gani ya chakula cha mwanzo kuliwa na watu wa Peponi? Kwa nini mtoto anafanana na baba yake au kwa nini anafanana na mama yake?” Mtume ﷺ alimjibu, “*Jibril amenipa majibu sasa hivi*”. Abdullah akasema, “Jibril?” Mtume ﷺ akasema: “Ndiyo”. Abdullah akasema, “Huyo (Jibril عليه السلام) miongoni mwa Malaika wote, ni adui wa Mayahudi.” Mtume ﷺ alisoma Aya,

مَنْ كَانَتْ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ

“Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeiteremsha Qur’an moyoni mwako.”

Kisha Mtume ﷺ alisema,

“Dalili ya mwanzo ya Kiyama itakuwa moto ambao utawakusanya pamoja watu kutoka Mashariki kwenda Magharibi, chakula cha mwanzo kwa watu wa Peponi kitakuwa maini ya samaki. Ama kuhusu mtoto kufanana na Wazazi wake. Endapo mume atamuingilia mkewe na akawa wa mwanzo kushusha manii, mtoto atafanana na baba. Na ikiwa mke atashusha manii mwanzo, mtoto atafanana na familia ya upande wake.”

Baada ya hayo, Abdullah bin Salam akasema, “Nakiri kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى na wewe ni Nabii wa Allah.” Abdullah bin Salam akaongeza kusema, “Ewe Mtume ﷺ! Mayahudi ni waongo, na kama watajua habari zangu kabla ya kuwauliza wao, watakueleza uongo kuhusu mimi.” Mayahudi walikuja kwa Mtume ﷺ na Abdullah akaingia ndani ya nyumba. Nabii wa Allah akawauliza (Mayahudi), “Abdullah bin Salam ni mtu wa namna gani kwenu?” Wakamjibu, “Ni mbora miongoni mwetu, mtoto wa mbora miongoni mwetu na bwana wetu.” Nabii wa Allah ﷺ akasema,

“Mnaonaje kama atasilimu?” Mayahudi wakasema, “Tunamuomba Allah تعالی Amuokoe katika hilo.” Kisha Abdullah bin Salam akatoka nje na akasimama mbele yao akisema, “Nathibitisha ya kuwa hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالی na kuwa Muhammad ﷺ ni Nabii wa Allah.” Wakati ule ule wakasema, “Huyu ni muovu kuliko sote, na mtoto wa muovu miongoni mwetu.” Na wakaendelea kumsema vibaya. Ibn Salam akasema, “Hili ndilo nililochelea, Ewe Nabii wa Allah!” Al-Bukhari na Muslim walipokea *Hadith* hii kwa *Isnadi* hii ya upokezi.¹ Al-Bukhari na Muslim walipokea *Hadith* hii kutoka kwa Anas رضي الله عنه wakitumia *Isnadi* nyengine ya upokezi.²

Baadhi ya watu wanasema “*il*” Maana yake: Ni mja wakati ikiongezwa kwenye neno lolote linakuwa Jina la Allah تعالی, kwa sababu “*il*” haibadiliki. Hii ni sawa katika majina; Abdullah, Abdur-Rahman, Abdul-Malik, Abdul-Qudus, Abdus-Salam, Abdul-Kafi, Abdul-Jalil na kadhalika. Hivyo ‘*Abd*’ haibadiliki katika maneno ambatano, wakati sehemu iliyobaki inabadilika kati ya jina na jina. Hii ni sawa na Jibril, Mikail, Izrail, Israfil na kadhalika. Allah تعالی ni Mjuzi wa Yote.

Kutofautisha Baina ya Malaika, ni Sawa na Kutofautisha Baina ya Mitume.

Ama tafsiri ya Kauli Yake Allah تعالی

مَنْ كَانَتْ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ

“Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeiteremsha Qur’an moyoni mwako kwa Idhini ya Allah.”

Ina maana: Yeyote anayekuwa adui wa Jibril عليه السلام, anatakiwa afahamu kuwa yeye ni *Ruh Al-Qudus* Roho Mtakatifu ambaye aliiteremsha *Dhikr* Takatifu (Qur’an) kwenye moyo wako kutoka kwa Allah تعالی kwa Idhini Yake. Hivyo ni Mjumbe kutoka kwa Allah تعالی. Yeyote atakayemfanya Mjumbe adui, atakuwa adui wa Wajumbe wote. Zaidi ya hayo, yeyote anayemuamini Mjumbe mmoja anatakiwa awaamini Wajumbe wote. Yeyote anayemkana Mjumbe mmoja, amewakana Wajumbe wote. Vile vile Allah تعالی Amesema,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:15 na 7:319.

² Bukhari 3329, 3911, 3938 na Muslim 315.

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ
نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ

“Hakika wale wanaomkataa Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, na wanataka kutenganisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa.” (4:150)

Allah تعالی Amehukumu kuwa ni Makafiri, kwa sababu wanaamini baadhi ya Mitume na wanawakanusha wengine. Hii ni sawa na wale wanaomchukulia Jibril عليه السلام kuwa adui yao. Kwa sababu Jibril عليه السلام hakufanya mambo kwa utashi wake bali aliamrisha na Mola Wake. Kama Allah تعالی Alivyosema,

وَمَا نَنْزِلُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ ط

“(Nao watasema): Wala hatuteremki ila kwa Amri ya Mola wako.” (19:64)

Na Allah تعالی Amesema

وَإِنَّهُ لَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٩٢﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾

“Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameuteremsha Roho mwaminifu. Ju ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji.” (26:192-194)

Al-Bukhari aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ عَادَى لِي وَلِيًّا فَقَدْ بَارَزَنِي بِالْحَرْبِ»

“Yeyote atakayemfanya adui walii wangu (rafiki yangu), atakuwa amenitambia kwa vita.”¹

Kwa hiyo, Allah تعالی Aliwaghadhibikia wale waliomfanya Jibril عليه السلام adui yao. Allah تعالی Amesema,

¹ Fat’hul Al-Bari 11:348.

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَيَّ قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeiteremsha Qur’an moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, inayothibitisha yaliyo kuwa kabla yake.” Maana yake Vitabu Vilivyopita.

وَهُدًى وَنُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾

“Na ni uongofu na bishara njema kwa Waumini.”

Maana yake: Uongozi kwa nyoyo zao na mletaji wa habari njema za Peponi ambazo ni mahsusi kwa Waumini. Vile vile Allah تعالى Amesema,

قُلْ هُوَ الَّذِي هَدَىٰ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ط

“Sema: Qur’an hii ni uongofu na pozo.” (41:44) Aidha Amesema,

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۝

“Na Tumeteremsha katika Qur’an yaliyo ponyo na rehema kwa Waumini.” (17:82) Kisha Allah تعالى Akasema,

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِّلْكَافِرِينَ ﴿٧٨﴾

“Aliyekuwa adui wa Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na Mitume Wake na Jibril na Mikail, basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.”

Allah تعالى Alisema kuwa yeyote anayemchukulia Yeye, Malaika Wake na Manabii kama maadui. Hivyo, Wajumbe wa Allah تعالى ni pamoja na Malaika na wanadamu, kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema,

اللَّهُ يَصْطَفِي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ ۚ

“Mwenyezi Mungu Huteua Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu.” (22:75)

Allah تعالى Amesema,

وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ

“Jibril na Mikail.” Allah تعالى Aliwataja Jibril عليه السلام na Mikail عليه السلام peke yao katika Aya hii, kwa sababu Aya hii ilikusudiwa kumuunga mkono Jibril

Mjumbe kati ya Allah تعالى na Mitume Wake. Aidha Allah تعالى Alimtaja Mikail عليه السلام hapa, kwa sababu Mayahudi walidai kuwa Jibril عليه السلام alikuwa ni adui yao na Mikail عليه السلام alikuwa rafiki yao. Allah تعالى Aliwafahamisha kuwa yeyote ambaye ni adui wa mmoja wao, basi ni adui pia wa mwingine, pamoja na Allah تعالى. Inafaa kueleza hapa kuwa kuna wakati Mikail عليه السلام naye aliwashukia Mitume. Lakini, kwa sababu zaidi hii ilikuwa kazi ya Jibril عليه السلام, Israfil عليه السلام yeye amepewa dhamana ya kupuliza parapanda kama mwanzo wa Ufufuo, siku ya Hukumu. Kutokana na hilo, imeandikwa ndani ya Sahih kuwa kila Mtume ﷺ alipoamka usiku aliomba dua hii,

«اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرَائِيلَ وَمِيكَائِيلَ وَإِسْرَافِيلَ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ، أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ، اهْدِنِي لِمَا اخْتَلَفَ فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ»

“Ewe Allah, Mola wa Jibril, Mikail na Israfil, Muumba wa mbingu na ardhi na Muelewa wa dhahiri na ghaibu! Unawahukumu waja Wako katika yale wanayotofautiana, hivyo niongoze katika ukweli wanaotofautiana, kwa Ridhaa Yako. Kwa hakika, Unamuongoza Umtakaye katika njia iliyonyooka.”¹

Kauli ya Allah تعالى,

فَإِرْبًا اللَّهُ عَدُوًّا لِلْكَافِرِينَ ﴿١٠٤﴾

“Basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa Makafiri.”

Makafiri walifahamishwa kuwa yeyote atakayemfanya adui rafiki wa Allah تعالى, hivyo amemfanya Allah تعالى kuwa adui yake, na yeyote anayemfanya Allah تعالى adui yake, hivyo atakuwa adui wa Allah تعالى. Kwa hakika, yeyote ambaye ni adui wa Allah تعالى, basi atakuwa amekula hasara hapa duniani na kesho Akhera, kama yasemavyo maelezo ya Hadithi iliyotangulia,

«مَنْ عَادَى لِي وَلِيًا فَقَدْ آذَنَهُ بِالمَحَارَبَةِ»

“Mwenye kumfanya uadui walii wangu, namtangazia vita.”²



¹ Muslim 1:534.

² Fat’hul Al-Bari 11:348.

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۖ وَمَا يَكْفُرُ بِهَا إِلَّا
 الْفَاسِقُونَ ﴿٩٩﴾ أَوْكُلْمَا عَاهَدُوا عَهْدًا نَّبَذَهُ فَرِيقٌ
 مِنْهُمْ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٠﴾ وَلَمَّا جَاءَهُمْ
 رَسُولٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَهُمْ نَبَذَ فَرِيقٌ مِنَ الَّذِينَ
 أُوتُوا الْكِتَابَ كِتَابَ اللَّهِ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ كَأَنَّهُمْ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾ وَأَتَّبَعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيَاطِينُ عَلَىٰ مُلْكٍ
 سَلِيمٍ ۖ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَنُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا
 يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَىٰ الْمَلَائِكَةِ بِبَابِلَ
 هَدْرٍ وَمَمْرُوكَ ۚ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَا إِنَّمَا
 نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۖ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ
 بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ ۚ وَمَا هُمْ بِضَآئِرِينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا
 بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ ۚ وَلَقَدْ عَلِمُوا
 لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ وَلَبِئْسَ مَا
 شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ ۚ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ
 ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَمَثُوبَةٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ خَيْرٌ لَوْ كَانُوا
 يَعْلَمُونَ ﴿١٠٣﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقُولُوا رَاعِنَا
 وَقُولُوا أَنْظِرْنَا وَاسْمِعُوا ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٤﴾
 مَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ
 يُنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِنْ خَيْرٍ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ وَاللَّهُ تَخْتَصُّ
 بِرَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿١٠٥﴾

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۖ وَمَا
 يَكْفُرُ بِهَا إِلَّا الْفَاسِقُونَ ﴿٩٩﴾
 أَوْكُلْمَا عَاهَدُوا عَهْدًا نَّبَذَهُ فَرِيقٌ
 مِنْهُمْ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٠﴾
 وَلَمَّا جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
 مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَهُمْ نَبَذَ فَرِيقٌ مِنَ
 الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ كِتَابَ اللَّهِ
 وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ كَأَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾

99. "Hakika Tumekute-remshia Ishara zilizo wazi na hapana wanaozikataa ila wapotovu."

100. "Je! Ati wanapofunga ahadi huwapo kikundi miongoni mwao kikaivunja? Bali wengi wao hawaamini."

101. "Na alipowajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyonayo, kundi moja miongoni mwa wale walio-pewa Kitabu lilitupa Kitabu cha Mwenyezi Mungu hicho nyuma ya migongo yao kama kwamba hawajui."

Dalili za Utume wa Muhammad ﷺ

Imam Abu Jafar bin Jariri رحمه الله تعالى alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ^ط

“Hakika Tumekuteremshia Ishara zilizo wazi.” Maana yake, “Tumekupelekea wewe, Ewe Muhammad ﷺ, dalili zilizo wazi kuthibitisha utume wako.” Aya hizi zimo ndani ya Kitabu cha Allah تعالى (Qur’an) zinaelezea siri ya maarifa waliyokuwa nayo Mayahudi, ambayo waliyaficha, na historia ya vizazi vilivyopita (vya mwanzo). Kitabu cha Allah تعالى pia kinataja maandiko ndani ya Vitabu vya Mayahudi ambayo yanajulikana kwa makasisi na wanazuoni wao, na vifungu vilivyobadilishwa na kupotoshwa vya kanuni za Taurati. Kwa kuwa Allah تعالى Alikwishayataja yote haya katika Kitabu Chake Alichomteremshia Mtume Wake Muhammad ﷺ, hivyo ukweli huu peke yake unatosha kuwa ushahidi kwa wale ambao ni waumini na wale wanaotaka kujiepusha na maangamizi yanayotokana na inda na kuchupa mipaka. Zaidi ya hayo, silka ya mwanadamu inathibitisha kuwa ukweli aliotumwa nao Muhammad ﷺ ni dalili iliyo wazi kuwa alilileta ambalo hakujifunza au kuiga kutoka kwa binadamu. Adh-Dhahhak amesimulia, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa،

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ^ط

“Hakika Tumekuteremshia Ishara zilizo wazi.” “Utawasomea na kuwafikishia Kitabu hiki mchana na usiku, japokuwa wewe ni *Ummi* ambaye hujui kusoma wala kuandika. Bado unawafahamisha yaliyokuwemo ndani ya vitabu vyao. Allah تعالى Ameeleza kuwa ukweli huu unatosha kuwa mfano, dalili iliyo wazi na Ushahidi dhidi yao, kama wanalijua.”¹

Kuvunja Ahadi ni Desturi ya Mayahudi

Wakati Mtume ﷺ Alipobaathiwa na Allah تعالى Akawakumbusha Mayahudi kuhusu ahadi waliyofunga Naye, hasa kuhusu Muhammad ﷺ, Malik bin As-sayi alisema, “Wallah! Allah Hakufanya ahadi nasi juu ya Muhammad, na wala hakuchukua ahadi ya utii kwa Muhammad ﷺ kutoka kwetu, wala hatukuchukua ahadi ya utii wake.” Kisha Allah تعالى Akateremsha،

¹ At-Tabari 2:297.

أَوْ كَلَّمَا عَنْهَدُوا عَهْدًا نَبَذَهُ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ^٤

“Je! Ati wanapofunga ahadi huwapo kikundi miongoni mwao kikaivunja?”¹

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٠﴾

“Basi wengi wao hawaamini.”

Ndio hakuna ahadi waliyoiweka, bali waliivunja na kuitelekeza. Wanaweka ahadi leo na kesho wanaivunja.²

Mayahudi Walitupa Kitabu cha Allah تعالى na Kufuata Uchawi.

As-Suddi aliitolea maelezo Aya hii،

وَلَمَّا جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ

“Na alipowajia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye kuthibitisha yale waliyonayo.”

Muhammad ﷺ alipowajia, walitaka kupingana na kukinzana naye kwa kutumia Taurati. Pamoja na hayo, Taurati na Qur’an vinathibitishana, havikinzani. Hivyo Mayahudi walikata tamaa kutumia Taurati, na wakachukua Kitabu cha Asaf³, na uchawi wa Harut na Marut, ambayo kwa hakika haikukubaliana na Qur’an.

Hivyo Allah تعالى Akasema،

كَانَتْهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥١﴾

“Kama kwamba hawajui.”⁴

Aidha Qatadah alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

¹ At-Tabari 2:400.

² Ibn Abi Hatim 1:295.

³ Lisa’n Al-Arab imetaja Asaf kuwa ni jina la Kitabu alichoteremshiwa Sulayman عليه السلام.

⁴ At-Tabari 2:404.

كَأَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾

“Kama kwamba hawajui.”

Maana yake, “Walijua ukweli lakini wakaukataa, waliuficha na wakakanusha ukweli japo walikuwa nao.”¹

وَاتَّبَعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيْطِينُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ ۗ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَٰكِنَّ الشَّيْطِينَ
كَفَرُوا يَعْلَمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَىٰ الْمَلَائِكَةِ بِبَابِلَ هُنُوتَ وَمُرُوتَ ۗ وَمَا
يُعْلَمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۗ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ
بَيْنَ بَيْنَ الْأَمْرِ وَرُوحِهِ ۗ وَمَا هُمْ بِضَآئِرِينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا
يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ ۗ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ
وَلَيْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٣﴾

102. “Na wakafuata yale waliyozua mashetani kuuzulia Ufalme wa Sulayman. Na wala Sulayman hakukufuru, bali mashetani ndio walikufuru, wakiwafundisha watu uchawi, na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili, Haaruta na Maaruta katika Baabil. Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamuambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa Kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatakayowadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hakika ni kiovu mno walichojiuzia nafsi zao laiti wangalijua.

¹ At-Tabari 2:404.

Uchawi Ulikuwepo kabla ya Sulayman عليه السلام.

As-Suddi alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَأَتَّبِعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيْطَانُ عَلَىٰ مَلِكٍ سُلَيْمَانَ

“Na wakafuata yale waliyozua mashetani kuuzulia Ufalme wa Sulayman.”

Maana yake: “Wakati wa enzi za Nabii Sulayman عليه السلام.” Mashetani walikuwa wakipanda mbinguni na kusikiliza kwa siri mazungumzo ya Malaika kuhusu yale yatakayotokea ardhini kuhusiana na kifo, matukio mengine au mambo ya ghaibu. Hivyo walizipeleka habari walizozipata kwa Makuhani na wapiga ramli (watabiri), na Makuhani upande wao walizifikisha kwa watu. Watu waliamini habari hizo Makuhani walipowaamini mashetani, mashetani walianza kuwadanganya, kwa kuongeza maneno katika habari za kweli walizozisikia, mpaka wakafikia kuongeza maneno sabini kwa kila neno la kweli. Watu waliyaandika maneno hayo katika Vitabu. Baadaye, Wana wa Israeli walisema kuwa mashetani wanajua mambo ya ghaibu. Sulayman عليه السلام alipotumwa na Allah تعالى kuwa Mtume ﷺ, alivikusanya Vitabu hivyo na akavitia ndani ya sanduku na akavizika chini ya kiti cha enzi, shetani yeyote aliyethubutu kulikaribia sanduku hilo alichomwa moto. Sulayman عليه السلام alisema, “Sitaki kusikia mtu yeyote akisema kuwa mashetani wanajua ghaibu, vinginevyo nitamkata kichwa chake.” Sulayman عليه السلام alipofariki dunia, na kikaja kizazi kipya. Alijitokeza shetani katika umbile la binadamu na akawaambia baadhi ya Wana wa Israeli, “Je, niwaelekeze hazina ambayo hamtaweza kuimaliza iwapo mtaitumia?” Wakajibu, “Ndiyo”. Akawaambia, “Chimbeni chini ya kiti cha enzi.” Na akaenda nao akawaonesha kiti cha enzi cha Sulayman عليه السلام. Wakamuambia, “Sogea karibu.” Akasema, “Hapana. Nitawangojeni hapa na kama hamtaiona hazina mniue.” Walichimba na kukuta vitabu vilivyozikwa, na shetani akawaambia, “Sulayman عليه السلام aliwadhibiti, binadamu, mashetani na ndege kwa uchawi huu.” Baada ya hapo, habari kuwa Sulayman عليه السلام alikuwa mchawi zilienea miongoni mwa watu, na Wana wa Israeli walivipokea hivyo Vitabu. Muhammad ﷺ alipokuja walibishana naye wakitegemea Vitabu hivyo.

Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema,

وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَنُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا

“Na wala Sulayman hakukufuru, bali mashetani ndio walikufuru.”

Kisa cha Harut na Marut na Ufafanuzi ya kuwa Wao ni Malaika.

Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَى الْمَلَائِكَةِ بِبَابِلَ هَرُوتَ وَمَرْوَتَ^٤ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا
 إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ^٥ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ^٤

“Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamuambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe.”

Kuna maoni tofauti kuhusu kisa hiki. Kuna mtazamo unaosema kuwa Ayah hii inakanusha kushushwa kitu chochote kwa Malaika hao wawili, hoja yao ipo katika herufi “maa” ambayo katika sarufi ya lugha ya kiarabu ina maana ya ukanushaji. Kama Qurtubi رحمه الله تعالى alivyosema na kisha akarejea kwenye Aya,

وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَنُ

“Na wala Sulayman hakukufuru.”

Mtiririko wa kukanusha umeanzia mwanzoni mwa Aya na unahusu hali zote. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أَنْزَلَ عَلَى الْمَلَائِكَةِ

“Bali mashetani ndio walikufuru, wakiwafundisha watu uchawi, na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili.”

Mayahudi wanadai Malaika wawili Jibril عليه السلام na Mikail عليه السلام waliwatere-mshia uchawi, lakini Allah تعالى Amekanusha madai hayo batili.² Na mtazamo huu, ndio sahihi katika ufafanuzi wa Aya hii. Na wala si vizuri kuifafanua Aya

¹ At-Tabari 2:405.

² Al-Qurtubi 2:50.

kwa mtazamo mwengine. Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَائِكَةِ بِبَابِلَ

“Na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili, Haaruta na Maaruta katika Baabil.”¹

“Allah تعالى، Hakuteremsha uchawi.” Aidha, Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ar-Rabi bin Anas alilizungumzia.

وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَائِكَةِ

“Na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili”.

“Allah تعالى Hakuwapeleka Malaika na uchawi.”² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alitoa maoni yafuatayo, “Haya ni maelezo sahihi kwa Aya hii.”

وَاتَّبِعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيْطَانُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ

“Na wakafuata yale waliyozua mashetani kuuzulia Ufalme wa Sulayman.”

Maana yake: Uchawi. Hata hivyo, Sulayman عليه السلام hakukufuru wala Allah تعالى Hakupeleka uchawi pamoja na Malaika wawili. Mashetani, kwa upande mwingine walikufuru na wakawafundisha uchawi watu wa Babeli wa Harut na Marut

Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliendelea, “Endapo mtu atauliza maelezo ya Aya hii kwa mtindo huu, tunasema kuwa,

وَاتَّبِعُوا مَا تَتْلُوا الشَّيْطَانُ عَلَىٰ مُلْكِ سُلَيْمَانَ

“Na wakafuata yale waliyozua mashetani kuuzulia Ufalme wa Sulayman.”

¹ At-Tabari 2:419.

² At-Tabari 2:419.

Maana yake, uchawi. Sulayman عليه السلام hakukufuru wala Allah تعالى Hakupeleka uchawi pamoja na Malaika wawili. Hata hivyo, Mashetani, walikufuru na wakawafundisha uchawi watu wa Babeli wa Harut na Marut. Hivyo basi, maana ya “Malaika” wawili katika Aya hii ni Jibril عليه السلام na Mikail عليه السلام, kwani wachawi wa Kiyahudi walidai kuwa Allah تعالى Alipeleka uchawi kupitia ulimi wa Jibril عليه السلام na Mikail عليه السلام, kwa Sulayman عليه السلام, mtoto wa Daud عليه السلام. Allah تعالى Alikanusha madai potofu na alimueleza Mtume Wake Muhammad ﷺ kuwa Jibril عليه السلام na Mikail عليه السلام hawakupewa uchawi. Pia Allah تعالى Alimtakasa Sulayman عليه السلام na kufanya uchawi, ambao ni amali ya mashetani waliwafundisha watu wa Babeli kwa mikono ya watu wawili, Harut na Marut. Hivyo, Harut na Marut walikuwa watu wawili wa kawaida¹ (sio malaika wala Jibril au Mikail). Haya yalikuwa maneno ya At-Tabari رحمه الله تعالى, na maelezo haya yalipingwa kwa kuwa ndani yake kuna kujikalifisha kwa wazi. Wengi miongoni mwa *Salaf* walisema kuwa Harut na Marut walikuwa Malaika ambao walishuka duniani kutoka mbinguni na wakafanya waliyoyafanya kama aya ilivyosema. Maoni haya yanalingana na ukweli kuwa Malaika wamehifadhika na makosa. Tunasema ya kuwa Allah تعالى Alikuwa na ufahamu usio na kikomo kuhusu yatakayofanywa na Malaika hao, kama alivyokuwa na ufahamu kuwa Iblis angefanya aliyoyafanya, wakati Allah تعالى Alimtaja kuwa miongoni mwa Malaika. Pale Aliposema تعالى,

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ فَسَجَدُوْٓا اِلَّاۤ اِبْلِيسَ اَبٰٓى ﴿۱۱۶﴾

“Na Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Wakasujudu, isipo kuwa Iblis, alikataa.” (20:116)

Na kadhalika. Pamoja na hayo, walichofanya Harut na Marut ni uovu mdogo ukilinganishwa na aliyoyafanya Iblis, Allah تعالى Amlaani. Al-Qurtubi رحمه الله تعالى aliandika rai hii kutoka kwa Ali ibn Ma’ud, Ibn Abbas, Ibn ‘Umar, Ka’b Al-Ahbar, As-Suddi na Al-Kalbi رضي الله عنهم.² Na ama kisa cha “*Azzuhraj*” ni cha kubuni mia kwa mia.

¹ Ibid.

² Al-Qurtubi 2:51.

Kujifunza Uchawi ni Kufuru.

Allah تعالی Amesema,

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ^ط

“Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamuambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru.”

Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالی alisema kutoka kwa Ar-Rabi bin Anas kutoka kwa Qays bin Abbad kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtu alipowajia malaika kujifunza uchawi, walimkataza sana na kumuambia, “Sisi ni mtihani, tahadharini na kukufuru.” Walikuwa wanajua lipi ni jema na lipi ni ovu na mambo yanayopelekea kwenye imani au ukafiri hivyo walijua kuwa uchawi ni aina ya ukafiri. Na anaposisitiza kufundishwa, walimuamuru kwenda sehemu fulani, na alipokwenda, shetani alimpokea na kumfundisha uchawi. Baada ya mtu huyu kujifunza uchawi, nuru (imani) itamkimbia, na ataiona ina meremeta (na inapaa) kwenda angani. Kisha Atatangaza, “Oh! Huzuni! Ole wangu! Nitafanyaje?”¹ Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema kuwa Ayah hii maana yake, “Ndio malaika wawili waliteremshiwa uchawi, ili wapate kuwafundisha watu mtihani ambao Allah تعالی Ametaka Kuwajaribu watu. Hivyo, Allah تعالی Akachukua ahadi kwao kwamba wasimfunze yeyote, hadi wamuambie kwamba sisi tumeteremshwa kuwa mtihani. Hivyo basi, msikufuru.”² Ilirekodiwa na Ibn Abu Hatim, Pia Qatadah alisema, “Allah تعالی Alichukua ahadi yao ya kutomfundisha uchawi mtu yeyote mpaka wamuambie, “Sisi ni mtihani, kwa hiyo usikufuru.”³ Pia As-Suddi alisema, “Akitokezea mtu kwa Malaika wale wawili basi atashauriwa na kuambiwa, “Usikufuru, sisi ni mtihani.” Yule aliyepuuza ushauri wao, walimuambia, “Nenda katika rundo la jivu na ukojolee! Atakapokojolea majivu, nuru ya imani, itamtoka na itametameta mpaka iingie mbinguni kisha kitu cheusi mithili ya moshi kitashuka na kuingia masikioni na mwili wote, na hii ni ghadhabu ya Allah تعالی. Na mtu atakapowaeleza Malaika jambo hilo, walimfundisha uchawi.” Hivyo Allah تعالی Akasema,

¹ Ibn Abi Hatim 1:312.

² Ibn Abi Hatim 1:310.

³ At-Tabari 2:443.

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ^ط

“Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamuambie: Hakika sisi ni mthani; basi usikufuru.”¹

Sunayd alisema kutoka kwa Hajaji kutoka kwa Ibn (Jurayj) alitolea maelezo Aya hii, “Hakuna anayethubutu kufanya uchawi isipokuwa kafiri.” Ama kuhusu *Fitnah*, inahusu mitihani na majaribio.² Wanazuoni waliosema kuwa kujifunza uchawi ni ukafiri walitegemea Aya hii kuwa ni ushahidi. Pia alitaja ushahidi mwengine wa *Hadith* ambayo Abubakar Al-Bazzar aliipokea kutoka kwa Abdullah,

«مَنْ أَتَى كَاهِنًا أَوْ سَاحِرًا فَصَدَّقَهُ بِمَا يَقُولُ فَقَدْ كَفَرَ بِمَا أَنْزَلَ عَلَى مُحَمَّدٍ ﷺ»

“Yeyote anayemuendea mpiga ramli au mchawi na akaamini alichosema, ‘Basi amekufuru aliyoteremshiwa Muhammad ﷺ.”³

Hadith hii ina *Isnadi* ya upokezi sahihi na kuna *Hadithi* nyingine zinazokubaliana na hii.

Kusababisha Kuvunjika kwa Ndoa ni Moja ya Madhara ya Uchawi.

Allah تعالى Amesema,

فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ^ع

“Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe”.

Ina maana, “Watu walijifunza uchawi kutoka kwa Harut na Marut na wakajiingiza katika vitendo viovu ambavyo ni pamoja na kuvunja ndoa, japo wanandoa wako katika uhusiano wa ndani kabisa. Hii ni kazi ya shetani”. Muslim aliandika kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 2:443

² At-Tabari 2:443.

³ Kashf Al-Astar 2:443.

«إِنَّ الشَّيْطَانَ لَيَضَعُ عَرْسَهُ عَلَى الْمَاءِ ثُمَّ يَبْعَثُ سَرَايَاهُ فِي النَّاسِ فَأَقْرَبُهُمْ عِنْدَهُ مَنْزِلَةً أَكْثَرُهُمْ عِنْدَهُ فِتْنَةً وَيَجِيءُ أَحَدَهُمْ فَيَقُولُ: مَا زِلْتُ بِفُلَانٍ حَتَّى تَرَكَتُهُ وَهُوَ يَقُولُ كَذًا وَكَذًا، فَيَقُولُ إِبْلِيسُ: لَا وَاللَّهِ مَا صَنَعْتَ شَيْئًا، وَيَجِيءُ أَحَدَهُمْ فَيَقُولُ: مَا تَرَكَتُهُ حَتَّى فَرَّقْتُ بَيْنَهُ وَبَيْنَ أَهْلِهِ، قَالَ: فَيَقْرَبُهُ وَيُذْنِبُهُ وَيَلْتَزِمُهُ وَيَقُولُ: نَعَمْ أَنْتَ»

“Shetani husimika kiti chake cha enzi juu ya maji na hutuma Wajumbe wake kwa watu. Mtu aliye karibu naye kihadhi ni yule anayefanya Fitna kubwa. Mmoja wao (shetani) atamjia na kumuambia, “Nilimchochea fulani, mpaka akaniambia maneno kadha wa kadha. Iblis atamuambia “Hapana, Wallahi, bado hujafanya kitu”. Shetani mwengine atamjia na kumuambia, “Nilikuwa nikimshawishi fulani mpaka akavunja ndoa na mkewe”. Shetani atamvuta kwake na kumkumbatia, huku akimuambia, “Naam, umefanya vizuri”¹.

Kuachana baina ya mume na mke kunatokea hapa kwa sababu kila mmoja hufanyiwa mauzauza na kumfikiria mwenzake ana sura mbaya au ana tabia mbaya, husuda, bughudha n.k

Hukumu ya Allah تعالی Iko Juu ya Kila Kitu.

Allah تعالی Amesema,

وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ

“Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.”

Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالی alielezea kuwa “Isipokuwa kwa Qudra ya Allah تعالی.”²

Pia Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema kuwa,

¹ Muslim 4:2167.

² Ibn Abi Hatim 1:312.

وَمَا هُمْ بِضَآئِرِينَ بِإِذْنِ اللَّهِ
إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ

“Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: “Allah تعالى Huruhusu wachawi wamdhuru yeyote Anayemtaka na kumuokoa yeyote Amtakaye kati yao. Wachawi hawawezi kumdhuru yeyote isipokuwa kwa Idhini ya Allah تعالى.”¹ Kauli ya Allah تعالى,

وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ

“Na wanajifunza yatakayowadhuru wala hayawanufaishi.”

Maana yake, “Inadhuru Dini yao na haina faida ukilinganisha na madhara.”

وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ

“Na hakika wanajua kwamba aliyekhiari haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera.”

Maana yake: “Mayahudi walichagua uchawi badala ya kumfuata Nabii wa Allah walijua ya kuwa wale waliofanya kosa sawa na hilo hawatakuwa na *khalaq* siku ya Kiyama.” Ibn Abbas, Mujahid na As-Suddi رضي الله عنهم walisema kuwa, “hawana fungu.”²

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَلَيْسَ مَا شَرَوْا بِهِمَ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٢٦﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ ءَامَنُوا وَأَتَّقَوْا

لَمَثُوبَةٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ خَيْرٌ لَّوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٢٧﴾

“Na hakika ni kiovu mno walichojiuzia nafsi zao laiti wangalijua.”

“Na lau kuwa wangeamini na wakaogopa, bila ya shaka malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yangukuwa bora. Laiti wange likuwa wanajua!”

¹ Ibn Abi Hatim 1:311.

² Ibn Abi Hatim 1:314.

وَلَيْسَ

“Na hakika ni kiovu.”

Ina maana: Walipendelea uchawi, badala ya kuamini na kumfuata Mtume ﷺ. Kama wangelikuwa na ujuzi wa kile walichoidhinishwa nacho.

وَلَوْ أَنَّهُمْ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَمَثُوبَةٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ خَيْرٌ لَّوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٣﴾

103. “Na lau kuwa wangeamini na wakaogopa, bila ya shaka malipo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu yangukuwa bora. Laiti wangelikuwa wanajua!”

Maana yake: “Kama wangemuamini Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ na wangeacha yaliyokatazwa, kisha Allah تعالى Angewalipa kwa amali hizi njema ingekuwa bora kwao kuliko walichochagua na kukipendelea.” Vile vile, Allah تعالى Amesema,

وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ ثَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ لِّمَن ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا وَلَا يُلْقِيهَا إِلَّا الصَّابِرُونَ ﴿١٠٤﴾

“Na wakasema wale waliopewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye kusubiri.”(28:80)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقُولُوا رَاعِنَا وَقُولُوا أَنْظِرْنَا وَاسْمَعُوا ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٥﴾ مَا يُوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الْمَشْرِكِينَ أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِنْ خَيْرٍ مِّنْ رَبِّكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿١٠٦﴾

104. “Enyi mlioamini! Msiseme: “Raainaa” bali semeni “Ndhurnaa” na sikieni! Na makafiri watapata adhabu chungu.”

105. “Waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na Washirikina Hawapendi mteremshiwe kheri yoyote kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na Mwenyezi Mungu Humkusudia kumpa Rehema Yake Ampendaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa.”

Adabu katika Kuchagua Maneno.

Allah تعالى Aliwakataza waja Wake waumini, kuiga tabia na matendo ya makafiri. Mayahudi walikuwa wakitumia maneno yenye mzunguko yanayoficha yale waliyokusudia. Laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie. Walipotaka kusema, "tusikilize" walitumia neno *Ra'inaa* ambalo ni tusi (kwa kiebrania, lakini lina maana "tusikilize" kwa Kiarabu) Allah تعالى Amesema,

مِنَ الَّذِينَ هَادُوا يُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِ وَيَقُولُونَ سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَأَسْمَعُ غَيْرَ مُسْمَعٍ
وَرَاعَيْنَا لِيَّا بِالسِّنِّيهِمْ وَطَعْنَا فِي الَّذِينَ ءَلَوْ أَنَّهُمْ قَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأَسْمَعُ وَأَنْظُرْنَا لَكَانَ
خَيْرًا لَهُمْ وَأَقْوَمَ وَلَٰكِن لَّعَبَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٦﴾

"Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahali pake, na husema: Tumesikia na tumeasi, na sikia bila ya kusikilizwa. Na husema: "Raa'inaa", kwa kuzipotoa ndimi zao ili kuitukana Dini. Na lau kama wangelisema: Tumesikia na tumetii, na usikie na "Undhurna" (Utuangalie), ingeli kuwa ni kheri kwao na sawa zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru yao; basi hawaamini ila wachache tu." (4:46)

Aidha, Hadith inaeleza kuwa walipowasalimu Waislam, walisema *As-samu alaykum*, maana yake "mfikwe na kifo." Na sisi tumeamrisha tujibu, *Wa-alaykum*, ikiwa na maana, "na nyie pia." Kisha dua zenu dhidi yao zitajibiwa, minghairi ya zao dhidi yetu.

Allah تعالى Aliwakataza Waumini kuwaiga Makafiri kwa ulimi au matendo. Allah تعالى Alisema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقُولُوا رَاعِنَا وَقُولُوا أَنْظِرْنَا وَأَسْمَعُوا ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ
أَلِيمٌ ﴿١٠٤﴾

"Enyi mlio amini! Msiseme: "Raa'inaa" bali semeni "Ndhurnaa" na sikilizeni (amri). Na makafiri watapata Adhabu inayoumiza." (2:104)

Pia, Imam Ahmad alisimulia kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«بُعِثْتُ بَيْنَ يَدَيْ السَّاعَةِ بِالسَّنْبِ حَتَّى يُعْبَدَ اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَجُعِلَ رِزْقِي تَحْتَ ظِلِّ رُمْحِي، وَجُعِلَتِ الدُّلَّةُ وَالصَّغَارُ عَلَى مَنْ خَالَفَ أَمْرِي، وَمَنْ تَشَبَّهَ بِقَوْمٍ فَهُوَ مِنْهُمْ».

“Nilitumwa Mkononi nikiwa na upanga kabla ya Kiyama, mpaka Allah Aabudiwe Peke Yake bila mshirika. Nimejaaliwa riziki yangu chini ya kivuli cha mkuki wangu. Wale waliopinga maamrisha yangu walidhalilishwa na yeyote anayewaiga watu, atakuwa miongoni mwao.”¹

Abu Dawud alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ تَشَبَّهَ بِقَوْمٍ فَهُوَ مِنْهُمْ»

“Anayejishabihisha na watu, ni miongoni mwao.”²

Hadith hizi zinaonesha, pamoja na vitisho na tahadhari, kuwa haturuhusiwi kuwaiga Makafiri katika kauli zao, vitendo, mavazi, sherehe, ibada nk, haturuhusiwi kuiga vitendo vyovyote vya makafiri ambavyo havikufaradhiswa kwetu. Adh-Dhahhak ameripot kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akielezea,

لَا تَقُولُوا رَاعِنَا

“Enyi mlioamini! Msiseme: “Raainaa.”

Walikuwa wakimuambia Mtume ﷺ, *“Arina samak* (ambalo ni tusi).³ Ibn Abu Hatim alisema kuwa iliripotiwa kuwa Abu al-Aliyah, Abu Malik, Ar-Rabi bin Anas, Atiyah Al-Awfi na Qatadah walisema vivyo hivyo.⁴

Zaidi ya hayo, Mujahid alisema, *“Msiseme Raaina* ina maana, *“Msikanushe.”⁵* Mujahid alisema katika Mapokezi mengine, *“Msiseme, “Tunakusikiliza, nawe tusikilize.”* Pia Ata alisema, *“Msiseme, “Raaina”* ilikuwa lahaja iliyotumiwa na Ansar ambayo Allah تعالى Aliwakataza kuitumia.⁶

¹ Ahmad 2:50.

² Abbu Dawud 4:314.

³ At-Tabari 2:461.

⁴ Ibn Abi Hatim 1:317.

⁵ Ibn Abi Hatim 1:318.

⁶ Ibn Abi Hatim 1:318.

Pia, As-Suddi alisema, Rifaah bin Zayd, Myahudi kutoka kabila la Qaynuqa, alikuwa akifika kwa Mtume ﷺ na kumuambia, “Sikiliza, *Ghayr Musmain* (usisikie chochote).”

Waislam walidhani kuwa Mitume walikuwa wanasalimiwa na kuheshimiwa na aina hiyo ya maamkizi, na hii ndio sababu baadhi yao walikuwa wakisema, “Sikia, usisikie chochote.” kama ilivyo tajwa katika Surat An-Nisaa.

Baadaye, Allah تعالى Aliwakataza Waumini kutamka neno *Raaina*.¹ Abdul-Rahman bin Zayd bin Aslam. Pia alisema vivyo hivyo.²

Ukubwa wa Uadui wa Makafiri na Watu wa Kitabu kwa Waislam.

Allah تعالى Amesema,

مَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الْمُشْرِكِينَ أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِنْ خَيْرٍ مِنْ رَبِّكُمْ

“Waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na Washirikina Hawapendi mteremshiwe kheri yeyote kutoka kwa Mola wenu Mlezi.” (2:105)

Allah تعالى Aliuelezea uhasama mkubwa ambao walikuwa nao Washirikina na Watu wa Kitabu, ambao Allah تعالى Ameonya wasiigwe, dhidi ya Waumini, ili Waislam wavunje urafiki nao. Pia, Allah تعالى Ametaja kuwa Aliwapa Waumini Sharia madhubuti ambazo Alizitunga kwa ajili ya Mtume Muhammad ﷺ. Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ

“Na Mwenyezi Mungu Humkusudia Kumpa Rehema Yake Ampendaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa.” (2:105)

* * *

¹ At-Tabari 2:462.

² Ibn Abi Hatim 3:965.

* مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنسِهَا نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّمَّهَا أَوْ مِثْلَهَا أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾ أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٧﴾ أَمْ تُرِيدُونَ أَن تَسْأَلُوا رَسُولَكُمْ كَمَا سُئِلَ مُوسَىٰ مِن قَبْلُ ۗ وَمَن يَتَّبِعِ الْكُفْرَ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٠٨﴾ وَذَكَرْنَا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ مِن بَعْدِ إِيمَانِكُمْ كُفَّارًا حَسَدًا مِّنْ عِنْدِ أَنفُسِهِمْ مِّنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ ۗ فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٩﴾ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ يَّجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١١٠﴾

* مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنسِهَا نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّمَّهَا أَوْ مِثْلَهَا أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾ أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٧﴾

106. "Ishara yoyote Tunayo-ifuta au Tunayoisahaulisha Tunaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu?"

107. "Hujui kwamba Mwenyezi Mungu Ana Ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi

hamna ulinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu."

Maana ya Naskh na Maelezo Yake

Ibn Abu Talha alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake,

* مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ

"Ishara yoyote Tunayoifuta."

Maana yake: "Aya yoyote Tunayoibatilisha."¹ Pia, Ibn Jurayj alisema kutoka kwa Mujahid kuwa alisema,

¹ At-Tabari 2:473.

✽ مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ

“Ishara yoyote Tunayoifuta.”

“Aya yoyote Tunayoifuta.”¹ Pia Ibn Abu Najih alisema kuwa Mujahid alisema kuwa,

✽ مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ

“Ishara yoyote Tunayoifuta.”

Maana yake: “Tunahifadhi maneno, lakini tunabadilisha hukumu yake.” Aliyahusisha maelezo haya kwa wafuasi wa Abdullah bin Mas’ud رضى الله عنه.² Ibn Abu Hatim alisema kuwa, kauli sawa na hizi zilitajwa na Abu Al-Aliyah na Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi.³

Aidha As-Suddi alisema kuwa,

✽ مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ

“Ishara yoyote Tunayoifuta.”

Maana yake: “Tunaifuta.”⁴ Zaidi ya hayo, Ibn Abu Hatim alisema kuwa ina maana: “Kuifuta na kuiondosha, kama vile kufutwa kwa maneno yafuatayo (kutoka ndani ya Qur’an), ***“Mzinifu aliyeoa na aliyeolewa: Wapigwe mawe mpaka wafe.”*** na ***“Mwana wa Adam angepewa mabonde mawili ya dhahabu, angetaka la tatu.”***⁵ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa,

✽ مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ

“Ishara yoyote Tunayoifuta.”

Maana yake: “Sharia yoyote Tunayoifuta kwenye Aya kwa kuharamisha kilichohalalishwa na kuhalalisha kilichoharamishwa. Na Mubaha kuwa Haramu na Haramu kuwa Mubah.” ***“Nasakh”*** uondoshaji huu, hutokea tu kwa amri, vilivyokatazwa, vilivyoruhusiwa, na kadhalika. Ama Hadithi hazifanyiwi ***Nasakh***.

¹ Ibn Abi Hatim 1:321.

² Ibn Abi Hatim 1:322.

³ Ibn Abi Hatim 1:322.

⁴ Ibn Abi Hatim 1:322.

⁵ Ibn Abi Hatim 1:324.

Neno *Nasakh* Kilugha lina maana, "Kunakili kitabu." Maana ya *Nasakh* katika amri ni kuiondoa amri na kuibadili na nyingine. Na kama *Nasakh* inahusu maneno, sheria au yote mawili, bado inaitwa *Nasakh*.¹

Baada ya hapo Allah تعالى Anasema,

أَوْ نُنْسِهَا

"Au (Nunsiha) Tunayoisahaulisha."

Inasomeka kwa namna mbili, *Nansaha* au *Nunsiha*. Ali bin Abu Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

✽ مَا نَنْسَخُ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنْسِهَا

"Ishara yoyote Tunayoifuta au Tunayoisahaulisha."

Maana yake: "Aya yoyote Tunayoifuta haitufanyii mabadiliko." Pia Mujahid alisema kuwa wafuasi wa Ibn Masud رضي الله عنه (wanao soma neno hili *Nansaha*) walisema lina maana, "Tunathibitisha maneno yake na Tunabadilisha hukumu."² 'Ubayd bin Umary, Mujahid na Ata walisema, "*Nansaha*' ina maana, "Tunaichelewesha (hatuibatilishi)."³

Atiyah Al-Awfi alisema kuwa Aya hii maana yake, "Tunachelewesha kuifuta."⁴ *Tafsir* hii ni sawa na iliyotolewa na As-Suddi na Ar-Rabi bin Anas.⁵

Abdur-Razzaq alisema kuwa Ma'mar alisema kuwa Qatadah alizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

✽ مَا نَنْسَخُ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنْسِهَا

"Ishara yoyote Tunayoifuta au Tunayoisahaulisha."

Allah تعالى Alimsahaulisha Mtume Wake ﷺ Aliyoyataka na Alibatilisha Alichotaka kibatilike." Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 2:472.

² At-Tabari 2:476.

³ At-Tabari 2:473.

⁴ At-Tabari 2:474.

⁵ Ibn Abi Hatim 1:326.

نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلَهَا ۗ

“Tutaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake.”

Maana yake: Katika Hukumu kulingana na maslahi ya wahusika, kama ilivyoandikwa na Ali bin Abu Talhah kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,¹

نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلَهَا ۗ

“Tutaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake.”

Maana yake: “Hatufanyi kazi tunaiwacha kwetu na bali tunaleta nyingine au mfano wake.”² Pia As-Suddi alisema kuwa,

نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلَهَا ۗ

“Tutaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake.”

Maana yake: “Tunaleta Aya bora, kuliko tuliyoifuta au sawa na iliyoachwa.”³ Qatadah pia alisema kuwa,

نَأْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَا أَوْ مِثْلَهَا ۗ

“Tutaileta iliyo bora kuliko hiyo, au iliyo mfano wake.”

Maana yake: “Tunaibadilisha na Aya ambayo ina wepesi, au ruhusa, au amri, au makatazo.”⁴

Ubainifu wa Kusihi kwa *Naskh* na Majibu kwa Mayahudi Kuhusu Ukanushaji Wao wa Jambo Hilo.

Allah تعالى Amesema,

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾ أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ

وَالْأَرْضِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٧﴾

¹ At-Tabari 2:481.

² Ibn Abi Hatim 1:326.

³ Ibn Abi Hatim 1:327.

⁴ Rejea.

“...Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu? Hujui kwamba Mwenyezi Mungu Ana Ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna ulinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu.” (2:106-107)

Allah تعالی Anawaelekeza waja Wake kwenye ukweli kuwa Yeye Peke Yake Ndiye Mwenye Umiliki wa Viumbe Wake na Huwatendea Atakavyo. Kwa uhakika, Yeye Ndiye Mwenye Mamlaka ya Juu na Viumbe wote ni Wake, na Amewaumba kama Atakavyo, Huwapa furaha Awatakao, taabu kwa Awatakao, afya kwa Awatakao na maradhi kwa wale Awatakao. Pia Huwajaalia ufanisi Awatakao, na kushindwa kwa Awatakao. Huwahukumu Waja Wake kama Apendavyo, Huruhusu Atakavyo na Hukataza vile Atakavyo. Huamua Atakavyo, hapana mpinzani kwa Hukumu Zake, na hakuna awezaye kumuuliza kwa yale Ayafanyayo bali wao ndio watakaoulizwa. Huwajaribu waja Wake na utiifu wao kwa Manabii Wake kwa Kufanya mabadiliko “*Naskh*.” Huamrisha jambo lenye manufaa ambayo Anayafahamu, na kisha kwa Busara Zake Hulikataza. Hivyo, unapatikana utii wa dhati kwa kufuata Amri Zake, kuwafuata Manabii Wake, kuamini walichokuja nacho, kutekeleza maamrisho yao na kujiepusha na Aliyoyakataza. Kauli ya Allah تعالی hapa ina faida isiyo kifani, inathibitisha kuwa Mayahudi ni Makafiri na Anakanusha madai yao kuwa mabadiliko *Naskh* hayatokei, Allah تعالی Awalaani Mayahudi. Kutokana na ujinga na ufidhuli wao, walidai kuwa akili timamu inaeleza kuwa *Naskh* haitokei. Baadhi yao walitoa madai ya uongo kuwa yapo maandiko matukufu yanayopinga kutokea kwa *Naskh*. Imamu Abu Jafar bin Jarir رحمه الله تعالی alisema, “Aya hii ina maana, “Hufahamu Ewe Muhammad, kuwa Mimi Pekee ni Mmiliki wa mbingu na ardhi na kuwa Huamua lolote Nilitakalo? Nakataza chochote Nitakacho, Nabadili na Kufuta chochote Nitakacho kuhusu Maamrisho Yangu yaliyotangulia na wakati wowote Nitakao. Pia Nathibitisha lolote Nilitakalo.”

Kisha Ibn Jariri رحمه الله تعالی alisema, “Japokuwa Kauli Yake Allah تعالی ilikuwa ni Kumsemesha Mtume Wake kwa njia ya Kumhabarisha kuhusu Ukuu Wake. Pia, ilikuwa ni Kukanusha uongo wa Mayahudi ambao walikanusha kuwa hukumu za Taurati haziwezi kufanyiwa *Naskh*. Aidha Mayahudi walikana Utume wa Isa عليه السلام na Muhammad ﷺ, kwa sababu waliyachukia waliyokuja nayo kutoka kwa Allah تعالی, kama vile kubadilishwa kwa hukumu zilizokuwemo ndani ya Taurati, kama Allah تعالی Alivyoamrisha. Hivyo Allah تعالی Akawaeleza

Mayahudi kuwa Yeye ni Mmiliki wa mbingu na ardhi na pia Ana Mamlaka kamili juu ya vyote. Viumbe Wake ni raia katika Mamlaka Yake, na wanatakiwa kusikia na kutii Amri Zake na Makatazo Yake. Allah تعالی Ana Mamlaka kamili ya Kuamrisha viumbe Wake kama Apendavyo, Kubatilisha Apendavyo, Kuthibitisha kama Apendavyo na Kuamua yapi ya Kuamrisha na Kukataza kama Apendavyo.”¹

Mimi (Ibn Kathir) nasema kuwa Mayahudi walikanusha kuwepo kwa *Nasakh* kama sehemu ya ukafiri na uasi. Akili timamu haiwezi kukanusha kuwepo kwa *Nasakh* katika Maamrishi ya Allah تعالی, kwani Huamua kwa Utashi Wake kama Afanyavyo kama Apendavyo. Zaidi *Nasakh* ilitokea kwenye Vitabu na Sheria zilizopita. Kwa mfano, Allah تعالی Alimruhusu Adam عليه السلام kuwaozesha watoto wake na kisha baadaye Akaharamisha mwenendo huu. Aidha Allah تعالی Alimruhusu Nuhu عليه السلام kula kila aina ya mnyama baada ya kutoka katika Safina, baadaye Aliharamisha kuliwa baadhi ya vyakula. Zaidi, iliruhusiwa mwanaume kuo na ndugu wawili wa kike kwa Wana wa Israeli, lakini mazoea haya yalikatazwa baadaye ndani ya Taurati. Allah تعالی Aliamuru Ibrahim عليه السلام amchinje mwanaye, kisha Aliifuta amri hiyo kabla ya kutekelezwa. Aidha Allah تعالی Aliwaamrisha Wana wa Israeli wawaue wale walioabudia Ng’ombe kisha Akaifuta amri hiyo, hivyo Wana wa Israeli hawakuangamizwa wote. Kuna matukio mengine mengi ambayo Mayahudi wanakiri kuwa yalitokea, lakini wanayapuza. Pia, ni ukweli usiopingika kuwa vitabu vyao vilielezea kuhusu Muhammad ﷺ na vilikuwa na maamrishi ya kumfuata. Maandiko hayo kwenye Vitabu vyao, yanaelezea kuwa Mayahudi walitakiwa kumfuata Muhammad ﷺ na amali zao njema zisingekubaliwa mpaka zikubaliane na Sharia ya Muhammad ﷺ. Mtume ﷺ alileta kitabu kingine, Qur’an ambayo ni Ufunuo wa mwisho kutoka kwa Allah تعالی. Mpaka kufikia hatua hiyo, Allah تعالی Amebainisha Kujuzu kwa *Nasakh* na Kuwakanusha Mayahudi, laana ziwaendee. Ni pale Allah تعالی Aliposema,

أَلَمْ تَعَلَّمْ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾ أَلَمْ تَعَلَّمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مَلَكٌ مُّسْمَوَاتٍ

وَالْأَرْضِ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٠٧﴾

¹ At-Tabari 2:488.

“Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu? Hujui kwamba Mwenyezi Mungu Ana Ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna ulinzi wala msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.”

Ni kama vile Alivyo na Ufalme usio na mipaka, basi pia Anahukumu Atakavyo,

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْآمْرُ^٥

“...Bila shaka, Uumbaji ni Wake na Amri zote ni Zake.” (7:54).

Katika *Surat Aali Imran*, kuna mazungumzo ya Allah تعالى Kuwaambia watu wa Kitabu, ambayo yanaonesha kuwepo kwa *Nasakh* kwa Mayahudi. Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿ كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حَلَالًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا مَا حَرَّمَ إِسْرَائِيلُ عَلَى نَفْسِهِ مِنْ قَبْلِ أَنْ تُنَزَّلَ التَّوْرَةُ^٥ ﴾

“Kila chakula kilikuwa halali kwa kizazi cha Israeli (Mayahudi) isipokuwa kile alichojiharamishia Israel mwenyewe kabla hajateremshwa Taurati...”. (3:93)

Kama tutakavyobainisha maelezo huko mbele Inshaallah. Na waislamu wote wamekubaliana ruhusa ya kuwepo “*Nasakh*” - mabadiliko katika hukumu za Allah تعالى kwa kuwa ndani yake kuna hekima timilifu.

أَمْ تُرِيدُونَ أَنْ تَسْأَلُوا رَسُولَكُمْ كَمَا سُئِلَ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلُ^٥ وَمَنْ يَتَّبِعِ الْكُفْرَ بِلَا إِيمَانٍ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٠٨﴾

108. “Au mnataka kumuomba Mtume wenu kama alivyoombwa Musa zamani? Na anayebadilisha Imani kwa ukafiri bila ya shaka huyo ameipotea njia iliyo sawa.”

Katazo la Kukithirisha Maswali.

Katika Aya hii, Allah تعالى Aliwakataza Waumini kumuuliza Mtume maswali juu ya mambo ambayo yalikuwa hayajatokea. Kama Allah تعالى Alivyoosema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبَدَّ لَكُمْ فَسْأَلْكُمْ وَإِن تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنَزَّلُ الْقُرْءَانُ تُبَدَّ لَكُمْ

“Enyi mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na mkiyauliza inapoteremshwa Qur’an mtabainishiwa...”. (5:101)

Aya hii ina maana, “Ukiulizia juu ya jambo baada ya kuteremshwa, litaelezwa kwa urefu. Kwa hiyo, msiulize juu ya mambo ambayo bado kutokea, kwani yanaweza kuharamishwa kutokana na kuuliza kwenu.” Hii ndiyo sababu Sahihi ilisimulia,

«إِنَّ أَكْبَرَ الْمَسْئَلِ جُزْأًا مَنْ سَأَلَ عَن شَيْءٍ لَّمْ يُحَرِّمْ، فَحَرَّمَ مِنْ أَجْلِ مَسْأَلِهِ»

“Muislamu mwenye dhambi kubwa zaidi ni mwenye kuuliza jambo lisiloharamishwa, na likaharamishwa kwa sababu ya maswali yake.”

Hii ndio sababu Mtume ﷺ alichukia pale alipoulizwa kuhusu mume anayemkuta mwanaume na mkewe, endapo atazungumzia uzinifu wake atakuwa anaweka wazi jambo kubwa; na kama atalinyamazia, atakuwa amenyamazia jambo kubwa. Mtume ﷺ hakupenda maswali ya aina hiyo. Baadaye, Allah تعالى Aliteremsha hukumu ya Mula’ana (Rejea Nur 24:6-9) ndani ya Qur’an. Na kwa kuzingatia hilo, ndio maana imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Al-Mughirah bin Shu’bah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ, “Alikataa kusema, “Ilisemwa” na “alisema” na kufuja fedha au kuuliza maswali mengi.”¹. Muslim aliandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

«دُرُونِي مَا تَرَكْتُمْ، فَإِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِكَثْرَةِ سَوَالِهِمْ وَاخْتِلَافِهِمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ، فَإِذَا أَمَرْتُمْ بِأَمْرٍ فَأَتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَإِنْ نَهَيْتُمْ عَنْ شَيْءٍ فَاجْتَنِبُوهُ»

“Msinidadisi yale ambayo sikuwabainishia, hakika si vingine; wale waliokuwa kabla yenu waliangamizwa kwa sababu ya maswali yao mengi na kuwabishia Mitume wao. Kwa hiyo nikiwaamrisha jambo lifanyeni, muwezavyo, na ninapowakataza jambo epukaneni nalo.”

Mtume ﷺ aliyasema haya baada ya kuwaambia Masahaba kuwa Allah تعالى Amewaamuru kufanya Hijja. Mtu mmoja aliuliza, “Kwa kila mwaka, Ewe Mjumbe wa Allah?” Mtume ﷺ hakumjibu, lakini alirejea maswali yake mara tatu. Kisha Mtume ﷺ akasema,

¹ Fat’hul al-Bari 3:398 na Muslim 3:1341.

«لَا، وَلَوْ قُلْتُ: نَعَمْ، لَوَجِبَتْ وَلَوْ وَجِبَتْ لَمَّا اسْتَطَعْتُمْ»

“Hapana. Ningalisema ndio ingelifaradhihwa, lau ingefaradhihwa nanyi msingeweza kuitekeleza.”¹

Hii ndio sababu Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Tulikatazwa kumuuliza Mtume ﷺ mara kwa mara kuhusu vitu. Hivyo tulifarijika wakati bedui alipokuja kuuliza, nasi tukasikiliza.”²

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa Muhammad Abu Muhammad alimuhadithia kutoka kwa Ikrimah au Said bin Jubayr kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: Rafi bin Huraymilah au Wahb bin Zayd رضي الله عنه, “Ewe Muhammad ! Tuletee Kitabu kilichoshushwa kutoka mbinguni ambacho tutaweza kukisoma, na ufanye mito itiririke, baada ya hayo tutakufuata na kukuamini.” Allah تعالى Aliteremsha majibu kwa changamoto hii,

أَمْ تُرِيدُونَ أَنْ تَسْأَلُوا رَسُولَكُمْ كَمَا سُئِلَ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلُ ۗ وَمَنْ يَتَّبِعِ الْكُفْرَ

بِالْإِيمَانِ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٠٨﴾

“Au mnataka kumuomba Mtume wenu kama alivyoombwa Musa zamani? Na anayebadilisha Imani kwa ukafiri bila ya shaka huyo ameipotea njia iliyo sawa.” (2:108)³

Allah تعالى Aliwakosoa wale waliomuuliza Mtume ﷺ kuhusu suala fulani kwa njia ya kebehi na ubishi kama ambavyo Wana wa Israeli walivyomuuliza Musa عليه السلام kwa ukorofi, ufidhuli na kukataa waliyoambiwa. Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَتَّبِعِ الْكُفْرَ بِالْإِيمَانِ

“Na anayebadilisha Imani kwa ukafiri.” Ina maanisha, yeye mwenye kuchagua ukafiri badala ya Imani.

فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿١٠٨﴾

“...bila ya shaka huyo ameipotea njia iliyosawa.” Maana: Ameetoka kutoka njia sahihi, na kufuata njia ya ujinga na upotofu. Hii ni hali ya wale waliokataa kuwakubali Mitume na kuwatii na wale waliokuwa wakiwauliza Mitume maswali yasiyo ya msingi kwa kupinga na kukufuru.

¹ Muslim 2:975.

² Muslim 1:41.

³ At-Tabari 2:490.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْآبَوَارِ ﴿١٠٦﴾ جَهَنَّمَ يَصَلُّونَهَا مِنْ مَوْبِقِ الْقَرَارِ ﴿١٠٧﴾ ﴾

“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo? Nayo ni Jahannamu! Wataingia Maovu yaliyoje makazi yao!” (14:28-29)

Abu Al-Aliyah alitoa maelezo, “Walibadilisha faraja kwa hali ngumu.”¹

﴿ وَذَكَرْنَا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِكُمْ كُفْرًا حَسَدًا مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٨﴾ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ مِنْ خَيْرٍ نَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٠٩﴾ ﴾

109. “Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wangekurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao, baada ya kuisha wapambanukia Haki. Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake. Hakika Mwenyezi Mungu juu ya kila kitu ni Muweza.”

110. “Na simamisheni Sala na toeni Zaka; na kheri mnazojitangulizia mafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyafanya.”

Kukatazwa Kufuata Njia za Watu wa Kitabu.

Allah تعالى Aliwatahadharisha waja Wake Waumini kutofuata njia za Watu wa Kitabu, ambao kwa dhahiri au kwa siri wanawafanyia uadui na kuwachukia Waumini, na ambao wanawaonea inda waumini, wakati wanapogundua

¹ Ibn Abi Hatim 1:330.

utukufu wa Waumini na Mtume wao. Pia Allah تعالی Aliwaamrisha waja Wake Waumini kuwasamehe na kuwa na subira nao, mpaka Allah تعالی Atakapotoa msaada Wake na Kuwapa ushindi. Allah تعالی Aliwaamrisha Waumini kusimamisha Sala kwa usahihi, na kutoa Zaka na Akawashajiisha kuendeleza matendo mema. Ibn Abu Hatim alipokea kutoka kwa Abdullah bin Ka'b bin Malik alisema kuwa Ka'b bin al-Ashraf, ambaye alikuwa Myahudi na mshairi, ambaye alikuwa akimkosoa Mtume ﷺ katika mashairi yake, hivyo Allah تعالی Aliteremsha kuhusu yeye,

وَدَّ كَثِيرٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ

“Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wangekurudisheni.”

Kuhusu jambo hili.¹ Pia, Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas alisema, “Nabii asiyejua kusoma wala kuandika, aliwajulisha watu wa Kitabu kuhusu yale yaliyomo kwenye vitabu vyao yaliyozungumzia Mitume na Ishara za Allah تعالی. Aidha anaamini yote haya, kama wanavyoamini. Bado, walimkataa Mtume kwa kufuru, kuwaonea wivu na kuchupa mipaka. Hii ndio sababu Allah تعالی Amesema,

كُفَّارًا حَسَدًا مِّنْ عِنْدِ أَنْفُسِهِمْ مِّنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ

“Muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao, baada ya kwisha wapambanukia Haki.”

Allah تعالی Alisema kuwa baada ya Kuwaangazia ukweli, kiasi ambacho hawakuwa wajinga na jambo lolote, bado walimuonea inda na kumkana Mtume ﷺ. Hivyo Allah تعالی Aliwakosoa, Akawatia adabu na Akawakanusha.² Allah تعالی Aliamuru sifa bainifu ambazo Mtume Wake ﷺ na Waumini washikane nazo. Imani, Itikadi na kukubali Aliyoteremsha Allah تعالی kwa waliokuja kabla yao kutokana na Ukarimu Wake na Wema Wake usio mithilika. Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa,

مِّنْ عِنْدِ أَنْفُسِهِمْ

“Ndani ya nafsi zao.” Maana yake: Kutoka kwao³. Pia Abu Al-Aliyah alisema kuwa,

¹ Ibn Abi Hatim 1:331.

² At-Tabari 2:502.

³ Ibn Abi Hatim 1:332.

مَنْ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ

“Baada ya kuisha wapambanukia Haki.” Maana, “Baada ya kubainika kuwa Muhammad ﷺ ni Nabii wa Allah تعالى ambaye walikuta ameandikwa ndani ya Taurati na Injili. Walimkataa kwa kukufuru na Kuchupa mipaka kwa sababu hakuwa miongoni mwao”¹. Qatadah na Ar-Rabi bin Anas walisema vivyo hivyo². Allah تعالى Amesema,

فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهَ بِأَمْرِهِ

“Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake.” Hii ni sawa na Kauli Yake hii,

وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا

“Na bila shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutoka kwa waliopewa Kitabu kabla yenu na wale walio washirikina.” (3:186)

Ali ibn Abu Talhah alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهَ بِأَمْرِهِ

“Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake.” Ilifutwa na Aya,

فَأَقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ

“Waueni washirikina popote muwakutapo.” (9:5) Na Kauli Yake,

فَقَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Piganeni na wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho.” (9:29). Mpaka

وَهُمْ صَافِرُونَ

“Hali wametii.” (9:29)

Msamaha wa Allah تعالى kwa makafiri ulifutwa.³ Abu Al-Aliyah, ar-Rabi bin Anas, Qatadah na As-Suddi⁴ walisema vivyo hivyo. Ulifutwa na Aya ya upanga.

¹ Ibn Abi Hatim 1:335.

² Ibn Abi Hatim 1:335.

³ Ibn Abi Hatim 1:334.

⁴ Ibn Abi Hatim. 1:335.

حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهَ بِأَمْرِهِ^١

“Mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake.”

Inaipa nguvu rai hii. Ibn Abu Hatim aliandika kuwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ na Masahaba wake walikuwa wakiwasamehe makafiri na Watu wa Kitabu, kama Alivyowaamrisha katika Kauli Yake,

فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهَ بِأَمْرِهِ^٢ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٠٦﴾

“Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”

Mtume ﷺ alikuwa akiwasamehe na akiwavutia subira kama walivyoamrisha na Allah تعالى، mpaka Allah تعالى Alipowaruhusu kuwapiga. Kisha Allah تعالى Aliwaangamiza wale Aliowahukumu wauawe miongoni mwa watu maarufu wa Ki-Quraysh na jeshi la Mtume ﷺ.¹ *Isnadi* ya masimulizi ya maandiko haya ni Sahih, lakini sikuona maandiko yake katika makusanyo ya vitabu sita vya *Hadith*, japokuwa msingi wake upo ndani ya Sahih mbili, ikisimuliwa kutoka kwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه.²

Kutiwa Moyo Kufanya Amali Njema.

Allah تعالى Amesema.

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ يَّجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ^٣

“Na shikeni Sala na toeni Zaka; na kheri mnazojitangulizia nafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyafanya.”

Allah تعالى Aliwatia moyo Waumini wajishughulishe kufanya amali njema ambazo zitawafaidisha na malipo siku ya Kiyama, kama vile Sala na kutoa Zaka. Kwa njia hii, watapata msaada wa Allah تعالى katika maisha ya leo na ya kesho ambayo shahidi atashuhudia.

¹ Ibn Abi Hatim 1:333.

² Fat'hul Al-Bari 8:87 na Muslim 3:1422.

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ۝

“Siku ambayo hautawafaa madhalimu udhuru wao, nao watapata laana, na makazi mabaya kabisa.” (40:52)

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema,

إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝

“Hakika Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyafanya.”

Ina maana: Hapitwi na amali ya mtu yeyote, wala amali hizo hatozipoteza. Ima amali hizo ni njema au mbovu, Allah تعالى Atazilipa kwa mujibu ya stahiki ya muhusika kwa kuzingatia amali zake.

* * *

وَقَالُوا لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ نَصْرِيًّا ۗ تِلْكَ أُمَّاتُهُمْ ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١١١﴾ بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرُهُ عِنْدَ رَبِّهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾ وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتِ النَّصْرِيُّ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ النَّصْرِيُّ لَيْسَتِ الْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُمْ يَتْلُونَ الْكِتَابَ ۗ كَذَلِكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ مِثْلَ قَوْلِهِمْ ۗ فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١١٣﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن مَنَعَ مَسْجِدَ اللَّهِ أَنْ يُذَكَرَ فِيهَا اسْمُهُ وَسَوَّىٰ فِي خَرَابِهَا ۗ أُولَٰئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ أَنْ يَدْخُلُوهَا إِلَّا خَافِينَ ۗ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١١٤﴾ وَاللَّهُ الشَّرِيفُ الْكَرِيمُ ۗ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا فَنَمَّ وَجْهُ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾ وَقَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ لَّهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ كُلُّ لَّهُ قٰنِیْنٌ ﴿١١٦﴾ بَدِيعَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَإِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿١١٧﴾ وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ لَوْلَا يُكَلِّمُنَا اللَّهُ أَوْ تَأْتِينَا آيَةٌ ۗ كَذٰلِكَ قَالَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِثْلَ قَوْلِهِمْ ۗ تَشٰبَهَتْ قُلُوْبُهُمْ ۗ قَدْ بَيَّنَّا الْآيٰتِ لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿١١٨﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ۗ وَلَا تُسْأَلُ عَنْ أَصْحَابِ الْجَبْرِ ﴿١١٩﴾

وَقَالُوا لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ نَصْرِيًّا ۗ تِلْكَ أُمَّاتُهُمْ ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١١١﴾ بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهُ أَجْرُهُ عِنْدَ رَبِّهِ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾ وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتِ النَّصْرِيُّ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ النَّصْرِيُّ لَيْسَتِ الْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُمْ يَتْلُونَ الْكِتَابَ ۗ كَذَلِكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ مِثْلَ قَوْلِهِمْ ۗ فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١١٣﴾

111. "Na walisema: Hataingia Peponi ila aliye-kuwa Yahudi au Mkristo. Hayo ni matamanio yao. Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli."

112. "Sivyo hivyo! Yeyote anayeelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye ni mtenda mema, basi

ana malipo yake kwa Mola Wake Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika."

113. "Na Mayahudi husema: "Wakristo hawana chochote." Na Wakristo husema, "Mayahudi hawana chochote." Na hali wote wanasoma Kitabu. Na hivi ndivyo wale wasiojua wasemavyo. Ni mfano wa kauli yao basi Allah Atahukumu baina yao siku ya kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitilafiana."

Matarajio ya Watu wa Kitabu.

Allah تعالی Aliondoa mkanganyiko wa Mayahudi na Wakristo, kwani walidai kuwa hapana atakayeingia Peponi isipokuwa Mayahudi na Wakristo. Vile vile Allah تعالی Alitaja madai yao katika *Surat Al-Maidah*. Pale waliposema,

فَخَنُّوا أَيْدِيَهُمْ وَأَحْسِنُوا لَهُمْ

"Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake." (5:18)

Allah تعالی Aliyakanusha madai haya ya uongo na Akawafahamisha kuwa wataadhibiwa kwa sababu ya madhambi yao. Mwanzo tulitaja madai yao kuwa moto hautawagusa bali kwa siku chache, baada ya hapo wataingizwa Peponi. Allah تعالی Alikemea dai hili, na Akasema dai hili halina msingi wowote.

تِلْكَ أَمَانِيُّهُمْ

"Haya ni matamanio yao."

Abu Al-Aliyah alitoa maelezo, "Haya ni matarajio waliyotarajia kuwa Allah تعالی Angewatunuku, bila kigezo chochote."¹

Qatadah na Ar-Rabi bin Anas² walisema sawa na hayo. Kisha Allah تعالی Alisema,

قُلْ

"Sema." Maana yake, "Sema Ewe Muhammad."

¹ Ibn Abu Hatim 1:336.

² Ibn Abu Hatim 1:336.

قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ

“Leteni ushahidi wenu.” Maana yake: “Ushahidi wenu” kama Abu Al-Aliyah, Mujahid, As-Suddi na Ar-Rabbi bin Anas walivyosema.¹ Qatadah alisema kuwa Aya ina maana, “Leteni ushahidi wenu unaounga mkono kauli yenu.”

إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٧﴾

“Kama nyinyi ni wasema kweli.” Katika madai yenu.²

Kisha Allah تعالی Akasema,

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ

“Sivyo hivyo! Yeyote anayeelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye ni mtenda mema.”

Maana yake: “Yeyote anayefanya amali njema kwa dhati kwa Allah تعالی Pekee bila kumshirikisha.” Katika Kauli sawa na hii, Allah تعالی Amesema,

فَإِنْ حَاجُّوكَ فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ اتَّبَعَنِ

“Na pindi wakikuhaji (Muhammad) basi sema: Mimi nimeusalimisha uso wangu kumuelekea Mwenyezi Mungu, na kadhalika walionifuata (wamefanya vivyo hivyo).” (3:20)

Abu Al-Aliyah na Ar-Rabi walisema kuwa,

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ

“Sivyo hivyo! Yeyote anayeelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu.” Maana yake: “Yeyote ambaye ni mkweli kwa Allah تعالی.”³ Pia, Said bin Jubayr alisema kuwa,

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ

“Sivyo hivyo! Yeyote anayeelekeza.” Maana yake: Ni mkweli.

وَجْهَهُ

“Uso wake.” Maana yake: Katika Dini yake.⁴

¹ Ibn Abu Hatim 1:337.

² Ibn Abu Hatim 1:337.

³ Ibn Abu Hatim 1:337.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:338.

وَهُوَ مُحْسِنٌ

“Naye ni Muhsin” Maana yake: Akamfuata Mtume ﷺ kwani amali inayokubaliwa ina masharti mawili, mosi, amali lazima ifanywe kwa ajili ya Allah تعالى Peke Yake. Pili, na iwe kwa mujibu wa Sharia. Iwapo amali ina Ikhlas ndani yake, lakini haikukubaliana na Sharia, hivyo haitakubaliwa. Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ»

“Mwenye kufanya jambo lisiloendana na jambo letu (Dini yetu) litakataliwa.”

Hadithi hii iliandikwa na Muslim.¹ Kwa Hiyo, Amali njema za Makasisi na Maruhubani hazitapokelewa, japokuwa ni Watiifu kwa Allah تعالى Peke Yake, kwani amali hizi hazilingani na njia ya Mtume ﷺ, ambaye alitumwa kwa binadamu wote. Allah تعالى Amesema kuhusu hali hiyo,

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنثُورًا ﴿٢٣﴾

“Na Tutayaenda yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye kama mavumbi yaliyo tawanyika.” (25:23) Na,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُمْ كَسْرَابٍ بِقَيْعَةٍ يَخْسَبُهُ الظَّمْثَانُ مَاءً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ

شَيْئًا

“Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaenda hapati chochote.” (24:39) Na Allah تعالى Amesema,

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَدَشَعَةٌ ﴿٢٤﴾ عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٢٥﴾ تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٢٦﴾ تُسْقَىٰ مِن عَيْنٍ

ءَانِيَةٍ ﴿٢٧﴾

“Siku hiyo nyuso zitainama. Zikifanya kazi, nazo taabani. Ziingie katika moto unaowaka. Zikanyweshwa kutoka chemchemu inayo chemka.” (88:2-5)

Na Amali itakapowafikiana na Sharia kwa nje, lakini mtu hakufanya amali kwa Ikhlas, maana kwa ajili ya Allah تعالى Peke Yake, Amali hiyo itakataliwa,

¹ Muslim 3:1344.

ilivyo katika suala la Wanafiki na wale wanaofanya amali kwa kujionesha. Kama Allah تعالى Alivyosema,

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالَى يُرَاءُونَ
النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١١٢﴾

“Hakika wanafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye Ndiye Mwenye Kuwakhadaa wao. Na wanapoinuka kusali huinuka kwa unyong’onyo, wanajionesha kwa watu tu, wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.” (4:142) Aidha Allah تعالى Amesema,

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ﴿١١٣﴾ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿١١٤﴾ الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿١١٥﴾
وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونَ ﴿١١٦﴾

“Basi, ole wao wanaosali, ambao wanapuuza Sala zao; ambao wanajionesha, nao huku wanazuia msaada.” (107:4-7)

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema,

فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا ﴿١١٧﴾

“Mwenye kutaraji kukutana na Mola Wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi.” (18:110)

Pia Amesema katika Ayah hii,

بَلَىٰ مَنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ

“Sivyo hivyo! Yeyote anayeelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu naye ni mtenda mema.” Na Kauli ya Allah تعالى,

فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٨﴾

“Basi ana malipo yake kwa Mola Wake Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.”

Allah تعالى Aliwathibitishia malipo na usalama kutokana na waviogopavyo na wanapaswa kuepukana navyo.

وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“Wala haitakuwa khofu juu yao.” Siku zijazo.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١١﴾

“Wala hawatahuzunika.” Kuhusu yale waliyoyaacha siku zilizopita. Pamoja na hayo, Said bin Jubyr alisema,

وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“Wala haitakuwa khofu juu yao.” Siku ya Kiyama, na

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١١٢﴾

“Wala hawatahuzunika.” Kuhusu kifo chao ambacho kipo karibuni.¹

Mayahudi na Wakristo Wanakanushana Wenyewe kwa Wenyewe Kutokana na Ukafiri na Ukaidi.

Allah تعالى Amesema,

وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتِ النَّصْرَىٰ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ النَّصْرَىٰ لَيْسَتِ الْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ
وَهُمْ يَتْلُونَ الْكِتَابَ^١

“Na Mayahudi husema: Wakristo hawana lao jambo. Na Wakristo husema: Mayahudi hawana lao jambo. Na ilhali wote wanasoma Kitabu hicho (Biblia).” (2:113)

Allah تعالى Ameelezea makinzano, chuki na usafihi waliokuwa nao watu wa Kitabu wao kwa wao. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ujumbe wa Wakristo kutoka Najran walikuja kwa Mtume ﷺ, Marabbi wanazuoni wa Kiyahudi walikuja na kuanza kubishana nao mbele ya Mtume ﷺ.” Rafi bin Huraymilah alisema, “Hamfuati chochote.” Na alirejea rejea kumkanusha Isa عليه السلام na Injili. Kisha mtu miongoni mwa Ujumbe wa Wakristo kutoka Najran aliwaambia Mayahudi, “Bali nyie hamfuati chochote.” Na akarejea rejea kukataa Utume wa Musa عليه السلام na kuikanusha Taurati. Hivyo Allah تعالى Akateremsha Aya,

¹ Ibn Abu Hatim 1:338.

وَقَالَتِ الْيَهُودُ لَيْسَتْ الْنَّصْرَىٰ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ النَّصْرَىٰ لَيْسَتْ الْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ
وَهُمْ يَتْلُونَ الْكِتَابَ^٤

“Na Mayahudi husema: Wakristo hawana lao jambo. Na Wakristo husema: Mayahudi hawana lao jambo. Na ilhali wote wanasoma Kitabu.”¹

Allah تعالی Aliweka wazi kuwa kila kundi lilisoma uthibitisho wa kile walichodai kukikataa Kitabu chao. Kwa hiyo, Mayahudi walimkana Isa عليه السلام, japokuwa walikuwa na Taurati ambayo iliandika juu ya Allah تعالی Kuchukua Ahadi kwa ulimi wa Musa عليه السلام kumuamini Isa عليه السلام. Pia Injili ina uthibitisho wa Isa عليه السلام kuwa Utume wa Musa عليه السلام na Taurati vilitoka kwa Allah تعالی. Bado kila kundi lilikanusha kile walichokuwa nacho wenzi wao.

كَذَٰلِكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ مِثْلَ قَوْلِهِمْ^٥

“Na kadhalika walisema wale wasiojua kitu mfano wa kauli yao hii.”

Hivyo kufichua ujinga uliooneshwa na Mayahudi na Wakristo kuhusu kauli zao tulizozitaja. Kuna tofauti ya maoni kuhusu maana ya Kauli ya Allah تعالی,

الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

“Wale wasiojua kitu.” Kwa mfano, Ar-Rabi bin Anas na Qatadah walisema kuwa,

كَذَٰلِكَ قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

“Na kadhalika walisema wale wasiojua kitu.”Maana yake: “Wakristo walitoa kauli sawa kwa Mayahudi.”² Ibn Jurayj alimuuliza Ata, “Ni nani hao wasiojua kitu?” Ata akasema, “Mataifa yaliyokuwepo kabla ya Mayahudi na Wakristo na kabla ya Taurati na Injili.”³ Pia, As-Suddi alisema kuwa,

قَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

“Walisema wale wasiojua.” Hii ni kuhusu Waarabu ambao walisema kuwa Muhammad ﷺ hakuwa anafuata chochote⁴ (hakufuata ukweli au dini iliyokuwepo). Abu Jafar bin Jarir رحمه الله تعالی alichagua rai, kuwa Ayah hii ni ya

¹ Ibn Abu Hatim 1:339 Sanadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 1:341.

³ Ibn Abu Hatim 1:340.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:340.

jumla na hapana ushahidi kuwa inaunga mkono moja ya maelezo yaliyotolewa. Hivyo kuifanua Aya kwa ujumla ni njia bora. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Allah تعالى Amesema,

فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١١١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.”

Maana yake: Kuwa Allah تعالى Atawakusanya wote siku ya kurejea. Siku hiyo, Allah تعالى Atawahukumu baina yao kwa uadilifu mkubwa, kwani Yeye Hamdhulumu yeyote, hata iwe amali ni ndogo kama upunje. Ayah hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى kwenye Surat Al-Hajj.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّالِحِينَ وَالنَّصِرَىٰ وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ

اللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٢﴾

“Hakika walioamini, na ambao ni Mayahudi na Wasabai na Wakristo na Majusi na wale walio washirikina hakika Mwenyezi Mungu Atawapambanua baina yao Siku ya Kiyama. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.” (22:17)

Allah تعالى Amesema,

قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَاتِحُ الْعَلِيمُ ﴿١١٣﴾

“Sema: Mola Wetu Mlezi Atatukusanya, kisha Atatuhukumu kwa haki; na Yeye Ndiye Mwenye Kujua.” (34:26)

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن مَنَّ مَسْجِدَ اللَّهِ أَنْ يُذَكَّرَ فِيهَا بِاسْمِهِ وَسَعَىٰ فِي خَرَابِهَا ۗ أُولَٰئِكَ مَا

كَانَ لَهُمْ أَنْ يَدْخُلُوهَا إِلَّا خَائِفِينَ ۗ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ

عَظِيمٌ ﴿١١٤﴾

114. “Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa ndani yake Jina Lake na akajitahidi kuiharibu? Watu hao haitawafalia kuingia humo ila nao wanaogopa. Duniani watapata fedheha na Akhera watapata adhabu kubwa.”

Madhalimu wakubwa ni Wale wanaowazuia Watu Katika Misikiti na Wanajitahidi Kuiharibu.

Wanaokusudiwa hapa kuzuia Misikiti ya Allah na wanajitahidi kuiharibu ni Maquraishi. Ibn Jariri رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Ibn Zayd alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ مَنَعَ مَسْجِدَ اللَّهِ أَنْ يُذَكَّرَ فِيهَا اسْمُهُ وَسَعَىٰ فِي خَرَابِهَا

“Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa ndani yake Jina Lake na akajitahidi kuiharibu?”

Ni madhalimu wa Kiquraish ambao walimzuia Mtume ﷺ kuingia Makkah kutoka Al-Hudaibiyah, mpaka alipomchinja mnyama wa kafara (*Hadi*) hapo Dhi-Tuwa. Kisha alikubali kufanya nao Mkataba wa amani na akawaambia, “Hajawahi kutokea yeyote ambaye aliwazuia watu kuingia Nyumba ya Mungu. Huko nyuma Mtu angemuona muuaji wa baba yake au kaka yake, lakini asingemzuia (kuingia Nyumba ya Allah).” Walisema, “Yeyote aliyewaua baba zetu katika Badr, hatoingia katika Ka’aba muda wa kuwa sisi bado tupo hai.” Kauli ya Allah تعالى،

وَسَعَىٰ فِي خَرَابِهَا

“Na akajitahidi kuiharibu.” Maana yake: Wale wanaowazuia wanaoimarisha Misikiti kwa kumdhukuru Allah تعالى na kuzuru Nyumba ya Allah تعالى kwa ibada ya *Hajj* na *Umrah*.¹ Ibn Abu Hatim alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Maquraish walimzuia Mtume ﷺ kusali katika Al-Ka’bah ndani ya *Al-Masjid Al-Haram*, hivyo Allah تعالى Akateremsha،

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ مَنَعَ مَسْجِدَ اللَّهِ أَنْ يُذَكَّرَ فِيهَا اسْمُهُ

“Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayezuia misikiti ya Mwenyezi Mungu Kutajwa ndani yake Jina Lake.”²

Baada ya Allah تعالى Kutoa karipio kwa Mayahudi na Wakristo. Pia Aliwakosoa madhalimu waliomfukuza Mtume ﷺ na Masahaba zake kutoka Makkah, wakiwazuia kusali ndani ya *Al-Masjid Al-Haram*, ambao waliufanya mahsusi kwa ajili ya masanamu yao na ushirikina wao. Kama Allah تعالى Alivyosema،

¹ At-Tabari 2:521.

² Ibn Abu Hatim 1:341. Isnadi yake ni dhaifu.

وَمَا لَهُمْ آلَا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ وَهُمْ يَصُدُّونَ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ^٤
 إِنْ أَوْلِيَاءَهُ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَلَكِنْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١١١﴾

“Lakini wana jambo gani hata Mwenyezi Mungu Asiwaadhibu, na hali ya kuwa wanawazuilia watu Msikiti Mtakatifu? Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa ila wacha Mungu tu. Lakini wengi katika wao hawajui.” (8:34) Na Allah تعالى Amesema,

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ
 أَعْمَالُهُمْ فِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿١١١﴾ إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ^٥ فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَنْ
 يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ ﴿١١٢﴾

“Haiwi kuwa makafiri ndio waamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika, na katika Moto watadumu. Hakika wanaoamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala, na wakatoa Zaka, na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu. Basi huenda hao wakawa katika waongofu.” (9:17-18) Aidha Allah تعالى Amesema,

هُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَالْهَدَىٰ مَعْكُوفًا أَنْ يَبْلُغَ حِلَّهُ^٦
 وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ مُّؤْمِنَاتٌ لَّمَّ تَعَلَّمُوهُمْ أَنْ تَطَّعُوهُمْ فَتُصِيبَكُمْ مِنْهُم مَّعْرَةٌ
 بِغَيْرِ عِلْمٍ^٧ لَّيُدْخِلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ^٨ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ
 عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١١٢﴾

“Hao ndio waliokufuru na wakakuzieni msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia kufika mahali pao. Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini msiowajua mkawasaga na

mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua na kwa hiyo mkipata Masikitiko kwa ajili yao. Mwenyezi Mungu (Amefanya haya) ili Amuingize Amtakaye katika Rehema Yake. Lau wangelitengana bila ya shaka Tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.” (48:25)

Kwa hiyo Allah تعالى Amesema hapa,

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ
وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ^ط

“Hakika wanaoamirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala, na wakatoa Zakah, na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu.” (9:18)

Kwa hiyo, endapo Waumini wanaofuata maadili yaliyotajwa katika Ayah walizuiwa kuingia Msikitini, hivi kuna uharibifu mkubwa kushinda jambo hilo? Kuimarisha Misikiti haina maana kuifanya ipendeze, lakini inahusu kumkumbuka Allah تعالى, kusimamisha Sala, kusimamisha Sharia Zake Misikitini na kuitakasa kutokana na uchafu wa Ushirikina.

Habari Njema kwa Ushindi wa Uislam

Kauli ya Allah تعالى inayofuata,

أُولَئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ أَنْ يَدْخُلُوهَا إِلَّا خَائِفِينَ^ع

“Watu hao haitawafalia kuingia humo ila nao wanaoogopa.”

Ayah hii ina maana, “Msiwaruhusu – makafiri – kuingia Misikitini, isipokuwa kwa kutimiza masharti ya mikataba au kusimamisha vita kwa muda.” Mtume ﷺ alipoiteka Makkah, katika mwaka wa tisa Hijiria. Alimuamrisha sahaba mmoja kwenda Minah kutangaza, “Baada ya mwaka huu tulionao, washirikina hawataruhusiwa Kuhiji, na watu walio uchi hawataruhusiwa kutufu katika Haram, isipokuwa wale wenye mkataba. Kwa hali hii, mikataba itatekelezwa mpaka mwisho wake.”¹ Aya hii inaunga mkono Aya,

¹ Fat’hul Al-Bari 3:565.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ
عَامِهِمْ هَذَا^٤

“Enyi mlioamini! Hakika Washirikina ni najisi, kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu.” (9:28)

Imeelezwa pia kuwa Ayah (2:114) ina khabari nzuri kwa Waislamu kutoka kwa Allah تعالى kuwa Atawaruhusu kuichukua *Al-Masjid Al-Haram* na Misikiti yote na kuwafedhehesha washirikina. Baadaye Aya ilionesha, hakuna Mshirikina atakayeingia Haram, isipokuwa kwa kuchelea kutekwa nyara na kuuawa, mpaka atakaposilimu. Allah تعالى Aliitimiza ahadi hiyo na baadaye Alitoa Amri ya Kuwazuia washirikina kuingia *Al-Masjid Al-Haram*. Mtume ﷺ aliridhia kuwa Dini moja tu ndio inayotakiwa kuwepo katika Rasi ya Arabia, na Mayahudi na Wakristo lazima wafukuzwe. Sifa zote Njema Anastahiki Allah تعالى. Hukumu zote hizi zinahakikisha kudumisha heshima ya *Al-Masjid Al-Haram* na kulitakasa eneo ambalo Allah تعالى Alimtuma Mjumbe Wake ﷺ kuonya na kuleta habari njema kwa binadamu wote, Rehema na Amani zimfikie.

Aya pia inaelezea fedheha waliyoipata Makafiri katika dunia na methali ya muosha naye huoshwa, iliwasibu Makafiri. Kama walivyowazuia Waumini kuingia *Al-Masjid Al-Haram*, nao walikuja kuzuiwa kuingia. Kama walivyowafukuza Waumini kutoka Makkah, nao walikuja kufukuzwa kutoka Makkah.

وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١١٤﴾

“Na Akhera watapata adhabu kubwa”.

Kwa sababu walivunja utukufu wa *Haram* na wakaleta uchafu ndani yake kwa kusimika masanamu kuizunguka, wakiwaomba ghairi ya Allah تعالى na wakitufu wakiwa uchi nk.

Inafaa kutaja hapa Hadithi inayohusu kutaka hifadhi kutokana na fedheha ya maisha ya dunia na mateso ya Kiyama. Imam Ahmad alinukuu kuwa Busr bin Artah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alikuwa akiomba dua ifuatayo,

«اللَّهُمَّ أَحْسِنْ عَاقِبَتَنَا فِي الْأُمُورِ كُلِّهَا وَأَجِرْنَا مِنْ خِيَرِ الدُّنْيَا وَعَذَابِ الْآخِرَةِ»

“Ewe Allah! Ufanye mwisho wetu uwe mzuri katika mambo yote,

na Utuokoe kutokana na fedheha katika maisha ya dunia na adhabu ya Akhera.” Hadithi hii ni Hasan.¹

وَلِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ۚ فَأَيُّمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهُ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾

115. “Na Mashariki na Magharibi ni za Mwenyezi Mungu. Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mjuzi.”

Kuelekea Qiblah Wakati wa Sala.

Amri hii ilileta faraja kwa Mtume ﷺ na Masahaba zake, ambao walitolewa Makkah na walitakiwa kuondoka kutoka Al-Masjid Al-Haram. Mtume ﷺ alipokuwa Makkah alikuwa akielekea Qiblah. Mtume ﷺ alipohamia Al-Madinah, aliekea Bayt Al-Maqdis kwa miezi kumi na sita au kumi na saba, na kisha Allah تعالی Alimueleza kuelekea Al-Ka’abah wakati wa Sala. Ndio maana Allah تعالی Akasema,

وَلِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ۚ فَأَيُّمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهُ اللَّهِ ۚ

“Na Mashariki na Magharibi ni za Mwenyezi Mungu. Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo.”

Ali Ibn Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Hukumu ya mwanzo kufutwa katika Qur’an ilikuwa kuhusu Qiblah. Mtume ﷺ alipohamia Al-Madina, ilikuwa inakaliwa na Mayahudi, mwanzo aliamrisha kuelekea Bayt Al-Maqdis. Mayahudi walifurahi, na Mtume ﷺ alielekea Bayt Al-Maqdis kwa kiasi cha miezi kumi. Pamoja na hayo, Mtume ﷺ alipenda kuelekea Qiblah cha Ibrahim (Al-Ka’bah – Makkah) na alikuwa akiangalia mbinguni na kuomba dua.” Hivyo Allah تعالی Aliteremsha,

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ۚ

“Kwa yakini Tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni.” Mpaka,

فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۚ

“Zielekezeni nyuso zenu upande huo.” (2:144)

¹ Ahmad 4:181.

Mayahudi walisumbuliwa sana na mabadiliko hayo na wakasema, "Kitu gani kilichowafanya wabadilishe mwelekeo wa Qiblah kutoka kule walikokuwa wakielekea?" Allah تعالى Akateremsha,

قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ

"Sema (Ewe Muhammad): Mashariki na Magharibi zote ni za Mwenyezi Mungu." (2:142) Na,

فَأَيُّمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهُ اللَّهِ

"Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo."

Ikrimah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

فَأَيُّمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهُ اللَّهِ

"Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo." Maana yake: "Mwelekeo wa Allah تعالى ni Popote unapoelekea, Mashariki au Magharibi."² Mujahid alisema kuwa,

فَأَيُّمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهُ اللَّهِ

"Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo." Maana yake: "Popote utakapokuwa, una Qiblah cha kuelekea, nacho ni Al-Ka'bah."³

Hata hivyo, ilisemwa kuwa Allah تعالى Aliteremsha Aya hii kabla ya Amri ya kuelekea Ka'abah. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, "Wengine wanasema kuwa Aya hii iliteremshwa kwa Mtume ﷺ ikitoa ruhusa kwa anayesali Sala ya Sunnah aelekee aendapo, Mashariki au Magharibi, awapo safarini, anapokuwa na khofu au anakabiliana na adui."⁴ Kwa mfano, Ibn Umar رضي الله عنهما alikuwa anasali huku akielekea kule alikoelekea mnyama wake na akasema. Hivyo ndivyo alivyomuona Mtume ﷺ akifanya, akielezea Ayah,

فَأَيُّمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهُ اللَّهِ

"Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo."⁵

¹ At-Tabari 2:527.

² Ibn Abu Hatim 1:347.

³ Ibn Abu Hatim 1:345.

⁴ At-Tabari 2:530.

⁵ Ibn Abu Hatim 2:345.

Hadithi hiyo ilikusanywa pia na Muslim, At-Tirmidhi, An-Nasai, Ibn Abu Hatim na Ibn Marduwyah. Na asili yake imo katika Sahih mbili kutoka kwa Ibn Umar na Amr bin Rabiah رضي الله عنها bila kutaja Ayah hii.¹ Katika Sahihi yake, Al-Bukhari alinukuu kuwa Nafi alisema kuwa kila Ibn Umar رضي الله عنهما alipoulizwa kuhusu Sala wakati wa khofu, alikuwa akielezea wasifu wake, “Kama hofu imekuwa kubwa zaidi walisali huku wakitembea kwa miguu au wakiwa juu ya mnyama, hali ya kuelekea *Qiblah* au bila kuelekea (upande wowote).” Kisha Nafi akasema, “Nadhani Ibn Umar رضي الله عنهما alimsikia Mtume ﷺ² akisema hivyo.” Inasemekana kuwa Ayah hii ilishuka kwa ajili ya wale walioshindwa kupata *Qiblah* sahihi kutokana na kiza au mawingu, hivyo Wakaelekea pasipo *Qiblah* kwa makosa.

***Qiblah* kwa Watu wa Madinah ni Baina ya Mashariki na Magharibi.**

Katika *Tafsir* yake ya Ayah hii, Al-Hafidh Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ قِبْلَةٌ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَأَهْلِ الشَّامِ وَأَهْلِ الْعِرَاقِ»

“Sehemu iliyo kati ya Mashariki na Magharibi ni *Qiblah* kwa watu wa Al-Madinah, Ash-Sham na Iraq.”³

At-Tirmidhi na Ibn Majah waliandika Hadithi hii kwa maneno yafuatayo,

«مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ قِبْلَةٌ»

“*Qiblah* kipo baina ya Mashariki na Magharibi.”⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Maana ya Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٠﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mjuzi.”

Ni kuwa Allah تعالى Anawatoshleza viumbe Wake kwa kukidhi mahitaji yao kutokana na Ukarimu Wake na Fadhila Zake. Kauli Yake,

¹ Muslim 1:486, Tuh’fatul Al-Ahwadhiy 8:292, An-Nasai, Al-Kubra 1:244, Ibn Abu Hatim 1:344 na Al-Hakim 2:266.

² Fat’hul Al-Bari 8:46.

³ Al-’Uqayli 4:309 Isnadi yake ni dhaifu.

⁴ Tuhfatul Al-Ahwadhi 2:317 na Ibn Majah 1:323.

عَلِيمٌ

“Mjuzi.”

Ina maana: Anazifahamu amali zao na hakuna kimpitacho, wala hapana asiye kijua. Bali, Ufahamu Wake unajumuisha kila kitu.¹

وَقَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ لَّهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ كُلٌّ لَّهُ فٰتِنٰتٌ ۗ

بَدِيعُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ وَاِذَا قَضٰٓءُ اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهُ كُنْ فَيَكُوْنُ ۗ

116. “Na ati wanasema: Mwenyezi Mungu Ana mwana. Subhanahu! Ametakasika na hayo. Bali vyote viliomo mbinguni na duniani ni Vyake. Vyote vinamtii Yeye.”

117. “Yeye Ndiye Muumba wa mbingu na ardhi pasi na ruwaza; na Anapotaka jambo basi Huliambia tu: Kuwa! Nalo huwa.”

Kuwajibu Wanaosema Kuwa Allah تعالی Ana Mwana.

Ayah hii na inayofuatia inakanusha madai ya Wakristo, Allah تعالی Awalaani, na wenye fikra sawa na hizo miongoni mwa Mayahudi na Washirikina wa Kiarabu, kuwa Malaika ni mabinti wa Allah, Allah تعالی Aliwakadhibisha wote hao katika madai yao kuwa Yeye Ana mtoto wa kiume. Allah تعالی Amesema,

سُبْحٰنَهُ ۗ

“Subhanahu!”

Ina maana: Yeye ni Mtakatifu sana na Muadilifu kuliko madai yao hayo:

بَلْ لَّهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ

“Bali vyote viliomo mbinguni na duniani ni Vyake.”

Maana yake: Ukweli si kama Makafiri wanavyoasi, bali, Ufalme wa mbinguni na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake ni wa Allah تعالی, Naye ni Muumba, Mlishi wao na Mhimili Anayeamua mambo yote ya viumbe Wake kama Apendavyo. Viumbe wote ni waja wa Allah تعالی na Anawamiliki. Kwa hiyo inawezekanaje mmoja wao akawa mtoto Wake? Mtoto wa binadamu anazaliwa

¹ At-Tabari 2:537.

kutokana na muungano wa viumbe wawili. Allah تعالى Hana mwenza au mshindani anayeshirikiana Naye katika Rehema na Ukuu Wake, hivyo Anawezaje kuwa na mwana wakati Hana mke?. Allah تعالى Amesema,

بَدِيعُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنِّي يَكُونُ لَهُ وَلَدٌ وَلَمْ تَكُنْ لَهُ صَاحِبَةٌ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٠١﴾

“Yeye Ndiye Muumba wa mbingu na ardhi. Inamkinikaje Awe na mwana, hali Hana mke? Naye Ndiye Aliyeumba kila kitu. Naye ni Mwenye Kujua kila kitu.” (6:101)

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿١٠٢﴾ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿١٠٣﴾ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ۗ وَمَا يُبْغِي لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ۗ ﴿١٠٤﴾ إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ عَبْدًا ۗ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ۗ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ۗ ﴿١٠٥﴾

“Na wao ati husema kuwa A-Rahmani Mwingi wa Rehema Ana Mwana! Hakika mmeleta jambo la kuchosha mno! Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. Kwa kudai kwao kuwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema ana Mwana. Wala hahitajii Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema kuwa na mwana. Hapana yeyote aliye mbinguni na ardhini ila atafika kwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.” (19:88-95) Na Allah تعالى Amesema,

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ اللَّهُ الصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ﴿٤﴾

“Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala Hana anaye fanana Naye hata mmoja.” (112:1-4)

Katika Ayah hizi Allah تعالى Amedhukuru kuwa Yeye ni Bwana wa mabwana, Hapana mfano Wake wala mshindani, kila kitu na kila mtu aliumbwa na Yeye, vipi Atakuwa na mwana kutokana na wao? Hii ndio sababu katika *Tafsir* ya Ayah hii, Bukhari aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«قَالَ اللهُ تَعَالَى: كَذَّبَنِي ابْنُ آدَمَ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، وَسَتَمَنِي وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، فَأَمَّا تَكْذِيبُهُ إِيَّايَ فَبِزَعْمِ أَنِّي لَا أَقْدِرُ أَنْ أُعِيدَهُ كَمَا كَانَ، وَأَمَّا سَتْمُهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ لِي وَلَدًا فَسُبْحَانِي أَنْ أَتَّخِذَ صَاحِبَةً أَوْ وَلَدًا»

"Hakika Allah Alisema, "Mwana wa Adam amenikadhibisha, na hiyo siyo haki yake. Na Amenishutumumu na hiyo siyo haki yake, Ama kunikadhibisha Mimi, anadai Sitoweza Kumrejisha kama alivyokuwa (baada ya kufa). Ama kunishutumumu (Mimi), alidai kuwa Nina mwana. Na Kutakasika ni Kwangu tu, ni muhali Kwangu kuwa na mke au mwana." Hadithi hii iliandikwa na Al-Bukhari¹.

Imeandikwa ndani ya Sahihi Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا أَحَدٌ أَضَبَّرَ عَلَيَّ أَدَى سَمِعَهُ مِنْ اللهِ: إِنَّهُمْ يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا وَهُوَ يَرْزُقُهُمْ وَيُعَافِيهِمْ»

"Hakuna msiburifu zaidi juu ya maudhi anayoyasikia, kuliko Allah, kwani wao wanamfanya kuwa Ana mtoto. Lakini bado Anawapa riziki na afya".

Kila Kitu Kinamnyenyekea Allah تعالى na Kumtii.

Allah تعالى Amesema,

كُلُّ لَّهُ قَانِتُونَ ﴿٢٣٨﴾

"Vyote vinamtii Yeye."

Ibn Abu Hatim alisema kuwa abu Said Al-Ashaj aliwafahamisha kuwa Asbat aliwafahamisha kutoka kwa Mutarif, kutoka kwa Atiyah, kutoka kwa Ibn Abbas ambaye alisema kuwa,

قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾

"Qanitin" (2:238)

¹ Fat'hul Al-Bari 13:372 na Muslim 4:2160.

Maana yake: Wanamuabudu Yeye.¹ Ikrimah na Abu Malik pia walisema kuwa,

كُلُّ لَهُ قَنِيْتُونَ ﴿١١١﴾

“Vyote vinamtii Yeye.” Maana yake: Vinamnyenyekea Yeye.² Said bin Jubayr alisema kuwa *Qanitin* ni kuwa na Ikhlas.³ Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa,

كُلُّ لَهُ قَنِيْتُونَ ﴿١١١﴾

“Vyote vinamtii Yeye.” Maana yake: “Kusimama – mbele Yake – Siku ya Kiyama.⁴ Pia As-Suddi alisema kuwa,

كُلُّ لَهُ قَنِيْتُونَ ﴿١١١﴾

“Vyote vinamtii Yeye.”

Maana yake: “Watiifu siku ya Kiyama.”⁵ Khusaif alisema kuwa Mujahid alisema kuwa,

كُلُّ لَهُ قَنِيْتُونَ ﴿١١١﴾

“Vyote vinamtii Yeye.” Maana yake: “Vinamfuata.” Anasema, “Kuwa binadamu” na anakuwa, “binadamu.”⁶ Pia alisema, “(Allah تعالی Anasema), “kuwa punda” na anakuwa, “punda”. Pia Ibn Abu Najih alisema kuwa Mujahid alisema,

كُلُّ لَهُ قَنِيْتُونَ ﴿١١١﴾

“Vyote vinamtii Yeye.”

Ina maana: “Vinamnyenyekea .” Mujahid pia alisema, “Utii wa kafiri hudhihiri pale kivuli chake kinaposujudu, wakati yeye anachukia.”⁷ Kauli ya Mujahid ambayo ilipendelewa na Jariri رحمه الله تعالی, inakusanya maana zote, na kuwa *Qunut* ina maana ya utii na kujisalimisha kwa Allah تعالی. Kuna aina mbili za *Qunut* zilizoamriwa na zilizoteuliwa. Kwa ajili hiyo Allah تعالی Anasema,

¹ Ibn Abu Hatim 1:349.

² Isnadi yake ni dhaifu.

³ Ibn Abu Hatim 1:350.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:350.

⁵ At-Tabari 2:538.

⁶ Ibn Abu Hatim 1:349.

⁷ Ibn Abu Hatim 1:348.

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَظِلَالُهُمْ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿١١٥﴾

“Na vilivyomo mbinguni na katika ardhi vinamsujudia Mwenyezi Mungu tu vitake visitake. Na pia vivuli vyao asubuhi na jioni.”
(13:15)

Maana ya Muumbaji “Badii”

Allah تعالی Amesema,

بَدِيعُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Yeye Ndiye Muumba wa mbingu na ardhi.”

Ambayo ina maana, Aliziumba bila ya kiigizo chochote kabla yake. Mujahid na As-Suddi walisema kuwa hii ni maana ya Muktaadha wa kilugha, kwani mambo mapya yanaitwa *Bad’ah*. Muslim aliandika, Mtume ﷺ alisema,

«فَإِنَّ كُلَّ مُحَدَّثَةٍ بِدْعَةٌ»

“Kila kinachozushwa (katika dini) ni Bid’ah”.

Kuna aina mbili za *Bid’ah*: Kuna *Bid’ah* ya Kisheria, kama ilivyotajwa katika Hadithi.

«فَإِنَّ كُلَّ مُحَدَّثَةٍ بِدْعَةٌ وَكُلُّ بِدْعَةٍ ضَلَالَةٌ»

“Hakika kila kilichozushwa ni Bid’ah na kila Bid’ah ni upotevu.”¹

Na kuna *Bid’ah* yenye maana kilugha, kama vile kauli ya Kiongozi wa Waumini Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alipowakusanya Waislamu kusali *Tarawih* kwa jamaa (pia iliwahi kufanywa na Mtume ﷺ) na alisema, “*Bid’ah* nzuri iliyoje”.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Hivyo maana ya Aya (2:116-117) inakuwa, “Allah تعالی ni Mtakatifu mno kuliko kuwa na mwana, kwani ni Mmiliki wa kila kitu kilichopo mbinguni na duniani. Vyote vinashuhudia Uumoja Wake na unyenyekevu wao Kwake. Yeye Muumbaji na Mtengenezaji Wao. Bila kuwepo kiigizo, Aliwasawiri viumbe kwa maumbile yao ya sasa. Pia Allah تعالی Anashuhudia kwa waja Wake kuwa Isa عليه السلام, ambaye baadhi ya watu wanadai ni mwana wa Allah, ni miongoni mwa wale wanaoshuhudia Upekee Wake. Allah تعالی Alieleza kuwa Aliumba mbingu na dunia bila kuwepo kitu au kiigizo. Vivyo hivyo, Alimuumba Isa عليه السلام (Masihi) kwa Nguvu Zake na bila baba.”¹ Maelezo haya ni kutoka kwa Ibn Jarir رحمه الله تعالى, ni sahihi na mazuri.

¹ Muslim 2:592.

Allah تعالی Amesema,

وَإِذَا قُضِيَٰٓ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿١١٧﴾

“Na Anapotaka jambo basi Huliambia tu: Kuwa! Nalo huwa.”

Hivyo kuonesha Uwezo Wake thabiti na kamilifu na Mamlaka yasiyo na kikomo. Anapambanua jambo, Hutoa amri ya “Kuwa” na inakuwa. Kama Allah تعالی Alivyosema,

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذْ أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿١٦٧﴾

“Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa”. (36:82) Allah تعالی Amesema;

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذْ أَرَدْنَاهُ أَنْ نَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿١٦٨﴾

“Kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka kiwe, ni Kukiambia: Kuwa! Basi kinakuwa”. (16:40) Na Amesema tena:

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَّمَجْ بِالْبَصْرِ ﴿١٦٩﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50)

Hivyo Allah تعالی Ametufahamisha kuwa Alimuumba Isa عليه السلام kwa kusema, “Kuwa na akawa, kama Allah تعالی Alivyotaka.” Allah تعالی Amesema;

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ ءَادَمَ ۗ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿١٧٠﴾

“Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam, Alimuumba kwa udongo kisha Akamuambia: Kuwa! Basi akawa.” (3:59)

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ لَوْلَا يُكَلِّمُنَا اللَّهُ أَوْ تَأْتِينَا ءَايَةً ۗ كَذَٰلِكَ قَالَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

مِثْلَ قَوْلِهِمْ تَشَابَهَتْ قُلُوبُهُمْ ۗ قَدْ بَيَّنَّا ءَالَآئِنَا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿١٧١﴾

118. “Na walisema wale wasiojua kitu: Mbona Mwenyezi Mungu hasemi nasi au zikatufika Ishara. Kama hivyo walisema wale walio kuwa kabla yao mfano wa kauli yao hii. Nyoyo zao zimefanana. Hakika Sisi Tumeziweka wazi Ishara kwa watu wenye yakini.”

¹ At-Tabari 2:550.

Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضى الله عنهما alisema kuwa Rafi bin Huraymilah alimuambia Mtume ﷺ, “Ewe Muhammad kama ulikuwa Mjumbe wa kweli wa Allah تعالى kama unavyodai, basi muambie Allah تعالى Azungumze nasi moja kwa moja, ili tusikie Sauti Yake.” Hivyo Allah Aliteremsha,

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ لَوْلَا يُكَلِّمُنَا اللَّهُ أَوْ تَأْتِينَا آيَةٌ

“Na walisema wale wasiojua kitu: Mbona Mwenyezi Mungu Hasemi nasi au zikatufika Ishara?”¹

Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas, Qatadah na As-Suddi walisema katika tafsiri ya Aya hii kuwa ilikuwa kauli halisi ya Makafiri wa Kiarabu.

كَذَلِكَ قَالَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ مِثْلَ قَوْلِهِمْ

“Kama hivyo walisema wale waliokuwa kabla yao mfano wa kauli yao hii.”

“Hawa ni Mayahudi na Wakristo.”² Hii inathibitisha zaidi kuwa washirikina wa Kiarabu ndio walisema kwa Kauli hii katika Ayah,

وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَن نُّؤْمِنَ حَتَّى نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ

يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا

يَمْكُرُونَ ﴿١١٤﴾

“Na inapowajia Ishara, wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote Kujua wapi Anaweka ujumbe wake. Itawafikia hao waliokosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyokuwa wakifanya.” (6:124) Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَقَالُوا لَن نُّؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنبُوعًا ﴿١١٤﴾

“Na walisema (Ewe Muhammad): Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchemi katika ardhi hii.” Mpaka Aya,

¹ Ibn Abu Hatim 1:352. Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 1:353.

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا ﴿١١٣﴾

“Sema (Ewe Muhammad): Subhana Rabi, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipokuwa ni mwanadamu na Mtume?” (17:90-93) Na Kauli Yake Allah تعالى,

﴿ وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْآمَاتُكُمُ أَو نَرَى رَبَّنَا ۗ ﴾

“Na walisema wale wasiotaraji kukutana Nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika na hatumuoni Mola wetu Mlezi?” (25:21) Na,

﴿ بَلْ يُرِيدُ كُلُّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ أَنْ يُؤْتَىٰ صُحُفًا مُّنشَرَةً ﴾ ﴿٧٤﴾

“Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka zilizo-funuliwa.” (74:52).

Kuna Aya mbalimbali zinazothibitisha ukafiri wa washirikina wa Kiarabu, kuchupa kwao mipaka, ufidhuli na kuwa wakiuliza maswali yasiyo na maana kutokana na ukafiri wao na ufasiki. Kauli za washirikina Waarabu zilifuatia kauli za Mataifa ya Watu wa Vitabu viwili na dini nyingine kabla yao. Kama Allah تعالى Alivyosema,

﴿ يَسْأَلُكَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَنْ تُنزِلَ عَلَيْهِمْ كِتَابًا مِّنَ السَّمَاءِ ۖ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَىٰ أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا آلِهَةً جَهْرَةً ﴾

“Watu wa Kitabu wanakutaka uwatremshie Kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walikwishamtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walisema: Tuoneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi.” (4:153)

﴿ وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَىٰ آلِهَةً جَهْرَةً ﴾

“Na mliposema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumuone Mwenyezi Mungu wazi wazi.” (2:55) Kauli ya Allah تعالى,

﴿ تَشَدَّبَتْ قُلُوبُهُمْ ﴾

“Nyoyo zao zimefanana.” Maana yake: Mioyo ya washirikina wa Kiarabu ni sawa na nyoyo za watu wa kabla yao, zenye uasi, ukorofi na udhalimu. Vile vile Allah تعالى Amesema,

كَذَلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْتَنُونَ ﴿٥٢﴾ أَتَوَصَّوْا بِهِمْ

“Basi ndio hivyo hivyo, hawakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwenda wazimu. Je, Wameambizana kwa haya?” (51:52-53)

Baada ya hapa Allah تعالى Alisema,

قَدْ بَيَّنَّا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٣﴾

“Hakika Sisi Tumeziweka wazi Ishara kwa watu wenye yakini.”

Maana yake: Tumeziweka wazi hoja, Tukithibitisha ukweli wa Manabii, bila kuuliza maswali zaidi au uthibitisho kwa wale wanaoamini, kufuata Manabii na kuzingatia yale Allah تعالى Aliyowatuma kuyafikisha. Ama kwa wale ambao mioyo yao na usikivu wao ulipigwa muhuri na Allah تعالى na ambao macho yao yalifumbwa, Allah تعالى Amewaelezea,

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٤﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ

يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٥٥﴾

“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitisha juu yao, hawataamini, ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.” (10:96-97)

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ۗ وَلَا تُسْئَلُ عَنْ أَصْحَابِ الْجَحِيمِ ﴿٥٦﴾

119. “Hakika Sisi Tumekutuma kwa Haki uwe mbashiri, na Mwonyaji. Na wala hutaulizwa juu ya watu wa Motoni.”

Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تُسْئَلُ عَنْ أَصْحَابِ الْجَحِيمِ ﴿٥٦﴾

“Na wala hutaulizwa juu ya watu wa Motoni.”

Maana yake: “Hatutakuuliza kuhusu kukufuru kwa wale waliokukataa.” Vile vile Allah تعالى Amesema,

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٥٧﴾

“Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hesabu.” (13:40)

Na kama ilivyo Kauli Yake تعالى،

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿١١١﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿١١٢﴾

“Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia.” (88:21-22)

Na kama Kauli Yake Allah تعالى،

لَوْ كُنَّا نَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ ﴿٥٠﴾ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ﴿٥١﴾ فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ ﴿٥٢﴾

“Sisi Tunajua kabisa wasemayo. Wala wewe si mwenye kuwatawalia kwa ujabari. Basi mkumbushe kwa Qur’an anaye liogopa onyo.” (50:45)

Na Aya nyingine nyingi zinazoshabihiana na hizi katika maudhui hii.

Mtume ﷺ Alivyoelezewa Ndani ya Taurati.

Imam Ahmad alimnukuu Ata bin Yassar alisema kuwa alikutana na Abdullah bin Amr bin Al-As na akamuambia,

“Nieleze jinsi Mtume alivyoelezewa ndani ya Taurati.” Akasema, “Naam Wallahi, ameelezewa ndani ya Taurati na sifa bainifu kama alivyoelezewa ndani ya Qur’an: “Ewe Mtume! Tumekutuma kama shahidi, mbashiri wa habari njema, na kimbilio salama kwa watu ummi wasiojua kusoma wala kuandika. Wewe ni mja Wangu na Mjumbe Wangu. Nimekupa jina la Mutawakkil (anayemtegemea Allah تعالى kwa kila kitu). Wewe si mwenye pupa, wala mgumu, wala mwenye kuudhi masokoni. Hulipizi uovu kwa uovu. Bali unasamehe na kuwia radhi. Allah تعالى Hatoichukua roho yako. Mpaka Atakapozinyoosha dini potofu kwa mikono yake mpaka watangaze: Hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah. Kwa mikono yako, Allah Atawafungua vipofu, viziwi na mioyo iliyopigwa muhuri.”¹

Hii imeandikwa na Bukhari peke yake.²



¹ Ahmad 2:174.

² Fat’hul Al-Bari 4:402, 8:449 na Al-Adab Al-Mufrad 72.

وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ۗ
 قُلْ إِنَّ هُدَىٰ اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ ۗ وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ
 بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۗ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا
 نَصِيرٍ ﴿١٢٠﴾ الَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ
 أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَمَن يَكْفُرْ بِهِ ۗ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْخَاسِرُونَ ﴿١٢١﴾ يٰٓبَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِيَ الَّتِي أَنْعَمْتُ
 عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٢٢﴾ وَاتَّقُوا يَوْمًا لَا
 تَجْزِي نَفْسٌ عَن نَّفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنهَا عَدْلٌ وَلَا
 تَنْفَعُهَا شَفَعَةٌ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿١٢٣﴾ * وَإِذِ ابْتَلَىٰ
 إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ
 إِمَامًا ۗ قَالَ وَمِن ذُرِّيَّتِي ۗ قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ
 ﴿١٢٤﴾ وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمَّا وَاتَّخِذُوا مِن
 مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۗ وَعَهِدْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن
 طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ
 ﴿١٢٥﴾ وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَارْزُقْ
 أَهْلَهُ مِن الثَّمَرَاتِ ۗ مَن ءَامَنَ مِنهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ قَالَ
 وَمَن كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۗ

وَيُسَّسَ الْمَصِيرُ ﴿١٢٦﴾

وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا
 النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ۗ قُلْ
 إِنَّ هُدَىٰ اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ ۗ وَلَئِنِ
 اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ
 مِنَ الْعِلْمِ ۗ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِن وَلِيٍّ
 وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٢٠﴾ الَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ
 الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ ۗ أُولَٰئِكَ
 يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَمَن يَكْفُرْ بِهِ
 فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٢١﴾

120. "Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Manasara, mpaka ufuata mila yao. Sema: Hakika uwongofu ni wa Mwenyezi Mungu. Na kama ukifuata matamano yao baada ya ujuzi uliokwisha kujia, hutapata Mlinzi wala msaidizi kwa Mwenyezi Mungu."

121. "Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa, hao ndio kweli wanakiamini. Na wanao kukataa basi hao ndio wenye kupata hasara."

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, "Allah تعالى Amesema",

وَلَنْ نَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودَ وَلَا النَّصْرَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ¹

"Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Wakristo, mpaka ufuate mila yao."

Maana yake: "Mayahudi na Wakristo hawatakupenda, Ewe Muhammad! Kwa hiyo usifanye yanayowaridhisha au kuwafurahisha, na shikamana na yale yanayo mridhisha Allah تعالى kwa kuwalingania kwenye haki aliyokuleta nayo Allah تعالى." Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ إِبْرَاهِيمَ هَدَىٰ اللَّهُ هُوَ الْهُدَىٰ²

"Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu."

Maana yake: "Sema: Ewe Muhammad, uongozi wa Allah تعالى Ambao Alinituma nao ni mwongozo wa kweli. Maana yake uwongofu ulio wazi wa uhakika na dini iliyo kamilifu."¹ Qatadah alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى.

قُلْ إِبْرَاهِيمَ هَدَىٰ اللَّهُ هُوَ الْهُدَىٰ²

"Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu."

Ni, "Hoja ya kweli ambayo Allah تعالى Alimfundisha Muhammad ﷺ na Masahaba zake na ambazo walizitumia dhidi ya watu waliopotoka."² Qatadah alisema, tuliambiwa Mtume ﷺ alikuwa akisema,

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي يُقَاتِلُونَ عَلَى الْحَقِّ ظَاهِرِينَ، لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَالَفَهُمْ حَتَّىٰ يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ»

"Halitaacha kuwepo kundi katika Ummah wangu litalopigania haki, watakuwa washindi na hawatadhuriwa na wapinzani mpaka ije Amri ya Allah (Kiyama)."³

Mimi bin Kathir nimesema: Hadithi hii ilikusanywa katika Sahih na ilisimuliwa na Abdullah bin Amr رضي الله عنه.⁴

¹ At-Tabari 2:562.

² Ibn Abu Hatim 1:356.

³ Ibn Abu Hatim 1:355.

⁴ Muslim 1924.

وَلَيْنِ أَتَّبَعَتْ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١٢٠﴾

“Na kama ukifuata matamanio yao baada ya ujuzi uliokwisha kujia, hutapata Mlinzi wala msaidizi kwa Mwenyezi Mungu.”

Aya hii ina maonyo makali kwa Ummah wa Kiislamu dhidi ya kuiga njia na tabia za Mayahudi na Wakristo, baada ya kuwa na elimu ya Qur’an na Sunnah, Allah تعالی Atukinge kutokana na tabia hii. Japokuwa maneno haya ya Aya hii yalielekezwa kwa Mtume ﷺ, hukumu yake inahusu Ummah wote.

Maana ya Kusoma Kitabu Ipasavyo.

Allah تعالی Amesema,

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ

“Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa.”

Abdur-Razzak alisema kutoka kwa Ma’mar, kutoka kwa Qatadah, “Hao ni Mayahudi na Wakristo.” Haya ni maoni ya Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam, na pia yalichaguliwa na Ibn Jariri رحمه الله تعالی. Said alipokea kutoka kwa Qatadah, “Hao ni masahaba wa Mtume ﷺ.” Abu Al-Aliyah alisema kuwa Ibn Mas-ud رضي الله عنه alisema, “Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko Mikononi Mwake! usomaji sahihi wa Kitabu uliokusudiwa ni kuhalalisha Halali, na kuharamisha Haramu, na kuisoma kama ilivyoteremshwa na Allah تعالی, bila kubadilisha maneno kutoka kwenye sehemu zake, na kutoifasiri tofauti na vile ilivyofasiriwa.”¹ As-Suddi alipokea kutoka kwa Abu Malik kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه ambaye alizungumzia Aya hii (2:121), “Wanahalalisha kile kilichoharamishwa, na wanakataza kile kilichoharamishwa, na hawabadili maneno yake.” Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, “Hawa ni wale wanaposoma Aya inayotaja mateso wanaomba Hifadhi ya Allah تعالی.”² Maana hii ilinasibishwa na Mtume ﷺ, kwani alipokuwa akisoma Aya ya Rehema, alimuomba Allah تعالی Rehema, na aliposoma Aya ya mateso, aliomba Hifadhi ya Allah تعالی.³ Na Kauli Yake Allah تعالی,

¹ At-Tabari 2:567.

² Al-Qurtubi 2:95. Isnadi yake ni dhaifu.

³ Ibn Majah 429.

أُولَئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ^٥

“Hao ndio kweli wanakiamini.”

Inaelezea Aya,

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ

“Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa.”

Aya hizi zina maana: “Miongoni mwa Watu wa Kitabu wako ambao walishikamana na Vitabu vilivyoteremshwa kwa Mitume, wataamini kile Tulichokuteremshia, Ewe Muhammad!” Kama Allah تعالى Alivyosema;

وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أَنْزَلْنَا إِلَيْهِمْ مِنَ الْكِتَابِ لَأَكْلُوا مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ
أَرْجُلِهِمْ^٥

“Na lau kuwa wangeliishika Taurati na Injili na yote waliyo teremshiwa kutokana na Mola wao Mlezi, basi hapana shaka wangalikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao.” (5:66).

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَسْتُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ حَتَّىٰ تُقِيمُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ مِنَ
رَبِّكُمْ^٥

“Sema, Enyi Watu wa Kitabu! Hamna lenu jambo mpaka muishike Taurati na Injili na yote mlioteremshiwa na Mola wenu Mlezi...” (5:68)

Ina maana: “Kama mnafuata Taurati na Injili katika njia sahihi, na mkaiamini ipasavyo, na mkasadikisha habari zinazohusu Utume wa Muhammad ﷺ na wasifu wake. Na amri ya kumfuata yeye pamoja na kumuhami, kufanya hivyo kungewaelekeza nyinyi kushikamana na ukweli, na uadilifu duniani na kesho Akhera.” Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema,

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ
وَالْإِنْجِيلِ

“Ambao wanamfuata huyo Mtume, Nabii asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili.”
(7:157) Na Allah تعالى Amesema:

قُلْ ءَامِنُوا بِهِمْ أَوْ لَا تُوْمِنُوا ۗ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِمْ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ
لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٧٧﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٧٨﴾

“Sema: laminini au msiiamini. Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa hii Qur’an, huanguka kifudi fudi wanasujudu. Na wanasema: Subhana Rabbina, Ametakasika Mola Wetu Mlezi! Hakika Ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe.” (17:107-108)

Aya hizi zinadhiri hisha kwamba alichohidiwa Muhammad ﷺ na Allah تعالى kwa hakika kitatokea. Allah تعالى pia Alisema,

الَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِمْ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿١٧٧﴾ وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَأَمَنَّا
بِهِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿١٧٨﴾ أُولَٰئِكَ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ
بِمَا صَبَرُوا وَيَدْرَءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٧٩﴾

“Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki. Na wanapo somewa wanasema: Tunakiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyeka. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyovumilia, na wakaondoa ubaya kwa wema, na wakatoa katika Tuliowaruzuku.” (28:52-54) Na Allah تعالى Amesema,

وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ ۗ فَإِنْ ءَأَسْلَمْتُمْ فَقَدْ ءَهْتَدُوا ۗ وَإِنْ تَوَلَّوْا
فَإِنَّمَا عَلَيْكُمُ الْبَلَاغُ ۗ وَاللَّهُ بِصِرِّ الْعِبَادِ لَبِيبٌ ﴿١٧٩﴾

“Na waambie waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja Wake.” (3:20)

Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٢٠﴾

“Na wanaokukataa basi hao ndio wenye kuhasiri.”

Kama Alivyosema katika Aya nyengine,

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالِنَارُ مَوْعِدُهُ ۗ

“Na anayemkataa katika makundi, basi moto ndio pahala pa miadi yao.” (11:17)

Kama alivyonukuliwa katika Sahih, Mtume ﷺ alisema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ يَهُودِيٍّ وَلَا نَصْرَانِيٍّ ثُمَّ لَا يُؤْمِنُ بِي إِلَّا دَخَلَ النَّارَ»

“Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko Mikononi Mwake! Hapana mja katika Ummah huu (binadamu na Majini) Myahudi au Mkristo, ambaye atanisikia halafu asiniamini, ila ataingia Motoni.”¹

يَدِينِي إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٢١﴾
وَأَتَّقُوا يَوْمًا لَا تَجْزَى نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا تَنْفَعُهَا شَفْعَةٌ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿١٢٢﴾

122. “Enyi Wana wa Israil! Kumbukeni neema Yangu Niliyo kuneemesheni, na hakika Mimi Nikakufadhilisheni kuliko wengineo wote.”

123. “Na iogopeni siku ambayo hatamfaa mtu mwenziwe kwa lolote, wala hakitakubaliwa kwake kikomboleo, wala maombezi hayatamfaa, wala hawatanusuriwa.”

¹ Muslim 1:134.

Tumetaja Aya inayofanana na hii mwanzo wa Surah hii, na imerudiwa tena kutajwa hapa kuisitiza umuhimu wa kumfuata Mtume na Nabii ambaye hajui kusoma wala kuandika kikasomwa - *Ummi*, ambaye ameelezewa sifa zake katika Vitabu vyao kwa ubainifu. Hadi jina lake pamoja na habari njema zinazomhusu yeye pamoja na Ummah wake. Allah تعالی Aliwaonya kuhusu kuficha taarifa hizi, ambazo ni fadhila walizopewa na Allah تعالی. Aidha Allah تعالی Aliwaamuru wayakumbuke maisha yao ya kila siku na mambo yao ya kidini na namna Alivyowabariki. Wasiwaonee inda wapwa zao, Waarabu, kwa yale waliyozukikiwa na Allah تعالی, Mtume wa mwisho akiwa Mwarabu. Inda haitakiwi kuwashawishi kumpinga au kumkanusha Mtume au kujizuia kumfuata, Rehema na Amani za Allah تعالی ziwe juu yake mpaka siku ya Hukumu.

﴿ وَإِذْ أَبْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۗ قَالَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي ۗ قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴿١٢٤﴾ ﴾

124. "Na (Kumbuka) Mola wako Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa kumpa amri fulani, naye akatimiza, Akamuambia: Hakika Mimi Nitakufanya uwe Kiongozi wa watu. Akasema: Je, na katika vizazi vyangu pia? Akasema: Ahadi Yangu haitawafikia wenye kudhulumu".

Ibrahim Al-Khalil عليه السلام Kipenzi cha Allah تعالی na Kumfanya Kiongozi kwa Watu.

Allah تعالی Anatufahamisha juu ya heshima ya Ibrahim Al-Khalil عليه السلام, mwandani Wake, ambaye Alimfanya kiongozi wa watu, na mfano wa kuigwa kwa sababu ya mwenendo wake mzuri. Na alishikamana na *Tawhid* yaani kumfanya Allah تعالی kuwa ni Mmoja tu. Mtume Ibrahim عليه السلام alipewa heshima hii baada ya kushikamana na maamrishi na makatazo ya Allah تعالی.

Hii ndio sababu Allah تعالی Akasema,

﴿ وَإِذْ أَبْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ ۗ ﴾

"Na (kumbuka) Mola wako Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa Kumpa amri fulani."

Aya hii ina maana, "Ewe Muhammad! Wakumbushe washirikina na Watu wa Kitabu, ambao wanajidai kuwa wafuasi wa Dini ya Ibrahim عليه السلام, wakati kwa hakika hawaifuati, wakati wewe, Ewe Muhammad, na wafuasi wako ndio wafuasi wa kweli wa Dini yake; Wakumbushe amri na makatazo ambayo kwayo Allah تعالى Alimjaribu Ibrahim عليه السلام."

فَاتَّمَّهُنَّ

"Akatimiza."

Inaonesha kuwa Ibrahim عليه السلام alitekeleza Amri zote za Allah تعالى. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿٣٧﴾

"Na Ibrahim aliyetimiza ahadi?" (53:37).

Ina maana, alikuwa mkweli na mtiifu kwa Amri za Allah تعالى. Aidha Allah تعالى Alisema,

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٣٧﴾ شَاكِرًا لِأَنْعُمِهِ
 أَجْتَبَهُ وَهَدَنَاهُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٣٨﴾ وَءَاتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿٣٩﴾ ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ
 الْمُشْرِكِينَ ﴿٤٠﴾

"Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, Mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa Washirikina. Mwenye kuzishukuru Neema Zake, Mwenyezi Mungu. Yeye Kamteua, na Akamuongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka. Na Tukampa wema duniani, na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema. Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa Washirikina."
 (16:120-123)

Aidha Allah تعالى Amesema,

قُلْ إِنِّي هَدَيْتَنِي رَبِّيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قَدِيمًا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنْ

الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

“Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi Ameniongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliyekuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa Washirikina.” (6:161)

Na Allah تعالى Amesema,

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

﴿١٦١﴾ إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَاللَّهُ وَلِيُّ

الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٢﴾

“Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika Washirikina. Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata yeye na Nabii huyu na walioamini. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa Waumini.” (3:67-68)

بِكَلِمَةٍ

“Amri fulani”

Ambayo ina Maana: Sharia, Maamrisho na Makatazo. “Kalimat” Kama lilivyotumiwa hapa, wakati mwingine lina maana Atakayo Allah تعالى, yaani Utashi wa Uwezo Wake wa kimataifa. Na Kauli ya Allah تعالى juu ya Maryam,

وَصَدَقَتْ بِكَلِمَتِ رَبِّهَا وَكُتِبَ عَلَيْهَا مِنَ الْقَنَاتِينِ ﴿١٦٣﴾

“Na Akayasadiki maneno ya Mola Wake Mlezi na Vitabu Vyake, na alikuwa miongoni mwa Watiifu.” (66:12)

“Kalimat” pia ina maana ya Sharia za Allah تعالى, katika Kauli ya Allah تعالى,

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ﴿١٦٤﴾

“Na yametimia Maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli, au Amri adilifu.” (6:115)

Maana yake: Maneno Yake ya kisheria ambayo ima yanaelezea Habari ya kweli au yana lengo la kuutafuta uadilifu ikiwa ni Amri au Makatazo. Kama ambavyo imekuja katika Aya hii Tukufu,

﴿ وَإِذْ أَبْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ ﴾

“Na (Kumbuka) Mola wake Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa Kumpa Amri fulani, naye akatimiza...”

Maana yake: Aliyashika mafundisho hayo. Allah تعالى Amesema,

﴿ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۗ ﴾

“Hakika Mimi Nitakufanya uwe Kiongozi wa watu.”

Kama malipo kwa matendo mema ya Ibrahim عليه السلام, alishikamana na maamrisha na kuepukana na makatazo. Hii ndio sababu Allah تعالى Alimfanya Ibrahim عليه السلام mfano kwa watu, na kiongozi ambaye mwenendo wake na njia yake vinaigwa na kufuatwa.

Ibrahim عليه السلام Alijaribiwa kwa Maneno Yapi?

Kuna tofauti ya rai kuhusu Maneno ambayo Allah تعالى Alimjaribu nayo Ibrahim عليه السلام. Kuna maoni mengi yanayohusishwa na kauli hii, na Ibn Abbas alisema, “Allah تعالى Alimjaribu na *ibadat* (za Hajj).”¹ Abu Is-haq aliandika sawa na hivyo.² Abdur-Razzaq pia alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

﴿ وَإِذْ أَبْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ ۗ ﴾

“Na (kumbuka) Mola Wake Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa Kumpa Amri fulani.”

Ina maana: Alimjaribu na *Twaharah* (usafi, udhu): Vitano juu ya kichwa na vitano katika mwili. Ama kichwa, ni kupunguza masharubu, kusukutua kinywa, kuingiza na kutoa maji puani, kupiga mswaki na kuchana nywele. Ama katika mwili, ni kukata kucha, kunyoa nywele za kinena, kutahiri, kung’oa nywele za makwapa na kustanji kwa maji baada ya kujisaidia.³ Ibn Hatim alisema, “Kauli sawa na hii iliripotiwa kutoka kwa Said bin Al-Musayyib, Mujahid, Ash-Shabi,

¹ At-Tabari 3:13.

² At-Tabari 3:13.

³ Abdur-Razzaq 1:57.

An-Nakhai, Abu Salih, Abu Al-Jald na kadhalika.¹ Kuna kauli inayolingana na hiyo ambayo Imam Muslim anasema ilisimuliwa kutoka kwa Aishah رضي الله عنها ambaye alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«عَشْرٌ مِنَ الْفِطْرَةِ: قَصُّ الشَّارِبِ وَإِعْتَاءُ اللَّحِيَةِ وَالسَّوَاكُ وَاسْتِنْسَاقُ الْمَاءِ وَقَصُّ الْأَظْفَارِ وَغَسْلُ الْبَرَاجِمِ وَتَنْفُ الْإِبْطِ وَحَلَقُ الْعَانَةِ وَاتِّقَاصُ الْمَاءِ وَنَسِيبُ الْعَاشِرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ الْمُضْمَضَةَ»

“Kumi ni miongoni mwa Fitrah: Kupunguza masharubu, kufuga ndevu, kupiga mswaki, kutia na kutoa maji puani (katika udhu), kukata kucha, kuosha kati ya vidole, kung’oa nywele za kwapa, kunyoya nywele za kinena, kunawa kwa maji baada ya kwenda haja, (nimesahau cha kumi; Nadhani ilikuwa) kusukutua kinywa (katika udhu).”²

Sahihi mbili zimeandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْفِطْرَةُ حَمْسٌ: الْخِتَانُ وَالْأَسْتِحْدَادُ وَقَصُّ الشَّارِبِ وَتَقْلِيمُ الْأَظْفَارِ وَتَنْفُ الْإِبْطِ»

“Vitano ni miongoni mwa Fitrah: Kutahiri, kunyoya nywele za kinena kupunguza masharubu, kukata kucha na kung’oa nywele za makwapa.” Haya ni maneno ya Muslim.³

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maneno ambayo Allah تعالى Alimjaribu nayo Ibrahim السلام عليه na akayatekeleza yalikuwa, ni kuwatelekeza watu wake (waliokufuru) Allah تعالى Alipomuamrisha kufanya hivyo; kumlingania Nimrodh (Mfalme wa Babeli) kuhusu Allah تعالى; subira aliyokuwa nayo alipotupwa ndani ya moto (japokuwa hili lilikuwa linatia kiwewe); kuhama kutoka kwao wakati Allah تعالى Alipomuamrisha kufanya hivyo; kusubiri juu ya matarajio ya kifedha na vitu; ya kuwakarimu wageni kwa Amri ya Allah تعالى, na Amri ya Allah تعالى kuwa Amchinje mtoto wake.” Allah تعالى Alipomjaribu Ibrahim السلام عليه na maneno haya, naye alikuwa tayari kwa Mtihani mkubwa. Allah تعالى Akamuambia,

¹ Ibn Abu Hatim 1:359.

² Muslim 1:223.

³ Fat’hul Al-Bari 10:347 na Muslim 1:222.

أَسْلِمَ ۖ قَالَ أَسَلَّمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢٠﴾

“Silimu, Nyenyekaa! Akajibu, ‘Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.” (2:131)

Japokuwa hii ilikuwa na maana ya kuwapinga na kuachana na watu wake.¹

Madhalimu Hawatapata Ahadi ya Allah تعالى.

Allah تعالى Amesema kuwa Ibrahim عليه السلام alisema,

وَمِنْ ذُرِّيَّتِي ۖ

“Je, na katika vizazi Vyangu pia?”

Na Allah تعالى Akamjibu,

لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴿١٢١﴾

“Ahadi Yangu haitawafikia wenye kudhulumu.”

Allah تعالى Alipomfanya Ibrahim عليه السلام Imam (kiongozi wa Watiifu), akamuomba Allah تعالى kuwa Maimamu baada yake wachaguliwe kutokana na kizazi chake. Allah تعالى Aliridhia ombi lake, lakini Alimuambia kuwa watakuwepo watu madhalimu miongoni mwa vizazi na hawatanufaika na Ahadi ya Allah تعالى. Hivyo, hawatakuwa Maimamu wala hawatakuwa kiigizo (kwani hawatakuwa Waadilifu). Ushahidi kuwa dua ya Ibrahim عليه السلام ilikubaliwa na Allah تعالى ni Maneno ya Allah تعالى katika Surat Al-Ankabut (29:27)

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuriya yake - Unabii na Kitabu.”

Hivyo, kila Mtume aliyepelikwa na Allah تعالى baada ya Ibrahim عليه السلام walikuwa miongoni mwa kizazi chake, na kila Kitabu Alichokiteremsha Allah تعالى kiliteremshwa kwao. Kama Kauli ya Allah تعالى isemavyo. Na Ama Kauli Yake Allah تعالى,

¹ Ibn Abu Hatim 1:360. Isnadi yake ni dhaifu.

قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴿١٢٠﴾

“Akasema: Ahadi Yangu haitawafikia wenye kudhulumu.”

Allah تعالی Alitaja kuwa kuna watu madhalimu miongoni mwa kizazi cha Ibrahim عليه السلام, hao hawatanufaika na Ahadi ya Allah تعالی, wala hawatapewa dhamana yoyote, japokuwa ni miongoni mwa watoto wa Khalil wa Allah تعالی (mwandani, Nabii Ibrahim عليه السلام). Watakuwepo wale wanaofanya mema miongoni mwa Watoto wa Ibrahim عليه السلام, na hao ndio watakaonufaika na dua ya Ibrahim عليه السلام. Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema Aya hii inaonesha kuwa madhalimu hawatakuwa Maimamu wa watu. Pamoja na hayo, Aya ilimfahamisha Ibrahim عليه السلام kuwa watakuwepo watu waliozidhulumu nafsi zao miongoni mwa kizazi chake. Pia, Ibn Khuways Min-dad Al-Maliki alisema, “Mtu dhalimu hafai kuwa Khalifah, Mtawala, mtu anayetoa Fatawa, shahidi au mpokezi wa Hadithi.”

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى وَعَهِدْنَا إِلَىٰ

إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿١٢١﴾

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِن الثَّمَرَاتِ مَن ءَامَنَ مِنهُمْ

بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ قَالَ وَمَن كَفَرَ فَأُمْتِعْهُ قَلِيلًا ۖ ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۗ وَبِئْسَ

الْمَصِيرُ ﴿١٢٢﴾

“Na kumbukeni Tulipoifanya ile Nyumba (ya Al-Ka’aba) iwe pahala pa kukusanyika watu na pahala pa amani. Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia. Na Tuliagana na Ibrahim na Ismail: Itakaseni Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu na wanao jitenga huko kawa ibada, na wamo wanao inama na kusujudu. Na alipo sema Ibrahim: Ee Mola Wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea. ” (2:125-126)

Utakatifu wa Nyumba ya Allah تعالى.

Al-Awfi aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى,

وَأَذِّجَعَلْنَا أَلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ

“Na kumbukeni Tulipoifanya ile Nyumba (ya Al-Ka’aba) iwe pahala pa kukusanyika watu.”

“Hawabakii katika Nyumba hiyo, huizuru na kisha kurejea majumbani kwao, na kisha huizuru tena.” Pia Abu Ja’far Ar-Razi رحمه الله تعالى alisimulia baada ya kupokea kutoka kwa Ar-Rabi bin Anas kutoka kwa Al-Aliyah ambaye alisema kuwa,

وَأَذِّجَعَلْنَا أَلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمَّنَّا

“Na kumbukeni Tulipoifanya ile Nyumba (ya Al-Ka’aba) iwe pahala pa kukusanyika watu na pahala pa amani.”

Ina maana: Kusalimika na maadui na mapigano ya kutumia silaha. Katika zama za Jahiliya, watu walikuwa waathirika wa uvamizi na utekaji nyara, wakati watu waliokuwa pambizoni mwa *Al-Masjid Al-Haram* walikuwa salama na hawakuwa hatarini kutekwa nyara.¹ Aidha Mujahid, Ata, As-Suddi, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas waliripotiwa kuwa walisema Aya (2:125) hii maana yake, “Yeyote atakayeingia atakuwa salama.”² Aya hii inaonesha kuwa Allah تعالى Aliitukuza Nyumba Takatifu, ambayo Aliifanya makimbilio salama na mapumziko salama. Kwa hiyo, nyoyo zinakuwa na hamu na hazichoshwi, kuzuru Nyumba Tukufu, japo kila mwaka. Hii ni kwa sababu Allah تعالى Aliipokea dua ya *Khalil* wake, Ibrahim عليه السلام, wakati alipomuomba kufanya nyoyo za watu kuwa na hamu ya kuzuru Nyumba Tukufu. Ibrahim عليه السلام alisema, hadi kauli yake,

رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ

“Ewe Mola Wetu Mlezi, na ipokee dua yangu.” (14:40)

Allah تعالى Aliieleza Nyumba kama makimbilio na makazi salama, kwa wale wanaoizuru wako salama, hata kama waliwahi kufanya vitendo viovu. Heshima

¹ At-Tabari 3:29.

² Ibn Abu Hatim 1:370.

hii inatokana na heshima ya mtu aliyejenga mwanzo, *Khalil Ar-Rahman*, kama Allah تعالى Alivyosema,

وَأَذِّبُوا نَارًا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَنْ لَا تُشْرِكَ بِي شَيْئًا

“Na pale Tulipomueka Ibrahim pahala penye ile Nyumba Tukamuambia: Usinishirikishe na chochote.” (22:26)

Na Allah تعالى Amesema,

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٢٥﴾ فِيهِ ءَايَاتٌ بَيِّنَاتٌ مَّقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ ءَامِنًا ۗ

“Hakika Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu kufanya ibada ni ile iliyoko Bakka, iliyobarikiwa na yenye uwongofu kwa walimwengu wote. Ndani yake zipo ishara zilizo wazi – masimamo ya Ibrahim na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani.” (3:96-97)

Aya Tukufu ya mwisho imesitiza heshima ya *Maqam Ibrahim* عليه السلام na maelekezo ya kusali pambizoni mwake,

وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”

Maqam Ibrahim.

Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى aliripoti kuwa Said bin Jubayr alitolea Aya hii maelezo,

وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى ۖ

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”

“Jive la *Maqam* ni mahali alipokuwa akisimama Ibrahim عليه السلام. Mahali hapo Allah تعالى Amepafanya kuwa ni rehema. Ibrahim عليه السلام Alisimama juu ya jiwe hilo huku mwanawe Ismail عليه السلام akimpa mawe (ya kujenga Ka’abah).¹

¹ Ibn Abu Hatim 1:371.

As-Suddi alisema, “Maqam Ibrahim عليه السلام ni jiwe ambalo mke wa Ismail عليه السلام aliliweka chini ya nyayo za Ibrahim عليه السلام alipokuwa akiosha kichwa chake.”¹ Al-Qurtubi رحمه الله تعالى aliitaja rai hii, lakini alichukulia kuwa sio sahihi, japo wengine waliipa umuhimu. Ar-Razi aliripoti katika Tafsir yake kutoka kwa al-Hasan Al-Basri, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas.² Ibn Abu Hatim aliripoti kutoka kwa Jabir, akielezea Hijja ya Mtume ﷺ, “Wakati Mtume ﷺ akitufu, Umar رضي الله عنه alimuuliza, “Haya ndio Maqam ya baba yetu?” Alijibu, “Ndiyo.” Umar رضي الله عنه alisema, “Tupafanye pahala pa kusali?” Hivyo Allah تعالى Aliteremsha Aya,

وَأَتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّىً

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”⁴

Bukhari alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى isemayo,

وَأَتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّىً

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”

Maana yake: Wanarudi mara kwa mara. Kisha alisimulia kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, “Nilikubaliana na Mola Wangu, au Mola Wangu Aliniwafikisha mimi, kuhusu masuala matatu. Nikasema, “Ewe Mtume! Nataraji upafanye Maqam Ibrahim mahali pa kusalia.” Aya,

وَأَتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّىً

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”

Iliteremshwa. Pia Nilisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Watu wema na waovu wanaingia nyumbani kwako. Nataraji utawaamrisha Mama wa Waumini (Wakeze Mtume ﷺ) kuvaa Hijab. Allah تعالى Alishusha Ayah iliyotaka ivaliwe Hijab. Na nilipojua ya kuwa Mtume ﷺ aliwakasirikia wakeze, niliwaenda na kuwaambia, “Ama muache mnayoyafanya, au Allah تعالى Atambadilishia Mtume Wake ﷺ, wake bora kuliko nyie.” Nilimshauri mmoja wa wakeze na akaniambia, “Ewe Umar! Hivi Mtume ﷺ hajui kuwashauri wakeze, mpaka wewe ufanye kazi hiyo badala yake?” Kisha Allah تعالى Akateremsha,

¹ At-Tabari 3:35.

² Ar-Razi 4:45.

³ Ibn Abu Hatim 1:370.

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّنْكَنَّ مَسَامِنٍ

“Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, Akampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi, wanyenyekevu.”
(66:5)

Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Jabir رضي الله عنه alisema, “Baada ya Mjumbe wa Allah kulibusu Jiwe Jeusi, aliizunguka Al-Kaaba mara tatu kwa mwendo wa haraka na mara nne kwa mwendo wa pole pole. Kisha akaenda Maqam Ibrahim akasoma:

وَأَتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”
(2:125)

Kisha akaiweka “Maqaam” kati yake na Nyumba (Al-Ka’aba) na akasali Rakaa mbili.¹ Hii ni sehemu ya Hadithi ndefu ambayo imeandikwa katika Sahih Muslim.² Al-Bukhari aliandika kuwa Amr bin Dinar alisema kuwa alimsikia Ibn Umar رضي الله عنهما akisema, “Mtume ﷺ alitufu kuizunguka Al-Kaaba mara saba na kisha akasali Rakaa mbili nyuma ya Maqam.”³

Maandiko yote yanaonesha kuwa Maqam ni jiwe ambalo Ibrahim عليه السلام alikuwa akisimamia wakati akijenga Ka’aba. Kuta za Ka’aba zilipokuwa juu, Ismail عليه السلام alimpa baba yake mawe ili asimame juu yake, na ampatie yeye mawe. Ibrahim عليه السلام aliyaweka mawe hayo juu ya ukuta ili apate kuuinua, na alipomaliza upande mmoja, alikwenda upande mwingine mpaka kukamilisha mzunguko wa jengo. Ibrahim عليه السلام aliendelea na utaratibu huu mpaka alipomaliza kujenga Ka’aba, kama tutakavyoeleza kisa cha Ibrahim عليه السلام na Mwanawe Ismail عليه السلام na jinsi walivyojenga Al-Kaaba (Nyumba ya Allah Takatifu), kama ilivyosimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na kukusanywa na Al-Bukhari. Nyayo za Ibrahim عليه السلام zilikuwa zinaonekana kwenye jiwe na Waarabu walijua ukweli huu wakati wa Jahiliyyah. Hii ndio sababu Abu Talib alisema katika shairi lake linaloitwa Al-Lamiyyah; “Na nyayo za Ibrahim akiwa miguu mitupu zinaonekana juu ya jiwe.”

¹ At-Tabari 3:36.

² Muslim 2:920.

³ Fat’hul Al-Bari 3:586.

Waislamu pia waliona nyayo juu ya jiwe, kama Anas bin Malik رضي الله عنه alivyosema, “Niliiona Maqam ikiwa na alama za vidole na mguu wa Ibrahim, lakini alama hizo zilitoweka kwa sababu watu walikuwa wakipangusa jiwe kwa mikono yao.” Mimi bin Kathir nimesema: Siku za mwanzo, Maqam iliwekwa karibu na ukuta wa Ka’aba. Katika zama zetu, Maqam imewekwa baada ya Al-Hijr, upande wa kulia kwa wale wanaoingilia mlangoni katika eneo la wazi.¹ Ibrahim عليه السلام alipomaliza kujenga Nyumba, aliweka jiwe baada ya ukuta wa Ka’aba. Au, Al-Kaaba ilipomalizika kujengwa, Ibrahim عليه السلام aliliacha jiwe lilipokuwa limesimama. Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi, imeamrisha kusali sunna pembeni ya jiwe wakati mtu anapomaliza Tawaf. Ilifaa Maqam ya Ibrahim عليه السلام iwe pale ujenzi wa Ka’aba ulipoishia. Amir Al-Muuminin, Umar Al-Khattab رضي الله عنه, mmoja wa Makhalfi Wanne Waongofu, ambao tuliamrisha kuwaiga, alilisogeza jiwe hilo kutoka ukuta wa Ka’aba wakati wa uongozi wake. Umar رضي الله عنه ni mmoja wa watu wawili ambao Mtume ﷺ aliwaeleza aliposema,

«اقتدوا بالَّذِينَ مِنْ بَعْدِي أَبِي بَكْرٍ وَعُمَرَ»

“Waigeni watu wawili watakaokuja baada yangu: Abubakar na Umar.”²

Qur’an inakubaliana na Umar رضي الله عنه kuhusu kusali karibu na Maqam Ibrahim عليه السلام. Hii ndiyo sababu hapana miongoni mwa Masahaba aliyepinga kuhamishwa kwake. Abdur-Razzaq alipokea kutoka kwa Ibn Jurayj kutoka kwa Ata na watu wengine, amesema, “Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alikuwa wa mwanzo kuisogeza nyuma Maqam.”⁴ Pia Abdur-Razzaq alisimulia kutoka kwa Mujahid alisema ‘Umar رضي الله عنه alikuwa mtu wa kwanza aliyesogeza nyuma pahala lilipo sasa.” Al-Hafiz Abu Bakar, Ahmad bin Al-Husayn Al-Bayhaqi aliandika Aishah رضي الله عنها, “Enzi za Mjumbe wa Allah na Abubakar, Maqam ilikuwa jirani sana na Nyumba Tukufu (Al-Kaaba), Umar akaisogeza kutoka mahali pake wakati wa Utawala wake.” Hadithi hii ina isnadi sahihi ya upokezi.

¹ Katika eneo hilo iliondolewa, na kuwekwa katika nguzo ya kioo inayoonekana.

² At-Tirmidhi (3662).

³ Al-Musannafu (8955) 5:48.

⁴ Al-Musannafu (8953) 5:47-48.

Amri ya Kusafisha Al-Ka'abah Nyumba ya Allah تعالى.

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema kuwa,

وَعَهْدَنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ

“Na Tuliagana na Ibrahim na Ismail”.

Ina maana: “Allah تعالى Aliwaamuru waitakase na uchafu na najisi na baada ya hapo si ruhusa kuisibu kwa uchafu wowote.”¹

Aidha, Ibn Jurayj alisema, “Nilimuuliza Ata, Nini Ahadi ya Allah تعالى?” Alisema, “Maamrishi Yake.” Pia, Said bin Jubayr alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo Aya,

أَنْ طَهَّرَا بَيْتِي لِلطَّائِفِينَ وَالْعَاكِفِينَ

“Itakaseni Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu na wanaojitenga huko kwa Ibada.”

“Itakaseni kutokana na masanamu.” Zaidi, Mujahid na Said bin Jubayr alisema kuwa,

أَنْ طَهَّرَا بَيْتِي لِلطَّائِفِينَ

“Itakaseni Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu.”

Maana yake: “Kutokana na masanamu, mambo ya ngono, ushahidi wa uongo na madhambi ya kila aina.”

Allah تعالى Amesema,

لِلطَّائِفِينَ

“Kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu.”

Tawafkatika kuizunguka Al-Kaaba ni ibada kongwe. Said bin Jubayr amesema, katika ufafanuzi wa Kauli hii,

لِلطَّائِفِينَ

“Kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu.”

¹ Ibn Abu Hatim 1:373.

Ina maana: Wageni (watu wasioishi Makkah), wakati,¹

وَالْعَكْفِينَ

“Na wanajitenga huko kwa Ibada (Itikafu).”

Ni juu ya wale wanaoishi katika eneo la Nyumba Tukufu. Aidha, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas alisema kuwa *Itkaf* inawahusu wale wanaoishi katika eneo la Nyumba Tukufu, kama Said bin Jubayr alivyosema.² Allah تعالى Amesema,

وَالرُّكْعَ السُّجُودِ

“Na wanaoinama na kusujudu.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, inapokuwa ni mahali pa Sala inawahusisha wale walioelezwa kuwa wanainama na kusujudu.³ Pia, Ataa na Qatadah walitoa Tafsir hiyo.⁴ Aya hii inataka Misikiti yote ipewe hadhi yake ya kuwa sehemu takatifu.

Na pia Kauli hii ya Allah تعالى,

فِي بُيُوتٍ أُذِنَ لِلَّهِ أَنْ تَرْفَعَ وَيُذْكَرَ فِيهَا أَسْمُهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿٣٦﴾

“Katika Nyumba ambazo Mwenyezi Mungu Ameamrisha zitukuzwe, na humo litajwe Jina Lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni.” (24:36)

Kuna Hadithi nyingi zinazotoa amri ya jumla ya kuitakasa Misikiti na kuiweka mbali na uchafu. Hii ndio sababu Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّمَا بُنِيَ الْمَسَاجِدُ لِمَا بُنِيَ لَهُ»

“Misikiti imejengwa kwa madhumuni iliyojengewa (kumuabudu Allah Peke Yake).”⁵

Nimeandika kitabu juu ya somo hili, shukrani zote zinamstahikia Allah تعالى.

¹ Ibn Abu Hatim 1:375.

² Ibid 1:375.

³ Ibn Abu Hatim 1:376.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:376.

⁵ Muslim 1:397.

Makkah ni Mahali Patakatifu.

Allah تعالى Amesema,

وَأَذَّ قَالَ إِبْرَاهِيمَ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنْ الثَّمَرَاتِ مَنْ آمَنَ مِنْهُمْ
بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ^ط

“Na aliposema Ibrahim: Ee Mola Wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na Uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Imam Abu Ja'far bin Jariri At-Tabari رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Jabir bin Abdullah عنه رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ إِبْرَاهِيمَ حَرَّمَ بَيْتَ اللَّهِ وَأَمْنَهُ وَإِنِّي حَرَّمْتُ الْمَدِينَةَ مَا بَيْنَ لَابَتَيْهَا، فَلَا يُصَادُ صَيْدُهَا وَلَا يُقَطَعُ عِضَاهُهَا»

“Ibrahim aliifanya Nyumba ya Allah ni Eneo Takatifu na makimbilio salama. Nami nimezifanya pande mbili za Madinah kuwa Eneo Takatifu. Kwa hiyo, wanyama wake wasiwindwe na miti yake isikatwe.”¹

An-Nasai² na Muslim³, waliandika Hadithi hii. Kuna Hadithi inaonesha kuwa Allah تعالى Aliifanya Makkah sehemu Takatifu kabla ya Kuumba Mbingu na Ardhi. Sahihi mbili zilimnukuu Abdullah bin Abbas عنهما رضي الله عنهما akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ هَذَا الْبَلَدَ حَرَّمَهُ اللَّهُ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَإِنَّهُ لَمْ يَجَلَّ الْقِتَالُ فِيهِ لِأَحَدٍ قَبْلِي وَلَمْ يَجَلَّ لِي إِلَّا سَاعَةً مِنْ نَهَارٍ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا يُعْضَدُ شَوْكُهُ وَلَا يُتَفَرَّقُ صَيْدُهُ، وَلَا يُلْتَقَطُ لِقَطْعَتِهِ إِلَّا مَنْ عَرَفَهَا وَلَا يُخْتَلَى خَلَاهَا» فَقَالَ الْعَبَّاسُ: «يَا رَسُولَ اللَّهِ: إِلَّا الْإِدْخِرَ فَإِنَّهُ لِعَيْنَيْهِمْ وَلِيُسْرَتِهِمْ فَقَالَ: «إِلَّا الْإِدْخِرَ»

“Hakika Allah Aliufanya mji huu mahali patakatifu siku Alipoumba mbingu na ardhi. Kwa hiyo ni mahali patakatifu mpaka siku ya Kiyama kwa sababu Allah Aliifanya Takatifu. Iliharamishwa kwa mtu yeyote kupigana humo, kabla ya kuletwa kwangu na iliruhusiwa

¹ At-Tabari 3:48.

² An-Nasai katika Al-Kubra 2:487.

³ Muslim 2:992.

kwangu kwa saa chache katika siku moja. Kwa hiyo ni eneo Takatifu. Hapana anayeruhusiwa kung'oa vichaka vya miba, au kusaka wanyama, au kuokota kitu kilichoanguka, ila kitangazwe Hadharani, wala miti yake isikatwe." Al-Abbas رضي الله عنه alisema, "Ewe Mtume! Isipokuwa Al-Idhkhir, kwa ajili ya masonara wetu na kwa makaburi yetu." Mtume ﷺ akaongeza, "Isipokuwa Al-Idhkhir."¹

Hii ni kwa mujibu wa maandishi ya Muslim. Sahih mbili pia zilimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه akisimulia Hadith sawa na hii, ambapo Al-Bukhari alinukuu Hadithi sawa na hii kutoka kwa Safiyah bint Shaybah رضي الله عنها aliyesimulia kutoka kwa Mtume ﷺ.²

Abu Shurayh Al-Adawi alisema kuwa alimuambia Amr bin Said alipokuwa akipeleka majeshi Makkah, "Ewe Kamanda! Niruhusu nisimulie Hadith ambayo Mtume ﷺ alisema siku iliyofuata ya Fat-hu Makkah. Masikio yangu yalisikia Hadith, moyo wangu uliizingatia, na macho yangu yalimuona Mtume alipokuwa akisema. Alimshukuru na akamsifu Allah kisha akasema,

«إِنَّ مَكَّةَ حَرَّمَهَا اللَّهُ وَلَمْ يُحَرِّمْهَا النَّاسُ فَلَا يَجُزُّ لِأَمْرِي لِيُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
أَنْ يَسْفِكَ بِهَا دَمًا وَلَا يَغْضِدَ بِهَا شَجَرَةً، فَإِنْ أَحَدٌ تَرَخَّصَ بِقِتَالِ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ
فَقُولُوا: إِنَّ اللَّهَ أَذِنَ لِرَسُولِهِ وَلَمْ يَأْذَنْ لَكُمْ، وَإِنَّمَا أَذِنَ لِي فِيهَا سَاعَةً مِنْ نَهَارٍ وَقَدْ
عَادَتْ حُرْمَتُهَا الْيَوْمَ كَحُرْمَتِهَا بِالْأَمْسِ فَلْيُبَلِّغِ الشَّاهِدَ الْغَائِبَ»

"Hakika Makkah haikutukuzwa na watu bali Allah, hivyo mtu yeyote anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho, hatakiwi kumwaga damu wala kukata miti. Endapo mtu atatoa hoja kuwa inaruhusiwa kupigana kwa kigezo kuwa Mjumbe wa Allah alipigana ndani ya Makkah, mjibu, "Allah Alimruhusu Mjumbe Wake na hajakuruhusu wewe." Allah Alimruhusu kwa saa chache siku ile ya 'Fat-hu', na leo utukufu wake bado upo kama ilivyokuwa kabla. Hivyo, wale waliopo wanapaswa kuwaeleza wasiokuwepo (kuhusu ukweli huu)."

Abu Shurayh aliulizwa, "Amr alijibu nini?" Akasema, (Amr akasema), "Ewe Abu Shurayh! Mimi najua zaidi kuliko wewe kuhusu hili, Nyumba Takatifu haimpi

¹ Fat'hul Al-Bari 4:56 na Muslim 2:986.

² Fat'hul Al-Bari 3:253.

hifadhi muovu, muuaji au mwizi.” Hadithi hii ilikusanywa na Al-Bukhari na Muslim.¹ Na hii ni lafudhi yake. Baada ya maelezo haya hakuna mgongano kati ya Hadithi zinazosema kuwa Allah تعالی Aliifanya Makkah kuwa mahali Patakatifu tokea Alipoumba mbingu na ardhi, na Hadithi zinazosema kuwa Ibrahim عليه السلام aliifanya Takatifu, kwa kuwa Ibrahim عليه السلام alifikisha Amri ya Allah تعالی kuwa Makkah ni mahali Patakatifu kabla ya kujenga Ka’aba. Vile vile, Mtume ﷺ aliandikwa kuwa Mtume wa Mwisho wakati Adam عليه السلام bado alikuwa katika hali ya udongo. Na kwa kuzingatia hilo Ibrahim عليه السلام alisema,

رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ

“Ewe Mola Mlezi Wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao.”
(2:129)

Allah تعالی Aliijibu dua ya Ibrahim عليه السلام, japokuwa alikuwa Anafahamu kabla ya kuwa itatokea kwa Amri Yake (Allah تعالی). Ili kufafanua zaidi somo hili tutataja Hadithi ambayo Mjumbe wa Allah ﷺ alijibu baada ya kuulizwa, “Ewe Mjumbe wa Allah! Tueleze ulivyoanza utume wako.” Mtume ﷺ akasema,

«دَعْوَةُ أَبِي إِبْرَاهِيمَ، عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَبُشْرَىٰ عِيسَىٰ ابْنِ مَرْيَمَ، وَرَأَتْ أُمِّي كَأَنَّهُ خَرَجَ مِنْهَا نُورٌ أَضَاءَتْ لَهُ فُضُورُ الشَّامِ»

“Dua ya baba yangu Ibrahim, ubashiri wa Isa bin Maryam na aliona mama yangu mwanga uliotoka kwake ambao uliangaza makasri ya Ash-Sham (Syria).”²

Katika Hadith hii, Masahaba walimuuliza Mtume ﷺ kuhusu mwanzo wa Utume wake. Suala hili tutalielezea baadaye, Allah تعالی Akipenda.

Ibrahim عليه السلام Anamuomba Allah تعالی Aifanye Makkah Eneo Salama na la Riziki Nyingi

Allah تعالی Anasema kuwa Ibrahim عليه السلام alisema,

رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا

“Ewe Mola Wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani.” (2:126)

¹ Fat’hul Al-Bari 4:50 na Muslim 2:987.

² Ahmad 5:262.

Kutokana na hali ya kuogofya, ili watu wake wasikae kwa hali ya woga. Allah تعالى Aliipokea dua ya Ibrahim عليه السلام. Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا^١

“Na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani.” (3:96)

Na Kauli ya Allah تعالى,

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا آمِنًا وَيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ^٢

“Je! Hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi Takatifu ina amani, na hali ya watu wengine wananyakuliwa kote kwa majirani zao?” (29:67)

Tumeshataja Hadith zinazozuia kupigana katika Eneo Takatifu. Muslim alinukuu kuwa Jabir رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا يَجِلُّ لِأَحَدٍ أَنْ يَحْمِلَ بِمَكَّةَ السَّلَاحَ»

“Si halali kwa yoyote kubeba silaha awapo Makkah.”¹

Allah تعالى Alitaja kuwa Ibrahim عليه السلام alisema,

رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا

“Ewe Mola Wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani.”

Maana yake: Ufanye mji huu salama. Haya yalijiri kabla ya kujengwa kwa Al-Ka’aba. Allah تعالى Amesema ndani ya Surat Ibrahim,

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا

“Na Ibrahim aliposema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani...” (14:35)

Zaidi ya hapo, Ibrahim عليه السلام aliomba dua kwa mara ya pili, baada ya Nyumba kujengwa na watu kuanzisha makazi pambizoni mwake, baada ya kuzaliwa Is-haq عليه السلام ambaye alikuwa mdogo kwa Ismail عليه السلام kwa miaka kumi na tatu. Ndio sababu mwisho wa Dua Ibrahim عليه السلام alisema,

¹ Muslim 2:989.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿١٢٠﴾

“Alhamdulillah! Himidi zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kusikia maombi.” (14:39)

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَأَرْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ ءَامَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٢١﴾

“...na Uwaruzuku watu wake matunda, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia Nitamstarehesha kidogo, kisha Nitamsukumiza kwenye Adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه alitolea maelezo Aya hii,

قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٢١﴾

“Na mwenye kukufuru pia Nitamstarehesha kidogo, kisha Nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.”

“Haya ni maneno ya Allah تعالى (ina maana sio ya Ibrahim عليه السلام).”¹ Hii pia ni Tafsir ya Mujahid na Ikrimah.² Zaidi ya hayo, Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما Maneno ya Allah تعالى;

رَبِّ أَجْعَلْ هَذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَأَرْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ ءَامَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ

“Ewe Mola Wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani, na Uwaruzuku watu wake matunda, wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Ibrahim عليه السلام alimuomba Allah تعالى Awape riziki Waumini tu. Hata hivyo, Allah تعالى Aliteremsha, “Nitawapa pia waliokufuru, kama nitakavyowapa Waumini. Je! Nitaumba kitu kisha Nisikiwezeshe kuishi na Kukipa riziki?”

¹ At-Tabari 3:53.

² At-Tabari 3:54.

Nitawastarehesha kidogo waliokufuru, na kisha Nitawasukumiza kwenye adhabu ya moto, na ni mwisho mbaya ulioje?" Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما akasoma,

كُلًّا نُمِدُّ هُنُوْلًا ۖ وَهُنُوْلًا ۖ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ ۚ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿١٢٠﴾

“Wote hao Tunawakunjulia - hawa na hao - katika Neema za Mola wako Mlezi. Wala Neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki.” (17:20)

Haya yalinukuliwa na Ibn Marduwyah, ambaye naye alinukuu kauli sawa na hiyo kutoka kwa Ikrimah na Mujahid. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتُرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١٢١﴾ مَتَّعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ

إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُنذِقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿١٢٢﴾

“Hao wanaomzulia uongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.” (10:69-70) Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَمَنْ كَفَرَ فَلَا يَحْزُنكَ كُفْرُهُ ۚ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ فَنُنذِرُهُمْ بِمَا عَمِلُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ

الصُّدُورِ ﴿١٢٣﴾ نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿١٢٤﴾

“Na anayekufuru, isikuhuzunisha kufuru yake. Kwetu ndio marudio yao, na hapo Tutawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye Adhabu ngumu.” (31:23-24) Aidha Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَوْلَا أَنْ يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً لَجَعَلْنَا لِمَنْ يَكْفُرُ بِالرَّحْمَنِ لِيُوتِيَهُمْ سُقْفًا مِّنْ فَضَّةٍ

وَمَعَارِجَ عَلَيْهَا يَظْهَرُونَ ﴿١٢٥﴾ وَلِيُوتِيَهُمْ أَتُوبًا وَسُرْرًا عَلَيْنَا يَتَّكِبُونَ ﴿١٢٦﴾ وَزُخْرَفًا ۗ وَإِنْ

كُلُّ ذَلِكَ لَمَّا مَتَّعَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۗ وَالْآخِرَةُ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٧﴾

“Na lau isingekuwa watu watakuwa kundi moja Tungeliwajaalia wanaomkufuru Rahman nyumba zao zina dari ya fedha, na ngazi

¹ Ibn Abu Hatim 1:377.

zao pia wanazopandia. Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyoegemea juu yake. Na mapambo. Lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyoko kwa Mola Wako Mlezi ni ya wenye kumcha Mungu.” (43:33-35)

Kisha Allah تعالى Akasema,

ثُمَّ أَصْطَرَّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ وَيَسَّ الْأَمْصِرُ ﴿٣٥﴾

“Kisha Nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto, napo ni pahala pabaya mno pa kurejea.”

Maana yake: “Baada ya mwenye kukufuru kustarehe katika maisha ya dunia, Nitaufanya mwisho wake ni kuingia adhabu ya Moto, na ni mwisho mbaya.” Ayah hii inaonesha kuwa Allah تعالى Huwapa starehe waliokufuru na kisha Huwapokonya. Hii ni hali inayoonesha Ukubwa na Uwezo Wake. Ayah hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَيْتُ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ ثُمَّ أَخَذْنَا وَإِلَىٰ الْأَمْصِرُ ﴿٣٥﴾

“Ni miji mingapi Niliipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, na kisha Nikaitia Mkononi? Na Kwangu Mimi ndio marudio yote.” (22:48)

Aidha Sahih mbili zimenukuu,

«لَا أَحَدٌ أَضْبَرُ عَلَىٰ أَدَىٰ سَمْعِهِ مِنَ اللَّهِ إِنَّهُمْ يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا وَهُوَ يُرْزُقُهُمْ وَيُعَايِبُهُمْ»

“Hapana mwenye kusubiri kuliko Allah juu ya maudhi. Wanajaalia kuwa Ana mtoto, wakati Anawalisha na Kuwapa afya.”¹

Sahih pia imenukuu,

«إِنَّ اللَّهَ لَيُنْبِئِي لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُغْلِبْهُ»

“Allah Humpa muda dhalimu, mpaka Atakapomtia Mkononi; Hatachomoka.”² Kisha akasoma Kauli ya Allah تعالى,

وَكَذَٰلِكَ أَخَذْنَا مِنْكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola Wako Mlezi Anapo ikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika mkamato Wake ni mchungu na mkali.” (11:102)

¹ Fat’hul Al-Bari 13:372 na Muslim 4:2160.

² Fat’hul Al-Bari 8:205.

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا
 تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا
 مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا
 وَتُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَابْعَثْ
 فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ
 وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ وَمَنْ
 يَرْغَبْ عَن مِّلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَن سَفِهَ نَفْسَهُ ۗ وَلَقَدِ
 اصْطَفَيْنَاهُ فِي الْدُنْيَا ۗ وَإِنهٗ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ
 ﴿١٣٠﴾ إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۖ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ
 ﴿١٣١﴾ وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ يٰبَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ
 اصْطَفَىٰ لَكُمُ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾
 أَمْ كُنتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتَ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا
 تَعْبُدُونَ مِن بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ إِلَهَكَ وَإِلَهَ ءَابَائِكَ
 إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ ۗ إِنَّهَا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ
 مُّسْلِمُونَ ﴿١٣٣﴾ تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ ۗ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلكُمْ
 مَا كَسَبْتُمْ ۗ وَلَا تَسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٤﴾

Ujenzi wa Al-Ka'abah na Kumuomba Allah تعالى Aridhie Amali hiyo

Allah تعالى Amesema,

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ۗ إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾ رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا ۗ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾

“Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipoinyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe Ndiye Msikizi Mjuzi. Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie iwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi

vyetu wawe Umma uliosilimu kwako. Na Utuoneshe njia za ibada yetu na Utusamehe. Bila ya shaka Wewe Ndiye Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.” (2:127-128)

Allah تعالى Alisema: “Ewe Muhammad: Wakumbushe watu wako pale (Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام) walipojenga Nyumba na wakanyanyua msingi wake huku wakisema,

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Ewe Mola Mlezi Wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe Ndiye Msikizi na Mjuzi.”

Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alitaja kuwa Ubayy na Ibn Masud رضي الله عنهما walikuwa wakisoma Aya hii kama hivi,

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ

الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipoinyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe Ndiye Msikizi Mjuzi.” (2:127)¹

Kinachothibitisha kauli hii zaidi (ni nyongeza ya “wakaomba” katika Aya) Kwa rai ya Ubayy na Ibn Mas’ud رضي الله عنهما (Mimi) Bin Kathir nasema: Na kinachochagiza usomaji wao huo, ni kauli ya Ibrahim na mwanawe inayofuata katika Aya hii,

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُسْلِمَةً لَكَ

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe Umma uliosilimu Kwako.”

Mitume - Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام walikuwa wakifanya amali njema, bado walimuomba Allah تعالى Aridhie amali hii njema. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Wuhaybu bin Al-Ward alisoma,

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا

“Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipoinyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie!”

Alilia na akasema, “Ewe Khalil wa Ar-Rahman! Ulinyanyua msingi wa Nyumba ya Ar-Rahman (Allah), bado una wasi wasi wa kutopokewa kwako?”² Hii ni tabia ya Waumini wenye Ikhlaswi, ambao Allah تعالى Amewaelezea katika Kauli,

¹ Al-Qurtubi 2:126.

² Ibn Abu Hatim 1:384.

وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَا آتَوْا

“Na wale ambao wanatoa walichopewa.” (23:60)

Ina maana: Watoa sadaka, na bado wanafanya ibada za kujikurubisha,

وَقُلُوبِهِمْ وَجِلَةٌ

“Na hali nyoyo zao zinaogopa.” (23:60)


Wanaogopa kuwa amali hizi njema zinaweza zisikubaliwe. Kuna hadithi sahihi iliyosimuliwa na Aishah رضي الله عنها juu ya somo hili, ambayo tutaitaja baadaye, Allah تعالى Akipenda.

Bukhari alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, ‘Mwanamke wa kwanza aliyefunga Mkwaja katika tumbo lake, alikuwa mama yake Ismail عليه السلام, alifanya hivyo ili kuficha athari zake kwa Sara.’ Mtume Ibrahim عليه السلام aliwachukua Ismail عليه السلام na mama yake na akaondoka nao mpaka wakafika eneo la Nyumba Tukufu, ambapo aliwaacha karibu na mti mahali palipo kisima cha maji ya zamzam katika sehemu ya juu ya Masjid. Wakati huo, Mama yake Ismail عليه السلام alikuwa akimnyonyesha mwanawe. Wakati huo Makkah haikuwa na wakazi, na hapakuwa na chanzo cha maji. Ibrahim عليه السلام aliwaacha pale na mfuko wenye tende na kiriba cha ngozi chenye maji. Ibrahim عليه السلام alianza kuondoka na mama yake Ismail عليه السلام alimfuata na kumuambia, “Ewe Ibrahim! Unatuacha na nani katika bonde lisilo na kitu na watu?” Alirejea swali hilo mara kadha lakini Ibrahim عليه السلام hakumjibu. Akamuuliza, “Je, Allah تعالى Amekuamrisha kufanya hivi?” Akamjibu, “Ndiyo.” Akamuambia, “Nimeridhika kuwa Allah تعالى Hatotutupa mkono.” Ibrahim عليه السلام aliondoka na alipokuwa mbali ambapo hawakuweza kumuona, karibu na bonde, alielekea Al-Kaaba, akanyanyua mikono yake na akaomba Dua,

رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ

“Mola Wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya wangu katika bonde lisilokuwa na mimea, kwenye Nyumba Yako Takatifu (Al-Ka’abah iliyopo Makkah).”

Hadi mwisho wa Aya,



“Kushukuru.” (14:37)

Kisha mama yake Ismaili عليه السلام akarejea mahali pake, na akaanza kumnyonyesha mwanawe na kunywa maji yaliyokuwemo ndani ya kiriba na kumhudumia mwanawe. Maji yalipoisha, yeye na mwanae walisikia kiu. Alimuangalia, alikuwa akipata taabu kwa kiu, aliondoka kwa sababu hakupenda kuona uso wake katika hali ile. Alilikuta jabali jirani na alipokuwa, *As-Safa*, alilipanda na akaangalia lakini hakuona mtu yeyote. Aliporejea kwenye bonde, alipandisha nguo zake, akakimbia kama akimbiavyo mtu aliyechoka mpaka alipofika jabali *Marwah*. Aliangalia kila pahali lakini hakuona mtu yeyote. Akawa anakimbia kati ya majabali hayo mawili mara saba.” Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema, “*Hii ndio sababu watu wanakwenda baina ya As-Safa na Al-Marwah (wakati wa Hajj na Umrah).*” “Alipofika Marwah, alisikia sauti akasema: ‘Tulia nafsi!’ akiwa anajipa moyo kwa kuiambia nafsi yake hivyo na alijaribu kwa mara nyingine kusikiliza akawa anaendelea kusikia sauti hiyo, na alipoisikia alisema, “Nimekusikia. Utanipatia msaada?” Alimkuta Malaika akichimba kwa kisigino chake (au bawa lake) mahali ambapo ipo chemchemi ya Zamzam sasa, na maji yalibubujika. Mama yake Ismail عليه السلام alishangazwa na alianza kuchimba na kuchota maji kwa mikono yake na kuyatia ndani ya kiriba huku yakibubujika.” Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: Mtume ﷺ alisema, “Allah تعالى Amrehemu mama yake Ismail عليه السلام, kwani kama angeyaacha maji yamiminike bila kuyazuilia, yangukuwa yanapita na kutembea juu ya mgongo wa Ardhi.” Mama yake Ismail عليه السلام alianza kunywa maji na maziwa yake yakaongezeka. Malaika Jibril عليه السلام akamuambia, “Usiogope kuachwa peke yako. Nyumba ya Allah تعالى itajengwa na huyu mtoto na baba yake. Allah تعالى Hawatelekezi watu Wake.” Zama hizo eneo la Nyumba liliinuliwa kutoka usawa wa ardhi na mafuriko yalikuwa yakifikia pande zake za kulia na kushoto.

Baadaye baadhi ya watu wa kabila la Jurhum, waliopitia njia ya Kada, walipiga kambi chini ya bonde. Waliona ndege, wakashangaa na kusema, “Ndege wanaweza kuwepo pahala penye maji. Hatukupata kuona maji katika bonde hili kabla. Walimtuma mpelelezi au watu wawili kwenda kupeleleza eneo lile, waliyakuta maji na walirejea kutoa khabari ile. Kisha wote walimuendea mama

yake Ismail عليه السلام, pambizoni ya maji na wakamuambia, "Ewe Mama Ismail! Utaturuhusu tuishi nawe hapa?" Akawajibu, "Ndiyo, lakini hamtakuwa na haki yoyote katika maji haya." Wakasema, "Tumekubali." Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema, "Wakati ule Mama yake Ismail alitaka watu wa kuishi nao." Hivyo waliishi pale na wakawapelekea habari jamaa zao waje kuishi nao. Baadaye kijana wake alifikia umri wa balebeghe na akaoa mwanamke kutoka kabila la Jurhum, Ismail عليه السلام akajifunza Kiarabu kutoka kwao, na walipenda namna alivyolelewa. Baada ya hapo Mama yake Ismail عليه السلام alifariki.

Kisha ikamjia Ibrahim عليه السلام fikra ya kuwatembelea ahli zake. Hivyo alielekea Makkah. Alipowasili hakumkuta Ismail عليه السلام, hivyo akamuuliza mke wake. Akamuambia, "Amekwenda kuwinda." Alipomuuliza hali zao za maisha, alilalamika kuwa walikuwa katika maisha ya dhiki na umasikini. Ibrahim عليه السلام alimuambia, "Mumeo atakaporejea, mpe salamu zangu na muambie abadilishe kizingiti cha mlango wake." Ismail عليه السلام aliporejea, alihisi kuwa kulikuwa na mgeni na akamuuliza mke wake, "Je! Tulipata mgeni?" Akamjibu, "Ndiyo. Mzee mmoja alituzuru na akaniuliza khabari zako, na nikamueleza ulipokuwa. Aidha alitaka kujua hali zetu za maisha na nikamuambia kuwa tunaishi kwa tabu na tupo katika lindi la umasikini." Ismail عليه السلام akasema, "Je! Alikutaka ufanye chochote?" Akajibu, "Ndiyo. Alinitaka nikufikishie salamu na amekutaka ubadili kizingiti cha mlango wako." Ismail عليه السلام alimuambia, "Alikuwa baba yangu na wewe ndiye kizingiti, hivyo nenda kwenu (maana yake umeachika)." Hivyo alimpa talaka na akamuoa mwanamke mwingine.

Mara nyingine Ibrahim عليه السلام alitamani kuwatembelea ahli zake aliowaacha Makkah. Ibrahim عليه السلام alifika kwenye nyumba ya Ismail عليه السلام, lakini hakumkuta Ismail عليه السلام na akamuuliza mke wake, "Yupo wapi Ismail?" Mke wa Ismail akajibu, "Ametoka kwenda kuwinda." Akamuuliza kuhusu hali zao, akamjibu kuwa maisha yao ni mazuri na akamshukuru Allah تعالى, "Chakula chetu nyama na kinywaji chetu maji." Akasema, "Ewe Allah! Ibariki nyama yao na maji yao." Mtume Muhammad ﷺ alisema, "Wakati huo hawakuwa na mazao, vinginevyo Ibrahim عليه السلام angemuomba Allah تعالى Ayabariki pia." Wale wasioishi Makkah hawawezi kuvumilia kula chakula cha nyama na maji peke yake. Ibrahim عليه السلام akamuambia, "Ismail عليه السلام atakaporejea mpe salamu zangu, na muambie akiimarisha kizingiti cha mlango wake."

Ismail عليه السلام aliporejea aliuliza, “Kuna mtu aliyetutembelea.” Akajibu, “Ndiyo. Mzee mtanashati, na akamsifu Ibrahim عليه السلام. Na akaniuliza hali yetu ya maisha na nikamuambia kuwa tunaishi vizuri.” Akamuuliza, “Hakukupa ujumbe wowote unifikishie?” Akajibu, “Ndiyo.” Amenipa salamu nikufikishie na akaniambia uimarisha kizingiti cha mlango wako”. Ismail عليه السلام akasema, “Huyo ni baba yangu, na wewe ndiye kizingiti; ameniamrisha nidumu nawe.” Ibrahim عليه السلام alifanya ziara nyingine na safari hii alimkuta Ismail عليه السلام nyuma ya kisima cha Zamzam, karibu na mti, akitengeneza mishale yake. Alipomuona Ibrahim عليه السلام alisimama na wakasabahiana, kama baba na mwana wanavyolakiana. Ibrahim عليه السلام akasema, “Ewe Ismail, Mola Wako Ameniamrisha nifanye kitu.” Akamuambia, “Mtii Mola Wako.” Akamuuliza Ismail عليه السلام, “Je! Utanisaidia?” Akamjibu, “Ndiyo, nitakusaidia.” Ibrahim عليه السلام akasema, “Allah تعالى Ameniamrisha nimjengee Yeye Nyumba hapa.” Na akaonesha sehemu iliyokuwa imeinuka. Hivyo wote walisimama na wakaanza kuinua msingi wa Nyumba. Ibrahim عليه السلام akaanza kujenga Al-Ka’ba, wakati Ismail عليه السلام akiendelea kumpa mawe. Hivyo walikuwa wakijenga Nyumba, kidogo kidogo, wakiizunguka na kusema,

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe Ndiye Msikizi Mjuzi.” (2:127)¹

Utajo wa Makureshi Kujenga Upya Al-Kaaba Baada ya Nabii Ibrahim Al-Khaliil عليه السلام.

Katika kitabu chake cha *Sirah*, Muhammad bin Is-haq bin Yasar رحمه الله تعالى alisema, “Mtume ﷺ alipofikia umri wa miaka thelathini na mitano, Makuraish walijumuika kuijenga upya Al-Kaabah, hii ilikuwa pamoja na kuiezekka. Hata hivyo walikuwa na wasiwasi wa kuibomoa. Zama hizo, Al-Kaabah ilikuwa wazi na urefu wa mabega ya mtu, hivyo walitaka kuinua kuta zake na kuifunika juu. Kuna watu waliiba hazina iliyokuwemo ndani ya Al-Kaabah iliyokuwa ikihifadhiwa ndani ya kisima katikati ya Ka’abah. Hazina hiyo ilikuja kukutwa kwa mtu mmoja akiitwa Duwayk, mtumwa aliyeachwa huru wa Bani Mulayh

¹ Fat’hul Al-Bari 6:456.

bin Amr wa kabila la Khuza'ah. Makuraish waliukata mkono wake kama adhabu. Baadhi ya watu wanadai kuwa mwizi hasa aliondoka na kuiacha kwa Duwayk. Baadaye, bahari iliileta meli ya mfanyabiashara wa kirumi, iliyoharibika vibaya, katika fukwe za Jeddah. Hivyo walikusanya mbao za meli hiyo ili zitumike kupaua Al-Ka'bah. Fundi seremala Mkoptiki aliyekuwepo Makkah aliwaandalia kilichotakiwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Kulikuwepo nyoka ambaye alikuwa anatoka katika Kisima cha Al-Kaaba, upande ambao watu walikuwa wakitupa Hadiya na Zawadi. Kila siku, hudhihiri nyoka huyo hadi katika ukuta wa Al-Kaaba. Na walikuwa wakimuogopa, kwa kuwa alikuwa hamkurubii yeyote - isipokuwa nyoka huyo alimtisha kwa kufunua mdomo wake. Hivyo walikuwa wakimuogopa.

Siku moja akiwa amedhihiri juu ya ukuta kama desturi yake, Allah تعالی Alimpelekea ndege na kumnyakua na kuondoka naye. Makurayshi wakasema: Hakika bila ya shaka matarajio yetu Allah تعالی Ameridhia yale tuliyoyakusudia. Hapa tunaye fundi mzuri pamoja na mbao. Na Allah تعالی Ametusahilishia suala la kumtoa nyoka.

Walipoamua kuanza ubomoaji ili waijenge upya Al-Kaaba, Abu Wahb bin 'amr bin 'Aidh bin 'Abd bin 'Imran bin Makhzum alilitoa jiwe kutoka katika jengo la Al-Kaabah; jiwe lilimponyoka kutoka Mkononi mwake na likarudi mahali lilipokuwepo kabla ya kutolewa. Akasema, "Enyi Makuraishi! Msichangie mali yoyote kwa ajili ya kuijenga upya Al-Kaabah, isipokuwa mali iliyopatikana kwa njia za halali. Isiwe mali itakayotumika iliyopatikana kwa njia za uasherati, riba au dhuluma." Ibn Is-haq رحمه الله تعالی amesema kwamba watu waliyanasibisha maneno haya kwa Al-Walid bin Al-Mughirah bin 'Abdullah bin 'Amr bin Makhzum.¹ Ibn Is-haq aliendelea, "Makuraish walianza kujipanga kwa ajili ya kazi ya kuijenga upya Al-Ka'abah kila ukoo kuchukua jukumu la kujenga sehemu mahsusii." Upande wa mlangoni ulikuwa ni wa kabila la Abdi Manafi na Zuhrah. Ruknul Aswad na Ruknul Al-Yamaani ilikuwa ni ya kabila la Makhzumi pamoja na Qurayshi. Sehemu ya juu ya Al-Kaaba ilikuwa ni ya kabila la Jumah na Sahmi. Sehemu ya Hijri ilikuwa ni ya Bani Abdiddari bin Wusai, Bani Asadi bin Abdul-Uzza bin Qusai na Bani Adi bin Kaabi.

¹ Ibn Hisham 1:204.

Hata hivyo bado waliendelea kuwa na wasiwasi wa kuibomoa Al-Kaabah. Al-Walid bin Al-Mughirah alisema, “Nitaanza kuibomoa.” Alibeba shoka na akasimama karibu na Ka’bah na akasema, “Ewe Mwenyezi Mungu! Hatukusudii uharibifu. Ewe Mwenyezi Mungu! Tunataka kufanya kazi iliyo njema. Akaanza kukata mawe ya Al-Kaaba. Watu walisubiri usiku ule waone linalotokea.” Kama atapatwa na jambo, hatutaibomoa badala yake tutaijenga kama ilivyokuwa. Endapo hatopatwa na chochote, basi tutajua kuwa Mwenyezi Mungu Ameridhia tunalolifanya. Siku ya pili, Al-Walid alikwenda kufanya kazi katika Ka’bah, na watu wakaanza kuibomoa Al-Ka’bah pamoja naye. Walipofikia ule msingi uliojengwa na Ibrahim عليه السلام, wakaona mawe ya kijani yaliyokuwa juu ya mengine, kama rundo la mikuki. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى akasema kuwa aliambiwa na baadhi ya watu, “Mtu kutoka kabila la Maquraish aliyekuwa akisaidia ujenzi wa Al-Ka’bah aliweka beleshi kati ya mawe mawili ili ayang’oe, jiwe moja liliposogezwa, Makkah yote ilitikisika, hivyo wakaacha kuyachimba mawe hayo.¹”

Mvutano Katika Kuweka Jiwe Jeusi Mahali Pake na Hukumu ya Mtume Muhammad bin Abdillah ﷺ Ndio Hukumu Adilifu

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema, “Makabila ya Kikuraish yalikusanya mawe ili kuijenga upya Nyumba, kila kabila lilifanya kazi hiyo peke yake. Wakaanza kuijenga upya, mpaka walipofikia mahali ambapo Jiwe Jeusi lingewekwa pahala pake. Mgogoro ukazuka miongoni mwa makabila mbali mbali ya Kikuraish, na ulikaribia kuleta mapigano kati ya viongozi wa Kikuraish katika eneo la Nyumba Takatifu. Banu Abd d-Dar na Banu Adi bin Ka’b bin Lu’ay waliahidi kwa pamoja kuwa wangepigana mpaka kufa.

Hata hivyo, siku tano au nne baadaye, Abu Umayyah bin Al-Mughirah bin Abdullah bin Amr bin Makhzum, mtu mkubwa kutoka kwa Makuraish aliingilia kati katika wakati muafaka. Abu Umayyah aliwashauri Makuraish wamchague mtu atakayeingia kupitia Mlango wa Msikiti huu kuwa msuluhishi kati yao. Walikubaliana katika hilo. Mjumbe – Muhammad ﷺ – alikuwa mtu wa kwanza kuingia katika Msikiti. Viongozi mbali mbali wa Kikuraish walipotambua kuwa mtu wa kwanza kuingia ni Muhammad ﷺ, wote walitangaza, “Huyu ni Al-

¹ Ibn Hisham 1:207.

Amin wote tunamkubali, Huyu ni Muhammad.” Mtume ﷺ alipofika katika eneo walilokusanyika na wakamfahamisha mgogoro wao, aliwataka walete nguo na waiweke juu ya ardhi. Akaliweka Jiwe Jeusi juu yake kisha akawaomba viongozi kila mmoja ashike ncha ya nguo na wote waliinue Jiwe Jeusi na kulisogeza pahala pake. Baadaye Mtume ﷺ aliliinua Jiwe Jeusi peke yake na akaliweka katika sehemu yake na likajengewa. Makuraish walikuwa wakimuita Mtume ﷺ “Al-Amin” kabla hata ya kuletwa Wahyi.

Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما Ajenga Al-Ka’bah Kama Alivyotaka Mtume ﷺ.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema, Zama za Mtume ﷺ, Ka’bah ilikuwa na urefu wa dhira kumi na nane na ilifunikwa na kitani ya Misri pamoja na nguo ya mistari. Al-Hajjaj bin Yussuf alikuwa mtu wa kwanza kuifunika kwa Hariri.¹ Mimi bin Kathir ninasema: Ka’bah ilibaki kama ilivyojengwa upya na Makuraish mpaka ilipochomwa moto wakati wa Utawala wa Abdillah bin Az-Zubayr رضي الله عنهما, baada ya miaka 60H, na katika mwishoni mwa Utawala wa Yazid bin Mu’awiyah. Na Wakati, Ibn Zubayr رضي الله عنهما alipozingirwa – Makkah, aliibomoa Kaabah na akaijenga juu ya msingi wa Ibrahim عليه السلام, pamoja na Hijr ndani yake. Pia alitengeneza mlango wa Mashariki na wa Magharibi ya Ka’bah na akaliweka katika usawa wa ardhi. Kama alivyosikia kutoka kwa mama yake mdogo Aishah رضي الله عنها, Mama wa waumini, akihadithia kuwa Mtume ﷺ alipendelea hivyo. Ka’bah ilibaki hivyo katika kipindi chake chote cha Utawala, mpaka Al-Hajjaj alipomuua Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما na kisha akaijenga kama ilivyokuwa kwa amri ya Abdul-Malik bin Marwan.

Muslim alinukuu kutoka kwa Ata alisema, “Wakati Al-Kaaba ilipoungua katika Utawala wa Yazid bin Muawiyah, wakati watu wa Sham walipoivamia Makkah. Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما hakuigusa Al-Kaaba mpaka watu walipokuja kwa ajili ya Hajj kwani alitaka kuwachochea dhidi ya watu wa Ash-Sham. Aliwaambia, “Enyi watu! Nipeni ushauri juu ya Ka’abah, niifumue kisha niijenge upya, au nirekebishe sehemu zilizoharibika? Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema: “Mimi nashauri urekebishe sehemu zilizoharibika. Na uiache katika umbo lake na mawe yale ambayo Mtume ﷺ alitumwa yakiwa yapo na waliosilimu waliyashuhudia.” Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما alisema, “Endapo nyumba ya

¹ Ibn Hisham 1:209.

mmoja wenu itaungua, hatoridhika mpaka aijenge upya. Seuze Nyumba ya Allah تعالى? Nitamuomba Mola wangu kwa siku tatu na kisha nitafanya nitakaloamua." Siku tatu zilipopita aliamua kuivunja Al-Kaabah, watu walisita kuivunja, kila mtu alichelea kuwa wa kwanza kupanda juu ya Nyumba na akatupa mawe chini, na watu walipoona hakudhurika kwa kuyagusa, walianza kufanya hivyo. Waliporomosha Nyumba usawa wa ardhi. Ibn Zubayr رضي الله عنهما alizungushia eneo la ujenzi kwa mapazia yaliyoshikiliwa kwa nguzo, ili Nyumba ifunikwe, mpaka jengo litakapomalizika. Kisha Az-Zubayr رضي الله عنه alisema, "Nilimsikia Aishah رضي الله عنها akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَوْلَا أَنَّ النَّاسَ حَدِيثَ عَهْدِهِمْ بِكُفْرٍ، وَلَيْسَ عِنْدِي مِنَ الشَّقَقَةِ مَا يُقَوِّنِي عَلَى بِنَائِهِ
لَكُنْتُ أَدْخَلْتُ فِيهِ مِنَ الْحَجَرِ خُمْسَةَ أذْرَعٍ، وَلَجَعَلْتُ لَهُ بَابًا يَدْخُلُ النَّاسُ مِنْهُ وَبَابًا
يَخْرُجُونَ مِنْهُ»

"Kama sio kwa sababu watu wameacha ukafiri hivi karibuni, na kuwa sina fedha za kutumia, ningalijenga dhiraa tano katika Al-Kaaba kutoka Al-Hijr na ningeweka mlango wa kuingilia watu na mwingine wa kutokea."

Ibn Zubayr رضي الله عنهما akasema, "Ninaweza kutumia gharama kwa kazi hii na siwaogopi watu." Hivyo aliongeza dhiraa tano kutoka Hijr, ambayo itaonekana kama sehemu ya nyuma ya Al-Kaaba ambayo ilionekana wazi. Kisha akaijenga na akaifanya ndefu kwa dhiraa kumi na nane. Alidhani kuwa Al-Kaaba ilikuwa bado fupi na akaongeza dhira kumi kwa mbele na akaweka milango miwili, mmoja wa kuingilia na mmoja wa kutokea.

Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما alipouawa, Al-Hajaj alimuandikia Abdul Malik bin Marwan akimuuliza kuhusu Al-Kaaba na akamuambia kuwa Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما alipojenga sehemu ya nyuma ya Al-Kaaba alifanya marekebisho yaliyopingana na watu wa Makka. Abdul Malik akamjibu kwa barua, "Hatukubaliani na kitendo cha Ibn Az-Zubayr. Ama kuhusu urefu, acha kama ulivyo. Ama kile alichokiongeza kutoka Hijr, kibomoe, na ijenge Nyumba kama ilivyokuwa, na uzibe mlango." Kwa hiyo Al-Hajaj aliibomoa Al-Kaaba na akaijenga kama ilivyokuwa mwanzo.¹ Katika Sunan yake, An-Nasai alikusanya

¹ Muslim 2:970.

Hadith za Mtume ﷺ zilizosimuliwa kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, sio kisa chote.¹

Sunan sahihi inakubaliana na maamuzi aliyoyafanya Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما, kwa sababu hivi ndivyo Mtume ﷺ alivyopendelea afanye, lakini alichelea kuwa nyoyo za watu walioingia katika Uislamu karibuni wasingethubutu kuijenga upya Al-Kaaba. Sunnah haikueleweka kwa Abdul Malik bin Marwan. Hivyo Abdul Malik alipotanabahi ya kuwa Mama Aisha رضي الله عنها alisimulia Hadithi ya Mtume ﷺ kuhusiana na somo hilo, akasema, "Natamani tungeiacha kama Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما alivyoijenga." Muslim alinukuu kuwa Ubaydullah bin Ubayd kuwa Al-Harith bin Abdullah alifika kwa Abdul Malik bin Marwan wakati wa Utawala wake. Abdul Malik alisema, "Sikujua kuwa Abu Khubayb (Ibn Az-Zubayr) alimsikia Mama Aishah kwa yale aliyoyasema ameyasikia kutoka kwake." Al-Harith alisema, "Ndiyo alimsikia". Mimi mwenyewe nilisikia Hadithi kutoka kwake. Abdul Malik alisema, "Ulimsikia akisema nini?" Akasema, "Amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ قَوْمَكَ اسْتَفْضَرُوا مِنْ بَيْنِ الْبَيْتِ وَلَوْلَا حِدَاثَةُ عَهْدِهِمْ بِالشَّرْكِ أَعَدْتُ مَا تَرَكُوا مِنْهُ، فَإِنْ بَدَأَ لِقَوْمِكَ مِنْ بَعْدِي أَنْ يَبْنُوهُ فَهَلُمِّي لِأَرِيكَ مَا تَرَكُوهُ مِنْهُ»

"Watu wako walijenga upya Al-Kaaba lakini ndogo. Kama isingelikuwa watu wako ndio kwanza wametoka kwenye ushirikina, Ningeongeza kila kilichoachwa. Endapo watu wako watapenda kuijenga baadaye, acha nikuoneshe kilichoachwa katika ujenzi wa Al-Kaaba." Alimuonesha dhira saba kwa kuzunguka."

Mmoja wa Wasimulizi wa Hadithi, Al-Walid bin Ata, aliongeza kuwa Mtume ﷺ alisema,

«وَلَجَعَلْتُ لَهَا بَابَيْنِ مَوْضُوعَيْنِ فِي الْأَرْضِ: شَرْقِيًّا وَغَرْبِيًّا، وَهَلْ تَدْرِينَ لِمَ كَانَ قَوْمُكَ رَفَعُوا بَابَهَا؟» قَالَتْ: قُلْتُ: لَا. قَالَ: «تَعَزُّزًا أَنْ لَا يَدْخُلَهَا إِلَّا مَنْ أَرَادُوا، فَكَانَ الرَّجُلُ إِذَا هُوَ أَرَادَ أَنْ يَدْخُلَهَا يَدْعُوهُ يَرْتَقِي حَتَّى إِذَا كَادَ أَنْ يَدْخُلَ دَفَعُوهُ فَسَقَطَ»

¹ An-Nasai 5:218.

“Ningeweka milango miwili katika Al-Kaaba, katika sakafu ya chini, mmoja Mashariki na mmoja Magharibi. Unajua kwa nini Watu wako waliinua paa na mlango juu ya usawa wa ardhi?” Akasema, “Sijui” Akasema, “Ili kuwaruhusu wale tu waliotaka kuingia ndani. Alipopanda mtu ambaye hawakumtaka aingie ndani ya Nyumba, walimsukuma chini.”

Abdul Malik aliuliza, “Ulimsikia Aishah رضي الله عنها akiisimulia Hadith hii?’ Akajibu, “Ndiyo” Abdul Malik akasema, “Natamani ningeacha kama ilivyokuwa.”¹

Mhabeshi Ataivunja Al-Ka’bah kabla ya Kiyama.

Sahihi mbili zimeandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُخْرَبُ الْكَعْبَةَ ذُو السُّؤْيَقَتَيْنِ مِنَ الْحَبَشَةِ»

“Ka’bah itabomolewa na kuvunjwa na Dhus-Swuqatayn (mtu mwenye miguu myembamba) kutoka Habasha.”²

Aidha, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«كَأَنِّي بِهِ أَسْوَدَ أَفْحَجَ يَفْلَعُهَا حَجْرًا حَجْرًا»

“Kama kwamba namuona sasa: Mtu mweusi mwenye miguu myembamba aking’oa mawe ya Ka’bah moja baada ya jingine.” Al-Bukhari aliandika Hadith hii.³

Imam Ahmad bin Hambal aliandika katika Musnad yake kuwa Abdullah bin Amr bin Al-As رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«يُخْرَبُ الْكَعْبَةَ ذُو السُّؤْيَقَتَيْنِ مِنَ الْحَبَشَةِ وَيَسْلُبُهَا حِلْيَتَهَا وَيَجْرُدُهَا مِنْ كِسْوَتِهَا،
وَلَكَأَنِّي أَنْظَرُ إِلَيْهِ أَصِيلَعٍ وَ أَفِيدِعٍ يَضْرِبُ عَلَيْهَا بِمِسْحَاتِهِ وَمِعْوَلِهِ»

¹ Muslim 2:971.

² Fat’hul Al-Bari 3:538, Al-Bukhari na Muslim 4:2232.

³ Fat’hul Al-Bari 3:538.

“Dhus-Suqatayn kutoka Habasha ataiharibu Ka’bah na atapora mapambo na nguo inayofunika, ni kama namuona sasa: Ana Kipara, miguu myembamba, akiivunja Ka’bah kwa shoka na mtaimbo wake.”¹

Hili litajiri baada ya kutokea Ya’ajuj wa Maajuj. Al-Bukhari aliandika kuwa Abu Said Al-Khudhri رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لِيَحْجَنَّ الْبَيْتُ وَلِيَعْتَمِرَنَّ بَعْدَ خُرُوجِ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ»

“Nyumba itahijiwa (Al-Kaaba) baada ya kutoka Ya’ajuu wa Maajuj.”²

Dua ya *Al-Khalil* عليه السلام.

Allah تعالى Amesema kuwa Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام walimuomba Allah تعالى,

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَا إِنَّكَ

أَنْتَ أَلْوَدَّكَ الرَّحِيمُ

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu Kwako, na pia miongoni mwa vizazi vyetu uwe Umma uliosilimu Kwako. Na Utuoneshe njia za ibada yetu na Utusamehe. Bila ya shaka Wewe Ndiye Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.” (2:128)

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, “Dua yao ilikuwa na maana, “Tufanye wanyenyekevu na watii wa Amri Zako na tusikushirikishe na yeyote katika kuabudiwa.”¹ Pia Ikrimah aliitolea maelezo Aya hii,

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمِينَ لَكَ

“Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu Kwako.”

Allah تعالى Akasema, “Nitayafanya hayo.”

¹ Ahmad 2:220.

² Fat’hul Al-Bari 3:531.

³ At-Tabari 3:73.

وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَا أُمَّةٌ مُّسْلِمَةٌ لَّكَ

“Na pia miongoni mwa vizazi vyetu wawe Umma uliosilimu Kwako.”

Allah تعالى Akasema, “Nitafanya hayo.” Dua hii ya Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام ni sawa na yale Aliyotufahamisha Allah تعالى kuhusu waja Wake waumini.

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ

إِمَامًا ﴿٧٤﴾

“Na wale wanaosema, Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Allah).” (25:74)

Aina hii ya dua inaruhusiwa kwani kupenda kuwa na watoto ambao wanamuabudu Allah تعالى Peke Yake bila kumshirikisha ni alama ya mapenzi makubwa kwa Allah تعالى.

Hii ndiyo sababu Allah تعالى Alimuambia Ibrahim عليه السلام,

إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا

“Hakika Mimi Nitakufanya uwe mwongozi wa watu.”

Ibrahim عليه السلام akasema,

وَمِنْ ذُرِّيَّتِي قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾

“Na katika vizazi Vyangu pia? Akasema. Ahadi Yangu haitawafika wenye kudhulumu.”

Ambayo inaelezwa na,

وَاجْتَنِبِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ ﴿٧٦﴾

“Na Uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.” (14:35)

Muslim amesimulia ndani ya Sahih yake kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

إِذَا مَاتَ ابْنُ آدَمَ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثٍ: صَدَقَةٌ جَارِيَةٌ أَوْ عِلْمٌ يُسْتَفَعُ بِهِ أَوْ وَلَدٍ صَالِحٍ يَدْعُو لَهُ

*"Anapokufa binadamu, hukatika amali zake isipokuwa mambo tatu, sadaka inayoendelea, elimu inayonufaisha au mtoto mwema anayemuomba dua."*¹

Maana ya *Manasik* (Ibada)

Said bin Mansur alisema kuwa Attab bin Bashir alitufahamisha kutoka kwa Khusaif kutoka kwa Mujahid ambaye alisema, "Mtume ﷺ alisema Ibrahim عليه السلام aliomba dua,

وَأَرْنَا مَنَاسِكَنَا

"Na Utuoneshe njia za ibada yetu."

Kisha Jibril عليه السلام akashuka, akamchukua mpaka kwenye Kaaba Tukufu na akamuambia, "Inua Msingi wake." Ibrahim عليه السلام akainua msingi wa Nyumba Tukufu na akakamilisha ujenzi. Jibril عليه السلام alimshika mkono Ibrahim عليه السلام akampeleka As-Safa na akamuambia, "Hizi ni miongoni mwa Ibada za Allah تعالى." Kisha akampeleka Al-Marwah na akamuambia, "Na hii ni miongoni mwa ibada za Allah تعالى."

Kisha akampeleka Mina mpaka walipofika Aqabah, wakamkuta Iblis amesimama karibu na mti. Jibril عليه السلام akasema, "Sema *Takbir* (Allah Akbar) na mpige Iblis kwa vijiwe. Iblis akasogea kwenye Jamrah la katikati na wakati Jibril عليه السلام na Ibrahim عليه السلام walipompita, Jibril عليه السلام akamuambia Ibrahim عليه السلام, sema *Takbir* na mtupie kijiwe. Ibrahim عليه السلام alimtupia na akasema *Takbir*. Iblis aliyelaanika alitaka kuingiza vitendo viovu katika ibada ya Hajj, lakini hakufanikiwa. Jibril عليه السلام alimshika Ibrahim mkono wakaenda *Al-Mash'ar Al-Haram* na Arafat na akamuambia, "Je, umejifunza, umefahamu niliyokuonesha?" Mara tatu. Ibrahim عليه السلام akajibu, "Ndiyo nimefahamu."² Kauli sawa na hizi zilipokelewa kutoka kwa Abu Miljaz na Qatadah.³

¹ Muslim 3:1255.

² Said bin Mansur 2:615.

³ Ibn Abu Hatim 1:387.

رَبَّنَا وَأَتَعَتْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْنَا آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ
 إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾

129. "Ewe Mola Mlezi Wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao, awesomee Aya Zako, na awafundishe Kitabu na hikima na awatakase. Hakika Wewe Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima."

Ibrahim عليه السلام Anamuomba Allah تعالى Amlete Mtume ﷺ.

Allah تعالى Ametaja dua ya Ibrahim عليه السلام kwa faida ya watu wa Eneo Takatifu (kuwapa ulinzi na chakula), na ilikamilishwa kwa kumuomba Allah تعالى Alete Mtume kutokana na kizazi chake. Dua ya Ibrahim عليه السلام ilikubaliwa na ikalingana na uteuzi wa Allah تعالى kuwa Muhammad ﷺ atumwe awe Nabii kwa *Ummiyyin* na kwa wote ambao si Waarabu, miongoni mwa Majini na Binadamu.

Hivyo, Ibrahim عليه السلام ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kumtambulisha Mtume ﷺ kwa watu. Kuanzia wakati huo, Muhammad ﷺ alifahamika kwa watu, hadi kwa Mtume wa mwisho kwa Wana wa Israeli, Isa mwana wa Maryam عليه السلام, ambaye alimtaja Muhammad ﷺ kwa jina. Isa عليه السلام aliwahutubia Wana wa Israeli kwa kusema,

إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْ مِنْ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي
 اسْمُهُ أَحْمَدُ

"Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninayethibitisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakayekuja baada yangu, jina lake ni Ahmad." (61:6)

Hii ndio sababu Mtume ﷺ alisema katika hadithi iliyopokelewa na Abu Umama عنه رضي الله عنه aliyesema: Nilimuuliza Mtume ﷺ, "Mwanzo wa Utume wako ulianza vipi?"

Mtume ﷺ akasema:

«دَعْوَةُ أَبِي إِبْرَاهِيمَ وَبُشْرَى عِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ»

“Dua ya baba yangu Ibrahim na bishara njema ya Isa mwana wa Maryam.”

Mtume ﷺ akazidi kubainisha,

«وَرَأَتْ أُمِّي أَنَّهُ خَرَجَ مِنْهَا نُورٌ أَضَاءَتْ لَهُ فُصُورُ الشَّامِ»

“Mama yangu aliona mwanga uliotoka kwake na ukaangaza maeneo ya Sham.”¹

Inasemekana kuwa mama yake Mtume ﷺ aliona mwanga alipokuwa mjamzito, alielezea tukio hilo kwa jamaa zake, na kisa hiki kikawa maarufu miongoni mwao. Mwanga uliotajwa katika Hadith ulionekana Sham (Syria Kuu), ikithibitisha litakalotokea baadaye wakati Dini ya Mtume ﷺ itakuwa imeenea katika maeneo ya Ash-Sham.

Hii ndiyo sababu, mwisho wa dunia Sham itakuwa kimbilio la Uislam na Waislam.

Pia, Isa mwana wa Maryam عليه السلام atashukia Sham, karibu na Mnara mweupe wa Mashariki mjini Damascus. Sahihi Mbili zimeeleza,

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقِّ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَدَلَهُمْ وَلَا مَنْ خَالَفَهُمْ حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَذَلِكَ» وفي صحيح البخاري «وَهُمْ بِالشَّامِ»

“Halitaacha kuwepo kundi katika Ummah wangu ambalo hupigania katika haki, halitadhuriwa na wale waliolitekeleza kundi hilo au kulipinga, mpaka Amri ya Allah ilikute katika hali hiyo.” Al-Bukhari aliongeza katika Sahihi yake, “Na watakuwa Sham.”¹

¹ Ahmad 5:262.

Maana ya Al-Kitab Wal – Hikmah.

Allah تعالى Amesema,

وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ

“Na awafundishe Kitabu.” Maana yake: Al-Qur’an.

وَالْحِكْمَةَ

“Al-Hikma” Maana yake: Sunnah kama Al-Hasan, Qatadah, Muqatil bin Hayyan na Abu Malik walivyoitetea hoja hiyo.² Pia imesemwa kuwa **“Al-Hikmah”** ina maana ya ufahamu wa Dini na maana zote ni sahihi. Ali bin Abu Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَيُرَكِّبُكُمْ

“Na awatakase.” Maana yake, “ni utiifu kwa Allah عزوجل.”³

إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٣٠﴾

“Hakika Wewe Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Ayah hii inaeleza kuwa Allah تعالى Anaweza Kufanya chochote, na hakuna kinachoweza kuepuka Uwezo Wake. Yeye ni Mwenye Hekima katika Vitendo Vyake na Kauli Zake, na Kuyaweka mambo mahali panapo nasibu kutokana na Elimu Yake, Hekima na Uadilifu.

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنِ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ سَفِهَ نَفْسَهُ ۚ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي

الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٣٠﴾ إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمِ ۗ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

وَوَصَّى بِهَا إِبْرَاهِيمَ بَيْنَهُ وَيَعْقُوبَ يَنْبِيُّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَى لَكُمْ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ

مُسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾

130. “Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini Sisi Tulimteua yeye

¹ Fat’hul Al-Bari 6:731 na Muslim 2:1524.

² Ibn Abu Hatim 1:390.

³ Ibn Abu Hatim 1:391.

katika dunia; na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.”

131. “Na Mola wake Mlezi Alipomuambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.”

132. “Na Ibrahim akawausia Wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuleteeni Dini hii; msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu.”

Haachi Mila ya Ibrahim عليه السلام, Isipokuwa Mpumbavu

Allah تعالى Alikanusha uzushi wa makafiri wa kumshirikisha Allah تعالى ili kuikengeuka Dini ya Ibrahim عليه السلام, kiongozi wa walioongoka. Siku zote Ibrahim alimpwekesha Allah تعالى katika ibada, kwa unyenyekevu, na hakuwaomba wengine isipokuwa Allah تعالى. Hakufanya Ushirikina, japo chembe ndogo. Aliwakanusha wote waliokuwa wakiabudiwa badala ya Allah تعالى na alijitenga na watu wake kuhusiana na ushirikina. Mtume Ibrahim عليه السلام alisema,

يَنْقُومِ إِيَّيَّ بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾ إِيَّيَّ وَجْهَتْ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ
وَالْأَرْضِ حَنِيفًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

“Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyafanyia Ushirikina. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawasawa kwa Aliyeziumba mbingu na ardhi, wala mimi si miongoni mwa Washirikina.” (6:78-79)

Aidha Allah تعالى Alisema,

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢٦﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ
سَيَّئِدِينَ ﴿٢٧﴾

“Na pale Ibrahim alipomuambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu. Isipokuwa Yule Aliyeniumba, kwani Yeye Ananiongoa.” (43:26-27) Na Allah تعالى Amesema,

وَمَا كَانَ لِإِبْرَاهِيمَ لِأُتَىٰ إِلَّا عَنْ مُوعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ
 لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ ۚ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١١٤﴾

“Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu.”
 (9:114) Na Allah تعالى Amesema,

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١١٤﴾ شَاكِرًا لِأَنْعَمِهِ ۚ
 أَجْتَبَهُ وَهَدَاهُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١١٥﴾ وَءَاتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿١١٦﴾

“Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, ni mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa Washirikina. Mwenye kuzishukuru Neema Zake Akamchagua na Akamuongoza katika njia iliyonyooka. Na Kumpa wema katika dunia; na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.” (16:120-122)

Ndio sababu Allah تعالى Amesema hapa,

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنِ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ

“Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim.” Maana yake: Anayeacha njia na utaratibu wake.

إِلَّا مَنْ سَفِهَ نَفْسَهُ ۚ

“Isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu?” Ina maana: Anaye idhulumu nafsi yake kwa kuacha ukweli na kufuata uovu. Mtu wa aina hiyo atakuwa anaacha njia ya yule aliyechaguliwa kuwa kiongozi katika dunia hii, toka alipokuwa mdogo, mpaka Allah تعالى Alipomchagua kuwa kipenzi (*Khalil*) Chake, na ambaye atakuwa miongoni mwa waliofuzu siku ya Kiyama. Kuna wazimu zaidi ya kuacha njia hii na kufuata upotevu? Je kuna udhalimu zaidi ya huu? Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الْفِرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿٣١﴾

“Kwani hakika ushirikina bila shaka ni dhuluma iliyo kubwa.” (31:13)

Abu Al-Aliyah na Qatadah walisema, Aya hii (2:130) iliteremshwa kuhusu Mayahudi ambao walizua mambo ambayo hayakutoka kwa Allah تعالى na yalikuwa kinyume na Dini ya Ibrahim عليه السلام.¹ Kauli ya Allah تعالى inathibitisha hilo,

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُّسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

﴿٣١﴾ إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاللَّهُ وَلِيُّ

الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣١﴾

“Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika Washirikina. Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata yeye na Nabii huyu na walioamini. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa Waumini.” (3:67-68) Na,

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمِ ۗ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

“Na Mola wake Mlezi alipomuambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.” (2:131)

Aya hii inadhihirisha kuwa Allah تعالى Alimuamrisha Ibrahim عليه السلام awe na Ikhlas Kwake, na atii na kujisalimisha Kwake; Ibrahim عليه السلام alishikamana na maamrisha ya Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى,

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ

“Na Ibrahim akawausia Wanawe, na pia Yaaqub.” Ina maana Ibrahim عليه السلام aliwaamrisha Wanawe kufuata Dini hii, ya Uislam kwa ajili ya Allah تعالى. Kama Kauli Yake Allah تعالى Inavyosema,

أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

“Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.”

¹ Ibn Abu Hatim 1:392.

Ina maana kuwa Mitume hawa waliyapenda sana maneno haya kiasi cha kuyahifadhi mpaka siku ya kifo chao na wakawausia watoto washikamane nayo baada ya kuondoka kwao. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema,

وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ

“Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake.” (43:28)

Yamkini Ibrahim عليه السلام aliwashauri watoto wake, pamoja na Ya'aqub عليه السلام, mtoto wa Is-haq عليه السلام ambao walikuwepo. Inaelekea, na Allah ni Mjuzi wa yote, kuwa Is-haq عليه السلام alijaaliwa kumpata Ya'aqub عليه السلام wakati wa uhai wa Ibrahim na Sarah, kwani bishara njema zinawajumuisha wote katika Kauli ya Allah تعالى,

فَبَشِّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿٧١﴾

“Basi Tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq na baada ya Is-haq, Ya'aqub.” (11:71)

Pia kama Ya'aqub عليه السلام hakuwa hai wakati huo, pasingekuwa na sababu ya kumtaja hapa hususan miongoni mwa watoto wa Is-haq عليه السلام. Aidha Allah تعالى Amesema ndani ya *Surat Al-Ankabut*,

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tulimtukia (Ibrahim) Is-haq na Ya'aqub. Na Tukajaalia katika dhuria zake Unabii na Kitabu.” (29:27) Aidha Amesema:

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً^ط

“Naye Tukampa Is-haq na Ya'aqub kuwa ni ziada (mjukuu)”. (21:72)

Hivyo, kuonesha kuwa haya yalijiri wakati wa uhai wa Ibrahim عليه السلام. Pia, Ya'aqub عليه السلام ndiye aliyejenga *Bayt Al-Maqdis*, kama Vitabu vya mwanzo vinavyohibitisha. Sahihi mbili zilinukuu kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema, “Niliuliza Ewe Mjumbe wa Allah! Msikiti gani ulijengwa kwanza?” Akajibu, “*Al-Masjid Al-Haram (Al-Ka'bah)*.” Nikauliza, “Kisha upi?” Akajibu, “*Bayt Al-Maqdis*”, Nikauliza, “Kuna muda gani baina ya Misikiti hiyo?” Akajibu, “Miaka Arobaini.”¹ Zaidi, wasia aliowapa Ya'aqub عليه السلام watoto wake, ambao tutautaja punde, unathibitisha ya kuwa Ya'aqub عليه السلام alikuwa miongoni mwa wale waliopokea usia uliotajwa katika Aya (2:130-132).

¹ Fat'hul al-Bari 6:469 na Muslim 1:370.

Kudumu na Tawhid (Kumpwekesha Allah تعالى) Mpaka Kufa.

Allah تعالى Amesema,

يَنْبِئُ إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَىٰ لَكُمْ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٢٧﴾

“Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuleteeni Dini hii; msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu.”

Ina maana, tekelezeni amali njema wakati wa uhai wenu na bakini katika njia hii, ili Allah تعالى Awape fadhila ya kufa na Dini hii. Kwa kawaida mtu hufia njia aliyoishi nayo na kufufuliwa na alichokufa nacho. Allah تعالى Mwingi wa Rehema Huwasaidia wale wanaoamua kufanya mema na kubaki katika njia adilifu. Kwa vyovyote vile haya hayaendi kinyume na Hadithi Sahih isemayo,

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا بَاعٌ أَوْ ذِرَاعٌ فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ فَيَدْخُلُهَا. وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا بَاعٌ أَوْ ذِرَاعٌ فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ فَيَدْخُلُهَا»

“Mtu anafanya amali za watu wa peponi mpaka iwe baina yake na pepo ni shubiri au dhira, basi Kitabu kitamtangulia (hatima), na akafanya amali za watu wa motoni na hivyo akauingia. Aidha mtu anaweza kufanya amali za watu wa Motoni mpaka iwe baina yake na Moto ni shubiri au dhira, kisha kitabu kitamtangulia (hatima) na akafanya amali za watu wa Peponi na hivyo akaiingia.”

Hakika imekuja katika baadhi ya riwaya nyingine katika hadithi hii isemayo, *“Mtu anaweza kufanya amali za watu wa peponi, lakini kwa mtazamo wa watu Na akafanya amali za watu wa motoni kwa mtazamo wa watu.”*

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿٩٩﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿١٠٠﴾ فَسَنِّيَرُهُ لِلْعُسْرَىٰ ﴿٩٧﴾ وَأَمَّا مَنْ

حَمَلَ وَاسْتَفْتَىٰ ﴿٩٨﴾ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿١٠١﴾ فَسَنِّيَرُهُ لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٠٢﴾

“Ama mwenye kutoa na akamcha Mungu. Na akaliafiki lililo jema. Tutamsahilishia yawe mepesi. Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja na wenzake. Na akakanusha lililo jema. Tutamsahilishia yawe mazito!” (92:5-10)

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ
 إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٢٧﴾
 تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٨﴾

133. "Je! Mlikuwapo yalipomfikia Ya'aqub mauti, Akawaambia Wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-haq, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu Kwake."

134. "Hao ni watu waliokwishapita. Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakayoyachuma; wala hamtaulizwa nyinyi waliyokuwa wakiyafanya wao."

Usia wa Ya'aqub عليه السلام kwa Watoto Wake Alipofikwa na Kifo.

Aya hii inaeleza masimango ya Allah تعالى dhidi ya wapagani wa Kiarabu miongoni mwa Wana wa Ismail عليه السلام pamoja na makafiri miongoni mwa Wana wa Israeli, ambaye ni Ya'aqub عليه السلام Mwana wa Is-haq عليه السلام, mtoto wa Ibrahim عليه السلام. Mauti yalipomjia Ya'aqub عليه السلام, aliwashauri watoto wake kumuabudu Allah تعالى Pekee bila mshirika. Aliwaambia,

مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ

"Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-haq."

Kumtaja Ismail عليه السلام hapa ni tamathali ya usemi, kwa sababu Ismail عليه السلام ni baba mkubwa wake Ya'aqub عليه السلام. An-Nahas alisema kuwa Waarabu wanamuita ami, baba, kama Qurtubi رحمه الله تعالى alivyotaja.¹

Aya hii imetumika kama ushahidi katika masuala ya mirathi kuwa babu anaitwa baba na anarithi kuwazuia ndugu kurithi anapokuwepo yeye, kama Abubakar رضي الله عنه alivyotilia nguvu hoja hiyo, kwa mujibu wa Bukhari aliyesimulia kauli ya Abubakar رضي الله عنه kutoka kwa Ibn Abbas na Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما. Al-Bukhari alitoa maelezo kuwa hakuna tofauti ya rai kuhusu somo

¹ Ar-Qurtubi 2:138.

² Fat'hul Al-Bari 12:19.

hili.² Hii pia ni rai ya Aishah رضي الله عنها, mama wa Waumini, Al-Hasan Al-Basri, Tawus na Ata Malik. Ama Ash-Shafi na Ahmad walisema katika kauli iliyo mashuhuri kuwa hugawana pamoja na ndugu katika mirathi. Ilipokelewa rai hii kwa njia yenye shaka kutoka kwa Umar, Uthman, Ali bin Masud, Zayd bin Thabit رضي الله عنهم na wanazuoni kadha miongoni mwa *Salaf* na vizazi vinavyofuatia. Kauli Yake Allah تعالى،

إِلَيْهَا وَاجِدًا

“Mungu mmoja tu.”

Maana yake: “Tunampwekesha Yeye katika Uungu Wake na hatumshirikishi na chochote au mtu yeyote.”

وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٢٧﴾

“Na sisi tunasilimu Kwake.”

Kwa unyenyekevu, Maana yake: Utii na kujisalimisha. Vile vile, Allah تعالى Amesema,

وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿١٢٨﴾

“Na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumtii Yeye kikipenda kisipende, na Kwake Yeye watarejeshwa.”
(3:83)

Kwa hakika, Uislam ni Dini ya Mitume wote, hata kama sheria pekee zilitofautiana. Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿١٢٩﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana muabudiwa isipokuwa Mimi. Basi Niabuduni Mimi tu.” (21:25)

Kuna Aya na Hadithi nyingi kuhusu mada hii. Kwa mfano, Mtume ﷺ alisema,

«نَحْنُ مَعَشَرَ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عَالَمٍ دِينُنَا وَاجِدٌ»

“Sisi jopo la Mitume, ni kama ndugu wa mama tofauti, Dini yetu ni moja.”

Allah تعالى Amesema,

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ

“Hao ni watu waliokwisha pita.”

Maana yake: Waliishi kabla enzi zako.

لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلكُمْ مَا كَسَبْتُمْ

“Watapata waliyoyachuma, nanyi mtapata mtakayoyachuma.”

Ayah hii inatangaza, uhusiano na Mitume au watu wema miongoni mwa mababu zako hawatokusaidia, isipokuwa utakapofanya mema ambayo yatakuletea manufaa ya kidini. Wao wana amali zao na wewe una zako.

وَلَا تَسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Wala hamtaulizwa nyinyi waliyokuwa wakiyafanya wao.”

Hii ndio sababu Hadithi imebainisha,

«مَنْ بَطَأَ بِهِ عَمَلُهُ لَمْ يُسْرِعْ بِهِ نَسَبُهُ»

“Yeyote ambaye hesabu ya amali zake zinafanywa polepole, hatopata wepesi kwa hesabu ya ukoo wake.”¹

وَقَالُوا كُونُوا هُودًا أَوْ نَصْرَىٰ يَهْتَدُوا ۗ قُلْ بَلْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَمَا كَانَ مِنَ

الْمُشْرِكِينَ

“Na wakasema: Kuweni Mayahudi au Wakristo ndio mtaongoka. Sema: Bali tunashika mila ya Ibrahim mwongofu, wala hakuwa katika Washirikina.” (2:135)

Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما alipokea kuwa Ibn Abbas رحمه الله تعالى alisema kuwa, Abdullah bin Suriya Al-A'war alimuambia Mtume ﷺ, “Muongozo ni ule tu sisi (Mayahudi) tunaoufuata. Kwa hiyo, tufuate sisi, Ewe Muhammad, na

¹ Muslim 4:2074.

² Ibn Abu Hatim 1:396. Isnadi yake dhaifu.

utaongozwa njia sahihi." Pia, Wakristo walisema kama hayo. Hivyo Allah تعالى Aliteremsha,

وَقَالُوا كُونُوا هُودًا أَوْ نَصَارَى يَهْتَدُوا^١

"Na wakasema: Kuweni Mayahudi au Wakristo ndio mtaongoka."

Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ بَلَّ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا^٢

"Sema: Bali tunashika mila ya Ibrahim mwongofu."

Ina maana, "Hatuhitaji Uyahudi au Ukristo unaotulingania, bali,

مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا^٣

"Tunashika mila ya Ibrahim mwongofu"

Maana yake: Katika njia iliyonyooka kama Muhammad bin Ka'b Al-Quradhi na Isa bin Jariyah walivyosema.² Abu Qilabah alisema *hanif* ndiyo walivyoamini Manabii kutoka mwanzo mpaka mwisho.

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 1:397.

² Ibn Abu Hatim 1:397.

وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ
وَيُرِيدُونَ أَنْ يُتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٥١﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَقًّا

“Na wanataka kufarakisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kuchukua njia iliyo katikati ya haya. Hao ndio makafiri kweli.” (4:150-151)

Bukhari alisimulia kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Watu wa Kitabu walikuwa wakisoma Taurati kwa Kiebrania na kuifasiri kwa lugha ya Kiarabu kwa Waislamu.” Mtume ﷺ alisema,

«لَا تُصَدِّقُوا أَهْلَ الْكِتَابِ وَلَا تُكَذِّبُوهُمْ وَتَقُولُوا: آمَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا»

“Msiwasadikishe watu wa Kitabu, wala msiwakadhibishe. Na semeni, “Tunamuamini Allah na tulichoteremshiwa.”¹

Aidha, Muslim, Abu Dawud na An-Nasai walinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alikuwa “Mara kwa mara, alikuwa akisoma katika rakaa mbili za kabla ya Sala ya Alfajiri,

ءَامِنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا

“Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa sisi.” (2:136)

Aidha Kauli Yake Allah تعالى،

ءَامِنَّا بِاللَّهِ وَأَشْهَدُ بِأَنَا مُسْلِمُونَ ﴿٣٥﴾

“Tumemuamini Mwenyezi Mungu na shuhudia kwamba sisi hakika ni Waislamu.” (3:52)

Wakati wa kusali Rakaa mbili kabla ya Fajr.²

¹ Fat’hul Al-Bari 8:20.

² Muslim 11:502, Abu Dawud 2:46, An-Nasai katika Al-Kubra 6:339.

Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi na Qatadah walisema, “*Al-Asbat* ni watoto kumi na wawili wa Ya’aqub na kwamba kila mmoja alipata ummah uliotokana na vizazi vyao. Kwa sababu hii waliitwa *Al-Asbat*.”¹ Al-Khalil na wengineo walisema, “*Al-Asbat* katika Wana wa Israel ni kama makabila miongoni mwa Wana wa Israel, ina maana kuwa *Asbat* ni makabila mbalimbali ya Wana wa Israel, miongoni mwao, Allah ﷻ Alipeleka Mitume kadha kwao wao.” Musa عليه السلام aliwaambia Wana wa Israel,

أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِيكُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُلُوكًا

“Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, Alipowateua Manabii kati yenu, na Akakufanyeni watawala.”

(5:20) Pia,

وَقَطَعْنَهُمْ أَنْتَى عَشْرَةَ أَسْبَاطًا

“Na Tuliwagawanya katika makabila kumi na mawili.” (7:160)

Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema, “*Sibt* ni kundi la watu au kabila linalotokana na kizazi kimoja (mababu).”²

Qatadah alisema, “Allah تعالى Aliwaamrisha waumini wamuamini Yeye na Vitabu Vyake vyote na Manabii.”³ Pia Sulayman bin Habib alisema, “Tumeamrisha kuamini Taurati na Injili (za asili) lakini sio kutekeleza mafundisho yake.”⁴

فَإِنْ ءَامَنُوا بِمِثْلِ مَا ءَامَنْتُمْ بِهِ فَقَدِ اهْتَدَوْا ۗ وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا هُمْ فِي شِقَاقٍ ۗ

فَسَيَكْفِيكَهُمُ اللَّهُ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٧٧﴾ صِبْغَةَ اللَّهِ ۗ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ

صِبْغَةً ۗ وَنَحْنُ لَهُ عَابِدُونَ ﴿١٧٨﴾

137. “Basi wakiamini kama mnavyoamini nyinyi, itakuwa kweli wameongoka. Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani tu. Na Mwenyezi Mungu Atakutosheni kukukingeni na shari yao, na Yeye Ndiye Msikizi, Mjuzi.”

¹ Ibn Abu Hatim 1:399.

² Ar-Qurtubi 2:141.

³ Ibn Abu Hatim 1:400.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:400.

138. "Hili ni pambo la (Uislamu) Mwenyezi Mungu, na nani aliye mbora wa kupamba kuliko Mwenyezi Mungu? Na sisi ni wenye kumuabudu Yeye tu."

Allah تعالى Amesema, endapo, makafiri miongoni mwa Watu wa Kitabu na makafiri wengine, wanaamini Vitabu Vyote vya Allah تعالى na Mitume wote na wasiwatofautishe kati yao,

فَقَدْ أَهْتَدَوْا^ط

"Itakuwa kweli wameongoka."

Maana yake: Watakuwa wamepata ukweli na wakaongozwa kuufikia.

وَإِنْ تَوَلَّوْا

"Na wakikengeuka."

Kutoka kwenye ukweli kwenda kwenye upotofu hata baada ya ushahidi kufikishwa kwao.

فَأِنَّمَا هُمْ فِي شِقَاقٍ فَسَيَكْفِيكَهُمُ اللَّهُ^ط

"Basi wao wamo katika upinzani tu. Na Mwenyezi Mungu Atakutosheni Kukukingeni na shari yao."

Maana yake: Allah تعالى Atawasaidia Waumini dhidi yao.

وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٣٨﴾

"Na Yeye Ndiye Msikizi, Mjuzi."

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Ziyad bin Yunus kutoka kwa Ibn Abuu Nuaym amesema: Baadhi ya watawala walileta kwangu chapa ya msahafu wa Uthman bin Affan رضي الله عنه, kwa ajili ya kuuhakiki. Ziyad anasema: Na kamuambia watu wanasema: Hakika chapa ya msahafu wa Uthman رضي الله عنه alikuwa nayo mapajani mwake wakati alipouawa, hivyo damu yake ikaingia. Nafii akasema: 'Damu hiyo nimeiona kwa macho yangu.'

صِبْغَةَ اللَّهِ^ط

"Hiyo ndiyo Sibghah ya Mwenyezi Mungu."

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitolea maelezo, “Dini ya Allah تعالى.”¹ Tafsir hii ilipokewa na; Mujahid, Abu Al-Aliyah, Ikrimah, Ibrahim, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Abdullah bin Kathir, Atiya Al-Awfi, Ar-Rabi bin Anas, As-Suddi na wanazuoni wengine.²

قُلْ أَتَحَاجُّونَنَا فِي اللَّهِ وَهُوَ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ وَلِنَا أَعْمَلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ وَنَحْنُ لَهُ مُخْلِصُونَ
 ﴿١٣٩﴾ أَمْ تَقُولُونَ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَشْبَاطَ كَانُوا هُودًا
 أَوْ نَصَارَىٰ قُلْ ءَأَنْتُمْ أَعْلَمُ أَمِ اللَّهُ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَتَمَ شَهَادَةً عِنْدَهُ مِنَ اللَّهِ وَمَا
 اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا نَعْمَلُونَ ﴿١٤٠﴾ تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ وَلَا
 تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤١﴾

139. “Sema: Mnahojiana nasi juu ya Mwenyezi Mungu, Naye ni Mola wetu Mlezi na Mola wenu Mlezi, na sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu? Nasi tunamsifia Yeye tu.”

140. “Au mnasema kuwa Ibrahim na Ismail na Is-haq na Ya’aqub na Wajukuu zao walikuwa Mayahudi au Wakristo? Sema: Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule aliyeficha ushahidi alionao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na hayo myafanyayo.”

141. “Hao ni watu waliokwishapita. Wao watapata waliyo yachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma, wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyokuwa wakifanya wao.”

Allah تعالى Alimuelekeza Mtume ﷺ kuwatangulia washirikina kwa hoja:

قُلْ أَتَحَاجُّونَنَا فِي اللَّهِ

“Sema: Mnahojiana nasi juu ya Mwenyezi Mungu”.

¹ Ibn Abu Hatim 1:402.

² Ibn Abu Hatim 1:402.

Mnahojiana nasi kuhusu Umoja na Upekee wa Allah تعالى, utii na kujisalimisha Kwake na kujikanya na Alivyoharamisha,

وَهُوَ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ

“Naye ni Mola wetu Mlezi na Mola wenu Mlezi”.

Maaana yake: Ana Udhhibiti thabiti juu yetu na nyinyi, na Anastahili Kuabudiwa Peke Yake bila mshirika.

وَلَنَّا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ

“Na sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu?”

Maana yake: Tunawakanusha na mnachokiabudu, kama mnavyotukanusha. Allah تعالى Amesema katika Aya nyengine,

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ أَنْتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا

تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

“Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina amali yangu, na nyinyi mna amali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo”. (10:41)

Aidha Amesema,

فَإِنْ حَاجُّوكَ فَقُلْ أَسَلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ اتَّبَعَنِ

“Na pindi wakikuhoji (Muhammad), basi sema: Mimi nimeusalimisha uso wangu kumuelekea Mwenyezi Mungu, na kadhalika walionifuata”. (3:20)

Na Amesema Allah تعالى katika Kumuelezea Ibrahim عليه السلام,

وَحَاجَّهُ قَوْمُهُ قَالَ أَتُحْتَجُّونِي فِي اللَّهِ

“Na watu wake wakamhoji Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu”. (6:80)

Aidha Amesema,

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِي حَاجَّ إِبْرَاهِيمَ فِي رَبِّهِ

“Hukumuona yule aliyehojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi”. (2:258)

Alisema katika Aya tukufu,

وَلَنَا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ وَنَحْنُ لَهُ مَخْلُصُونَ ﴿٢٥٨﴾

“Na sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi mna vitendo vyenu? Nasi tunamsifia Yeye tu”.

Maana yake: Sisi tupo kinyume na nyinyi, kama ambavyo nyinyi mpo kinyume na sisi.

وَنَحْنُ لَهُ مَخْلُصُونَ ﴿٢٥٨﴾

“Nasi tunamsifia Yeye tu”.

Maana yake: Katika ibada na utii. Kisha Allah تعالى Aliwakosoa kwa madai yao kuwa Ibrahim عليه السلام, na Mitume waliokuja baada yake na Asbat walikuwa wafuasi wa dini yao, wawe ni Mayahudi au Wakristo. Allah تعالى Amesema,

قُلْ ءَأَنْتُمْ أَعْلَمُ أَمِ اللّٰهُ

“Sema: Mnahojiana nasi juu ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Allah تعالى ni Mjuzi zaidi na Ameerza kuwa hawakuwa Mayahudi, wala Wakristo. Kadhalika Allah تعالى Amesema katika Aya,

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُّسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٢٥٨﴾

“Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika Washirikina”. (3:67)

Na Aya inayofuata. Pia Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَتَمَ شَهَادَةَ عِنْدَهُ مِنْ أَللّٰهِ

“Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule aliyeficha ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu?”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Walikuwa wakisoma Kitabu cha Allah تعالى Alichowateremshia kinachoeleza kuwa Dini ya kweli ni Uislamu na kuwa Muhammad ni Mtume . Kitabu chao pia kimeeleza kuwa Ibrahim عليه السلام, Ismail عليه السلام, Is-haqi عليه السلام, Ya’aqub عليه السلام na makabila hawakuwa Mayahudi wala Wakristo. Walithibitisha ukweli huu lakini waliwaficha watu.” Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٣٦﴾

“Na Allah si Mwenye Kughafilika na hayo myafanyayo.”

Ni tishio na onyo kuwa Elimu Yake imevienea vitendo vya kila mmoja na Atawalipa kila mmoja kwa mujibu wa amali yake. Kisha Allah تعالى Akasema,

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ ط

“Hao ni watu walio kwisha pita”. Maana yake: Walikuwepo kabla yenu,

هَذَا مَا كَسَبْتُمْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ ط

“Wao watapata waliyoyachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma”.

Maana yake: Wao wana amali zao, nanyi mna zenu.

وَلَا تَسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٧﴾

“Wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyokuwa wakifanya wao.”

Maana yake: Haitoshi kuwa nyinyi ni jamaa zenu, mpaka mtakapoiga amali zao njema. Zaidi msihadaike na ukweli kuwa nyinyi ni vizazi vyao mpaka mtakapowaiga katika kutii Amri za Allah تعالى na kuwafuata Mitume Wake ambao walitumwa kuwa waonyaji na wawabashirie habari njema. Kwa hakika, yeyote asiyemuamini hata Mtume mmoja, atakuwa amewakanusha Mitume wote, hususan mtu akimkanusha Mtukufu wa Manabii na Mwisho wa Mitume, na mjumbe wa Mola wa viumbe wote kwenda kwa binadamu wote na Majini. Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake Muhammad ﷺ na baki ya Mitume wote wa Allah تعالى.

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 1:405.

* سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ مَا وَلَّيْنَاهُمْ عَن قِبَلَتِنَا الَّتِي
 كَانُوا عَلَيْهَا قُلْ لِلَّهِ الشَّرْقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَى
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾ وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا
 لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ
 شَهِيدًا ۗ وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَن
 يَتَّبِعَ الرَّسُولَ مِمَّن يَنْقَلِبُ عَلَى عَقْبَيْهِ ۗ وَإِن كَانَتْ لَكَبِيرَةً
 إِلَّا عَلَى الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضَيِعَ إِيمَانَكُمْ ۗ
 إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرُؤُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤٣﴾ قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ
 وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ۗ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا ۗ فَوَلِّ وَجْهَكَ
 شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ
 شَطْرَهُ ۗ وَإِنِّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِن
 رَبِّهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٤﴾ وَلَئِن أَتَيْتَ
 الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ بِكُلِّ آيَةٍ مَّا تَبِعُوا قِبْلَتَكَ ۗ وَمَا أَنْتَ
 بِتَابِعٍ قِبْلَتِهِمْ ۗ وَمَا بَعْضُهُمْ بِتَابِعٍ قِبْلَةَ بَعْضٍ ۗ وَلَئِن آتَبَعْتَ
 أَهْوَاءَهُمْ مِّن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۗ إِنَّكَ إِذًا لَمِنَ
 الظَّالِمِينَ ﴿١٤٥﴾

* سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ مَا
 وَلَّيْنَاهُمْ عَن قِبَلَتِنَا الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا
 قُلْ لِلَّهِ الشَّرْقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَن
 يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾
 وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا
 لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ
 وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا ۗ وَمَا
 جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا
 لِنَعْلَمَ مَن يَتَّبِعَ الرَّسُولَ مِمَّن يَنْقَلِبُ
 عَلَى عَقْبَيْهِ ۗ وَإِن كَانَتْ لَكَبِيرَةً إِلَّا
 عَلَى الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ
 لِيُضَيِعَ إِيمَانَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ
 لَرُؤُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤٣﴾

142. "Wapumbavu mio-
 ngoni mwa watu wata-
 sema: Nini kilicho wageuza
 wao kutoka kibla chao wali-
 chokuwa wakikielekea?
 Sema: Mashariki na

Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye Humuongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka."

143. "Na vivyo hivyo Tumekufanyeni muwe Umma wa kati na kati (muadilifu), ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kibla ulichokuwa nacho ila Tupate Kumjua yule

anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye kuipoteza Imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye Kuwarehemu.”

Kubadilishwa Qiblah:

Imam Bukhari aliandika kuwa Al-Bara bin Azib رضى الله عنه alisimulia “Mtume ﷺ alisali akielekea upande wa *Bayt Al-Maqdis* (Jerusalem) kwa miezi kumi na sita au kumi na saba, lakini alipendelea kama angeelekea upande wa Ka’bah. Na Sala ya kwanza kusali ilikuwa Alasiri akiwa pamoja na baadhi ya watu. Mmoja kati ya wale waliosali na Mtume ﷺ alitoka na akawakuta watu wakisali ndani ya Masjid wakiwa katika Rukuu’ huku wakiwa wameelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*. Aliwasemesha, ‘*Wallahi*’ Nashuhudia kuwa nimesali na Mtume ﷺ akielekea upande wa Makkah (*Ka’abah*). Waliposikia maneno hayo, watu wale walibadili mwelekeo mara moja kuelekea upande wa Nyumba Tukufu (*Ka’aba*) wakati wakiwa katika hali ile ile ya (Rukuu’). Kuna baadhi ya Waislamu ambao walikuwa wakisali wakielekea upande wa Kibla cha zamani (Jerusalem) kabla ya kubadilishwa kuelekea upande wa Nyumba Tukufu (*Ka’aba*) Makkah na tayari walikuwa wamefariki au walikuwa mashahidi, na hatukujua la kusema juu yao (khusus kuelekea upande wa Jerusalem wakati wa Sala). Kisha Allah تعالى Akateremsha Aya,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضَيِّعَ إِيمَانَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿١٤٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuipoteza Imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye Kuwarehemu.” (2:143)

Kwa njia hii ameipokea Al-Imamu Bukhari¹ na wakati Muslim² alikusanya kwa kutumia silsila nyingine ya upokezi. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alitaarifu kuwa Al-Bara alisimulia. Mtume ﷺ alikuwa akielekea upande wa *Bayt Al-Maqdis* (Jerusalem) wakati wa Sala, lakini akiangalia angalia mbinguni akisubiri Amri ya Allah تعالى ya kubadili Kiblah. Kisha Allah تعالى Akateremsha,

¹ Fat’hul Al-bari 8:20.

² Muslim 1:375.

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ط فَلَنَوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا ء

“Kwa yakini Tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi Tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho.” (2:144)

Mtu mmoja miongoni mwa Waislamu alisema, “Tunatamani kujua habari za wale waliofariki kabla ya kubadilishwa Kiblah (yaani kuelekea upande wa Makkah) na pia kuhusu Sala zetu, tulikuwa tunasali kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*. Kisha Allah تعالى Akateremsha,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ ء

“Na Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuipoteza Imani yenu.” (2:143)

Watu wapumbavu, yaani Watu wa Kitabu (Mayahudi na Wakristo) walisema, “Kitu gani kilichowafanya wabadilisha Kiblah walichokuwa wakikielekea?” Kisha Allah تعالى Akateremsha,

❖ سَيَقُولُ السُّفَهَاءُ مِنَ النَّاسِ

“Wapumbavu miongoni mwa watu watasema.” (2:142) mpaka mwisho wa aya.¹

Ali bin Abu Talhah alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: Mtume ﷺ alipohamia Madinah, Allah تعالى Alimuamrisha kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis* (Jeruselem). Mayahudi wakafurahi wakati huo. Nabii wa Allah alielekea upande wa Jeruselem kwa zaidi ya miezi kumi. Hata hivyo, alipenda kuelekea wakati wa Sala, Kiblah cha Mtume Ibrahim عليه السلام (*Ka'bah* – Makkah) na Allah تعالى kwa munasaba wa suala hili Aliteremsha,

قَوْلٍ وَجْهِكَ شَطَرَ

“Elekezeni Nyuso zenu upande huo.”

Ina maana, mwelekeo wake, Mayahudi wakawa na shaka nalo hilo wakasema, “Kitu gani kilichowafanya kubadili Kiblah walichokuwa wakielekea (yaani Jeruselem)?” Allah تعالى Aliteremsha:

¹ Al-Qurtubi 3:133.

قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾

“Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye Humuongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.” (2:142)¹

Kuna Hadithi nyingi juu ya somo hili. Kwa mukhtasari, Mtume ﷺ aliamrishwa kuelekea *Swakhra* - upande wa *Bayt Al-Maqdis*. Kwani Mtume ﷺ alipokuwa Makka alisali kati ya nguzo mbili, na Ka’aba inakuwa mbele yake huku anaelekea *Bayt Maqdis*.² Alipohamia Madinah, utaratibu huu wa kuvielekea vyote viwili kwa pamoja haukuwezekena; hivyo Allah تعالی Alimuamrisha asali kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengi wa wanazuoni walivyosema.

Bukhari aliandika ndani ya Sahih yake kutoka kwa Baraa bin Azib رضي الله عنه kuwa habari za mabadiliko ya Kiblah ilifikishwa kwa baadhi ya Ansar wakati wakisali Alasiri huku wakielekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*. Baada ya kusikia hivyo, walibadili mwelekeo mara moja na kuelekea upande wa *Ka’ba*.³ Imenukuliwa katika Sahih Mbili (Bukhari na Muslim) kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisimulia. Watu walipokuwa *Quba* (Masjid) wakisali *Fajr*, alikuja mtu na kusema, “Qur’an imeteremshwa kwa Mtume ﷺ usiku na ameamriwa aelekee *Ka’aba*. Kwa hiyo elekeeni *Ka’aba*. Walikuwa wameelekea upande wa Ash-Sham, hivyo wakaelekea *Ka’aba*.⁴

Hadithi hizi zinathibitisha kuwa hukumu ya *Nasikh* (kuondosha hukumu nyingine) haifanyi kazi ila baada ya kuifahamu. Hata kama *Nasikh* ilikuwa imeshateremshwa au imetangazwa. Hili ndio sababu Masahaba waliotajwa hapo juu hawakutakiwa kurudia Sala za *Alasiri*, *Maghrib* na *Isha* (japokuwa Kiblah kilishabadilishwa). Allah تعالی Ndiye Mjuzi wa yote.

Yalipotokea mabadiliko ya Kiblah (kuelekea upande wa Makkah) wale wenye unafiki na wasioamini; na makafiri wa kiyahudi, wote walipotoshwa kutoka kwenye mwongozo sahihi na wakachanganyikiwa. Wakasema

¹ Al-Tabari 3:133.

² Hili linapingana na kilichothibitishwa na Bukhari pindi Mtume ﷺ aliposali sehemu iitwayo Al-Hatwiim pindi alipokuwa Makka (Angalia Hadithi Na. 3856).

³ Al-Bukhari Na. 399. Watu hawa walikuwa wanatoka katika kabila la Banu Salamah na walikuwa wakikaa jirani na Msikiti wa Qiblatain.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:24 na Muslim 1:375.

مَا وَلَّهُمْ عَن قِبَلِهِمُ الَّذِينَ كَانُوا عَلَيْهَا^٤

“Nini kilichowageuza kutoka Qibla chao walichokuwa wakikielekea?” (2:142)

Wakauliza, “Hawa watu (Waislamu) wana matatizo gani kwani mara wanaelekea upande wa Jeruselem na mara wanaelekea upande wa Makkah.” Allah تعالى Aliyajibu maswali haya Aliposema:

قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ^٥

“Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu.” (2:142)

Maana yake: Amri, Uamuzi na Mamlaka ni Yake Allah تعالى Pekee. Hivyo:

فَأَيَّمَا تُولُوا فَتَمَّ وَجْهُ اللَّهِ^٥

“Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu Yupo?” (2:115),

❖ لَيْسَ الْبِرُّ أَنْ تُولُوا وُجُوهَكُمْ قَبْلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ

“Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu.” (2:177)

Kauli hii ina maana kuwa amali bora ni kutii Amri za Allah تعالى. Hivyo, upande wowote Anakotuamrisha kuelekea, lazima tuelekee huko, kwani, utiifu unapatikana kwa kutekeleza Amri za Allah تعالى, kama kila siku Atatuamrisha kuelekea upande tofauti, sisi ni waja Wake na ni watiifu Kwake, na tutaelekea upande wowote Atakaotuamuru tuuelekee. Kwa hakika, Huruma ya Allah تعالى kwa mja na Mjumbe wake Muhammad ﷺ na kwa Ummah wake (Taifa la Kiislamu) ni mkubwa sana. Ndiyo maana Allah تعالى Amewaongoza kwenye *Kiblah* cha (Mtume) Ibrahim – mwandani wa Allah (*Khalili* عليه السلام). Amewaamrisha waelekee upande wa *Ka'aba*, Nyumba Takatifu kuliko zote zilizoko juu ya uso wa dunia, ambayo ilijengwa na Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام kwa Jina la Allah تعالى, Asiye na mshirika. Hii ndio sababu Allah تعالى Alisema baadaye:

قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٨٧﴾

“Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye Humuongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka” (2:142)

Imam Ahmad alitaarifu kuwa Aisha (mke wa Mtume) رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alizungumzia juu ya Watu wa Kitabu (Mayahudi na Wakristo).

«إِنَّهُمْ لَا يَحْسِدُونَ عَلَيَّ شَيْءٍ كَمَا يَحْسِدُونَ عَلَيَّ يَوْمَ الْجُمُعَةِ الَّتِي هَدَانَا اللَّهُ لَهَا وَضَلُّوا عَنْهَا وَعَلَى الْقِبْلَةِ الَّتِي هَدَانَا اللَّهُ لَهَا وَضَلُّوا عَنْهَا وَعَلَى قَوْلِنَا خَلْفَ الْإِمَامِ: آمِينَ»

"Hawatuonei inda kwa jambo lolote kama wanavyotuonea inda kwa Ijumaa ambayo Allah Ametupa hidaya na Kutuongoza kwayo na wao wakapotoshwa kutokana nayo, na kwa Kiblah ambacho Allah Ametuongoza kwacho na wao walipotoshwa kutokana nacho na wanatuonea Inda kwa kusema kwetu, "Amin" nyuma ya Imam.¹

Ubora wa Umma wa Muhammad ﷺ.

Allah تعالى Amesema,

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا

"Na vivyo hivyo Tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu..."
(2:143)

Allah تعالى Ameeleza kuwa, kwa hakika Tumekubadilishieni ili mfate Kiblah cha Ibrahim عليه السلام na Tumekuchagulieni Kiblah hicho ili Tukufanyeni muwe bora kuliko Ummah wote uliotangulia. Hivyo mtakuwa mashahidi juu ya mataifa siku ya Kiyama. Kwani wote ni wenye kukiri kuhusiana na utukufu wenu. Neno *Wasat* hapa, limetumika kwa maana ya ubora au uzuri wa juu zaidi. Kama inavyosemwa: kuwa (kabila la) Maqurayshi ni kabila la *Wasat* miongoni mwa Makabila ya Waarabu kwa nasaba na eneo, ina maana ndilo bora kabisa. Vile vile Mtume ﷺ alikuwa katika *Wasat* wa watu wake, ina maana alikuwa anatokana na ukoo bora. Pia Alasiri, Sala inayoelezwa kuwa ya '*Wusta*' (mnyambulisho wa neno *Wasat*), ina maana ya Sala bora kabisa, kama Hadithi sahihi zilivyothibitisha hilo. Na kwa kuwa Allah تعالى Aliufanya Ummah (Taifa

¹ Ahmad 6:134.

la Waislamu) ni Wasat, Ameupa Sharia iliyokamilika, Manhaj bora na Madhhabi (mfumo) ulio wazi. Allah تعالى Amesema,

هُوَ أَحَبُّكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۚ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ ۗ هُوَ سَمُّكُمْ
 الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ ۗ

“Yeye Amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahim. Yeye (Mwenyezi Mungu) Alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur’ani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu.” (22:78)

Zaidi, Imam Ahmad alitaarifu kuwa Abu Said رضي الله عنه alisimulia: Mtume ﷺ alisema.

«يُدْعَى نُوحُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، فَيَقَالُ لَهُ: هَلْ بَلَّغْتَ؟ فَيَقُولُ: نَعَمْ، فَيُدْعَى قَوْمُهُ فَيَقَالُ لَهُمْ: هَلْ بَلَّغْتُمْ فَيَقُولُونَ: مَا آتَانَا مِنْ نَذِيرٍ وَمَا آتَانَا مِنْ أَحَدٍ، فَيَقَالُ لِنُوحٍ: مَنْ يَشْهَدُ لَكَ؟ فَيَقُولُ: مُحَمَّدٌ وَأُمَّتُهُ، قَالَ فَذَلِكَ قَوْلُهُ: ﴿وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا﴾ قَالَ: وَالْوَسْطُ الْعَدْلُ، فَتُدْعَوْنَ فَتَشْهَدُونَ لَهُ بِالْبَلَاغِ ثُمَّ أَشْهَدُ عَلَيْكُمْ»

“Nuhu ataitwa siku ya Kiyama, na ataulizwa, ‘Je, umefikisha (Ujumbe)?’ Atajibu, ‘Ndiyo.’ Wataitwa watu wake na wataulizwa, ‘Je, Nuhu amefikisha (Ujumbe) kwenu?’ Watajibu, ‘Hakuna muonyaji aliyetujia wala hakuna aliyetumwa kwetu.’ Nuhu ataulizwa, ‘Unaye shahidi?’ Atasema, ‘Muhammad na Ummah wake.’

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema,

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا

“Na vivyo hivyo Tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani.” (2:143)

Mtume ﷺ alisema *“Wasat maana yake Adl (Uadilifu), utaitwa (kuthibitisha) kutoa ushahidi kuwa Nuh alifikisha (Ujumbe wake). Nami Nitathibitisha ushahidi huo juu yenu.”*¹ Ilinukuliwa pia na Bukhari, At-Tirmidhi, An - Nasai na Ibn Majah.²

¹ Ahmad 3:32.

² Fat’h Al-Bari 8:21, Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:297 An-Nasai. Katika Al-Kubra 6:292: Bin Maja 2:432.

Pia Imam Ahmad alitaarifu kuwa Abu Said Khudhri رضي الله عنه alisimulia: Mtume
 ﷺ amesema,

«يَجِيءُ النَّبِيُّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمَعَهُ الرَّجُلَانِ وَأَكْثَرُ مِنْ ذَلِكَ هِيدَعَى قَوْمَهُ، فَيَقَالُ: هَلْ
 بَلَّغْتُمْ هَذَا؟ فَيَقُولُونَ: لَا فَيَقَالُ لَهُ: هَلْ بَلَّغْتَ قَوْمَكَ؟ فَيَقُولُونَ: نَعَمْ، فَيَقَالُ: مَنْ
 يَشْهَدُ لَكَ؟ فَيَقُولُونَ: مُحَمَّدٌ وَأُمَّتُهُ، فَيُدْعَى مُحَمَّدٌ وَأُمَّتُهُ، فَيَقَالُ لَهُمْ: هَلْ بَلَّغَ هَذَا
 قَوْمَهُ؟ فَيَقُولُونَ: نَعَمْ، فَيَقَالُ: وَمَا عَلِمْتُمْ؟ فَيَقُولُونَ: جَاءَنَا نَبِيًّا ﷺ فَأَخْبَرَنَا أَنَّ
 الرَّسُلَ قَدْ بَلَّغُوا، فَذَلِكَ قَوْلُهُ عَزَّ وَجَلَّ: ﴿وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا﴾ قَالَ: عَذَلَا
 ﴿وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا﴾

“Mtume mmojawapo atakuja siku ya Kiyama akiwa na wafuasi wawili au zaidi. Watu wake nao wataitwa na kuulizwa, ‘Je, Mtume wenu amefikisha ujumbe.’ Watajibu, ‘Hapana.’ Ataulizwa (Mtume wao), ‘Je umefikisha (ujumbe) kwa watu wako?’ Atajibu, ‘Ndiyo.’ Ataulizwa, ‘Nani shahidi yako?’ Atajibu, ‘Muhammad na Ummah wake,’ Muhammad na Ummah wake wataitwa na kuulizwa, ‘Je Amefikisha (ujumbe) kwa watu wake?’ “Watajibu, ‘Ndio.’ Wataulizwa, ‘Mmejuaje jambo hilo?’ Watasema, ‘Mtume wetu (Muhammad) alikuja kwetu na akatuambia kuwa Manabii wamefikisha (ujumbe wao).”

Hivyo Kauli ya Allah تعالى:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا

“**Na hivyo Tumekufanyeni muwe Ummah wa wastani (wasat).**” Akasema,
 “(Maana yake) *Adl Umma Muadilifu.*” (Kisha akaendelea kusoma Aya),

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ
 شَهِيدًا¹

“**Na hivyo hivyo, Tumekufanyeni muwe Ummah wa wastani (wasat) ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume Muhammad awe ni shahidi juu yenu**”.¹

Zaidi ya hayo, Imam Ahmad alitaarifu kuwa Abdul – Aswad alisimulia nilifika Madina na kukuta ugonjwa wa kuambukiza ambao ulisababisha maafa

¹ Ahmad 3:58.

makubwa. Nilikaa karibu na Umar bin Al-Khattab رضى الله عنه lilipita jeneza watu wakamtaja kwa heri maiti yake. Umar رضى الله عنه alisema “*Wajabat, Wajabat!*” Jeneza lingine likapita watu wakasema vibaya maiti yake. Umar رضى الله عنه akasema tena, “*Wajabat.*” Abdul Aswad akauliza, “*Wajabat ni nini Ewe kiongozi wa wumini?*” Akajibu, “Nimesema kama Mtume ﷺ alivyosema

«أَيُّمَا مُسْلِمٍ شَهِدَ لَهُ أَرْبَعَةٌ بِخَيْرٍ أَدْخَلَهُ اللَّهُ الْجَنَّةَ» قَالَ: فَقُلْنَا وَثَلَاثَةٌ؟ قَالَ: فَقَالَ: «وَالثَّلَاثَةُ» قَالَ: فَقُلْنَا وَاثْنَانِ: قَالَ «وَاثْنَانِ». ثُمَّ لَمْ نَسْأَلْهُ عَنِ الْوَاحِدِ.

“Muislamu yeyote atakayeshuhudiwa na watu wanne kuwa alikuwa muadilifu, Allah Atamuingiza Peponi!” Tukasema, “Vipi watu watatu?” Akasema, “Na watatu.” Tukamuambia, “Vipi wawili?” Akasema, “Na wawili?” Hatukumuuliza kuhusu (ushahidi) wa muumini mmoja.”¹

Hadithi hii ilinukuliwa na Al-Bukhari, Al-Tirmidhi na An-Nasai.²

Hekima ya Kubadilishwa Qiblah

Allah تعالى Alisema,

وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يَتَّبِعُ الرَّسُولَ مِمَّنْ يَنْقَلِبُ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ ۗ وَإِن كَانَتْ لَكَبِيرَةً إِلَّا عَلَى الَّذِينَ هَدَىٰ اللَّهُ ۗ

“Na Hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho ila Tupate kumjua yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale Alio waongoa Mwenyezi Mungu.” (2:143)

Allah تعالى Akaeleza kuwa, Tulikufaradhisia, Ewe Muhammad, kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis* kwanza na kisha tukakubadilishia, kuelekea upande wa *Ka'abah* ili Tupate Kumjua atakayekufuata na kukutii na hivyo kuelekea upande wowote utakaoelekea.

مِمَّنْ يَنْقَلِبُ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ ۗ

“Na yule anayegeuka akarejea nyuma.” (2:143) Kwa maana: Atakayeritadi na kuiacha dini yake.

¹ Ahmad 1:21.

² Fat'hul Al-Bari 3:271 Tuhfatul Al-Ahwadhi 4:166, na An – Nasai 4:51.

وَإِنْ كَانَتْ لَكَبِيرَةً

“Na kwa yakini hilo lilikuwa jambo gumu.” (2:143)

Aya inadhihirisha kuwa kubadilishwa kwa Kiblah kutoka *Bayt Al-Maqdis* kwenda *Ka'abah* ni jambo zito kwenye moyo, isipokuwa kwa wale mioyo yao, Ameiongoa Allah تعالى, ambao wanaamini ukweli wa Mtume ﷺ bila kuwa na shaka. Na kuwa kila alichokuja nacho ni ukweli usio na shaka. Na wale ambao wanaamini kuwa Allah تعالى Anafanya Ayapendayo, Anaamua Ayapendayo, Anawaamrisha waja Wake Apendavyo, na Ana Hikima iliyo kamili na ushahidi usio na shaka katika yote haya. Huu ndio Mtazamo wa waumini katika hili, tofauti na wale wenye maradhi ndani ya mioyo yao, yeyote kati yao anapopatwa na jambo, hupata wasiwasi. Kama ilivyo jambo hilo kwa waumini huwaongezea wao imani ya uhakika. Allah تعالى Amesema

وَإِذَا مَا أَنْزَلْنَا سُورَةً فَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هُدًىٰ ۖ إِمْنًا ۗ فَأَمَّا الَّذِينَ
ءَامَنُوا فزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٤٤﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ فزَادَتْهُمْ
رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ

“Na inapoteremshwa Sura wapo miongoni mwao wasemao: Ni nani miongoni mwenu Sura hii imemzidishia Imani? Ama wale walioamini inawazidishia Imani, nao wanafurahi. Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao.” (9:124-125) Na Allah تعالى Amesema,

وَنُزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۗ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿١٧٨﴾

“Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila hasara.” (17:82)

Hakika, wale walioendelea kumuamini Mtume ﷺ walimtii na wakafuata kila alichiamrisha Allah تعالى, bila ya kuwa na shaka au kusita, walikuwa Masahaba watukufu. Baadhi ya wanazuoni walieleza kuwa Muhajirina wa mwanzo (waliohama na Mtume) kutoka Makkah kwenda Madinah na Ansar (wakazi wa Al-Madinah) waliwasaidia na kuwahifadhi (Mtume ﷺ na Muhajirina), ni

ambao wale waliosali kuelekea upande wa *Kiblah (Bayt Al-Maqdsi)* kisha *Ka'abah*.

Al-Bukhari alipokuwa akiitolea maelezo Ayah (2:143) alitaarifu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisimulia: Wakati watu wakisali Al-Fajiri katika Masjid Quba, mtu aliingia na kusema, "Qur'an imeteremshwa kwa Mtume ﷺ na ameamrisha kuelekea upande wa *Ka'abah*, kwa hiyo elekeeni *Ka'abah*."¹ Kisha wakaelekea upande wa *Ka'abah*." Muslim naye alinukuu.²

At- Tirmidhi aliongezea kuwa walikuwa katika Rukuu na kisha wakabadilisha mwelekeo (wa *Kiblah*) kuwa *Ka'abah* wakiwa bado katika Rukuu.³ Muslim alitaarifu masimulizi haya ya mwisho kutoka kwa Anas رضي الله عنه.⁴ Hadithi zote hizi zinaonesha utii wa ukweli waliokuwa nao masahaba kwa Allahna Mjumbe wake na kuridhia kwao maamrisha ya Allah تعالى, Allah Awawie radhi wote. Allah تعالى Amesema,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ

"Na Mwenyezi Mungu Hakuwa mwenye Kuipoteza Imani yenu." (2:143)

Maana yake, malipo ya Sala zenu mlipokuwa mkielekea upande wa *Bayt Maqdsi* hatoyapoteza Allah تعالى. Imenukuliwa ndani ya Sahihi kuwa Abu Is-haq As – Sabiy alisimulia kuwa Barau alisema: "Watu waliuliza juu ya watu waliosali kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis* na wakafa (kabla ya kubadilishwa *Kiblah*) - kuelekea upande wa *Ka'ba*." Allah تعالى Aliteremsha:

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ

"Na Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuipoteza Imani yenu." (2:143)

Ilinukuliwa pia na At-Tirmidhi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, na At-Tirmidhi ameipa sifa kuwa ni *sahih*.⁵ Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisimulia:

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ

"Na Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuipoteza Imani yenu." (2:143)

¹ Fat'hul Al-Bari 8:22

² Muslim 1:375

³ Tuhfat ulAl-Ahwadhi 8:300.

⁴ Muslim 1:375

⁵ Fat'hul Al- Bari 8:20, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:300

Inafafanua: Sala yenu kuelekea upande wa Kiblah cha mwanzo na kumuamini kwenu Mtume ﷺ na kumtii kwa kuelekea upande wa Kiblah cha pili, Atawalipa kwa amali zote hizo. Kwa hakika

إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرءُوفٌ رءِيمٌ ﴿١٤٤﴾

“Kwani Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenye Kuwarehemu.” (2:143)¹

Zaidi, ilinukuliwa katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alimuona mwanamke miongoni mwa mateka ambaye alitenganishwa na mwanawe. Kila alipomuona mtoto miongoni mwa mateka, alimchukua na kumsogeza kifuni, kama alikuwa akimtafuta mwanaye. Alipompata mtoto wake, alimkumbatia na kumpa chuchu anyonye. Mtume ﷺ alisema,

« أُنزِلَ هَذِهِ طَارِحَةً وَلَدَهَا فِي النَّارِ وَهِيَ تَقْدِرُ عَلَى أَنْ لَا تَطْرَحَهُ؟ قَالُوا: لَا يَا رَسُولَ اللَّهِ. قَالَ: «فَوَاللَّهِ لَأَرْحَمُ بِعِبَادِهِ مِنْ هَذِهِ بِوَلَدِهَا»

“Mnadhani mwanamke huyu atamtupa mwanae motoni kwa hiari?” Walijibu, “Hapana, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! “Akasema, “Wallah! Allah ni Mreheemu zaidi kwa waja Wake kuliko alivyo mama huyu kwa mwanawe.”²

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ وَإِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٥﴾

144. “Kwa yakini Tunaona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi Tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu; na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo; na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na yale wanayo yatenda”.

¹ Ibn Abu Hatim 1:99. Sanadi yake ni dhaifu.

² Muslim 4:2109.

Hukumu ya Kwanza Kufutwa katika Qur'an ni Mabadiliko ya Qiblah

Ali bin Abu *Talhah* alisimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: Hukumu ya kwanza kufutwa ndani ya Qur'an ni inayohusu mabadiliko ya Kiblah Mtume ﷺ alipohamia Madinah, wakazi wengi walikuwa Mayahudi na Allah تعالى Alimuamrisha aelekee *Bayt Al-Maqdis*. Mayahudi walifarajika wakati huo. Mtume ﷺ alielekea huko kwa miezi kumi au zaidi kidogo, lakini alipenda kuelekea upande wa Kiblah cha Ibrahim عليه السلام (Ka'abah – Makkah). Alikuwa akimuomba Allah تعالى huku akiangalia mbinguni (akisubiri Amri ya Allah تعالى). Kisha Allah تعالى Akateremsha,

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ط

“Kwa yakini Tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni.”
(2:144) Mpaka,

فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ط

“Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu.” (2:144)

Mayahudi hawakuipenda Amri hii na walisema:

مَا وَلَدْنَاهُمْ مِّن قِبَلَتِهِمُ الَّتِي كَانُوا عَلَيْهَا ؕ قُلْ لِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ؕ

“Nini kilichowageuza kutoka Kibla chao walichokuwa wakikielekea? Sema (Ewe Muhammad) Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu.” (2:142)¹

Allah تعالى Amesema,

فَأَيَّمَا تَوَلَّوْا فَنَّمَّ وَجْهُ اللَّهِ ؕ

“Basi kokote mnakoelekea, huko Mwenyezi Mungu yupo.” (2:115)

Aidha Allah تعالى Amesema,

وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَن يَتَّبِعُ الرَّسُولَ مِمَّن يَنْقَلِبُ عَلَيَّ عَاقِبَتِهِ ؕ

“Na Hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho ila tupate Kumjua yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma.”
(2:143)

¹ Ibn Abu Hatim 1:103.

Hivi Kiblah ni Ka'aba yenyewe au Mwelekeo wa Mahali Ilipo?

Al-Hakim alisimulia kuwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema

فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ^١

“Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu.” Ina maana: Uelekeo wake.¹ Al-Hakim alieleza kuwa Silsila ya mapokezi yake ni sahihi na kuwa wao (yaani, Al-Bukhari na Muslim) hawakujumuisha katika maandiko yao. Hukumu hii kuhusu Kiblah pia ni kauli ya Abu Al-Aliyah, Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Qatadah, Ar- Rabi bin Anas na wengineo.² Ama Kauli ya Allah تعالى

وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ^٢

“Na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo.” (2:144)

Ni amri kutoka kwa Allah تعالى ya kueleka upande wa Ka'abah kutoka popote mtu alipo duniani, ikiwa Mashariki, Magharibi, Kaskazini au Kusini, isipokuwa Sala ya Sunna (*Nafilah*). Mtu awapo safarini anaruhusiwa kuelekea upande wowote ambao mwili wake unaelekea, huku moyo wake akihusisha na Ka'bah. Pia wakati wa kupigana vita, mtu anaruhusiwa kusali kama inavyomkinika. Wanaohusika na msamaha huu ni pamoja na wale wasio na uhakika na Kiblah na wakaelekea pasipo, wakidhani huko ndio Kiblah, kwa sababu Allah تعالى Hamlazimishi mja kufanya asiloliweza. Kadhalika wale walio katika mapambano ya vita.

Hukumu ya Kubadilishwa Kiblah Mayahudi walikuwa wanaifahamu Kabla:

وَإِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ^٣

“Na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi.” (2:144)

Aya hii ina maana kuwa Mayahudi ambao walipinga kuacha kwenu kuelekea *Baytul – Maqdis* walikuwa wanajua kuwa Allah تعالى Atakuamrisha (Ewe Muhammad ﷺ) kuelekea upande wa Ka'abah. Mayahudi waliyasoma katika Vitabu kwa maelezo yaliyotolewa na Mitume wao huhusu sifa za Mtume ﷺ

¹ Hakim 2:269.

² Ibn Abu Hatim 1:107-109.

na Ummah wake, kuwa Allah تعالى Amemjaalia na Akamtukuza kwa Kumpa sharia tukufu iliyo kamilika. Lakini bado, Watu wa Kitabu wanauficha ukweli huu kati yao kwa sababu ya inda, ukafiri na uasi. Ndio sababu Allah تعالى Aliwakhofisha Aliposema:

وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na yale wanayo yatenda.” (2:144)

وَلَيْنَ أَتَيْتَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ بِكُلِّ آيَةٍ مَّا تَبِعُوا قِبْلَتَكَ ۚ وَمَا أَنْتَ بِتَابِعٍ قِبْلَتِهِمْ ۚ وَمَا بَعْضُهُمْ بِتَابِعٍ قِبْلَةَ بَعْضٍ ۚ وَلَيْنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ مِّنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۚ إِنَّكَ إِذَا لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٥﴾

145. “Na hao waliopewa Kitabu, hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe hutafuata Kibla chao, wala baadhi yao hawatafuata Kibla cha wengineo; na kama ukiyafuata matamano yao baada ya kukufikia ujuzi, hakika hapo utakuwa miongoni mwa wenye kudhulumu”.

Ukorofi na Ukafiri wa Mayahudi

Allah تعالى Ameeleza kufuru ya Mayahudi, ukorofi wao na kukhalifu kwao kuhusu ukweli wa Mtume ﷺ. Pia Anaeleza kwamba hata kama Mtume ﷺ angeleta kila aina ya ushahidi kwa kuthibitisha yale aliyoletwa nayo, wasingemuamini au kuacha kufuata matamano yao.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٤٦﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١٤٧﴾

“Hakika wale ambao Neno la Mola Wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini, Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.” (10:96-97).

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema hapa:

وَلَيْنَ أَتَيْتَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ بِكُلِّ آيَةٍ مَا تَبِعُوا قِبْلَتَكَ

“Na hao waliopewa Kitabu, hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako...” (2:145)

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا أَنْتَ بِتَابِعٍ قِبْلَتِهِمْ

“...Wala wewe hutafuata Kibla chao...” (2:145)

Maana yake: Inaonesha juhudi anazozitumia Mtume ﷺ kutekeleza kila anacho amrisha na Allah تعالى. Kauli hii ya Allah تعالى pia inaonesha kuwa kama walivyo Mayahudi wanashikilia rai na utashi wao ilhali Mtume ﷺ nae anashikamana na Amri za Allah تعالى, anamtii Yeye na anafuata yanayo-mridhisha Yeye, na kwamba hatofuata utashi wao kwa namna yoyote ile. Hivyo, Kuelekea *Bayt Al-Maqdis* wakati wa Sala haikuwa kwa sababu ilikuwa Kiblah ya Mayahudi, lakini ni kwa sababu alitekeleza Amri ya Allah تعالى. Kisha Allah تعالى Amewaonya wale walioacha ukweli kwa makusudi, kwa sababu ushahidi dhidi ya wale wanaojua una nguvu kuliko dhidi ya watu wengine.

Kwa sababu hii Allah تعالى Alimuambia Mtume ﷺ kwa lengo la kuuambia Ummah wake:

وَلَيْنَ اتَّبَعَتْ أَهْوَاءَهُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ إِنَّكَ إِذَا لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٥﴾

“...na kama ukiyafuata matamano yao baada ya kukufikia ujuzi, hakika hapo utakuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.” (2:145)

* * *

الَّذِينَ آتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ آبَاءَهُمْ^ط
 وَإِنَّ فَرِيقًا مِّنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٤٦﴾
 الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ^ط فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١٤٧﴾ وَلِكُلِّ
 وَجْهَةٍ هُوَ مُوَلِّيهَا^ط فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ^ع أَيْنَ مَا تَكُونُوا يَأْتِ
 بِكُمْ اللَّهُ جَمِيعًا^ع إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٤٨﴾ وَمِنْ
 حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِنَّمَا^ط
 لِلْحَقِّ مِنْ رَبِّكَ^ط وَمَا لِلَّهِ بِغَفْلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٩﴾ وَمِنْ
 حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ^ع
 وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ^ط لِئَلَّا يَكُونَ
 لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ فَلَا
 تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي^ط وَإِلَّائِي^ط يَعْمَدُونَ وَعَلَيْكُمْ تَهْتَدُونَ
 ﴿١٥٠﴾ كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ
 آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ
 وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿١٥١﴾ فَادْكُرُونِي أذكُرْكُمْ
 وَأَشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُونِ ﴿١٥٢﴾

الَّذِينَ آتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ
 كَمَا يَعْرِفُونَ آبَاءَهُمْ^ط وَإِنَّ فَرِيقًا
 مِّنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ
 ﴿١٤٦﴾ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ^ط فَلَا تَكُونَنَّ
 مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١٤٧﴾

146. "Wale Tuliowapa Kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao; na kuna kikundi katika wao huificha haki na hali wanajua."

147. "Haki inatoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka."

Mayahudi Waliujua Ukweli wa Mtume ﷺ Lakini Waliuficha

Allah تعالیٰ Ameeru kuwa wanazuoni wa Watu wa Kitabu wanajua ukweli wa yale aliowaletea Mtume ﷺ

kama mmoja wao anavyomfahamu mtoto wake, usemi ambao Waarabu walikuwa wakiutumia katika kulielezea jambo lililokuwa dhahiri. Kama ilivyopokelewa katika Hadithi, Mtume ﷺ alimuambia mtu aliyekuwa na Kijana pamoja naye:

«ابْنُكَ هَذَا؟ قَالَ: نَعَمْ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَشْهَدُ بِهِ»

"Huyu ni mwanao?" Akajibu, 'Ndiyo, Ewe Mjumbe wa Allah Nathibitisha ukweli huu,' Mtume ﷺ alisema,

«أَمَّا إِنَّهُ لَا يَخْجِي عَلَيْكَ وَلَا تَخْجِي عَلَيْهِ»

*"Kwa hakika hutokwenda kinyume naye wala yeye hatokwenda kinyume nawe."*¹

Kwa mujibu wa Al-Qurtubi رحمه الله تعالى, Ilisimuliwa kuwa Umar رضي الله عنه alimuambia Abdullah bin Salam (mwanazuoni wa Kiyahudi aliyesilimu), 'Je, unamtambua Muhammad kama unavyomtambua mwanao?' Alijibu, "Ndio, na hata zaidi, Mwaminifu (Al-Amin - Malaika Jibril عليه السلام) alishuka kutoka mbinguni kuja duniani kwa Mwaminifu (Al-Amin) (maana yake Muhammad); nilimtambua kwa sifa zake, ingawa sijui lolote kuhusu kisa cha mama yake."¹ Kisha Allah تعالى Alieleza kuwa japokuwa walikuwa wanafahamu ukweli juu ya Mtume ﷺ, bado walificha haki.

لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ

"Huificha haki." Aya inaonesha kuwa wanawafichia watu yaliyomo katika vitabu vyao miongoni mwa yale yanayoeleza wasifu wa Mtume ﷺ yale wanayoyakuta katika Vitabu vyao,

وَهُمْ يَعْلَمُونَ

"Na hali wanajua..." Kisha Allah تعالى Anaimarisha azma ya Mtume ﷺ na waumini na Anathibitisha kuwa alichokuja nacho Mtume ﷺ ni ukweli usio na shaka. Kauli ya Allah تعالى,

الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ

"...Haki inatoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka." (2:147)

وَلِكُلِّ وِجْهَةٍ هُوَ مُوَلِّبُهَا فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ أَيْنَ مَا تَكُونُوا يَأْتِ بِكُمْ اللَّهُ جَمِيعًا إِنَّ اللَّهَ

عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"Na kila mmoja anao upande anaoelekea. Basi shindanieni mema. Popote mlipo Mwenyezi Mungu Atakuleteni nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu." (2:148)

¹ Ahmad 4:163.

² Al-Qurtubi 2:163. Isnadi yake ina mashaka.

Kila Umma Una Kiblah

Al-Awfi alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Aya:

وَلِكُلِّ وِجْهَةٌ هُوَ مُوَلِّيًا^ط

“Na kila mmoja anao upande anaoelekea.” (2:148)

Kwa Aya hii Anakusudia wafuasi wa dini mbalimbali. Anasema kila Taifa na kabila wana Kiblah chao walichokichagua, na uelekeo wa Allah تعالى uko kule wanakoelekea waumini.¹ Abdul – Aliyah alisema, “Myahudi ana upande anaoelekea (wakati wa Sala) na Mkristo ana upande anaouelekea na Allah تعالى Amewaongozeni Enyi Ummah wa Kiislamu kwenye Kiblah ambacho ni Kiblah cha kweli.”² Kauli hii ilisimuliwa pia na Mujahid, Ata, Adh-Dhahhak, Ar – Rabi, Anas, As – Suddi na wengineo.³ Aya hii ya mwisho inafanana na Kauli Yake Allah تعالى Alivyosema,

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَا^ط وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ لَيَبْلُوَكُمْ فِي مَاءِ آتَانَكُمْ^ط فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ^ط إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا

“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuekea sharia yake na njia yake. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka Angekufanyeni nyote umma mmoja, lakini ni Kujaribuni kwa aliyokupeni. Basi shindaneni kwa mambo ya kheri. Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo yenu nyote.” (5:48)

Allah تعالى Amesema tena,

أَيْنَ مَا تَكُونُوا يَأْتِ بِكُمْ اللَّهُ جَمِيعًا^ط إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٤٨﴾

“Popote mlipo Mwenyezi Mungu Atakuleteni nyote pamoja. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.” (2:148)

¹ Tabari 3:193. Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 1:121.

³ Ibn Abu Hatim 1:121-122.

Ina maana: Ana uwezo wa Kukukusanyeni kutoka kwenye udongo hata kama miili na nyama vimefarakana na kutawanyika,

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ وَإِنَّهُ لَلْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ ۗ وَمَا اللَّهُ
بِغَفِيلٍ ۗ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٦﴾ وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ
وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۗ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ
ظَلَمُوا مِنْهُمْ ۗ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي ۗ وَلَا تَمْنُنَ عَلَيْهِمْ ۗ وَاللَّهُ لَمَّا تَدُونُ ﴿١٤٧﴾

149. "Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na hiyo ndiyo Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na mnayoyatenda.

150. "Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo ili watu wasiwe na hoja juu yenu, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Basi msiwaogope wao, lakini Niogopeni Mimi - na ili Nikutimizieni Neema Yangu, na ili mpate kuongoka."

Kwa Nini Naskh Mabadiliko ya Kiblah Yamekaririwa Mara tatu?

Hii ni amri ya tatu kutoka kwa Allah تعالى Inayoamrisha kuelekea upande wa Al-Masjid al-Haram kwa watu wa pande zote za Dunia (wakati wa Sala). Imesemwa kuwa Allah تعالى Ameitaja tena Amri hii hapa kwa sababu inahusiana na kilichokuwa kabla au kilichokuwa baada yake. Mwanzoni Allah تعالى Amesema:

قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ۗ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا ۗ

"Kwa yakini Tukiona unavyogezageza uso wako mbinguni. Basi Tutakuelekeza kwenye Kibla ukipendacho." (2:144). Mpaka

وَإِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَيَعْلَمُونَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ ۗ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٨﴾

"...na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na yale wanayoyatenda". (2:144)

Allah تعالى Ametaja katika Aya hizi, Kumtekelezea Mtume ﷺ utashi wake na Akamuamrisha kuelekea upande wa Kiblah ambacho alikitaka na kukiridhia. Katika Amri ya pili. Allah تعالى Amesema,

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِنَّهُ لَلْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ وَمَا اللَّهُ

بِغَيْفٍ لِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٦﴾

“Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na hiyo ndiyo Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye Kughafilika na mnayoyatenda.” (2:149)

Kwa hiyo, Allah تعالى Ameeleza hapa kuwa kubadilishwa Kiblah ni ukweli kutoka kwake, hivyo ameipa uzito maudhui hii kuliko katika Aya ya mwanzo, ambapo Allah تعالى Alikubali lile alilolitamani Mtume wake ﷺ. Na hapa Allah تعالى Anaeleza kuwa huu ni ukweli Aupendao na Kuuridhia kutoka Kwake. Katika Amri ya tatu, Allah تعالى Anaeleza hekima ya Kuvunja hoja ya kuwakhaliifu Mayahudi, wao walikuwa wakihoji kuwa imekuwaje Mtume ﷺ anaelekea Kibla chao? Kwani kutoka katika vitabu vyao wanajua kuwa Mtume ﷺ ataamrishwa kuelekea Kiblah cha Ibrahim عليه السلام Ka'abah. Makafiri wa Kiarabu hawakuwa na hoja tena kuhusu Kiblah cha Mtume baada ya Allah تعالى kumuamrisha kuelekea upande wa Kiblah cha Ibrahim عليه السلام, ambacho walikuwa wanakiheshimu na kukitukuza. Waarabu walikuwa wakiiheshimu Ka'abah na walifurahia kuwa Mtume ﷺ aliamrishwa kuelekea Al-Kaaba.

Hekima ya Kubadilishwa (Nasikh) Kiblah Kilichotangulia

Allah تعالى Amesema:

لَعَلَّ يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ

“Ili watu wasiwe na hoja juu yenu.”

Maana yake: *Ahlu Kitaab.*

Kwa hiyo, watu wa Kitabu wanajua kutokana na sifa bainifu za Ummah wa Kiislamu kuwa wataamrishwa kuelekea upande wa Ka'abah. Iwapo Waislamu wangebaki kuelekea upande wa Kiblah – *Bayt Al-Maqdis*, ambacho kilikuwa

Kiblah cha Mayahudi, uhakika huu ungetumika kama kigezo cha Mayahudi kulumbana na Waislamu juu ya kulingana nao katika mweleko wa Kibla. Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ

“Isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao.”

Inamaanisha washirikina wa Kiquraysh. Hoja za watu hawa madhalimu zilikuwa hazina mashiko, kwani walisema, “Mtu huyu (Muhammad) anadai kuwa alikuwa akifuata Dini ya Ibrahim عليه السلام! Hivyo, kama kuelekea kwake *Bayt Al-Maqdis* ilikuwa ni katika Dini ya Ibrahim عليه السلام, kwa nini alibadilisha?” Jibu la swali hili ni kuwa Allah تعالى Alimchagulia Mtume wake ﷺ kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*, kwa hikima fulani, na alimtii Allah تعالى kuhusiana na amri hii. Kisha, Allah تعالى Alibadilisha Kiblah kuelekea upande wa Kiblah cha Ibrahim عليه السلام, ambacho ni Ka’abah na pia alimtii Allah تعالى kwa Amri hii. Yeye humtii Allah تعالى katika hali zote, na hajawahi kwenda kinyume hata chembe na Ummah unamuiga katika hilo. Ama Kauli Yake Allah تعالى،

فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي

“Basi msiwaogope wao, lakini Niogopeni Mimi.”

Maana yake: “Msiogope mashaka yanayoletwa na madhalimu na wakorofi bali mniogope Mimi Pekee.’ Kwa hakika, Allah تعالى Peke Yake Ndiye Anayestahiki Kuogopwa. Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَمَّ نِعْمَتِي عَلَيْكُمْ

“Na ili Nikutimizieni Neema Yangu.”

Aya hii inaelezea Kauli ya Allah تعالى،

لَعَلَّ يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ

“Ili watu wasiwe na hoja juu yenu.”

Maana yake: Nitakamilisha Ukarimu Wangu kwenu kwa Kuwafanyieni sheria ya kueleka upande wa *Ka’abah*, ili Shariah ya Kiislamu iwe kamili katika nyanja zote. Allah تعالى Amesema،

وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٤٦﴾

“Na ili mpate kuongoka.”

Maana yake: Kuelekezwa na kuongozwa kwa kile ambacho watu wengine walipotoshwa nacho. ‘Tumekuongozeni na Tukakupendeleeni kwacho.’ Hii ndio sababu Ummah huu ni bora na uliofadhilishwa kuliko Umma mwingine.

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِّنكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ
وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿١٤٧﴾ فَأَذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي وَلَا
تَكْفُرُونِ ﴿١٤٨﴾

151. “Kama Tulivyomtuma Mtume kwenu anayetokana na nyinyi, anakusomeeni Aya Zetu na kukukatazeni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyokuwa hamyajui.”

152. “Basi Nikumbukeni Nitakukumbukeni, na Nishukuruni wala msinikufuru.”

Utume wa Muhammad ﷺ ni Neema Kubwa ya Kumkumbuka na Kumshukuru Allah تعالی:

Allah تعالی Anawakumbusha waja Wake Waumini kwa kile Alichowaneemesha nacho, kwa Kuwapelekea Muhammad ﷺ kama Mjumbe wake, akiwasomea Ayat kutoka kwa Allah تعالی na akiwatakasaa kutokana na kila tabia mbaya, maradhi ya nyoyo na vitendo vya *Jahiliyyah*. Mjumbe ﷺ anawatoa kizani (ukafiri) na kuwatia kwenye nuru (Imani) na anawafundisha Kitabu nacho ni Qur’an; na Hikmah ambazo ni *Sunnah*. Pia anawafundisha wasiyoyajuwa.

Zama za *Jahiliyyah*, walikuwa wakitamka maneno ya kipuuzi. Baadaye kwa baraka za Ujumbe wa Mtume na uzuri wa utume wake, walinyanyuliwa kwenye daraja la *Awliyyaa* (marafiki waaminifu wa Allah تعالی) na daraja la wanazuoni. Hivyo wakawa ni watu wenye elimu ya ndani kuliko wengine; wenye mioyo ya uchamungu zaidi; na ndimi zitamkazo ukweli zaidi ya wengine. Allah تعالی Amesema,

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ ءَايَاتِهِ
وَيُزَكِّيهِمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile Alivyowaletea Mtume (Muhammad) aliye miongoni mwao wenyewe, anayewasomea Ayah Zake (Qur’an) na amewatakasa.” (3:164)

Allah تعالى Aliwasimbulia wale ambao hawakuthamini Neema Alizowapa, Aliposema:

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴾

“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha Neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo?” (14:28)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Neema za Allah تعالى, Maana yake: Muhammad ﷺ.”¹ Kwa hiyo, Allah تعالى Aliwaamrisha waumini kudumu na neema hizi na kuzifurahia kwa kumkumbuka na kumshukuru Yeye. Hivyo Akasema,

﴿ فَادْكُرُونِي أذْكُرْكُمْ وَأَشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُونِ ﴾

“Basi Nikumbukeni Nitakukumbukeni, na Nishukuruni wala msinikufuru.” (2:152)

Mujahid alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى:

﴿ كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِّنكُمْ ﴾

“Kama Tulivyomtuma Mtume (Muhammad) kwenu anayetokana nanyi.”

Maana yake: Kwa hiyo kama nilivyofanya hivyo basi Nikumbukeni Mimi kwa kushukuru Neema Zangu.² Al-Hasa Al-Basri رحمه الله تعالى aliitolea maelezo Ayah hii.

¹ Al-Bukhari Na. 3977.

² At-Tabari 3:210.

فَادْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ

“Basi Nikumbukeni, Nitakukumbukeni.”

“Nikumbukeni kwa yale Niliyokuamuruni Nami Nitawakumbukeni kuhusu yale Niliyojilazimisha kuyafanya kwa faida yenu (yaani Malipo na msamaha Wake).”¹ Hadithi sahihi inasema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: مَنْ ذَكَرَنِي فِي نَفْسِهِ ذَكَرْتُهُ فِي نَفْسِي وَمَنْ ذَكَرَنِي فِي مَالٍ ذَكَرْتُهُ فِي مَالٍ خَيْرٍ مِنْهُ»

*“Allah Aliyetukuka Amesema, Atakayenitaja katika nafsi yake, Nitamtaja katika Nafsi Yangu; na atakayenitaja katika hadhara, Nitamtaja katika hadhara bora zaidi.”*²

Imam Ahmad alitaarifu kuwa Anas رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: يَا ابْنَ آدَمَ، إِنْ ذَكَرْتَنِي فِي نَفْسِكَ ذَكَرْتُكَ فِي نَفْسِي، إِنْ ذَكَرْتَنِي فِي مَالٍ ذَكَرْتُكَ فِي مَالٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ - أَوْ قَالَ: فِي مَالٍ خَيْرٍ مِنْهُ - وَإِنْ دَنَوْتَ مِنِّي شِبْرًا دَنَوْتُ مِنْكَ ذِرَاعًا، وَإِنْ دَنَوْتَ مِنِّي ذِرَاعًا دَنَوْتُ مِنْكَ بَاعًا، وَإِنْ أَتَيْتَنِي تَمْشِي أَتَيْتُكَ هَرْوَلَةً»

“Allah Aliyetukuka Amesema, “Ewe mwana wa Adam! Iwapo utanitaja katika nafsi yako (kirohoroho), Nitakutaja katika Nafsi Yangu. Iwapo utanitaja Mimi katika hadhara, Nitakutaja katika hadhara ya Malaika (au hadhara bora zaidi). Iwapo utanikaribia Mimi kwa shibri, Nitakusogelea kwa dhira. Ukinisogelea kwa dhira, Mimi Nitakusogelea kwa urefu wa mkono. Na ukinijia Mimi kwa kutembea, Mimi Nitakujia kwa Kukimbia.”

Upokezi wake sahihi, ulinukuliwa na Al-Bukhari.³

¹ Ibn Abu Hatim 1:141.

² Fat’hul Al-Bari 13:395.

³ Ahmad 3:138, Fat’hul Al-Bari 13:521.

Allah تعالى Amesema;

وَأَشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُوا ۝

“Na Nishukuruni wala Msinikufuru.”

Katika Aya hii Allah تعالى Anaamrisha kuwa Yeye Ashukuriwe, na Anaahidi malipo zaidi kwa kumshukuru Yeye.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ ۖ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ۝

“Na alipotangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru Nitakuzidishieni na mkikufuru basi Adhabu Yangu ni kali.” (14:7)

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Raja Al-Utarid alisema: Imran bin Huswayn alikuja kwetu mara moja huku amevaa kanzu nzuri ya Hariri ambayo hatukuwahi kumuona nayo kabla au baadaye. Alisema, Mtume ﷺ Alisema:

«مَنْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ نِعْمَةً فَإِنَّ اللَّهَ يُجِيبُ أَنْ يَرَى أَثَرَ نِعْمَتِهِ عَلَى خَلْقِهِ»، وَقَالَ رَوْحُ
مَرَّةً: «عَلَى عَبْدِهِ»

“Wale ambao Allah Aliwaneemesha, Allah Anapenda Aone athari za Neema Zake kwa viumbe Wake” au alisema, “Kwa mja Wake” Kwa mujibu wa Rauh (mmoja wa wasimulizi wa Hadithi).¹

* * *

¹ Ahmad 4:438.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ
 الصَّابِرِينَ ﴿١٥٣﴾ وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
 أَمُوتٌ ۚ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَكِنْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿١٥٤﴾ وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ
 بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ
 وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ
 مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾ أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ
 صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾
 * إِنَّ الصَّافِيَ وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَائِرِ اللَّهِ ۗ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ
 اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّقَ بِهِمَا ۗ وَمَن تَطَوَّعَ
 خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٥٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا
 أَنزَلْنَا مِنَ الْكِتَابِ وَأَهْدَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي
 الْكِتَابِ ۗ أُولَئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّاعِنُونَ ﴿١٥٩﴾ إِلَّا
 الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَبَيَّنَّوْنَا فَأُولَئِكَ أَتُوبُ عَلَيْهِمْ ۗ وَأَنَا
 التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا
 أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٦١﴾
 خَالِدِينَ فِيهَا ۗ لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿١٦٢﴾
 وَإِلَهُكُمْ إِلَهُ وَاحِدٌ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ
 الصَّابِرِينَ ﴿١٥٣﴾ وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
 أَمُوتٌ ۚ بَلْ أَحْيَاءٌ وَلَكِنْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿١٥٤﴾

**153. "Enyi mlioamini!
 Takeni msaada kwa subira
 na Sala. Hakika Mwenyezi
 Mungu Yu pamoja na
 wanaosubiri."**

**154. "Wala msiseme kuwa
 wale waliouawa katika
 Njia ya Mwenyezi Mungu
 ni maiti; bali hao wako hai,
 lakini nyinyi hamtambui."**

Ubora wa Subira na Sala:

Baada ya Allah تعالى Kueleza
 Amri ya Kutaka Ashukuriwe,
 Alianza Kubainisha subira;
 na Alitoa mwongozo wa mja
 kujisaidia kwa subira na
 Sala. Ni ukweli kuwa mja,
 ama anakuwa katika neema

kwa hivyo anapaswa kushukuru kwayo, au anapatwa na maafa ambayo nayo
 yanamlazimu kuwa na subira. Hadithi inasema:

«عَجَبًا لِّلْمُؤْمِنِ لَا يَقْضِي اللهُ لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ: إِنَّ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ فَفَكَرَ كَانَ
 خَيْرًا لَهُ وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ فَصَبَرَ كَانَ خَيْرًا لَهُ»

“Ameshangaza muumini, kwa hukumu yoyote anayopewa na Allah ni bora kwake! Anapojarihiwa kwa neema anashukuru, na ni bora kwake; na anapofikwa na matatizo, anasubiri na hili ni bora kwake.”¹

Allah تعالى Ameeleza kuwa zana bora za kupunguza athari ya matatizo ni subira na Sala. Kama ilivyotangulia maelezo yake katika:

وَأَسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى الْخَاشِعِينَ ﴿١٥٣﴾

“Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.” (2:45)

Kuna aina mbalimbali za subira - *Sabr*, mojawapo ni kufanya subira katika kuacha makatazo na madhambi. Nyingine ni subira katika kufanya vitendo vya ibada na utiifu. Aina ya pili ina malipo zaidi kuliko ya mwanzo. Kuna aina ya tatu ya subira ambayo ni kuwa na uvumilivu katika taabu na mateso, kwa kuacha mambo ya aibu na subira hii nayo ni wajibu, kama vile kutubia. Abdur – Rahman bin Zayd bin Aslam alisema, *Sabr* ina sehemu mbili: Subira kwa ajili ya Allah تعالى inayohusu kile kinachomridhisha Yeye (vitendo vya ibada na utii), hata kama ni ngumu katika moyo na mwili, na subira ya wakati wa kuyaepuka Asiyoyapenda Allah تعالى, hata kama utashi wake wa nafsi unavutia katika hayo. Wale wenye sifa hizi watakuwa miongoni mwa watu wenye subira ambao Allah تعالى Atawalaki (watakapokutana Naye, Siku ya Kiama: Rejea Surat Ahzab 33:44) Akipenda Allah تعالى.²

Uhai wa Waliokufa Wakiwa Mashahidi:

وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ يُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمُوتَ بَلْ أَحْيَاءٌ

“Wala msiseme kuwa wale waliouawa katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni maiti, bali hao wako hai.”

Allah تعالى Anaeleza kuwa mashahidi katika *barzakh* wako hai na wanapata riziki. Muslim ameandika katika Sahih yake:

¹ Muslim 4:2292.

² Ibn Abu Hatim 1:144.

«أَنَّ أَرْوَاحَ الشُّهَدَاءِ فِي حَوَاصِلِ طَيْرٍ خُضِرٍ، تَسْرُحُ فِي الْجَنَّةِ حَيْثُ شَاءَتْ، ثُمَّ تَأْوِي إِلَى فَنَائِدِيلٍ مُعَلَّقَةٍ تَحْتَ الْعَرْشِ، فَاطَّلَعَ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ اطَّلَاعَةً، فَقَالَ: مَاذَا تَبْعُونَ؟ فَقَالُوا: يَا رَبَّنَا وَآيَّ شَيْءٍ نَبْعِي، وَقَدْ أَعْطَيْتَنَا مَا لَمْ تُعْطِ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ؟ ثُمَّ عَادَ إِلَيْهِمْ بِمِثْلِ هَذَا، فَلَمَّا رَأَوْا أَنَّهُمْ لَا يُتْرَكُونَ مِنْ أَنْ يُسْأَلُوا، قَالُوا: نُرِيدُ أَنْ تَرُدَّنَا إِلَى الدَّارِ الدُّنْيَا فَتُقَاتِلَ فِي سَبِيلِكَ حَتَّى نَقْتَلَ فِيكَ مَرَّةً أُخْرَى - لِمَا يَرَوْنَ مِنْ ثَوَابِ الشَّهَادَةِ - فَيَقُولُ الرَّبُّ جَلَّ جَلَالُهُ: إِنِّي كَتَبْتُ أَنَّهُمْ إِلَيْهَا لَا يَرْجِعُونَ.»

“Roho za mashahidi zimo ndani ya ndege wa kijani na wanazunguka Peponi kama watakavyo. Kisha zinajificha ndani ya taa zilizotundikwa chini ya Kiti cha Enzi (cha Allah). Mola wako Atawaangalia na Atawauliza, ‘Mnataka nini?’ Watajibu, ‘Tutake nini tena wakati Umetupa neema ambazo Hukuwapa viumbe wengine?’ Kisha Akalirejea suali kama hilo, Walipotanabahi kuwa wataulizwa (mpaka wajibu) walijibu, ‘Tunatamani Uturudishe katika maisha ya duniani, ili tupigane mpaka tuuawe katika njia Yako tena, (kwa sababu ya starehe wazipatazo kama malipo ya ushahidi).’ Kisha Mola Akasema, ‘Nimeshaandika kuwa hawatarejeshwa kwenye maisha ya dunia tena.”¹

Imam Ahmad alitaarifu kutoka kwa Imamu Shafii kutoka kwa Imamu Malik kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Abdur-Rahman bin Ka'b bin Malik alisimulia kutoka kwa baba yake kuwa Mtume ﷺ alisema:

«نَسَمَةُ الْمُؤْمِنِ طَائِرٌ تَعْلُقُ فِي شَجَرِ الْجَنَّةِ حَتَّى يَرْجِعَهُ اللهُ إِلَى جَسَدِهِ يَوْمَ يَبْعَثُهُ»

“Roho ya muumini ni (itageuzwa umbile la) ndege ambaye anakula kutoka katika miti ya Peponi mpaka Allah Atakapoirejeshwa kwenye mwili wake siku, Atakapomfufua.”²

Hadithi hii inawahusu waumini wote katika maana ya jumla. Hivyo, ukweli kwamba Qur'ani inawataja mashahidi hususani katika Aya ya hapo juu ambayo inakusudia kuwapa hadhi, kuwatukuza na kuwaneemesha (japokuwa waumini wengine wanapata malipo kama hayo).

¹ Muslim 3:1502.

² Ahmad 3:455.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ
 الصَّابِرِينَ ﴿١٥٣﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٤﴾
 وَأُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٥﴾

155. "Hapana shaka Tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri."

156. "wale ambao ukiwasibu msiba husema: hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Tutarejea."

157. "Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi na rehema. Nao ndio wenye kuongoka."

Subira ya Muumini Kutokana na Mateso Humfanya Alipwe Thawabu:

Allah تعالى Anatufahamisha kuwa, Huwapa mtihani na Kuwajaribu waja Wake, kama Alivyosema katika Aya nyingine.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجْتَهِدِينَ مِنكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَنَبْلُوا أَحْبَابَكُمْ ﴿٤٧﴾

"Na bila ya shaka Tutakujaribuni mpaka Tuwadhihirishe wapiganao Jihadi katika nyinyi na wanao subiri. Nasi Tutazifanyia mtihani habari zenu." (47:31)

Hivyo mara, Huwapa mtihani wa neema au mateso ya hofu na njaa.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

فَأَذِقَهَا اللَّهُ لِبَاسِ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ

"Kwa hivyo Allah Akauvika vazi la njaa na khofu." (16:112)

Watu wenye khofu na njaa huonesha athari za mateso kwa nje, na hii ndio sababu Allah تعالى Ametumia neno 'Libas' (nguo) ya khofu na njaa katika Aya hapo juu, Allah تعالى Ametumia maneno:

بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ

“Kwa chembe ya khofu na njaa.”

Maana yake: Kidogo kwa kila kimoja. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ

“Na upungufu wa mali.”

Maana yake: Baadhi ya mali itaangamizwa,

وَالْأَنْفُسِ

“Watu.”

Maana yake: Kupoteza marafiki, ndugu na vipenzi kwa mauti,

وَالْتَّمَرَاتِ

“Na matunda.”

Maana yake: Bustani na mashamba hayatatoa mazao kama ilivyo ada yake. Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema:

وَنَشِيراً الصَّابِرِينَ ﴿١٥٦﴾

“Na wabashirie wanaosubiri.”

Kisha Ameelezea Maana ya ‘wanaosubiri’, ambao Amewasifu:

الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

“Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye hakika tutarejea.” (2:156)

Wanasema kauli hii ya kujifariji baada ya kupotelewa, wanajua kuwa wao ni wa Allah تعالى na kuwa Yeye Hufanya Alitakalo kwa waja Wake. Pia wanajua kuwa amali yoyote hata yenye uzito wa chembe ndogo kabisa haitopotea Siku ya Hukumu. Hivyo ukweli huu unawafanya wakubali kuwa wao ni waja wa Allah تعالى na marejeo yao yatakuwa ni Kwake, Siku ya Kiyama. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema kuhusu kile Alichowapa:

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ

“Hao juu yao zitakuwa Baraka zilizo kwa Mola wao Mlezi na rehema.”

Maana yake: Rehema za Allah تعالى zitakuwa pamoja nao. Said bin Jubair aliongeza, “Maana yake ni, usalama dhidi ya mateso.”¹

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ

“Nao ndio wenye kuongoka.”

Amirul Muuminina Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, “Ni uadilifu wa pekee katika mizani, na ziada katika malipo.”

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ

“Hao juu yao zitakuwa baraka zilizo kwa Mola wao Mlezi na rehema.”

Nazo hizo ni amali njema za namna mbili.

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ

“Nao ndio wenye kuongoka.”

Hiki ndio kilele.² Kilele maana yake malipo, na watu hawa watalipwa wanachostahili na zaidi ya hivyo.

Ubora wa Kurejea kwa Allah تعالى Wakati wa Msiba (Istirjaa).

Zimepokelewa Hadithi nyingi zinazotaja malipo kwa kurejesha msiba kwa Allah تعالى kwa kusema:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

“Hakika sisi ni wa Allah, na Kwake Yeye hakika tutarejea.”

¹ Ibn Abu Hatim 1:158. Isnadi yake ni dhaifu ndani yake yupo Abdallah bin Luhai'ah.

² Al-Hakim 2:270.

Miongoni mwa Hadithi ni ile iliyopokelewa na Imam Ahmad aliyetaarifu kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisimulia: Siku moja, Abu Salamah رضي الله عنه alirejea baada ya kuwa na Mtume ﷺ na alisema: “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema maneno ambayo yalinifanya nifarijike.” Alisema,

«لَا يُصِيبُ أَحَدًا مِنَ الْمُسْلِمِينَ مُصِيبَةٌ تَسْتَرْجِعُ عِنْدَ مُصِيبَتِهِ ثُمَّ يَقُولُ: اللَّهُمَّ أَجْرِي فِي مُصِيبَتِي وَأَخْلِفْ لِي خَيْرًا مِنْهَا، إِلَّا فَعَلَ ذَلِكَ بِهِ»

“Hapana Muislam anayepatwa na msiba, kisha akasema: Istirjaa wakati wa msiba wake, na kisha akasema, “Ewe Allah Nilipe kutokana na msiba huu, na Unibadilishie kwa Kunipa kilicho bora kuliko hicho! Bali atafanyiwa hivyo kwa kurejesha msiba kwa Allah.”

Umm Salama رضي الله عنها alisema: Hivyo niliyahifadhi maneno hayo kutoka kwa Mtume ﷺ. Alipofariki Abu Salamah رضي الله عنه nilirejesha msiba kwa Allah تعالى kwa kusoma ile dua, ‘Inna lillahi Wainna ilayhi Rajiun:’ Allahumma Ajirniy...” Kisha niliuliza nafsi yangu kwa kusema: “Nitampata wapi mwanaume bora kwangu kuliko Abu Salamah?” Eda yangu ilipomalizika Mtume ﷺ aliomba ruhusa ya kuingia kuniona nilipokuwa naitia rangi ngozi (ya mnyama) niliyokuwa nayo. Niliosha uchafu kutoka katika mikono yangu, nikamruhusu aingie, nikampa mto akaukalia.

Kisha akaniposa, na alipomaliza maneno yake nilimuambia, “Ewe Mtume! Sio kwa sababu sikutaki, lakini nina wivu sana na nachelea kuwa mtovu wa adabu na kufikia kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu.

Pia mimi ni mzee na nina watoto.” Akajibu,

«أَمَّا مَا ذَكَرْتِ مِنَ الْغَيْرَةِ فَسَوْفَ يُذْهِبُهَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ عَنْكَ، وَأَمَّا مَا ذَكَرْتِ مِنَ السِّنِّ فَقَدْ أَصَابْتِي مِثْلُ الَّذِي أَصَابَكَ، وَأَمَّا مَا ذَكَرْتِ مِنَ الْعِيَالِ فَإِنَّمَا عِيَالُكَ عِيَالِي»

“Ama kwa wivu ulioutaja, Allah Aliyetukuka Atakuondolea. Na kwa suala la uzee kama ulivyosema, uzee wangu ni kama wako. Na jambo la kuwa una watoto, hao ni wanangu pia.”

Akasema, “Nimesalimu amri kwa Mtume ﷺ.” Mtume ﷺ alimuoa, naye Umm Salama رضي الله عنها akasema baadaye, “Allah تعالى Amenibadilishia kwa Kunipatia

aliye mbora kuliko Abu Salamah, maana yake Mtume ﷺ.¹ Muslim alieleza Hadithi hii kwa ufupi.²

﴿ إِنِّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ۖ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَنْ يَطَّوَّفَ بِهِمَا ۚ وَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴾

158. “Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji kwenye Nyumba hiyo na akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anayejitendea mwenyewe kheri basi bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye Shukrani na Mjuzi.”

Sababu ya Allah ﷻ kusema kuwa “Si Kosa” Kufanya Saayi baina ya As-Safa na Al-Marwah

Imam Ahmad alitaarifu kuwa Urwa alisema, nilimuambia Aisha رضي الله عنها: Unaonaje kuhusu Allah ﷻ Alivyosema:

﴿ إِنِّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ۖ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَنْ يَطَّوَّفَ بِهِمَا ۚ ﴾

“Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji kwenye Nyumba hiyo au kafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka.”

Nikasema (tena), “Wallah! Si kosa endapo mtu hatofanya Saayi.” Aisha رضي الله عنها akasema, “Umeelewa vibaya, Ewe mwana wa dada yangu! ya kuwa si kosa kuacha kuzunguka baina ya mlima Safwa na Marwa. Basi Ayah hii iliteremshwa kuhusiana na Ansar, ambao kabla ya Uislam, walikuwa wakifanya *Ihlal* au (Ihram kwa ajili ya Haj) katika eneo Mushallal kwa ajili ya sanamu Manat waliokuwa wakiliabudu. Wale waliokuwa ndani ya *Ihlal* kwa ajili ya Manat, walikuwa wakisita kufanya Sa’ayi kati ya Milima ya As-Safa na Al-Marwa. Hivyo wakati wa zama za Uislamu, walimuuliza Mtume ﷺ kuhusu hili, “Ewe

¹ Ahmad 4:27.

² Muslim 2:633.

Mjumbe wa Allah! Wakati wa Jahiliyyah, tulikuwa tunasita kufanya *Sa'ayi* kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah*, basi Allah تعالى Akateremsha.

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ۗ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَنْ يَطَّوَّفَ بِهِمَا ۗ ﴾

“Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji kwenye Nyumba hiyo au kufanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka.”

Kisha Aisha رضي الله عنها akasema, “Mtume ﷺ akaweka utaratibu wa kufanya *Sa'ayi* kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah* na hivyo hapana kuacha kufanya *Sa'ayi* kati yake.¹ Hadithi hii ilinukuliwa katika Bukhari na Muslim.

Katika masimulizi mengine, Imam Az-Zuhri alitaarifu kuwa Urwah alisema: Baadaye mimi (Urwa) nilimuambia Abubakar bin Abdur-Rahman bin Harith bin Hisham (kuhusu kauli ya Aisha رضي الله عنها) naye alisema, ‘Sijawahi kusikia habari hiyo. Hata hivyo, niliwasikia wanazuoni wakisema kuwa watu wote, isipokuwa wale waliotajwa na Aisha رضي الله عنها, walisema, “*Sa'ayi* yetu baina ya vilima hivi viwili ni ada za *Jahiliyyah*.” Wengine miongoni mwa Ansar walisema, “Tuliamrisha kufanya *Tawaf* ya *Ka'bah*, lakini sio kati ya *As-Safa* na *Al-Marwa*.” Hivyo, Allah تعالى Akateremsha:

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ۗ ﴾

“Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu.”

Kisha Abubakar bin Abdur-Rahman alisema, “Inaelekea kuwa Ayah hii iliteremshwa kuhusu makundi haya mawili.”² Al-Bukhari alikusanya masimulizi sawa na haya kutoka kwa Anas رضي الله عنه.

Ash-Shabi alisema, “*Isaf* (Sanamu) lilikuwa juu ya *As-Safa* ambapo *Naila* (Sanamu) lilikuwa juu ya *Al-Marwah*, na walikuwa wakiyagusa (au kuyabusu).

¹ Ahmad 6:144.

² Fa'thul Al-Bari #:581, na Muslim 2:929.

Uislam ulipokuja, walikuwa wanasita kufanya Sa'ayi kati ya vilima hivyo. Baadaye, Aya (2:258) hapo juu ikateremshwa."

Hukumu ya Sa'i (Kuenda matiti) Baina ya As-Safa na Al-Marwa:

Muslim aliandika Hadith ndefu katika Sahih yake kutoka kwa Jabir رضي الله عنه inayoeleza kuwa Mtume ﷺ alipomaliza kuzunguka Al-Ka'bah alikwenda kwenye Rukni (nguzo kwa maana Jiwe Jeusi) akalitolea salaam na akalibusu kisha akatoka nje kupitia mlango wa As-Safa huku akisoma,

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ط ﴾

"Hakika vilima vya Saafa na Marwah ni katika alama za Mwenyezi Mungu."

Kisha Mtume ﷺ alisema, "Ninaanza kwa kile ambacho Allah تعالى Alikianza katika kuamrisha (maana yake ni kuanzia Sa'i) (Kwenda haraka) katika Kilima cha As-Safa." Katika mapokezi mengine ya An-Nasai, Mtume ﷺ alisema, "Anzeni na kile Aliachoanza nacho Allah تعالى (yaani As-Safa)."¹

Imam Ahmad alitaarifu kuwa Habiba Bint Abu Tajrah رضي الله عنها alisema, nilimuona Mtume ﷺ akifanya Sa'ayi kati ya As-Safa na Al-Marwah, ambapo watu walikuwa mbele yake, naye alikuwa nyuma yao akitembea katika Sa'i. Niliona nguo yake ikizunguka magoti yake kwa sababu ya mwendo mkali katika Sa'i na huku akisema.

«اسْعُرَا فَإِنَّ اللَّهَ كَتَبَ عَلَيْكُمُ السَّعْيَ»

*"Fanyeni Sa'i, kwani Allah Amefaradhisha Sa'i juu yenu."*²

Hadithi hii ilitumiwa kama ushahidi kuwa Sa'i baina ya Kilima cha As-Safa na Mar'wa ni Rukn³ (nguzo) ya Hajj. Pia ilinenwa kuwa Sa'i ni Wajibu⁴ na si nguzo ya Hajj na iwapo mtu ataiacha kwa bahati mbaya au kwa makususdi, atafidia kosa hilo kwa Damm⁵ (kuchinja mnyama). Na husema kuwa ni Sunna. Na

¹ Muslim 2:886 na An-Nasai 5:239.

² Ahmad 6:421.

³ Nguzo ambayo ikiwa haikutekelezwa basi Ibada husika itabidi irudiwe upya.

⁴ Jambo la lazima, ambalo kama halikufanywa linaweza kufanyiwa kafara kama ilivyoelekezwa.

⁵ Namna ya kafara ambapo huchinjwa mnyama huko Makkah na kugawiwa masikini.

usahihi kuwa *Sai* nguzo na wala si wajibu. Allah تعالی Ameeleza kuwa kutufu kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah* ni miongoni mwa Alama za Allah تعالی, maana yake, miongoni mwa vitendo ambavyo Allah تعالی Alivifaradhisha kwa Mtume Ibrahim عليه السلام wakati wa Hajj. Mwanzoni tulitaja Hadithi ya Ibn Abbas رضي الله عنهما, kuwa chanzo cha *Sa'ikin*atokana na *Tawaf* ya Hajar (mke wa Nabii Ibrahim عليه السلام), alipotembea kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah* akitafuta maji kwa ajili ya mwanae (Ismail عليه السلام), Ibrahim عليه السلام aliwaacha Makka ambapo hapakuwa na mtu yeyote mwingine. Hajar alichelea kwamba mwanaye angekufa, alisimama na kumuomba Allah تعالی Amsaidie na akawa akienda na kurudi kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah*, sehemu iliyotukuka. Alikuwa mnyenyekevu, mwoga na msikivu mbele ya Allah تعالی. Allah تعالی Alijibu Dua yake, Akamuondoshea upweke, Akahitimisha mtanzuko wake na Akakifanya kisima cha Zamzam kutoa maji kwa ajili yake, ambacho maji yake ni:

«طَعَامٌ طَعْمٌ، وَشِبَاءٌ سُقْمٌ»

“Chakula chenye lishe na tiba ya maradhi.”

Kwa hiyo, yeyote anaye *Sa'i* kati ya *As-Safa* na *Al-Marwa* ni muhimu akumbuke unyenyekevu wake na haja yake kwa Allah تعالی ya kumuomba kuuongoza moyo wake, kuzipa ufanisi amali zake na kusamehewa madhambi yake. Pia amtake Allah تعالی Amuondolee mapungufu na makosa na Amuongoze katika njia iliyonyooka. Amuombe Allah تعالی Ampe uimara katika hayo mpaka yatakapomfika mauti, na Ambadilishie hali kutoka katika ile ya kufanya madhambi na makosa kuwa hali ya ukamilifu na kusamehewa, sawa na majaaliwa aliyopewa Hajar. Kisha Allah تعالی Amesema:

وَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا

“Na anayejitendea mwenyewe kheri.”

Ilisemwa kuwa Ayah hii inaelezea kufanya *Tawaf* zaidi ya idadi iliyowajibishwa (mara saba) kwa kufanya mara nane, au tisa au zaidi. Pia ilisemwa kuwa *Tawaf* hiyo ni katika Sunnah ya *Umrah* au *Hajj*. Pia imesemwa ina maana ya kuzidisha kufanya kheri katika ibada nyinginezo. Hayo ni maoni ya Ar-Razi رحمه الله تعالى¹. Maoni ya tatu yalitolewa na Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى. Allah Ndiye Mjuzi.

¹ Ar-Razi 4:146.

Allah تعالى Amesema:

فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٥٣﴾

“Basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye Shukrani na Mjuzi.”

Ina maana, Allah تعالى Hulipa malipo Makubwa kwa amali ndogo, na Anajua kiwango cha malipo hayo.

Hivyo, hakuna shaka kwamba Hatompunja yeyote katika malipo.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۗ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٥٤﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Hulizidisha na Hutoa kutoka kwake malipo makubwa.” (4:40)

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَأَهْدَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ ۗ

أُولَٰئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّعْنُونَ ﴿١٥٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَبَيْنُوا فَاُولَٰئِكَ

أَتُوبُ عَلَيْهِمْ ۗ وَأَنَا التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٥٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا ۗ أُولَٰئِكَ

عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٥٧﴾ خَالِدِينَ فِيهَا لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ

وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿١٥٨﴾

159. “Hakika wale wanaoficha Tuliyoateremsha – nazo ni hoja zilizo wazi na uwongofu baada ya Sisi Kuzibainisha kwa watu Kitabuni – hao Anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani kila wenye kulaani.”

160. “Ila wale waliotubu na wakafanya vitendo vyema na wakabainisha, basi hao Nitapokea toba yao, na Mimi ni Mwenye Kupokea toba na Mwenye Kurehemu.”

161. “Hakika waliokufuru na wakafa hali ni makafiri, hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote.”

162. “Watadumu humu. Hawatapunguziwa adhabu wala Hawatapewa muda wa kupumzika.”

Laana ya Milele kwa Wanaoficha Sheria za Dini:

Aya zinaonya kwa ukali dhidi ya wale wanaoficha dalili za wazi walizotumwa nazo Mitume ambazo zinaongoza katika njia sahihi na mwongozo unaonufaisha nyoyo. Ni baada ya Allah تعالى Kuyaweka wazi kwa Waja Wake Kupitia Vitabu Alivyowateremshia Manabii. Abu Al-Aliyah alisema kwamba Ayat hizi, "Ziliteremshwa kuhusu Watu wa kitabu walioficha sifa bainifu za Muhammad ﷺ."¹ Kisha Allah تعالى Amesema kuwa kila kitu kinawalaani watu hao kwa uovu wao. Bila shaka, kama ilivyo kila kitu kinamuomba msamaha mwanachuoni, hata samaki baharini na ndege hewani, hivyo basi wale wanaoficha elimu wanalaaniwa na Allah تعالى na viumbe wengine wenye kulaani.

Hadithi katika Musnad, iliyosimuliwa kupitia njia za hadithi zenye kuthibitishana zenyewe. Inasema kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه na wengineo walisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ سُئِلَ عَنْ عِلْمٍ فَكْتَمَهُ، أَلْجِمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِلِجَامٍ مِنْ نَارٍ»

*"Mwenye kuulizwa juu ya elimu aliyonayo, lakini akaificha, atafungwa hatamu ya moto kuzunguka mdomo wake, Siku ya Kiyama."*²

Pia imenukuliwa na Al-Bukhari kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, "Kama isingekuwa kuna Aya (hii) katika Kitabu cha Allah تعالى, nisingelisimulia Hadithi kwa mtu yeyote."

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَأَهْدَىٰ

"Hakika wale wanaoficha Tuliyoateremsha – nazo ni hoja zilizo wazi na uongofu."³

Mujahid alisema, "Ardhi inapopatwa na ukame, wanyama husema, "Hii ni kwa sababu ya wenye dhambi miongoni mwa Wana wa Adam. Allah تعالى Awalaani wenye dhambi miongoni mwa Wanadamu."⁴

¹ Ibn Abu Hatim 1:170.

² Ahmad 2:495.

³ Fat'hul Al-Bari 1:258.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:175.

Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bi Anas na Qatadah walisema kuwa,

وَيَلْعَنُكُمُ اللَّعْنُونَ ﴿١٥٣﴾

“Na wanawalaani kila wenye kulaani.”¹

Maana yake: Malaika na waumini huwalaani wao. Na imekuja katika Hadithi ya kuwa Mwanazuoni humtakia yeye msamaha kila kitu hadi samaki baharini. Aya (2:159) inaeleza kuwa wale wanaoficha elimu watalaaniwa (duniani) na siku ya Kiyama, na Allah تعالى, malaika, viumbe wote, na wale wanaolaani (pamoja na wanyama) kila mmoja kwa njia yake tofauti. Allah تعالى ni Mjuzi Zaidi. Allah تعالى Amewatoa katika adhabu ya laana waliotubia Kwake:

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَبَيَّنُوا

“...ila wanaotubu na wakafanya vitendo vyema na wakabainisha.”

Aya hii inawahusu wale wanaojutia waliyoyafanya na wakasahihisha tabia zao na wakarekebisha hali zao, hivyo wakawaeleza watu yale waliyokuwa wakiyaficha.

فَأُولَٰئِكَ أَتُوبُ عَلَيْهِمْ وَأَنَا التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٥٤﴾

“Basi hao Nitapokea toba yao, na Mimi ni Mwenye Kupokea toba na Mwenye Kurehemu.”

Aya hii inaonesha kuwa wale waliokuwa wanalingania kwenye bidaa, au hata kufuru, na wakatubia kwa Allah تعالى, Atawasamehe. Baadaye Allah تعالى Anaeleza kuwa wale watakaomkanusha Yeye na wakabaki katika hali hiyo mpaka wakafa, basi,

أُولَٰئِكَ عَلَيْهِمُ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٥٥﴾ خَلَدِينَ فِيهَا

“Hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote. Watadumu humo.”

لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ

“Hawatapunguziwa adhabu.” Hivyo, hawatapunguziwa adhabu.

¹ Ibn Abu Hatim 1:174.

وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿١٥٣﴾

“Wala hawatapewa muda wa kupumzika.”

Adhabu haitobadilishwa au kusitishwa hata kwa muda. Bali ni ya mfululizo na ya kudumu. Tunaomba hifadhi kwa Allah تعالی kutokana na mwisho mbaya.

Kuwalaani Makafiri Inaruhusiwa

Hakuna ubishi kuwa ni halali kuwalaani makafiri. Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه na Maimam waliomfuatia walikuwa wakiwalaani makafiri katika *Qunut* (aina ya Dua) wakati wa Sala na matukio mengine. Ama kuhusu kumlaani Kafiri Makhsusi, baadhi ya wanazuoni wanasema kuwa hairuhusiwi kumlaani, kwa sababu hatujui Allah تعالی Amemuandikia khatima ya namna gani. Wengine wamesema inaruhusiwa kumlaani Kafiri makhsusi. Ushahidi kwa hili, ni kisa cha mtu ambaye kila wakati akiadhibiwa kwa kunywa pombe, mtu mmoja akasema, “Allah تعالی Amlaani! Kila mara analetwa (kupigwa viboko kwa kunywa pombe).” Mtume ﷺ akasema:

«لَا تَلْعَنُهُ فَإِنَّهُ يُحِبُّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ»

“Msimlaani, kwani yeye anampenda Allah na Mtume Wake.”¹

Hadithi hii inadhihirisha kuwa inaruhusiwa kuwalaani wale wasiompanda Allah تعالی na Mjumbe Wake ﷺ. Allah تعالی ni Mjuzi wa yote.

وَاللَّهُ كَرِيمٌ إِنَّهُ وَاحِدٌ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾

163. “Na Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu, hapana muabudiwa ila Yeye. Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.”

Katika Aya hii, Allah تعالی Anasema kuwa Yeye Pekee Ndiye Mwenye haki ya kuabudiwa na kuwa Yeye Hana mshirika wala aliye sawa Naye. Yeye ni Allah تعالی, Mmoja Tu, Mlishaji, na hakuna Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye. Yeye ni Mwingi wa Rehema - *Ar-Rahman*, Mwenye Kurehemu - *Ar-Rahim*. Tulielezea maana ya Majina haya Mwanzoni mwa Surat Al-Fatihah. Shahr bin Hawshab alitaarifu kuwa Asma bint Yazid bin As-Sakan رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Abdur-Razaq 7:381, halikadhalika Al-Bukhari, Na. 6780.

«اسْمُ اللَّهِ الْأَعْظَمُ فِي هَاتَيْنِ الْآيَتَيْنِ

“Jina kubwa kabisa la Allah limo katika Ayah Mbili zifuatazo.”

﴿وَاللَّهُكَرِيمُ﴾ وَاللَّهُ وَاحِدٌ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾

“Na Mungu wenu ni Mmoja tu, hapana muabudiwa ila Yeye. Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.” (2:163),

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ﴾

“Alif Laam Miim. Mwenyezi Mungu, hakuna muabudiwa ila Yeye Aliye Hai, Msimamizi wa yote milele.” (3:1-2)¹

Kisha Allah تعالى Anataja, katika aya zifuatazo, baadhi ya ushahidi kuwa Yeye Peke Yake Ndiye Mungu. Kuwa Aliumba mbingu na ardhi na viumbe anuwai, na vyote vinashuhudia kuwa Yeye ni Mmoja.

* * *

¹ Abu Dawud 2:168.

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ
 وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنْزَلَ
 اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَّاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ
 فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيْحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ
 بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٦٤﴾ وَرَبِّ
 النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ
 يَرُونَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ
 الْعَذَابِ ﴿١٦٥﴾ إِذْ تَبَرَأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا
 وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٦﴾ وَقَالَ الَّذِينَ
 اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّا كُنَّا نَدْرِكُهُمْ لَسَأَلْنَا لَهُمْ أَنْ يَهْتَدُوا لَنَا
 كَمَا تَبَرَّءُوا مِنَّا كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَلَهُمْ حَسْرَتٍ عَلَيْهِمْ
 وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٧﴾ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ كُلُّوا مِمَّا فِي
 الْأَرْضِ حَلَلًا طَيِّبًا وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ
 لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿١٦٨﴾ إِنَّمَا يَأْمُرُكُمْ بِالسُّوْءِ وَالْفَحْشَاءِ
 وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٦٩﴾

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ الَّتِي
 تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ
 وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَّاءٍ
 فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ
 فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيْحِ
 وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ
 وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٦٤﴾

164. "Hakika katika Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kukhitilafiana usiku na mchana, na merikebu ambayo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji Anayoyate-remsha Mwenyezi Mungu kutoka Mbinguni, na kwa hayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na Akaeneza humo kila aina ya viumbe; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrisha kupita

baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo ishara kwa watu wanaozingatia."

Uthibitisho wa Tawhid:

Allah تعالى Amesema:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Hakika katika Kuumbwa kwa mbingu na ardhi.”

Kwa hiyo, Mbingu, na urefu wake, usanifu wake, kuenea kwake, sayari zizungukazo na zilizotulia, na njia zake na mzunguko wa dunia katika mhimili wake. Na uzito wa dunia hii, tambarare yake, na milima, bahari, majangwa, mabonde na maumbo mengine na majengo, na vitu vingine vyenye manufaa.

Allah تعالى Anaendelea:

وَأَخْتَلَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ

“Na kuhitilafiana usiku na mchana.”

Usiku huu unakuja na kuondoka ukifuatiwa na mchana ambao hauchelewi hata kwa muda mfupi, kama Allah تعالى Alivyosema:

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ ۚ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

“Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao.” (36:40)

Kuna wakati, mchana huwa mfupi na usiku mrefu, na kinyume cha hivyo, kimojawapo huchukua urefu kutoka kwa kingine kwa kuazimana.

Vilevile Allah تعالى Amesema:

يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ

“Anaingiza usiku katika mchana, na Anaingiza mchana katika usiku.” (57:6)

Maana yake: Anaongeza urefu wa kimojawapo kutoka kwa kingine na kinyume chake.

Kisha Allah تعالى Anaendelea:

وَالْفُلُكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ

“Na merikebu ambayo hupita baharini kwa viwafaavyo watu.”

Anaitiisha bahari, ili iweze kubeba meli kutoka ufukwe mmoja kwenda mwingine, na ili watu wafaidike kutokana na walichonacho wenzao, na kusafirisha bidhaa walizonazo kwenda nchi nyingine na kinyume chake.

Kisha Allah تعالى Ameendelea:

وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

“Na maji Anayoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى au Alivyosema katika Aya nyingine:

وَأَيُّهُمُ الْأَرْضُ الْأَمْيَةَ أَحْيَيْنَاهَا وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٣٦﴾

“Na Ishara hiyo kwao - ardhi iliyokufa, nasi Tukaifufua, na Tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!” (36:33) – Mpaka

وَمَا لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾

“Na katika wasivyovijua.”

Allah تعالى Anaendelea:

وَبَتْ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ

“Na Akaeneza humo kila aina ya viumbe.”

Pamoja na kutofautiana maumbile yao, rangi zao matumizi na vipimo vyao, ima vidogo au vikubwa. Allah تعالى Anawajua wote na Anawapa riziki na hapana kinachojificha Kwake. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema:

* وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۗ كُلٌّ فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿١١﴾

“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6)

وَتَصْرِيفِ الرِّبْحِ

“Na katika mabadiliko ya pepo...”

Baadhi ya wakati upepo huleta rehema na wakati mwingine adhabu. Wakati mwingine huleta bishara njema kwa kufatana na mvua, wakati mwingine unayaongoza mawingu, huyachunga, huyatawanya au kuyaelekeza yaende wapi. Wakati mwingine upepo huja kutokea kaskazini (Pepo za Kaskazi) na wakati mwingine kutoka Mashariki, na kutoka Kusini, na kupiga upande wa mbele wa Ka'bah, na wakati mwingine kutoka Magharibi, ukipiga kwa upande wa nyuma yake. Kuna maelezo mengi kuhusu pepo, mvua, na kanuni zinazohusiana nazo, lakini hapa si pahala pake, na Allah تعالی ni Mjuzi Zaidi.

Allah تعالی Anaendelea:

وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Na Mawingu yanayoamrisha kupita baina ya mbingu na ardhi.”

Mawingu yanakwenda kati ya mbingu na ardhi kule ambapo Allah تعالی Anapenda yaende kwenye ardhi na maeneo Ayatakayo. Baadaye Allah تعالی Anasema:

لَا يَتَّبِعُ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٧٠﴾

“Zimo ishara kwa watu wanaozingatia.”

Maana yake: Vitu vyote na alama zilizo wazi zinazothibitisha kuwa Allah تعالی ni Mmoja.

Vivyo hivyo, Allah تعالی Amesema:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٧١﴾

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٧٢﴾

“Kwa Hakika katika Kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitilafiana usiku na mchana ziko ishara kwa wenye akili. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala na hufikiri Kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya moto.” (3:190-191)

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ ﴿١٦٥﴾ إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٦﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّا كُنَّا نَدْرِكُهُمْ لَسَأَلْتُمُوهُم كَمَا تَبَرَّأُوا مِنَّا كَذَلِكَ يَرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَلْتُمْ حَسْرَتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٧﴾

165. "Na katika watu wapo wanaochukua waungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti waliodhulumu wakajua watakapoiona adhabu kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu na kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu!"

166. "Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwishaiona adhabu; na yatakatika mafungamano yao."

167. "Na watasema wale waliofuata: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyotukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyowaonesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni."

Hali za Washirikina Duniani na Akhera na Viongozi Kuwakana Wafuasi Wao Siku ya Kiyama

Katika Aya hizi Allah تعالی Anataja hali za washirikina katika maisha ya dunia na mwisho wao Kiyama. Waliwateua wenza na washindani wa Allah تعالی wakiwaabudu pamoja na Allah تعالی na wakiwapenda, kama inavyotakiwa kumpenda Allah تعالی. Pamoja na hayo, Allah تعالی Ndiye Pekee Mwenye Haki ya kuabudiwa, Ambaye hana Mpinzani wala mshindani wala mwenzia. Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema: Niliuliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Dhambi kubwa kuliko zote ni ipi?" Alisema:

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ»

*"Kumfanya Allah ana mshirika wakati Yeye Pekee Ndiye Aliyekuumba."*¹

¹ Fat'hul-Bari 8:3 na Muslim 1:90.

Allah تعالى Amesema:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ

“Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana.”

Kwa sababu waumini hawa wanampenda Allah تعالى, wanajua Ukubwa Wake, Wanamheshimu, wanaamini katika Umoja Wake, kisha hawamshirikishi na chochote au yeyote, wanamuabudu Yeye tu Peke Yake, wanamtegemea Yeye na wanatafuta msaada kutoka Kwake, kwa kila kitu kisha baada ya hapo Mwenyezi Mungu Anawatahadharisha washirikina, waliodhulumu nafsi zao kwa Kusema;

وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرُونَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

“Na laiti waliodhulumu wakajua watakapoiona adhabu kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu.”

Iwapo watu hawa wangejua adhabu kali itakayowapata, kwa sababu ya kukufuru na Ushirikina, wangeacha kukengeuka wanakoishi nako.

Allah تعالى Anataja imani zao potofu za kuabudu masanamu, na kuwa waliofuatwa watawakana waliowafuata. Allah تعالى Alisema:

إِذْ تَبَرَأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا

“Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata.”

Malaika watawakataa wale wanaodai kuwa walikuwa wakiwaabudu duniani. Malaika watasema:

تَبَرَأْنَا إِلَيْكَ ۗ مَا كَانُوا إِيَّانَا يَعْبُدُونَ ﴿٦٣﴾

“Tunajitenga nao mbele Yako. Hawakuwa wakituabudu sisi.”

(28:63) Na watasema;

سُبْحٰنَكَ اَنْتَ وَاٰلِئِنَّا مِن دُونِهِمْ ۗ بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ الْجِنَّ ۗ اَكْثَرُهُمْ يٰۤاٰمَنُوْنَ ﴿٤١﴾

“Umeebukana na kila upungufu! Wewe Ndiye Kipenzi chetu, si hao, bali walikuwa wakiwaabudu majini, wengi wao wakiwaamini hao.” (34:41)

Majini watawakataa makafiri ambao walikuwa wakiwaabudu, na watakataa kuabudiwa huko. Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ
دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٥٦﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٥٧﴾

“Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawataitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao. Na ambao watu watakapo kusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.”
(46:5-6)

Allah تعالى Amesema:

وَاتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لِيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٨١﴾ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ
عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٨٢﴾

“Na wamechukua miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati iwape nguvu. Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.” (19:81-82)

Mtume Ibrahim عليه السلام aliwaeleza watu wake

وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا مَوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
يَكْفُرُ بَعْضُكُمْ بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُمْ بَعْضًا وَمَأْوَأَتُكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ
نَاصِرِينَ ﴿٢٥﴾

“Hakika nyinyi mmeyashika masanamu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makaazi yenu ni Motoni. Wala hamtapata wa kukunusuruni.” (29:25)

Katika Aya nyingine tena Allah تعالى Anasema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ
الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٦٧﴾ قَالَ الَّذِينَ

اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا أَنحْنُ صَدَدْنَاكُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ۗ بَلْ كُنْتُمْ
 كُفْرًا ۗ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا
 أَن نَّكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا ۗ وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي
 أَعْنَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ هَلْ يَجْزُونَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٣﴾

“Na ungeliswaona madhaalimu watakaposimamishwa mbele ya Mola wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia waliotakabari: Lau kuwa si nyinyi, bila shaka tungeli kuwa Waumini sisi. Waliotakabari watawaambia wanyonge: kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu. Na wanyonge watawaambia walio takabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu. Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliokuwa wakiyatenda?” (34:31-33)

Allah تعالى Amesema:

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ ۗ وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطَانٍ إِلَّا أَن دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي ۗ فَلَا تَلْمُزُونِي وَلُومُوا
 أَنفُسَكُمْ ۗ مَا أَنَا بِمُصْرِخِكُمْ وَمَا أَنتُمْ بِمُصْرِخِي ۗ إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا أَشْرَكْتُمُونِ
 مِن قَبْلُ ۗ إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٣﴾

“Na Shetani atasema itapokatwa hukumu: Hakika Mwenyezi Mungu Alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nalikuahidini; lakini sikukutimizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe. Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu, wala nyinyi hamuezi kuwa watetezi wangu. Hakika mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha na Mwenyezi Mungu. Hakika madhaalimu watakuwa na adhabu chungu.” (14:22)

Kisha Allah تعالى Akasema:

وَرَأُوا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٤﴾

“Na hali ya kuwa wamekwishaiona adhabu, na yatakatika mafungamano yao.”

Maana Yake: Watakapoona adhabu ya Allah تعالى, nguvu zao na njia zao za uwokovu zitakatika na hawatokuwa na njia ya kujirekebisha, wala hawatopata njia ya kutoroka kutoka motoni. Ata alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu:

وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٤﴾

“Na yatakatika mafungamano yao.”

Maana Yake: Urafiki. Mujahid aliandika kauli sawa na hii katika upokezi wa Abu Najih.¹ Allah تعالى Amesema:

وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّا كُنَّا نَدْرِكُهُمْ لَسَخَّطْنَا لَهُمْ عَمَلَهُمْ وَجَعَلْنَاهُمْ كَالْحِجَارَةِ ﴿١٦٥﴾

“Na watasema wale waliofuata: Laiti tungeweza kurudi tutawakataa wao kama wanavyotukataa sisi.”

Aya hii ina maana: Iwapo tungepata nafasi ya kurudi kwenye maisha ya duniani ili tuweze kuwakanusha (masanamu, viongozi n.k.) na tusiwaabudu tena na tuwapuuze na tumuabudu Allah تعالى Peke Yake badala yao. Lakini wanatamka uongo kuhusu hili, kwani kama wangepewa fursa ya kurejea duniani, wangeparudia yale waliyokatazwa kuyafanya. Kama Allah تعالى Alivyosema:

كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ ﴿١٦٥﴾

“Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Atakavyowaonesha vitendo vyao kuwa majuto yao.”

Maana yake: Kazi zao zitapotea na kutoweka. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنثُورًا ﴿٢٣﴾

“Na Tutayaenda yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye mavumbi yaliyotawanyika.” (25:23)

¹ At-Tabari 3:290.

Aidha Allah تعالى Amesema:

مَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ أَعْمَلُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ ۝

“Mfano wa waliomkufuru Mola wao Mlezi – vitendo vyao ni kama jivu linalopeperushwa kwa nguvu za upepo katika siku ya dharba (upepo mkali).” (14:18)

Allah تعالى Amesema tena,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيعَةٍ مَحْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاءً

“Na waliokufuru vitendo vyao (wanavyoviona vizuri) ni kama mazigazi jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji....” (24:39)

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema mwisho wa Aya (2:167) Hapo juu.

وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٧﴾

“Wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.”

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ كُلُّوا مِمَّا فِي الْأَرْضِ حَلَلًا طَيِّبًا وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ إِنَّهُ لَكُمْ

عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿١٦٨﴾ إِنَّمَا يَأْمُرُكُم بِالسُّوءِ وَالْفَحْشَاءِ وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

168. “Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri, wala msifuata nyayo za shetani. Hakika yeye ni adui yenu aliye dhahiri.”

169. “Yeye Anakuamrisheni maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.”

Amri ya kula Vilivyohalalishwa na Makatazo ya Kufuata Nyayo za Shaytan:

Baada ya Allah تعالى Kusema kuwa hapana Mola mwenye kuabudiwa kwa haki min-ghairi ya Yeye na kusema kuwa ni Yeye Peke Yake Aliyeumba viumbe. Alielekeza kuwa Yeye ni Mlishaji wa viumbe Wake wote, na Akataja Neema Alizowapa; kisha Akawataka wale vitu visafi na vya halali vilivyomo duniani, ambavyo havina madhara kwa mwili au akili. Aidha Aliwakataza kufuata nyayo za Shaytan, yaani taratibu zake na njia zake ambazo huzitumia kuwapotosha wafuasi wake, kama kuharamisha *Bahira* (ngamia Jike ambaye maziwa yake

yalikuwa mahsusi kwa masanamu na hakuna aliyeruhusiwa kumkama), au *Saibah* (ngamia wa kike aliyeachwa kula bila kuchungwa, kwa ajili ya vijimungu na hawakuruhusiwa kupandwa au kubebeshwa mizigo) au *Wasilah* (ngamia Jike aliyeachwa huru kwa ajili ya vijimungu kwa sababu alizaa ndama jike – kifungua mimba, na kisha akazaa tena ndama jike katika mzao wa pili) na vitu vyote ambavyo Shaytan alivyovifanya kuwavutia katika zama za *Jahiliyah*. Muslim alimnukuu Iyad bin Himar رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Amesema,

يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: إِنَّ كُلَّ مَالٍ مَتَّحْتُهُ عِبَادِي فَهَوَ لَهُمْ حَلَالٌ، - وَفِيهِ - وَإِنِّي خَلَقْتُ
عِبَادِي حُرَفَاءَ، فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَاجْتَالَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ، وَحَرَمْتُ عَلَيْهِمْ مَا أَحَلَلْتُ
لَهُمْ

“Kila aina ya utajiri Niliyowapa Waja Wangu ni halali kwao, Nimewaumba Waja wangu Hunafa-a (safi bila ushirikina), lakini Shaytani aliwaghilibu na kuwapotosha kutoka kwenye Dini sahihi na anawakataza vile Nilivyowahalalishia.”¹

Allah تعالى Amesema:

إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١٧٨﴾

“Hakika yeye ni adui yenu aliye dhahiri.”

Akiwaonya dhidi ya Shetani. Allah تعالى pia Amesema:

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١٧٩﴾

“Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni.” (35:6) na,

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿١٨٠﴾

“Je! Mnamfanya yeye na dhuriya wake kama marafiki badala Yangu, hali wao ni adui zenu? Ni uovu mkubwa mno badala hii kwa wenye kudhulumu.” (18:50)

Qatadah na As-Suddi waliyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالى:

¹ Muslim 4:2197.

وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ

“Wala msifuuate nyayo za Shaytani.”

Kila tendo la kumuasi Allah تعالى ni miongoni mwa nyayo za Shaytani.¹

Abd bin Humayd alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kila Nadhiri au kiapo anachokiapa mtu huku akiwa na hasira, ni miongoni mwa nyayo za shetani, fidia yake ni kama fidia ya kiapo cha uongo.”² Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا يَأْمُرُكُمْ بِالسُّوءِ وَالْفَحْشَاءِ وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٦٩﴾

“Yeye anakuamrisheni maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.” (2:169)

Aya hii ina Maana: Adui yenu, Shaytani anakuamrisheni kufanya maovu na yaliyo mabaya kabisa, yaani kumzungumzia Allah تعالى bila elimu. Hukumu hii inawahusisha makafiri na kila wafanyao bid'a:

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 1:221.

² Kuwalisha watu kumi, kuwavisha, kumwacha huru mtumwa, au kufunga kwa siku tatu; rejea Qur'an 5:89.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ نَتَّبِعُ مَا
 أَلْفَيْنَا عَلَيْهِ ءِآبَاءَنَا ؕ أُولَٰئِكَ كَانُوا ءِآبَاءَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ
 شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٧٠﴾ وَمِثْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ
 الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً ؕ صُمُّ بِكُمْ
 عُمَىٰ فَهَمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٧١﴾ يَتَّبِعُهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا
 كُلُّوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَأَشْكُرُوا لِلَّهِ إِن كُنتُمْ
 إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾ إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالْدَّمَ
 وَلَحْمَ الْخَيْزِرِ وَمَا ءُهِلَّ بِهِ لِغَيْرِ اللَّهِ ؕ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ
 بَٰغٍ وَلَا عَادٍ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ؕ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٧٣﴾
 إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ الْكِتَابِ
 وَيُسْتَرُونَ بِهِ ؕ ثَمًّا قَلِيلًا ؕ أُولَٰئِكَ مَا يَأْكُلُونَ فِي
 بُطُونِهِمْ إِلَّا النَّارَ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا
 يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٤﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا
 الضَّلَالَةَ بِالْهَدَىٰ وَالْعَذَابَ بِالْمَغْفِرَةِ ؕ فَمَا أَصْبَرَهُمْ عَلَى
 النَّارِ ﴿١٧٥﴾ ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ
 الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِي الْكِتَابِ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿١٧٦﴾

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 قَالُوا بَلْ نَتَّبِعُ مَا أَلْفَيْنَا عَلَيْهِ ءِآبَاءَنَا
 ؕ أُولَٰئِكَ كَانُوا ءِآبَاءَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ
 شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٧٠﴾ وَمِثْلَ الَّذِينَ
 كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا
 يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً ؕ صُمُّ بِكُمْ
 عُمَىٰ فَهَمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٧١﴾

“170. Na wanapoambiwa: Fuateni Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyouakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuo-ngoka?”

171. “Na mfano wa waliokufuru ni kama mfano wa anayempigia kelele asiyesikia ila wito na sauti tu – ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hiyo hawaelewi.”

Tabia ya Washirikina Inatokana na Kuiga

Allah تعالى Amesema kuwa makafiri wa kishirikina wakilinganiwa kuwa: “Fuateni yale ambayo Allah تعالى Amemteremshia Mjumbe Wake ﷻ na muache vitendo vya kijinga na vya upotofu mvifanyavyo.” Wanajibu, “Bali tunafuata yale tuliyozaea, tuliyouyakuta baba zetu wakiyafuata.”

Maana, kuabudu masanamu na miungu kadhaa. Allah تعالى Alizikosoa fikra zao kwa Kusema:

أُولَئِكَ كَانُوا آبَاءَهُمْ

“Je, hata ikiwa baba zao.”

Maana yake: Wale wanaowafuata na ambao wanaiga vitendo vyao;

لَا يَعْقِلُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿٧٧﴾

“Walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?”

Maana yake: Hawakuwa na uelewa sahihi au mwongozo. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii iliteremshwa kuhusu kikundi cha Mayahudi ambao walilinganiwa katika Uislam na Mtume ﷺ, lakini walikataa, wakisema, “Bali tutafuata yale tuliyoyakuta yakifuatwa na babu zetu.” Hivyo Allah تعالى Aliteremsha Aya hii (2:170) hiyo hapo juu.¹

Kafiri ni kama Hayawani.

Allah تعالى Alipiga mfano wa makafiri, kama Alivyosema katika Ayah nyingine:

لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ مَثَلُ السَّوْءِ^ط

“Hali ya wasioamini Akhera ni ovu.” (16:60)

Vile vile, Allah تعالى Amesema katika Aya (2:171)

وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Na mfano wa waliokufuru.”

Maana yake: Katika udhalimu, kupotoka na ujinga, wao ni sawa na wanyama wanaovinjari, wasioelewa wanachoambiwa; kama mchungaji atapiga mbiu au kuwalingania katika yake yenye faida nao, hawataelewa wanachoambiwa, kwani wanasikia sauti zisizo na maana. Haya yamenukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah, Mujahid, Ikrimah, Ata, Al-Hasan, Qatadah, Ata Al-Khurasani² na Ar-Rabi bin Anas.

¹ At-Tabari 3:305. Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 1:228.

صَمُّ بِكُمْ عُمَىٰ

“Ni viziwi, mabubu, vipofu.”

Maana yake: Ni viziwi, kwa kuwa hawausikii ukweli, mabubu, kwa kuwa hawautamki; na vipofu, kwa kuwa hawauoni na hawaitambui njia yake.

فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٧٦﴾

“Kwa hivyo hawaelewi.”

Ina maana: Hawazingatii wala hawaelewi kitu chochote.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كَلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَأَشْكُرُوا لِلَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ
تَعْبُدُونَ ﴿٧٧﴾ إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالْدَّمَ وَالْخَنِزِيرَ وَمَأْأَهُلَ بَيْمِهِ لِعَٰلِمٍ
فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٨﴾

172. “Enyi mlioamini! Kuleni vizuri Tulivyo kurukuzuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye tu.”

173. “Yeye Amekuharamishieni mzoga na damu na nyama ya nguruwe na kilichotajiwa, katika kuchinjwa kwake, jina la asiye kuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliyefikiwa na dharura bila kutamani wala kupita kiasi, yeye hana dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Amri ya Kula Vyakula vya Halali na Maelezo ya Vyakula vya Haramu.

Allah تعالى Amewaamuru waja Wake waumini kula vyakula vilivyo halali ambavyo Ameviumba na wamshukuru kwa hayo, kama wao ni waja wake hasa. Kula kutokana na vyanzo vya halali ni sababu ya kupokelewa Dua na Ibada. Ni kama ilivyo kula kutokana na vyanzo vya haramu, kunazuia kupokelewa Dua na ibada. Hadithi iliyonukuliwa na Imam Ahmad, imeeleza kuwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

¹ Ibn Abu Hatim 1:228.

«أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ اللَّهَ طَيِّبٌ، لَا يَقْبَلُ إِلَّا طَيِّبًا، وَإِنَّ اللَّهَ أَمَرَ الْمُؤْمِنِينَ بِمَا أَمَرَ بِهِ الْمُرْسَلِينَ، فَقَالَ: ﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُلُوا مِن الطَّيِّبَاتِ وَاعْمَلُوا صَالِحًا إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ﴾¹، وَقَالَ: ﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ﴾ ثُمَّ ذَكَرَ الرَّجُلَ يُطِيلُ السَّفَرَ أَشْعَثَ أَغْبَرَ يَمُدُّ يَدَيْهِ إِلَى السَّمَاءِ: يَا رَبِّ يَا رَبِّ، وَمَطْعَمُهُ حَرَامٌ، وَمَشْرَبُهُ حَرَامٌ، وَمَلْبَسُهُ حَرَامٌ، وَغُذِيَ بِالْحَرَامِ فَأَنَّى يُسْتَجَابُ لِذَلِكَ؟»

“Enyi watu! Allah ni Tayyib (safi na mzuri) na Hakubali isipokuwa kilicho Tayyib. Kwa hakika Allah Amewaamuru Waumini kile Alichowaamuru Manabii, kwani Amesema: “Enyi Manabii! Kuleni Tayyibat na mtende amali njema. Kwa hakika Nayajua myatendayo.” (23:51) na ‘Enyi mlioamini! Kuleni vya halali Tulivyokuruzukuni.’ (21:72). Kisha akamtaja mtu anayesafiri masafa marefu, ambaye nywele zake zikiwa timtimu na amechafuka kwa vumbi, anainua mikono yake mbinguni, na anasema, ‘Ewe Mola! Ewe Mola!’ Ilhali chakula chake mtu huyo kinatokana na haramu, vinywaji vyake ni haramu, mavazi yake ni haramu na amenawirishwa kwa vitu vya haramu. Hivyo. Dua yake itakubaliwa vipi?”¹ Hadithi hii ilinukuliwa pia na Muslim na At-Tirmidhi.²

Baada ya Allah تعالى Kutaja namna Alivyowaneemesha waja Wake kwa Kuwaruzuku, na baada ya Kuwaamrisha kula vyakula vya halali Alivyowaruzuku. Kisha Ameerza kuwa Hakuwakataza chochote isipokuwa nyamafu. Nyamafu ni wanyama wanaokufa bila kuchinjwa, kama vile kunyongwa, kupigwa kwa nguvu, kuanguka na kutanguliza kichwa, kupigwa pembe au kuliwa sehemu na mnyama pori. Vyakula vya Baharini havihusiki na kanuni hii, kama itavyoelezwa baadaye, Allah تعالى Akipenda.

Allah تعالى Alisema:

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ

“Nyinyi mmehalalishiwa kuvua vinyama vya baharini na kuvila.”
(5:96)

¹ Ahmad 3:328.

² Muslim 2:703, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:333.

Kadhalika uthibitisho wa Hadithi inayohusu nyangumi iliyonukuliwa ndani ya Sahihi.¹ Katika Al-Musnad, Al-Muwatta na Sunnah iliyonukuliwa kutoka kwa Mtume ﷺ inayozungumzia bahari.

«هُوَ الطَّهُورُ مَاؤُهُ وَالْحِلُّ مَيْتَتُهُ»

“Maji yake ni safi na maiti wake wamehalalishwa.”²

Ash-Shafi, Ahmad, Ibn Majah na Ad-Daraqutni walitaarifu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَجِلٌّ لَنَا مَيْتَانِ وَدَمَانِ، السَّمَكُ وَالْجَرَادُ وَالْكَبِدُ وَالطَّحَالُ»

“Tumehalalishiwa maiti mbili na damu mbili: Samaki na nzige; na ini na wengu.”³

Tutajadili mada hii tena katika Surat *Al-Maidah* (Sura ya 5 ndani ya Qur’an), Inshaallah.

Mas-ala: Kwa mujibu wa Ash-Shafii رحمه الله تعالى na wanazuoni wengine, maziwa na mayai ambavyo viko ndani ya mnyama mfu ambaye hajachinjwa sio halali kwa maana ni najisi, kwa sababu ni sehemu ya mnyama mfu. Katika moja ya mapokezi ya Malik رحمه الله تعالى alisema kuwa hayo ni Twahara, lakini hunajisika kutokana na eneo waliopo. Vivyo hivyo, kuna rai tofauti kuhusu jibini (inayotengenezwa kwa maziwa) ya wanyama wafu. Rai maarufu ya wanazuoni ni kuwa ni najisi (chafu), japokuwa wanataja ukweli kuwa Masahaba walikula jibini iliyotengenezwa na Majusi (wanaoabudu moto). Hivyo, Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alitoa maelezo: “Jibini ya mnyama mfu ambayo sehemu kubwa imetokana na maziwa ni halali, kwa sababu najisi ndogo haidhuru endapo itachanganywa na maji mengi.”¹ Ibn Majah alitaarifu kuwa Salman رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu siagi, jibini na manyoya ya kondoo. Akasema:

«الْحَلَالُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ فِي كِتَابِهِ، وَالْحَرَامُ مَا حَرَّمَ اللَّهُ فِي كِتَابِهِ، وَمَا سَكَتَ عَنْهُ فَهُوَ
مِمَّا عَفَا عَنْهُ»

¹ Fat’hul Al-Bari 6:152.

² Ahmad 5:365 Al-Muwatta 1:22, An-Nasai 1:50, na Ibn Majah 1:136. Tuhfat Ahwadi 3:224

³ Tartib Musnad Ash-Shafi 2:173, Ahmad 2:97, Ibn Majah 2:1073, Ad-Daraqutni 4:272.

“Halali ni kile Alichokihalalisha Allah ndani ya Kitabu Chake, Na haramu ni kile Alichokiharamisha Allah ndani ya Kitabu Chake. Na kitu ambacho Hakukitaja ni sehemu ya Alichokisamehe.”¹

Allah تعالی Ameharamisha kula nyama ya nguruwe, iwe imechinjwa au laa. Mafuta yake nayo yanafuata hukumu ya nyama yake, ama kwa sababu ya kuhusiana nayo, au kwa sababu neno *Lahm* linajumuisha na mafuta, au kwa sababu ya mfanano (*Qiyas*) (ulinganifu, mshabihiano) wa maoni. Vile vile kimeharamishwa kilichochinjwa kwa ajili ya kitu min-ghairi ya Allah تعالی, kile kilichochinjwa kwa jina ambalo sio Lake, kama vile kwa ajili ya sanamu ya ukumbusho, miungu, na ramli, au desturi nyingine za Jahiliyah. Al-Qurtubi رحمه الله تعالی alitaja kuwa mama Aisha رضي الله عنها aliulizwa kuhusu vichinjwa visivyokuwa vya Waislamu, kisha wakatoa sehemu kama zawadi kwa Waislamu. Alijibu, “Msile katika kilichochinjwa kwa ajili ya siku zao (au karamu) lakini kuleni vitokanavyo na mimea (nafaka, mboga n.k.).”²

Vilivyoharamishwa Vinaruhusiwa kwa wenye Dharura:

Kisha Allah تعالی Alihalalisha kuliwa vyakula vilivyoharamishwa, katika hali ya dharura, ili mtu aishi au kama hakuna vyakula vya halali. Allah تعالی Amesema:

فَمَنْ أَضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ

“Lakini akifikwa na dharura bila ya kutamani wala kupita kiasi.”

Maana yake: Bila ya kuchupa mipaka,

فَلَا إِنَّمِ عَلَيْهِ

“Yeye hana dhambi.”

Ina maana: Iwapo mtu atakula aina hiyo ya vitu, kwa ajili ya dharura.

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

¹ Ibn Majah 2:1117.

² Al-Qurtubi 2:224 na Ibn Abii Shaiba (3334, 24856).

Mujahid alisema, “Endapo mtu atalazimika na akala bila kukusudia kuvunja Amri wala kuchupa mipaka iliyowekwa. Kwa mfano kama kupora watu barabarani, kuwaasi watawala, au aina nyingime za kumuasi Allah تعالى, hivyo anaruhusiwa. Lakini endapo mtu anachupa mipaka, au kwa lengo la kumuasi Allah تعالى, huyo ruhusa haimuhusu japo alikuwa na shida sana.” Maelezo sawa na haya yalitaarifiwa kutoka kwa Zaid bin Jubayr. Said na Muqatil bin Hayyan wamenukuliwa kuwa walisema: Maana ya,

غَيْرَ بَاغٍ

‘Bila kukusudia uasi’ Ni “Bila kuamini kuwa imehalalishwa.”¹ Ilinukuliwa kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maoni juu ya maneno ya Allah تعالى.

غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ

“Bila kutamani wala kupita kiasi.” “Bila kuchupa mipaka kwa kula nyamafu, wakati vyakula halali vinapatikana.”²

Qatadah amenukuliwa akitafsiri Ayah hii akisema, maana: ‘bila kuchupa mipaka katika kula nyamafu kwa kula haramu wakati vyakula vya halali vinapatikana.’

Mas-ala: Mtu akiwa na njaa inayohatarisha maisha kisha ikawepo nyamafu, na chakula halali, lakini cha watu, ambacho iwapo atakila hatapewa hukumu ya mwizi na kukatwa mkono wala hatapatwa na matatizo yoyote basi haruhusiwi kula nyamafu bali atakula kile chakula cha halali. Hilo halina ukindano.

Ibn Majah alitaarifu kuwa ‘Abbad bin Shurhabil Al-Ghubar alisema, “Tulikuwa na njaa kwa mwaka mzima. Nikaja Al-Madinah, nikaingia kwenye shamba. Nikachukua shuke moja, nikalipukuchua na nikala (punje zake), kisha kilichobakia niliweka kwenye nguo yangu. Mwenye shamba akaja akanifanyia fujo na akachukua nguo yangu. Kisha nilienda kwa Mtume ڤي na nikamueleza yaliyonisibu. Naye alimuambia yule mwenye shamba:

¹ Ibn Abu Hatim 1:236.

² At-Tabari 3:324.

«مَا أَطَعْتَهُ إِذْ كَانَ جَائِعًا - أَوْ سَاعِيًا - وَلَا عَلَّمْتَهُ إِذْ كَانَ جَاهِلًا» فَأَمَرَهُ فَرَدُّ إِلَيْهِ
نُوبَهُ، فَأَمَرَ لَهُ بِوَسْقٍ مِنْ طَعَامٍ أَوْ بِنَصْفِ وَسْقٍ.


*"Hukumlisha alipokuwa na njaa, pia hukumfundisha kama alikuwa mjinga." Mtume ﷺ alimuamrisha mwenye shamba amrudishie Abad nguo yake, na ampe wasaq au nusu wasaq ya chakula."*¹

Hadithi hii ina silsila madhubuti ya wapokezi na maelezo yake yanatiliwa nguvu na Hadithi. Kama vile Hadith ambayo Amri bin Shua'yb aliipokea kutoka kwa baba yake kuwa babu yao alisema: Mtume ﷺ aliulizwa juu ya chane la tende lililokuwa linaning'inia. Akasema:

«مَنْ أَصَابَ مِنْهُ مِنْ ذِي حَاجَةٍ بِفِيهِ غَيْرَ مُتَّخِذٍ حُبْنَهُ، فَلَا سِيءَ عَلَيْهِ»

*"Hapana madhara kwa yeyote anayechukua sehemu na akala kukidhi haja bila kuchukua katika nguo zake."*²

Muqatil bin Hayyan aliitolea maelezo:

فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ^ع إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ 

"Yeye hana dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."

Inakusudiwa chakula, "Kinacholiwa kutokana na dharura."³ Naye Said bin Jubayr alisema, "Allah تعالى Anamsamehe kutokana na kula chakuala cha haramu na ana huruma alipomruhusu yeye kula haramu wakati wa dharura."⁴ Masruq alisema, "Mtu ambaye atakuwa katika hali mbaya, halafu akaacha kula na kunywa mpaka akafa, ataingizwa motoni."⁵ Hii inadhihirisha kuwa kula nyamafu kwa wale wanaohitajia ili waendeleo kuishi sio tu imeruhusiwa bali inahitajika (inalazimika).

¹ Ibn Majah 2:770.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 4:510.

³ Ibn Abu Hatim 1:240.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:240.

⁵ Al-Bayhaqi katika As-Sunnah Al-Kubra 9:357.

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ الْكِتَابِ وَيَشْتُرُونَ بِهِ مِمَّا قَلِيلًا أُولَئِكَ مَا
 يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ إِلَّا النَّارَ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ
 عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٠﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالََةَ بِالْهُدَىٰ وَالْعَذَابَ بِالْمَغْفِرَةِ ۗ فَمَا
 أَصْبَرَهُمْ عَلَى النَّارِ ﴿١٧١﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِي
 الْكِتَابِ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿١٧٢﴾

174. "Hakika wale wafichao Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu, wakanunua kwacho thamani ndogo, hao hawali matumboni mwao isipokuwa moto, wala Mwenyezi Mungu Hatawasemeza siku ya Kiyama, wala Hatawatakasa. Nao watapata adhabu chungu."

175. "Hao ndio walionunua upotofu badala ya uwongofu, na adhabu badala ya maghira. Ama wavumilivu wa Moto watu hawa!"

176. "Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Ameteremsha Kitabu kwa haki. Na wale waliokhitilafiana katika kitabu wamo katika upinzani ulio mbali na haki."

Shutuma kwa Mayahudi kwa Kuficha Yaliyoteremshwa na Allah تعالى:

Allah تعالى Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ الْكِتَابِ

"Hakika wale wafichao Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu."

Ina Maana Mayahudi ambao walificha sifa bainifu za Muhammad ﷺ zilizoandikwa kwenye vitabu vyao, zote zinathibitisha ukweli kuwa ni Nabii na Mtume. Walizificha taarifa hizo ili wasipoteze madaraka na nafasi walizokuwa nazo kwa Waarabu, ambao walikuwa wanawaletea zawadi na kuwaheshimu. Mayahudi (Allah تعالى Awalaani) walihofia kutangaza walichokijua kuhusiana na Muhamad ﷺ kwa kuchelea kutelekezwa na watu na badala yake kumfuata yeye. Hivyo waliuficha ukweli ili walinde hadhi zao, na waliuza nafsi zao kwa faida hii ndogo. Walikhitari kidogo wanachopata badala ya uongofu na kufuata

ukweli, kumuamini Mtume ﷺ na kuamini yale ambayo Allah تعالى Alimtuma nayo. Kwa hiyo wamerudi patupu na wamechuma hasara duniani na Akhera. Ama kwa hapa duniani, Allah تعالى Aliufahamisha ukweli kuhusu Mtume Wake ﷺ, kwa dalili zilizo wazi na ushahidi usiopingika. Baadaye, wale ambao Mayahudi walikhofia kuwa wangemfuata Mtume ﷺ, walimuamini na kumfuata, na hivyo wakawa wafuasi waliomsaidia dhidi yao. Hivyo, Mayahudi walikasirikiwa juu ya laana ambayo iliwaifika kabla, na Allah تعالى Aliwashutumu mara kadhaa katika Kitabu Chake. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema katika Aya (2:174),

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ الْكِتَابِ وَشَرُّوا بِهِ نَمَتًا قَلِيلًا^١

“Hakika wale wafichao Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Kitabu, wakanunua kwacho thamani ndogo.”

Maana yake: Furaha na raha za maisha haya ya dunia. Allah تعالى Amesema:

أُولَئِكَ مَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ إِلَّا النَّارَ

“... hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto...”

Ina maana: Chochote wanachokula kama malipo ya kuficha ukweli, kitabadilika na kuwa moto matumboni mwao Siku ya Kiyama. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا^٢ وَسَيَصْلَوْنَ

سَعِيرًا ﴿٤١٠﴾

“Hakika wanaokula mali za mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia motoni.”
(4:10)

Pia, imenukuliwa katika Hadithi sahihi ya kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الَّذِي يَأْكُلُ أَوْ يَشْرَبُ فِي آيَةِ الذَّمِّ وَالْفِضَّةِ إِنَّمَا يُجْرَجُ فِي بَطْنِهِ نَارَ جَهَنَّمَ»

“Wale wanaokula kwa kutumia vyombo vya dhahabu au fedha wanajaza moto wa Jahanamu matumboni mwao.”¹

¹ Sahih Al-Bukhari Na 5634, na Muslim Na. 2065.

Allah تعالى Anasema:

وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٠﴾

“Wala Mwenyezi Mungu Hatawasemeza Siku ya Kiyama, wala Hatawatakasa. Nao watapata adhabu chungu.”

Hii ni kwa sababu Allah تعالى Amewakasirikia kwa kuuficha ukweli. Hivyo wanastahiki ghadhabu ya Allah تعالى, Allah تعالى Hatowaangalia au Kuwatakasa. Ina maana kuwa Hatowasifia bali Atawafanya waonje mateso makali.

Kisha Allah تعالى Amesema juu yao.

أُولَئِكَ الَّذِينَ اشْتَرُوا الضَّلَالََةَ بِالْهَدَىٰ

“Hao ndio walionunua upotofu badala ya uwongofu.”

Hivyo, waliupinga uongofu. Maana yake kuzitangaza sifa bainifu za Mitume ambazo walizikuta kwenye Vitabu vyao, taarifa za Utume wake na bishara njema za kuja kwake ambazo zilitangazwa na Mitume waliotangulia, pia kumfuata na kumuamini. Badala yake wakachagua upotofu kwa kumkanusha, kumkataa na kuzificha sifa zake ambazo zilitajwa katika Vitabu vyao.

Allah تعالى Amesema:

وَالْعَذَابَ بِالْمَغْفِرَةِ ۚ

“Na adhabu badala ya maghfira.”

Maana yake: Walipendelea adhabu badala ya maghfira kutokana na makosa waliyoyafanya. Kisha Allah تعالى Amesema:

فَمَا أَصْبَرَهُمْ عَلَى النَّارِ ﴿١٧١﴾

“Ama wavumilivu wa Moto watu hawa!”

Allah تعالى Anahabarisha ya kuwa wao watakuwa katika adhabu kali na kubwa, atashangaa atakayewaona wao, kutokana na adhabu na mateso watakayokutana nayo. Tunajilinda na Allah تعالى na adhabu hiyo. Na Kauli Yake,

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ ۚ

“Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Ameteremsha Kitabu kwa haki.”

Maana yake: Wanastahiki adhabu hii kali sababu Allah تعالى Aliteremsha kwa Wajumbe Wake Muhammad ﷺ, na Mitume kabla yake vitabu, na Wahyi huu unaudhihirisha ukweli na kuuweka wazi upotofu. Pamoja na hayo walizichukulia Alama za Allah تعالى kama jambo la masikhara. Vitabu vyao viliwaamrisha kuutangaza ukweli na kueneza elimu, lakini badala yake, walificha elimu hiyo na wakaipinga. Nabii wa Mwisho – Muhammad ﷺ - aliwalingania kwa Allah تعالى, aliwaamrisha kufanya mema na akawakataza kutenda maovu. Hata hivyo walikataa, walimkanusha na kumkengeuka na wakauficha ukweli walioujua kumhusu yeye. Hivyo wakaifanyia istihizai Aya ambayo Allah تعالى Alimteremshia Mjumbe Wake ﷺ, na kwa sababu hii wanastahili mateso na adhabu.

Allah تعالى Amesema,

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَّلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ الَّذِينَ أَحْتَلَفُوا فِي الْكِتَابِ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿١٧١﴾

“Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Ameteremsha Kitabu kwa haki. Na wale waliokhitilafiana katika Kitabu wamo katika upinzani ulio mbali na haki.”

* * *

* لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ
 وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ
 وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَءَاتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ
 وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَآثَرَ السَّبِيلِ وَالسَّالِينَ فِي آثَارِ
 وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا
 عَاهَدُوا^ط وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ^ط
 أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا^ط وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾ يَتَأْتِيهَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ^ط أَلْحَرُّ بِأَحْرَ
 وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ^ط فَمَنْ عَفَىٰ لَهُ مِنْ أَخِيهِ
 شَيْءٌ فَاتَّبِعْ بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ^ط ذَلِكَ تَخْفِيفٌ
 مِنْ رَبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ^ط فَمَنْ آعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ
 أَلِيمٌ ﴿١٧٨﴾ وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَاةٌ يَا أُولِيَ الْأَلْبَابِ
 لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧٩﴾

* لَيْسَ الْبِرُّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ
 الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ
 ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
 وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ
 وَءَاتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ ذَوِي
 الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَآثَرَ
 السَّبِيلِ وَالسَّالِينَ فِي آثَارِ
 وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ
 وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا^ط
 وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ
 الْبَأْسِ^ط أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا^ط
 وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

177. "Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema ni wa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali juu ya kuwa wanaipenda, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika wanaowaachia huru watumwa, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanaotimiza ahadi yao wanapoahidi, na wanaovumilia katika ufakiri na maradhi makubwa na wakati wa vita; hao ndio waliosadikisha, na hao ndio wamchao Mwenyezi Mungu."

Mjumuiiko wa Wema.

Aya hii ina hikma kubwa, inayojumuisha maamrisha, kanuni zilizo wazi na Imani sahihi na taratibu za jumla za kisharia. Ama kuhusu maelezo ya Aya, mwanzoni, Allah تعالی Aliwaamrisha waumini kuelekea upande wa *Bayt Al-Maqdis*, kisha kuelekea upande wa Ka'bah wakati wa Sala. Mabadiliko hayo yalikuwa magumu kwa baadhi ya Watu wa Kitabu, na hata kwa baadhi ya Waislamu. Kisha Allah تعالی Akateremsha Wahyi uliofafanua hikima ya Amri hii kwamba malengo ya kufanya hivyo ni utii kwa Allah تعالی na kuelekea popote Atakapoelekeza na kufuata Sheria Zake. Huu ndio wema, uchamungu na Imani iliyotimia na siyo kama kuelekea Mashariki au Magharibi ndiyo uadilifu au utiifu kama haikutokana na kutekeleza Amri na Sharia za Allah تعالی.

Allah تعالی Amesema:

﴿لَيْسَ الْبِرُّ أَنْ تُولُوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ

الْآخِرِ

“Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi. Bali wema ni wa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Ni sawa na mfano Alioulezea Allah تعالی katika *Adhahi* na *Kafara*:

﴿لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنكُمْ

“Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu Wala damu zao, lakini unamfikia uchamungu wenu.” (22:37)

Abu Al-Aliyah alisema, “Mayahudi walikuwa wakielekea Magharibi kama Kiblah chao, ambapo Wakristo walikuwa wakielekea Mashariki kama Kiblah chao.

Hivyo Allah تعالی Akasema:

﴿لَيْسَ الْبِرُّ أَنْ تُولُوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ

“Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi.” (2:177)

Maneno haya yanaonesha imani ni ipi na kuwa ukweli wa imani ni matendo. Maelekezo sawa na hayo yalitaarifiwa kutoka kwa Al-Hasan na Ar-Rabi bin Anas.¹ Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema:

وَلَيْكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ

“Bali wema ni wa anayemuamini Mwenyezi Mungu.”

Na Akasema, Aya hii imekusanya aina zote za wema.² Ni kweli aliyoyasema. Allah تعالى Amrehemu. Kwa hakika, anayesifika kwa sifa zilizotajwa katika Aya hii atakuwa ameingia katika Uislam kwa ukamilifu na atakuwa amekusanya aina zote za kheri, nazo ni Imani kwa Allah تعالى kwamba Yeye tu Ndiye Mwenye Kuabudiwa kwa haki, na kuamini kuwepo Malaika ambao ni wajumbe baina ya Allah تعالى na Manabii Wake. **“Na Vitabu”** Ni neno linalojumuisha Vitabu Vitakatifu vilivyoteremshwa kutoka Mbinguni kwenda kwa Mitume mpaka vikakamilishwa na Kitabu kitukufu kabisa Qur’an ambayo imevishinda Vitabu vyote vilivyotangulia, kina taja aina zote za uadilifu, na njia ya kuifikia furaha ya hapa duniani na kesho Akhera. Qur’an inafuta Vitabu vyote vilivyotangulia na inawathibitisha Mitume wote wa Allah تعالى, kuanzia Mtume wa Mwanzo Adam عليه السلام mpaka Mtume wa Mwisho, Muhammad ﷺ, Rehema na Amani za Allah تعالى ziwafikie wote.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ

“Na akatoa mali juu ya kuwa anaipenda.”

Maana yake: Akatoa mali akiwa anaipenda na ana haja nayo. Imenukuliwa ndani ya Sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَفْضَلُ الصَّدَقَةِ أَنْ تَصَدَّقَ وَأَنْتَ صَاحِبٌ سَجِيحٌ، تَأْمَلُ الْغِنَىٰ وَتَخْشَى الْفَقْرَ»

“Sadaka nzuri ni ile unayoitoa ukiwa na afya njema na roho ya hadhari ya ubakhili; ukitarajia kutajirika na ukiuogopa ufakiri.”³

¹ Ibn Abu Hatim 1:251.

² Ibn Abu Hatim 1:253.

³ Fat’hul Al-Bari 3:334, na Muslim 2:716.

Allah تعالی Amesema,

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٧٧﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا ﴿٧٨﴾

“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini na mayatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya kupata Radhi za Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.” (76:8-9) Na,

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ^٤

“Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda...” (3:92)

Kauli ya Allah تعالی,

وَيُؤْتِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ^٥

“Bali wanawapendelea wengine kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji.” (59:9)

Hawa ni watu wenye hadhi ya juu kuliko wale waliotajwa mwanzo wanaotoa wanachokihitajia, wakati wale waliotajwa katika Aya zilizotangulia wanatoa vile ambavyo hawavipendi sana. Kauli ya Allah تعالی ,

ذَوَى الْقُرْبَىٰ

“Jamaa.” Inakusudiwa Jamaa, ambao wana haki zaidi kuliko mtu yeyote mwingine katika Sadaka ya mtu, kama hadithi inavyounga mkono hilo.

«الصَّدَقَةُ عَلَى الْمَسَاكِينِ صَدَقَةٌ، وَعَلَى ذِي الرَّحِمِ اثْنَانِ: صَدَقَةٌ وَصِلَةٌ، فَهُمُ أَوْلَى النَّاسِ بِكَ وَبِبِرِّكَ وَإِعْطَائِكَ»

“Sadaka anayopewa masikini ni Sadaka. Sadaka wanayopewa jamaa ina faida mbili: ni Sadaqa na pia ni kuimarisha udugu. Kwani wao wanastahili zaidi kwako huruma yako na msaada wako.”¹

Allah تعالی Ameerisha kuwafanyia wema jamaa katika sehemu nyingi ndani ya Qur’an Tukufu.

¹ Ahmad 4:214.

وَالْيَتَامَىٰ

“Na mayatima,...” Mayatima ni watoto ambao hawana mtu wa kuwatunza, waliwapoteza baba zao wakiwa wadogo. Ni dhaifu na hawana uwezo wa kujitafutia mahitaji yao muhimu kwa kuwa hawajafikia baleghe na umri wa kufanya kazi. Abdur Razzaq alitaarifu kuwa Ali رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema: *“Hakuna uyatima baada ya baleghe.”*¹

وَالْمَسْكِينِ

“Na masikini,...” Masikini ni watu wasio na chakula, mavazi ya kuwatosha wala makazi. Hivyo Masikini wanapaswa kupewa mahitaji yao ya lazima ili yawasaidie kuondoa matatizo yao. Katika Sahihi mbili imenukuliwa kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَيْسَ الْمَسْكِينُ بِهَذَا الطَّرَافِ الَّذِي تَرُدُّهُ التَّمْرَةُ وَالتَّمْرَتَانِ، وَاللُّقْمَةُ وَاللُّقْمَتَانِ،
وَلَكِنَّ الْمَسْكِينُ الَّذِي لَا يَجِدُ غِنَىٰ يُغْنِيهِ وَلَا يُفْطِنُ لَهُ فَيَتَصَدَّقَ عَلَيْهِ»

*“Masikini si yule anayezurura, na mahitaji yake yanakidhiwa kwa kupewa tende mbili au moja au vitafunwa viwili. Bali, Masikini ni yule asiyepata mtu wa kumsaidia na ambaye watu hawana habari naye, hivyo hawampi Sadaka.”*²

وَأَبْنِ السَّبِيلِ

“Na Msafiri,...” Huyu ni msafiri mhitaji aliyeishiwa na uwezo wa kujikimu. Hivyo anatakiwa apewe kiasi cha fedha ili kimsaidie kurejea mjini mwake. Pia anayetaka kusafiri safari ya mambo ya kheri ya Allah تعالى atapewa mahitaji ya safari yake ya kwenda na kurudi. Wageni pia wanahusika katika fungu hili. Ali bin Abu Talhah alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, *“Ibn As-Sabil’ ni mgeni, na wenyeji wake ni Waislam.”*³ Zaidi, Mujahid, Said bin Jubayr, Abu Jafar Al-Baqir, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Az-Zuhri, Ar-Rabi bin Anas na Muqatil bin Hayyan walisema vivyo hivyo.⁴

¹ Abu Razzaq 6 / 416. Isnadi yake ni dhaifu.

² Fat’hul Al-Bari 3:399 na Muslim 2:719.

³ Ibn Abu Hatim 1:259.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:260.

وَالسَّابِغِينَ

“Na waombao,...” Hawa ni watu wanaojidhihirisha kuomba na wao hupatiwa Zaka na Sadaka.

وَفِي الرِّقَابِ

“Na katika ugombozi,...”

Hawa ni watumwa ambao wanataka kujikomboa, lakini hawawezi kupata fedha za kununua uhuru wao. Tutaeleza zaidi kuhusu makundi haya wakati wa kutafsiri katika Aya kuhusu Sadaqah katika *Surat Baraah* (Sura ya 9 ya Qur'an), Inshaallah.

وَأَقَامَ الصَّلَاةَ

“Na akawa anasimamisha Sala.” Maana yake: Akateleleza matendo yote ya Sala. Kama vile kusali kwa wakati wake uliopangwa, rukuu, sujudu, kutulizana na kunyenyekea kama inavyoelekeza Sharia. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَتَى الزَّكَاةَ

“Na akatoa zaka.” Maana yake: Zakah inayotakiwa kutokana na mali ya mtu. Ni kama Said bin Jubayr na Muqatil bin Hayyan walivyoieleza.¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَالْمُؤْفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا

“Na wanaotimiza ahadi yao wanapoahidi.”

Ni sawa na Kauli Yake Allah تعالى,

الَّذِينَ يُؤْفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْعِمَّةَ ﴿٢٠﴾

“Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano.” (13:20).

Sifa zilizo kinyume cha sifa hizi bainifu ni unafiki. Kama ilivyo katika Hadithi:

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبًا، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اتَّخَذَ خَانَ»

“Alama za mnafiki ni tatu; Anaposema, huongopa; na anapoahidi huvunja miadi; na anapoaminiwa, hufanya khiyana.”²

¹ Ibn Abu Hatim 1:264.

² Muslim 1:78.

Katika mapokezi mengine:

«إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا عَاهَدَ غَدَرَ، وَإِذَا خَاصَمَ فَجَرَ»

“Anapozungumza, huongopa; anapoapa, huvunja kiapo; na anapogombana hufanya vibaya.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالصَّرَآءِ وَحِينَ الْبَأْسِ²

“Na wanaovumilia katika ufakiri na maradhi makubwa na wakati wa vita.”

Maana yake: Wanavumilia katika hali ya umasikini na katika hali ya maradhi.

وَحِينَ الْبَأْسِ³

“Na wakati wa vita.”

Maana yake: Katika uwanja wa vita wanapokabiliana na adui, kama Ibn Masu'ud, Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah², Murrah Al-Hamdani³, Mujahid, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Qatadah⁴, Ar-Rabi bin Anas, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan, Abu Malik, Adh-Dhahhak na wengine رضي الله عنهم walivyoelezea.⁵

Na kuhimiza kusubiri katika hali hizi, ni kutokana na mateso na matatizo yanayoambatana nayo katika wakati huo. Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi, Kwake tunataka msaada na Kwake tunategemea. Kauli ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا^ط

“Na ndio waliosadikisha.”

Maana yake: Yeyote mwenye kuwa na sifa hizi, hao ndio wa kweli katika imani zao. Kwa sababu wana imani ndani ya nyoyo zao na wanazifasiri katika vitendo na kwa ndimi zao. Hivyo ni waaminifu.

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

“Hao ndio wajilindao.”

Kwa sababu wamejilinda na vilivyoharamishwa na wakafanya amali kwa utiifu.

¹ Muslim 1:78.

² Ibn Abu Hatim 1:270.

³ Ibn Abu Hatim 1:271.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:270.

⁵ At-Tabari 3:355.

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ ۗ أَحْرَ بِأَحْرٍ وَأَعْبُدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ
بِالْأُنثَىٰ ۗ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتَّبِعْ بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَنٍ ۗ ذَلِكَ
تَخْفِيفٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ ۗ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٨﴾ وَلَكُمْ فِي
الْقِصَاصِ حَيَوةٌ يَتَأْتِي الْآلِيبِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧٩﴾

178. "Enyi mlioamini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika walio uawa - muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema, na yeye alipe kwa ihsani. Huko ni kupunguziwa kulikotokana na Mola wenu Mlezi, na ni rehema. Na atakayevuka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu chungu."

179. "Mtakuwa nao uhai mzuri katika kulipiza kisasi enyi wenye akili, ili msalimike."

Sheria ya Kisasi na Ubainifu wa Maslahi Yaliyomo Ndani Yake.

Allah تعالیٰ Ameerleza: Enyi waumini! Sharia ya usawa imeandikwa kwenu na kuweni waadilifu katika hilo (kwa kesi za mauaji), Muungwana kwa Muungwana (huru kwa huru), mtumwa kwa mtumwa na mwanamke kwa mwanamke. Kwa hivyo, msichupe mipaka, kama wengine kabla yenu walivyoichupa, wakabadili yale waliyoandikiwa na Allah تعالیٰ. Sababu iliyopelekea kauli hii ni kuwa kabila la Kiyahudi (Banu An-Nadhir) waliwavamia Quraydhah (kabila jingine la Mayahudi) zama za Jahiliyyah (Kabla ya Uislam) na wakawashinda. Hivyo, (wakatunga sharia kuwa) mtu kutoka Nadhir akimuua mtu kutoka Quraidhah, hauliwi kulipiza kisasi, bali hulipa Wasq mia moja za tende.¹ Hata hivyo, mtu kutoka Quraydhah akimuua mtu wa Nadhir, atauwawa kulipiza kisasi. Kama Nadhir walitaka fidia kutoka kwa muuaji Quraidhah hulipa Wasq mia mbili za tende (mara mbili ya Nadhir wanayolipa kama fidia.) Hivyo Allah تعالیٰ Aliamuru kuwa haki itendeke kuhusiana na Sharia zinazoainisha makosa na adhabu zake na kuwa njia ya waliopotoshwa na watu mafasiki iepukwe, ni ya ambaye yuko

¹ Mzigo abebao Ngamia, Sa'sitini, kadiri ya lita 165. Au kilo gramu 13060 kwa mtazamo wa jopo la wanazuoni wa Kiislamu (Jamhuri).

katika kufuru na kuchupa mpaka, anakanusha na kubadili yale Aliyowaamrisha Allah تعالى. Allah تعالى Amesema:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ أَلْحُرُّ بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ ۗ

“Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouwawa, muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke.”

أَلْحُرُّ بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ ۗ

“Muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke.”

Ilifutwa kwa Kauli, *“Nafsi kwa Nafsi, Roho kwa Roho.”* (5:45). Pamoja na hayo, wanazuoni walio wengi wanaafikiana kuwa Muislam hauawi kwa kumuua kafiri. Al-Bukhari alitaarifu kuwa Ali رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«وَلَا يُقْتَلُ مُسْلِمٌ بِكَافِرٍ»

“Muislamu hauawi kwa kumuua kafiri.”¹

Hakuna maoni yanayopinga amri hii yakawa sahihi, wala hapana Hadithi sahihi inayopingana nayo. Hata hivyo, madhehebu ya Abu Hanifa رحمه الله تعالى yanasema kuwa Muislamu anauliwa naye kwa kumuua Kafiri, kufuatana na maana ya ujumla ya Ayah iliyopo katika Surat Al-Maidah (Sura ya 5:45 katika Qur’an).

Mas-ala: Maimamu wanne (Abu Hanifah, Malik, Shafii na Ahmad) na wengi wa wanazuoni walieleza kuwa watu wengi walioshirikiana kumuua mtu mmoja na wao huuliwa. Umar رضي الله عنه alisema kuhusu kijana aliyeuliwa na watu saba na Umar رضي الله عنه kuhukumu nao kuuliwa, “Endapo wakazi wote wa Sana’a (mji mkuu wa Yemen) washirikiane kumuua mtu, nitawaua wote.” Hakuna maoni yanayopinga hukumu hii yaliyofahamika kwa Masahaba zama hizo, ambayo ni sawa na *“Ijma’i.”* kwa maana ya makubaliano ya pamoja ya wanazuoni. Ila kuna rai inayotokana na Imam Ahmad kuwa kundi la watu haliuwawi kwa kumuua mtu mmoja, na kuwa mtu mmoja anauwawa kwa mtu mmoja. Wamelielezea hilo Ibn Al-Mundhir kutoka kwa Muadh na Ibn Al-Zubayr, Abdul Malik bin Marwan, Az-Zuhri, Ibn Sirin na Habib bin Abu Thabit. Kauli ya Allah تعالى,

¹ Sahih Al-Bukhari Na 111.

فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتَّبَاعُ بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ^١

“Na anayesamehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema, na yeye alipe kwa ihsani.”

Msamaha ni kukubaliwa Fidia (na jamaa wa maiti) iwapo ni mauaji ya kukusudia. Rai hi ni ya Abu Al-Aliyah, Abu Sha’thai, Mujahid, Said bi Jubayr, Ata Al-Hasan¹, Qatadah² na Muqatil bin Hayyan³. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ

“Na anayesamehewa na ndugu yake chochote.”

Maana yake: Muuaji anasamehewa na ndugu yake (yaani ndugu wa aliyeuawa) kwa kutoa *Diyah* (fidia) badala ya kuuwawa na huo ndio ‘Afw (msamaha uliotajwa katika Aya).⁴ Kauli ya Allah تعالى:

فَاتَّبَاعُ بِالْمَعْرُوفِ

“Basi ashikwe kulipa kwa wema.” Maana yake, ndugu wanapokubali kuchukuwa *Diyah* (fidia), waichukue kwa wema (bila kuwa na kinyongo).

وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ^٢

“Na yeye alipe ihsani.” Maana yake, muuaji lazima akubali taratibu za suluhu (malipo na makubaliano) bila kusababisha madhara zaidi au kukataa malipo.

Ndugu wa Aliyeuliwa wana Hiari ya Mambo Matatu

Kauli Yake Allah تعالى:

ذَلِكَ تَخْفِيفٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ^٣

“...huko ni kupunguziwa kulikotokana na Mola wenu Mlezi, na ni rehema.”

Maana yake: Sharia inayoruhusu kupokea fidia katika mauaji ya kukusudia ni kupunguziwa na ni rehema kutoka kwa Mola wako kwenu. Kuliko ilivyokuwa lazima kwa wale waliotangulia kabla yenu, wao ilikuwa ama kifo au kusamehe.

¹ Ibn Abu Hatim 1:278-279.

² At-Tabari 3:368.

³ Ibn Abu Hatim 1/279.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:280. Isnadi yake ni dhaifu.

Said bin Mansur alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: “Wana wa Israeli walitakiwa kutekeleza sharia ya kisasi katika kesi za mauaji na hawakuruhusiwa kutoa msamaha (kwa kutoa *Diyah*). Allah تعالى Aliuwekea Sharia Ummah huu (Waislamu).

كُيِّبَ عَلَيْكُمْ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ ۗ الْحَرُّ بِالْحَرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ ۗ فَمَنْ عُفِيَ
لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ

“Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouwawa – muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake chochote.”

‘Kusamehe’ Maana yake ni kukubali *Diyah* katika kesi za mauaji yaliyofanywa kwa makusudi.¹ Ibn Hibban, pia aliyankuu maneno haya hii katika Sahih yake.² Qatadah amesema:

ذَلِكَ تَخْفِيفٌ مِّن رَّبِّكُمْ

“Huko ni kupunguziwa kulikotokana na mola wenu Mlezi.”

Allah تعالى Ameurehemu Ummah huu kwa Kuupa *Diyah* (fidia) ambayo hawakupewa watu wa kabla yake. Watu wa Taurati (Mayahudi) waliruhusiwa ama kutekeleza Sharia ya kuua au kumsamehe muuaji, lakini hawakuruhusiwa kuchukua *Diyah*. Watu wa Injili (Wakristo) walitakiwa kumsamehe (muuaji, lakini hawakuandikiwa *Diyah*). Ummah huu (Waislamu) wanaruhusiwa kutekeleza adhabu ya kifo au kusamehe na kukubali “*Diyah*.” Maelezo sawa na haya yalipokelewa kutoka kwa Said bin Jubayr, Muqatil bin Hayyan na Ar-Rabi bin Anas.³ Kauli ya Allah تعالى:

فَمَنْ أَعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٩﴾

“Na atakayevuka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu chungu.”

Maana yake: Wale wanaoua kwa kulipiza kisasi baada ya kuchukua au kukubali *Diyah*, Allah تعالى Atawapa adhabu kali na iumizayo. Kauli kama hii pia ilinukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas, Mujahid, Ata, Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan kuwa ni mtu ambaye anaua baada ya kuwa tayari ameshapokea fidia.⁴

¹ Sunan Said bin Mansour 2/652.

² Ibn Hibban 7:601.

³ Ibn Abu Hatim 1:285.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:278-279.

Faida ya Sheria ya Usawa na Hekima Yake:

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَوةٌ

“Mtakuwa na uhai mzuri katika kulipiza kisasi.”

Kutekelezwa sharia ya kisasi, kwa kumuua muuaji, kuna hekima kubwa kwenu. Kwa njia hii, utukufu wa uhai utahifadhiwa kwa sababu muuaji atajizuia kuuwa, kwa kuwa ana uhakika wa kuuwawa endapo ataua. Hivyo maisha yatahifadhiwa. Na katika Vitabu vilivyotangulia, kuna kauli isemayo, kuuwa kunazuia mauaji zaidi! Maana hii imewekwa wazi na umbuji ndani ya Qur’an kwa ufupi na ufasaha mkubwa.

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَوةٌ

“Mtakuwa na uhai mzuri katika kulipiza kisasi.”

Abu Al-Aliyah alisema, “Allah تعالى Aliifanyia sharia ya Usawa kuwa ‘maisha’. Hivyo ni watu wangapi walifikiria kuuwa, lakini sharia hii ikawazuia kuuwa kwa kuogopa kuuwawa baada ya hapo.” Kauli sawa na hii zimenukuliwa kutoka kwa Mujahid, Said bin Jubayr, Abu Malik, Al-Hasan, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas na Muqatil bin Hayyan.¹

يَتَأُولَى الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧٩﴾

“Enyi wenye akili, ili msalimike.”

Maana yake: “Enyi wenye akili timamu, wenye uelewa na ufahamu! Pengine kutokana na hili mtalazimika kuepuka kuchupa mipaka ya yale yaliyokatazwa na Allah تعالى na yale Aliyoyabainisha kuwa ni makosa. Neno *Taqwa* (lililotumika katika Aya) lina maana ya kufanya vitendo vya utiifu na kujizuia na yaliyoharamishwa.

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 1:290-292.

كُتِبَ عَلَيْكُمُ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ إِن تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةَ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ بِالْمَعْرُوفِ ۗ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿١٨٠﴾

فَمَنْ بَدَّلَهُ بَعْدَمَا سَمِعَهُ فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ يُبَدِّلُونَهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٨١﴾

فَمَنْ خَافَ مِنْ مُوصٍ جَنَفًا أَوْ إِثْمًا فَأَصْلَحَ بَيْنَهُمْ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨٢﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۗ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۗ فَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ ۗ وَأَن تَصُومُوا خَيْرٌ لَّكُمْ ۗ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٤﴾

شَهْرَ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ ۗ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۗ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْتُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۗ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

كُتِبَ عَلَيْكُمُ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ إِن تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةَ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ بِالْمَعْرُوفِ ۗ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿١٨٠﴾

فَمَنْ بَدَّلَهُ بَعْدَمَا سَمِعَهُ فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ يُبَدِّلُونَهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٨١﴾

فَمَنْ خَافَ مِنْ مُوصٍ جَنَفًا أَوْ إِثْمًا فَأَصْلَحَ بَيْنَهُمْ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨٢﴾

180. "Mmeandikiwa – mmoja wenu anapofikwa na mauti, kama akiacha mali – afanye wasia kwa wazazi wake na jamaa zake kwa namna nzuri inayopendeza. Ni wajibu haya kwa wachamungu."

181. "Na atakayeubadilisha wasia baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale watakaoubadilisha; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua."

182. "Na mwenye kumkhofia muusiaji kwenda kombo au kupata dhambi akasuluhisha baina yao, basi hatakuwa na dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu."

Amri ya Kutoa Wasia kwa Wazazi Wawili na Jamaa, Kisha Amri Hiyo Kufutwa kwa Warithi:

Aya hii tukufu imebeba amri ya kutoa wasia kwa wazazi wawili na jamaa, utekelezaji wa amri hii hapo awali ulikuwa ni wa lazima kwa kauli sahihi (kabla ya kuteremka kwa Aya ya Mirathi). Ilipoteremka Aya ya mafungu ya Mirathi hukumu ya Aya hii ilifutwa. Hivyo basi viwango vya warithi vinatolewa kulingana na mgao wa Allah تعالى bila kutegemea wasia wa marehemu au fadhila za muusiaji. Imesimuliwa katika Sunah na vitabu vingine, kutoka kwa Amr bin Kharijah رضي الله عنه alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema katika hotuba yake.

«إِنَّ اللَّهَ فَذَّ أَعْطَى كُلَّ ذِي حَقٍّ حَقَّهُ، فَلَا وَصِيَّةَ لِرِوَاثٍ»

“Allah Amempa kila mrithi hisa yake. Hivyo hapana wasia kwa mrithi stahiki.”¹

Imam Ahmad alinukuu kuwa Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى alisema Kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisoma Surat Al-Baqarah (Sura ya 2- Qur'an) mpaka alipofikia Aya:

إِنْ تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةُ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ

“Kama akiacha mali – afanye wasia kwa wazazi wake na jamaa zake.”

Kisha akasema, “Aya hii ilifutwa.” Pia hadithi hii ilinukuliwa na Said bin Mansur na Al-Hakim katika kitabu chake, *Mustadrak*.²

Al-Hakim alisema, “Ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya (Al-Bukhari na Muslim).” Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alitaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

الْوَصِيَّةُ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ

“Afanye wasia kwa wazazi wake na jamaa zake.”

Alisema kwamba ilifutwa na Aya hii:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 6:313, An-Nasai 6:247, na Ibn Majah 2:905.

² Said bin Mansur 2:663, na Al-Hakim 2:273.

لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ
وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ ۖ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾

“Wanaume wana sehemu katika wanayoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizofaridhiwa.” (4:7)

Kisha Abu Hatimu رحمه الله تعالى alisema, “Ilinukuliwa kutoka kwa Ibn Umar, Abu Musa, Said, bin Mussayb, Al-Hasan, Mujahid, Ata, Said bin Jubayr, Muhammad bin Sirin,¹ Ikrimah,² Zayd bin Aslam na Ar-Rabi bin Anas. Qatadah, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan,³ Tawus,⁴ Ibrahim An-Nakhai, Shurayh, Adh-Dhahhak na Az-Zuhri walisema kuwa Aya hii (2:180) hapo juu ilifutwa na Ayah inayohusu warithi (4:7).”⁵

Wasia ni kwa Jamaa wasio na Haki ya Kurithi

Imependekezwa kuwa jamaa waliobaki, ambao hawana hisa katika Mirathi, waandikwe kwenye usia kutoka katika theluthi. Sheria hiyo inatokana na maana ya jumla ya Aya inayohusu wasia. Ilinukuliwa ndani ya Sahihi mbili kuwa Ibn Umar عنهما رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا حَقُّ امْرِئٍ مُسْلِمٍ لَهُ شَيْءٌ يُوصِي فِيهِ يَبِيتُ لِبَيْتَيْنِ إِلَّا وَوَصِيَّتَهُ مَكْتُوبَةٌ عِنْدَهُ».

“Hairuhusiwi kwa Muislam ambaye ana kitu cha kuusia, kukaa nacho siku mbili bila kutoa wasia wake wa mwisho na kuandikwa na kuhifadhiwa.”

Ibn Umar رضي الله عنهما alitoa maelezo, “Toka siku hiyo niliposikia kauli ya Mtume ﷺ, hapana usiku uliopita, ila wasia wangu uko tayari.”² Kuna Aya na Hadith nyingi zinazohimiza watu kufanya wema na ukarimu kwa jamaa.

¹ Ibn Abu Hatim 1:301-302

² At-Tabari 3:391.

³ Ibn Abu Hatim 1:302-303.

⁴ At-Tabari 3:389.

⁵ Ibn Abu Hatim 1:301-303.

⁶ Fat’hul Al-Bari 5:419 na Muslim 3:1249 na 1250.

Wasia lazima uzingatie haki:

Wasia unatakiwa uwe wa haki, mtu ampe sehemu ya mirathi jamaa yake bila kuwadhulumu warithi stahiki na bila kufanya israfu au ubakhili. Imenukuliwa ndani ya Sahihi mbili¹ kuwa Sa'ad bin Abu Waqqas رضي الله عنهما alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nina mali nyingi na nina binti mmoja wa kunirithi, "Je, niusie theluthi mbili za mali yangu (kwa wengine)?" Mtume ﷺ akajibu, "Hapana." Sa'ad رضي الله عنه akasema, "Je, Theluthi moja?" Mtume ﷺ akajibu, "Ndiyo, theluthi moja, japokuwa theluthi bado ni nyingi. Ni bora kuwaacha warithi wako wakiwa matajiri kuliko kuwaacha wakiwa masikini wenye kuomba kwa watu wengine." Al-Bukhari alitaja ndani ya Sahih kuwa ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, 'Nilipendekeza watu wapunguze sehemu wanayorithisha kwa wasia kuwa robo (ya urithi wote) badala ya theluthi." Kwani Mtume ﷺ alisema:

«الثُلُثُ وَالثُلُثُ كَثِيرٌ»

"Theluthi na theluthi ni nyingi."²

Kauli ya Allah تعالى,

فَمَنْ بَدَّلَهُ بَعْدَمَا سَمِعَهُ فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ يُبَدِّلُونَهُ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٨١﴾

"Na atakayeubadilisha wasia baada ya kumsikia, basi dhambi yake ni juu ya wale watakaubadilisha; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua." (2:181)

Maana yake: Yeyote aliyebadili wasia na agano au akaurekebisha kwa kuongeza au kufuta, ikiwa ni pamoja na kuuficha kama ulivyo, hivyo,

فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ يُبَدِّلُونَهُ

"Basi dhambi yake ni juu ya wale watakaubadilisha."

Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine wamesema, "Malipo ya aliyekufa yatahifadhiwa na Allah تعالى, ambapo makosa yatabebwa na wale walio-badilisha wasia."³

¹ Fat'hul Al-Bari 5:724 na Muslim 3:1250.

² Sahih Al-Bukhari Na. 2743.

³ At-Tabari 3:397.

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٨١﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.”

Maana yake: Allah تعالى Anajua Wasia aliouacha marehemu na kile walichobadilisha walengwa (au wengine) katika wasia. Na Kauli Yake Allah تعالى،

فَمَنْ خَافَ مِنْ مَوْصٍ جَنَفًا أَوْ إِثْمًا

“Na mwenye kumkhofia muusiaji kwenda kombo au kupata dhambi.”

Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah, Mujahid, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi bin Anas na As-Suddi رضي الله عنهم walisema, “Kosa.”² Makosa huwa ni pamoja na pale muusiaji anapoamua kumzidishia Mrithi kupitia kitu fulani au njia fulani, kwa mfano, kuusia mrithi auziwe kitu fulani kwa kumpelekea. Au, marehemu ausie kwa mjukuu wa bint yake ili kuongeza hisa ya binti yake katika mirathi na kadhalika jambo hili linaweza kufanyika kwa makosa bila ya kukusudia. Makosa hayo yanaweza kutokana na mapenzi ya moyo bila kufikiria madhara yatakayosababishwa na vitendo hivi, au kukusudia kufanya dhambi. Katika hali kama hizo, wasimamizi wa wasia na agano wanaruhusiwa kurekebisha makosa na kuweka badala yake yaliyo sahihi katika wasia, ili kuweka ulinganifu kilichokusudiwa na marehemu na utaratibu wa kisharia, vyote viheshimiwe na vitekelezwe. Kitendo hicho hakitohesabiwa ni mabadiliko katika wasia na ndio sababu Allah تعالى Amelitaja waziwazi, ili ifahamike kwamba kufanya masahihisho kama hayo katika wasia, hakuhesabiwi kuwa ni kuufanyia mabadiliko yanayosababisha dhambi.

Ubora wa kufanya uadilifu katika wasia:

Abdur-Razzaq alitaarifu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْخَيْرِ سَبْعِينَ سَنَةً، فَإِذَا أَوْصَى خَافَ فِي وَصِيَّتِهِ، فَيُخْتَمَ لَهُ بِشَرِّ عَمَلِهِ، فَيَدْخُلُ النَّارَ. وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الشَّرِّ سَبْعِينَ سَنَةً، فَيَعْدِلُ فِي وَصِيَّتِهِ، فَيُخْتَمَ لَهُ بِخَيْرِ عَمَلِهِ، فَيَدْخُلُ الْجَنَّةَ.»

² Ibn Abu hatim 1:310 -311.

"Hakika Mtu anaweza kufanya amali za watu wa kheri kwa miaka sabini, lakini anapousia hatendi haki katika wasia wake; (maisha yake) huishia katika amali mbaya na kuingia motoni. Mtu anaweza kufanya amali za watu waovu, lakini anapousia hufanya uadilifu na hivyo huishia kwa amali njema na kisha huingia Peponi."

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, "Mkitaka Someni."

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا

"Hii ndio Mipaka ya Mwenyezi Mungu basi msikiuke." (2:229)

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كَتَبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كَتَبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢٢٩﴾ أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۚ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۚ فَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ ۗ وَأَن تَصُومُوا خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

183. "Enyi mlioamini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyo andikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumchamungu."

184. "(Mfunge) siku maalumu za kuhisabika. Na atakayekuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine. Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kuwalisha masikini. Na atakayefanya wema kwa kujitolea, basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu, kama mnajua."

Amri ya Kufunga:

Katika Kuwaelezea waumini wa Ummah huu, Allah تعالیٰ Anawaamrisha kufunga, yaani, kuacha kula, kunywa na kufanya ngono kwa nia ya kumkusudia Yeye Peke Yake. Hii ni kwa sababu kufunga kunatakasa moyo na kunazisafisha kutokana na uovu ambao unaweza kuchanganyika na tabia mbaya na chafu. Allah تعالیٰ Ametaja kuwa Amefaradhisha kufunga kwa Waislamu kama

¹ Abdur-Razzaq 9:88.

Alivyowafaradhishia waliokuwepo kabla yao, wao wakiwa kigezo kwao katika hilo. Hivyo wanatakiwa watekeleze jukumu hilo kwa nguvu zao zote kwa unyenyekevu zaidi kuliko watu waliotangulia.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَاءَ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ ۗ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ ۗ

“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuekea sharia yake na njia yake. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka Angekufanyeni nyote ummah mmoja, lakini ni Kukujaribuni kwa Aliyokupeni. Basi shindaneni kwa mambo ya kheri.” (5:48)

Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلَيْكُمْ أَصْيَامٌ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

“Enyi mlioamini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyoandikiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumchamungu.” (2:183)

Hiyo ni kwa kuwa fungua inautakasa mwili na kuzifanya njia za Shaytan ziwe nyembamba. Ndiyo maana katika Sahihi mbili Hadith ifuatayo ilinukuliwa:

«يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ مَنِ اسْتِطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصَّوْمِ فَإِنَّهُ لَهُ وِجَاءٌ.»

“Enyi kongamano la vijana! Yeyote miongoni mwenu anayemudu gharama za kuoja, basi aoe. Yeyote asiyemudu, na afunge, kwani itakuwa ngao yake.”¹

Kisha Allah تعالى Akaeleza kiwango cha siku za kufunga kuwa idadi yake ni ndogo; Amefanya hivyo ili nafsi zisione tabu katika utekelezaji wake.

¹ Fat’hul Al-Bari 9:8 na Muslim 2:1018.

Hatua mbalimbali za Funga:

Bukhari na Muslim walinukuu kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, "(Siku ya 'Ashura ilikuwa siku ya kufunga. Faradhi ya kufunga Ramadhani ilipoteremshwa, wale waliotaka walifunga Ashura, na wengine hawakufunga."¹ Bukhari alinukuu sawa na hiyo kutoka kwa Umar na Ibn Mas'udi رضي الله عنهما.² Allah تعالى Amesema:

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ^ط

"Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini."

Muadh رضي الله عنه alitoa maelezo, "Hapo mwanzo wale waliotaka walifunga na wale wasiotaka kufunga, hawakufunga, bali walilisha masikini kila siku."

Bukhari alimnukuu Salamah bin Al-Ak'wai kuhusu kuteremshwa:

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ^ط

"Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini."

Wale ambao hawakutaka kufunga walikuwa wakitoa *Fidyah* (kuwalisha masikini kwa kila siku wasiyofunga) mpaka Ayah (2:185) ilipoteremshwa na kuifuta amri ya Aya³ iliyotangulia. Pia ilielezwa kutoka kwa Ubaydullah kutoka kwa Naafi kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema: "ilifutwa."⁴ As-Suddi alieleza kuwa Murrāh alisimulia kuwa Abdullah aliizungumzia Aya hii.

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ^ط

"Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kuwalisha masikini."

Ina maana wale wanaoona ugumu (kufunga). Abdullah amesema, "Mwanzoni wale waliotaka walifunga, na wale wasiotaka kutofunga hawakufunga lakini waliwalisha masikini badala yake."⁵ Kisha Allah تعالى Amesema:

¹ Fat'hul Al-Bari 8:26 na Muslim 2:792.

² Fat'hul Al-Bari 8:26.

³ Fat'hul Al-Bari 8:29

⁴ Fat'hul Al-Bari 8:20.

⁵ Fat'hul Al-Bari 8:28.

فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا

“Na atakayefanya wema kwa kujitolea, basi ni bora kwake.”

Maana yake: Yeyote anayemlisha masikini mwingine zaidi,

فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُ ۚ وَأَنْ تَصُومُوا خَيْرٌ لَكُمْ ۗ

“Basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu.”

Hali iliendelea hivyo mpaka baadaye ilipofutwa na Aya hii.

فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

“Basi atayekuwa mjini katika mwezi huu na afunge.” (2:185)

Iliteremshwa na hii ilifuta Aya iliyotangulia (2:185).

Fidiya ya kutofunga kwa wazee na wagonjwa

Bukhari alieleza kuwa Ataa alimsikia Ibn Abbas رضي الله عنهما akisoma

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامٌ مِسْكِينٍ ۗ

“Na wale wasioweza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini.”

Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, “(Aya hii) haikufutwa, ni kwa wanaume na wanawake wazee wasioweza kufunga, lakini badala yake wanawalisha masikini kila siku (hawafungi).”¹ Wengine walieleza kuwa Said bin Jubayr aliipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Hivyo kufutwa (kwa hukumu ya Aya hiyo) kunamhusu mtu mwenye afya, ambaye hayuko safarini, na ambaye anatakiwa kufunga.

Ni kama Allah تعالى Alivyosema:

فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

“Basi atayekuwa mjini katika mwezi huu na afunge.” (2:185)

¹ Fat’hul Al-Bari 8:218.

Ama wazee wasioweza kufunga, wanaruhusiwa kula na hawatakiwi kulipa, kwa sababu hawatarajiwi kuwa na hali nzuri ya kuwawezesha kufunga siku nyingine. Hivyo anatakiwa kulipa *Fidiyah* kwa kila siku asizofunga. Hii ni rai ya Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine wengi miongoni mwa *Salaf* waliosoma Ayah hii kwa *Qiraa*: Maana yake: Usomaji,

عَلَى الَّذِينَ يُطَوَّقُونَهُ

“Na wale wasioweza.”

Ina maana: Kuna uzito wa kufunga¹ kama Ibn Mas’ud رضي الله عنهما na wengine walivyoeleza. Hii pia ameiafiki Bukhari ambaye alisema, “Ama kwa mzee ambaye hawezi kufunga, anatakiwa afanye kama Anas رضي الله عنه, ambaye kwa mwaka mmoja au miwili baada ya kuwa mzee aliwalisha masikini mikate na nyama kila siku ambayo hakufunga.”²

Hoja hii, ambayo Bukhari aliinasibisha na Anas رضي الله عنه bila kuwepo *Isnad* ya wapokezi, ilikusanywa na mfululizo wa *Isnad* ya wapokezi akiwemo Al-Haafidh Abu Yaala Mawsuli katika Musnad wake, kuwa Ayyub bin Abu Tamimah alisema; “Anas hakuweza kuendelea kufunga. Hivyo aliandaa *Tharid* (mchanganyiko wa mkate na nyama) na aliwaalika masikini thelathini na akawalisha.”³ Sharia hii inawahusu pia waja wazito na wanaonyonyesha, kama watachelea hali zao au za watoto wao au vijusi (vilenge) vyao. Kwa hali hii, watalipa *fidiyah* tu na hawatakiwi kuzilipa siku walizokula mchana.

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَن
 شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۗ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ يُرِيدُ
 اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا
 هَدَانَكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢١٨﴾

¹ At-Tabari 3:431

² Fat’hul Al-Bari 8:179

³ Musnad Abu Ya’la 7:204

185. "Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani, kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi. Basi atakaye uona mwezi huu na afunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu Anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa Amekuongoeni ili mpate kushukuru."

Utukufu wa Ramadhani na kuteremshwa kwa Qur'an katika mwezi huo:

Allah تعالى Ameutukuza mwezi wa Ramadhani kuliko miezi mingine kwa kukhitari kuteremsha Qur'an Takatifu ndani ya mwezi huo, kama Alivyofanya kwa Vitabu vyote Vitukufu Alivyoviteremsha kwa Mitume. Imam Ahmad alieleza kutoka kwa Wathilaj bin Al-Asqa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أُنزِلَتْ صُحُفُ إِبْرَاهِيمَ فِي أَوَّلِ لَيْلَةٍ مِنْ رَمَضَانَ، وَأُنزِلَتْ التَّوْرَةُ لَيْسَتْ مَضِينٍ مِنْ رَمَضَانَ، وَالْإِنْجِيلُ لِثَلَاثِ عَشْرَةَ خَلَّتْ مِنْ رَمَضَانَ، وَأُنزِلَ اللَّهُ الْفُرْقَانَ لِأَرْبَعِ وَعِشْرِينَ خَلَّتْ مِنْ رَمَضَانَ»

*"Suhuf Ibrahim ziliteremshwa usiku wa kwanza wa Ramadhani. Taurati iliteremshwa usiku wa sita wa Ramadhani, Injili iliteremshwa usiku wa kumi na tatu wa Ramadhani. Allah Aliiteremsha Qur'an usiku wa ishirini na nne wa Ramadhani."*¹

Utukufu wa Qur'an:

Allah تعالى Amesema:

هُدًى لِلنَّاسِ وَيَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ

"Kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi."

Allah تعالى Ameitukuza Qur'an hapa, ambayo Aliiteremsha iwe uongofu kwa nyoyo za wale wanaoiamini na kuisadikisha na kuifuata. Allah تعالى Amesema:

وَيَبَيِّنَاتٍ

"Na hoja zilizo wazi."

¹ Ahmad 4:107.

Maana yake: Dalili zilizo wazi na ushahidi usiopingika kwa wale wanaoifahamu. Ushahidi huu unathibitisha usahihi wa yote yaliyokuja na Qur'an, yenye uongofu, inayokanusha upotofu, inayoongoza kwenye njia iliyonyooka, kinyume cha njia iliyopotoka, inayotofautisha kati ya ukweli na batili, na halali na haramu.

Kufaradhishwa kwa Funga ya Ramadhani

Allah تعالی Amesema:

فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

“Basi atakaye uona mwezi huu na afunge.”

Aya hii inamtaka mtu anayeshuhudia kuanza kwa mwezi, mwenye afya njema, akiwa katika mji wake, afunge mwezi mzima. Aya hii ilifuta Aya iliyokhiyarisha kwa mwenye afya njema kufunga au kulipa fidyah kwa kuwalisha masikini kila siku kama tulivyoeleza huko nyuma. Allah تعالی Alipoamrisha kufunga kisha akataja ruhusa ya kufungua kwa mgonjwa na msafiri na kuzilipa baaadaye. Allah تعالی Amesema:

وَمَنْ كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

“Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyingine.”

Aya inaonesha kuwa wagonjwa wasioweza kufunga au kuchelea madhara ya fungu, na wasafiri, wanaruhusiwa kufungua. Na asiyefunga kwa hali hii, analazimika kufunga siku nyingine. Allah تعالی Amesema:

يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ

“Mwenyezi Mungu Anakutakieni yaliyo mepesi wala Hakutakieni yaliyo mazito.”

Aya inaonesha kuwa Allah تعالی Aliwaruhusu watu, kutokana na Rehema Zake na Kuwasahilishia mambo, kufungua wakati wakiwa wagonjwa au safarini, ambapo fungu bado inaendelea kuwa ni wajibu kwa watu wenye siha njema na wasio kuwa safarini.

Hukumu kadhaa kuhusu funga ya safari:

Sunnah sahihi inaeleza kuwa Mtume ﷺ alisafiri mwezi wa Ramadhan kwa ajili ya vita ya *Fat'hu Makkah*. Mtume ﷺ alitembea mpaka akafika eneo la Kadid, akafungua na akawaamrisha aliokuwa nao wafungue. Hadithi hii ilinukuliwa katika Sahih Mbili.¹ Amri ya kuacha kufunga iliyotajwa ndani ya Hadithi hii ni amri ya hiyari na siyo ya wajibu kwani Masahaba walikuwa wakitoka na Mtume ﷺ wakati wa mwezi wa Ramadhan, kisha baadhi yao wakifunga na baadhi yao hawakufunga na hapana kundi lililolikosoa jingine.

Endapo Amri iliyotajwa katika Hadithi ingewajibisha kufungua Saumu, wangekatazwa kufunga. Pia imethibiti wakati wa uhai wa Mtume ﷺ kwamba kuna wakati alikuwa akisafiri huku akiwa amefunga. Imethibiti katika Sahih mbili kwamba Abu Ad-Dardai رضي الله عنه amesema: 'Tulitoka pamoja na Mtume ﷺ katika siku iliyokuwa na joto kali sana baadhi yetu waliweka mikono juu ya kichwa kwa sababu ya joto kali.' Mtume ﷺ na Abdullah bin Rawahah رضي الله عنه ndio peke yao waliokuwa na Saumu kwa wakati huo.² Inafaa tueleze hapa kuwa kutumia ruhusa ya kufungua mtu awapo safarini ni bora. Kama Mtume ﷺ alivyosema kuhusu kufunga safarini:

«مَنْ أَطْرَفَ فَحَسَنٌ، وَمَنْ صَامَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ»

*"Watakaofungua safarini wamefanya vyema, na waliofunga hawana makosa."*³

Katika Hadithi nyingine, Mtume ﷺ amesema:

«عَلَيْكُمْ بِرُخْصَةِ اللَّهِ الَّتِي رُخِّصَ لَكُمْ»

*"Shikamaneni na ruhusa Aliyokupeni Allah."*⁴

Baadhi ya wanazuoni wanasema matendo yote mawili ni sawa, kama Aisha رضي الله عنها alivyosimulia kuwa Hamza bin Amr Al-Aslami رضي الله عنه alimuuliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi ni mwingi wa kufunga, je, nifunge nikiwa safarini?" Mtume ﷺ alimjibu:

¹ Fat'hul Al-Bari 3:213, Muslim 2:784.

² Fat'hul Al-Bari 4:215, Muslim 2:790.

³ Muslim 2:790.

⁴ Muslim 2:786.

«إِنْ شِئْتَ فَصُمْ، وَإِنْ شِئْتَ فَأَفْطِرْ»

“Ukipenda funga, ukipenda kula.”

Hadithi hii iko katika Sahih Mbili.¹ Ilikezwa kuwa kama Saumu imekuwa kali (wakati wa safari), kufungua ni bora. Jabir رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ alimuona mtu amefunikwa na wenzake wakati wakisafiri. Mtume ﷺ akauliza kuhusu habari zake, akaambiwa mtu yule alikuwa amefunga. Mtume ﷺ akasema:

«لَيْسَ مِنَ الْبِرِّ الصِّيَامُ فِي السَّفَرِ».

“Kufunga safarini sio sehemu ya Birr (ucha – Mungu).”

Ilinukuliwa na Bukhari na Muslim.²

Ama wale wanaopuuza Sunnah na wanaoamini nyoyo zao kuwa kula safarini kunachukiza, hawatakiwi kufunga na hawaruhusiwi kufunga.

Ama katika kulipa siku alizokula mchana, halazimishwi kuzifunga kwa mfululizo. Mtu ana hiari kufunga mfululizo au kwa kupumzika. Kuna uthibitisho wa kutosha kuhusu hili. Inafaa tutaje kuwa kufunga kwa mfululizo, ni maalumu kwa funga ya Ramadhani. Na baada ya Ramadhani, kinachotakiwa ni kulipa siku alizozikosa. Ndiyo sababu Allah تعالى Akasema:

فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

“Basi atimize hisabu katika siku nyingine.”

Ni Wepesi wala Hakuna Mazito:

Kisha Allah تعالى Akasema:

يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمْ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمْ الْعُسْرَ

“Mwenyezi Mungu Anakutakieni yaliyo mapesi wala Hakutakieni yaliyo mazito.”

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Fat’hul Al-Bari 4:211, Muslim 2:789.

² Fat’hul Al-Bari 4:216, Muslim 2:786.

«يَسْرُوا وَلَا تَعْسُرُوا وَاسْكُنُوا وَلَا تُتْفَرُوا».

“Tangazeni habari njema kwa watu wala msitangaze habari za kufarakanisha, wala msiwe wagumu kwao, watulizeni wala msiwafarakishe.”

Hadithi hii ilikusanywa katika Sahih Mbili.¹ Imeelezwa katika Sahih mbili kuwa Mtume ﷺ aliwaambia Muadh na Abu Musa رضي الله عنهما alipowatuma kwenda Yemen.

«بَشْرًا وَلَا تَتَفَرَّا، وَيَسْرًا وَلَا تَعْسُرًا، وَتَطَاوَعًا وَلَا تَخْتَلِفًا»

“Tangazeni habari njema kwa watu wala msitangaze habari za kuwafarakisha na kuweni wepesi wala msiwe wagumu, na mshikamane wala msikhitilafiane.”²

Wakusanyaji wa Sunnah na Musnad waliandika kuwa Mtume ﷺ alisema:

«بُعِثْتُ بِالْحَنِيفِيَّةِ السَّمْحَةِ»

“Nilitumwa na mafundisho ya Dini iliyokuwa safi yenye usamehevu.”³

Kauli ya Allah تعالى:

يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمْ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمْ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ

“Mwenyezi Mungu Anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu.”

Maana yake: Mliruhusiwa kufungua mlipokuwa wagonjwa, mlipokuwa safarini na kadhalika, kwa sababu Allah تعالى Alitaka kuwasahilishieni mambo. Alikuamrisheni kulipa siku mlizozikosa ili kukamilisha siku za mwezi mmoja.

Kumdhukuru Allah تعالى wakati inapotimia Ibada:

Kauli ya Allah تعالى:

وَلِتُكْمِلُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْتَكُمْ

“Na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa Amekuongoeni.”

¹ Ahmad 3:131, na 209, Fath Al-Bari10:541, na Muslim 3:1359.

² Fat’hul Al-Bari 7:660, Muslim 3:1587

³ Ahmad 5:266

Maana yake: Ili mumkumbuke Allah تعالى wakati wa ibada. Na Kauli ya Allah تعالى:

فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَسِكَكُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ ءَابَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا

“Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi.” (2:200) au,

فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِن فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ

تُفْلِحُونَ ﴿٦٢﴾

“Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute Fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa.” (62:10) Na,

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ ﴿٦٣﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَأَدْبَرَ

السُّجُودِ ﴿٦٤﴾

“Na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa. Na katika usiku pia mumtakase, na baada ya kusujudu.” (50:40)

Kwa sababu hii Sunnah imeshajiisha *Tasbih* (kusema *Subhana Allah*, maana yake, ‘Utakasifu wote unamstahiki Allah تعالى), *Tahmid* (kusema, *Al-Hamdu Lillah* maana yake ‘Shukrani zote Anastahiki Allah تعالى’) na *Takbir* (*Allah Akbar*, maana yake, ‘Allah تعالى ni Mkubwa’) baada ya Sala zilizofaradhiwa. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, ‘Hatukujua kuisha kwa Sala ya Mtume ﷺ ila kwa *Takbir*.’¹ Vile vile, wanazuoni wengi wameeleza kuwa kusoma *Takbir* wakati wa *Id-ul-Fitr* ni mahsusi kama Aya inavyoeleza:

وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْنَاكُمْ

“Na ili mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongozeni.”

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦٥﴾

“Ili mpate kushukuru.”

¹ Sahih Al-Bukhari Na 842.

Maana yake: Iwapo mtashikamana na yale Aliyowaamrisha Allah تعالى, kumtii Yeye kwa kutekeleza wajibu, kuacha yaliyoharamishwa na kuzitii sharia - huenda mkawa miongoni mwa wenye shukrani.

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۗ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

186. "Na waja Wangu watakapokuuliza khabari Zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka."

Allah تعالى Anasikia dua za Waja wake:

Imam Ahmad alieleza kuwa Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema, "Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ wakati wa vita. Kila tulipopanda kwenye muinuko, tulipopanda kilima au kushuka bondeni, tulikuwa tukisema, "Allahu Akbar" kwa sauti ya juu." Mtume ﷺ alitupitia na kusema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ، ازْبِعُوا عَلَىٰ أَنفُسِكُمْ، فَإِنَّكُمْ لَا تَدْعُونَ أَصَمًّا وَلَا غَائِبًا، إِنَّمَا تَدْعُونَ سَمِيعًا بَصِيرًا، إِنَّ الَّذِي تَدْعُونَ أَقْرَبُ إِلَيَّ أَحَدِكُمْ مِنْ عُنُقِي رَاحِلَتِي، يَا عَبْدَ اللَّهِ بْنِ قَيْسٍ، أَلَا أَعْلَمُكَ كَلِمَةً مِنْ كُنُوزِ الْجَنَّةِ؟ لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ»

"Enyi watu! Zihurumieni nafsi zenu (msitoe sauti) kwani hamumuombi kiziwi wala aliye mbali, lakini mnamuomba Yule Asikiaye na Aonaye. Hakika mnayemuomba Yuko karibu sana na mmoja wenu kuliko shingo ya mnyama wake (aliyempanda). Ewe Abdullah bin Qaisi (jina la Abu Musa)! Je, nikufundishe kauli ambayo ni hazina ya peponi? 'La hawla wala quwwata illa billah (hapana hila, wala nguvu ila zinatoka kwa Allah).'"¹

Hadith hii iliandikwa ndani ya Sahih Mbili² na Abu Dawud, An-Nisai, At-Tirmidh na Ibn Majah waliandika kwa maneno hayo hayo kwa ziada, Imam Ahmad

¹ Ahmad 4:402.

² Fat'hul Al-Bari 2:509, Muslim 4:2076.

ameandika kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa, Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى أَنَا عِنْدَ ظَنِّ عَبْدِي بِي وَأَنَا مَعَهُ إِذَا دَعَانِي».

“Mimi Niko katika fikra za mja Wangu na Niko pamoja naye Anaponiomba.”¹

Dua Hupokelewa, na Hakuna Inayopotea.

Imam Ahmad pia ameandika kuwa Abu Said رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنْ مُسْلِمٍ يَدْعُو اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ بِدَعْوَةٍ لَيْسَ فِيهَا بِإِثْمٍ وَلَا قَطِيعَةٌ رَجِمَ، إِلَّا أَعْطَاهُ اللَّهُ بِهَا إِحْدَى ثَلَاثِ خِصَالٍ: إِمَّا أَنْ يُعْجَلَ لَهُ دَعْوَتُهُ، وَإِمَّا أَنْ يَدَّخِرَهَا لَهُ فِي الْآخِرَى، وَإِمَّا أَنْ يَصْرِفَ عَنْهُ مِنَ الشَّرِّ مِثْلَهَا، قَالُوا: إِذَا نُكِّرُ؟ قَالَ: «اللَّهُ أَكْثَرُ».

“Hapana Muislam yeyote anayemuomba Allah kwa Dua ambayo haina dhambi au kukata udugu isipokuwa Allah Atampa moja kati ya mambo matatu. Ataharakisha majibu ya Dua yake, Atamhifadhia mpaka Siku ya Kiyama au Atamuondolea uovu ulio sawa na hiyo. Wakauliza, ‘Kama ni hivyo tuombe dua kwa wingi?’ Akawajibu, ‘Kuna vingi kwa Allah.’”²

Abdullah mtoto wa Imam Ahmad aliandika kutoka kwa Jubair bin Nafiir kuwa Abdallah bin As-Samit رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا عَلَى ظَهْرِ الْأَرْضِ مِنْ رَجُلٍ مُسْلِمٍ يَدْعُو اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ بِدَعْوَةٍ إِلَّا آتَاهُ اللَّهُ بِهَا، أَوْ كَفَّ عَنْهُ مِنَ الشَّرِّ مِثْلَهَا مَا لَمْ يَدْعُ بِإِثْمٍ أَوْ قَطِيعَةٍ رَجِمَ»

“Hapana Muislam aliye juu ya uso wa ardhi anayemuomba Allah ila Allah Atampa, au Atabadilisha uovu kwa vipimo sawa, madhali Dua yake haina dhambi au kukata uhusiano na ndugu wa damu.”³

At-Tirmidh aliandika Hadith hii.⁴ Imam Malik رحمه الله تعالى Aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Ahmad 3:210.

² Ahmad 3:18.

³ Ahmad 5:329.

⁴ Tuhfatul Al-Ahwadhi 10:24.

«يُسْتَجَابُ لِأَحَدِكُمْ مَا لَمْ يَجْعَلْ، يَقُولُ: دَعَوْتُ فَلَمْ يُسْتَجَبْ لِي»

“Dua ya mmoja wenu itapokelewa madhali hatafanya haraka na kusema, “Nimeomba lakini Dua yangu haijajibiwa.”¹

Hadith hii imeandikwa katika Sahih Mbili² kutoka kwa Malik, na haya ni maneno ya Al-Bukhari. Muslim aliandika kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَزَالُ يُسْتَجَابُ لِلْعَبْدِ مَا لَمْ يَدْعُ بِإِنْمٍ أَوْ قَطِيعَةٍ رَّحِمَ مَا لَمْ يَسْتَعْجِلْ» قِيلَ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، وَمَا الِاسْتِعْجَالُ؟ قَالَ: «يَقُولُ: قَدْ دَعَوْتُ وَقَدْ دَعَوْتُ، فَلَمْ أَرِ يُسْتَجَابْ لِي، فَيَسْتَحْسِرُ عِنْدَ ذَلِكَ وَيَدْعُ الدُّعَاءَ»

“Dua ya mja itajibiwa pale tu ambapo hataomba dhambi au kukata uhusiano na ndugu wa damu na asiwe na pupa.” Aliulizwa, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ni vipi mtu anakuwa na pupa?” Alijibu, “Anasema, ‘Niliomba na kuomba, lakini sikuona dua yangu ikijibiwa.’ Hivyo huvunjika moyo na kuacha kumuomba (Allah).”³

Dua za Watu wa Ana Tatu Hazikataliwi:

Katika Musnad wa Imam Ahmad na Sunnah za At-Tirmidh, An-Nasai na Ibn Majah ilinukuliwa kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«ثَلَاثَةٌ لَا تُرَدُّ دَعْوَتُهُمْ: الْإِمَامُ الْعَادِلُ، وَالصَّائِمُ حَتَّى يُفْطِرَ، وَدَعْوَةُ الْمَظْلُومِ، يَرْفَعُهَا اللَّهُ دُونَ الْعَمَامِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَتُنْفَعُ لَهَا أَبْوَابُ السَّمَاءِ، يَقُولُ: بِعِزِّي لِأَنْصُرَنَّكَ وَلَوْ بَعْدَ جِيْنٍ».

“Dua za watu watatu hazitokataliwa: Mtawala muadilifu, mfungaji wakati anapofuturu na dua ya aliyedhumiwa. Siku ya Kiyama, Allah Ataiinua juu ya mawingu, Milango ya Mbingu itafunguliwa kisha Allah Atasema, ‘Naapa kwa Utukufu Wangu! Nitakunusuru hata baada ya muda mfupi.”⁴

¹ Ahmad 2:396.

² Fat’hul Al-Bari 11:145, na Muslim 4:2095.

³ Muslim 4:2096.

⁴ Ahmad 3:544, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:229 na Ibn Majah 1:557.

أَحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَائِكُمْ ۚ هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ۗ عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ ۗ فَالْقَنَ بِنِسْوَتِهِنَّ وَاتَّقُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَبَيِّنَ لَكُمْ الْحَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْحَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ۗ ثُمَّ أَنْمُوا الصِّيَامَ إِلَىٰ اللَّيْلِ ۗ وَلَا تُبَشِّرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسْجِدِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرُبُوهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١٨٧﴾ وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُم بَيْنَكُم بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوا بِهَآ إِلَى الْحُكْمِ إِنَّا كُنَّا لَمَآكُلُوا فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٨﴾ * يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ ۗ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ ۗ وَلَا يَسَّ الْبِرَّ بِأَنَّ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ ظُهُورِهَا وَلَكِنَّ الْبِرَّ مِنَ اتَّقَىٰ ۗ وَأَتُوا الْبُيُوتَ مِنْ أَبْوَابِهَا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٨٩﴾

أَحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَائِكُمْ ۚ هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ۗ عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ ۗ فَالْقَنَ بِنِسْوَتِهِنَّ وَاتَّقُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَبَيِّنَ لَكُمْ الْحَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْحَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ۗ ثُمَّ أَنْمُوا الصِّيَامَ إِلَىٰ اللَّيْلِ ۗ وَلَا تُبَشِّرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسْجِدِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَقْرُبُوهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١٨٧﴾

187. "Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu. Wao ni vazi

kwenu, na nyinyi ni vazi kwao. Mwenyezi Mungu Anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu. Kwa hivyo Amekukubalieni toba yenu na Amekusameheni. Basi sasa changanyikeni nao na takeni Aliyokuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku. Wala msichanganyike nao, na hali mnakaa Itikafu msikitini. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikaribie. Namna hivi Mwenyezi Mungu Anabainisha Ishara Zake kwa watu ili wapate kumcha."

Kula, Kunywa na Kujamiiana Vinaruhusiwa usiku wa Ramadhani:

Aya hii inaonesha kwamba Allah تعالی Aliwapa Waislamu ahueni kwa Kuondoa kawaida iliyokuwepo miaka ya mwanzo ya Uislam. Waislam waliruhusiwa kula, kunywa na kujamiiana baada ya kufuturu mpaka Sala ya Isha tu, isipokuwa kama mtu atalala kabla ya Sala ya Isha. Wale waliolala kabla ya Isha au waliosali Isha hawakuruhusiwa kunywa, kula au kujamiiana mpaka usiku uliofuata. Hili lilikuwa ngumu kwa Waislamu. Aya imetumia neno 'Rafath' kuashiria kujamiiana. Hiyo ni kwa mujibu wa Ibn Abbas, Ata na Mujahid رضي الله عنهم. Tafsir sawa na hiyo ilitolewa na Said bin Jubayr, Tawus, Salim bin Abdillah, Amri bin Dinar Al-Hasan, Az-zuhri,¹ Adh-dhahak, Ibrahim, An-Nakhai, As-Suddi, Ata Al-Khurasani na Muqatil bin Hayyan.² Allah تعالی Amesema:

هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ

“Wao ni vazi kwenu na nyinyi ni vazi kwao.”

Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم walisema kuwa Aya hii ina maana, “Wake zenu ni mapumziko kwenu na nyie ni mapumziko kwao.”³ Ar-Rabi bin Anas alisema, “Wao ni kifuniko kwenu na nyie ni kifuniko kwao.”⁴ Kwa ufupi, mke na mume ni wandani na wanaingiliana kimwili, na hii ndio sababu wameruhusiwa kufanya ngono wakati wa usiku katika mwezi wa Ramadhani, hivyo mambo yamesahilishwa kwao.

Abu Is-haq رحمه الله تعالی alieleza kuwa Al-Baraa bin Azib رضي الله عنه alisema; “Masahaba wa Mtume ﷺ walipokuwa katika Saumu lakini wakalala kabla ya kufuturu, waliendelea na Saumu mpaka usiku uliofuata. Qays bin Sirmah Al-Ansari رضي الله عنهم alikuwa amefunga huku akifanya kazi shambani kwake. Wakati wa kufuturu ulipowadia alikwenda kwa mkewe na akamuuliza, ‘Una chakula?’ Akajibu: “Hapana. Lakini nitajaribu kutoka kwenda kutafuta.” Akapatwa na usingizi na mkewe aliporejea, alimkuta amelala akasema, “Inasikitisha! Umelala?” Siku ya pili mchana, alipoteza fahamu na akamueleza Mtume ﷺ yaliyomfika. Kisha Aya hii iliteremshwa:

¹ Ibn Abu Hatim 1:367-371.

² Ibn Abu Hatim 1:368.

³ Ibn Abu Hatim 1:368.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:381.

أَحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَى نِسَائِكُمْ

“Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu...”

(2:187) Mpaka...

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ

“... Na kuleni na kunywa mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku.”

Kwa hivyo, wakawa wamefurahishwa sana.¹ Bukhari aliieleza Hadith hii ya Abu Is-haq ambayo aliisimulia kwamba, Al-Baraa رضي الله عنه alisema, “Saumu ya Ramadhani ilipofaradhiwa, Waislamu walikuwa wakijizuia kulala pamoja na wake zao kwa mwezi wote, lakini watu wengine wakawa wanajidanganya nafsi zao.” Allah تعالى Akateremsha:

عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ

“Mwenyezi Mungu Anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu. Kwa hiyo Amekukubalieni toba yenu na Amekusameheni.”²

Ali bin Abu Twalha alieleza kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema; “Wakati wa mwezi wa Ramadhani, Waislamu walipomaliza kusali Sala ya Isha, hawakuwagusa wake zao wala hawakula chakula mpaka unapoingia usiku wa siku inayofuata. Kisha, baadhi ya Waislamu, akiwemo Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, waliingiliana na wake zao na wakala chakula baada ya Isha katika mwezi wa Ramadhani wakamjulisha Mtume ﷺ. Basi Allah تعالى Akateremsha:

عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ فَالآنَ

بَشِرُوهُمْ

“Mwenyezi Mungu Anajua kwamba mlikuwa mkizikhini nafsi zenu. Kwa hiyo Amekukubalieni toba yenu na Amekusameheni. Basi sasa changanyikeni nao...”

Haya ni masimulizi sawa na ya Al-Awfi, kama alivyoyapokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.³ Allah تعالى Amesema:

¹ At-Tabari 3:495.

² Fat’hul - Bari 8:30.

³ At-Tabari 3:496 - 498. Isnadi yake ni dhaifu.

وَأَتَّبِعُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ^ع

“Na takeni aliyokuandikieni Mwenyezi Mungu.”

Abu Hurayrah, Ibn Abbas, Anas, Shurayh Al-Qadhi, Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Ata, Ar-Rabi bin Anas, As-Suddi, Zayd bin Aslam, Al-Hakam bin Utba, Mukatil bin Hayyan, Al-Hasan, Al-Basri, Adh-dhahhak, Qatadah na wengine رضي الله عنهم walisema kuwa Aya hiyo maana yake kupata watoto.¹ Qatadah amesema kwamba Aya hii ina maana, “Tumieni ruhusa Aliyokupeni Allah تعالى.” Said alisimulia kuwa Qatadah alisema,

وَأَتَّبِعُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ^ع

“Na takeni Aliyokuandikieni Mwenyezi Mungu.” Maana yake: Yale Aliyokuhalalishieni Allah تعالى juu yenu.”

Mwisho wa Wakati wa Kula Daku:

Allah تعالى Amesema:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ^ط ثُمَّ أَمُومَا
الصَّيَامِ إِلَىٰ اللَّيْلِ^ع

“Na kuleni na kunywa mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku.”

Allah تعالى Amehalalisha kula na kunywa, pamoja na kuingiliana usiku wowote anaoutaka mfungaji, kama tulivyoeleza hapo kabla, mpaka ubainike mwanga wa Alfajiri dhidi ya weusi wa usiku. Allah تعالى katika kueleza hilo Ametumia maneno ‘Mstari (uzi) mweupe na mweusi.’ Kisha Akaweka wazi Aliposema:

مِنَ الْفَجْرِ^ط

“Wa alfajiri.”

Kama ilivyoelezwa katika Hadith kuwa Imam Abu Abdullah Al-Bukhari aliandika, kutoka kwa Sahl bin Saad alisema; Wakati Ayah ilipoteremshwa.

¹ Ibn Abu Hatim 1:377-378, na At-Tabari 3:506-507.

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ

“Na kuleni na kunywa mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku.”

Na maneno **‘wa alfajiri’** yalikuwa Hayajateremshwa, baadhi ya watu waliokusudia kufunga, walijifunga uzi mweusi na mweupe katika miguu yao wakawa wanakula mpaka watofautishe kati ya nyuzi mbili hizo. Na kisha akateremsha maneno, **‘wa alfajiri’** na ikawa wazi kwao kuwa ilikuwa na maana ya (kiza cha) usiku na (mwangaza wa) mchana.¹ Bukhari aliandika kuwa Ash-Shabi alisema kuwa ‘Adii رضي الله عنه alisema, “Alichukua nyuzi mbili, moja nyeusi na nyingine nyeupe na akaziweka chini ya mto na akawa anaziangalia usiku kucha lakini hakuweza kutofautisha, mbili hizo. Hivyo, asubuhi ilipofika alikwenda kwa Mtume ﷺ na akamueleza kisa chake akasema:

«إِنَّ وَسَادَكَ إِذَا لَعْرِيسٌ، أَنْ كَانَ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ وَالْأَسْوَدُ تَحْتَ وَسَادَتِكَ»

“Kama uzi mweupe na mweusi unaweza kufunikwa na mto wako basi mto huo ni mpana sana.”² Hadithi hii pia imeelezwa,

«إِنَّكَ لَعْرِيسٌ الْقَمَّاءُ»

“Hakika wewe ni mpana wa kichogo.”³

Baadhi ya watu walisema kuwa maneno haya yalikuwa na maana kuwa “Adii hakuwa makini.” Hayo yana udhaifu bali yanamaanisha kuwa mto wako ni mpana basi na shingo yako ni pana vile vile. Allah تعالى Anajua zaidi. Mapokezi yaliyokusanywa na Bukhari yanaelezea sehemu ya Hadithi. Bukhari aliandika kuwa ‘Adii bin Hatim رضي الله عنه alisimulia: Nilimuuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Nini tofauti kati ya uzi mweupe na uzi mweusi? Hivi ni nyuzi hasa?” Alisema,

«إِنَّكَ لَعْرِيسٌ الْقَمَّاءُ أَنْ أَبْصُرْتَ الْخَيْطَيْنِ، ثُمَّ قَالَ: لَا بَلْ هُوَ سَوَادُ اللَّيْلِ وَيَبَاضُ النَّهَارِ»

“Hakika wewe ni mpana wa kichogo, kama utaziona nyuzi mbili, Kisha Mtume akasema wala haimaanishi hivyo, bali ni weusi wa usiku na weupe wa mchana.”⁴

¹ Fat’hul Al-Bari 8:31.

² Fat’hul Al-Bari 8:31.

³ Fat’hul Al-Bari 8:31.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:31.ul

Sunnah ya kula Daku¹ na wakati wake

Allah تعالی Ameruhusu kula na kunywa mpaka Alfajiri, inathibitisha kuwa Daku (*Sahur*) inahimizwa, kwa kuwa ni *Rukhsah* (tahfifu) na Allah تعالی Anapenda *Rukhsah* ikubaliwe na kutekelezwa. Sunnah sahihi inaonesha kuwa imehimizwa kula daku. Imeandikwa kwenye Sahih Mbili kuwa Anas رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«تَسَحَّرُوا فَإِنَّ فِي السَّحُورِ بَرَكَةً»

*"Kuleni Daku (Suhur) kwani kuna Baraka katika Sahur."*²

Muslim aliandika kuwa Amri bin Al-Aas رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ فَضْلَ مَا بَيْنَ صِيَامِنَا وَصِيَامِ أَهْلِ الْكِتَابِ أَكْثَلُ السَّحْرِ»

*"Tofauti kati ya funga yetu na funga ya Watu wa Kitabu ni kula Sahur."*³

Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Said رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«السَّحُورُ أَكْثَلُهُ بَرَكَةٌ فَلَا تَدْعُوهُ، وَلَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ تَجَرَّعُ جُرْعَةَ مَاءٍ، فَإِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى الْمُتَسَحِّرِينَ»

*"Sahur ni chakula kilichobarikiwa. Hivyo, msikiache, hata kama mmoja wenu atakunywa fundu la maji. Kwa hakika, Allah na Malaika Wake wanawatakiwa Rehema wale wanao kula Sahur."*⁴

Kuna Hadith nyingine kadhaa zinazohimiza kula *Sahur*, hata kama ni fundu la maji ili kuonesha kuwa ameamka na kula.

Inapendekezwa *Sahur* icheleweshwe mpaka karibu na Alfajiri. Imeandikwa katika Sahih Mbili kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisimulia kuwa Zayd bin Thabit رضي الله عنه alisema, "Tulikula *Sahur* na Mtume ﷺ na kisha tukaenda kusali." Anas رضي الله عنه aliuliza, "Kuna kitambo gani baina ya *Adhan* na *Sahur*?" Akajibu, "Kuna kitambo cha kusoma Aya hamsini."¹

¹ Fat'hul Al-Bari 4:165 na Muslim 2:770.

² Muslim 2:771.

³ Ahmad.

⁴ Chakula kinacholiwa usiku kabla ya Alfajiri (kabla ya kuanza Saumu).

Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا تَزَالُ أُمَّتِي بِخَيْرٍ مَا عَجَّلُوا الْإِنْفَاطَارَ وَأَخْرَجُوا الشُّحُورَ.»

“Ummah wangu wakati wote watakuwa kwenye kheri iwapo watafanya haraka kufuturu na kuchelewesha Sahur.”²

Kuna Hadith nyingi zinazosimulia kuwa Mtume ﷺ aliita Sahur, “Chakula kilicho barikiwa,” Kuna mapokezi kutoka kwa Salaf kuwa waliruhusu Sahur icheleweshwe kuliwa mpaka karibu na Alfajiri. Hadith kama hii imeelezwa kutoka kwa Abubakar, Umar, Ali, Ibn Masud, Hudhayfah, Abu Hurayrah, Ibn Umar, Ibn Abbas na Zayd bin Thabit رضي الله عنهم. Na imeelezwa pia kutoka kwa kundi kubwa la Tabin, kama vile Muhammad bin Ali bin Husayn, Abu Mijlaz, Ibrahim An-Nakhai, Abu Adh-Dhuha, Abu Wail na wengineo katika wafuasi wa Ibn Masud رضي الله عنه. Hii pia ni rai ya Ata, Al-Hasan, Hakam bin Uyainah, Mujahid, Urwah bin Az-Zubayr, Abu Sha’tha, Jabir bin Zayd, Al-A’mash na Ma’mar bin Rashid. Tumeandika Isnad za upokezi wao katika (Ibn Kathir), kitabu cha Siyam (kufunga). Shukrani zote Anastahiki Allah. Pia ilinukuliwa kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَنْتَعِمُكَ أَذَانُ بِلَالٍ عَنْ سَحُورِكَمْ، فَإِنَّهُ يُنَادِي بِلَيْلٍ، فَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى تَسْمَعُوا أَذَانَ ابْنِ أُمِّ مَكْتُومٍ، فَإِنَّهُ لَا يُزِدُّنُ حَتَّى يَطْلُعَ الْفَجْرُ»

“Adhana inayotolewa na Bilal isikuzieni kula Sahur, kwani anatoa Adhana usiku. Hivyo kuleni na kunyweni mpaka mtakaposikia Adhana ya Ibn Umm Makhtum, kwani yeye haadhini mpaka iwe Alfajiri.”³

Maneno haya ni kama yalivyokusanywa na Bukhari.

Imam Ahmad alieleza kuwa Qays bin Talq alimnukuu baba yake kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَيْسَ الْفَجْرُ الْمُسْتَطِيلَ فِي الْأَفْقِ وَلَكِنَّ الْمُتَعَرِّضَ الْأَخْمَرَ»

“Alfajiri sio mng’aro wa mwanga mweupe unaonekana upeo wa

¹ Fat’hul Al-Bari 4:164 na Muslim 2:771.

² Ahmad 5:147.

³ Fat’hul Al-Bari 4:162 na Muslim 2:768.

macho. Bali ni mnururisho wa mwanga mwekundu (uliotanda toka kulia kwenda kushoto) ndio unao dhihiri.”¹

Abu Daud na At-Tirmidh pia wameinukuu Hadith hii, lakini kwa maneno tofauti:

«كُلُوا وَاشْرَبُوا، وَلَا يَهِيدَنَّكُمْ السَّاطِعُ الْمُضْعِدُ، فَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَغْتَرِضَ لَكُمْ الْأَحْمَرُ»

“Kuleni na kunywa na wala msiharakishwe na mwangaza mweupe unaopanda. Kuleni na kunywa mpaka wekundu wa alfajiri udhihiri.”²

Ibn Jarir (At-Tabari) رضي الله عنه alinukuu kuwa Samurah bin Jundab رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَغْرُنْكُمْ أَذَانُ بِلَالٍ وَلَا هَذَا الْبَيَاضُ - لِعَمُودِ الصُّبْحِ - حَتَّى يَسْتَطِيرَ»

“Msighurike na Adhana ya Bilal au weupe unaopanda, mpaka utawanyike.”³

Muslim pia alinukuu Hadith hii.⁴

Hapana Ubaya kwa Mwenye Janaba Kufunga

Mas-ala: kutokana na Allah تعالى Kuifanya Alfajiri kuwa ndio mwisho wa kula, kunywa kwa mtu mwenye nia ya kufunga, Ulamaa wamechukulia hiyo kuwa ni dalili tosha kuwa atakayeamka na janaba anachotakiwa ni kuoga kisha aendelee na funga. Hii ni rai ya Maimamu wanne na wanazuoni walio wengi. Imamu Bukhari na Muslim walinukuu kuwa mama Aisha na Ummu Salamah رضي الله عنهما walisema kuwa Mtume ﷺ alikuwa akiamka na janaba kutokana na kitendo cha jimai, sio kuota na alikoga na kuendelea na Saumu. Ummu Salamah رضي الله عنها aliongeza kwa kusema kuwa hakuacha kufunga na wala hakuilipa siku hiyo.⁵ Imamu Muslim alinukuu kuwa mama Aisha رضي الله عنها alisema kuwa mtu mmoja aliuliza:

¹ Ahmad 4:23.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 3:389.

³ At-Tabari 3:517.

⁴ Muslim 2:769.

⁵ Fat’hul Al-Bari 4:182 na Muslim 2:781.

يَا رَسُولَ اللَّهِ، تُدْرِكُنِي الصَّلَاةُ وَأَنَا جُنْبٌ فَأَصُومُ؟ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «وَأَنَا تُدْرِكُنِي الصَّلَاةُ وَأَنَا جُنْبٌ فَأَصُومُ».

"Ewe Mjumbe wa Allah! Sala ya Alfajiri hunikuta nikiwa nina janaba, inafaa kufunga?" Mjumbe wa Allah ﷺ akamjibu: "Na mimi wakati wa Sala ya Alfajiri hunikuta nina janaba na huwa nafunga."

Akamuambia, "Wewe si kama sisi, Ewe Mjumbe wa Allah! Allah Amekusamehe madhambi yaliyopita na yajayo." Mtume ﷺ Akasema,

«وَاللَّهِ إِنِّي لَأَزْجُرُ أَنْ أَكُونَ أَحْسَنَكُمْ لِلَّهِ وَأَعْلَمَكُمْ بِمَا أَنْتَبِي».

"Wallah! Nadhani ninamcha zaidi Allah miongoni mwenu na nauelewa vizuri zaidi uchamungu."¹

Funga Huisha Pale Jua Linapozama

Allah تعالى Amesema:

ثُمَّ أَتَمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ

"Kisha timizeni saumu mpaka usiku."

Aya hii inaamrisha kufuturu jua linapokuchwa. Imenukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Sayyidina Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا أَقْبَلَ اللَّيْلُ مِنْ هُنَا، وَأَذْبَرَ النَّهَارَ مِنْ هُنَا فَقَدْ أَفْطَرَ الصَّائِمُ»

"Usiku unapokuja kutoka upande (wa Mashariki) na mchana unapoondoka kutoka upande ule (Magharibi). Hivyo mfungaji hufuturu."²

Imeelezwa kuwa Sahal bin As-Sadi رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ Alisema:

«لَا يَزَالُ النَّاسُ بِخَيْرٍ مَا عَجَلُوا الْفِطْرَ»

"Watu watabaki kwenye kheri madhali wanafanya haraka kufuturu."³

¹ Muslim 2:781.

² Fat'hul Al-Bari 4:231 na Muslim 2:772.

³ Fat'hul Al-Bari 4:234 na Muslim 2:771

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: إِنَّ أَحَبَّ عِبَادِي إِلَيَّ أَعْجَلُهُمْ فِطْرًا»

“Allah Aliyetukuka, Anasema; “Wapenzi Wangu miongoni mwa waja Wangu, ni wale wanaofanya haraka kufuturu.”¹

At-Tirmidhi alinukuu Hadith hii na akasema kuwa Hadith hii ni Hasan Gharib.²

Kuharamishwa kwa Funga ya Mfululizo (*Wiswal*)

Kuna Hadith Sahihi kadhaa zinazoharamisha *Al-Wiswal*, ambayo ina maana kufunga usiku na mchana bila kula. Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا تُوَاصِلُوا، قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ إِنَّكَ تُوَاصِلُ، قَالَ: «فَإِنِّي لَنْتُ مِثْلَكُمْ إِنِّي أَبِيثُ يُطْعِمُنِي رَبِّي وَيَسْقِيَنِي».

“Msiunganishe kufunga.” Hivyo wakamuambia, “Ewe Mjumbe wa Allah, mbona wewe unafunga usiku na mchana?” Mtume ﷺ akajibu, “Mimi si kama nyinyi, mimi ninalishwa na kunyweshwa na Mola Wangu wakati nikiwa nimelala.”

Hivyo, watu walipokataa kuacha kuunganisha kufunga, Mtume ﷺ alifunga siku mbili pamoja na usiku wake (pamoja na wale waliunganisha kufunga usiku na mchana na kisha waliona mwezi mwandamo (wa Mwezi *Shawwal*). Mtume ﷺ aliwaambia (kwa hasira):

«لَوْ تَأَخَّرَ الْهَيْلَالُ لَرِذْتُكُمْ»

“Lau mwezi usingeandama, ningekuzidishieni (masiku mengine ya) kufunga.”

Hivyo ilikuwa adhabu kwao (walipokataa kuacha kufunga usiku na mchana).³ Hadithi hii ilinukuliwa katika sahihi mbili. Kuharamishwa kufunga usiku na mchana kumetajwa katika mapokezi mengi. Ni ukweli kuwa kufunga usiku na mchana ilikuwa moja ya sifa maalum za Mtume ﷺ kwani yeye alikuwa ana

¹ Ahmad 2:237.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 3:386.

³ Ahmad, Fat'hul Al-Bari 4:238 na Muslim 2:774.

uwezo na alisaidiwa katika hilo. Ni dhahiri kuwa chakula na kinywaji alichokuwa akikipata Mtume wakati akifunga usiku na mchana (*Al-Wiswaal*) ilikuwa ni cha kiroho na si kama hiki ambacho tunakijua sisi, vinginevyo asingeweza kufunga usiku na mchana (*Al-Wiswaal*). Inafaa kutaja kuwa inaruhusiwa kujizuia kufuturu kuanzia mawio mpaka kabla ya Alfajiri (*Sahur*). Hadith iliyosimuliwa na Abi Said al-Khudhri رضى الله عنه inasema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا تُؤَاصِلُوا فَأَيُّكُمْ أَرَادَ أَنْ يُؤَاصِلَ فَلْيُؤَاصِلْ إِلَى السَّحْرِ»

"Msiunganishe kufunga (Al-Wiswaal) lakini yeyote anayetaka kufanya hivyo, basi anaruhusiwa mpaka wakati wa Sahur."

Wakasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah, unafunga usiku na mchana (*Al-Wiswaal!*) Akajibu,

«إِنِّي لَسْتُ كَهَيْئَتِكُمْ، إِنِّي أَبِيْتُ لِي مُطْعِمٌ يُطْعِمُنِي وَسَاقٍ يَسْقِينِي»

"Mimi sio sawa na nyie, kwani Mimi Ninaye Ambaye Ananifanya mimi nile, ninywe wakati wa usiku."

Hadithi hii pia imekusanywa katika Sahih Mbili.¹

Hukumu za Itikafu:

Ali bin Abu Talhah alieleza kuwa Ibn Abbas رضى الله عنهما alisema, "Aya hii inamhusu mwanaume aliyekaa Itikafu msikitini katika mwezi wa Ramadhani au miezi mingine. Allah تعالى Amemkataza kuwagusa (kuingiliana kimwili na) wanawake, usiku au mchana mpaka aikamiilishe Itikafu² yake. Adh-Dhahhak alisema, "Hapo mwanzoni, mwanaume aliyekaa Itikafu angeweza kutoka msikitini kama apendavyo na angeweza kumuingilia mkewe. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَلَا تُبَشِّرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَلَيْكُنَّ فِي الْمَسْجِدِ

"Wala msichanganyike nao, na hali mkiwa Itikafu msikitini."

Maana yake: "Msiwaguse wake zenu wakati mko katika Itikafu, msikitini au nje ya msikiti."³ Hii pia ni rai ya Mujahid, Qatadah na wanazuoni kadha, ni kuwa Waislam walikuwa wakiwajimai wake zao wakati wakiwa katika Itikafu

¹ Fat'hul Al-Bari 4:338.

² At-Tabari 3:540.

³ At-Tabari 3:541.

⁴ At-Tabari 3:541.

walipotoka msikitini, mpaka Ayah ilipotoremshwa.⁴ Ibn Abu Hatim alitolea maoni, “Ilielezwa kuwa Ibn Mas’ud, Muhammad bin Ka’b. Mujahid, Ata’ Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na Muqatil walisema kuwa Ayah ina maana, “usimguse mke ukiwa katika Itikafu.”¹

Jambo hili alilolieza Ibn Abu Hatim kutoka kwa hao watu linakubaliwa na wanazuoni. Wale walio katika Itikafu hawaruhusiwi kuwaingilia wake zao wakiwa wanaendelea na Itikafu msikitini. Endapo mtu mmojawapo atalazimika kutoka msikitini kwa ajili ya kwenda msalani au kula, hawaruhusiwi kumbusu au kumkumbatia mkewe au kujishughulisha na jambo jingine zaidi ya Itikafu. Aidha haruhusiwi hata kumtembelea mgonjwa, lakini anaweza kuulizia hali zao anapopita njia. Itikafu ina masharti mengine, hayo tumeyaeleza mwishoni mwa kitabu chetu juu ya *Siyam* (funga), shukrani zote Anastahiki Allah تعالى. Zaidi ya hayo, wanazuoni wa Fiqh walikuwa wakifuatisha maelezo ya *Siyam* (funga) na maelezo ya Itikafu, kwa kuwa hivi ndivyo maelezo hayo yalivyotajwa ndani ya Qur’an. Kwa kuitaja Itikafu baada ya funga, Allah تعالى Anatutaka tukae Itikafu wakati wa mwezi wa kufunga, hususan sehemu ya mwisho wa mwezi. Sunnah ya Mtume ﷺ ni kuwa alikuwa akikaa Itikafu usiku katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhani mpaka alipofariki dunia. Baadaye, wakeze Mtume walikuwa wakikaa Itikafu kama Sahih Mbili zilivyonukuu kutoka kwa Aisha رضي الله عنها, Mama wa Waumini.²

Imeandikwa ndani ya Sahih Mbili kuwa Safiyyan bint Huyay رضي الله عنها, alikwenda msikitini kumtembelea Mtume ﷺ akiwa katika Itikafu. Akazungumza naye kwa muda mfupi, kisha akasimama kurejea nyumbani. Mtume ﷺ alimsindikiza kwa sababu ilikuwa usiku. Nyumba yake ilikuwa jirani na nyumba ya Usamah bin Zayd رضي الله عنه pambizoni mwa Al-Madinah. Wakati wakitembea walikutana na wanaume wawili wa kiansari ambao walipita kwa haraka baada ya wao kumuona Mtume ﷺ. Na katika mapokezi mengine, “(Ansari hao wawili) walijificha, yaani waliona haya kwa Mtume baada ya kumuona akiwa na ahli yake, Mtume ﷺ akawaambia:

«عَلَىٰ رَسَلِكُمَا، إِنَّهَا صَفِيَّةُ بِنْتُ حُيَيٍّ»

“Hapo hapo mlipo Msikimbie! Huyu ni (mke wangu) Safiyyah bint Huyay.”

¹ Ibn Abu Hatim 1:385 -387.

² Fat’hul Al-Bari 4:318 na Muslim 2:831.

Wote wawili wakasema: "Utakasifu ni wa Allah تعالى, (vipi tutakufikiria vibaya). Ewe Mjumbe wa Allah!" Mtume ﷺ akawaambia:

«إِنَّ الشَّيْطَانَ يَجْرِي مِنْ ابْنِ آدَمَ مَجْرَى الدَّمِ، وَإِنِّي خَشِيتُ أَنْ يَفْذِفَ فِي قُلُوبِكُمْمَا
شَيْئًا، أَوْ قَالَ: شَرًّا»

*"Shaytani hupita mwilini mwa binadamu katika mapito ya damu. Nimechelea Shaytani asije akapandikiza fikra mbovu katika akili zenu. Au alisema, "Shari."*¹

Imam Ash-Shafi alitoa maelezo, "Mtume ﷺ alikusudia kuufundisha Ummah kuondoa haraka fikra mbovu, ili wasiingie katika yaliyoharamishwa. Wao (wanaume wawili wa Kiansari) walikuwa wakimuogopa zaidi Allah تعالى kuliko kumdhania vibaya Mtume ﷺ." Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Aya (2:187) inakataza jimai na mengine kama kubusu au kukumbatia ambako hakuruhusiwi kufanywa wakati wa Itikafu. Ama kuwa na mke anayemsaidia mumewe, ni ruhusa. Imeelezwa katika Sahih Mbili kuwa Aisha رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ alikuwa akinisogezea kichwa (ndani ya chumba chake) nami nilimchana nywele zake, na nilipokuwa ndani ya siku zangu alikuwa haingiii nyumbani isipokuwa kwa haja za kawaida za kibinaadamu." Amesema Aisha رضي الله عنها, 'Anaweza kuwepo mgonjwa nyumbani lakini asimuulize ila akipitapita.'² Kauli ya Allah تعالى,

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ

"Hiyo ni Mipaka ya Mwenyezi Mungu." Maana yake: Hili ambalo tumelibainisha na kuliweka kuwa jambo la lazima, na tukalifanya kuwa ni jambo la kisharia miongoni mwa swaumu pamoja na hukumu zake. Na yale ambayo tumeruhusu na kuharamisha ndani yake, na kutaja malengo yake na ruhusa zake yote hayo ni mipaka ya Allah تعالى, kwa maana ya ishara Zake Allah تعالى Ambazo Amezibainisha Yeye Mwenyewe. Hiyo ni;

أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَى نِسَائِكُمْ

"Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu."

¹ Fat'hul Al-Bari 4:326 na Muslim 2:1712

² Fat'hul Al-Bari 4:320 na Muslim 1:244

Alisoma mpaka:

ثُمَّ أَتَمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ

“Kisha timizeni Saumu mpaka usiku.”

“Baba yangu na wengine katika masheikh zetu wakisema kama hivi na wanatusomea Aya hiyo.”

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ

“Namna hivi Mwenyezi Mungu Anabainisha Ishara Zake kwa watu.”

Maana yake: Kama Alivyoielezea fungu na masharti yake na hukumu zake, sharia zake na ufafanuzi wake. Pia Anabainisha hukumu zingine kupitia kwa mjumbe Wake Muhammad ﷺ. Allah تعالى Anaendelea:

لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

“Kwa watu ili wapate kumcha.”

Maana yake: “Ili waweze kujua namna ya kupata uongozi wa kweli na wajue namna ya kumuabudu (Yeye)”.

Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema:

هُوَ الَّذِي يُزِيلُ عَلَى عَبْدِهِ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٧٨﴾

“Yeye Ndiye Anayemteremshia mja Wake Aya zinazobainisha wazi ili Akutoeni gizani muingie kwenye nuru. Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye Kurehemu.” (57:9)

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُم بَيْنَكُم بِالْبَاطِلِ وَتُدْخُلُوا بِهَا إِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٧٩﴾

188. “Wala msiliane mali zenu kwa baatili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua.”

Rushwa Imekatazwa na ni Haramu

Ali bin Abu Talhah alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Aya hii (2:188) inamkusudia kila mtu anayedaiwa ambapo hapana ushahidi wa deni. Hivyo anakana kuchukua mkopo, na kesi inakwenda kwenye mamlaka husika na yeye anajua kwamba hana haki katika mali hiyo na anakula mali ya haramu."¹ Rai hii ilielezwa pia kutoka kwa Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan na Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Wote walisema, "Usipinge wakati unajua kuwa unadhulumu."²

Hukumu ya Kadhi (Hakimu, Jaji n.k) Haihalalishi cha Haramu wala Haiharamishi cha Halali

Imeelezwa katika Sahih Mbili kuwa Ummu Salamah رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَلَا إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ، وَإِنَّمَا يَأْتِينِي الْخِصْمُ، فَلَعَلَّ بَعْضَكُمْ أَنْ يَكُونَ أَلْحَنَ بِحُجَّتِهِ مِنْ بَعْضٍ فَأَقْضِي لَهُ، فَمَنْ قَضَيْتَ لَهُ بِحَقِّ مُسْلِمٍ فَإِنَّمَا هِيَ نِطْعَةٌ مِنْ نَارٍ، فَلْيُحْمِلْهَا أَوْ لِيَذُرْهَا»

"Tambueni kuwa mimi ni mwanaadamu! na si vinginevyo watesi wananjia. Huenda baadhi yenu ni wambuji na mna ushawishi mkubwa mnapowasilisha hoja zao. Na kwa Ajili hiyo nikampa ushindi. Hivyo, ikasababisha nimpe haki ya Muislam mwingine. Ajue amechukuwa kipande cha moto. Ana hiyari kukichukuwa au kukiacha."³

Aya na Hadith zinathibitisha kuwa hukumu ya mamlaka husika, kwa hali yoyote ile iwayo haibadili ukweli. Hivyo, hukumu haihalalishi vilivyoharamishwa wala haiharamishi vilivyohalalishwa. Hivyo, hukumu ikienda sawa na ukweli, hapana madhara katika hali hiyo. Vinginevyo, jaji atapata malipo yake, ambapo mwongo atapata mzigo wa uovu.

Ndiyo sababu Allah تعالى Akasema:

¹ At-Tabari 3:550.

² Ibn Abu Hatim 1:393-394 na At-Tabari 3:550-551.

³ Fat'hul Al-Bari 13:190 na Muslim 3:1373.

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوا بِهَا إِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ

النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٨﴾

“Wala msiliane mali zenu kwa baatili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali za watu kwa dhambi, na hali mkijua.” (2:188)

Maana yake: “Japokuwa mnajua upotofu wa yale mnayodai.” Qatadah alisema, “Ewe mwana wa Adamu! Tambua kuwa hukumu ya Hakimu haihalalishi yale yaliyoharamishwa au kukataza yaliyohalalishwa. Hakimu huhukumu kwa mujibu wa uelewa wake na ushahidi wa mashahidi. Hakimu ni binadamu tu na ni mwenye kufanya makosa. Fahamu kuwa endapo Hakimu atakosea katika kuhukumu na akampendelea mtu, basi mtu huyo bado atapambana na wadai pindi watakapokutana na Allah تعالی katika Siku ya Kiyama. Kisha, mtu mwovu atahukumwiwa kwa haki ili kusahihisha makosa yaliyofanywa katika hukumu iliyotolewa humu duniani.”

* يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ وَلَيْسَ الْبِرُّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ
مِنْ ظُهُورِهَا وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنِ اتَّقَى وَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ أَبْوَابِهَا وَأَتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ ﴿١٨٩﴾

189. “Wanakuuliza khabari ya miezi. Sema: Hivyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu wa Hija. Wala sio wema kuziingia nyumba kwa nyuma, bali mwema ni mwenye kumchamungu. Na ingieni majumbani kupitia milangoni. Na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.”

Suala la miezi Miandamo

Al-Awfi alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Watu walimuuliza Mtume ﷺ kuhusu miezi miandamo. Baada ya hapo Aya hii iliteremshwa:

* يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ

“Wanakuuliza habari za mwezi. Sema: Hivyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu wa Hija.”

Ni ili waweze kuvipima vitendo vyao vya kiibada, Eda za wanawake na kipindi cha Hajj (kuhiji Makkah).¹ Abdur-Razaq alielezea kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«جَمَلَ اللهُ الْأَهْلَةَ مَوَاقِيَتَ لِلنَّاسِ، فَصُومُوا لِرُؤْيَيْتِهِ، وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَيْتِهِ، فَإِنَّ غَمَّ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ يَوْمًا»

“Allah Ameufanya mwezi mwandamo kuwa nyakati za watu. Hivyo, fungeni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa Ramadhan) na fungueni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa Shawwal). Iwapo mwezi ukizingwa hesabuni siku thelathini za mwezi mliionao.”² Na Al-Hakim amielezea katika Mustadraki wake na akasema Isnadi yake ni sahihi. Bukhari na Muslim.

Kipimo cha Wema Kizingatiwe kwa Kumchamungu

Allah تعالى alisema:

وَلَيْسَ الْبِرُّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ ظُهُورِهَا وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنِ اتَّقَى³ وَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ أَبْوَابِهَا⁴

“Wala sio wema kuziingia nyumba nyuma. Bali mwema ni mwenye kumcha Mungu. Na ingieni majumbani kupitia milangoni.”

Bukhari aliandika kuwa Al-Baraa رضي الله عنه alisema, “Wakati wa *Jahiliyyah*, waki-shahirimia (kutia nia ya ibada ya Hijja) walikuwa wakiingia ndani ya Al-Kaaba kupitia nyuma.” Baada ya hapo, Allah تعالى Akateremsha Aya ifuatayo:

وَلَيْسَ الْبِرُّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ ظُهُورِهَا وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنِ اتَّقَى³ وَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ أَبْوَابِهَا⁴

“Wala sio wema kuziingia nyumba nyuma. Bali mwema ni mwenye kumcha Mungu. Na ingieni majumbani kupitia milangoni.”³

¹ At-Tabari 3:554. Isnadi yake ni dhaifu.

² Abdur-Razaq 4:156.

³ Al-Hakim 1:423.

Abu Dawud At-Tayalisi alinukuu pia Hadith hiyo kutoka kwa Al-Baraa رضي الله عنه lakini kwa maneno yafuatayo: “Ansar walikuwa wakiingia kwenye majumba kila wanaporejea kutoka safarini kupitia nyuma ya nyumba.”

Baada ya hapo, Aya hii ikashuka (2:189).¹

Al-Hasan alisema, “Baadhi ya watu katika zama za Jahiliyyah walipotoka nyumbani ili kusafiri, halafu akaahirisha safari, hawakuingia majumbani kupitia milangoni, bali waliruka ukuta wa nyuma.

Allah تعالى Anasema:

وَلَيْسَ الْبِرُّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ ظُهُورِهَا

“Wala sio wema kuziingia nyumba kwa nyuma.”²

وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.”

Kuwa na *Taqwa* kwa Allah تعالى, ina maana kutekeleza yale Aliyoyaamrisha na kuyaacha yale Aliyoyakataza.

لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

“Ili mpate kufanikiwa.”

Kesho mtakaposimama mbele Yake na Yeye Atakulipeni kwa ukamilifu na utimilifu.

* * *

¹ Musnad At-Tayalisi 98.

² Ibn Abu Hatim 1:401.

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿١٩٠﴾ وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجَكُمُ ۗ وَالْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنَ الْقَتْلِ ۗ وَلَا تُقَاتِلُوهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّى يُقَاتِلَكُمُ فِيهِ ۗ فَإِنْ قَتَلَكُمُ فَاقْتُلُوهُمْ ۗ كَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿١٩١﴾ فَإِنْ أَنْهَوْا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٩٢﴾ وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الَّذِينَ لِلَّهِ ۗ فَإِنْ أَنْهَوْا فَلَا عُدْوَانَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٩٣﴾ الشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَتُ قِصَاصٌ ۗ فَمَنْ أَعْتَدَى عَلَيْكُمْ فَأَعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا أَعْتَدَى عَلَيْكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٩٤﴾ وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ ۗ وَأَحْسِنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٥﴾ وَأَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ ۗ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۗ وَلَا تَحْلِفُوا زُهُوسَكُمْ حَتَّى يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحَلَّهُ ۗ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ بِمَهْ أَدَى مِنْ رَأْسِهِ ففِدْيَةٌ مِنْ صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ۗ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۗ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامٌ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةً إِذَا رَجَعْتُمْ ۗ تِلْكَ عَشْرَةٌ كَامِلَةٌ ۗ ذَلِكَ لِمَنْ لَمْ يَكُنْ أَهْلُهُ حَاضِرِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿١٩٠﴾ وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ أَخْرَجَكُمُ ۗ وَالْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنَ الْقَتْلِ ۗ وَلَا تُقَاتِلُوهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّى يُقَاتِلَكُمُ فِيهِ ۗ فَإِنْ قَتَلَكُمُ فَاقْتُلُوهُمْ ۗ كَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿١٩١﴾ فَإِنْ أَنْهَوْا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٩٢﴾ وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الَّذِينَ لِلَّهِ ۗ فَإِنْ أَنْهَوْا فَلَا عُدْوَانَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٩٣﴾

190. "Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu Hawapendi waanza uadui."

191. "Na wauweni popote muwakutapo, na muwatoe popote walipokutoeni; kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kuua. Wala msipigane nao

kwenye Msikiti Mtakatifu mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni huko basi nanyi pia wapigeni. Na hivi ndivyo yalivyo malipo ya makafiri.”

192. “Lakini wakiacha basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

193. “Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina, na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu.”

Amri ya kupigana na wale wanaowapiga

Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى alisema kuwa Ar-Rabii bin Anas alisema kuwa Abu Al-Aliyah aliyatolea maelezo Maneno ya Allah تعالى:

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ

“Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni.” (17:55)

Abu Al-Aliyah alisema, “Hii ilikuwa Aya ya mwanzo kuhusu kupigana ambayo iliteremshwa Madinah. Tangu siku hiyo ilipoteremshwa, Mtume ﷺ alikuwa akiwapiga wale waliompiga na akawaacha wasiokuwa wapiganaji. Baadaye Suratul Bara-ah (Sura ya 9 katika Qur’an) iliteremshwa.”¹ Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema vivyo hivyo, kisha akasema kuwa hii ilifutwa na Aya hii:

فَأَقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ

“Basi waueni washirikina popote muwakutapo.” (9:5)

Hata kauli hii sio kamili, kwa sababu ya Kauli ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يُقَاتِلُونَكُمْ

“Wale wanaokupigeni.” Inawahusu tu wale maadui wanaoupiga vita Uislam na Waislam. Hivyo Aya hii ina Maana, ‘Wapige wale wanaokupiga, kama Allah تعالى Alivyosema (katika Aya nyingine):

¹ At-Tabari 3:561.

وَقَاتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقَاتِلُونَكُمْ كَافَّةً

“Na piganeni na washirikina wote kama wao wanavyopigana nanyi nyote.” (9:36)¹

Hii ndio sababu Allah تعالى Alisema baadaye katika Aya:

وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُم

“Na waueni popote muwakutapo, na muwatoe popote walipokutoeni...”

Maana yake: Nguvu zenu zitumike kuwapiga wao, kama nguvu zao zinavyotumika kukupigeni, na katika kuwafukuza kutoka maeneo ambamo walikufukuzeni nyie, kama ilivyo sharia ya kisasi katika kuadhibu.

Makatazo ya Kuvuka Mipaka Katika Ulipizaji Kisasi kwa Kukatakata Viungo vya Maiti na Kuiba Ngawira:

Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٥٦﴾

“...wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu Hawapendi waanza uadui.”

Aya hii ina maana kuwa, ‘Piganeni kwa ajili ya Allah تعالى na usichupe mipaka, kama vile, kufanya yaliyoharamishwa.’ Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alieleza kuwa kuchupa mipaka (ilivyoenezwa na Ayah) ni pamoja na kukatakata viungo vya maiti, kuiba (kutoka kwenye ngawira), kuwaua wanawake, watoto na vikongwe ambao hawashiriki katika vita, kuwaua makasisi na wakazi katika nyumba za ibada, kuchoma miti na kuuu wanyama bila manufaa yoyote.” Hii pia ni rai ya Ibn Abbas, Umar bin Abdul-Aziz, Muqatil bin Hayyan na wengineo. Muslim alinukuu katika Sahihi yake kuwa Buraydah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«اغزوا في سبيل الله، قاتلوا من كفر بالله، اغزوا ولا تغلوا ولا تغدروا ولا تمثلوا ولا تقتلوا وليداً ولا أضحاب الصوامع»

¹ At-Tabari 3:562.

“Piganeni kwa ajili ya Allah na piganeni na wale wanaomkufuru Allah. Piganeni lakini msiibe (kutokana na ngawira), msifanye usaliti, msiwakatekate (maiti), wala msiwaue watoto wala wale waliomo ndani ya nyumba za ibada.”¹

Imeelezwa katika Sahih Mbili kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, “Alikutwa mwanamke amekufa katika moja ya vita alivyopigana Mtume ﷺ na hapo Mtume ﷺ alikataza kua wanawake na watoto.”² Kuna Hadith nyingi kuhusu somo hili.

Ushirikina ni mbaya kuliko kua:

Baada ya kuwa Jihad inaambatana na kumwaga damu za watu. Allah تعالى Ameonesha kuwa watu wanaomshirikisha Yeye (katika kuabudu), wanamkufuru Yeye na wanazuia kufuatwa kwa Njia Yake, wanafanya uovu mkubwa na maangamivu kuliko kua. Abu Malik ametoa maelezo juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَأَلْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنْ الْقَتْلِ^٣

“Kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kua.”

Abu Malik amesema, maana yake kile makafiri wanachokifanya ni kibaya zaidi kuliko kua.³ Abu Al-Aliyah, Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahak na Ar-Rabi bin Anas walitafsiri Kauli ya Allah تعالى:

وَأَلْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنْ الْقَتْلِ^٣

“Kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kua.”

‘Ushirikina ni mbaya zaidi kuliko kua’

Uharamu wa vita katika maeneo matakatifu na kuruhusiwa kujihami:

Allah تعالى Amesema:

وَلَا تُقْبَلُ لَهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

“Wala msipigane nao kwenye Msikiti Mtakatifu.”

¹ Muslim 3:1357.

² Fat’hul Al-Bari 6:172 na Muslim 3:1364.

³ Ibn Abu Hatim 1:412.

Imeandikwa ndani ya Sahih Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ هَذَا الْبَلَدَ حَرَمٌ لِلَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، وَلَمْ يَجِئْ لِي إِلَّا سَاعَةٌ مِنْ نَهَارٍ، وَإِنَّهَا سَاعَتِي هَذِهِ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، لَا يُعْضَدُ شَجَرُهُ، وَلَا يُخْتَلَى خَلَاهُ، فَإِنْ أَحَدٌ تَرَخَّصَ بِقِتَالِ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ، فَقُولُوا: إِنَّ اللَّهَ أَدِنَ لِرَسُولِهِ وَلَمْ يَأْذَنْ لَكُمْ»

“Allah Aliufanya mji huu, kuwa Mtakatifu toka siku Alizoumba mbingu na ardhi. Hivyo, ni sehemu Takatifu kwa Amri ya Allah mpaka siku ya Kiyama. Na kupigana ndani yake kulihalalishwa kwangu tena kwa saa chache za mchana. Hivyo, ni sehemu Takatifu kwa Amri ya Allah mpaka silu ya Kiyama. Miti yake isikatwe na majani yake yasing’olewe. Endapo mtu atataja mapigano yaliyofanywa na Mjumbe wa Allah kuwa ni hoja inayoruhusu watu kupigana katika mji huo, basi semeni kuwa Allah Alimruhusu mjumbe Wake, lakini hakukuruhusuni ninyi.”¹

Katika Hadith hii, Mtume ﷺ anazungumzia kuwapiga watu wa Makkah alipoiteka kwa nguvu na kusababisha vifo vya baadhi ya makafiri kwenye eneo la Khandamah. Hili lilijiri baada ya Mtume ﷺ kutangaza,

«مَنْ أَغْلَقَ بَابَهُ فَهُوَ آمِنٌ، وَمَنْ دَخَلَ الْمَسْجِدَ فَهُوَ آمِنٌ، وَمَنْ دَخَلَ دَارَ أَبِي سُفْيَانَ فَهُوَ آمِنٌ»

“Yeyote atakayejifungia ndani yu Salama. Yeyote atakayeingia Msikiti Mtakatifu yu Salama. Yeyote atakayeingia nyumba ya Abu Sufyan pia yu Salama.”²

Allah تعالى Amesema:

حَتَّى يُقْتَلُوكُمْ فِيهِ ۖ فَإِنْ قَتَلُوكُمْ فَأَقْتُلُوهُمْ ۗ كَذَلِكَ جَزَاءُ الْكٰفِرِينَ ﴿١٩٦﴾

“Mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni huko basi nanyi pia wapigeni. Na hivi ndivyo yalivyo malipo ya makafiri.”

¹ Fat’h Al-Bari 6:327 na Muslim 3:986-987.

² Ahmad 2:292.

Allah تعالى Amesema: ‘Wala msipigane nao katika eneo la Msikiti Mtakatifu mpaka watakapoanza kukupigeni humo.’ Katika hali hii, mnaruhusiwa kuwapiga na kuwaua ili kuzuia shari yao. Kama vile, Mtume ﷺ alivyochukua ahadi kutoka kwa Masahaba zake chini ya mti (katika eneo la Hudaibiyah) kuwapiga (makafiri), baada ya makabila ya Quraysh na washirika wao, Thaqif na makundi mengine, waliposaidiana dhidi ya waislam (kuwazuia kuingia Makkah kwa ajili ya kuuzuru Msikiti Mtakatifu).

Kisha, Allah تعالى Aliizuia vita kabla ya kuanza kati yao na Akasema:

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ بَعْدِ أَنْ أَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ

“Na Yeye Ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makkah baada ya Kukupeni Ushindi juu yao.” (48:24)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ مُّؤْمِنَاتٌ لَّمَّ تَعَلَّمُوهُمْ أَنْ تَطَّعُوهُمْ فَتَصِيْبُكُمْ مِنْهُمْ مَعْرَةٌ
بِغَيْرِ عِلْمٍ لَّيُدْخِلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ
عَذَابًا أَلِيمًا

“Na lau si wanaume waumini na wanawake waumini msiwajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua. Mwenyezi Mungu (Amefanya haya) ili Amuingize Amtakaye katika Rehema Yake. Lau wengelitengana bila ya shaka Tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.” (48:25)

Kauli ya Allah تعالى:

فَإِنْ أَنْتَهُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Lakini wakiacha basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

Ina Maana: “Iwapo (makafiri) wakiacha kuwapiga waislamu katika Eneo Takatifu, na wakaingia katika Uislam na kutubia, Allah تعالى Atawasamehe madhambi yao, japokuwa waliwaua katika siku zilizopita katika eneo Takatifu

la Allah تعالى. Hakika msamaha wa Allah تعالى Unajumuisha kila dhambi, bila kujali ukubwa wake, wakati mkosaji anapotubia.

Amri ya kupigana ili pasiwe na fitnah:

Kisha Allah تعالى Aliamrisha kupigana na makafiri Aliposema:

حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةً

“Mpaka pasiwepo fitina.”

Fitna hapa ni Ushirikina. Haya ni maoni ya Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah, Mujahid, Al-Hasan, Qatadah, Ar-Rabi, Muqatil bin Hayyan, As-Sudi na Zaid bin Aslam

رضي الله عنهم¹. Kauli ya Allah تعالى:
وَيَكُونَ آلَ دِينٍ لِلَّهِ

“Na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: ‘Ili Dini ya Allah تعالى iwe juu ya dini nyingine zote.’

Imeelezwa ndani ya Sahih Mbili kuwa Abu Musa Al-Ash’ari رضي الله عنه alisema: “Mtume ﷺ aliulizwa, “Ewe Mjumbe wa Allah! Mtu anayepigana kuonesha ushujaa na mwingine anapigana kwa kasumba ya ukabila na mwingine anapigana kwa kujionesha ni yupi kati yao anayepigana kwa ajili ya Allah تعالى.” Mtume ﷺ alijibu:

«مَنْ قَاتَلَ لِتَكُونَ كَلِمَةً لِلَّهِ هِيَ الْعُلْيَا فَهُوَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Anayepigana ili Neno la Allah liwe juu, huyo anapigana katika Njia ya Allah.”²

Kwa nyongeza, Imeandikwa katika Sahih Mbili:

«أَمِزْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَقُولُوا لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَإِذَا قَالُوا عَصَمُوا مِنِّي دِمَاءَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ إِلَّا بِحَقِّهَا وَحَسَابُهُمْ عَلَى اللَّهِ»

“Nimeamrisha (na Allah) kuwapiga watu mpaka waseme kwamba: ‘Hapana Apasaye Kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.’ Yeyote

¹ Ibn Hatim 1:415 416.

² Fat’hul Al-Bari 13:450 na Muslim 3:1513.

atakayesema, atakuwa amesalimisha maisha na mali zake kwangu, isipokuwa kwa haki yake, na hesabu yake itakuwa kwa Allah.”¹

Kauli ya Allah تعالی:

فَإِنْ أَنْتَهُوَ فَلَا عُذْرَانَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٩٦﴾

“Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu.”

Inaonesha kuwa: “Iwapo wataacha Ushirikina na jambo la kuwapiga waumini, basi muache kuwapiga vita. Yeyote atakayewapiga baada ya hapo atakuwa anadhulumu. Kwa hakika mashambulizi yanaweza kufanywa dhidi ya udhalimu. Hii ni maana ya kauli ya Mujahid kuwa wapiganaji tu ndio wapigwe.² Au, maana ya Aya inaonesha kuwa, “Iwapo wataacha udhalimu, ambao ni Ushirikina, basi msianze mashambulizi dhidi yao baadaye.” Mashambulizi hapa ina maana, kulipiza kisasi na kuwapiga. Kama Allah تعالی Alivyosema:

فَمَنْ أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَأَعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ

“Anayekushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadri alivyokushambulieni.” (2:194)

Vivo hivyo, Allah تعالی Amesema:

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا

“Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo.” (42:40)

Na Kauli Yake Allah تعالی

وَأَنْ عَاقِبَتُهُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ

“Mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa.” (16:126)

Ikrimah na Qatadah walisema, “Mtu dhalimu ni yule anayekataa kutangaza na kukiri, “Hapana Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالی.”³ Kufuatia Kauli ya Allah تعالی:

² Fat’hul Al-Bari 1:592 na Muslim 1:53.

² At-Tabari 3:584.

³ At-Tabari 3:573.

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ

“Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina.”

Bukhari alinukuu kuwa Nafi alisema kuwa watu wawili walikuja kwa Ibn Umar رضي الله عنهما zama za Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما na walimuambia, “Watu wamekwenda kinyume na mafundisho nawe ni mtoto wa Umar na Sahaba wa Mtume. Hivyo ni kitu gani kinachokuzuia kutoka?”

Akajibu, “Kilichonizuia ni kuwa Allah تعالى Amekataza kumwaga damu ya ndugu yangu (Muislam).” Wakamuambia, “Hukumbuki Allah تعالى Alivyosema:

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ

“Na piganeni nao mpaka isiwepo fitina.”

Naye alijibu, “Tulipigana mpaka Fitnah haikuwepo tena na Dini ikawa ni ya Allah تعالى Peke Yake. Nanyi mnataka kupigana mpaka kuwe na Fitnah au Dini isiwe minghairi ya Allah تعالى.” Uthman bin Salih aliongezea kuwa mtu mmoja alimjia Ibn Umar رضي الله عنهما na kumuuliza, “Ewe Abu Abdur-Rahman! Kitu gani kilikufanya kuhiji mwaka mmoja na Umra mwaka mwingine na ukaacha Jihad katika njia ya Allah تعالى, japokuwa unajua jinsi ilivyohimizwa na Allah تعالى?”

Akajibu, “Ewe mpwa wangu! Uislam umejengwa juu ya nguzo Tano: Kumuamini Allah تعالى na Mjumbe Wake, Sala Tano kila siku, Kufunga Ramadhani, Kutoa Zakah, na kwenda katika Nyumba kwa ajili ya Hajj.” Wakasema, “Ewe Abu Abdur-Rahman! Hukusikia Alivyosema Allah تعالى katika Kitabu Chake:

وَإِنْ طَافَتَا مِنْ الْمُؤْمِنِينَ أَقْتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۗ فَإِنْ بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ

فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّى تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّهِ ۗ

“Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na ikiwa moja la hao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni lililodhulumu mpaka lirejee kwenye Amri ya Mwenyezi Mungu.” (49:9)

Na Kauli Yake,

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ

“Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina.”

Naye alijibu, "Tulipigana katika zama za Mtume ﷺ wakati Uislam ulipokuwa bado dhaifu na Muislamu alikuwa akipata mitihani katika Dini yake, kama vile kuuwawa na kuteswa. Uislam ulipokuwa na nguvu (na kudhihiri), hapakuwa na Fitnah tena." Akaulizwa, "Unasemaje juu ya Ali na Uthman?" Akajibu, "Ama kuhusu Uthman رضي الله عنه, Allah تعالى Amemsamehe. Hata hivyo, mlichukia Allah تعالى kumsamehe! Ama kuhusu Ali رضي الله عنه, ni bin-ami yake Mtume ﷺ na mkwe wake." Kisha akaashiria kwa mkono, akisema, "Hapa ndipo nyumba yake ilipo (akiwa na maana, karibu sana na nyumba ya Mtume) kama ilivyokuwa, Ali رضي الله عنه alikuwa karibu sana na Mtume ﷺ mwenyewe."¹

الشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَتُ قِصَاصٌ ۚ فَمَنْ أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَأَعْتَدُوا عَلَيْهِ
بِمِثْلِ مَا أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٩٤﴾

194. "Mwezi mtakatifu kwa mwezi mtakatifu. Na vitu vitakatifu vimewekewa kisasi. Anayekushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadri alivyokushambulieni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wachamungu."

Imeharamishwa Kupigana Katika Miezi Mitukufu, Isipokuwa kwa Kujihami:

Amesema Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Qatadah Miqsam, Ar-Rabii bin Anas na Ata رضي الله عنهم walisema, "Mtume ﷺ alikwenda Umrah mnamo mwaka wa sita wa Hijrah. Kisha washirikina walimzuia kuingia ndani ya Nyumba Tukufu (Ka'abah – Makkah) akiwa pamoja na Waislam wengine."

Tukio hili lilijiri wakati wa mwezi mtukufu *Dhul-Qa'dah* (mfungo pili). Washirikina waliwaruhusu kuingia ndani ya Ka'aba, mwaka uliofuatia, pamoja na Waislam aliofuatana nao, na Allah تعالى Alimruhusu kulipiza kisasi kwa kitendo hicho cha washirikina pale Aliposema:

الشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَتُ قِصَاصٌ ۚ

"Mwezi mtukufu kwa mwezi mtukufu, na vitu vitakatifu vimewekewa kisasi."

¹ Al-Fat'hi 8:32 Ahmad 3:345.

Imam Ahmad alinukuu kuwa Jabir bin Abdullah رضى الله عنه alisema, “Mtume ﷺ hakuingia vitani wakati wa miezi mitukufu isipokuwa kama alianza kushambuliwa, basi naye huingia katika mapambano. Vinginevyo anapumzika mpaka Miezi Mitakatifu ipite. Hadith hii ina Isnad sahihi ya wapokezi.¹

Kutokana na hilo, Mtume ﷺ aliweka kambi katika eneo la Hudaybiyah na akamtuma Uthman رضى الله عنه awe balozi wake kwenda kwa washirikina. Kisha akapokea habari kuwa Uthman رضى الله عنه ameuwawa, tukio hilo likamfanya achukue ahadi kutoka kwa Masahaba chini ya mti kuwapiga washirikina, Masahaba walikuwa elfu moja na mia nne kwa wakati huo. Na aliposikia ya kuwa tetesi za kuuliwa Uthman رضى الله عنه si za kweli, aliachana na suala la mapigano. Na akashughulikia suala la amani na kutafuta suluhu. Hivyo ikatokea haya yaliyotokea.

Kadhalika Mtume ﷺ alipomaliza kupigana na (makabila) ya Hawazini wakati wa vita vya Hunayn. Hawazini walijificha katika (jiji la) Taif, basi akauzingira mji kwa silaha nzito. Kisha mwezi (Mtukufu) wa *Dhul-Qadah* (mfungo pili) ulianza, wakati Taif ilikuwa bado imezingirwa. Kuzingirwa huko kuliendelea kwa siku arubaini (kuanzia mwanzo wa vita vya Hunayn mpaka Mtume ﷺ aliporejea Madinah kutoka Jiranah zilikuwa siku arubaini) kama ilivyoandikwa ndani ya Sahih Mbili na ilisimuliwa na Anas رضى الله عنه. Baada ya kuona kuwa vifo kwa Masahaba vimekuwa vingi (wakati wa kuzingira), Mtume ﷺ aliacha kuizingira Taif na wala hakuufungua. Kisha akaenda Makka kufanya Umra akitokea Jiranah, na hapo aligawa ngawira za vita ya Hunayn. Ibada hii ya Umrah ilifanyika mwezi wa *Dhul-Qadah* (mfungo pili) ya mwaka wa nane wa Al-Hijrah.² Kauli ya Allah تعالى:

فَمَنْ أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَأَعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا أَعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ^٤

“Anayekushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadri alivyokushambulieni.”

Inaamrisha kufanya uadilifu hata kwa washirikina. Pia Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

¹ Ahad 3:345.

² Fat’hul Al-Bari 3:701 na Muslim 2:916.

وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ^ط

“Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa.” (16:126)

Kauli ya Allah تعالى

وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٩٤﴾

“Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wachamungu.” (2:194)

Anaamrisha kuwa Allah تعالى Atiiwe na Aogopwe kwa kumcha Yeye. Aya inatufahamisha kuwa Allah تعالى Yupo na wachamungu kwa msaada Wake na usaidizi Wake duniani na Akhera.

وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ وَأَحْسِنُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ

الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٥﴾

“Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.” (2:195)

Amri ya Kutoa kwa Ajili ya Allah تعالى:

Bukhari aliandika kuwa Hudhaifah رضي الله عنه alisema:

وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ

“Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo.”

“Iliteremshwa kuhusu kutoa.”¹ Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu vivo hivyo. Kisha ilinukuliwa Hadithi kama hii kutoka kwa Ibn Abbas, Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Ata, Adh –Dhahak, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم. Al-Layth bin Said kutoka kwa Yazid bin Abi Habiib kutoka kwa Aslam Abu Imran alisema, “Mtu mmoja miongoni mwa Ansar alivuka mstari wa adui (Waturuki) katika Konstantinopoli (Istanbul). Abu Ayyub Al-Ansar رضي الله عنه alikuwa

¹ Fat’hul Al-Bari 8:33.

pamoja nasi. Hivyo baadhi ya watu walisema, 'Anajilingiza mwenyewe katika maangamizi.' Abu Ayub رضي الله عنه alisema, "Tunajua vizuri zaidi Aya hii (2:195) kwani iliteremshwa kutuhusu sisi Masahaba wa Mtume ﷺ tulioshiriki katika jihadi pamoja naye, tulimsaidia na kumuunga mkono. Uislam ulipokuwa na nguvu, sisi Ansar, tulikutana na tukawa na mazungumzo, Allah تعالى Ametupa heshima kwa kuwa Masahaba wa Mtume Wake ﷺ na kwa kumsaidia mpaka Uislam ukashinda na wafuasi wake wakaongezeka. Kabla ya hapo tulipuuza mahitaji ya familia zetu, mali na watoto wetu. Vita ilipokoma, tukarejea kwa familia na watoto wetu na kuwahudumia. Hivyo Aya hii iliteremshwa kutuhusu."

وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizi."

Neno Maangamizi lina maana ya "kukaa na familia na mali na kuacha kutekeleza Jihad." Ilinukuliwa na Abu Dawud, At-Tirmidhi, An-Nasai, Abd bin Humayd katika Tafsir yake, Ibn Abu Hatim, Ibn Jarir, Ibn Mardawayh, Al-Hafiz Abu Ya'la katika Musnad wake, Ibn Hibban katika Sahih Yake na Al-Hakim katika Al-Mustadrak.¹ At-Tirmidhi alisema, "Hasan, Sahih Gharib."¹ Al-Hakim alisema, "Inafikia vigezo vya Masheikh Wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawakuiandika."

Abu Dawud ametaja kuwa Aslam Abu Imran alinukuu Hadith hii kwa maneno yafuatayo, "Tulikuwa (tumeizingira) Konstantinopoli. Uqbah bin Amr alikuwa akiongoza majeshi ya Kimisri, ambapo majeshi ya Syria yaliongozwa na Fadhalah bin Ubayd. Baadaye, safu kubwa ya askari wa Kirumi walitufuata, nasi tulijipanga mistari dhidi yao. Mtu mmoja alivamia safu za Jeshi la Warumi na kulitawanya kwa kulishambulia kati yao kisha akarejea kwetu. Watu wakapiga kelele, "Subhana Allah" Shukrani zote Anastahiki Allah تعالى! Anajipeleka mwenyewe kwenye kifo! Abu Ayyub رضي الله عنه alisema, "Enyi watu! Ayah hii mmeielewa vibaya. Iliteremshwa kutuhusu sisi Ansar wakati Allah تعالى Alipoipa ushindi Dini Yake na Wafuasi wake wakaongezeka. Tukazungumza kati yetu, 'Itakuwa bora kwetu sasa tukarejea kwenye mali zetu na kuzishughulikia.' Kisha Allah تعالى Akateremsha Aya (2:195).²

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:311, An-Nasai katika Al-Kubra 6:299, Ibn Abu Hatim 1:424, At-Tabari 3:590, Ibn Hibban 7:105 na Al-Hakim 2:775

² Abu Daud 3:27.

Abu Bakar bin A'yash alieleza kuwa Abu Is-haq As-Subaiy alisimulia kuwa mtu mmoja alimwambia Al-Bara bin Azib رضي الله عنه, "Kama ningevamia na kushambulia safu za maadui peke yangu na wakaniua, ningekuwa nimejitupa mwenyewe kwenye kifo?" Akasema, "Hapana Allah تعالى Alimuambia Mjumbe Wake ﷺ,

فَقَبِيلٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا تَكْلَفُ إِلَّا نَفْسَكَ^٤

"Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu." (4:84)

Aya (2:195) inahusu (kujizuia) kutoa matumizi." Ibn Marduwayh alieleza Hadith hii, pia Al-Hakim katika Mustadrak wake alisema; "Inatimiza vigezo vya Mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawakuiandika." Ath-Thawri رحمه الله تعالى na Qays bis Ar-Rabi walipokea kutoka kwa Al-Baraa رضي الله عنه, lakini aliongeza baada ya Kauli Yake Allah تعالى,

لَا تَكْلَفُ إِلَّا نَفْسَكَ^٤

"Hukalifishwi ila nafsi yako tu." (4:84)

"Maangamizi yana maana: Mtu anayefanya makosa na anaacha kutubia, hivyo hujitia mwenyewe katika maangamizi." Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

وَأَنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ^٥

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo."

"Aya hii haihusu kupigana inahusu kutoa ambapo mtu huacha kutumia kwa ajili ya Allah تعالى, kwa hali hiyo, atakuwa anajitupa mwenyewe katika maangamizo." Madhumuni ya Aya hii, (2:195) inahusu amri ya kutoa katika njia ya Allah تعالى katika maeneo tofauti na njia ambazo zinahusu utiifu na kujikurubisha kwa Allah تعالى. Hususani kutoa mali kwa matayarisho ya kupambana na adui. Allah تعالى Anaeleza kuwa wale wanaozuia kutumia katika njia hizi watakabiliana na hilaki na maangamizo. Kwa maana wale wenye kulazimiana na mwenendo huu. Kisha baada ya hapo Allah تعالى Ameerisha kufanya ihsan, ambayo ni kiwango cha juu kabisa cha utii. Allah تعالى Amesema:

¹ Abu Dawud 3:27.

وَأَحْسِنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٦﴾

“Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao wema”

وَأَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ ۚ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ وَلَا تَحْلِقُوا رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحَلَّهُ ۚ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيضًا أَوْ بِهِ أَذًى مِنْ رَأْسِهِ فَفِدْيَةٌ مِنْ صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ۚ فَإِذَا أُمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامٌ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ۚ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ ۚ تِلْكَ عَشْرَةٌ كَامِلَةٌ ۚ ذَلِكَ لِمَنْ لَمْ يَكُنْ أَهْلَهُ حَاضِرِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ

الْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾

196. “Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa mtazuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana. Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjioni mwao. Na atakayekuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidiya kwa kufunga au kutoa sadaka au kuchinja mnyama, basi mwenye kujistaherasha kwa kufanya Umra ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi kumpata. Na asiyepata, afunge siku tatu katika hija na siku saba mtaporudi; hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.”

Amri ya Kutimiza Hajj na Umrah:

Baada ya Allah تعالى Kutaja hukumu za Saumu na Jihad, Alielezea *Manasik* (Ibada ya matendo) kwa Kuwaamrisha Waislam wakamilishe *Hajj* na *Umrah*, yaani, kumaliza matendo ya *Hajj* na *Umrah* baada ya kuyaanza. Hii ndio sababu Allah تعالى Alisema baadaye

فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ

“Na ikiwa mkizuiwa.”

Hukumu hiyo ni ikiwa njia ya kuelekea kwenye Ka'aba imezuiwa, na mumezuiwa kuikamilisha. Na kwa sababu hii wanazuoni wamekubaliana kuwa vitendo vya *Hajj* na *Umra* vikianzwa lazima vikamilishwe. Ama Mak'hul amesema, 'Kukamilisha' maana yake, kuanza kutoka *Miqat* (maeneo aliyoyapasisha Mtume kutia nia ya Hija).¹ Abdur-Razak alisema kuwa Az-Zuhri alisema, "Tuliambiwa kuwa Umar رضي الله عنه alitoa maelezo juu ya:

وَأْتُمُوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ

"Na timizeni Hajj na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

"Timizeni *Hajj* na *Umrah*." Maana yake: Kuifanya kila moja peke yake, na kufanya *Umrah* nje ya miezi ya Hajj, kwa hilo Allah تعالى Amesema:

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ

"Hija ni miezi maalum." (2:197)²

As-Suddi amesema:

وَأْتُمُوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ

"Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Maana yake: 'Mdumu kuitekeleza *Hajj* na *Umrah*."³ Amenukuu Qatada kutoka kwa Zurara kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Hajj ni *Arafat*, na *Umrah* ni *Tawaf*."⁴ Al-A'mash alisimulia kuwa Alqamah aliitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى:

وَأْتُمُوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ

"Na timizeni Hija na Umrah kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Abdullah (Ibn Masud) رضي الله عنه aliisoma hivi: 'Kamilisheni *Hajj* na *Umrah* kwenye Ka'aba', ili mmoja wenu asilivuke eneo la Ka'aba wakati wa *Umrah*. Kisha Ibrahim akasema, "Niliitaja kauli hii kwa Said bin Jubayr alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza hivyo."⁵ Sufyan kutoka kwa A'mash alinukuu kutoka kwa Mansur naye kutoka kwa Ibrahim alisema kuwa Alqamah alisema

¹ Ibn Abu Hatim 1:437.

² Ibn Abu Hatim 1:437.

³ At- Tabari 4:12.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:439

⁵ At- Tabari 4:7.

(kuhusiana na Aya (2:196), "Tekelezeni *Hajj* na *Umrah* katika Ka'aba."¹ Ath-Thawri رحمه الله تعالى alieleza kuwa Ibrahim aliisoma (Aya), 'Na Simamisheni *Hija* na *Umrah* kwenye Nyumba ya Allah تعالى."

Endapo Mtu Atazuiwa Akiwa Njiani, Atachinja Hapohapo, Kunyoa Nywele na Kuhitimisha Ibada Yake:

Kauli ya Allah تعالى:

فَإِنْ أَحْصَرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۗ

"Na mkzuiwa basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana."

Iliteremshwa mwaka wa sita wa Hijrah, mwaka wa Mkataba wa *Al-Hudaibiyah* wakati washirikina walipomzuia Mtume ﷺ kufika katika Nyumba ya Allah تعالى. Allah تعالى Aliteremsha *Surat Al-Fat'h* (Sura ya 48) katika Qur'an kisha akawaruhusu Waislam kuchinja wanyama walio wepesi kupatikana. Walikuwa na ngamia sabini kwa ajili hiyo. Aidha waliruhusiwa kunyoa vichwa vyao na kutoka katika *Ihram*. Mtume ﷺ alipowaamrisha wanyoe nywele zao na wamalize *Ihram*, hawakumtii, kwa kuwa walikuwa wakingoja amri hiyo ifutwe. Walipomwona Mtume ﷺ akitoka nje baada ya kunyoa kichwa chake walimuiga. Baadhi yao hawakunyoa, bali walipunguza nywele zao. Hii ndio sababu Mtume ﷺ alisema:

«رَجِمَ اللَّهُ الْمُحْلِقِينَ»

"Mwenyezi Mungu Awarehemu walionyoa."

Wakasema, "Vipi wale waliopunguza nywele?" Akasema katika mara ya tatu. **"Na wale waliopunguza."**² Kila watu saba walichinja ngamia mmoja kama kafara. Walikuwa maswahaba elfu moja na mia nne, na walipiga kambi katika eneo la *Al-Hudaybiyyah*, nje ya eneo Takatifu (Haram). Pia imeelezwa kuwa walikuwa ndani ya mipaka ya Haram. Allah تعالى ni Mjuzi Zaidi. Kuzuiwa (*Hasru*) kuingia katika nyumba Tukufu (*Kaa'ba*) kunahusisha mambo mengi zaidi na siyo tu kuugua au kumwogopa adui bali pia ni kupotea njia unapoelekea Makkah. Imam Ahmad alieleza kuwa *Al-Hajjaj bin Amr Al-Ansari* kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema:

¹ At - Tabari 4:7.

² Muslim 2:946.

«مَنْ كُسِرَ أَوْ عَرَجَ فَقَدْ حَلَّ وَعَلَيْهِ حَجَّةٌ أُخْرَى»

“Yeyote aliyevunjika mfupa au kiungo, atakuwa ametoka katika Ihram na atatakiwa kuhiji tena.”

Alisema, “Nilitaja Hadithi hii kutoka kwa Ibn Abbas na Abu Hurayrah رضي الله عنهما na wote wakasema, ‘Yeye (Al- Hajjaj) amesema kweli.”¹ Hadithi hii pia ilinukuliwa katika vitabu vinne.² Kwa masimulizi ya Abu Dawud na Ibn Majah, Mtume ﷺ alisema, “Yeyote anayechechemea, aliyevunjika mguu au ambaye ni mgonjwa...”³ Ibn Abu Hatim, pia alinukuu na kusema, “Ilielezwa kuwa Ibn Masud, Ibn Az-Zubayr, An-Nakhai, Ata na Muqatil bin Hayyan walisema, “Kuzuiwa (*Hasr*) kunahusu uadui, ugonjwa au kuvunjika mfupa.”⁴ Ath-Thauri رحمه الله تعالى pia alisema, “Kuzuiwa kunahusu, kila kitu kinachomdhuru mtu.”⁵

Imeelezwa katika Sahihi Mbili kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alikwenda kwa Duba’ah bint Az-Zubayr bin Abdul- Muttalib رضي الله عنها ambaye alisema, “Ewe mjumbe wa Allah! Nakusudia kufanya Hajj lakini ninaumwa.” Alimjibu, “Fanya Hajj na weka sharti useme wakati wa kuhirimia, “Mahali pangu ni pale utakaponizuia.”⁶ Muslim alinukuu vivyo hivyo kutoka kwa Ibn Abbas.⁷ Hivyo kuweka sharti kama hilo katika Hajj kunaruhusiwa kwa mujibu wa Hadith hii. Kauli ya Allah تعالى:

فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ

“Basi (chinjeni) Hady walio wepesi kupatikana.”

Imam Malik amenukuu kutoka kwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه, kwamba alikuwa akisema kuwa: ‘Ni Mbuzi mmoja.’⁸ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, ‘Kuchinja (*Hady*) ni aina nane za wanyama: Ngamia, ng’ombe, mbuzi na kondoo (wa kike na kiume).’⁹ Abdur-Razaq alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ahmad 3:450.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 4:8 na An-Nasai 5:198.

³ Abu Dawud 2:434 na Ibn Majah 2:1028.

⁴ Ibn Abu Hatim 1:444-445.

⁵ Ibn Abu Hatim 1:444-445.

⁶ Fat’hul Al-Bari 9:34.

⁷ Muslim 2:868.

⁸ Al-Muwatta 1:385.

⁹ Ibn Abu Hatim 1:450.

فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ^ط

“Basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana.”

“Kadri mtu atakavyomudu.”¹ Al - Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Iwapo mtu atakuwa tajiri basi achinje ngamia. Vinginevyo ng’ombe au kondoo.”² Hisham bin Urwah alimnukuu baba yake,

فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ^ط

“Basi (chinjeni) wanyama (kondoo, ng’ombe au ngamia) walio wepesi kupatikana.”

‘Kutegemea urahisi na ughali wa bei zake.’³

Ushahidi kuwa kuchinja Mbuzi peke yake kunaruhusiwa iwapo mtu amezuiwa kuendelea na ibada, ni kuwa Allah تعالى Ametaka kuchinjwe chochote kitakachopatikana kama vile Hady. Hady ni aina yoyote ya wanyama ambao ni Ngamia, Ng’ombe, Mbuzi au Kondoo. Haya ni maoni ya Ibn Abbas رضي الله عنهما, mpwa wa Mtume ﷺ na mwanachuoni wa Tafsir. Imeelezwa katika Sahihi Mbili kuwa Aishah رضي الله عنها, mama wa waumini alisema, “Mtume ﷺ siku moja alitoa Mbuzi na Kondoo kwa ajili ya Hady.”⁴ Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَحْلِقُوا رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحَلَّهُ^ع

“Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjioni mwao.”

Haya ni maendelezo ya Kauli Yake.

وَأْتِمُوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ^ع

“Na timizeni Hija na Umra kwa ajili Mwenyezi Mungu.”

Na haitegemei kwayo:

¹ Ibn Abu Hatim 1:451.

² At-Tabari 4:30.

³ Ibn Abu Hatim 1:452.

⁴ Fat’hul Al-Bari 3:639 na Muslim 2:958.

فَإِنْ أَحْصَرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۗ

“Na mkizuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana.”

Kama Ibn Jarir رحمه الله تعالى alivyodai kwa makosa. Kwani Mtume ﷺ na Masahaba wake walipozuiwa kuingia Nyumba Tukufu wakati wa Hidaybiyyah na washirikina wa Kikuraish, walinyoa vichwa vyao na kuchinja Hady nje ya Haram. Ama katika hali ya kawaida, na endapo mtu atawasili kwa amani Haram, hataruhusiwa kunyoa nywele zake mpaka:

حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحَلَّهُ ۗ

“Mpaka wanyama hao wafike machinjioni mwao.” Alhaj atamaliza matendo yote ya ibada za Hija na Umra kama alinuia Qirani au matendo ya kimojawapo kama anahitaji kwa nia ya Ifraad au Tamatui, Ilinukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Hafsah رضي الله عنها alisema, “Ewe mjumbe wa Allah! Mbona watu wote tayari wametahalali (kutoka katika Ihram na Umra) lakini wewe bado?” Mtume ﷺ alisema:

«إِنِّي لَبَدْتُ رَأْسِي وَقَلَدْتُ مَذْيِي، فَلَا أَجِلُّ حَتَّىٰ أَنْحَرَ»

“Mimi niligandamiza nywele zangu na nimemvalisha shada la alama mnyama wangu wa kuchinja, hivyo sitotoka kwenye Ihram mpaka nichinje.”¹

Yeyote Atakayenyoa Kichwa Chake Akiwa Katika Nia ya Hijja Atatoa Fidyah

Allah تعالى Amesema,

فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ بِهِ أَذًى مِنْ رَأْسِهِ فَفِدْيَةٌ مِنْ صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسْكَ

“Na atakayekuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidiya kwa kufunga au kwa kutoa sadaka.”

Bukhari alieleza kuwa Abdur-Rahman bin Asbahani alisema kuwa alimsikia Abdullah bin Maqil akisema kuwa alikaa na Ka’ab bin Ujrah رضي الله عنه ndani ya msikiti huu (yaani wa Kufa) nikamuuliza kuhusu Fidyah ya kufunga. Ka’b alijibu, “Hii iliteremshwa maalum kwa ajili yangu, lakini pia inakuhusuni ninyi nyote. Nilipelekwa kwa Mtume ﷺ huku nikiwa na chawa wengi waliokuwa wameenea mpaka juu ya uso wangu. Mtume ﷺ alisema:

¹ Fat’hul Al-Bari 3:493 na Muslim 2:902.

«مَا كُنْتُ أَرَى أَنْ الْجَهْدَ بَلَغَ بِكَ هَذَا، أَمَا تَجِدُ سَاءَةً؟ قُلْتُ: لَا

“Sikufikiria kuwa unapata taabu hiyo na kuwa umefikia hali ninayoiona sasa. Je, unaweza kumudu Mbuzi wa Fidiyah?” Nikajibu, ‘Hapana.’

Kisha akasema:

«صُمِّمَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ أَوْ أَطْعِمَ سِتَّةَ مَسَاكِينَ، لِكُلِّ مِسْكِينٍ نِصْفُ صَاعٍ مِنْ طَعَامٍ،
وَإِخْلِقْ رَأْسَكَ»

“Funga siku tatu au walishe masikini sita, kila mmoja nusu Pishi ya chakula (Pishi 1= kilo 3) na nyoa kichwa chako.”

Hivyo, hii ni hukumu ya jumla iliyotokana na suala mahsusi.¹ Imam Ahmad alinukuu kuwa Ka’ab bin Ujrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alitupitia wakati nikiwasha moto chini ya chungu huku chawa wakianguka usoni mwangu kwenye kope zangu, akasema:

«يُؤْذِيكَ هَوَائِمُ رَأْسِكَ؟ قُلْتُ: نَعَمْ

“Je hawa chawa walio kichwani mwako wanakughasi?”

Nikajibu, ‘Ndiyo.’ Akasema,

«فَاخْلِقْهُ، وَصُمِّمَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ، أَوْ أَطْعِمَ سِتَّةَ مَسَاكِينَ، أَوْ ائْسُكْ نَسِيكَةً»

“Nyoa, kisha funga kwa siku tatu, au walishe masikini sita au chinja mnyama.”

Ayyub (mmoja wa wasimulizi wa hadithi) alitoa maelezo; “Sijui katika hayo ipi iliyotajwa mwanzo.² Kwa kuwa hapa Qur’an inazungumzia ruhusa ndio maana maneno yake yameanza na lile lililo jepesi, kisha gumu zaidi: “Toa Fidyah ya kufunga (siku tatu), kuwalisha (Masikini sita) au kuchinja (mnyama).” Wakati huo Mtume ﷺ alimshauri Ka’ab رضي الله عنه kwanza, achinje Mbuzi, au alishe masikini sita, au afunge kwa siku tatu. Kila andiko linafaa kwa ubora wake na muktadha wake, shukrani zote zinamstahiki Allah تعالى.

¹ Fat’hul Al-Bari 8:34.

² Ahmad 4:241.

Ubainifu wa Hijja ya Tamattui

Allah تعالى Alisema:

فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ

“Na mtakapokuwa salama basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi.”

Kama mnaweza kukamilisha vitendo vya *Hajj*. Hivyo yeyote kati yenu atayeunganisha *Umra* na *Hajj ya Tamattui* kwa nia ya *Ihram* moja. Na hii inajumuisha Mtu aliyetia nia ya *Umra* na *Tamattui* kwa pamoja. Au alitia nia ya kufanya *Umra* kwanza, alipomaliza *Umra* ndio akatia nia ya *Hijja*. Na hii ndio aina ya *Hijja* iitwayo *Tamattui* mahususi ambayo ni maarufu miongoni mwa kauli mbalimbali za wanazuoni, ambapo kwa ujumla kuna aina mbili za *Tamattui* kama inavyohibitishwa na Hadithi zilizo sahihi, kwa kuwa miongoni mwa wasimulizi kuna wale waliosema, “Mtume ﷺ alifanya *Tamattui*, na wengine waliita “*Qiran*” lakini kauli hizo hazitofautiani juu ya kuwa Mtume alikwenda na mnyama wa (*Hady*).”

فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ

“Na mtakapokuwa salama basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi.”

Maana yake: Achinje mnyama wa *Hady* yoyote atakayempata wa chini kabisa ni Mbuzi. Mtu anaruhusiwa kuchinja ng’ombe kwa sababu Mtume ﷺ alichinja ng’ombe kwa niaba ya wakeze. Al- Awzai رحمه الله تعالى alieleza kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alichinja ng’ombe kwa niaba ya wakeze wakati walipofanya *Tamattui*.¹ Hili lilielezwa na Abubakar bin Marduwah. Hadithi hii ya mwisho inathibitisha kuwa *Tamattui* imo ndani ya sheria. Imeelezwa ndani ya Sahih Mbili kuwa Imran bin Husayn alisema, ‘Tulitekeleza *Hajj ya At - Tamattui* wakati wa uhai wa Mtume ﷺ na kisha *Qur’an* iliteremshwa (kuhusu *Hajj At - Tamattui*) wala haikuharamisha au kukataza.” Kwa mujibu wa

¹ Abu Dawud 2:362.

maoni yake.¹ Imamu Bukhari alisema kuwa Imran alikuwa akimzungumzia Umar رضي الله عنه. Ilielezwa katika Hadith sahihi kuwa Umar رضي الله عنه alikuwa akiwavunja watu nguvu wasifanye *Tamattui*. Alikuwa akisema, "Iwapo tutafanya rejea katika Kitabu cha Allah تعالى, lazima tukamilishe." Maana yake:

فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ

"Basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio ahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi."

Pamoja na hayo. Umar رضي الله عنه hakusema kuwa *Tamattu* ni haramu. Aliwazua watu ili waongeze safari za kwenda Al-Kaaba kwa ajili ya *Hajj* (wakati wa miezi ya *Hajj*) na *Umrah* (mwaka mzima) kama alivyoeleza yeye mwenyewe.

Yeyote Anayefanya *Tamattui* Lazima Afunge Siku Kumi Ikiwa Hana Mnyama wa Kuchinja (*Hady*)

Allah تعالى Amesema:

فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ تِلْكَ عَشْرَةٌ كَامِلَةٌ

"Na asiyepata afunge siku tatu katika hija na siku saba mtakaporudi, hizi ni kumi kamili."

Aya hii ina maana: "Wale wasio na uwezo wa Kuchinja Mnyama (*Hady*), wafunge siku tatu wakati wa msimu wa *Hajj*." Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Iwapo mmoja hatokuwa na Mnyama wa kuchinja (*Hady*), lazima afunge siku tatu wakati wa *Hajj*, kabla ya siku ya *Arafah*. Iwapo siku ya *Arafah* itakuwa ni siku ya tatu basi funga yake imekamiliika. Na lazima afunge siku saba atakapofika nyumbani."² Abu Is-haq رحمه الله تعالى alieleza kutoka kwa Wabrah kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما ambaye alisema, "Mtu hufunga siku moja kabla ya siku ya *Tarwiyah* (siku ya nane ya *Dhul Hijjah*) na siku ya *Tarwiyah* yenyewe na kisha siku ya *Arafah* (siku ya tisa ya *Dhul- Hijjah*)."³ Kauli hiyo ilielezwa na Ja'far bin Muhammad رحمه الله تعالى kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ali رضي الله عنه.⁴

¹ Fat'hul Al-Bari 8:34 na Muslim 2:900.

² At-Tabari 4:97.

³ At-Tabari 4:95.

⁴ At-Tabari 4:94.

Endapo mmoja hakuweza kufunga siku hizi tatu au baadhi yake kabla ya siku ya Idd (Siku ya kumi ya *Dhul-Hijjah*), anaruhusiwa kufunga wakati wa siku za *Tashriq* (siku ya ya 11-12-13 katika mwezi wa *Dhul Hijjah*). Aishah رضي الله عنها na Ibn Umar رضي الله عنهما walisema kutoka katika sahihi Bukhari, "Kufunga siku ya *Tashriq* kuliruhusiwa tu kwa wale ambao hawakumudu kuchinja mnyama (*Hady*).” Kama alivyoeleza Bukhari, Sufyan alisimulia kuwa Ja'far bin Muhammad alisimulia kuwa baba yake alisema kuwa Ali رضي الله عنه alikuwa akisema, "Yeyote ambaye hakufunga siku tatu wakati wa Hajj, lazima azifunge wakati wa siku za *Tashriq*." Huu pia ni msimamo uliochukuliwa na Ubayd bin Umayr Al - Laythi, Ikrimah, Al-Hasan Al-Basri na Urwah bin Az-Zubayr,¹ ikirejea maana ya jumla ya Kauli ya Allah تعالى:

فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ

"Afunge siku tatu katika Hijja."

Ama kwa kile alichoeleza Muslim kuwa Qutaybah A-Hudhali رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَيَّامُ التَّشْرِيقِ أَيَّامُ أَكْلِ وَشُرْبٍ، وَذِكْرِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

*"Siku za Tashriq ni siku za kula na kunywa na kumdhukuru Allah Aliyetukuka."*²

Hadithi hii ina maana ya jumla ambapo ile ya Aisha رضي الله عنها na Ibn Umar رضي الله عنهما ni mahsusi. Allah تعالى Amesema:

وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ³

"Na siku saba mtakaporudi."

Kuna rai mbili kuhusiana na maana ya Aya hii. Mosi, ina maana: "Mtakaporudi kwenye eneo la kambi." Ya pili, 'mtakaporudi nyumbani." Abdur-Razzaq alieleza kuwa Salim alisimulia kuwa alimsikia Ibn Umar رضي الله عنهما akisema:

فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ⁴

"Na asiyepata, afunge siku tatu katika Hijja na siku saba mtaporudi."

¹ At-Tabari 4:98-99.

² Muslim 2:800.

Maana yake: “Atakaporejea kwa familia yake.”¹ Rai hiyo ilielezwa pia kutoka kwa Said bin Jubayr, Abu Al-Aliyah, Mujahid, ‘Ata, Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, Imam Az- Zuhri na Ar- Rabi bin Anas.²

Bukhari alieleza kuwa Salim bin Abdullah alisimulia kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, “Wakati wa *Hajj* ya kuaga ya Mtume ﷺ alifanya *Tamattu* kwa kunuiya *Umrah* na *Hajj*. Aliwaswaga wanyama wake wa *Hady* kutoka *Dhul Hulayfa*. Mtume ﷺ alianza kutia nia kwa ajili ya *Umrah* na kisha *Hajj*. Na watu, pia walifanya *Umrah* na *Hajj* pamoja na Mtume ﷺ. Baadhi yao walileta wanyama wa kuchinja (*Hady*) pamoja nao, ambapo wengine hawakufanya hivyo. Hivyo, Mtume ﷺ alipowasili Makkah, aliwaambia watu:

«مَنْ كَانَ مِنْكُمْ أَهْدَىٰ فَإِنَّهُ لَا يَجِلُّ مِنْ شَيْءٍ حَرَّمَ مِنْهُ حَتَّىٰ يَقْضِيَ حَجَّهُ، وَمَنْ لَمْ
يَكُنْ مِنْكُمْ أَهْدَىٰ فَلْيَطْفُفْ بِالْبَيْتِ وَبِالصَّفَا وَالْمَرْوَةِ وَلْيَقْصِرْ وَلْيَحْلِلْ، ثُمَّ لِيَهْلِ
بِالْحَجِّ، فَمَنْ لَمْ يَجِدْ هَدْيًا فَلْيُضْمِ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ، وَسَبْعَةَ إِذَا رَجَعَ إِلَىٰ
أَهْلِيهِ.»

“Yeyote miongoni mwenu aliyekuja na mnyama wa kuchinja (*Hady*), asitoke katika *Ihram* mpaka akamilishe *Hajj* yake. Na miongoni mwenu ambaye hakuja na mnyama wa kuchinja (*Hady*) afanye *Tawaf* katika *Ka’bah* na kati ya *As-Safa* na *Al-Marwah*. Kisha anyoe au apunguze nywele, kisha avue nguo za *Ihram*, na kisha ahirimie *Hajj* (lakini achinje *Hady*). Na kama hakumudu mnyama wa kuchinja (*Hady*), atalazimika kufunga siku tatu wakati wa *Hajj* na siku saba atakaporudi nyumbani.”

Kisha akataja hadithi iliyobakia, ambayo imeelezwa katika Sahihi Mbili Allah تعالى Amesema:³

تِلْكَ عَشْرَةٌ كَامِلَةٌ

“Hizo ni siku kumi kamili.”

Ni kwa ajili ya kutilia mkazo amri iliyotajwa hapo juu. Njia hii ni ya kawaida katika lugha ya Kiarabu, kwani wangesema, “Nimeona kwa macho yangu, nimesikia kwa masikio yangu na nimeandika kwa mkono wangu ili kutilia mkazo maelezo.” Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema:

¹ Adur-Razaq 1:76.

² Ibn Abu Hatim 2:498.

³ Fat’hul - Bari 3:630, Muslim 2:91.

وَلَا تَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ

“Wala ndege arukaye kwa mbawa zake mbili.” (6:38)

وَلَا تَخْطُرُ بِمِمينَاكَ

“Wala hukukiandika kwa mkono wako wa kulia.”(29:48) Na

* وَوَأَعَدْنَا مُوسَىٰ ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتَمَمْتَهَا بِعَشْرٍ فَتَمَّ مِيقَاتُ رَبِّهِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً

“Tulimuahidi Musa siku thelathini na Tukatimiza kumi, ikatimia miadi ya Mola wake Mlezi siku arubaini.” (7:142)

Imesemwa pia, maana ya: “Siku kumi kwa jumla inatilia mkazo amri ya kufunga siku kumi na si pungufu ya hiyo.”

Wakazi wa Makka hawaruhusiwi kufanya Tamattui:

Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ لِمَنْ لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُ حَاضِرِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

“Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu.”

Aya hii inawahusu wakazi wa eneo la Haram, kwani wao hawafanyi *Tamattui*. Abdur-Razzaq alieleza kuwa Tawus alisema, “*Tamattui* ni kwa watu ambao familia zao haziishi katika eneo la Haram (Makkah) Kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ لِمَنْ لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُ حَاضِرِي الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

“Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu.”

Kisha Abdur-Razaq akasema, “Imenifikia kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنهما yenye kufanana na kauli ya Tawus.”¹ Allah تعالى Amesema:

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu.” Maana yake: Katika yale Aliyowaamrisheni na yale Aliyowakatazeni. Kisha Akasema:

¹ At-Tabari 4:111

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَةٌ ۖ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ
 وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ ۗ وَمَا تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ
 يَعْلَمُهُ اللَّهُ ۗ وَتَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ وَاتَّقُوا
 يَتَأُولَى الْأَلْبَابِ ﴿١٩٧﴾ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا
 فَضْلًا مِنْ رَبِّكُمْ ۗ فَإِذَا أَفَضْتُمْ مِنْ عَرَفَاتٍ فَاذْكُرُوا
 اللَّهَ عِنْدَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ ۗ وَاذْكُرُوهُ كَمَا هَدَيْتُمْ وَإِنْ
 كُنْتُمْ مِنْ قَبْلِهِ لَمَنِ الضَّالِّينَ ﴿١٩٨﴾ ثُمَّ أَفِيضُوا مِنْ
 حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ
 رَحِيمٌ ﴿١٩٩﴾ فَإِذَا قَضَيْتُمْ مِنْسِكَكُمْ فَادْكُرُوا اللَّهَ
 كَذِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا ۗ فَمِنَ النَّاسِ مَنْ
 يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ
 ﴿٢٠٠﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي
 الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾ أُولَئِكَ لَهُمْ
 نَصِيبٌ مِمَّا كَسَبُوا ۗ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٢﴾

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَةٌ ۖ فَمَنْ فَرَضَ
 فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا
 فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ ۗ وَمَا
 تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمُهُ اللَّهُ ۗ وَتَزَوَّدُوا
 فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ وَاتَّقُوا
 يَتَأُولَى الْأَلْبَابِ ﴿١٩٧﴾

197. "Hija ni miezi maalum. Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu Anaijua. Na jitengenezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili."

Wakati wa Kuhirimia Hija

Allah تعالى Amesema;

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَةٌ ۖ

"Hija ni miezi maalum."

Aya hii inaashiria kuwa kunaia kwa ajili ya lbada ya Hija huanza wakati wa miezi ya Hija. Hili lilipokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما¹, Jabir, Ata,

¹ At-Tabari 4:115.

Tawus na Mujahid. Ushahidi wa hili ni kauli ya Allah تعالی kuwa *Haji* hairuhusiwi kabla ya muda huo kama vile nyakati za Sala. Ash-Shafi رحمه الله تعالی alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Hapana mtu anayeruhusiwa kuhirimia kwa ajili ya *Hija* kabla ya miezi ya *Hija*, kwani Allah تعالی Amesema,

أَحَجُّ أَشْهُرَ مَعْلُومَاتٍ

"Hija ni (katika) miezi maalum."¹

Ibn Khuzaymah alieleza katika sahihi yake kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Hapana kuhirimia kwa ajili ya *Hija* isipokuwa katika miezi ya *Hija*.² Kwani miongoni mwa Sunnah za *Hija* ni kuhirimia katika miezi ya Hajj." Haya ni masimulizi sahihi na kauli ya Maswahaba wanaposema kuwa jambo kadha wa kadha ni miongoni mwa Sunnah: Inachukuliwa kuwa ni Hadithi ya Mtume ﷺ, kwa mujibu wa wanazuoni walio wengi. Hii ni mahsusi kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, aliyetoa kauli hii, kwani yeye ni Mtarjumi (Mfasiri, Mfafanuzi, Mwelezaji) wa Qur'an. Kuna Hadith nyingine kuhusu somo hili. Ibn Mardawyah alisimulia kuwa Jabiri رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَتَّبِعِي لِأَحَدٍ أَنْ يُحْرِمَ بِالنَّحْيِ إِلَّا نَبِيَّ أَشْهُرِ النَّحْيِ»

*"Hapana anayeruhusiwa kuhirimia kwa ajili ya Hija, isipokuwa katika miezi ya Hija."*³

Isnad ya wapokezi wa Hadithi hii ni ya kuaminika. Imamu Shafii رحمه الله تعالی na Al-Bayhaqi رحمه الله تعالی waliinukuu Hadithi hii kutoka kwa Ibn Jurayj walisimulia kuwa Abu Az-Zubayr alisema kuwa alimsikia Jabir bin Abdullah akiulizwa, "Je mtu anaweza kuhirimia *Hajj* kabla ya miezi ya *Hajj*?" Alijibu, "Hapana."⁴ Masimulizi haya ni ya kutegemewa zaidi kuliko yale tuliyoyataja kutoka kwa Mtume ﷺ. Kwa ufupi, kauli hii ni maoni ya Sahaba, iliyongwa mkono na kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنهما, kuwa ni sehemu ya Sunnah kutohirimia *Hija* kabla ya miezi ya *Hija*. Allah تعالی ni Mjuzi zaidi.

¹ Al-Umm 2:132

² Ibn Khuzaymah 4:162

³ Al-Musannaf Ibn Abu Shaybah (361)

⁴ Al-Umm 2:132 na Al-Bayhaqi 4:343.

Miezi ya Hajj:

Allah تعالى Amesema:

أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ

“Ni miezi maalum.”

Imamu Bukhari alisema kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa miezi hii ni *Shawwal, Dhul-Qadah* na siku kumi za mwanzo za *Dhul-Hijjah*.¹ Masimulizi haya ambayo Bukhari hakutaja *Isnaad* ya mapokezi, yalikusanywa moja kwa moja na *Isnaad* ya wapokezi ambao Ibn Jariri رحمه الله تعالى amewataja kuwa sahihi. Maarufu kwa Ibn Umar رضي الله عنهما, ambaye alisema:

أَحْسَبُ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ

“Hija ni miezi maalum.”

“Ambayo ni *Shawwal, Dhul-Qa-dah* na siku kumi za mwanzo za *Dhul-Hijjah*.”² *Isnaad* yake ni Sahih. Pia Al-Hakim aliinukuu katika Mustadrak wake, na alisema, “Inatimiza vigezo vya Bukhari na Muslim.”³

Mimi bin Kathir - nasema Kauli hii imeelezwa pia kutoka kwa Umar, Ali, Ibn Mas'ud, Abdullah bin Az-Zubayr, Ibn Abbas, Ata, Tawus, Mujahid, Ibrahim An-Nakhai, Imam Ash-Shabi, Al-Hasan, Ibn Sirin, Mak'hul, Qatadah, Adh-Dhahhak bin Muzahim, Ar-Rabi bin Anas na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم.⁴ Rai ilikubaliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى ambaye alisema, “Ni jambo la kawaida kuita miezi miwili na sehemu ya mwezi mmoja kwa jina la wingi - “Miezi”. Ni sawa na usemi wa kiarabu, “Mwaka huu au siku ya leo nilimtembelea mtu fulani.” Ilhali alimtembelea kwa kipindi cha sehemu tu ya mwaka au ya siku. Allah تعالى Amesema,

فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ

“Mwenye kufanya haraka ya kuondoka kwa siku mbili, hapana madhambi juu yake.” (2:203)

Na hakika si vingine kuharakisha huko ni muda wa siku moja na sehemu ya siku ya pili.⁵ Allah تعالى Amesema,

¹ Fat'hul Al-Bari 3:490.² At-Tabari 4:116.³ Al-Hakim 2:276.⁴ Ibn Abu Hatim 2:486.⁵ At-Tabari 4:120.

فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ

“Na anayekusudia (faradha) kufanya Hija (Kwa kukusudia Ihram).”

Inamaanisha kwamba mtu anayekusudia kufanya *Ihram* anahitajika afanye *Hajj* kwa kuwa inahitajika mtu akamilishe ibada za *Hajj* baada ya kukusudia kufanya *Ihram*. Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesema kuwa Al- Awfi alisema, “Wanazuoni wana kubaliana kuwa (*faradha*) “kukusudia” iliyotajwa katika Ayah ina maana, ni uwajibu na ulazima kulifanya jambo hilo.¹ Ali bin Abu Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ

“Na anayekusudia kufanya Hija”

Inahusu: “Wale wanaohirimia kwa *Hajj* na *Umrah*.” Ataa alisema, “Faradhi, ina maana, “Kuhirimia.”” Kauli sawa na hizo zilitoka kwa Ibrahim, Adh-Dhahhak na wengineo.²

Kuharamishwa kwa Tendo la Ndoa kwa Aliyehirimia Hajj:

Allah تعالى Amesema:

فَلَا رَفَثَ

“Basi asiseme maneno machafu.”

Aya hii ina maana kuwa wale wanaohirimia kwa ajili ya *Hajj* au *Umrah* wanatakiwa wajiepushe na *Rafath*, yaani, kuingiliana kimwili. Kauli ya Allah تعالى Hapa ni sawa na Kauli Yake.

أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَائِكُمْ

“Mmehalalishwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu.” (2:187)

Chochote kitakachopelekea kuingiliana kimwili, kama vile kukumbatia, kubusu na kuzungumza na wanawake kuhusu mambo ya ngono, ni haramu. Ibn Jariri رضي الله عنهما alisema kuwa Nafi alisimulia kuwa Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “*Rafath* maana yake kuingiliana kimwili au kutaja kitendo hicho kwa ulimi, hili ni kwa wote wanaume au wanawake.”³ Ata bin Abu Rabah alisema

¹ At-Tabari 4:121.

² At-Tabari 4:123.

³ At-Tabari 4:126.

kuwa *Rafath* ina maana kuingiliana kimwili au lugha chafu.¹ Hii ni rai ya Amr Bin Dinar. Pia Ata alisema kuwa walikuwa wakijizuia kuzungumzia suala Hili.² Tawus alisema kuwa *Rafath* ni pamoja na mtu kusema, “Nikitoka ndani ya *Ihram* nitakuingilia.”³ Haya Ni sawa na maelezo yaliyotolewa na Abu Al-Aliyah kuhusu *Rafath*. Ali bin Abu Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Rafath* ina maana kumwingilia mke, kumbusu, kumkumbatia na kumwambia maneno ya kimapenzi, na vitendo vya mfano huo.”⁴ Ibn Abbas na Ibn Umar رضي الله عنهما walisema kuwa *Rafath* ina maana kufanya kitendo cha ndoa na wanawake.⁵ Hii pia ni rai ya Said bin Jubayr, Ikrimah, Ibrahim, Mujahid, Arr-Rabi, Ata Al-Khurasani, Ata bin Yasar, Atiyah, Az- Zuhri, As-Suddi, Malik bin Anas, Muqatil bin Hayyan, Abdul- Karim bin Malik, Al- Hassan, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengineo.

Kuharamishwa kwa Ufuska Wakati wa Hija

Allah تعالى Amesema:

وَلَا فُسُوقَ

“Wala asifanye vitendo vichafu.”

Miqsam na wanazuoni wengine wanasimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ni utovu wa adabu au maasi.” Hii pia ni rai ya Ata, Mujahid, Tawus, Ikrimah, Said bin Jubarr, Muhammad bin Ka’b, Al-Hassan, Qatadah, Ibrahim An-Nakhai, Az- Zuhur, Ar-Rabi bin Anas, Ata bin Yasar, Ata Al - Khurasan na Muqatil bin Hayyan.⁶

Ibn Wahb alieleza kutoka kwa Yunus kuwa Naafi alisimulia kuwa Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “*Fusuq* (kosa lililotajwa katika Aya (2:197) inahusu kufanya lile Allah تعالى Aliloliharamisha katika sehemu Takatifu.”⁷

Wengine wengi walisema kuwa *Fusuq* ina maana kuwatusi wengine: walitegemea hili kwa mujibu wa maelezo ya Hadithi sahihi,

¹ At-Tabari 4:127.

² At-Tabari 4:128.

³ At-Tabari 4:128.

⁴ At-Tabari 4:129.

⁵ At-Tabari 4:129.

⁶ Ibn Abu Hatim 2:497-500.

⁷ Ibn Abu Hatim 2:497.

«سَبَابُ الْمُسْلِمِ فُسُوقٌ وَقِتَالُهُ كُفْرٌ»

“Kumtusi Muislamu ni Ufuska ambapo kupigana naye ni Ukafiri.”¹

Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema *Fusuq* hapa maana yake kumchinja mnyama kwa ajili ya masanamu, kama Allah تعالى Alivyosema:

أَوْ فَسَقًا أَهْلٌ لِعَيْرِ اللَّهِ بِهِ

“Au kwa upotofu kimechinjwa kwa jina la asiye kuwa Mwenyezi Mungu.” (6:145)

Adh- Dhahhak alisema kuwa *Fusuq* ni kumtukana kwa lakabu mbaya (Kumpa mtu jina baya ambalo si lake). Wale wote waliosema kuwa *Fusuq* ina maana ya kila aina ya utovu wa adabu wako sahihi. Pia Allah تعالى Amekataza kudhulumu wakati wa miezi ya *Hija* hasa, japokuwa udhalimu umezuiwa mwaka mzima. Hii ndiyo sababu Allah تعالى Amesema:

مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرْمٌ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ

“Katika hiyo iko miezi minne mitakatifu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa. Basi msidhulumu nafsi zenu humo.” (9:36)

Allah تعالى Amezungumzia maeneo matakatifu:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِالْحَادِ بِظُلْمٍ نُدِقَهُ مِنْ عَذَابِ الْيَمْرِ

“Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhulma, basi Tutamwonjesha humo adhabu chungu.” (22:25)

Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ حَجَّ هَذَا الْبَيْتَ، فَلَمْ يَرُفْ وَلَمْ يَنْسُقْ خَرَجَ مِنْ ذُنُوبِهِ كَيَوْمِ وَلَدَتْهُ أُمُّهُ»

“Mwenye kuhiji Nyumba hii Takatifu na wala hakusema maneno machafu au kufanya ufuska, atarejea hana dhambi, kama siku aliyozaliwa na mama yake.”²

¹ Fat’hul Al-Bari 1:135.

² Fat’hul Al-Bari 4:25 na Muslim 2:983.

Uharamu wa Kubishana Wakati wa Hija

Allah تعالیٰ Amesema:

وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ^١

“Wala asibishane katika Hija.”

Maana yake: Malumbano na mabishano. Ibn jarir رحمه الله تعالیٰ alisimulia kuwa Abdullah bin Mas’ud عنه رضي الله عنه alisema yale yaliyosemwa na Allah تعالیٰ.

وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ^٢

“Wala asibishane katika Hija.”

Ina maana ya kubishana na mwenzako mpaka ukamkasirisha. Hii ni sawa na rai ya Miqsam na Adh-Dhahhak waliyoinasibisha na Ibn Abbas رضي الله عنهما.¹ Hii pia ina maana sawa iliyoenezwa kutoka kwa Abu Al-Aliyah, Ata, Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Jaabir bin Zayd, Ata Al-Khurasani, Mak’hul, As- Suddi, Muqatil bin Hayyan, Amr bin Dinar, Adh- Dhahhak, Ar - Rabi, Anas, Ibrahim An - Nakhai, Ata bin Yassar, Al-Hassan, Qatadah na Az- Zuhri رضي الله عنهم.²

Kushajiisha Katika Kutenda Kheri na Kuandaa Zawadi ya Hija:

Allah تعالیٰ Amesema:

وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمُهُ اللَّهُ^١

“Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu Anajua.”

Baada ya Allah تعالیٰ Kuharamisha maovu kwa maneno na vitendo, Alishajiisha uadilifu, amali njema, Akieleza kuwa Anayajua mazuri wayafanyayo, na Atawalipa kwa malipo mazuri siku ya Kiyama. Kisha Allah تعالیٰ Amesema:

وَتَرَوُوهَا فَايُّ خَيْرٍ أَلَزَادِ التَّقْوَىٰ^٢

“Na jitengenezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu.”

Imamu Bukhari na Abu Dawud walieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Watu wa Yemen walikuwa wakienda Hija bila kuchukua chakula cha kutosha. Wakawa wanasema, “Sisi ni wale wenye kumtegemea Allah تعالیٰ.” Allah تعالیٰ Aliteremsha Aya hii.

¹ At-Tabari 4:141.

² Ibn Abu Hatim 2:503-505.

وَتَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ

“Na jitengenezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى walisimulia kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, “Watu walipoingia katika *Ihram*, walivitupa vyakula walivyokuwa navyo na kununua vyakula vya aina nyingine.” Allah تعالى Aliteremsha:

وَتَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ

“Na jitengenezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu.”

Allah تعالى Aliwakataza mwenendo huo na wakatakiwa kuchukua unga na *Sawiq* (aina ya chakula ambacho kwa kawaida kikiliwa pamoja na tende) na mikate.²

Zawadi ya Safari ya Kwenda Nayo Akhera

Allah تعالى Amesema:

فَأِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ

“Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu.”

Allah تعالى Alipowataka binadamu kuchukua mahitaji yatakayowasaidia katika safari za hapa duniani, amewaeleza zawadi muhimu ya Akhera nayo ni: *Taqwa*. (uchamungu) Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَرِيْدًا ۗ وَلِبَاسٍ ۗ التَّقْوَىٰ ۗ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۗ

“Na nguo za pambo. Na nguo za Uchamungu ndio bora.” (7:26)

Allah تعالى Alipotaja mavazi ya kawaida Aliwazindua watu wajipambe na vazi la kiimani, ambalo ni unyenyekevu, utiifu na kumchamungu. Na Akataja yakuwa vazi hili ni bora zaidi na lenye manufaa.

وَأَتَّقُونَ يَتَأْوَلِي الْأَلْبَابَ ﴿٢٧﴾

“Na nicheni Mimi, enyi wenye akili.”

¹ Fat’hul Al-Bari 3:449 na Abu Dawud 2:349.

² At-Tabari 4:156.

Maana yake: "Ogopeni Mateso Yangu, Adhabu, na Maangamizi kwa wale wanaonikengeuka Mimi na hawafuati Amri Zangu, enyi watu wenye kutafakari na kuelewa."

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ^٤ فَإِذَا أَقَضْتُم مِّنْ عَرَفْتُمْ
فَأَذْكُرُوا اللَّهَ عِندَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ^٥ وَأَذْكُرُوهُ كَمَا هَدَيْتُمْ وَإِنْ كُنْتُمْ مِّنْ قَبْلِهِ

لَمِنَ الضَّالِّينَ ﴿١٩٨﴾

198. "Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi. Na mtakapomiminika kutoka A'rafat mtajeni Mwenyezi Mungu penye Masha'ril Haram. Na mkumbukeni kama Alivyokuongoeni, ijapo kuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea."

Kufanya biashara wakati wa Hija:

Imamu Bukhari alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Ukaz, Mijannah na Dhul Majaz vilikuwa vituo vya biashara enzi za Jahiliyah. Wakati wa zama hizo, hawakupenda fikra za kufanya biashara wakati wa msimu wa Hija. Baadaye Aya hii iliteremshwa.

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ^٤

"Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi (wakati wa msimu wa Hija)."¹

Abu Dawud na wengine walinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Walikuwa wakijizuia kufanya biashara wakati wa msimu wa Hajj. Wakisema kuwa hizo ni siku za Dhikr. Allah تعالى Aliteremsha

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ^٤

"Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi."²

Haya ni maelezo ya Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Mansur bin Al-Mu'tamir, Qatadah, Ibrahim An-Nakhai, Ar-Rabi bin Anas na wengine رضي الله عنهم. Ibn Jarir

¹ Fat'hul Al-Bari 8:34.

² Abu Dawud 2:350.

رضي الله عنهما alieleza kuwa Abu Umaymah alisema Ibn Umar رضي الله عنهما alipoulizwa kuhusu mtu kufanya biashara wakati wa *Hija*, alisoma Aya hii:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ

“Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi.”¹

Hadithi hii imepokewa kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما na *Isnad* madhubuti ya wapokezi. Hadithi hii pia inatokana na Mtume ﷺ, kama Ahmad alivyoeleza kuwa Abu Umamah At -Taymi alisema, “Nilimuuliza Ibn Umar رضي الله عنهما, “Tunanunua (na kuuza wakati wa *Hija*) kwa ajili hiyo Hajj yetu inasihiki?” Akajibu, “Je hamfanyi *Tawaf* kuzunguka nyumba ya Allah تعالى, kusimama *Arafat*, kutupa vijawe na kunyoka vichwa vyenu?” Nikajibu, “Tunafanya hivyo”. Ibn Umar رضي الله عنهما akasema, “Alikuja mtu kwa Mtume ﷺ na akamwuliza kama ulivyoniuliza, na Mtume ﷺ hakujibu mpaka Jibril عليه السلام aliposhuka na Ayah hii:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ

“Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi.”

Mtume ﷺ alimwita yule mtu na kumwambia. “*Nyie ni mahujaji.*”² Ibn Jariri رضي الله عنه alisimulia kuwa Abu Salih alimuuliza Sayyidina Umar رضي الله عنه, “Ewe Amiri wa waumini! Mlifanya biashara wakati wa *Hija*?” Alimjibu, “Haikuwepo njia nzuri ya maisha kama wakati wa msimu wa *Hija*...”³

Kusimama Arafat:

Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا أَفَضْتُمْ مِنْ مَّوْجِ عَرَفَاتٍ فَادْكُرُوا اللَّهَ عِنْدَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ

“Na mtakapomiminika kutoka Arafat mtajeni Mwenyezi Mungu (hapa) Masha’ril Haram.”

Arafat ni mahali ambapo mtu anasimama wakati wa *Hija* na ni nguzo za *Ibadat* za *Hija*. Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan* walinukuu kuwa Abdur-Rahman bin Ya’mar Ad- Diyli رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema:

¹ At-Tabari 4:165.

² Ahmad 2:155.

³ At-Tabari 4:168.

«الْحَجَّ عَرَفَاتٍ - ثَلَاثًا - فَمَنْ أَدْرَكَ عَرَفَةَ قَبْلَ أَنْ يَطْلُعَ الْفَجْرُ فَقَدْ أَدْرَكَ، وَأَيَّامٌ
وَيَوْمِ ثَلَاثَةٍ، فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِيَّامَ عَلَيْهِ، وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِيَّامَ عَلَيْهِ»

*"Hija ni Arafat" (alisema hivyo) mara tatu. Atakayediriki kufika Arafat kabla ya Alfajir atakuwa amediriki. Siku za kukaa Mina ni tatu, na si makosa kwa wale watakaondoka baada ya siku mbili na si makosa kwa wale watakaobaki."*¹

Muda wa kusimama Arafat unianza mchana wa siku ya Arafat mpaka alfajiri ya siku inayofuata, ambayo ni siku ya Kuchinja (Siku ya kumi ya Dhul-Hajjah). Mtume ﷺ alisimama Arafat wakati wa Hija ya kuaga, baada ya kuswali Dhuhr, mpaka machweo. Alisema, "Jifunzeni matendo yenu ya Ibada kutoka kwangu."² Katika Hadithi alisema, "Yeyote aliyesimama Arafat kabla ya Alfajiri, atakuwa amediriki (ibada za Hija)."

Urwah bin Mudharris bin Harithah bin Lam At-Tai رضى الله عنه alisema, "Nilikwenda kwa Mtume ﷺ tulipokuwa Muzdalifa alipotoka kwenda kuswali. Nilisema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Natoka kwenye milima miwili ya Tayy na mnyama wangu amechoka. Na mie nimechoka. Sikuacha mlima wowote ila nilisimama juu yake. Je, Hija yangu imeswihi?" Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ شَهِدَ صَلَاتَنَا هَذِهِ، فَوَقَفَ مَعَنَا حَتَّى نَذْفَعُ، وَقَدْ وَقَفَ بِعَرَفَةَ قَبْلَ ذَلِكَ لَيْلًا أَوْ
نَهَارًا فَقَدْ تَمَّ حَجُّهُ وَقَضَى تَقَاتُهُ»

"Yeyote aliyediriki Swala hii pamoja nasi, na akasimama nasi mpaka tukaondoka, na akawa ameshasimama Arafat mchana au usiku, atakuwa ametimiza Hija na kukamilisha ibada zake."

Hadithi hii ilikusanywa na Imam Ahmad na wakusanyaji wa Sunan, na At-Tirmidhi ameipa daraja la sahihi.³ Ilielezwa kuwa sababu ya kuitwa Arafat ni Hadithi iliyonukuliwa na Abdur Razak رحمه الله تعالى kuwa Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliniambia kuwa alinukuu kwa Bin Musayyib kutoka kwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه kuwa alisema, "Allah تعالى Alimtuma Jibril عليه السلام kwa Nabii Ibrahim

¹ Ahmad 4:310, Abu Dawud 2:485, Tuhfat Al-Ahwadhi 3:635, An-Nasai 5:256 na Ibn Majah 2:1003.

² Muslim 2:943.

³ Ahmad 4:261, Abu Dawud 2:486, Tuhfat Al-Ahwadhi 3:633, An-Nasai 5:264 na Ibn Majah 2:1004.

عليه السلام ili amfundishe ibada ya *Hija* walipofika *Arafat* Nabii Ibrahim عليه السلام alisema, '*Araftu*' maana yake hapa napajua; alikuwa kishafika hapo kabla. Baada ya hapo pakaitwa *Arafat*."¹ Ibn Al-Mubarak رحمه الله تعالى alisema kuwa Ata alisema. "Iliitwa *Arafat* kwa sababu Jibril عليه السلام alikuwa akimfundisha Ibrahim عليه السلام ibada ya *Hija*. Ibrahim عليه السلام akimwambia, *Araftu, Araftu.*' Baadaye ikaitwa *Arafat*." Kauli kama hizo zinanasibishwa kwa Ibn Abbas,² Ibn Umar na Abu Mijlaz رضي الله عنهم.³ Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. *Arafat* pia inaitwa *Al-Mash'ar Al-Haram, Al-Masha'ar Al-Aqsa* na *Ilal*, ambapo mlima ulio katikati ya *Arafat* unaitwa *Jabal Ar-Rahmah*.

Muda wa kuondoka Arafat na Muzdalifah:

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Katika zama za *Jahiliyyah*, watu walikuwa wakisimama *Arafat* mpaka jua likiwa juu ya milima, kama ilivyokuwa kwa kilemba juu ya kichwa, waliondoka. Mtume ﷺ akachelewesha kuondoka kutoka *Arafat* mpaka wakati wa machweo ya jua."⁴ Ibn Marduwyah aliisimulia Hadithi hii na akaongeza; Kisha alisimama-*Muzdalifah* na akasali *Fajr* mapema. Kulipopambazuka, aliondoka." Hadithi hii ina *Isnad* ya upokezi *Hasan*. Hadithi ndefu ambayo ilisimuliwa na Jabir bin Abdullah رضي الله عنه, ambayo ilikusanywa na Muslim, alisema, "Mtume ﷺ aliendelea kusimama (yaani *Arafat*) mpaka machweo, wakati mwanga wa njano ulipopotea na kisahani cha jua kimepotea, kisha Mtume ﷺ alimbeba (kwenye kipando) Usamah nyuma yake, na ili kumdhibiti *Al-Qaswa* alivuta lijamu kwa nguvu mpaka kichwa kikagusa tandiko la Ngamia wake. Aliashiria kwa mkono wa kulia na akasema, '*Enyi watu piteni kwa utulivu, kwa utulivu!*' Kila alipopita sehemu iliyoinuka kwa mchanga, alilegeza lijamu ya Ngamia wake mpaka alipopanda na hivi ndivyo walivyofika *Muzdalifah*. Hapo alisalisha Maghrib na *Isha* kwa *Adhan* moja na *Iqama* mbili na hakusali *Sunnah* kati ya hizo mbili. Mtume ﷺ alilala mpaka *Alfajir* aliposali *Fajr* kwa *Adhana* na *Iqamah*, wakati mwanga wa asubuhi ulipodhihiri. Kisha alimpanda *Al-Qaswa*, na alipowasili *Al-Mash'ar Al-Haram*, alielekea Qiblah, akimwomba Allah تعالى, akimtukuza na kusema, *La ilaha Illallah*, na akaendelea kusimama mpaka mwanga wa mchana ulipokomaa. Kisha alikwenda haraka kabla ya mawio."⁵

¹ Abdur-Razzak 5:96.

² At-Tabar 4:173 - 174.

³ Ibn Abu Hatim 2:519.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:517.

⁵ Muslim 2:886.

Ilielezwa katika sahihi mbili kuwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه aliulizwa, "Hatua za Mtume zilikuwaje alipokuwa akitembea?" Akajibu, "Polepole. Lakini ilipotokea haja alikwenda mwendo wa haraka."¹

Al-Masha'r Al-Haram (Maeneo Matukufu).

Abdur-Razzaq alieleza kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Al-Muzdalifah yote ni Al-Mash'ar Al-Haram.² Ilielezwa kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما aliulizwa kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

فَأَذْكُرُوا اللَّهَ عِنْدَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ^ط

"Mtajeni Mwenyezi Mungu penye Masha'ril Haram."

Alisema ni, 'Mlima na maeneo yanayozunguka.'³ Ilielezwa kuwa Al-Mash'aril Al-Haram ni ardhi iliyo kati ya Milima mwili,⁴ kama Ibn Abbas Said bin Jubayr, Ikrimah, Mujahid, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas, Al-Hasan na Qatadah رضي الله عنهم walivyoeleza. Imam Ahmad alinukuu kuwa Jubayr bin Mutim رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«كُلُّ عَرَفَاتٍ مَوْقِفٌ، وَارْفَعُوا عَنْ عُرْنَةِ، وَكُلُّ مُزْدَلِفَةَ مَوْقِفٌ، وَارْفَعُوا عَنْ مُحَسَّرٍ، وَكُلُّ فِجَاجٍ مَكَّةَ مَنْحَرٍ، وَكُلُّ أَيَّامِ التَّنْزِيلِ ذَبِيحٌ»

*"Arafat yote ni mahali pa kusimama na muwe mbali na Uranah. Muzdalifah yote ni sehemu ya kisimamo, na muwe mbali na Muhassir. Maeneo yote ya Makkah ni sehemu za kuchinja, na siku za Tashriq ni siku za kuchinja."*⁵

Kisha Allah تعالى Amesema:

وَأَذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا هَدَيْتُكُمْ

"Na mkumbukeni kama Alivyokuongoeni."

Aya hii inawakumbusha Waislam neema walizopewa na Allah تعالى kuwa Aliwaelekeza na Kuwafundisha Ibadat za Hajj kwa mujibu wa Alivyomwongoza Mtume Ibrahim Al-Khalil عليه السلام. Ndiyo sababu Allah تعالى Akasema:

¹ Fat'hul Al-Bari 3:605 na Muslim 2:936.

² Ibn Abu Hatim 2:521.

³ At-Tabari 4:176.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:521 -522.

⁵ Ahmad 4:82.

وَإِنْ كُنْتُمْ مِنْ قَبْلِهِ لَمَنِ الضَّالِّينَ ﴿١٩٨﴾

“Ijapokuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea.”

Imesemwa kuwa Aya hii inahusu hali ilivyokuwa kabla ya mwongozo huu au kabla ya kushushwa Qur’an au Mtume ﷺ, zote ni maana sahihi.

ثُمَّ أٰفِيضُوٓا۟ مِنْ حَيْثُ اَفَاضَ النَّاسُ وَاَسْتَغْفِرُوٓا۟ لِلّٰهِ ۗ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٩٩﴾

199. “Kisha miminiken kutoka pale wanapomiminika watu, na muombeni Mwenyezi Mungu msamaha: hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

Amri ya kusimama na kuondoka Arafat:

Aya hii ina Amri ya Allah تعالی kwa wale waliosimama Arafat kuondoka kwenda Muzdalifah, ili wamdhukuru Allah تعالی katika *Al-Mash’aril Al-Haram*. Allah تعالی Anamwamrisha Muislam kusimama Arafat pamoja na mahujaji wengine, kinyume na Maquraish ambao (kabla ya Uislam) walikuwa wakibaki katika maeneo matakatifu, jirani na Muzdalifah, wakisema kuwa wao ni watu wa Mji wa Allah تعالی na watumishi wa Nyumba Yake Tukufu. Al-Bukhari alieleza kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Quraysh na washirika wao, walikuwa wakiitwa *AL-Hums*,¹ wakisimama Muzdalifah wakati Waarabu wengine walisimama Arafat. Uislamu ulipokuja, Allah Alimuamrisha Mtume wake ﷺ kusimama Arafat na kisha aendelee mbele kutokea pale.” Kwa ajili hiyo Allah تعالی Amesema:

مِنْ حَيْثُ اَفَاضَ النَّاسُ

“Kutoka pale wanapomiminika watu.”²

Hili lilisemwa pia na Ibn Abbas, Mujahid, Ata, Qatadah na As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم.³ Ibn Jarir رحمه الله تعالی alichagua rai hii na Ijmaa (makubaliano miongoni mwa wanazuoni) walichukuwa pia rai hii.

Imam Ahmad alieleza kuwa Jubayr bin Mutim alisema, “Ngamia wangu alipotea na nilitoka kwenda kumtafuta, siku ya *Arafat*, hapo nilimuona Mtume ﷺ akiwa

¹ Maana yake halisi: “hasa ya kidini” Makuraishi waliitwa hivyo kutokana na mazoea yao ya kusema, “sisi ni watu wa Allah, sisi hatutaondoka mahali patakatifu.”

² Fat’hul Al-Bari 8:35

³ At Tabari 4:186 - 187

amesimama Arafat. Nilisema katika nafsi yangu, 'Wallah, huyu anatoka katika Hums. Kitu gani kimemleta hapa!'"¹ Hadithi hii imo pia ndani ya Sahihi mbili.²

Imamu Bukhari alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa maana ya neno 'Ifadha' ni kuondoka Muzdalifah kuelekea Mina kwenda kupiga maguzo.³ Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

Amri ya Kuomba Maghufira (Msamaha) na Dua Zake.

Allah تعالى Amesema:

وَأَسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٥﴾

"Na muombeni Mwenyezi Mungu msamaha; Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu"

Allah تعالى Aameamrisha mara nyingi kumkumbuka Yeye baada ya kumaliza vitendo vya Ibada. Imamu Muslim ameandika kuwa Mtume ﷺ alikuwa akimwomba Allah تعالى maghufira mara tatu baada ya kumaliza Sala.⁴ Imeelezwa katika sahih mbili kuwa Mtume ﷺ alihimiza *Tasbih* (kusema *Subhana Allah* - Ametakasika Allah), *Tahmid* (kusema, *Alhamdu lillah* - Shukrani zinamstahiki Allah تعالى) na *Takbir* (kusema, *Allah Akbar*, maana Allah تعالى ni Mkubwa kabisa) mara thelathini na tatu kwa kila moja (baada ya Sala). Angalia fadhila za Arafa.⁵

Ibn Marduwyah alikusanya Hadithi iliyoelezwa na Bukhari kutoka kwa Shaddad bin Awas رضي الله عنه, ambaye alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«سَيِّدُ الْإِسْنِغَارِ أَنْ يَقُولَ الْعَبْدُ: اللَّهُمَّ أَنْتَ رَبِّي، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، خَلَقْتَنِي وَأَنَا عَبْدُكَ، وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ، أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ، وَأَبُوءُ بِذَنْبِي، فَاغْفِرْ لِي فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، مَنْ قَالَهَا فِي لَيْلَةِ فَمَاتَ فِي لَيْلَتِهِ دَخَلَ الْجَنَّةَ، وَمَنْ قَالَهَا فِي يَوْمِهِ فَمَاتَ دَخَلَ الْجَنَّةَ»

"Bwana wa dua ya maghufira, ni kwa mja kusema: 'Ewe Allah Wewe ni Bwana wangu, hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa"

¹ Ahmad 4:80.

² Fat'hul Al-Bari 3:602, na Muslim 2:894.

³ Fat'hul Al-Bari 8:35.

⁴ Muslim 1:414.

⁵ Fat'hul Al-Bari 2:378 na Muslim 1:417.

*isipokuwa Wewe. Umeniumba, nami ni mja wako. Niko katika kiaga chako kadiri itakavyoyumkinika na ninasubiri Ahadi Yako. Najilinda Kwako kwa makosa niliyoyafanya. Nashukuru kwa Neema Ulizonipa. Hivyo nisamehe kwani hapana msamehevu wa makosa isipokuwa Wewe.' Yeyote atakayesema maneno haya usiku kisha akafa usiku huo, ataingia Peponi; na yeyote atayesema mchana na akafa mchana huo ataingia Peponi."*¹

Zaidi ya hayo, ilielezwa ndani ya sahihi kuwa Abdullah bin Amr alisema kuwa Abubakar رضي الله عنه alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nifundishe Dua ya kumuomba Allah تعالى nikiwa ndani ya Sala. Aliniambia sema:

«قُلْ: اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا وَلَا بَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ فَاعْفِرْ لِي
مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ، وَارْحَمْنِي إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ»

*"Ewe Allah! Nimeidhulumu nafsi yangu kwa kiasi kikubwa na hapana isipokuwa Wewe Ndiye Msamehevu wa Makosa, hivyo nakuomba Unisamehe na Uwe mrehemevu kwangu, kwani Wewe ni Msamehevu, na Mrehemevu."*²

Kuna Hadithi nyingi kuhusu somo hili la kuomba maghfira.

فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَسِكَكُمْ فَادْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ ءَابَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا فَمِنَ
النَّاسِ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا ءَاتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ ﴿٢٠٠﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ
يَقُولُ رَبَّنَا ءَاتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾ أُولَئِكَ
لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٢﴾

200. "Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi. Na wapo baadhi ya watu wanaosema; Mola wetu Mlezi tupe duniani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote."

201. "Na katika wao wapo wanaosema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na Utulinde na adhabu ya Moto!"

¹ Fat'hul Al-Bari 11:100.

² Fat'hul Al-Bari 13:484 na Muslim 4:2078.

202. "Hao ndio watakaopata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu."

Amri ya kumdhukuru Allah تعالى na Kuomba Maisha Mema Duniani na Akhera baada ya Kumaliza Ibada za Hajj:

Allah تعالى Ameamrisha Adhukuriwe baada ya kukamilishwa ibada. Na Kauli Yake:

كَذِّكْرُكُمْ ءَابَاءَكُمْ

"Kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu."

Said bin Jubayr alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Katika enzi za Jahiliyyah, watu walikuwa wakisimama wakati wa msimu wa Hija, na mmoja wao husema, "Baba yangu alikuwa akiwalisha (masikini), akiwasaidia wengine (kumaliza migogoro yao kwa fedha zake), kulipa Diyah, na kadhalika. Dhikr waliyokuwa nayo ni kukumbuka matendo ya baba zao, Kisha Allah تعالى Akateremsha Wahyi kwa Mtume Muhammad ﷺ,

فَأذْكُرُوا اللَّهَ كَذِّكْرِكُمْ ءَابَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا

"Basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi."¹

Lengo la Aya hii ni, kumdhukuru Allah تعالى Aliye juu ya kila kitu, nako kunahimizwa kila wakati. Tunalazimika kutaja kuwa Allah تعالى Alitumia neno: "au" katika Aya, na Alikusudia Kuwashajiisha wamdhukuru Yeye zaidi ya vile wanavyowadhukuru mababu zao, na au hapa si neno lenye kuonesha utata (kuwa kipi ni kikubwa). Kauli hii ni sawa na Aya:

فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدَّ قَسْوَةً

"Hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi." (2:74)

Na Kauli Yake,

يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً

"Waliwaogopa watu kama kumwogopa Mwenyezi Mungu au kwa khofu kubwa zaidi." (4:77)

¹ Ibn Abu Hatim 2:530.

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٧٧﴾

“Na Tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi.” (37:147)

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili au karibu zaidi.” (53:9)

Allah تعالی Anawashajiisha viumbe wake wamkumbuke Yeye na kumtaja katika Dua, kwa sababu hii itafanya maombi yakubaliwe. Aidha Allah تعالی Anawalaumu wale wanaomwomba kuhusu mambo ya hapa duniani tu, huku wakiyapuuzia mambo ya Akhera.

Allah تعالی Amesema:

فَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِن خَلْقٍ ﴿١٧٧﴾

“Na wapo baadhi ya watu wanaosema: Mola wetu Mlezi, tulipe duniani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote.”

Maana yake: Hawana fungu Akhera. Ukosoaji huu una lengo la kuwavunja nguvu wengine wenye nia ya kuwaiga wale tuliowataja. Said bin Jubayr alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Baadhi ya mabedui wakija Arafat na kuomba wakisema, “Ewe Allah! Ufanye mwaka huu wa mvua, mwaka wenye rutuba, na mwaka mzuri wa kuzaa watoto.” Hawakuomba lolote kuhusu Akhera.

Hivyo Allah تعالی Akateremsha Aya kuwahusu:

فَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِن خَلْقٍ ﴿١٧٧﴾

“Na wapo baadhi ya watu wanaosema: ‘Mola wetu Mlezi, tupe duniani. Naye katika Akhera hana sehemu yoyote.’”

Waumini waliokuja baada yao walikuwa wakisema:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾

“Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema na Akhera mema na Utulinde na adhabu ya Moto”.

Baada ya hapo Allah تعالی Aliteremsha.

أُولَئِكَ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٢﴾

“Hao ndio watakaopata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhesabu.”

Hivyo Allah تعالى Amewasifu wale wanaoomba mambo ya dunia na Akhera Amesema:

وَمِنَهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾

“Na katika wao wapo wanaosema: Mola wetu Mlezi tupe duniani mema, na Akhera mema, na Utulinde na adhabu ya moto!”

Dua iliyotajwa na shukrani zilizomo katika Aya ni pamoja na mambo yote mazuri ya maisha ya duniani na kuomba hifadhi kutokana na maovu yote. Maisha mazuri ya hapa duniani ni pamoja na kuomba hali nzuri, wenza wanaoridhisha, chakula cha kutosha, elimu yenye manufaa, amali njema, kipando kizuri (gari n.k) na sifa nzuri, ambazo zimetajwa na wanazuoni wa Tafsir kuhusiana na somo hili. Yote hayo ni sehemu tu ya mazuri yanayo tafutwa katika maisha ya duniani.

Ama kwa mazuri ya Akhera, mazuri yake ni pamoja na kupata Pepo, ambayo ni pamoja na kupata usalama kutokana na vitisho vya Mkusanyiko wa siku hiyo. Aidha, ni pamoja na kupata wepesi ataposailiwa na neema nyingine za siku ya Kiama.

Ama kuhusu kusalimika na Moto, ni pamoja na kuelekezwa kwa yale yanayosababisha mwisho mwema wa dunia, kama kujiepusha na yaliyoharamishwa, makosa ya kila aina na mambo tatanishi na ya Haramu.

Al-Qasim bin Abdur-Rahman alisema, “Yeyote aliyezawadiwa moyo wa uchaji, ulimi unaodhukuru na mwili wenye subira, atakuwa ameruzukiwa mema ya hapa duniani na mema ya kesho Akhera na atakuwa amekingwa na adhabu ya moto.”¹

Kwa sababu hii, Sunnah imehimiza kusomwa kwa Dua hii (katika Aya kuhusu kupata amali njema hapa duniani na Akhera). Imamu Bukhari alieleza kuwa Sayyidina Anas bin Malik رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema;

¹ Ibn Abu Hatim 2:542.

«اللَّهُمَّ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً، وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً، وَوَقْنَا عَذَابَ النَّارِ»

“Ewe Allah, Mola wetu Mlezi! Tupe duniani mema na Akhera mema, na Utulinde na adhabu ya Moto”¹

Imam Ahmad ameeleza kuwa Anas رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alimtembelea mwanaume wa Kiislamu ambaye alidhoofika na akawa kama kifaranga cha ndege mdogo mwenye maradhi. Mtume ﷺ akamuuliza, “*Ulikuwa na tabia ya kumwomba Allah chochote?*” Akajibu, ‘Ndiyo. Nilikuwa nikisema: “Ewe Allah تعالی! Adhabu yoyote Uliyopanga kuniadhibu Akhera niadhibu mapema hapa duniani.” Mtume ﷺ Akasema:

«سُبْحَانَ اللَّهِ لَا تُطِيقُهُ أَوْ لَا تَسْتَطِيعُهُ، فَهَلَّا قُلْتَ: ﴿رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ﴾»

“Ametakasika Allah! Huiwezi adhabu hiyo, kwa nini hukuomba: “Ewe Mola wetu mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na Utulinde na adhabu ya Moto!”

Yule mtu akaanza kuisoma Dua hii na alipona.”² Muslim aliandika pia.³

Al-Hakim alieleza katika Al-Mustadrak kuwa Said bin Jubayr رضي الله عنه alisema, “Mtu mmoja alikuja kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na kusema, “Niliwafanyia kazi watu fulani wakanilipa sehemu kwa kunipeleka *Hija* pamoja nao. Je, inakubalika?”

Ibn Abbas رضي الله عنهما akajibu, “Wewe ni miongoni mwa wale walioelezwa na Allah:

«أَوْلَيْتِكَ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٤﴾»

“Hao ndio watakaopata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.”⁴

Kisha Al-Hakim alisema; Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Mashaykh wawili (Imamu Bukhari na Muslim) japokuwa wao hawakuiandika.”

¹ Fat’hul Al-Bari 8:35.

² Ahmad 3:107.

³ Muslim 4:2068.

⁴ Al-Hakim 2:227.

* وَأَذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ ۚ فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ
 فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ لِمَنِ اتَّقَىٰ ۙ وَاتَّقُوا
 اللَّهَ وَعَلِمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٣﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ
 يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهَدُ اللَّهُ عَلَىٰ مَا فِي
 قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَدُّ الْخِصَامِ ﴿٢٠٤﴾ وَإِذَا تَوَلَّىٰ سَعَىٰ فِي الْأَرْضِ
 لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ
 الْفُسَادَ ﴿٢٠٥﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُ اتَّقِ اللَّهَ أَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْإِثْمِ ۗ
 فَحَسْبُهُ جَهَنَّمُ ۚ وَلَبِئْسَ الْأَلْبَاءُ ﴿٢٠٦﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ
 يَشْرِي نَفْسَهُ أُتْبِغَاءَ مَرَضَاتٍ آلِهَةٍ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ
 ﴿٢٠٧﴾ يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا آذْخُلُوا فِي السَّلَامِ كَأَقْفَةٍ وَلَا
 تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠٨﴾
 فَإِنْ زَلَلْتُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْكُمْ الْبَيِّنَاتُ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
 عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٠٩﴾ هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي
 ظُلْمٍ مِّنَ الْعَمَامِرِ وَالْمَلَكِئِكَةِ وَقُضِيَ الْأَمْرُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ

تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٢١٠﴾

* وَأَذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ ۚ
 فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ
 وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ لِمَنِ اتَّقَىٰ ۙ
 وَاتَّقُوا اللَّهَ وَعَلِمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ
 تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٣﴾

203. "Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazo hisabiwa. Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake; na wenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa Kwake."

Kumdhukuru Allah تعالى
 Katika Siku za Tashriq
 Ambazo ni Siku za Kula na
 Kunywa.

Ibn Abbas رضي الله عنهما
 alisema, "Siku zinazohe-
 sabiwa ni siku za Tashriq

(Tarehe 11, 12 na 13 za mwezi wa Dhul- Hijjah) ambapo Siku zinazojulikana ni siku kumi za mwanzo za Dhul-Hijjah."¹ Ikrimah alisema kuwa:

* وَأَذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ ۚ

"Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazohesabiwa."

¹ Al-Qurtubi 3:3.

Maana yake: Kusoma *Takbir - Allahu Akbar, Allahu Akbar, katika siku za Tashriq baada ya Swala za faradhi.*¹ Imam Ahmad ameeleza kuwa Uqbah bin Amr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema

«يَوْمُ عَرَفَةَ، وَيَوْمُ النَّحْرِ، وَأَيَّامُ التَّشْرِيقِ، عِيدُنَا أَهْلَ الْإِسْلَامِ، وَهِيَ أَيَّامُ أَكْلٍ وَشُرْبٍ»

*“Siku ya Arafah (Tarehe 9 katika mwezi wa Dhul- Hijjah), na siku za kuchinja (mwezi 10) na siku za Tashriq (Tarehe 11,12 na 13) ni sikukuu zetu sisi waislamu. Nazo ni siku za kula na kunywa.”*²

Imam Ahmad ameeleza kuwa Nubayshah Al- Hudhalil رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَيَّامُ التَّشْرِيقِ أَيَّامُ أَكْلٍ وَشُرْبٍ وَذِكْرِ اللَّهِ»

“Siku za Tashriq ni siku za kula kunywa na kumdhukuru Allah.”

Pia Muslim aliinukuu Hadithi hii.³

Aidha tumekwisha kuitaja Hadithi ya Jubayr bin Mutim رضي الله عنه:

«عَرَفَةَ كُلُّهَا مَوْقِفٌ، وَأَيَّامُ التَّشْرِيقِ كُلُّهَا ذَبْحٌ»

*“Arafat yote ni sehemu ya kisimamo na siku zote za Tashriq ni siku za Kuchinja.”*⁴

Pia tulitaja Hadithi ya Abdur- Rahman bin Ya’ mar Add- Diyli رضي الله عنه:

«وَأَيَّامُ مِنَى ثَلَاثَةٌ فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ»

*“Siku za kukaa Mina ni tatu, wale wanaoharakisha kwa siku mbili, hawana makosa, na wale wanaochelewesha (kubaki Mina kwa siku ya tatu), hapana makosa kwa hilo.”*⁵

Ibn Jarir رحمته الله تعالى ameeleza kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Ibn Abu Hatim 2:545.

² Ahmad 4:152.

³ Ahmad 5:75 na Muslim 2:800.

⁴ Ahmad 4:82.

⁵ Abu Dawud 2:485.

«أَيَّامُ النَّشْرِيقِ أَيَّامُ طَعْمٍ وَذِكْرِ اللَّهِ»

“Siku za Tashriq ni siku za kula na kumdhukuru Allah.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameeleza tena kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alimtuma Abdullah bin Hudhaifah رضي الله عنه kwenda Mina kutangaza:

«لَا تَصُومُوا هَذِهِ الْأَيَّامَ، فَإِنَّهَا أَيَّامُ أَكْلِ وَشُرْبٍ وَذِكْرِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Msifunge katika siku hizi (siku za Tashriq) kwani ni siku za kula, kunywa na kumdhukuru Allah Aliyetukuka.”²

Maelezo ya Siku Zinazohesabiwa.

Miqsam alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa siku zinazohesabiwa ni siku za *Tashriq* nazo ni siku nne: Siku ya kuchinja (tarehe 10, mwezi wa Dhulhijjah) na siku tatu baada ya hapo.³

Rai hii ilinukuliwa pia na Ibn Umar, Ibn Az- Zubayr, Abu Musa, Ata Mujahid, Ikrimah. Said bin Jubayr, Abu Malik, Ibrahim An- Nakhai, Yahya bin Abu Kathir, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi, Az-Zuhri, Ar-Rabi Bin Anas na wengineo.⁴ Kwa ziada maana ya Aya ifuatayo inaunga mkono rai hii pale Allah تعالى Aliposema;

فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ

“Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake, na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake.”

Hivyo aya imetaja siku tatu baada ya siku ya kuchinja na hufungamana na Kauli Yake Allah تعالى،

* وَأَذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَعْدُودَاتٍ

“Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazohesabiwa.”

Inahusiana na kumdhukuru Allah تعالى katika kuchinja wanyama, baada ya Swala zilizowekewa nyakati maalumu na ambazo hazikuwekewa nyakati. Pia inahusiana na *Takbirah* na kumdhukuru Allah تعالى wakati wa kutupa vijawe kila siku katika siku za *Tashriq*. Hadithi ambayo Abu Dawud na wengine wameeleza:

¹ At-Tabari 4:211.

² At-Tabari 4:211.

³ At-Tabari 4:213.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:547-549.

إِنَّمَا جُعِلَ الطَّوَافُ بِالْبَيْتِ وَالسَّعْيُ بَيْنَ الصَّفَا وَالْمَرْوَةِ وَرَمِي الْجِمَارِ لِإِقَامَةِ ذِكْرِ اللَّهِ
عَزَّ وَجَلَّ

*"Tawaf kuzunguka nyumba ya Allah, Sai baina ya As-Safa na Al-Marwah na kutupa vijiwe kulifaradhiwa ili kudumishwe kutajwa Allah kwenye Dhikr."*¹

Baada ya Allah تعالی Kutaja mtawanyiko wa kwanza na wa pili, ambako ni kutawanyika watu (rejea 2:199) na kurejea majumbani mwao, baada ya kumalizika msimu wa Hijja na baada ya kukusanyika katika viwanja vitukufu vya Al-Mash'aril Har'am, Allah تعالی Amesema,

وَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٤﴾

"Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake."

Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

وَهُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٥﴾

"Na Yeye Ndiye Aliyekuenezeni katika ardhi na Kwake Yeye mtakusanywa." (23:79)

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهَدُ اللَّهُ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَدُّ

الْخِصَامِ ﴿٢٠٦﴾ وَإِذَا تَوَلَّىٰ سَعَىٰ فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ ۗ وَاللَّهُ

لَا يُحِبُّ الْفُسَادَ ﴿٢٠٧﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُ اتَّقِ اللَّهَ أَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْإِثْمِ ۗ فَحَسْبُهُ جَهَنَّمُ ۚ

وَلَيْسَ بِالْمِهَادِ ﴿٢٠٨﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ

رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠٩﴾

204. "Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia hukufurahisha; naye humshuhudia Mwenyezi kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu."

¹ Abu Dawud 2:447.

205. “Na anapotawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.”

206. “Na akiambiwa: Mwogope Mwenyezi Mungu, hupandwa na mori wa kutenda madhambi. Basi huyo inamtosha Jahannam. Paovu mno hapo kwa mapumziko.”

207. “Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja Wake.”

Tabia na Hali za Wanafiki.

As-Suddi alisema kuwa Aya hizi ziliteremshwa kumhusu Al-Akhnas bin Shuraig Ath-Thaqafi aliyekuwa kwa Mtume ﷺ na akatamka kusilimu kwake ilihali moyoni mwake amenuia kinyume chake.¹

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisimulia kuwa Aya hizi ziliteremshwa juu ya baadhi ya wanafiki ambao walimsema vibaya Khubayb na marafiki zake رضي الله عنهم ambao waliuawa wakati wa tukio la Ar-Raji.² Allah تعالى Akateremsha Aya za Kuwakosoa wanafiki na Akamsifia Khubayb na marafiki zake رضي الله عنهم.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْرِي نَفْسَهُ أُتْبِغَاءَ مَرَضَاتٍ ۗ وَاللَّهُ

“Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu.”

Pia ilisemwa kuwa inawahusu wanafiki wote na waumini wote kwa ujumla.³ Hii ni rai ya Qatadah, Mujahid, Ar-Rabi bin Anas na wengine wengi, na ni kauli sahihi.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Al-Quradhi alisema kuwa Nawf ambae ni Al-Bikali, aliyekuwa miongoni mwa waliokuwa wakisoma vitabu (vitakatifu vilivyotangulia) alisema, “Nimekuta maelezo ya baadhi ya watu wa Ummah

¹ At-Tabari 4:229

² Pindi makabila ya Adal na Qarah walipowaua masahaba kumi waliotumwa na Mtume ﷺ kuwafundisha Qur'an

³ At-Tabari 4:230.

huu katika Kitabu cha Allah ﷻ kilichoteremshwa; Wanafiki ni watu wanaotumia dini kupata faida za kidunia. Ndimi zao ni tamu kuliko asali, lakini mioyo yao ni michungu kuliko shubiri wanawaonesha watu mavazi ya kondoo wakati nyoyo zao ni za mbwa mwitu. Allah ﷻ Anasema, ‘Wanadiriki kushindana Nami, na kunifanyia hadaa? Naapa kwa Nafsi Yangu Nitawapelekea Fitnah? (mtihani, maana) ambayo itamfanya mtu mwenye busara kutatizika.’ Al-Qurtubi رحمه الله تعالى alisema, ‘Nilizingatia kauli hizi na nikazikuta ndani ya Qur’an zikielezea sifa za mnafiki:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهَدُ اللَّهَ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ

“Na katika watu kuna ambao kauli zao zinakufurahisha hapa duniani. Nao humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwao.”¹

Kauli hii ya Al-Quradhi ni *Hasan Sahih*. Ama Kauli Yake:

وَيُشْهَدُ اللَّهَ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ

“Nao humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwao.”

Maana yake: Ni kwamba watu wa aina hiyo huwadhihirishia watu kwamba wao ni Waislamu, lakini wanamkiuka Allah ﷻ kutokana na ukafiri na unafiki wao ambao wameuficha katika mioyo yao. Vile vile Allah ﷻ Amesema:

يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ مِنَ اللَّهِ

“Wanataka kujificha kwa watu, wala hawataki kujificha kwa Mwenyezi Mungu.” (4:108)

Ibn Is- haq رحمه الله تعالى aliinukuu Tafsir hii kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.² Na wapo waliosema kuwa Aya ina maana kuwa watu hao wanapotamka shahada, wanaapa kwa jina la Allah ﷻ kuwa kilichomo ndani ya nyoyo zao ni sawa na kile kinachotamkwa na ndimi zao. Maana hii ni sahihi. Na aliyasema hayo Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam.³ Huu pia ni mtazamo wa Ibn Jarir رحمه الله تعالى ambaye alisimuliwa na Mujahid aliihusisha tafsiri hii na Ibn Abbas رضي الله عنهما. Allah ni Mjuzi zaidi. Allah ﷻ Amesema:

¹ At-Tabari 4:232.

² At-Tabari 4:230.

³ At-Tabari 4:233.

وَهُوَ الَّذِي الْخَصَامِ ﴿٢٠٤﴾

“Na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu.” (2:204)

Maana ya neno *Aladd* kilugha ni “mpotovu.” (Hapa ina maana ‘mgomvi mno’). Mabadiliko ya neno *ludda* yametumika pia katika Aya nyingine:

وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُّدًّا ﴿١٧﴾

“Na (Muhammad) uwaonye kwayo (Qur’an) watu wanao gombana.” (19:97)

Halikadhalika, mnafiki katika hali ya ugomvi wake, husema uongo, na huubadilisha ukweli. Hawi imara katika ukweli, bali huwa anazua, hudanganya na huwa muovu. Imenukuliwa ndani ya Sahihi kuwa Mtume ﷺ alisema:

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا عَاهَدَ غَدَرَ، وَإِذَا خَاصَمَ فَجَرَ»

“Alama za mnafiki ni tatu: Anapozungumza, husema uongo. Anapoahidi, huvunja ahadi. Na anapokuwa na mgogoro, huwa mgomvi sana.”¹

Imam Bukhari ameeleza kuwa Aishah رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ أَبْغَضَ الرِّجَالِ إِلَى اللَّهِ الْأَلَدُّ الْخَصِيمُ»

“Mtu anayechukiwa zaidi na Allah ni aliye Aladdul- Khasim (yaani mgomvi mno).”²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا تَوَلَّى سَعَىٰ فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

﴿٢٠٥﴾

“Na anapotawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu Hapendi Ufisadi.” (2:205)

Maana yake: Mtu huyo ni mpotofu katika ayasemayo, muovu katika amali zake, maneno yake ni kuzua, imani yake imeharibika na anayoyafanya ni

¹ Fat’hul Al-Bari 1:111.

² Fat’hul Al-Bari 8:36.

mabaya. Aya imetumia (neni la Kiarabu) *Sa'a* ('kukusudia' au 'dhamira'). Neno hili lilitumiwa kumwelezea Firauni:

ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَى ﴿٧٩﴾ فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٨٠﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَى ﴿٨١﴾ فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ
الْآخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٨٢﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِمَن يَخْشَى ﴿٨٣﴾

“Kisha alirudi nyuma, akaingia kufanya juhudi. Akakusanya watu akanadi. Akasema: “Mimi ndiye Mola wenu Mlezi mkuu kabisa.” “Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo. Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanaogopa.” (79:22-26)

[*Sa'a* ilitumiwa pia katika Aya]

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ

“Enyi mliaoamini! Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu.” (62:9)

Aya hii ina maana (Adhana ya Sala ya Ijumaa ikishasomwa) tia nia na *kisha* uelekee msikitini kusali Ijumaa. Inafaa tutaje hapa kuwa *Sunnah* imekemea jambo la kwenda mbio kukimbilia Sala Msikitini (ni kuwa hii ni maana nyingine ya neno *Sa'a*)

«إِذَا أَتَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَلَا تَأْتُوهَا وَأَنْتُمْ نَسَوْنَ، وَأْتُوهَا وَعَلَيْكُمْ السَّكِينَةُ وَالرَّقَابُ»

“Unapokuja kuhudhuria Sala, usije (haraka): Bali uje ukitembea taratibu na kwa utulivu.”¹

Mnafiki hana jingine katika maisha isipokuwa kufanya fujo na kuharibu mazao na vinavyozaliwa, ikiwa ni pamoja na mazao, matunda na viumbe. Tena ni mazao ya wanyama ambao watu wanawategemea katika maisha yao. Mujahid amesema, “Iwapo mnafiki atakwenda kufanya uharibifu katika ardhi, Allah huzuia mvua kunyesha na hivyo mazao na mimea michanga kuangamia.” Ayah inaendelea,

وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْفُسَادَ ﴿١٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Hapendi uharibifu.” Maana yake: Mwenyezi Mungu Hapendi sifa hizi.

¹ Muslim 1:420.

Miongoni mwa sifa za Mnafiki ni kukataa kupokea Nasaha:

Allah تعالى Amesema,

وَإِذَا قِيلَ لَهُ اتَّقِ اللَّهَ أَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْإِثْمِ ۗ

“Na akiambiwa: Mwogope Mwenyezi Mungu, hupandwa na mori wa kutenda madhambi.”

Maana yake: Muovu huyu anapopewa mawaidha kuihusu kauli na vitendo vyake, na akaambiwa amche Allah تعالى kwa vitendo vyake viovu na arejee katika haki, hukataa na hupandwa na jazba na hasira kwa kutenda madhambi, maana kwa sababu ya mazoea yake katika madhambi.

Aya hii inashabihiana na Alivyosema Allah تعالى:

وَإِذَا تَتَلَوْا عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا بَيِّنَاتٍ تَعْرِفُ فِي وُجُوهِ الَّذِينَ كَفَرُوا الْمُنْكَرَ يَكَادُونَ
يَسْطُونَ بِالَّذِينَ يَتْلُونَ عَلَيْهِمْ ءَايَاتِنَا ۗ قُلْ أَفَأَنْتُمْ بِشِرِّ مِّنْ ذَلِكُمْ أَتَّارٌ وَعَدَّهَا
اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَسَّ الْمَصِيرُ ﴿٧٦﴾

“Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi utaona chuki katika nyuso za waliokufuru. Hukaribia kuwavamia wale wanaowasomea hizo Aya zetu. Sema: Je! Nikwambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni Moto. Mwenyezi Mungu Amewaahidi waliokufuru, na ni marudio mabaya hayo.” (22:72)

Hii ndio sababu katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

فَحَسْبُهُمْ جَهَنَّمُ ۗ وَلَيْسَ الْمَهَادُ ﴿٧٦﴾

“Basi huyo inamtosha Jahannam. Paovu mno hapo kwa mapumziko.”

Maana yake: Huko ndiko kuadhibiwa kwake kunakomtosha kwa madhambi hayo.

Miongoni mwa Sifa za Muumini Mtiifu ni kutafuta radhi za Allah تعالى:

Allah تعالى Amesema,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ¹

“Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu.”

Baada ya Allah تعالى Kuelezea sifa mbovu za wanafiki, Ametaja sifa nzuri za Waumini. Allah تعالى Amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ¹

“Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu.”

Ibn Abbas, Anas, Said bin Musayyib, Abu Uthman An-Nahdi, Ikrimah na wanazuoni wengine رضي الله عنهم walisema kuwa Aya hii iliteremshwa kumhusu Suhayb bin Sinan Ar- Rumi رضي الله عنه.

Suhaib رضي الله عنه aliposilimu akiwa Makkah na akakusudia kuhamia Madinah, Makuraish walimzuia kuhama pamoja na mali yake. Walimwambia kama angeacha mali yake nyuma, wangemruhusu aondoke. Alijinusu dhidi yao na akawaachia mali yake.

Allah تعالى Akateremsha Aya hii kwa ajili yake: Umar bin Khattab رضي الله عنه na Maswahaba wengine wakamlaki katika sehemu inayoitwa Al-Harrah (ardhi tambarre yenye mawe meusi). Wakamwambia, “Biashara imeleta faida.” Akawajibu, “Na nyie pia, Allah تعالى Awajaalie biashara zenu zisipate hasara. Kuna jambo gani?” Wakamuambia kuwa Allah تعالى Ameteremsha Ayah hii (2:207) inayomhusu. Pia ilitaarifiwa kuwa Mtume ﷺ alisema, kumwambia yeye, “Biashara imetononoka, Ewe Suhayb!”¹

Na maana ya Aya hii imeenea, na anaingia kila mwenye jitihada katika njia ya Allah تعالى.

¹ Fat-hul Qadir 1:210.

Ni sawa na Kauli Yake:

﴿ إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنْ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقْتُلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدَا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ ۗ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِالَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ ۗ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Amenunua Waumini nafsi zao na mali zao kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanaua na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa haki katika Taurati na Injili na Qur’an. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.”
(9:111)

Hisham bin Amr alipopenya ngome za maadui, baadhi ya watu walimkosoa. Umar bin Al-Khattab na Abu Hurayrah رضي الله عنهما waliwakatalia na wakasoma Aya hii.

﴿ وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴾

“Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake”.

﴿ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَدْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴾ فَإِنْ زَلَلْتُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْكُمْ الْبَيِّنَاتُ فَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

208. “Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu, wala msifuate nyayo za Shetani; hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi”.

¹ At-Tabari 4:252, Ibn Abu Hatim 2:584-585.

209. "Na ikiwa mtateleza baada ya kukufikieni hoja zilizo wazi, basi jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima."

Imefaradhishwa Kuingia katika Uislam kwa Ukamilifu Wake:

Allah تعالی Amewaamrisha waja wake ambao wanamwamini Yeye na wanamsadiki Mjumbe wake ﷺ kutekeleza sharia zote za Uislam, na kushikamana na maamrishi Yake yote na kujiepusha na yote yaliyoharamishwa kwa kadri ya uwezo wao. Al- Awfi aliwanukuu Ibn Abbas, Mujahid, At- Tawus, Adh- Dhahhak, Ikrimah, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd رضي الله عنهم, kuwa maana ya Kauli ya Allah تعالی inasema:

أَدْخُلُوا فِي السِّلْمِ

"Ingieni katika Uislam". Ni, Uislam.¹

Na Kauli ya Allah تعالی:

كَافَّةً

"Kwa ukamilifu."

Amesema Ibn Abbas, Mujahid, Abu Al-Aliyah, Ikrimah, Ar- Rabi bin Anas, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan, Qatadah na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم 'Wote.'¹ Maana yake: Ni Uislamu wote.

Mujahid alisema kuwa Aya ina maana, "Fanyeni kazi zote nzuri na amali mbalimbali za uchaji Mungu."² Hili linawahusu waumini wa kweli miongoni mwa watu wa Kitabu. Ibn Abu Hatim ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اَدْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً

"Enyi mlioamini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu."

Wanakusudiwa waumini miongoni mwa watu wa Kitabu. Hii ni kwa sababu walimuamini Allah تعالی, na baadhi yao bado walishikamana na sehemu ya Taurati na wahyi ulioteremshwa kwao, Allah تعالی Akasema,

¹ Ibn Abu Hatim 2:586-588.

² Ibn Abu Hatim 2:585.

أَدْخُلُوا فِي الْإِسْلَامِ كَافَّةً

“Ingieni katika Uislam kwa ukamilifu.”

Kwa hiyo, Allah تعالیٰ Anawaamuru: Ingieni katika Dini ya Muhammad ﷺ, wala msiache chochote katika Dini yake. Wala hakuna haja ya kuendelea kuing'ang'ania Taurat na yaliyomo ndani yake. Na Kauli Yake,

وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ

“Wala msifuate nyayo za Shetani.”

Maana yake: Fanyeni ibada na mjiopushe na anayokuamuruni Shetani. Hii ni kwa sababu:

إِنَّمَا يَأْمُرُكُمْ بِالسُّوءِ وَالْفَحْشَاءِ وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٦٩﴾

“Yeye anakuamrishi maovu na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.” (2:169) Na;

إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٣٦﴾

“Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni.” (35:6)

Hivyo, Allah تعالیٰ Amesema:

إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿١٦٨﴾

“Hakika yeye kwenu ni adui aliye wazi.”

Na Kauli Yake,

فَإِنْ زَلَلْتُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْكُمْ الْبَيِّنَاتُ

“Na Mkikengeuka baada ya kukujieni yaliyo wazi.”

Maana yake: Mkiukengeuka ukweli baada ya ushahidi uliowazi kudhihiri dhidi yako,

¹ Ibn Abu Hatim 2:582.

فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ

“Basi jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu.”

Maana yake: Katika Adhabu Yake, na hapana anayeweza kuepa kisasi Chake au kumshinda Yeye.

حَكِيمٌ

“Na Mwenye Hekima.”

Katika Maamuzi Yake: Vitendo na Hukumu. Hivyo Abu Al-Aliyah, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas walisema, “Ana Nguvu katika Kulipiza kisasi, Mwenye Busara katika Maamuzi Yake.”¹

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَإِلَى اللَّهِ

تُرْجَعُ الْأُمُورُ

210. “Je wanangoja mpaka Mwenyezi Mungu Awajie katika vivuli vya mawingu pamoja na Malaika, na hukumu iwe imekwisha tolewa? Na kwa Mwenyezi Mungu ndio hurejeshwa mashauri yote.”

Msisitizo wa Kutokuchelewa Kusilimu (Kutamka Shahada):

Katika kuwazungumzia waliomkufuru Mtume Muhammad ﷺ, Allah تعالیٰ Amesema:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ

“Kuna jingine wanalongoja ila kuwafikia Mwenyezi Mungu katika vivuli vya mawingu na Malaika.”

Maana yake: Atakuja siku ya Kiyama Kuwahukumu viumbe wa mwanzo na waliokuja baadaye. Ili Amlipe kila mmoja kulingana na amali zake. Ikiwa alifanya mema atalipwa wema wake na kama alitenda maovu atalipwa uovu wake. Kwa sababu hii Allah تعالیٰ Amesema:

¹ Ibn Abu Hatim 2:591.

وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٢٠٣﴾

“Na liishe (mara moja) hilo jambo (la kuadhibiwa kwao)? na mambo yote hurudishwa kwa Mwenyezi Mungu.”

Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema:

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢٠٤﴾ وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٠٥﴾ وَجِئْنَا بِبُحْبُورٍ ﴿٢٠٦﴾

“Sivyo hivyo! Itakapo vunjwa ardhi vipandevipande. Na Akaja Mola wako Mlezi na Malaika safusafu. Na ikaletwa Jahannamu siku hiyo, siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?” (89:21-23)

Na Allah تعالى Amesema,

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ

“Wanangoja jingine ila wawafikie Malaika au Awafikie Mola wako Mlezi au Zifike baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi?” (6:158)

Abu Jafar Razi رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Ar-rabii bin Anas amesema kuwa Abu Al-Aliyah alisimulia kuwa:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ

“Hakuna jingine wanalongojea ila kuwafikia Mwenyezi Mungu kutoka katika vivuli vya mawingu na Malaika.”

Anasema kuwa Malaika wanateremka katika vivuli vya mawingu ilhali Allah تعالى Anakuja kwa namna Aitakayo.¹ Baadhi ya wasomaji huisoma hivi:

¹ At-Tabari 4:264.

**“Hal yandhuruna illa an - ya’atiahumu Llahu wal malaikatu
fy dhulalin minal ghamami.’**

“Hakuna jingine wanalongojea ila Kuwafikia Mwenyezi Mungu na
Malaika kutoka katika vivuli vya mawingu.”

Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ تَشْقُقُ السَّمَاءُ بِالْغَمِّمْ وَتُرِلَّ الْمَلٰٓئِكَةُ تَنْزِيْلًا ﴿٢٥﴾

**“Na siku zitakapofunguka mbingu kwa mawingu na wateremshwe
Malaika kwa wingi.” (25:25)**

* * *

سَلَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَمَا آتَيْنَهُمْ مِنْ آيَةٍ بَيِّنَةٍ ۖ وَمَنْ يُبَدِّلْ نِعْمَةَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢١١﴾
 زَيْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَيَسْخَرُونَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ وَالَّذِينَ اتَّقَوْا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢١٢﴾ كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّينَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَأَنْزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ فِي مَا اخْتَلَفُوا فِيهِ ۗ وَمَا اخْتَلَفَ فِيهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ ۗ وَاللَّهُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٢١٣﴾ أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ ۗ مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالصَّرَاءُ ۖ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصُرُ اللَّهُ ۗ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾ يَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ ۗ قُلْ مَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ خَيْرٍ فَلِللَّذِينَ وَاللَّذِينَ وَالْأَقْرَبِينَ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢١٥﴾

سَلَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَمَا آتَيْنَهُمْ مِنْ آيَةٍ بَيِّنَةٍ ۖ وَمَنْ يُبَدِّلْ نِعْمَةَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢١١﴾
 زَيْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَيَسْخَرُونَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ وَالَّذِينَ اتَّقَوْا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢١٢﴾

211. "Waulize wana wa Israili: Tumewapa ishara ngapi zilizo wazi? Na anayezibadili neema za Mwenyezi Mungu baada ya kumfikia basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu."

212. "Waliokufuru wamepambiwa maisha ya duniani; na wanawafanyia maskhara walioamini. Na wenye kuchamungu watakuwa juu yao siku ya kiyama. Na Mwenyezi

Mungu Humruzuku Amtakaye bila ya hisabu."

Adhabu kwa Kubadilisha Neema za Allah تعالی na Kuwakejeli Waumini.

Allah تعالی Amewataja Wana wa Israil kuwa walishuhudia ishara nyingi zikithibitisha ukweli wa Mussa عليه السلام kuhusu lile alilotumwa nalo kwao. Walishuhudia mkono wake (ulipotoa mwanga), ulivyopasua bahari, alipopiga mwamba na maji yakabubujika, mawingu yaliyowapa kivuli wakati wa joto kali, *manna* na *salwa*, nk.

Ishara hizi zinathibitisha kuwepo kwa Muumba na ukweli wa Mussa عليه السلام ambaye Ishara hizi zilipitia mkononi mwake. Bado, wengi miongoni mwao walikataa Neema za Allah تعالی na kuchagua kukufuru na kupuuza Neema za Allah تعالی.

وَمَنْ يُبَدِّلْ نِعْمَةَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢١١﴾

“Na anayezibadili Neema za Mwenyezi Mungu baada ya kumfikia basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.”

Kama vile Allah تعالی Alivyowazungumzia makafiri wa Kikureishi:

* أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴿٢١٢﴾ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا وَيُبْسَسُ الْقَرَارُ ﴿٢١٣﴾

“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha Neema za Mwenyezi Mungu kwa kukufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizi? Nayo ni jahannamu! Wataingia. Maovu yaliyoje makazi hayo!” (14:28-29)

Kisha Allah تعالی Alielezea kuwa Ameyafanya maisha ya ulimwengu huu kuwa mazuri kwa makafiri ambao wameridhika nayo na kuyatumainia, ambao wanalimbikiza mali lakini hawaitumii katika njia walizoamrisha kwayo, ambazo zingewapatia radhi za Allah تعالی. Badala yake wanawakejeli waumini ambao wanayapuuza maisha ya dunia na wanatumia kila walichokichuma ili kumridhisha Mola wao. Waumini wanatumia muda mrefu kumuelekea Allah تعالی, na kwa sababu hii wamepata furaha isiyo na kikomo na malipo mazuri katika siku ya hukumu. Kwa hiyo, watanyanyuliwa juu ya makafiri juu ya uwanja wa mkutano, katika kukusanywa kwao wakati wa kufufuliwa na katika makazi ya kudumu. Waumini watakaa katika nafasi ya kudumu na sehemu

iliyo juu, ambapo makafiri watakaa sehemu iliyo chini kabisa motoni. Ndipo Allah تعالى Akasema:

وَاللَّهُ يَرزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢١١﴾

“Na Mwenyezi Mungu Humruzuku Amtakaye bila ya hesabu.”

Aya hii inaonesha kuwa Allah تعالى Anampa riziki yeyote Amtakaye katika waja Wake bila hesabu au kikomo hapa duniani na kisha Akhera. Hadithi imeeleza kuwa (Allah تعالى Amesema).

«ابنِ آدَمَ أَتَيْنُكَ عَلَيْنَا»

“Ewe Mwana wa Adam! Toa (katika njia ya Allah) na Mimi (Allah) Nitakupa matumizi.”¹

Mtume ﷺ amesema:

«أَتَيْنُكَ بِبِلَالٍ وَلَا تَخْشَ مِنْ ذِي الْعَرْشِ إِفْلَاحًا»

“Ewe Bilal! Toa na usichelee kupungukiwa kwani Mmiliki wa Arshi (Allah) Hapungukiwi.”²

Allah تعالى Amesema:

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ^ط

“Na chochote mtakacho kitoa Yeye Atakilipa.” (34:39)

Zaidi ya hayo, Imenukuliwa katika Sahih (kuwa Mtume ﷺ alisema):

«أَنَّ مَلَكَئِنِ يَنْزِلَانِ مِنَ السَّمَاءِ صَبِيحَةً كُلِّ يَوْمٍ يَقُولُ أَحَدُهُمَا: اللَّهُمَّ أَعْطِ مُتَقِيًا خَلْفًا، وَيَقُولُ الْآخَرُ: اللَّهُمَّ أَعْطِ مُنْسِيكَ تَلْفًا»

“Kwamba kila siku asubuhi Malaika wawili huteremka kutoka mbinguni. Basi mmoja wao husema: ‘Ewe Allah! Mpatie badala (kila) mwenye kutumia (kwa lengo la kupata Radhi za Allah).’ Na mwenzake husema; ‘Ewe Allah! ‘Mwangamize (kila) aliye mbahili.’”³

¹ Al-Humaydi 2:459.

² At-Tabari 10:192.

³ Fat’hul Al-Bari 3:357.

Kadhalika imekuja katika Hadithi Sahihi,

«يَقُولُ ابْنُ آدَمَ: مَالِي مَالِي. وَهَلْ لَكَ مِنْ مَالِكَ إِلَّا مَا أَكَلْتَ فَأَنْتَيْتَ، وَمَا لَيْسَتْ فَأَبْلَيْتَ، وَمَا تَصَدَّقْتَ فَأَمْضَيْتَ، وَمَا سِوَى ذَلِكَ فَذَاهِبٌ وَتَارِكُهُ لِلنَّاسِ»

“Mwana wa Adam anasema, ‘Mali zangu, mali zangu!’ (Na huambiwa) ziko wapi mali zako? (Mali zako ni) ulizotumia kwa chakula ukakimaliza, ulizotumia kwa mavazi ukayachakaza na ulizotoa sadaka na hivyo kuziweka katika kumbukumbu zako. Na zisizokuwa hizo utakwenda na utaziacha zitumiwe na watu (warithi).”¹

Imam Ahmad ameeleza katika Musnad kuwa Mtume ﷺ alisema:

«الدُّنْيَا دَارٌ مَنْ لَا دَارَ لَهُ، وَمَالٌ مَنْ لَا مَالَ لَهُ، وَلَهَا يَجْمَعُ مَنْ لَا عَقْلَ لَهُ»

“Dunia (maisha ya dunia) ni makazi ya yule asie na makazi, ni utajiri kwa yule asie na utajiri, na ni mavuno kwa yule asie na akili (ya kutafakari).”²

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّنَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَأَنْزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ فِي مَا اخْتَلَفُوا فِيهِ وَمَا اختلفَ فِيهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَا اختلفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ وَاللَّهُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٢١٣﴾

213. “Watu wote walikuwa ummah mmoja. Mwenyezi Mungu Akapeleka Manabii wabashiri na waonyaji. Na pamoja nao Akateremsha Kitabu kwa haki, ili kihukumu baina ya watu katika yale waliyokhitilafiana. Na wala hawakukhitilafiana ila wale waliopewa Kitabu hicho baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu kwa Idhini Yake Akawaongoa walioamini kwendea haki katika mambo waliyokhitilafiana. Na Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.”

¹ Muslim 4:2273.

² Ahmad 6:71.

Kubishana baada ya kuona ishara zilizowazi ni alama ya ujeuri na kupotoka:

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kuna karne (vizazi) kumi baina ya Adam عليه السلام na Nuh عليه السلام vyote hivyo vilikuwa katika dini ya ukweli. Baadaye watu walikhitilafiana hivyo Allah تعالى Alipeleka Mitume waonyaji na wabashiri wa kheri.” Kisha akasema hivi ndivyo Abdullah alivyosoma Aya hii:

(كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا)⁽¹⁾.

“Watu walikuwa Ummah mmoja kisha wakakhitilafiana.”¹

Al-Hakim alipokea hivyo katika kitabu chake, *Al-Mustadrak*,² halafu akasema, “Isnad yake *Sahih*, lakini (Al-Bukhari na Muslim) hawakuinukuu.” Kadhalika, Abu Jafar Ar-Razi رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Abu Al-Aliyah رضي الله عنه amesema kuwa Ubay bin Kaab alikuwa akiisoma kama hivi,

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّنَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ

“Watu walikuwa Ummah mmoja kisha wakakhitilafiana, na Allah Akapeleka Mitume waonyaji na wabashiri wa kheri.”³

Abdur-Razzaq alisema kuwa Ma'mar alisema kuwa Qatadah alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Watu wote walikuwa Umma mmoja.”

Maana yake: “Wote walikuwa katika muongozo.”

فَاخْتَلَفُوا فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّنَ

“Wakakhitilafiana Allah Akapeleka Manabii.”

Wa kwanza kupelekwa alikuwa Nuh عليه السلام.⁴ Abdur-Razzaq alisema kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَا اَخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِآيَاتِهِ

“Ndipo Mwenyezi Mungu kwa Idhini Yake Akawaongoa walioamini kwendea haki katika mambo waliyokhitilafiana.”

¹ At-Tabari 4:275.

² Al-Hakim 2:546.

³ At-Tabari 4:78.

⁴ Abdur-Razzaq 1:82.

Akasema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«نَحْنُ الْآخِرُونَ الْأَوَّلُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، نَحْنُ أَوَّلُ النَّاسِ دُخُولًا الْجَنَّةَ، بِيَدِ أَنَّهُمْ
أَوْتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِنَا وَأَوْتَيْنَاهُ مِنْ بَعْدِهِمْ، فَهَدَانَا اللَّهُ لِمَا ائْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ
بِأَذْنِهِ، فَهَذَا الْيَوْمَ الَّذِي ائْتَلَفُوا فِيهِ فَهَدَانَا اللَّهُ لَهُ، فَالْنَّاسُ لَنَا فِيهِ تَبِعٌ، فَعَدَا
لِلْيَهُودِ، وَتَعَدَّ غَدٍ لِلنَّصَارَى»

*“Sisi ni Umati wa mwisho, lakini tutakuwa wa kwanza siku ya Kiyama. Sisi ni watu wa kwanza kuingia Peponi, japokuwa Mayahudi na Wakristo walipewa Kitabu kabla yetu nasi tukapewa baada yao. Allah Alituongoa kwenye haki wakati walipokhitilafiana kwa Idhini Yake. Leo (siku ya ijumaa) ndio siku waliyokhitilafiana kwayo, Allah Alituongoa kwayo. Hivyo, watu wanatufuata, kuwa kesho ni ya Mayahudi na kesho kutwa ni ya Wakristo.”*¹

Ibn Wahb alisimulia kuwa Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema kuwa baba yake aliizungumzia Aya hii.

فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَا ائْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِأَذْنِهِ²

“Ndipo Mwenyezi Mungu kwa Idhini Yake Akawaongoa walioamini kuiendea haki katika mambo waliyokhitilafiana.”

Walikhitilafiana kuhusu siku ya Ijumaa. Mayahudi wakaifanya Jumamosi kuwa siku yao, ambapo Wakristo walichagua Jumapili. Allah تعالی Aliuongoza Ummah wa Muhammad ﷺ kwenye Ijumaa. Pia Walikhitilafiana kuhusu Qiblah cha kweli. Wakristo walielekea Mashariki ambapo mayahudi walielekea Bayt Al-Maqdis (Ardhi Takatifu). Allah تعالی Aliuongoza Ummah wa Muhammad ﷺ kwenye Qiblah cha kweli (Ka'bah – Makkah). Walikhitilafiana pia juu ya Sala, kama ambavyo wengine walirukuu, lakini hawakusujudu, ambapo wengine walisujudu bila kurukuu. Na miongoni mwao walikuwa wakisali huku wakizungumza na wengine wakisali huku wakitembea. Allah تعالی Akauongoza Ummah wa Muhammad ﷺ katika usahihi wa jambo hilo. Walikhitilafiana kuhusu funga; baadhi yao walifunga sehemu ya mchana tu na wengine wakafunga kwa baadhi tu ya vyakula. Allah تعالی Akauongoza Ummah wa

¹ Abdur-Razzaq 1:82.

Muhammad ﷺ kwenye usahihi wa jambo hilo. Pia walikhitilafiana kuhusu Nabii Ibrahim عليه السلام. Mayahudi walisema, "Alikuwa Myahudi ambapo Wakristo walisema kuwa alikuwa Mkristo. Allah تعالى Alimfanya *Haniyfan Musliman*. (Hali ya kuwa ameshikamana na Uislamu na kuachana na mila zote). Allah تعالى Akauongoza Ummah wa Muhammad ﷺ kwenye usahihi wa jambo hilo. Pia walikhitilafiana kuhusu Issa عليه السلام; Mayahudi walimkana na wakamzushia mama yake uzushi mkubwa, ambapo Wakristo walimfanya mungu na mwana wa Mungu. Allah تعالى Alimuumba kwa Neno Lake na Kumpa roho. Allah تعالى Aliuongoza Ummah wa Muhammad ﷺ kwenye usahihi wa hilo."¹ Na Kauli Yake:

بِإِذْنِهِ

"Kwa idhini Yake." Maana yake: "Kwa Ujuzi Wake na kwa kile Alichowaongoza nacho, kwa mujibu wa Ibn Jarir رحمه الله تعالى."²

وَاللَّهُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

"Na Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye." Maana yake: Miongoni mwa waja Wake.

إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

"Kwenye njia iliyonyooka." Maana yake: Ni ya Kwake Maamuzi na Hoja Nzito. Bukhari na Muslim wameeleza kuwa Aishah رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alipokuwa akiamka usiku alikuwa akisema:

«اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرَائِيلَ وَمِيكَائِيلَ وَإِسْرَافِيلَ، فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ، أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ، اهْدِنِي لِمَا اخْتَلَفَ فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ، إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ»

*"Ewe Allah, Mola wa (Malaika) Jibril, Mikail na Israfil, Muumba wa mbingu na ardhi na Mwenye Kujua ya ghaibu na yanayoonekana. Unawahukumu waja wako katika yale waliyokhitilafiana, hivyo niongoze katika yale waliyokhitilafiana kwenda kwenye ukweli kwa Idhini Yako. Hakika, Wewe Unamuongoza Umtakaye katika njia iliyonyooka."*³

¹ At-Tabari 4:284.

² At-Tabari 4:286.

³ Muslim 1:534.

Na Dua nyingine ilikuwa;

«اللَّهُمَّ أَرِنَا الْحَقَّ حَقًّا، وَأَرِنَا الْبَاطِلَ بَاطِلًا، وَأَرِنَا اجْتِنَابَهُ، وَلَا تَجْعَلْهُ مُلْتَبِسًا عَلَيْنَا فَتَضِلَّ، وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا»

*"Ewe Allah! Tuoneshe haki kuwa haki, na Utujaalie kuifuata. Na tuonyeshe batili kuwa batili, na Utuwezeshe kuiepuka, na Utubainishie uhalisi na uovu ili tusiende mrama, na Utujaalie tuwe viongozi wa waumini."*¹

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصُرُ اللَّهُ ۗ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ

قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

214. "Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyowajia wale waliopita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa Nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu."

Ushindi na kuingia peponi havipatikani isipokuwa baada ya kufaulu mitihani:

Allah تعالى Amesema:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ

"Mnadhani kuwa mtaingia Peponi."

Kabla hamjatahiniwa na kujaribiwa kama Ummah uliokuwa kabla yenu? Ndiyo sababu Allah تعالى Akasema:

وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ

"Bila kukujieni kama yaliyowajia wale waliopita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara."

¹ Takhrij Al-Ihya 3:1418.

Maana yake: Maradhi, maumivu, machungu, maafa na shida. Ibn Mas'ud, Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah, Mujahid, Said bin Jubayr, Murrah Al-Hamdani, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi, As-Sudi na Muqatil bin Hayyan walisema kuwa:

الْبِئْسَاءُ

“**Shida.**” Maana yake: Ni Ufukara.¹ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa:

وَالصَّرَاءُ

“**Na Madhara.**” Maana yake: Maradhi.

وَزُلُوفًا

“**Na wakatikiswa.**” Kwa kuwaogopa maadui, mtikisiko mkubwa, na walijaribiwa na kupewa mtihani mkubwa. Kama ilivyosimuliwa katika Hadithi sahihi kuwa Khabab bin Al-Aratt رضي الله عنه alisema, “Tulisema, Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa nini hutuombei Dua kwa Allah تعالى?” Akasema:

«إِنَّ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ كَانَ أَحَدُهُمْ يُرْضِعُ الْبَيْتَانِ عَلَى تَفْرِقِ رَأْسِهِ فَيَخْلُصُ إِلَى قَدَمَيْهِ لَا يَضْرِفُهُ ذَلِكَ عَنْ دِينِهِ، وَيُنْشِطُ بِأَمْشَاطِ الْحَدِيدِ مَا بَيْنَ لَحْمِهِ وَعَظْمِهِ، لَا يَضْرِفُهُ ذَلِكَ عَنْ دِينِهِ.»

“Msumeno ulikuwa ukiwekwa katikati ya kichwa cha mmoja wa watu wa kabla yenu (waumini) na kupasuliwa mpaka kwenye miguu yake, lakini hilo halikumtoa katika Dini yake. Na anakwanguliwa kwa chanuo la chuma kati ya ngozi na mifupa hata hivyo hilo halikumwondoa katika Dini yake.” Kisha akasema:

«وَاللَّهِ لَيَمَنَّ اللَّهُ هَذَا الْأَمْرَ حَتَّى يَسِيرَ الرَّايِبُ مِنْ صَنْعَاءَ إِلَى حَضْرَمَوْتِ، لَا يَخَافُ إِلَّا اللَّهَ وَالذُّلْبَ عَلَى غَنَمِهِ، وَلَكِنَّكُمْ قَوْمٌ تَسْتَعْجِلُونَ»

“Wallah! Allah Atatimiza Jambo hili (Dini), mpaka msafiri atasafiri kutoka San'a kwenda Hadhramawt (miji yote ipo Yemen, lakini kuna masafa marefu baina ya sehemu mbili hizo) lakini hataogopa kitu isipokuwa Allah, na mbwa mwitu kwa Kondoo wake. Lakini nyie ni watu wenye haraka.”²

¹ Ibn Abu Hatim 2:616.

² Fat'hul Al-Bari 6:716.

Na Allah تعالى Amesema:

الَّذِينَ أَحْسَبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢١١﴾ وَلَقَدْ فَتَنَّا
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ فَلْيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلْيَعْلَمَنَّ الْكٰذِبِينَ ﴿٢١٢﴾

“Alif Lam Mim (A.L.M) Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema. Tumeamini! Nao wasijaribiwe? Hakika Tuliwajaribu waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walio waongo.” (29:1-3)

Maswahaba walipata mitihani mizito wakati wa vita vya Al-Ahzab. Allah تعالى Amesema:

إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَكَلَّتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ
وَتَنظَّرُونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا ﴿٣٣﴾ هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُونَ وَزُلْزِلُوا زِلْزَالًا شَدِيدًا ﴿٣٤﴾ وَإِذْ
يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ مَّا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٣٥﴾

“Walipokujieni kutoka juu yenu, na kutoka chini yenu; na macho yalipokodoka, na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali. Hapo ndipo Waumini walipo jaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali. Na waliposema wanaafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu.” (33:10-12)

Heraclius alipomuuliza Abu Sufyani, “Mlimpiga vita (Mtume Muhammad)?” Alijibu, “Ndiyo.” Heraclius akasema, “Nini matokeo ya vita baina yenu?” Abu Sufyan akajibu, “Kuna wakati tunashindwa na wakati mwingine tunamshinda.” Akasema, “Hivi ndivyo itokeavyo kwa Mitume, wanajaribiwa lakini mwisho hushinda.”¹ Kauli ya Allah تعالى:

مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِكُمْ

“Bila ya kukujieni kama yaliyowajia wale waliopita kabla yenu?”

Maana yake: Njia yao ya maisha. Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema:

¹ Fat’hul Al-Bari 9:25.

فَأَهْلَكْنَا أَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا وَمَصَّوْا مَثَلُ الْآوَلِينَ ﴿٢١١﴾

“Na Tuliwaangamiza waliokuwa na nguvu kushinda wao. Na mfano wa watu wa zamani umekwisha pita.” (43:8)

Na Kauli Yake,

وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ ۗ

“...na wakatikiswa hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja?”

Walimuomba Allah تعالى Awape ushindi dhidi ya maadui zao na wakamwomba msaada na ukombozi kutokana na mateso na mitihani. Allah تعالى Akasema,

أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٢﴾

“Juwani kuwa Nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.”

Allah تعالى Amesema:

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٢١٣﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٢١٤﴾

“Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.” (94:5-6)

Kadiri shida (tabu) inavyokuwa kubwa basi huteremka nusra inayofanana na shida ilivyo. Ndiyo maana Allah تعالى Akasema:

أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٥﴾

“Jueni kuwa Nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.”

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ ۗ قُلْ مَا أُنْفِقْتُمْ مِنْ خَيْرٍ فَلِلَّوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ وَالْيَتَامَىٰ

وَالسَّكِينِ وَأَبْنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢١٦﴾

215. “Wanakuuliza watoe nini? Sema: kheri mnayoitoa ni kwa ajili ya wazazi na jamaa na mayatima na masikini na wasafiri. Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu Anaijua.”

Kina Nani Wanaostahiki *Nafaqah* (Kuwakimu na kuwapatia sadaka)?

Muqatil bin Hayyan alisema kuwa Aya hii iliteremshwa kuhusu Sadaka.¹ Aya hii ina maana, “Wanakuuliza (Ewe Muhammad) namna wataka - vyotumia.” Waliyasema hayo Ibn Abbas رضي الله عنهما na Mujahid. Naye Allah تعالى Aliwabainishia hili kwa kusema:

قُلْ مَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ خَيْرٍ فَلِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ

“Sema: Kheri mnayoitoa ni kwa ajili ya wazazi na jamaa na mayatima na masikini na wasafiri.”

Maana Yake: Matumizi ni katika namna hiyo. Vile vile, Hadith inaeleza (Wale wanaostahili ukarimu zaidi ni):

«أُمَّكَ وَأَبَاكَ وَأُخْتَكَ وَأَخَاكَ ثُمَّ أَدْنَاكَ أَدْنَاكَ»

*“Mama yako, baba, dada, kaka, ndugu wa karibu kisha wa mbali.”*²

Kuna wakati Maymun bin Mihran aliisoma Aya (2:215) na akatoa maelezo, “Haya ni maeneo yanayohusu kutoa. Allah تعالى Hakutaja miongoni mwao, ngoma, filimbi, vinyago au mapazia ya ukutani.”³

Kisha Allah تعالى Akasema:

وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢١٥﴾

“Na kheri yoyote mnayoifanya Mwenyezi Mungu Anaijua.”

Maana yake: Kheri yoyote mnayoifanya, Mwenyezi Mungu Anaijua na Atakulipeni juu ya hayo, malipo makubwa kabisa, hakuna mtu atakaye-dhulumiwa hata kwa uzito ulio sawa na chembe ndogo kabisa.

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 2:619.

² Al-Hakim 3:611.

³ Ibn Abu Hatim. 2:620.

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كَرْهٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

السَّيِّئِ مِنَ الْقِتَالِ فِيهِ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ بِهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِندَ اللَّهِ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقِتَالِ وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَعُوا وَمَنْ يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَن دِينِهِ فَمَا كَانَ مِنكُمْ عَلَيْهِ مِنْ شَيْءٍ أُولَٰئِكَ هُمُ الْعَاكِفُ بِاللَّهِ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢١٧﴾

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كَرْهٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

216. "Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua na nyinyi hamjui."

Kuwajibishwa kwa Jihadi:

Katika Aya hii, Allah تعالیٰ Amewajibisha Waislam

kupigana Jihadi dhidi ya uovu wa adui waliochupa mipaka dhidi ya Uislam. Az-Zuhri alisema, "Jihad ni wajibu kwa kila mtu, aliye katika uwanja wa vita na hata aliyebaki nyumbani. Yeyote anayebaki nyumbani anapotakiwa msaada anatakiwa atoke haraka kwenda mstari wa mbele na kama hatahitajika atabaki nyumbani." Mimi (Ibn Kathir) nasema, kwa ajili hiyo imethibiti katika Hadithi Sahih kuwa:

«مَنْ مَاتَ وَلَمْ يَغْزُ وَلَمْ يُحَدِّثْ نَفْسَهُ بِالْغَزْوِ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً»

"Yeyote atakayekufa bila kupigana (katika njia ya Allah), wala hakuazimia kupigana, atakufa kifo cha Jahiliyyah."¹

¹ Muslim 3:1517.

Siku ya *Fat-h Makkah* Mtume ﷺ alisema:

«لَا هِجْرَةَ بَعْدَ الْفَتْحِ وَلَكِنْ جِهَادٌ وَبَيْتَةٌ، وَإِذَا اسْتَنْفِرْتُمْ فَانْفِرُوا»

“Hapana Hijrah (kuhama kutoka Makkah kwenda Madinah) baada ya ushindi wa Fat-hu Makkah, bali Jihad na niya. Na kama mtatakiwa kwenda mstari wa mbele basi nendeni.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ كُرْهُ لَكُمْ ط

“Navyo vinachusha kwenu.” Maana yake: “Kupigana ni jambo gumu na zito katika nafsi zenu, kwa hakika, kupigana kama kunavyoelekezwa na Ayah, ni pamoja na kuuwawa, kujeruhiwa, kupambana na maadui na kustahamili mashaka ya safari.” Kisha Allah تعالى Amesema:

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ط

“Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni cha kheri kwenu.” Maana yake: Mapigano hufuatiwa na ushindi, kumtawala adui, kuteka ardhi yao, mali na watu wao.

وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ط

“Na huenda mkakipenda kitu nacho ni cha shari kwenu.” Maana ya Aya hii inaingia katika kila jambo. Kwani mmoja wenu anaweza kupenda kitu, lakini kwa uhakika kikawa kibaya au chenye manufaa naye, kama vile kujizuia kujiunga na Jihad, kwani inaweza kufanya maadui kuchukua nchi na serikali. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anajua na nyinyi hamjui.” Maana yake: Yeye Anajua kuliko nyie mambo yatakavyokuwa baadaye, na yale yenye manufaa nanyi katika maisha ya dunia na Akhera. Hivyo, Mtii Yeye na fuata amri Zake, ili mpate mwongozo wa kweli.

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ط قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ط وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ

بِهِ ط وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجِ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ ط وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ ط وَلَا

¹ Fat’hul Al-Bari 4:56.

يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّى يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَعُوا ۗ وَمَن يَرْتَدِدْ مِنكُمْ عَن
 دِينِهِ فَمَا يَكْفُرْ فَأُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَلُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَأُولَٰئِكَ
 أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢١٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا
 وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَولَٰئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢١٧﴾

217. *“Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu. Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasende katika njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye, na kuzuilia watu wasende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuu. Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika Dini yenu kama wakiweza. Na yeyote katika nyinyi akiacha Dini yake akafa naye ni kafiri, basi hao ndio ambao a'mali zao zimeharibika duniani na Akhera. Na hao ndio watu wa Motoni; humo watadumu.”*

218. *“Hakika wale walioamini na wale waliohama wakapigania njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanaotaraji rehema za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.”*

Kikosi cha Nakhlah, na Sheria ya Kupigana Wakati wa Miezi Mitakatifu

Ibn Abu Hatim رضي الله عنه ameeleza kuwa Jundub bin Abdullah رضي الله تعالى عنه alisema: Mtume ﷺ alikusanya kundi la askari chini ya uongozi wa Sayyidina Abu Ubaidah bin Jarrah رضي الله عنه. Alipokaribia kuanza msafara, alianza kulia kwa kufikiria kumkosa Mtume ﷺ. Hata hivyo, Mtume ﷺ alimpumzisha Abu Ubaydah رضي الله عنه katika kuongoza na akamteua Abdullah bin Jahsh رضي الله عنه badala yake, alimpa maelekezo kwa maandishi na akamuamuru asisome maelekezo hayo mpaka afike eneo fulani. Pia alimwambia Abdullah رضي الله عنه:

«لَا تُكْرِهَنَّ أَحَدًا عَلَى السَّيْرِ مَعَكَ مِنْ أَصْحَابِكَ».

“Usimlazimishe yeyote katika askari wako kuendelea na msafara pamoja nawe.”

Abdullah رضي الله عنه aliposoma maelekezo, alisoma *Istirja* (akisema), **“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake tutarejea,”** na akarejea (2:156) na akasema, “Nimemsikia na ninamtii Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ.” Kisha akawaambia wafuasi wake habari hiyo na akawasomea maelekezo, na watu wawili wakarejea na wengine wakasalia. Baadae kidogo, walimkuta Ibn Al-Hadhrani (mmoja wa Makafiri wa Kikuraishi), wakamwua bila kujua kuwa siku ile ilikuwa mwezi wa Rajab au Jumadal Akhir (ambapo Rajab ni Mwezi Mtukufu). Washirikina wakawaambia Waislam, “Mmeua katika Mwezi Mtukufu.” Kisha Allah تعالى Akateremsha:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ

“Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu Sema: Kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa.”¹

Abdul Malik bin Hisham رحمه الله تعالى, ambaye aliitayarisha *Sirah* (Maelezo kuhusu Maisha ya Mtume ﷺ) alisema kwamba Ziyad bin Abdullah Bakkai alisema kuwa Muhammad bin Is-haq bin Yasar Al-Madani رحمه الله تعالى aliandika katika kitabu chake cha *Sirah*: “Mtume ﷺ alimpeleka Abdullah bin Jahsh bin Ria’b Al-Asadi katika mwezi wa Rajab, baada ya Mtume ﷺ kurejea kutoka vita vya mwanzo vya Badr. Mtume ﷺ alimpa watu wanane kufuatana nao, wote walikuwa miongoni mwa Muhajirina na hawakuwepo Answar. Pia alimpa maelekezo kwa maandishi na akamtaka asiyasome mpaka watembe kwa siku mbili. Abdullah alitakiwa kuwasomea maelekezo na aende kuyatekeleza, lakini asimlazimisha yeyote kufuatana naye.

Maswahaba pamoja na Abdullah bin Jahsh رضي الله عنهم walikuwa miongoni mwa Muhajirina, kutoka kabila la Banu Abd Shams bin Abd Manaf, alikuwepo Abu Hudhaifah bin Utbah bin Rabia bin Abd Shams bin Abd Manaf. Kutoka kwa washirika wao, alikuwepo Abdullah bin Jahsh, ambaye alikuwa kamanda wa kikosi, na Ukkashah bin Mihsan kutoka kabila la Banu Asad bin Khuzaymah. Kutoka kabila la Banu Nawfal bin Abd Manaf, alikuwepo Utbah bin Ghazwan bin Jabir, mmoja wa washiriki wao kutoka kabila la Banu Zuhrah bin Kilab, alikuwepo Sa’d bin Abu Waqqas, kutoka Banu ‘Adi bin Ka’b, alikuwepo, ‘Amr bin Ar-Rabiah, mshirika wao, katika kabila la Ibn Wail. Waqid bin Abdullah bin Abdi Manaf bin Arin bin Tha’laban bin Yarbu kutoka Banu Tamim; na Khalid

¹ Ibn Abu Hatim 2:628.

bin Bukair kutoka kabila la banu Sa'd bin Fihri Layth alikuwa miongoni mwao. Na kutoka kwa Banu Al-Harith bin Fihri alikuwepo Suhail bin Baydhawaa. Abdullah رضي الله عنه alipotembea kwa siku mbili, aliifungua barua na akasoma maelekezo ya Mtume ﷺ, "Ukishayasoma maelekezo haya, nenda na upige kambi Nakhlah kati ya Makkah na At-Taif. Ukiwa hapo iangalie misafara ya biashara ya Maquraish na utujulishe taarifa zao." Alipomaliza kusoma, Abdullah bin Jahsh رضي الله عنه, alisema, "Nimesikia na Nimetii." Kisha akawaambia Maswahaba, "Mjumbe wa Allah ﷻ ameniamrisha niende Nakhlah kuchunguza nyendo za misafara ya biashara ya Makuraish na nimfahamishe khabari zao." Amenizua kumlazimisha yeyote kati yenu kufuatana nami. Hivyo wale wanaotaka kuwa mashahidi, wafuatane nami. wale wasiolipenda hilo, warejee nyumbani, kwa hakika nitatekeleza amri ya Mtume ﷺ." Yeye pamoja na wafuasi wake wote waliendelea na msafara.

Abdullah رضي الله عنه aliingia eneo la Hijaz (Magharibi mwa Arabia) mpaka alipofika eneo linaloitwa Bahran, karibu na Furu'. Wakiwa hapo, Sa'd bin Abu Waqqas na Utbah bin Ghazwan walipoteza ngamia waliyekuwa wakimpanda kwa zamu, walirudi nyuma kumtafuta, ambapo Abdullah bin Jahsh na maswahaba waliobakia waliendelea mpaka wakafika Nakhlah. Kisha msafara wa Makuraish ulipita umebeba vyakula, zabibu kavu, ngozi za wanyama na bidhaa za biashara kwa ajili ya Makuraish. Ndani ya msafara huo alikuwemo Amr bin Hadhrami ambaye jina lake akiitwa Abdullah bin 'Abbad, 'Uthman bin Abdullah bin Al-Mughirah na kaka yake Nawfal bin Abdullah kutoka kabila la Makhzum, na Al-Hakam bin Kaysan, mtumwa aliyeachwa huru wa Hisham bin Al-Mughirah. Walipowaona maswahaba waliogopa na walikuwa karibu yao sana. Lakini walimwona Ukkashah bin Mihsan woga wao ulipungua kwa kuwa alikuwa amenyoa kichwa. Wakasema, "Hawa watu wanataka kufanya Umrah, hivyo msiwaogope."

Maswahaba رضي الله عنهم wakashauriana wao kwa wao. Siku hiyo ilikuwa mwisho wa mwezi mtukufu wa Rajab. Wakaambiana, "Wallah! Kama mtawaachia wapite, wataingia eneo Tukufu na watajihifadhi humo na kama mtawaua, mtakuwa mmewaua katika Mwezi Mtukufu!" Mwanzoni walisita na hawakutaka kuwashambulia. Baadaye wakaanza kujishajiisha na wakaamua kumwua yeyote waliyemmudu miongoni mwa makafiri na kuchukua kila alichokuwa nacho. Hivyo, Waqib bin Abdullah At-Tamimi alimpiga mshale Amr

bin Al-Hadhrami na akamuua. Uthman bin Abdullah na Al-Hakam bin Kaysan walijisalimisha, ambapo Nawfal bin Abdullah alimudu kuwatoroka. Baadaye, Abdullah bin Jahsh na wafuasi wake رضي الله عنهم walirejea Madinah kwa Mtume ﷺ na msafara wa biashara na mateka wawili. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى aliendelea: Nilielezwa kuwa baadhi ya wanafamilia wa Abdullah bin Jahsh walisema kuwa Abdullah alisema kwa wafuasi wake: “Mtume ﷺ atapata Khumsi (1/5) ya mali yote iliyochukuliwa. Hili lilijiri kabla Allah تعالى Kuamrisha khumsi kwa Mjumbe wake kutokana na ngawira ya vita. Hivyo, Abdullah alimtengea khumsi (1/5) ya msafara wa biashara Mtume ﷺ na iliyobaki aliwagawia wafuasi wake.” Ibn Is-haq رحمه الله تعالى pia alisema kuwa, pale kikosi (Sariyah) kiliporejea kwa Mtume ﷺ, aliwaambia.

«مَا أَمَرْتَكُمْ بِقِتَالِ فِي الشَّهْرِ الْحَرَامِ»

“Sikuwaamrisha mpigane wakati wa mwezi mtukufu.”

Akauacha msafara pamoja na mateka wawili bila kuchukua ngawira walizokuja nazo. Mtume ﷺ alipofanya hivyo, askari waliohusika na mashambulizi wakawa na wasiwasi na wakahisi wameangamia, na ndugu zao Waislam wakawakosoa kwa walichofanya. Maquraish wakasema kuwa Muhammad ﷺ na Maswahaba wake walivunja mwiko wa Miezi Mitakatifu na kumwaga damu, wakanyang’anya mali na wakachukua mateka. Waislam ambao walibakia Makkah waliwajibu kwa kusema: Waislam wamefanya hivyo wakati wa mwezi wa Shaabani (ambao sio mwezi Mtakatifu). Wakati huo huo; Mayahudi walifurahishwa na lile lililotokea kwa Mtume ﷺ. Walisema, Amr bin Hadhrami, *Hadhrami* maana yake vita vimefika, na kwamba *Waqid* (bin Abdullah) ambaye ndiye aliyemwua kwamba amewasha moto (kutumia maana za maneno haya kuunga mkono utabiri wao!). watu walipozidi sana kulizungumza jambo hili, Allah تعالى Alimteremshia Mjumbe Wake ﷺ,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ۖ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ۖ وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ

بِهِ ۖ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجِ أَهْلِهِ مِنهُ أَكْبَرُ عِندَ اللَّهِ ۗ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ ۗ

“Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika mwezi mtakatifu, Sema: kupigana vita wakati huo ni dhambi kubwa. Lakini kuzuilia watu wasiende katika njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye,

na kuzuilia watu wasiende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu Wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuu.”

Aya hii ina maana, ‘Kama mliua wakati wa Miezi Mitakatifu, wao (Makafiri wa Kiquraishi) waliwazuia katika njia ya Allah تعالى na wakanikadhibisha. Pia waliwazuia kuingia Msikiti Mtakatifu, na wakawafukuzeni kutoka humo, ambapo nyie ni watu wake,

أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ

“Ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Kuliko kuuu mlikowaua miongoni mwao.’ Pia,

وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ

“Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuu.” Maana yake: “Kujaribu kuwalazimisha Waislam waache Dini yao na warejee kwenye ukafiri baada ya kuwa wameamini, ni uovu mkubwa kwa Allah تعالى kuliko kuuu.”

وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّى يَرُدُّوكُمْ عَنْ دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا

“Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika Dini yenu kama wakiweza.”

Hivyo wataendelea kukufanyieni yaliyo machafu kuliko hilo na makubwa zaidi bila kutubu wala kukoma.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى aliendelea kusema: Qur’an ilipogusia somo hili, na Allah تعالى Akawaletea Waislam nafuu mahali pa majonzi yaliyowapata. Mtume ﷺ alichukua ule msafara wa biashara na wale mateka wawili, Uthman bin Abdullah na Hakam bin Kaysan. Mtume ﷺ alisema:

«لَا تَقْدِيكُمْ مَهْمًا حَتَّى يَفْتَدِمَ صَاحِبَانَا»

“Hatutakubali fidia yenu mpaka maswahaba wetu wawili warudi salama.”

Maana yake: Saad bin Abu Waqqas na Utbah bin Ghazwan, “kwani tuna wasiwasi na usalama wao wakiwa kwenu. Mkiwaua, nasi tutawaua jamaa zenu hawa wawili.”

Baadaye, Saad na Utbah walirejea salama na Mtume ﷺ alikubali fidia ya Maquraish kwa mateka wao. Ama kuhusu Al-Hakam bin Kaysan, alisilimu na Uislam wake uliimarika. Alikuwa na Mtume ﷺ mpaka alipokufa shahidi katika tukio la *Bir Ma'unah* wakati Mtume ﷺ alipowatuma Maswahaba sabini Najd kuwafundisha Uislam, lakini Banu Sulaim waliwaua wote isipokuwa wawili. Ama kuhusu Uthman bin Abdullah, alirejea Makkah na alikufa akiwa kafiri.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى aliendelea: Abdullah bin Jahsh na wafuasi wake رضي الله عنهم walipu- mzishwa na fikra zilizokuwa zikiwadhili, baada ya Qur'an kuteremshwa juu ya somo hili, walitafuta malipo ya wapiganaji (katika Njia ya Allah تعالى), walisema, "Ewe Mtume! Tunataraji kuwa tukio hili litahesabiwa ni vita kwetu, ili tupate malipo ya *Mujahidin*." Kisha Allah تعالى Akateremsha:

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَؤَلِيكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ ۚ

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢١٨﴾

"Hakika wale walioamini na wale waliohama na wakapigania Njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanaotaraji Rehema za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu." (2:218)

Kwa ajili hiyo Allah تعالى Amenyanyua matumaini yao ya kupata lile walilolitarajia.¹

* * *

¹ Ibn Hisham 2:252-255.

* يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ۗ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ
 وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ وَإِنَّهُمَا أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهِمَا ۗ وَيَسْأَلُونَكَ
 مَاذَا يُنْفِقُونَ قُلِ الْغَفْوُ ۗ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١٩﴾ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَيَسْأَلُونَكَ
 عَنِ الَّتِي تَمَنَّى ۗ قُلْ إِصْلَاحٌ لَّهُمْ خَيْرٌ ۗ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ
 فَإِخْوَانُكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ
 لَأَعْتَبْتَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٠﴾ وَلَا تَنْكِحُوا
 الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ ۗ وَلَا مُمْسِكٌ بِعَمْرِهَا كَيْفَ هِيَ مِنَ الْمُشْرِكَةِ
 وَلَا تَعْبَتُمْ لَهَا عُقْبًا ۗ وَلَا تُنكِحُوا الْمُشْرِكِينَ حَتَّىٰ يُؤْمِنُوا ۗ وَلَعَبْدٌ
 مُؤْمِنٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكٍ ۗ وَلَوْ أَعْجَبَكُمْ ۗ أُولَٰئِكَ يَدْعُونَ إِلَى
 النَّارِ ۗ وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَىٰ الْجَنَّةِ وَالْمَغْفِرَةِ بِإِذْنِهِ ۗ وَيُبَيِّنُ
 ءَايَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٢١﴾ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ
 الْمَحْجِصِ ۗ قُلْ هُوَ أَذَىٰ فَاعْتَرِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحْجِصِ ۗ
 وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهَرْنَ ۗ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ
 حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ
 الْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢٢﴾ نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَأَتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ
 شِئْتُمْ ۗ وَقَدِّمُوا لِأَنفُسِكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ
 مُلْقَوَةٌ ۗ وَنَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٢٣﴾

* يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ۗ
 قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ
 وَإِنَّهُمَا أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهِمَا ۗ
 وَيَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ قُلِ الْغَفْوُ ۗ
 كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١٩﴾ فِي الدُّنْيَا
 وَالْآخِرَةِ ۗ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الَّتِي تَمَنَّى ۗ
 قُلْ إِصْلَاحٌ لَّهُمْ خَيْرٌ ۗ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ
 فَإِخْوَانُكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ الْمُفْسِدَ مِنَ
 الْمُصْلِحِ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَعْتَبْتَكُمْ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٠﴾

219. "Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari, Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake. Na wanakuuliza watote nini? Sema: kilicho chepesi. Namna hivi Mwenyezi Mungu Anaku- bainishieni Ayah zake mpate kufikiri.

220. Katika mambo ya dunia na mambo ya Akhera. Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu Anamjua mharibifu na mtengenezaji.

***Na Mwenyezi Mungu Angelipenda Angelikutieni katika udhia.
Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”***

Kuharamishwa Pombe (*Khamr*) Hatua kwa Hatua

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Maysarah alisema kuwa Umar رضي الله عنه wakati mmoja alisema, “Ewe Allah تعالى! Tupe hukumu iliyo wazi kuhusu Ulevi! Allah تعالى Akateremsha Aya ya *Surat Al-Baqarah*:

﴿يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ﴾

“Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: katika hivyo zipo dhambi kubwa...”

Umar رضي الله عنه aliitwa na akasomewa Ayah hii. Bado akasisitiza, “Ewe Allah! Tupe hukumu iliyo wazi kuhusu Ulevi (*Al-Khamr*).” Kisha Ayah hii katika *Surat An-Nisa* ikateremshwa;

﴿يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ﴾

“Enyi mlioamini! Msikaribie Sala hali mmelewa.” (4:43)

Kisha, Ikawa mnadi Sala wa Mtume ﷺ inapokurubia Sala hunadi kwa kusema, “Mtu aliyekunywa Ulevi haruhusiwi kusali.” Umar رضي الله عنه aliitwa tena na akasomewa Aya hii. Bado alisema, “Ewe Allah! Tupe hukumu iliyo wazi kuhusu Pombe (*Al-Khamr*).” Kisha Aya iliyomo katika *Surat Al-Maidah* ikateremshwa. Umar رضي الله عنه aliitwa tena na akasomewa Aya. Alipofikia;

﴿فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ﴾

“Basi je, mmeacha?” (5:91)

Umar رضي الله عنه alisema, “Tumeacha, tumeacha.”¹ Haya pia ni masimulizi yaliyokusanywa na Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai katika vitabu vyao.² Ali bin Al-Madini na At-Tirmidh walisema kuwa isnad ya wapokezi wa Hadithi hii ni sahihi. Tutaitaja Hadithi hii tena pamoja na kile alichokusanya Imam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, Allah تعالى Alivyosema katika *Surat Al-Maidah*,

¹ Ahmad 1:531.

² Abu Daud 4:79, Tuhfatul-Ahwadhi 8:415, An-Nasai 8:287.

إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رَجَسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ

تُفْلِحُونَ ﴿٥٩﴾

“...Bila shaka ulevi, na kamari, na Ansaab,¹ na Azlam², ni uchafu katika kazi za shetani, basi jiepusheni navyo ili mpate kufanikiwa.”
(5:90)

Allah تعالى Amesema:

﴿ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ط

“Wanakuuliza (Ewe Muhammad) juu ya ulevi na kamari.” Ama kuhusu Ulevi (Al-Khamr) Umar bin Khattab رضي الله عنه, kiongozi wa Waumini, alikuwa akisema: “Inahusu vitu vyote vinavyoleweshwa akili.” Tutaitaja kauli hii tena wakati wa kuelezea Surat Al-Maidah, pamoja na mada ya kucheza kamari.³ Allah تعالى Amesema:

قُلْ فِيهِمَا إِتْمٌ كَبِيرٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ

“Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu.” Ama kuhusu dhambi za Ulevi (Khamr) na kamari ni katika upande wa Kidini. Ama manufaa yake ya kidunia, ni pamoja na kunufaisha mwili, kusaga chakula, kuondosha kinyesi, kunoa akili, kulisimua, na kupata fedha kutokana na mauzo. Pia (faida zake ni pamoja na) kupata fedha kutokana na kamari na kuzitumia kwa mahitaji yake binafsi na familia. Lakini manufaa haya yanazidiwa na madhara yaliyo wazi yanayoathiri akili na Dini. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema:

وإِنَّهُمَا أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهِمَا

“Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake.” Aya hii ilikuwa mwanzo wa mchakato wa kuharamisha Khamr - pombe, haikuwa wazi, lakini ilikuwa na maana hiyo. Hivyo Ayah hii aliposomewa Umar رضي الله عنه, bado alisema, “Ewe Allah تعالى! Tueleze hukumu iliyo wazi kuhusu Ulevi “Al-Khamr.” Baadaye kidogo, Allah تعالى Aliteremsha Aya za kuharamisha Ulevi (Khamr) kwa uwazi katika Surat Al-Maidah.

¹ Mahali ambapo wanyama walikuwa wakichinjwa kwa ajili ya asiyekuwa Allah.

² Mishale iliyokuwa ikitumika kupigia ramli.

³ Ahmad 2:351.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ
فِي الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾

“Enyi mlioamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuziieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuswali. Basi je, mmeacha?” (5:90-91)¹

Tutalitaja somo hili, Akipenda Allah تعالى, tutakapoelezea Surat Al-Maidah. Ibn Umar, Ash-Shabi, Mujahid, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas na Abdu-Rahman bin Aslam walisema kuwa Aya ya mwanzo kuteremshwa kuhusu Ulevi ilikuwa:

﴿ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ ﴾

“Wanakuuliza (Ewe Muhammad) juu ya ulevi na kamari. Sema; katika hivyo zipo dhambi kubwa.” (2:219)

Kisha, Aya iliyo katika Surat An-Nisa iliteremshwa (juu ya somo hili) na kisha Aya iliyo katika Surat Al-Maidah ambayo iliharamisha Ulevi.²

Amri ya Kutoa Sadaka kwa Kilichozi Katika Mali

Allah تعالى Amesema:

﴿ وَيَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ قُلِ الْاَعْفَىٰ ﴾

“Na wanakuuliza watoe nini? Sema Vilivyokuzidieni.” Al-Hakam alisema kutoka kwa Miqsam kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii ina maana: Chochote cha ziada baada ya kuikimu familia.³ Hii pia ni Rai ya Ibn Umar, Mujahid, Ata, Ikrimah, Said bin Jubayr, Muhammad bin Ka’b, Al-Hasan, Qatadah, Al-Qasim, Salim, Ata Al-Khurasani na Ar-Rabi bin Anas na wengineo رضي الله عنهم.⁴ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa mtu mmja alisema “Ewe Mjumbe wa Allah! Ninayo Dinar (Sarafu).’ Mtume ﷺ alisema:

¹ Ibn Abu Hatim 2:636.

² At-Tabari 4:331-336.

³ Ibn Abu Hatim 2:656.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:656-657.

«أَنْتِفَعُهُ عَلَى نَفْسِكَ» .

“Itumie kwa ajili yako.” Akasema: Mtume! “Ninayo Dinar (Sarafu) nyingine.” Mtume ﷺ akasema:

«أَنْتِفَعُهُ عَلَى أَهْلِكَ» .

“Itumie kwa ajili ya mkeo.” Akasema, “Ninayo Dinar nyingine.” Akasema:

«أَنْتِفَعُهُ عَلَى وَدَيْكَ» .

“Itumie kwa wanao.” Akasema, “Ninayo Dinar nyingine.” Akasema:

«فَأَنْتَ أَبْصَرُ»

“Wewe unafahamu (namna gani na wapi pa kuitumia sadaka)?”¹

Muslim pia alinukuu Hadith hii katika Sahih yake na alinukuu kuwa Jabir رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alimwambia mtu mmoja:

«ابْدَأْ بِنَفْسِكَ فَتَصَدَّقْ عَلَيْهَا، فَإِنْ فَضَلَ شَيْءٌ فَلِأَهْلِكَ، فَإِنْ فَضَلَ شَيْءٌ عَنْ أَهْلِكَ فَلِذِي قَرَابَتِكَ، فَإِنْ فَضَلَ عَنْ ذِي قَرَابَتِكَ شَيْءٌ فَهَكَذَا وَهَكَذَا»

“Anza kutumia wewe mwenyewe. Iwapo chochote kitabakia tumia kwa ajili ya familia yako. Iwapo kitabaki kitu, wape jamaa zako wa karibu iwapo kitabaki kitu, tumia hivi na vile (toa sadaka katika mambo mbalimbali).”² Kadhalika imekuja katika Hadithi.

«ابْنَ آدَمَ إِنَّكَ أَنْ تَبْدُلَ الْفَضْلَ خَيْرٌ لَكَ، وَأَنْ تُمَسِكَهُ شَرٌّ لَكَ، وَلَا تُلَامُ عَلَى كَفَافٍ»

“Ewe mwana wa Adam! Kwa hakika wewe kutoa kilichozidi matumizi yako ni kheri kwako; lakini ukizuia, itakuwa shari kwako. Hutolaumiwa kwa kuwa na kile kinachokutosha mwenyewe.”³

Allah تعالى Amesema:

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١٩﴾ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Namna hivi Mwenyezi Mungu Anakubainisheni Ayah Zake mpate kufikiri katika mambo ya dunia na mambo ya Akhera.”

¹ At-Tabari 4:340.

² Muslim 2:692.

³ Muslim 2:1036.

Maana yake: Kama Alivyoeleza maamrisha haya kwako, Ameeleza sehemu iliyobaki ya Aya kuhusiana na maamrisha na Ahadi na maonyo Yake; ili muweze kutafakari maisha ya dunia na Akhera. Ali bin Abu Talhah alisema kutoka Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo kuhusu Ayah hii kuwa, “Maana yake: Ni mauti yanayokaribia kutokea na ufupi wa maisha haya, na ukaribu wa kuja maisha ya akhera na kudumu kwake.”¹

Kutunza Mali za Mayatima:

Allah تعالى Amesema:

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْيَتَامَىٰ ۖ قُلْ إِصْلَاحٌ لَهُمْ خَيْرٌ ۖ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَارْحَمُواهُمْ ۚ وَاللَّهُ يَعْلَمُ
الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَعْتَبْتَكُمْ

“Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu Anamjua mharibifu na mtengenezaji. Na Mwenyezi Mungu Angelipenda Angelikutieni katika udhia.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Wakati Aya hii iliposhuka,

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

“Wala msikaribie mali ya mayatima ila kwa njia ya wema kabisa...”
(6:152). Na,

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ

سَعِيرًا

“Hakika wanaokula mali ya mayatima kwa dhuluma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia motoni.” (4:10)

Aya hizi zilipotemshwa, wale waliokuwa wakiwatunza mayatima, walivitenganisha vyakula na vinywaji vyao kando na vinywaji vya mayatima. Vyakula na vinywaji vyao vilipobaki walivihifadhi mpaka walipovila au kuharibika hali hii ilikuwa ngumu kwao mpaka wakamueleza Mtume تعالى.

¹ At-Tabari 4:348.

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْيَتَامَىٰ قُلْ إِصْلَاحٌ لَهُمْ خَيْرٌ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَإِخْوَانُكُمْ^ع

“Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu.”

Kwa ajili hiyo, walivichanganya vyakula na vinywaji vyao pamoja na vyakula na vinywaji vya mayatima.¹ Hadithi hii ilikusanywa pia na Abu Dawud, An-Nasai na Al-Hakim katika Mustadrak wake.² Wengine wengi walisema sawa na hayo kuhusu hali iliyoizingira kuteremshwa kwa Aya (2:220). Ikiwa ni pamoja na Mujahid, Ata, Ash-Shabi, Ibn Abu Layla, Qatadah na wengine miongoni mwa Salaf na waliokuja baada yao.³ Na alisimulia Waqii bin Al-Jarrah kutoka kwa Aisha رضي الله عنها alisema, “Sipendi fedha za yatima ziwe chini ya uangalizi wangu, isipokuwa nitachanganya chakula chake na changu na kinywaji chake na changu.”⁴ Allah تعالى Amesema:

قُلْ إِصْلَاحٌ لَهُمْ خَيْرٌ^ع

“Sema: kuwatengenezea ndio heri.” Maana yake: Kwa upande mmoja (ndivyo inavyotakikana). Kisha Allah تعالى Akasema;

وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَإِخْوَانُكُمْ^ع

“Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu.” Maana yake: Hapana madhara kuchanganya chakula na kinywaji chenu na chakula na kinywaji chao, kwani ni ndugu zenu katika Dini. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema baadaye:

وَاللَّهُ يَعْلَمُ الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ^ع

“Na Mwenyezi Mungu Anamjua mharibifu na mtengenezaji.” Maana yake: Anawajua wenye nia ya kufanya uharibifu na uadilifu. Pia Amesema:

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَعْتَبْتُمْ^ع إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٠﴾

“Na Mwenyezi Mungu Angelipenda Angelikutieni udhia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima.”

¹ At-Tabari 4:350. Sanadi yake ni dhaifu,

² Abu Dawud 3:291, An-Nasai 6:256 na Al-Hakim 2:103.

³ At-Tabari 4:350-353.

⁴ At-Tabari 4:355.

Ali bin Abu Talhah alinakili kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa maana ya Aya hii ni:

وَلَا تَنكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ

“Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini.”

Allah تعالى Amewatoa wanawake wa Watu wa Kitabu katika hukumu hii.¹ Haya pia ni maelezo ya Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Mak-hul, Al-Hasan, Adh-Dhahhak, Zayd bin Aslam na Rabi bin Anas na wengineo.² Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa Ayah hii ni mahsusi kwa wanaoabudu masanamu na sio Watu wa Kitabu, na maana hii ni sawa na ile ya mwanzo tuliyoitaja. Allah ni Mjuzi zaidi.

Abu Jafar bin Jarir (At-Tabari) رحمه الله تعالى alisema, baada ya kutaja makubaliano ya pamoja na wanazuoni (Ijmai) kuwa inaruhusiwa kuoa wanawake kutoka watu wa Kitabu, “Umar رضي الله عنه hakupenda hali hii kwa kuchelea Wanaume wa Kiislam kuacha kuwaoa Wanawake wa Kiislam au kwa sababu zinazofanana na hizo.” Kadhalika Abu Quraib amesimulia kutoka kwa Shaiq kuwa alisema: Wakati mmoja Hudhaifah رضي الله عنه alimuoa mwanamke wa Kiyahudi na Umar رضي الله عنه akamuandikia Hudhaifa رضي الله عنه “Mpe talaka.” Alimjibu, “Je unadai hairuhusiwi kwangu hivyo nimuache?” Akasema. “Hapana lakini nachelea unaweza kuoa mwanamke mchafu miongoni mwao.”³ Sanadi yake ni sahihi. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Zayd bin Wahb alisema kuwa Umar bin Khattab رضي الله عنه alisema, “Mwanamume Muislam anamuoa mwanamke Mkristo, lakini mwanaume Mkristo hamuoi mwanamke Muislam.”⁴ Hadithi hii ina isnadi yenye nguvu kuliko Hadithi iliyotangulia. Ibn Abu Hatimu رحمه الله تعالى⁶ alisema kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alichukia Muislam kuoa mwanamke kutoka watu wa Kitabu. Alitegemea maelezo yake binafsi juu ya Aya:

وَلَا تَنكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ

“Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini.”¹⁵

¹ At-Tabari 4:362.

² Ibn Abu Hatim 2:669-671.

³ At-Tabari 4:66.

⁴ At-Tabari 4:366. Sanadi yake ni dhaifu.

⁵ Ibn Abu Hatim 2:671.

Bukhari pia ameeleza kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Sijui ushirikina mkubwa zaidi kuliko kwa yeye (mwanamke) kusema, Isa ni Mola Wake."¹ Allah تعالى Amesema:

وَلَأَمَةٌ مُّؤْمِنَةٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكَةٍ وَلَوْ أَعْجَبَتْكُمْ

"Na mjakazi Muumini ni bora kuliko mshirikina hata akikupendezeni."

Imenukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«تُنكحُ المرأةُ لأربعٍ: لِمَالِهَا وَلِحَسَبِهَا وَلِجَمَالِهَا وَلِدِينِهَا، فَمَا ظَفَرُ بِذَاتِ الدِّينِ، تَرَبَّتْ بِذَلِكَ»

*"Mwanamke huolewa kwa sifa nne; Utajiri wake, cheo chake, uzuri wake na dini yake. Hivyo oeni wanawake wenye Dini, mkono wako ujazwe mchanga (kauli ya kushajiisha)."*²

Muslim ameeleza Hadithi sawa na hii kutoka kwa Jabir رضي الله عنه.³ Pia Muslim ameeleza kuwa Ibn Amr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«الدُّنْيَا مَتَاعٌ، وَخَيْرُ مَتَاعِ الدُّنْيَا الْمَرْأَةُ الصَّالِحَةُ»

*"Maisha ya Dunia ni starehe, na furaha iliyo bora ya dunia ni mke mwema."*⁴

Na Allah تعالى Amesema,

وَلَا تُنكحُوا الْمُشْرِكِينَ حَتَّىٰ يُؤْمِنُوا

"Wala msiwaozeshe (wanawake) kwa washirikina mpaka waamini."

Maana yake: Msiwaozeshe wanaume Washirikina kwa wanawake waumini. Kauli hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى.

لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهَا

"Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalaliki kwa wanawake Waumini."

¹ Fa'thul Al-Bari 9:326

² Fa'thul Al-Bari 9:35 na Muslim 2:1087

³ Muslim 2:1087

⁴ Muslim 2:1090

Baada ya hapo Allah تعالی Amesema:

وَلَعَبْدٌ مُّؤْمِنٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكٍ وَلَوْ أَعْجَبَكُمْ ۗ

“Na mtumwa Muumini ni bora kuliko mshirikina hata akikupendezeni.”

Aya hii inaonesha kuwa Muumini mwanamume hata akiwa mtumwa wa Kihabeshi, ni bora kuliko mwanaume mshirikina, hata kama alikuwa tajiri au ni mtawala mkubwa.

أُولَئِكَ يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ ۗ

“Hao wanaitia kwenye Moto.” Maana yake: Kuwa na mahusiano na kuchanganyika na makafiri kunapelekea kupenda maisha ya dunia kuliko maisha ya Akhera, na kusababisha matatizo makubwa. Allah تعالی Amesema:

وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَى الْجَنَّةِ وَالْمَغْفِرَةِ بِإِذْنِهِ ۗ

“Na Mwenyezi Mungu Anaitia kwenye Pepo na maghufira kwa Idhini Yake.”

Maana yake: Kwenye Sharia Yake, Maamrishi na Makatazo. Allah تعالی Amesema:

وَيُبَيِّنُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٢٠﴾

“Naye Huzibainisha Ayah Zake kwa watu ili wapate kukumbuka.”

وَدَسَّلُوْنَكَ عَنِ الْمَحِيضِ ۗ قُلْ هُوَ أَذَىٰ فَاعْتَرَلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ ۗ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ

حَتَّىٰ يَطْهَرْنَ ۗ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ

الْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢١﴾ نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَأَتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ ۗ وَقَدِمُوا لِأَنفُسِكُمْ

وَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ مُّلْقَوُهُ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٢٢﴾

222. “Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie, huo ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi. Wala msiwaingilie mpaka Watahirike. Wakisha tahirika basi waendeeni Alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu na Huwapenda wanaojisafisha.”

223. "Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeeni konde zenu mpendavyo. Lakini jitangulizieni kheri nafsi zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kuwa hakika nyinyi mtakutana Naye. Na wape bishara njema waumini."

Makatazo ya kumwingilia mwanamke mwenye Hedhi:

Imam Ahmad alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mayahudi walikuwa wakiwaepuka wake zao waliokuwa kwenye hedhi, hawakula nao, au kuchanganyika nao ndani ya nyumba. Masahaba wa Mtume ﷺ waliuliza kuhusu suala hili na Allah تعالى Akateremsha.

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْمَحِيضِ ۗ قُلْ هُوَ أَذَىٰ فَأَعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ ۗ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ
حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ ۗ

"Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie, huo ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi. Wala msiwaingilie mpaka watahirike."

Mtume ﷺ amesema:

«اصْنَعُوا كُلَّ شَيْءٍ إِلَّا النِّكَاحَ»

"Fanyeni nao kila mlitakalo, isipokuwa tendo la ndoa."

Mayahudi walipoelezwa kuhusu kauli hii ya Mtume ﷺ, walisema, "Mtu huyu ana matatizo gani? kila akisikia taratibu (ada) zetu huzipinga." Kisha Usayd Bin Hudhayyr na Abbad bin Bishr رضي الله عنهما walikuja na wakasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Mayahudi walisema hili na lile, je, tuwaingilie wake zetu (wakiwa katika hedhi?)" Uso wa Mtume ﷺ ulibadilika rangi mpaka tukadhani kuwa alikuwa amewakasirikia. Waliondoka. Baadaye kidogo, Mtume ﷺ aliletewa zawadi ya maziwa, aliwapelekea sehemu ili wanywe. Kwa kitendo hicho tukajua kuwa Mtume ﷺ hakuwakasirikia.¹ Aidha Muslim aliandika Hadithi hii, Allah تعالى Alisema:

فَاعْتَزِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ ۗ

"Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi."

¹ Ahmad 3:132.

Maana yake: Epukeni tupu zao. Mtume ﷺ alisema:

«اضنُّوا كُلَّ شَيْءٍ إِلَّا النِّكَاحَ»

*"Fanyeni nao kila kitu, isipokuwa tendo la ndoa (wanapokuwa katika siku zao)."*¹

Kwa sababu hii, wanazuoni wengi wamesema kwamba mwanamke anapokuwa katika siku zake, inaruhusiwa kumpapasa isipokuwa kumwingilia kimwili. Abu Dawud ameeleza kuwa Ikrimah alipokea kutoka kwa mmoja wa wakeze Mtume ﷺ kuwa Mtume kila alipotaka kumpapasa mmoja wa wake zake wakati wa hedhi alimfunika kwa nguo sehemu zake za siri.²

Abu Jafar bin Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Masruq alikwenda kwa Bi Aishah رضي الله عنها na akamsalimu, na Aishah رضي الله عنها akamjibu salamu. Masruq alisema, "Nataka kukuuliza kitu, lakini naona haya." Akamjibu, "Mimi ni mama yako nawe ni mwanangu." Akasema, "Ni kitu gani anachoruhusiwa kufanya mume kwa mke wake mwenye hedhi?" Alimjibu, "Kila kitu isipokuwa sehemu zake za siri."³ Hii pia ni rai ya Ibn Abbas, Mujahid, Al-Hasan na Ikrimah رضي الله عنهم.

(Mimi Bin Kathir nasema) Mmoja wenu anaruhusiwa kulala na mkewe tandiko moja na kula naye (akiwa katika hedhi). Aishah رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alikuwa akitaka nimwoshe nywele zake wakati nikiwa katika hedhi, alilala juu ya paja langu huku akisoma Qur'an nikiwa kwenye hedhi.⁴ Pia imenukuliwa katika Sahih kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, "Nilipokuwa katika hedhi, nilikuwa nikila kipande cha nyama na kisha nikimpa Mtume ﷺ ambaye aling'ata sehemu ile ile niliyokula. Nilikuwa nikinywa na kumpa Mtume ﷺ ambaye aliweka midomo yake ambapo niliweka mdomo wangu."⁵ Imenukuliwa pia ndani ya Sahih Mbili kuwa Maymunah bint Al-Harith Al-Hilaliyah رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ alipotaka kumtomasa tomasa yeyote miongoni mwa wake zake akiwa katika hedhi, alikuwa akimtaka avae Izar (gaguro)." Maneno haya ni kwa mujibu wa mapokezi ya Bukhari.⁶ Sawa na hayo yalipokelewa kutoka kwa

¹ Muslim 1:246.

² Abu Dawud 1:286.

³ At-Tabari 4:378.

⁴ Fat'hul Al-Bari 1:479.

⁵ Muslim 1:245.

⁶ Fat'hul Al-Bari 1:483, Muslim 1:243.

Aishah رضي الله عنها.¹ Imam Ahmad, Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah wameeleza kuwa Abdullah bin Sa'd Al-Ansari رضي الله عنه alimwuliza Mtume ﷺ, "Nina rufusiwa kufanya nini na mke wangu anapokuwa kwenye hedhi?" Akasema, "Unarufusiwa sehemu iliyo juu ya *Izar*."² Hivyo Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ^ط

"Wala msiwaingilie mpaka wataharike." Inaelezea Kauli Yake,

فَاعْتَرِلُوا أَلْيَسَاءَ فِي الْمَحِيضِ^ط

"Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi."

Allah تعالى Ameharamisha kufanya ngono na mke akiwa katika hedhi, ikiwa na maana jimai inarufusiwa wakati mwingine (atakapokatikiwa na hedhi na akatoharika). Kauli ya Allah تعالى.

فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ^ط

"Wakishataharika basi waendeeni kama Alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu."

Inaonesha katika Aya hii kuwa ni Suna na muongozo kuwaingilia wake baada ya kuoga kisharia. Na Wanazuoni wamekubaliana kuwa mwanamke aoge joshu la faradhi au atayamamu kwa mchanga, kama akishindwa kupata maji, kabla hajarufusiwa kuingiliana kimwili na mume wake, baada ya siku zake za mwezi kwisha. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ^ط

"Mpaka wataharike." Maana yake: Kutokana na damu ile ya mwezi,

فَإِذَا تَطَهَّرْنَ

"Wakishataharika."

Maana yake: Kwa maji. Hii pia ni Tafsiri ya Mujahid, Ikrimah, Al-Hassan, Muqatil bin Hayyan na Al-Lath bin Sa'd na wengine.³

¹ Fat'hul Al-Bari 1:480, Muslim 1:242.

² Ahmad 4:342, Abu Dawud 1:145, Tuhfatul-Ahwadhi 1:415, Ibn Majah 1:213.

³ Ibn Abu Hatim 2:682 - 683.

Uharamu wa Kulawiti - Kumuingilia Mwanamke Kinyume na Maumbile

Allah تعالی Amesema:

مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ

“Alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu.”

Hii inahusu *Al-Farj* (uke) kama walivyoeleza, Ibn Abbas, Mujahid na wanazuoni wengine رضي الله عنهم.¹ Kwa hiyo liwati imeharamishwa, kama tutakavyotilia mkazo baadaye, Allah تعالی Akipenda. Abu Razin, Ikrimah na Adh-Dhahak na wengineo walisema kuwa:

فَأْتَوْهُ بِمِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ

“Basi waendeeni pale Alipokuamrisheni Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wakiwa safi, na sio wakiwa katika hedhi.² Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالی Amesema:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu.”

Kutokana na dhambi hata kama limekariri kosa la kuingilia mke mwenye hedhi.

وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

“Na Huwapenda wanaojisafisha.”

Maana yake: Wale wanojitakasa wenyewe kutokana na uchafu ikiwa ni pamoja na kutomwingilia mke akiwa kwenye hedhi au sehemu zingine zilizokatazwa.

Sababu Iliyofanya Kushuka Kauli ya Allah تعالی: “wake zenu ni konde zenu.”

Allah تعالی Amesema:

نَسَأَوْكُم حَرْثَ لَكُمْ

“Wake zenu ni konde zenu.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo kuwa, “Ina maana mahali pa kubebewa mimba.”³ (kisha Allah تعالی Amesema)

¹ Ibn Abu Hatim 2:684

² Ibn Abu Hatim 2:684, 685

³ At-Tabari 4:397

فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْتُمْ

“Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.”

Maana yake: Kutokea upande mpendao; mbele au nyuma madhali jimai inafanywa kwenye kilango (uke), kama ilivyoeleza Hadithi sahihi.

Al-Bukhari alinukuu kuwa Ibn Al-Munkadir alisema kuwa alimsikia Jabir akisema kuwa Mayahudi walikuwa wakisema kuwa, endapo mtu atamwingilia mkewe kutoka nyuma (ndani ya uke), mtoto atazaliwa akiwa mwenye makengeza. Kisha Aya hii iliteremshwa:

نَسَاؤُكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْتُمْ

“Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeni konde zenu mpendavyo.”¹

Muslim na Abu Dawud, pia waliandika Hadithi hii.²

Ibn Abu Hatim alisema kuwa Muhammad bin Al-Munkadir alisimulia kuwa Jabir bin Abdullah alimweleza kuwa Mayahudi walidai mbele ya Waislam kuwa iwapo mmojawapo atamuingilia mkewe kutokea nyuma (ndani ya uke) watoto wao watakuwa wenye makengeza. Baadae Allah تعالى Akateremsha:

نَسَاؤُكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْتُمْ

“Wake zenu kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.”

Ibn Jurayj (mmoja wa Waandishi wa Hadithi) alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مُضِلَّةٌ وَمُنْذِرَةٌ إِذَا كَانَ ذَلِكَ فِي الْفَرْجِ»

“Kutokea mbele au nyuma, madhali inafanyika ndani ya Farj (uke).”³

Imam Ahmad alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:37

² Muslim 2:1058, Abu Dawud 2:618

³ Ibn Abu Hatim 2:693

نَسَاؤُكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ

“Wake zenu ni konde zenu.”

Hii iliteremshwa kuhusu baadhi ya watu wa Ansar ambao walikuja kwa Mtume na wakamuuliza (juu ya kumingilia mke kutokea upande wa nyuma), akawajibu,

«الَّتِيهَا عَلَى كُلِّ حَالٍ إِذَا كَانَ فِي الْفَرْجِ»

“Muingilie mkeo kama upendavyo, madhali ni ukeni.”¹

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abdullah bin Sabit alisema: Nilikwenda kwa Hafsah bint Abdur-Rahman bin Abubakar رضي الله عنها na akasema, “Nina jambo la kukuuliza lakini naona haya.” Nikamjibu, “Usione haya ewe mtoto wa ndugu yangu.” Akasema kuhusu kuwaingilia wanawake katika tupu ya uke kupitia nyuma, akasema Hafsah رضي الله عنها: Umm Salama رضي الله عنها aliniambia kuwa Ansar walikuwa wakijizuia kuwaingilia wake zao kutokea nyuma (ndani ya uke). Mayahudi walidai kuwa wale waliowaingilia wake zao kwa mtindo huo walizaa watoto waliokuwa na makengeza. Muhajiruna walipofika Madinah waliwaoa wanawake wa Ansar na waliwaingilia (ukeni) kwa kutokea nyuma. Mmoja wa wanawake hao alimkatalia mumewe na akamwambia, “Hutofanya hivyo mpaka niende kwa Mtume ﷺ (na nimuulize kuhusu jambo hili). Alikwenda kwa Umm Salamah رضي الله عنها na akamueleza kile kisa. Ummu Salamah akamwambia, ‘Ngoja mpaka Mtume ﷺ afike. Mtume ﷺ alipofika, Mwanamke wa Kiansari aliona aibu kumwuliza, hivyo aliondoka. Umm Salamah رضي الله عنها alimweleza Mtume ﷺ kisa chote na alisema:

«أَدْعِي الْأَنْصَارِيَّةَ»

“Niitie mwanamke wa Kiansari.”

Aliitwa na alisomewa Aya hii:

نَسَاؤُكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْمٌ

“Wake zenu ni konde zenu basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.”

Akaongeza:

¹ Ahmad 1:268.

«صَمَامًا وَاجِدًا»

“Kwenye kilango kimoja tu (Uke)”¹

Hadithi hii ilikusanywa pia na At-Tirmidh ambaye aliipa daraja la *Hasan*.² An-Nasai ameeleza kuwa Ka’b bin Alqamah alisema kuwa Abu An-Nadhr alisema kuwa alimwuliza Nafi, mtumwa aliyeachwa huru na Ibn Umar رضي الله عنهما, “Watu wanaizungumzia sana kauli yako uliyoisimulia kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما kuwa aliruhusu kuwaingilia wake zao kwa nyuma.” Akasema, “Wameniongopea lakini ngojeni niwaeleze ukweli uliotokea. Ibn Umar رضي الله عنهما wakati mmoja alikuwa anasoma Qur’an nami nilikuwa naye, na akafikia Aya:

نَسَأُوكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْتُمْ

“Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.”

Kisha akaniambia, ‘Ewe Nafi! Je, unajua kisa kuhusiana na Ayah hii?’ Nikamwambia, ‘Hapana.’ Akasema, ‘Sisi Maquraish tulikuwa tukiwaingilia wake zetu kupitia nyuma (ndani ya uke). Tulipohamia Madinah na kuwaoa wanawake wa Ansari, tulitaka kufanya vivyo hivyo. Hawakupenda na wakalifanya kubwa jambo hilo. Wanawake wa Ansari walifuata tabia ya Mayahudi ambao walikuwa wakiwaingilia wake zao huku wamelala kiubavubavu. Kisha Allah تعالى Akateremsha.

نَسَأُوكُمْ حَرَّتْ لَكُمْ فَاتُوا حَرَّتْكُمْ أَنِّي شِعْتُمْ

“Wake zenu ni konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo.”³

Hadithi hii ina isnadi za wapokezi zenye kuaminika .

Imam Ahmad ameeleza kuwa Khuzaymah bin Thabit Al-Khatami رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَسْتَحْيِي اللهُ مِنَ الْحَقِّ - ثَلَاثًا - لَا تَأْتُوا النِّسَاءَ فِي أَعْجَازِهِنَّ»

“Allah Hauonei haya ukweli – alisema mara tatu, msiwalawiti wake zenu.”⁴

¹ Ahmad 6:305.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:322.

³ An-Nasai katika Al-Kubra 5:315.

⁴ Ahmad 5:215.

Hadithi hii ilikusanywa na An-Nasai na Ibn Majah.¹ Abu Isa At-Tirmidhi na An-Nasai wameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَنْظُرُ اللَّهُ إِلَى رَجُلٍ أَتَى رَجُلًا أَوْ امْرَأَةً فِي الدُّبْرِ»

“Allah Hamwangelii (kwa jicho la huruma) mwanaume aliyemlawiti mwanaume mwenzake au mwanamke.”²

Hadithi hii ni *“Hasan Gharib”* kwa mujibu wa At-Tirmidhi. Haya ni masimulizi ambayo Ibn Hibban aliyakusanya katika Sahih yake, ambapo Ibn Hazm alieleza kuwa ni Hadithi sahihi.

Kwa nyongeza, Imam Ahmad ameeleza kuwa Ali bin Talq رضي الله عنه alisema, ‘Mtume ﷺ alikataza kulawiti wanawake, kwani Allah تعالى Hauonei aibu ukweli.’³ Abu Isa At-Tirmidhi pia ameeleza juu ya Hadithi hii na akasema ni *“Hasan”*.

Abu Muhammad Abdullah bin Abdur - Rahman Darimi رحمه الله تعالى aliandika katika Musnad wake kuwa Said bin Yassar Abu Hubab alisema: Nilimuuliza Ibn Umar رضي الله عنهما, “Unasemaje juu ya kumwingilia mwanamke kwa kupitia nyuma?” Akanijibu, ‘Una maana gani?’ Nikasema, “Liwati” Akasema, “Ushasikia kuna Muislamu yeyote anafanya uchafu huo?”⁴ Hadithi hii ina isnadi nzuri ya wapokezi na ni kauli ya wazi ya Ibn Umar رضي الله عنهما ya kuharamisha jambo hilo. Abubakar bin Ziyad Naysaburi رحمه الله تعالى ameeleza kutoka kwa Ismail bin Hisn kutoka kwa Ismail bin Rawhi alisema kuwa alimuuliza Malik bin Anas رحمه الله تعالى, “Unasemaje kuhusu kuwaingilia wanawake kwenye kinyo (kinyume cha maumbile).” Akajibu, “Mbegu haipandwi isipokuwa mahali inapoweza kumea (maana, jimai haifanywi ila sehemu ya mimba)? Fanya ndani ya *Farj* (uke).” Nikasema, “Ewe Abu Abdullah! Watu wanasema kuwa wewe unaruhusu desturi hiyo.” Alisema, “Wananizulia, wanasema uongo.” Huu ndio msimamo thabiti wa Malik رحمه الله تعالى. Pia ni rai ya Sa’d bin Musayyib, Abu Salamah, Ikrimah, Tawas, Ata, Said bin Jubayr, Urwah bin Az-Zubayr, Mujahid bin Jabr, Al-Hasan na wanazuoni wengine wa *Salaf* (masahaba na vizazi viwili baada yao). Wote, pamoja na wanazuoni walio wengi, wamekemea vikali liwati

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 5:316, Ibn Majah 1:619.

² Tuhfatul – Ahwadhi 4:329, An-Nasai katika Al-Kubra 5:320, Sahih Ibn Hibban 6:202.

³ Ibn Hajar alitaja katika Atraf Al-Musnad 4:384. Lakini haimo katika kitabu kilichochapishwa.

⁴ Tuhfatul-Ahwadhi 4:274.

na wengi wao wameiita ni tabia ya ukafiri na haya ndio maoni ya jopo la wanazuoni wa Kiislamu. Allah Amesema:

وَقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ^٤

“Lakini zitangulizieni kheri nafsi zenu.”

Maana yake: Kwa kufanya ibada na huku ukijiepusha na yale Aliyoyakataza Allah تعالى. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema baadaye:

وَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ مُلْغُوهُ^٥

“Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kuwa hakika nyinyi mtakutana Naye.”

Maana yake: Atakuwajibisheni kwa matendo yenu yote.

وَنَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ^٦

“Na wape bishara njema Waumini.”

Maana yake: Wale waliotii maamrishi ya Allah تعالى na wakaacha Aliyoya-haramisha. Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Ata alisema, au alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

وَقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ^٤

“Lakini zitangulizieni kheri nafsi zenu.”

Maana yake: Taja Jina la Allah تعالى, kwa kusema “Bismillah” kabla ya kuanza jimai.¹ Al-Bukhari pia ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ إِذَا أَرَادَ أَنْ يَأْتِيَ أَهْلَهُ قَالَ: بِاسْمِ اللَّهِ، اللَّهُمَّ جَنَّبْنَا الشَّيْطَانَ وَجَنَّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْتَنَا، فَإِنَّهُ إِنْ يُقَدَّرُ بَيْنَهُمَا وَلَدٌ فِي ذَلِكَ، لَمْ يَضُرَّهُ الشَّيْطَانُ أَبَدًا»

“Iwapo mmoja wenu atamuingilia mke wake kisha akasema: “Bismillah” Kwa Jina la Allah. Ewe Allah! Tulinde na Shaytan pia kilinde Utachoturuzuku (mtoto) kutokana na shetani, iwapo watakuwa wameandikiwa kupata mtoto, Shetani hatoweza kumdhuru.”²

¹ At-Tabari 4:417.

² Fat’hul bari 9:136.

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ أَنْ تَبَرُّوا وَتَتَّقُوا
 وَتُضِلُّوهُا بَيْنَ يَدَيْ النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٤﴾ لَا
 يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا
 كَسَبْتُمْ قُلُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٢٥﴾ لِلَّذِينَ يُؤْلُونَ مِنْ
 دَسَائِهِمْ تَرِيصٌ أَرْبَعَةٌ أَشْهُرٌ ۖ فَإِنْ فَأَوْ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ
 ﴿٢٢٦﴾ وَإِنْ عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٧﴾
 وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ۗ وَلَا يَحِلُّ لَهُنَّ
 أَنْ يَكْتُمَنَّ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي أَرْحَامِهِنَّ إِنْ كُنَّ يُؤْمِنَنَّ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ وَنَعُولُهُنَّ أَحَقُّ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَلِكَ إِنْ أَرَادُوا
 إِصْلَاحًا ۗ وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَلِلرِّجَالِ
 عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾ الطَّلَاقُ مَرَّتَانٍ ۖ
 فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ ۗ وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ
 تَأْخُذُوا بِمَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا
 حُدُودَ اللَّهِ ۗ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ
 عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۗ
 وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾ فَإِنْ
 طَلَّقَهَا فَلَا نَحْلُ لَهُ مِنْ بَعْدِ حَتَّى تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ فَإِنْ
 طَلَّقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا إِنْ ظَنَّا أَنْ يُقِيمَا
 حُدُودَ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ
 أَنْ تَبَرُّوا وَتَتَّقُوا وَتُضِلُّوهُا بَيْنَ
 النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٤﴾ لَا
 يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ
 وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا كَسَبْتُمْ قُلُوبَكُمْ ۗ
 وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٢٥﴾

224. "Wala msifanye Jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kuacha kufanya wema na kumchamungu na kupatanisha baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua."

225. "Mwenyezi Mungu Hakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi. Bali Anaku shikeni kwa yanayochuma nyoyo zenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusa-mehe na Mpole."

Makatazo ya kuapa kuacha kufanya amali njema:

Allah تعالى Anaamrisha, "Msitekeleze viapo vyenu

kwa jina la Allah تعالى kuacha amali njema na kukata udugu, iiwapo mtaapa kuachana na hayo. Kama Allah تعالى Asemavyo katika Aya nyingine.

وَلَا يَأْتِلِ أَوْلُوا الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْمُهَاجِرِينَ
فِي سَبِيلِ اللَّهِ^ط وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ^ط

“Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na waliohama kwa njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu Akusameheni?” (24:22)

Kuendelea na viapo vya makosa ni dhambi kwa muapaji kuliko kuvivunja kwa kulipia fidia. Mtume ﷺ amesema: *“Sisi umma wa mwisho ndio tutakaokuwa wa kwanza siku ya kiyama.”*¹ Akasema tena,

«وَاللَّهِ لَأَنْ يَلْجَأَ أَحَدُكُمْ بِبَيْتِهِ فِي أَهْلِهِ أَنْتُمْ لَهُ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ أَنْ يُعْطِيَ كَفَّارَتَهُ الَّذِي
افْتَرَضَ اللَّهُ عَلَيْهِ»

“Wallah! Ni dhambi zaidi kwa Allah mmoja wenu anapotekeleza kiapo chake (kuhusu kuvunja mahusiano) na jamaa zake kuliko (kuvunja kiapo) na kulipa Kafara² kama inavyotakiwa na Allah katika hali kama hizi.”

Hivi ndivyo Muslim alivyoripoti Hadithi hii³ na pia Imam Ahmad.⁴

Ali bin Abu Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kutokana na Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ

“Wala msilifanye Jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio.”

Maana: *“Msile kiapo kwa kukwepa kufanya amali njema iwapo mtafanya viapo hivyo vivunjeni, toeni Kaffarah na fanyeni amali njema.”*⁵ Hili lilisemwa pia na Masruq, Ash-Shabi, Ibrahim An-Nakhai, Mujahid, Tawus, Said bin Jubayr, Ata, Ikrimah, Mak-hul, Az-zuhr, Al-Hasan, Qatadah, Muqatil bin Hayyan, Ar-Rabi bin Anas, Adh-Dhahhak, Ata Al-Khurasani na As-Suddi.⁶

¹ Fat’hul Al-Bari 12:441.

² Fidias. Rejea Surat Al Maida Aya 89.

³ Muslim 3:1276.

⁴ Ahmad 2:317.

⁵ At-Tabari 4:422.

⁶ Ibn Abii Hatim 2:700-702.

Akiunga mkono kauli hii ambayo ni ya Jamhuri, Abu Musa Al-Ash-a'ri رضي الله عنه alinukuliwa ndani ya sahih mbili akisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنِّي وَاللَّهِ إِن شَاءَ اللَّهُ، لَا أَحْلِفُ عَلَى يَمِينٍ فَأَرَى غَيْرَهَا خَيْرًا مِنْهَا إِلَّا أَنْتَ الَّذِي هُوَ خَيْرٌ وَتَحَلَّلْتُهَا»

“Wallahi! Inshaallah, Siapi kufanya kitu na kisha nikaona kitendo kizuri zaidi bali nitafanya kile kilicho bora na kuvunja kiapo changu. Kisha najivua katika dhima hiyo (Kwa kutoa kafara).”¹

Muslim ameeleza kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ حَلَفَ عَلَى يَمِينٍ فَأَرَى غَيْرَهَا خَيْرًا مِنْهَا فَلْيُكْفَرْ عَنْ يَمِينِهِ، وَلْيَفْعَلِ الَّذِي هُوَ خَيْرٌ».

“Yeyote anayeapa kiapo na kisha akaona jambo bora kuliko kiapo chake (analazimika kuvunja yamini yake) kwa kutoa kafara na kufanya amali njema.”²

Viapo vya *Laghw* (Upuuzi):

Allah تعالى Amesema:

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ

“Mwenyezi Mungu Hakushikenki kwa viapo vyenu vya upuuzi.”

Ayah hii ina maana: Allah تعالى Hamuadhibu mja au Kumuwajibisha kwa viapo vya *Laghw* avifanyavyo. Viapo vya *Laghw* havidhamiriwi na ni sawa na maneno ya kawaida ambayo hutamkwa mara nyingi na ulimi bila kudhamiria. Kwa mfano, imenukuliwa katika sahihi mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema.

«مَنْ حَلَفَ فَقَالَ فِي حَلْفِهِ بِاللَّاتِ وَالْعُزَّى، فَلْيُقَلِّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ»

“Yeyote aliyeapa (bila kudhamiria) na akawataja Al-Lat na Al-Uzza (masanamu mawili) katika kiapo chake anatakiwa aseme, “Hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.”

¹ Fat'hul Al-Bari 11:525, Muslim 2:1268.

² Muslim 3:1272.

Mtume ﷺ aliwaeleza maneno haya baadhi ya Waislamu wapya ambao ndimi zao kabla ya Uislamu, zilikuwa zikila kiapo kwa masanamu ya Al-Lat. Kwa hiyo, Mtume ﷺ aliwaamrisha wasome Ikhlas kwa kudhamiria kama walivyotamka maneno haya kwa makosa, (*neni Ikhlas*) lifute *neni* (*ushirikina*). Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema:

وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا كَسَبَتْ قُلُوبُكُمْ

“Bali Anakushikeni kwa yanayochumwa na nyoyo zenu.”

Na katika Aya nyingine:

بِمَا عَقَّدْتُمُ الْأَيْمَانَ

“Kwa mnavyoapa kweli kweli kwa makusudio.” (5:89)

Abu Dawud ameeleza katika mlango wa *laghw*: Viapo vya kipuuzi. Kisha akasimulia kutoka kwa Ata kuhusu kiapo cha kipuuzi amesema: Kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«اللَّغْوُ فِي الْيَمِينِ هُوَ كَلَامُ الرَّجُلِ فِي بَيْتِهِ: كَلًّا وَاللَّهُ، وَبَلَى وَاللَّهُ»

*“Laghw katika yamini ni pamoja na yale ayasemayo mtu nyumbani kwake, kama vile, Hapana, Wallahi, na ‘Ndiyo, Wallahi.’”*¹

Ibn Abu Hatim ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kiapo cha *Laghw* ni pamoja na kuapa ukiwa umekasirika.”²

Pia ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Kiapo cha Laghw ni pamoja na kuapa kuharamisha kilichohalalishwa na Allah, na aina hii haihitajii kaffarah.*”³ Said bin Jubayr naye amepokea kama hivyo.⁴

Katika Mlango wa ‘Kuapa ukiwa na Ghadhabu’, Abu Dawud alisimulia kuwa Said bin Musayyib alisema kuwa; ndugu wawili wa Kiansar walikuwa na urithi na mmoja wao alitaka urithi ugawanywe. Kaka yake akasema, “kama ukinijia tena unanitaka nigawe urithi, basi vyote nilivyo navyo nitavitumia kwa ajili ya mlango wa Ka’bah,” Umar رضي الله عنه akamuambia kuwa, “Ka’bah haihitaji fedha zako. Hivyo vunja yamini yako, toa kafara na patana na nduguyo. Nilimsikia Mtume ﷺ Akisema;

¹ Fat’hul Al-Bari 11:545, Muslim 2:1268.

² Abu Dawud 3:572.

³ Ibn Abu Hatim 2:716.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:715.

«لَا يَمِينُ عَلَيْكَ وَلَا نَذْرَ فِي مَعْصِيَةِ الرَّبِّ عَزَّ وَجَلَّ، وَفِي قَطِيعَةِ الرَّجْمِ، وَفِيمَا لَا تَمْلِكُ»

“Usile yamini dhidi yako mwenyewe, kumuasi Mola, kukata undugu wa damu au kutoa vitu usivyomiliki.”¹

Allah تعالى Amesema:

وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا كَسَبَتْ قُلُوبُكُمْ

“Bali Anakushikeni kwa yanayochuma nyoyo zenu.”

Ibn Abbas, Mujahid na wengine wengi رضي الله عنهم walisema kuwa Ayah hii ina maana kuwa ni kuapa kwa jambo wakati unajua ni uongo. Mujahid na wengine walisema Ayah hii ni sawa na Alivyo sema Allah تعالى:

وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَّدْتُمُ الْأَيْمَانَ

“...Lakini Atakushikeni kwa mnavyoapa kweli kweli kwa makusudio.” (5:89)

Allah تعالى Amesema: (2:225 hapo juu)

وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mpole.”

Maana yake: Ni Mwenye Kusamehe waja Wake na Mpole kwao.

لِّلَّذِينَ يُؤَلُّونَ مِن نِّسَابِهِمْ تَرِيبٌ أَرْبَعَةُ أَشْهُرٍ ط فَإِن فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٢٦﴾ وَإِن عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٧﴾

226. “Kwa wanaoapa kuwa watajitenga na wake zao, wangojee miezi minne. Wakirejea basi Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.”

227. “Na wakiazimia kuwapa talaka basi, Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mjuzi.”

¹ Abuu Daudi 3:581.

Kiapo cha *Iy/laa* na Hukumu zake:

Iy/laa ni aina ya kiapo ambapo mume anaapa kuwa hatomjamii mkewe kwa kipindi fulani, ima chini au zaidi ya miezi minne. Iwapo kiapo cha *Iy/laa* kitakuwa chini ya miezi minne, Mume anatakiwa kusubiri muda wa kiapo kisha ataruhusiwa kuingiliana kimwili na mkewe. Mke anatakiwa awe na subira na hawezi kumtaka mumewe, katika hali hii ya kumaliza kiapo chake kabla ya kwisha muda. Imenukuliwa katika Sahih Mbili kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ aliapa atajitenga mbali na wake zake kwa mwezi mmoja. Kisha akaja chini baada ya siku ishirini na tisa akasema:

"الشَّهْرُ تِسْعٌ وَعِشْرُونَ"

*"Mwezi una siku ishirini na tisa."*¹

Hadithi sawa na hiyo ilisimuliwa na Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه na iliandikwa ndani ya sahih mbili.² Iwapo muda wa *Iy/laa* ni zaidi ya miezi minne, mke anaruhusiwa katika hali hii kumtaka mumewe baada ya kwisha miezi minne, amalize *Iy/laa* na amwingilie kimwili. Vinginevyo ampe talaka, kwa kulazimishwa na mamlaka katika shauri hili, ili mke asidhurike. Allah تعالى Amesema:

لِّلَّذِينَ يُؤَلُّونَ مِن نِّسَائِهِمْ

"Kwa wanaoapa kuwa watajitenga na wake zao."

Maana yake: Wanaoapa kutofanya jimai na wake zao. Ayah hii inaonesha kuwa *Iy/laa* inawahusu wake na sio vijakazi, hivyo ndivyo walivyokubaliana wanazuoni wengi (Jamhuri).

تَرِيصُ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ^ط

"Wangojee miezi minne."

Maana yake: Mume anangoja kwa miezi minne kuanzia alipoapa na kisha humaliza *Iy/laa* (endapo kiapo kilikuwa kwa miezi au zaidi) na anahitajika kurejea kwa mke wake au kumpa talaka. Hii ndiyo sababu Allah تعالى Alisema baadaye.

فَإِن فَآءُوا

"Wakirejea basi."

¹ Fat'hul Al-Bari 8:380, Muslim 2:1113.

² Fat'hul Al-Bari 4:143, Muslim 2:1110.

Maana yake: Wakirudisha mahusiano ya kawaida ya kuingiliana na mke wake. Hii ni tafsiri ya Ibn Abbas, Masruq, Ash-Sha'bi, Said bin Jubayr na Ibn Jarir.¹

فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٢٤﴾

“Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye Kusamehe na Kurehemu.”

Pamoja na upungufu uliotokea kuhusu haki za mke kwa sababu ya kiapo cha *lylaa*. Allah تعالى Amesema:

وَإِنْ عَزَمُوا الطَّلَاقَ

“Na wakiazimia kuwapa talaka basi.”

Huu ni uthibitisho kuwa talaka haitokei mara tu inapopita miezi minne (wakati wa *lylaa*). Malik ameeleza kutoka kwa Nafi kuwa Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “Iwapo mume ataapa *lylaa* kwa mkewe, hali hiyo haimaanishi kuwa ni Talaka, hata kama miezi minne itapita. Hadi atakapobainisha, ima aendelee na mkewe au amwache.² Al-Bukhari pia ameeleza Hadithi hii.³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Suhayl bin Abu Salih alisema kuwa baba yake alisema, “Niliwauliza Masahaba kumi na wawili kuhusu mwanamume anayefanya *lylaa* na mke wake. Wote wameeleza kuwa hatakiwi kufanya kitu mpaka miezi minne ipite na kisha anaweza kubaki naye au kumwacha.”⁴ Ad-Daraqutni pia ameeleza kutoka kwa Suhayl.⁵

(Mimi bin Kathir nasema) Aidha imenukuliwa kutoka kwa Umar, Uthman, Ali, Abu Ad-Dardai, Aishah, Ibn Umar na Ibn Abbas رضي الله عنهم. Hii pia ni rai ya Said bin Mussayib, Umar bin Abdul-Aziz, Mujahid, Tawus, Muhammad bin Ka'b na Al-Qasim رضي الله عنهم.

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَضْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ۚ وَلَا يَحِلُّ لَهُنَّ أَنْ يَكْتُمَنَّ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي
أَرْحَامِهِنَّ إِنْ كُنَّ يُؤْمِنُنَّ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ وَتُعْوَظُهُنَّ أَحْقُ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَلِكَ إِنْ أَرَادُوا
إِصْلَاحًا ۚ وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْنَّ بِالْعُرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْنَّ دَرَجَةٌ ۚ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٥﴾

¹ At-Tabari 4:466, 467.

² Al-Muwatta 2:556.

³ Fat'hul Al-Bari 9:335.

⁴ At-Tabari 4:493.

⁵ Ad-Daraqutni 4:61.

228. “Na wanawake walioachwa wangoje peke yao mpaka t’ahara (au hedhi) tatu zipite. Wala haiwajuzii kuficha alichoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya suluhu. Nao wanawake wanayo haki kwa sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima.”

Ubainifu wa Eda ya Mwanamke Aliyeachwa

Aya hii ina amri ya Allah ﷻ kwa wanawake walioachwa na waume zao miongoni mwa wale ambao bado wanapata siku zao za mwezi iwapo kama wamejamiwa. Anatakiwa asubiri (akae eda) kwa muda wa tohara tatu (*Quru-u*) yaani akae miezi mitatu baada ya talaka na kisha ni ruhusa kuolewa na mume mwingine kama akipenda.

Maana ya *Al-Quru-u*

Ath-Thaur رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Alqamah alisema: Tulikuwa na Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akaja mwanamke na kusema, “Mume wangu aliniacha kiasi cha hedhi moja au mbili zilizopita. Kisha alirejea kwangu nilipokuwa nimeandaa maji ya kuoga, nimevua nguo na nimefunga mlango.” Umar رضي الله عنه alimuuliza Abdallah bin Mas’ud رضي الله عنه, “Unaonaje?” Akajibu, “Nadhani bado ni mkewe madhali bado haruhusiwi kuswali (mpaka hedhi ya tatu iishe kabla hajamrejea).” Umar رضي الله عنه naye alisema; ‘Nami naona hivyo hivyo.’¹ Hii pia ni rai ya Abubakar As-siddiq, Umar, Uthman, Ali, Abu Dardai, Ubadah bin as-Samit, Anas bin Malik, Ibn Masud, Muadh, Ubbay bin Ka’b, Abu Musa Al-sh’ari na Ibn Abbas رضي الله عنهم. Zaidi ya hayo hii ni rai ya Said bin Musayyib, Al-Qamah, Aswad, Ibrahimu, Mujahid, Ata, Tawus, Said bin Jubayr, Ikrimah, Muhammad bin Sirin, Al-Hassan, Qatadah, ash-Shabi, Ar-Rabi, Muqatil bin Hayyan, a-Suddi, Mak’hul, Adh-Dhahhak na Ata Al-Khurassani. Wote walieleza kuwa *Quru-u* ni kipindi cha hedhi. Ushahidi wa hili ni Hadithi ambayo Abu Dawud na An-Nasai wameeleza kuwa Fatimah binti Abu Hubaish رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alimuambia;

¹ At-Tabari 4:502.

«دَعِيَ الصَّلَاةَ أَيَّامَ أَقْرَانِكَ»

“Msiswali mkiwa katika Aqra (Wingi wa Quru-u) kipindi cha hedhi yake.”¹

Kama Hadithi hii ilikuwa sahihi, ingekuwa ushahidi ulio wazi kuwa *Quru-u* ni siku ya hedhi. Hata hivyo, mmoja wa wasimulizi wa Hadithi hii, Al-Mundhir, hafahamiki (katika Istilahi za Hadithi), kama Abu Hatim رحمه الله تعالى alivyosema, japokuwa Ibn Hibban رحمه الله تعالى alimtaja Al-Mundhir ndani ya kitabu chake *Ath-Thiqat*.

Kauli ya mwanamke kuwa yupo hedhini au katika tohara ndiyo inayochukuliwa

Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَحِلُّ هُنَّ أَنْ يَكْتُمَنَّ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي أَرْحَامِهِنَّ

“Wala haiwajuzii kuficha Alichoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao.”

Maana yake: Ujauzito wa kipindi cha hedhi. Hii ni tafsiri ya Ibn Abbas, Ibn Umar, Mujahid, Ash-Shabi, Al-Hakam bin Utaybah, Ar-Rabi bin Anas, Adh-Dhahhak na wengine رضي الله عنهم.²

Kisha Allah تعالى Amesema:

إِنْ كُنَّ يُؤْمِنَنَّ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ^ع

“Ikiwa wanamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.”

Aya hii inawaonya wanawake dhidi ya kuficha ukweli (wanapokuwa waja wazito au katika hedhi), ikionesha kuwa wao pekee ndio wajuao ukweli wa nafsi zao. Kwa kuwa kuthibitisha masuala haya si rahisi, Allah تعالى Aliwaachia wenyewe waamue. Hata hivyo, wanawake walionywa wasifiche ukweli endapo wanataka kumaliza *Iddah* mapema au baadaye, kwa mujibu wa utashi wao. Hivyo wanawake waliamrisha kusema ukweli (kama walikuwa waja wazito au kwenye hedhi) wasizidishe wala wasipunguze.

¹ Abu Dawud 1:191, An Nasai 6:211.

² Ibn Abu Hatim 2:744, 745.

Katika Kipindi cha *Idda*, Mume Ndie Mwenye Haki ya Kumrejea Mke Aliyemuacha:

Allah تعالى Amesema:

وَبُعُولَتُهُنَّ أَحَقُّ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَلِكَ إِنْ أَرَادُوا إِصْلَاحًا

“Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya suluhu.”

Hivyo, mume anayemwacha mke wake anaweza kumrejea, ili mradi bado yuko kwenye *Iddah* na kuwa nia yake, ya kumrejea, ni ya uadilifu na anataka kuyarejesha mambo katika hali yake, hukumu hii inatumika katika Talaka Rejea. Tunalazimika kutaja kuwa wakati Aya 2:228 iliposhuka, sheria ya talaka tatu hazimruhusu mume kumrejea mke ilikuwa bado kushushwa. Hapo mwanzo, mume alikuwa akimwacha mke na kumrejea hata kama alimwacha talaka mia kwa nyakati tofauti. Baada ya hapo, Allah تعالى Aliteremsha Aya (2:229) ambayo ilifanya talaka iwe ni mara tatu tu. Kwa hiyo kukawa na talaka tatu, ambazo haifai kumrejea mke. Na Talaka Rejea ambazo ni kuanzia Talaka moja na mbili tu.

Haki za mume na mke:

Allah تعالى Amesema:

وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ

“Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao.”

Aya hii inaonesha kuwa mke ana haki juu ya mume wake, kama naye alivyo na haki juu mkewe, na kila mmoja anawajibika kumpa mwenza haki zake.

Muslim ameeleza kuwa Jabir alisema kuwa Mtume ﷺ alisema katika *Hijjat Al-Wadaa*: Hija yake ya mwisho.

«فَاتَّقُوا اللَّهَ فِي النِّسَاءِ، فَإِنَّكُمْ أَخَذْتُمُوهُنَّ بِأَمَانَةِ اللَّهِ، وَاسْتَحْلَلْتُمْ فُرُوجَهُنَّ بِكَلِمَةِ اللَّهِ، وَلَكُمْ عَلَيْهِنَّ أَنْ لَا يُوطِئَنَّ فُرُوسَكُمْ أَحَدًا تَكْرَهُونَهُ، فَإِنْ فَعَلْنَ ذَلِكَ فَاضْرِبُوهُنَّ ضَرْبًا غَيْرَ مُبْرَحٍ، وَلَهُنَّ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ»

“Mcheni Allah kuhusu wake zenu, kwani mmewachukua kwa amana ya Allah na mkahalalishiwa uke wao kwa neno la Allah. Haki yenu

juu yao, wasimruhusu yeyote msiyempenda kukaa juu ya busati zenu. Na wakivunja amri wapigeni kwa kitu laini kisichojeruhi. Wao pia wana haki ya kupewa matumizi na mavazi kwa kiasi cha kutosha.”¹

Bahzi bin Hakim alisema kuwa Muawiyah bin Haydah Al-Qushayshi alisimulia kuwa babu yake alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ipi haki ya mke wa mmoja wetu?” Mtume ﷺ alisema:

«أَنْ تُطْعِمَهَا إِذَا طَعِمْتَ، وَتَكْسُوَهَا إِذَا اكْتَسَبْتَ، وَلَا تَضْرِبَ الْوَجْهَ، وَلَا تُقْبِحَ، وَلَا تَهْجُرَ إِلَّا فِي الْبَيْتِ»

“Kumlisha unapokula, mnunulie nguo unapojinunulia zako na kujizuia kumpiga usoni, kumtukana au kukaa mbali naye isipokuwa katika nyumba moja.”²

Wakisimulia kutoka kwa Bashir bin Sulayman kuwa Ikrimah alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Napenda kujipamba kwa ajili ya mke wangu kama ninavyopenda mke wangu ajipambe kwa ajili yangu. Hii ni kwa sababu Allah تعالى Anasema:

وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْنَ بِالْمَعْرُوفِ³

“Nao wanawake wanayo haki kwa sharia kama ile haki iliyo juu yao.” Kauli hii imenukuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى.³

Daraja ya Wanaume juu ya Wanawake:

Allah تعالى Anasema:

وَلِلرِّجَالِ عَلَيْنَ دَرَجَةٌ⁴

“...Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao.”

Aya hii inaonesha kuwa wanaume wana daraja zaidi kuliko wanawake kimaumbile pia kitabia, cheo, utiifu, matumizi na kushughulikia masuala mbalimbali, katika maisha ya dunia na Akhera.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

¹ Muslim 2:886.

² Abu Dawud 2:606.

³ At-Tabari 4:532, Ibn Abu Hatim 2:750. Ibn Abuu Shaiba (1908)

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ وَبِمَا أَنْفَقُوا مِنْ
أَمْوَالِهِمْ

“Wanaume ni wasimamizi wa wanawake, kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi, na kwa mali yao wanayoyatoa...” (4:34)

Na Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

Maana yake: Mwenye Nguvu katika Kuwaadhibu walioasi na kupinga Maamrisha Yake na Mwenye Hekima katika Yale Anayoamrisha, Kufaradhisha na Kuyatungia sheria.

الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ ۗ وَلَا تَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا
ءَاتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۗ وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ
فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾ فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِنْ بَعْدُ حَتَّىٰ تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ
فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا إِنْ ظَنَّا أَنْ يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ
يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

229. “Talaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri. Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kuwa hawateza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiikiuke. Na watakao ikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhaalimu.”

230. “Na kama amempa talaka ya tatu basi si halali kwake baada ya hizo mpaka aolewe na mume mwengine. Na akiachwa basi

hapana ubaya kwao kurejeana wakiona kuwa watashikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu Anayoibainisha kwa watu wanaojua."

Kwa nini talaka ni tatu tu na talaka rejea ni ipi? na Bain ni ipi?:

Aya hii Tukufu ilifuta yaliyotangulia mwanzoni mwa Uislamu, wakati mume alikuwa na haki ya kumrejea mkewe aliyemwacha hata kama alimuacha mara mia moja, madhali alikuwa hajamaliza *Iddah*. Hali hii ilikuwa na madhara kwa wake, na kwa sababu hii Allah تعالى Alifanya talaka iwe mara tatu, ambapo mume anaruhusiwa kumrejea mke wake baada ya talaka ya mwanzo na ya pili, kama Allah تعالى Alivyosema:

الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ ط فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ ط

"Talaka ni mara mbili, Kisha ni kukaa kwa wema na kuachana kwa vizuri."

Katika Sunani yake, Abu Dawud aliandika mlango: "Kumrejea mke baada ya talaka tatu ni hukumu iliyofutwa." Ilinukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa maana ya Aya hii;

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ط وَلَا سِحْلٌ لَهُنَّ أَنْ يَكْتُمْنَ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي أَرْحَامِهِنَّ ط

"Na wanawake walioachwa wangoje peke yao mpaka tohara (au hedhi) tatu zipite, wala haiwajuzii kuficha Alichoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao." (2:228)

Mume alikuwa na haki ya kumrejea mkewe hata kama alimuacha Talaka tatu. Allah تعالى Aliifuta na kusema:

الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ ط

"Talaka ni mara mbili."¹

Hadithi hii pia ilikusanywa na An-Nasai.² Ibn Abu Hatim ameeleza kuwa Urwah alisema kuwa mume alimwambia mke wake, "Sitokuacha wala sitokurejea."

¹ Abu Dawud 2:644.

² An-Nasai 6:212.

Akamuuliza, “Vipi?” Akajibu, “Nitakupa talaka na muda wako wa *Iddah* ukikaribia kwisha, nitakurejea. (Mke) alikwenda kwa Mtume ﷺ na akamweleza yaliyojiri.” Na Allah تعالى Aliteremsha:

أَلطَّلِقُ مَرَّتَانِ^١

“Talaka ni mara mbili.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى pia ameeleza Hadithi hii katika Tafsiri yake.² Allah تعالى Amesema:

فَأِمْسَاكِ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٍ بِإِحْسَانٍ^٢

“Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri.”

Maana yake: Ukimwacha talaka moja au mbili, una khiyari kumrejea, endapo atakuwa bado kwenye *Iddah*, ukimfanyia wema na kusuluhisha mtafaruku. Vinginevyo asubiri kwisha kwa *Iddah*, na talaka itakuwa imefikia mwisho, na umwache aende zake kwa usalama, bila kumdhuru au kumdhulumu. Ali bin Abu Talhah ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: “Mtu anapompa mkewe talaka mbili, amwogope Allah تعالى, kuhusu talaka ya tatu. Amrejee awe naye amtunze kwa wema au amruhusu kwa wema aende zake bila kumpora haki zake.”³

Makatazo juu ya Kuomba Kurejeshewa Mahari:

Allah تعالى Amesema:

وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا

“Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu.”

Maana yake: Hamruhusiwi kuwabughudhi au kuwashinikiza wake zenu wajikomboe kwa kurudisha mahari mlizowapa au nusu yake. Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَآءِ آتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُبِينَةٍ^٣

“Wala msiwadhikishe ili muwapokonye baadhi ya mlivyowapa isipokuwa wakifanya uchafu ulio wazi.” (4:19)

¹ Ibn Abu Hatim 2:754.

² At-Tabari 4:539.

³ At-Tabari 4:543.

Hata hivyo, ni ruhusa endapo mke atarudisha chochote kwa moyo mkunjufu, kisha Allah تعالى Akaizungumzia hali hii:

فَإِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِيئًا مَّرِيئًا ﴿٤﴾

“Lakini wakikutunukieni kitu katika mahari kwa radhi yao, basi kileni kiwashuke kwa raha.” (4:4)

Ruhusa ya Kujivua Mwanamke katika Ndoa (*khulu’u*) na Kurejesha Mahari

Endapo mume na mke watakuwa na ugomvi usiosuluhishika, ambapo mke anapuuza haki za mume, anamchukia na hawezi kuendelea kuishi naye, anaruhusiwa kujikomboa (kutoka katika ndoa) kwa kurejesha alivyopewa na mume (zawadi na mahari). Si dhambi kwa mume au mke kupokea. Ndio sababu Allah تعالى Amesema:

وَلَا حَيْلَ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ^ط

فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ^ط

“Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kuwa hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu hapo itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa.”

Kuna wakati, mwanamke hana sababu ya kisheria na bado anataka talaka kwa hali hiyo, Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliripoti kutoka kwa Thawban رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَيُّمَا امْرَأَةٍ سَأَلَتْ زَوْجَهَا طَلَاقًا فِي غَيْرِ مَا بَأْسٍ، فَحَرَامٌ عَلَيْهَا رَائِحَةُ الْجَنَّةِ»

“Mwanamke yeyote anayem dai mumewe talaka katika pasipokuwa na ubaya, mwanamke huyo hatoonja harufu ya pepo.”¹

At-Tirmidhi alinukuu Hadithi hii na akaitaja kuwa *Hasan*.²

¹ At-Tabari 4:569.

² Tuhfatul-Ahwadhi 4:367.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Aya (2:229) iliteremshwa kumhusu Thabit bin Qays bin Shammas na mkewe Habibah bint Abdullah bin Ubayy bin Salul.¹ Katika Muwatta, Imam Malik رحمه الله تعالى ameeleza kuwa Habibah bint Sahl Al-Ansariyah رضي الله عنها aliolewa na Thabit bin Qays bin Shammas رضي الله عنه. Mtume ﷺ wakati mmoja alienda kuswali *Alfajr* na akamkuta Habiba bint Sahl رضي الله عنها mlangoni kwenye kiza. Mtume ﷺ akauliza, "Huyu ni nani?" Akajibu,

«هَذِهِ حَبِيبَةُ بِنْتُ سَهْلٍ قَدْ ذَكَرْتُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَذَكَّرَ».

"Huyu ni Habiba bint Sahl, ameyasema yale aliyosahilishiwa na Allah kuyasema"

Akajibu, "Mimi na Thabit bin Qays رضي الله عنه wapi na wapi." Akiwa na maana (hawezi kuendelea kuwa naye). Thabit bin Qays alipokuja, Mtume ﷺ alimuambia: "Huyu hapa Habiba binti Sahli, kwa Uwezo Wake Allah تعالى amekushitakia tabia yako kiasi alichojaaliwa." Habiba رضي الله عنها akasema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Kila alichonipa nimekihifadhi kwangu.' Mtume ﷺ akasema kumuambia Qays رضي الله عنه:

«أُحِذُّ مِنْهَا»

"Vichukue kutoka kwake." Akachukua mali yake kutoka kwa mke, naye mke alibaki anaishi na familia yake.² Hadithi hii ilinukuliwa na Ahmad, Abu Dawud, na An-Nasai.³ Al-Bukhari ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa mke wa Thabit bin Qays bin Shammas رضي الله عنه alikuja kwa Mtume ﷺ na akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Siitoi dosari dini yake wala tabia yake. Lakini nachelea kufanya vitendo vya Ukafiri (kwa kudharau haki zake)." Mtume ﷺ alisema:

«أَتُرُدِّينَ عَلَيَّ حَدِيثَهُ؟»

"Je, utamrejeshea bustani yake?"

Alisema, "Ndiyo". Mtume ﷺ akasema:

«اقْبَلِ الْحَدِيثَ وَطَلِّقْهَا تَطْلِيقًا»

*"Chukua bustani na mpe talaka moja."*⁴

An-Nasai pia aliandika, (6:169)

¹ At-Tabari 4:556.

² Al-Muwatta 2:564.

³ Ahmad 6:433, Abu Dawud 2:667, An-Nasai 6:169.

⁴ Fat'h Al-Bari 9:306.

Iddah ya Khulu'u - Eda ya Mke Aliyekomboa kwa Mumewe

At-Tirmidhi ameeleza kuwa Rubayi bint Muawwidh bin Afra رضي الله عنها aliji *Khulu'u* (kujikomboa kutoka kwa mume) zama za Mtume ﷺ na Mtume ﷺ alimuamuru akae *Iddah* ya hedhi moja.¹

Kuchupa Mipaka ya Allah تعالى ni Dhulma:

Allah تعالى Amesema:

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾

“Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiikiuke, na watakaokiuka mipaka ya Mwenyezi, hao ndio madhalimu.”

Hii ina maana kuwa Sharia ambazo Allah تعالى Ameziamrisha, ndiyo mipaka Aliyoweka, hivyo msiichupe. Hadithi sahihi inaeleza:

«إِنَّ اللَّهَ حَدَّ حُدُودًا فَلَا تَعْتَدُوهَا، وَفَرَضَ فَرَائِضَ فَلَا تُضَيِّعُوهَا، وَحَرَّمَ مَحَارِمَ فَلَا تَنْتَهِكُوهَا، وَسَكَتَ عَنْ أَشْيَاءَ رَحْمَةً لَكُمْ مِنْ غَيْرِ نَسْيَانٍ فَلَا تَسْأَلُوا عَنْهَا»

“Allah Ameweka mipaka, hivyo msiipindukie, na ametoa maamrisha, hivyo msiyadharau na kuyaharamisha baadhi ya mambo msiyaendee mambo hayo, na ameyanyamazia baadhi ya mambo basi msiyafanye, na ameyanyamazia mambo bila kuyawekea sharia kwa kuwahurumia, sio kwa sababu Aliyasahau, basi msiulizie khabari zake.”²

Kutoa Talaka Tatu kwa Pamoja ni Haramu:

Ayah hii ya mwisho tuliyoitaja ni ushahidi tosha wa kuthibitisha kuwa haijuzu kutamka Talaka tatu kwa pamoja. Kinachothibitisha zaidi sheria hii ni kuwa Mahmud bin Labid alisema – kama An-Nasai alivyoandika katika Sunan yake kuwa Mtume ﷺ alimzungumzia mtu aliyemtamkia mkewe talaka tatu kwa mpigo, hivyo Mtume ﷺ alisema akiwa amekasirika:

«أُبَلِّغُ بِكِتَابِ اللَّهِ وَأَنَا بَيْنَ أظْهَرِكُمْ؟»

“Kitabu cha Allah kinachezewa wakati bado nipo miongoni mwenu?”

¹ Tuhfatul-Ahwadhi 4:363.

² Ad-Daraqutni 4:298.

Mtu mmoja alisimama na kusema, Je, nimwue mtu huyo, Ewe Mtume ?¹

Hakuna Rejea Baada ya Talaka ya Tatu

Allah تعالی Amesema:

فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِنْ بَعْدُ حَتَّى تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ²

“Na kama amempa talaka (ya tatu) basi si halali kwake baada ya hizo mpaka aolewe na mume mwengine.”

Aya hii inaonesha kuwa iwapo mume atamwacha mke kwa mara ya tatu, basi hatoruhusiwa kumrejea. Allah تعالی Amesema:

حَتَّى تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ³

“Mpaka aolewe na mume mwengine.” Maana yake: Mpaka aolewe na mwanaume mwengine. Kama hataingiliwa na mume mwengine bila ya ndoa au bwana wake (kama ni mjakazi), atakuwa bado hajahalalika kuolewa na mume wa kwanza - mtalaka wake. Muslim ameeleza kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu mwanamke anayeolewa na mwanamume mwingine na anampa talaka kabla ya kumuingilia, je ataruhusiwa kuolewa na mume wa kwanza? Mtume ﷺ alisema:

«لَا، حَتَّى يَذُوقَ عُسَيْلَتَهَا»

“Hapana mpaka aonje asali yake (jimai).”²

Bukhari ameeleza pia juu ya Hadithi hii.³

Imam Ahmad رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Mke wa Rifaah Al-Quradhi alikuja wakati mimi na Abubakar رضي الله عنه tulikuwa na Mtume ﷺ na akasema, “Nilikuwa mke wa Rifaah, lakini aliniacha na talaka isiyorejewa. Kisha niliolewa na Abdur-Rahman bin Az-Zubayr, lakini dhakari yake ilikuwa haina nguvu, “Kisha akachukua ncha ya nguo yake kuonesha udogo wa dhakari yake. Khalid bin Said bin Al-As رضي الله عنه, ambaye alikuwa mlangoni akisubiri kuruhusiwa kuingia, alisema, ‘Ewe Abubaka! Kwa nini humzui mwanamke huyu kusema haya wazi mbele ya Mtume?’” Mtume ﷺ alicheka tu. Kisha Mtume ﷺ alimuuliza mwanamke yule:

¹ An-Nasai 6:142.

² Muslim 2:1057.

³ Fat’hul Al-Bari 9:284.

«كَأَنَّكَ تُرِيدِينَ أَنْ تَرْجِعِي إِلَى رِفَاعَةَ، لَا، حَتَّى تَذُوقِي عُسَيْلَتَهُ، وَيَذُوقَ عُسَيْلَتِكَ»

*"Je, unataka kurudi kuolewa na Rifaah? Huwezi mpaka uonje Usaylah yake naye aonje Usaylah yako (muwe na jimai iliyokamilika na mumeo wa sasa)."*¹

Al-Bukhari, Muslim, na An-Nasai pia waliinukuu Hadithi hii.² Kwa maneno ya Muslim ni kuwa, "Rifaah alimwacha mke wake talaka ya tatu na ya mwisho." Neno *Usaylah* lililotajwa katika Hadithi lina maana kitendo cha jimai. Imam Ahmad na An-Nasai wameeleza kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَلَا إِنَّ الْعُسَيْلَةَ الْجَمَاعُ»

*"Fahamu kuwa, Usaylah ni kuingiliana kimwili."*³

Wamelaaniwa wahalalishaji na wahalalishiwa:

Kinachokusudiwa hapa, ni kuwa Mume anayetaka kumuoa mke aliyeachwa Talaka tatu, lazima iwe amempenda mwanamke huyo kwa ridhaa yake na ana nia ya kuishi naye kwa muda mrefu, kujenga familia. Haya ndio yawe malengo na madhumuni ya ndoa. Endapo sababu ya ndoa ya pili ni kumwezesha mwanamke kuhalalika kwa mtalaka wake wa kwanza aliyemwacha Talaka tatu, hii ni *Tahlil* ambayo hadithi hii ina ilaani na kuikosoa. Na ikiwa madhumuni ya ndoa (iwapo mbinu hiyo chafu ya uhalalishaji) imebainishwa katika mkataba, itaufanya mkataba huo uwe batili kwa mujibu wa wanazuoni wengi.

Imam Ahmad ameeleza kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alimlaani mwenye kuchora tatu na anayechorwa, anaye-unganisha nywele na anayeunganishwa, anayehalalisha ndoa ya mke aliyeachwa Talaka tatu (*muhallil*), na anayefanyiwa uhalalishaji huo (*muhallalulahu*), anayekula riba na anayetoa riba."⁴ At-Tirmidhi na An-Nasai waliandika Hadithi hii⁵ na At-Tirmidhi alisema, Hadithi hii ni Hasan. Hili ndilo linalofanyiwa kazi kwa mujibu

¹ Ahmad 6:34.

² Fat'hul Al-Bari 10:518, Muslim 2:1057, An-Nasai 6:146.

³ Ahmad 6:62.

⁴ Ahmad 1:448.

⁵ Ahmad 1:448; Tuhfat Al-Ahwadhi 4:268; An-Nasai 6:149.

wa watu wenye elimu miongoni mwa Maswahaba, miongoni mwao ni Umar, Uthman na Ibn Umar رضي الله عنهما. Pia ni maneno ya wanazuoni wa Fiqh miongoni mwa Tabiin. Na imenukuliwa kutoka kwa Ali, Ibn Mas'ud na Ibn Abbas رضي الله عنهم. Katika Mustadrak wake, Al-Hakim ameeleza kuwa Nafi alisema: "Mtu alikuja kwa Ibn Umar رضي الله عنهما na akamwuliza kuhusu mtu aliyemwacha mkewe Talaka tatu. Kisha ndugu wa mume aliyeacha akamuoa mwanamke huyo, kwa nia ya kumuhalalishia ndugu yake, bila mwenyewe kujua, Je, Mwanamke huyo ni halali kwa mumewe aliyemtaliki kwanza?" Akasema, "Hapana isipokuwa ndoa hiyo imedhamiriwa. Kitendo hicho tulikuwa tukikichukulia kuwa ni kitendo cha upumbavu wakati wa Mtume ﷺ." Al-Hakim alisema, "Hadithi hii ina isnadi sahihi japokuwa wao (Al-Bukhari na Muslim) hawakuinukuu."¹ Maneno ya Hadithi hii yanaonesha kuwa hukumu hii ilitoka kwa Mtume ﷺ. Kadhalika amesimulia Abubakar bin Abu Shaybah, Al-Jawzajani, Harb Al-Kirmani na Abubakar Al-Athram kutoka kwa Qabisah bin Jabir alisema kuwa Umar رضي الله عنه alisema, "Iwapo wanaofanya kazi ya kuhalalisha ndoa na wanaohalalishiwa wataletwa kwangu, ningeamrisha warujumiwe."²

Ni Wakati Gani Mke Aliyearchwa Talaka Tatu Anahalalika Kuolewa na Mume wa Kwanza:

Allah تعالى Amesema:

فَإِنْ طَلَّقَهَا

"Na kama amempa talaka (ya tatu)."

Maana yake: Mume wa pili akishamuingilia kimwili kwa ukamilifu.

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا

"Basi hapana ubaya kwao kurejeana."

Maana yake: Mke na mume wa kwanza,

إِنْ ظَنَّا أَنْ يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ

"Wakiona kuwa watashikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu."

¹ Al Hakim 2:199.

² Ibn Abi Shaybah 4:294.

Maana yake: Wanaishi pamoja kwa wema. Mujahid alisema “Iwapo watadhani kuwa ndoa yao haitakuwa na mgogoro.”¹

Baada ya hapo Allah تعالى Amesema:

وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ

“Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu.”

Amri Zake na Sharia Zake,

يُبَيِّنُهَا

“Inayobainisha”

لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٢٤﴾

“Kwa watu wanaojua.”

* * *

¹ At-Tabari 4:598.

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ
 أَوْ سَرِّحُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ ۖ وَلَا تُمْسِكُوهُنَّ ضِرَارًا لِّتَعْتَدُوا ۗ وَمَنْ
 يَفْعَلْ ذَلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ ۚ وَلَا تَتَّخِذُوا آيَاتِ اللَّهِ
 هُزُوًا ۗ وَادْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمَا أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنَ
 الْكِتَابِ وَالْحِكْمَةِ يَعِظُكُمْ بِهِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
 بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٣١﴾ وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا
 تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَبْكْنَ أَرْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضُوا بَيْنَهُمْ
 بِالْمَعْرُوفِ ۗ ذَلِكَ يُوعِظُ بِهِ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ ذَلِكَ أَرْكَى لَكُمْ وَأَطْهَرُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا
 تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٢﴾ * وَالْوَالِدَاتُ يُرْضَعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ
 كَامِلَيْنِ ۗ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُنْفِقَ الرِّضَاعَةَ ۗ وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ
 رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ لَا تُكَلِّفُ نَفْسٌ إِلَّا وُسْعَهَا ۗ لَا
 تُضَارُّ وَالِدَةُ بَوْلِدِهَا وَلَا مَوْلُودٌ لَهُ بِوَالِدِهِ ۗ وَعَلَى الْوَارِثِ
 مِثْلُ ذَلِكَ ۗ فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِنْهُمَا وَتَشَاوُرٍ فَلَا
 جُنَاحَ عَلَيْهِمَا ۗ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَسْتَرْضِعُوا أَوْلَادَكُمْ فَلَا
 جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ مَا آتَيْتُم بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ
 وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٣﴾

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ
 فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرِّحُوهُنَّ
 بِمَعْرُوفٍ ۖ وَلَا تُمْسِكُوهُنَّ ضِرَارًا
 لِّتَعْتَدُوا ۗ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ
 نَفْسَهُ ۚ وَلَا تَتَّخِذُوا آيَاتِ اللَّهِ هُزُوًا
 ۗ وَادْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمَا أَنْزَلَ
 عَلَيْكُمْ مِنَ الْكِتَابِ وَالْحِكْمَةِ يَعِظُكُمْ
 بِهِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ
 شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٣١﴾

231. "Na mtakapowapa wanawake talaka, nao wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema na waachilieni kwa wema. Wala msiwarejee kwa kuwadhuru mkafanya uadui. Na atayefanya hivyo, amejidhulumu nafsi yake. Wala msizichukulie Aya za Mwenyezi Mungu kwa maskhara. Na kumbukeni Neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu, na Aliyokuteremshieni

katika kitabu na hikima Anachokuonyeni kwacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

Amri ya Kumfanyia Wema Mke Aliyeachwa:

Hii ni amri kutoka kwa Allah تعالى kwa wanaume kuwa mmoja wao anapomwacha mke wake talaka rejea, amtunze na amfanyie wema, ili muda wake wa *Iddah* unapokaribia kumalizika, ama amrejee kwa njia iliyo nzuri, ikiwa ni pamoja na kuwa na mashahidi kuwa amemrejea, na aishi naye kwa ihsani, au, amruhusu kuondoka nyumbani baada ya kumaliza *Iddah*, bila ugomvi, kubishana au kumtukana. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَلَا مَسْكُوهُنَّ ضِرَارًا لِّتَعْتَدُوا^ع

“Wala msiwarejee kwa kuwadhuru.”

Ibn Abbas, Mujahid, Masruq, Al-Hassan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم walisema: mtu alikuwa akimwacha mke, na *Iddah* inapokaribia kumalizika humrejesha tena, ili muda wa *Iddah* uendelee. Baada ya hapo, Allah تعالى Aliharamisha desturi hiyo.¹ Pia Allah تعالى Amewakemea wenye tabia hiyo,

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ^ع

“Na atayefanya hivyo, amejidhulumu nafsi yake.”

Maana yake: Kwa kukadhibisha maamrisha ya Allah تعالى. Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَا تَتَّخِذُوا آيَاتِ اللَّهِ هُزُوًا^ع

“Wala msizichukulie Aya za Mwenyezi Mungu kwa maskhara.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Abu Musa (Al-Ash'ari) رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ siku moja aliwakasirikia kabila la Ash'ari. Abu Musa رضي الله عنه alimwendea na akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Umewakasirikia Ash'ariyyin?” Mtume ﷺ akasema,

«يَقُولُ أَحَدُكُمْ: قَدْ طَلَّقْتُ، فَذَرَجْتُ، لَيْسَ هَذَا طَلَاقَ الْمُسْلِمِينَ، طَلَّقُوا الْمَرْأَةَ فِي قُبُلِ عِدَّتِهَا»

¹ Ibn Abi Hatim 2:772-774 na At-Tabari 49201.

"Mmoja wao anasema, "Nimempa talaka - kisha anasema 'Nimemrejea!" Hii sio talaka ya Waislamu. Mpe talaka mke atakapo kamilisha muda uliowekwa."¹

Masruq alisema kuwa Aya inamhusu mtu anayemduru mke wake kwa kumpa talaka, na kisha akamrejea, ili muda wake wa *Iddah* uwe mrefu.² Al-Hasan, Qatadah, Ata, Al-Khurasani, Ar-Rabi na Muqatil bin Hayyan alisema, "Ni mtu ambaye anamwacha mke wake na anasema, "Nilikuwa nafanya masikhara." Au anamwacha huru mtumwa au anaoa na kusema: "Nilikuwa nafanya mzaha." Akateremsha:

وَلَا تَتَّخِذُوا آيَاتِ اللَّهِ هُزُوًا^٤

"Wala msizichukulie Ayah za Mwenyezi Mungu kwa Maskhara."³

Kisha watu wa aina hiyo walitakiwa kubeba madhara ya matendo yao. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ

"Na kumbukeni Neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu..."

Maana yake: Kwa kumtuma Mjumbe wake kwenu na muongozo ulio sahihi na bishara zilizo wazi.

وَمَا أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ أَلْحُكْمِ وَالْحِكْمَةِ

"Na aliyokuteremshieni katika kitabu na hikima." (Maana yake Sunnah).

يَعْظُمُكُمْ بِهِ^٥

"Anachokuonyeni kwacho."

Maana yake: Anawaamrisha, Anawakataza na Anawakhofisha kwa kuchupa makatazo Yake. Allah تعالى Amesema:

وَاتَّقُوا اللَّهَ

"Na mcheni Mwenyezi Mungu."

Maana yake: Kuhusu mnayoyafanya na mnayoyaepuka.

¹ At-Tabari 5:14

² At-Tabari 5:14

³ Ibn Abi hatim 2:775, 776

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٣٢﴾

“Na jeuri kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Hapana siri yenu wala mambo yenu ya dhahiri yanayoweza kuwa nje ya ufahamu Wake, na Atakushughulikia kwa mujibu wa amali zako.

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَنْكِحْنَ أَزْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَضَوْا بَيْنَهُمْ
بِالْمَعْرُوفِ ۚ ذَٰلِكَ يُوعَظُ بِمِ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكُمْ أَزْكَى لَكُمْ
وَأَطْهَرُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٢﴾

232. “Na mtakapowapa wanawake talaka nao wakamaliza eda yao, basi msiwaziue kuolewa na waume zao endapo baina yao wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hayo ni bora zaidi kwenu na safi kabisa. Na Mwenyezi Mungu Anajua, lakini nyinyi hamjui.”

Makatazo kwa Walii wa Mwanamke Aliyeachwa Asimzuie Kurejewa na Mume Wake:

Ali bin Abu Talhah ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Aya hii iliteremshwa kuhusu mwanamume aliyemtaliki mkewe Talaka moja au mbili na *Iddah* yake ilikwisha. Baadaye akafikiria kumuoa tena na mwanamke akakubali, lakini familia yake inamzuia kuolewa tena na mwanamume huyo. Hivyo Allah تعالي Akaikataza familia kumzuia. Masruq, Ibrahim An-Nakhai, Az-Zuhri na Adh-Dhahhak wameeleza kuwa hii ndio sababu ya kushushwa kwa Aya (2:232).¹ Kauli hizi zinalandana na maana ya wazi ya Aya hii.

Ndoa Haisihi Bila Kuwepo Walii (Msimamizi) wa Mwanamke

Aya (2:232) inaonesha pia mwanamke haruhusiwi kujiozesha. Bali anahitaji Walii (Msimamizi: Baba, Kaka, Mtoto wa kiume baleghe n.k) wa kumuoza, kama Ibn Jarir na At-Tirmidhi walivyoelezea walipoitaja Aya hii. Pia, Hadithi inaeleza kuwa;

¹ At-Tabari 5:22,23.

«لَا تُزَوِّجُ الْمَرْأَةَ الْمَرْأَةَ، وَلَا تُزَوِّجُ الْمَرْأَةَ نَفْسَهَا، فَإِنَّ الرَّأْيَةَ هِيَ الَّتِي تُزَوِّجُ نَفْسَهَا»

"Mwanamke hamwozeshi mwanamke mwenzake, wala yeye hawezi kujiozesha, isipokuwa mwanamke mzinifu ndiye anayejiozesha mwenyewe."¹

Hadithi nyingine inasema:

«لَا نِكَاحَ إِلَّا بِوَلِيِّ مُرْتَبِدٍ وَشَاهِدَيْنِ عَدْلٍ»

"Hapana ndoa inayosihhi bila kuwepo Walii (msimamizi) balebhe na mashahidi wawili waadilifu."²

Madhumuni ya Kuteremshwa Aya (2:232):

Ilinukuliwa kuwa Aya hii iliteremsha kumhusu Ma'qil bin Yasar Al-Muzani na dada yake. Al-Bukhari aliandika katika Sahih yake, alipotaja tafsiri ya Ayah hii (2:232), kuwa mume wa dada yake Maaqil bin Yasar alimtaliki. Alisubiri mpaka *Iddah* yake ilipokwisha kisha akamwomba amwoe tena, lakini Ma'qil alikataa. Kisha, Ayah hii iliteremshwa.

فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَنْكِحْنَ أَزْوَاجَهُنَّ

"Basi msiwazuie kuolewa na waume wao."³

Abu Dawud, Al-Tirmidh, Ibn Abu Hatim, Ibn Jarir na Ibn Marduwyah na Al-Bayhaqi walipokea Hadithi hii kutoka kwa Al-Hasan kutoka kwa Ma'qil bin Yasar.⁴ At-Tirmidh amesema Hadithi hii ni sahihi, na katika upokezi wake amesema, Ma'qil bin Yasar alimwozesha dada yake kwa mwanamume Muislam, katika zama za Mtume ﷺ. Alikaa naye kwa muda kisha akamwacha talaka moja na hakumrejea mpaka *Iddah* yake ilipomalizika. Kisha wakataka kuoana tena, kisha akatuma Mshenga. Ma'qil akamwambia, "Ewe mja usio na hisani! Nilikuheshimu nikakuozesha lakini ulimpa talaka. Wallah!

¹ Ibn Majah 1:606.

² Al-Ummu cha Shafi 5:22 na Al-Bayhaqi 7:112 - 124 .

³ Fat'hul Al-Bari 8:40.

⁴ Abu Dawud 2:569, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:325, Ibn Abi Hatim 2:778, At-Tabari 5:17-19, Al-Bayhaqi 7:104.

Sitakuozesha tena. Lakini Allah تعالى Alijua kuwa mume alimhitaji mke na mke alimhitaji mume. Akashusha:

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَلَبِغْنَ أَجَلَهُنَّ

“Na mtakapowapa wanawake talaka nao wakamaliza eda yao...”

Mpaka Aliposema.

وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣١﴾

“Lakini nyinyi hamjui.”

Ma'qil aliposikia Ayah hii, alisema, “Nimesikia na ninamtii Mola wangu.” Kisha alimwita bwana yule na akamwambia, “Nakuozesha dada yangu na nitakukarimu.”¹ Ibn Marduwyah aliongeza kuwa (Ma'qil alisema), “Na nimelipa fidia kwa kuvunja kiapo.”² Allah تعالى Amesema:

ذَلِكَ يُوعَظُ بِهِ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ^٤

“Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Maana yake: Kukuzuia wewe kumzuia mwanamke kuolewa tena na mtalaka wake, iwapo wote wameridhia kuoana tena kwa wema. Na Anawawaidhi:

مَنْ كَانَ مِنْكُمْ

“Yule miongoni mwenu.” Enyi watu,

يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ^٤

“Anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho.” Maana yake: Kuamini maamrisha ya Allah تعالى na kuogopa Maonyo Yake na Adhabu yake Siku ya Kiyama. Allah تعالى Amesema:

ذَلِكَمُزَكَّىٰ لَكُمْ وَأَطْهَرُ^٤

“Hayo ni bora zaidi kwenu na safi kabisa.”

Maana yake: Kutii Amri za Allah تعالى kwa kuwarejesha wanawake kwa waume zao wa mwanzo, na kuacha chuki zenu, ni bora na safi kwa mioyo yenu.

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:324.

² Bayhaqi 7:104.

وَاللَّهُ يَعْلَمُ

“Na Mwenyezi Mungu Anajua.” Manufaa muypatayo kutokana na Maamrishi Yake na vile Anavyovikataza.

وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣١﴾

“Lakini nyinyi hamjui.” Manufaa katika yale mnayoyafanya au yale mnayoacha kuyafanya.

﴿٢٣٢﴾ وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُنْمِيَ الرِّضَاعَةَ وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ لَا تُكَلِّفُ نَفْسٌ إِلَّا وُسْعَهَا ۚ لَا تُضَارُّ وَالِدَةُ بَوْلِدِهَا وَلَا مَوْلُودٌ لَهُ بِوَالِدِهِ ۚ وَعَلَى الْوَارِثِ مِثْلُ ذَلِكَ ۚ فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِنْهُمَا وَتَشَاوُرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا ۚ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَسْتَرْضِعُوا أَوْلَادَكُمْ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ مَا آتَيْتُمْ بِالْمَعْرُوفِ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٣﴾

233. “Na wazazi wanawake wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili kwa anayetaka kutimiza kunyonyesha. Na juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada. Wala halazimishwi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mwanawe. Na ni juu ya mrithi mfano wa hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si vibaya kwao. Na mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha basi hapana ubaya kwenu mkitoa mlichohidi kwa mujibu wa ada. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Anayaona yote mnayoyatenda.”

Muda wa Kunyonyesha Usizidi Miaka Miwili

Huu ni mwongozo kutoka kwa Allah تعالى kwa akina mama kuwa, wawanyonyeshe watoto wao kwa kipindi kilichokamilika cha miaka miwili. Hivyo, kuendelea kunyonyesha baada ya miaka miwili hakuitwi kuwa ni kunyonyesha ndio maana Allah تعالى Akasema:

لَمَنْ أَرَادَ أَنْ يُيَمَّ الرِّضَاعَةَ

“Kwa anayetaka kutimiza kunyonyesha.”

Kwa hiyo, kunyonyesha kunakoharamisha kuoana baina ya walionyonya ziwa moja ni katika kipindi kabla ya kwisha miaka miwili, hivyo lau mtoto atanyonya na umri wake zaidi ya miaka miwili, haitazingatiwa kuwa ni kunyonyesha kunakoharamisha kuonana. A-Tirmidhi katika mlango wa, “Kunyonya kunakosababisha uharamu ni ndani ya miaka miwili ya mwanzo.” Ameerleza kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَخْرُومُ مِنَ الرِّضَاعِ إِلَّا مَا فَتَقَ الْأُمْعَاءُ فِي التَّدْيِ وَكَانَ قَبْلَ الْفِطَامِ»

“Kunyonya kunakosababisha Uharamu (wa kuoana) ikiwa ni kunyonya chuchu kabla ya Fitam (kabla ya kuachisha ziwa, kabla ya kwisha miaka miwili ya mwanzo).”¹

At-Tirmidhi alisema, “Hadithi hii ni Hasan Sahih.” Wanazuoni wengi miongoni mwa Masahaba wa Mtume na wengine waliafikiana juu ya hili, kuwa kunyonya kunakosababisha (uharamu wa kuoana au kuolewa) kabla ya kwisha miaka miwili na chochote kitakachotokea baada ya hapo hakisababishi uharamu. At-Tirmidhi pekee ndiye aliyenukuu Hadithi hii na wasimulizi wake wanakidhi viwango vya masharti vya Bukhari na Muslim. Kauli ya Mtume ﷺ.

«إِلَّا مَا كَانَ فِي التَّدْيِ»

“Katika matiti.” Inaashiria kiungo kinachonyonywa kabla ya miaka miwili. Imam Ahmad ameeleza Hadithi ambayo Al-Barau bin Azib رضي الله عنه aliisimulia, “Ibrahim, mtoto wa Mtume, alipokufa, Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ ابْنِي مَاتَ فِي التَّدْيِ، إِنَّ لَهُ مُرْضِعًا فِي الْجَنَّةِ»

“Mwanangu amekufa akiwa bado kwenye maziwa na hakika ana mtu wa kumnyonyesha Peponi.”²

Zaidi ya hayo, Ad-Daraqutni alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 4:313.

² Umdat At Tafsir 1:126.

«لَا يَحْرُمُ مِنَ الرِّضَاعِ إِلَّا مَا كَانَ فِي الْحَوْلَيْنِ»

“Kunyonyesha hakusababishi uharamu (wa kuoana) ila ndani ya miaka miwili ya mwanzo tu.”¹

Imam Malik رحمه الله تعالى ameieleza Hadithi katika Muwatta, hii kutoka kwa Thawr bin Zayd ambaye alisimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliipokea kutoka kwa Mtume ﷺ.² Darawardi ameeleza Hadithi kutoka kwa Thawr aliyoipokea kutoka kwa Ikrimah ambaye aliipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Katika masimulizi haya ambayo ni sahihi, na akaongeza.

«وَمَا كَانَ بَعْدَ الْحَوْلَيْنِ فَلَيْسَ بِشَيْءٍ»

“Chochote kitakachotokea baada ya miaka miwili hakitohisabiwa.”

Kunyonyesha baada ya Miaka Miwili:

Imeandikwa katika Sahih kuwa Aishah رضي الله عنها alikuwa anaona kama mwanamke atanyonyesha mtoto mkubwa (Mwenye zaidi ya miaka miwili), kitendo hiki, kinasababisha uharamu (kuoana).³ Hii pia ni kauli ya Ata bin Abu Rabah na Layth bin Sa'd. Hoja ya Aisha رضي الله عنها ilikuwa ni Hadithi ya Salim, mtumwa aliyeachwa huru na Hudhaifah, alipoamrisha na Mtume ﷺ mwanamke wa Abu Hudhaifa رضي الله عنه amnyonyeshe, hali ya kuwa wakati huo alikuwa ni mkubwa. Hivyo kwa kunyonya huko akawa anaingia nyumbani kwake bila kipingamizi. Hata hivyo, wakeze Mtume ﷺ waliobaki hawakukubaliana na suala hilo na wakaona kuwa hili lilikuwa tukio mahsus.⁵ Na hii ndiyo rai ya wanazuoni walio wengi (Jamhuri).

Kunyonyesha kwa Malipo ya Fidia.

Allah تعالى Amesema:

وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ^٤

“Na ni juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada.”

¹ Ad-Daraqutni 4:174.

² Al-Muwatta 2:602.

³ Muslim 2:1077.

⁴ Abu Dawud 2:549,550.

Maana yake: Baba wa mtoto anawajibika kumpa mama matumizi na kumnunulia nguo, zenye thamani inayoendana na hali ya maisha ya watu wa eneo wanaloishi, bila kufanya isirafu au ubadhirifu. Baba anatumia kwa mujibu wa uwezo wake. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

لِيُنْفِقَ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ ۗ وَمَن قُدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ ۚ لَا يُكْفُ اللَّهُ
نَفْسًا إِلَّا مِمَّا آتَاهَا ۗ سَيَجْعَلُ اللَّهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٦٥﴾

“Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake, na mwenye dhiki atoe katika alichompa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu ila kwa kadiri ya Alichompa. Mwenyezi Mungu Atajaalia baada ya dhiki faraji.” (65:7)

Adh-Dhahhak alisema, “Iwapo mume atamwacha mke wake ambaye alizaa naye mtoto, na bado anamnyonyesha mtoto huyo, anatakiwa kumpa matunzo na nguo kwa kadiri ya uwezo wake.”¹

Hapana *Dharar* (madhara) au *Dhirar* (kulipiza kisasi)

Allah تعالى Amesema:

لَا تُضَارَّ وَالِدَةٌ بِوَلَدِهَا

“Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mwanawe...”

Maana yake: Mama asiache kumlea mtoto wake akamwachia baba yake peke yake ili kumkomoa. Mama hana haki ya kuacha kumnyonyesha baada ya kujifungua anatakiwa amnyonyeshe maziwa ambayo ni lazima kwa maisha yake. Baadaye, anaruhusiwa, kuacha kumlea madhali hafanyi hilo kwa nia ya kumdhuru baba. Zaidi ya hayo, baba haruhusiwi kumchukua mtoto kutoka kwa mama kwa lengo la kumdhuru mama na kwa sababu hii Allah تعالى Amesema:

وَلَا مَوْلُوهُ لَهٗ بِوَلَدِهِ ۗ

“Wala baba kwa ajili ya mwanawe...” Maana yake: Kwa kumchukua mtoto kutoka kwa mama yake kwa nia ya kumdhuru mama. Hii ni tafsir ya Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahhak, Az-Zuhuri, As-Suddi, Ath-Thawri na Ibn Zayd na wengine katika Aya hii.² Kisha Allah تعالى Amesema:

¹ At Tabari 5:39.

² At Tabari 5:50.

وَعَلَى الْوَارِثِ مِثْلُ ذَلِكَ¹

“Na juu ya mrithi mfano wa hivyo.”

Maana yake: Kutowadhuru jamaa (wa baba), kama Mujahid, Ash-Shabi na Adh-Dhahhak walivyosema. Ilinukuliwa kuwa (Aya inamuusia) mrithi (wa baba) kumpa matumizi mama wa mtoto kama baba alivyokuwa akimpa, na kulinda haki zake za kutomdhuru, kwa mujibu wa Tafsiri ya wanazuoni wengi. Inatupasa tueleze kuwa Ibn Jarir رحمه الله تعالى amelielezea somo hili kwa urefu katika Tafsiri yake na ameeleza kuwa kumnyonyesha mtoto baada ya miaka miwili kunaweza kumdhuru mtoto kimwili au kiakili. Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Alqamah alimkataza mwanamke kuendelea kumnyonyesha mtoto baada ya kwisha mwaka wa pili.¹

Mtoto Kuachishwa Ziwa Kufanyike kwa Maridhiano:

Allah تعالى Amesema:

فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِّنْهُمَا وَتَشَاوُرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا¹

“Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si kosa juu yao.”

Ayah hii inaonesha kuwa endapo baba na mama wataamua kuhusu *Fitam* (kumwachisha ziwa mtoto) kabla ya miaka miwili (ya kunyonyesha) kumalizika, na kwa manufaa ambayo wote wamejadili na kukubaliana, hivyo si kosa katika hali hiyo. Hivyo, Ayah inaonesha kuwa mzazi mmoja hawezi kufanya maamuzi peke yake bila ya majadiliano ya wawili. Mtazamo huu ni wa At-Thauri رحمه الله تعالى na wengine. Kadhalika tendo hili limelinda masilahi ya mtoto. Pia ni rehema kutoka kwa Allah kwa waja wake, kwani Yeye Aameamrisha njia nzuri kwa wazazi kuwalea watoto wao na sheria yake inawaelekeza wazazi na watoto kwenye ufanisi na maslahi. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema katika *Surat At-Talaq* (Sura ya 65 ndani ya Qur'an):

فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ^ط وَأْتَمِرُوا بَيْنَكُمْ بِمَعْرُوفٍ^ط وَإِنْ تَعَاَسَرْتُم فَسَرِّضُوهَا^ط

أُخْرَى ﴿٦٥﴾

¹ At Tabari 5:36.

“Na wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao, na shaurianeni kwa wema. Na mkiona uzito kati yenu, basi amnyonyeshee mwanamke mwingine.” (65:6)

Kisha Allah تعالى Akasema:

وَأِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَسْتَزْعِمُوا أَوْلَادَكُمْ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ مَا آتَيْتُمْ بِالْعُرُوفِ

“Na mkitaka kuwa patia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha basi hapana ubaya kwenu mkitoa mlichohidi kwa mujibu wa ada.”

Maana yake: Ikiwa mama na baba watakubaliana kuwa baba anachukua ulezi wa mtoto kutokana na hali ambayo inamlazimisha mama au inamruhusu baba kufanya hivyo, hivyo hakuna makosa katika hali hiyo. Hivyo, mama anaruhusiwa kumtoa mtoto na baba anaruhusiwa kumtunza mtoto. Baba anatakiwa ampe mama matumizi kwa hisani, ya kipindi kilichopita (wakati akimlea na kumnyonyesha mtoto) na amtafute mwanamke mwingine amnyonyeshe kwa malipo ya fedha. Baada ya hapo. Allah تعالى Amesema:

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Katika mambo yenu yote,

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

“Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Anaona yote mnayoyatenda.”

Maana yake: Hapana jambo lenu au maneno yenu yanayompita.

* * *

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ
 أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا ۖ فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ
 فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ۝
 وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا عَرَضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ
 النِّسَاءِ أَوْ أَكْنُتُمْ فِي أَنْفُسِكُمْ ۗ عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ
 سَتَذْكُرُونَهُنَّ وَلَكِنْ لَا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا
 مَعْرُوفًا ۖ وَلَا تَعْزِمُوا عُقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّى يَبْلُغَ الْكِتَابُ
 أَجَلَهُ ۗ وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ ۗ
 وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ۝ لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ
 طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ مَا لَمْ تَمْسُوهُنَّ أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً ۗ
 وَمَتَّعُوهُنَّ عَلَى التُّوسِعِ قَدَرُهُ وَعَلَى الْمَقْتَرِ قَدَرُهُ مَتَّعًا
 بِالْمَعْرُوفِ ۖ حَقًّا عَلَى الْمُحْسِنِينَ ۝ وَإِنْ طَلَقْتُمُوهُنَّ
 مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَيَصِفُ مَا
 فَرَضْتُمْ إِلَّا أَنْ يَعْفُونَ أَوْ يَعْفُوا الَّذِي بِيَدِهِ عُقْدَةُ
 النِّكَاحِ ۗ وَأَنْ تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَى ۗ وَلَا تَنْسُوا الْفَضْلَ
 بَيْنَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا
 يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا
 فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ
 فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ
 وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ۝

234. "Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakaacha wake, wake hawa wangoje peke yao miezi mine na siku kumi. Na wanapotimiza eda yao basi hapana ubaya kwao kwa wanaojifanyia kwa mujibu wa ada. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote manyo yatenda."

Eda ya Mjane:

Hii ni amri kutoka kwa Allah kama kwa wanawake walio-fiwa na waume zao, ni kuwa wanatakiwa kukaa eda kwa miezi mine na siku kumi, hii ni pamoja na ndoa ambazo hazikukamilika kwa jimai au

vinginevyo, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.

Ushahidi kuwa sheria hii inahusu ndoa zisizokamilika kwa kuingiliwa mke, unapatikana katika maana ya jumla ya Aya. Katika masimulizi yaliyoandikwa na Imam Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan*, ambayo Tirmidhi ameyapa daraja

la *Sahih*. Ibn Mas'ud رضى الله عنه aliulizwa kuhusu mtu aliyemuoa mwanamke, lakini akafariki kabla ya kumjamii. Pia hakuwahi kutoa mahari. Wakawa wanamuuliza Ibn Mas'ud رضى الله عنه kuhusu suala hili mpaka aliposema, "Nitawapeni rai yangu, na iwapo itakuwa *Sahihi* itakuwa imetoka kwa Allah تعالى, na ikiwa ni makosa itakuwa kwa sababu ya makosa yangu na kwa sababu ya juhudi za Shetani. Allah تعالى na Mtume wake ﷺ wametakasika na hilo. Akasema, 'Mwanamke anastahili mahari sawa na mwanamke wa hadhi yake, bila kufanya ubakhili au isirafu." Kisha akaendelea, "Anatakiwa kukaa *Iddah* na ana haki ya kurithi." Ma'qil bin Yasar Al-Ash'jai alisimama na kusema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akitoa hukumu sawa na hii kwa shauri la Barwa bint Washiq رضى الله عنها." Abdullah bin Mas'ud alifurahi sana baada ya kusikia kauli hii. Katika masimulizi mengine, wanaume kadha kutoka kabila la Ashjai walisimama na kusema, "Tunathibitisha kuwa Mtume ﷺ alitoa hukumu sawa na hiyo kwa maslahi ya Bar'wa binti Washiq رضى الله عنها."¹

Ama kuhusu mjane ambaye mume wake amekufa akiwa mjamzito, muda wake wa kukaa eda unamalizika anapojifungua, hata ikitokea mara tu baada ya kufariki mume wake. Hukumu hii imechukuliwa kutoka Kauli ya Allah تعالى:

وَأُولَاتُ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

"Na wenye mimba, eda yao mpaka watakapozaa." (65:4)

Pia kuna Hadithi kutoka kwa Subay'ata Al-Aslamiyah رضى الله عنها ndani ya *Sahih* Mbili, kupitia isnadi mbalimbali za masimulizi. Mume wake, Sa'd bin Khawlah رضى الله عنه, alikufa akiwa mjamzito na alijifungua siku chache baada ya kifo chake. Alipomaliza *Nifas*, alioga na kujikwatua tayari kwa kuposwa kwa amtakaye. Kisha, Abu Sanabil bin Ba'bak رضى الله عنه alimjia na kumuambia, "Kwa nini umejikwatua, unataraji kuolewa? Wallah! Hutoolewa mpaka ipite miezi mine na siku kumi." Subay'ata رضى الله عنها akasema, "Aliponiambia hivyo, nilikusanya nguo zangu usiku ulipoingia nikaenda kwa Mtume ﷺ na nikamuuliza kuhusu suala lile. Akanijibu kuwa eda yangu ilikuwa imekwisha baada ya kujifungua na akaniruhusu kuolewa kama nilitaka."²

¹ Ahmad 3:480, Abu Dawud 2:588, Tuhfat Ahwadh 4:299, Nasai 6:198, na Ibn Majah 1:609.

² Fat'hul Al-Bari 9:379, Muslim 2:1122.

Hekima ya Kufaradhiwa Kukaa Eda ya Kufiwa:

Alisema Said bin Musayyib, Abu Al-Aliyah na wengine, kuwa hekima ya kuifanya eda ya mjane miezi mine na siku kumi ni kuwa inawezekana kuwepo mimba. Mwanamke anaposubiri kwa kipindi hicho, itathibitika kama ana mimba. Vivyo hivyo, kuna Hadithi katika *Sahih* Mbili iliyosimuliwa na Ibn Mas'ud رضي الله عنه ikieleza.

«إِنَّ خَلْقَ أَحَدِكُمْ يُجْمَعُ فِي بَطْنِ أُمِّهِ أَرْبَعِينَ يَوْمًا نُطْفَةً، ثُمَّ يَكُونُ عَلَقَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَكُونُ مُضْغَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَبْعَثُ إِلَيْهِ الْمَلَكُ فَيَنْفُخُ فِيهِ الرُّوحَ»

“(Umbaji wa) binadamu unakusanywa pamoja ndani ya tumbo la mama yake kwa siku arubaini katika hali ya mbegu na baadaye kuwa bongwe la damu kwa kipindi sawa na hicho, na kisha funda la nyama kwa kipindi sawa. Kisha, Allah Humtuma Malaika ambaye anaamriwa kumpulizia roho kijusi (mimba ya miezi mine).”¹

Hizi arobaini tatu ni miezi minne, na imeongezewa siku kumi mbele, iwapo kama kuna mapungufu yatajitokeza kwa baadhi ya miezi au kutodhihiri mtoto kucheza baada ya kupuliziwa roho ndani yake. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Eda ya Mjakazi Aliyefiwa na Bwana Wake:

Tunataja hapa kuwa Eda ya mjakazi ni sawa kama Eda ya kufiwa mwanamke huru. Imam, Ahmad alisimulia kuwa Amr bin Al-As رضي الله عنه alisema, “Msitutatanishe katika Taratibu na mienendo (*Sunnah*) ya Mtume wetu. Eda ya mama ambaye ni mjakazi, anapofiwa na bwana wake, ni miezi mine na siku kumi.”²

Abu Dawud na Ibn Majah pia wameinukuu.³

¹ Fat'hul Al-Bari 13:449, Muslim 4:2036.

² Ahmad 4:302, Abu Dawud 2:370.

³ Ibn Majah 1:673.

⁴ Fat'hul Al-Bari 9:394 na Muslim 2:1123.

Uwajibu wa Msiba Wakati wa Eda ya Kufiwa:

Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيَمَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ

خَبِيرٌ

“Na wanapotimiza eda yao basi hapana ubaya kwao kwa wanayojifanyia kwa mujibu wa eda. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayotenda.”

Aya hii inaonesha inamlazimu aliye kwenye eda ya kufiwa kuendelea na msiba mpaka eda itakapomalizika. Imesimuliwa ndani ya *Sahih* Mbili kuwa Umm Habibah na Zaynab bint Jahsh رضي الله عنهما walisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَجِلُّ لِامْرَأَةٍ تُوْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ تُجِدَّ عَلَى مَيِّتٍ فَوْقَ ثَلَاثِ، إِلَّا عَلَى زَوْجٍ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا»

“Si halali kwa mwanamke anayemwamini Allah na Siku ya Mwisho kumwomboleza maiti kwa zaidi ya siku tatu, isipokuwa kwa mume, ni miezi minne na siku kumi.”⁴

Imesimuliwa katika Sahih Mbili kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisema kuwa mwanamke alimwambia, “Ewe Mjumbe wa Allah! Mume wa binti yangu amefariki na ameshitakia maumivu katika macho yake, je tumpake wanja (Kohl) kwenye macho yake?” Akajibu, “Hapana” na kila akiulizwa hujibu, ‘Hapana’ mara mbili au mara tatu. Kisha akasema:

«إِنَّمَا هِيَ أَرْبَعَةُ أَشْهُرٍ وَعَشْرٌ، وَقَدْ كَانَتْ إِحْدَاكُنَّ فِي الْجَاهِلِيَّةِ تَمُكُّتُ سَنَةً»

“Hakika hiyo miezi minne na siku kumi! Wakati wa Jahiliyah, mfiwa alikuwa katika msiba kwa mwaka mzima.”¹

Zaynab bintiye Umm Salamah رضي الله عنها alisema (kuhusu enzi za Jahiliyyha), “Mume alipofariki dunia, mke alijitenga mahali duni na kuvaa nguo chafu na

¹ Muslim 2:1124.

kuukuu. Aliacha kujitia uturi au kujipamba kwa muda wa mwaka mmoja. Kisha alitoka na kupewa kinyesi cha mnyama na kutupa. Kisha huletwa mnyama, punda, kondoo au ndege. Halafu damu hutolewa, na mara nyingi husababisha kifo cha mnyama husika.”

Kwa kifupi, mwanamke aliye kwenye eda hatakiwi kutumia vipodozi, kama kujitia uturi na kuvaa nguo na mapambo ya vito ambavyo vitamshajiisha mwanamume kumposa mwanamke. Wajane wote wanatakiwa waizingatie eda bila kujali kuwa ni kijana, mzee, huru au mjakazi, Muislam au Kafiri, kama maana ya jumla ya Aya inavyoonesha. Pia Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ

“Na wanapotimiza eda yao...”

Maana yake: Eda inapokwisha, kwa mujibu wa Adh-Dhahhak na Ar-Rabi bin Anas.

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

“...basi hapana ubaya juu yenu...”

Az-Zuhri alisema, “Maana yake: Watu Wake.”

فِيمَا فَعَلْنَ

“...kwa wanayojifanyia...”

Maana yake: Wanawake waliomaliza Eda zao.² Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mwanamke anapoachwa au kufiwa na mume na Eda yake ikaisha, hapana makosa kujikwatua, ili awe tayari kuposwa. Hii ni njia iliyo sawa na ya kuheshimika.³ Ilisimuliwa kuwa Muqatil bin Hayyan alitoa maelezo hayo.⁴ Ibn Jurayj alisimulia kuwa Mujahid alisema:

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ

“... basi hapana ubaya kwao kwa wanaojifanyia kwa mujibu wa ada.”

¹ Ibn Abu Hatim 2:812.

² Ibn Abu Hatim 1:813.

³ Ibn Abu Hatim 2:813.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:812.

“Inahusu walioruhusiwa na waliotakasika kwa kuolewa.”¹ Pia ilisimuliwa kuwa Al-Hasan, Az-Zuhri na As-Suddi walisema kama hivyo.²

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَّضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ النِّسَاءِ أَوْ أَكْنَنْتُمْ فِي أَنْفُسِكُمْ عَلِمَ اللَّهُ
أَنْكُمْ سَتَذَكَّرُونَهُنَّ وَلَكِنْ لَا تُؤَاعِدُوهُنَّ سِرًّا إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَعْرُوفًا وَلَا تَعْزَمُوا
عُقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّى يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ ۗ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ
فَاحْذَرُوهُ ۗ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٣٥﴾

235. “Wala si vibaya kwenu katika kupeleka posa kwa ishara tu kwa wanawake waliomo edani au mkadhamiria katika nyoyo zenu. Mwenyezi Mungu Anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka. Lakini msiwaahidi kwa siri, ila mnene maneno mema. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka eda ifike mwisho wake. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini Naye. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mpole.”

Kuruhusiwa Posa kwa Ishara Wakati wa Eda, na Kukatazwa Ndoa kwa Wakati Huo.

Allah تعالى Amesema:

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

“Wala si vibaya kwenu.”

Maana yake: Kumposa mjane kwa kuashiria wakati akiwa kwenye eda ya kufiwa na mume. At-Thawri, Shu’bah na Jarir walieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَّضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ النِّسَاءِ

“Wala si vibaya kwenu katika kupeleka posa ya ishara tu kwa wanawake waliomo edani...”

¹ At-Tabari 5:93.

² Ibn Abu Hatim 2:8140.

“Posa ya ishara ni kama kusema, “Nataka kuoja na namtafuta mwanamke mwenye sifa kadha wa kadha, hivyo kuzungumza kwake naye mazungumzo ya kawaida katika hali nzuri.”¹ Katika masimulizi mengine (kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما), “Posa ya ishara ni kama mtu kusema, “Nataraji Allah تعالى Anijalie mke mwema! Lakini asiwasilisha posa kwa uwazi.”² Al-Bukhari alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya:

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَّضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ النِّسَاءِ

“Wala si vibaya, kwenu katika kupeleka posa ya ishara tu kwa wanawake waliomo edani...”

Maana yake: Kama, “mwanamume kusema, ‘Nataraji kuoja’, ‘Natamani kuwa na mke’, ‘Natamani ningempata mke mzuri.’”³ Mujahid, Tawus, Ikrimah, Said bin Jubayr, Ibrahim An-Nakhai, Ash-Shabi, Al-Hasan, Qatadah, Az-Zuhri, Yazid bin Qusayt, Muqatil bin Hayyan na Al-Qasim bin Muhammad⁴ na wengine wengi miongoni mwa *salaf* na Maimamu walisema kuwa mtu anaruhusiwa kutaja Posa kwa ishara kwa mwanamke aliyefiwa na mume.

Pia inaruhusiwa kumposa kwa ishara mwanamke aliye katika hatua za mwisho baada ya kuachwa Talaka tatu. Mtume ﷺ alimwamuru Fatimah bint Kays رضي الله عنها abaki nyumbani kwa Ibn Umm Makhtum رضي الله عنه kwa ajili ya eda alipoachwa na mume wake, Abu Amr bin Hafs رضي الله عنه talaka ya tatu. Alimuambia:

«إِذَا حَلَلْتِ فَأَذِينِي»

“Nifahamishe Eda yako itapomalizika.”

Alipomaliza eda, Usamah bin Zayd رضي الله عنه, aliyeachwa huru na Mtume alimposa na Mtume ﷺ alimwozesha.⁵ Ama, kama mke aliyeachwa (talaka rejea), wamekubaliana wanazuoni kuwa hairuhusiwi kwa mtu mwingine asiyekuwa mume wake kumposa moja kwa moja au kwa ishara (kabla ya kuisha eda). Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

¹ At-Tabari 5:95

² At-Tabari 5:96.

³ Fat’hul Al-Bari 9:84.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:817-818.

⁵ Muslim 2:1114.

Allah تعالى Amesema:

أَوْ أَكُنْتُمْ فِي أَنْفُسِكُمْ

“... au mkadhamiria katika nyonyo zenu...”

Maana yake: Iwapo utaficha dhamira ya kutaka kuwapa wao. Allah تعالى Amesema:

وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٦٩﴾

“Na Mola wako Mlezi Anayajua yaliyoficha vifua vyao, na wanayoyatangaza...” (28:69)

Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema,

وَأَنَا أَعْلَمُ بِمَا أَحْفَيْتُمْ وَمَا أَعْلَنْتُمْ

“Na Mimi nayajua mnayoyaficha na mnayodhihirisha.” (60:1)

Hivyo Allah تعالى Amesema:

عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ سَتَذْكُرُونَهُنَّ

“Mwenyezi Mungu Anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka.”

Maana yake: Katika nyoyo zenu, hivyo Aliwasahilishieni. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَلَكِنْ لَا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا

“Lakini msiwaahidi kwa siri.” Ali bin Abu Talhal alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa:

وَلَكِنْ لَا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا

“...Lakini msiwaahidi kwa siri...” Maana yake: Usimuambie Mwanamke, “Nakupenda” au, “Niahidi kuwa hutoelewa na mtu mwingine (baada ya kwisha kwa eda) na kama hivyo.”¹ Said bin Jubayr, Ash-Shabi, Ikrimah, Abu Adh-Dhuha, Adh-Dhahhak, Az-Zuhri,² Mujahid na At-Thawri walisema kuwa (Ayah) ina maana kuchukua ahadi kuwa hatoolewa na mtu mwingine.³

¹ At-Tabari 5:107

² Ibn Abu Hatim 2:821

³ At-Tabari 5:109

Baada ya hapo Allah تعالى Amesema:

إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَّعْرُوفًا^٤

“...Ila mnene maneno mema...”

Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr,¹ As-Suddi, Ath-Thawri na Ibn Zayd رضي الله عنهم walisema kuwa Ayah hii ina maana kuposa kwa maneno ya kuzunguka, kama kusema, “Natamani kuwa na mtu kama wewe.”² Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى alisema: Nilimwuliza Ubaydah juu ya maana ya Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَّعْرُوفًا^٤

“...Ila mnene maneno mema...”

Akasema: “Anamuambia Walii wa mwanamke, ‘Usimuozeshe mpaka unifahamishe kwanza.” Kauli hii ilisimuliwa na Ibn Abu Hatim.³ Kisha Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَعْرَمُوا عُقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ^٤

“...wala msiazimie kufunga ndoa mpaka eda ifike mwisho wake.”

Maana yake: Msikusudie kufunga ndoa mpaka eda iishe. Ibn Abbas, Mujahid, Ash-Shabi, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas, Abu Malik, Zayd bin Aslam, Muqatil bin Hayyan, Az-Zuhri, Ata Al-Khurasani, As-Suddi, Ath-Thawri na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم walisema kuwa:

حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ^٤

“...mpaka eda ifike mwisho wake.”

Maana yake: “Msikamilishe ndoa kabla ya kumalizika eda.”⁴ Wanazuoni wamekubaliana kuwa posa kabla ya kwisha eda ni batili. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ^٤

“Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini Naye.”

¹ Ibn Abu Hatim 2:824.

² At-Tabari 5:114.

³ Ibn Abu Hatim 2:826.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:828-829.

Aya hii inawaonya wanaume dhidi ya kuficha dhamira zao ndani ya nyoyo zao kuhusu wanawake, ikiwaelekeza kuwafikiria mema badala ya uovu, na Allah تعالی hatowaacha wakate tamaa kupata Neema Zake, kama Alivyosema:

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٣٦﴾

“Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mpole.”

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ مَا لَمْ تَمْسُوهُنَّ أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً وَمَتَّعُوهُنَّ

عَلَى الْمَوْسَعِ قَدْرُهُ وَعَلَى الْمَقْتَرِ قَدْرُهُ مَتَّعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْإِحْسَانِ ﴿٢٣٦﴾

236. “Hapana ubaya kwenu mkiwapa talaka wanawake ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari yao. Lakini wapeni cha kuwaliwaza, mwenye wasaa kadiri awezavyo na mwenye dhiki kadiri awezavyo - maliwaza kwa mujibu wa dasturi kuwa ni haki juu ya watendao mema.”

Talaka Kabla ya Kufanyika Tendo la Ndoa

Allah تعالی Ameruhusu Talaka baada ya ndoa na kabla ya kufanyika kwa tendo la ndoa. Ibn Abbas, Tawus, Ibrahim na Al-Hasan Al-Basri رضي الله عنهم walisema kuwa “kugusa” (kulikotajwa ndani ya Ayah) ina maana kuingiliana kimwili.¹ Mume anaruhusiwa kumwacha mkewe kabla ya kujamiana naye na kutoa mahari endapo iliahirishwa kulipwa.

Mut’ah (Zawadi) ya Talaka:

Allah تعالی Anamwamrisha mume kumpa mke (aliyemwacha bila ya kujamiiana naye na wala kubainishwa kwa mahari yake) zawadi kulingana na hali aliyo nayo mume, tajiri kwa mujibu wa uwezo wake na masikini kwa mujibu wa uwezo wake. Al-Bukhari alisimulia kwenye *Sahih* yake kuwa Sahl bin Sa’d na Abu Usayd walisema kuwa Mtume ﷺ alimwoa Umaymah bint Shurahil. Alipoletwa kwa Mtume ﷺ alimnyooshea mkono, lakini hakulipenda hilo. Kisha Mtume ﷺ akamuamrisha Abu Usayd ampe vyakula na zawadi ya nguo mbili.²

¹ Ibn Abu Hatim 2:831.

² Fat’hul Al-Bari 9:269.

وَإِنْ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَيَصِفْ مَا فَرَضْتُمْ إِلَّا أَنْ
يَعْفُونَ. أَوْ يَعْفُوا الَّذِي بِيَدِهِ عَقْدَةُ الزَّكَاحِ ۗ وَأَنْ تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۗ وَلَا تَنْسُوا
الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٧﴾

237. “Na mkiwapa Talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari mlio agana, isipokuwa ikiwa wanawake wenyewe wamesamehe, au mume ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake awe amesamehe. Na kusameheana ndiko kulio karibu zaidi na uchamungu. Wala msisahau fadhila baina yenu. Hakika Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda.”

Mke Hupewa Nusu ya Mahr Iwapo Ataachwa Kabla ya Kuingiliwa:

Aya hii tukufu ni miongoni mwa zinazojulisha masuala ya *Mut’ah* (zawadi) iliyotajwa katika Aya iliyotangulia (kuacha kabla ya kujamiiana). Ayah hii (2:237) inamtaka mume aondoe nusu ya mahari iwapo atamtaliki mke kabla ya kumwingilia. Iwapo Aya ilikuwa inaelezea aina nyingine ya zawadi, basi ingetajwa, ukizingatia kuwa Ayah hii inafuatia iliyotangulia inayohusu somo hili. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Kulipa nusu ya mahari katika hali hii ni hali inayokubaliwa kwa mujibu wa wanazuoni. Hivyo, mume analipa nusu mahari iliyopangwa atakapomwacha kabla ya kujamiiana. Na Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا أَنْ يَعْفُونَ

“Isipokuwa ikiwa wanawake wenyewe wamesamehe.”

Maana yake: Wanawake, kuhusu nusu iliyowajibishwa kwake juu ya mumewe, basi hatawajibika kupatiwa kitu. Kisha Allah تعالى Amesema:

إِلَّا أَنْ يَعْفُونَ

“Isipokuwa ikiwa wanawake wenyewe wamesamehe.”

Maana yake: Mke anaposamehe haki zake.¹ Zaidi ya hayo, Imam Abu Muhammad bin Abu Hatim alisema kuwa ilisimuliwa kuwa Shurayh, Said bin

¹ Ibn Abu Hatim 2:839.

Musayyib, Ikrimah, Mujahid, Ash-Shabi, Al-Hasan, Nafi, Qatadah, Jabir bin Zayd, Ata Al-Khurasani, Adh-Dhahhak, Az-Zuhri, Muqatil bin Hayyan, Ibn Sirin, Ar-Rabi bin Anas na As-Suddi walisema vivyo hivyo.¹ Kisha Allah تعالى Amesema:

أَوْ يَعْفُوا الَّذِي بِيَدِهِ عَقْدَةُ النِّكَاحِ ؕ

“Au mume ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake awe amesamehe.”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Amr bin Shu’ayb alisema kuwa babu yake alimsimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«وَلِيُّ عَقْدَةِ النِّكَاحِ الرَّزْجُ»

“Ufanikishaji wa mkataba wa ndoa upo mikononi mwa mume.”²

Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى, pia ameandika Hadithi hii, na ni maoni yaliyokhitariwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Hadithi inasema kuwa mume ndiye mtu ambaye ndoa iko katika dhima yake akitaka anaiendeleza au kuivunja. Kwa upande mwingine, watu wa mke haruhusiwi kuchukua au kutoa chochote bila ruhusa ya mke, hususan mahari. Kisha Allah تعالى Amesema;

وَأَنْ تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ؕ

“Na kusameheana ndiko kulio karibu zaidi ya uchamungu.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa kauli hii inawahusu wanaume na wanawake wote.”³ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

وَأَنْ تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ؕ

“Na kusameheana ndiko kuliko karibu zaidi ya uchamungu.”

Mchamungu zaidi ni yule anaesamehe.⁴ Hivi ndivyo pia Ash-a’bi alivyonukuliwa.

¹ Ibn Abu Hatim 2:840-842.

² Ibn Abu Hatim 2:842.

³ At-Tabari 5:162.

⁴ At-Tabari 5:162.

Mujahid, An-Nakhai, Adh-Dhahhak, Muqatil bin Hayyan, Ar-Rabi bin Anas na Thawri walisema kuwa 'fadhila' zilizotajwa kwenye Aya zinahusu mke kusamehe nusu yake ya Mahari au mume kulipa mahari yote.¹ Hii ndiyo sababu Allah تعالى Amesema hapa,

وَلَا تَنسُوا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ

“Wala msisahau fadhila baina yenu.”

Maana: Wema (au ukarimu), kama Said alivyosema.² Allah تعالى Amesema:

إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anayaona mnayotenda.”

Maana yake: Hapana katika mambo yenu yanayoepa Uoni wa Allah تعالى ulio madhubuti, na Atamlipa kila mmoja kwa mujibu wa amali zake.

* * *

¹ At-Tabari 5:165-166.

² At-Tabari 5:166.

حَفِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَىٰ وَقُومُوا لِلَّهِ
 قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾ فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنْتُمْ
 فَأَذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُمْ مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ
 ﴿٢٣٩﴾ وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا وَصِيَّةً
 لِأَزْوَاجِهِمْ مَتَاعًا إِلَى الْحَوْلِ غَيْرَ إِخْرَاجٍ ۖ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا
 جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ مِنْ مَّعْرُوفٍ ۗ
 وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٤٠﴾ وَلِلْمُطَلَّقَاتِ مَتَاعٌ بِالْمَعْرُوفِ ۗ
 حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿٢٤١﴾ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ
 آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٤٢﴾ * أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا
 مِنْ دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ فَقَالَ لَهُمُ اللَّهُ مُوتُوا
 ثُمَّ أَحْيَاهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ
 أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٢٤٣﴾ وَقَتِلُوا فِي سَبِيلِ
 اللَّهِ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٤﴾ مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ
 اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ أَمْعَافًا كَثِيرَةً ۗ وَاللَّهُ
 يَقْبِضُ وَيَبْصُطُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٤٥﴾

حَفِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ
 الْوُسْطَىٰ وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾
 فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ
 فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَأَذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا
 عَلَّمَكُمْ مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ
 ﴿٢٣٩﴾

238. "Zilindeni Sala, na khasa Sala ya katikati, na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kuqunuti (kunyenyeke)."

239. "Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda. Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama Alivyokufunzeni yale mliyo kuwa hamyajui."

Allah تعالى Ameamrisha kuwa Sala isaliwe kwa makini na kwa wakati. Imeandikwa katika Sahih

Mbili kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, "Nilimuuliza Mtume ﷺ, "Amali gani bora zaidi (kwa Allah)?" Akajibu:

«الصَّلَاةُ عَلَى وَقْتِهَا»

"Kusali kwa wakati wake."

Nikauliza, "Ni ipi hiyo inayofuatia (kwa ubora)?" Akajibu:

«الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Jihad katika njia ya Allah.”

Nikauliza tena, “Ipi inayofuatia (kwa ubora)?” Akajibu:

«بِرُّ الْوَالِدَيْنِ»

“Kuwafanyia wema wazazi wawili.”

Kisha Abdallah رضي الله عنه aliongeza, “Mtume ﷺ alinieleza maneno haya, na kama ningauliza zaidi, Mtume ﷺ angenieleza zaidi.”¹

Sala ya Katikati:

Allah تعالى Ameetaja Sala ya katikati ambayo ni Swala ya Alasiri kwa mujibu wa kauli ya wanazuoni walio wengi miongoni mwa Maswahaba, kama At-Tirmidhi na Al-Baghawi walivyosema. Kadhi Al-Mawardi رحمه الله تعالى aliongeza kuwa wanazuoni wengi katika *Tabiin* wana rai hii pia. Al-Hafidh Abu Umar bin Abdul-Barr رحمه الله تعالى alisema kuwa hii ni rai ya wanazuoni wengi wa Athar (Hadithi na kauli za *Salaf*). Kwa nyongeza, Abu Muhammad bin Atiyah رحمه الله تعالى alisema kuwa hii ni Tafsiri (ya Sala ya kati) ya wanazuoni wengi. Al-Hafidh Abu Muhammad Abdul-Mu'min bin Khalaf Ad-Dimyati رحمه الله تعالى alieleza ndani ya kitabu chake kuhusu Sala ya kati ya Alasiri. Na kauli hiyo pia imesimuliwa kutoka kwa Umar, Ali, Ibn Mas'ud, Abu Ayyub, Abdullah bin Amir, Samurah bin Jundab, Abu Hurayrah, Abu Said, Hafsa, Umm Habibah, Umm Salamah, Ibn Abbas na Aishah رضي الله عنهم. Hii pia ni Tafsir ya Ubaydah, Ibrahim An-Nakhai, Razin, Zirr bin Hubaysh, Said bin Jubayr, Ibn Siriin, Al-Hassan, Qatadah, Adh-Dhahhak, Al-Kalbi, Muqatil, Ubayd bin Abu Maryam na wengine.

Ushahidi kuwa Sala ya Alasiri ni Sala ya Katikati:

Imam Ahmad alisimulia kuwa Ali رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema wakati wa vita vya Al-Ahzab.

«سَعَلُونَا عَنِ الصَّلَاةِ الْوُسْطَى، صَلَاةِ الْعَصْرِ، مَلَأَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ وَبَيَّنَّوْتَهُمْ نَارًا»

“Wao (makafiri) walitushughulisha ili tuisali Swala ya kati na kati Swala ya Alasiri, Allah Ajaze nyoyo zao na nyumba zao kwa moto.”

¹ Fat'hul At-Bari 2:12 na Muslimu 1:90.

Halafu aliswali Alasiri baina ya Maghrib na Isha.¹ Muslim² na An-Nasai waliandika Hadithi hii. Kwa nyongeza, Mashaikh Wawili, Abu Dawud, At-Tirmidhi, An-Nasai na wakusanyaji wengine wa Sunan waliinukuu Hadithi hii wakitumia isnadi ya wapokezi mpaka kwa Ali رضي الله عنه.³

Hadithi kuhusu vita vya Al-Ahzab, wakati Washirikina walipomzuia Mtume ﷺ na Maswahaba wake, kusali Alasiri, imesimuliwa na Masahaba kadha. Tumetaja masimulizi yanayoelezea Sala ya kati ni Sala ya Alasiri. Zaidi ya hivyo, Muslim alisimulia Hadithi sawa na hii kutoka kwa Ibn Mas'ud na Al-Baral bin Azib رضي الله عنهما.⁴

Kwa nyongeza, Imam Ahmad alisimulia kuwa Samurah bin Jundab رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«صَلَاةُ الْوُسْطَى: صَلَاةُ الْعَصْرِ»

“Sala ya kati na kati ni Sala ya Alasiri.”⁵

Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ alitaja:

حَنَفُظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى

“Zilindeni Sala khasa Swala ya katikati...”

Na akataja kuwa ni Sala ya Alasiri.⁶ Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«هِيَ الْعَصْرُ»

“Ni Sala ya Asr.”

Na Ibn Jafar رضي الله عنه alitaja kuwa Mtume ﷺ alikuwa ameulizwa juu ya Sala ya kati na kati.⁷

¹ Ahmad 1:113.

² Muslim 1:437.

³ Fat'hul Al-Bari 6:124, 7:467, 8:43, 11:197; Muslim 1:436; Abu Dawud 1:287, Tufat Al-Ahwadhi 8:328; An-Nasai 1:236 na Ahmad 1:137.

⁴ Muslim 1:437 - 438.

⁵ Ahmad 5:22.

⁶ Ahmad 5:8.

⁷ Ahmad 5:7

At-Tirmidhi aliisimulia Hadithi hii na akaitaja kuwa ni *"Hasan Sahih."*¹ Kwa nyongeza, Abu Hatim bin Hibban رحمه الله تعالى alisimulia katika *Sahih* yake kuwa Abdallah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«صَلَاةُ الْوَسْطَى صَلَاةُ الْعَصْرِ»

*"Sala ya kati na kati ni Sala ya Alasiri."*²

At-Tirmidhy amesema kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alipokea kuwa Mtume ﷺ amesema,

«صَلَاةُ الْوَسْطَى صَلَاةُ الْعَصْرِ»

"Sala ya kati na kati ni Sala ya Alasiri."

At-Tirmidhi pia, alielezea kuwa Hadithi hii ni *Hasan Sahih.*³ Muslim alisimulia kuwa imo Hadithi katika *Sahih* na maneno yake ni:-

«شَغَلُونَا عَنِ الصَّلَاةِ الْوَسْطَى صَلَاةِ الْعَصْرِ»

*"Wao (makafiri) walitushughulisha ili tuisali Sala ya kati na kati, Sala ya Alasiri."*⁴

Maandiko haya yanatilia mkazo ukweli (kuwa Sala ya Alasiri ni Sala ya katikati). Kinachothibitisha zaidi ukweli huu, katika Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ alisisitiza umuhimu wa kuchunga Sala ya Alasiri, aliposema, kama Ibn Umar رضي الله عنهما alivyosimulia:

«مَنْ قَاتَهُ صَلَاةُ الْعَصْرِ فَكَأَنَّمَا وَتَرَ أَهْلَهُ وَمَالَهُ»

*"Yeyote anayekosa kusali sala ya Alasiri atakuwa kama mtu aliyepoteza familia yake na mali yake."*⁵

Imesimuliwa kwenye *Sahih* kutoka kwa Buraydah bin Al-Husayb رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:328

² Ibn Hibban 3:121

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:329

⁴ Muslim 1:437

⁵ Muslim 1:436

«بَكُرُوا بِالصَّلَاةِ فِي يَوْمِ الْغَيْمِ، فَإِنَّهُ مَنْ تَرَكَ صَلَاةَ الْعَصْرِ، فَقَدْ حَيَّطَ عَمَلُهُ»

“Siku ya mawingu, salini swala ya (Alasiri) mapema, kwa anayekosa kuswali Alasiri, amali zake njema zitafutwa.”¹

Imekatazwa Kuzungumza wakati wa Sala:

Allah تعالى Amesema:

﴿قَوْمُوا لِلَّهِ قَنِينًا﴾

“Na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kukunuti (kunyenyekoa).”

Maana yake: Kwa unyenyekevu na utiifu mbele Yake (wakati wa Sala). Amri hii inaonesha kuwa hairuhusiwi kuzungumza wakati wa Sala, kwa kuwa kuzungumza ni kinyume na mazingira ya Sala. Hii ndiyo sababu Mtume ﷺ alikataa kumjibu Ibn Mas’ud رضي الله عنه alipomsalimu akiwa ndani ya Sala na alisema baada ya hapo:

﴿إِنَّ فِي الصَّلَاةِ لَشُغْلًا﴾

“Sala inamshughulisha mtu vya kutosha.”²

(Maana yake: Kwa vitendo mbalimbali mwili, ulimi na moyo kuhusika kwenye Sala). Muslim alisimulia kuwa Mtume ﷺ alimwambia Muawiyah bin Hakam As-Sulami رضي الله عنه alipozungumza wakati wa Sala:

﴿إِنَّ هَذِهِ الصَّلَاةَ لَا يَضْلُحُ فِيهَا شَيْءٌ مِنْ كَلَامِ النَّاسِ، إِنَّمَا هِيَ التَّسْبِيحُ وَالتَّكْبِيرُ وَذِكْرُ اللَّهِ﴾

“Hakika hizi Sala haifai ndani yake Mazungumzo ya watu. Hakika hiyo ni kwa ajili ya Tasbihi, Takbir na Dhikri.”³

Imam Ahmad alisimulia kuwa Zayd bin Arqam رضي الله عنه alisema, “Mtu mmoja alikuwa akiwahadithia rafiki zake mambo mbalimbali wakati wa Sala. Kisha Aya hii ikateremshwa:

¹ Ibn Majah 1:224.

² Muslim 1:382.

³ Muslim 1:381.

وَقَوْمًا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾

“Na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kukunuti (kunyenyekoa).”

Tunaamriwa kunyamaza.¹ Kundi yaani Wakusanyaji wa Hadithi isipokuwa Ibn Majah waliandika Hadithi hii.²

Sala ya Khofu:

Allah تعالی Amesema:

فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَأَدْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا

تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٩﴾

239. “Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda. Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama Alivyokufunzeni yale yaliyokuwa humyajui.”

Baada ya Allah تعالی Kuwaamuru waja Wake kusali kwa ukamilifu na kusesitizia amri hii, Alitaja hali ambayo mtu anaweza kushindwa kusali kwa utulivu, wakati wa vita na mapambano. Allah تعالی Amesema:

فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ

“Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda.”

Maana yake: Salini katika hali inayofaa katika mazingira haya, ima ni kwa miguu au kwa kupanda, yaani kwa kuelekea Qiblah au vinginevyo. Imam Malik alisimulia kuwa Nafi alisimulia kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alikuwa akiielezea Sala ya Khofu mkienda kwa miguu, mmepanda, mkielekea Qiblah au vinginevyo.” Nafi alitoa maelezo yafuatayo, “Nadhani aliipokea kutoka kwa Mtume ﷺ.³ Al-Bukhari na Muslim waliandika Hadithi hii.⁴

¹ Ahmad 4:368.

² Fatuhl Bari 3:88 na Muslim 1:383, Abu Dawud 1:583, Tuhfatul Ahwadh 3:330 na An-Nasai 3:18.

³ Al-Muwatta 1:184.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:46, Muslim 1:574.

Imamu Muslim, Abu Dawud, An-Nasai, Ibn Majah na Ibn Jarir walisimulia kuwa Sayyidina Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Allah تعالى Amefaradhisha Sala kwa maneno ya Mtume ﷺ: Rakaa nne ukiwa katika makazi na rakaa mbili ukiwa safarini na rakaa moja wakati wa Khofu."¹ Hii pia ni rai ya Al-Hassan Al-Basri, Qatadah, Adh-Dhahhak, na wengine.²

Kwa nyongeza, Bukhari ameipa kichwa cha habari: "Sala wakati wa kukabiliana na Ngome ya Maadui." Al-Awzai رحمه الله تعالى alisema, Iwapo Waislam wamekaribia kupata ushahidi na hawawezi kusali kwa kawaida, waswali kwa ishara kila mmoja ndani ya nafsi yake mpaka mapigano yaishe. Endapo watashindwa kabisa, waakhirishe Sala mpaka mapigano yaishe. Watakapohisi wako salama, wasali rakaa mbili. Iwapo hawatamudu, wasali rakah moja yenye sijida mbili. Wakishindwa, basi Takbir peke yake haitoshelezi, hivyo waakhirishe Sala mpaka kutakapokuwa na usalama." Rai hii ni sawa na ya Mak-hul. Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, "Nilishiriki katika uvamizi wa ngome ya Tustar, wakati mwangaza wa alfajiri ulipoanza kuwa wazi. Ghafla, mapambano yalianza na Waislamu wakashindwa kusali mpaka mwangaza wa mchana ulipoangaza. Kisha tuliswali (Sala ya Subhi) na Abu Musa رضي الله عنه na tulishinda vita. Anas رضي الله عنه akasema: Na hakuna sala iliyonifaharisha kuliko ya siku hiyo, kushinda hata dunia na vilivyomo ndani yake. Tamko la upokezi wa Hadithi hii ni la Bukhari.³

Amri ya Kutimiza Sala Wakati wa Amani:

Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا أُمِنْتُمْ فَأَذْكُرُوا اللَّهَ

"Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu."

Maana yake: "Swalini kama Nilivyokuamrisheni kwa kukamilisha; rukuu, sijida, kusimama, kitako na utulivu wa moyo na Dua." Allah تعالى Amesema

كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ

"Kama Alivyokufunzeni yale mliyokuwa hamyajui."

¹ Muslim 1:478, 479; Abu Dawud 2:40, An-Nasai 3:169; Ibn Majah 1:339 na At-Tabari: 5:247

² At-Tabari 5:240 - 241

³ Fat'hul Al-Bari 2:503

Maana yake: Kama Alivyowaruzuku, Akawaongoza na Akawafundisha kuhusu manufaa mtakayoyapata katika maisha ya dunia na Akhera hivyo mshukuruni na mdhukuruni Yeye. Hivyo, Allah تعالى Alisema baada ya kutaja Sala ya Khofu.

فَإِذَا أَطْمَأْنَنْتُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا ﴿١٥٣﴾

“Na mtapotulia basi shikeni Swala kama desturi. Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyowekewewa wakati maalumu.”
(4:103)

Tutataja Hadithi juu ya Sala ya Khofu na maelezo yake kwenye Surat An-Nisa wakati wa kutaja Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذَا كُنْتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ

“(Ewe Mjumbe Muhammad!) Na unapokuwa pamoja nao, ukawasalisha.” (4:102)

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذُرُونَ أَزْوَاجًا وَصِيَّةً لِأَزْوَاجِهِمْ مَتْنَعًا إِلَى الْحَوْلِ غَيْرَ إِخْرَاجٍ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ مِنْ مَّعْرُوفٍ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٥٣﴾ وَلِلْمُطَلَّقاتِ مَتْنَعٌ بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿١٥٤﴾ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٥٥﴾

240. “Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakawacha wake, na wausie kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kuwatoa nyumbani. Na wanawake wenyewe wakiondoka, basi hapana ubaya kwenu kwa waliyojifanyia wenyewe kwa mujibu wa sharia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

241. “Na wanawake walioachwa wapewe cha kuwaliwaza kwa mujibu wa Sharia. Haya ni wajibu kwa wachamngu.”

242. “Namna hivi Anakubainishieni Mwenyezi Mungu Aya Zake ili mpate kufahamu.”

Kufutwa kwa Aya hii: (2:240)

Wanazuoni wengi walisema kuwa Aya (2:240) ilifutwa na Ayah (2:234) kwa lile Alilosema Allah تعالى:

يَتَرْتَضْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا^ط

“Hawa wake wangoje peke yao miezi minne na siku kumi.” (2:234)

Kwa mfano, Al-Bukhari alisimulia kuwa Ibn Az-Zubayr رضي الله عنه alisema: Nilimwambia Uthman bin Affan رضي الله عنه, Aya,

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا

“Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakaacha wake...”

Ilifutwa na Aya nyengine (2:234), kwa hiyo, kwa nini uliikusanya (Maana yake: Ndani ya Qur’an)?” Kama jibu, “Ewe mpwa wangu! Sitabadili sehemu yoyote ya Qur’an kutoka mahala pake.”¹

Swali ambalo Az-Zubayr رضي الله عنه alimuuliza Uthman رضي الله عنه lina maana: Kama hukumu ya aya (2:240), ilifutwa kwa miezi minne (eda ya mjane na kurejea katika Aya ya 2:234) basi kuna hekima gani kuibakiza ndani ya Qur’an, japokuwa hukumu yake ilifutwa? Iwapo Aya (2:240) inabaki (ndani ya Qur’an) baada ya Aya iliyoifuta (2:234), inaweza ikachukuliwa kuwa hukumu yake bado inafanya kazi. Uthman رضي الله عنه, Amiri wa Waumini, alimjibu kwa kusema kuwa haya ni masuala ya wahyi, ambao umeitaja Ayah hiyo kwa utaratibu huu. Kwa hiyo nitaiacha Aya pale nilipoikuta ndani ya Qur’an.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Kauli ya Allah تعالى.

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا وَصِيَّةً لِأَزْوَاجِهِمْ مَتَاعًا إِلَى الْاَحْوَالِ غَيْرِ
إِخْرَاجٍ^ع

“Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakawaacha wake, na wausie kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kuwatoa nyumbani.”

¹ Fat’hul Al-Bari 8:48.

“Mjane alikuwa akiishi, na kupewa matumizi kwa mwaka mmoja, katika nyumba ya marehemu na mume wake. Baadaye, Aya iliyoweka wazi mirathi (4:12) ilifuta Aya (2:240), hivyo mjane hurithi robo au thumuni ya mali aliyoiacha mumewe aliyefariki.”¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى pia alisimulia kuwa Ali bin Talhah alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtu anapokufa na kuacha mjane, alitakiwa kubakie eda nyumbani mwaka mzima, na wakati huu akipewa mahitaji yake.” Kwa hiyo Allah تعالى Aliteremsha Aya hii:

وَالَّذِينَ يَتُوفُونَ مِنْكُمْ وَيَذُرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا^ط

“Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakaacha wake, hawa wake wangoje peke yao miezi minne na siku kumi.” (2:234)

Hii ndio eda ya mjane, isipokuwa kama alikuwa mja mzito, huyu eda yake inakwisha anapojifungua. Pia Allah تعالى Amesema:

وَلَهُنَّ الرُّبُعُ مِمَّا تَرَكْتُمْ إِنْ لَمْ يَكُنْ لَكُمْ وَلَدٌ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ وَلَدٌ فَلَهُنَّ الثُّمُنُ مِمَّا تَرَكْتُمْ^ع

“...Na wake zenu watapata robo ya mlichokiacha, ikiwa hamna mtoto. Mkiwa mna mtoto basi sehemu yao ni thumuni ya mlichokiacha....” (4:12)

Hivyo Allah تعالى Ameweka wazi kiwango cha mjane katika mirathi na hapahitajiki Wasia au Nafaqah (matunzo ambayo yalitajwa katika (2:240)²

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alieleza kuwa Mujahid, Al-Hassan, Ikrimah, Qatadah Adh-Dhahhak, Ar-Rabi na Muqatil bin Hayyan walisema kuwa Aya (2:240) ilifutwa na:

أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا^ط

“...miezi minne na siku kumi.” (2:234)³

Bukhari alisimulia kuwa Mujahid alisema kuwa:

¹ Ibn Abu Hatim 2:871.

² At-Tabari 5:255.

³ Ibn Abu Hatim 2:875.

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا

“Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakaacha wake” (2:234)

Hiyo ilikuwa eda ya mjane alitakiwa kubaki na familia ya mumewe aliye kufa (katika kipindi hicho, miezi minne na siku kumi). Ikiwa ni wajibu Kisha Allah تعالی Akateremsha:

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا وَصِيَّةً لِّأَزْوَاجِهِمْ مَّتَّعًا إِلَى الْاَحْوَالِ غَيْرِ
اِخْرَاجٍ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ مِنْ مَّعْرُوفٍ^٤

“Na wale miongoni mwenu wanaokufa na wakawaacha wake, na wausie kwa ajili ya Wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kuwatoa nyumbani. Na wanawake wenyewe wakiondoka, basi hapana ubaya kwenu kwa waliojifanyia wenyewe kwa mujibu wa sharia.” (2:240)

Hivyo, Allah تعالی Aliifanya sehemu iliyobaki ya mwaka, ambayo ni miezi saba na siku ishirini, kama muda uliobaki na agano kwake. Pamoja na hayo, kama anapenda, anaweza kutumia haki yake na akabaki ndani ya nyumba ya marehemu baada ya miezi minne na siku kumi kwisha. Hii ndiyo maana Alivyosema Allah تعالی:

غَيْرِ اِخْرَاجٍ^٤ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

“Bila kuwatoa katika nyumba. Na wanawake wenyewe wakiondoka basi hapana ubaya kwenu.”

Kwa hiyo, muda unaotakiwa kwa eda haujabadilika (rejea 2:234) Ni Wajibu juu yake. Inadaiwa kuwa huo ni mtazamo wa Mujahid. Ata alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما, “Aya hii (2:240) ilifuta (muda unaohitajika) kwa mjane kukaa eda pamoja na familia ya marehemu. Hivyo atautumia muda wa eda popote atakapo.” Hii ni maana ya Kauli ya Allah تعالی.

غَيْرِ اِخْرَاجٍ^٤

“...bila kuwatoa katika nyumba...” Pia Ata alisema: “Iwapo anataka, atakaa eda na familia yake na atakaa hapo kwa sehemu ya mwaka iliyobaki. Iwapo anataka, anaruhusiwa kuondoka, Allah تعالی Amesema:

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْتُمْ

“...basi hapana ubaya kwenu kwa waliyojifanyia wenyewe...”

Kisha Ata Akasema: “Kisha (Aya kuhusu) mirathi (rejea 4:12) ilikuja na kufuta suala la ukazi. Hivyo mjane anakaa eda popote apendapo na hatokuwa na ukazi mahususi.”¹

Kauli ya Ata na wale wenye maoni kuwa Ayah (2:240) ilifutwa na Ayah juu ya mirathi (4:12), ni sahihi iwapo tu ni kwa zaidi ya miezi minne na siku kumi (zilizohitajika katika 2:234). Hata hivyo, iwapo wana maana kuwa ukazi wa mwanamke kwa muda wa miezi minne na siku kumi si wajibu katika mali ya marehemu. Ikiwa wanakusudia hivyo, hili ni suala ambalo maimamu wametofautiana mitazamo yao, wapo wanazuoni waliotoa hoja ya kuwa mjane anatakiwa kubaki katika nyumba ya mumewe aliyofariki kwa (miezi minne na siku kumi) kwa mujibu wa simulizi ya Malik aliyopokea kutoka kwa Zaynab bint Ka’b bin Ujrah. Alisema kuwa Fariah bint Malik bin Sinan رضي الله عنها, dadake Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه alimuambia kuwa alikwenda kwa Mtume ﷺ alimwomba arejee kwenye nyumba ya familia ya banu Khudhrah. Mume wake aliwafuatilia baadhi ya watumishi wake waliokimbia, lakini alipofika eneo la Al-Qadam, walimuua. Akasema, “Hivyo nikamwomba Mtume ﷺ nikae na familia yangu, Banu Khud’hrah, kuwa marehemu mume wangu hakuniachia nyumba aliyokuwa akiimiliki au Nafaqah (matumizi), Mtume ﷺ alinikubalia. Nilipokuwa chumbani, Mtume ﷺ aliniita au alimtuma mtu aniite na akasema:”

«كَيْفَ قُلْتِ؟»

“Umesema nini?”

Nikarudia kumuelezea kile kisa cha marehemu mume wangu. Akasema:

«امْكُنِّي فِي بَيْتِكَ حَتَّى يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ»

“Kaa nyumbani kwako mpaka eda iishe.”

Hivyo nikakaa eda kwa miezi minne na siku kumi katika nyumba ya marehemu mume wangu. Baadaye Uthman bin Affan رضي الله عنه wakati wa utawala wake akamuuliza juu ya suala hili na nikamweleza yaliyo jiri. Alitoa hukumu sawa na ile ya mwanzo.²

¹ Al-Bukhari 4531,5344.

² Al-Muwattaa’ 2:591.

Hadithi hii ilikusanywa pia na Abu Dawud, An-Nassai na Ibn Majah.¹ At-Tirmithi alisema kuwa ni “*Hasan Sahih*”

Uwajibu wa *Mut'ah* (Zawadi) wakati wa kutaliki:

Allah تعالی Amesema:

وَلَمَّا طَلَّقْتِ مَتْعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿٢٣٨﴾

“Na wanawake walioachwa wapewe cha kuwaliwaza kwa mujibu wa Sharia. Haya ni wajibu kwa wachamungu.”

Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema kuwa wakati Kauli ya Allah تعالی.

مَتْعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْحَسِينِ ﴿٢٣٦﴾

“Maliwaza kwa mujibu wa desturi kuwa ni haki juu ya watendao mema.” (2:236)

Ilipoteremshwa, mtu akasema, “Nikitaka, nitakuwa mwema na kama sitaki, sitokuwa.” Baada ya hapo, Allah تعالی Aliteremsha Ayah hii.

وَلَمَّا طَلَّقْتِ مَتْعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿٢٣٩﴾

“Na wanawake walioachwa wapewe cha kuwaliwaza kwa mujibu wa Sharia. Haya ni wajibu kwa wachamungu.”²

Wanazuoni waliohukumu kuwa *Mut'ah* wakati wa kumwacha mke inatakiwa kutolewa kwa kila anayeachwa, ima alipewa mahari au hakupewa na kama tendo la ndoa lilikamilika au halikukamilika, walitegemea Ayah (2:241) walipotoa hukumu yao. Hii ni rai iliyochukuliwa juu ya somo hili na Said bin Jubayr na wengine wengi miongoni mwa *Salaḥ*³ na pia Ibn Jarir رحمه الله تعالی. Kwa hivyo, Kauli ya Allah تعالی:

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَقْتُمْ الْبِئْسَاءَ مَا لَمْ تَمْسُوهُنَّ أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً وَمَتَّعُوهُنَّ

عَلَى الْمَوْسِعِ قَدْرُهُ وَعَلَى الْمُقْتَرِ قَدْرُهُ مَتْعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْحَسِينِ ﴿٢٤١﴾

¹ Abu Dawud 2:773; Tuhfat Al-Ahwadhi 4:319; An-Nasai 6:200; Ibn Majah 1:654.

² At-Tabari 5:264.

³ At-Tabari 5:263.

“Hapana ubaya kwenu mkiwapa talaka wanawake ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari yao. Lakini wapeni cha kuwaliwaza, mwenye wasaa kadiri awezavyo na mwenye dhiki kadri awezavyo - maliwaza kwa mujibu wa dasturi kuwa ni haki juu ya watendao mema.” (2:236)

Aya (2:236) inataja mambo mahususi ya hukumu hii ya jumla. Kisha Allah تعالی Amesema:

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ

“Namna hivi Anakubainishieni Mwenyezi Mungu Aya Zake...”

Maana yake: Anachoruhusu, kukataza, mahitaji, mipaka Aliyoiweka, Amri Zake na Aliyoyaharamisha, yote yameelezwa na kuwekwa wazi kwenu. Hapana Aliloliacha katika hali ya jumla mlipohitaji mambo makhsusi,

لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“...ili mpate kufahamu...”

Maana yake: Kuelewa na kuzingatia.

• أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ فَقَالَ لَهُمُ اللَّهُ مُوتُوا ثُمَّ أَحْيَاهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَئِنْ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٢٤٣﴾
 وَقَتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٤﴾ مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ أَمْعَافًا كَثِيرَةً وَاللَّهُ يَقْبِضُ وَيَبْصُطُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٤٥﴾

243. “Hukuwaona wale waliotoka majumbani mwao kwa maelfu kwa kuogopa mauti? Mwenyezi Mungu Akawaambia: Kufeni! Kisha Akawahauisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila juu ya watu, lakini wengi wa watu hawashukuru.”

244. “Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwentenzi Mungu ni Msikizi na Mjuzi.”

245. “Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili Amzidishie mzidisho mwingi, na Mwenyezi Mungu Hukunja na Hukunjua. Na Kwake Yeye mtarejea.”

Kisa cha Watu Hawa Waliokufa

Ibn Abu Hatim alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa watu hawa waliotajwa humu, walikuwa wakazi wa kijiji kiitwacho Dawardan. 'Ali bin' Asim alisema kuwa walitokea Dawardan, kijiji kilichopo maili kadha kutoka Wasit (Iraq). Katika Tafsiri yake, Waki bin Jarrah ilisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliitolea Aya hii maelezo,

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ

“Hukuwaona wale waliotoka majumbani kwao kwa maelfu kwa kuogopa kifo?”

Walikuwepo watu elfu nne walisalimika na ugonjwa wa Tauni uliotokea katika mji wao. Wakasema, “Lazima tuhamie mji usio na maafa!” Walipofika eneo Fulani, Allah تعالى Akawaambia:

﴿ مُوتُوا

“...*kufeni...*” Na wote wakafa. Baadaye, mmoja wa Mitume alipita mahala pale na akamwomba Allah تعالى Awafufue na Allah تعالى Akawarejeshea uhai. Hivyo Allah تعالى Akasema:

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ

“Hukuwaona wale waliotoka majumbani mwao kwa maelfu kwa kuogopa mauti?”

Zaidi ya hayo, wanazuoni wengi miongoni mwa *Salaf* walisema kuwa watu hao walikuwa wakazi wa mji zama za Wana wa Israel. Hali ya hewa katika mji huo haikuwafaa na ugonjwa wa kuambukiza ulitokea. Waliukimbia mji wao wakiogopa kifo na wakakimbilia maporini. Baadaye waliwasili katika (ardhi) bonde lenye rutuba na wakajaza pande zote. Kisha Allah تعالى Akawatuma malaika wawili, mmoja kutoka juu ya bonde na mwingine chini ya bonde. Malaika walipiga ukelele mara moja na watu wote walikufa papo hapo, kama kifo cha mtu mmoja. Hivyo basi, wakawekea uzio na ukuta na kaburi zao zikajengewa. Miili yao ilisambaratika na kuozeana. Baada ya kupita muda mrefu, Nabii mmoja wa wana wa Israel, ambaye jina lake akiitwa Hizqil (Ezekiel), alipita pale na akamuomba Allah تعالى Awarejeshee uhai kwa mkono

wake. Allah تعالی Aliipokea Dua yake na akamuamrisha aseme, “Enyi mifupa iliyooza, Allah تعالی Anakuamrisheni muwe pamoja. Mifupa ya kila mwili ilikusanyika pamoja. Kisha Allah تعالی Akamuamrisha aseme, “Enyi mifupa, Allah تعالی Anawaamrisha mfunikwe na nyama, mishipa na ngozi.” Hayo yalijiri wakati Hizqil alikuwa akiangalia. Kisha Allah تعالی Akamuamrisha aseme, “Enyi roho, Allah تعالی Anawaamuru mrejee, kila moja kwenye mwili ambao ukikaa. “ Wote walifufuka, wakiangalia sehemu iliyozingira baada ya kuteketea muda mrefu na kusema, “Utakatifu ni Wako (ewe Allah تعالی!) na hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa, isipokuwa Wewe.”

Inafaa kueleza kuwa kuwarejeshea watu uhai ni ushahidi ulio wazi kuwa ufufuo wa kimwili utatokea siku ya Kiyama. Ndio sababu Allah تعالی Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila juu ya watu...”

Maana yake: Ni kuwa Anawaonesha ishara kubwa, ushahidi madhubuti na dhahiri. Bali,

وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ

“...lakini wengi wa watu hawashukuru.”

Kwa kuwa hawamshukuru Allah تعالی kwa yale Aliyowapa katika maisha yao ya dunia na mambo ya kidini. Kisa cha watu waliokufa (2:244 hapo juu) pia kinaonesha kuwa hapana tahadhari inayoweza kubadili Khatima na Kudura ya Allah تعالی, hakuna uokovu isipokuwa kwa Allah تعالی Pekee. Watu hawa waliukimbia mji wao wakichelea ugonjwa mbaya na wakitaraji kufurahia maisha marefu. Walichochuma ni kinyume na walichokitafuta, kwani kifo kiliwajia haraka na kuwachukua wote.

Kuna Hadithi *Sahih* kuwa Imam Ahmad alisimulia kutoka kwa Abdullah bin Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه wakati mmoja alikwenda Sham (Syria). Alipofika mahali panapoitwa Sargha, alilakiwa na Majemedari wa Jeshi. Abu Ubaydah bin Jarrah na wafuasi wake رضي الله عنهم wakamwambia ugonjwa wa kuambukiza umetokea Ash-Sham. Kisha Hadithi

¹ At-Tabari 5:266.

ikataja kuwa Abdur-Rahman bin Awf رضي الله عنه ambaye hakuwepo, alikuwa na shughuli nyingine, alikuja na kusema, "Nazifahamu khabari hizi. Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:"

«إِذَا كَانَ بِأَرْضٍ وَأَنْتُمْ بِهَا فَلَا تَخْرُجُوا فِرَارًا مِنْهُ، وَإِذَا سَمِعْتُمْ بِهِ بِأَرْضٍ فَلَا تَقْدُمُوا عَلَيْهِ»

"Iwapo mpo katika ardhi fulani, (kuna mlipuko wa Tauni) msitoke kwa kuukimbia. Na mkisikia upo katika mji mwingine, basi msiingie humo."

Umar رضي الله عنه alimshukuru Allah تعالى na kuondoka.¹ Hadithi hii imeandikwa pia katika *sahih* mbili.²

Kukwepa Jihadi Hakubadilishi Hatima ya Mtu

Allah تعالى Amesema:

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٤﴾

"Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Msikivu na Mjuzi." (2:244)

Ayah hii inaonyesha kuwa, kama vile tahadhari isivyobadilisha Kadari ya Allah تعالى. Halikadhalika, kuacha Jihad hakutousogeza muda uliopangwa au kuahirisha. Bali hatima na riziki iliyopangwa haibadiliki na haitobadilishwa kamwe, ama kwa kuongezwa au kufutwa. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema:

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا قُلْ فَادْرَءُوا عَنِّي أَنْفُسِكُمُ الْمَوْتُ

إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٤٥﴾

"Hao ndio waliowaambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wengelitutii wasingeliuliwa. Sema: Ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli." (3:168) Allah تعالى Amesema:

وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ قُلْ مَتَّعْتُ الدُّنْيَا قَلِيلًا

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَىٰ وَلَا تُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٢٤٦﴾ أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكَكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ

كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ ﴿٢٤٧﴾

¹ Ahmad 1:194.

² Fat'hul Al-Bari 10:189, 190; 12:361; Muslim 4:1740.

“Na wakasema: Mola Mlezi Wetu! Kwa nini Umetuamrisha kupigana? Laiti Ungetuahirishia kiasi ya muda kidogo hivi! Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa wenye kumchamungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende. Popote mlipo mauti yatakufikieni na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu”. (4:77-78)

Abu Sulayman, Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه, Jemedari wa majeshi ya Kiislamu, mzoefu miongoni mwa askari wa Kiislamu, mlinzi wa Uislamu na upanga wa Mwenyezi Mungu ambao ulinyanyuliwa juu ya Maadui Zake, alisema wakati wa kufa, “Nilishiriki katika vita kadha wa kadha. Hakuna sehemu ya mwili wangu iliyokosa kuchomwa, nikachomwa na mkuki au pigo la upanga. Pamoja na hayo, bado nipo, nafia kitandani mwangu kama anavyokufa ngamia! Macho ya waoga na ya kuonja usingizi.” Allah تعالى Amuwie radhi, alisikitika na kuwa na uchungu kwa sababu hakufa shahidi katika vita. Alihuzunika kwa kufia juu ya kitanda chake.¹

Karadha Njema na Malipo Yake:

Allah تعالى Amesema:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ أضعافًا كَثِيرَةً

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili amzidishie mzidisho mwingi.”

Katika Aya hii, Allah تعالى Anawashajiisha waja Wake watoe katika njia Yake. Allah تعالى Ameitaja Aya hii katika sehemu mbalimbali za Qur'an Takatifu. Hadithi inayosema kuwa Allah تعالى Hushuka (kila usiku katika mbingu iliyo karibu nasi inapobakia theluthi ya usiku) inaeleza kuwa Allah تعالى Anasema:

«مَنْ يُقْرِضْ غَيْرَ عَدِيمٍ وَلَا ظَلُومٍ»

“Mwenye kumkopesha mtu ambaye si masikini wala dhalimu.”²

¹ Tahdhib At-Tahdhid 3:124.

² Muslim 758, Musnad Abu 'Awanah 1:145.

Kauli ya Allah تعالى:

فَيُضَعِفُهُ لَهُرَ أَضْعَافًا كَثِيرَةً

“...ili amzidishie mzidisho mwingi.”

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أُنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُنبُلَةٍ
مِائَةٌ حَبَّةٌ وَاللَّهُ يُضَعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ

“Mfano wa wanaotumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje iliyochipuka mashuke saba katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye...”
(2:261)

Tutaitaja Aya hii baadaye kisha Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ يَقْبِضُ وَيَبْصُطُ

“Na Mwenyezi Mungu Hukunja na Kukunjua.”

Maana yake: Toeni (katika njia ya Allah تعالى) na msiwe na wasi wasi. Kwa hakika Allah تعالى ni Mlishaji Ambaye Humuongezea au Kumpunguzia Amtakaye miongoni mwa waja Wake. Allah تعالى Ana Hekima kubwa katika Kufanya hilo. Na,

وَالِيهِ تُرْجَعُونَ

“...na Kwake Yeye mtarejea.”

* * *

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ سَوَّاهُ اللَّهُ
 قُلُوبَهُمْ قَالُوا لَا نُكْفِلُ فِي سَبِيلِ
 اللَّهِ شَيْئًا وَقَالُوا قَوْلَ كُفَّارٍ
 فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَن يَكُونُوا لَنَا
 آيَةً يُنذِرُ أَوْلِيَاءَهُمْ أَن يَحْمِلُوا
 صِغَارَ الَّذِينَ كَفَرُوا خَالِدِينَ فِيهَا
 سِوَىٰ آلِ أَبِي سَلَمَةَ الَّذِينَ فَتَنُوا
 مَوْلَاهُ سِجِّينَ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً
 لِّمَن كَانَ عَالِمًا بِالْحَقِّ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٦﴾ وَقَالَ لَهُمْ
 نَبِيُّهُمْ إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ
 التَّابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ
 وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آوَالُ مُوسَىٰ
 وَآلُ هَارُونَ تَحْمِلُهَا الْمَلَائِكَةُ ۗ
 إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّكُم إِن كُنْتُمْ
 مُّؤْمِنِينَ ﴿٢٤٧﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ سَوَّاهُ اللَّهُ
 قُلُوبَهُمْ قَالُوا لَا نُكْفِلُ فِي سَبِيلِ
 اللَّهِ شَيْئًا وَقَالُوا قَوْلَ كُفَّارٍ
 فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَن يَكُونُوا لَنَا
 آيَةً يُنذِرُ أَوْلِيَاءَهُمْ أَن يَحْمِلُوا
 صِغَارَ الَّذِينَ كَفَرُوا خَالِدِينَ فِيهَا
 سِوَىٰ آلِ أَبِي سَلَمَةَ الَّذِينَ فَتَنُوا
 مَوْلَاهُ سِجِّينَ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً
 لِّمَن كَانَ عَالِمًا بِالْحَقِّ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٦﴾

246. "Hukuwaona watu-kufu katika Wana wa Israili baada ya Musa, walipomwambia Nabii wao: Tuwekee mfalme ili tupigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Akasema: je, haelekei ikiwa mtaandikiwa vitakuwa msipigane? Wakasema: Itakuwaje tusi-

igane katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu? Lakini walipoandikiwa kupigana waligeuka, isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu Anawajua madhalimu."

Kisa cha Mayahudi Ambao Walitaka Wateuliwe Mfalme Washirikiane Naye Katika Vita

Mujahid alisema kuwa Mtume (aliyetajwa katika Aya 2:246 hapo juu) ni Shamwil (Samuel).¹ Wahb bin Munabbih alisema: Wana wa Israil walibaki katika njia iliyonyooka kwa kipindi kirefu baada ya Musa عليه السلام. Kisha walizua mambo kwenye dini na baadhi yao waliabudu masanamu. Bado, wakati wote Mitume walitumwa miongoni mwao wakiwaamrisha kufanya amali njema, na kuwaepusha kufanya maovu na ambaye angewatawala kwa mujibu wa mafundisho ya Taurati. Wayahudi walipofanya maovu, Allah تعالى Aliwawezesha maadui zao kuwashinda, na wakafikwa na maafa mengi. Maadui wao waliwateka wengi kati yao, na wakachukua ardhi yao kubwa. Kabla ya hapo yeyote aliyepigana na Wayahudi alishindwa, kwa sababu walikuwa na Taurati na Tabut,² ambazo walizirithi kizazi baada ya kizazi, tangu zama za Musa عليه السلام, ambaye alizungumza na Allah تعالى moja kwa moja. Bali, Wayahudi waliendelea na upotofu mpaka mfalme mmoja alichukua umiliki wa Tabut kutoka kwao wakati wa vita. Mfalme huyo alichukua pia umiliki wa Taurati na Walibaki Wayahudi wachache walioihifadhi kwa moyo. Utume ulisimama miongoni mwa makabila mbalimbali, isipokuwa kwa mwanamke mjamzito wa kizazi cha Lawi (Levi), ambapo bado kwake walitokea Mitume. Mume wake aliuawa, hivyo Mayahudi walimuweka ndani ya nyumba ili huenda Allah تعالى Angempa mtoto wa kiume ambaye angekuwa Mtume wao. Mwanamke naye akawa anamuomba Allah تعالى Amjaalie mtoto wa Kiume. Allah تعالى Aliyasikia maombi yake na Akampa mtoto wa kiume, aliyemwita "Shamwil" maana yake Allah تعالى Amesikia maombi yangu. Baadhi ya watu walisema kuwa jina la mtoto huyo lilikuwa Shamun (Simeon), ambalo lina maana inayofanana.

Mtoto alipokua, Allah تعالى Alimjaalia kuwa mtu mwema. Alipofikia umri wa Utume Allah تعالى Alimteremshia ufunuo na alimwamuru kuwalingania watu kuhusu Yeye (Allah تعالى) na Tawhid Yake. Shamwil aliwaita Wana wa Israil katika njia ya Allah تعالى na wakamtaka ateue mfalme awaongoze, na ili waweze kupigana na maadui zao chini ya uongozi wake. Ufalme uliokuwa umekoma kwao. Mtume wao aliwaambia, "Mnaonaje kama Allah تعالى Atawateulia

¹ At-Tabari 5:293.

² "Sanduku la Agano."

mfalme wa kuwaongoza, Je, mtatekeleza kiapo chenu cha kupigana chini ya utawala wake?”

قَالُوا وَمَا لَنَا أَلَّا نُقَاتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَدْ أُخْرِجْنَا مِنْ دِيَارِنَا وَأَبْنَاءِنَا^ط

“Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu?”

Maana yake: Baada ya Ardhi yetu kuporwa na kunyang’anywa watoto wetu?

Allah تعالى Amesema:

فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ تَوَلَّوْا إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ^ط وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٢٤٦﴾

“Lakini walipoandikiwa kupigana waligeuka, isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu Anawajua madhalimu.”

Maana yake: Wachache tu ndio waliotekeleza ahadi zao, lakini wengi walisusia Jihad na Allah تعالى Anawafahamu vilivyo.

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا^ع قَالُوا أَنَّى يَكُونُ لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ الْمَالِ^ع قَالَ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ^ط وَاللَّهُ يُؤْتِي مُلْكَهُ مَن يَشَاءُ^ع وَاللَّهُ وَاسِعٌ

عَلِيمٌ ﴿٢٤٧﴾

247. “Na Nabii wao akamwambia: Mwenyezi Mungu Amekuteulieni Taluti (Sauli) kuwa ni mfalme. Wakasema: vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tuna haki zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Mwenyezi Mungu Amemteua yeye juu yenu na Amemzidishia ukunjufu wa ilimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu Humpa ufalme wake Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mjuzi.”

Wayahudi walipomtaka Mtume wao awateulie mfalme, alimteua Talut (Saul), ambaye alikuwa askari. Lakini Talut hakuwa kizazi cha nyumba ya wafalme miongoni mwao, ufalme ambao ulikuwa mahsusi kwa kizazi cha Yahudha (Judah). Ndio sababu walisema:

أَنْ يَكُونَ لَهُ الْمَلِكُ عَلَيْنَا

“Vipi atakuwa na ufalme juu yetu.”

Maana yake: Anawezaje kuwa mfalme wetu,

وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِنَ الْمَالِ^ع

“Na hali sisi tuna haki zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali?”

Walisema kuwa Talut alikuwa pia masikini na hakuwa na mali iliyo mhalalishia kuwa mfalme. Baadhi ya watu walisema kuwa Talut alikuwa akiwaletea watu maji, wengine wakasema kuwa kazi yake ilikuwa kutia rangi ngozi. Mayahudi walibishana na Mtume wao ambapo walitakiwa kumtii na kuzungumza naye kwa lugha nzuri. Mtume wao aliwajibu,

إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَنَاهُ عَلَيْكُمْ

“Mwenyezi Mungu Amemteua yeye juu yenu.”

Maana yake: Allah تعالى Alimchagua Talut kutoka miongoni mwenu, ilhali anamjua zaidi Mtume wao akawaambia, “sikumchagua Talut kuwa mfalme wenu kwa utashi wangu. Bali, Allah تعالى Ameliamrisha hilo kutokana na maombi yenu. Zaidi ya hayo:

وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ^ط

“Na Amemzidishia ukunjufu wa ilmu na kiwiliwili.”

Maana yake: Talut ana elimu zaidi yenu na anaheshimika zaidi yenu, na ana nguvu na subira zaidi wakati wa mapambano, na ana maarifa zaidi ya kivita. Kwa ufupi, ana maarifa zaidi na ana nguvu zaidi yenu. Mfalme lazima awe na elimu ya kutosha, awe anawajibika na lazima awe na nguvu za moyo na mwili! Kisha akasema.

وَاللَّهُ يُؤْتِي مَلِكَهُ مَن يَشَاءُ^ع

“Na Mwenyezi Mungu Humpa ufalme Wake Amtakaye.”

Maana yake: Allah تعالى Pekee ndio Mwenye Mamlaka ya Juu kabisa Ambaye Hufanya Ayatakayo na hapana awezaye kumuliza kuhusu Matendo Yake,

ambapo wao wataulizwa (juu ya matendo yao na Yeye). Hii ni kwa sababu Allah تعالى Ana elimu iliyotimia, Hekima na Mapenzi kwa viumbe Wake. Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mjuzi.”

Maana yake: Neema Zake ni zenye kuenea na Humrehemu Amtakaye. Anawajua wale wanaostahili kuwa wafalme na wale wasiostahili.

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِمْ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْتَابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ
وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ تَحْمِلُهُ الْغَلَابِيُّكَ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لَّكُمْ إِنْ

كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٤٧﴾

248. “Na Nabii wao akawaambia: Alama ya ufalme wake ni kukuleteeni lile sanduku ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu Mlezi, na mna mabaki ya waliyoyaacha kina Musa na kina Harun, wanalichukua Malaika. Bila shaka katika hayo zimo dalili kwenu ikiwa nyinyi mnaamini.”

Kisha Mtume wao akatangaza, “Alama ya Baraka za ufalme wa *Talut* kwenu ni kuwa Allah تعالى Atawarejesheni *Tabut* (sanduku la mbao) lililochukuliwa kutoka kwenu.” Allah تعالى Amesema:

فِيهِ سَكِينَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ

“...mna ndani yake kituliza nyoyo zenu...” Maana yake: Amani (au neema)¹ na Uhakika. Abdur-Razzaq alisema kuwa Qatadah alisema:

فِيهِ سَكِينَةٌ

“...mna ndani yake kituliza...” Maana yake: Neema kwa nyongeza, Ar-Rabi alisema kuwa *Sakina* ina maana, huruma. Maana hii pia imetolewa na Ibn Abbas رضي الله عنهما kama alivyosimulia Al-Awfi. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ

“...na mna mabaki ya waliyoyaacha kina Musa na kina Harun...”

¹ Abdur-Razzaq 1:98.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya hii:

وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ

“...na mna mabaki ya waliyoyaacha kina Musa na kina Harun...”

Maana yake: Fimbo ya Mussa عليه السلام, na mabaki ya mbao za kuandikia.¹ Tafsir hii pia imetolewa na Qatadah, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na Ikrimah, ambao waliongeza, “Na pia Taurati.”² Abdur-Razzaq alisema kuwa alimwuliza Ath-Thawri رحمه الله تعالى juu ya maana ya,

وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ

“...na mna mabaki ya waliyoyaacha kina Musa na kina Harun...”

Ath-Thawr رحمه الله تعالى, alisema “Baadhi wamesema kuwa ilikuwa na chungu cha manna na mabaki ya mbao za kuandikia, ambapo wengine walisema ilikuwemo fimbo (ya Musa عليه السلام) na jozi ya viatu (rejea 20:12).”³ Kisha Allah تعالى Akasema:

تَحْمِلُهُ الْمَلَائِكَةُ

“...wanalichukua Malaika...” Ibn Jurayj alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Malaika walishuka huku wamebeba sanduku (*Tabut*) kati ya mbingu na ardhi mpaka mbele ya Talut huku wakiangalia.” As-Suddi alisema, Sanduku (*Tabut*) lililetwa nyumbani kwa Talut, hivyo watu wakaamini Utume wa Shamun (Simeon) na wakamtii Talut.”⁴ Kisha Allah تعالى Akasema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّكُمْ

“Bila shaka katika hayo zimo dalili kwenu...”

Wakithibitisha ukweli nilio tumwa nao, utume wangu, na amri yangu kuwa mumtii Talut.

إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ

“...ikiwa nyinyi mnaamini.” Maana yake: Allah تعالى na Siku ya Mwisho:

* * *

¹ At-Tabari 5:331.

² At-Tabari 5:331,332.

³ At-Tabari 5:333.

⁴ At-Tabari 5:335.

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوتُ بِالْجُنُودِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ
 بِنَهَرٍ فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ مِنِّي
 إِلَّا مَنْ اغْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهِ ۖ فَشَرِبُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۗ
 فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ قَالُوا لَا طَاقَةَ لَنَا
 الْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ ۗ قَالَ الَّذِينَ آمَنُوا يَظُنُونَ أَنَّهُمْ
 مُلْقُوا بِاللَّهِ كَمَ مِنْ فِتْنَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةٌ كَثِيرَةٌ بِإِذْنِ اللَّهِ
 ۗ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٤٩﴾ وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ
 قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أقدامَنَا وَأَنْصُرْنَا عَلَى
 الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾ فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ
 دَاوُدُ جَالُوتَ وَءَاتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ
 مِمَّا يَشَاءُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ
 الْأَرْضُ وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾
 تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ۗ وَإِنَّكَ لَمِنَ
 الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوتُ بِالْجُنُودِ قَالَ
 إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ بِنَهَرٍ فَمَنْ
 شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ
 فَإِنَّهُ مِنِّي إِلَّا مَنْ اغْتَرَفَ غُرْفَةً
 بِيَدِهِ ۖ فَشَرِبُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۗ
 فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا
 مَعَهُ قَالُوا لَا طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ
 بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ ۗ قَالَ الَّذِينَ
 يَظُنُونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا بِاللَّهِ كَمَ مِنْ
 فِتْنَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةٌ كَثِيرَةٌ بِإِذْنِ
 اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٤٩﴾

249. "Basi Taluti alipo-
 ondoka na majeshi alisema:
 Mwenyezi Mungu Ataku-
 jaribuni kwa mto. Atakaye-
 kunywa humo si pamoja
 nami, na asiyekunywa

atakuwa pamoja nami: Ila atakayeteka kiasi ya kitanga cha mkono wake. Lakini walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Alipovuka mto yeye na wale walioamini pamoja naye, walisema: Leo hatumwezi Jaluti (goliati) na majeshi yake. Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mwenyezi Mungu: Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kusubiri."

Allah تعالی Anaeleza kuwa Talut, Mfalme wa Wana wa Israil alisonga mbele na askari wake, na Waisrail waliomtii. Jeshi lake wakati huo lilikuwa na askari elfu themanini, kwa mujibu wa As-Suddi,¹ lakini Allah تعالی Anajua zaidi. Talut alisema,

إِنَّ اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ

“...Mwenyezi Mungu Atakujaribuni kwa mto...”

Maana yake: Atawajaribu na mto, ambao ukitiririka kati ya Jordan na Palestina. Maana yake: Mto ambao ni maarufu. Kwa mujibu wa Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine.² Akaendelea,

فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّي

“...atakayekunywa humo si pamoja nami...”

Maana yake: Hatokuwa pamoja nami leo,

وَمَنْ لَمْ يَطْعَمَهُ فَإِنَّهُ مِنِّي إِلَّا مَنْ اغْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهِ³

“Na asiyekunywa atakuwa pamoja nami: ila atakayeteka kiasi ya kitanga cha mkono wake...”

Maana yake: Hapana madhara katika hali hii. Kisha Allah تعالی Amesema:

فَتَّخِرُوا مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ⁴

“...lakini Walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao...”

Ibn Jurayj رحمه الله تعالی alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo, “Yeyote aliyechota maji katika kiganja chake, kiu yake ilikatika, ama aliyekunywa kutoka kwenye mto, kiu yake haikukatika.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisimulia kuwa Al-Bara bin Azib عنه رضي الله عنهما alisema, “Tulikuwa tukisema kuwa Masahaba wa Muhammad ﷺ waliofuatana naye katika vita vya Badr walikuwa zaidi ya mia tatu na kumi, ukilinganisha na idadi ya askari waliovuka mto na Talut. Ni wale tu walioamini ndio waliovuka naye mto.”³ Al-Bukhari pia alilisimulia hili.⁴ Hii ndiyo sababu Allah تعالی Amesema:

¹ At-Tabari 5:339.

² At-Tabari 5-340.

³ At-Tabari 5:345, 346, 347.

⁴ Fat'hul Al-Bari 7:339.

فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ قَالُوا لَا طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ^٤

“Alipovuka mto yeye na wale walioamini pamoja naye walisema leo hatumwezi Jalut (Goliati) na majeshi yake.”

Aya hii inaonesha kuwa Waisrail (waliobaki na Talut) walidhani kuwa walikuwa wachache mbele ya maadui waliokuwa wengi. Hivyo, wanazuoni wao wajuzi wa mambo walikazia nia yao kwa kusema kuwa ahadi ya Allah تعالى ni ya kweli na kuwa ushindi unatoka kwa Allah تعالى Pekee, na si kutokana na idadi kubwa au mahitaji yanayotosha. Wakamwambia:

كَمْ مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٤٩﴾

“Makundi mangapi madogo yameyashinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kusubiri.”

وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾ فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُدُ جَالُوتَ وَءَاتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ^٥ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾ تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

250. “Na walipotoka kupambana na Jalut na majeshi yake walisema: Mola wetu Mlezi! Tumiminie subira, na Isimamisha imara miguu yetu, na Utusaidie tuwashinde watu makafiri.”

251. “Kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu waliwatimua, na Daudi akamuua Jaluti, na Mwenyezi Mungu Akampa Daudi ufalme na hekima na Akamfundisha Aliyoyapenda. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Hawapambanishi watu kwa watu basi dunia ingeliharibika.

¹ At-Tabari 5:345, 346, 347.

² Fat’hul Al-Bari 7:339.

Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila juu ya walimwengu wote.”

252. “Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu Tunakusomea kwa haki. Na hakika wewe ni miongoni mwa Mitume.”

Kundi lililoamini, lilikuwa na watu wachache chini uongozi wa Talut, walikabiliana na adui yao, ambao walikuwa wengi chini ya uongozi wa Jalut.

قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا

“...Mola wetu Mlezi! Tumiminie subira...”

Maana yake: Tuteremshie uvumilivu.

وَوَثِّبْتَ أَقْدَامَنَا

“...na Isimamishe imara miguu yetu...”

Maana yake: Dhidi ya maadui na Utuokoe kukimbia na kutokana na udhaifu.

وَأَنْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٢﴾

“... na Utusaidie tuwashinde watu Makafiri.”

Allah تعالى Amesema:

فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ

“Kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu waliwatimua...”

Maana yake: Wakawashinda, wakawazidi nguvu kwa usaidizi wa Allah تعالى, Kisha,

وَقَتَلَ دَاوُدُ جَالُوتَ

“... na Daudi akamuua Jaluti...”

Waisrail wanadai kuwa (Mtume) Daudi عليه السلام alimuua Jaluti (Goliath) kwa teo aliyokuwa nayo, ambayo alimpiga nayo Jaluti na kusababisha kifo chake. Talut alimuahidi kuwa yeyote atakayemuua Jalut, atamuoa binti yake na atagawana naye ufalme na madaraka yake. Alitimiza ahadi yake. Baadaye, ufalme ulihamishiwa kwa Mtume Daudi عليه السلام pamoja na nyongeza ya kupewa Utume na Allah. Allah تعالى Alisema:

وَأَتَتْهُ اللَّهُ الْمَلَكَ

“...na Mwenyezi Mungu Akampa Daudi ufalme...”

Aliokuwa nao Talut na,

وَالْحِكْمَةَ

“...na Hekima...”

Ambayo inaambatana na Utume, Maana yake: Baada ya Shamwil (Kisha Allah تعالى Akasema),

وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ

“...na Akamfundisha Aliyoyapenda...”

Maana yake: Akamfunza Apendavyo katika elimu yenye manufaa ambayo pia alimtunukia elimu hiyo Mtume Muhammad ﷺ. Allah تعالى Alisema baadaye:

وَلَوْلَا دَفَعُ اللَّهُ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ

“...na lau kuwa Mwenyezi Mungu Hawapambanishi watu kwa watu basi dunia ingeliharibika...”

Aya hii inaonesha kuwa: Kama isingekuwa kwamba Allah تعالى Kuwahami watu dhidi ya watu wengine, kama ilivyokuwa wakati Talut na ushupavu wa Dawud عليه السلام uliwasaidia Wana wa Israil (dhidi ya Goliath). Vinginevyo watu wangeangamia. Hivyo Allah تعالى Amesema:

وَلَوْلَا دَفَعُ اللَّهُ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ هُدًى مَّتَّ صَوَامِعَ وَبَيْعَ وَصَلَوَاتٍ وَمَسَاجِدُ يُذَكَّرُ

فِيهَا أَسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingelivunjwa nyumba za watawa na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi.” (22:40)

Kisha Allah تعالى Akasema:

وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٤٠﴾

“...Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila juu ya walimwengu wote...”

Maana yake: Kwa Huruma na Fadhila Zake Huwahami watu dhidi ya watu wengine. Kwa hakika Allah تعالى, Ana hekima, Mamlaka ya mwisho na dalili zilizo wazi dhidi ya viumbe Wake katika Matendo na Kauli Zake zote.

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

“Hizi ni Ayah za Mwenyezi Mungu Tunakusomea kwa haki. Na hakika wewe ni miongoni mwa Mitume.” (2:252)

Aya hii inaelezea kuwa, “Aya hizi za Allah تعالى Tulizowasimulia kwa uhakika zinakubaliana na mwenendo kuwa visa hivyo vilitokea na kwa ukweli ambao umebaki kwenye Vitabu Vitakatifu ambavyo wanazuoni wa Wana Israil wanavyo na wanavijua.”

Allah تعالى Amesema: Wewe Muhammad ﷺ,

وَإِنَّكَ

“Hakika yako”

لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

“...ni miongoni mwa Mitume.”

Anaelezea kwa mkazo wa ukweli wa Utume wake.

* * *

* تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ مِّنْهُمْ مَّنْ كَلَّمَ
 اللَّهُ^ط وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ^ع وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ
 الْبَيِّنَاتِ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ^ا وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَلَل
 الَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ وَلَكِنْ
 اخْتَلَفُوا فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ وَمِنْهُمْ مَّنْ كَفَرَ^ع وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا
 أَقْتَلُوا وَلَكِنْ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿٢٥٣﴾ يَأْتِيهَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُمْ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ
 فِيهِ وَلَا خُلَّةٍ وَلَا شَفِيعَةٍ^ا وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٤﴾
 اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ^ع لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ^ع
 لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ^ا مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ
 عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ^ع يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ^ط
 وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ^ع وَسِعَ كُرْسِيُّهُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ^ط وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا^ع وَهُوَ الْعَلِيُّ
 الْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾ لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ^ط قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ
^ع فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِرْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ
 بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انْفِصَامَ لَهَا^ا وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾

* تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى
 بَعْضٍ مِّنْهُمْ مَّنْ كَلَّمَ اللَّهُ^ط وَرَفَعَ
 بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ^ع وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ
 مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ^ا
 وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَلَل الَّذِينَ مِنْ
 بَعْدِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ
 وَلَكِنْ اخْتَلَفُوا فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ
 وَمِنْهُمْ مَّنْ كَفَرَ^ع وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا
 أَقْتَلُوا وَلَكِنْ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿٢٥٣﴾

253. "Mitume hao Tume watukuza baadhi yao juu ya wengineo. Katika wao wapo ambao Mwenyezi Mungu Alisema nao, na wengine Akawapandisha vyeo. Na Tukampa Isa mwana wa Mariyam hoja zilizo wazi, na Tukamtia nguvu kwa Roho Mtakatifu. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Alipenda wasingelipigana waliokuwa baada yao baada ya kuwa jia

hoja zilizo wazi. Lakini walikhitilafiana. Basi wapo kati yao walioamini na wengine kati yao waliokufuru. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelipenda wasingelipigana. Lakini Mwenyezi Mungu Hutenda Atakavyo."

Allah تعالی Amewatukuza Baadhi ya Mitume Juu ya Wenzao:

Allah تعالی Ameeleza kuwa Amewatukuza baadhi ya Mitume kuliko wengine. Kwa mfano, Allah تعالی Amesema,

وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَىٰ بَعْضٍ ۖ وَءَاتَيْنَا دَاوُدَ زُبُورًا ﴿٥٥﴾

“Na hakika Tumewafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine, na Daudi Tulimpa Zaburi.” (17:55)

Katika Aya hapo juu Allah تعالی Amesema;

﴿ تِلْكَ الْأَرْسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ مِّنْ كَلِمٍ مَّا اللَّهُ ۖ

“Mitume hao Tumewatukuza baadhi yao juu ya wengineo. Katika wao wapo ambao Mwenyezi Mungu Alisema nao.”

Maana yake: Musa عليه السلام na Muhammad ﷺ, na pia Adam عليه السلام kwa mujibu wa Hadithi iliyonukuliwa katika Sahih Ibn Hiban kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه.

وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ ۚ

“Na wengine Akawapandisha daraja.” Kama ilivyo katika Hadithi juu ya safari ya Isra, wakati Mtume ﷺ alipowaona Mitume katika mbingu mbalimbali kwa mujibu wa vyeo vyao walivyopewa na Allah تعالی.

Iwapo mtu atauliza maana inayozikusanya Ayah hii na Hadithi ambayo Sahih Mbili zilikusanya kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه ambayo inasema: Wakati fulani, Muislam na Yahudi walikuwa wakibishana. Yahudi akaapa, ‘Hapana, na Yule Ambaye (Allah تعالی) Alimteua Musa عليه السلام kuwa mbora kwa walimwengu wote!’ Muislam aliinua mkono wake akampiga kibao cha uso Yahudi na akasema, “Amemzidi Muhammad pia, Ewe muovu?!” Yahudi alikwenda kwa Mtume ﷺ na kumlalamikia. Mtume ﷺ alisema,

﴿ لَا تَفْضُلُونِي عَلَى الْأَنْبِيَاءِ، فَإِنَّ النَّاسَ يَضَعُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَكُونَ أَوَّلَ مَنْ يُبْقَى، فَأَجِدُ مُوسَىٰ بَاطِنًا بِمَائِمَةِ الْعَرْشِ، فَلَا أَدْرِي أَفَأَقِ قَبْلِي أَمْ جُوزِي بِصَعْتَةِ الطُّورِ؟ فَلَا تَفْضُلُونِي عَلَى الْأَنْبِيَاءِ﴾

“Msinifadhilisha zaidi ya Mitume, kwani watu watapoteza fahamu siku ya kiyama na nitakuwa wa kwanza kuzinduka na nitamkuta

Musa ameshika nguzo ya Arshi. Sitajua kama Musa alizinduka kabla yangu ama kulimtoша kupoteza kwake fahamu kulikom-pata mlimani.¹ Hivyo msinitukuze juu ya Mitume.”² Katika mapokezi mengine, Mtume ﷺ alisema, “Msinitukuze juu ya mitume.” Katika mapokezi mengine Mtume ﷺ alisema, “msiwatukuze baadhi ya Mitume zaidi ya wengine.”³

Jibu la swali hili ni kuwa Hadith hii inakataza kuwafanya bora baadhi ya Mitume juu ya wengine wakati wa migongano na mabishano, kama ilivyo katika suala lililotajwa ndani ya Hadithi. Hadithi inaonesha kuwa si juu ya viumbe kuamua ni Mtume gani aliye mbora, kwani huo ni uamuzi wa Allah تعالى. Nyinyi mnatakiwa kusalimu amri, kutii na kuamini uamuzi wa Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْيَسَّيْنَةَ

“Na Tukampa Isa mwana wa Maryam hoja zilizo wazi.”

Inahusu ushahidi usio na shaka unaothibitisha ukweli kuwa Isa عليه السلام alitumwa kwa Wana wa Israil, hivyo kuthibitisha kuwa alikuwa mja wa Allah تعالى na Nabii Wake kwao.

وَأَيَّدَنَّهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ

“Na Tukamtia nguvu kwa Roho Mtakatifu.”

Maana yake: Allah تعالى alimpa msaada kwa kumtuma Jibril عليه السلام. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَتَلِ الَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ وَلَكِنْ اٰخْتَلَفُوا

فَمِنْهُمْ مَنْ ءَامَنَ وَمِنْهُمْ مَنْ كَفَرَ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَقْتَتَلُوا

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelipenda wasingelipigana waliokuwa baada yao baada ya kuwajia hoja zilizo wazi, lakini walikhitilafiana. Basi wapo kati yao walioamini na wengine kati yao waliokufuru. Na kuwa Mwenyezi Mungu Angelipenda wasingelipigana.”

¹ Rejea Aya mbili za Suratul-Baqarah 2:55-56.

² Fat’hul Al-Bari 6:508, Muslim 4:43.

³ Muslim 4:43, Fath Al-Bari 6:519.

Maana yake: Haya yote yalitokea kwa amri ya Allah تعالى, na hii ndiyo sababu Allah تعالى Amesema:

وَلَكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿٢٥٣﴾

“Lakini Allah Hutenda Ayatakayo.”

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُمْ مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفِيعَةٌ ۗ وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

254. “Enyi mlioamini! Toeni katika Tulivyokupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhalimu.”

Allah تعالى Anawaamrisha waja Wake watoe mali zao kwa ajili ya kupata radhi Zake, katika njia ya kheri, kutokana na vile Alivyowaruzuku, ili waweze kupata malipo kutokana na amali njema kutoka kwa Bwana na Mfalme wao. Basi wapupie kufanya amali hapa duniani,

مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ

“Kabla haijafika siku.” Maana yake: Siku ya kiyama,

لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفِيعَةٌ

“Ambayo hapatakuwepo biashara, wala urafiki, wala uombezi.”

Aya hii inaonesha kuwa siku hiyo, hapana mtu atakayeweza kumwomba mwenzake, au yeye mwenyewe au kujiokoa na mateso kwa kutoa mali yake yoyote, hata kwa ardhi iliyojaa dhahabu. Wala rafiki zake au jamaa zake hawataweza kumsaidia. Hivyo Allah تعالى Amesema,

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٥٥﴾

“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwepo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.” (23:101)

وَلَا شَفِيعَةٌ

“Wala uombezi.” Maana yake: Hawatanufaika na uombezi wa yeyote. Kauli ya Allah تعالى,

وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٣﴾

“Na makafiri ndio madhalimu.” Inaonesha hapana dhalimu mkubwa kuliko atakayekutana na Allah تعالى siku hiyo akiwa kafiri. Ibn Abu Hatim alinukuu kutoka kwa Ata bin Dinar alisema. “Shukrani zote Anastahiki Allah تعالى Aliyesema;

وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

“Na makafiri ndio madhalimu.” Wala hakusema, ‘Na madhalimu ndio makafiri’¹

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ ۚ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۗ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ ۗ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ ۗ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا ۗ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾

255. “Mwenyezi Mungu – hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni Vyake pekee vyote vilivyomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya Idhini Yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika Ujuzi Wake, ila kwa Atakalo Mwenyewe. Kiti Chake cha Enzi Kimetanda mbinguni na duniani; na wala Haelemewi na Kuvilinda hivyo. Na Yeye Ndiye Aliye juu, na Ndiye Mkuu.”

Ubora wa Ayatul-Kursi:

Ayatul-Kursi imehusishwa na fadhila kubwa kwani Hadithi sahihi imeieleza kuwa hiyo ni Aya yenye fadhila zaidi katika Kitabu cha Allah تعالى. Imam Ahmad alimnukuu Ubbay bin Ka'b رضي الله عنه kuwa alisema kuwa Mtume ﷺ alimwuliza: “Ni Aya gani iliyo kuu ndani ya kitabu cha Allah?” Ubbay رضي الله عنه akajibu, “Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ wanajua zaidi.” Mtume ﷺ akarejea mara kadha kuuliza swali hilo. Ubbay رضي الله عنه akasema, “Ayat Al-Kursi.” Mtume ﷺ akasema,

¹ Ibn Abu Hatim 3:966.

«لَيْهَيْكَ الْعِلْمُ أَبَا الْمُنْذِرِ، وَالَّذِي تَفْسِي بِيَدِهِ، إِنَّ لَهَا لِسَانًا وَشَفَتَيْنِ، تُقَدِّسُ الْمَلِكُ
عِنْدَ سَاقِ الْعَرْشِ»

"Hongera kwa kuwa na elimu, ewe Abu Mundhir! Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko katika Mkono Wake! Ayah hii ina ulimi na midomo miwili ambayo inamtukuza Mfalme (Allah) katika mguu wa Arshi."¹

Hadithi hii ilikusanywa pia na Muslim² na wala haina ziada. *"Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko katika Mkono Wake!..."*

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Ayyub رضي الله عنه alisema kuwa alikuwa na kiasi cha tende na *Ghul* (aina ya Jini) alikuwa akija na kuzichukua, hivyo akamlalamikia Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akamuambia, "Utakapomuona, sema, Kwa Jina la Allah تعالى, mtii Mtume ﷺ." Abu Ayyub رضي الله عنه akasema maneno yale alipokuja tena, Na akamudu kumshika. Akamuomba, "Niachie, sitorudia tena." Basi Abu Ayyub رضي الله عنه akamuachia. Abu Ayyub رضي الله عنه akaja kwa Mtume ﷺ na Mtume ﷺ akamuuliza, "Mateka wako amefanya nini?" Abu Ayyub رضي الله عنه akajibu, "Nilimshika, akasema, 'Kwa hakika sitorudia tena; nami nikamuachilia. Lakini alirudi, nami nikamkamata mara ya pili au tatu, na katika mara zote hizo alikuwa akisema, 'Sitarudi'. Nami nikawa nakuja kwa Mtume ﷺ ambaye aliniuliza, "Nipe khabari za mateka wako?" Nilimjibu, 'Nilikuwa namkamata, na yeye akiniambia, 'Sitarudia'. Na yeye (Mtume ﷺ) huniambia, "Atarudi." Basi nikamkamata tena, akasema, 'Niachie, nami nitakufundisha kitu cha kusoma ili usidhuriwe na chochote, nacho ni, *Ayat Al-Kursi*'. Abu Ayyub رضي الله عنه akaenda kwa Mtume ﷺ na akamueleza, naye Mtume ﷺ akasema, "Amesema kweli ilhali ni mwongo." At-Tirmidhi aliinukuu Hadithi hii katika Mlango au Surah ya "Fadhila za Qur'an", na akasema, Hadithi hiyo ni "Hasan Gharib" katika lugha ya Kiarabu, *'Ghul'* ni Jini anapojitokeza usiku.

Bukhari alikitaja kisa sawa na hiki kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه. Alikisimulia ndani ya Sahihi katika mlango wa "Fadhila za Qur'an", na katika mlango wa *"Al-Wakalah"* na katika "Sura juu ya sifa za Ibilisi". Kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema, Mtume ﷺ alinipa kazi ya kutunza na kulinda

¹ Ahmad 5:141.

² Muslim 1:556.

³ Ahmad 5:423.

Zaka ya Ramadhan. Mtu mmoja aliingia ghalani na kuanza kuchukua chakula. Nilimshika na kumuambia, "Wallahi, nitakupeleka kwa Mtume ﷺ." Akaniambia, 'Niachie, kwani mimi ni mwenye dhiki, nina familia kubwa na nina shida sana. Nikamuachilia, na asubuhi Mtume ﷺ akaniuliza, "Ewe Abu Hurayrah! Mahabusu wako alifanya nini jana?"

Nikasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Alinilalamikia kuwa ana shida sana na ana familia kubwa, hivyo, nilimhurumia na nikamuachilia. Mtume ﷺ akasema, "Kwa hakika, alikudanganya na atakuja tena." Niliamini kuwa angekuja tena kutokana na kauli ya Mtume ﷺ: "Kwa hakika, atarudi tena." Nikamsubiri kwa mara nyingine. Alipokuja alianza kuiba vyakula kwa wingi. Nikamshika tena na nikamuambia, 'nitakupeleka kwa Mtume ﷺ, akaniambia, 'Niachie, kwani nina shida sana na nina familia kubwa, nakuahidi sitarudia tena.' Nilimhurumia na nikamuachilia. Asubuhi Mtume ﷺ aliniuliza, "Ewe Abu Hurayrah! Mahabusu wako alifanya nini jana usiku." Nikajibu, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Alilalamika kuwa ana shida sana na alikuwa na watu wengi wanaomtegemea, hivyo nilimhurumia na nikamuachilia huru." Mtume ﷺ alisema, 'Kwa hakika amekudanganya, atarudi tena.' Nilimsubiri kwa mara ya tatu, na alipofika na kuanza kuiba chakula, nilimshika na nikamuambia, "Kwa uhakika nitakupeleka kwa Mtume ﷺ kwa kuwa hii ni mara ya tatu unadai kwamba hutorudi lakini unarudi."

Akasema, "Ngoja nikufundishe maneno ambayo kwayo, Allah تعالی Atakupa manufaa." Nikamuuliza, "Ni yapi hayo?" Akajibu, 'Kila unapokwenda kulala, soma, Ayat Al-Kursi, "Allahu laa ilaha ilaaha illaa Huwal-Hayyul – Qayyum," Mpaka mwisho wa Aya, Allah تعالی Atakupa mlinzi ambaye atakuwa nawe, na hapana Shetani atakayekukaribia mpaka asubuhi. Hivyo, nilimuachilia. Asubuhi, Mtume ﷺ aliniuliza, 'Mhalifu wako alifanya nini jana?' Nilijibu 'Ewe Mjumbe wa Allah! Alidai kunifundisha maneno ambayo kwayo Allah تعالی Angeninufaisha, hivyo nikamruhusu. Aliniambia: Unapokwenda kulala, soma Ayat Al-Kursi, mwanzo mpaka mwisho, "Allahu laa ilaha illau Huwal- Hayyul-Qayyum." Zaidi ya hayo akaniambia: 'Allah تعالی Atakupa mlinzi ambaye atakuwa nawe, na hapana Shetani atakayekukaribia mpaka asubuhi.' Na wao (Masahaba) walikuwa na bidii kubwa katika kufanya mambo mema. Akasema Mtume ﷺ, "Amekueleza ya kweli, japokuwa yeye ni mwongo. Je, unamjua uliyekuwa ukizungumza naye katika siku hizo tatu, Ewe Abu Hurayra?" Nikajibu.

'Hapana.' Akasema, "*Huyo alikuwa Shetani.*"¹ An-Nasai pia aliinukuu Hadithi hii katika *Al-Yaum wal-Laylah*.²

Jina Kuu la Allah تعالى Limo Katika Ayatul-Kursi:

Imam Ahmad aliandika kuwa Asma bint Yazid bin Assakan رضي الله عنها alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akizizungumzia Aya hizi mbili,

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

"Mwenyezi Mungu – hapana Muabudiwa ila Yeye Aliye Hai, Msimamia mambo yote milele." (2:55) Na,

الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

"Alif Laam Miim. Mwenyezi Mungu, hakuna Muabudiwa ila Yeye Aliye Hai Msimamizi wa yote milele." (3:1-2)

«إِنَّ فِيهِمَا اسْمَ اللَّهِ الْأَعْظَمِ»

*"Hakika katika Aya hizo mbili lipo Jina Tukufu la Allah."*³

Halikadhalika, hivi ndivyo walivyopokea akina Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah⁴ na At-Tirmidhi alisema kuwa ni Hasan Sahih."

Zaidi ya hayo, Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Abu Umama رضي الله عنه aliyesimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«اسْمُ اللَّهِ الْأَعْظَمِ، الَّذِي إِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ، فِي ثَلَاثٍ: سُورَةُ الْبَقَرَةِ وَآلِ عِمْرَانَ وَطُهُ»

*"Jina Tukufu la Allah ambalo akiombwa nalo, hujibu Dua, Liko ndani ya Surah tatu- Al-Baqarah, Aali-Imran na Ta-Ha."*⁵

Hisham bin Ammar, Khatib wa Damascus, alisema, "Ama Al-Baqarah, imo ndani ya,

¹ Fat'hul Al-Bari 8:672, 4:568, 6:386.

² Ad-Darimi 532. Na Asunan Al-Kubra cha Annisai 6:238 (10795)

³ Ahmad 6:461.

⁴ Abu Dawud 2:168, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:447, Ibn Majah 2:1267.

⁵ At –Tabarani 8:282. (7758, 7925) na Silslatul - Ahadithi Asa-sahihi. (746)

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

“Mwenyezi Mungu – hapana Muabudiwa ila Yeye Aliye Hai, Msimamia wa mambo yote milele.” (2:255)

Na katika Aali ‘Imran ni,

الْحَمْدُ لِلَّهِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

“Alif Laam Miin, Mwenyezi Mungu, hakuna Muabudiwa ila Yeye Aliye Hai Msimamizi wa yote milele.” (3:1-2)

Ambapo kwenye Ta-Ha imo katika,

وَعَسَىٰ أَلْوَجْهُ لِلْحَيِّ الْقَيُّومِ

“Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele.” (20:111)

Ayatul-Kursi Ina Jumla ya Sentensi Kumi Kamili Zinzajitegemea:

1. Kauli ya Allah تعالى،

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Mwenyezi Mungu – hapana Muabudiwa ila Yeye.”

Inatoa habari kwamba Yeye ni Mpweke katika Uungu kwa viumbe wote.

2. Kauli ya Allah تعالى،

الْحَيُّ الْقَيُّومُ

“Aliye Hai, Msimamia wa mambo yote milele.” Maana yake: Aliye Hai milele Yeye Mwenyewe, kamwe Hafi, Ambaye Anamkimu kila asiyekuwa Yeye. Viumbe wote kwa hiyo, humhitajia Yeye, Na Yeye si Mwenye uhitaji kwao, wao hawawezi pa kuegemea pasi na Amri Yake. Hivyo, Allah تعالى Amesema,

وَمِنَ آيَاتِهِ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ

“Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake.” (30:25)

3. Kauli ya Allah تعالى،

لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ

“Hashikwi na usingizi wala Kulala.”

Maana yake: Hana upungufu, kughafilika wala kujingikiwa na jambo. Bali, Anaudhibiti wa kila nafsi inachochuma, Anaangalia kila kitu, hapana kinachoepa Ufahamu Wake, wala hakuna chenye kufichika Kwake. Miongoni mwa Ukamilifu wa Usimamizi Wake ni kwamba Hasinzii wala Halali. Kwa hiyo Kauli ya Allah تعالى ifuatayo:

لَا تَأْخُذْهُ رِسْنَةٌ

“Hashikwi na Usingizi.” Maana yake: Hapatwi *“na Usingizi.”* Inaonesha kwamba hapatwi na jambo wala Allah تعالى Hasinzii. Baadaye Allah تعالى Alisema:

وَلَا نَوْمٌ

“Wala kulala.” Ambako ni zaidi ya kusinzia. Imenukuliwa kwenye Sahih¹ kuwa Abu Musa رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisimama na kutuhutubia juu ya mambo manne.

«إِنَّ اللَّهَ لَا يَنَامُ، وَلَا يَتَّبِعِي لَهُ أَنْ يَنَامَ، يَخْفِضُ الْقِسْطَ وَيَرْفَعُهُ، يُرْفَعُ إِلَيْهِ عَمَلُ النَّهَارِ قَبْلَ عَمَلِ اللَّيْلِ، وَعَمَلُ اللَّيْلِ قَبْلَ عَمَلِ النَّهَارِ، حِجَابُهُ النُّورُ - أَوِ النَّارُ - لَوْ كُنْتُمْ لِأَخْرَقْتُمْ سُبْحَاتٍ وَجَنِّهِ مَا انْتَهَى إِلَيْهِ بَصَرُهُ مِنْ خَلْقِهِ»

“Hakika Allah Halali, wala haiyumkini kulala. Huteremsha vipimo na Kuvipandisha. Amali za mchana zinapandishwa mbele Yake kabla ya amali za usiku, amali za usiku kabla ya amali za mchana. Hijabu Yake ni Nuru, au Moto, na lau kama Angeliiondoa, basi miale ya Uso Wake, ingeunguza kila kiumbe chake kinachofikiwa na Macho Yake.”¹

4. Na Kauli Yake,

لَهُمْ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Ni Vyake pekee vyote vilivyomo mbinguni na duniani”.

Inatoa khabari kuwa wote ni waja wa Allah تعالى na wako katika ufalme Wake na chini ya nguvu Zake na Mamlaka Yake. Kama Kauli Yake,

إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ عَبْدًا ﴿٢٥٤﴾ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٢٥٥﴾ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٢٥٦﴾

¹ Muslim 1:162.

"Hapana yeyote aliye mbinguni na ardhini ila atafika kwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema akiwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao atamfikia Siku ya kiyama peke yake." (19:93-95)

5. Na Kauli Yake,

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

"Ni nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya Idhini Yake?"

Ni kama Kauli Yake,

﴿ وَكَرَّمْنَا فِي الْمَلَكِ فِي السَّمَوَاتِ لَأُتَغْنَى شَفَعْتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ

وَيَرْضَى ۝﴾

"Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa Idhini kwa amtakaye na kumridhia." (53:26) Na,

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنْ آذَنَ

"Wala hawamuombei yeyote ila yule Anayemridhia Yeye." (21:28)

Aya hizi zinatilia mkazo Ukubwa wa Allah تعالیٰ, Utukufu na Majivuno ya Mwenyezi Mungu, na kwamba hapana yeyote anayeweza kuthubutu kumwombea mtu yeyote, isipokuwa kwa ruhusa Yake. Ni kama ilivyoelezwa katika Hadithi inayozungumzia juu ya kumwombea mtu mwingine, inasema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَتَيْتُ نَحْتَ الْعَرْشِ فَأَخِرْتُ سَاجِدًا، فَبَدَعَنِي مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَدْعَنِي. ثُمَّ يُقَالُ: اذْفَعْ رَأْسَكَ، وَقُلْ تَسْمَعُ، وَاشْفَعْ تُشْفَعُ - قَالَ: - فَيَحْدُ لِي حَدًّا فَأَدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ»

"Nitasimama chini ya Arshi na nitasujudu, na Allah Ataniruhusu nibaki hapa kwa muda Aupendao. Baadaye nitaambiwa, 'Inua kichwa chako, sema na utasikilizwa, ombea na maombezi yako yatakubaliwa. Kisha Mtume ﷺ akasema, "Ataniruhusu idadi Fulani niwaingize Peponi."¹

¹ Muslim 1:180.

6. Kauli ya Allah تعالیٰ،

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ^ط

"Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao."

Inajulisha juu ya Ufahamu Wake Uliovizunguka viumbe wote wa siku zilizopita, waliopo na wajao. Ni kama Kauli Yake Kuwaambia malaika,

وَمَا نَنْزِلُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ^ط لَهُ مَا بَيْنَ أَيْدِينَا وَمَا خَلْفَنَا وَمَا بَيْنَ ذَلِكَ^ع وَمَا كَانَ رَبُّكَ

نَسِيًّا ﴿٦٤﴾

"(Nao watasema:) Wala hatuteremki ila kwa Amri ya Mola wako Mlezi. Ni Yake Yeye yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu, na yaliyomo katikati ya hao. Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kusahau." (19:64)

7. Kauli ya Allah تعالیٰ،

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ^ع

"Wala wao hawajui chochote katika Ujuzi Wake, ila kwa Atakalo Mwenyewe."

Maana yake: Hapana anayeweza kupata sehemu ya Elimu ya Allah تعالیٰ isipokuwa kile Anachofundishwa na Allah تعالیٰ. Na inachukulika kwamba kusudio ni hawataweza kujua Dhati na Sifa za Allah تعالیٰ, isipokuwa kile Anachowafahamisha. Ni kama katika Kauli Yake,

وَلَا تُحِيطُونَ بِهِ عِلْمًا ﴿١١٠﴾

"Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo." (20:110)

8. Allah تعالیٰ Amesema,

وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ^ط

"Kiti Chake cha Enzi kimetanda mbinguni na duniani."

Wakii alisimulia katika tafsiri yake kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Al-Kursi ni kiti chenye miguu, na hapana mtu yeyote awezaye kuelezea 'Arsh.'¹

¹ At-Tabarani 12:39.

Al-Hakim aliinukuu Hadithi hii katika *Mustadrak*¹ wake na kusema kuwa, ‘Ni sahih kwa mujibu wa kigezo cha mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawakuiandika. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Iwapo mbingu saba na ardhi saba zingekunjuliwa na kulazwa sambamba, zisingeweza kufunika *Al-Kursi* bali ingekuwa ni kama vile Pete inapokuwa katika jangwa.”²

9. Allah تعالى Alisema,

وَلَا يُؤَدُّهُ حِفْظُهُمَا

“Na wala Haemewi na Kuvilinda hivyo.”

Maana yake: Hakumuelemei wala Hakumchoshi Kuzihifadhi mbingu na ardhi, pamoja na vilivyomo humo, na vilivyo baina ya hivyo. Bali hili ni jambo jepesi sana Kwake, na Yeye Anaipatia kipato kila nafsi, Anavichunga vitu vyote, hapana kilichomkwepa na hapana chenye kufichikana Kwake. Vitu vyote ni duni, dhalili, vinyenyekevu na vinamhitajia Yeye. Yeye ni Tajiri Anayestahili Shukrani zote na Hufanya Alitakalo, na hapana wa kumuuliza kuhusu Ayafanyayo, ambapo wao wataulizwa. Ana Nguvu juu ya vitu vyote na Mwenye Kujitosheleza kwa kila kitu. Yeye ni Msimamizi juu ya kila kitu, wa Juu Kabisa, Mkuu, hapana Mola wa Haki Kuabudiwa isipokuwa Yeye wala hapana Mola Mwingine Asiyekuwa Yeye.

10. Kauli ya Allah تعالى,

وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

“Na Yeye Ndiye Aliye juu, na Ndiye Mkuu.”

Ni sawa na Kauli Yake,

الْكَبِيرُ الْمُتَعَالَى

“Mkuu Aliyetukuka.” (13:9)

Aya hizi na nyingine sawa na hizi na Hadithi sahihi kuhusu Sifa za Allah تعالى lazima zichukuliwe kama *Salaf* (watangu waadilifu) walivyo zichukulia kwa kukubali maana za wazi bila ya kuzilinganisha (na sifa za maumbile) na kubadilisha maana zake.

¹ Al-Hakim 2:282.

² Ibn Abu Hatim 3:981.

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ^ط قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ^ع فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِرْ بِاللَّهِ فَقَدْ
 اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ^ط وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾

256. “Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwishapambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila shaka amekamata kishikio madhubuti, kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

Hapana Kulazimisha Katika Dini

Allah تعالى Amesema,

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ^ط

“Hapana kulazimisha katika Dini.” Maana yake: Msimlazimisha mtu yeyote kuingia katika Dini ya Kiislam, kwani Uislam uko dhahiri na ushahidi wake uko wazi, wala hapana haja ya kumlazimisha yeyote kusilimu. Bali yeyote aliyeongozwa na Allah تعالى kwenye Uislamu, na kumfungua moyo wake na kumtia nuru katika uoni wake, ataingia kwenye Uislam kwa dhati. Na yule ambaye Allah تعالى Ameupofusha moyo wake na Akaziba kuona na kusikia kwake, hivyo hatafaidika kwa kulazimishwa kusilimu.

Ilisimuliwa kuwa sababu za kuteremshwa Aya hii ni juu ya baadhi ya Annsar, japokuwa hukumu yake ni ya jumla. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mwanamke (wa Ansar) alipozaa mtoto na kufa, alikula kiapo kuwa, endapo atazaa mtoto na akaishi angemfanya kufuata uyahudi. Walipohamishwa Banu An-Nadhir (kabila la Kiyahudi kutoka Al-Madinah), baadhi ya watoto wa Ansar walikuwa wakilelewa nao, na Ansar wakasema, ‘Hatutowatelekeza watoto wetu.’ Allah تعالى Akateremsha,

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ^ط قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ^ع

“Hapana kulazimisha katika Dini, kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.”¹

Abu Dawud na An-Nasai² pia waliandika Hadithii hii.

¹ At-Tabari 5:407.

² Abu Dawud 3:132, Anasai katika Al-Kubra 6:304.

Ama kuhusu Hadithi iliyoandikwa na Ahmad, ambapo Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alimwambia mtu,

«أَسْلِمُهُ» قَالَ: إِنِّي أَجِدُنِي تَكَرَّهًا قَالَ: «وَأِنْ كُنْتَ تَكَرَّهًا»

“Silimu” Yule mtu akasema, “Nauchukia Uislamu.” Mtume ﷺ akamwambia hata kama unauchukia.”¹

Kwanza, hii ni Hadithi Sahihi, yenye wapokezi watatu tu kutoka kwa Imam Ahmad mpaka kwa Mtume ﷺ. Hata hivyo haina uhusiano na mada tunayojadili, kwa kuwa Mtume ﷺ hakumlazimisha yule mtu kuukubali Uislamu. Mtume ﷺ alimlingania mtu huyu katika Uislamu, na akamjibu kuwa nafsi yake haikuwa ikiukubali, bali iliuchukia Uislam. Mtume ﷺ alimwambia yule mtu, ‘hata kama unauchukia Uislamu, kwani Allah تعالی Atakupa nia njema na dhamira ya kweli.”

Tawhid ni kishikio madhubuti:

Allah تعالی Amesema,

فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِرْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا
وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾

“Basi anayemkataa Shetani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

Maana yake: “Mwenye kujitenga na washirikishwao na Allah تعالی, masanamu na wale ambao Shetani anawaita waabudiwe badala ya Allah تعالی. Pia akawa anampwekesha Allah تعالی, anamuabudu Yeye Pekee na anakariri kuwa hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, basi,

فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ

“Bila shaka amekamata kishikio madhubuti.”

Maana yake: Amekuwa imara (katika Dini) na kuendelea katika njia iliyo sawa na iliyonyooka. Abu Al-Qasim Al-Baghawi alinukuu kuwa Hasan bin Faid Al-

¹ Ahmad 3:181.

Absy amesema kuwa Umar رضي الله عنه alisema, "Jibt ni uchawi, Taghut ni Shetani. Na kwa hakika, Ujasiri na woga ni silika mbili zinazodhihiri kwa wanaume, jasiri huwapigania asiowajua na mwoga hukimbia na kuacha kumhami mama yake. Heshima ya mtu imo katika Dini yake na hadhi yake inategemea tabia yake, hata kama alikuwa Mfursi au Mnabati."¹ Kauli ya Umar رضي الله عنه kuwa Taghut ni Shetani, ina nguvu sana kwani maana hii ni pamoja na kila aina ya uovu ambao walizama watu wa Jahiliyyah, kama vile kuabudu masanamu, wakiyaendea kuhukumiwa na kutaka kupewa nusura.

Na Kauli Yake:

فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ هَا

"Bila shaka amekamata kishikio madhubuti kisichovunjika."

Maana yake: "Atakuwa ameishika Dini ya kweli kwa kamba imara, na mfano wake ni kishikio madhubuti ambacho hakivunjiki, kwani chenyewe ni imara, kimejengwa kwa umadhubuti na kwa sababu kishikio chake ni madhubuti. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ هَا

"Bila shaka amekamata kishikio madhubuti kisichovunjika."

Mujahid alisema, "Kishikio madhubuti, maana yake ni Imani."² As-Suddi alisema, "Ni Uislamu."³ Imam Ahmad alinukuu kuwa Qays bin Ubadi alisema, 'Nilikuwa ndani ya Masjid, akaja mtu ambaye uso wake ulionesha unyenyekevu. Akaingia, akasali Rakaa mbili zenye urefu wa wastani. Watu wakasema, 'Huyu ni miongoni mwa watu wa peponi.' Alipoondoka nilimfuata mpaka alipoingia nyumbani kwake, na nikaingia baada yake na nikazungumza naye. Alipokuwa amepumzika, Nikamwambia, 'Ullipoingia Masjid, watu walisema maneno kadha wa kadha.' Akasema, 'Subhanallah' (Utakasifu ni wa Allah عزوجل!) Haifai mtu kuzungumza jambo asilo na ilmu nalo. Nitakuambia kwanini nasema hivyo? Niliota wakati wa Mtume ﷺ, na nikamsimulia. Niliona kana kwamba nilikuwa katika bustani ya kijani." Ibn Awn amesema, na

¹ At-Tabari 5:417, wanabat ni watu waliokuwa wakiishi Jordan, yaani hata kama hakuwa mwarabu.

² At-Tabari 5:421.

³ At-Tabari 5:421.

akaelezea mimea yake na upana wake. Katikati yake kulikuwa na nguzo ya chuma ambayo ilifika ardhini na kwa juu ilifika kwenye mbingu. Juu ya ncha yake kulikuwa na kishikio na nikaambiwa: 'Panda juu yake.' Nikajibu, 'Siwezi' Akanijia mtumishi. Akanyanyua nguo zangu kwa nyuma na akaniambia, 'Panda.' Nikapanda mpaka nikakamata kishikio. Akaniambia, "Shikilia kishikio." Nikaamka na mpini uko mkononi. Nikaenda kwa Mtume ﷺ na kumhadithia ile ndoto naye akasema,

«أَمَّا الرَّوْضَةُ فَرَوْضَةُ الْإِسْلَامِ، وَأَمَّا الْعَمُودُ فَعَمُودُ الْإِسْلَامِ، وَأَمَّا الْعُرْوَةُ فَهِيَ
الْعُرْوَةُ الْوُثْقَى، أَنْتَ عَلَى الْإِسْلَامِ حَتَّى تَمُوتَ»

*"Ama bustani, ni bustani ya Uislamu, ama Nguzo Nguzo za Uislamu;
na kishikio ni kishikio madhubuti. Wewe utabaki ukiwa Muislam
mpaka kufa kwako."*

Sahaba huyu alikuwa Abdullah bin Salam رضي الله عنه.¹

Hadithi hii ilikusanywa katika Sahihi Mbili,² na Al-Bukhari pia alinukuu kwa isnadi tofauti.³



¹ Ahmad 5:452.

² Fat'hul Al-Bari 7:161, Muslim 4:1930.

³ Fat'hul Al-Bari 2:418.

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ حَاجَّ إِبرَاهِيمَ فِي رَيْبِهِ أَنِ ءَاتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ إِذْ قَالَ إِبرَاهِيمُ رَبِّيَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ قَالَ أَنَا أُحْيِي وَأُمِيتُ ۗ قَالَ إِبرَاهِيمُ فَإِنَّ اللَّهَ يَأْتِي بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَأْتِ بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ فَبُهِتَ الَّذِي كَفَرَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥٨﴾ أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَى قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَى عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّى يُحْيِي هَذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ ۗ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ۗ قَالَ لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۗ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِائَةَ عَامٍ فَانظُرْ إِلَى طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّه ۗ وَانظُرْ إِلَى حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ ءَايَةً لِّلنَّاسِ ۗ وَانظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِئُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۗ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٥٩﴾

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

257. "Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na Kuwaingiza kwenye mwangaza. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni mashetani. Huwatoa kwenye mwa-ngaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni na humo watadumu."

Allah تعالى Amesema kuwa yeyote anayefuata yale Anayoyaridhia, Anawatoa kutoka katika kiza cha Ukafiri, mashaka na wasi-wasi na Kuwaongoza waja wake Waumini kwenye Nuru ya haki, kunjufu, dhahiri,

rahisi na inayoangaza. Pia alieleza kuwa shetani ni msaidizi wa makafiri ambaye huwapambia mambo waliyo nayo, miongoni mwa mambo ya kijinga na upotofu, hivyo kuwafanya kuacha njia ya ukweli na kufuata ukafiri na ufisadi.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

“Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu.”

Hii ndio sababu Allah تعالى Aliitaja nuru kwa umoja na Akataja kiza kwa wingi, kwa sababu ukweli ni mmoja na ukafiri ni wa namna nyingi na zote ni batili. Hivyo, Allah تعالى Amesema,

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَٰلِكُمْ وَصَنَعْنَا بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢٥٨﴾

“Na kwa hakika hii ndiyo Njia Yangu iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuatate njia nyingine, zikakutengeni na Njia Yake. Haya Amekuusieni ili mpate kuchamungu.”(6:153),

Na Allah تعالى Amesema, وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ

“Amejaalia viza na nuru.” (6:1) Na,

عَنِ الَّتِيْمِيْنَ وَالشَّمَايِلِ

“Kuliani na kushotoni.” (16:48)

Kuna Aya nyingi nyingine juu ya somo hili ambazo zimetaja ukweli kwa umoja na batili kuwa ina matawi mengi.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِي حَاجَّ إِبْرَاهِيمَ فِي رَبِّهِ أَنْ ءَاتَهُ اللَّهُ الْمَلْكَ إِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّيَ
الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ قَالَ أَنَا أُحْيِي وَأُمِيتُ قَالَ إِبْرَاهِيمُ فَإِنَّ اللَّهَ يَأْتِي بِالشَّمْسِ
مِنَ الْمَشْرِقِ فَأْتِ بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ فَبُهِتَ الَّذِي كَفَرَ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الضَّالِّينَ ﴿٢٥٨﴾

258. “Hukumuona yule aliyehojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi kwa sababu Mwenyezi Mungu Alimpa ufalme? Ibrahim aliposema: Mola wangu ni Yule Ambaye Huhuisha na Kufisha. Yeye akasema: Mi pia nahuisha na kufisha. Ibrahim akasema: Mwenyezi Mungu Hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi. Akafedheheka yule aliyekufuru; na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhalimu.

Mjadala Kati ya Nabii Ibrahim Khalilul-Llah عليه السلام na Numrud:

Mfalme aliyebishana na Ibrahim عليه السلام alikuwa Mfalme wa Babil, Numrud bin Kan'aan bin Kush bin Sam bin Nuh. Inasemekana pia alikuwa akiitwa Namrud bin Falikh bin Abir bin Shalikh bin Arfahshadh bin Sam bin Nuh. Kauli ya kwanza ni ya Mujahid na wengineo. Mujahid alisema, "Wafalme wenye umashuhuri waliotawala sehemu za Mashariki na Magharibi ya dunia ni wanne, waumini wawili na makafiri wawili. Ama wafalme waumini wawili walikuwa Sulayman bin Dawud عليه السلام na Dhul-Qarnayn. Ama wafalme makafiri wawili, walikuwa Namrud na Bukhtunaswar (Nebuchad Nezzar).¹ Allah Ndiye Mjuzi zaidi. Allah تعالى Amesema:

أَلَمْ تَرَ

"Hukumuona." "Kwa moyo wako Ewe Muhammad!"

إِلَى الَّذِي حَاجَّ إِبْرَاهِيمَ فِي رَيْبِهِ

"Yule aliyehojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi."

Maana yake: Kuhusu kuwepo Allah تعالى. Numrud alikanusha kuwepo Mola asiyekuwa yeye kwa madai yake, kama Firauni alivyowaambia watu wake,

مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرِي

"Sijui kama mnaye mola asiyekuwa mimi." (28:38)

Kilichomfanya Numrud achupe mipaka, kukufuru na kuasi ni utawala wake wa mabavu uliodumu kwa muda mrefu. Ndio sababu Aya iliendelea,

أَنْ آتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ

"Kwa sababu Mwenyezi Mungu Alimpa ufalme?"

Inaelekea kuwa Namrud alimtaka Ibrahim عليه السلام kuthibitisha kuwa Allah تعالى yupo, Ibrahim عليه السلام akajibu,

رَبِّي الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ

"Mola wangu ni Yule Ambaye Huhuisha na Kufisha."

¹ At-Tabari 5:433.

Maana yake: “Uthibitisho kuwa Allah تعالى Yupo ni kupatikana kwa vitu hivi mbalimbali baada ya kutokuwepo kwake, na kutokuwepo baada ya kuwepo. Huu ni uthibitisho wa kuwepo kwa Muumba. Anayefanya Ayatakayo, kwani vitu hivi visingelitokea vyenyewe bila kuwepo Muumba Aliyeviumba, na Yeye ni Mola Ambaye ninalingania kwamba aabudiwe Yeye Peke Yake bila mshirika.” Ndipo mbishi, Numrud akasema,

أَنَا أُخِيءُ وَأُمِيتُ

“Mimi pia nahuisha na kufisha.”

Qatadah, Muhammad bin Ishaq na As-Suddi walisema kuwa alikuwa na maana, “Watu wawili waliostahiki kuuwawa, wangeletwa mbele yangu na ningeamrisha mmoja wao auwawe, angeuwawa. Na nitaamrisha kwa mtu wa pili asamehewe na angesamehewa. Hivi ndivyo nahuisha mtu na kumfisha.”¹ Hata hivyo, inaelekea kuwa, kwa kuwa Numrud hakukanusha kuwepo kwa Muumba, kauli yake haikumaanisha yale aliyoyasema Qatadah. Maelezo haya hayatupi jibu kwa yale aliyoyasema Ibrahim عليه السلام. Numrud kwa ufedhuli na kwa kuasi alidai kuwa yeye alikuwa muumbaji na kujifanya kuwa analeta uhai na kifo. Baadaye, Firauni alimuiga na akatangaza,

مَا عَلَّمْتُ لَكُمْ مِنَ الْدِينِ غَيْرِي

“Sijui kama mnaye mola asiyekuwa mimi.” (28:38)

Hii ndiyo sababu Ibrahim عليه السلام alimuambia Numrud,

فَإِنَّ اللَّهَ يَأْتِي بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَأْتِ بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ

“Mwenyezi Mungu Hulichomozesha jua Mashariki, basi wewe lichomozeshe Magharibi.”

Aya hii ina maana: Unadai kuwa unaleta uhai na kifo. Ambaye analeta uhai na kifo Anaudhibiti uhai na Anaumba kila kilichomo ndani yake, ikiwa ni pamoja na Kudhibiti sayari na mizunguko yake. Kwa mfano, jua linapanda kila siku upande wa mashariki. Kwa hiyo, kama ungekuwa Mungu, kama unavyodai, kuleta uhai na kifo, basi litokeze jua kutoka Magharibi. Kwa kuwa mfalme alikuwa anajua udhaifu wake na upungufu wake na kuwa hakuweza kutekeleza

¹ At –Tabari 5:433, 436, 437.

ombi la Ibrahim عليه السلام, alikaa kimya, maana yake akashindwa kuzungumza. Kwa hiyo, ushahidi uliotolewa ulikuwa dhidi yake. Allah تعالى Amesema;

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhalimu.”

Maana yake: Allah تعالى Huwakosesha madhalimu ushahidi wa wazi na hoja zenye nguvu. Zaidi ya hayo, hoja zao hazina nguvu na ni batili na Mola Amewakasirikia na wataadhibiwa vikali. Maana tuliyoitoa ni sahihi zaidi kuliko iliyotolewa na watu wa mantiki. Kwa hakika, Ibrahim عليه السلام alitumia hoja ya pili badala ya ile ya kwanza kwa sababu ndiyo iliyokuwa wazi zaidi, na inadhihirisha ubatilifu wa madai ya Numrud katika hoja ya kwanza na ya pili. Shukrani zote Anastahiki Allah تعالى. As-Suddi alieleza kuwa mdahalo baina ya Ibrahim عليه السلام na Numrud ulitokea baada ya Ibrahim عليه السلام kutupwa ndani ya moto, kwani Ibrahim عليه السلام hakukutana na mfalme kabla ya siku ile.

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِي هَذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ
فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ ۗ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ۗ قَالَ لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۗ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِائَةَ عَامٍ فَانظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ ۗ وَانظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ
وَلِنَجْعَلَكَ ءَايَةً لِلنَّاسِ ۗ وَانظُرْ إِلَىٰ الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۗ
فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٥٩﴾

259. “Au kama yule aliyepita karibu na mji mtupu wenye magofu tu, akasema; Ataufufuaje Mwenyezi Mungu mji huu baada ya kufa kwake? Basi Mwenyezi Mungu Alimfisha yeye muda wa miaka mia. Kisha Akamfufua. Akamuuliza: Je umekaa muda gani? Akajibu: Labda nimekaa siku moja au sehemu ya siku. Akamuambia: Bali umekaa miaka mia wewe. Hebu angalia chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika. Na muangalie punda wako, na ili Tukufanye uwe ni ishara kwa watu, iangalie hii mifupa jinsi Tunavyoinyanyua kisha Kuivisha nyama. Basi yalipombainikia alinena: Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”

Kisa cha Uzayr:

Kauli ya Allah تعالى iliyotangulia Aliyosema;

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِي حَاجَّ إِبْرَاهِيمَ فِي رَبِّهٖ

“Hukumuona yule, aliyehojiana na Ibrahim juu ya Mola wake Mlezi.” (2:258)

Maana yake: “Je umemuona mtu kama yule aliyebishana na Ibrahim عليه السلام kuhusu Mola wake?” Kisha, Allah تعالى Aliziunganisha Aya,

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا

“Au kama yule aliyepita karibu na mji mtupu wenye magofu tu.”

Na Aya hapo juu kwa kutumia ‘au.’

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Najiyah bin Ka’b kuwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema kuwa huyo anayezungumzwa ni ‘Uzayr.’¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى naye alisimulia kutoka kwa Najiyah mwenyewe. Na maelezo haya yalisimuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abbas, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na Sulayman bin Buraydah رضي الله عنهم.³

Mujahid bin Jabr alisema kuwa Aya hii inamhusu mtu mmoja miongoni mwa Wana wa Israil, na mji uliozungumziwa ulikuwa *Baytul Muqaddas*, baada ya kuangamizwa na Nebuchad Nezzar (Bukhtunaswar) pamoja na kuuu watu wake.

وَهِيَ خَاوِيَةٌ

“Mji mtupu.” Maana yake: Hakuwa na Mtu. Kauli ya Allah تعالى,

عَلَىٰ عُرُوشِهَا

“Wenye magofu tu.” Inaonesha kuwa mapaa na kuta (za kijiji) zilianguka chini. ‘Uzayr alisimama akiwaza kuhusu yaliyojiri katika mji ule, baada ya kuwa kulikuwa na watu waliostaarabika walioishi hapo. Akasema,

¹ Ibn Abu Hatim 3:1009.

² At-Tabari 5:439.

³ At-Tabari 5:439– 440, Ibn Abu Hatim 3:1009 – 1010.

أَنِّي يُحْيِي هَذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا^ط

“Ataufufuaje Mwenyezi Mungu mji huu baada ya kufa kwake?”

Kwa sababu ya uharibifu mkubwa aliouona na kutowezekana kurejea kama ulivyokuwa mwanzo. Allah تعالى Amesema:

فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ^ط

“Basi Mwenyezi Mungu Alimfisha yeye muda wa miaka mia.”

Mji ulijengwa upya baada ya miaka sabini kupita baada ya kufa Uzayr, na wakazi wake waliongezeka na Wana wa Israil walirejea kwenye mji ule. Allah تعالى Alipomfufua Uzayr baada ya kufa, kiungo cha kwanza kufufuliwa kilikuwa macho, ili ashuhudie mwenyewe alichokuwa anafanyiwa na Allah, تعالى Anavyourejesha uhai kwenye mwili. Kufufuliwa kwake kulipotimia, Allah تعالى Alimwambia, kupitia malaika,

كَمْ لَبِثْتُمْ^ط قَالِ لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ^ط

“Je, Umekaa muda gani? Akajibu: Labda nimekaa siku moja au sehemu ya siku.”

Wanazuoni walisema kuwa, yule mtu alikufa mwanzo wa siku na Allah تعالى Alimfufua jioni, alipoona jua bado halijazama, akadhani lilikuwa jua la siku ile ile. Akasema,

أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ^ط قَالِ بَلْ لَبِثْتَ مِائَةَ عَامٍ فَانظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ^ط

“Au sehemu ya siku, Akamwambia: Bali umekaa miaka mia wewe. Hebu angalia chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika.”

Alikuwa na zabibu, tini na maji ya matunda, na alivikuta kama alivyoviacha; juisi haikuharibika wala tini hazikuwa chungu wala zabibu hazikuoza.

وَأَنْظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ

“Na mwangalie Punda wako.”Maana yake: “Jinsi Allah تعالى Anavyomrudishia maisha huku yeye mwenyewe akiangalia.”

وَلَنَجْعَلَكَ آيَةً لِلنَّاسِ ط

“Na ili tukufanye uwe ni ishara kwa watu.” Kuwa ufufuo hutokea,

وَأَنْظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ تُنْشِرُهَا

“langalie hii mifupa yake jinsi Tunavyoinyanyua.”Maana yake: Tunainyanyua na Kuiweka tena pamoja. Katika Mustadrak wake, Al-Hakim, alinukuu kuwa Kharijah bin Zayd bin Thabit alisema kuwa baba yake alisema kuwa Mtume ﷺ alisoma Aya hii,

كَيْفَ تُنْشِرُهَا

“Kaifa Nunshizuha.”Kwa kutumia herufi *Zai*, halafu (Al-Hakim) akasema, “Isnad yake ni Sahihi na wao (Bukhari na Muslim) hawakuiandika.”¹

Na Aya ilisomwa pia,

(نُشِرُهَا)

(Nunshiruha.) Maana yake: Tunaurejesha uhai. Haya yalisemwa na Mujahid.²

ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا

“Kisha Tunaivisha nyama.” As-Suddi alisema, “Uzayr aliona mifupa ya punda upande wake iliyotawanyika kuzunguka kuliani na kushotoni; na Allah تعالى Alituma upepo ambao ulikusanya mifupa katika maeneo yote. Akaitazama ikiwa na rangi ya weupe wa kuchakaa. Kisha Allah تعالى Akaurejesha kila mfupa mahali pake, mpaka akawa punda mzima asiye na nyama. Kisha Allah تعالى Aliifunika kwa nyama, neva, mishipa na ngozi. Allah تعالى Alimtuma malaika ambaye alimpulizia katika tundu mbili za pua ya punda na akaanza kulia. Yote haya ni kwa Idhini ya Allah تعالى.”³ Yote hayo yalijiri wakati Uzayr akitazama, na hapa ndipo aliponadi,

قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٥٨﴾

“Alinena: Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”

Maana yake: “Nayajua hayo, na nilishuhudia kwa macho yangu. Kwa hiyo suala hili nalifahamu zaidi miongoni mwa watu wa zama zangu.”

¹ Al-Hakim 2:234.

² At-Tabari 5:476.

³ At – Tabari 5:468.

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ قَالَ أَرَأَيْتَ إِنْ أَخَذَ مِنْ الطَّيْرِ فَصْرَهُنَّ لِيَلْجَأَنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ أَجْعَلَ عَلَىٰ كُلِّ جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ أَدْعُهُنَّ يَأْتِينَكَ سَعْيًا ۗ وَاعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦٠﴾

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَتَتْ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُنبُلَةٍ مِّائَةٌ حَبًّا ۗ وَاللَّهُ يُضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ لَا يُتْبِعُونَ مَا أَنْفَقُوا مَنًّا وَلَا أَذًى ۗ هُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٦٢﴾

* قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّنْ صَدَقَةٍ يَتَّبِعُهَا أَذًى ۗ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَلِيمٌ ﴿٢٦٣﴾

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَبْطُلُوا صَدَقَتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَىٰ كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ رِثَاءَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابُهُ وَابِلٌ فَتَرَكَهُ صَلْدًا ۗ لَا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوا ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦٤﴾

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ قَالَ أَرَأَيْتَ إِنْ أَخَذَ مِنْ الطَّيْرِ فَصْرَهُنَّ لِيَلْجَأَنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ أَجْعَلَ عَلَىٰ كُلِّ جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ أَدْعُهُنَّ يَأْتِينَكَ سَعْيًا ۗ وَاعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦٠﴾

260. "Na aliposema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nioneshe jinsi unavyofufua wafu. Mwenyezi Mungu Akasema: kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wagu utue. Akamwambia: Twaan ndege wanne na uwaozeshe kwako, kisha uweke juu ya kila kilima sehemu, kisha uwaite, watakuja mbio. Na ujue kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mtu-kufu Mwenye Nguvu, na Mwenye Hikima."

Khalil (Ibrahim عليه السلام) Alimuomba Allah تعالى Amuoneshe Anavyowafufua Wafu

Wanazuoni wanasema kuwa kuna sababu nyingi zilizomfanya Ibrahim عليه السلام kumwomba Allah تعالى amuoneshe Anavyowafufua wafu, mojawapo ni wakati Ibrahim عليه السلام alipomuambia Numrud.

رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ

“Mola wangu mlezi! Nioneshe vipi Unavyofufua wafu.”

Alitaka kuimarisha elimu yake juu ya ufufuo kwa kushuhudia kwa macho yake. Mtume Ibrahim عليه السلام alisema,

رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ قَالَ أُولَٰئِكَ تُؤْمِنُ ۗ قَالَ بَلَىٰ ۗ وَ لَٰكِن لِّيُطَمِّئَنَّ قَلْبِي ۗ

“Mola wangu mlezi! Nioneshe vipi Unavyofufua wafu. Mwenyezi Mungu Akasema: Kwani Huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue.”

Bukhari alinukuu kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«نَحْنُ أَحَقُّ بِالسُّكِّ مِنْ إِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ

“Sisi tuna haki zaidi ya kuwa na wasiwasi kuliko Ibrahim aliposema,

رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ قَالَ أُولَٰئِكَ تُؤْمِنُ ۗ قَالَ بَلَىٰ ۗ وَ لَٰكِن لِّيُطَمِّئَنَّ قَلْبِي ۗ

“Mola wangu! Nioneshe unavyohuisha wafu.” Allah Akamuambia, “Je Huamini?” Ibrahim akasema, “Ndiyo (Naamini), lakini (Nauliza) ili moyo wangu utulie (ili niimarisha uhakika).”¹

Maana yake: Ni kwamba, “Sisi tunastahiki zaidi katika kuitafuta yakini.”

Majibu kwa Maombi ya Ibrahim Al-Khalil عليه السلام:

Allah تعالى Amesema,

قَالَ فَخُذْ أَرْبَعَةً مِّنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ إِلَيْكَ

“Akamuambia: Twaa ndege wanne na uwaozeshe kwako.”

Wanazuoni wa Tafsir wametofautiana kuhusu aina ya ndege wanne waliotajwa hapa. Jambo hili halina umuhimu hapa kwa kuwa halikutajwa katika Qur’an. Kauli ya Allah تعالى,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:49.

فَصَرَّهُنَّ إِلَيْكَ

“Na uwazoeshe kwako.”

Maana yake: Kuwakatakata vipande. Haya ni maelezo ya Ibn Abbas, Ikrimah, Said bin Jubayr, Abuu Malik, Abuu Al-As'wad Ad-Dili, Wahb bin Munabbil, Al-Hasan, na As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم¹. Wamesema kwamba, Ibrahim عليه السلام aliwashika ndege wanne, akawachinja, akawanyonyoa, akawakatakata vipande kisha akavichanganya pamoja. Kisha akaviweka vipande hivyo vilivyochanganyika juu ya vilima vine au saba. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ibrahim عليه السلام aliviweka vichwa vya ndege hao kwenye mkono wake. Baada ya hayo, Allah تعالى Alimuamrisha Ibrahim kuwaita wale ndege, na akafanya kama Alivyoamrishwa na Allah تعالى. Ibrahim عليه السلام alishuhudia manyoya, damu na nyama za ndege hao zikipaa kuelekeana, na vipande viliruka kuelekea miili yao, mpaka kila ndege akawa hai, na wakatembea kwa kasi kuelekea kwa Ibrahim عليه السلام, ili ashuhudie vyema liile aliloliomba. Kila ndege alikuja kuchukua kichwa chake kilichokuwa mkononi kwa Ibrahim عليه السلام. Alipompa ndege kichwa ambacho hakikuwa chake, alikikataa, na alipompa kile cha kwake kiliwekwa kwenye mwili kwa Uweza na Nguvu za Allah تعالى.² Ndio sababu Allah تعالى Amesema,

وَأَعْلَمَ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦٠﴾

“Na ujue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

Maana yake: Ni Mwenye Nguvu, Hakimshindi kitu, wala hakuna cha kujizuia dhidi Yake. Lolote Alitakalo Allah تعالى, Hutokea bila kipingamizi, kwa sababu Yeye ni Mkuu, Mwenye Uweza juu ya kila kitu, na Mwenye Hikima katika Kauli Yake, Matendo, Sharia na Maamrisho.

Abdur-Razzak amesema kuwa Ma'mar alisema kuwa Ayyub alizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

وَلَكِنْ لِّيَطْمَئِنَّ قَلْبِي

“Lakini ili moyo wangu utue.”

¹ Ibn Abu Hatim 3:1039, 1040.

² Al-Qurtubi 3:300.

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kwangu mie, hapana Aya ndani ya Qur’an ambayo inaleta matumaini zaidi ya hii¹.” Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Muhammad bin Al-Munkadir alisema kuwa Abdullah bin Abbas رضي الله عنه alikutana na Abdullah bin Amr bin Al-As رضي الله عنه na alimuuliza bin Amr رضي الله عنه, “Ni Ayah ipi katika Qur’ani inayokupa matumaini?” Ibn Amr alisema ni Kauli ya Allah تعالى isemayo:

﴿ قُلْ يَاعِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا

“Sema: Enyi Waja wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tama...” (39:53)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Lakini mimi ninasema kuwa ni Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۗ قَالَ أُولَٰئِكَ تُؤْمِنُونَ ۗ قَالَ بَلَىٰ

“Na aliposema Ibrahim: Mola wangu Mlezi! Nioneshe vipi Unavyofufua wafu. Mwenyezi Mungu Akasema: kwani huamini? Akasema: Hasha!”

Allah تعالى Aliridhia uthibitisho wa Ibrahim عليه السلام kwa kusema, ‘Hasha.’ Ayah hii inahusu wasiwasi unaoupata moyo na fikra zinazotokana na msukumo wa shetani.² Al-Hakim aliinukuu katika Al-Mustadrak na alisema: Isnad Yake ni Sahih lakini hawakuinukuu.³ Bukhari na Muslim.

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أُنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُنبُلَةٍ

مِائَةٌ حَبَّةٌ ۗ وَاللَّهُ يُضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

261. “Mfano wa wanaotumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuzwa mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mwenye Kujua.”

¹ At-Tabari 5:489.

² Ibn Abu Hatim 3:1032.

³ Al-Hakim 4:260.

Malipo ya kutoa kwa Ajili ya Allah تعالی:

Huu ni mfano Alioutoa Allah تعالی kuhusu kuzidisha malipo kwa wale wanaotoa katika Njia Yake, na kutafuta ridhaa Yake. Allah تعالی Huzidisha amali njema mara kumi mpaka mia saba. Allah تعالی Amesema,

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

“Mfano wa wanaotumia mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu.”

Said bin Jubayr aliitolea maelezo kuwa, “Ina maana: Kwa ajili ya kumtii Allah تعالی.”¹ Mak-hul alisema kuwa Aya ina maana, “Kutoa kwa ajili ya Jihad miongoni mwa kamba za kuwafungia farasi na kuandaa silaha.”² Mfano huu unavutia zaidi katika nafsi kuliko kutaja tu nambari mia saba kwani hii ni ishara kwamba Allah تعالی “Hukuza” amali njema kwa watendaji wake, kama ambavyo Huukuza mmea kwa wale wanaopanda mbegu kwenye ardhi yenye rutuba. Sunnah pia inataja kuwa amali zinazidishwa mara mia saba. Kwa mfano, Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa kuna mtu alitoa ngamia na hatamu yake, kwa ajili ya Allah تعالی na Mtume ﷺ alisema,

لَنَأْتِيَنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِسَبْعِمِائَةِ نَاقَةٍ مَخْطُومَةٍ

“Siku ya Kiyama, utakuwa na ngamia mia saba pamoja na hatamu zao.”

Muslim na An-Nasai pia waliinukuu Hadithi hii, na usimulizi wa Muslim unasomeka, “Mtu alileta ngamia pamoja na hatamu yake na akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Hii ni kwa ajili ya Allah!” Mtume ﷺ alisema,

«لَكَ بِهَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ سَبْعِمِائَةِ نَاقَةٍ»

“Kwa kutoa huku Siku ya Kiyama utapata ngamia mia saba.”³

Katika Hadithi nyingine, Ahmad amemnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa alisema kwamba Mtume ﷺ amesema:

¹ Ibn Abu Hatim 3:1047.

² Ibn Abu Hatim 3:1047.

³ Muslim 3:1505, An-Nasai 6:49.

«كُلَّ عَمَلِ ابْنِ آدَمَ يُضَاعَفُ، الْحَسَنَةُ بِعَشْرِ أَمْثَالِهَا، إِلَى سَبْعِمِائَةِ ضِعْفٍ، إِلَى مَا شَاءَ اللَّهُ، يَقُولُ اللَّهُ: إِلَّا الصَّوْمَ فَإِنَّهُ لِي، وَأَنَا أَجْزِي بِهِ، يَدْعُ طَعَامَهُ وَشَهْوَتَهُ مِنْ أَجْلِي، وَلِلصَّائِمِ فَرْحَتَانِ: فَرْحَةٌ عِنْدَ نِطْرِهِ وَفَرْحَةٌ عِنْدَ لِقَاءِ رَبِّهِ، وَلَخَلُوفٌ فَمِ الصَّائِمِ أَطْيَبُ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ رِيحِ الْمَسْكِ، الصَّوْمُ جُنَّةٌ، الصَّوْمُ جُنَّةٌ»

“Kila amali njema atakayofanya mwanadamu itazidishwa mara kumi mpaka mara mia saba, kwa mara nyingi kama Anavyotaka Allah. Allah Amesema, ‘Isipokuwa Funga, kwani hiyo ni Yangu.’ Mfungaji ana furaha mbili, anapofuturu na atakapokutana na Mola wake. Kwa hakika harufu inayotoka kinywani mwake mfungaji ni nzuri zaidi kwa Allah kuliko harufu ya miski. Kufunga ni ngao (dhidi ya kufanya makosa), funga ni ngao.”² Muslim aliinukuu Hadithi Hii.³

Na Kauli ya Allah تعالى

وَاللَّهُ يُضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ⁴

“Na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye.”

Kwa mujibu wa unyenyekevu kwenye amali zake.

وَاللَّهُ وَسِعَ عَلِيمٌ ﴿٣٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mwenye Kujua.”

Maana yake: Rehema Zake Huwaenea waja Wake wote, na Anamfahamu kwa dhati yule anayestahiki au asiyestahiki. Shukurani na Sifa zote zinamstahiki Allah تعالى.

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ لَا يُتَّبِعُونَ مَا أَنْفَقُوا مَنًّا وَلَا أَدَىٰ ۗ لَهُمْ أَجْرُهُمْ
عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٧﴾ * قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّنْ
صَدَقَةٍ يَتَّبِعُهَا أَدَىٰ ۗ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَلِيمٌ ﴿٣٨﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُبْطَلُوا صَدَقَتِكُمْ
بِأَمْنٍ وَالَّذِينَ كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ رِئَاءَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَمَثَلُهُ

¹ Ahmad 2:443.

² Muslim 2:807.

كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُ وَابِلٌ فَتَرَكَهُ صَلْدًا ۖ لَا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّمَّا
كَسَبُوا ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦٤﴾

262. "Wanaotoa mali zao kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii masimbulizi wala udhia kwa walichotoa, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika."

263. "Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko Sadaka inayofuatiwa na maudhi. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitoshia na Mpole."

264. "Enyi mlioamini! Msiharibu Sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anayetoa mali yake kwa kuwaonesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyochuma. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri."

Makatazo ya Kutoa Sadaka kwa Masimango na Masimbulizi

Allah تعالی Amewasifu wanaotoa mali zao katika Njia Yake, na wakaacha kujisifu kwa wale waliopokea Sadaka, ima kwa maneno au matendo.

Kauli ya Allah تعالی,

وَلَا أُذِي

"Wala udhia." Maana yake: Hawaleti karaha kwa wale waliowafanyia ihsani, kwani madhara hayo yatabatilisha Sadaka. Imefuatiwa na Ahadi ya Allah تعالی kuwa Atawalipa malipo bora kwa amali yake njema,

هُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ

"Wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi."

Inaonesha kuwa malipo ya matendo yao mema si kutoka kwa mwingine isipokuwa Allah تعالی Mwenyewe. Zaidi ya hapo,

وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“Wala haitokuwa khofu juu yao.” Kutokana na vitisho vya siku ya Kiyama.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٦٠﴾

“Wala hawatahuzunika.” Kuhusu watoto watakaowaacha nyuma na mateso na furaha za dunia hii. Hawatahuzunika kwa hili, kwa sababu watapata yaliyo bora kwao. Kisha Allah تعالى Amesema,

* قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ

“Kauli njema.” Maana yake: Maneno mazuri na dua kwa ajili ya Muislamu.

وَمَغْفِرَةٌ

“Na usamehevu.” Maana yake: Kusamehe dhuluma ya kivitendo au maneno,

حَسْرَةٌ مِّنْ صَدَقَةٍ يَتَّبِعُهَا أَذَىٰ

“Ni bora kuliko sadaka inayofualitiliwa na Maudhi.”

وَاللَّهُ غَنِيٌّ

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitosheleza.” Hahitaji msaada wa viumbe wake.

حَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

“Mpole.” Anayefanya huruma, Anaghufiria, Anasamehe na Anarehemu. Kuna Hadithi nyingi zinakataza kukumbushia watu Sadaka uliyotoa.

Kwa mfano, Muslim alinukuu kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«ثَلَاثَةٌ لَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ، وَلَا يُرَكِّبُهُمْ، وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ: الْمَنَانُ بِمَا أُعْطِيَ، وَالْمُسْبِلُ إِزَارَهُ، وَالْمُنْتَفِقُ بِلِعْتِنَةِ بِالْحَلْفِ الْكَاذِبِ»

“Watu watatu Allah Hatosema nao siku ya Kiyama wala Kuwatazama au Kuwatakasa, na watapata adhabu kali: mwenye kusumbulia watu anachotoa na anayeburuza kikoi chake, nguo zake chini ya tindi ya mguu, na anayekula yamini ya uongo ili auze bidhaa yake.”¹

¹ Muslim 1:102.

Hii ndiyo sababu Allah تعالى Akasema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُبْطِلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَى

“Enyi mlioamini! Msiharibu Sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi.”

Inaeleza kuwa malipo ya Sadaka yatafutwa endapo yatafuatiwa na masimbulizi na maudhi. Kwa hali hii, malipo ya kutoa Sadaka hayatoshelezi kufuta maudhi na masimbulizi. Kisha Allah تعالى Amesema,

كَالَّذِي يُنْفِقُ مَالَهُ رِثَاءَ النَّاسِ

“Kama anayetoa mali yake kwa kuwaonesha watu.”

Maana yake: “Msiharibu Sadaka zenu kwa kuzifuatishia masimbulizi na maudhi, kama wale wanaotoa Sadaka zao kwa kuwaonesha watu.” Watu wenye majivuno hujidai kutoa kwa ajili ya Allah تعالى, lakini kwa uhakika wanataka kusifiwa kuwa ni wema na wakarimu, au kupata manufaa mengine ya kidunia. Wakati huo, hafikirii juu ya Allah تعالى au kupata Ridhaa Yake na malipo mazuri, na kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema,

وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya Mwisho.”

Kisha Allah تعالى Ametoa mifano ya wale wanaotoa Sadaka kwa kujionesha. Adh-Dhahhak ameelezea kuwa mfano unamfaa yule anayefuatilia Sadaka yake kwa masimulizi au maudhi.¹ Allah تعالى Amesema,

فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ

“Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali.”

Neno *Swafwaan* lililotumika hapa ni wingi wa neno *Swafwaanah*. Wengine wamesema kuwa neno hilo, *Swafwaan* huleta neno *Aswafaa* katika umoja wake, na maana yake ni jabali (jiwe) linaloteleza sana.

¹ At-Tabari 5:527.

عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُ وَابِلٌ

“Ambalo juu yake kuna udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa.”

Maana yake: Mvua kubwa,

فَتَرَكَهُ صَلْدًا

“Ikaliacha tupu.”

Maana yake: Mvua kubwa iliacha Swafaa ikiwa kavu na laini bila mchanga. Halikadhalika matendo ya wale wanaojionesha yanaondoka na kupotea bila kumfikia Allah تعالی, Japokuwa watu watakaoziona watadhani kuwa amali hizi ni nyingi kama chembe za Mchanga. Allah تعالی Amesema,

لَا يَفْدُرُونَ عَلَى شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوا وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦٠﴾

“Basi hawatakuwa na uwezo wowote kwa walivyo vichuma. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.”

* * *

وَمَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ مَرْضَاتِ اللَّهِ
 وَتَثْبِيتًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ كَمَثَلِ جَنَّةٍ بِرَبْوَةٍ أَصَابَهَا وَابِلٌ فَتَاتَتْ
 أَكْلَهَا ضِعْفَيْنِ فَإِن لَّمْ يُصِبْهَا وَابِلٌ فَطَلَّ ۗ وَاللَّهُ بِمَا
 تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٦٥﴾ أَيُّودُ أَحَدَكُمُ أَن تَكُونَ لَهُ
 جَنَّةٌ مِّنْ نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ لَهُ
 فِيهَا مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَأَصَابَهُ الْكِبَرُ وَلَهُ ذُرِّيَةٌ ضُعْفَاءُ
 فَأَصَابَهَا إِعْصَارٌ فِيهِ نَارٌ فَاحْتَرَقَتْ ۗ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ
 لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٦٦﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا أَنْفِقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ
 مِنَ الْأَرْضِ ۗ وَلَا تَمَمُوا الْحَيْثُ مِنْهُ تُنْفِقُونَ وَلَسْتُمْ
 بِبَاحِدِيهِ إِلَّا أَنْ تَغْمِضُوا فِيهِ ۗ وَعَلِمُوا أَنَّ اللَّهَ عِنْدَ حَمِيدٍ
 ﴿٢٦٧﴾ الشَّيْطَانُ يَعِدُكُمُ الْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُمْ بِالْفَحْشَاءِ ۗ وَاللَّهُ
 يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦٨﴾ يُؤْتِي
 الْحِكْمَةَ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَمَنْ يُؤْتَ الْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ
 خَيْرًا كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٢٦٩﴾

وَمَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ
 مَرْضَاتِ اللَّهِ وَتَثْبِيتًا مِّنْ
 أَنفُسِهِمْ كَمَثَلِ جَنَّةٍ بِرَبْوَةٍ أَصَابَهَا
 وَابِلٌ فَتَاتَتْ أَكْلَهَا ضِعْفَيْنِ فَإِن
 لَّمْ يُصِبْهَا وَابِلٌ فَطَلَّ ۗ وَاللَّهُ بِمَا
 تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٦٥﴾

265. "Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na kuzipa nguvu roho zao ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta mazao yake maradufu; na hata kama haifikiwi na mvua kubwa basi manyunyuhutosha. Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayo-yatenda."

Huu ni mfano wa waumini wanaotoa Sadaka kwa kutaraji radhi za Allah تعالى,

وَتَثْبِيتًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ

"Na Kuzipa nguvu roho zao."

Maana yake: Wana uhakika kuwa Allah تعالى Atawalipa kwa uadilifu wao kwa malipo yaliyo mazuri kabisa. Vile vile, katika Hadithi iliyokusanywa na Al-Bukhari na Muslim, Mtume ﷺ alisema.

«مَنْ صَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا»

“Yeyote anayefunga Ramadhan kwa Imani na kwa Matarajio...”¹

Maana yake: Anaamini ya kuwa Allah تعالی Alifaradhisha funga na wafungaji wanatarajia malipo kutoka Kwake. Kauli ya Allah تعالی,

كَمَثَلِ جَنَّةٍ بِرَبْوَةٍ

“Ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu.”

Ina maana: Ya mfano wa bustani iliyo katika sehemu ya ardhi iliyo juu ya kilima, maana hiyo ni kulingana na mtazamo wa jopo la wanazuoni. Ibn Abbas na Adh-Dhahhak waliongeza kwamba pia ina mito itiririkayo.²

أَصَابَهَا وَايِلٌ

“Ikaifikia mvua kubwa.”

Maana yake: Mvua nyingi kama tulivyoeleza, Hivyo,

أَكَلَهَا

“Na ikaleta mazao.” Maana yake: Matunda au mazao yake,

ضَعْفَيْنِ

“Mara mbili.” Ikilinganishwa na bustani nyingine.

فَإِنْ لَّمْ يُصِبْتَهَا وَايِلٌ فَطَلٌّ

“Na hata kama haifikiwi na mvua kubwa basi manyunyu hutosha.”

Adh-Dhahhak alisema kuwa “*Tall*” ni mvua za rasharasha.¹ Ayah inaonesha kuwa bustani juu ya kilima *Rabwah*, wakati wote ina rutuba, kwani mvua kubwa isiponyesha, manyunyu yanatosha. Mfano huu ni kama amali njema za muumini kwani haziachi kuzaa. Bali Allah تعالی Hupokea amali njema za muumini na Huziongoza, kila mmoja kwa mujibu wa amali zake. Kwa sababu hii Kauli ya Allah تعالی inayofuatia ni.

¹ Fat’hul Al-Bari 4:300.

² At-Tabari 5:537.

³ At-Tabari 5:539.

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٦٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.”

Maana yake: Hapana amali ya Mja Wake iliyopita uoni Wake uliothibiti.

أَيُّودٌ أَحَدَكُمُ أَنْ تَكُونَ لَهُ جَنَّةٌ مِّن نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ لَهُ فِيهَا مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَأَصَابَهُ الْكِبَرُ وَلَهُ ذُرِّيَةٌ ضُعْفَاءُ فَأَصَابَهَا إِعْصَارٌ فِيهِ نَارٌ فَاحْتَرَقَتْ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٦٦﴾

266. “Je yupo mmoja wenu anayependa kuwa na kitalu cha mitende au mizabibu ipitayo mito kati yake, naye humo hupata mazao ya kila namna, na uzee ukamfikia naye hali ana watoto wanyonge, kikapigwa na kimbunga chenye moto, kikaungua? Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni Ishara ili mpate kufikiri.”

Mfano wa Amali Mbaya Zinavyoharibu Amali Njema

Bukhari alinukuu kutoka kwa Ibn Abass na Ubayd bin Umayr رضي الله عنهما walisema kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه aliwauliza Maswahaba wa Mtume ﷺ, “Kwa mujibu wa rai yenu, Aya hii iliteremshwa kwa sababu gani?”

أَيُّودٌ أَحَدَكُمُ أَنْ تَكُونَ لَهُ جَنَّةٌ مِّن نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ

“Je! yupo mmoja wenu anayependa kuwa na kitalu cha mtende na mizabibu...”

Wakasema, “Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.” Umar رضي الله عنه akakasirika na akawaambia, “semeni, ‘tunajua au hatujui.’” Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, “Ewe Amiri wa Waumini! Nina rai kuhusu hilo.” Umar رضي الله عنه akamuambia, “Ewe mtoto wa kaka yangu! Toa rai yako na usijidunisha.” Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, “Huu ni mfano uliopigiwa amali.” Umar رضي الله عنه akauliza, “Aina gani ya amali?” Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema: “Ni kwa tajiri anayefanya amali kwa ajili ya kupata Radhi za Allah تعالى, kisha Allah تعالى Akampa mtihani kwa kughilibiwa na Shetani, akawa anafanya maasi, mpaka maasi yake yakafuta amali zake njema.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 8:49.

Hadithi hii inatosha kuielezea Aya, kwa kuwa inaelezea mifano inayowekwa na mtu anayefanya amali njema mwanzo na kisha kufuatiwa na uovu, Allah تعالی Atuokoe na mwisho huu. Hivyo, mtu huyu alifuta amali zake njema zilizotangulia na akabakia na amali zake mbovu zilizofuatia. Alipozihitaji amali zilizopita huku akiwa amedhikika, hazikuwepo.

Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

وَأَصَابَهُ الْكِبَرُ وَلَهُ ذُرِّيَّةٌ ضُعَفَاءُ فَأَصَابَهَا إِعْصَارٌ

“Na uzee ukamfikia naye hali ana Watoto wanyonge, kikapigwa na kimbunga.”

Nao ni upepo mkali,

فِيهِ نَارٌ فَأَحْرَقَتْ

“Chenye moto, kikaungua?”

Maana yake: Matunda yake yaliungua na miti yake iliharibiwa. Kwa hiyo hali yake itakuwaje? Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالی alinukuu kuwa Al-Awfi alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالی Ametoa mfano mzuri, na mithali zake zote nzuri.” Amesema,

أَيُّودٌ أَحَدَكُمْ أَنْ تَكُونَ لَهُ جَنَّةٌ مِّنْ نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ لَهُ

فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ

“Je yupo mmoja wenu anayependa kuwa na kitalu cha mitende na mizabibu ipitayo mito kati yake, naye humo hupata mazao ya kila aina.”

Lakini aliyapoteza yote haya alipokuwa mzee,

وَأَصَابَهُ الْكِبَرُ

“Na uzee ukamfikia.”

Ambapo wajukuu na watoto wake wote wako dhaifu kabla ya kufikia mwisho wa maisha yake. Kisha kimbunga chenye radi kikaja na kuangamiza bustani yake. Kisha hakuwa na nguvu za kumsaidia kupanda bustani nyingine. Na kadhalika kizazi chake hakikuwa na nguvu cha kumsaidia yeye. Hii ndiyo hali ya siku ya Kafiri Kiyama atakaporejea kwa Allah تعالی, ambapo hatokuwa na

amali njema atajilaumu kama ilivyokuwa katika Mithali hii. Mtu hakuwa na nguvu ya kupanda tena bustani yake. Makafiri hawatopata pa kukimbilia kwa ajili ya msaada, kama alivyo mtu aliyeelezwa katika mithali hakupata msaada kutoka kwa kizazi chake. Hivyo atapokonywa malipo yake wakati anayahitajia sana, kama ilivyo mtu katika mithali alipopokonywa bustani na Allah تعالی alipokuwa anaihitaji sana alipokuwa mzee na wakati huo huo wanawe dhaifu.¹

Ndani ya Mustadrak wake, Al-Hakim amenukuu kwamba Mtume ﷺ alikuwa akiomba Dua,

«اللَّهُمَّ اجْعَلْ أَوْسَعَ رِزْقِكَ عَلَيَّ عِنْدَ كِبَرِ سِنِيَّ وَإِنْقِضَاءِ عُمْرِي»

*"Ewe Allah! Nijaalie riziki yenye wasaa zaidi nitakapokuwa na umri mkubwa na umri wangu utakapofika mwisho."*²

Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٦٥﴾

"Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni Ishara ili mpate kufikiri."

Maana yake: Kuifahamu na kuzingatia mithali na matokeo yaliyotarajiwa.

Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نُضْرِبُهَا لِلنَّاسِ ۗ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٢٦٦﴾

"Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu." (29:43)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفِقُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ ۗ وَلَا تَتَمَنَّوْا الْخَيْبَتِ مِنهُ تَنْفِقُونَ وَلَسْتُمْ بِأَخِيذِهِ إِلَّا أَن تُعْمَضُوا فِيهِ ۗ وَعَلِمُوا أَنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٢٦٧﴾ الشَّيْطَانُ يَعِدُكُمُ الْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُم بِالْفَحْشَاءِ ۗ وَاللَّهُ يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ

¹ Ibn Abu Hatim 3:1074.

² Al-Hakim 1:542.

وَفَضْلًا ۗ وَاللَّهُ وَسِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦٥﴾ يُؤْتِي الْحِكْمَةَ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَمَنْ يُؤْتَ الْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٢٦٦﴾

267. *“Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile Tulivyokutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea ila huku mkiwa mmevifumbia macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitoshia na msifiwa.”*

268. *“Shetani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu Anakuahidini Msamaha na fadhila zitokazo Kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa, Mwenye Kujua.”*

269. *“Yeye Humpa Hikima Amtakaye; na aliyepewa hikima bila shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili.”*

Kuhimizwa Kutoa Mali Halali kwa Ajili ya Allah تعالی:

Allah تعالی Anawaamrisha waja Wake waumini kutumia mali zao kwa ajili ya sadaka, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما alivyoeleza, fedha halali walizozichuma kutokana na matunda na mbogamboga alizowaoteshea katika ardhi. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالی Aliwafaradhishia kutoa katika mali halali na Akawakataza kutoa kutokana na mali ya haramu. Sababu Allah تعالی ni Msafi na Mzuri na Hupokea vile vilivyo safi na vizuri. Hii ndiyo sababu Allah تعالی Amesema,

وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنْفِقُونَ

“Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya.” Maana yake: Mali chafu,

وَلَسْتُمْ بِعَاجِزِيهِ

“Hali nyinyi wenyewe msingevipokea.” Maana yake: “Iwapo mngepewa msingepokea isipokuwa mngevipuuza. Kwa hakika, Allah تعالی ni tajiri sana kuliko nyie, basi msikitoe kwa Allah تعالی kile msichokipenda.” Ilisimuliwa kuwa,

وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنْفِقُونَ

“Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya.”

Maana yake: 'Msitoe kutokana na dhuluma na fedha haramu badala ya fedha halali na safi.' Ibn Jarir رضي الله عنه alinukuu kuwa Al-Bara bin Azib رضي الله عنه aliitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفُقُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنْفِقُونَ

“Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma na vile Tulivyokutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya.”

Iliteremshwa kuwahusu Ansar. Msimu wa kuvuna tende kila ulipowadia, Ansar walikusanya tende mbivu katika bustani zao na kuzitundika kwenye kamba iliyofungwa kati ya nguzo mbili ndani ya Msikiti wa Mtume ﷺ. Muhajiruna masikini walikula kutokana na tende hizo. Hata hivyo, baadhi ya Ansar waliweka tende duni kati ya tende mbivu zilizokomaa, walidhani kwamba iliruhusiwa kufanya hivyo, ndipo Allah تعالى Alipoteremsha Aya hii juu ya wale waliofanya hivyo،

وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنْفِقُونَ

“Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya.” Ali bin Abi Talha alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo juu ya Aya

وَلَسْتُمْ بِأَخَذِيهِ إِلَّا أَنْ تُغْمِضُوا فِيهِ

“Hali nyinyi wenyewe msingeipokea ila huku mkiwa mmeifumbia macho.”

Anasema, kama mmoja wenu angelikuwa na haki yenu, kisha kakuleteeni haki iliyo pungufu ya ile ya kwenu, msingeipokea kwa kuichukulia kwamba ni nzuri, bali mtaichukulia kwamba ina kasoro. Hii ndiyo sababu Allah تعالى Amesema،

إِلَّا أَنْ تُغْمِضُوا فِيهِ

“Ila huku mkiwa mmeifumbia macho.” Maana yake: “Vipi mnaona sawa kunipatia Mimi kitu ambacho nyinyi wenyewe hamkuridhika nacho, ilhali haki Yangu kutoka kwenu yatokana na vizuri na vyenye thamani?” Ibn Abu Hatim na Ibn Jarir رضي الله عنه waliinukuu Hadithi hii na Ibn Jarir رضي الله عنه aliongezea، “Na hii ndio maana ya Kauli ya Allah تعالى،

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ^ع

“Kabisa hamtamfikia Wema Mpaka Mtoe Katika Vile Mnavyovipenda. (4:92)”¹ Kisha Allah تعالى Akasema,

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٢٧﴾

“Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitoshia na Msifiwa.”

Maana yake: Japokuwa Allah تعالى Amewafaradhishia kutoa vilivyo safi katika mali zenu kama Sadaka. Yeye ni Mkwasi na Hahitaji Sadaka zenu, lakini kufanya hivyo, ni kupunguza tofauti iliyo kati ya tajiri na maskini. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَاؤَهَا وَلَكِنَّ بِنَايِهِ أَتَّقَوْنَ مِنْكُمْ^ع

“Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamungu wenu.” (22:37)

Allah تعالى ni Mkwasi na Hahitaji chochote kutoka kwa viumbe Wake, ambapo viumbe Wake wote wanamhitajia Yeye. Yeye ni Mwenye Ukunjufu wa Fadhila na hayana ukomo yaliyo Kwake. Kwa hiyo, yeyote anayetoa vizuri na safi kama sadaka, ifahamike kuwa Allah تعالى Ndiye Mkwasi zaidi, Rehema zake ni nyingi bila kiasi na Yeye ni Mkarimu zaidi, Mwenye Kurehemu, na Atamlipa kwa sadaka yake na kuizidisha mara nyingi. Hivyo nani atamkopesha Yule Ambaye si masikini au dhalimu, Yule Anayestahiki Shukrani zote kwa vitendo Vyake, kauli Zake, na Maamuzi Yake, Ambaye hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye, wala hapana Mola mwingine zaidi Yake.

Sheitani Huwatia Shaka, Wasiwasi na Khofu

Allah تعالى Amesema,

الشَّيْطَانُ يَعِدُكُمُ الْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُمْ بِالْفَحْشَاءِ^ط وَاللَّهُ يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا^ك وَاللَّهُ

وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾

¹ Ibn Abu hatim 3:1088, At-Tabari 5:565.

“Shetani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu Anakuahidini Msamaha na Fadhila zitokazo Kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa, Mwenye Kujua.” (2:268)

Ibn Hatim رضى الله عنه alinukuu kutoka kwa Abdullah bin Masud رضى الله تعالى alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِلشَّيْطَانِ لَمَّةً بِإِبْنِ آدَمَ، وَلِلْمَلِكِ لَمَّةً، فَأَمَّا لَمَّةُ الشَّيْطَانِ فإِبْعَادُ بِالشَّرِّ، وَتَكْذِيبُ بِالْحَقِّ، وَ أَمَّا لَمَّةُ الْمَلِكِ فإِبْعَادُ بِالْخَيْرِ، وَتَضْدِيقُ بِالْحَقِّ، فَمَنْ وَجَدَ ذَلِكَ فَلْيَعْلَمْ أَنَّهُ مِنَ اللَّهِ، فَلْيَحْمَدِ اللَّهَ، وَمَنْ وَجَدَ الْآخَرَ فَلْيَتَعَوَّذْ مِنَ الشَّيْطَانِ»

“Hakika Shetani humuathiri mwana wa Adamu, na Malaika pia humuathiri. Ama kuhusu athari za Shetani ni kumuahidi mambo ya shari na kukadhibisha haki. Ama athari za malaika ni ahadi ya mambo ya kheri na kuisadikisha. Yeyote anayeona haya ya mwisho ajue yanatoka kwa Allah na amshukuru Allah kwa hilo. Yeyote anayeona ya mwanzo basi, akimbilie kwa Allah kujilinda dhidi ya shetani.”

Kisha Mtume ﷺ alisema,

الشَّيْطَانُ يَعِدُكُمْ الْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُمْ بِالْفَحْشَاءِ ط وَاللَّهُ يَعِدُكُمْ مَغْفِرَةً مِنْهُ وَفَضْلًا

“Shetani anakutieni Khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu Anakuahidini Msamaha na Fadhila zitokanazo Kwake.”¹

Hii ni Hadithi ambayo At-Tirmidhi na An-Nasai waliikusanya katika Kitabu cha Tafsiri na katika Sunan zao.² Allah تعالى Amesema,

الشَّيْطَانُ يَعِدُكُمْ الْفَقْرَ

“Shetani anakutieni khofu ya ufakiri.”

Ili mzuie chochote mlichonacho kukitoa kwa kupata radhi za Allah تعالى.

¹ Ibn Abu Hatim 3:1090.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:332, An-Nasai Al-Kubra 6:305.

وَيَأْمُرُكُمْ بِالْفَحْشَاءِ ط

“Na anakuamrishi ni mambo machafu.”

Maana yake: Pamoja na Shetani kuwazuia kutoa sadaka kwa sababu ya woga usio na sababu wa kuwa masikini, anawashajiisha matendo maovu, makosa, kujiingiza katika mambo yaliyoharamishwa, maadili potofu. Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ يَعِدُكُمْ مَغْفِرَةً مِّنْهُ

“Na Mwenyezi Mungu Anakuahidini Msamaha.”

Maana yake: Katika kujiepusha na uovu anaokuamuruni Shetani.

وَفَضْلًا ط

“Na Fadhila.”

Maana yake: Katika kuukabili ufakiri anaokutishieni Shetani.

وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa, Mwenye Kujua.”

Maana ya Al-Hikmah:

Allah تعالى Amesema,

يُؤْتِي الْحِكْمَةَ مَن يَشَاءُ ج

“Yeye Humpa hikima Amtakaye”

Ali bin Abi Talhah aliripoti kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maana yake: Ni kujua Qur’an, Aya zenye kubadilisha na kubadilishwa (*Nasikh* na *Mansukh*), kilicho dhahiri na chenye mshabaha, cha halali na cha haramu na mifano yake.¹

“Imam Ahmad alinukuu kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 5:576.

«لَا حَسَدَ إِلَّا فِي اثْنَتَيْنِ: رَجُلٌ آتَاهُ اللَّهُ مَالًا فَسَلَّطَهُ عَلَىٰ هَلْكَتَيْهِ فِي الْحَقِّ، وَرَجُلٌ آتَاهُ اللَّهُ حِكْمَةً فَهُوَ يَقْضِي بِهَا وَيُعَلِّمُهَا»

“Hapana Hasad ila katika mambo mawili: mtu aliyeruzukiwa mali na Allah akaisaliti na kuiangamiza katika haki na mtu aliyepewa Hikma na Allah kwa hiyo anahukumu kwayo na anaifundisha.”¹

Al-Bukhari, Muslim, An-Nasai, Ibn Majah waliikusanya pia.²

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٢٦٥﴾

“Na hawakumbuki ila wenye akili.”

Maana yake: “Wale watakaofaidika na ushauri ni wale wenye akili timamu, na uweza wa kuzingatia unaowa wezesha kufahamu maneno ya ushauri na ukumbusho na matokeo yake.”

* * *

¹ Ahmad 1:432.

² Fath Al-Bari 1:199, Muslim 1:559, An-Nasai katika Al-Kubra 3:426, Ibn Majah 2:1407.

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُهُ ^ط وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنَ أَنْصَارٍ ﴿٢٧٠﴾ إِنَّ الصَّدَقَاتِ فَبِعَمَّا هِيَ ^ط وَإِنْ تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا الْفُقَرَاءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ^ع وَيُكَفِّرْ عَنْكُمْ مِّنْ سَيِّئَاتِكُمْ ^ط وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٧١﴾ * لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ ^ط وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَأَنْفُسِكُمْ ^ع وَمَا تُنْفِقُونَ إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ ^ع وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٢٧٢﴾ لِلْفُقَرَاءِ الَّذِينَ أُحْصِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ صَرْبًا فِي الْأَرْضِ يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ أَغْنِيَاءَ مِنَ التَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُمْ بِسِيمَاهُمْ لَا يَسْأَلُونَ النَّاسَ إِلْحَافًا ^ط وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢٧٣﴾ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٤﴾

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُهُ ^ط وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنَ أَنْصَارٍ ﴿٢٧٠﴾ إِنَّ الصَّدَقَاتِ فَبِعَمَّا هِيَ ^ط وَإِنْ تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا الْفُقَرَاءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ^ع وَيُكَفِّرْ عَنْكُمْ مِّنْ سَيِّئَاتِكُمْ ^ط وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٧١﴾

270. "Na chochote mnacho toa au nadhiri mnazoweka basi hakika Mwenyezi Mungu Anajua. Na walio-dhulumu hawana wa kuwanusuru."

271. "Mkidhirisha Sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu, na zitakuondoleeni baadhi ya

maovu yenu. Na Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda."

Allah تعالی Anaeleza kuwa Anazijua amali njema zilizofanywa na viumbe Wake, kama Sadaka na viapo mbalimbali, na Analipa sana kwa amali hizi, ilimradi zinafanywa kutarajia ahadi Yake na kuelekea Kwake.

Pia Allah تعالی Amewaonya wasiojishughulisha na utiifu Kwake, na badala yake wanavunja Amri Zake, wanakataa Ufunuo Wake na wanaabudu wengine wasiokuwa Yeye.

وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ ﴿٢٧٠﴾

“Na waliodhulumu hawana wa kuwanusuru.”

Maana yake: Nani atakayewaokoa kutokana na mateso ya Allah تعالی siku ya kiyama.

Fadhila za Kudhihirisha au Kuficha Sadaka:

Allah تعالی Amesema,

إِنْ تُبْدُوا الصَّدَقَاتِ فَنِعِمَّا هِيَ ۗ

“Mkizidhihirisha Sadaka ni vizuri.”

Maana yake: “Ni vizuri kama utaweka wazi Sadaka unayoitoa.” Kauli ya Allah تعالی

وَإِنْ تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا الْفُقَرَاءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ ۗ

“Na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu.”

Hii inadhihirisha kuwa kuficha Sadaka ni bora kuliko kinyume chake, kwa sababu inamlinda mtu kufanya ria na kujisifu. Hata hivyo, kama kuna sababu ya msingi ya kudhihirisha Sadaka, kama vile watu kuiga tendo hili adilifu, hivyo kudhihirisha kunakuwa bora kuliko kutoa kwa siri. Mtume ﷺ amesema,

«الْجَائِرُ بِالْقُرْآنِ كَالْجَاهِرِ بِالصَّدَقَةِ، وَالْمُسِرُّ بِالْقُرْآنِ كَالْمُسِرِّ بِالصَّدَقَةِ»

“Yeyote anayesoma Qur’an kwa sauti kubwa ni kama mwenye kudhihirisha Sadaka. Yeyote anayesoma Qur’an kisirisiri ni sawa na mwenye kutoa sadaka kwa siri.”¹

Aya inaonesha kuwa ni bora kutoa sadaka kwa siri, kama ilivyorejewejewewa na Hadithi ambayo ilinukuliwa katika sahih Mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema,

«سَبْعَةٌ يُظِلُّهُمُ اللَّهُ فِي ظِلِّهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ: إِمَامٌ عَادِلٌ، وَشَابٌّ نَشَأَ فِي عِبَادَةِ اللَّهِ، وَرَجُلَانِ تَحَابَّا فِي اللَّهِ، اجْتَمَعَا عَلَيْهِ وَتَفَرَّقَا عَلَيْهِ، وَرَجُلٌ قَلْبُهُ مُعَلَّقٌ

¹ Abu Dawud 2:83.

بِالْمَسْجِدِ، إِذَا خَرَجَ مِنْهُ حَتَّى يَرْجِعَ إِلَيْهِ، وَرَجُلٌ ذَكَرَ اللَّهَ خَالِيًا فَفَاضَتْ عَيْنَاهُ،
 وَرَجُلٌ دَعَتْهُ امْرَأَةٌ ذَاتُ مَنْصِبٍ وَجَمَالٍ، فَقَالَ: إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ،
 وَرَجُلٌ تَصَدَّقَ بِصَدَقَةٍ فَأَخْفَاهَا، حَتَّى لَا تَعْلَمَ شِمَالَهُ مَا تُنْفِقُ بيمينه،

*"Watu saba watafunikwa kivuli na Allah siku ambayo hapatakuwa na kivuli ila kivuli Chake. Hao ni; Kiongozi muadilifu, kijana aliyetua akimuabudu Allah. Watu wawili wanaopendana kwa ajili ya Allah, wanajumuika kwa ajili yake na kufarakana kwa ajili Yake. Mtu ambaye moyo wake umeshikamana na Masjid tangu wakati anapotoka Masjid mpaka anaporejea tena Masjid. Mtu anayemd hukuru Allah kwa kujiweka faragha na huku macho yake yanabubujika machozi. Mtu anayekataa wito wa mwanamke mwenye hadhi kuzini naye, na anamwambia, 'Namuogopa Allah, Bwana wa dunia na akhera.' Na mtu anayetoa Sadaka kwa siri kiasi cha mkono wa kushoto kutojua kinachotolewa na mkono wa kulia."*¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَيُكْفِرُ عَنْكُمْ مِّنْ سَيِّئَاتِكُمْ^٥

"(Allah) Atakuondoleeni baadhi ya maovu yenu." Maana yake: Kwa malipo ya kutoa Sadaka, hasa ingekuwa kwa siri. Kwa hiyo, mtalipwa mema kwa kupandishwa daraja, na madhambi yenu yatasamehewa. Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٦﴾

"Na Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda."

Maana yake: "Hapana amali njema muifanyayo Asiyofahamu, na Atawalipa kwayo."

* لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ^٥ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ
 فَلِأَنْفُسِكُمْ^٦ وَمَا تُنْفِقُوا إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ^٦ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُؤَفَّ إِلَيْكُمْ
 وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٦﴾ لِلْفُقَرَاءِ الَّذِينَ أَحْصَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَطِيعُونَ

¹ Fat'hul Al-Bari 3:344, Muslim2:715.

صَرَبًا فِي الْأَرْضِ مَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ أَغْيَاءَ مِنَ التَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُمْ بِسِيمَاهُمْ لَا
يَسْأَلُونَ النَّاسَ إِحْفَافًا ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢٧٢﴾ الَّذِينَ
يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٣﴾

272. "Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye. Na kheri yoyote mnayotoa ni kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta wajihi wa Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakayotoa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa."

273. "Uwapatie mafakiri waliozuilika kwa njia za Mwenyezi Mungu, wasioweza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiyewajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa kujizua kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang'ang'anii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayotoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu Anajua,"

274. "Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika."

Kuwapa Sadaka Washirikina

Abu Abdul-Rahman An-Nasai رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas alisema kuwa, "Walichukia kuwapa sadaka jamaa zao walio washirikina, lakini baadae waliruhusiwa kuwapa walipoulizia suala hili, na Aya hii iliteremshwa,

* لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ
فَلَا نُنْفِسُكُمْ ۗ وَمَا تُنْفِقُونَ إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ
وَأَنْتُمْ لَا تَظْلَمُونَ ﴿٢٧٤﴾

"Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humwongoa amtakaye. Na kheri yoyote mnayotoa ni kwa nafsi

zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta wajahi wa Mwenyezi Mungu. Na kheri yoyote mtakayotoa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa.” (2:272)¹

Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَا نُنْفِسِكُمْ

“Na kheri yoyote mnayotoa ni kwa nafsi zenu.”

Ni sawa na Kauli Yake nyengine,

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ

“Yeyote anayefanya amali njema ni kwa manufaa yake binafsi.” (41:46)

Kuna Aya nyingi ndani ya Qur’an sawa na hizo.

Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

وَمَا تُنْفِقُونَ إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ

“Wala msitoe ila kwa kutafuta wajahi wa Mwenyezi Mungu.”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالیٰ alitoa maelezo, “Matumizi ya Muumini ni kwa manufaa yake, na wala hatumii bali ni kwa ajili ya kutafuta wajahi wa Allah تعالیٰ.”² Ata Al-Khurasani alisema kuwa Ayah hii ina maana kuwa unatoa sadaka kwa ajili ya Allah تعالیٰ, kwa hiyo hutoulizwa kuhusu amali za wale waliopokea.”³ Hii ina maana inayoingia akilini - inaonesha kuwa, mmoja anapotoa Sadaka kwa ajili ya kupata radhi za Allah تعالیٰ, hivyo malipo yake yatatoka kwa Allah تعالیٰ. Hatoulizwa kama Sadaka ilimfikia mtu mwadilifu, mwovu, anayestahili au asiyestahiki, kwani atalipwa kwa nia yake njema. Ushahidi wa kauli hii ni Aya,

وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُؤَفِّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ

“Na kheri yoyote mtakayotoa mtalipwa kwa ukamilifu, wala hamtadhulumiwa.”

Sahih Mbili zilinukuu Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه Kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:305.

² Ibn Abu Hatim 3:1115.

³ Ibn abu Hatim 3:1115.

«قَالَ رَجُلٌ: لَأَتَصَدَّقَنَّ اللَّيْلَةَ بِصَدَقَتِهِ، فَخَرَجَ بِصَدَقَتِهِ فَوَضَعَهَا فِي يَدِ زَانِيَةٍ، فَأُضْبِحَ النَّاسُ يَتَحَدَّثُونَ: تُصَدِّقُ عَلَى زَانِيَةٍ، فَقَالَ: اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ عَلَى زَانِيَةٍ، لَأَتَصَدَّقَنَّ اللَّيْلَةَ بِصَدَقَتِهِ، فَخَرَجَ بِصَدَقَتِهِ فَوَضَعَهَا فِي يَدِ غَنِيِّ، فَأُضْبِحُوا يَتَحَدَّثُونَ: تُصَدِّقُ اللَّيْلَةَ عَلَى غَنِيِّ، قَالَ: اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ عَلَى غَنِيِّ، لَأَتَصَدَّقَنَّ اللَّيْلَةَ بِصَدَقَتِهِ، فَخَرَجَ بِصَدَقَتِهِ فَوَضَعَهَا فِي يَدِ سَارِقٍ، فَأُضْبِحُوا يَتَحَدَّثُونَ: تُصَدِّقُ اللَّيْلَةَ عَلَى سَارِقٍ، فَقَالَ: اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ عَلَى زَانِيَةٍ، وَعَلَى غَنِيِّ، وَعَلَى سَارِقٍ. فَأَتَيْتُ فَيَلَّ لَهُ: أَمَا صَدَقَتُكَ فَقَدْ قُبِلَتْ، وَأَمَا الزَّانِيَةُ فَلَعَلَّهَا أَنْ تَسْتَعِفَّ بِهَا عَنْ زَانَاهَا، وَلَعَلَّ الْغَنِيَّ يَتَعَبَّرُ فَيَنْفِقُ بِمَا أُعْطَاهُ اللَّهُ، وَلَعَلَّ السَّارِقَ أَنْ يَسْتَعِفَّ بِهَا عَنْ سَرِقَتِهِ»

"Mtu alisema, "Nitatoa Sadaka usiku." Alitoka na sadaka yake na akampa mzinzi mwanamke (bila kujua). Asubuhi watu wakawa wanasema kuwa mzinzi amepewa Sadaka. Yule mtu akasema, "Ewe Allah! Shukrani zote Unastahiki Wewe. Nilimpa Sadaka yangu mzinzi mwanamke. Leo usiku, nitatoa Sadaka tena." Alitoka na Sadaka yake na bila kujua alimpa tajir. Asubuhi iliyofuata (watu) walisema, "Usiku uliyopita tajiri alipewa Sadaka." Alisema, "Ewe Allah! Shukrani zote zinakustahiki Wewe. (Nilimpa Sadaka) tajiri. Usiku nitatoa tena Sadaka." Hivyo alitoka na sadaka yake (na bila kujua) alimpa mwizi. Siku ya pili yake (watu) walisema, "Usiku uliopita mwizi alipewa sadaka." Alisema, "Ewe Allah! Shukrani zote unastahiki Wewe (Nimempa sadaka) mzinzi mwanamke, tajiri na mwizi." Kisha, alimjia mtu na kumwambia, "Sadaka ulizotoa zimekubaliwa. Ama kuhusu mwanamke mzinzi, Sadaka inaweza kumfanya kuacha uzinzi. Ama kuhusu tajiri, itamfanya kujifunza na kumfanya kutumia utajiri wake aliopewa na Allah. Ama kwa mwizi, inaweza kumfanya kuacha wizi."¹

Wanaostahiki Zaidi Kupatiwa Sadaka:

Allah تعالى Amesema,

لِلْفُقَرَاءِ الَّذِينَ أَحْصَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ

"Na wapewe mafakiri waliozuilika katika njia za Mwenyezi Mungu."

¹ Fat'hul Al-Bari 3:340, Muslim 2:709.

Maana yake: Muhajirina waliohajiri kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ, walifanya makazi Al-Madinah na hawakuwa na rasilimali zilizokidhi haja zao,

لَا يَسْتَطِيعُونَ ضَرْبًا فِي الْأَرْضِ

“Wasioweza kusafiri katika nchi kutafuta riziki.”

Maana yake: Hawawezi kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Na neno *Dhwarban fil-ardh* kama lilivyotumika katika Aya linamaanisha safari. Kwa mfano, katika mifano ya neno hilo, Allah تعالى Amesema,

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ

“Na mnaposafiri (Waidhaa dhwarabtum) katika nchi si vibaya kwenu kama mkifupisha Sala.” (4:101) Na,

عَلِمَ أَنْ سَيَكُونُ مِنْكُمْ مَّرْضَىٰ ۖ وَءَاخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِنْ فَضْلِ اللَّهِ ۖ
وَءَاخَرُونَ يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ

“Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa na wengine wanasafiri katika ardhi (yadhribuna fil-ardh) wakitafuta Fadhila ya Mwenyezi Mungu na wengine wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu... (73:20). Kisha Allah تعالى Amesema,

نَحْسِبُهُمُ الْجَاهِلُ أَعْيَاءَ مِنْ بِنْتِ الْعَرْفِ

“Asiyewajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao.”

Maana yake: Wale wasiojua hali zao wanadhani kuwa ni matajiri, kwa sababu ya staha katika mavazi na mazungumzo yao. Kuna Hadithi yenye maana hii ambayo ilinukuliwa katika Sahih mbili kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَيْسَ الْمِسْكِينُ بِهَذَا الطَّوَابِ الَّذِي تَرُدُّهُ الثَّمَرَةُ وَالْتَمَرَانِ، وَاللَّقَمَةُ وَاللَّقَمَانِ،
وَالْأَكْلَةُ وَالْأَكْلَتَانِ، وَلَكِنَّ الْمِسْكِينُ الَّذِي لَا يَجِدُ غِنًى يَغْنِيهِ، وَلَا يَفْطَنُ لَهُ فَيَصْدَقَ
عَلَيْهِ، وَلَا يَسْأَلُ النَّاسَ شَيْئًا»

“Masikini si yule anayezurura na mahitajio yake yanatosha kwa kupewa tende moja au mbili, au kupata tonge moja au mbili, au

kupata mlo mmoja au miwili. Bali, Masikini ni yule asiye na kitu cha kumuwezesha kuishi, wakati huo huo watu hawana khabari juu ya mahitaji yake hivyo hawamsaidii, na wala yeye hawaombi watu msaada.”¹

Imam Ahmad pia alinukuu Hadith hii kutoka kwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه.²

Kauli ya Allah تعالى،

تَعْرِفُهُمْ بِسِيمَاهُمْ

“Utawajua kwa alama zao.” Maana yake: Kutokana na muonekano wao, hali yao haijifichi kwa watu wenye utambuzi mpevu. Kama Allah تعالى Alivyosema،

سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ

“Alama zao ni katika nyuso zao.” (48:29). Na،

وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ^ع

“Lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao.” (47:30)

Kauli ya Allah تعالى،

لَا يَسْأَلُونَ النَّاسَ إِلْحَافًا*

“Hawang’ang’anii watu kwa kuwaomba.” Maana yake: Hawaombi na hivyo, hawawahitaji, watu wawape zaidi ya mahitajio yao halisi. Bila shaka, wale wanaoomba msaada kutoka kwa watu wengine, na huku wana uwezo wa kujikimu, hao ni ombaomba. Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Said رضي الله عنه alisema, “Mama yangu alinituma kwa Mtume ﷺ kuomba msaada, lakini nilipofika nilikaa kitako. Mtume ﷺ aliniangalia na kuniambia،

مَنْ اسْتَعْنَىٰ أَغْنَاهُ اللَّهُ، وَمَنْ اسْتَعْفَىٰ أَعْفَاهُ اللَّهُ، وَمَنْ اسْتَكْفَىٰ كَفَّاهُ اللَّهُ، وَمَنْ سَأَلَ
وَلَهُ يَمَّةٌ أَوْقِيَّةٌ فَقَدْ أَلْحَفَ»

“Yeyote anayeridhika, Allah Atamtajirisha. Yule anayejistahi, Allah Atamfanya aheshimike. Anayewaomba watu, ambapo ana kiasi cha waqia (kidogo), basi atakuwa ombaomba mbobezi.”

Abu Said رضي الله عنه alisema, nikajisemea, “Ngamia wangu, Al-Yaqutah, ni mbora

¹ Fat’hul Al-Bari 3:399.

² Ahmad 1:384.

kuliko wakia moja (Sarafu ya fedha iliyokuwa na thamani ndogo). Na nikarejea bila kumwomba Mtume ﷺ chochote.”¹ Maneno ya Hadithi hii ni sawa na ile iliyokusanywa na Abu Dawud na An-Nasai.² Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ فإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢٧٤﴾

“Na kheri yeyote mnayoitoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu Anajua!”

Inaonesha kuwa hapana Sadaka Asiyofahamu, na Atalipa kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, wakati itakapokuwa inahitajika sana.

Kuwasifu Wenye kutoa Sadaka:

Allah تعالى Amesema,

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٤﴾

“Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na kwa dhahiri, wana ujira wao kwa mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika. (2:274)

Hivi ndivyo Allah تعالى Anavyowasifu wanaotoa katika Njia Yake na katika kutafuta radhi Zake mchana na usiku, kwa uwazi na kwa siri, ikiwa ni pamoja na kile anachokitumia kwa ajili ya familia yake. Sahih Mbili zimenukuu Mtume ﷺ alimwambia Sa'd bin Abu Waqqas رضي الله عنه wakati alipomzuru mgonjwa na katika mapokezi mengine yanasema kuwa, ni katika Hijjah ya kuaga:

«وإِنَّكَ لَنْ تَنْفِقَ نَفَقَةً تَبْتَغِي بِهَا وَجْهَ اللَّهِ إِلَّا أزدَدَتْ بِهَا دَرَجَةً وَرِفْعَةً، حَتَّى مَا تَجْعَلُ فِي فِي امْرَأَتِكَ»

“Hakika wewe hutatoa Sadaka ukitarajia wajahi wa Allah, ila utapanda daraja na utukufu, hata kile unachokitia kwenye kinywa cha mkeo.”³

¹ Ahmad 3:9.

² Abu Dawud 2:279, An-Nasai 5:98.

³ Fat'hul Al-Bari 3:196, Muslim 4:1250.

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Masud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الْمُسْلِمَ إِذَا أَنْفَقَ عَلَىٰ أَهْلِهِ نَفَقَةً يَحْتَسِبُهَا، كَانَتْ لَهُ صَدَقَةً»

“Muislam anapotoa matumizi kwa familia yake na huku akisubiri malipo ya Allah, itaandikwa kama Sadaka yake.”¹

Al-Bukhari na Muslim pia walinukuu Hadith hii,²

Allah تعالى Amesema,

فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi.”

Maana yake: Siku ya Kiyama, kama malipo kwa vile walivyotoa na kuhesabiwa katika vitendo vya utiifu. Tuliielezea Aya hii kabla,

فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

“Wala haitakuwa khofu juu yao, na wala hawatahuzunika.”
(2:38)

Aya hii tumeshaijeleza tafsiri yake huko nyuma.

* * *

¹ Ahmad 4:122.

² Bukhari: 55, Muslim: 1002.

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ
الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا
إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا ۗ وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا ۗ
فَمَنْ جَاءَهُ مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّهِ فَاتْتَهَىٰ فَلَهُ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُ
إِلَى اللَّهِ ۗ وَمَنْ عَادَ فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
خَالِدُونَ ﴿٢٧٥﴾ يَمْحَقُ اللَّهُ الرِّبَا وَيُرْبِي الصَّدَقَاتِ ۗ
وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ﴿٢٧٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا
وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ لَهُمْ
أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ
﴿٢٧٧﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ
الرِّبَا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٧٨﴾ فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا
بِحَرْبٍ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَإِن تُبْتِغُوا فَكَيْفَ تُرِيدُونَ
أَمْوَالِكُمْ لَا تَظْلِمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ ﴿٢٧٩﴾ وَإِن
كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ ۗ وَأَن تَصَدَّقُوا خَيْرٌ
لَّكُمْ ۗ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾ وَاتَّقُوا يَوْمًا
تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ
وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨١﴾

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ
إِلَّا كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ
الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا ۗ وَأَحَلَّ
اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا ۗ فَمَنْ جَاءَهُ
مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّهِ فَاتْتَهَىٰ فَلَهُ مَا
سَلَفَ وَأَمْرُهُ إِلَى اللَّهِ ۗ وَمَنْ عَادَ
فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
خَالِدُونَ ﴿٢٧٥﴾

275. "Wale walao riba hawasimami ila kama anavyosimama aliyezugwa na Shetani kwa kumgusa. Hayo ni kwa kuwa wame-sema: Biashara ni kama riba. Lakini Mwenyezi Mungu Ameihalalisha biashara na Ameiharamisha riba. Basi aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akajizuia, basi yake ni yaliyokwishapita, na mambo yake yako kwa

Mwenyezi Mungu. Na mwenye kurudia basi hao ndio watu wa motoni, humo watadumu."

Ubaya wa Kula Riba:

Baada ya Allah ﷻ Kuwataja waumini wema, wanaotekeleza vyema matumizi yao na wanatoa Zaka na wanapata fadhila kwa kufanya wema, kutoa Sadaka kuwapatia wenye haja na ndugu katika hali zote na nyakati mbalimbali na hali, Ameingia katika kuwataja wanaojishughulisha na riba na kuchukua fedha za watu kwa njia batili na namna mbalimbali zenye utata. Allah ﷻ Ameelezea hali za watu hao watakapofufuliwa kutoka kwenye makaburi yao na kurejeshewa uhai siku ya Ufufuo. Allah ﷻ Akasema,

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ

“Wale walao riba hawasimami ila kama anavyosimama aliyezugwa na Shetani kwa kumgusa.”

Aya hii ina maana: Siku ya Kiyama, watu hao watatoka kwenye makaburi yao kama mtu aliyepata wazimu na kupagawa. Maana yake: Watafufuliwa wakiwa na hali mbaya. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Siku ya Ufufuo, mla riba atafufuliwa Siku ya Kiyama akiwa na wazimu na huku ana kifafa.”¹ Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu Hadith hii na kisha akatoa maelezo.

Pia masimulizi hayo yalipokewa kutoka kwa Awf bin Malik, Said bin Jubayr, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas, Qatadah na Muqatil bin Hayyan. Bukhari alinukuu kutoka kwa Samurah bin Jundub رضي الله عنه alisema katika Hadith ndefu kuhusu ndoto ya Mtume ﷺ, Msimulizi alisema,

«فَأْتَيْنَا عَلَى نَهْرٍ - حَبِيبْتُ أَنَّهُ كَانَ يَقُولُ-: أَحْمَرَ مِثْلَ الدَّمِ، وَإِذَا فِي النَّهْرِ رَجُلٌ سَابِحٌ يَسْبُحُ، وَإِذَا عَلَى شَطِّ النَّهْرِ رَجُلٌ قَدْ جَمَعَ عِنْدَهُ حِجَارَةً كَثِيرَةً، وَإِذَا ذَلِكَ السَّابِحُ يَسْبُحُ مَا يَسْبُحُ، ثُمَّ يَأْتِي ذَلِكَ الَّذِي قَدْ جَمَعَ الْحِجَارَةَ عِنْدَهُ، فَيَقْرَأُ لَهُ فَأَهُ فَيُلْقِيهِ حَجْرًا»

“Tukafika kwenye mto, nilidhani alisema: Mto ulikuwa mwekundu kama damu, na tukamwona mtu akiogelea mtoni, na kwenye kingo zake alikuwepo mtu mwingine akikusanya mawe mengi. Ghafila Mtu ndani ya mto aliyekuwa akiogolea akaja kwa mtu aliyekusanya mawe na kuyasokomeza kinywani mwake, na mkusanya mawe akamtupia mawe kinywani mwake.” Tafsiri yake ni kwamba huyo ni mla riba.¹

¹ Fat’hul Al-Bari 3:295.

Kauli ya Allah تعالى،

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا

“...Hayo ni kwa kuwa wamesema: Biashara ni kama riba lakini Mwenyezi Mungu Ameihalalisha biashara na Ameiharamisha riba...”

Inaonesha kuwa makafiri walidai kuwa riba iliruhusiwa kutokana na ukweli kuwa walikanusha maamrisha ya Allah تعالى، na siyo kuwa walilinganisha riba na biashara ya kawaida. Makafiri hawakujua kuwa Allah تعالى Alihalalisha biashara ndani ya Qur'an, na kama wangejua wangesema, “riba ni biashara.” Bali walisema،

إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا

“Biashara ni kama riba.”

Maana yake: Ni sawasawa, hivyo kwa nini Allah تعالى Alihalalisha hili lakini Hakuhalalisha lile, waliuliza kwa kukengeuka maamrisha ya Allah تعالى maana hili ni mithili ya hili, Akahalalisha hili na Akaharamisha hili. Allah تعالى Anasema،

وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا

“Mwenyezi Mungu Ameihalalisha biashara na Ameiharamisha riba.”

Inawezekana ikawa ni ukamilisho wa jibu kwa madai ya makafiri, waliolitamka, japokuwa walijua kuwa Allah تعالى Aliamua hukumu juu ya biashara iwe tofauti na ile ya riba. Kwa hakika, Allah تعالى ni Mjuzi zaidi, Mwenye Hikima, Ambaye Maamuzi Yake Hayapingwi. Allah تعالى Haulizwi kwa Ayafanyayo, ambapo wao wataulizwa. Yeye Anajua ukweli wa kila kitu na faida zake. Anajua kinachomfaidia mja Wake, hivyo hukiruhusu, na kinachowadhuru, Anawakanya nacho. Mwenye Kuwahurumia kuliko mama afanyavyo kwa mtoto wake mchanga. Baada ya hapo Allah تعالى Amesema،

فَمَنْ جَاءَهُدْ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّهِ فَاتَّبَعَهَا فَلَهُدْ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُ إِلَى اللَّهِ

“Basi aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akajizuia, basi yake ni yaliyokwishapita na mambo yake yako kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wale wenye kujua kuwa Allah تعالى Aliharamisha riba, na waliacha kujiingiza mara tu baada ya kufahamu, kisha Allah تعالى Atawasamehe makosa yao yaliyotangulia na kujishughulisha kwao na riba. Pale aliposema,

﴿عَمَّا أَثَمَّ عَنْمَا سَلَّتْ﴾

“Allah Amemsamehe yaliyopita.”

Siku ya *Fat-hu Makkah*, Mtume ﷺ alisema,

«وَكُلُّ رِبَا فِي الْجَاهِلِيَّةِ مَوْضُوعٌ تَحْتَ قَدَمَيْ هَاتَيْنِ، وَأَوَّلُ رِبَا أُضْعُ، رِبَا الْعَبَّاسِ»

“Riba zote za Jahiliyyah zimefutwa na ziko chini ya nyayo zangu hizi mbili. Na ya mwanzo niyoifuta ni riba ya Al-Abbas (ami yake Mtume).”¹

Wala hakuwaamuru warejeshe ziada waliyoipata kwenye riba zao enzi za Jahiliyyah. Bali, alizisamehe zote zilizokwishapita.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

فَلَهُ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُ إِلَى اللَّهِ ط

“Basi yake ni yaliyokwishapita, na mambo yako kwa Mwenyezi Mungu.”

Said bin Jubayr na As-Suddi walisema kuwa,

فَلَهُ مَا سَلَفَ

“Basi yake ni yaliyokwishapita.”

Inahusu riba iliyoliwa kabla ya kuharamishwa.² Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمَنْ عَادَ

“Na wenye kurudia.”

Maana yake: Miamala ya riba baada ya kufahamu kuwa Allah تعالى Aliharamisha wanastahili adhabu, na katika hali, ushahidi utakuwa umepatikana dhidi ya mtu huyo. Ndio sababu Allah تعالى Amesema,

¹ Abu Dawud 3:628.

² Ibn Abu Hatim 3:1135.

فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٧٥﴾

“Basi hao ndio watu wa Motoni, humo watadumu.”

Abu Dawud alinukuu kuwa Jabir رضي الله عنه alisema, wakati ilipoteremshwa Aya hii

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ۗ

“Wale walao riba hawasimami ila kama anavyosimama aliyezugwa na Shetani kwa kumgusa.”

Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ لَمْ يَذْرِ الْمَخَابِرَةَ فَلْيُؤْذِنْ بِحَرْبٍ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ»

“Yeyote asiyejizua kufanya Mukhabarah (kukodisha shamba kwa malipo ya kugawana sehemu ya mazao) basi apokee tangazo la vita kutoka kwa Allah na Mjumbe wake.”¹

Al-Hakim pia alinukuu katika Mustadrak wake,² na akasema, “Ni sahih kwa mujibu wa kigezo cha Muslim na hakuinukuu.” *Mukhabarah*, kulima shamba kwa malipo ya sehemu ya mazao; halikadhalika, *Muzabanah* ambako ni kuuza tende zikiwa mtini kwa tende kavu zilizovunwa. *Muhaqalah*, kuuza nafaka zilizo bado katika mashuke yake kwa zilizopukuchuliwa. Yote haya na yanayofanana nayo yameharamishwa ili kuondosha uwezekano wa kuwepo riba. Kwa kuwa ubora na usawa wa mazao hayo hufahamika baada ya kukauka ama kabla ya hapo inakuwa vigumu. Suala la riba ni gumu sana kwa wanazuoni wengi. Inatosha kutaja hapa kuwa kiongozi wa waumini, Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, alisema, “Natamani kuwa Mtume ﷺ angeyaweka mambo matatu wazi kwetu, ili tuweze kurejea katika maamuzi yake.

Kwanza: Babu mzaa baba na sio babu mzaa mama (Ni kuhusiana na shauri la mirathi pamoja na ndugu wa marehemu) Je, anakuwa kama baba anawazuia ndugu kurithi, au anashirikiana nao pamoja? Masiala haya Abubakar na Umar رضي الله عنهما wamehitalifiana ndani yake. Pili: *Kalalah* (wale ambao hawakuacha wazazi au watoto wa kuwarithi).

¹ Abu Dawud 3:695.

² Al-Hakim 2:285. Sanadi yake ni dhaifu.

Tatu: Ni aina za riba (Riba hapa ni ya "al-Fadhli" sio ya "an-Nnasia" kwani hiyo ipo wazi)"¹ Maana yake: Akikusudia masuala yenye kuhisiwa kuwa na riba. Shariah inaunga mkono hukumu kwamba njia zinazosababisha jambo la haram nazo ni haramu. Linaloelekezea kwenye haramu ni haramu kwa sababu ikiwa jambo la wajibu halitimii isipokuwa kwa kuwepo kitu au jambo jingine, kwa hiyo jambo hilo nalo ni wajibu. Sahih Mbili zilinukuu kuwa An-Nu'man bin Bashir رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ الْخَلَائِلَ بَيْنَ وَإِنَّ الْحَرَامَ بَيْنَ، وَبَيْنَ ذَلِكَ أُمُورٌ مُسْتَبْهَاتٌ، فَمَنْ اتَّقَى الشُّبُهَاتِ
اشْتَبَرًا لِدِينِهِ وَعِرْضِهِ، وَمَنْ وَقَعَ فِي الشُّبُهَاتِ وَقَعَ فِي الْحَرَامِ، كَالرَّاعِي يَرْعَى حَوْلَ
الْجَمَى يُوشِكُ أَنْ يَرْتَعَ فِيهِ»

*"Hakika halali iko wazi na haramu iko wazi, lakini kati yake kuna mambo yenye utata. Hivyo yeyote anayejiipusha na mambo ya utata, anahifadhi Dini yake na heshima yake. Na yeyote anayejiingiza katika mambo ya utata, atakuwa ameingia katika haramu, ni sawa na mchungaji anayelisha pembeni ya mpaka, inahofiwa wakati wowote anaweza lisha ndani yake."*²

Sunan imenukuu kuwa Al-Hasan bin Ali رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«دَعُ مَا يَرِيكَ إِلَى مَا لَا يَرِيكَ»

*'Liache ulilo na mashaka nalo na ufanye usilo na mashaka nalo.'*³

Ahmad alinukuu kuwa Said bin Al-Mussayib alisema kuwa Umar رضي الله عنه alisema, "Aya inayohusu riba ni moja ya Aya za mwisho kuteremshwa, na Mtume ﷺ alifariki dunia kabla ya kutufafanulia Aya hizo. Hivyo acheni riba pamoja na lenye mashaka."⁴

Ibn Majah alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Fat'hul Al-Bari 10:48, Muslim 4:2322.

² Fat'hul Al-Bari 1:153, Muslim 1:1219.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:221, An-Nasai 8:328.

⁴ Ahmad 1:36, Ibn Majah Na.2276.

«الرِّبَا سَبْعُونَ حُوبًا، أَيْسَرُهَا أَنْ يَبْخَعَ الرَّجُلُ أُمَّهُ»

“Riba ina aina sabini, na ndogo kuliko yote ni sawa na mtu kumuoa mama yake.”¹

Tukiendelea na jambo hili, ambalo ni kuelekeza njia zilizoelekeza katika yaliyoharamishwa, kuna Hadithi ambayo ilinukuliwa na Ahmad kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Aya katika surat *Al-Baqarah* zilipotemshwa juu ya riba, Mtume ﷺ alitoka kwenda Masjid na akawasomea na pia akaharamisha kufanya biashara ya pombe.”²

Vitabu sita vya Hadithi vimeandika Hadithi hii isipokuwa At-Tirmidhi.³ Sahihi Mbili ziliandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَعَنَ اللَّهُ الْيَهُودَ، حُرِّمَتْ عَلَيْهِمُ الشُّحُومُ فَجَمَلُوهَا فَبَاعُوهَا، وَأَكَلُوا أَثْمَانَهَا»

“Mwenyezi Mungu Awalaani Mayahudi! Allah Aliwaharamishia kula shahamu (mafuta ya wanyama), lakini waliyayeyusha na kuyauza, na kula thamani yake.”⁴

Ali na Ibn Mas’ud رضي الله عنهما na wengineo walisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema wakati alipomlaani “*Almuhallil*” Mtu anayemkuwadia mtu mwengine kumuhalalishia ndoa yake kwa mara nyingine baada ya kutoa Talaka tatu.

Katika Tafsiri ya Kauli yake Allah تعالى:

«لَعَنَ اللَّهُ آكِلَ الرِّبَا وَمُوكِلَهُ وَشَاهِدِيهِ وَكَاتِبَهُ»

“Mwenyezi Mungu Amemlaani mla riba, anayetoa riba, mashahidi wawili na anayeandika.”⁵

¹ Ibn Majah 3:764. Vivyo hivyo alinukuu Al-Hakim 2:37, na akasema, “ni sahih kwa mujibu wa vigezo vya mashekhe wawili, lakini hawakuinukuu.”

² Ahmad 6:46.

³ Fat’hul Al-Bari 8:51, Muslim 3:1206, Abu Dawud 3:759, An-Nasai katika Al-Kubra 6:306, Ibn Majah 2:1122.

⁴ Fat’hul Al-Bari 6:572, Muslim 3:1207.

⁵ Muslim 3:1219.

Wanasema kuwa wanapaswa tu wawepo mashahidi na mwandishi wa kuandika mkataba wa Riba pindi wanapoutaka katika mkataba wa halali bado haitafaa kwa sababu hukumu inatumika katika makubaliano yenyewe, si katika namna unavyojitokeza. Hakika amali hupimwa kulingana na nia.

يَمَحَقُ اللَّهُ الرِّبَا وَيُرِيى الصَّدَقَتِ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ﴿٢٧٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ
ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا
خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٦﴾

276. "Mwenyezi Mungu Huiondolea Baraka riba, na Huzibariki Sadaka. Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila kafiri (na) afanyae dhambi."

277. "Hakika wale walioamini na wakatenda mema na wakashika Swala na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika."

Allah تعالی Haibariki Riba.

Allah تعالی Ameeleza kuwa Anaiangamiza riba, ama kwa Kuiondoa kutoka mikononi mwa wanaoila, au Kutoibariki, na hivyo kutopata manufaa yake. Allah تعالی Atawaadhibu katika maisha ya dunia na Atawatesa siku ya Kiyama. Allah تعالی Amesema,

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ ۗ

"Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza wingi wa viovu." (5:100)

وَيَجْعَلُ الْخَبِيثَ بَعْضُهُ عَلَىٰ بَعْضٍ فَيَرْكُمُهُمْ جَمِيعًا فَيَجْعَلُهُمْ فِي جَهَنَّمَ

"Na Kuwaweka waovu juu ya waovu wengine, na Kuwarundika wote pamoja, na Kuwatupa katika Jahannam." (8:37) Na Amesema,

وَمَا ءَاتَيْتُمْ مِّن رِّبَا لِّيَرْبُوَ فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا يَرْبُوا عِنْدَ اللَّهِ ۗ

"Na mnachokitua kwa riba ili kiongezeke katika mali ya watu, binafsi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu." (30:39)

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى

يَمَحَقُ اللَّهُ الرِّبَا

"Mwenyezi Mungu Huiondolea Baraka riba."

Ni sawa na kauli iliyosimuliwa na Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه, "Riba, hata kama itakuwa nyingi sana, itapungua mpaka kumalizika."¹

Imam Ahmad alinukuu kauli sawa na hii katika Al-Musnad.²

Allah Huzilea (Huziongeza) Sadaka, kama Mtu Anavyofuga Mnyama Wake

Kauli ya Allah تعالى،

وَيُرِي الصَّدَقَاتِ

"Na Huzibariki Sadaka."

Maana yake: Allah تعالى Huifanya mali iliyotolewa Sadaka kuongezeka. Al-Bukhari alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ تَصَدَّقَ بِعَدْلِ تَمْرَةٍ مِنْ كَسْبٍ طَيِّبٍ، وَلَا يَقْبَلُ اللَّهُ إِلَّا الطَّيِّبَ، فَإِنَّ اللَّهَ يَقْبَلُهَا بِمِثْلِهِ، ثُمَّ يُرِيهَا لِصَاحِبِهِ، كَمَا يُرِي أَحَدَكُمْ فَلَوْهُ حَتَّى تَكُونَ مِثْلَ الْجَبَلِ»

"Mwenye kutoa Sadaka inayolingana na tende kutokana na chumo halali, na Allah Hakubali isipokuwa kilicho kizuri. Hakika Allah Hukipokea kwa Mkono Wake wa Kulia na kisha Hukiinua kwa mtoaji, kama mtu anayefuga mwanafarasi wake, mpaka inakuwa (Sadaka hiyo) kama mlima."³

Hadithi hii iliandikwa na Muslim katika kitabu cha Zakah.⁴

¹ At-Tabari 6:15.

² Ahmad 1:395.

³ Fat'hul Al-bari 3:326, 13:426.

⁴ Muslim 2:702.

Allah تعالی Hawapendi Makafiri Wafanyao Dhambi

Kauli ya Allah تعالی،

وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ﴿٢٧٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila kafiri (na) afanyaye dhambi.”

Inaonesha kuwa Allah تعالی Hampendi mwenye moyo wa kukadhibisha, ambaye anafanya dhambi kwa ulimi na matendo. Hapana budi kunasibisha ukomo wa Aya hii na sifa hii. Nayo ni kwamba, anayekula riba huwa haridhiki na vile vya halali na ambavyo Allah تعالی Amempatia, wala hatosheki na vile Alivyomuwekea, miongoni mwa chumo la halali. Badala yake, kwa ubatili, anakula mali za watu kwa njia zilizo chafu. Huku ni kukanusha neema, huku akiwa ni dhalimu, mwenye madhambi kwa ulaji wa mali za watu kwa ubatilifu.

Kuwasifu Wanaomshukuru Allah تعالی:

Allah تعالی Amewasifu wale wanaomwamini Mola wao, wanaotii Amri Zake, wanaomshukuru, wanaowatendea wema viumbe Wake kwa kusimamisha Swala na kutoa Zaka ya mali zao; huku Akiwajulisha heshima Aliyowaandalia na kuwa watakuwa salama na mateso siku ya Hukumu. Allah تعالی Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَءَاتَوُا الزَّكَاةَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ

عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٦﴾

“Hakika wale walioamini na wakatenda mema na wakashika Swala na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.” (2:277)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبَا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٧٧﴾ فَإِن لَّمْ

تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَإِن تُبْتِغُوا فَلَکُمْ رُءُوسُ أَمْوَالِكُمْ لَا

تُظْلَمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ ﴿٢٧٨﴾ وَإِن كَانِ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ ۗ وَأَن تَصَدَّقُوا

خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٧٩﴾ وَاتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّىٰ

كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾

278. *"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni riba zilizobakia, ikiwa nyinyi ni Waumini."*

279. *"Basi mkitofanya jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mkitubu, basi haki yenu ni rasilmali zenu. Msidhulumu wala msidhulumawe."*

280. *"Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkilifanya deni kuwa ni Sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua."*

281. *"Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilichochuma. Nao hawata dhulumwiwa."*

Amri ya Kuwa Wachamungu (Taqwa) na Kuiepuka Riba:

Allah تعالى Amewaamrisha waja Wake kumcha Yeye na Anawaonya kujiweka mbali na mambo yatakayowakurubisha katika Hasira Yake na yakawapeleka mbali na Ridhaa Yake. Allah تعالى Amesema,

يَتَّيِبُهَا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَتَّقُوا اللَّهَ

"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu." Maana yake: Mcheni Yeye na kumbukeni kuwa Anayaona yote muyafanyayo.

وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبَا

"Na acheni riba zilizobakia." Maana yake: Mziache riba zilizopo katika rasilimali zenu mnazowadai watu baada ya kusikia maonyo haya.

إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

"Ikiwa nyinyi ni Waumini."

Kuamini katika biashara Alizoziruhusu na kuharamishwa riba na mengineyo. Zayd bin Aslam, Ibn Jurayj, Muqatil bin Hayyan na As-Suddi walisema kuwa Ayah hii iliteremshwa kuwahusu Bani 'Amr bin 'Umayr, kabila dogo la Thaqif, na Bani Al-Mughirah, kutoka kabila la Bani Makhzum, kati yao kulikuwa na miamala ya riba iliyoachwa toka zama za Jahilliyah. Uislam ulipokuja na makabila yote yakasilimu. Thaqif waliwataka Bani Al-Mughirah kulipa riba ya

makubaliano yaliyopita, lakini Bani Al-Mughirah walisema, “Hatulipi riba katika Uislamu.” Attab bin Usayd رضي الله عنه, Msaidizi wa Mtume, Makkah, alimuandikia Mtume ﷺ kuhusiana na suala hilo. Ayah hii iliteremshwa na Mtume ﷺ aliifikisha kwa Attab رضي الله عنه,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنَ الرِّبَا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٧٥﴾ فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ^ط

“Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni riba zilizobakia, ikiwa nyinyi ni waumini. Basi mkitofanya jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake.”

Walisema, “Tunatubia kwa Allah تعالى na tunaacha chochote kilichobakia katika riba zetu,” na wote waliacha.¹ Ayah hii ni onyo kali kwa wale wanaoendelea na riba baada ya Allah تعالى Kuteremsha onyo hili.

Riba ni Kutangaza Vita Dhidi ya Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ:

Ibn Jurayj alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ

“Jitangazieni vita.” Maana yake: “Kuweni na uhakika wa vita kutoka kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ.”² Pia alisema, “Katika Siku ya Kiyama, wale waliokula riba wataambiwa, “Chukueni silaha kwa ajili ya vita’.” Kisha alisoma,

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ^ط

“Basi mkitofanya jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.”

Ali bin Abu Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Ayah:

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ^ط

“Basi mkitofanya jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.”³

¹ Ibn Abu Hatim 3:1140, 1141: Hadithi hii sii Sahih.

² At-Tabari 6:26.

³ At-Tabari 6:25.

“Yeyote aliyeendelea kula riba na hakuacha kula riba, Kiongozi wa Kiislam amkate kichwa chake.”¹ Kisha Allah تعالى Amesema,

وَأِنْ تَبْتَأْ فَالْكُفْرَ الَّذِي كُنْتُمْ تُكْفِرُونَ لَا تَنْظِمُونَ

“Na mkitubu, basi haki yenu ni rasilimali zenu. Msidhulumu.”

Kwa kuchukua ziada,

وَلَا تُظْلَمُونَ

“Wala msidhulumiwe.”

Maana yake: Kwa kuweka mitaji. Bali, mtapata kile mlichokopesha bila kuongezeka au kupunguka. Ibn Abu Hatim رضي الله عنه alinukuu kuwa Amr bin Al-Ahwas رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alitoa hotuba. Wakati wa Haji ya Kuaga kwa kusema,

«أَلَا إِنَّ كُلَّ رَبَا كَانَ فِي الْجَاهِلِيَّةِ، مَوْضُوعٌ عَنْتِكُمْ كُلُّهُ، لَكُمْ رُؤُوسٌ أَمْوَالِكُمْ لَا تَنْظِمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ، وَأَوَّلُ رَبَا مَوْضُوعٍ، رَبَا الْعَبَّاسِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ مَوْضُوعٌ كُلُّهُ»

“Kwa hakika kila riba iliokuwa wakati wa Jahiliyyah imefutwa yote kwenu. Mtachukua mitaji yenu wala hamtadhulumu wala hamtadhulumiwa. Riba ya kwanza ninayoibatilisha ni ya Al-Abbas bin Abdul-Muttalib, yote imefutwa.”²

Kuwahurumia Wadaiwa Wenye Matatizo ya Kifedha

Allah تعالى Amesema,

وَأِنْ كَانَتْ دُونُ عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ وَأَنْ تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

“Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkiifanya deni kuwa Sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua.”
(2:280)

Allah تعالى Ameamrisha wadai kuwavumilia wadaiwa ambao wana hali ngumu ya kifedha, Aidha Amesema,

وَأِنْ كَانَتْ دُونُ عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ

“Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike.”

¹ At-Tabari 6:25.

² Ibn Abu Hatim 3:1147.

Si kama wakati wa Jahiliyyah, wakati muda wa deni ulipokwisha, mdai alimwambia mdaiwa, "ama lipa sasa au riba itaongezwa kwenye deni." Allah تعالی Amewashajiisha Wadai kuwavumilia wadaiwa na Akawaahidi yote mazuri, na malipo makubwa kutoka Kwake kutokana na amali njema hii, Allah تعالی Amesema,

وَأَنْ تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٧٥﴾

"Na mkiifanya deni kuwa ni Sadaka, basi ni bora kwenu ikiwa mnajua."

Maana yake: Iwapo utawasamehe madeni au kuyafuta kabisa. Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Sulayman bin Buraydah alisema kuwa baba yake alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَنْ أَنْظَرَ مُعْسِرًا، فَلَهُ بِكُلِّ يَوْمٍ مِثْلُهُ صَدَقَةٌ»

"Yeyote anayempa muda mdaiwa anayekabiliwa na matatizo, kila siku mfano wake sawa na kutoa Sadaka."

Nilisema, 'Ewe Mtume! Nilikusikia ukisema, 'Yeyote anayempa muda mdaiwa anayekabiliwa na matatizo kila siku atalipwa sawa na kutoa Sadaka' Kisha nilikusikia tena ukisema, "Yeyote anayempa muda wa kulipa mdaiwa anayekabiliwa na matatizo, kila siku atalipwa mara mbili sawa na kutoa Sadaka kwa kila siku atakayompa mdaiwa." Yeye Mtume ﷺ alisema,

«لَهُ بِكُلِّ يَوْمٍ مِثْلُهُ صَدَقَةٌ قَبْلَ أَنْ يَجِلَّ الدَّيْنُ، فَإِذَا حَلَّ الدَّيْنُ فَأَنْظَرَهُ، فَلَهُ بِكُلِّ يَوْمٍ مِثْلَهُ صَدَقَةٌ»

"Atalipwa sawa na Sadaka kwa viwango vilivyo sawa kwa kila siku aliyotoa kabla ya kukamilika muda wa deni, na muda ukiisha atalipwa mara mbili ya kila siku aliyoiongeza."¹

Ahmad alinukuu kutoka kwa Muhammad bin Ka'b Al-Quradhi alisema kuwa Abu Qatadah alikuwa anam dai mtu, ambaye alikuwa akijificha, Abu Qatadah asimwone alipokuwa anam tafuta amlipe. Siku moja, Abu Qatadah alikuwa akim tafuta mdaiwa na kijana akatoka, na akamwuliza juu ya mdaiwa na akajua kuwa alikuwa ndani akila. Abu Qatadah akasema kwa sauti ya juu, "Ewe Fulani!

¹ Ahmad 5:360.

Toka nje, kwani nimeambiwa umo ndani." Mtu yule alitoka nje na Abu Qatadah akamwuliza, "Kwa nini unajificha?" Mtu yule akamjibu, "Nina hali ngumu ya kifedha." Abu Qatadah alilia na kusema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَنْ نَفَسَ عَنْ غَرِيْبِهِ أَوْ مَحَا عَنْهُ، كَانَ فِي ظِلِّ الْعَرْشِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*"Yeyote anayempa muda mdaiwa wake, au kumsamehe deni, atakuwa chini ya kivuli cha Arshi (ya Allah), Siku ya Kiyama."*¹

Pia Muslim alinukuu Hadithi hii katika Sahih.² Al-Hafiz Abu Yala Al-Mawsili alinukuu kuwa Hudhaifah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَتَيْتُ اللَّهَ بِعَبْدٍ مِنْ عِبْدِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ قَالَ: مَاذَا عَمِلْتَ لِي فِي الدُّنْيَا؟ فَقَالَ: مَا عَمِلْتُ لَكَ يَا رَبِّ بِفَقَالَ ذَرَّةٌ فِي الدُّنْيَا أَرْجُوكَ بِهَا - قَالَهَا ثَلَاثَ مَرَّاتٍ - قَالَ الْعَبْدُ عِنْدَ آخِرِهَا: يَا رَبِّ إِنَّكَ كُنْتَ أَعْطَيْتَنِي فَضْلَ مَالٍ، وَكُنْتُ رَجُلًا أَبَايَعُ النَّاسَ، وَكَانَ مِنْ خُلُقِي الْجَوَازُ، فَكُنْتُ أَيْسَرُ عَلَى الْمُوَسِّرِ وَأَنْظِرُ الْمُعْسِرَ، قَالَ: يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: أَنَا أَحَقُّ مَنْ يَيْسَرُ، ادْخُلِ الْجَنَّةَ»

"Siku ya kiyama, mmoja wa waja wa Allah ataitwa mbele Yake na Atamuuliza, 'Umefanya amali gani kwa ajili Yangu katika maisha yako.' Atajibu, 'Ewe Mola! Katika uhai wangu, sikuwahi kufanya amali kwa ajili Yako iliyo sawa na chembe ndogo.' Mara tatu. Mara ya tatu, mja ataongeza, 'Ewe Mola! Ulinijaalia mali na nilikuwa nauziana na watu. Nilikuwa mpole, nikawapa masharti mepesi wenye uwezo na nikiwapa muda wa kulipa wadaiwa.' Allah Atamuambia, 'Mimi Ndiye Mwenye Haki zaidi ya Kutoa masharti mepesi kwa hiyo, ingia Peponi."

Bukhari, Muslim na Ibn Majah waliinukuu Hadithi hii kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه, na Muslim aliinukuu kutoka kwa Uqbah bin Amiri na Abu Mas'ud Al-Badri رضي الله عنهما.³ Mfano wake

¹ Ahmad 5:308.

² Muslim 4:2074.

³ Fat'hul Al-Bari 6:570, Muslim 3:1195, Ibn Majah 2:808.

Zaidi ya hayo, Allah تعالی Aliwaidhi waja Wake kwa kuwakumbusha kuwa maisha haya yatakoma karibuni na utajiri wote utatoweka. Pia aliwakumbusha kuwa hapana shaka Kiyama kitakuja, ambapo marejeo yatakuwa Kwake, na kuwa Atawahesabu viumbe Wake kwa yale waliyoyafanya, Atawalipa au Atawaadhibu kwa mintarafu ya amali zao. Pia Allah تعالی Aliwaonya dhidi ya mateso Yake.

وَأَتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨١﴾

“Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilichochuma. Nao hawatadhulumiwa.”
(2:281)

Ilisimuliwa kuwa hii ilikuwa Aya ya mwisho kute remshwa katika Qur’an Takatifu. An-Nasai alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Ayah ya mwisho kuteremshwa ndani ya Qur’an ilikuwa,

وَأَتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨١﴾

“Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilichochuma. Nao hawatadhulumiwa.”
(2:281)¹

Haya ni masimulizi yaliyosimuliwa na Adh-Dhahhak na Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.²

* * *

¹ An-Nasai Katika Al-Kubra 6:307.

² At-Tabari 6:40.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَدَايَنْتُمْ بِدَيْنٍ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى
فَأَكْتَبُوهُ ۖ وَلْيَكْتُب بَيْنَكُمْ كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ ۚ وَلَا يَأْب
كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ ۚ فَلْيَكْتُبْ وَلْيَمْلِكِ
الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ وَلَا يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْئًا ۚ
فَإِنْ كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيهًا أَوْ ضَعِيفًا أَوْ لَا
يَسْتَطِيعُ أَنْ يُمِلَّ هُوَ فَلْيَمْلِكْ وَلِيَهُ بِالْعَدْلِ ۚ وَأَسْتَشْهِدُوا
شَهِدَيْنِ مِنْ رِجَالِكُمْ ۖ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ
وَآخَرَاتَانِ مِمَّنْ تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ أَنْ تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا
فَتُذَكَّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى ۚ وَلَا يَأْبَ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا
دُعُوا ۚ وَلَا تَسْمَعُوا أَنْ تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَىٰ أَجَلِهِ ۚ
ذَٰلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمٌ لِلشُّهَدَةِ وَأَدَقُّ ۚ أَلَّا تَرْتَابُوا ۖ
إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجْرَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ
عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ ۚ أَلَّا تَكْتُبُوهَا ۚ وَأَشْهِدُوا إِذَا تَبَايَعْتُمْ ۚ وَلَا
يُضَارَّ كَاتِبٌ وَلَا شَهِيدٌ ۚ وَإِنْ تَفَعَّلُوا فَإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ ۚ
وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ ۚ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَدَايَنْتُمْ
بِدَيْنٍ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ فَآكْتُبُوهُ ۚ
وَلْيَكْتُب بَيْنَكُمْ كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ ۚ
وَلَا يَأْب كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا
عَلَّمَهُ اللَّهُ ۚ فَلْيَكْتُبْ وَلْيَمْلِكِ الَّذِي
عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ وَلَا
يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْئًا ۚ فَإِنْ كَانَ الَّذِي
عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيهًا أَوْ ضَعِيفًا أَوْ لَا
يَسْتَطِيعُ أَنْ يُمِلَّ هُوَ فَلْيَمْلِكْ وَلِيَهُ
بِالْعَدْلِ ۚ وَأَسْتَشْهِدُوا شَهِدَيْنِ مِنْ
رِجَالِكُمْ ۖ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ
فَرَجُلٌ وَآخَرَاتَانِ مِمَّنْ تَرْضَوْنَ مِنَ
الشُّهَدَاءِ أَنْ تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا
فَتُذَكَّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى ۚ وَلَا
يَأْبَ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا دُعُوا ۚ وَلَا

تَسْمَعُوا أَنْ تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَىٰ أَجَلِهِ ۚ
ذَٰلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمٌ لِلشُّهَدَةِ وَأَدَقُّ ۚ أَلَّا
تَرْتَابُوا ۖ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجْرَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ
فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ ۚ أَلَّا تَكْتُبُوهَا ۚ وَأَشْهِدُوا
إِذَا تَبَايَعْتُمْ ۚ وَلَا يُضَارَّ كَاتِبٌ وَلَا شَهِيدٌ ۚ وَإِنْ تَفَعَّلُوا
فَإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ ۚ

وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

282. “Enyi mlioamini! Mnapokopeshana deni kwa mda uliowekwa, basi andikeni. Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika. Aandike kama Alivyomfunza Mwenyezi Mungu. Na mwenye deni juu yake aandikishe; naye amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi. Wala asipunguze chochote ndani yake. Na akiwa mwenye kudaiwa ni mtu aliyepumbaa au mnyonge au hawezi kuandikisha mwenyewe, basi aandikishe mlinzi wake kwa uadilifu. Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu. Ikiwa hapana wanaume wawili, basi mwanaume mmoja na wanawake wawili katika mnao waridhia kuwa mashahidi. Ili ikiwa mmoja wao akilopolea, mmoja wao amkumbushe mwengine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuuze kuliandika deni likiwa dogo au kubwa mpaka muda wake. Hayo ndio haki zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo sawa zaidi kwa ushahidi, na vyema zaidi ili msiwe na shaka. Ila ikiwa ni biashara ya mkono kwa mkono baina yenu, basi hapo si vibaya kwenu msipoiandika. Lakini mnapouziana wekeni mashahidi. Wala asitiwe matatani mwandishi wala shahidi. Na mkifanya hivyo basi hakika hilo ni kosa kwenu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Umuhimu wa Kuandikiana Miamala Yenye Kuwekewa Muda:

Aya hii ndefu kuliko zote ndani ya Qur’an Tukufu. Imam Abu Jafar bin Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Said bin Al-Musayyib alisema kuwa aliambiwa kuwa Aya iliyoteremshwa karibuni kutoka juu ya Arshi – Ayah ya mwisho kuteremshwa ndani ya Qur’an – ilikuwa Aya kuhusu madeni.¹

Kauli ya Allah تعالى،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَدَايَنْتُمْ بِدِينٍ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى فَاكْتُبُوهُ

“Enyi mlioamini! Mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa basi andikeni.”

¹ At-Tabari 6:41.

Inawaelekeza waja waumini wa Allah تعالى kuandikiana miamala ya biashara muda wake unapoakhirishwa, ili kuhifadhi masharti na muda wa miamala hiyo, na kumbukumbu ya mashahidi, kama ilivyotajwa mwisho wa Aya. Pale Allah تعالى Aliposema,

ذَلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَأَدْنَىٰ أَلَّا تَرْتَابُوا^١

“Hayo ndiyo haki zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo sawa zaidi kwa ushahidi, na vyema zaidi ili msitatizike.”

Sahihi Mbili zilinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alikuja Madinah, wakati watu wakiwa na desturi ya kutanguliza malipo ya kununua matunda ambayo angeyatoa katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili. Mtume ﷺ alisema.

«مَنْ أَسْلَفَ، فَلْيَسْلِفْ فِي كَيْلٍ مَعْلُومٍ، وَوَزَنٍ مَعْلُومٍ، إِلَىٰ أَجَلٍ مَعْلُومٍ»

“Yeyote anayelipa fedha kwa kutanguliza (kwa tende atakazopewa baadaye) lazima alipe kwa kipimo kinachofahamika na uzito unaofahamika (wa tende) kwa muda mahsusi.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

فَأَكْتُبُوهُ^٢

“Basi andikeni.”

Ni amri ya kutoka Kwake kuandika miamala hiyo kwa kuidhinisha na kuhifadhi masharti yake. Ibn Jurayj alisema, “Yeyote aliyekopa lazima aandike masharti, na yeyote aliyenunua lazima awe na mashahidi.”² Abu Said, Ash-Shabi, Ar-Rabi bin Anas, Al-Hasan, Ibn Jubayr na Ibn Zayd na wengineo walisema kuwa kunukuu miamala hiyo ni lazima kabla, lakini baadaye ilifutwa na Kauli ya Allah تعالى،

فَإِنْ أَمِنَ بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُؤْتِمِنَ أَمْنَتَهُ^٣

“Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliyeaminiwa arudishe amana ya mwenzake.” (2:283)³

¹ Fat’hul Al-Bari 4:105, Muslim 3:1226.

² At-Tabari 6:47.

³ At-Tabari 6:47, 49:50.

Kauli ya Allah تعالى،

وَلْيَكْتُبْ بَيْنَكُمْ كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ

“Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu.”

Na katika ukweli. Kwa hiyo, mwandishi haruhusiwi kudanganya sehemu yoyote ya mkataba na anatakiwa kunukuu yale yaliyokubaliwa na pande mbili, bila kuongeza au kufuta. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَأْبَ كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ

“Wala mwandishi asikatae kuandika. Aandike kama alivyomfunza Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: “Wale wanaojua kuandika wasiache kuandika miamala ya mikataba wanapotakiwa kufanya hivyo.” Zaidi ya hayo, kuandika mikataba ni aina ya Sadaka kwa Mwandishi anapowaandikia wasiojua kusoma wala kuandika, kama ambavyo Allah تعالى Alivyomfundisha asiyoyajua. Kwa hiyo, aandike, kama Hadith ilivyoieleza,

«إِنَّ مِنَ الصَّدَقَةِ أَنْ تُعَيِّنَ صَانِعًا، أَوْ تَضَعِ لِأَخْرَقٍ»

“Hakika katika Sadaka ni kumsaidia mfanyakazi au kumsaidia mtu dhaifu.”¹

Katika Hadithi nyingine, Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ كَتَمَ عِلْمًا يَعْلَمُهُ، أُلْجِمَ بِزَمِ الْقِيَامَةِ يَلْجِمُ مِنْ نَارٍ»

“Mwenye kuficha elimu anayojua, atafungwa lijamu ya moto siku ya Kiyama.”²

Mujahid na Ata walisema kuwa akiombwa kufanya hivyo, “Mwandishi anatakiwa kunukuu.”

¹ Fat’hul Al-Bari 5:176.

² At-Tabarani 5:11.

Kauli ya Allah تعالى،

وَلِيْمَلِلِ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلِيَتَّقِيَ اللَّهَ رَبَّهُ

“Na mwenye deni juu yake aandikishe, naye amche Mwenyezi Mungu Mola wake Mlezi.”

Inaonesha kuwa mkopaji anawajibika kumsomea mwandishi kila anachodaiwa, hivyo amche Allah تعالى،

وَلَا يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْئًا

“Wala asipunguze chochote ndani yake.”

Maana yake: Kutoficha sehemu yoyote anayodaiwa.

فَإِنْ كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيهًا

“Na akiwa mwenye kudaiwa ni mtu aliyepumbaa!”

Hatakiwi kuamua katika masuala hayo, kwa sababu ya ufujaji wa fedha, kwa mfano،

أَوْ ضَعِيفًا

“Au mnyonge.”

Kama kuwa mdogo wa umri au wazimu.

أَوْ لَا يَسْتَطِيعُ أَنْ يُعْمَلَ هُوَ

“Au hawezi kuandikisha mwenyewe.”

Kwa sababu ya maradhi, au kujingikiwa juu ya masuala hayo،

فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهُ بِالْعَدْلِ

“Basi aandikishe walii wake kwa uadilifu.”

Mashahidi Lazima Wahudhurie Imla ya Mikataba:

Allah تعالى Amesema,

وَأَشْتَشْهِدُوا شَهِيدَيْنِ مِنْ رَجَالِكُمْ

“Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu.”

Inawahitaji mashahidi kuhudhuria uandishi wa mikataba na baadaye kuhifadhi maudhui yake,

فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَأَمْرَأَتَانِ

“Ikiwa hapana wanaume wawili, basi mwanaume mmoja na wanawake wawili.”

Sharti hilo ni kwa ajili ya mikataba ambayo moja kwa moja au vinginevyo inahusu fedha tu.

Allah تعالى Amefaradhisha wanawake wawili kuchukua nafasi ya shahidi mmoja mwanaume, kwa sababu ya upungufu wa mwanamke, kama Mtume ﷺ alivyoeleza,

«يَا مَعْشَرَ النِّسَاءِ تَصَدَّقْنَ وَأَكْمِرْنَ الْإِسْتِغْفَارَ، فَإِنِّي رَأَيْتُكُمْ أَكْثَرَ أَهْلِ النَّارِ»

“Enyi kundi la wanawake! Toeni Sadaka na mkirithishe kuomba msamaha, kwani nimewaona wengi wenu ni watu wa motoni.”

Mwanamke m-buji alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Kwanini sisi ndio wengi katika watu wa motoni?” Alijibu,

«تُكْمِرْنَ اللَّغْنَ، وَتَكْفُرْنَ الْعَشِيرَ، وَمَا رَأَيْتُ مِنْ نَاقِصَاتِ عَقْلِ وَدِينٍ، أَغْلَبَ لِيذِي لُبٍّ مِنْكُمْ»

“Mnalaani mno na wepesi kukanusha hisani ya mume, sijawaona wenye upungufu wa akili na dini mwenye kuwashinda wenye akili kuliko nyinyi.”

Akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ni udhaifu gani wa akili na dini?” Akasema:

«أَمَّا نَقْصَانُ عَقْلِهَا، فَشَهَادَةُ امْرَأَتَيْنِ تَعْدِلُ شَهَادَةَ رَجُلٍ، فَهَذَا نَقْصَانُ الْعَقْلِ، وَتَمَكُّتُ اللَّيَالِي لَا تُصَلِّي وَتُنْفِطِرُ فِي رَمَضَانَ، فَهَذَا نَقْصَانُ الدِّينِ»

“Ama upungufu katika akili yake (mwanamke), ushahidi wa wanawake wawili ni sawa na ushahidi wa mwanaume mmoja, na huu ndio upungufu wa akili. Ama upungufu katika dini, wanawake wakati mwingine baadhi ya siku huwa hawasali na hufungua katika mwezi wa Ramadhani.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

مِمَّن تَرَضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ

“Katika mnaowaridhia kuwa mashahidi.”

Inahitaji uadilifu katika ushahidi. Kauli ya Allah تعالى inaendelea،

أَنْ تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا

“Ili ikiwa mmoja wao akilopolea.”

Inahusu wanawake wawili mashahidi, iwapo mmojawao atasahau sehemu ya mkataba،

فَتَذَكَّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى

“Mmoja wao amkumbushe mwingine.”Maana yake: Ushahidi wa mwanamke mwingine unaziba udhaifu wa kusahau kwa mwanamke wa mwanzo. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَأْبَ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا دُعُوا

“Na mashahidi wasikatae waitwapo.”

Maana yake: Watu wanapotakiwa kuwa mashahidi, wakubali kama alivyoeleza Qatadah na Ar-Rabi bin Anas. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema،

وَلَا يَأْبَ كَاتِبٌ أَنْ يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ فَلْيَكْتُبْ

“Wala mwandishi asikatae kuandika. Aandike kama Alivyomfunza Mwenyezi Mungu.”

Baadhi wanasema kuwa Ayah hii inaonesha kukubali kuwa shahidi ni *Faradhi Kifayah*. Huu ni mtazamo wa jopo la wanazuoni wa Kiislamu. Na imesemwa kuwa maana ya Kauli Yake Allah تعالى،

¹ Muslim 1:87.

وَلَا يَأْبُ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا دُعُوا^١

“Na mashahidi wasikatae waitwapo.”

Kwa ajili ya kufikisha walichokishuhudia.¹ Na shahidi kiuhakika ni yule ambaye kabeba jukumu hilo. Kwa hiyo, shahidi anapoitwa kuthibitisha alichokishuhudia, anatakiwa kutoa ushahidi, isipokuwa kama jukumu hilo lilikwisha kutekelezwa, kwa hali hiyo ushahidi huo huwa *Fardhi Kifayah*. Mujahid na Abu Mijlaz walisema, “Iwapo utaitwa kuwa shahidi basi una chaguo la kukubali kama ulishuhudia na uliitwa kutoa ushahidi, nenda katoe ushahidi.”²

Ilisimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas na Hassan Al-Basri رضي الله عنهما walisema kuwa jukumu lipo kwa hali zote, kukubali kwa shahidi na kutolea ushahidi alichokishuhudia mtu. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا تَسْمَعُوا أَنْ تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَىٰ أَجْلِهِ^٢

“Wala msipuuzze kuliandika deni likiwa dogo au kubwa mpaka muda wake.”

Allah تعالى Anaamrisha kuwa deni lazima liandikwe, ima ni dogo au kubwa Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَسْمَعُوا

“Wala msipuuzze.” Maana yake: Msipuuzze kuandika deni na masharti yake, ima ni kikubwa au kidogo. Kauli ya Allah تعالى،

ذَلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمُ لِلشَّهَدَةِ وَأَدْنَىٰ أَلَّا تَرْتَابُوا

“Hayo ndiyo haki zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo sawa zaidi kwa ushahidi, na vyema zaidi ili msiwe na shaka.”

Maana yake: Kuliandika deni ambalo litalipwa baadaye ni haki zaidi kwa Allah تعالى، maana ni bora zaidi na inafaa zaidi ili kuhifadhi masharti ya mkataba. Kwa hiyo kuandika mikataba ya aina hiyo inawasaidia mashahidi, wanapoona maandishi yao au sahihi baadaye na kuwakumbusha kile walichokishuhudia, kwani kuna uwezekano kuwa mashahidi wamesahau kile walichokishuhudia.

¹ At-Tabari 6:68.

² Ibn Abu Hatim 3:1181, At-Tabari 6:71.

وَأَدَّتْ أَلَّا تَزْتَابُونَ^ط

“Na vyema zaidi ili msiwe na shaka.”

Maana yake: Hii inasaidia kuondoa wasiwasi. Kwa kuwa ukitaka kuurejea mkataba uliouandika na wasiwasi utaondoka. Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجْرَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَلَّا تَكْتُبُوهَا^٤

“Ila ikiwa ni biashara ya mkono kwa mkono baina yenu, basi hapo si vibaya kwenu msipoandika.”

Inaonesha kuwa muamala ukikamilika mara moja, hivyo hapana makosa kama hautoandikwa kwa kukosekana kile kinachohofiwa. Ama ulazima wa kuwepo mashahidi wakati wa kuuziana, Allah تعالى Anasema,

وَأَشْهَدُوا إِذَا تَبَايَعْتُمْ^ع

“Lakini mnapouziana wekeni mashahidi.”

Hata hivyo, Amri hii ilifutwa na Aya hii,

فَإِنْ أَمِنَ بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُؤْتِمِنَ أَمْنَتَهُ

“...Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi airudishe amana ya mwenzake...” (2:283)

Au, inayumkinika kuwa na mashahidi katika hali kama hizo imependekezwa tu na sio lazima, kama ushahidi uliopo katika Hadith ambayo imesimuliwa na Khuzaymah bin Thabit Al-Ansar ambayo ilikusanywa na Imam Ahmad. Kutoka kwa Umara bin Khuzaymah alisema kuwa ami yake, ambaye alikuwa Swahaba, alimwelezea kuwa Mtume ﷺ alifanya makubaliano ya kununua farasi kutoka kwa bedui. Mtume ﷺ alimwambia bedui yule amfuate ili amlipe thamani ya farasi yule. Mtume ﷺ alikwenda mbele ya bedui. Bedui alikutana na watu kadhaa waliotaka kumnunua yule farasi, bila kujua kuwa Mtume ﷺ alikusudia kwa dhati kumnunua. Baadhi ya watu walitoa bei ya juu kuliko ile ya Mtume ﷺ bedui yule akamwambia Mtume ﷺ, “Kama unataka kumnunua farasi huyu, mnunue vinginevyo nitamuuzia mtu mwingine.” Mtume ﷺ aliposikia maneno ya bedui, Mtume ﷺ alisimama na kusema, “Je, mimi sijamnunua farasi huyo kutoka kwako?” Bedui alijibu, “Wallah! Sijakuuzia.” Mtume ﷺ alisema, “Bali,

nimemnunua kutoka kwako." Watu walimzingira Mtume ﷺ na bedui wakati wakibishana, na bedui akasema, "Mlete shahidi ambaye atathibitisha kuwa nimekuuzia farasi." Wakati huo, Waislamu waliokuwepo pale walimwambia bedui, "Umeangamia! Mtume ﷺ husema ukweli tu." Khuzaymah bin Thabit رضي الله عنه alifika na kusikia yale mabishano kati ya Mtume ﷺ na bedui ambaye alikuwa anasema, "Mlete shahidi ambaye atathibitisha kuwa nimekuuzia farasi: "Khuzaymah رضي الله عنه alisema, "Nina shuhudia kuwa ulimuzia farasi." Mtume ﷺ alimuambia Khuzaymah رضي الله عنه, "Nini msingi wa ushahidi wako?" Khuzaymah رضي الله عنه alisema, "Nimekuamini wewe, Ewe Mjumbe wa Allah! "Kwa hiyo, Mtume ﷺ alifanya ushuhuda wa Khuzaymah رضي الله عنه sawa na ushahidi wa watu wawili.¹ Hadith ilinukuliwa pia na Abu Dawud na An-Nasai"² Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا يُضَارُّ كَاتِبٌ وَلَا شَهِيدٌ

"Wala asitiwe matatani mwandishi wala shahidi." Pia inaonesha kuwa mwandishi na shahidi wasilete madhara, kama vile, mwandishi kuandika tofauti na alivyosomewa, au shahidi kutolea ushahidi tofauti na alivyosikia au kuficha ushahidi. Haya ni maelezo ya Al-Hasan na Qatadah.³ Kauli ya Allah تعالى.

وَأِن تَفْعَلُوا فَإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ

"Na mkifanya hivyo basi hakika hilo ni kosa kwenu." Maana yake: "Ukiasi yale uliyoamrisha na ukafanya yaliyoharamishwa, basi ni kwa sababu ya madhambi uliyo nayo, madhambi ambayo huwezi kuachana nayo." Kauli ya Allah تعالى,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

"Na mcheni Mwenyezi Mungu." Maana yake: Mcheni Allah تعالى, kwa kumuogopa kwa kuwa na hadhari naye kwa kutekeleza amri yake na kuacha aliyoharamisha,

وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ

"Na Mwenyezi Mungu Anakuelimisheni." Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 5:215.

² Abu Dawud 4:31, An-Nasai 7:301.

³ At-Tabari 6:85,86. Aya hii maana yake yapo sehemu mbili. Inafaa kutafsiri Shahidi na Mwandishi wasilete madhara katika ushuhuda na uandishi. Pia inaweza kutafsiriwa wenye kudaiana wasiwadhuru Shahidi na Mwandishi. Na rai hii ndio yenye nguvu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ فُرْقَانًا

“Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu Atakupeni kipambanuo.” (8:29)

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَءَامِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَل لَّكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ

“Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume Wake, Atakupeni sehemu mbili katika Rehema Yake, na Atakujalieni muwe na nuru ya kwenda nayo.” (57:28)

Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Inaeleza kuwa Allah تعالى Anajua masuala yote na yenye maslahi nao, au matokeo hasi, na hapana kinachopita Usoni Mwake, kwani Anajua kila kitu.

* * *

* وَإِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ سَفَرٍ وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا فَرِهِنَّ مَقْبُوضَةً ۗ
 فَإِنْ أَتَىٰ بَعْضُكُم مَّقْبُوضَةٌ ۗ فَإِنْ أَمِنَ
 بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُوتِيَ
 اللَّهُ رِيبَهُ ۗ وَلَا تَتَّخِذُوا الشَّهَادَةَ
 عَمَّا بَيْنَكُمْ فَإِنَّهُ
 ءَاثِمٌ قَلْبُهُ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨٣﴾ ۗ اللَّهُ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَإِنْ تُبَدُّوا مَا فِي
 أَنْفُسِكُمْ أَوْ
 تُخْفَوهُ يُحَاسِبْكُمْ بِهِ اللَّهُ ۗ فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ
 وَيُعَذِّبُ مَن
 يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾ ۗ ءَاَمَنَ
 الرَّسُولُ
 بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ ۗ وَالْمُؤْمِنُونَ ۗ كُلٌّ
 ءَاَمَنَ بِاللَّهِ
 وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ ۗ لَا تُفَرِّقُ
 بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْ
 رُّسُلِهِ ۗ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ غُفْرَانَكَ
 رَبَّنَا وَإِلَيْكَ
 الْمَصِيرُ ﴿٢٨٥﴾ ۗ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا
 إِلاَّ وُسْعَهَا ۗ لَهَا مَا
 كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا
 اكْتَسَبَتْ ۗ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا
 إِن كُنَّا سَآئِئًا
 أَوْ
 أَخْطَاءْنَا ۗ رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ
 عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا
 حَمَلْتَهُ عَلَى
 الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا ۗ رَبَّنَا
 وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا
 طَاقَةَ لَنَا بِهِ ۗ
 وَاعْفُ عَنَّا
 وَأَغْفِرْ لَنَا
 وَأَرْحَمْنَا ۗ أَنْتَ
 مَوْلَانَا فَانصُرْنَا
 عَلَى
 الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾

* وَإِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ سَفَرٍ وَلَمْ تَجِدُوا
 كَاتِبًا فَرِهِنَّ مَقْبُوضَةً ۗ فَإِنْ أَمِنَ
 بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُوتِيَ
 اللَّهُ رِيبَهُ ۗ وَلَا تَتَّخِذُوا
 الشَّهَادَةَ عَمَّا بَيْنَكُمْ فَإِنَّهُ
 ءَاثِمٌ قَلْبُهُ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ
 عَلِيمٌ ﴿٢٨٣﴾

283. "Na mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, yatosha kukabidhiwa rehani. Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi. Wala msifiche ushahidi. Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mnayoyatenda."

Ubainifu wa Rehani

Allah تعالى Amesema,

* وَإِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ سَفَرٍ

"Na mkiwa safarini..."

Maana yake: Mkiwa safarini na mmekopa fedha ambazo zinatakiwa kulipwa baadaye,

وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا

“... na hamkupata mwandishi...”

Ambaye atakuandikia deni. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Na hata kama watapata mwandishi, lakini hakupata karatasi, wino au kalamu, basi. Rehani hiyo akabidhiwe mwenye haki.

فَرَهْنٌ مَّقْبُوضَةٌ

“Yatosha kukabidhiwa rehani.”

Kwa sababu rehani hailazimiki bali kwa kuikabidhi. Sahih Mbili zilinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alikufa huku ngao yake akiwa ameiweka rehani kwa Myahudi na kupewa Wasq thelathini (sawa na kilo 180) za ngano, ambazo Mtume ﷺ alinunua kwa mkopo kwa ajili ya chakula cha nyumbani kwake. Katika mapokezi mengine, Hadith ilieleza kuwa Yahudi huyu alikuwa miongoni mwa Mayahudi wa Madinah.¹

Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ أَمِنَ بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُؤْتِمِنَ أَمْنَتَهُ

“Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake.”

Ibn Abbu Hatim رحمه الله تعالى aliandika, na Isnad nzuri, kutoka kwa Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه, amesema “Aya hii ilifuta kilichokuja kabla yake (Yaani ambayo ilihitaji kuandikwa deni na kuwepo mashahidi).”² Ash-Shabi alisema, “kama mnaaminiana, basi hapana madhara kama hamtoandikiana deni au kuwepo mashahidi.”³ Kauli ya Allah تعالى,

وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ

“Na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi.”

Maana yake: Mdaiwa.

¹ Fat’hul Al-Bari 4:354, Muslim 3:1226.

² Ibn Abu Hatim 3/1202.

³ Ibn Abu Hatim 3:1202.

Imam Ahmad na Sunan walinukuu kuwa Qatadah alisema kuwa Al-Hasan alisema kuwa Samurah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«عَلَى الْيَدِ مَا أَخَذْتُ، حَتَّى تُؤَدِّيَهُ»

*"Mkono wa mkopaji utabeba mzigo wa kile ulichochukua mpaka utakapolipa."*³

Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ

"Wala msifiche ushahidi."

Maana yake: Msiufiche au kukataaa kuutangaza. Ibn Abbas رضي الله عنهما na wanazuoni wengine walisema, "Ushahidi wa uongo ni moja kati ya makosa makubwa, na hilo ni sawa na kuuficha ushahidi wa kweli."

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ

"Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi."⁴

As-Suddi alitoa maelezo, "Ikiwa na maana ni mtenda dhambi ndani ya moyo wake."

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَكْتُمُوا شَهَادَةَ اللَّهِ إِنَّا إِذَا لَمِنَ الْأَثِمِينَ ﴿١٠٦﴾

"Na wala hatutaficha ushahidi wa Mwenyezi Mungu, hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye madhambi." (5:106)

Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Abu Hatim 3:1203.

² Ahmad 5:13, Abu Dawud 3:822, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:482, An-Nasai katika Al-Kubra 3:411, Ibn Majah 2:802.

³ At-Tabari 6:100.

﴿ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُفُونًا قَوَّيْمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلّٰهِ وَلَوْ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ ءَوِ ٱلْوَالِدِينَ
وَٱلْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا ءَوْ فَقِيرًا فَٱللّٰهُ ءَوَّلَىٰ بِهِمَا ۗ فَلَا تَتَّبِعُوا ٱهْوَىٰٓ أَن تَعْدِلُوا ۗ وَإِن
تَلَوْدًا ءَوْ تَعْرِضُوا فَإِنَّ ٱللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ۝﴾

“Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtoao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wawili na jamaa zenu. Akiwa tajiri au masikini Mwenyezi Mungu Anawastahikia zaidi. Basi msifuate matamania, mkaacha kufanya uadilifu. Na mkiupotoa au mkajitenga nao basi Mwenyezi Mungu Anajua vyema mnayoyatenda.” (4:135)

Na katika Aya hii (2:283) Alisema,

﴿ وَلَا تَكْتُمُوا ٱلشَّهَدَةَ ۚ وَمَن يَكْتُمهَا فَإِنَّهُ ءِٔٓثْمَ قَلْبِهِ ۗ وَٱللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ۝﴾

“Wala msifiche ushahidi. Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa Mnayoyatenda.”

﴿ لِلّٰهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَاتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ ۗ وَإِن تُبَدُّوٓاْ مَا فِيٓ أَنفُسِكُمْ ءَوْ تَخْفُوهُ يُحَاسِبْكُم بِهِ
ٱللّٰهُ ۗ فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَآءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَآءُ ۗ وَٱللّٰهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝﴾

284. “Vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani ni vya Mwenyezi Mungu. Na mkidhihirisha yaliyomo katika nafsi zenu au mkayaficha, Mwenyezi Mungu Atakuhisabuni kwayo. Kisha Amsamehe Amtakaye na Amuadhibu Amtakaye. na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.”

Je, Waja Wataulizwa kwa Yale Waliyoyaficha Katika Nyoyo Zao?

Allah تعالى Anaeleza kuwa ni Wake Yeye Ufalme wa mbinguni na duniani na chochote kilicho kati ya hizo, kuwa hakimpiti chochote. Hapana kilicho wazi wala siri na yaliyofichwa katika nafsi zenu ambacho kitafichikana Kwake, hata kiwe kidogo vipi. Allah تعالى pia Anaeleza kuwa waja Wake watawajibika kwa yale wanayoyadhihirisha na kuyaficha ndani ya nyoyo zao.

Katika kauli sawa na hiyo, Allah تعالى Amesema,

قُلْ إِنْ تَخَفُوا مَا فِي صُدُورِكُمْ أَوْ تُبْدُوهُ يَعْلَمَهُ اللَّهُ وَيَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
الْأَرْضِ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾

“Sema: Mkificha yaliyomo vifuani mwenu au mkiyafichua Mwenyezi Mungu Anayajua; na Anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”
(3:29) Na Allah تعالى Amesema,

يَعْلَمُ الْبَيْتَ وَالْحَفَىٰ ﴿٢٠﴾

“Anajua siri na kile ambacho bado kimejificha.” (20:7)

Kuna Ayah nyingi juu ya somo hili. Katika Ayah hii (2:284). Allah تعالى Ameeleza kuwa Ana Elimu ya yale yaliyofichwa katika nyoyo, na kwa hivyo, Atawajibisha waja kwa vile vilivyomo ndani ya mioyo yao. Hii ndio sababu Ayah hii ilipotemshwa, ilikuwa ngumu kwa Masahaba kwani kwa imani yao thabiti na yakini, walichelea kuwa hesabu hizo zingepunguza amali zao njema kutokana na Allah تعالى Kuhesabu amali kubwa na ndogo. Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema,

لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَإِنْ تُبْدُوا مَا فِي أَنْفُسِكُمْ أَوْ تُخْفُوهُ يُحَاسِبْكُمْ بِهِ
اللَّهُ فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾

“Vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani ni vya Mwenyezi Mungu. Na mkidhirisha yaliyomo katika nafsi zenu au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu Atakuhisabuni kwayo. Kisha Amsamehe Amtakaye na Amuadhibu Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.” (2:284)

Ilipotemshwa kwa Mtume ﷺ, ilikuwa ngumu sana kwa Maswahaba wa Mtume ﷺ. Na Masahaba walikuja kwa Mtume ﷺ wakapiga magoti na kusema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Tuliambiwa tufanye amali tunazozimudu: Swala, Funga, Jihad na kutoa Sadaka. Hata hivyo, imeteremshiwa Ayah hii, nasi hatuimudu. Na huu ni uthibitisho wa yakini kwa Imani yao yenye nguvu. Mtume ﷺ alisema,

«أَتُرِيدُونَ أَنْ تَتُولُوا كَمَا قَالَ أَهْلُ الْكِتَابَتَيْنِ مِنْ قَبْلِكُمْ: سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا؟ بَلَى قُولُوا: سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ»

“Je, mnataka kurudia walichosema watu wa Kitabu waliokuwepo kabla yenu, yaani “Tumesikia na hatutii!” bali semeni, “Tumesikia na tumetii, na Tunaomba maghufira, Ewe Mola na tutarejea Kwako.”

Watu walipoikubali Kauli hii na ndimi zao kuisoma, baadaye Allah تعالى Aliteremsha,

ءَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ ۗ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ ۗ لَا تَفَرُّقَ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ۗ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ

الْمَصِيرُ ﴿٢٨٥﴾

“Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola Wake Mlezi, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake na Mitume Wake, hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume Wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumetii. Tunakutaka maghufira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni Kwako.” (2:285)

Walipofanya hivyo, Allah تعالى Alifuta Aya (2:284) na Akateremsha Ayah;

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ ۗ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِن كُنَّا مُسِيئِينَ أَوْ أَخْطَاءَنَا ۗ

“Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi ya mtu yoyote ila kwa kadri ya iwezavyo. Faida ya iliyoyachuma ni yake, na khasara ya iliyoyachuma ni juu yake pia (ombeni) Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea...” Mpaka mwisho.¹

Muslim aliinukuu kwa maneno kama hayo, na akasema, “Walipofanya hivyo, Allah تعالى Aliifuta (2:284), Allah تعالى Akateremsha,

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ ۗ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِن

كُنَّا مُسِيئِينَ أَوْ أَخْطَاءَنَا ۗ

¹ Ahmad 2:412.

“Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo. Faida ya iliyo ya chuma ni yake, na khasara iliyo ya chuma ni juu yake pia (ombeni) Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea.”

Allah تعالى Akasema, “Ndiyo.”

رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِنَا

“Mola wetu Mlezi! Usitubebezhe mzigo kama Uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu...” (2:286)

Allah تعالى Akasema, “Ndiyo.”

رَبَّنَا وَلَا تُحْمِلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ

“Usitutwike tusiyoyaweza.”

Allah تعالى Akasema, “Ndiyo.”

وَأَعْفُ عَنَّا وَاعْفِرْ لَنَا وَأَرْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلَانَا فَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ

“...Na Utusamehe, na Utughufirie na Uturehemu. Wewe Ndiye Mlinzi wetu. Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri.” (2:286)

Allah تعالى Alisema, ‘Ndiyo’¹ Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Mujahid kuwa alisema, “Niliingia kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na nikamwambia, ‘Ewe Abu Abbas! Nilikuwa kwa Ibn Umar رضي الله عنهما, na alisoma Aya hii na kulia, akasema Aya gani? Nikamjibu,

وَأِن تَبَدُّوا مَا فِي أَنفُسِكُمْ أَوْ تُخَفُّوهُ

“Na mkidhihirisha yaliyomo katika nafsi zenu au mkayaficha.” (2:284)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Aya hii ilipotemshwa, ilikuwa ngumu sana kwa Maswahaba wa Mtume ﷺ na waliogopa sana. Kisha walisema, “Ewe Mtume! Hakika sisi tumeangamia ikiwa tutaadhibiwa kwa mujibu wa kauli zetu, na vitendo vyetu, lakini vinavyotokea katika mioyo yetu hatuwezi kudhibiti vilivyomo ndani yake. Mtume ﷺ Alisema,

¹ Muslim 1:115.

«قُولُوا: سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا»

“Semeni, Tumesikia na Tumetii.”

Wakasema, ‘Tumesikia na Tumetii’ Aya hii ilifuta Aya iliyotangulia,

ءَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامَنَ بِاللَّهِ

“Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile Wote wanamuamini Mwenyezi Mungu.”Mpaka

لَا يُكْفِ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ

“Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadri ya iwezavyo. Faida ya iliyoyachuma ni yake, na khasara ya iliyoyachuma ni juu yake pia.”

Hivyo, walisamehewa yale yaliyopita kwenye mioyo yao, na wakawajibishwa kwa vitendo vyao tu.¹ Kikundi kimepokea katika vitabu vyao sita kutoka kwa Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ alisema kuwa Mtume ﷺ, alisema,

«إِنَّ اللَّهَ تَجَاوَزَ لِي عَنْ أُمَّتِي مَا حَدَّثتَ بِهِ أَنْفُسَهَا مَا لَمْ تَكَلِّمْ أَوْ تَعْمَلْ»

“Allah Ameusamehe Ummah wangu kwa kile wanachojisemesha ndani ya nafsi zao, madhali hawatamki au kuvitenda.”²

Sahih Mbili zilinukuu kuwa Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«قَالَ اللهُ: إِذَا هَمَّ عَبْدِي بِسَيِّئَةٍ فَلَا تَكْتُبُهَا عَلَيْهِ، فَإِنْ عَمِلَهَا فَاتَّكَبُهَا سَيِّئَةً، وَإِذَا هَمَّ بِحَسَنَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا فَاتَّكَبُهَا حَسَنَةً، فَإِنْ عَمِلَهَا فَاتَّكَبُهَا عَشْرًا»

“Allah Aliwaambia Malaika Wake, ‘Iwapo mja wangu atanuia kutenda ovu, msandike kosa kwake, na akitenda, mwandikieni kosa moja. Iwapo atanuia kufanya amali njema, lakini hakuitekeleza, basi mwandikieni jema moja, na akifanya mwandikieni mema kumi.”³

¹ Ahmad 1:332.

² Fat’hul Al-Bari 9:300, Muslim 1:117, Abu Dawud 2:657, Tuhfat Al-Ahwadhi.

³ Fat’hul Al-Bari 9:300, Muslim 1:117, Abu Dawud 2:657, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:361, An-Nasai 6:156, Ibn Majah 1:658.

ءَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ
 وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ؕ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ؕ غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ
 الْمَصِيرُ ﴿٢٨٥﴾ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لَا
 تُؤَاخِذْنَا إِن نَّسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ
 مِن قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ ؕ وَاعْفُ عَنَّا وَارْحَمْنَا ؕ أَنْتَ
 مَوْلَانَا فَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾

285. "Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi Wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake na Mitume Wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume Wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumetii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni Kwako."

286. "Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo. Faida ya iliyoyachuma ni yake, na khasara ya iliyoyachuma ni juu yake pia. (Ombeni:) Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea. Mola wetu Mlezi! Usitubebehe mzigo kama Uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi Usitutike tusiyoyaweza na Utusamehe, na Utughufirie, na Uturehemu. Wewe Ndiye Mlinzi wetu. Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri."

Hadithi juu ya Utukufu wa Aya Mbili Hizi, Allah تعالیٰ Atunufaishe Nazo.

Al-Bukhari alinukuu kuwa Abu Ma'sud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَرَأَ بِالْآيَتَيْنِ مِنْ آخِرِ سُورَةِ الْبَقَرَةِ فِي لَيْلَةٍ، كَفَّتَاهُ»

"Yeyote atakayezisoma Ayah mbili za mwisho za Suratil – Baqarah usiku, zitamtosha."¹

¹ Fat'hul Al-Bari 8:672.

Maimamu wa hadithi sita waliobakia walinukuu Hadithi zenye maneno sawa na haya.¹ katika Sahih Mbili zilinukuliwa Hadith zikitumia isnadi mbalimbali za upokezi.² Na Imam Ahmad pia alinukuu.³

Muslim alinukuu kuwa Abdullah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alipokwenda safari ya Isra, alipanda katika *Sidrat Al-Muntaha*,⁴ katika mbingu ya sita, mahali ambapo hukoma kila kitu kutoka duniani, na kinachoshuka kutoka juu hukoma hapo.

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ

“Kilipoufunika huo mkunazi hicho kilichoufunika.” (53:16)

Akasema: Maana yake: Mkeka uliotengenezwa kwa dhahabu.

Kisha Mtume ﷺ alipewa mambo matatu, “Sala tano, Aya za mwisho ya *Surat Al-Baqarah* na msamaha kwa mtu yeyote katika Ummah wake ambaye hakumshirikisha Allah تعالى ya yeyote au chochote.”⁵

Mwanzoni tulitaja Hadith inayohusu utukufu wa *Surat Al-Fatihah* kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما ambayo ilisema, Mtume ﷺ alipokuwa na Jibril عليه السلام alisikia sauti inatoka juu. Jibril عليه السلام aliangalia juu kisha akasema, “Huu ni mlango uliofunguliwa sasa hivi Peponi, na haujawahi kufunguliwa kabla. Malaika alishuka kupitia mlango ule mpaka kwa Mtume ﷺ na akamuambia, “Pokea habari njema za nuru mbili ulizopewa na hapana Mtume kabla yako aliyepewa. *Al-Fatihah* na Aya za mwisho za *Surat Al-Baqarah*. Hutasoma herufi zake, ukazipita hivi hivi tu lakini utalipwa manufaa yake.” Hadithi hii ilikusanywa na Muslim na An-Nasai, na haya ni maneno yaliyokusanywa na An-Nasai.⁶

¹ Muslim 1:555, Abu Dawud 2:118, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:188, An-Nasai katika Al-Kubra 5:14, Ibn Majah 1:435.

² Fat’hul Al-Bari 8:712, 7:369, Muslim 1:554.

³ Ahmad 4:118.

⁴ Mkunazi ulioko kikomoni ambao hapana mwenye kuvuka.

⁵ Muslim 1:157.

⁶ Muslim 1/554 Annasai katika Al-Kubra 5:12

Tafsiri ya Aya Mbili za Mwisho za Surat Al-Baqarah

Allah تعالی Amesema,

كُلٌّ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ۗ

“Wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Yake, Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume Wake.”

Kwa hiyo, kila muumini anaamini kuwa Allah تعالی ni Mmoja Pekee na ni Yeye Pekee Mkusudiwa, hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye na hapana Mola isipokuwa Yeye. Waumini wanaamini Mitume wote wa Allah تعالی na Manabii, ambao kwa hakika ni waja wa Allah تعالی. Zaidi, waumini hawatofautishi kati ya Mitume, kama vile, kuamini baadhi na kukanusha wengine. Bali, Mitume wote na Manabii wa Allah ni wakweli na waadilifu kwa waumini, na kila mmoja Aliongozwa katika njia ya uadilifu, hata wakati baadhi yao walikuja na sheria zilizofuta nyingine kwa Amri ya Allah تعالی. Baadaye, sharia ya Muhammad ﷺ, Mtume wa Mwisho na Mjumbe kutoka kwa Allah تعالی, ilifuta sharia zote za Mitume wa kabla yake. Hivyo Siku ya Mwisho itasimama huku sharia ya Muhammad ﷺ ikitawala wakati huo huo kundi la umma wake wakati wote litakuwa kwenye njia ya haki, wazi na iliyoshinda wote. Kauli ya Allah تعالی,

وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ

“(Waumini) husema: Tumesikia na tumetii.”

Maana yake: Tumesikia Kauli Yako, Ewe Mola Wetu. Walizingatia na kutekeleza, na wakashikamana na matokeo yake.

غُفْرَانَكَ رَبَّنَا

“Tunakuomba maghufira Mola wetu Mlezi.”

Ina maombi na Dua kwa Usamehevu wa Allah تعالی, Rehema na Upole Wake. Kauli ya Allah تعالی,

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ

“Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo.”

Maana yake: Allah تعالی Hailazimishi roho kile kilicho nje ya uwezo wake. Hili linaonesha Huruma, Ukarimu wa Allah تعالی kwa viumbe Wake. Aya hii ndio iliyofuta Aya iliyowaogofya Maswahaba, nayo ni Kauli ya Allah تعالی,

وَإِنْ تُبَدُّوْا مَا فِي أَنْفُسِكُمْ أَوْ تُخَفُّوْهُ يُحَاسِبْكُمْ بِهِ اللهُ

“Na iwapo utadhahirisha yaliyomo ndani ya nafsi zenu au mkayaficha Allah Atawahesabu kwayo.” (2:284)

Inaonesha kuwa japokuwa Allah تعالی Atawauliza waja Wake na Kuwahukumu, na Atamuadhibu kwa lile ambalo anaweza kujikinga nalo. Ama yale wasiyoweza kujikinga nayo kama mazungumzo ya ndani ya nafsi au kufikiria Hatawaadhibu kwa hilo. Inafaa tutaje hapa kuwa, kuchukia fikra mbovu zinazompitia mtu kwenye akili yake ni sehemu ya imani. Kisha Allah تعالی Amesema,

لَهَا مَا كَسَبَتْ

“Faida ya aliyoyachuma ni yake.”

Mambo mazuri,

وَعَلَيْهَا مَا كَسَبَتْ

“Na hasara ya iliyoyachuma ni juu yake pia. (Ombeni).”

Maana yake: Mambo mabaya. Na haya yanaingia katika amali ambazo ataulizwa nazo mtu.

Kisha Allah تعالی Akawapa muongozo waja wake kumuomba Yeye tu. Na Amedhamini kujibu maombi yao, pale Alipowaongoza na Kuwafundisha Kusema:

رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ كُنَّا مُسِيئِينَ أَوْ نَحْنُ مُجْرِمُونَ

“Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau na tukikosea.”

Maana yake: “Iwapo tutayasahau majukumu au tukaangukia katika maovu au tukakosea wakati hatujui sharia.” Tulitaja Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه iliyokusanywa na Muslim, humo Allah تعالی Amesema, “Nitapokea Dua zenu.”¹

¹ Muslim 1:115.

Pia kuna Hadithi ya Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Allah تعالى Alisema, "Nilikubali Dua zenu."¹ Na Kauli Yake Allah تعالى,

رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِنَا

"Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo kama Uliowabebesha wale waliyokuwepo kabla yetu (Mayahudi na wakristo)."

Maana yake: "Hata kama tuna uwezo wa kuyatekeleza, Usitutwike magumu kama Uliyowatwika ummah uliokuwa kabla yetu. Ulimpeleka Mtume Muhammad ﷺ, Mtume wa rehema, ili afute hiyo mizigo kupitia sharia Uliyomteremshia, *Hanifi* (Tawhid ya Uislam), Dini nyepesi." Muslim alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Alisema, "Nitajibu Dua zenu."² Ibn Abbas رضي الله عنهما alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Alisema, "Nilijibu Dua zao." Kuna Hadithi iliyonukuliwa kupitia isnadi mbalimbali za wapokezi kuwa Mtume ﷺ alisema,

«بُعِثْتُ بِالْحَنِيفِيَّةِ السَّمْحَةِ»

*"Nimetumwa na njia rahisi ya Hanifiyyah."*³

رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ

"Mola wetu Mlezi Usitutwike tusiyoyaweza."

Miongoni mwa majukumu, hali ngumu, mateso, Usitubebeshe tusiyoyamudu. Makhut amesema kuhusu Kauli Yake Allah تعالى,

رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ

"Mola wetu Mlezi Usitutwike tusiyoyaweza."⁴

Tulitaja kuwa Allah تعالى Alisema, "Ndiyo."⁵ Katika Hadithi moja na nilishapokea Dua, katika Hadithi nyingine. Ama Kauli Yake:

¹ Muslim 1:116.

² Muslim 1:115.

³ Muslim 1:116.

⁴ Ibn Abu Hatim 3:1235.

⁵ Ahmad 5:266, 6:116,233. Kuna rejea nyinginezo zenye maneno sawa na haya. Ya kwanza imenukuliwa pia na Al-Humaydi, angalia As-Sahihah 1829,2935.

وَأَعْفُ عَنَّا

“Na Utusamehe.”

Maana yake: Baina yetu na Wewe kuhusu Uyajuayo kuhusu udhaifu wetu na makosa yetu.

وَأَغْفِرْ لَنَا

“Na Utughufirie.”

Kuhusu lililo baina yetu na waja Wako. Hivyo Usiwaoneshe makosa yetu na amali zetu mbaya.

وَأَرْحَمْنَا

“Na Uturehemu.”

Katika yatakayokuja baadaye. Kwa hiyo, Usituachie tukaingia ndani ya makosa mengine. Wanasema kuwa wale wanaofanya makosa wanahitaji mambo matatu; Msamaha wa Allah تعالى kwa lile lililo baina Yake na wao, Ayafiche makosa kuonekana kwa waja wengine, na hivyo Asiyaweke wazi mbele ya waja, na Awape kinga ya kutokosea tena. “Tumetaja kuwa Allah تعالى Aliyakubali maombi yao.” “Nita” na mapokezi mengine, “Nili”.

أَنْتَ مَوْلَانَا

“Wewe Ndiye Mlinzi wetu.”

Maana yake: Wewe ni Msaidizi wetu na Mlinzi wetu, tunakuamini Wewe, Unaendewa kwa kila aina ya msaada na mategemeo yetu yote yako Kwako.

فَأَنْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ

“Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri.”

Wale wanaokataa Dini Yako, waliokanusha Tawhidi Yako, waliokataa Ujumbe wa Mtume wako, wakamuabudu asiyekuwa Wewe na wakakushirikisha na wengine katika ibada. Tunusuru dhidi yao. Tupe ushindi na tuwashinde hapa duniani na Akhera. “Allah تعالى Alisema, “Ndiyo.” Katika Hadithi iliyokusanywa na Muslim kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, “Allah تعالى Alisema, “Nilishafanya hivyo.”

Zaidi, Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Abu Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa kila Muadh رضي الله عنه alipomaliza kusoma sura hii,

فَأَنْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾

“Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri.”

Alikisema, “Amin.”¹

* * *

¹ At-Tabari 6:146. Isnadi yake ni dhaifu.